
ELLEN G. WHITE



# SHUHUDA KWA KANISA

GOMBO LA 1

RohoYaUnabii.Org MaarifaMtandaoni.Org
RevivalPlan.Org RohoYaUnabii.Net
Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani Ministry

**2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo.**

**Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4T 472)**

Kitabu hiki kimetafsiriwa kwa ajili ya kila mtu. Habari hizi ni muhimu sana hivyo wewe uko huru kunakili na kusambaza kwa wengine kama kilivyo. Kwa nakala ya kidijitali ya kitabu hiki, tafadhali tembelea R***ohoYaUnabii.Org, RohoYaUnabii.Net, MaarifaMtandaoni.Com, MaarifaMtandaoni.Africa*** au kwa Kingereza ***WhiteEstate.org***. Kugushi Maandishi ya namna hii au kuyakaba koo yasinene, ni kujiletea taabu kubwa. Yeremia 36:27 na Ufunuo 22:18, 19 na Kumbukumbu la Torati 4:9

‘Karibu watu 1000 Wataamini Siku moja kwa Ule ujumbe wa Kimya wa Machapisho.’ Unabii huu unatimia, Maelfu ya watu duniani kote wanabatizwa kwa siku moja, kwa wazi au kwa faragha. Tafsiri zetu ni kama Wikipedia, ukitaka kuboresha bila kupoteza maana, boresha tu, ila usipoteze kabisa ujumbe na maana iliyokusudiwa. Tumeweka Pointers (2T 45.5) na kadhalika ili ujihakikishie mwenyewe na kutafsiri kwa ubora zaidi unapotaka. Kiswahili kinazidi kupanuka, Machapisho ya Wamishenari kama Nuru kwa Kanisa sasa tukiyaona tunashangaa, ila enzi hizo yalikuwa yenyewe kabisa kwa uzuri!

Asante kwa Wasomaji, Watafsiri, Wahariri, Washauri, Waombezi, Wanaufundi na wote ambao wanasaidia hii kazi ya Machapisho duniani kote. Kama umeshiriki hii kazi na jina lako halikuweka tuandikie, Asante

1. Alex Ngamije -PreciousPresentTruth.org Rwanda
2. Mr and Mrs Kumbuka Mlazi Misibo -Kigoma, Tanzania
3. Samuel Mhololo -Kigoma, Tanzani
4. Musa Budodi -Shinyanga Tanzania
5 Isack Msusu-Kigoma, Tanzania
5. Stephen Letta-Masasi, Tanzania
6. Aimo Abayo –Morogoro, Tanzania
6. Daudi Jabez Masaka-Pennslvyania, Marekani
7. Paul Masaka -Oklahoma, Marekani
8. Mwalimu Peter Marwa -Mwanza, Tanzania
9. Faustine Momadi Mkama -Dar Es Salaam,Tanzania
10. Geoffrey Herman -Manyara, Tanzania
12. Pendo Makori -Visiga,Tanzania
13. John Mmari Mugane -Siha, Tanzania
14. Kikundi cha Mbaki/Ngulu Maombi -TAUS—USA
16. Women Prayer Warriors WPM -California, Marekani
17. Ezekiel Ojwang -Kiterere,Tanzania

18. John Mugane -Nakuru, Tanzania
19. Sandra Barron -Kentucky, Marekani
20. Eliphas Sambeke -Arusha, Tanzania
21. Stefano Kasiri -Kibaha, Tanzania
22.Gideon Christian - Ukerewe, Tanzania
25.Musa Muneja -Bariadi, Tanzania
26. Victoria Swai Mhololo -Arusha, Tanzania
27. Julius Letta -Morogoro, Tanzania
28. Aimo Abayo –Morogoro, Tanzania
29. John Chilala -Dar Es Salaam, Tanzania
30. Bariki Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
31. Mbaraka Hamisi -Kilimanjaro, Tanzania
32. Mbusi Mpagalushu -Bariadi, Tanzania
33. James Benedicto- Mara, Tanzania
34. Basanthi Thavamani-Lazar -Madras, India
35. Stefano Kasiri- Bariadi, Tanzania
36. Kwandu and Stefano Kasiri -Pwani,Tanzania
37. Elinath Elisante Kukome -Kilimanjaro, Tanzania
38. Sharifa Athuman Seleman -Dar-es-Salaam, Tanzania
39. Jackson Musa Singano -Dar-es-Salaam, Tanzania
40. Daniel Masaka -Kisii, Kenya
41. Sharifa Athuman Seleman -Dar-es-Salaam, Tanzania
42. John Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
43. Walter Nehemia -Dar Es Salaam, Tanzania
44. Gerard Nyafanga -Mara, Tanzania
47. Kilango Makala -Kilimanjaro, Tanzania
48. Loyce Pima -Bunda, Tanzania
49. Niwaeli Mburuja -Hedaru, Tanzania
50. Cindy Tustch -Washington, Marekani
51. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
52. Sandra Barron -Kentucky, Marekani
53. John Ngasa -Mwanza, Tanzania
54. Milinje Momadi -Kibaha, Tanzania
55. Zablon Mgonja -Arusha, Tanzania
56. Luck Rahim Datoo -Arusha, Tanzania
57. Ruth Lilian Bango -Arusha, Tanzania
58. Mohammed Mboi -Kisii, Kenya
59. William Kalokaza-Rukwa, Tanzania
60.Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani

Wenu katika huduma ya MaarifaMtandaoni.Com, RohoYaUnabii.Org, RohoYaUnabii.Net
Daniel Masaka and Grace Momadi Masaka -New Jersey, Marekani

## YALIYOMO

MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI…....................................................1
UTANGULIZI............................................................................4
ASILI YA JUZUU YA 1.................................................................10
SURA YA 1
NIKIWA MTOTO MDOGO...........................................................13
SURA YA 2
WONGOFU WANGU....................................................................17
SURA YA 3
HISIA ZA KUKATA TAMAA........................................................23
SURA YA 4
KULIACHA KANISA LA METHODIST.............................................33
SURA YA 5
UPINZANI WA NDUGU.............................................................40
SURA YA 6
UZOEFU WA MAREJEO.............................................................43
SURA YA 7
MAONO YANGU YA KWANZA.....................................................51
SURA YA 8
WITO WA KUSAFIRI.................................................................54
SURA YA 9
MAONO YA NCHI MPYA............................................................59
SURA YA 10
KUZUIA MAKEMEO...................................................................62
SURA YA 11
NDOA NA KAZI ZINAZOANDAMANA NAYO....................................65
SURA YA 12
UCHAPISHAJI NA KUSAFIRI......................................................74
SURA YA 13
KUONDOLEWA KWENDA MICHIGAN............................................81

SURA YA 14
KIFO CHA MUME WANGU....................................................................87
SURA YA 15
MLINZI WA NDUGU YAKO.................................................................92
SURA YA 16
MUDA WA KUANZA SABATO............................................................94
SURA YA 17
WAPINZANI WA UKWELI................................................................95
SURA YA 18
WAJIBU WA WAZAZI......................................................................97
SURA YA 19
IMANI KATIKA MUNGU .................................................................98
SURA YA 20
CHAMA CHA "MJUMBE"...............................................................100
SURA YA 21
JITAYARISHE KUKUTANA NA BWANA..........................................101
SURA YA 22
NJIA MBILI....................................................................................104
SURA YA 23
KUUFUATISHA ULIMWENGU.......................................................107
SURA YA 24
WAKE ZA WACHUNGAJI..............................................................112
SURA YA 25
KUWA NA BIDII, UKATUBU..........................................................115
SURA YA 26
MASHARIKI NA MAGHARIBI.......................................................119
SURA YA 27
VIJANA WATUNZA SABATO.........................................................124
SURA YA 28
MAJARIBU YA KANISA..................................................................131
SURA YA 29
“JIHADHARINI”.............................................................................134
SURA YA 30
KIJANA TAJIRI...............................................................................136
SURA YA 31
UPENDELEO NA WAJIBU WA KANISA..........................................142

SURA YA 32
KUPEPETWA....................................................................144
SURA YA 33
KANISA LA LAODIKIA..........................................................148
SURA YA 34
NYUMBA ZA IBADA............................................................156
SURA YA 35
MASOMO KUTOKA KATIKA MIFANO...................................158
SURA YA 36
DHAMANA KWA WASIOAMINI.............................................160
SURA YA 37
KUAPA.........................................................................161
SURA YA 38
MAKOSA KATIKA LISHE......................................................163
SURA YA 39
UVIVU WAKEMEWA............................................................167
SURA YA 40
WAJIBU KWA WATOTO.......................................................172
SURA YA 41
UTOAJI WA MPANGO.........................................................175
SURA YA 42
JINA LA DHEHEBU LETU....................................................177
SURA YA 43
MASIKINI.....................................................................178
SURA YA 44
ULANGUZI....................................................................179
SURA YA 45
WAKILI ASIYE MWAMINIFU..................................................180
SURA YA 46
USHUPAVU HUKO WISCONSIN...........................................182
SURA YA 47
KUFICHA MAONYO............................................................185
SURA YA 48
KAZI YA MUNGU HUKO OHIO............................................187
SURA YA 49
WAKFU KAMILI...............................................................191

SURA YA 50
UZOEFU BINAFSI....................................................................194
SURA YA 51
KAZI HUKO MAGHARIBI.............................................................199
SURA YA 52
SWALI LAJIBIWA....................................................................201
SURA YA 53
KASKAZINI NA KUSINI.............................................................202
SURA YA 54
DHIKI KUBWA INAKUJA............................................................207
SURA YA 55
UTUMWA NA VITA..................................................................210
SURA YA 56
NYAKATI ZA HATARI...............................................................214
SURA YA 57
MUUNDO.............................................................................216
SURA YA 58
WAJIBU KWA WAHITAJI..........................................................218
SURA YA 59
NGUVU YA MFANO.................................................................220
SURA YA 60
KUJIWEKA WAKFU.................................................................230
SURA YA 61
FALSAFA NA UDANGANYIFU WA BURE........................................232
SURA YA 62
DINI YA FAMILIA....................................................................241
SURA YA 63
WIVU NA KUTAFUTA MAKOSA..................................................247
SURA YA 64
UMOJA WA IMANI..................................................................256
SURA YA 65
WISCONSIN KASKAZINI...........................................................258
SURA YA 66
NGUVU ZA SHETANI...............................................................268
SURA YA 67
MATAJI MAWILI.....................................................................273

SURA YA 68
WAKATI UJAO......................................................................278
SURA YA 69
UASI.................................................................................279
SURA YA 70
HATARI NA WAJIBU WA WATENDAKAZI...........................................288
SURA YA 71
MATUMIZI MABAYA YA MAONO......................................................298
SURA YA 72
WAZAZI NA WATOTO...................................................................300
SURA YA 73
KAZI HUKO MASHARIKI................................................................304
SURA YA 74
HATARI ZA VIJANA.....................................................................305
SURA YA 75
KUTEMBEA KATIKA NURU.............................................................316
SURA YA 76
KAZI HUKO MASHARIKI................................................................319
SURA YA 77
MAOMBI YA DAUDI.....................................................................329
SURA YA 78
KUKITHIRI KATIKA MAVAZI..........................................................331
SURA YA 79
MAWASILIANO NA MZEE HULL.......................................................333
SURA YA 80
WACHUNGAJI WASIOTAKASWA.......................................................341
SURA YA 81
MKE WA MCHUNGAJI...................................................................349
SURA YA 82
HAKI ZA AMANA.........................................................................353
SURA YA 83
MATENGENEZO KATIKA MAVAZI.....................................................354
SURA YA 84
WACHUNGAJI WETU...................................................................362
SURA YA 85
MATENGENEZO YA AFYA..............................................................376

SURA YA 86
HOTUBA KWA VIJANA....................................................................383
SURA YA 87
BURUDANI KWA WAKRISTO..........................................................396
SURA YA 88
MATENGENEZO YA MAVAZI.........................................................401
SURA YA 89
BATTLE CREEK YASHUKIWA.........................................................405
SURA YA 90
KUHAMISHA MAJUKUMU..............................................................407
SURA YA 91
UTUNZAJI SAHIHI WA SABATO....................................................410
SURA YA 92
HISIA ZA KISIASA.....................................................................411
SURA YA 93
RIBA..........................................................................................412
SURA YA 94
UDANGANYIFU WA UTAJIRI.........................................................413
SURA YA 95
UTII KWENYE UKWELI..............................................................418
SURA YA 96
BIMA YA MAISHA.....................................................................423
SURA YA 97
KUSAMBAZA MACHAPISHO.........................................................425
SURA YA 98
MWANAMATENGENEZO WA AFYA..............................................426
SURA YA 99
TAASISI YA AFYA.....................................................................427
SURA YA 100
AFYA NA DINI..........................................................................435
SURA YA 101
KAZI NA MABURUDISHO.............................................................438
SURA YA 102
KIELELEZO CHA UZOEFU............................................................440
SURA YA 103
WAFANYAKAZI KATIKA OFISI......................................................451

SURA YA 104
MIGOGORO NA USHINDI....................................................................456
SURA YA 105
MAJIBU KUTOKA KANISA LA BATTLE CREEK..........................................469
SURA YA 106
KUKATA NA KUFYEKA.....................................................................471
SURA YA 107
HATARI YA KUJIAMINI....................................................................478
SURA YA 108
USIDANGANYIKE............................................................................483
SURA YA 109
KUCHAPISHA USHUHUDA BINAFSI....................................................484
SURA YA 110
TAASISI YA AFYA............................................................................486
SURA YA 111
KIELELEZO CHA UZOEFU.................................................................493
SURA YA 112
WACHUNGAJI, UTARATIBU NA MFUMO.............................................494
SURA YA 113
KAZI ZAIDI.....................................................................................500
SURA YA 114
KESI YA HANA MORE......................................................................510
SURA YA 115
MAPISHI YENYE AFYA.....................................................................521
SURA YA 116
VITABU NA MAJARIDA.....................................................................526
SURA YA 117
USIKIVU WA MKRISTO....................................................................528
SURA YA 118
HURUMA NYUMBANI.......................................................................531
SURA YA 119
NAFASI YA MUME..........................................................................540

## MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI…

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni ROHO MTAKATIFU, ushauri, na Maombi yako msomaji. Wako watu wanaoishi nje ya Afrika wanahitaji pia kusoma kwa Lugha ya asili. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la MUNGU limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi karibu 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window'

'Sambaza Biblia popote,' ndiyo kauli mbiu ya muumini; sambaza Neno la MUNGU kote.

Jiunge nasi katika kuandika vitabu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ikiwa kuna kosa lo lote la kiuandishi au kiutafsiri, tafadhali wasiliana nasi na endapo ukiamua kuchapa, usibadilishe cho chote labda typos tu.

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa hapa Kwetu Afrika Mashariki, tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu; mada za afya, lishe, mahusiano kama ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake; haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandano ya magharibi na ni mema tu, lakini kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine.

Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabu, nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu na kuelezea kisa fulani. Kwa nini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vitu vizuri, ikiwemo nyimbo za watoto?. Tuna wataalamu wengi wa nyimbo. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi kubwa kama Kifaransa na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko

sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu, na wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au wawe na mwenendo kama ule.

Mfano mdogo sana ni, waandishi wengi wa nje huandika vitu vingine visivyoendana na muktadha wetu, mfano vyakula kama Pizza, Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je viwanda vyetu hutengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana. Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! tunaelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya!

Si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii; wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Kitabu cha Jando na Unyago kwa Waumini ni vizuri tupate watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti, na hii inafanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio umma. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ikiwa ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani, tafadhali usisite kuutoa na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, fundisha wengine, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku.

UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au simu -1 -908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo BWANA!

**Back of the BOOK cover** -Mkakati wa uamsho au Tumaini linalotiririka ni msaada mkubwa kwetu leo ambao hatuelewi vyema tufanye nini ili Maisha yetu yampendeze MUNGU na watu, katika muda ambao maadili yanamomonyoka na ulimwengu hauna mafundisho mema au haufundishi kabisa. Mafundisho haya ni mazuri kwa kila binadamu anayeelewa Kiswahili!

“Nilichukua Biblia ya thamani, na kuizingira kwa “Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa,” zilizotolewa kwa ajili ya watu wa MUNGU ili kusahihisha tabia zao. na "Hapa," nilisema na kuona kwamba, "karibu kesi za watu wote zinawakilishwa na maonyo haya waliyopewa watu hawa. Dhambi wanazopaswa kuepuka zimeonyeshwa. Shauri ambalo wangetamani linaweza kupatikana kuhusiana na jambo fulani la maisha yao, lipo hapa kwenye hizi shuhuda, limetolewa tayari, kwani kuna kesi zingine zinazofanana na zao wenyewe kabisa, na ambazo zitatatua tatizo lao wakifuata ushauri wake. MUNGU amependezwa kukupa amri juu ya amri na kanuni juu ya kanuni Lakini wengi wenu hamyajui mashauri yaliyomo ndani ya Shuhuda, hamyafahamu Maandiko jinsi mnavyopaswa. Endapo mngelifanya Neno la MUNGU kuwa Ndiyo mada kuu ya elimu/mafunzo kwenu, mkiwa na shauku ya kufikia vigezo vya Biblia na ukamilifu wa Kikristo, basi msingezihitaji Shuhuda. Ila ni kwa sababu mmepuuzia kujielimisha na Kitabu cha MUNGU kilichovuviwa, yaani Biblia na ndio maana Yeye ametafuta kuwafikia kwa Shuhuda rahisi na nyofu, zinazolenga moja kwa moja mada, akivutia usikivu wenu/wako kwa Maneno yaliyovuviwa. ambayo mlikuwa mmepuuzia kuyatii, na kuwasihi mtengeneze maisha yenu kulingana na mafundisho Yake safi na yaliyotukuka." 5T 664.3

## UTANGULIZI

Wapendwa vitabu hivi ni vyetu sote! Maana kila mtu anahitaji Mashauri. Kwenye wingi wa Ushauri hapaanguki jambo, na kuna usalama. Masihi Yu karibu kuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya na yatuchome sana, na kutuvutia tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na ROHO MTAKATIFU kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na

kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Hivi ndivyo vitu pekee ambavyo tutaenda navyo mbinguni.

Shuhuda zimejaa mashauri, Makaripio na maonyo ya maisha ya kila siku kwa undani zaidi. Tumeambiwa kwenye maagizo kwamba shuhuda zina kila namna ya kukamilisha tabia zetu. Tulisikia kuhusu kuwepo kwa Shuhuda kwa Kanisa ila hatukujua sana kwamba zinahusiana na nini! Ila baada ya kuanza kusoma kila siku katika mpango wa kusoma Shuhuda Revivalplan.com kwa lugha ya Kingereza tuliona kuna haja kubwa ya kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili maana Divisheni yetu ambayo ina watu wengi wanaozungumza lugha ya Kiswahili, ndiyo Divisheni iliyo na watu wengi duniani (East-Central Africa Division of Seventh-day Adventists) kwa sasa, na takwimu zinaonesha kuwa Afrika sasa ina asilimia 50% ya waumini wanaotarajia marejeo ya YESU (Waadventista). Asilimia 3% ya Maandishi ya Roho ya Unabii yametafsiriwa Kiswahili.

Wana Marejeo wanaozungumza Kiswahili duniani sasa ni 11%. Kutokana na Google wale wanaozungumza Kingereza 'fluently' katika nchi za Kiswahilii ni asilimia ndogo sana kuliko tunavyofikiria! Tumepewa ulimwengu wa Kiswahili tuufikie. Hivyo Kutafsiri mambo haya ni jambo la dharura. Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

1. Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."

2. Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha Neno la MUNGU

3. Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania

4. Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa.

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua 'Google App' ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

Google imesaidia mambo kadhaa mfano Kujua mitindo na mavazi ya sketi za hoops miaka ya 1800BK; itakupa maoni waliyokuwa nayo wakati ule. Japo hekima haiongezeki kwa urahisi, maarifa yameongezeka, hivyo angalia mambo haya kwa kichujio cha Biblia zaidi ya teknolojia. Usiogope kurejelea kamusi, ndio kujifunza. Muumini daima ni mwanafunzi na anasaidiwa zaidi kukumbuka mambo mengi anapotumia machapisho zaidi ya njia zingine. Mengine ya Kingereza imebidi tuweke maana tunayatumia na hivyo utapata utambuzi wa

jambo haraka, mfano mara nyingi hatusemi Jimbo, ila Konferensi/conference, majina ya magonjwa au mitindo n.k Tunashauri kila kanisa liwe na magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua miezi 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com)

Wenu wadhamini, watafsiri, wahariri, washauri, wahakiki, marafiki, wajoli na ndugu katika safari ya kwenda mbinguni.

“Mashaka na hata kutokuamini shuhuda za ROHO WA MUNGU, kunayachachua makanisa yetu kila mahali. Shetani angependa iwe hivi. Wachungaji wanaohubiri ubinafsi badala ya Kristo wangependa iwe hivi. Shuhuda hazisomwi na wala hazithaminiwi. MUNGU amezungumza na wewe. Nuru imekuwa ikiangaza kutoka kwa Neno Lake na Kutoka kwa Shuhuda, na zote zimechukuliwa kwa urahisi na kupuuzwa”. 5T 217.2

“Mwokozi wangu alinitangazia kwa mjumbe WAKE. "Kazi yako," Alinielekeza “Ni kubeba Neno langu... kuchukua Neno langu mbele ya wale wasioamini, na kwa kalamu na sauti kukemea kutokana na Neno matendo ambayo sio sawa ... Kwa ushawishi thabiti wa unyenyekevu, kwa sauti na kalamu, ujumbe nitakaoutoa utasikika kutoka kwa mtu ambaye hajawahi kujifunza shuleni… “Usimwogope mwanadamu, Sio wewe unayezungumza: ni Bwana Anayetoa jumbe kwa siku hizi za mwisho; nazo zitaandikwa katika vitabu, na zitasimama milele zote, ili kushuhudia dhidi ya wale ambao wameongozwa kuziacha kwa sababu ya ushawishi wa udanganyifu wa uovu.” RH, Julai 26, 1906

Niliona kwamba wote wanapaswa kuchunguza mioyo na Maisha yao kwa ukaribu na kuona ikiwa hawakuwa wamefanya makosa yaleyale ambayo wengine walisahihishwa, na ikiwa maonyo yaliyotolewa kwa wengine hayakuhusu kesi zao wenyewe. Ikiwa ndivyo, wanapaswa kuhisi kwamba ushauri na maonyo yalitolewa haswa kwao na wanapaswa kufanya matumizi hayo kwao kana kwamba walikuwa wanaambiwa wao wenyewe. {2T 687.2}

“Zamani MUNGU alinena na wanadamu kwa kinywa cha manabii na mitume. Katika siku hizi Anazungumza na wanadamu kwa Shuhuda za Roho WAKE. Hakukuwa na wakati ambapo MUNGU aliwafundisha watu WAKE kwa bidii zaidi ya vile anavyowafundisha sasa juu ya mapenzi Yake na njia ambayo angewataka wafuate…. Acha Ushuhuda upimwe kwa matunda yake .... kwamba kazi hii ni ya MUNGU, au sio ya MUNGU. MUNGU hafanyi chochote kwa kushirikiana na Shetani… Hakuna kazi nusu ya 12 Shetani au nusu ya MUNGU katika jambo hilo. Ushuhuda ni wa ROHO WA MUNGU, au wa shetani. Udanganyifu wa mwisho kabisa wa Shetani utakuwa ni kuzifanya Shuhuda za ROHO WA MUNGU zisiwe na ushawishi. "Mahali ambapo hakuna maono, watu huangamia." Mithali 29:18.

Shetani atafanya kazi kwa ustadi na kwa njia tofauti na kupitia wakala tofauti kutia mashaka imani ya watu wa MUNGU wa masalio katika Ushuhuda wa kweli…. FLB: 296 "Jambo moja ni hakika: Wale Waadventista Wasabato ambao wanachukua msimamo wao chini ya bendera ya Shetani kwanza wataacha imani yao katika maonyo na makaripio yaliyomo katika Shuhuda za ROHO WA MUNGU. Lt156-1903

"Ukikosa Imani katika Shuhuda utaondoka kwenye Ukweli wa Biblia. 5T: 674

"Nimejawa na huzuni ninapofikiria hali ya watu wetu. BWANA hajatufungia mbingu, lakini njia yetu wenyewe ya kurudi nyuma imetutenga na MUNGU … Na bado cha kushangaza ni kuwa maoni ya jumla ni kwamba kanisa linastawi na kwamba amani na ustawi wa kiroho uko katika mipaka yake yote. "Kanisa limeacha kumfuata Kristo Kiongozi Wake na linarudi nyuma kuelekea Misri. Walakini ni wachache wanaochukua tahadhari dhidi ya uhitaji wao wa nguvu za kiroho… 5T: 217

"Nimeonyeshwa kuwa kutokuamini Shuhuda kumekuwa kukiongezeka kadiri watu wanavyorudi nyuma kutoka kwa MUNGU. Hali hii ipo katika safu zetu zote, katika nyanja zote. Lakini ni wachache wanaojua ni uzoefu gani kanisa linaenda kupitia. Niliona kwamba kwa sasa tuko chini ya uvumilivu wa BWANA; lakini hakuna anayejua ukubwa wa rehema ambayo imetolewa kwetu. Lakini ni wachache waliojitoa kwa MUNGU kwa moyo wote. Kuna wachache tu ambao, ni kama nyota katika usiku wenye dhoruba kali, huangaza hapa na pale kati ya wingu… RH, Agosti 30,1906

"Wakati Shuhuda, ambazo ziliaminiwa wakati mmoja, zinapotiliwa shaka na kuachwa, Shetani anajua waliodanganywa hawataachia hapo; na huongeza juhudi zake mara dufu hadi atakapowaingiza kwenye uasi wa wazi, ambao huwa hauwezi kupona na huishia katika uharibifu. "Ushuhuda haupaswi kuhafifisha Neno la MUNGU, bali kuliinua na kuzivutia akili kwake, ili Ukweli mzuri wa unyenyekevu uweze kuwavutia wote... Ikiwa ungefanya Neno la MUNGU kuwa Somo lako, na hamu ya kufikia Kiwango cha Biblia na kufikia kwa ukamilifu wa Kikristo, usingehitaji Shuhuda… Ukweli wa ziada haujatolewa: lakini MUNGU kupitia Ushuhuda amerahisisha Kweli kuu ambazo tayari zimetolewa na kwa njia Yake Mwenyewe aliyochagua amezileta mbele ya watu ili ziamshe na zivutie akili. ili wote wasiwe na udhuru FLB: 295

"Wengi sasa wanadharau maonyo ya uaminifu yaliyotolewa na MUNGU katika ushuhuda…. Lakini Upinzani dhidi ya vitisho vya MUNGU hautazuia utekelezaji wake. Kukataa Maneno ya Bwana, yaliyosemwa kupitia chombo CHAKE alichokichagua, itasababisha hasira Yake tu na mwishowe italeta uharibifu kwa mkosaji. 5T: 678

"Uelewa wa wale wanaodharau Shuhuda zilizo wazi za Neno la MUNGU, na kukataa kuamini kwa sababu ni jambo linawabugudhi au lisilovutia wengi kufanya, utatiwa giza; Ukweli utaonekana kwao kama uongo, na uongo utakubaliwa kama Ukweli…. Lakini upendo kwa Kristo na kwa roho ambazo alizifia kwa ajili yake, zitamwongoza mtumishi wa MUNGU kutoa maonyo na wito kwa uaminifu. SW, Juni 23, 1908

"Kupuuza Nuru ni Kuikataa." 13 Agizo nilipewa na Mwokozi, "Sio wewe ambaye wamekukataa, lakini Mimi, Mwokozi wao …… Wale ambao wamepuuza Jumbe ambazo nimempa mjumbe wangu kubeba wamemtukana YULE aliyetoa jumbe hizo. …Watunze Watu, kundi la malisho yangu, wasifundishwe na matabibu au walimu wanaokataa maonyo ambayo nimetoa kupitia mjumbe wangu.' SpM: 384

"Wengi wanaenda kinyume kabisa na nuru ambayo MUNGU amewapa watu WAKE, kwa sababu hawasomi vitabu ambavyo vina nuru na maarifa yenye tahadhari, makaripio, na maonyo…. Nuru ya thamani sana, inayotoka kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, imefichwa chini ya pishi. MUNGU atawafanya watu WAKE wawajibike kwa uzembe huu. Hesabu lazima itolewe KWAKE kwa kila mwale wa nuru ambayo imeangazia njia yetu, ikiwa imeboreshwa kwa maendeleo yetu katika mambo ya mbingu au imekataliwa kwa sababu ilikubalika kwao kufuata mwelekeo wa mambo." 5T: 681

"Ushuhuda huu, ukipokelewa utaamsha utendaji, na kusababisha kujishusha, na kukiri dhambi. Shahidi wa Kweli anasema, "Najua kazi zako, ya kuwa hu baridi wala hu moto." Na tena, " Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu." Halafu inakuja ahadi, "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.…. "Makosa na dhambi hizi, ambazo zimewaleta watu wa MUNGU katika hali yao ya unyonge, upofu, na umasikini, lazima zionekane, na zinaamsha toba ya bidii, na kuondoa dhambi hizi ambazo zimewaleta katika hali mbaya sana. hali ya upofu na udanganyifu wa kutisha. Ushuhuda ulio wazi lazima uishi kanisani. Na hii peke yake itajibu ujumbe kwa Walaodikia…. RH, Septemba 16, 1873

"Hatupaswi kuogopa na kuomba msamaha ulimwengu kwa kuwaambia Ukweli: Tunapaswa kudharau kuficha mambo.Dhihirisha rangi zako halisi ili kukidhi mahitaji ya wanadamu na malaika (1Wakor 4:9 kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu). Wacha ieleweke kwamba Waadventista Wasabato hawawezi kufanya mapatano yoyote. Kwa maoni yako na imani yako lazima kusiwe na kuonekana kidogo kwa kutetereka: ulimwengu una haki ya kujua nini cha kutarajia kutoka kwetu. - Sisi ni wamoja katika imani katika Ukweli wa kimsingi wa Neno la MUNGU … Tuna ujumbe kwaajili ya ulimwengu

wote, Amri za MUNGU  na Shuhuda za YESU KRISTO ni mzigo wa kazi yetu Ev: 16 na 179

"Niliichukua Biblia ya thamani na kuizingira kwa Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa, zilizotolewa kwa ajili ya watu wa MUNGU. Hapa, nilisema, kesi za karibu zote zinapatikana. Dhambi wanazopaswa kuacha zimeianishwa. Shauri wanalotaka linaweza kupatikana hapa, likitolewa kwa kesi zingine zinazofanana na wao wenyewe. MUNGU  ameridhika kuwapatia kanuni juu ya kanuni na amri juu ya amri. Lakini si wengi wenu ambao wanajua kwa hakika kile kilichomo katika Shuhuda. Hamyafahamu Maandiko. Laiti mngelifanya Neno la MUNGU kuwa funzo kwenu, kwa shauku ya kufikia kiwango cha Biblia na kufikia ukamilifu wa Kikristo, msingehitaji Shuhuda. Ni kwa sababu mmepuuza kujifunza Kitabu cha MUNGU  kilichovuviwa ndio maana Yeye ametaka kuwafikia kwa ushuhuda rahisi na wa moja kwa moja, akiita usikivu wenu kwenye maneno ya uvuvio ambayo mlikuwa mmepuuza kuyatii, na kuwahimiza kuyatengeneza/kuyaumba maisha yenu kulingana na mafundisho yake safi na yaliyotukuka. {5T 664.3}

"Bwana anakusudia kuwaonya, kuwakaripia, kuwashauri, kupitia shuhuda zinazotolewa, na kuzivutia akili zenu kwa umuhimu wa ukweli wa Neno Lake. Shuhuda zilizoandikwa siyo kutoa nuru mpya, bali kusisitiza kwa uwazi kwenye moyo ukweli wa uvuvio ambao tayari umefunuliwa.Wajibu wa mwanadamu kwa MUNGU na kwa wanadamu wenzake umebainishwa waziwazi katika Neno la MUNGU, lakini ni wachache miongoni mwenu wanaotii nuru iliyotolewa. Ukweli wa ziada haujatolewa; bali MUNGU  kupitia Shuhuda amerahisisha zile Kweli kuu zilizokwisha kutolewa na kwa njia Yake aliyoichagua Mwenyewe kuzileta mbele ya watu ili kuziamsha na kuzivutia akili, ili wote waachwe bila kisingizio. {5T 665.1}

“Kiburi, kujipenda, ubinafsi, chuki, husuda na wivu vimefunika nguvu za ufahamu, na Ukweli, ambao ungewafanya muwe na hekima ili kufikia wokovu, mmepoteza uwezo Wake wa kuvutia na kutawala akili. Kanuni muhimu sana za utauwa hazieleweki kwa sababu hakuna njaa na kiu ya ujuzi wa Biblia, usafi wa moyo, na utakatifu wa maisha. Shuhuda si kwa ajili ya kulidharau Neno la MUNGU, bali kuliinua na kuvutia akili, kwamba usahili mzuri wa Ukweli unaweza kuwavutia wote. {5T 665.2}

"Nilisema zaidi: Kama vile Neno la MUNGU  linavyozingirwa ndani ya vitabu hivi na vipeperushi, ndivyo ambavyo MUNGU  amewawekea ukuta kwa ajili ya maonyo, mashauri, makemeo na kutia moyo. Hapa mlipo mnalia mbele za MUNGU, katika uchungu wa nafsi zenu, kwa ajili ya nuru zaidi. Nimeidhinishwa kutoka kwa MUNGU  kuwaambia kwamba hakuna mwale mwingine wa nuru kupitia Shuhuda utakaoangaza katika njia yenu mpaka muitumie kwa vitendo

nuru iliyokwishatolewa. Bwana amewazingira kwa nuru; lakini hamjaithamini, mmeikanyaga, na wengine wameidharau nuru, wengine wameipuuza au kuifuata lakini kwa kutojali, wachache wameweka mioyo yao kuitii nuru ambayo MUNGU ameridhika kuwapatia. {5T 666.1}

Shuhuda zina Kila mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kuziona uso kwa Uso, Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, "Njoo!" Kila mtu asikiaye hili, na aseme, "Njoo!" Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina

## ASILI YA JUZUU YA 1

MAGOMBO TISA YA SHUHUDA KWA KANISA YANAYOJUMUISHA KURASA 4,738 ZA MAANDIKO, YANAHUSIANA NA MAKALA NA BARUA ZILIZOANDIKWA NA ELLEN G. WHITE, ZILIZOKUWA NA MAELEKEZO, YANAYOHUSIANA NA USTAWI WA KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO. KITINI CHA KURASA KUMI NA SITA, KILICHOTOLEWA DESEMBA 1855, KILIKUWA ASHIRIO LA MWANZO WA MIFUATANO YA MASHAURI AMBAYO MARA KWA MARA ILITOKEA KWENYE VITINI NA VITABU VILIVYOENDELEA KUTOLEWA. JUMBE HIZI KWA KAWAIDA ZILIHUSU HOJA ZILIZOKUWA ZA MOTO-MOTO KWA WAKATI HUO, LAKINI KWA NAMNA FULANI

HATA LEO BADO TUNGALI TUNAKABILIWA NA MATATIZO HAYO HAYO. SISI LEO TUNAKABILIWA NA MATATIZO, HATARI, NA FURSA ZILIZOLIPATA KANISA KATIKA MIAKA YA MWANZO. {1T 5.1}

SHUHUDA ZA KWANZA ZILICHAPISHWA MIAKA KAMA SABA BAADA TU YA KUMBUKUMBU YA "MIKUTANO YA SABATO" YA 1848, WAKATI WAUMINI WA KIADVENTISTA KATIKA MSINGI MPYA ULIOFANYIWA MATENGENEZO UHUSUO UKWELI WA SABATO NA HEKALU TAKATIFU WALIPOWEKA MSINGI KATIKA IMANI ZA MSINGI ZINAZOSHIKWA NA MADHEHEBU YA WAADVENTISTA WA SABATO. KATIKA KIPINDI CHA MIAKA HII MICHACHE, KAZI ILISONGA MBELE KWA NAMNA ILIYO DHAHIRI. MWANZONI KULIKUWA NA WAHUBIRI WATATU AU WANNE, AU "WAJUMBE" KAMA WALIVYOKUWA WAKIJIITA WAKATI HUO, WOTE WAKITEGEMEA KIPATO WALICHOKUWA WANAJIINGIZIA KWA KAZI YA MIKONO YAO NA SADAKA ZA HIARI KUTOKA KWA WAUMINI WACHACHE, AMBAO PIA WALIKUWA MASKINI KATIKA VIPIMO VYA UTAJIRI WA DUNIA HII. MIANZO HII ILIKUWA INAPATIKANA KARIBU NA ENEO LOTE LA MAJIMBO SITA LILIYOJULIKANA KAMA UINGEREZA MPYA PALE KASKAZINI MASHARIKI MWA MAREKANI (Connecticut, Maine, Massachusetts, New Hampshire, Rhode Island, na Vermont). {1T 5.2}

KUFIKIA MWAKA 1855, MWAKA WA UTOAJI WA KITINI CHA USHUHUDA WA KWANZA, KULIKUWA NA KARIBIA WAHUBIRI KAMA KUMI WA UJUMBE WA SABATO NA KUJA KWA YESU MARA YA PILI. IDADI YA WASHIRIKI ILIONGEZEKA KUTOKA CHINI YA WATU MIA MOJA HADI KUFIKIA ELFU MBILI. {1T 5.3}

KAZI YA UCHAPISHAJI, ILIYOANZISHWA NA MZEE WHITE MAJIRA YA JOTO 1849 KATIKA MJI WA MIDDLETOWN, HUKO CONNECTICUT, ILIKUWA IMEFANYIKA KATIKA MAENEO MBALIMBALI CHINI YA MAZINGIRA MAGUMU. SASA MNAMO 1855 ILIANZISHWA KATIKA JENGO LAKE LENYEWE KULE BATTLE CREEK, MICHIGAN. {1T 5.4}

WAKATI UNAOELEZWA NA SHUHUDA 14 ZA KWANZA UNAOPATIKANA SASA KWENYE GOMBO LA 1 ULIKUWA NI MIAKA KUMI NA TATU. TUMEWEKA UZOEFU MCHACHE NA MAENDELEO YALIYOFANYIKA KWA NJIA YA UJUMBE ULIOTOLEWA KATIKA KIPINDI HIKI CHA 1855 HADI 1868. {1T 6.1}

UPUNGUFU WA AWALI, UKENGEUFU NA UPINZANI WA BAADHI YA NDUGU WA AWALI KATIKA HUDUMA, WALIOJULIKANA KAMA WAJUMBE WA UKWELI, VILILETA HUZUNI NA MKANGANYIKO. SHUHUDA ZA KWANZA ZINAZUNGUMZIA KUNDI HILI NA ZINATABIRI ANGUKO LAO LA KASI LITAKALOISHIA KATIKA KUCHANGANYIKIWA. {1T 6.2}

HARAKATI ZA KISHUPAVU, ZENYE MWELEKEO WA KUVUTA NAFSI ZISIZO IMARA KWA SABABU YA MATUMAINI BANDIA YA "UTAKASO," YALIONEKANA KATIKA MAENEO MBALIMBALI, HASA KATIKA BAADHI YA MAJIMBO YA MASHARIKI NA HUKO WISCONSIN. KWENYE MAENEO MENGINE MAFUNDISHO HAYA YALIANDAMANA NA UDHIHIRISHO WA KILE KILICHODHANIWA "KARAMA YA

KUNENA KWA LUGHA.” LAKINI MAFUNDISHO DHAHIRI YALITOLEWA KWA KANISA NAYO YALIIOKOA KAZI KUTOKA KWA UDANGANYIFU WA ADUI. {1T 6.3}

KUPITA KWA MUDA NA KUKAWIA KWA UJIO WA PILI WA KRISTO, NA KUJIUNGA NA KANISA WALE AMBAO HAWAKUWA SEHEMU YA KUNDI LA 1844, PAMOJA NA UTAKASO WA KIROHO WA KINA, VILISABABISHA KUPOTEA KWA UPENDO WA KWANZA. ULIKUWA NI WAKATI WA TETESI KWA WALIO MASHAMBANI NA MAJUMBANI WAKATI MAJIMBO YA MAGHARIBI YAKIWAFUNGULIA MAKABAILA, NA WENGI WAO WAKIWA WAUMINI KUTOKA MAJIMBO YALIYOFURIKA WATU YA MASHARIKI. MAONYO NA MIITO MINGI MIKALI ILITOLEWA KUHUSIANA NA HATARI ILIYOKUWA INAFANANA NA DUNIA IKILINYEMELEA NA KULIITA KANISA KUFANYA UTAKASO WA KINA. {1T 6.4}

KATIKA SEHEMU YA MWISHONI MWA MWAKA 1856, ANGALIZO LILITOLEWA JUU YA UJUMBE WA UFUNUO 3 WA “LAODIKIA” HAPO MWANZO UJUMBE HUU ULIELEWEKA KUWAHUSU WAUMINI WA KIADVENTISTA AMBAO HAWAKUFUATILIA KWA KIREFU NURU ILIYOONGEZEKA YA MALAIKA YULE WA TATU, NA AMBAO WALIJIUNGA PAMOJA NA KUUNDA KANISA JINGINE, WAKIUPINGA KWA NGUVU UKWELI WA SABATO. SASA WALIJIONA WAO WENYEWE KAMA “VUGUVUGU” WANAOHITAJI KUSIKILIZA USHAURI WA SHAHIDI WA KWELI. KWA MIAKA MIWILI AU ZAIDI WAUMINI WALIONGEZEKA NA KUWA NA NGUVU ZAIDI. WAKIWA WAMECHOCHEWA NA UJUMBE HUU, WAKITARAJIA KUWA UTAWAONGOZA MOJA KWA MOJA KWENYE KILIO KIKUU CHA MALAIKA WA TATU. JUMBE NYETI ZILIZO KWENYE SHUHUDA ZINAZOHUSIANA NA HARAKATI HIZI ZINAWEZA KUELEWEKA VIZURI ZAIDI UKIWA NA UELEWA HUU WA KILICHOKUWA KINATOKEA NYUMA YAKE. {1T 6.5}

KILIKUWA NI KIPINDI CHA MAJADILIANO NA MIDAHALO. WACHUNGAJI WETU WENGI WALIPATA CHANGAMOTO ZA KUJADILI SABATO NA KWELI ZINGINE, NA WENGINE WAKIWA WANACHUKUA MISIMAMO MIKALI KATIKA MIJADALA HIYO. JAMBO HILI LILIHITAJI USHAURI KUTOKA MBINGUNI. MMOJA WA WAHUBIRI WETU MAARUFU, MOSES HULL, ALIJIINGIZA KATIKA MIDAHALO NA KUNDI LA WATU WA UMIZIMU, MWANZO AKIWASHAMBULIA NA BAADAYE AKISHAMBULIWA. KAMA MATOKEO YA JAMBO HILI ALISOMBWA KWENYE KUNDI HILI LA UMIZIMU. HAPA NDIPO MAMA WHITE ALIPOCHAPISHA “MAWASILIANO NA MZEE HULL,” AKIANDIKA BARUA ZA WAZI ZILIZOANDIKWA KWAKE MIAKA ILIYOPITA AMBAZO KAMA ZINGEZINGATIWA ZINGEMSAIDIA ASIENDE MRAMA KATIKA IMANI YAKE-ASIVUNJE IMANI. {1T 7.1}

HIYO ILIKUWA NI MIAKA AMBAYO HATUA ZILIKUWA ZINACHUKULIWA KWENYE MUUNDO WA KANISA. DHIDI YA HATUA HII KULIKUWA NA HOFU YA BAADHI YA WALIOPITIA UZOEFU WA UJUMBE WA MALAIKA WA PILI, KWAMBA KUUNDA KANISA ILIKUWA NI ALAMA YA “BABELI.” MASUALA YA MUUNDO KWA NAMNA YALIVYOKUWA YAKIONWA NA KUJADILIWA MIONGONI MWA NDUGU YAMEJIONESHA KATIKA MAWASILIANO YALIYOTOLEWA KWA KANISA NA MAMA

WHITE. NA MNAMO MWAKA 1860 KAZI YA UCHAPISHAJI ILIPOANZA KUFANYIWA MIKAKATI, NA AMBAPO BAADA YA MAJADILIANO MENGI NA MASWALI, JINA LA WAADVENTISTA WA SABATO LILIPOKUBALIKA, KIKUNDI NA JINA LAKE VILIONEKANA KUPATANA NA MAPENZI YA MUNGU. {1T 7.2}

MARA TU BAADA YA HATUA ZA MWISHO KATIKA MAJADILIANO YA MUUNDO WA KANISA KULIKOKAMILISHWA NA UUNDWAJI WA KONFERENCE KUU MAY, 1863 (General Conference of sda), KULIKUJA NJOZI INAYOKUMBUKWA SANA YA OTSEGO MWEZI JUNI, AMBAPO BI WHITE ALIPEWA MAONO YA KANUNI ZILIZOKUJA KUITWA "MATENGENEZO YA AFYA," KUKIWA NA MAFUNUO YA UHUSIANO BAINA YA UTII KWA SHERIA ZA AFYA NA KUFIKIA TABIA ZILIZO ZA LAZIMA KUMFANYA MSHIRIKI WA KANISA AFAE KUCHUKULIWA KWENDA MBINGUNI. KINGINE KILICHOKUWA KARIBU ZAIDI NA HICHO NI MATENGENEZO YA MAVAZI. MIAKA MIWILI BAADAYE, USHAURI ULITOLEWA KUWA "TUNAPASWA KUWA NA NYUMBA YA AFYA YETU WENYEWE," ILIYOPELEKEA KUANZISHWA KWA TAASISI YA MATENGENEZO YA AFYA, AMBAYO NA KUTOKANA NAYO NA KWA AJILI YAKE MASHAURI MENGI YALITOLEWA. KADRI NURU ILIVYOFUATWA, TAASISI HII ILIKUA HATA IKAWA MOJA YA TAASISI BORA ZA AINA YAKE DUNIANI. KATIKA KIPINDI KINACHOELEZWA KWENYE GOMBO HILI, KANUNI ZA UTAWALA ZILIZOPELEKEA MAFANIKIO ZILIUNDWA. MATATIZO YA VITA VYA WANANCHI-WENYEWE KWA WENYEWE, YALIKABILIWA KATIKA KIPINDI HIKI WAKATI WAADVENTISTA WA SABATO WALIPOKABILIWA NA ULAZIMA WA KUUFAFANUA UHUSIANO WAO NA SERIKALI YA WANANCHI WAKATI WA VITA. {1T 7.3}

UMUHIMU WA NYUMBA KWENYE UJENZI WA TABIA ZA KIKRISTO, NA UWAJIBIKAJI WA WAZAZI, VILISISITIZWA, NA JUMBE NYINGI KALI, ZILIZOTOLEWA HASA KWA VIJANA, ZILIPEWA PIA MSISITIZO KATIKA KURASA HIZI. {1T 8.1}

PAMOJA NA MASUALA MAALUM YALIYOFANYIKA KWA KARIBU KATIKA HARAKATI ZA WAKATI HUO, KULIKUWA NA USHAURI MWINGI NA MAKEMEO YA JUMLA JUU YA NIDHAMU YA KANISA NA MAANDALIZI YA KUNYAKULIWA. HIKI KILIKUWA KIPINDI MUHIMU KATIKA MAENDELEO YA KANISA LA WALIOSALIA, NA MASHAURI YA SHUHUDA YALILETA MVUTO MKUBWA WA UUNDAJI WA TABIA. {1T 8.2}

Wadhamini Wa Machapisho Ya Ellen G. White.

## SURA YA 1

## NIKIWA MTOTO MDOGO

Nilizaliwa huko Gorham, Maine, Novemba 26, 1827. Wazazi wangu, Robert na Eunice Harmon, walikuwa wakazi wa jimbo hili kwa miaka mingi. Katika maisha

ya awali walikuwa washiriki wenye wanyofu na bidii na wenye kujitoa wa Kanisa la Methodist Episcopal (mchanganyiko wa Anglican na Methodist, mwanzilishi wake John Wesley alikuwa Mwingereza). Katika kanisa hilo. washiriki walishikamana sana, na kuwa na bidii ya kuongoa wenye dhambi, na kutengeneza mapito ya MUNGU, kwa kipindi cha miaka arobaini. Wakati huu walikuwa na furaha ya kuona watoto wao, wanane wakiwa wote wameongoka na kukusanyika katika zizi la Kristo. Mtazamo wao juu ya ujio wa Kristo mara ya pili ulisababisha kutengwa kwa familia yao kutoka kwa Kanisa la Methodist lenye msimamo mkali, mnamo mwaka wa 1843. {1T 9.1}

Nilipokuwa mtoto, wazazi wangu walihama kutoka Gorham kwenda Portland, Maine, Marekani. Hapa, katika umri wa miaka tisa, ajali ilinitokea ambayo ilikuwa inaenda kuathiri maisha yangu yote. Huku nikiwa nimeandamana na dada yangu pacha na mmoja wa wanafunzi wenzangu nilikuwa nikivuka kama kawaida katika jiji la Portland, wakati msichana aliye na umri wa miaka kumi na tatu, akiwa na hasira juu ya kitu kidogo, alikuwa anatufuatilia huku, akitishia kutupiga. Wazazi wetu walikuwa wametufundisha kamwe kutoshindana na mtu yeyote, lakini ikiwa tulikuwa katika hatari ya kunyanyaswa au kujeruhiwa, basi tuharakishe kurudi nyumbani mara moja. Tulikuwa tukifanya hivyo kwa kasi kubwa kadri tulivyoweza, lakini msichana huyo alitufuata haraka sana, akiwa na jiwe mkononi mwake. Niligeuza kichwa changu kuangalia yupo umbali wa kiasi gani na wakati nikifanya hivyo, alitupa jiwe, na likanigonga puani. Nilishikwa na butwaa kwa kipigo hicho na nikaanguka hoi chini, na kuishiwa na fahamu. {1T 9.2}

Fahamu ziliporudi, nilijikuta katika duka la mfanyabiashara; nguo zangu zikiwa zimetapakaa damu, ambayo ilikuwa ikimiminika toka puani mwangu na kutiririkia sakafuni. Mgeni mkarimu alijitolea kunipeleka nyumbani kwa gari lake la kukokotwa na farasi, lakini mimi, bila kutambua udhaifu niliokuwa nao, nikamwambia napendelea niende nyumbani mwenyewe nisije nikachafua gari lake kwa damu zangu. Wale waliokuwepo hawakujua kuwa jeraha langu lilikuwa kubwa sana, na waliniruhusu nifanye kama nilivyotaka; lakini baada ya kutembea hatua chache tu, nilisikia kizunguzungu na kisha nikazimia. Dada yangu pacha na mwanafunzi mwenzangu walinibeba kuelekea nyumbani. {1T 10.1}

Sikumbuki chochote baada ya hapo kwa muda fulani, baada ya ajali ile. Mama yangu aliniambia kuwa sikuwa natambua chochote, bali nililala usingizi kwa majuma matatu mfululizo. Hapakuwa na mtu aliyedhani kuwa ningeweza kupona ila yeye [mama] kwa namna fulani alihisi kuwa ningeishi. Jirani mwema, ambaye alikuwa akipendezwa nami sana, wakati mmoja alidhani nilikuwa nakufa. Alitamani kuninunulia joho la mazishi (sanda), lakini mama yangu akamwambia, bado, subiri kwanza; kwani kitu fulani kilikuwa kinamwambia kuwa sitakufa. {1T 10.2}

Wakati nilipoamka tena na kupata fahamu, ilionekana kwangu kuwa nilikuwa nimelala. Sikuwa nakumbuka kuhusu ajali, na wala sikujua sababu ya ugonjwa wangu. Kadri nilivyoendelea kupata nguvu kidogo, udadisi wangu uliamshwa nilipowasikia watu wakisema, "Inasikitisha sana!" "Sikuweza kumtambua, masikini, ingekuwa bora nisingemjua," nk. Niliomba niletewe kioo na nilipojichungulia nilipata mshtuko na mabadiliko ya sura yangu. Kila kipengele cha uso wangu kilionekana kubadilishwa. Mifupa ya pua yangu ilikuwa imevunjika, ambayo ilisababisha shepu ya uso iharibike (disfigurement). {1T 10.3}

Wazo la kubebana na mkosi wangu maisha yangu yote halikuungwa mkono na hisia zangu. Sikuweza kuona raha katika kuishi kwangu. Sikupenda kuishi, lakini pia niliogopa kufa, maana nilikuwa sijajiandaa. Marafiki ambao walitutembelea walininitazama kwa sikitiko/huruma, na wakawashauri wazazi wangu wamshtaki baba wa msichana yule ambaye, kama walivyosema wenyewe, alikuwa ameniharibu. Lakini mama yangu alikuwa mpenda amani; yeye alisema kama jambo hilo lingeweza kunirudishia afya na mwonekano wa asili, pangekuwa na kitu ambacho kingepatikana; lakini kwa kuwa jambo hilo halingewezekana, basi haikuwa busara kutengeneza maadui kwa kufuata ushauri kama huo. {1T 10.4}

Matabibu walidhani kwamba waya wa madini ya fedha ungeweza kuwekwa puani mwangu ili kuishikilia pua. Jambo hili lingekuwa lenye kuleta uchungu sana, na waliogopa huenda lingekuwa na manufaa kidogo sana, kwani nilikuwa nimepoteza damu nyingi na kupata mshtuko wa neva, hata kupona kwangu kulikuwa na mashaka sana. Hata kama ningerejea kwenye afya yangu, kwa maoni yao ilionekana ningeweza kuishi kwa muda mfupi tu. Nilikuwa nimekonda na kubakia mifupa. {1T 11.1}

Wakati huu nilianza kumwomba Bwana aniandae kwa ajili ya kifo. Marafiki Wakristo walipotembelea familia yangu, wangeweza kumuuliza mama yangu ikiwa alikuwa amezungumza nami juu ya kufa. Nilisikia mazungumzo hayo, na yalinizindua. Nilitamani kuwa Mkristo, na niliomba kwa dhati na bidii msamaha wa dhambi zangu. Nilihisi amani ya akili ikija moyoni, na nikampenda kila mtu, nikitamani kuwa wote wangesamehewa dhambi zao na wampende Yesu kama ilivyo kwangu. {1T 11.2}

Nakumbuka vizuri usiku mmoja katika kipindi cha baridi wakati theluji ilipokuwa imedondoka ardhini, mbingu zilikuwa angavu, anga likionekana kuwa jekundu na lililonuna kwa hasira, na likionekana kufunguka na kufungwa, wakati theluji ilionekana kama damu. Majirani waliogopa sana. Mama alinibeba kwa mikono yake kutoka kitandani na kunibeba hadi dirishani. Nilifurahi; Nilidhani Yesu anakuja, na nilitamani kumwona. Moyo wangu ulikuwa umejaa; Nilipiga makofi kwa furaha, na nilifikiri mateso yangu yamefika mwisho wake.

Lakini nilikata tamaa; muonekano ule ulififia na kutoweka mbali na mbingu, na asubuhi iliyofuata jua lilichomoza kama kawaida. {1T 11.3}

Nilipata nguvu polepole sana. Nilipoweza kushiriki kucheza na marafiki zangu wadogo, nililazimika kujifunza somo chungu kwamba mwonekano wetu wa nje, kama sura zetu, mara nyingi huleta tofauti ya vile tunayotendewa na wenzetu. Wakati wa matukio haya yenye huzuni, baba yangu alikuwa safarini huko Georgia. Aliporudi, alimkumbatia kaka na dada zangu, na kisha akaulizia nilipo. Kwa aibu nilijivuta nyuma na ndipo mama yangu akanitambulisha kwa kuninyoshea kidole, lakini baba yangu mwenyewe hakunitambua. Ilikuwa vigumu kwake kuamini kwamba mimi ni Ellen binti yake mdogo, ambaye alikuwa amemwacha miezi michache tu akiwa mtoto mwenye afya, na mwenye furaha. Jambo hili liliumiza sana hisia zangu, lakini nilijaribu kujifanya nionekane mchangamfu, ingawa moyo wangu ulionekana kuvunjika. {1T 11.4}

Mara nyingi katika siku hizo za utoto nilifanywa kuhisi hali yangu hiyo mbaya. Hisia zangu zilikuwa kali isivyo kawaida na zilinisababishia hali ya kutokuwa na furaha. Mara nyingi nikiwa na kiburi kilichojeruhiwa, roho mbaya na mnyonge, nilitafuta mahali pa upweke na kutafakari kwa kina juu ya majaribu ambayo nililazimika kuyapitia kila siku. {1T 12.1}

Nilinyimwa faraja ya machozi. Sikuweza kulia kwa urahisi, kama vile dada yangu pacha; ingawa moyo wangu ulikuwa mzito, wenye maumivu kwa uchungu, na kama unaovunjika, bado sikuweza kutoa machozi. Mara nyingi nilihisi kuwa kulia kungeweza kunipunguzia maumivu na huzuni zangu. Wakati mwingine huruma njema ya marafiki zangu ilifukuza giza langu na kuliondoa, kwa muda, mzigo nzito uliokuwa unaukandamiza moyo wangu. Raha za dunia zilionekana bure na tupu jinsi gani kwa wakati huo! Urafiki wa vijana wenzangu ulikuwa ukibadilika sana! Hata hivyo hawa wanafunzi wenzangu wa shule hawakuwa tofauti na watu wengi wa hapa ulimwenguni. Uso mzuri, mavazi mazuri, huwavutia; lakini wacha misiba iondoe haya, ule urafiki usio imara huganda kwa ubaridi na huvunjika. Lakini nilipomgeukia Mwokozi wangu, Naye Alinifariji. Nilimtafuta Bwana kwa dhati na bidii katika shida yangu, na nikapata faraja. Nilihisi kuwa na hakika kwamba Yesu ananipenda hata mimi. {1T 12.2}

Afya yangu ilionekana kuharibika bila matumaini. Kwa miaka miwili sikuweza kupumua kupitia pua yangu, na niliweza kwenda shule lakini mara chache sana. Ilionekana ingekuwa vigumu kwangu kusoma na kubaki na yale niliyojifunza. Msichana yule yule ambaye alikuwa sababu ya msiba wangu aliteuliwa na mwalimu wetu kuwa kiranja wa darasa na mojawapo ya majukumu yake ilikuwa ni kufuatilia na kunisaidia katika uandishi wangu na masomo mengine. Mara nyingi alionekana kujuta kwa dhati kwa jeraha kubwa alilonisababishia, ingawa nilikuwa mwangalifu kutomkumbusha juu ya tukio hilo. Alikuwa mpole na mvumilivu kwangu, na alionekana mwenye huzuni na mwenye mawazo wakati

aliponiona nikifanya juhudi katika mazingira magumu ili kupata elimu. {1T 12.3}

Mfumo wangu wa neva ulidhoofika, na mkono wangu ulitetemeka kiasi kwamba nilikuwa na maendeleo hafifu katika kuandika na kufanikiwa kupata nakala chache zilizotokana na maandishi yangu ya mkono. Nilipojitahidi kuelekeza akili yangu kwenye masomo yangu, maandishi kwenye karatasi yalionekana kama yanayokimbia pamoja, matone makubwa ya jasho yakining'inia juu ya uso wangu, na huku hali ya kuzimia na kizunguzungu vikinikamata. Nilikuwa na kikohozi kibaya, na mfumo wangu wote ulionekana kudhoofika. Waalimu wangu walinishauri niache shule na nisiendelee na masomo yangu zaidi hadi afya yangu itakapokuwa bora. Lilikuwa pambano gumu sana katika maisha yangu ya ujana kukubaliana na udhaifu wangu na kuamua kwamba lazima niachane na masomo yangu na kupoteza kabisa tumaini la kupata elimu. {1T 13.1}

Miaka mitatu baadaye nilijaribu tena kupata elimu. Lakini nilipojaribu kuendelea na masomo yangu, afya yangu ilidhoofika haraka, na ikaonekana kuwa ikiwa ningebaki shuleni, ingekuwa kwa gharama ya maisha yangu. Sikuhudhuria shule baada ya kuwa na umri wa miaka kumi na mbili. {1T 13.2}

Matamanio yangu ya kuwa msomi yalikuwa kubwa sana, na wakati nilipotafakari juu ya matumaini yangu yaliyovunjiliwa mbali, na mawazo kwamba ningekuwa mtu nisiye na thamani kwa maisha yangu yote kwaajili ya ulema, sikuweza kumwelewa MUNGU na wakati mwingine nilinung'unikia namna MUNGU alivyoruhusu niteseke. Laiti ningemfungulia mama yangu mawazo yangu, angeliweza kunielekeza, kunituliza, na kunitia moyo; lakini nilificha hisia zangu zenye shida kutoka kwa familia na marafiki zangu, nikihofia kwamba wasingeweza kunielewa. Imani ya furaha katika upendo wa Mwokozi wangu niliyokuwa ninaifurahia wakati wa ugonjwa wangu ilikuwa imekwisha. Matarajio yangu ya raha ya ulimwengu yalififia, na mbingu zilionekana kufungwa dhidi yangu. {1T 13.3}

## SURA YA 2

## WONGOFU WANGU.

Mnamo Machi, 1840, William Miller alitembelea Portland, Maine, na kutoa kozi ya mafunzo yake ya kwanza juu ya ujio wa pili wa Kristo. Hotuba hizi zilileta msisimko mkubwa, na kanisa la Kikristo kwenye Mtaa wa Casco, mahali ambapo hotuba hizi zilitolewa na Miller, lilikuwa linashonana usiku na mchana. Hakuna msisimko kama wa wendawazimu ulioandamana na mikutano hiyo, lakini kujitoa wakfu kwa umakini kulijaa akilini mwa wale waliosikia. Siyo tu shauku kubwa ilidhihirishwa katika mji huo, bali pia watu wa vijijini pia walimiminika

siku baada ya siku, wakileta vikapu vyao vya chakula cha mchana, na kubakia hapo tangu asubuhi hadi mwisho wa mkutano wa jioni. {1T 14.1}

Nikiwa na marafiki zangu, nilihudhuria mikutano hii na nilisikiliza tangazo la kushitusha kuwa Kristo alikuwa anakuja mnamo 1843, miaka michache tu! Bwana Miller alifuatilia unabii huo kwa usahihi, ambao uligusa usadikisho kwa mioyo ya wasikilizaji wake. Alikita kwenye kufundisha juu ya vipindi vya unabii, na kuleta uthibitisho mwingi kuimarisha msimamo wake. Halafu miito yake mikali na yenye nguvu na ushauri wake kwa wale ambao hawakuwa wamejiandaa, iliuteka ule umati na kuwafanya kama waliotekewa (Alikuwa anasoma Danieli, na Ufunuo, mfano Danieli 8:14). {1T 14.2}

Mikutano maalum iliandaliwa ambapo wenye dhambi wangeweza kupata fursa ya kumtafuta Mwokozi wao na kujiandaa kwa matukio ya kutisha ambayo yangetokea hivi karibuni. Hofu na usadikisho vilienea katika jiji lote. Mikutano ya maombi ilianzishwa, na kulikuwa na mwamko wa jumla kati ya madhehebu mbali mbali; kwani wote walihisi zaidi au kidogo ushawishi uliotokana na mafundisho ya kuja karibu kwa Kristo. {1T 14.3}

Wakati wenye dhambi walioketi vitini mwao wakijawa na wasiwasi walipoalikwa kuja mbele, mamia waliitikia wito; na mimi, nikiwa kati ya hao, nilijipenyeza katika umati na nikachukua nafasi yangu na watafutaji wa Ukweli. Lakini moyoni mwangu kulikuwa na hisia kwamba nisingeweza kamwe kustahili kuitwa mtoto wa MUNGU. Ukosefu wa kujiamini mwenyewe, na kusadiki kuwa isingewezekana kumfanya mtu yeyote aelewe hisia zangu, kulinizuia kutafuta ushauri na msaada kutoka kwa marafiki zangu Wakristo. Hivyo nilitangatanga bila sababu gizani katika kukata tamaa, wakati wao, bila kuingia kwenye hisia zangu za ndani kwa kuwa nilizificha, wakawa hawajui kabisa hali yangu halisi. {1T 14.4}

Jioni moja ndugu yangu Robert na mimi tulikuwa tunarudi nyumbani kutoka kwenye mkutano ambapo tulikuwa tumesikiliza hotuba ya kupendeza juu ya utawala wa Kristo unaokaribia duniani, ikifuatiwa na ombi na wito wa dhati na ari kwa Wakristo na watenda dhambi, ukiwasihi wajiandae hukumu na kuja kwa Bwana. Nafsi yangu ilikuwa imechochewa ndani yangu na yale niliyosikia. Na ilikuwa ya kina sana, hisia ya kusadisha moyoni mwangu, hata niliogopa kwamba Bwana hataweza kunihurumia nifike nyumbani. {1T 15.1}

Maneno haya yalizidi kusikika masikioni mwangu: "Siku kuu ya Bwana imekaribia! Ni nani atakayeweza kusimama Yeye atakapotokea!" Lugha ya moyo wangu ilikuwa: "Nihurumie na kuniepusha ee Bwana usiku kucha! Usinichukue katika dhambi zangu, nirehemu, niokoe!" Kwa mara ya kwanza nilijaribu kuelezea hisia zangu kwa kaka yangu Robert, ambaye alikuwa amenizidi kwa umri wa miaka miwili; Nilimwambia kuwa nisingethubutu kupumzika wala kulala mpaka nijue kwamba MUNGU  alikuwa amenisamehe dhambi zangu. {1T 15.2}

Kaka yangu hakujibu mara moja, lakini sababu ya ukimya wake ilikuwa dhahiri kwangu; alikuwa akilia kwa huruma kutokana na shida yangu. Hii ilinitia moyo kumwamini zaidi, na kumwambia siri yangu, kwamba nilikuwa nikitamani kifo katika siku ambazo maisha yalionekana kuwa mzigo mzito kwangu kuweza kuubeba; lakini sasa mawazo ya kwamba nitaweza kufa katika hali yangu ya sasa ya dhambi na kupotea milele, ilinijaza hofu kubwa. Nilimwuliza ikiwa anadhani MUNGU angeweza kuepusha maisha yangu kwa usiku huo mmoja, ikiwa kama ningeutesa moyo wangu katika kufanya maombi kwake. Alijibu: "Nadhani atafanya kama utamuomba kwa imani, nami nitakuombea na nitajiombea mimi mwenyewe pia. Ellen, hatupaswi kusahau maneno tuliyoyasikia usiku huu." {1T 15:3}

Nilipofika nyumbani, nilitumia saa nyingi za giza katika kuomba kwa machozi. Sababu moja ambayo ilinisababisha kuficha hisia zangu kutoka kwa marafiki zangu ni kuogopa kusikia neno la kukatisha tamaa. Tumaini langu lilikuwa dogo sana, na imani yangu ilikuwa dhaifu sana, kiasi kwamba niliogopa iwapo mtu mwingine angechukua mtazamo kama huo wa hali yangu, ingenitumbukiza katika hali mbaya zaidi ya kukata tamaa. Hata hivyo nilitamani mtu aniambie ni nini nifanye ili niokolewe, na ni hatua gani ninazopaswa kuchukua kukutana na Mwokozi wangu na kujitoa kabisa kwa Bwana. Niliona ni jambo kubwa kuwa Mkristo, na nilihisi kwamba zinahitajika juhudi za kipekee kwa upande wangu. {1T 16.1}

Akili yangu ilibaki katika hali hii kwa miezi. Kwa kawaida nilikuwa nimehudhuria mikutano ya Wamethodisti nikiwa na wazazi wangu; lakini tangu nipendezwe na ujumbe wa kuonekana kwa Kristo hivi karibuni, nilikuwa nimehudhuria mikutano kwenye Mtaa wa Casco. Majira ya joto yaliyofuata wazazi wangu walienda kwenye mkutano wa makambi ya Wamethodisti huko Buxton, Maine, wakinichukua na mimi. Niliazimia kabisa kumtafuta Bwana kwa bidii nikiwa huko, na kupata, ikiwa ingewezekana, msamaha wa dhambi zangu. Kulikuwa na hamu kubwa moyoni mwangu kutokana na lile tumaini la Mkristo na ile amani ipatikanayo kwa njia ya kuamini. {1T 16.2}

Nilitiwa moyo sana wakati niliposikiliza hotuba kutoka kwenye maneno, "nitaingia kwa mfalme," "nami nikiangamia, na niangamie." Katika matamshi yake mzungumzaji alirejelea wale ambao walikuwa wakitetemeshwa na kumangamanga kati ya tumaini na hofu, wakitamani kuokolewa kutoka katika dhambi zao na kupokea upendo wa msamaha wa Kristo, lakini wakiwa wameshikwa na mashaka na utumwa wa woga, na kuhofia kutofaulu. Aliwashauri watu hao kujisalimisha kwa MUNGU, na kujitosa katika rehema Yake bila kuchelewa. Wangempata Mwokozi mwenye neema aliye tayari kuwakabidhi fimbo ya enzi ya huruma, hata Ahasuero alipompa Esta ishara ya neema yake. Yote yaliyohitajika kwa mwenye dhambi, akitetemeka mbele ya Bwana wake, ilikuwa ni kuweka mkono wa imani na kugusa fimbo ya neema na fadhila Yake. Mguso huo ulinihakikishia msamaha na amani. {1T 16.3}

Wale waliokuwa wakingojea kujifanya wanaostahili zaidi neema ya Kiungu kabla ya kujitosa na kudai ahadi za MUNGU, walikuwa wakifanya makosa mazito na ya kufisha. Yesu peke yake Ndiye asafishaye dhambi; Yeye tu Ndiye awezaye kusamehe makosa yetu. Yeye Ameahidi kusikiliza maombi na kuwapatia yale waliyomuomba wale wanaomjia kwa imani. Wengi walikuwa wanajua kwa udogo sana, nao walifikiri ni lazima wafanye juhudi zao ili kupata kibali cha MUNGU. Lakini hali yoyote ile ya mwanadamu kujitegemea wenyewe ni kazi bure. Ni kwa kuungana tu na Yesu kwa njia ya imani ndipo mwenye dhambi anapoweza kuwa mtoto wa MUNGU, mwenye matumaini, na anayeamini. Maneno haya yalinifariji na kunipa maono ya kile ambacho ni lazima nikifanye ili niweze kuokoka. {1T 16.4}

Sasa nilianza kuona njia yangu iliyo wazi zaidi, na giza likaanza kutoweka. Nilitafuta msamaha wa dhambi zangu kwa dhati na bidii, na nilijitahidi kujitoa kabisa kwa Bwana. Lakini akili yangu mara nyingi ilikuwa katika mfadhaiko mkubwa kwa sababu sikupata furaha ya kiroho na msisimko ambao nilifikiri ingekuwa ushahidi wa kukubaliwa kwangu na MUNGU, na sikuthubutu kujiaminisha kuwa nimeongoka bila kuhisi kuwepo kwa hali hiyo. Nilihitaji maelekezo kwa kiasi gani kuhusu unyenyekevu wa jambo hili! {1T 17.1}

Nikiwa nimeinama madhabahuni pamoja na wengine ambao walikuwa wakimtafuta Bwana, lugha yote ya moyo wangu ilikuwa: "Nisaidie, Yesu, niokoe la sivyo nitaangamia! Sitaacha kuomba hadi sala yangu itakaposikiwa na dhambi zangu zitakaposamehewa!" Nilihisi hali yangu ya uhitaji, isiyo na msaada kuliko ilivyokuwa hapo awali. Nikiwa nimepiga magoti na kuomba, ghafla mzigo wangu uliondoka, na moyo wangu ukawa mwepesi. Mwanzoni hisia ya wasiwasi ilinijia, na nilijaribu kuanza tena kubeba mzigo wangu wa dhiki. Ilionekana kwangu kuwa sikuwa na haki ya kujisikia mwenye shangwe na nderemo. Lakini Yesu alionekana kuwa karibu sana nami; Nilihisi kuweza kumjia na huzuni zangu zote, misiba, na majaribu, kwa namna ile ile wahitaji walivyomjia ili kupata unafuu wakati akiwa hapa duniani. Kulikuwa na uhakika moyoni mwangu kwamba Yeye aliyaelewa majaribu yangu ya kipekee na alinihurumia. Siwezi kamwe kusahau uhakikisho huu wa thamani wa huruma ya Yesu kwa yule aliyeonekana kutofaa kabisa hata kuangaliwa Naye. Niliielewa kwa kina zaidi tabia ya Kiungu ya Kristo katika kipindi hiki kifupi nikiwa nimeinama kati ya wale wanaoomba kuliko nilivyoielewa hapo awali. {1T 17.2}

Mmoja wa akina mama katika Israeli alikuja kwangu na kuniambia: "Mpendwa mtoto, Je, umempata Yesu?" Nilikuwa karibu kujibu, "Ndiyo," wakati yeye aliponiambia: "Kwa kweli unaye, wewe umempata, Amani yake iko pamoja nawe, naiona katika uso wako!" Tena na tena nilijiambia mwenyewe: "Je! Hii yaweza kuwa ndiyo dini? Je, sikukosea?" Ilionekana kuwa kubwa sana kwangu kuweza kuidai, ilikuwa ni fursa iliyoinuliwa sana. Ingawa nilikuwa mwoga sana kukiri hadharani, nilihisi kwamba Mwokozi alikuwa amenibariki na kunisamehe dhambi zangu. {1T 18.1}

Mara tu baada ya hili, mkutano ulifungwa, na tukaanza kurudi nyumbani. Akili yangu ilijaa mahubiri, mashauri, na maombi tuliyoyasikia. Kila kitu katika uumbaji kilionekana kubadilika. Katika kipindi cha mkutano, mawingu na mvua zilitawala sehemu kubwa ya wakati, na hisia zangu zilikuwa zikipatana na hali ya hewa. Sasa jua liliangaza kwa mwanga mkali na ulio wazi, na likaijaza dunia kwa nuru na joto. Miti na nyasi vilikuwa kijani kibichi kipya zaidi, na mbingu ikiwa bluu zaidi. Dunia ilionekana kutabasamu chini ya amani ya MUNGU. Kwa hivyo miale ya Jua la Haki ilikuwa imepenya kwenye mawingu na giza la akili yangu, na kuondoa utusitusi wake.{1T 18.2}

Ilionekana kwangu kana kwamba kila mtu lazima awe na amani na MUNGU  na kuhuishwa na Roho WAKE. Kila kitu ambacho macho yangu yalikiangalia kilionekana kuwa na mabadiliko. Miti ilikuwa mizuri zaidi na ndege waliimba nyimbo kwa utamu zaidi ya hapo awali; ilielekea kwamba yote haya yanamsifu Muumba katika nyimbo zake. Sikuogopa kuongea, kwa kuhofia furaha hii isije ikayoyoma, na kisha nipoteze ushahidi muhimu wa upendo wa Yesu kwangu. {1T 18.3}

Tulipokaribia nyumba yetu huko Portland, tuliwakuta watu wanaofanya kazi barabarani. Walikuwa wakiongea wao kwa wao juu ya mada za kawaida, lakini masikio yangu yalikuwa kiziwi kwa kila jambo isipokuwa sifa ya MUNGU, na maneno yao yalinijia kama shukrani na hosana zenye furaha. Nikamgeukia mama yangu, nikasema: "Kwa nini, watu hawa wote wanamsifu MUNGU, na hawajaenda kwenye mkutano wa makambi." Sikuelewa wakati huo ni kwa nini machozi yalikusanyika machoni pa mama yangu, na tabasamu nyororo liliangaza uso wake, aliposikiliza maneno yangu rahisi ambayo yalikumbusha uzoefu kama wake mwenyewe. {1T 18.4}

Mama yangu alikuwa mpenda maua na alifurahi sana kuyalima na kwa hivyo kuifanya nyumba yake ipendeze na kupendwa na watoto wake. Lakini bustani yetu ilikuwa haijawahi kuonekana nzuri sana kwangu kama siku hiyo niliporudi. Nilitambua kielelezo cha upendo wa Yesu katika kila kichaka, katika kila chipukizi, na katika kila maua. Vitu hivi vya urembo vilionekana kuongea kwa lugha bubu ya upendo wa MUNGU. {1T 19.1}

Kulikuwa na ua zuri la waridi kwenye bustani liitwalo Sharon. Nakumbuka nililikaribia na kugusa vikonyo vyake dhaifu kwa heshima; vilionekana kumiliki utakatifu machoni pangu. Moyo wangu ulifurika upole, moyo uliolainika na mwororo na upendo kwa uumbaji huu mzuri wa MUNGU. Niliweza kuona ukamilifu wa Mwenyezi Mungu katika maua yaliyopamba dunia. MUNGU aliyachunga, kwa macho yake yenye kuona yote yaliyokuwa juu yao. Alikuwa ameyaumba na kutamka ‘tazama ni mema sana’. {1T 19.2}

"Ah," nilitafakari, "ikiwa Yeye anayapenda sana na kuyajali maua ambayo ameyapamba kwa uzuri, ni kwa moyo mwororo zaidi kiasi gani Yeye atawalinda watoto ambao wameumbwa kwa mfano Wake." Nilirudia kwa upole maneno

hayo nikijiambia mimi mwenyewe: "Mimi ni mtoto wa MUNGU, utunzaji WAKE wa upendo uko karibu nami. Mimi nitakuwa mtiifu na sitamchukiza kwa namna yoyote ile, bali nitalisifu Jina Lake pendwa na kumpenda Yeye daima." {1T 19.3}

Maisha yangu yalitokezea kwa njia nyingine. Mateso yaliyokuwa yametia giza utotoni mwangu yalionekana kutumika kwa rehema kwa faida yangu, yakigeuza moyo wangu kutoka kwa ulimwengu na raha zake zisizoridhisha moyo, na kuuelekeza kwenye vivutio vya kudumu vya mbinguni. {1T 19.4}

Mara tu baada ya kurudi kutoka kwenye mkutano wa makambi, mimi, pamoja na wengine kadhaa, tulipelekwa kanisani kwa kipindi cha angalizo/majaribio IProbationI. Akili yangu ilikazwa sana juu ya somo la ubatizo. Japokuwa nilikuwa mchanga, nilikuwa naiona njia moja tu ya ubatizo iliyoidhinishwa na Maandiko, na hiyo ilikuwa ni ile ya kuzamishwa majini. Baadhi ya dada zangu wa Methodisti walijaribu bila mafanikio kunishawishi kwamba kunyunyiza ulikuwa ubatizo wa Biblia. Mchungaji wa Methodist alikubali kuwatumbukiza majini wataradhia ikiwa wangependelea njia hiyo kutoka kwenye dhamiri zao, ingawa bado alishikilia kuwa kunyunyiza lingekuwa jambo linalokubalika kwa MUNGU sawa na kuzamishwa. {1T 19.5}

Hatimaye muda mahsusi ukapangwa sisi kupokea agizo hili la Bwana lililo adhimu. Ilikuwa siku ya upepo mwingi wakati sisi, watu kumi na wawili kwa idadi yetu, tuliposhuka baharini ili kubatizwa. Mawimbi yalizidi kwenda juu na kujitupa kwa nguvu pwani; lakini nilipochukua msalaba huu mzito, amani yangu ilikuwa kama mto. Nilipopanda kutoka majini, nguvu zangu zimekaribia kwisha, kwani nguvu ya Bwana ilikuwa juu yangu. Nilihisi kuwa tangu sasa sikuwa wa ulimwengu huu, bali nilikuwa nimepanda kutoka kwenye kaburi lenye maji na kuingia katika upya wa maisha. {1T 20.1}

Siku hiyo hiyo alasiri nilipokelewa kanisani kwa ushirika kamili. Binti muumini mchanga aliyepata idhini ya kujiunga na kanisa kwa njia ya ubatizo pamoja nasi, alisimama kando yangu. Akili yangu ilikuwa na amani na furaha mpaka nilipoona pete za dhahabu zikimetameta juu ya vidole vya dada huyu, na heleni kubwa, zikining'inia masikioni mwake. Kisha nikagundua kwamba kofia yake ilipambwa kwa maua bandia, na kuzungushiwa na utepe wa gharama kubwa uliopambwa kwa mtindo maalum kama upinde na viputo. Furaha yangu ilipunguzwa na jambo hili la ubatili nililoliona kwa yule aliyedai kuwa ni mfuasi wa Yesu aliye mpole na mnyenyekevu. {1T 20.2}

Nilitarajia kwamba mchungaji angempatia karipio kwa kumnong'oneza au kumpa ushauri dada huyu; lakini ilikuwa dhahiri kuwa hakujali mwonekano wa mavazi yake ya kujionyesha, na hapakuwa na karipio lolote lililotolewa. Sote tulipokelewa kwa kushikwa mkono wa kulia wa ushirika. Mkono uliopambwa kwa vito ulishikwa na wawakilishi wa Kristo, na majina yetu yote yakaingizwa kwenye kitabu cha ushirika cha kanisa. {1T 20.3}

Hali hii ilinisumbua sana na kunitia majaribuni hasa nilipokumbuka maneno ya mtume, “Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri/kujistahi, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani.” Mafundisho ya Maandiko haya yalionekana kupuuzwa waziwazi na wale ambao niliwachukulia kama Wakristo waliojitoa wakfu, na ambao walikuwa na uzoefu mkubwa kuliko wangu. Kama ni kweli kuiga mavazi ya kupindukia ya walimwengu, ilikuwa ni dhambi kama nilivyodhani, hakika Wakristo hawa walipaswa kulielewa hilo na kufuata kile kiwango kilichowekwa na Biblia. Hata hivyo niliazimia kufuata usadikisho wa dhamira yangu na kutimiza wajibu wangu. Nilihisi ilikuwa ni kinyume na roho ya injili kutumia wakati na mali tulizopewa na MUNGU kujipamba wenyewe na kwamba unyenyekevu na kujinyima vingekuwa vipengele vyenye kutufaa zaidi sisi ambao dhambi zetu ziligharimu kafara isiyo na kipimo ya Mtoto wa MUNGU. {1T 20.4}

## SURA YA 3

## HISIA ZA KUKATA TAMAA

Mnamo Juni, 1842, Bwana Miller alitoa kozi yake ya pili ya mihadhara huko Portland. Nilihisi ni fursa kubwa kuhudhuria mihadhara hii, kwani nilikuwa nimevunjika moyo na sikujisikia tayari kukutana na Mwokozi wangu. Hotuba hii ya pili ilileta msisimko zaidi katika jiji kuliko ile ya kwanza. Madhehebu mengi yalifunga milango ya makanisa yao dhidi ya Bwana Miller, hivyo yalibaki madhehebu machache tu yenye milango wazi kwake. Hotuba nyingi kutoka kwenye mimbari mbalimbali zilitaka kufichua kile walichodai ni makosa ya ushupavu wa mhadhiri; lakini umati wa wasikilizaji wenye tashwishwi

walihudhuria mikutano yake, wakati wengi hawakuweza kuingia ndani ya jumba hilo. {1T 21.1}

Umati ulikuwa na ukimya na umakini usio wa kawaida. Njia yake ya kuhubiri haikuwa ya madoido, kupamba-pamba au umbuji, lakini alishughulikia Ukweli kwa uwazi na kutoa habari halisi za kushangaza ambazo ziliwaamsha wasikilizaji wake kutoka kwenye uzembe wao wa kutojali. Aliunga mkono matamshi yake na nadharia zake kwa uthibitisho wa Maandiko wakati anaendelea. Nguvu inayoshawishi iliongoza maneno yake ambayo ilionekana kuyapiga muhuri kama lugha ya Ukweli. {1T 21.2}

Alikuwa mwenye adabu, mwungwana, anayejistahi na mwenye huruma. Wakati kila kiti ndani ya nyumba kilipokuwa kimekaliwa, na jukwaa na maeneo karibu na mimbari yakionekana kufurika, nilimuona akiondoka kwenye dawati na kutembea kwenye nafasi ya wazi, akimshika mkono mzee wa kiume au wa kike aliye dhaifu na kumtafutia kiti, kisha akarudi na kuendelea na mazungumzo yake. Hakika ndiyo maana aliitwa kiusahihi baba Miller, kwani alikuwa na uangalizi mzuri juu ya wale waliokuwa chini ya huduma zake, alikuwa mwenye upendo kwa watu, akionyesha mapenzi yake kwao, mwenye tabia ya kirafiki na moyo mwororo. {1T 21.3}

Alikuwa mzungumzaji wa kuvutia, na mawaidha yake, kwa wale wanaodai kuwa ni Wakristo na hata kwa wale wasio na toba, yalikuwa sahihi na yenye nguvu. Wakati mwingine utulivu wa kicho wenye kuleta maumivu ya ndani vilitamalaki, kwenye mikutano yake. Wengi walijitoa kutokana na usadikisho wa ROHO WA MUNGU. Waume wenye nywele zenye mvi na wanawake wazee wenye mwendo wa kutetemeka walitafuta viti vya kuketi kwa shauku. Wale walio na nguvu ya ukomavu, vijana na watoto, walitekewa sana. Miguno na sauti ya kulia na ya kumsifu MUNGU vilichanganyika kwenye madhabahu ya sala. {1T 22.1}

Niliamini maneno haya mazito yaliyonenwa na mtumishi wa MUNGU, na moyo wangu uliumia wakati yalipopingwa au kufanywa ionekane ni mada ya mzaha. Mara kwa mara nilihudhuria mikutano, na niliamini kwamba Yesu alikuwa karibu kuja katika mawingu ya mbinguni; lakini wasiwasi wangu mkubwa ulikuwa kuwa tayari kukutana naye. Akili yangu ilikaa kila wakati juu ya mada ya utakatifu wa moyo. Nilitamani zaidi ya yote kupata baraka hii kuu na kuhisi kwamba nilikubaliwa kabisa na MUNGU. {1T 22.2}

Nikiwa kati ya Wamethodisti nilikuwa nimesikia mengi kuhusu utakaso. Nilikuwa nimeona watu wakipoteza nguvu zao za mwili chini ya ushawishi wa msisimko mkubwa wa kiakili, na nilikuwa nimesikia hili likitambulishwa kama ushahidi wa utakaso. Lakini sikuweza kuelewa jambo gani lilikuwa muhimu ili mtu apate kujitoa kikamilifu kwa MUNGU. Rafiki zangu Wakristo waliniambia: "Mwamini Yesu sasa! Amini kwamba Yeye anakupokea sasa!" Hili nilijaribu kufanya, lakini niliona ni vigumu kwangu kuamini kwamba nilikuwa nimepokea baraka ambayo, ilionekana kwangu, inapaswa kuchangamsha mwili wangu wote. Nilishangazwa

sana kwa ugumu wangu wa moyo kwa kutokuwa na uzoefu wa kuinuliwa kwa roho ambao wengine waliudhihirisha. Ilionekana kwangu kwamba nilikuwa tofauti nao na nimefungwa milele nisiifikie furaha kamili ya utakatifu wa moyo. {1T 22.3}

Mawazo yangu kuhusu kuhesabiwa haki na utakaso yalichanganyikiwa. Hali hizi mbili ziliwasilishwa kwenye akili yangu kama zilizo tofauti na kila moja ikijitegemea; lakini bado nilishindwa kuelewa tofauti au maana ya maneno hayo, na maelezo yote ya wahubiri yaliniongezea ugumu. Sikuweza kudai baraka yangu mwenyewe, na nilijiuliza kama Baraka inapatikana tu kati ya Wamethodisti, je, katika kuhudhuria kwangu mikutano ya ujio wa pili wa Kristo, sikuwa najifungia mbali na kile ambacho nilikitamani kuliko vyote, yaani Roho inayotakasa ya MUNGU. {1T 23.1}

Bado, niliona kwamba baadhi ya wale waliodai kutakaswa, walidhihirisha roho ya uchungu wakati mada ya kuja kwa Kristo hivi karibuni ilipoletwa kwao kwa mara ya kwanza; hili halikuonekana kwangu kama dhihirisho la utakatifu waliodai kuwa nao. Sikuweza kuelewa ni kwa nini wahudumu kutoka mimbarini wanapaswa kupinga mafundisho kwamba kuja kwa Kristo mara ya pili ambako kulikuwa karibu. Matengenezo yalikuwa yamefuata mahubiri ya imani hii, na wengi wa wahudumu waliojitoa zaidi na walei walikuwa wameupokea kama Ukweli. Ilionekana kwangu kuwa wale ambao walimpenda Yesu kwa dhati wangekuwa tayari kupokea habari za ujio wake na kufurahia kuwa ulikuwa umekaribia. {1T 23.2}

Nilihisi kwamba ningeweza kudai tu kile walichokiita kuhesabiwa haki kwa njia ya imani. Katika Neno la MUNGU nilisoma kwamba bila utakatifu hakuna mtu anayeweza kumwona MUNGU. Halafu kulikuwa na hatua ya kiwango cha juu sana niliyopaswa kuifikia kabla ya kuwa na uhakika wa uzima wa milele. Niliendelea kusoma juu ya mada hii kila wakati; kwani nikiamini kwamba Kristo alikuwa karibu kuja, na niliogopa atanikuta nikiwa sijajiandaa kukutana naye. Maneno ya kunihukumu yalipiga kengele masikioni mwangu mchana na usiku, na kilio changu cha kila mara kwa MUNGU kilikuwa, Nifanye nini ili niokolewe? {1T 23.3}

Kwa mawazo yangu haki ya MUNGU ilizidi rehema na upendo Wake. Nilikuwa nimefundishwa kuamini kuzimu inayowaka moto milele, na mawazo ya kutisha yalikuwa mbele yangu kwamba dhambi zangu zilikuwa kubwa sana kuweza kusamehewa, na kwamba itanipasa nipotee milele. Maelezo ya kuogofya ambayo nilikuwa nimeyasikia ya roho zilizoangamia yalizama ndani ya akili yangu. Wachungaji mimbarani walichora picha wazi za hali ya waliopotea. Walifundisha kwamba MUNGU hakusudii kuokoa yeyote isipokuwa wale waliotakaswa. Jicho la MUNGU lilikuwa juu yetu kila wakati; kila dhambi iliandikwa na ingetimiza adhabu yake ya haki. MUNGU Mwenyewe alikuwa

akitunza vitabu kwa usahihi wa hekima isiyo na mwisho, na kila dhambi tuliyofanya ilirekodiwa kwa uaminifu dhidi yetu. {1T 23.4}

Shetani aliwakilishwa akiwa na hamu ya kushika mawindo yake na kutuchukua kwa kina cha chini cha uchungu, akifurahi juu ya mateso yetu ya kutishia kwa kuzimu inayowaka milele, ambapo, baada ya mateso ya maelfu kwa maelfu ya miaka, ndimi za moto zilizotapakaa kote zingewatupa juu ya uso wa nchi wahanga, ambao wangepiga mayowe makali: "kwa muda gani, Bwana, kwa muda gani?" Kisha jibu lingeunguruma kutoka kilindini mwa kuzimu: "Kwa umilele wote!" Tena ndimi za moto zilizoyeyuka na kuwa kama vimiminika zingewakumba waliopotea, zikiwachukua hadi chini ya bahari ya moto ya milele isiyo na utulivu. {1T 24.1}

Wakati nikisikiliza maelezo haya mabaya na ya kutisha, mafikara yangu yalielekezwa huko kiasi kwamba jasho lilianza kunitoka, na ilikuwa vigumu kukomesha kilio cha uchungu, kwani nilionekana tayari nimesikia maumivu ya upotevu. Kisha mchungaji angeelezea hali ya kutokuwa na uhakika wa maisha. Kwamba wakati mmoja tungeweza kuwa hapa, na muda ujao kuzimu, au wakati mmoja hapa duniani, na wakati ujao mbinguni. Je! Tungechagua ziwa la moto na ushirika wa pepo, au raha ya mbinguni na ushirika wa malaika? Je! Tungesikia sauti ya kilio na laana ya roho zilizopotea kwa umilele wote, au tungeimba nyimbo za Yesu mbele ya kiti cha enzi? {1T 24.2}

Baba yetu wa mbinguni aliwasilishwa mbele ya akili yangu kama dhalimu, ambaye alifurahia maumivu ya wale waliohukumiwa; siyo rafiki mpole, mwenye huruma nyororo kwa wenye dhambi, Yule ambaye anapenda viumbe Wake kwa upendo upitao ufahamu wote na anatamani waokolewe katika ufalme wake. {1T 24.3}

Hisia zangu zilikuwa nyeti sana. Niliogopa kusababisha maumivu kwa kiumbe chochote kilicho hai. Nilipoona wanyama wakitendewa vibaya, moyo wangu uliumia kwa ajili yao. Huenda huruma zangu ziliamshwa kwa urahisi na mateso, kwa sababu mimi mwenyewe nilikuwa muathirika wa ukatili wa mtu ambaye hakujali, ambao ulisababisha jeraha ambalo lilikuwa limetia giza utoto wangu. Lakini wakati wazo hili likiendelea kuzitesa fikra zangu kwamba MUNGU alifurahia kuteswa kwa viumbe vyake, ambao waliumbwa kwa mfano Wake, ukuta wa giza ulionekana kunitenga mimi na Yeye. Wakati nikitafakari kwamba Muumba wa ulimwengu atawatumbukiza waovu motoni, ili waungue kwa nyakati zisizokoma za umilele, moyo wangu ulizama kwa hofu, na nilikata tamaa kwamba nafsi gani katili na yenye udhalimu wa aina hiyo itakayoweza kujishusha na kuniokoa mimi kutoka kwenye ole na adhabu ya dhambi. {1T 25.1}

Nilifikiri kwamba hatima ya mwenye dhambi aliyehukumiwa itakuwa yangu, kuvumilia moto wa jehanamu milele, maadamu MUNGU ataendelea kuwapo. Maoni haya yalizidi kuingia  kwa kina akilini mwangu hadi nikaogopa kwamba

nitapoteza ufahamu wangu. Niliwaangalia wanyama hawa wasioongea na wasio na akili nyingi kwa wivu, kwa sababu hawakuwa na roho ya kuadhibiwa baada ya kifo. Mara nyingi nilitamani kwamba heri nisingelizaliwa. {1T 25.2}

Giza kamili lilinizingira, na haikuonekana njia ya kutoka kwenye utusitusi ule. Je! Kama Kweli ingeweza kuwasilishwa kwangu jinsi ninavyoielewa sasa, hakika mimi ningeepushwa na mashaka na huzuni nyingi. Endapo upendo wa MUNGU ungezungumzwa zaidi na wahubiri hawa, na kisha haki Yake yenye ukali na isiyo na huruma ingezungumzwa kwa udogo zaidi, uzuri na utukufu wa tabia Yake vingenihuisha/vingenihamasisha na kuibua ari ya upendo wa kina na wa dhati kwa Muumba wangu. {1T 25.3}

Tangu hapo nimefikiria kuwa wagonjwa wengi kwenye mawodi ya wendawazimu walipelekwa kule kwa kupitia uzoefu kama wangu. Dhamiri zao zilipigwa viboko na hisia ya dhambi, na imani yao inayotetemeka haikuthubutu kudai msamaha wa MUNGU ulioahidiwa. Walisikiliza maelezo maarufu ya imani kuhusiana na mahali panapoitwa kuzimu hadi hali hiyo ikaleta mgando wa damu kwenye mishipa yao, na kuchoma hisia juu ya vibao vya kumbukumbu zao. Wakiwa wameamka au wakiwa wamelala, ile picha ya kutisha ilikuwa mbele yao, hadi uhalisia wa maisha ulipotea katika mawazo, na kisha waliona tu miali ya moto ya ajabu ya kuzimu, na wakasikia tu mayowe makali ya vilio vya watu walioangamizwa. Uwezo wa kufikiri ulishushwa kutoka kwenye kiti cha enzi, na ubongo ukajazwa na mawazo mabaya ya ndoto mbaya za kufikirika, zile ambazo hazipo katika uhalisia. Wale wanaofundisha Fundisho la imani la kuzimu ya milele wangefanya vizuri kutathmini kwa uangalifu mamlaka inayowasukuma kufundisha imani ya kikatili kama hiyo (Fundisho la imani - Doctrine, Dogma). {1T 25.4}

Sikuwa nimewahi kuomba hadharani na nilikuwa nimeongea tu maneno machache ya woga katika mkutano wa maombi. Ilikuwa dhahiri sasa kuwa nilikuwa nimepata mguso moyoni kwamba ni lazima nimtafute MUNGU kwa maombi katika mikutano yetu midogo ya kijamii (social meetings). Hili sikuthubutu kulifanya, nikiogopa kuchanganyikiwa na kushindwa kutoa maoni yangu. Lakini jukumu hilo lilisukumwa akilini mwangu kwa nguvu sana kiasi kwamba nilipojaribu kuomba kwa siri nilionekana kumdhihaki MUNGU kwa sababu nilishindwa kutii mapenzi Yake. Kukata tamaa kulinizidi nguvu, na kwa muda wa majuma matatu marefu hakuna mionzi ya nuru iliyotoboa kiza kilichonizunguka. {1T 26.1}

Mateso yangu ya akili yalikuwa makali. Wakati mwingine kwa usiku mzima sikuweza kuthubutu kufumba macho yangu, lakini ningengoja mpaka dada yangu pacha awe amelala usingizi mzito, kisha kimya kimya niliacha kitanda changu na kupiga magoti sakafuni, nikisali kimya kwa uchungu na bila kutoa sauti kwa namna ambayo isingeweza kuelezewa. Hofu ya kuzimu inayowaka

milele ilikuwa mbele yangu daima. Nilijua kuwa isingewezekana kwangu kuendelea kuishi kwa muda mrefu katika hali hii, na sikuwa natamani kufa na kukutana na hatima mbaya ya mwenye dhambi. Kwa wivu kiasi gani niliwaangalia wale ambao walitambua kukubaliwa kwao na MUNGU ! Tumaini la Mkristo lilionekana kuwa la thamani kiasi gani kwa roho yangu yenye uchungu mkali! {1T 26.2}

Mara kwa mara nilibaki nimeinama katika maombi karibu usiku kucha, nikigugumia na kutetemeka kwa uchungu usioweza kuelezeka na kutokuwa na tumaini kusikoweza kuelezeka. Bwana, nihurumie! lilikuwa ombi langu, na, kama mtoza ushuru masikini, sikuthubutu kuinua macho yangu mbinguni, bali niliinamisha uso wangu sakafuni. Nilidhoofika sana katika mwili na nguvu na kukonda, lakini nikayatunza mateso yangu na kukata tamaa kwangu moyoni mwangu. {1T 26.3}

Nikiwa katika hali hii ya kukata tamaa nilikuwa na ndoto ambayo ilinivutia sana akilini mwangu. Niliota ndoto, na nikaona hekalu ambalo watu wengi walikuwa wakimiminika kuingia humo ndani. Ni wale tu waliokimbilia katika hekalu hilo ndio ambao wangeokolewa wakati mlango ulipokuwa unaenda kufungwa. Ndipo wote ambao walibaki nje wangepotea milele. Umati wa watu uliokuwa nje ambao ulikuwa ukiendelea na shughuli zao mbali mbali, uliwadhihaki na kuwakejeli wale ambao walikuwa wakiingia hekaluni, na kuwaambia kwamba mpango huu wa usalama ulikuwa udanganyifu wa kijanja, na kwamba kwa hakika hapakuwa na hatari yoyote ya kuepukwa. Waliwashikilia hata wale wengine wakiwazuia wasifanye haraka kuingia ndani ya kuta. {1T 27.1}

Nikiogopa kudhihakiwa, nilifikiri bora kusubiri hadi umati utawanyike, au hadi niingie bila kutambuliwa nao. Lakini idadi iliongezeka badala ya kupungua, na huku nikiogopa kuchelewa sana, niliondoka haraka nyumbani kwangu nikipenya katikati ya umati wa watu. Katika wasiwasi wangu wa kutaka kufika hekaluni sikuona wala kujali umati wa watu ambao walinizunguka. Wakati wa kuingia ndani ya jengo hilo, niliona kuwa hekalu kubwa lilikuwa limebebwa na nguzo moja kubwa, na kwenye nguzo hii alikuwa amefungwa Mwana-Kondoo akiwa amechanwa-chanwa na kutokwa na damu. Sisi tuliokuwepo mule tulionekana kujua kwamba Mwana-Kondoo huyu alikuwa amechanwa na kupigwa kwa sababu yetu. Wote walioingia hekaluni iliwalazimu kuja mbele Yake na kuungama dhambi zao. {1T 27.2}

Kabla tu ya Mwana-Kondoo kulikuwa na viti vilivyoinuliwa, ambavyo juu yake iliketi jamii iliyoonekana yenye furaha sana. Nuru ya mbinguni ilionekana kuwaangazia nyuso zao, nao walimsifu MUNGU na kuimba nyimbo za shukrani za furaha ambazo zilionekana kama muziki wa malaika. Hawa ndiyo waliokuja mbele ya Mwana-Kondoo, wakakiri dhambi zao, wakapata msamaha, na sasa walikuwa wakingojea kwa matarajio ya furaha tukio fulani la kufurahisha. {1T 27.3}

Hata baada ya kuingia ndani ya jengo hilo, hofu ilinijia, na hali ya aibu kwamba lazima ninyenyekee mbele ya watu hawa. Lakini nilionekana kulazimika kusonga mbele, na nilikuwa nikizunguka ile nguzo pole pole ili kumkabili Mwana-Kondoo, wakati tarumbeta ilipopigwa, hekalu likatetemeka, na kelele za ushindi ziliibuka kutoka kwa watakatifu waliokusanyika, mwangaza mkali uliangaza jengo hilo, punde tena yote yalikuwa giza kali. Watu wenye furaha wote walikuwa wametoweka na mwangaza, nami nilibaki peke yangu kwa hofu kuu ya usiku. Niliamka nikiwa na uchungu wa akili na sikuweza kujiridhisha kuwa nilikuwa nimeota. Ilionekana kwangu kwamba adhabu yangu ilikuwa imewefanywa kuwa ya kudumu, na kwamba Roho wa Bwana alikuwa ameniacha, kamwe asirudi tena. {1T 27.4}

Mara tu baada ya hili nikaota ndoto nyingine. Nilionekana kuketi katika hali ya kukata tamaa na uso wangu ukiwa umefumbatwa mikononi, nikitafakari hivi: Ikiwa Yesu angekuwa hapa duniani, ningeenda Kwake, nikajitupe miguuni Pake, na kumwambia mateso yangu yote. Asingegeuka kutoka kwangu, Angekuwa na rehema juu yangu, na ningempenda na kumtumikia Yeye kila wakati. Mara tu mlango ukafunguliwa, na mtu mwenye umbo na sura nzuri aliingia. Alinitazama kwa huzuni na akasema: "Je! Unatamani kumwona Yesu? Yuko hapa, na unaweza kumwona ikiwa unatamani. Chukua kila kitu chako na unifuate." {1T 28.1}

Nililisikia jambo hili kwa furaha isiyoelezeka, na kwa furaha nikakusanya mali zangu zote chache, kila kidude cha hazina changu, na kumfuata mwongozaji wangu. Aliniongoza kwenye ngazi ya mwinuko iliyoonekana kuwa dhaifu. Nilipoanza kupandisha ngazi, alinionya nikaze macho yangu juu, nisije nikasikia kizunguzungu na kuanguka. Wengine wengi ambao walikuwa wakipanda mwinuko walianguka kabla ya kufika kileleni. {1T 28.2}

Hatimaye tulifikia hatua ya mwisho, na tukasimama mbele ya mlango. Hapa kiongozi wangu alinielekeza niache vitu vyote ambavyo nilikuwa nimekuja navyo. Niliviweka chini kwa furaha; kisha akafungua mlango na kuniambia niingie. Kwa muda mfupi nilisimama mbele ya Yesu. Hapakuwa na makosa kuhusu uso huo mzuri. Maneno hayo ya wema na ukuu yasingeweza kumilikiwa na mwingine. Wakati macho Yake yalipokuwa juu yangu, nilijua mara moja kwamba Yeye alikuwa anafahamu kila hali ya maisha yangu na mawazo yangu yote ya ndani na hisia. {1T 28.3}

Nilijaribu kujikinga na namna alivyokuwa akinitazama, nikihisi kushindwa kuvumilia macho Yake yanayochunguza, lakini Yeye alisogea karibu akiwa mwenye tabasamu, na, aliweka mkono wake juu ya kichwa changu, akasema, Usiogope. Mlio wa sauti yake tamu ulisisimua moyo wangu kwa hisia kali, nilisujudu miguuni Pake. Wakati nikiwa nimelala hoi hapo, picha za uzuri na utukufu zilipita mbele yangu, na ilionekana kuwa nimefika mbingu ya salama na amani. Mwishowe nguvu zangu zilirudi, nami nikainuka. Macho ya upendo ya

Yesu bado yalikuwa juu yangu, na tabasamu Lake liliijaza roho yangu kwa furaha. Uwepo Wake ulinijaza kicho chenye utakatifu na upendo usioelezeka. {1T 28.4}

Mwongozaji wangu sasa alifungua mlango, na sisi wote tukapita. Aliniambia nichukue tena vitu vyote nilivyoacha nje. Baada ya hili kufanyika, alinipa kamba ya kijani iliyofungwa mafundo ya karibu karibu. Hii alinielekeza kuweka karibu na moyo wangu, na wakati nitakapohitaji kumwona Yesu, niichukue kutoka kifuani mwangu na niinyooshe kabisa mpaka mwisho. Alinionya nisiiruhusu ibaki imefunikwa kwa kitambo chochote cha muda, isije ikajifunga na hivyo kuwa ngumu kuifungua. Niliweka kamba karibu na moyo wangu na kwa furaha nikashuka kwenye ngazi nyembamba, nikimsifu Bwana na kuwaambia wale wote niliokutana nao, kwa wapi wangeweza kumpata Yesu. Ndoto hii ilinipa matumaini. Kamba ya kijani iliwakilisha imani kwa akili yangu, na uzuri na unyenyekevu wa kumtegemea MUNGU ulianza kunipambazukia rohoni. {1T 29.1}

Sasa nilimwambia mama yangu huzuni na mashaka yangu yote. Alinihurumia na kunitia moyo kwa upole, akinishauri niende kupata ushauri kwa mzee Stockman, ambaye wakati huo alihubiri mafundisho ya ujio wa Yesu huko Portland. Nilimwamini sana, kwani alikuwa mtumishi wa Kristo aliyejitoa. Aliposikia kisa changu, aliweka mkono wake kwa upendo juu ya kichwa changu, akisema hali akitiririkwa na machozi machoni mwake: “Ellen, wewe ni mtoto tu. Huo ulionao ni uzoefu wa pekee sana kwa mtu wa umri wako mdogo. Yesu lazima atakuwa anakuandaa wewe kwa kazi maalum.”{1T 29.2}

Kisha aliniambia hata kama ningekuwa mtu wa umri mkubwa na nikasumbuliwa na mashaka na hali ya kukata tamaa, yeye angeniambia kuwa kuna tumaini kwangu kupitia upendo wa Yesu. Uchungu ule wa akili niliokuwa nimeupata ulikuwa ushahidi mzuri kwamba Roho wa Bwana alikuwa anashughulika nami. Alisema wakati mdhambi anapofanywa mgumu wa moyo kutokana na hatia, huwa hatambui ukubwa wa kosa lake, lakini hujidanganya kwamba yuko sawa na hayupo katika hatari yoyote. Roho wa Bwana humwacha, na huwa mzembe na asiyejali au mwenye dharau au mpinzani. Mtu huyu mzuri aliniambia juu ya upendo wa MUNGU kwa watoto wake wanaokosea, kwamba badala ya kufurahia uharibifu wao, alitamani kuwavuta Kwake kwa imani rahisi na yenye tumaini. Alijielekeza sana katika kuongelea upendo mkuu wa Kristo na mpango wa ukombozi. {1T 29.3}

Alizungumza juu ya mkasa wangu wa mapema na akasema kweli ilikuwa shida mbaya, lakini aliniambia niamini kwamba mkono wa Baba Mwenye upendo haukuondolewa kwangu; kwamba katika maisha ya baadaye, wakati ukungu uliotia giza akili yangu utakapokuwa umetoweka, ningegundua hekima ya mpaji ambayo hapo kabla ilionekana kama ya kikatili na ya kushangaza sana. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake: “Nifanyalo wewe hujui sasa; lakini utalifahamu

baadaye.” Katika siku zijazo zile nzuri hatutaona tena kwa utusitusi kama kupitia kwenye kioo, bali tutakutana uso kwa uso na mafumbo ya upendo wa Muungu. {1T 30.1}

“Nenda uwe huru, Ellen,” alisema; “rudi nyumbani kwako ukimtumaini Yesu, kwa maana hatazuia upendo Wake kutoka kwa mtafutaji wa Kweli.” Kisha aliniombea kwa dhati na ari, na ilionekana kuwa MUNGU hakika angejali sala ya mtakatifu wake, hata ikiwa maombi yangu ya unyenyekevu hayajasikiwa. Niliuacha uwepo wake nikiwa nimefarijiwa na kutiwa moyo. {1T 30.2}

Katika kipindi cha dakika chache nilizopokea maelekezo kutoka kwa Mzee Stockman, nilikuwa nimepata maarifa zaidi juu ya mada ya upendo wa MUNGU na huruma yenye hisia kuliko kutoka kwa mahubiri na mawaidha yote ambayo nilikuwa nimeyasikiliza kabla. Nilirudi nyumbani na nikaenda tena mbele za Bwana, nikiahidi kufanya chochote na kuteseka kwa ajili ya chochote ambacho Yeyey atahitaji kutoka kwangu, alimradi matabasamu ya Yesu yaufurahishe moyo wangu. Wajibu ule ule ulioisumbua akili yangu hapo kabla, ulikuwa ukiwasilishwa kwangu yaani – kubeba msalaba wangu kati ya watu wa MUNGU waliokusanyika. Fursa haikuwa ya kutafutwa kwa muda mrefu kwani kulikuwa na mkutano wa maombi jioni hiyo hiyo, ambao nilihudhuria. {1T 30.3}

Niliinama nikitetemeka wakati maombi yakitolewa. Baada ya wachache kuomba, niliinua sauti yangu kwa maombi kabla sijajua nifanyalo. Ahadi za MUNGU zilionekana kwangu kama lulu nyingi za thamani ambazo zilipaswa kupokelewa tu kwa kumwomba Mungu. Wakati nikiomba, mzigo na uchungu wa roho ambao nilikuwa nimevumilia kwa muda mrefu ulitoweka moyoni mwangu, na baraka ya Bwana ilinishukia kama umande mwororo. Nilimsifu MUNGU kutoka ndani ya moyo wangu. Kila kitu kilionekana kufungwa kutoka kwangu isipokuwa Yesu na utukufu Wake, na nikapoteza fahamu ya kile kilichokuwa kinanizunguka. {1T 31.1}

ROHO WA MUNGU alikaa juu yangu kwa nguvu sana kiasi kwamba sikuweza kwenda nyumbani usiku huo. Niliporudi, siku iliyofuata, mabadiliko makubwa yalikuwa yametokea akilini mwangu. Ilionekana kwangu kuwa siwezi kuwa mtu yule yule aliyeondoka nyumbani mwa baba yangu jioni iliyopita. Fungu hili lilikuwa kila wakati katika mawazo yangu: “Bwana Ndiye mchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu.” Moyo wangu ulijawa na furaha huku nikirudia Maneno haya kwa upole. {1T 31.2}

Maoni yangu juu ya Baba yalibadilishwa. Sasa nilimwangalia Yeye kama Mzazi Mwenye huruma nyororo na mpole, badala ya yule jeuri na mkali anayewalazimisha watu wamtii kiupofu. Moyo wangu ulimwendea kwa upendo wenye kina na unaowaka. Kutii mapenzi Yake kulionekana kuwa furaha; ilikuwa raha kuwa katika huduma Yake. Hakuna kivuli kilichofifisha nuru iliyonifunulia mapenzi kamili ya MUNGU. Nilihisi hakikisho la Mwokozi anayekaa ndani yangu,

na kugundua Ukweli wa kile Kristo alichosema: "Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima." {1T 31.3}

Amani yangu na furaha yangu ilikuwa tofauti sana na giza na maumivu yangu ya zamani kiasi kwamba ilionekana kana kwamba nimeokolewa kutoka kuzimu na kusafirishwa kwenda mbinguni. Ningeweza hata kumsifu MUNGU kutokana na ile bahati mbaya iliyokuwa jaribu la maisha yangu, kwani ilikuwa ndiyo njia ya kurekebisha mawazo yangu milele. Kutokana na asili yangu ya majivuno, kiburi na kutaka matamanio ya ukuu, huenda nisingekuwa na mwelekeo wa kutoa moyo wangu kwa Yesu kama si kwa sababu ya maumivu makali yaliyonikata, kutoka kwenye ule unaoitwa ushindi na ulimwengu na ubatili wake. {1T 31.4}

Kwa miezi sita hakuna kivuli kilichotia ukungu akili yangu, wala sikupuuza jukumu moja linalojulikana. Jitihada yangu yote ilikuwa kufanya mapenzi ya MUNGU na kumtunza Yesu na mbingu kila wakati akilini mwangu. Nilishangazwa na kunaswa na muonekano wa wazi uliowasilishwa kwangu juu ya upatanisho na kazi ya Kristo. Sitajaribu kuelezea zaidi mazoezi ya akili yangu; Inatosha tu kusema kuwa mambo ya kale yalikuwa yamepita, vitu vyote vimekuwa vipya. Hakukuwa na wingu la kuharibu raha yangu kamili. Nilitamani kusimulia kisa cha upendo wa Yesu, lakini sikuhisi mwelekeo wa kushiriki mazungumzo ya kawaida na mtu yeyote. Moyo wangu ulijaa upendo kwa MUNGU na amani inayopita ufahamu hata nilipenda kutafakari na kuomba. {1T 32.1}

Usiku baada ya kupokea baraka kubwa sana, nilihudhuria mkutano wa ujio wa Kristo. Wakati ulipofika wa wafuasi wa Kristo kusema kumhusu Yeye, mimi sikuweza kukaa kimya, lakini nilisimama na kusimulia uzoefu wangu. Hakuna wazo lililoingia akilini mwangu juu ya nini nilipaswa kusema; lakini kisa sahili cha upendo wa Yesu kwangu kilidondoka kutoka midomoni mwangu kwa uhuru kamili, kwa urahisi kabisa, na moyo wangu ulifurahi sana kukombolewa kutoka kwenye kifungo cha giza la kukata tamaa hata nikawasahau watu waliokuwepo kwa kuwa sikuwaona tena mawazoni mwangu na nikaonekana nimebaki peke yangu na MUNGU. Sikupata shida kuelezea amani na furaha yangu, isipokuwa kwa machozi ya shukrani yaliyotatiza matamshi yangu wakati nilisimulia juu ya upendo wa ajabu ambao Yesu alikuwa amenionesha. {1T 32.2}

Mzee Stockman alikuwepo. Alikuwa ameniona hivi majuzi katika hali ya kukata tamaa sana, na mabadiliko ya ajabu katika sura na hisia zangu yaliugusa moyo wake; alilia kwa sauti, akifurahi pamoja nami na kumsifu Mungu kwa uthibitisho huu wa rehema Zake nyororo na fadhili zenye upendo.{1T 32.3}

Muda mfupi baada ya kupokea baraka hii kuu, nilihudhuria mkutano wa konferensi katika kanisa la Kikristo, ambapo Mzee Brown alikuwa mchungaji. Nilialikwa kuelezea uzoefu wangu, na nilihisi siyo tu uhuru mkubwa wa kujieleza, bali furaha, ya kusimulia kisa changu rahisi cha upendo wa Yesu na furaha ya kukubaliwa na MUNGU. Nilipozungumza, kwa moyo uliotawaliwa na

utiifu na macho yaliyogubikwa na machozi, roho yangu ilionekana kuvutwa kuelekea mbinguni kwa shukrani. Nguvu ya Bwana iyeyushayo iliwajia watu waliokusanyika. Wengi walikuwa wakilia na wengine wakimsifu MUNGU. {1T 33.1}

Wenye dhambi walialikwa kujitokeza kwa maombi, na wengi waliitikia wito huo. Moyo wangu ulimshukuru sana MUNGU kwa baraka aliyonipa kiasi kwamba nilitamani wengine washiriki furaha hii takatifu. Akili yangu ilivutiwa sana na wale wanaoweza kuwa wanateseka chini ya hisia ya kutoridhika na Bwana na hisia za mzigo wa dhambi. Wakati nikisimulia uzoefu wangu, nilihisi kuwa hakuna mtu anayeweza kupinga ushahidi wa upendo wa msamaha wa MUNGU ambao umesababisha mabadiliko ya ajabu ndani yangu. Uhalisia wa uongofu wa kweli ulionekana wazi sana kwangu kiasi kwamba nilijisikia kama kusaidia rafiki zangu wadogo kuingia kwenye nuru, na kwa kila fursa nilitumia ushawishi wangu kuelekea hatima hii. {1T 33.2}

Nilipanga mikutano na rafiki zangu wadogo, ambao wengine walikuwa wakubwa zaidi yangu, na wachache walikuwa watu waliooa. Baadhi yao walikuwa ni watu wenye kuendekeza ubatili na wasiojali; uzoefu wangu ulisikika kwao kama hekaya za kufikirika zisizokuwa na maana, na hawakuwekea umakini kusihi kwangu. Lakini niliamua kwamba juhudi zangu hazipaswi kusitishwa hadi hizi roho pendwa, ambazo nilikuwa na shauku kubwa nazo, zijitoe kwa MUNGU. Usiku mzima ulitumika na mimi kwa maombi ya dhati kwa wale ambao nilikuwa nimewatafuta na kuwaleta pamoja kwa kusudi la kufanya kazi na kuomba pamoja nao. {1T 33.3}

Baadhi ya hawa walikuwa wamekutana nasi kutokana na udadisi uliowanasa, nao wasikie kile nilichokisema; wengine walidhani mimi nimechanganyikiwa, na hata kukosa kuthibiti akili katika juhudi zangu, hasa walipoonesha kujali kwao wenyewe. Lakini katika kila moja ya mikutano yetu midogo niliendelea kuhimiza na kumwombea kila mmoja peke yake, hadi kila mmoja alipojitoa kwa Yesu, akikiri sifa za upendo Wake wa msamaha. Kila mmoja aliongolewa awe wa MUNGU. {1T 33.4}

Usiku baada ya usiku katika ndoto zangu nilionekana nikifanya kazi kwa wokovu wa roho. Wakati kama huo kesi maalum ziliwasilishwa akilini mwangu; Watu hawa baadaye niliwatafuta na kuomba nao. Katika kila tukio, isipokuwa kwa mtu mmoja, watu walijitoa kwa Bwana. Baadhi ya ndugu zetu wenye kupenda urasmi waliogopa kwamba nilikuwa usongo na bidii sana kwa uongofu wa roho, lakini wakati ulionekana kwangu ni mfupi sana kiasi kwamba uliwafanya wote waliokuwa na tumaini la kutokufa kubarikiwa na walitarajia kuja kwa Kristo hivi karibuni, kufanya kazi bila kukoma kwa wale ambao walikuwa bado katika dhambi zao na wakiwa wamesimama kwenye ukingo mbaya wa uharibifu. {1T 34.1}

Ingawa nilikuwa mdogo sana, mpango wa wokovu ulikuwa wazi kabisa akilini mwangu, na uzoefu wangu binafsi ulikuwa umewekwa alama, kiasi kwamba, kwa kuzingatia jambo hilo, nilijua ni jukumu langu kuendelea na juhudi zangu kwa ajili ya wokovu wa roho za thamani na kuomba na kumkiri Kristo kwa kila fursa. Nafsi yangu yote ilitolewa kwa kumtumikia Bwana wangu. Acha kitokee chochote kinachoweza kutokea, lakini mimi nilidhamiria kumpendeza MUNGU, na kuishi kama mtu atarajiaye kuja kwa Mwokozi na kuwapa waaminifu tuzo. Nilijiona kama mtoto mdogo ajaye kwa MUNGU kama kwa baba yangu, nikimuuliza ni nini angependa mimi nifanye. Basi wakati jukumu langu lilipowekwa wazi kwangu, ilikuwa furaha yangu kubwa kulifanya. Majaribu ya kipekee wakati mwingine hunikabili. Wale wazee wenye uzoefu kuliko wangu walijitahidi kunizuia, na kunivuta nirudi nyuma na kutuliza bidii ya imani yangu; lakini kwa tabasamu la Yesu lililoangaza maisha yangu, na upendo wa MUNGU moyoni mwangu, niliendelea na roho ya furaha jatuja ===. {1T 34.2}

Mara nyingi ninapokumbuka uzoefu wa maisha yangu ya awali, kaka yangu, msiri wa matumaini yangu na hofu yangu, mtulizi mwenye huruma ya dhati katika uzoefu wangu wa Kikristo, huja akilini mwangu na mafuriko ya kumbukumbu nzuri. Alikuwa ni miongoni mwa wale ambao dhambi huwasilisha vishawishi vichache. Kwa kawaida alikuwa na hulka ya kujitoa wakfu kwa ibada, hakutafuta jamii ya vijana na wale watu wenye furaha mambo ya dunia, lakini alichagua ushirika wa Wakristo ambao mazungumzo yao yangemfundisha njia ya maisha. Mwenendo wake ulikuwa kama wa mtu mzima, hakika mafikara yake yalikuwa mbele ya umri wake; alikuwa mpole na mwenye amani, na akili yake ilikuwa karibu kila mara imejazwa na mawazo ya kiroho/kidini. Maisha yake yalioneshwa, na wale waliomjua, kama mfano kwa vijana, mfano hai wa neema na uzuri wa Ukristo wa kweli. {1T 34.3}

## SURA YA 4

## KULIACHA KANISA LA METHODIST

Familia ya baba yangu bado ilikuwa ikihudhuria kanisa la Methodist mara chache chache sana, na pia mikutano ya madarasa iliyofanyika katika nyumba za watu binafsi. Jioni moja ndugu yangu Robert na mimi tulienda kwenye mkutano wa darasa. Mzee kiongozi alikuwepo. Ilipofika zamu ya kaka yangu, alizungumza kwa unyenyekevu mkubwa, lakini kwa uwazi, juu ya umuhimu wa uimara mkamilifu wa kukutana na Mwokozi wetu atakapokuja katika mawingu ya mbinguni na nguvu na utukufu mwingi. Wakati kaka yangu akiwa anaongea, nuru ya mbinguni iliwaka juu ya uso wake ambao kwa kawaida ulikuwa wenye rangi ya iliyopauka. Alionekana kubebwa na Roho juu ya mazingira ya sasa, na aliongea kana kwamba yupo mbele ya Yesu. Nilipoitwa kuzungumza, niliamka, kwa uchangamfu na moyo mkunjufu, moyo uliojaa upendo na amani. Nami

nikawa huru kukisimulia kisa cha mateso yangu makubwa chini ya usadikisho na kutuhumiwa na dhambi, jinsi ambavyo kwa muda mrefu hatimaye nilikuwa nimepokea baraka iliyotafutwa kwa muda mrefu, kupatana kwa hakika na mapenzi ya MUNGU, na kuelezea furaha yangu katika habari ya kuja kwa haraka kwa Mkombozi wangu ili awachukue watoto Wake nyumbani. {1T 35.1}

Kwa unyenyekevu wangu nilitarajia kwamba kaka na dada zangu wa Kimethodisti wangeelewa hisia zangu na kushangilia pamoja nami. Lakini nilikata tamaa; akina dada kadhaa waliugua na kuguna na kisha kusogeza viti vyao kwa kelele, wakinipa kisogo. Sikufikiria kile kilichosemwa kwamba hata kingeweza kuwaudhi, nami nikamalizia kuzungumza kwa ufupi sana, nikihisi ushawishi wa kutisha wa kutokubaliwa kwao. Nilipokuwa nimeacha kuongea, Mzee B. aliniuliza ikiwa haitapendeza zaidi kuishi maisha marefu yenye faida, kuwafanyia wengine mema, kuliko kumfanya Yesu aje haraka na kuwaangamiza wadhambi maskini. Nilijibu kwamba ninatamani kuja kwa Yesu. Kwani dhambi ingekuwa na mwisho, na tungefurahia utakaso milele, bila shetani wa kutujaribu na kutuongoza kwenye njia ya uovu. {1T 35.2}

Kisha akauliza ikiwa nisingependa kufa kwa amani kitandani mwangu kuliko kupita kwenye uchungu wa kubadilishwa, nikiwa hai, kutoka hali ya kufa na kuingia hali ya kutokufa. Jibu langu lilikuwa kwamba nilitamani Yesu aje kuchukua watoto Wake mbinguni; kwamba nilikuwa tayari kuishi au kufa kwa namna ile MUNGU alivyotaka, na ningeweza kuvumilia kwa urahisi maumivu yote ambayo yangeweza kubebwa kwa muda mfupi, kama ule wa kufumba na kufumbua jicho; kwamba nilitamani magurudumu ya wakati yazunguke haraka, na kuileta siku ile ambayo miili hii mibaya ya uharibifu ingebadilishwa, na kuumbwa upya kwa mfano wa mwili wa Kristo uliotukuka. Nilisema pia wakati nilipoishi karibu na Bwana, basi nilitamani sana kwa dhati na ari ujio wake. Hapa wengine waliokuwepo walionekana kukasirika kabisa. {1T 36.1}

Wakati mzee msimamizi alipozungumza na wengine darasani, alionesha furaha kubwa kwa kutarajia milenia ya muda, wakati ambao dunia itapaswa kujazwa na maarifa ya kumjua Bwana kama maji yafunikavyo bahari. Alitamani kuona kipindi hiki kizuri kikikaribishwa. Baada ya mkutano kufungwa, nilibakiwa na kumbukumbu ya kupokelewa ubaridi ulioweka alama kwangu na wale ambao hapo awali walikuwa sio wema na wenye urafiki kwangu. Mimi na kaka yangu tulirudi nyumbani tukiwa na huzuni kwamba tulieleweka vibaya na ndugu zetu, na kwamba mada ya kuja karibu kwa Yesu ilipaswa kuamsha upinzani mkali wa namna ile vifuani mwao. Hata hivyo tulishukuru kwamba tunaweza kutambua nuru ya thamani na kufurahi katika kutazamia kuja kwa Bwana. {1T 36.2}

Muda si mrefu baada ya tukio hii tulihudhuria tena mkutano wa darasa (Class meeting). Tulitaka nafasi ya kusema juu ya upendo wa MUNGU wa thamani ambao ulihuisha roho zetu. Nilitamani sana kusimulia wema na rehema za Bwana kwangu. Mabadiliko makubwa sana yalikuwa yamefanyika ndani yangu

kiasi kwamba ilionekana ni jukumu langu kuboresha kila fursa ya kushuhudia upendo wa Mwokozi wangu. {1T 36.3}

Wakati wangu ulipofika wa kuzungumza, nilisema ushuhuda jinsi nilivyofurahia upendo wa Yesu, na kwamba nilitazamia mbele na matarajio mazuri ya kukutana na Mkombozi wangu hivi karibuni. Imani kwamba kuja kwa Kristo ilikuwa karibu ilikuwa imechochea roho yangu kutafuta kwa dhati na bidii zaidi utakaso wa ROHO WA MUNGU. Hapa kiongozi wa darasa alinikatisha, akisema: "Ulipokea utakaso kupitia Umethodisti, kupitia Umethodisti dada, siyo kupitia nadharia potofu." Nilihisi kulazimika kukiri Ukweli, kwamba haikuwa kupitia Umethodisti ambapo moyo wangu ulipokea baraka zake mpya, lakini ilitokana na zile Kweli zinazochochea juu ya ujio binafsi wa Yesu (mbashara). Kupitia hizi Kweli, nilikuwa nimepata amani, furaha, na upendo mkamilifu. Hivyo ndivyo ushuhuda wangu ulivyofungwa, ushuhuda uliokuwa wa mwisho kuutoa darasani mbele ya ndugu zangu wa kanisa la Methodisti. {1T 37.1}

Ndipo Robert akazungumza kwa namna yake ya unyenyekevu na upole, lakini kwa namna iliyo na mguso ulio wazi, kiasi kwamba wengine watu walilia na kuguswa zaidi; lakini wengine walitoa kikohozi cha uongo wakionesha kutokubaliana na uelewa huo usiopatana na wa kanisa na wakawa katika hali isiyo tulivu kabisa. Baada ya kutoka kwenye chumba cha darasa, tukazungumza tena juu ya imani yetu, na tukashangaa kwa namna ndugu na dada zetu Wakristo walivyoshindwa kustahimili Neno lililosemwa kuhusu kurejea kwa Mwokozi wetu. Tulifikiri kama wangekuwa wanampenda Yesu kama ilivyokuwa ikiwapasa, kusingekuwa na usumbufu mkubwa kusikia juu ya ujio Wake wa pili, lakini, badala yake, wangepongeza habari hizo kwa shwangwe-wangerindima. {1T 37.2}

Tulikuwa na hakika kwamba hatupaswi tena kuhudhuria mkutano wa darasa. Tumaini la kuonekana kwa utukufu kwa Kristo lilijaza mioyo yetu na lingekuja kujidhihirisha pale ambapo tu tungeinuka ili kuongea. Hii ilionekana kuwasha hasira ya wale waliokuwepo dhidi ya watoto wawili wanyenyekevu waliothubutu, mbele ya upinzani, kusema juu ya imani iliyoijaza mioyo yao na amani na furaha. Ilikuwa dhahiri kwamba sisi tusingeweza kuwa na uhuru katika mkutano wa darasa; kwani ushuhuda wetu ulichochea kejeli na maneno ya jeuri yenye uchokozi ambayo yalifika masikioni mwetu wakati wa mkutano, kutoka kwa kaka na dada ambao tuliwaheshimu na kuwapenda. {1T 37.3}

Waadventista walifanya mikutano wakati huu huko kwenye kumbi ya Beethoven. Baba yangu, na familia yake, walihudhuria mara nyingi sana. Kipindi cha ujio wa pili wa Kristo kilidhaniwa kuwa katika mwaka wa 1843. Wakati ulionekana kuwa mfupi sana ambao roho zingeweza kuokolewa hata nikaamua kufanya yote yaliyokuwa katika uwezo wangu kuwaongoza watu wenye dhambi kwenye nuru ya Ukweli. Lakini ilionekana kuwa haiwezekani kwa

yule aliyekuwa mchanga sana, na mwenye afya dhaifu, kufanya mengi katika kazi hii kubwa. {1T 38.1}

Nilikuwa na dada wawili nyumbani, Sarah, ambaye alikuwa ananizidi umri wa miaka kadhaa, na dada yangu pacha, Elizabeth. Tulizungumza jambo hili kati yetu, na tukaamua kufanya kazi na kupata pesa kadri tuwezavyo, na kuzitumia kununua vitabu na machapisho ya kusambazwa bure. Hii ilikuwa njia bora tuliyoweza kuifanya, na tulifanya jambo hili kwa furaha kidogo. Ningeweza kupata senti ishirini na tano tu kwa siku; lakini mavazi yangu yalikuwa ya sahili, hakuna kilichotumiwa kwa mapambo yasiyo ya lazima, na kujionesha kulionekana kuwa dhambi ya ubatili tu machoni mwangu; kwa hivyo nilikuwa na akiba kidogo kwenye hazina yangu ili kununua vitabu vinavyofaa. Hivi vitabu niliviweka mikononi mwa watu wenye uzoefu watakaovituma nje ya nchi. {1T 38.2}

Kila ukurasa wa jarida hili ulionekana kuwa wa thamani machoni pangu, kwani ulikuwa kama mjumbe wa nuru kwa ulimwengu, akiwataka watu wajiandae kwa hafla hiyo kubwa iliyokaribia. Siku baada ya siku nilikaa kitandani nikishikiliwa na mito, nikitimiza jukumu langu nililopewa na vidole vinavyotetemeka ili nijipatie kipato kidogo. Nilitunza kwa uangalifu mkubwa vipande vya thamani vya fedha vilivyopatikana baada ya mauzo, ambavyo vingetumika kuchapisha machapisho ili kuwaangazia na kuwaamsha wale ambao walikuwa gizani. Sikuwa na kishawishi cha kutumia mapato yangu kwa kujiridhisha mimi mwenyewe; wokovu wa roho ulikuwa mzigo wa akili yangu, na moyo wangu uliumia kwa wale ambao walikuwa wakijidanganya wenyewe kuwa walikuwa wakiishi kwa usalama, wakati ujumbe wa onyo ukitolewa kwa ulimwengu. {1T 38.3}

Siku moja nilisikiliza mazungumzo kati ya mama na dada katika Kristo, kwa kurejelea mazungumzo ambayo walikuwa wameyasikia hivi karibuni, kwamba roho haikuwa na hali ya kutokufa ya asili. Baadhi ya maandishi ya uthibitisho ya mchungaji yalirudiwa. Miongoni mwao nakumbuka haya, nayo yalinivutia kwa nguvu sana: “Nafsi itendayo dhambi itakufa- Ezekiel 18:20.” “Walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote- Mithali 9:5.” “ambako Yeye kwa majira Yake atakudhihirisha, Yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana.ambaye Yeye peke yake hapatikani na mauti 1Tim 6:15,16” “wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika, watapewa uzima wa milele-Rumi 2:7.” "Kwa nini," mama yangu aliuliza, baada ya kunukuu kifungu kilichotangulia, "wanapaswa kutafuta kile ambacho tayari wanacho?" {1T 39.1}

Nilisikiliza maoni haya mapya kwa shauku kali na chungu. Nikiwa peke yangu na mama yangu, nilimuuliza ikiwa kweli aliamini roho ya mwanadamu haifi haifi Iimmortal soulI. Jibu lake ni kuwa anahofia tulikuwa tumekosea juu ya mada hiyo na juu ya mada zingine pia. {1T 39.2}

“Lakini, mama,” nikasema, “unaamini kweli kwamba roho ya mtu hulala kaburini hadi ufufuo? Je! Unafikiri kwamba Mkristo, wakati akifa, haendi mbinguni mara moja, wala mwenye dhambi kwenda kuzimu papo hapo (Jehanamu)?” {1T 39.3}

Alijibu: “Biblia haitoi uthibitisho wowote kwamba kuna moto wa Jehanamu wa milele. Kama kuna mahali kama hapo, panapaswa kutajwa katika Kitabu Kitakatifu-Biblia.”{1T 39.4}

“Kwa nini mama!” Nilipaza kwa mshangao, “haya ni mazungumzo ya ajabu kwako! Ikiwa unaamini nadharia hii ya ajabu, usiruhusu mtu yeyote aijue; kwani nahofia kuwa wenye dhambi wangejikusanyia uhakikisho wa usalama kutokana na imani hii, na wasingetamani kamwe kumtafuta Bwana.” {1T 39.5}

“Kama huu ndiyo Ukweli wa kuaminika wa Biblia,” alijibu, “badala ya kuzuia wokovu wa wenye dhambi, itakuwa njia ya kuwavuta kwa Kristo. Ikiwa upendo wa MUNGU hautawashawishi waasi kujitoa, hofu ya kuzimu ya milele haitamshawishi kutubu. Kwa kuongezea, je, hii haionekani kama njia sahihi ya kuvuna roho kwa Yesu, kwa kupitia moja ya sifa za chini kabisa za akili, yaani woga usiofaa. Upendo wa Yesu una sumaku; utaivuta mioyo migumu. "{1T 39.6}

Ilikuwa miezi kadhaa baada ya mazungumzo haya kabla ya kusikia chochote zaidi juu ya Mafundisho haya makuu ya imani (Doctrines); lakini wakati huu akili yangu ikiwa imetumika kuicheua sana mada hiyo. Niliposikia ikihubiriwa, niliamini kuwa ni Kweli. Tangu wakati huo nuru kuhusu usingizi wa wafu ilipoingia akilini mwangu, siri iliyokuwa imefunika ufufuo ilitoweka, na tukio kuu lenyewe lilichukua umuhimu mpya na wa hali ya juu. Akili yangu mara nyingi ilisumbuliwa na juhudi zake za kupatanisha thawabu ya haraka au adhabu ya wafu na Ukweli usio na shaka wa ufufuo wa baadaye na hukumu. Ikiwa wakati wa kifo roho iliingia kwenye furaha ya milele au taabu, kulikuwa na haja gani tena basi ya ufufuo wa mwili duni na mbovu? {1T 40.1}

Lakini imani hii mpya na nzuri ilinifundisha sababu iliyofanya waandishi waliovuviwa kuzungumzia sana juu ya ufufuo wa mwili; ni kwa sababu kiumbe chote kilikuwa kimelala kaburini. Ningeweza sasa kutambua wazi uongo wa msimamo wetu wa zamani juu ya hoja/swali hili. Mkanganyiko na kutokuwa na haja au maana kwa hukumu ya mwisho, baada ya roho za marehemu kuhukumiwa wakati fulani na kuteuliwa kwa kura yao, lilikuwa wazi kwangu sasa. Niliona kwamba tumaini la wafiwa ni katika kutazamia siku tukufu wakati Mpaji wa Uhai atakayevunja pingu za kaburi, na wafu wema watakapoinuka na kuacha nyumba yao ya gereza na kuvikwa maisha matukufu ya kutokufa. {1T 40.2}

Familia yetu wote tulipendezwa na Mafundisho ya imani kuja kwa Bwana hivi karibuni. Baba yangu alikuwa amechukuliwa kwa muda mrefu kama moja ya nguzo za kanisa la Methodist alikokuwa akiishi, na familia yetu nzima ilikuwa washiriki wenye bidii; lakini hatukufanya iwe siri kuhusu imani yetu mpya, ingawa hatukuihimiza kwa wengine katika nyakati zisizofaa, au kuonesha hali ya kutokuwa rafiki kwa kanisa letu wakati wowote. Hata hivyo, mchungaji wa Methodist alitutembelea na akachukua nafasi hiyo kutujulisha kwamba imani yetu na Umethodisti havikukubaliani. Hakutuuliza sababu zetu za kuamini vile tulivyoamini, wala hakurejelea Biblia ili kutuaminisha juu ya makosa yetu; lakini alisema kuwa tumepokea imani mpya na ngeni ambayo Kanisa la Methodist haliwezi kuikubali. {1T 40.3}

Baba yangu alijibu na kumwambia atakuwa amekosea kuliita hili kuwa ni Fundisho jipya na geni, kwamba Kristo Mwenyewe, katika mafundisho Yake kwa wanafunzi Wake, alikuwa akihubiri ujio wake wa pili. Alikuwa amesema: “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi Mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe Kwangu; ili nilipo Mimi, nanyi mwepo.” “Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, Yeye alipokuwa akienda Zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, Yesu atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda Zake mbinguni.” {1T 41.1}

“Na,” alisema baba yangu, akiipa joto na uchangamfu mada yake, “Paulo aliyevuviwa aliandika barua kuwatia moyo ndugu zake huko Thesalonike, akisema: ‘na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa Kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza Wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua MUNGU, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu ZAKE; Yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu Wake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile.’ ‘Kwa sababu Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya MUNGU ; nao  wale waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi, farijianeni kwa Maneno hayo.’” {1T 41.2}

"Hii ni mamlaka ya juu kwa imani yetu. Yesu na mitume Wake walikita juu ya tukio la ujio wa pili kwa furaha na ushindi; na malaika watakatifu wanatangaza kwamba Kristo, ambaye alipaa mbinguni, atakuja tena. Hili ndilo kosa letu,

kuamini Neno la Yesu na wanafunzi Wake. Hili ni Fundisho la imani la zamani sana, na halina doa lolote la uzushi.” {1T 42.1}

Mchungaji hakujaribu kutaja hata fungu moja linalothibitisha kuwa tumekosea, lakini alitoa udhuru kuwa tumpe muda. Alitushauri tujiondoe kanisani kimya kimya na tuepuke kufanyiwa kesi hadharani. Tulikuwa tukifahamu kuwa ndugu zetu wengine walikuwa wakikutana na madhila kama hayo kwa sababu kama hizo, na hatukutamani ieleweke kwamba tunaona haya kutambulisha imani yetu, au hatuna uwezo wa kuithibisha kwa Maandiko; kwa hiyo wazazi wangu walisisitiza kwamba wanapaswa kufahamishwa sababu za ombi hili. {1T 42.2}

Jibu pekee kwa swali hili lilikuwa ukwepaji wa mchungaji  kutoa tamko kuwa tumekiuka sheria za kanisa, na njia bora ilikuwa ni kujitoa ushirika kwa hiari ili kuokoa kuwepo kwa kesi. Tulijibu kwamba sisi tunapendelea kuwepo kwa kesi kama taratibu wa kawaida unavyofanywa, na tukadai kujua ni dhambi gani tunayoshtakiwa nayo, kwani hatukujua kosa katika kutafuta mioyoni mwetu na kupenda kutokea kwa Mwokozi. {1T 42.3}

Haikuchukua muda, tukaarifiwa kuwapo kwenye mkutano utakaofanyika katika ukumbi wa kanisa. Kulikuwa na watu wachache tu. Ushawishi wa baba yangu na familia yake ulikuwa kwamba wapinzani wetu hawakuwa na hamu ya kuwasilisha kesi yetu mbele ya idadi kubwa ya kutaniko. Shitaka moja lililopendelewa ni kwamba tulikuwa tumeenda kinyume na sheria zao. Baada ya kuuliza ni sheria gani tumekiuka, ilielezwa, baada ya kusita kidogo, kwamba tumehudhuria mikutano mingine, na tumepuuza kukutana mara kwa mara na darasa letu. Tulisema kwamba sehemu ya familia hiyo ilikuwa vijijini kwa muda mrefu uliopita, na kwamba hakuna yeyote aliyebaki mjini ambaye hakuwepo kwenye mkutano wa darasa zaidi ya majuma machache, na walilazimishwa kimaadili kukaa mbali kwa sababu shuhuda walizotoa zilikutana na hali ya kutokukubalika. Tuliwakumbusha pia kuwa watu fulani ambao hawakuhudhuria mkutano wa darasa kwa mwaka bado walikuwa wakisimama kama washiriki wazuri. {1T 42.4}

Iliulizwa kama tutakiri tumekiuka sheria zao, na ikiwa tunakubali kuzifuata katika siku zijazo. Tulijibu kwamba hatukuwahi kukana imani yetu au kukataa ukweli mtakatifu wa MUNGU; kwamba hatuwezi kuacha tumaini la kuja kwa Mkombozi wetu hivi karibuni; kwamba kwa njia ambayo waliiita uzushi lazima tuendelee kumwabudu Bwana. Baba yangu katika utetezi wake alipokea baraka ya MUNGU, na sisi sote tulikiacha kile chumba kilichounganishwa na kanisa na mioyo iliyo huru kwa uchangamfu, tukiwa na furaha katika dhamira ya haki na uthibitisho wa tabasamu la Yesu. {1T 43.1}

Jumapili iliyofuata, mwanzoni mwa sikukuu ya upendo au love feast, mzee wa kanisa alisoma majina yetu saba wakati akiyaondoa kutoka kanisani. Alisema kwamba hatukufukuzwa kwa sababu ya mwenendo wowote mbaya au usio wa maadili, bali kwamba tulikuwa na tabia isiyo na hatia na sifa nzuri, lakini

tulikuwa na hatia ya kutembea kinyume na sheria za kanisa la Methodist. Alitangaza pia kuwa mlango ulikuwa wazi sasa, kwa watu wowote waliokuwa na hatia ya ukiukaji kama huo wa sheria kushughulikiwa kwa jinsi hiyo hiyo. {1T 43.2}

Kulikuwa na wengi kanisani ambao walingojea kuonekana kwa Mwokozi, na tishio hili lilifanywa kwa kusudi la kuwaogopesha ili wawe watii kwa kanisa (na siyo kwa Mwenyezi Mungu). Katika visa vingine sera hii ilileta matokeo yanayotarajiwa, na neema ya MUNGU iliuzwa kwa nafasi ya ushirika kanisani. Wengi waliamini, lakini hawakuthubutu kukiri imani yao, wasije wakafukuzwa nje ya sinagogi. Lakini wengine waliondoka muda mfupi baadaye na kujiunga na kikundi cha wale ambao walikuwa wakimtafuta Mwokozi. {1T 43.3}

Kwa wakati huu maneno ya nabii yalikuwa makubwa sana na ya thamani: "Ndugu zenu wawachukiao ninyi, waliowatupa kwa ajili ya Jina Langu, wamesema, Na atukuzwe Bwana, tupate kuiona furaha yenu; lakini watatahayarika." {1T 43.4}

## SURA YA 5

## UPINZANI WA NDUGU

Kwa miezi sita hakuna wingu lililoingilia kati yangu na Mwokozi wangu. Wakati wowote kulipokuwa na fursa inayofaa, nilitoa ushuhuda wangu, na nilibarikiwa sana. Wakati mwingine Roho wa Bwana alikaa juu yangu kwa nguvu nyingi kiasi kwamba nguvu yangu iliondolewa kwangu. Hili lilikuwa jaribio kwa wengine ambao walikuwa wametoka katika makanisa yenye urasmi, makanisa kwa majina tu, na maoni yaliyotolewa mara nyingi yalinihuzunisha sana. Wengi hawakuweza kuamini kwamba mtu anaweza kuzidiwa nguvu na ROHO WA MUNGU hata kupoteza nguvu zote. Msimamo wangu ulikuwa wenye maumivu

mno. Nilianza kujadili mwenyewe kama sikuwa na haki ya kuzuia ushuhuda wangu katika mkutano, na kwa hivyo kuzuia hisia zangu, wakati kulikuwa na upinzani kama huo katika mioyo ya wengine ambao walikuwa wazee kwa umri na uzoefu kuliko mimi. {1T 44.1}

Nilichukua msimamo huu wa ukimya kwa muda, nikijaribu kujiridhisha kwamba kukandamiza ushuhuda wangu hakunizuii mimi kuishi dini yangu kwa uaminifu. Mara nyingi nilijisikia kuvutiwa sana na jukumu langu la kuzungumza katika mkutano, lakini nilijizuia kufanya hivyo, na nilihisi kuwa kwa kufanya hivyo nilimhuzunisha ROHO WA MUNGU. Hata mimi nilibaki mbali na mikutano wakati mwingine kwa sababu ilikuwa ikihudhuriwa na wale ambao ushuhuda wangu uliwaudhi. Nilijizuia kuwakwaza ndugu zangu, na katika hii niliruhusu hofu ya mwanadamu ivunje ule ushirika na MUNGU usioweza kukatizwa ambao ulikuwa umebariki moyo wangu kwa miezi mingi sana. {1T 44.2}

Tulikuwa tumeteua mikutano ya maombi ya jioni katika maeneo tofauti ya jiji ili kuwapa nafasi wote waliopenda kuhudhuria. Familia ambayo ilikuwa mbele zaidi kunipinga ilihudhuria moja ya mikutano hii. Katika mkutano huu, wakati wale waliokusanyika wakiwa wanasali, Roho wa Bwana alikuja juu ya mkutano, na mmoja wa washiriki wa familia hii alilala chini kama aliyekufa. Ndugu zake walisimama wakilia karibu naye, wakisugua mikono yake na kujaribu kumfanyia njia za urejeshaji. Mwishowe alipata nguvu za kutosha kumsifu MUNGU, na akatuliza hofu yao kwa kupiga kelele kwa ushindi juu ya ushahidi uliowekwa wazi wa nguvu za Bwana juu yake. Kijana huyo hakuweza kurudi nyumbani usiku huo. {1T 44.3}

Hii iliaminiwa na familia kuwa dhihirisho la ROHO WA MUNGU, lakini haikuwasadikisha kwamba ni nguvu ile ile ya  Bwana ndiyo ambayo ilikuwa imekaa juu yangu wakati mwingine, ikiniondolea nguvu zangu za asili na kujaza roho yangu na amani na upendo wa Yesu. Walikuwa huru kusema kwamba udhati na unyofu wangu mkamilifu visingeweza kutiliwa shaka, lakini waliniona kwamba najidanganya kwa kudai kuwa na nguvu ya Bwana ambayo kwao ilikuwa ni matokeo ya hisia zangu zilizozidi kipimo. {1T 45.1}

Akili yangu ilishangaa sana na kufadhaika kutokana na upinzani huu, na wakati muda ulipokaribia wa mkutano wetu wa kawaida, nilikuwa na shaka kama lingekuwa ni jambo bora kwangu kuhudhuria. Kwa siku kadhaa zilizopita nilikuwa katika dhiki kubwa kwa sababu ya hisia zilizooneshwa kwangu. Mwishowe niliamua kubaki nyumbani, na hivyo kuepukana na ukosoaji wa ndugu zangu. Katika kujaribu kuomba, nilirudia maneno haya tena na tena: “Bwana, Unataka nifanye nini?” Jibu lililokuja moyoni mwangu lilionekana kunitaka kumtumainia Baba yangu wa mbinguni na kungojea kwa subira kujua mapenzi Yake. Nilijitoa kwa Bwana kwa imani rahisi ya mtoto mdogo, nikikumbuka Yeye alikuwa ameahidi kwamba wale wanaomfuata hawatatembea gizani. {1T 45.2}

Hisia ya wajibu ilinisukuma kwenda kwenye mkutano, na nilienda na uhakikisho kamili akilini mwangu kwamba yote yatakuwa sawa. Tulipokuwa tumeinama mbele za Bwana, moyo wangu ulivutwa kwa maombi na kujazwa na amani ambaye ni Kristo tu anaweza kuitoa. Nafsi yangu ilifurahi kwa upendo wa Mwokozi, na nguvu za mwili ziliniacha. Kwa imani kama ya mtoto ningeweza kusema tu: “Mbingu ni nyumba yangu, na Kristo Mkombozi wangu.”{1T 45.3}

Mmoja wa familia hapo awali aliyetajwa kama anayepinga udhihirisho wa nguvu za MUNGU juu yangu, katika hafla hii alisema imani yake inamuonesha kwamba nilikuwa chini ya msisimko ambao alidhani ni jukumu langu kuupinga, lakini badala ya kufanya hivyo, alidhani mimi niliuhimiza msisimko huo ili iwe alama ya kibali cha MUNGU. Mashaka na upinzani wake haukuniathiri kwa wakati huu, kwani nilionekana kufungwa na Bwana, na kuinuliwa juu ya ushawishi wote wa nje; punde alipokuwa ameacha kusema nami,ikawa mtu mwenye nguvu, na Mkristo aliyejitoa na mnyenyekevu, alipoangushwa chini mbele ya macho yake na nguvu za MUNGU, na chumba kilijazwa na ROHO MTAKATIFU. {1T 46.1}

Baada ya kurudi kwenye hali yake ya kawaida huyu Mkristo mnyekekevu, nilifurahi sana kutoa ushuhuda wangu kwa Yesu na kusema juu ya upendo Wake kwangu. Nilikiri ukosefu wangu wa imani katika ahadi za MUNGU na kosa langu katika kuangalia msukumo wa Roho Wake kutokana na kuwahofu wanadamu, na nikakubali kwamba, licha ya kutokuamini kwangu, Yeye Alinipa ushahidi wa upendo usiopuuzwa wa wema Wake na neema idumuyo. Ndugu aliyekuwa akinipinga aliinuka, na kwa machozi alikiri kwamba hisia zake kunihusu mimi zote zilikuwa ni makosa. Aliniomba msamaha kwa unyenyekevu, na akasema: “Dada Ellen, sitaweka tena kizuizi, hata cha jani moja kavu katika njia yako. MUNGU amenionesha ubaridi na ukaidi wa moyo wangu, ambao ameuvunja kwa ushahidi wa nguvu ZAKE. Hakika nimekosa sana.” {1T 46.2}

Halafu, akigeukia watu, akasema: “Wakati Dada Ellen alipoonekana kuwa mwenye furaha sana, nilifikiria, Je, kwa nini mimi sijisikii hivyo? Kwa nini Ndugu R. hapokei ushahidi kama huo? Kwa kuwa nilikuwa natambua kwa hakika alikuwa Mkristo aliyejitoa lakini hakuna nguvu kama hiyo iliyoanguka juu yake. Nilitoa sala ya kimya kimya, ya kwamba, ikiwa hili lilikuwa ni ushawishi mtakatifu wa MUNGU, basi Ndugu R aupate huo ushawishi jioni hii. {1T 46.3}

“Wakati shauku ya kuona hili ilipokaribia kupanda kutoka moyoni mwangu, Ndugu R. alianguka, akisujudu kwa nguvu ya MUNGU, akilia: 'Bwana afanye kazi!' Moyo wangu umeshawishika kwamba nimekuwa nikipigana vita na ROHO MTAKATIFU, lakini sitamhuzunisha tena kwa kutokuamini kwa ukaidi. Karibu, nuru! Karibu Yesu! Nimerudi nyuma na kuwa mgumu, nikisikia kukerwa kama mtu yeyote angemsifu MUNGU na kudhihirisha utimilifu wa furaha katika upendo Wake; lakini sasa hisia zangu zimebadilishwa, upinzani wangu umefikia mwisho, Yesu amefungua macho yangu, na bado mimi ninaweza kupiga kelele kwa kutoa sifa Zake Yesu mwenyewe. Nimesema mambo machungu na ya

kuwakatakata watu na ya kukatisha tamaa ya dada Ellen ambayo nina huzuni kwa sasa, na ninamuomba anisamehe yeye na wale wengine wote waliopo.” {1T 46.4}

Ndugu R. kisha akatoa ushuhuda wake. Uso wake uliangazwa na utukufu wa mbinguni wakati akimsifu Bwana kwa maajabu aliyoyafanya usiku huo. Alisema: “Mahali hapa pana utakatifu wa ajabu kwa sababu ya uwepo wa Aliye Juu. Dada Ellen, katika siku za usoni utapata msaada wetu na huruma za kukutegemeza, badala ya upinzani mkali ambao umeoneshwa. Tumekuwa vipofu kwa udhihirisho wa ROHO MTAKATIFU wa MUNGU.” {1T 47.1}

Wapinzani wote sasa walileтwa ili wayaone makosa yao na kukiri kwamba kazi hiyo kweli ilikuwa ya Bwana. Katika mkutano wa maombi mara baada ya hapo, kaka ambaye alikuwa amekiri kwamba alikuwa amekosea katika upinzani wake, alipata nguvu ya MUNGU kwa kiwango kikubwa sana kiasi kwamba uso wake uling'aa kwa nuru ya mbinguni, na akaanguka chini akiwa hoi asiye na msaada. Nguvu zake ziliporudi, alikiri tena kwamba alikuwa akipigana kijinga dhidi ya Roho wa Bwana kwa kuthamini hisia alizokuwa nazo dhidi yangu. Katika mkutano mwingine wa maombi bado mtu mwingine wa familia hiyo hiyo alitumiwa kwa namna ile ile na akatoa ushuhuda wa aina ile ile. Majuma machache baadaye, wakati familia kubwa ya Ndugu P. walipokuwa wakisali nyumbani mwao, ROHO WA MUNGU alipita kwenye chumba kama ufagio na kuwaangusha chini waombaji waliopiga magoti. Baba yangu aliingia muda mfupi baadaye, na akawakuta wote, wazazi na watoto, wakiwa wanyonge chini ya nguvu ya Bwana. {1T 47.2}

Utaratibu wenye ubaridi na urasmi ulianza kuyeyuka kabla ya ushawishi mkubwa wa aliye Juu. Wote ambao walikuwa wakinipinga walikiri kwamba walikuwa wamemhuzunisha ROHO MTAKATIFU kwa kufanya hivyo, na waliungana kwa huruma na mimi na kwa upendo kwa Mwokozi. Moyo wangu ulifurahi kwamba rehema ya Mwenyezi Mungu ilikuwa imelainisha njia ili miguu yangu ipate kukanyaga, na Bwana ameithawabisha imelipa imani yangu na tumaini langu kwa ukarimu. Umoja na amani sasa vilikaa kati ya watu wetu ambao walikuwa wakitarajia kuja kwa Bwana. {1T 48.1}

# SURA YA 6

# UZOEFU WA MAREJEO

Kwa umakini na kutetemeka tulikaribia wakati huo [mwaka 1843, katika Kalenda ya Wayahudi, uliaminiwa kufikiwa kuanzia Machi 21, 1843, hadi Machi 21, 1844. Wale waliopata imani ya mbali walitarajia kuja kwa Kristo wakati wa mwaka huo.] Wakati Mwokozi wetu alitarajiwa kuonekana, kwa bidii kubwa

tulitafuta, kutakasa maisha yetu ili tuwe tayari kukutana naye wakati wa kuja kwake. Licha ya upinzani wa wachungaji na makanisa, Ukumbi wa Beethoven hall, katika jiji la Portland, ulikuwa unafurika kila usiku; na kusanyiko kubwa zaidi lilikuwa siku ya jumapili. Mzee stockman alikuwa mtu wa uchaji Mungu wa kina. Alikuwa na afya dhaifu; lakini aliposimama mbele ya watu, alionekana kuinuliwa juu ya udhaifu wa mwili, na uso wake ulikuwa umeangaziwa na ufahamu unaodhihirisha kwamba alikuwa akifundisha Ukweli mtakatifu wa MUNGU. {1T 48.2}

Kulikuwa na nguvu, nguvu ya dhati inayotafiti katika maneno yake iliyogusa mioyo ya wengi. Wakati mwingine alionesha hamu ya dhati ya kuishi mpaka atakapomkaribisha Mwokozi ajapo katika mawingu ya mbinguni. Chini ya huduma yake ROHO WA MUNGU aliwashawishi wenye dhambi wengi na kuwaleta katika zizi la Kristo. Mikutano bado ilifanyika katika nyumba za watu binafsi katika sehemu tofauti za jiji na matokeo yalikuwa mazuri. Waumini walihamasishwa kufanya kazi kwa rafiki na jamaa zao, na uongofu ulikuwa ukiongezeka siku hadi siku. {1T 48.3}

Makundi yote yalifurika kwenye mikutano huko Beethoven Hall. Tajiri na maskini, wa juu na wa chini, wachungaji na washiriki au walei wa kawaida, wote, kutoka katika nyanja mbali mbali, walikuwa na hamu ya kusikia wenyewe Fundisho la imani la ujio wa pili wa Kirsto. Watu wengi walikuja, ambao, baada ya kukosa nafasi ya kusimama, walikwenda wakiwa wamekata tamaa. Mpangilio wa mikutano ulikuwa rahisi. Hotuba fupi na yenye mwelekeo mmoja ilitolewa, kisha kukawa na uhuru juu ya mawaidha ya jumla. Kulikuwa, na sheria, iliyosababisha utulivu kamili kwa kadri ilivyowezekana kwa umati mkubwa sana. Bwana alishikilia roho ya upinzani wakati watumishi Wake walipokuwa wakielezea sababu za imani yao. Wakati mwingine chombo kinachobeba Ujumbe kilikuwa dhaifu, lakini ROHO WA MUNGU aliupa uzito na nguvu Ukweli Wake. Uwepo wa malaika watakatifu ulihisiwa katika mkutano huo, na idadi iliongezeka kila siku kwa kikundi hicho kidogo cha waumini. {1T 49.1}

Wakati mmoja, wakati Mzee Stockman alipokuwa akihubiri, Mzee Brown, mhudumu Mkristo wa Baptisti, ambaye jina lake limetajwa hapo awali katika kisa hiki, alikuwa amekaa kwenye dawati akisikiliza mahubiri hayo kwa hamu kubwa (wote wawili walikuwa huko kibwetani). Ndipo alipoguswa sana, na ghafla uso wake ukawa mweupe sana kama umepauka au kama mtu aliyekufa, kisha akapoteza balansi kwenye kiti chake, na Mzee Stockman akamdaka mikononi mwake kabla hajaanguka chini, na kumlaza kwenye sofa nyuma ya kibweta, ambapo alilala akiwa hana nguvu mpaka hubiri/mazungumzo yalipomalizika. {1T 49.2}

Kisha akainuka, uso wake ungali mweupe kupindukia*, lakini akiangazwa na nuru kutoka Jua la Haki, na kutoa ushuhuda wa kuvutia sana. Alionekana kupokea mafuta matakatifu kutoka juu. Kwa kawaida alikuwa mzito kuongea,

mwenye maneno machache ya dhati na bidii, na huru kabisa kutokana na msisimko. Katika hafla hii maneno yake adhimu ambayo ni machache, na yaliyopimwa yalibeba nguvu mpya wakati alipowaonya watenda dhambi na ndugu zake wachungaji/hudumu waweke mbali kutokuamini, ubaguzi, na urasmi, ratiba na desturi zisizo na ari, kaida, ubaridi, na, kama Waberoya waungwana, wayachunguze Maandiko matakatifu, wakilinganisha andiko na andiko, kuhakikisha ikiwa mambo haya hayakuwa ya kweli. Yeye aliwasihi wachungaji waliokuwepo wasijisikie kujeruhiwa kwa njia ya moja kwa moja na ya kujichunguza ambayo Mzee Stockman alikuwa amewasilisha mada muhimu ambayo ilivutia akili zote *(Watu wa rangi nyeupe mara zingine rangi yao ya uso hubadilika kutokana na hisia, mfano nyekundu sana akiwa amekasirika au amepata aibu ya ghafla na nyeupe sana kuliko kawaida kama amepata mshtuko, au ana afya mbaya, ikionyesha mzunguko wa damu siyo mzuri nk hii nyeupe huitwa pale). {1T 49.3}

Alisema: "Tunataka kuwafikia watu; tunataka wenye dhambi wasadikishwe moyoni na watubu kweli kweli kabla hawajachelewa kuokolewa, wasije wakaomboleza," ‘Mavuno yamepita, majira yamekwisha, na sisi hatujaokoka Yeremia 8:20”. 'Ndugu zangu katika huduma (wachungaji) husema kwamba mishale yetu inawagonga; Je! Wanaweza kusimama kando kati yetu na watu wasiowekewa mkono ili sisi tufikie mioyo ya wenye dhambi? Ikiwa wanajifanya wao ndiyo walengwa wa lengo letu, basi hawana sababu ya kulalamika kuhusu jeraha wanazopata. Simameni kando, ndugu, na humtapata kipigo! " {1T 50.1}

Alisimulia uzoefu wake mwenyewe kwa unyenyekevu, usahili, ujasiri na akawa mwazi na mkweli, kiasi kwamba wengi ambao walikuwa na ubaguzi mkubwa waliathiriwa na kulia machozi. ROHO WA MUNGU alihisiwa katika maneno yake na kuonekana juu ya uso wake. Kwa kuinuliwa kutakatifu alitangaza kwa ujasiri kwamba amelichukua Neno la MUNGU kama mshauri wake, kwamba mashaka yake yameondolewa na imani yake imethibitishwa. Kwa bidii aliwaalika ndugu zake wachungaji, wahudumu, washiriki wa kanisa, watenda dhambi, na makafiri kuichunguza wenyewe Biblia, na kuwaamuru wasiruhusu mtu yeyote awaondoe kutoka kwa kusudi la kujua Ukweli ni upi. {1T 50.2}

Mzee Brown wakati huo na baadaye hakukatisha uhusiano wake na Kanisa la Kikristo la Kibaptisti, lakini alitazamwa kwa heshima kubwa na watu wake. Alipomaliza kusema, wale waliotamani maombi ya watu wa MUNGU walialikwa kusimama. Mamia waliitikia wito huo. ROHO MTAKATIFU akakaa juu ya mkutano. Mbingu na dunia zilionekana kukaribiana. Mkutano ulidumu hadi saa moja usiku. Nguvu ya Bwana ilihisiwa juu ya vijana, wazee, na wenye umri wa kati. {1T 50.3}

Tuliporudi majumbani mwetu kwa njia mbali mbali, sauti ya kumsifu MUNGU ingeweza kutufikia kutoka katika uelekeo mmoja, kama namna ya mwitikio, wa sauti hiyo, ilitoka sauti kwingine na upande ule pia, na mwingine ukapaza

sauti kelele: “Utukufu kwa MUNGU, Bwana anatawala!” Watu waliziendea nyumba zao wakitoa sifa kwenye midomo yao, na sauti ya shangwe ilisikika juu ya anga tulivu la usiku ikipaa. Hakuna mtu aliyehudhuria mikutano hii anayeweza kusahau matukio hayo ya kupendeza sana. {1T 50.4}

Wale wanaompenda Yesu kwa dhati wanaweza kufahamu hisia za wale ambao walitazamia kwa hamu kubwa sana kuja kwa Mwokozi wao. Pointi ya matarajio ilikuwa inakaribia. Wakati ambao tulitarajia kukutana Naye Yesu ulikuwa umekaribia. Tulikaribia saa hii kwa utulivu na kicho. Waumini wa kweli walijituliza juu ya mahusiano mazuri na MUNGU-Ushirika mtamu Naye - amani ya dhati ambayo ingekuwa yao katika maisha angavu ya baadaye huko mbinguni. Hakuna aliyepata tumaini, uhakikisho na ujasiri huu anayeweza kusahau masaa hayo ya kumngojea Bwana. {1T 51.1}

Biashara za kidunia kwa sehemu kubwa ziliwekwa kando kwa majuma kadhaa. Tulichunguza kwa uangalifu kila wazo na hisia za mioyo yetu, kana kwamba tuko juu ya vitanda vyetu vya kifo tukisubiria kifo, kama watu wanaochungulia kaburi, kwamba masaa machache watafumba macho yetu milele kwa mambo ya ulimwengu huu. Hapakuwa na kujishonea “mavazi ya kupaa kwenda mbinguni au ascension robes (kama machapisho mengine yanavyosema)” kwa ajili ya tukio lile kuu; tulisikia hitaji la ushahidi wa ndani kwamba tulikuwa tunaandaliwa kukutana na Kristo, na mavazi yetu meupe yalikuwa utakaso wa roho, tabia iliyosafishwa kutoka dhambini kwa damu ya upatanisho ya Mwokozi wetu. {1T 51.2}

Lakini wakati wa matarajio ya Yesu kuja ulipita. Huu ulikuwa mtihani wa kwanza wa karibu ulioletwa ili wale walioamini waubebe na kutumaini kwamba Yesu atakuja katika mawingu ya mbinguni. Kukatishwa tamaa kwa watu wa MUNGU waliokuwa wakingoja kulikuwa kukubwa. Wenye dhihaka walishinda na wakawashinda watu walio dhaifu na waoga kwa safu zao. Wengine ambao walionekana kuwa na imani ya kweli walionekana kushawishiwa tu na hofu; na sasa ujasiri wao ulirudi baada ya muda kupita, na kwa ujasiri waliungana na wafanya dhihaka, wakitangaza kwamba wao hawajawahi kudanganyika kuamini mafundisho ya Miller kuwa ni ya kweli, kwa kuwa alikuwa mtu mwenye misimamo mikali ya kidini na mwendawazimu. Na wengine, kwa asili walikuwa na misimamo ya kujisalimisha kirahisi, na inayomangamanga, mara wakubali mara wakatae na hatimaye kimya kimya wakajitoa. Nilijiuliza, kama kweli Kristo angekuja, ingekuwaje kwa wale dhaifu na vigeugeu waliokuwa wakibadilika badilika? Walijidai kumpenda Yesu na kutamani ujio Wake, lakini wakati hakutokea, walionekana wamefarijika na wakashusha pumzi kwamba ni afadhali imekuwa hivyo na kisha wakarudi katika hali ya uzembe na hali ya kutojali mambo ya dini ya Kweli. {1T 51.3}

Tulifadhaika na kuvunjika moyo, lakini hatukuikana imani yetu. Wengi bado walishikilia matumaini kwamba Yesu asingechelewesha ujio wake kwa muda

mrefu; Neno la Bwana lilikuwa thabiti, lisingeweza kushindwa. Tulihisi kuwa tumetimiza wajibu wetu, tumeishi kwa imani yetu ya thamani; tulikata tamaa, lakini hatukuvunjika moyo. Ishara za nyakati zilionesha kwamba mwisho wa vitu vyote umekaribia; lazima tujichunge na kujiweka tayari kwa kuja kwa Bwana wakati wowote. Lazima tungoje kwa matumaini na uaminifu, bila kupuuza kujikusanya pamoja kwa ajili ya kufundishana, kutiana moyo, na kufarijiana, ili nuru yetu iangaze katika giza la ulimwengu (Ebra 10:25). {1T 52.1}

Hesabu ya wakati huo ilikuwa rahisi na wazi kiasi kwamba hata watoto wangeweza kuielewa. Kuanzia tarehe ya amri ya mfalme wa Uajemi, inayopatikana katika Ezra 7, ambayo ilitolewa mnamo 457 kabla ya Kristo, miaka 2300 ya Danieli 8:14 lazima ikome ifikapo 1843 BK. Kwa hivyo tuliangalia mwisho wa mwaka huu kwa kuja ya Bwana. Tulisikitishwa sana wakati mwaka wote ulipopita kabisa na Mwokozi asije. {1T 52.2}

Haikufahamika mwanzoni kwamba ikiwa agizo halikutolewa mwanzoni mwa mwaka 457 KK, miaka 2300 isingekamilishwa mwishoni mwa 1843BK. Lakini ilibainika kuwa amri hiyo ilitolewa karibu na mwisho wa mwaka 457 KK, na kwa hivyo kipindi cha kinabii lazima kifikie hadi mwisho wa mwaka wa 1844 BK. Kwa hivyo maono ya wakati hayakukawia, ingawa yalionekana kama yanafanya hivyo. Tulijifunza kuweka pumziko letu juu ya lugha ya nabii. "Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia-Habakuki 2:3." {1T 52.3}

MUNGU aliwapima na kuwathibitisha watu wake kwa kupitisha muda mnamo 1843. Makosa yaliyofanywa katika kuhesabu vipindi vya kiunabii hayakugundulika mara moja hata na watu wenye elimu ambao walipinga maoni ya wale ambao walikuwa wanatafuta kuja kwa Kristo. Wasomi walitangaza kwamba Bwana Miller alikuwa sahihi katika hesabu yake ya wakati huo, ingawa walimpinga kwa sababu ya tukio ambalo alidai lingetokea kipindi hicho. Lakini wao, na watu wa MUNGU waliokuwa wakingoja, walikuwa kwenye kosa lile lile juu ya swali la wakati. {1T 52.4}

Tunaamini kabisa kwamba MUNGU, kwa hekima Yake, alipanga watu Wake wakutane na hali ya kukata tamaa, ambayo ilikuwa imepigiwa mahesabu vizuri iweze kufunua mioyo na kukuza tabia za Kweli za wale ambao walidai kumtafuta na kufurahi katika kuja kwa Bwana. Wale waliokumbatia ujumbe wa malaika wa kwanza (Angalia Ufunuo 14: 6, 7) kwa kuogopa hasira ya hukumu za MUNGU, si kwa kuwa walipenda Ukweli na walitamani urithi katika ufalme wa mbinguni, sasa walionekana katika nuru yao halisi. Walikuwa kati ya watu wa kwanza kuwadhihaki wale waliokata tamaa ambao walitamani na kupenda kwa dhati kutokea kwa Yesu. {1T 53.1}

Wale ambao walikuwa wamekata tamaa hawakubaki kwa muda mrefu gizani; kwani kwa kuchunguza vipindi vya unabii na kwa kuomba kwa bidii, kosa

liligunduliwa, na ufuatiliaji wa maandishi ya kiunabii kupitia nyakati za kukawia ukafuatia. Katika matarajio ya furaha ya kuja kwa Kristo, ucheleweshaji dhahiri wa maono haukutiliwa maanani, maana ulikuwa mshangao usiotarajiwa na mchungu. Hata hivyo jaribu hili lilikuwa la lazima katika kukuza na kuimarisha waumini wanyofu katika Ukweli. {1T 53.2}

Matumaini yetu sasa yalilenga kuja kwa Bwana mnamo 1844. Huu pia ulikuwa wakati wa ujumbe wa malaika wa pili, ambaye, akiwa anaruka katikati ya mbingu, alilia: "Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa." Ujumbe huo ulitangazwa kwa mara ya kwanza na watumishi wa MUNGU katika msimu wa joto wa 1844. Matokeo yake, wengi waliyaacha makanisa yaliyoanguka. Kuhusiana na ujumbe huu wa kilio cha usiku wa manane [Tazama Mathayo 25: 1-13.] kilitolewa: "Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki." Katika kila sehemu ya nchi, nuru ilitolewa kuhusu ujumbe huu, na kilio kiliamsha maelfu. Kilienda kutoka mji hadi mji, kutoka kijiji hadi kijiji, na katika maeneo ya mashambani. Kiliwafikia wasomi na wenye talanta, hali kadhalika wale wasiojulikana na wanyenyekevu. {1T 53.3}

Huu ulikuwa mwaka wa furaha zaidi maishani mwangu. Moyo wangu ulijaa matarajio ya furaha, lakini nilihisi huruma na wasiwasi mkubwa kwa wale ambao walikuwa wamevunjika moyo na hawakuwa na tumaini ndani ya Yesu. Tuliungana, katika maombi ya dhati kwa uzoefu wa Kweli na ushahidi dhahiri wa kukubalika kwetu na MUNGU. {1T 54.1}

Tulihitaji uvumilivu mkubwa, kwani wafanya dhihaka walikuwa wengi. Mara kwa mara tulisalimiwa kwa kurejelewa/kumbukizi ya dhihaka juu ya kukatishwa tamaa kwetu kulikopita. "Bado haujapanda kwenda mbinguni juu; Je, unatarajia kwenda juu lini?" Na kejeli kama hizo mara nyingi zilimwaga juu yetu kwa jeuri na watu tuliowajua vyema, na hata na wengine waliojiita Wakristo ambao waliikubali Biblia, lakini walishindwa kujifunza Ukweli Wake mkubwa na wa muhimu. Macho yao yaliyopofushwa yalielekea kuona jambo katika hali isiyo ya wazi na ya mbali katika onyo kali, MUNGU " Yeye ameweka siku atakayowahukumu walimwengu-Matendo 17:31," na katika uhakikisho kwamba watakatifu watanyakuliwa pamoja ili wamlaki Bwana hewani (1Thes 4:12). {1T 54.2}

Makanisa ya kawaida yalitumia kila njia kuzuia kuenea kwa imani ya kwamba Kristo atakuja hivi karibuni. Hakuna uhuru uliotolewa katika mikutano yao kwa wale waliothubutu kutaja tumaini la kuja kwa Kristo hivi karibuni. Waliodai kumpenda Yesu kwa dharau walikataa habari kwamba Yeye ambaye walidai kuwa rafiki yao wa karibu, atawatembelea hivi karibuni. Walisisimka na kukasirika dhidi ya wale waliotangaza habari za kuja Kwake, na ambao walifurahi kwamba wangemwona Yesu haraka katika utukufu Wake. {1T 54.3}

Kila muda ulionekana kwangu kuwa wenye umuhimu mkubwa. Nilihisi kuwa tunafanya kazi kwa umilele na kwamba wazembe na wasio na hamu walikuwa katika hatari kubwa. Imani yangu haikufunikwa na wingu, na nilijitwalia ahadi za Yesu na kuzifanya zangu. Yeye Alikuwa amewaambia wanafunzi Wake: “Ombeni, nanyi mtapewa.” Niliamini kabisa kwamba chochote nitakachoomba kulingana na mapenzi ya MUNGU  hakika nitapewa. Nilizama kwa unyenyekevu miguuni pa Yesu, huku moyo wangu ukipatana na mapenzi Yake. {1T 54.4}

Mara nyingi nilizitembelea familia na kuwaombea kwa bidii wale ambao walikuwa wameonewa na hofu na kukata tamaa. Imani yangu ilikuwa na nguvu sana kiasi kwamba sikuwahi kutilia shaka wakati wowote kwamba MUNGU angejibu maombi yangu, na hapakuwa na wakati hata mmoja ambapo baraka na amani ya Yesu ziliacha kutulia juu yetu kama majibu ya maombi yetu ya unyenyekevu, na mioyo ya wale waliokata tamaa ilifanywa kuwa ya furaha kwa nuru na tumaini. {1T 55.1}

Tukitafuta kwa bidii na uadilifu na maungamo ya moyo na ya unyenyekevu tulikuja kwenye maombi katika wakati uliotarajiwa. Kila asubuhi tulihisi kuwa kazi yetu ya kwanza ilikuwa kupata ushahidi kwamba maisha yetu yalikuwa tuliyaweka sawa mbele za MUNGU. Shauku na upendo wetu kwa watu na wengine miongoni mwetu uliongezeka; tuliomba kwa ajili ya wenzetu na tuliombeana. Tulikusanyika bustanini na kwenye vijisitu vya miti ili kuzungumza na MUNGU  na kutoa ombi letu Kwake, tukijisikia kuwa vyema na kamili zaidi mbele Yake tukiwa tumezungukwa na kazi zake za asili. Furaha ya wokovu ilikuwa muhimu zaidi kwetu kuliko chakula na vinywaji. Ikiwa mawingu yalificha akili zetu, sisi hatukuthubutu kupumzika au kulala mpaka yawe yamesombwa na ufahamu wa kukubaliwa kwetu na Bwana. {1T 55.2}

Afya yangu ilikuwa mbaya sana, mapafu yangu yaliathiriwa vibaya, na sauti yangu ilishindwa kutoka. ROHO WA MUNGU  mara nyingi alikaa juu yangu kwa nguvu kubwa, na mwili wangu dhaifu haukuweza kuvumilia utukufu uliofurikia roho yangu. Nilionekana kupumua katika anga la mbinguni, na nilifurahi katika matarajio ya hivi karibuni kukutana na Mkombozi wangu na kuishi milele katika nuru ya uso Wake. {1T 55.3}

Watu wa MUNGU  waliokuwa wakingoja walikaribia saa ambayo walitumaini kuwa furaha yao ingekuwa kamili katika kuja kwa Mwokozi. Lakini wakati ulipita tena bila kuwepo kwa tukio la ujio wa Yesu. Ilikuwa vigumu kuyaanza tena maisha ambayo tulidhani tumeondokana nayo milele. Kulikuwa kukatishwa tamaa kuchungu kulikoliangukia kundi dogo ambalo imani yake ilikuwa imara na matumaini yake yalikuwa ya juu sana. Lakini tulishangaa kwamba tulijihisi huru sana katika Bwana kwa kuwa na moyo mkunjufu na tulitegemezwa sana na nguvu na neema Yake. {1T 55.4}

Uzoefu wa mwaka uliopita, hata hivyo, ulijirudia kwa kiasi kikubwa. Jamii kubwa iliikana imani yao. Wengine, ambao walikuwa wamejiamini sana,

walikuwa wameumizwa sana kutokana na majivuno yao kiasi kwamba walihisi kuukimbia ulimwengu. Kama Yona, walimlalamikia MUNGU, na wakachagua kifo badala ya uzima. Wale ambao walikuwa wamejenga imani yao juu ya ushahidi wa wengine, na siyo juu ya Neno la MUNGU, walikuwa sasa wapo tayari kubadilisha mtazamo wao. Wanafiki, ambao walikuwa na matumaini ya kumdanganya Bwana na kujidanganya wao wenyewe kwa mwonekano wa toba yao ya bandia na kwa kujitoa kwao kwa bandia, sasa walijihisi kufarijika, kupata afueni na hatari inayowakaribia, na waliipinga waziwazi kazi waliyodai kuipenda. {1T 56.1}

Wanyonge na waovu waliungana katika kutangaza kwamba sasa hapawezi kuwa na hofu au matarajio zaidi sasa. Wakati ulikuwa umepita, Bwana alikuwa hajaja, na ulimwengu ungeendelea kuwa vile vile kwa maelfu ya miaka. Jaribio/Mtihani huu wa mkubwa wa pili ulifunua mkondo mkubwa usio na manufaa wa matembezi yasiyofaa ambayo yalikuwa yamevutwa katika mkondo wenye nguvu ya imani ya ujio wa mara ya pili wa Bwana, na umeendelea kubebwa kwa muda na waumini wa kweli na watendakazi dhati na wenye bidii. {1T 56.2}

Tulikata tamaa, lakini hatukuvunjika moyo. Tuliazimia kuwasilisha kwa subira mchakato wa kutakasa ambao MUNGU aliona ni muhimu kwetu, na kungojea kwa tumaini la subira kwa Mwokozi kuwakomboa wale waliojaribiwa na waaminifu. {1T 56.3}

Tulikuwa thabiti katika imani kiasi kwamba hubiri juu ya wakati mahsusi (uliobainishwa) lilikuwa la MUNGU. Ilikuwa hali hii ndiyo iliyowasukuma watu kuichunguza Biblia kwa juhudi, wakagundua Ukweli ambao hawakuwa wameona hapo awali. Yona alitumwa na MUNGU kutangaza katika mitaa ya Ninawi kwamba ndani ya siku arobaini mji utaangamizwa; bali MUNGU alikukubali kujidhili kwa Waninawi na kuongeza muda wao wa kupimwa. Hata hivyo ujumbe ambao Yona aliuleta ulitumwa na MUNGU, na Ninawi ilitathminiwa kulingana na mapenzi Yake. Ulimwengu uliangalia tumaini letu kama udanganyifu, na kukata tamaa kwetu kama kutofaulu kwake. {1T 56.4}

Maneno ya Mwokozi katika kisa cha mtumwa mwovu yanatumika kwa nguvu sana kwa wale wanaodhihaki ukaribu wa kuja kwa Mwana wa Adamu: "Lakini mtumwa yule mbaya alisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia; akaanza kuwapiga wajoli wake, na kula na kunywa pamoja na walevi; bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani, na saa asiyojua, atamkata vipande viwili, na kumwekea fungu lake pamoja na wanafiki-Luka 12."{1T 57.1}

Tuliwakuta kila mahali wenye kudhihaki ambao Petro alisema watakuja siku za mwisho, wakifuata tamaa zao wenyewe, wakisema: "Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake? Kwa maana, tangu hapo babu zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa." Lakini wale ambao walikuwa wakikutazamia kuja kwa Bwana hawakukosa faraja. Walikuwa wamepata

maarifa muhimu katika kutafuta Neno. Mpango wa wokovu ulikuwa wazi na sahili kwa uelewa wao. Kila siku waligundua uzuri mpya kwenye kurasa takatifu, na mapatano, na ulinganifu wa kushangaza ulikuwa katika Maandiko yote, Andiko moja likifafanua Andiko jingine, na hakuna Neno lililotumika isivyotakiwa. {1T 57.2}

Kukata tamaa kwetu hakukuwa kukubwa kama kule kwa wanafunzi. Wakati Mwana wa Adamu alipopanda kwa ushindi kwenda Yerusalemu, walitarajia kuwa angetawazwa awe mfalme. Watu walimiminika kutoka miji yote ya karibu, wakipiga kele: "Hosana Mwana wa Daudi." Wakati makuhani na wazee walipomsihi Yesu autulize umati, alitangaza kwamba ikiwa watanyamaza hata mawe yatapiga kelele, kwa kuwa unabii lazima utimizwe. Hata hivyo katika siku chache wanafunzi hawa walimwona Bwana wao mpendwa, ambaye waliamini atatawala kwenye kiti cha enzi cha Daudi, akiwa ametundikwa juu ya msalaba kikatili ilihali Mafarisayo wakimdhihaki na kumsuta kwa maneno ya jeuri. Matumaini yao makubwa yalikatishwa tamaa, na giza la mauti likawafunga. {1T 57.3}

Lakini Kristo alikuwa mwaminifu kwa ahadi Zake. Faraja aliyowapatia watu wake ilikuwa tamu, na thawabu ya watu wakweli na waaminifu ilikuwa ya thamani. {1T 58.1}

Bwana Miller na wale ambao walikuwa katika ushirika naye walidhani utakaso wa Patakatifu unaozungumziwa katika Danieli 8:14 ulimaanisha utakaso wa dunia kwa njia ya moto kabla haijawa makao ya watakatifu. Jambo hili lilikuwa lifanyike wakati wa kuja kwa Kristo; na kwa hivyo tulikuwa tukilisubiria tukio hilo mwishoni mwa siku au miaka 2300. Lakini baada ya kukatishwa tamaa kwetu, Maandiko yalichunguzwa kwa maombi na kwa kutafakari kwa dhati na ari, na baada ya kipindi cha mashaka, mwanga ulimiminika juu ya giza letu; mashaka na kutokuwa na uhakika vikafagiliwa mbali. {1T 58.2}

Badala ya unabii wa Danieli 8:14 kutuelekeza kwenye utakaso wa dunia, ilikuwa wazi sasa kuwa uliashiria kazi ya kufunga kazi kwa Kuhani wetu Mkuu mbinguni, akikamilisha upatanisho, na kuandaa watu katika kuikabili siku ya kuja Kwake. {1T 58.3}

## SURA YA 7

## MAONO YANGU YA KWANZA

Haikuchukua muda mrefu baada ya kupita kwa wakati wa kumngoja Bwana arudi, hii mnamo 1844 nilipopewa maono yangu ya kwanza. Nilikuwa

nikimtembelea dada mpendwa katika Kristo, ambaye moyo wake uliunganishwa na moyo wangu; watano wetu, wote wanawake, tulikuwa tukipiga magoti kimya kimya kwenye madhabahu ya familia. Tulipokuwa tunaomba, nguvu ya MUNGU ilinijia kwa namna ambayo sikuwahi kuihisi hapo kabla. Nilionekana niliyezungukwa na nuru, na niliyekuwa nikisogea kuelekea juu na juu zaidi kutoka duniani. Niligeuka kuwatafuta Waadventista ulimwenguni yaani watu waliokuwa wanamngoja Yesu kurudi, lakini sikuwapata, wakati sauti iliponiambia: "Angalia tena, angalia kidogo juu." Wakati huu niliinua macho yangu na kuona njia iliyonyooka na nyembamba, iliyoinuliwa juu ya ulimwengu. Kwenye njia hii Waadventista walikuwa wakisafiri kuelekea mjini. Nyuma yao, mwanzoni mwa njia, kulikuwa na mwanga mkali ambao malaika aliniambia ulikuwa kilio cha usiku wa manane. Nuru hii iliangaza njiani kote, ili miguu yao isije ikakwazwa.Yesu Mwenyewe alienda mbele tu ya watu wake akiwaongoza, na kwa kadri walivyomkazia macho, walibaki salama. Lakini punde wengine walichoka, na kusema mji ulikuwa mbali sana, na walikuwa wametarajia kuwa wangekuwa wameuingia hapo kabla. Ndipo Yesu angewatia moyo kwa kuinua mkono wake wa kulia wa utukufu, ambao kutoka Kwake ukaja mwanga uliopepea juu ya kundi la Wanamarejeo; nao wakapiga kelele: "Haleluya!" Wengine kwa haraka wakaikana nuru iliyoangaza kutoka nyuma yao, wakisema siyo MUNGU aliyewaongoza hadi sasa. Nuru nyuma yao ikazimwa, ikiacha miguu yao katika giza kamili, na wakakwazwa na kumpoteza Yesu na alama iliyowaongoza nao wakadondoka kando ya njia hadi chini kwenye korongo la ulimwengu wa giza na maovu. {1T 58.4}

Mara tulisikia sauti ya MUNGU kama ya maji mengi, iliyotujulisha siku na saa ya kuja kwa Yesu. Watakatifu walio hai, 144,000 kwa idadi yao, waliifahamu na kuielewa sauti, wakati waovu wakidhani ni radi na tetemeko la ardhi. Wakati MUNGU alipotamka muda, alimimina juu yetu ROHO MTAKATIFU, na nyuso zetu zilianza kuwaka na kuangaza kwa utukufu wa MUNGU, kama Musa wakati aliposhuka kutoka Mlima Sinai. {1T 59.1}

144,000 wote walikuwa wamepigwa mihuri na wameunganishwa kikamilifu. Kwenye paji la uso wao palikuwa na maneno MUNGU, Yerusalemu Mpya, na nyota tukufu iliyo na Jina jipya la Yesu. Katika hali yetu ya furaha na takatifu waovu walikuwa wamekasirika, na walitamani kutukimbilia kwa ukatili ili watukamate na kututia gerezani, ndipo tulinyosha mkono kwa Jina la Bwana, na wakaanguka chini bila msaada wowote. Ndipo sinagogi la Shetani likatambua kwamba MUNGU alikuwa ametupenda sisi ambao tungeweza kuoshana miguu, na kuwasalimu ndugu kwa busu takatifu, hivyo wakaabudu miguuni mwetu. {1T 59.2}

Punde macho yetu yalivutwa kuelekea mashariki, kwa kuwa wingu dogo jeusi lilikuwa likitokea, lenye ukubwa wa nusu ya mkono wa mtu, ambalo sisi sote tulijua ni ishara ya Mwana wa Adamu. Kimya kwa kicho, sisi sote tuliliangalia wingu lilipokuwa linakaribia, likiwa jepesi, tukufu, na linaloongezeka utukufu

zaidi, mpaka likawa wingu kubwa jeupe. Chini palionekana kama moto; upinde wa mvua ulikuwa juu ya wingu, likiwa limezungukwa na malaika elfu kumi, wakiimba wimbo mtamu zaidi; na juu yake Mwana wa Adamu ameketi. Nywele zake zilikuwa nyeupe na zilizojisokota mpaka juu ya mabega Yake, na juu ya kichwa CHAKE kulikuwa na taji nyingi. Miguu Yake ilionekana kama moto; katika mkono Wake wa kulia alikuwa na mundu mkali, katika mkono Wake wa kushoto tarumbeta ya fedha. Macho Yake yalikuwa kama mwali wa moto, ambao uliwachunguza watoto Wake kila mahali,na hata ndani kabisa. {1T 60.1}

Kisha nyuso zote zikawa na rangi nyeupe, na zile ambazo MUNGU alikuwa amezikataa zikawa nyeusi. Ndipo tukalia wote: "Ni nani atakayeweza kusimama? Je! Vazi langu halina doa?" Malaika waliacha kuimba, na kulikuwa na wakati wa ukimya wa kutisha, ndipo Yesu aliposema: "Wale walio na mikono safi na mioyo safi wataweza kusimama; Neema Yangu inawatosha ninyi." Wakati huu, nyuso zetu ziliangaza, na furaha ilijaa kwenye kila moyo. Na malaika kwa kupiga noti za juu wakaimba tena, wakati wingu likisogea karibu na dunia. Kisha tarumbeta ya Yesu ya fedha ikasikika, aliposhuka juu ya wingu, akiwa amevishwa na kuzungukwa kwa miali ya moto. Alitazama juu ya makaburi ya watakatifu waliolala, kisha akainua macho Yake na mikono mbinguni, na kupaza sauti: "Amkeni! Amkeni! Amkeni! Ninyi mnaolala kwenye mavumbi, simameni." Kisha kulikuwa na tetemeko kubwa la ardhi. Makaburi yakafunguliwa, na wafu wakaja wakiwa wamevavishwa mavazi ya kutokufa. Wale 144,000 walipiga kelele, "Haleluya!" kwa vile waliwatambua marafiki zao waliokuwa wametengwa nao kwa kifo, na katika wakati huo huo kufumba na kufumbua tulibadilishwa, na kunyakuliwa pamoja nao kukutana na Bwana hewani. {1T 60.2}

Sisi sote tuliingia ndani ya wingu pamoja, na kwa siku saba tulikuwa tukipaa tukielekea bahari ya kioo, wakati Yesu alipoleta taji, na kwa mkono Wake wa kulia aliziweka juu ya vichwa vyetu. Yeye Alitupatia vinubi vya dhahabu na mitende ya ushindi. Hapa kwenye bahari ya kioo wale 144,000 walisimama kwenye mraba kamili. Wengine walikuwa na taji zenye kung'aa sana, na wengine zisizo za kung'aa sana. Taji zingine zilionekana kuwa na nyota nyingi, wakati zingine zilikuwa na chache tu. Wote waliridhika kabisa na taji zao. Na wote walikuwa wamevikwa joho jeupe tukufu kutoka mabegani mwao hadi miguuni. Malaika walikuwa wakituongoza sisi wakati tulipokuwa tukizunguka bahari ya kioo hadi kwenye lango la jiji. Yesu aliinua mkono Wake wenye nguvu na utukufu, akalishika lango la lulu, akalirudisha nyuma kwenye bawaba zake zenye kung'aa, na kutuambia: "Mmeosha mavazi yenu katika damu Yangu, mmesimama kwa bidii kwa ajili ya Ukweli Wangu, ingieni." Sisi sote tuliandamana na kuhisi tunayo haki kamili hapo. {1T 60.3}

Ndani ya mji huo tuliona mti wa uzima na kiti cha enzi cha MUNGU. Kutoka kwenye kiti cha enzi ulitoka mto safi wa maji, na upande mwingine wa mto kulikuwa na mti wa uzima. Upande mmoja wa mto kulikuwa na shina la mti, na

shina lingine upande wa pili wa mto, yote ya dhahabu safi, iliyo wazi. Mwanzoni nilifikiri niliona miti miwili; Nikaangalia tena, na kuona kuwa ilikuwa imeungana kwa juu katika mti mmoja. Kwa hivyo ulikuwa mti wa uzima pande zote za mto wa uzima. Matawi yake yaliinama mahali pale tuliposimama; na matunda yalikuwa matukufu, ambayo yalionekana kama dhahabu iliyochanganywa na fedha. {1T 61.1}

Sisi sote tulikwenda chini ya mti, na tukakaa kuangalia utukufu wa mahali hapo, wakati ndugu Fitch na Stockman, ambao walikuwa wamehubiri injili ya ufalme, na ambao MUNGU alikuwa amewalaza kaburini ili kuwaokoa, walipokuja kwetu, na kutuuliza tulipitia nini wakati wao walipokuwa wamelala. Tulijaribu kukumbuka majaribu yetu makuu, lakini yalionekana kuwa madogo sana yakilinganishwa na uzito wa utukufu uliozidi zaidi na wa milele uliotuzunguka, kiasi kwamba hatukuweza kuyaongelea, na sisi wote tukapaza sauti, “Haleluya!
Mbinguni ni rahisi kama nini,” na tukagusa vinubi vyetu vya dhahabu na kufanya matao ya mbinguni kurindima. {1T 61.2}

## SURA YA 8

## WITO WA KUSAFIRI

Nilielezea maono haya kwa waumini wa Portland Maine, Marekani, ambao walikuwa na imani kamili kuwa ilitoka kwa MUNGU. Roho wa Bwana aliuwezesha ushuhuda, na dhihirisho la adhima ya umilele kutulia juu yetu. Hofu ya Mungu isiyoelezeka ilinijaa, kwamba mimi, niliyekuwa mchanga na dhaifu, nichaguliwe kama chombo ambacho kwacho MUNGU angetoa nuru kwa watu Wake. Wakati nikiwa chini ya nguvu ya Bwana nilijawa na furaha, nikaonekana kuzungukwa na malaika watakatifu katika nyua tukufu za mbinguni, ambapo yote ni amani na furaha, na lilikuwa badiliko la kusikitisha na lenye uchungu kiasi gani, kuamka na kujikuta katika uhalisia wa maisha ya kufa. {1T 62.1}

Katika maono ya pili, ambayo punde yalifuata yale ya kwanza, nilioneshwa majaribu ambayo ni lazima niyapitie, na kwamba lilikuwa ni jukumu langu kwenda kuwaambia wengine yale ambayo MUNGU alikuwa amenifunulia. Ilioneshwa kwangu kwamba kazi zangu zitakutana na upinzani mkubwa, na kwamba moyo wangu utapasuka kwa uchungu, lakini kwamba neema ya MUNGU itatosha kunitegemeza kwa yote. Mafundisho ya maono haya yalinisumbua sana, kwani yalionesha jukumu langu la kwenda kati ya watu na kuwasilisha Ukweli. {1T 62.2}

Afya yangu ilikuwa duni sana kiasi kwamba nilikuwa nikiteseka mwilini kila wakati, na kwa mwonekano wa mambo yote, nilikuwa na muda mfupi tu wa kuishi. Nilikuwa na umri wa miaka kumi na saba tu, mdogo kwa umbo na dhaifu, nisiye mzoefu wa jumuiya/jamii, na kwa asili nilikuwa mwoga na ninayependa kujificha na hivyo lilikuwa jambo lenye uchungu kwangu kukutana na watu nisiowajua au wageni kwangu. Niliomba kwa dhati na bidii kwa siku kadhaa, na mpaka usiku wa manane, ili mzigo huu uondolewe kutoka kwangu na kuwekwa juu ya mtu anayeweza kuubeba. Lakini uzito wa wajibu haukubadilika, na maneno ya malaika yalisikika kila wakati masikioni mwangu: “Wajulishe wengine kile ambacho nimekufunulia.” {1T 62.3}

Sikuwa nimejiandaa kwenda ulimwenguni, na niliogopa kukutana na kung’ongwa na kejeli zake na upinzani. Nilikuwa na kiwango kidogo cha ujasiri au kujiamini. Lakini pale ROHO WA MUNGU aliponihimiza kuifanya kazi, niliamka na kusahau hofu yote na woga katika mawazo ya upendo wa Yesu na kazi ya ajabu aliyokuwa amenifanyia. Uhakikisho wa kila wakati kwamba nilikuwa nikitimiza wajibu wangu na kutii mapenzi ya Bwana ulinipa ujasiri ambao ulinishangaza. Wakati kama huo nilihisi kuwa tayari kufanya au kuvumilia chochote ili kusaidia wengine kuingia katika nuru na amani ya Yesu. {1T 63.1}

Lakini ilionekana kuwa haiwezekani kwangu kufanya kazi hii ambayo iliwasilishwa mbele yangu; na kujaribu kuifanya kulionekana kutofaulu kabisa. Majaribu ya kuifanya yalionekana mazito zaidi kuliko ninavyoweza kuvumilia. Je! Mimi, niliye mtoto kwa umri, ningewezaje kutoka mahali hadi mahali,

nikiwafunulia watu Kweli takatifu za MUNGU ? Moyo wangu ulitetemeka na kusinyaa kwa hofu kutokana na mawazo. Ndugu yangu Robert, aliyekuwa na umri wa miaka miwili zaidi kuliko mimi, hakuweza kuongozana nami, kwani alikuwa dhaifu kiafya na woga wake ulikuwa mkubwa kuliko wangu; hakuwa na kitu kinachoweza kumshawishi achukue hatua kama hiyo. Baba yangu alikuwa na familia inayohitaji msaada wake katika kujikimu kimaisha na hivyo hakuweza kuacha biashara yake; lakini alinihakikishia kwamba ikiwa MUNGU angeniita kufanya kazi katika maeneo mengine, asingeshindwa kunifungulia njia. Lakini maneno haya ya kutia moyo yalileta faraja kidogo kwa moyo wangu uliofadhaika; njia iliyokuwa mbele yangu ilionekana kuzungukwa na shida ambazo sikuweza kuzishinda. {1T 63.2}

Nilitamani kifo kama njia ya kuniweka huru kutoka katika majukumu yaliyokuwa yakinisonga. Mwishowe amani tamu niliyokuwa nimeifurahia kwa muda mrefu iliniacha, na kukata tamaa tena kuligandamiza roho yangu. Maombi yangu yote yalionekana kuwa ya bure, na imani yangu ilikuwa imeondoka. Maneno ya faraja, kukaripia, au kutiwa moyo yalikuwa hayatofautiani kwangu kwani yalifanana tu; kwani ilionekana kuwa hakuna mtu anayeweza kunielewa isipokuwa MUNGU, ambaye alikuwa ameniacha. Washiriki wenzangu huko Portland hawakujua lolote kuhusiana na mazoezi yaliyokuwa yanaendelea ndani ya akili yangu ambayo yalinileta katika hali hii ya kukata tamaa; lakini walijua kwamba kwa sababu fulani akili yangu ilikuwa imefadhaika na kusononeka, na walihisi kwamba hii ilikuwa dhambi kwangu, kwa kuzingatia njia ya neema ambayo Bwana alikuwa amejidhihirisha kwangu. {1T 63.3}

Niliogopa kwamba MUNGU alikuwa ameondoa kibali CHAKE kutoka kwangu milele. Nilipofikiria juu ya nuru ambayo hapo awali ilikuwa imeibariki roho yangu, ilionekana kuwa ya thamani maradufu ukilinganisha na giza ambalo sasa lilinigubika. Mikutano ilifanywa nyumbani kwa baba yangu, lakini smsongo wangu wa akili ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba sikuhudhuria kwa muda. Mzigo wangu ulikua mzito mpaka uchungu wa roho yangu ulionekana kuwa zaidi ya nilivyoweza kuvumilia. {1T 64.1}

Mwishowe nikashawishiwa kuwepo kwenye moja ya mikutano nyumbani kwangu. Kanisa lilifanya kesi yangu kuwa mada maalum ya sala. Mzee Pearson, ambaye kwa uzoefu wangu wa awali alikuwa amepinga udhihirisho wa nguvu ya MUNGU juu yangu, sasa aliniombea kwa bidii, na akanishauri nisalimishe mapenzi yangu kwa mapenzi ya Bwana. Kama baba mpole alijaribu kunitia moyo na kunifariji, akinisihi niamini kwamba sikuwa nimeachwa na Rafiki wa wenye dhambi. {1T 64.2}

Nilijihisi kuwa dhaifu sana na niliyekata tamaa kufanya juhudi yoyote maalum kwa ajili yangu mwenyewe, lakini moyo wangu uliungana na maombi ya rafiki zangu. Nilijali kidogo sasa kuhusiana na upinzani wa ulimwengu, na nilihisi niko

tayari kutoa kila dhabihu ikiwa tu ukubali na neema ya MUNGU ungeweza kurejeshwa kwangu. Wakati maombi yalipokuwa yakitolewa kwa ajili yangu, giza nene lililokuwa likinizunguka lilirudi nyuma, na ghafla nuru ikanijia. Nguvu zangu ziliondolewa. Nilionekana kuwa mbele ya malaika. Mmoja wa viumbe hawa watakatifu alirudia tena maneno haya: “Wajulishe wengine yale ambayo nimekufunulia.” {1T 64.3}

Hofu moja kubwa iliyonikandamiza ni kwamba ikiwa ningetii wito wa wajibu, na kwenda kujitangaza mwenyewe kuwa ni mmoja aliyependelewa na aliye juu kwa maono na mafunuo kwa watu, ningeweza kujitumbukiza kwenye dhambi ya kujiinua na kujikuta nipo mahali ambapo sikupaswa kuwepo, na kujiletea hali ya kumchukiza/kutomfurahisha MUNGU, na kuipoteza roho yangu mwenyewe. Nilikuwa na matatizo kadhaa kama hayo kabla kama nilivyoeleza hapo awali, ambapo moyo wangu ulisinyaa kutokana na majaribu hayo. 1T 64.4}

Sasa niliomba kwamba ikiwa ni lazima niende na kusimulia kile Bwana alichonionesha, napaswa kulindwa kutoka katika hatari ya kujiinua isivyostahili. Malaika alisema: “Maombi yako yamesikiwa na yatajibiwa. Ikiwa uovu huu unaouchukia unakutishia, mkono wa MUNGU utanyooshwa kukuokoa wewe; kwenye dhiki Yeye atakuvuta Kwake na kuuhifadhi unyenyekevu wako. Toa ujumbe kwa uaminifu. Vumilia hata mwisho, nawe utakula matunda ya mti wa uzima na kunywa maji ya uzima.”{1T 65.1}

Baada ya kupata fahamu ya kutoka kwenye vitu vya kidunia, nilijitoa kwa ajili ya Bwana, nikawa tayari kufanya yale Bwana anayoniagiza kwa gharama iwayo yote. Kwa muda mfupi, majaliwa ya Mungu yakafunguka kwa njia ya mimi kwenda pamoja na shemeji yangu kwa dada zangu huko Portland ilifunguliwa, maili thelathini kutoka nyumbani kwangu. Hapa nilikuwa na nafasi ya kutoa ushuhuda wangu. {1T 65.2}

Kwa miezi mitatu koo na mapafu yangu vilikuwa vimeugua sana kiasi kwamba ningeweza kuongea kidogo tu, tena kwa sauti ya chini kama kunong’ona na inayokwaruza. Katika hafla hii nilisimama kwenye mkutano na kuanza kuongea kwa kunong'ona. Niliendelea hivyo kwa takribani dakika tano, wakati uchungu na vizuizi vilipoliachilia koo na mapafu yangu, sauti yangu ikawa wazi na yenye nguvu, na nikazungumza kwa urahisi kikamilifu na uhuru kwa karibu masaa mawili. Ujumbe wangu ulipomalizika, sauti yangu ilikapotea tena hadi niliposimama mbele za watu tena, wakati urejeshwaji ule ule ulipojirudia. Nilihisi hakikisho la mara kwa mara kwamba mimi nilikuwa nikifanya mapenzi ya MUNGU, na nikaona matokeo makubwa yakiziandama juhudi zangu. {1T 65.3}

Njia ilifunguliwa tena kama majaliwa ya Bwana kwa urahisi kwenda sehemu ya mashariki ya Maine. Ndugu William Jordan alikuwa akifanya biashara kwenda Orrington, akifuatana na dada yake, na nilihimizwa kwenda nao. Kama nilivyokuwa nimemuahidi Bwana kutembea katika njia aliyofungua mbele

yangu, nami sikuthubutu kukataa. Huko Orrington nilikutana na Mzee James White. Alikuwa akifahamiana na marafiki zangu, na yeye mwenyewe alikuwa akifanya kazi ya wokovu. {1T 65.4}

ROHO WA MUNGU aliuwezesha ujumbe nilioubeba; mioyo ilifurahishwa katika Kweli, na wale waliokata tamaa walichangamshwa na kutiwa moyo kuanza upya imani zao. Huko Garland idadi kubwa ilikusanyika kutoka sehemu tofauti ili kusikia ujumbe wangu. Lakini moyo wangu ulikuwa mzito sana; Nilikuwa nimepokea tu barua kutoka kwa mama yangu akinisihi sana nirudi nyumbani, kwani taarifa za uongo zilikuwa zikizunguka kunihusu. Hili lilikuwa pigo lisilotarajiwa. Jina langu daima lilikuwa miongoni mwa wale waliokuwa bila lawama, na sifa yangu ilikuwa nzuri. Nilihisi kuhuzunishwa ya kuwa mama yangu anapaswa kuumia kwa ajili yangu; moyo wake ulikuwa umefungwa kwa watoto wake, na alikuwa na moyo nyeti sana juu yao. Kama kungekuwa na mpenyo, ningepaswa kwenda nyumbani mara moja; lakini hili halikuwezekana. {1T 65.5}

Huzuni yangu ilikuwa kubwa sana hata nilihisi unyong'ovu na sononeko la moyo sana usiku ule kiasi cha kutoweza kutoa hotuba. Rafiki zangu walinisihi nimtumaini Bwana; na kwa muda mrefu ndugu walishiriki katika kuniombea. Baraka ya Bwana ilikaa juu yangu punde, na nikatoa ushuhuda wangu jioni ile kwa uhuru mkubwa. Ilionekana kuna malaika aliyesimama kando yangu kunitia nguvu. Kelele za utukufu na ushindi zilipanda kutoka kwenye nyumba hiyo, na uwepo wa Yesu ulionekana kati yetu. {1T 66.1}

Katika kazi zangu niliitwa kupinga mwenendo wa wengine ambao kwa ushabiki na kupitiliza kwao walikuwa wakiiletea aibu kazi ya MUNGU. Hawa washupavu walionekana kufikiria kwamba dini ilikuwa na msisimko mkubwa na kelele. Waliongea kwa namna ambayo iliwakera wale wasioamini, na kusababisha wawachukie wao na mafundisho waliyokuwa wakiyafundisha; na kisha wakafurahia kwamba mateso yaliwaandama. Wale wasioamini hawakuweza kuona mwendelezo katika mambo yao. Ndugu mahali fulani walizuiwa kukusanyika kwa ajili ya mikutano. Mtu asiye na hatia aliteseka pamoja na mwenye hatia. Nilibeba moyo wa huzuni na mzito wakati mwingi. Kilionekana kitendo cha ukatili kwamba ni lazima kusudi la kazi ya Kristo liumizwe na mwenendo wa watu hawa wapotovu, na wasio na maamuzi ya busara. Hawakuwa wanaharibu nafsi zao tu, bali waliweka unyanyapaa juu ya kazi hiyo ambao usingeondolewa kirahisi. Na Shetani alipenda iwe hivyo. Ilimfaa vizuri kuona Ukweli ukibebwa na watu wasiotakaswa; ili uchanganyike na makosa, halafu wote kwa pamoja wanaswe kwenye vumbi. Alitazama kwa ushindi hali ya kuchanganyikiwa na kutawanyika kwa watoto wa MUNGU. {1T 66.2}

Mmoja wa watu hawa wenye ushabiki alifanikiwa kuwageuza marafiki zangu na hata jamaa zangu kuwa kinyume changu. Kwa kuwa nilikuwa nimeelezea kwa uaminifu yale niliyooneshwa kuhusu mwenendo wake ambao siyo wa Kikristo,

alisambaza uongo ili kuharibu ushawishi wangu na kujihesabia haki mwenyewe. Fungu langu lilionekana kuwa ngumu. Nilibanwa sana na hali ya kukata tamaa; na hali ya watu wa MUNGU ilinijaza uchungu sana kiasi kwamba kwa majuma mawili nililala kwa ugonjwa. Rafiki zangu walidhani siwezi kuishi; lakini ndugu na dada ambao walinihurumia katika shida hii walikutana kuniombea. Punde nikatambua kwamba maombi ya dhati na bidii, na yenye ufanisi yalitolewa kwa niaba yangu. Maombi yalishinda. Nguvu za yule adui hodari zilivunjika, nikaachiliwa, na mara nikapelekwa kwenye maono. Kwa maoni haya nilitambua kuwa ikiwa nitahisi ushawishi wa kibinadamu unaoathiri ushuhuda wangu, bila kujali nipo wapi, mimi napaswa kulia kwa MUNGU pekee, na malaika angetumwa kuniokoa. Tayari nilikuwa na malaika mlinzi mmoja ambaye alikuwa akinihudumia kila wakati, lakini ilipobidi, Bwana angemtuma mwingine kuniinua juu ya nguvu ya kila ushawishi wa kidunia. {1T 67.1}

# SURA YA 9

# MAONO YA NCHI MPYA

**[Maono Haya Yanaelezea Matukio Yatakayotokea Karibu Na Kufungwa Kwa Miaka Elfu Moja Baada Ya Kuja Kwa Kristo Mara Ya Pili. Ufunuo 20; 21; 22; Zekaria 14: 4.]**

Yesu akiwa anatuongoza, sisi sote tulishuka kutoka jijini na kuelekea kwenye dunia hii, juu ya mlima mkubwa na wenye nguvu, ambao haukuweza kumbeba Yesu, nao uligawanyika, na pakawa tambarare kubwa. Kisha tukaangalia juu na kuliona lile jiji mkubwa, lenye misingi kumi na miwili, na malango kumi na mawili, matatu kila upande, na malaika katika kila lango. Sisi sote tulipaza sauti: "Jiji, jiji kubwa, linakuja, linashuka kutoka kwa MUNGU mbinguni," na lilikuja na kukaa mahali ambapo tulisimama. Ndipo tukaanza kutazama vitu vya utukufu nje ya jiji. Hapo niliona nyumba nzuri zaidi, ambazo zilikuwa na mwonekano wa fedha, zikishikiliwa na nguzo nne zilizotengenezwa kwa lulu, zenye utukufu zaidi kuziona, ambazo zilikaliwa na watakatifu, na ndani yake kulikuwa na rafu ya dhahabu. Niliona watakatifu wengi wakiingia ndani ya nyumba, wakivua taji zao zenye kung'aa na kuziweka kwenye rafu, kisha kwenda katika shamba lililo jirani na nyumba zao kushugulika na kilimo cha ile ardhi; siyo kama tunavyoilima ardhi hapa; hapana, hapana. Nuru tukufu iliangaza kote vichwani mwao, na walikuwa wakimtolea MUNGU sifa kila wakati. {1T 67.2}

Na nikaona shamba lingine lililojaa maua ya kila aina, na nilipoyachuma, nikapaza sauti: "Hayatanyauka kamwe." Baadaye nikaona uwanja wa nyasi ndefu, mtukufu sana kutazama; ulikuwa wa kijani kibichi hai, chenye mwonekano wa fedha na dhahabu, huku kikipepea kwa fahari kwa utukufu wa Mfalme Yesu. Kisha tukaingia kwenye uwanja uliojaa kila aina ya wanyama - simba, mwana-kondoo, chui, na mbwa mwitu, wote wakiishi pamoja kwa umoja kamili. Tulipita katikati yao, nao wakafuata kwa amani baadaye. Kisha tukaingia kwenye msitu wa miti, siyo kama misitu yenye giza tuliyonayo hapa; hapana, hapana; bali yenye mwanga, na utukufu kote; matawi ya miti yalipeperushwa huku na huko, na sisi sote tukalia kwa sauti: "Tutakaa salama jangwani na kulala msituni." Tulipita msituni, kwa maana tulikuwa tukielekea Mlima Sayuni. {1T 68.1}

Tulipokuwa tukisafiri, tulikutana na kundi ambalo pia lilikuwa likiutazama utukufu wa mahali hapo. Niliona upindo mwekundu kwenye mavazi yao; taji zao zikiwa zinang'aa; mavazi yao yalikuwa meupe na safi. Tulipowasalimu, nilimuuliza Yesu ni akina nani. Alisema hawa walikuwa ni mashahidi waliouawa kwa ajili Yake. Pamoja nao kulikuwa na kundi lisilohesabika la watoto wadogo;

wenye pindo la rangi nyekundu kwenye nguo zao pia. Mlima Sayuni ulikuwa mbele yetu, na juu ya mlima huo kulikuwa na hekalu tukufu, na juu yake kulikuwa na milima mingine saba, ambayo juu yake yalimea maua ya waridi. Nikaona watoto wadogo wakipanda, au kama wangechagua, wangetumia mabawa yao madogo na kuruka juu ya milima, na kuchuma maua yasiyokauka. Kulikuwa na kila aina ya miti kuzunguka hekalu ili kupamba mahali hapo na kupafanya paonekane pazuri -, kama mti wa mafuta, mkaratusi, msonobari, manemane, komamanga, na mtini viliinama chini kwa uzito wa tini zake kwa wakati; haya yalifanya mahali pote kutukuka. Na tulipokuwa tunakaribia kuingia kwenye hekalu, Yesu alipaza sauti Yake nzuri na akasema, "Ni wale 144,000 tu ndiyo wanaoingia mahali hapa," na tukapiga kelele, "Haleluya!" {1T 68.2}

Hekalu hili lilishikiliwa na nguzo saba, zote zenye dhahabu angavu, iliyowekwa na lulu nyingi tukufu zaidi. Mambo mazuri niliyoyaona hapo, siwezi kuyaelezea. Lo, laiti ningeweza kuzungumza kwa lugha ya Kanaani, basi ningeweza kusema kidogo juu ya utukufu wa ulimwengu bora. Niliona kuna meza za mawe ambazo majina ya wale 144,000 yalinakshiwa kwa herufi za dhahabu. {1T 69.1}

Baada ya kuona utukufu wa hekalu, tulitoka, na Yesu alituacha na kwenda jijini. Punde tu tukasikia sauti Yake ya kupendeza tena, ikisema: "Njooni, watu Wangu, mmetoka katika dhiki kuu, na mmefanya mapenzi Yangu, mmeteseka kwa ajili Yangu, ingieni mle chakula cha jioni; kwa maana nitajifunga na kuwatumikia." Tulipiga kelele, "Haleluya, utukufu," na tukaingia jijini. Hapa niliona meza ya fedha safi; ilikuwa maili nyingi kwa urefu, hata hivyo macho yetu yaliweza kuona hadi mwisho. Niliona matunda ya mti wa uzima, mana, lozi, tini, makomamanga, zabibu, na matunda mengine mengi. Nilimuuliza Yesu aniruhusu kula tunda hilo. Alisema: "Siyo sasa. Wale wanaokula matunda ya nchi hii, hawatarudi tena duniani. Lakini katika muda mfupi, mkiwa waaminifu, mtakula matunda ya mti wa uzima na kunywa maji ya chemichemi. Na, "akasema," lazima urudi tena duniani, na uwaambie wengine yale niliyokufunulia. Kisha malaika alinichukua kwa upole chini kwenye ulimwengu huu wenye giza tena. Wakati mwingine nafikiri kuwa siwezi kukaa hapa duniani zaidi, vitu vyote vya hapa vinaonekana kuwa vya kusikitsha na kukatisha tamaa sana. Ninajisikia mpweke sana hapa, kwani nimeona nchi iliyo bora. Laiti ningekuwa na mabawa kama hua, basi ningaliruka na kupata pumziko. {1T 69.2}

Ndugu Hyde, ambaye alikuwepo wakati wa maono haya, alitunga aya zifuatazo, ambazo zimezunguka kwenye machapisho ya kiroho/kidini, na zimepata nafasi katika vitabu vya nyimbo kadhaa. Wale ambao wamezichapisha, kuzisoma, na kuziimba hawajui hata kidogo kwamba zilitokana na maono ya msichana aliyeteswa kwa ushuhuda wake mnyenyekevu. {1T 70.1}

Tumesikia kutoka nchi angavu, takatifu;

Tumesikia, na mioyo yetu inafurahi;
Kwa maana tulikuwa timu ya upweke ya mahujaji,
Tuliochoka, na kuchakaa, na wenye huzuni.
Wanatuambia watakatifu wana makao huko--
Wasio na makazi hawapo tena;
Na tunajua ya kuwa nchi bora ipo.
Ambapo mto safi wenye uhai unatiririka. {1T 70.2}

Wanasema mashamba ya kijani yanapepea huko,
Kwamba kamwe ugonjwa hautakuwepo;
Na pori la jangwa linakua vyema,
Na maua ya Sharon yanakua.
Kuna ndege wazuri kwenye kijani kibichi,
Nyimbo zao zimejaa furaha na uzuri; Na nyimbo zao, zinavyoendelea kuwa mpya,
Kinubi cha malaika husalimu. {1T 70.3}

Tumesikia juu ya mitende, joho, taji,
Na furushi la fedha lenye rangi nyeupe;
Ya haki ya jiji, na milango ya lulu,
Yote yanang'aa na nuru.
Tumesikia juu ya malaika huko, na watakatifu,
Na vinubi vyao vya dhahabu, jinsi wanavyoimba;
Ya mlima, na mti wa matunda wa uzima,
Ya majani ambayo huleta uponyaji. {1T 70.4}

Mfalme wa nchi hiyo, Yeye ni mwadilifu,
Yeye Ndiye furaha na mwangaza wa mahali hapo;
Kwa uzuri Wake tutamwona hapo,
Na kufurahi katika uso Wake wenye tabasamu.
Tutakuwa huko, tutakuwa hapo kwa muda mfupi,
Tutajiunga na wasafiri waliobarikiwa;
Tutakuwa na mitende, joho, taji,
Na milele tutakuwa kwenye pumziko. {1T 70.5}

# SURA YA 10

## KUZUIA MAKEMEO-Kutosahihisha au Kutoonya

Katika kipindi hiki nilijaribiwa vikali. Endapo ROHO WA MUNGU alikuwa juu ya mtu yeyote katika mkutano, naye akamtukuza MUNGU kwa kumsifu, wengine walileta kilio kwamba huo ni ushawishi wa kishirikina/kichawi (mesmerism/hyponotism*); na ikiwa ilimpendeza Bwana kunipa maono katika mkutano, wengine wangesema kwamba ilikuwa athari ya msisimko na ushirikina wa sumaku na hyponosis au mesmerism. Nikiwa na huzuni na kukata tamaa, mara nyingi nilikwenda peke yangu mahali pa faragha ili kumwaga roho yangu mbele Yake ambaye anawaalika waliochoka na wenye kulemewa kuja kupata pumziko. Kadri imani yangu ilivyodai ahadi, Yesu alionekana kuwa karibu sana. Nuru tamu ya mbinguni ingeangaza karibu nami, na ningeonekana kuzungukwa na mikono ya Mwokozi wangu, na kutoka huko ningechukuliwa kwenye maono. Lakini nilipoelezea kile ambacho MUNGU alikuwa amenifunulia mimi peke yangu, bila ushawishi wowote wa kidunia ambao ungeweza kuniathiri, nilihuzunika na kushangaa kusikia watu wa karibu sana wakisema kuwa wale walioishi karibu na MUNGU walikuwa vyombo rahisi kudanganywa na Shetani (*Franz Mesmer wa California aliingiza tiba ya kuponya watu kwa njia za ushirikina ikiwa sumaku, na jinsi ya kuvuta watu kwa hyponosis). {1T 71.1}

Kulingana na mafundisho haya, usalama wetu dhidi ya imani zenye udanganyifu ingekuwa katika kukaa mbali na MUNGU, katika hali ya kurudi nyuma. Ah, nilijisemea moyoni, Je! Hii imefikia hatua hii? Kwamba wale ambao kwa uaminifu humwendea MUNGU peke yake ili kudai ahadi Zake, na kudai wokovu Wake, watasingiziwa kuwa chini ya ushawishi mbaya wa ushirikia wa mesmerism? Je! Tunamwomba Baba yetu mwema wa mbinguni mkate, ili tupokee jiwe au ng'e? Vitu hivi kukamua roho yangu kwa maumivu, na kusumbua akili yangu kwa uchungu mkali, karibia na kukata tamaa. Wengi wangefanya niamini kwamba hapakuwa na ROHO MTAKATIFU, na kwamba mazoezi yote ambayo watu watakatifu wa MUNGU waliyapitia kama uzoefu, yalikuwa tu athari ya ushirikina wa mesmerism au udanganyifu wa Shetani. {1T 71.2}

Wengine walikuwa wamechukua mitazamo iliyokithiri ya mafungu fulani ya Maandiko, wakiacha kabisa kwenda kazini au kufanya kazi, na kuwakataa wale wote ambao hawatapokea mtazamo wao juu ya hoja hii na zingine zinazohusu wajibu wa kidini. MUNGU alinifunulia makosa haya katika maono, na akanituma kuwafundisha watoto Wake waliokosea; lakini wengi wao walikataa kabisa ujumbe huo, na wakanituhumu kwa kupatana na ulimwengu. Kwa upande mwingine, Waadventista wa jina walinishtaki kwa ushabiki, kuchukulia mambo

kwa kupitiliza, na niliwakilishwa kwa kusingiziwa uongo kwamba ni kiongozi wa watu wenye msimamo mkali wa kidini, shabiki aliyepitiliza, ambao binafsi nilikuwa nikifanya kazi kila wakati kuepukana nao. {1T 72.1}

Nyakati tofauti ziliwekwa kwa ajili ya ujio wa Bwana, na zilihimizwa kwa ndugu. Lakini Bwana alinionesha kuwa nyakati hizo zitapita, kwani wakati wa taabu ni lazima utokee kabla ya kuja kwa Kristo, na kwamba kila wakati uliotabiriwa, na ukapita, utadhoofisha imani ya watu wa MUNGU zaidi. Kwa hili nilishtakiwa kwa kuwa mtumwa mwovu aliyesema: "Bwana wangu anakawia kuja." {1T 72.2}

Kauli hizi zinazohusiana na upangaji wa muda zilichapishwa karibu miaka thelathini iliyopita, na vitabu vyenye taarifa hizi vimesambazwa kila mahali; lakini baadhi ya wachungaji wanaodai kunifahamu vizuri, wanasema mimi ndiye nilipanga wakati wa kuja kwa Bwana, na ya kwamba nyakati hizo zimepita, na kwa hiyo njozi zangu ni za uongo. Bila shaka taarifa hizi za uongo zinapokelewa na wengi kama ukweli; lakini hakuna anayefahamiana na mimi au kazi zangu anayeweza kutoa taarifa hiyo kwa uwazi. Huu ndiyo ushuhuda ambao nimewahi kuutoa tangu kupita kwa wakati mnamo 1844: "Wakati baada ya wakati utapangwa na watu tofauti, nao utapita; na ushawishi wa upangaji huu wa wakati utaelekea kuharibu imani ya watu wa MUNGU." Kama ningeona wakati dhahiri katika maono, na ningekuwa na ushuhuda wangu juu yake, nisingeweza kuandika na kuchapisha, kabla ya ushuhuda huu, kwamba nyakati zote zinazowekwa zitapita, kwani wakati wa taabu ni lazima ufike kabla ya kuja kwa Kristo. Hakika kwa miaka thelathini iliyopita, ambayo ni, tangu kuchapishwa kwa matamko haya, nisingependa kuweka wakati wa Kristo kuja, na kwa hivyo kujiweka chini ya hukumu sawa na wale ambao nilikuwa nikiwakemea. Na sikuwa na maono hadi 1845, ambayo ilikuwa baada ya kupita kwa wakati wa matarajio ya jumla mnamo 1844. Kisha nikaoneshwa yale niliyoyasema hapa. {1T 72.3}

Na je! Ushuhuda huu haujatimizwa katika kila kipengele? Wanamarejeo wa siku ya kwanza wameweka muda baada ya muda, na licha ya kushindwa mara kwa mara, wamekusanya ujasiri wa kuweka nyakati mahsusi mpya. MUNGU hajawaongoza katika hili. Wengi wao wamekikataa kipindi cha Kweli cha unabii, na wamepuuza utimilifu wa unabii, kwa sababu wakati ulipita katika 1844, na haukuleta tukio lililotarajiwa. Waliukataa Ukweli, na adui alikuwa na nguvu ya kuleta udanganyifu mkali juu yao kwamba waamini uongo. Jaribio kubwa la muda lilikuwa mnamo 1843 na 1844; na wote ambao wameweka muda mahsusi wa kuja kwa Yesu tangu wakati huo wamekuwa wakijidanganywa na kudanganya wengine. {1T 73.1}

Hadi wakati wa maono yangu ya kwanza sikuweza kuandika; mkono wangu uliotetemeka haukuweza kushikilia kalamu yangu kwa utulivu. Nikiwa katika maono, niliamriwa na malaika kuandika maono hayo. Nilitii, na niliandika kwa urahisi. Mishipa yangu ya fahamu iliimarishwa, na mkono wangu ukawa thabiti. {1T 73.2}

Ulikuwa msalaba mzuri kwangu kuwaelezea wakosaji kile ambacho nilikuwa nimeoneshwa juu yao. Nilifadhaika sana kuona wengine wakisumbuka au kuhuzunika. Na nilipolazimika kutangaza ujumbe huo, mara nyingi ningeulainisha, na kuufanya uonekane kuwa mzuri kwa mtu binafsi kwa kadri nilivyoweza, na kisha ningeenda peke yangu na kulia kwa uchungu wa roho. Niliwatazama wale ambao walikuwa na wajibu wa kuzitunza roho zao pekee, na nikafikiria kama ningekuwa katika hali yao nisingelalamika. Ilikuwa ngumu kuelezea shuhuda zilizo wazi, zenye kukata-kata ambazo nilipewa na MUNGU. Niliangalia matokeo kwa wasiwasi, na ikiwa watu waliokemewa waliinuka dhidi ya maonyo, na baadaye wakapinga Ukweli, maswali haya yangeibuka akilini mwangu: Je! nilipeleka ujumbe vile vile niivyopaswa? Je! kusingekuwa na njia nyingine ya kuwaokoa (au kufanya mambo kuwa rahisi bila kugombana nao au kuwakasirisha na bado wapate ujumbe wa Bwana)? Na kisha dhiki kama hiyo iliiminyanafsi yangu kiasi kwamba mara nyingi nilihisi kifo kitakuwa mjumbe aliyekaribishwa, na kaburi mahali pazuri pa kupumzika. {1T 73.3}

Sikugundua hatari na dhambi ya njia kama hiyo, hadi nilipochukuliwa katika maono mbele ya Yesu. Yeye alinitazama akiwa amekunja uso, na akageuza uso wake kutoka kwangu. Haiwezekani kuelezea utisho na maumivu niliyoyahisi wakati huo. Nilianguka kifudifudi mbele Zake, lakini sikuwa na nguvu ya kutamka neno. Lo, jinsi nilivyotamani sana kufunikwa na kujificha kutokana na ule mwonekano wa kutisha! Hapo ndipo niliweza kutambua, kwa kiwango fulani, hisia za watu watakaopotea jinsi zitakavyokuwa watakapolia: “wakiiambia milima na miamba, “Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso Wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo.” {1T 74.1}

Mara malaika aliniambia niinuke, na kile kilichokutana na macho yangu hakiwezi kuelezewa. Mbele yangu kulikuwa na kundi la watu ambao nywele na mavazi yao viliraruliwa, na sura zao zilikuwa na mwonekano wa kukatisha tamaa na kutisha. Walinikaribia, na kusugua nguo zao kwenye nguo zangu. Nilipoangalia mavazi yangu, niliona yamechafuliwa na damu. Tena nilianguka kama mtu aliyekufa miguuni mwa malaika wangu aliyeandamana nami. Sikuweza kuomba udhuru hata mmoja, na nilitamani kuwa mbali na mahali pale Patakatifu. Malaika aliniinua na kunisimamisha, akasema: “Hili siyo tatizo lako sasa, lakini jambo hili limepitishwa mbele yako kukuonesha hali yako itakavyokuwa kama ukipuuzia kuwaambia wengine kile Bwana alichokufunulia. Lakini ikiwa wewe ni mwaminifu hata mwisho, utakula matunda ya mti wa uzima, na utakunywa maji katika mto wa uzima. Utalazimika kuteseka sana, lakini neema ya MUNGU inatosha.” Nilihisi kuwa tayari kufanya yote ambayo

Bwana anaweza kunihitaji nifanye, ili nipate ukubali Wake, na nisikutane na sura Yake ya kutisha. {1T 74.2}

## SURA YA 11

## NDOA NA KAZI ZINAZOANDAMANA NAYO

Agosti 30, 1846, niliunganishwa katika ndoa na Mzee James White. Mzee White alikuwa amefurahia uzoefu wa kina katika harakati za ujio wa Bwana, na kazi yake katika kuutangaza Ukweli ilikuwa imebarikiwa na MUNGU. Mioyo yetu ilikuwa imeungana katika kazi kubwa, na kwa pamoja tulisafiri na kufanya kazi kwa wokovu wa roho. {1T 75.1}

Tuliingia katika kazi yetu bila fedha, tukiwa na marafiki wachache, na wenye afya dhaifu (iliyovunjika). Mume wangu alikuwa amerithi mwili wenye nguvu, lakini afya yake ilikuwa imedhoofika sana kwa kusoma sana na katika kufundisha. Nilikuwa na afya mbaya tangu nikiwa mtoto, kama nilivyoelezea. Katika hali hii, na bila mali, nikiwa na wachache wanaonihurumia katika mitazamo yetu, bila karatasi, na bila vitabu, tukaingia katika kuanza kazi yetu. Hatukuwa na nyumba za ibada wakati huo. Wazo la kutumia hema lilikuwa halijatokea kwetu wakati huo. Mikutano yetu mingi ilifanywa katika nyumba binafsi. Mikusanyiko yetu ilikuwa midogo. Ilikuwa ni nadra kwa yeyote kuja kwenye mikutano yetu isipokuwa Waadventista, labda pale waliposikia mwanamke anahubiri wakavutwa na udadisi wa kumsikia mwanamke akizungumza. {1T 75.2}

Mwanzoni nilisonga mbele kwa woga katika kazi ya kuzungumza mbele ya watu. Kama nilikuwa na ujasiri, nilipewa na ROHO MTAKATIFU. Ikiwa nilizungumza kwa uhuru na nguvu, nilipewa na MUNGU. Mikutano yetu kawaida ilifanywa kwa njia ambayo sisi wawili tulishiriki. Mume wangu alikuwa akitoa hotuba ya mafundisho makuu ya imani (doctrines), kisha ningefuata kwa mawaidha ya kitambo kirefu, nikiyeyusha njia yangu katika hisia za mkutano. Kwa hivyo mume wangu alipanda na nikamwagilia mbegu ya Ukweli, na MUNGU Ndiye aliyekuza. {1T 75.3}

Katika msimu wa joto wa 1846 tulianza kuitunza Sabato ya Biblia, na kuifundisha na kuitetea. Umakini wangu wa kwanza nilioupokea kwenye Sabato

wakati nikiwa ziarani New Bedford, Massachusetts, mapema mwaka huo huo. Mimi huko nilifahamiana na Mzee Joseph Bates, ambaye mapema alikuwa ameikubali imani ya marejeo ya Yesu mara ya pili, na alikuwa mfanyakazi mwenye bidii katika kazi hiyo. Mzee Bates alikuwa akiitunza Sabato, na alisisitiza umuhimu wake. Sikuhisi umuhimu wake, na nilifikiri kwamba Mzee Bates alikosea kuweka mkazo juu ya amri ya nne kuliko zile nyingine tisa. Lakini Bwana alinipa mwonekano wa Patakatifu pa mbinguni.
Hekalu la MUNGU lilifunguliwa mbinguni, na nilioneshwa sanduku la MUNGU lililofunikwa na kiti cha rehema. Malaika wawili walisimama, mmoja kila mwisho wa Sanduku la Agano, na mabawa yao yalitandazwa juu ya Kiti cha Rehema, na nyuso zao zeligeuzwa kulielekea. Malaika wangu aliyeandamana nami alinijulisha kuwa hizi zinawakilisha jeshi lote la mbinguni likitazama kwa kicho kikubwa kuelekea sheria takatifu ambayo ilikuwa imeandikwa kwa kidole cha MUNGU. Yesu aliinua kifuniko cha sanduku, na nikaona mbao za mawe ambazo Amri Kumi ziliandikwa. Nilishangaa nilipoona amri ya nne katikati kabisa ya zile amri kumi, na mduara laini wa nuru ukiizunguka. Malaika akasema: “Ni moja tu kati ya zile kumi inayomfafanua MUNGU aliye hai aliyeumba mbingu na dunia na vitu vyote vilivyomo. Wakati misingi ya dunia ilipowekwa, ndipo msingi wa Sabato pia uliwekwa.” {1T 75.4}

Nilioneshwa kwamba kama Sabato ya Kweli ingetunzwa siku zote, kusingekuwa na kafiri, Mkana-Mungu, miungu ya uongo au mtu asiyeamini kuwa kuna MUNGU. Utunzaji wa Sabato ungeuhifadhi ulimwengu kutoka katika ibada ya sanamu. Amri ya nne imekanyagwa-kanyagwa; kwa hivyo tunaombwa kukarabati uvunjaji wa sheria, na kuomba [irejeshwe] Sabato iliyodhulumiwa (Isaya 58:12 Kukarabati mvunjiko, mbomoko wa Sheria). Mtu wa kuasi, au mwana wa uasi aliyejiinua juu ya MUNGU, na akafikiria kubadilisha nyakati na sheria, alileta mabadiliko ya Sabato kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza ya juma. Kwa kufanya hivyo, alivunja sheria ya MUNGU. Kabla tu ya siku kuu ya MUNGU, ujumbe unatumwa kuonya watu warudishe utii wao kwa sheria ya MUNGU ambayo mpinga Kristo ameivunja. Kwa amri na mfano, tahadhari lazima ipelekwe kwa uvunjaji wa sheria. Nilioneshwa kuwa malaika wa tatu, atangazaye amri za MUNGU na imani ya Yesu, anawakilisha watu wanaopokea ujumbe huu na kuinua sauti ya onyo kwa ulimwengu, kushika amri za MUNGU kama mboni ya jicho, na kwamba kwa kuitikia onyo hili wengi wangeikumbatia Sabato ya Bwana (Ufunuo 14). {1T 76.1}

Tulipopokea nuru juu ya amri ya nne, kulikuwa na Waadventista ishirini na watano huko Maine ambao waliitunza Sabato; lakini hawa walikuwa tofauti katika hisia juu ya mambo mengine ya mafundisho, na walitawanyika kila mahali, na kwamba ushawishi wao ulikuwa mdogo sana. Kulikuwa na idadi sawa, katika hali sawa, katika sehemu zingine za New England, Mashariki ya Marekani. Ilionekana kuwa ni jukumu letu kuwatembelea watu hawa mara kwa mara kwenye nyumba zao, na kuwaimarisha katika Bwana na katika Ukweli

Wake, na kwa kuwa walikuwa wametawanyika sana, ilikuwa ni lazima kwetu kuwa barabarani muda mwingi. Kwa ajili ya kukosa uwezo wa kifedha tulichukua usafiri wa bei rahisi wa mtu binafsi, magari ya daraja la pili, na treni zinazoendeshwa kwa mvuke. Katika hali yangu dhaifu niliona kusafiri kwa usafiri binafsi ingekuwa vizuri zaidi. Tulipokuwa kwenye gari za daraja la pili, kwa kawaida tulifunikwa na moshi wa tumbaku, na kutokana na athari zake mara nyingi nilizimia. Tulipokuwa kwenye stima, kwenye safu ya chini, tulipatwa vivyo hivyo na moshi wa tumbaku, kando ya mazungumzo machafu na matusi ya watumishi wa meli na abiria wa madaraja ya chini tuliosafiri nao. Usiku tulijilaza kwenye sakafu ngumu, maboksi ya bidhaa kavu, au magunia ya nafaka, na mabegi yetu yakawa mito ya kulalia, na tukajifunika kwa makoti na mitandio yetu. Kama tungekabiliwa na baridi ya kipupwe kwenye mashua, tungetembea kwenye usawa wa chini ili kupata joto (deck). Kama tungepata joto la majira ya kiangazi, tungepanda kwenye dari ya juu ili kupata hewa baridi ya usiku. Jambo hili lilisababisha uchovu kwangu, hasa wakati wa kusafiri na mtoto mchanga nikiwa nimempakata mikononi mwangu. Njia hii ya maisha haikuwa chaguo letu. MUNGU alituita katika umaskini wetu, na kutuongoza kupitia tanuru la mateso, kutupatia uzoefu ambao unapaswa kuwa wa thamani kubwa kwetu, na mfano kwa wengine ambao baadaye wangejiunga nasi katika kazi. {1T 77.1}

Bwana wetu alikuwa Mtu ajuaye sikitiko; alikuwa anafahamu huzuni; na wale wanaoteseka pamoja Naye watatawala pamoja Naye. Wakati Bwana alipomtokea Sauli katika uongofu wake, hakukusudia kumwonesha ni uzuri gani anapaswa kuufurahia, bali ni mambo gani makuu anayopaswa kuteseka kwayo kwa ajili ya Jina Lake. Mateso yamekuwa sehemu ya watu wa MUNGU tangu siku za shahidi Habili. Wahenga waliteswa kwa kuwa waaminifu kwa MUNGU na kwa kutii amri zake. Kiongozi mkuu wa kanisa aliteseka kwa ajili yetu; Mitume Wake wa kwanza na kanisa la awali waliteswa; mamilioni ya wafia dini waliteseka, na Wanamatengenezo waliteseka. Na kwa nini basi sisi, ambao tuna tumaini lenye baraka la kutokufa, tutakaokamilishwa wakati wa kuonekana kwa Kristo hivi karibuni, tusinyae au tukimbie tukiona maisha ya mateso? Kama ingewezekana kufikia mti wa uzima ulio katikati ya Paradiso ya MUNGU bila mateso, tusingefurahia tuzo kubwa sana ambayo hatukuitesekea. Tungeshuka nyuma kutoka kwenye utukufu; aibu ingetukamata mbele ya wale ambao wamepiga vita vizuri, ambao wamekimbia mbio kwa uvumilivu, na wameushikilia uzima wa milele. Lakini hakuna atakayekuwepo pale ambaye, hakuchagua kama Musa, kuteseka na watu wa MUNGU. Nabii Yohana aliona umati wa watu waliokombolewa, na akauliza ni akina nani. Jibu la haraka lilikuja: “Hawa ndiyo wale waliotoka katika dhiki kuu, na wameosha mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo.” {1T 78.1}

Tulipoanza kuwasilisha nuru juu ya suala la Sabato, hatukuwa na wazo la wazi la ujumbe wa malaika wa tatu wa Ufunuo 14: 9-12. Mzigo wa ushuhuda wetu tulipofika mbele ya watu ni kwamba harakati kubwa ya ujio wa pili ilikuwa ya MUNGU, kwamba ujumbe wa kwanza na wa pili ulikuwa umetoka, na kwamba ule wa tatu utatolewa. Tuliona kuwa ujumbe wa tatu umefungwa na Maneno haya: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za MUNGU, na imani ya Yesu." Na sisi tuliona wazi kama tunavyoona sasa kuwa Maneno haya ya unabii yalidokeza matengenezo/marekebisho ya Sabato; lakini kuhusu ibada ya mnyama aliyetajwa katika ujumbe huo ilikuwa ipi, au chapa au sanamu na alama ya mnyama zilikuwaje, hatukuwa na msimamo uliofafanuliwa. {1T 78.2}

MUNGU  kwa ROHO WAKE MTAKATIFU aliangaza nuru juu ya watumishi Wake, na mada hiyo ilifunguliwa pole pole katika akili zao. Ilihitaji kujifunza kwingi, tashwishwi na uangalifu katika kuchunguza, kifungu baada ya kifungu. Kwa masumbufu, hofu, na shughuli isiyokoma kazi imeendelea hadi ukweli mkuu wa ujumbe wetu, wa wazi, uliounganishwa, kamili kabisa, umetolewa kwa ulimwengu. {1T 79.1}

Tayari nimesema juu ya kufahamiana kwangu na mzee Bates. Nilimwona kuwa muungwana wa kweli wa Kikristo, mwenye adabu, aliyejistahi kwa nidhamu na fadhili. Alinitendea kwa upendo mwororo kana kwamba nilikuwa mtoto wake mwenyewe. Mara ya kwanza kunisikia nikizungumza, alionesha kupendezwa sana. Baada ya kumaliza kuzungumza, aliinuka na kusema: "Mimi ni Tomasi mwenye mashaka. Mimi siamini katika maono. Lakini ikiwa ningeweza kuamini kwamba ushuhuda ambao dada huyo amesimulia usiku wa leo ilikuwa sauti ya MUNGU kwetu, ningekuwa mtu aliye na furaha zaidi kuliko watu wote wanaoishi leo. Moyo wangu umeguswa sana. Ninaamini mzungumzaji ni mkweli, lakini hawezi kuelezea kuhusiana na kuoneshwa kwake mambo mazuri na ya ajabu, ambayo ametuambia." {1T 79.2}

Miezi michache baada ya ndoa yangu, nilihudhuria mkutano na mume wangu, huko Topsham, Maine, ambapo mzee Bates alikuwepo. Wakati huo hakuamini kabisa kuwa maono yangu yalikuwa ya MUNGU. Mkutano huo ulikuwa msimu wa kupendeza sana. ROHO WA MUNGU  alikuwa juu yangu; Nilikuwa nimefungwa katika maono ya utukufu wa MUNGU, na kwa mara ya kwanza nilikuwa na mtazamo wa sayari zingine. Baada ya kutoka kwenye maono, nilielezea kile nilichoona. Mzee Bates ndipo akauliza ikiwa nilikuwa nimesoma unajimu. Nilimwambia sikuwa na kumbukumbu kama niliwahi mambo yahusuyo unajimu. Alisema: "Hii ni ya Bwana." Sikuwahi kumuona akiwa huru na mwenye furaha kama hivi. Sura yake iliangaza na nuru ya mbinguni, na akalitia moyo na kulibariki kanisa kwa nguvu. {1T 79.3}

Kutoka kwenye mkutano huo nilirudi na mume wangu Gorham, mahali ambapo wazazi wangu walikuwa wakiishi wakati huo. Hapa niliugua sana, na nikateseka

mno. Wazazi wangu, mume wangu, na dada zangu waliungana katika sala kwa ajili yangu, lakini niliteseka kwa majuma matatu. Mara nyingi nilizimia kama mtu aliyekufa, lakini katika jibu la maombi nilihuishwa tena. Uchungu wangu ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba niliwasihi wale walio karibu nami wasiniombee; kwani nilidhani maombi yao yalikuwa yakirefusha mateso yangu. Majirani zetu walichoka wakaniacha ili nife. Kwa muda ilimpendeza Bwana kuijaribu imani yetu. Mwishowe, marafiki zangu walipoungana tena katika kuniombea, ndugu aliyekuwepo alionekana kulemewa sana na mzigo, na nguvu ya MUNGU ikiwa juu yake, aliinuka kutoka katika magoti yake, akaja kwenye chumba hicho, na kuweka mikono yake juu ya kichwa changu, akisema: "Dada Ellen, Yesu Kristo akuponye," na akaanguka nyuma, na kulala akiwa amezimia kwa nguvu ya MUNGU. Niliamini kuwa kazi hiyo ni ya MUNGU, na maumivu yaliniacha. Nafsi yangu ilijawa na shukrani na amani. Lugha ya moyo wangu ilikuwa: "Hakuna msaada kwetu ila kwa MUNGU. Tunaweza kuwa na amani pale tu tunapopumzika ndani Yake na kungojea wokovu Wake." {1T 80.1}

Siku iliyofuata kulikuwa na dhoruba kali, na hakuna hata mmoja wa majirani aliyekuja nyumbani kwetu. Niliweza kuwa juu kwenye chumba cha sebule; na wengine walipoona madirisha ya chumba changu yamefunguliwa, walidhani kuwa nimekufa. Hawakujua kwamba Tabibu Mkuu alikuwa ameingia kwa fadhili kwenye nyumba hiyo, Naye aliukemea ugonjwa huo, na kuniweka huru. Siku iliyofuata tulisafiri maili thelathini na nane kwenda Topsham. Maswali yaliulizwa na baba yangu, mazishi yatakuwa saa ngapi. Baba aliuliza: "Mazishi gani?" "Mazishi ya binti yako," ndilo lililokuwa jibu. Baba alijibu: "Ameponywa kwa maombi ya imani, na yuko njiani kwenda Topsham." {1T 80.2}

Wiki chache baada ya hii, tukiwa njiani kwenda Boston, tulichukua stima huko Portland. Dhoruba kali ilitokea, na tulikuwa katika hatari kubwa. Mashua ilizunguka-zunguka kwa hofu, na kuashiria hatari na mawimbi yakaingia kupitia madirisha ya chumba. Kulikuwa na hofu kubwa katika chumba cha wanawake. Wengi walikuwa wakiungama dhambi zao, na kumlilia MUNGU awahurumie. Wengine walikuwa wakimwomba Bikra Maria awatunze, wakati wengine walikuwa wakitoa nadhiri kwa MUNGU kwamba ikiwa watafika nchi kavu watayatoa maisha yao kumtumikia. Lilikuwa tukio la hofu na mkanganyiko. Mashua ilipotikisika, mwanamke mmoja alinigeukia na kusema: "Je! Wewe Hauogopi? Nadhani ni ukweli kwamba hatuwezi kufika nchi kavu." Nilimwambia kwamba nilikuwa nimemfanya Kristo kuwa kimbilio langu, na ikiwa kazi yangu ingekamilika, ningeweza pia kulala chini ya bahari kama mahali pengine popote; lakini ikiwa kazi yangu haikumalizika, maji yote ya bahari yasingeweza kunizamisha. Tumaini langu lilikuwa kwa MUNGU; Yeye Angeweza kutuleta salama kwenye nchi kavu kama hilo lingekuwa kwa ajili ya utukufu Wake. {1T 80.3}

Wakati huu nilithamini tumaini la Mkristo. Tukio lililokuwa mbele yangu lilileta akilini mwangu kwa uwazi hali itakavyokuwa siku ya hasira kali ya Bwana,

wakati dhoruba ya ghadhabu yake itakapomjia yule mwenye dhambi maskini. Kisha kutakuwa na kilio cha uchungu na machozi, kukiri dhambi, na kuomba rehema, wakati wakiwa wamechelewa. “Kwa kuwa nimeita, nanyi mkakataa; Nimeunyosha mkono Wangu, asiangalie mtu; Bali mmebatilisha shauri Langu, Wala hamkutaka maonyo Yangu; Mimi nami nitacheka siku ya msiba wenu, Nitadhihaki hofu yenu ifikapo; Hofu yenu ifikapo kama tufani, Na msiba wenu ufikapo kama kisulisuli, Dhiki na taabu zitakapowafikia-Mithali 1.” {1T 81.1}

Kupitia rehema ya MUNGU sote tulikuwa salama. Lakini baadhi ya abiria ambao walidhihirisha hofu kubwa katika dhoruba hiyo hawakutafakari na kurejelea tukio hilo, ila tu walipuuzia hofu zao. Mama ambaye alikuwa ameahidi kwa kiapo kwamba ikiwa atahifadhiwa na kuiona nchi kavu atakuwa Mkristo, kwa kejeli alilia wakati akikiacha mashua: “Utukufu kwa MUNGU, ninafurahi kukanyaga tena ardhini!” Nilimuuliza arudi nyuma masaa machache, na kukumbuka nadhiri zake kwa MUNGU. Lakini aligeuka kutoka kwangu kwa kejeli. {1T 81.2}

Nilikumbushwa kwa nguvu juu ya toba inayofanywa na mtu akiwa kwenye kitanda cha kifo. Wengine hujitumikia wenyewe na Shetani maisha yao yote, na ugonjwa unapowashinda, na hali ya kutokuwa na uhakika inapokuwa mbele yao, hudhihirisha huzuni kwa ajili ya dhambi, na pengine hata kusema kuwa wapo tayari kufa, na marafiki zao wanajifanya kuamini kwamba watu wale wameongoka kweli na wamekidhi vigezo vya kwenda mbinguni. Lakini kama watu hawa wangepona, wangekuwa waasi kama zamani. Nimekumbushwa Mithali 1:27, 28: “Hofu yenu ifikapo kama tufani, Na msiba wenu ufikapo kama kisulisuli, Dhiki na taabu zitakapowafikia. Ndipo watakaponiita, lakini sitaitika; Watanitafuta kwa bidii, wasinione.” {1T 81.3}

Huko Gorham, Maine, Agosti 26, 1847, mtoto wetu mkubwa, Henry Nichols White, alizaliwa. Mnamo Oktoba, Ndugu na dada Howland wa Topsham kwa fadhili walitupatia sehemu ya makazi yao, ambayo tuliyakubali kwa furaha, na kuanza uangalizi wa nyumba na samani zilizokopwa. Tulikuwa masikini, na tuliona nyakati zinakaribia. Tulikuwa tumeamua kutokuwa tegemezi, bali kujitegemea, na kuwa na kitu cha kuwasaidia wengine. Lakini hatukufanikiwa. Mume wangu alifanya kazi kwa bidii akivuta mawe kwenye reli, lakini hakuweza kupata kile kinachostahili kwa kazi yake. Ndugu na dada Howland kwa uhuru walitugawia chochote wakati wowote ambao wangeweza; lakini walikuwa katika mazingira ya magumu. Waliamini kabisa ujumbe wa kwanza na wa pili (Ufunuo 14), na walikuwa wametoa vitu vyao kwa ukarimu ili kusambaza kazi, hadi wakawa wategemezi wa kazi yao ya kila siku. {1T 82.1}

Mume wangu aliacha kazi ya reli, na kwa shoka lake akaenda msituni kukata kuni. Akiwa na maumivu ya kila wakati upande wake mmoja, alifanya kazi kutoka asubuhi hadi giza lilipoingia ili kupata senti hamsini kwa siku. Alizuiwa kulala usiku kwa maumivu makali. Tulijitahidi kumtia moyo, kwa kumtegemea

Bwana. Sikunung'unika. Asubuhi nilihisi shukrani kwa MUNGU kwamba alikuwa ametuhifadhi kupitia usiku mwingine, na usiku nilishukuru kwamba alikuwa ametuhifadhi kwa siku nyingine. Siku moja chakula chetu kilipokwisha, mume wangu alikwenda kwa mwajiri wake kuomba pesa au chakula. Ilikuwa siku ya dhoruba, na alitembea maili tatu na kurudi akitembea kwenye mvua. Alikuja nyumbani na begi lenye vitu mgongoni mwake likiwa limefungwa vifungo mbalimbali, akiwa amepitia kijiji cha Brunswick, ambapo alikuwa akifundisha mara nyingi. Alipoingia ndani ya nyumba, akiwa amechoka sana, moyo wangu ulizama ndani yangu. Hisia zangu za kwanza zilikuwa kwamba MUNGU alikuwa ametuacha. Nikamwambia mume wangu: "Je! Tumefika kwenye hatua hii? Je! Bwana ametuacha?" Sikuweza kuyazuia machozi yangu, nikalia kwa sauti kwa masaa, hadi nikazimia. Maombi yalitolewa kwa niaba yangu. Nilipopumua tena, nilihisi ushawishi wenye kunichangamsha wa ROHO WA MUNGU, na kujuta kwamba nilikuwa nimezama chini katika viwango vya kukata tamaa. Tunatamani kumfuata Kristo na kuwa kama Yeye; lakini wakati mwingine tunazimia chini ya majaribu, na kubaki mbali kutoka Kwake. Mateso na majaribu hutuleta karibu na Yesu. Tanuru huunguza taka na kufanya dhahabu ing'ae sana. {1T 82.2}

Wakati huu nilioneshwa kwamba Bwana alikuwa akitujaribu kwa faida yetu, na kutuandaa kufanya kazi kwa ajili ya wengine; kwamba alikuwa akikisukasuka kiota chetu, tusije tukatulia kwa raha na maisha rahisi. Kazi yetu ilikuwa kufanya kazi kwa ajili ya roho; kama tungekuwa tumefanikiwa, nyumbani pangekuwa mahali pa kupendeza sana hata tusingekuwa tayari kupaacha; majaribio yalikuwa yameruhusiwa kuja juu yetu kutuandaa kwa mapambano makubwa zaidi tutakayokutana nayo katika safari zetu. Punde tulipokea barua kutoka kwa ndugu katika majimbo mengine wakitualika kuwatembelea; lakini hatukuwa na uwezo wa kututoa nje ya jimbo. Jibu letu lilikuwa kwamba njia haikuwa wazi mbele yetu. Nilifikiri kwamba isingewezekana kwangu kusafiri na mtoto wangu. Hatukutaka kuwa tegemezi, na tulikuwa waangalifu kuishi kulingana na uwezo wetu. Tuliazimia kuteseka badala ya kupata deni. Nilijiruhusu mimi na mtoto kunywa vikombe viwili vya maziwa kila siku. Asubuhi moja kabla ya mume wangu kwenda kazini kwake, aliniachia senti tisa kununua maziwa kwa asubuhi tatu. Ulikuwa ni mtihani kwangu kama ninunue maziwa kwa ajili yangu mwenyewe na mtoto mchanga au ninunue vazi kwa ajili yake. Niliachana na wazo la maziwa, na kumnunulia nguo inayofunika mikono wazi ya mtoto wangu. {1T 83.1}

Punde Henry aliyekuwa mdogo aliugua sana, na hali ikazidi kuwa mbaya kwa kasi mno kiasi kwamba tulishtuka sana. Alilala katika hali isiyo na matumaini; kupumua kwake kukiwa kwa hali ya haraka na nzito. Tulitibu na tiba rahisi bila mafanikio. Kisha tukamwita mtu mwenye uzoefu wa magonjwa, ambaye alisema kuwa kupona kwake kulikuwa na mashaka. Tulikuwa tumemuombea, lakini hakukuwa na mabadiliko. Tulimfanya mtoto huyo kuwa kisingizio cha

kutosafiri na kufanya kazi ya Mungu kwa faida ya wengine, na tuliogopa kuwa Bwana alikuwa karibu kumwondoa. Kwa mara nyingine tena tulikwenda mbele za Bwana, tukiomba kwamba atuonee huruma, na aepushe maisha ya mtoto, nasi kwa kicho sisi tutajitahidi kwenda mbele, tukimtumaini MUNGU, popote atakapotutuma. {1T 84.1}

Maombi yetu yalikuwa ya bidii na yenye uchungu. Kwa imani tulidai ahadi za MUNGU, na tuliamini kwamba Yeye alisikiza kilio chetu. Nuru kutoka mbinguni ilikuwa ikivunja mawingu na kutuangazia. Maombi yetu yalijibiwa kwa neema. Kuanzia saa hiyo mtoto alianza kupona. {1T 84.2}

Tulipokuwa Topsham tulipokea barua kutoka kwa ndugu Chamberlain wa Connecticut, akituhimiza kuhudhuria mkutano katika jimbo hilo mnamo Aprili, 1848. Tuliamua kwenda kama tungeweza kupata pesa. Mume wangu aliweka mambo sawa na mwajiri wake, na akagundua kwamba kulikuwa na dola kumi za kwake. Dola tano kati ya hizo nilinunua aina za nguo ambazo tulizihitaji sana, kisha nikashona koti la mume wangu, hata kuweka viraka, kiasi cha kufanya iwe vigumu kutambua kipi ni kitambaa cha asili na kipi ni kiraka kwenye mikono ya koti. Tulikuwa tumebakiza dola tano kutupeleka Dorchester, Massachusetts. Sanduku letu lilikuwa na karibu kila kitu tulichokuwa nacho duniani; lakini tulifurahia amani ya akili na dhamiri safi, na mambo haya tuliyathamini kuliko raha za kidunia. Huko Dorchester tuliitembelea nyumba ya ndugu Nichols, na tulipoondoka, dada N. alimkabidhi mume wangu dola tano, ambazo zililipia nauli yetu kwenda Middletown, Connecticut. Tulikuwa wageni katika jiji hilo, na hatujawahi kumtambua ndugu mwenye imani kama yetu katika jimbo hilo. Tulikuwa tumebaki na senti hamsini. Mume wangu hakuthubutu kuzitumia kukodisha gari, kwa hivyo tukalitupa sanduku juu ya rundo la mizigo mingine, na tukaendelea kutembea tukimtafuta mtu wa imani kama yetu. Upesi tulimpata ndugu C., ambaye alitupeleka nyumbani kwake. {1T 84.3}

Mkutano huo ulifanyika Rocky Hill, katika chumba kikubwa, ambacho hakijakamilika cha nyumba ya ndugu Belden. Ndugu waliingia mpaka tukafikia idadi ya takribani hamsini; lakini hawa hawakuwa wote waliojitoa kikamilifu katika Ukweli. Mkutano wetu ulikuwa wa kupendeza. Ndugu Bates aliziwasilisha amri hizo wazi, na umuhimu wake ulihimizwa kwa shuhuda zenye nguvu. Neno hilo lilikuwa na nguvu ya kuwathibitisha wale walio tayari katika Kweli, na kuwaamsha wale ambao hawakuwa wameamua kikamilifu. {1T 85.1}

Tulialikwa kukutana na ndugu katika Jimbo la New York msimu wa majira ya joto uliofuata. Waumini walikuwa maskini, na wasingeweza kuahidi kufanya mengi kulipia gharama zetu. Hatukuwa na fedha za kusafiria. Afya ya mume wangu ilikuwa mbaya, lakini njia ilimfungukia kufanya kazi katika shamba la nyasi kwaajili ya ng’ombe, ambazo zilikaushwa baadaye (hay) naye akaamua kufanya kwa bidii. Ilionekana wakati huo kwamba lazima tuishi kwa imani. Tulipoamka asubuhi, tuliinama kando ya kitanda chetu na kumwomba MUNGU

atupe nguvu ya kufanya kazi kwa siku nzima. Tusingeweza kuridhika hadi tutakapokuwa na uhakikisho kwamba Bwana alitusikia tulipomuomba. Mume wangu kisha akaenda kukata nyasi, si kwa nguvu zake mwenyewe, bali kwa nguvu za Bwana. Wakati wa usiku, aliporudi nyumbani, tungemsihi tena MUNGU kwa ajili ya nguvu za kutuwezesha kupata fedha za kueneza Ukweli Wake. Mara nyingi tulibarikiwa sana. Katika barua kwa ndugu Howland, Julai, 1848, mume wangu aliandika: "MUNGU ananipa nguvu ya kufanya kazi kwa bidii siku nzima. Jina Lake lisifiwe! Natumai kupata dola chache za kutumia katika kusudi Lake. Tumesumbuliwa na kazi, uchovu, maumivu, njaa, baridi, na joto, wakati tukijitahidi kuwatendea ndugu na dada zetu mema, na tunajiweka tayari kuteseka zaidi ikiwa ni mapenzi ya MUNGU yanahitaji hilo. Ninafurahi leo kwamba urahisi wa maisha, raha, na faraja katika maisha haya ni dhabihu juu ya madhabahu ya imani yangu na tumaini langu. Ikiwa furaha yetu inajumuisha kuwafurahisha wengine, tunayo furaha kweli kweli. Mwanafunzi wa kweli hataishi ili kujifurahisha mwenyewe na kujipenda, bali kwa ajili ya Kristo, na kwa faida ya wale watoto Wake walio wadogo. Anapaswa kutoa kafara kwa mapumziko yake, maisha ya mtelemko, raha yake, faraja, hali yake ya kutosumbuliwa, mapenzi yake, na matakwa yake binafsi kwa ajili ya Kristo, vinginevyo hatatawala kamwe pamoja Naye kwenye kiti CHAKE cha enzi. "{1T 85.2}

Fedha zilizopatikana katika shamba la nyasi zilitosha kutupatia mahitaji yetu ya sasa, na pia kulipa gharama zetu kwenda magharibi mwa New York na kurudi. {1T 86.1}

Mkutano wetu wa kwanza huko New York ulifanyika Volney, katika zizi la ndugu. Karibu watu thelathini na tano walikuwepo – wote walioweza kukusanywa katika sehemu hiyo ya jimbo. Lakini kati ya idadi hii, ni wawili tu waliokubaliwa. Wengine walikuwa wakishikilia makosa makubwa, na kila mmoja akishinikiza maoni yake mwenyewe, akisema kwamba yapo kwa mujibu wa Maandiko. {1T 86.2}

Tofauti hizi za ajabu za mitazamo ziliniletea uzito mkubwa, kwani ilionekana kwangu kuwa MUNGU alikuwa amedharauliwa; na nilizimia chini ya mzigo. Wengine waliogopa kwamba nilikuwa nakufa; lakini Bwana alisikia maombi ya waja Wake, nikaamka. Nuru ya mbinguni ilikaa juu yangu, na punde nilipotea kutoka katika vitu vya kidunia. Malaika aliyeongozana nami aliwasilisha mbele yangu baadhi ya makosa ya wale waliokuwepo, na pia Ukweli tofauti na makosa yao. Maoni haya ya kutofautiana ambayo walidai kuwa ni kulingana na Biblia yalikuwa tu kulingana na maoni yao kuhusu Biblia, na lazima watoe makosa yao na kuyasalimisha na kuungana pamoja juu ya ujumbe wa malaika watatu (au wa tatu). Mkutano wetu ulifungwa kwa ushindi. Ukweli ulipata ushindi. Ndugu waliachana na makosa yao ya Mafundisho ya imani potofu, na wakaungana juu ya ujumbe wa malaika wa tatu, na MUNGU akawabariki sana na akaongeza idadi yao. {1T 86.3}

Kutoka Volney tulienda Port Gibson kuhudhuria mkutano uliofanyikia katika ghala la ndugu Edson. Kulikuwa na wale waliopenda Ukweli, lakini walikuwa wakisikiliza na kuthamini makosa. Bwana alitutendea kwa nguvu kabla ya mkutano huo kumalizika. Nilioneshwa tena katika maono umuhimu wa ndugu huko magharibi mwa New York kuweka kando tofauti zao, na kuungana juu ya Ukweli wa Biblia. {1T 86.4}

Tulirudi Middletown, ambapo tulikuwa tumemwacha mtoto wetu wakati wa safari yetu ya magharibi. Na sasa jukumu chungu lilijitokeza. Kwa faida ya mioyo yetu tulihisi kwamba itatulazimu tuutoe kafara uwepo wa mtoto wetu mdogo Henry, ili tujitoe bila kizuizi katika kazi hiyo. Afya yangu ilikuwa duni, na mtoto angehitaji kuchukua sehemu kubwa ya wakati wangu. Lilikuwa ni tatizo kubwa sana, lakini sikuthubutu kumruhusu mtoto asimame katika njia ya wajibu wangu. Niliamini kwamba Bwana alikuwa amemuhifadhi kwetu alipokuwa mgonjwa sana, na kwamba ikiwa nitamruhusu anizuie kufanya jukumu langu, MUNGU atamwondoa kutoka kwangu. Peke yangu mbele za Bwana, nikiwa na hisia zenye uchungu na machozi mengi, nilitoa kafara, na kumpatia mwingine mtoto wangu wa pekee, mwenye umri wa mwaka mmoja, ili ampatie hisia za mama kwake, na kufanya sehemu ya mama. Tulimwacha katika familia ya ndugu Howland, ambaye tulikuwa na imani naye kabisa. Walikuwa tayari kubeba mizigo ili kutuacha tukiwa huru kadri iwezekanavyo kufanya kazi kwa ajili ya MUNGU. Tulijua kuwa wangeweza kumtunza Henry kuliko sisi wakati tukiwa safarini, na kwamba ilikuwa kwa faida yake mtoto kuwa katika nyumba thabiti yenye nidhamu nzuri. Ilikuwa ngumu kuachana na mtoto wangu. Uso wake mdogo wa kusikitisha, nilipomwacha, ulikuwa mbele yangu usiku na mchana; lakini kwa nguvu ya Bwana nilimwondoa akilini mwangu, na nikatafuta kuwafanyia wengine mema. Familia ya ndugu Howland ilimtunza Henry kwa miaka mitano. {1T 86.5}

## SURA YA 12

## UCHAPISHAJI NA KUSAFIRI

Mnamo Juni, 1849, njia ilifunguliwa kwetu kufanya makazi yetu kwa muda huko Rocky Hill, Connecticut. Hapa, mnamo Julai 28, mtoto wetu wa pili, James Edson, alizaliwa. {1T 87.1}

Wakati tukiishi mahali hapa, mume wangu alivutiwa kwamba ni jukumu lake kuandika na kuchapisha Ukweli wa leo. Alitiwa moyo sana na kubarikiwa kwa kadri alivyoamua kufanya hivyo. Lakini tena akaingiwa na mashaka na kuchanganyikiwa, kwani hakuwa na pesa. Kulikuwa na ndugu ambao walikuwa na mali, lakini walichagua kubania pesa zao kibindoni. Baadaye alikata tamaa, na kuamua kutafuta uwanja ili akate nyasi. Alipotoka nje ya nyumba, ule mzigo

uliniangukia ukanifunika, nikazimia. Maombi yalitolewa kwa ajili yangu, na nikabarikiwa, na kupelekwa kwenye maono. Niliona kwamba Bwana alikuwa amembariki na kumtia nguvu mume wangu kufanya kazi shambani mwaka mmoja uliopita; kwamba alikuwa ametumia vizuri mali aliyopata; na kwamba angepata mara mia maishani mwake, na, ikiwa ni mwaminifu, tuzo kubwa katika ufalme wa MUNGU; lakini kwamba Bwana hatampa sasa nguvu ya kufanya kazi shambani, kwani alikuwa na kazi nyingine kwa ajili yake; kwamba lazima atembee nje kwa imani, na aandike na atangaze Ukweli wa sasa. Mara moja akaanza kuandika, na alipofika kwenye aya ngumu, tulimwomba Bwana atupe maana halisi ya Neno Lake. {1T 87.2}

Karibu katika wakati huo huo alianza kuchapisha karatasi ndogo yenye kichwa, Ukweli wa Sasa. Ofisi ya uchapishaji ilikuwa Middletown, maili nane kutoka Rocky Hill, na mara nyingi alitembea umbali huu na kurudi tena, ingawa wakati huo alikuwa kilema. Alipoleta nambari ya kwanza kutoka ofisi ya uchapishaji, sisi sote tuliiinamia kuzunguka machapisho haya, tukimwomba Bwana kwa maombi ya dhati na bidii, kwa mioyo ya unyenyekevu na machozi mengi, aache baraka Yake ikae juu ya juhudi dhaifu za mtumishi Wake. Kisha akaelekeza karatasi hizo kwa wale wote aliofikiri wangezisoma, na akazibeba hadi kwenye ofisi ya posta zikiwa ndani ya mkoba. Kila makala ilichukuliwa kutoka Middletown hadi Rocky Hill, na kila wakati kabla ya kuziandaa kwa ajili ya ofisi ya posta, tulizisambaza mbele za Bwana, na kwa maombi ya dhati yaliyochanganyika na machozi, tuliomba baraka Yake iandamane na wajumbe wa kimya (machapisho). Punde barua zilikuja zikiwa na fedha za kuchapisha jarida hilo, na habari njema ya roho nyingi zilizokumbatia Ukweli. {1T 88.1}

Na mwanzo wa kazi hii ya uchapishaji, hatukuacha kazi zetu katika kuhubiri Ukweli, lakini tulisafiri kutoka mahali hadi mahali, kutangaza mafundisho makuu (doctrines) ambayo yalileta nuru kubwa na furaha kwetu, kutia moyo waumini, kurekebisha makosa ya Neno la Mungu, na kuweka mambo sawa kanisani. Ili kuendeleza shughuli ya kuchapisha, na wakati huo huo kuendelea na kazi zetu katika sehemu tofauti za maeneo ya kazi, na magazeti hayo yalikuwa yakihamishwa mara kwa mara kwenda sehemu mbalimbali. {1T 88.2}

Mnamo 1850 [gazeti] lilitolewa huko Paris, Maine. Hapa liliongezwa, na jina lake likabadilishwa kuwa lile linalotumika sasa, 'The Advent Review na Sabath Herald.' Marafiki wa kazi walikuwa wachache kwa idadi na masikini katika utajiri wa ulimwengu, na bado ilitulazimu kupambana na umasikini na kukata tamaa kukubwa. Kazi nyingi, masumbufu, na wasiwasi, ukosefu wa chakula kizuri na chenye lishe, na kuambukizwa na baridi katika safari zetu ndefu za msimu wa baridi, yalikuwa ni mambo mengi ya kushinikiza sana kwa mume wangu, naye akazama chini ya mzigo huo. James White alikuwa dhaifu sana kiasi kwamba hakuweza kutembea hadi ofisi ya uchapishaji. Imani yetu ilijaribiwa sana. Tulikuwa tumevumilia kwa hiari suluba, shida, na mateso; lakini nia zetu zilitafsiriwa vibaya, na tulichukuliwa katika hali ya kutoaminika

na wivu. Wachache wa wale ambao tulikuwa tumeteseka nao, walionekana kuthamini juhudi zetu. Tulikuwa tumesumbuliwa sana kiasi cha kushindwa kulala au kupumzika. Saa ambazo tulipaswa kuburudishwa na usingizi, mara nyingi zilitumika kujibu barua ndefu zilizosababishwa na kijicho; na masaa mengi wakati wengine wakiwa wamelala tuliyatumia katika machozi yenye maumivu, na kuomboleza mbele za Bwana. Mwishowe mume wangu alisema: “Mke wangu, haina maana kujaribu kujitahidi tena. Vitu hivi vinaniponda-ponda, na hivi punde vitanibeba kwenda kaburini. Siwezi kwenda mbali zaidi. Nimeandika tangazo kwenye gazeti kwamba sitachapisha tena.” Alipotoka mlangoni kuipeleka kwenye ofisi ya uchapishaji, nilizimia. Alirudi na kuniombea; sala yake ilijibiwa, na nikafarijika. {1T 89.1}

Asubuhi iliyofuata, wakati wa maombi ya familia, nilichukuliwa katika maono, na nilioneshwa kuhusu mambo haya. Niliona kwamba mume wangu hatakiwi aachane na magazeti hayo; ni Shetani aliyekuwa anajaribu kumuongoza kuchukua hatua hiyo, na alikuwa akifanya kazi kupitia mawakala kulitimiza hili. Nilioneshwa kwamba lazima tuendelee kuchapisha, na kwamba Bwana atatutegemeza; kwamba wale ambao walikuwa na hatia ya kututupia mizigo hiyo wangehitaji kuona kiwango cha mwenendo wao wa kikatili, na kurudi kukiri udhalimu wao, la sivyo uso wa MUNGU ungekuwa juu yao; kwamba hawakusema na kutenda dhidi yetu tu; bali dhidi Yake Yeye ambaye alikuwa ametuita kujaza nafasi aliyotutaka tuichukue; na kwamba tuhuma zao zote, wivu, na ushawishi wao wa siri uliandikwa kwa uaminifu mbinguni, na hautafutwa mpaka kila mtu ambaye alishiriki katika hayo aone kiwango cha mwenendo wake mbaya, na kurudi nyuma kila hatua ili aone ubaya alioufanya. {1T 89.2}

Gombo la pili la Review lilichapishwa huko Saratoga Springs, New York. Mnamo Aprili, 1852, tulihamia Rochester, New York. Katika kila hatua tulilazimika kuondoka kwa imani. Bado tulikuwa tumetiwa ulemavu na umasikini, na tukalazimika kuishi na uchumi duni zaidi na kujikana nafsi kwingi. Nitatoa dondoo fupi kutoka katika barua iliyokwenda kwa familia ya ndugu Howland, ya Aprili 16, 1852: “Ndipo tu tumeanza kuishi Rochester. Tumekodisha nyumba ya zamani kwa dola mia moja sabini na tano kwa mwaka. Tuna kiwanda cha kuchapa ndani ya nyumba. Kama isingekuwa hivyo, tungelipaswa kulipa dola hamsini kwa mwaka kwa chumba cha ofisi. Ungetabasamu kama ungekuja kutuangalia na kuziona samani zetu. Tumenunua vitanda viwili vya zamani kwa senti ishirini na tano kila kimoja. Mume wangu aliniletea nyumbani viti sita vya zamani ambavyo hakuna viwili kati ya hivyo vinavyofanana, ambayo alivilipia dola moja, na punde alinipatia viti vingine vinne vya zamani visivyo na mito au foronya, ambavyo alivilipia senti sitini na mbili. Fremu za viti hivyo ni imara, na nimekuwa nikivikalia. Siagi ni gharama kubwa sana hivyo hatuinunui, wala hatuwezi kumudu kununua viazi. Tunatumia mchuzi mahali pa siagi, na kabeji badala ya viazi. Milo yetu ya kwanza tuliila ikiwa imewekwa kwenye ubao

ulioegemezwa kwenye mapipa mawili matupu, na tupo tayari kuvumilia shida ikiwa tu kazi ya MUNGU inaweza kusonga mbele. Tunaamini mkono wa Bwana ulikuwa katika ujio wetu mahali hapa. Kuna shamba kubwa la kazi, na wafanyakazi ni wachache. Sabato iliyopita mkutano wetu ulikuwa mzuri sana. Bwana alituburudisha kwa uwepo Wake. "{1T 90.1}

Mara kwa mara tulitoka kwenda kuhudhuria Mikutano katika maeneo mbalimbali ya kazi. Mume wangu alihubiri, aliuza vitabu, na alifanya kazi kwa bidii ili kupanua usambazaji wa magazeti. Tulisafiri kwa usafiri binafsi, na tukasimama saa sita mchana kulisha farasi wetu kando ya barabara, na kula chakula chetu cha mchana. Kisha akiwa na karatasi na penseli, kwenye kifuniko cha sanduku letu la chakula cha jioni au juu ya kofia yake, mume wangu aliandika nakala za gazeti la 'Review' and Instructor'. Bwana alizibariki sana kazi zetu, na Ukweli uligusa mioyo mingi na kuleta matokeo. {1T 91.1}

Katika msimu wa joto wa mwaka 1853, tulifanya safari yetu ya kwanza kwenda jimbo la Michigan. Baada ya kuchapisha makubaliano yetu, mume wangu aliugua homa kali. Tuliungana kumwombea, na ingawa alipata nafuu lakini bado alibaki kuwa dhaifu sana. Tulikuwa tumefadhaishwa sana. Je! Tunapaswa kuondolewa kutoka katika kazi hiyo kwa sababu ya udhaifu wa mwili? Je! Shetani ataruhusiwa kutumia nguvu zake juu yetu, na kushindania kufaa kwetu katika maisha kwa kadri tunavyoendelea kuishi duniani? Tulijua kwamba MUNGU anaweza kuzipunguza nguvu za Shetani. Angeweza kutuacha tujaribiwe katika tanuru, lakini atatutoa tukiwa tumetakasika na kufaa zaidi kwa kazi Yake. {1T 91.2}

Nikiwa peke yangu nilimimina roho yangu mbele za MUNGU kwa maombi kwamba akemee ugonjwa huo na kumtia nguvu mume wangu kuendelea na safari. Tatizo hilo lilikuwa nyeti, dharura na imani yangu ilizishikilia kabisa ahadi za MUNGU. Hapo nilipata ushahidi kwamba ikiwa tungeendelea na safari yetu ya Michigan, malaika wa MUNGU angeenda nasi. Nilipomuelezea mume wangu yaliyokuwa akilini mwangu, alisema kwamba akili yake nayo imetufikiri vivyo hivyo, na tukaamua kwenda, tukimtumaini Bwana. Kila maili tuliyosafiri alijihisi kuimarika. Bwana alimtegemeza. Na alipokuwa akihubiri Neno, nilihisi kuhakikishiwa kwamba malaika wa MUNGU walikuwa wamesimama kando yake kumsaidia katika kazi zake. {1T 91.3}

Katika safari hii akili ya mume wangu ilishughulishwa sana juu ya somo la umizimu, na mara tu baada ya kurudi alijishughulisha na kuandika kitabu kilichoitwa, Dalili za Nyakati (Signs of the Times). Alikuwa bado dhaifu, na aliweza kulala kidogo, lakini Bwana alikuwa msaada wake. Wakati akili yake ikiwa katika hali ya kuchanganyikiwa, ya kuteseka, tungeinama mbele za MUNGU, na katika shida zetu tukamlilia Yeye. Yeye Alisikia sala zetu za dhati, na mara nyingi alimbariki mume wangu ili kwa roho zilizoburudishwa aendelee

na kazi. Mara nyingi kwa siku tulienda mbele za Bwana kwa maombi ya dhati na bidii. Kitabu hicho hakikuandikwa kwa nguvu zake mwenyewe. {1T 92.1}

Katika msimu wa baridi na majira ya kuchipua mimea niliteseka sana na ugonjwa wa moyo. Ilikuwa ngumu kwangu kupumua wakati nimelala, na sikuweza kulala isipokuwa kama ningeinuliwa na kuwa kwenye mkao karibu na ule wa kukaa. Pumzi yangu mara nyingi ilisimama, na mara nyingi nilizimia. Nilikuwa na uvimbe kwenye kope yangu ya kushoto ambao ulionekana kuwa saratani. Ulikuwa ukiongezeka polepole kwa zaidi ya mwaka, mpaka ikawa unaumiza sana, na kuathiri macho yangu. Wakati wa kusoma au kuandika, nililazimika kufunga jicho lililokuwa limeumia bandeji. Niliogopa kwamba lingeharibiwa na saratani. Nilitazama nyuma kwa usiku na siku zilizotumiwa kusoma karatasi, ambazo zilikuwa zimeleta mkazo kwa macho yangu, na kufikiria: "Ikiwa nitapoteza jicho langu na maisha yangu, vitatolewa kafara kwa kazi ya MUNGU." {1T 92.2}

Wakati huu daktari mashuhuri ambaye alitoa ushauri bila malipo alitembelea Rochester, na niliamua kwenda kuchunguzwa jicho langu. Alidhani uvimbe huo ungekuwa saratani. Lakini baada ya kusikiliza mapigo yangu ya moyo, alisema: “Unaumwa sana, na utakufa kwa sababu ya ugonjwa wa upungufu wa damu (apoplexy) kabla ya uvimbe huo wa jicho kupasuka. Uko katika hali ya hatari na ugonjwa wa moyo.” Hii haikunishtua, kwani nilikuwa najua kuwa bila msaada wa haraka lazima nishuke kaburini. Wanawake wengine wawili ambao walikuwa wamekuja kupata ushauri walikuwa wanaugua ugonjwa huo pia. Daktari alisema kwamba nilikuwa katika hali ya hatari zaidi kuliko mmoja wa hao wanawake wawili, na naweza nisifikishe majuma matatu kabla sijapooza. Nilimuuliza ikiwa anafikiria dawa yake itaniponya. Hakunitia moyo sana. Nilijaribu tiba ambazo aliagiza, lakini sikupata faida yoyote. {1T 92.3}

Kwa muda wa majuma matatu nilizimia na kuanguka sakafuni, nikakaa bila fahamu kwa takribani masaa thelathini na sita. Watu waliogopa kuwa siwezi kuishi, lakini kwa jibu la maombi nilihuishwa tena. Juma moja baadaye nilipata mshtuko upande wangu wa kushoto. Nilikuwa na hisia ya kushangaza ya ubaridi na ganzi kichwani mwangu, na maumivu makali katika paji la uso wangu. Ulimi wangu ulionekana kuwa mzito na wenye ganzi; Sikuweza kuongea waziwazi. Mkono wangu wa kushoto na ubavu vilikuwa hoi. Nilidhani nilikuwa nikifa, na wasiwasi wangu mkubwa ulikuwa juu ya ushahidi katika mateso yangu kwamba Bwana ananipenda. Kwa miezi kadhaa nilikuwa nikiumia kila wakati moyoni mwangu, na roho yangu ilikuwa ikinyong’onyea kila wakati. Nilikuwa nimejaribu kumtumikia MUNGU kutokana na kanuni siyo hisia, lakini sasa nilikuwa na kiu ya wokovu wa MUNGU, nilitamani kutambua baraka Zake bila kujali mateso yangu ya mwili. {1T 93.1}

Ndugu na dada walikutana pamoja ili kufanya kesi yangu kuwa mada maalum ya maombi. Nilipewa haja yangu; Nilipokea baraka za MUNGU, na nilikuwa na

uhakika kwamba Yeye ananipenda. Lakini uchungu uliendelea, na nilizidi kuwa dhaifu kila saa. Tena ndugu na dada walikusanyika kutoa hoja yangu kwa Bwana. Nilikuwa dhaifu sana hata sikuweza kuomba kwa sauti. Mwonekano wangu ulionekana kudhoofisha imani ya wale walio karibu nami. Ndipo ahadi za MUNGU zilipambwa safu mbele yangu ambazo sikuwahi kuziona hapo awali. Ilionekana kwangu kwamba Shetani alikuwa akijitahidi kuniondoa kutoka kwa mume wangu na watoto na kunilaza kaburini, na maswali haya yalipendekezwa akilini mwangu: Je! Unaweza kuamini ahadi ya MUNG kama ilivyo? Je! Unaweza kutembea kwa imani, bila kujali mwonekano uko vipi? Imani yangu ilifufuka, ilihuhishwa. Nilimnong'oneza mume wangu: "Ninaamini kwamba nitapona." Akajibu: "Natamani na mimi ningeamini hivyo." Nilienda kupumzika usiku ule bila raha, lakini nikitegemea imani thabiti juu ya ahadi za MUNGU. Sikuweza kulala, bali niliendelea na maombi yangu ya kimya. Kabla hakujapambazuka nililala. {1T 93.2}

Niliamka wakati wa kuchomoza jua kabisa bila maumivu. Shinikizo juu ya moyo wangu lilikuwa limekwisha, na nilikuwa na furaha sana. Ah, ni mabadiliko makubwa kiasi gani! Ilionekana kwangu kuwa malaika wa MUNGU alikuwa amenigusa wakati nilipokuwa nimelala. Nilijawa na shukrani. Sifa ya MUNGU ilikuwa juu ya midomo yangu. Nilimwamsha mume wangu, na kumsimulia kazi nzuri ambayo Bwana alikuwa amenifanyia. Mwanzoni hakuweza kuelewa; lakini nilipoamka na kuvaa na kuzunguka nyumba, ndipo aliweza kumsifu MUNGU pamoja nami. Jicho langu lenye mateso halikuwa na maumivu. Katika siku chache uvimbe ulipotea, na macho yangu yakarejeshwa kabisa. Kazi ilikuwa imekamilika. {1T 94.1}

Nilimtembelea tena daktari, na mara tu aliposikia mapigo yangu ya moyo, akasema: "Mama, mabadiliko kamili yametokea katika mfumo wako; lakini wanawake wawili walionitembelea kupata ushauri ulipokuwa hapa mara ya mwisho, wamefariki." Nilimwambia dawa yake haikuniponya, kwani sikuweza kuitumia hata mara moja. Baada ya kuondoka, daktari alimwambia rafiki yangu: "Tatizo lake ni fumbo, kitendawili hakika. Mimi silielewi." {1T 94.2}

Punde tulitembelea Michigan tena, na nilivumilia safari ndefu na zenye kuchosha katika njia mbaya, na kupitia chochoro zenye matope, na nguvu zangu hazikushindwa. Tulihisi kwamba Bwana angetutaka tutembelee Wisconsin, na tukapanga kuchukua gari huko Jackson saa kumi jioni. {1T 94.3}

Tulipokuwa tukijiandaa kuchukua garimoshi, tulijisikia huzuni sana, na tukapendekeza kuwa na wasaa wa maombi. Na tulipojitoa kwa MUNGU huko, hatukuweza kujizuia kulia. Tulikwenda kwenye depo, yaani kitu cha treni tukiwa na hisia za shughuli makini. Tulipopanda gari moshi, tuliingia kwenye behewa la mbele, ambalo lilikuwa na viti vyenye migongo ya juu, tukitumaini kwamba tunaweza kulala kiasi usiku huo. Behewa lilikuwa limejaa, na tukapita tena, na huko mbele tukapata behewa lenye viti. Sikuvua kofia/kilemba changu

kama kawaida yangu wakati wa kusafiri usiku, bali nilishikilia mkoba wangu mkononi, kama mtu anayengojea kitu fulani. Sisi sote tulizungumza juu ya hisia zetu za tashwishi moyoni, kwamba kuna jambo lisilo sawa hapa. {1T 94.4}

Garimoshi lilikuwa limekimbia karibu maili tatu kutoka Jackson, Michigan wakati mwendo wake ulipokuwa mkali sana, ukiruka nyuma na mbele, na mwishowe likasimama. Nilifungua dirisha, na nikaona behewa moja limeinuliwa kule karibu na mwisho. Nikasikia watu wakilia kwa maumivu, na kulikuwa na machafuko makubwa. Injini ilikuwa imetupwa kutoka kwenye gari; lakini behewa tulilokuwamo lilikuwa juu ya njia ya reli, na lilitengwa kama futi mia moja kutoka kwa yale mabehewa yaliyotangulia. Behewa la kubeba mizigo halikuharibika sana, na sanduku letu kubwa la vitabu halikuharibika. Behewa la daraja la pili lilikandamizwa, na vipande, pamoja na abiria, vilitupwa pande zote za garimoshi. Behewa ambalo tulijaribu kupata kiti lilikuwa limevunjika sana, na mwisho mmoja uliinuliwa juu ya lundo la magofu. Kiunganishi hakikuvunjika, lakini behewa tulilokuwa ndani yake lilikuwa limefunguliwa kutoka kwa lile lililokuwa mbele yake, kana kwamba malaika alikuwa ametenganisha. Wanne waliuawa au kujeruhiwa vibaya, na wengi walijeruhiwa vibaya sana. Tungeweza kuhisi tu kwamba MUNGU alikuwa ametuma malaika kuhifadhi maisha yetu. {1T 95.1}

Tulirejea Jackson, Michigan na siku iliyofuata tukachukua gari-moshi kuelekea Wisconsin. Ziara yetu katika jimbo hilo ilibarikiwa na MUNGU. Nafsi ziliongolewa kwa Bwana kama matokeo ya juhudi zetu. Bwana aliniimarisha kuvumilia safari ya uchovu. {1T 95.2}

Agosti 29, 1854, jukumu lingine liliongezwa katika familia yetu wakati alipozaliwa Willie (mtoto wa mwisho na wa nne). Kufikia wakati huu idadi ya kwanza ya magazeti yaliyoitwa kwa uongo Mjumbe wa Ukweli yalipokelewa (Messengers of Truth). Wale waliotusingizia na kutuchafua majina kupitia magazeti hayo walikuwa wamekemewa kwa matendo na makosa yao. Hawakuweza kuvumilia karipio, na kwa njia ya siri mwanzoni, na baadaye kwa waziwazi, walitumia ushawishi wao dhidi yetu. Tungeweza kustahimili jambo hili, lakini baadhi ya wale ambao wangepaswa kusimama nasi waliathiriwa na watu hawa waovu. Baadhi ya wale tuliowaamini, na waliokiri kuwa kazi wetu zilibarikiwa sana na MUNGU, wakaondoa huruma yao kutoka kwetu, na kuwapatia wale watu wasiowajua kabisa. {1T 95.3}

Bwana alikuwa amenionesha tabia na mwisho wa kile kikundi; mkunjo wa uso wake ulikuwa dhidi ya wale waliounganika na gazeti, na mkono Wake ulikuwa dhidi yao. Na ingawa wangeonekana kufanikiwa kwa muda, na wengine waaminifu kudanganywa, lakini Ukweli hatimaye utashinda, na kila mtu mwaminifu angejitenga na udanganyifu uliokuwa umemshikilia, na kutoka nje kwa wazi kutokana na ushawishi wa watu hao waovu; kwa kuwa mkono wa MUNGU ulikuwa juu yao, na ilikuwa lazima wadondoke chini. {1T 96.1}

Kisha afya ya mume wangu ikawa mbaya sana tena. Alisumbuliwa na kikohozi na maumivu ya mapafu, na mfumo wake wa neva ulitindikiwa. Kukosa utulivu kwa akili yake, mizigo aliyokuwa anaibeba Rochester, kazi yake ofisini, magonjwa na vifo katika familia, ukosefu wa huruma kutoka kwa wale ambao walipaswa kushiriki kazi zake, pamoja na safari zake na mahubiri, zilikuwa mzigo mzito sana kulingana na nguvu zake, na alionekana kwenda chini kwa kasi na kuelekea kaburi linalomeza kupitia ugonjwa wa kifua kikuu. Huo ulikuwa wakati wa huzuni na giza. Mionzi michache ya nuru mara kwa mara ilisambaratisha mawingu mazito, ikitupatia tumaini kidogo, vinginevyo tungezama kwa kukata tamaa. Ilionekana wakati mwingine kwamba MUNGU alikuwa ametuacha,ametutelekeza kabisa. {1T 96.2}

Chama cha Mjumbe (*Messenger Party*) kiliunda kila aina ya uongo kutuhusu sisi. Maneno haya ya Mwandishi wa-Zaburi mara nyingi yaliletwa kwa nguvu akilini mwangu: "Usikasirike kwa sababu ya watenda mabaya, Usiwahusudu wafanyao ubatili. Maana kama majani watakatika mara, Kama miche mibichi watanyauka." Baadhi ya waandishi wa magazeti hayo hata walijiona washindi kwa udhaifu wa mume wangu, wakisema MUNGU angemshugulikia haswa, na kumwondoa katika njia. Mume wangu aliposoma mambo haya wakati akiwa mgonjwa amelala, imani yake ilifufuka, akasema: "Sitakufa, bali nitaishi, na kutangaza kazi za Bwana, na bado naweza kuhubiri katika mazishi yao-Zaburi 118:17." {1T 96.3}

Mawingu meusi zaidi yalionekana kufungwa juu yetu. Watu wabaya wanaodai utauwa, chini ya amri ya Shetani waliharakishwa kughushi uongo, na kuleta nguvu ya vikosi vyao dhidi yetu. Kama kazi ya MUNGU ingekuwa yetu peke yetu, tungekuwa tumetetemeka; lakini ilikuwa mikononi mwa Yeye ambaye angeweza kusema: "Hakuna mtu awezaye kuinyakua kutoka mikononi Mwangu." Tulijua kwamba Yesu aliishi na kutawala kila kitu. Tungeweza kusema mbele za Bwana: Kazi ni yako, na unajua kwamba haikuwa hiari yetu wenyewe, lakini ni kwa amri Yako, kwamba tumetenda sehemu tuliyotenda. {1T 97.1}

## SURA YA 13

## KUONDOLEWA KWENDA MICHIGAN

Mnamo mwaka wa 1855 ndugu huko Michigan walifungua njia kwa ajili ya ofisi ya uchapishaji kuondolewa kwenda Battle Creek. Wakati huo mume wangu alikuwa anadaiwa kati ya dola elfu mbili hadi elfu tatu hivi, na yote aliyokuwa nayo kando na vitabu vilivyokuwa mikononi mwake ni idadi za vitabu, na vingine vilikuwa vyenye mashaka (kuuzika). Ni dhahiri kuwa kazi ilikuwa imefikia hatua ya kutoendelea mbele, maagizo ya machapisho yalikuwa machache sana na yenye idadi ndogo, na alikuwa anahofia kwamba angekufa na madeni. Ndugu huko Michigan walitusaidia kupata uwanja na kujenga nyumba. Hati hiyo iliandikwa kwa jina langu, ili niweze kuitoa kiurahisi baada ya kifo cha mume wangu. {1T 97.2}

Hizo zilikuwa siku za huzuni. Niliwatazama wavulana wangu watatu, punde nikapatwa na hofu, wataachwa bila baba, na mawazo kama haya yalijisukuma juu yangu: Mume wangu anakufa kwa kufanya kazi kupita kiasi kwa sababu ya Ukweli wa sasa; na ni nani anayetambua kile alichoteseka kwacho, mizigo aliyonayo kwa miaka mingi, masumbufu yaliyokithiri ambayo yamevunja roho yake na kuharibu afya yake, yakimleta kaburini kabla ya wakati, akiacha familia yake ikiwa fukara na tegemezi? Nimekuwa mara nyingi nikijiuliza swali, Je! MUNGU hajali vitu hivi? Je! Yeye huyapita haya matatizo bila kuyaona au kuyatambua? Nilifarijika kujua kuwa Yuko mmoja anayehukumu kwa haki, na kwamba kila dhabihu, kila kujinyima, kujikana nafsi na kila maumivu ya uchungu yaliyovumiliwa kwa ajili Yake, yameandikwa kwa uaminifu mbinguni, na yataleta thawabu yake. Siku ya Bwana itatangaza na kuleta nuruni mambo ambayo bado hayajadhihirishwa sasa. {1T 97.3}

Nilioneshwa kuwa MUNGU amekusudia kumwinua mume wangu pole pole; kwamba ni lazima tuwe na imani thabiti, kwani kwa kila juhudi tunapaswa kuchapwa vibaya na Shetani; kwamba lazima tuangalie mbali na mwonekano wa nje, na tuamini. Mara tatu kwa siku tulikwenda peke yetu mbele za MUNGU, na tukafanya maombi ya dhati ili arejeshewe afya yake. Mara kwa mara mmoja wetu angeangushwa chini na nguvu za MUNGU. Bwana kwa neema alisikia kilio chetu cha dhati, na mume wangu akaanza kupona. Kwa miezi mingi sala zetu zilipaa mbinguni mara tatu kwa siku ili afya ifanye mapenzi ya MUNGU. Nyakati hizi za sala zilikuwa za thamani sana. Tuliletwa katika ukaribu mtakatifu na MUNGU, na tulikuwa na ushirika mzuri Naye. Siwezi kuelezea vizuri hisia zangu kwa wakati huu kuliko zinavyooneshwa katika dondoo zifuatazo kutoka katika barua niliyomwandikia dada Howland: {1T 98.1}

"Ninajisikia kushukuru kwamba sasa ninaweza kuwa pamoja na watoto wangu, chini ya uangalizi wangu mwenyewe, na ninaweza kuwafundisha vizuri katika njia sahihi. Kwa majuma kadhaa nimehisi kuwa na njaa na kiu ya wokovu, na tumefurahia ushirika usiokatishwa pamoja na MUNGU. Kwa nini tunakaa mbali na chemchemi, wakati ambapo tungeweza kuja na kunywa? Kwa nini tunakufa kwa kukosa mkate, wakati kuna ghala kamili iliyojaa tele? Iliyojaa tena iliyo bure kwa wote. Ee nafsi yangu, sherekea, na kila siku unywe katika furaha ya

mbinguni. Sitanyamaza kimya. Sifa za MUNGU ziko moyoni mwangu na kwenye midomo yangu. Tunaweza kufurahi kwa ukamilifu wa upendo wa Mwokozi wetu. Tunaweza kufanya karamu juu ya utukufu Wake bora. Nafsi yangu inashuhudia jambo hili. Huzuni yangu imetawanywa na nuru hii ya thamani, na siwezi kusahau hili kamwe. Bwana, nisaidie kuiweka katika ukumbusho mzuri. Amka, nguvu zote za roho yangu! Amka, na umwabudu Mkombozi wako kwa upendo wake wa ajabu! {1T 98.2}

“Nafsi zinazotuzunguka lazima ziamshwe na kuokolewa, la sivyo zitaangamia. Hatuna nukta yoyote au muda wa kupoteza. Sisi sote tuna ushawishi ambao unaelezea kuhusu Ukweli au kinyume chake. Ninatamani kubeba pamoja nami uthibitisho usiokosea kwamba mimi ni mmoja wa wafuasi wa Kristo. Tunahitaji kitu kando ya dini ya Sabato. Tunahitaji kanuni inayoishi, na kila siku tuhisi wajibu wetu binafsi. Jambo hili linaepukwa na wengi, na matokeo yake ni uzembe, kutokujali, na ukosefu wa uangalifu na kukesha kiroho. Hali ya kiroho ya kanisa iko wapi? Je, wako wapi wanaume na wanawake waliojaa imani na ROHO MTAKATIFU? Ombi langu ni hili: Litakase kanisa Lako, Ee MUNGU. Kwa miezi kadhaa nimefurahia uhuru, na nimeazimia kuelekeza mazungumzo yangu na njia zangu zote ziwe sawa mbele za Bwana. 1T 99.1}

“Adui zetu wanaweza kushinda. Wanaweza kusema maneno machungu, na ulimi wao ukatengeneza kashfa, udanganyifu, na uongo, lakini hatutatikiswa. Tunamjua tunayemwamini. Hatukukimbia bure (Fip 2:16), wala hatukufanya kazi bure. Siku ya kutoa hesabu inakuja, ambapo wote watahukumiwa kulingana na matendo yaliyofanywa mwilini. Ni kweli ulimwengu uko gizani. Upinzani unaweza kuwa na nguvu. Wadanganyifu na wenye dhihaka wanaweza kuwa hodari katika uovu wao. Lakini kwa haya yote hatutahamishwa, bali tutaegemea juu ya mkono wa Mwenye nguvu ili tupate nguvu. {1T 99.2}

“MUNGU anawapepeta watu Wake. Yeye Atakuwa na kanisa safi na takatifu. Sisi hatuwezi kusoma moyo wa mwanadamu. Lakini Bwana ametoa njia na fedha ya kuliweka kanisa safi. Watu waovu, mafisadi wameibuka ambao wasingeweza kuishi na watu wa MUNGU. Walidharau karipio, na hawakurekebishwa. Walikuwa na nafasi ya kujua kwamba vita yao ilikuwa vita isiyo ya haki. Walikuwa na wakati wa kutubu makosa yao, lakini ubinafsi, umimi ulikuwa umependwa sana. Waliupatia virutubisho, nao ukawa na nguvu, nao wakajitenga na watu wa MUNGU wanaomtumaini Yeye, ambao Yeye Mwenyewe amekuwa akiwatakasa kwa ajili yake mwenyewe. Sote tunayo sababu ya kumshukuru MUNGU kwamba njia imefunguliwa kuliokoa kanisa; kwani ghadhabu ya MUNGU lazima ingekuja juu yetu kama hawa wadanganyifu na waigizaji wangebaki pamoja nasi (watu feki). {1T 99.3}

Kila roho ya uaminifu inayoweza kudanganywa na hawa wasioridhika, itakuwa na nuru ya Kweli kuhusiana nao, hata ikiwezekana kila malaika kutoka mbinguni awatembelee, ili kuwaangazia akili zao. Hatuna cha kuhofia juu ya jambo hili.

Tunapokaribia hukumu, wote wataonesha tabia zao halisi, na zitawekwa wazi kwamba zimetokana na kundi gani. Pepeto linaendelea. Tusiseme: Zuia mkono wako, Ee MUNGU. Kanisa lazima lisafishwe, na itakuwa hivyo. MUNGU anatawala; wacha watu wamsifu. Sina wazo la mbali kabisa la kuzama chini. Namaanisha kuwa sawa na kutenda sawa. Hukumu itawekwa, vitabu vifunguliwa, na tunapaswa kuhukumiwa kulingana na matendo yetu. Uongo wote ambao unaweza kutungwa dhidi yangu hautanifanya nizidi kuwa mbaya, au bora zaidi isipokuwa utakuwa na kawaida ya kunisogeza karibu zaidi na Mkombozi wangu." {1T 100.1}

Kuanzia wakati tulipohamia Battle Creek, Bwana alianza kugeuza mateka yetu. Tulipata marafiki wenye huruma huko Michigan, ambao walikuwa tayari kushiriki mizigo yetu na kutupatia mahitaji yetu. Marafiki wa zamani, wema katikati mwa New York na New England, hasa huko Vermont, walituhurumia katika shida zetu, na walikuwa tayari kutusaidia wakati wa shida. Katika Mkutano huko Battle Creek mnamo Novemba, 1856, MUNGU alitutendea makuu. Akili za waja wake zilitumika kama karama za kanisa. Kama mkunjo wa uso wa MUNGU ungeletwa juu ya watu Wake kwa sababu ya vipawa vilivyopuuzwa na kutelekezwa, kungekuwa na matarajio ya kufurahisha kwamba tabasamu Zake zingekuwa tena juu yetu, kwamba kwa neema angefufua karama hizo, na zingeendelea kuwepo kanisani ili kuzitia moyo roho zinazozimia, na kusahihisha na kukaripia wakosaji. Maisha mapya yangetolewa katika kazi, na mafanikio yangeandamana na kazi za wahubiri wetu. {1T 100.2}

Machapisho yalihitajika, na ilithibitika kuwa ndiyo tu kile ambacho kazi ilihitaji. Mjumbe wa Ukweli punde alishuka chini, na roho za kutatanisha zilizozungumza kupitia yeye zilitawanyika. Mume wangu aliwezeshwa kulipa madeni yake yote. Kikohozi chake kilikoma, maumivu na uchungu viliondoka kwenye mapafu na koo, na polepole alirejeshwa kuwa mzima, ili aweze kuhubiri mara tatu siku ya Sabato na siku ya kwanza kwa urahisi. Kazi hii ya ajabu katika urejeshwaji wake afya, ilikuwa ya MUNGU, na yeye anapaswa kuwa na utukufu wote. {1T 100.3}

Wakati mume wangu akiwa dhaifu sana, kabla ya kuondolewa kwetu Rochester, alitaka kujikomboa kutoka kwenye jukumu la kazi ya uchapishaji. Alipendekeza kanisa lisimamie kazi hiyo, na kwamba iwe inasimamiwa na kamati ya uchapishaji ambayo wangeichagua, na kwamba hakuna mtu anayeunganishwa na ofisi atakayepata faida yoyote ya kifedha zaidi ya mshahara anaoupokea kwa kazi yake. {1T 101.1}

Ingawa jambo hilo lilikuwa likihimizwa mara kwa mara kwenye mawazo yao, ndugu zetu hawakuchukua hatua yoyote hadi mwaka 1861. Mpaka wakati huu mume wangu alikuwa mmiliki halali wa nyumba ya uchapishaji, na msimamizi pekee wa kazi. Alifurahia ujasiri ambao marafiki wenye bidii kwa kazi hiyo walimwosha, wale ambao waliamini uchapaji katika uangalizi wake kwa mali

walizochangia mara kwa mara, kwa kadri kazi inayoongezeka ilivyohitaji, kujenga taasisi ya uchapishaji. Lakini ingawa taarifa hiyo ilirudiwa mara kwa mara kupitia gazeti la Review, kwamba nyumba ya uchapishaji ilikuwa mali ya kanisa, lakini kwa kuwa alikuwa msimamizi pekee halali, maadui zetu walitumia fursa hiyo, na kwa kilio cha uvumi, walifanya yote yaliyo ndani ya uwezo wao kuanzisha suala la muundo, ambalo lilisababisha kuundwa kwa Shirika la Uchapishaji la Waadventista Wasabato, kulingana na sheria za Michigan, katika majira ya kupukutisha majani ya 1861. {1T 101.2}

Ijapokuwa masumbufu yaliyotujia kuhusiana na kazi ya uchapishaji na matawi mengine ya kazi hiyo yalihusisha mkanganyiko sana, kujitoa kafara kukubwa zaidi nilikokuwa nimeitwa kuifanya kwa habari ya kazi ilikuwa ni kuwaacha watoto wangu katika uangalizi wa wengine. {1T 101.3}

Henry alikuwa mbali nasi kwa miaka mitano, na Edson alikuwa amepata uangalizi wetu mdogo tu. Kwa miaka mingi familia yetu ambayo ilikuwa kubwa sana, na nyumba yetu ilikuwa kama hoteli, na sisi tulikuwa hatupo hapo nyumbani muda mwingi. Nilikuwa nimehisi wasiwasi mkubwa sana kwamba watoto wangu wanapaswa kulelewa bila kuwa na tabia mbaya, na mara nyingi nilikuwa na huzuni nilipofikiria tofauti kati ya hali yangu na ya wengine ambao hawatachukua mizigo na fadhaa, ambayo wangeweza kuwa na watoto, kuwashauri na kuwaelekeza, na ambao walitumia muda wao karibu wote katika familia zao. Na nimeuliza: Je! MUNGU anatuhitaji sana, na kuwaacha wengine bila mizigo? Je! Huu ni usawa? Je! Tunapaswa kuharakishwa kutoka huduma moja hadi nyingine, sehemu moja ya kazi hadi nyingine, na kuwa na wakati mdogo tu wa kulea watoto wetu? Usiku mwingi, wakati wengine wakiwa wamelala, nimeutumia katika kulia kwa uchungu. {1T 102.1}

Ningepanga hatua nzuri zaidi zinazowafaa watoto wangu, kisha pingamizi zingeibuka ambazo zingefagilia mbali mipango hii yote. Nilijali sana makosa ya watoto wangu, na kila kosa walilofanya liliniletea maumivu ya moyo kiasi cha kuathiri afya yangu. Nilitamani akina mama wengine wangekuwa kwa muda mfupi na mazingira kama niliyokuwa nayo kwa miaka kadhaa; basi wangethamini baraka wanazofurahia, na wangeweza kunionea huruma zaidi katika hali yangu ya upweke na shida zangu. Tuliomba na kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watoto wetu, na tukawadhibiti. Hatukupuuzia fimbo, lakini kabla ya kuitumia tulijitahidi kwanza kuwasaidia waone makosa yao, kisha tukaomba pamoja nao. Tulitafuta kuwafanya watoto wetu waelewe kwamba tutastahili hasira ya MUNGU ikiwa tutawaacha waendelee katika dhambi. Na juhudi zetu zilibarikiwa kwa faida yao. Raha yao kubwa ilikuwa kutufurahisha. Hawakuwa huru kutoka kwa makosa ya wengine, bali tuliamini kwamba watakuwa bado ni kondoo wa zizi la Kristo. {1T 102.2}

Mnamo mwaka 1860 kifo kilipita juu ya kizingiti chetu, na kuvunja tawi la mwisho kabisa la familia yetu. Herbert mdogo, aliyezaliwa Septemba 20, 1860,

alikufa desemba 14 mwaka huo huo. Wakati tawi hilo laini likivunjwa, jinsi mioyo yetu ilivyotokwa damu hakuna mwingine awezaye kujua isipokuwa wale ambao waliwafuata watoto wao wa ahadi kaburini. {1T 102.3}

Lakini! wakati mtoto wetu mwungwana Henry alipokufa, [KIFO CHA HENRY N. WHITE KILITOKEA HUKO TOPSHAM, MAINE, DESEMBA 8, 1863.] akiwa na umri wa miaka kumi na sita; wakati mwimbaji wetu mwenye sauti tamu alipochukuliwa kaburini (sweet singer), na tusiweze kuusikia tena wimbo wake wa alfariji mapema, nyumba yetu ilikuwa na upweke. Wazazi wote wawili na watoto wawili waliobaki walihisi pigo hilo kwa nguvu. Lakini MUNGU alitufariji katika msiba wetu, na kwa imani na ujasiri tuliendelea kusonga mbele katika kazi aliyotupatia, kwa matumaini mazuri ya kukutana na watoto wetu ambao waliraruliwa na kifo kutoka kwetu, katika ulimwengu huo ambao magonjwa na mauti hayatakuja kamwe. {1T 103.1}

Mnamo Agosti, 1865, mume wangu alipigwa ghafla na kupooza. Hili lilikuwa pigo zito, siyo kwangu na watoto wangu tu, bali kwa kusudi la kazi ya MUNGU. Makanisa yalizikosa kazi zote za mume wangu na mimi mwenyewe. Shetani alishinda alipoona kazi ya Ukweli ikizuiliwa. Lakini, asante MUNGU ! hakuruhusiwa kutuangamiza. Baada ya kukatwa kutoka katika kazi yote kwa miezi kumi na tano, tulijitosa tena kwa pamoja kufanya kazi kati ya makanisa. {1T 103.2}

Baada ya kuridhika kabisa kuwa mume wangu hatapona ugonjwa wake wa muda mrefu wakati akiendelea kukaa bila kazi, na kwamba muda ulikuwa umefika kabisa kwangu kwenda kutoa ushahidi wangu kwa watu, niliamua kufanya ziara kaskazini mwa Michigan, niliandamana na mume katika hali yake dhaifu sana, katika baridi kali kabisa ya msimu wa baridi. Haikuhitaji ujasiri mdogo wa kimaadili na imani kwa MUNGU kuiongoza akili yangu kwa uamuzi wa kuthubutu kujihatarisha kiasi hicho; lakini nilijua kwamba nilikuwa na kazi ya kufanya, na ilionekana kwangu kwamba Shetani alikuwa ameazimia kunizuia kushiriki kazi. Nilikuwa nasubiri kwa muda mrefu mateka yetu yageuzwe, na nilihofia hizo roho za thamani zisije zikatapotea kwa sababu ya kucheleweshwa. Kukaa muda mrefu bila kwenda kazini kwangu kulionekana kuwa jambo baya zaidi kuliko kifo, na niliamini nikitoka nje naweza kuangamia. Kwa hivyo, mnamo 19 Desemba, 1866, tulitoka Battle Creek katika dhoruba ya theluji kuelekea Wright, Michigan. Mume wangu aliweza kuvumilia safari ya maili tisini vizuri zaidi kuliko nilivyoogopa, na alionekana katika hali hiyo hiyo wakati wa kwenda na wakati wa kurudi Battle Creek. {1T 103.3}

Hapa tulianza kazi yetu ya kwanza yenye ufanisi tangu ugonjwa wake. Hapa alianza kazi kama miaka ya zamani, ingawa alikuwa katika udhaifu mwingi. Angeongea dakika thelathini au arobaini kabla ya siku ya Sabato na siku ya kwanza, wakati mimi ningetumia muda wote, kisha nikaongea alasiri ya kila siku, karibu saa moja na nusu kila wakati. Tulisikilizwa kwa umakini mkubwa.

Niliona mume wangu alikuwa akiongezeka nguvu, kwa uwazi zaidi, na kuyaunganisha vizuri zaidi masomo yake. Na wakati katika hafla moja alipozungumza kwa saa moja kwa uwazi na kwa nguvu, akiwa na mzigo wa kazi ukiwa juu yake kama alivyokuwa kabla ya ugonjwa wake, hisia zangu za shukrani zilivuka mpaka. Niliamka katikati ya mkutano, na kwa karibu nusu saa nilijaribu kutamka jambo kwao huku nalia. Kutaniko liliguswa sana. Nilihisi kuhakikishiwa kwamba hii ilikuwa alfajiri ya siku bora kwetu. {1T 104.1}

Mkono wa MUNGU katika urejeshwaji Wake ulikuwa dhahiri zaidi. Huenda hakuna mtu mwingine aliyewahi kupata pigo kama hilo na akapona. Hata hivyo mshtuko mkali wa kupooza, ulioathiri sana ubongo wa mume wangu, uliondolewa kwa mkono mwema wa MUNGU kutoka kwa mtumishi Wake, na nguvu mpya ikatolewa kwa mwili na akili. {1T 104.2}

Katika kipindi cha miaka iliyofuatia kupona kwa mume wangu, Bwana alifungua mbele yetu shamba kubwa la kazi. Ingawa nilichukua msimamo kama mzungumzaji mkuu kwa woga mwanzoni, lakini kwa majaliwa ya MUNGU yalipofungua njia mbele yangu, nilikuwa na ujasiri wa kusimama mbele ya hadhira kubwa. Kwa pamoja tulihudhuria mikutano yetu ya makambi na mikusanyiko mingine mikubwa, kutoka Maine hadi Dakota, kutoka Michigan hadi Texas na California. {1T 104.3}

Kazi iliyoanza kwa unyonge, utusitusi na upofu imeendelea kuongezeka na kuimarika. Nyumba za kuchapisha huko Michigan na huko California, na misheni huko England, Norway, na Uswisi, zinathibitisha ukuaji wake. Badala ya toleo la gazeti letu la kwanza lililopelekwa ofisini kwenye mkoba wa zulia, karibu nakala laki moja na elfu arobaini za majarida yetu mbalimbali sasa zinatumwa kila mwezi kutoka ofisi za uchapishaji. Mkono wa MUNGU umekuwa pamoja na kazi Yake kuifanikisha na kuijenga. {1T 105.1}

Historia ya baadaye ya maisha yangu ingehusisha historia ya shughuli mbalimbali ambazo zimeibuka kati yetu, na ambazo zimekuwa zikiingiliana kwa karibu na kazi yangu ya maisha. Kwa ujenzi wa taasisi hizi, mume wangu na mimi tulifanya kazi kwa kalamu na sauti. Kutambua, hata kwa ufupi, uzoefu wa miaka hii ya kazi na yenye shughuli nyingi, kunazidi sana mipaka ya maelezo haya nayoandika sasa. Jitihada za Shetani za kuzuia kazi na kuwaangamiza wafanya kazi hazijakoma; lakini MUNGU amekuwa na uangalizi kwa watumishi wake na kwa kazi Yake. {1T 105.2}

# SURA YA 14

# KIFO CHA MUME WANGU

Pamoja na kazi, wasiwasi, na majukumu ambayo yaliyajaza maisha ya mume wangu, mwaka wake wa sitini ulimkuta akifanya kazi na mwenye nguvu katika akili na mwili. Mara tatu alikuwa ameanguka chini kwa kiharusi na kupooza; lakini kwa baraka za MUNGU, kwa uimara wa mwili aliopewa na Mungu kwa asili, na kwa umakini mkubwa wa kanuni za afya, alikuwa amewezeshwa kufika hapo. Tena alisafiri, akahubiri, na akaandika kwa nguvu, ari/usongo na bidii yake ya kawaida. Bega kwa bega tulikuwa tumetumika katika kazi ya Kristo kwa miaka thelathini na sita; na tulitumai kuwa tungeweza kusimama pamoja kushuhudia ushindi wa hii kazi na kufungwa kwake. Lakini hayo hayakuwa mapenzi ya MUNGU. Mlinzi mteule wa ujana wangu, mwenza wa maisha yangu, mshiriki wa kazi na taabu zangu, amechukuliwa kutoka upande wangu, nami nimebaki kumaliza kazi yangu na kupigana vita peke yangu. {1T 105.3}

Majira ya vuli na mapema majira ya joto ya mwaka 1881 tulikaa pamoja nyumbani kwetu huko Battle Creek. Mume wangu alitarajia kupanga shughuli yake ili tuweze kwenda Pwani ya Pasifiki huko California na kujitoa kwa ajili ya kuandika. Alihisi kuwa tumekosea kwa kuruhusu mahitaji dhahiri ya kazi na maombi ya ndugu zetu kutusukuma tufanye kazi ya kuhubiri wakati tulipaswa kuwa tunaandika. Mume wangu alitaka kuwasilisha kikamilifu zaidi somo tukufu la ukombozi, na kwa muda mrefu nilikuwa nimefikiria utayarishaji wa vitabu muhimu. Sisi sote tulihisi kuwa wakati nguvu zetu za akili zikiwa hazijaharibika tunapaswa kukamilisha kazi hizi - kwamba lilikuwa ni jukumu tunalodaiwa na sisi wenyewe na kusudi la kazi ya MUNGU kupumzika kutokana na joto la vita, na kuwapa watu wetu mwangaza wa thamani wa Ukweli ambao MUNGU alikuwa ameufungua kwa akili zetu. {1T 106.1}

Majuma kadhaa kabla ya kifo cha mume wangu, nilimsihi juu ya umuhimu wa kutafuta uwanja wa kazi ambapo tutafunguliwa kutoka katika mizigo inayotupata huko Battle Creek. Kwa kujibu alizungumza juu ya mambo anuwai ambayo yanahitaji umakini kabla hatujaondoka - majukumu ambayo lazima mtu ayafanye. Halafu kwa hisia kali aliuliza: "Wako wapi watu wa kuifanya kazi hii? Wako wapi wale ambao watakuwa na nia isiyo ya ubinafsi katika taasisi zetu, na ni akina nani watakaosimama kwa haki, bila kuathiriwa na ushawishi wowote ambao wanaweza kukutana nao? " {1T 106.2}

Kwa machozi alielezea wasiwasi wake kwa taasisi zetu huko Battle Creek. Alisema: “Maisha yangu yametolewa kafara kwa ajili ya ujenzi wa taasisi hizi. Kuziacha taasisi hizi kwangu ni kama kifo. Taasisi hizi ni kama watoto wangu, na siwezi kutenganisha masilahi yangu kutoka kwazo. Taasisi hizi ni nyenzo za Bwana kwa ajili ya kutenda kazi maalum. Shetani anatafuta kuzuia na kuishinda kila mbinu na njia ambayo Bwana anafanyia kazi kwa ajili ya wokovu wa

wanadamu. Kama adui mkuu anaweza kuzifinyanga hizi taasisi zilingane na kiwango cha ulimwengu, lengo lake litakuwa limetimia. Ni mzigo wangu unaoniletea fadhaa kubwa kuwa na mtu sahihi katika mahali sahihi. Ikiwa wale wanaosimama katika nafasi za uwajibikaji ni dhaifu kwa nguvu ya maadili, na wanayumba katika usimamizi wa kanuni, na uelekeo wa kutaka kuongoza sawa sawa na ulimwengu, watu watakaoongozwa kuelekea huko watakuwa wengi. Ushawishi mbaya haupaswi kushinda. Ningependelea kufa kuliko kuishi na kuziona taasisi hizi zikisimamiwa vibaya, au kupinda kona ya mbali na kusudi la kuanzishwa kwazo. {1T 106.3}

"Katika uhusiano wangu na kazi hii nimekuwa mtu wa muda mrefu zaidi na nimeunganishwa sana na kazi ya uchapishaji. Mara tatu nimeanguka, nimepigwa na kupooza, kutokana na kujitoa kwangu kwa ajili ya tawi hili la kazi. Sasa kwa kuwa MUNGU amenipa nguvu zilizohuishwa za mwili na akili, nahisi kwamba ninaweza kulitumikia jukumu langu kuliko nilivyowahi kulitumikia hapo kabla. Lazima nione kazi ya uchapishaji ikifanikiwa. Kazi hii imeunganishwa na uwepo wangu. Ikiwa nitasahau maslahi ya kazi hii, hebu mkono wangu wa kulia na usahau uhodari wake-Zaburi 137:5." {1T 107.1}

Tulikuwa na miadi ya kuhudhuria mkutano wa kambi huko Charlotte, Sabato na Jumapili, Julai 23 na 24. Kwa kuwa nilikuwa na afya dhaifu, tuliamua kusafiri kwa usafiri binafsi. Njiani, mume wangu alionekana kuchangamka, lakini hisia nzito ilikuwa juu yake. Alimsifu Bwana mara kwa mara kwa rehema na baraka tulizopokea, na akaelezea hisia zake kwa uhuru kuhusiana na nyakati zilizopita na zijazo: "Bwana ni mwema, na Mkuu, Naye anapaswa kusifiwa sana (Zaburi 145:3). Yeye ni msaada wa wakati wa shida. Wakati ujao unaoonekana kuwa na mawingu na usio na hakika, lakini Bwana hakutaka tufadhaike juu ya mambo haya. Wakati shida itakapokuja, Yeye atatupatia neema ya kuvumilia. Vile Bwana alivyokuwa kwetu, na kile alichotufanyia, vinapaswa kutufanya tuwe wenye shukrani na tusionung'unika au kulalamika. Kazi zetu, mizigo yetu, na dhabihu zetu kamwe havitathaminiwa kikamilifu na watu wote. Ninaona kwamba nimepoteza amani yangu ya akili na baraka za MUNGU kwa kujiruhusu nisumbuliwe na mambo haya. {1T 107.2}

"Limeonekana kuwa ni jambo lililo gumu kwangu pale nia yangu inapohukumiwa vibaya, na pale juhudi zangu bora za kuwasaidia, kuwatia moyo na kuwaimarisha ndugu zangu zinapopuuzwa tena na tena na kugeuzwa dhidi yangu. Lakini nilipaswa kumkumbuka Yesu na jinsi alivyokatishwa tamaa. Nafsi yake ilikuwa ya kuhuzunisha kwa kuwa hakuthaminiwa na wale aliokuja kuwabariki. Ningepaswa kukaa juu ya rehema na fadhili za upendo wa MUNGU, nikimsifu zaidi, na kulalamika kidogo juu ya kutokuwa na moyo wa shukrani kwa ndugu zangu. Kama ningeacha shida na fadhaa zangu zote kwa Bwana, na kufikiria kidogo juu ya kile wengine wanachosema na walichofanya dhidi yangu, ningekuwa na amani na furaha zaidi. Sasa nitatafuta kwanza kujilinda nisije nikamkwaza mtu kwa neno au tendo, na kisha kuwasaidia ndugu zangu

kutengeneza njia zilizonyooka, na kuacha kuomboleza kwa kosa lolote nililofanyiwa. Nimetarajia mengi kutoka kwa wanadamu kuliko ninavyostahili. Ninampenda MUNGU  na kazi Yake, na ninawapenda ndugu zangu pia.” {1T 108.1}

Sikufikiria, wakati tunasafiri, kwamba hii ndiyo ilikuwa safari ya mwisho ambayo tunaweza kuifanya pamoja. Hali ya hewa ilibadilika ghafla kutoka joto dhalimu hadi baridi kali. Mume wangu alipata baridi, lakini alidhania afya yake ni nzuri sana kwamba hatapata madhara ya kudumu. Alifanya kazi kwa bidii katika mikutano huko Charlotte, akiwasilisha Ukweli kwa uwazi na nguvu kubwa. Alizungumza juu ya raha aliyohisi wakati wa kuhutubia watu ambao walionesha kupendezwa sana na masomo anayoyapenda sana. “Kwa kweli Bwana ameiburudisha roho yangu,” alisema, “wakati nilipokuwa naumega kwa wengine mkate wa uzima. Kote huko Michigan watu wanaita tukawasaidie. Ninatamani kiasi gani kuwafariji, kuwatia moyo, na kuwaimarisha na Ukweli wa thamani unaofaa kwa wakati huu!” {1T 108.2}

Tuliporudi nyumbani, mume wangu alilalamika juu ya shida kidogo, lakini aliendelea kujishughulisha na kazi yake kama kawaida. Kila asubuhi tulitembelea shamba karibu na nyumba yetu, na kuungana katika maombi. Tulikuwa na tashwishwi ya kujua wajibu wetu. Barua zilikuwa zikija kila wakati kutoka sehemu tofauti, zikituhimiza tuhudhurie mikutano ya kambi. Pamoja na dhamira yetu ya kujitolea kuandika, ilikuwa ngumu kukataa kukutana na ndugu zetu katika mikutano hii muhimu. Tuliomba kwa bidii hekima ya kujua njia sahihi. {1T 108.3}

Asubuhi ya Sabato, kama kawaida, tulienda visitu vyenye miti midogo ya matunda pamoja, na mume wangu aliomba kwa bidii mara tatu. Alionekana kusita kuacha kumwomba MUNGU  kwa mwongozo maalum na baraka. Maombi yake yalisikilizwa, na amani na nuru zilikuja mioyoni mwetu. Alimsifu Bwana, na akasema: “Sasa ninampa Yesu yote. Ninahisi amani tamu, ya mbinguni, hakikisho kwamba Bwana atatuonesha wajibu wetu; kwani tunatamani kufanya mapenzi Yake.” Alinisindikiza kwenda kwenye eneo la ibada, na kufungua huduma kwa kuimba na kuomba. Ilikuwa mara ya mwisho kabisa kusimama kando yangu kwenye mimbari. {1T 109.1}

Siku ya Jumatatu iliyofuata alikuwa na baridi kali, na siku iliyofuata mimi pia nilishambuliwa. Kwa pamoja tulipelekwa kwenye Sanitarium, Kliniki ya tiba rahisi. Ijumaa dalili zangu zikawa njema zaidi. Daktari alinijulisha kuwa mume wangu alikuwa na mwelekeo wa kulala, na hatari hiyo ilishughulikiwa. Mara moja nikapelekwa chumbani kwake, na mara tu nilipomtazama usoni nilijua kwamba alikuwa anakufa. Nilijaribu kumuamsha. Alielewa yote aliyoambiwa, na akajibu maswali yote ambayo yangeweza kujibiwa kwa kusema Ndiyo au Hapana, lakini alionekana kushindwa kusema zaidi. Nilipomwambia nilidhani anakufa, hakuonesha mshangao. Niliuliza ikiwa Yesu alikuwa wa thamani

kwake. Akasema “Ndiyo, oh, ndiyo.” “Je! Hauna hamu ya kuishi?” Niliuliza. Akajibu: Hapana. {1T 109.2}

Kisha tulipiga magoti kando ya kitanda chake, na nilimwombea. Maneno ya amani yalikaa juu ya uso wake. Nikamwambia. “Yesu anakupenda. Mikono ya milele iko chini yako.” Alijibu: “Ndiyo, ndiyo.” {1T 109.3}

Ndugu Smith na wengine basi waliomba karibu na kitanda chake, na wakatumia muda mwingi wa usiku katika maombi. Mume wangu alisema hakuhisi maumivu; lakini alikuwa akiendelea kuwka dhaifu kwa kasi. Dk Kellogg na wasaidizi wake walifanya yote yaliyokuwa ndani ya uwezo wao kumzuia asife. Alizinduka polepole, lakini aliendelea kuwa dhaifu sana. {1T 109.4}

Asubuhi iliyofuata alionekana kuzinduka kidogo, lakini kufikia saa sita mchana alikuwa na ubaridi, ambao ulimfanya apoteze fahamu. Saa 11 jioni, Sabato, Agosti 6, 1881, alitoa pumzi ya maisha yake kimya kimya, bila mapambano wala kelele. {1T 110.1}

Mshtuko wa kifo cha mume wangu – kilichotokea kwa ghafla, na bila kutarajiwa – uliniangukia kwa uzani mzito. Katika hali yangu dhaifu nilikuwa nimetafuta nguvu ya kubaki karibu na kitanda chake hadi mwisho, lakini nilipoona macho yake yakifungwa kwa kifo, hali ya uchovu ikapita, na nikaanguka na kupoteza fahamu. Kwa muda nilionekana kuwa katikati ya maisha na kifo. Mwali wa moto wa maisha yangu ulikuwa ukiwaka kwa chini sana kiasi kwamba pumzi ingeweza kuuzima. Usiku mapigo yangu yalikuwa dhaifu, na kupumua kwangu kuliendelea kuwa dhaifu na dhaifu zaidi hadi ikaonekana kana kwamba pumzi inakaribia kukoma. Ni kwa baraka ya MUNGU  tu na utunzaji usiokoma na uangalizi wa daktari na wahudumu ndipo maisha yangu yaliweza kuhifadhiwa. {1T 110.2}

Ingawa sikuinuka kitandani mwangu baada ya kifo cha mume wangu, nilifikishwa kanisani siku ya Sabato iliyofuata kuhudhuria mazishi yake. Mwisho wa mahubiri nilihisi jukumu la kushuhudia thamani ya tumaini la Mkristo katika saa ya huzuni na kufiwa. Nilipoinuka, nikapewa nguvu, na nikazungumza kwa dakika kumi, nikiziinua rehema na upendo wa MUNGU  mbele ya mkutano huo uliofurika. Mwisho wa huduma hiyo nilimfuata mume wangu hadi kwenye makaburi ya Oak Hill, Battle Creek, Michigan ambapo alilazwa hadi asubuhi ya ufufuo. {1T 110.3}

Nguvu zangu za mwili zilikuwa zimemalizwa na pigo hilo, lakini nguvu ya neema ya kiungu iliniimarisha katika msiba wangu mkubwa. Nilipoona mume wangu anapumua mara yake ya mwisho, nilihisi kuwa Yesu alikuwa wa thamani zaidi kwangu wakati huo kuliko vile alivyokuwa katika saa yoyote iliyopita ya maisha yangu. Niliposimama karibu na mzaliwa wangu wa kwanza, na kufumba macho yake katika kifo, nilisema: “Bwana ametoa, na Bwana ametwaa; jina la Bwana libarikiwe.” Na nilihisi wakati huo kwamba nilikuwa na mfariji katika Yesu. Na

wakati mtoto wangu wa mwisho alipotwaliwa mikononi mwangu, na nisiweze kuona tena kichwa chake kidogo juu ya mto kando yangu, ndipo nilipoweza kusema: “Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; jina la Bwana libarikiwe.” Na wakati yule ambaye mapenzi yangu makubwa yaliegemea kwake, ambaye nilikuwa nimefanya naye kazi kwa miaka thelathini na sita, alipochukuliwa, niliweza kuweka mikono yangu juu ya macho yake, na kusema: Ninaweka hazina yangu kwako mpaka asubuhi ya ufufuo. {1T 110.4}

Nilipomwona akipita, na kuwaona marafiki wengi wakinionea huruma, nilifikiri: Ni tofauti kubwa kiasi gani kwa kifo cha Yesu wakati alipokuwa akining'inia msalabani! Ni tofauti kubwa iliyoje! Katika saa ya uchungu Wake, watukanaji walipokuwa wakimtukana na kumdhihaki. Lakini alikufa, na alipitia kaburi ili kuangaza, na kuiweka nuru, ili tupate kuwa na furaha na matumaini hata katika tukio la kifo; ili tuweze kusema, tunapowaweka rafiki zetu kaburini wapumzike katika Yesu: Tutakutana nao tena. {1T 111.1}

Kuna wakati nilihisi kwamba sikupaswa kumruhusu mume wangu afe. Lakini maneno haya yalionekana kuleta mguso akilini mwangu: “Tulia, utambue kuwa mimi ni MUNGU.” Hakika ninahisi upotevu wangu, lakini sithubutu kujitoa kwa huzuni isiyo na maana. Hii haiwezi kuwarudisha wafu. Wala mimi si mbinafsi hata kutamani, ikiwa ningeweza, kumleta kutoka kwenye usingizi wake wa amani ili kushiriki tena katika vita ya maisha. Kama shujaa aliyechoka, mume wangu amelala usingizi. Nitaangalia kwa raha mahali pake pa kupumzika. Njia bora ambayo mimi na watoto wangu tunaweza kuheshimu kumbukumbu ya yule aliyeanguka, ni kuchukua kazi ambazo aliziacha, na kwa nguvu ya Yesu kusonga mbele hadi kuikamilisha. Tutashukuru kwa miaka yenye manufaa ambayo alitunukiwa-(miaka ya kunufaisha kazi na watu); na kwa ajili yake, na kwa ajili ya Kristo, tutajifunza kutokana na kifo **chake** somo ambalo hatutalisahau kamwe. Tutaruhusu msiba huu utufanye kuwa wenye fadhili zaidi na wapole, wenye uvumilivu zaidi, na kuwafikiria walio hai. {1T 111.2}

Ninachukua kazi yangu ya maisha peke yangu, kwa ujasiri kamili nikitambua kwamba Mkombozi wangu atakuwa pamoja nami. Sisi tuna muda kidogo tu wa kupiga vita; ndipo Kristo aje, na onesho hili la vita litafungwa. Ndipo juhudi zetu za mwisho zitakuwa zimefanyika ili tufanye kazi na Kristo, na kuendeleza ufalme Wake. Wengine ambao wamesimama mbele ya vita, wakipinga kwa bidii uovu unaokuja, huanguka wakiwa kazini. Wale walio hai huwakodolea macho mashujaa walioanguka, lakini hakuna muda wa kuiacha kazi. Lazima wazibe pengo lililoachwa; wachukue bendera kutoka katika mkono uliopoozeshwa na kifo, na kwa nguvu mpya wathibitishe Ukweli na heshima ya Kristo. Kuliko ilivyokuwa hapo awali, upinzani ni lazima ufanywe dhidi ya dhambi - dhidi ya nguvu za giza. Muda unahitaji shughuli ya nguvu na yenye kudhamiria kwa wale wanaoamini Ukweli wa sasa. Ikiwa wakati unaonekana kuwa mrefu kumsubiri Mkombozi wetu aje; ikiwa, tumeinamishwa na taabu na kuchoshwa na taabu, tunajisikia papara kupokea unafuu wenye heshima kutoka katika vita, hebu

tukumbuke - na tuache ukumbusho uangalie kila manung'uniko - kwamba tumebaki duniani kukutana na dhoruba na pambano, kukamilisha tabia ya Kikristo, kumjua vizuri MUNGU  Baba yetu, na Kristo Kaka yetu mkubwa, na kufanya kazi na Bwana katika kuleta roho nyingi kwa Kristo. “Wale walio na hekima wataangaza kama mwangaza wa anga; na wale wanaowaongoza wengi kuwa waadilifu kama nyota milele na milele.” {1T 111.3}

## SURA YA 15

## MLINZI WA NDUGU YAKO

Novemba 20, 1855, wakati nilipokuwa katika maombi, Roho wa Bwana alikuja ghafla na kwa nguvu juu yangu, na nikachukuliwa mbali katika maono. {1T 113.1}

Niliona kwamba Roho wa Bwana alikuwa anaondoka taratibu kutoka kanisani. Watumishi wa Bwana wameamini sana nguvu ya hoja, na hawajamtegemea sana MUNGU  ambaye wangepaswa kuwa Naye. Niliona kwamba kubishania tu hoja  ya Ukweli isingezihamasisha roho kuchukua msimamo na waliosalia; kwani Ukweli haupendwi na wengi (siyo maarufu). Watumishi wa MUNGU  lazima wawe na Ukweli rohoni. Malaika alisema: “Lazima wapate joto kutoka kwenye utukufu, wachukue vifuani mwao, na wamimine kwa joto na bidii ya roho kwa wale wanaosikia.” Wachache ambao ni waangalifu wako tayari kuamua kutoka kwenye uzito wa ushahidi; lakini haiwezekani kuwaongoa wengi kwa nadharia tu ya Ukweli. Lazima kuwe na nguvu ya kuuwezesha Ukweli, ushuhuda ulio hai wa kuwafanya wajongee. {1T 113.2}

Niliona kwamba adui anahangaika sana na pilikapilika ya kuharibu roho. Kujiinua kumeingia miongoni mwa safu zetu; lazima kuwe na unyenyekevu mwingi zaidi. Kuna uhuru mwingi wa roho ulioingizwa kati ya wajumbe. Jambo hili lazima liwekwe kando, na watumishi wa MUNGU  ni lazima wakaribiane karibu, kuwa pamoja.  Kumekuwa na roho nyingi sana zinazouliza, “Je! Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” Malaika akasema: “Naam, wewe ni mlinzi wa ndugu yako. Wewe unapaswa kuwa na uangalifu kwa ndugu yako, uwe na hamu ya ustawi wake, na ujali roho ya fadhili na ya upendo kwake. Karibianeni pamoja, karibianeni pamoja.” MUNGU  alimuumba mwanadamu awe mwenye moyo ulio wazi na mwaminifu, bila kujifanya (usiwe mtu feki), mpole, mwenye urahisi, na asiye na makuu. Hii ndiyo kanuni ya mbinguni; MUNGU  aliamuru hivyo. Lakini maskini, mtu dhaifu ametafuta kitu tofauti – kufuata njia zake mwenyewe, na kuzingatia  katika kushugulikia ka uangalifu masilahi yake mwenyewe. {1T 113.3}

Nilimuuliza malaika kwa nini urahisi ulikuwa umefungwa nje ya kanisa, na kiburi na kujiinua vikaingia ndani. Niliona kwamba hii ndiyo sababu kwa nini tumetiwa mikononi mwa adui. Malaika akasema: "Angalia, utaona kuwa hisia hii inatawala miongoni mwa watu: Je! Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" Malaika akasema tena: "Ndiyo wewe ni mlinzi wa ndugu yako. Kukiri kwako, imani yako, inakuhitaji ujikane mwenyewe na ujitoe dhabihu kwa MUNGU, la sivyo hautastahili uzima wa milele; kwani [huo uzima wa milele] ulinunuliwa kwa ajili yako, kupitia uchungu, mateso na damu ya Mwana mpendwa wa MUNGU." {1T 114.1}

Niliona wengi katika maeneo mbalimbali, Mashariki na Magharibi, walikuwa wakiongeza shamba juu ya shamba, na ardhi juu ya ardhi, na nyumba juu ya nyumba, na kuifanya kazi ya MUNGU kuwa sababu ya udhuru wao, wakidai wanafanya hivyo ili wasaidie kazi ya MUNGU. Wanajifunga minyororo wenyewe kwa nguvu ili waweze kuwa na faida kidogo kwa kazi hiyo. Wengine hununua kipande cha ardhi, na wanafanya kazi kwa nguvu zao zote kukilipia. Wakati wao mwingi unachukuliwa na shughuli hizo na wanapata wakati mdogo wa kuomba, na kumtumikia MUNGU, na kupata nguvu kutoka kwake kushinda mateso yao. Wana madeni, na wakati kazi inapohitaji msaada wao wanakuwa hawawezi kusaidia; kwani lazima walipe madeni kwanza na kuwa huru. Lakini mara tu wanapokuwa huru kutoka kwenye madeni hujiweka mbali zaidi katika kusaidia kazi kuliko ilivyokuwa hapo awali; kwa kuanza tena kujihusisha na kuongeza mali zao. Wanajifariji na kujidanganya wenyewe kwamba jambo hilo lipo sawa, na kwamba watatumia faida [watakayoipata] katika kusaidia kazi, wakati wanaweka hazina zao hapa duniani. Wanapenda Ukweli kwa maneno, lakini siyo kwa vitendo. Wanapenda kazi ya Mungu tu kama vile ambavyo kazi zao zenyewe zinavyoonesha kwa macho. Wanaupenda ulimwengu zaidi na kazi ya MUNGU kidogo; kivutio cha dunia kinakuwa na nguvu na mvuto wa mbinguni unakuwa dhaifu. Moyo wao uko pamoja na hazina yao. Kwa mfano wanaouonesha ni kama wanawaambia wale walio karibu nao kuwa wanakusudia kukaa hapa duniani, kwamba ulimwengu huu ulimwengu ndiyo nyumba yao. Malaika akasema: "Wewe ni mlinzi wa ndugu yako." {1T 114.2}

Wengi wamejiendekeza kwenye gharama isiyo ya lazima, ili tu kuridhisha hisia, tamaa, na macho, wakati kazi ilihitaji mali hizo hizo zilizotumika katika mambo hayo, na wakati baadhi ya watumishi wa MUNGU wakiwa wamevaa vibaya na wakiwa vilema katika utumishi wao kwa kukosa mali. Malaika alisema: "Wakati wao wa kufanya hivi upo karibu kwisha. Kazi zao zinaonesha kuwa ubinafsi ni sanamu yao, na wanatoa kafara kwa hizo sanamu." Ubinafsi ni lazima kwanza uridhishwe; hisia zao ni: "Je! mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" Wengi wamepokea onyo baada ya onyo, lakini hawakutii maonyo. Ubinafsi (mimi) ndiyo lengo kuu, na kila kitu kinapaswa kuinamia [kwenye huo ubinafsi]. {1T 115.1}

Niliona kwamba kanisa lilikuwa limekaribia kupoteza roho ya kujikana na kujitolea; wanafanya nafsi na kujipenda nafsi kuwa jambo la kwanza, na kisha katika kazi ya MUNGU hufanya kile wanachofikiria kuwa wanaweza au la. Niliona dhabihu kama hiyo, ni kilema, na haikubaliki kwa MUNGU. Wote wanapaswa kuwa na shauku ya kufanya kwa bidii na uwezo wao wote ili kuendeleza jambo hilo. Niliona kwamba wale ambao hawana mali, bali wana nguvu ya mwili, wanawajibika kwa MUNGU kwa nguvu zao. Wanapaswa kuwa na uadilifu katika shughuli na wenye bidii katika roho; hawapaswi kuwaacha wale ambao wana mali zao wafanye dhabihu zote. Niliona kwamba wanaweza kujitolea dhabihu, na kwamba ni wajibu wao kufanya hivyo, na hilo lapaswa kufanywa pia na wale ambao wana mali. Lakini mara nyingi wale ambao hawana mali hawatambui kuwa wanaweza kujikana wenyewe nafsi zao kwa njia nyingi, wanaweza kuhangaikia kidogo sana miili yao (kujipamba, kuvaa, kula), wakijizuia kuridhisha ladha na hamu zao, na kubakiwa na mali ya kutosha kwa ajili ya kazi, na hivyo kuweka hazina mbinguni. Niliona kwamba kuna upendo na uzuri katika Ukweli; lakini [hebu jaribu] ukiondoa nguvu ya MUNGU, nao utakuwa hauna nguvu. {1T 115.2}

## SURA YA 16

## MUDA WA KUANZA SABATO

Niliona kuwa ni hivyo hivyo: “Tangu jioni hata jioni, mtaishika Sabato yenu.” Malaika alisema: “Chukua Neno la MUNGU, lisome, lielewe, na wewe hautakosea. Soma kwa uangalifu, na hapo utagundua ni kipi kilichopo, na kipo kwa wakati gani (Hesabu 23:32). Nikamuuliza malaika ikiwa mkunjo wa uso wa MUNGU umekuwa juu ya watu Wake kuhusiana na namna Sabato ilivyokuwa inaanza na kuwafuatilia watu wa MUNGU walivyokuwa wanafanya. Nilielekezwa kurejea kwenye namna Sabato ilivyoanza, na kufuatilia watu wa MUNGU hadi wakati huu, lakini sikuona kwamba Bwana hakufurahishwa nao, au aliwakunjia uso. Nikauliza imekuwaje wakati huu tukiwa tumechelewa tunabadilisha wakati wa kufungua Sabato kwanini ilikuwa hivi, kwamba katika siku hii ya mwisho lazima tubadilishe wakati wa kuanza Sabato. Malaika alisema: “Utaelewa, lakini bado, bado.”

Malaika akasema: “Ikiwa nuru inakuja, na nuru hiyo imewekwa kando au kukataliwa, hapo ndipo huja hukumu na uso wa MUNGU uliokunjamana; lakini kabla nuru haijaja, hakuna dhambi, kwa maana hakuna nuru ya watu kuikataa. “Niliona ilikuwa katika mawazo ya wengine kwamba Bwana alikuwa ameonesha kuwa Sabato ilianza saa sita, wakati nilikuwa nimeona tu kwamba ilianza majira ya “jioni”, na hata ikadhaniwa kuwa ilikuwa saa kumi na mbili. Nikaona kwamba watumishi wa MUNGU lazima waje pamoja, wajikusanye pamoja. Njooni pamoja, Njooni pamoja.{1T 116.1}

# TIME TO COMMENCE THE SABBATH – James White

IT is generally known to most of the readers of the Review that for several years in the early history of Seventh-day Adventists, believers adopted six o'clock P. M. as the time for the Sabbath to commence and close. It is also known that in the autumn of 1855, the Review taught that sunset was the Bible time to commence the Sabbath, and that our people generally changed from six o'clock to sunset. Some of the circumstances connected with this change I wish here to state:

1. The six o'clock time was called in question by a portion of believers as early as 1847, some maintaining that the Sabbath commenced at sun-rise, while others claimed Bible evidence in favor of sunset.

2. Eld. Joseph Bates, who was the first to teach the Sabbath in its importance, and faithfully labor to bring out a people from among the Adventists to observe it, was very decided upon the six o'clock time. His decided stand upon the question, and respect for his years, and his godly life, might have been among the reasons why this point was not sooner investigated as thoroughly as some other points.

3. In the autumn of 1855 Eld. J. N. Andrews called on me at Battle Creek, on his way to Iowa, and set before me the scriptural reasons for commencing the Sabbath at sunset. He had written a clear article upon the subject which he left with me, and which appeared in the Review for Dec. 4, 1855. This article, however, before it appeared in the Review was read at the Conference at Battle Creek about that time, and the subject was discussed resulting in settling the minds of the : brethren on the sunset-time, with the exception of Bro. Bates, and a few others. Since that time there has been general agreement among us upon the subject.

But there are persons who seek to injure us as a people– and this class we hope to help by this article— who "report and publish to the world that Mrs. White did profess to be shown that the time to commence the Sabbath, was six o'clock, and that at a later period she was shown that sunset was the true time. It is also stated that in vision she saw the dial-plate of a clock with one hand pointing to vi, the other to xii, showing that six o'clock was the commencement and close of the Sabbath.

A simple statement of the facts in the case are sufficient to show these reports false. Hence, we give the following statements which we are ready to prove by most competent witnesses.

1. Mrs. W. has in two visions been shown something in regard to the time of the commencement of the Sabbath. The first was as early as 1847, at Topsham, Me. In that vision she was shown that to commence the Sabbath at sunrise was wrong. She then heard an angel repeat these words, "From

even unto even shall ye celebrate your Sabbaths." Bro. Bates was present, and succeeded in satisfying all present that "even" was six o'clock. Mark this: The vision at Topsham did not teach the six o'clock time. It only corrected sunrise time. I never received the idea that the six o'clock time was sustained by the visions, hence the following which I copy from a statement I made in the Review upon this subject, Dec. 4, 1855, as follows:

"We have, never been fully satisfied with the testimony presented in favor of six o'clock, while the various communications received for a few years past advocating both sunrise and sunset time, have been almost destitute of argument, and the spirit of humility and candor. The subject has troubled us, yet we have never found time to thoroughly investigate it.
" In June, 1854 we urged Eld. D. P. Hall to prepare an article on the subject for the Review. When with him in Penn. last winter we repeated the request. When in Maine last summer we stated our feelings on this subject to Bro. Andrews, and have fears of division unless the question could be settled by good testimony. He decided to devote his time to the subject till he ascertained what the Bible taught in regard to it, and his article in this number is the result of his investigation. Some have the impression that six o'clock time has been taught among us by the direct manifestation of the Holy Spirit. This is a mistake, 'From even unto even' was the teaching for which six o'clock time has been inferred."

2. In regard to the clock face, twenty competent witnesses are ready to testify that neither Mrs. W. nor her visions had anything to do with it whatever. When at Rocky Hill, Conn., in 1849, at a meeting on the Sabbath at the house of Bro. Albert Belden, the time to commence the Sabbath was agitated. A brother present in whose spiritual exercises there was great confidence, seemed to be very powerfully exercised, and, amid groans and tears, he called for the chalk, and marked out upon the floor the figure of a clock face, the hands pointing out six o'clock. A general impression prevailed that this was the work of the Spirit of God; but Mrs. W. had nothing to do with it whatever.

3. At the close of the conference at Battle Creek referred to above, the ministers and others, especially interested in the cause had a special season of prayer for the prosperity of the cause, and in that meeting Mrs. W. had a vision, one item of which was that sunset time was correct. This settled the matter with Bro. Bates and others, and general harmony has since prevailed among us upon this point.

But the question naturally arises, If the visions are given to correct the erring, why did she not sooner see the error of the six o'clock time? For one I have ever been thankful that God corrected the error in his own good time, and did not suffer an unhappy division to "exist among us upon the point. But, dear reader, the work of the Lord upon this point is in perfect harmony

with his manifestations to us on others, and in harmony with the correct position upon spiritual gifts.

It does not appear to be the desire of the Lord to teach his people by the gifts of the Spirit on the Bible questions until his servants have diligently searched his word. When this was done upon the subject of time to commence the Sabbath, and most were established, and some were in danger of being out of harmony with the body on this subject, then, yes, then, was the very time for God to magnify his goodness in the manifestation of the gift of his Spirit in the accomplishment of its proper work.

The sacred Scriptures are given us as the rule of faith and duty, and we are commanded to search them. If we fail to understand and fully obey the truths in consequence of not searching the Scriptures as we should, or a want of consecration' and spiritual discernment, and God in mercy in his own time corrects us by some manifestation of the gifts of his Holy Spirit, instead of murmuring that he did not do it before, let us humbly acknowledge his mercy, and praise him for his infinite goodness in condescending to correct us at all.

Let the gifts have their proper place in the church. God has never set them in the very front, and commanded us to look to them to lead us in the path of truth, and the way to Heaven. His word he has magnified. The Scriptures of the Old and New Testament are man's lamp to light up his path to the kingdom. Follow that. But if you err from Bible truth, and are in danger of being lost, it may be that God will in the time of his choice correct you, and bring you back to the Bible, and save you. And would it become you in such a case to murmur and say, "Lord, why didst thou not do this before?" Take care! "Be still, and know that I am God." Our necessity is his opportunity to teach us by the gifts of his Holy Spirit.

JAMES WHITE

The Review and Herald, February 25, 1868, Vol. 31, No. 11, page 168

## SURA YA 17

## WAPINZANI WA UKWELI

Nilioneshwa kesi ya Stephenson na Hall wa Wisconsin. Niliona kwamba tulipokuwa Wisconsin, mnamo Juni, 1854, watu hawa walishawishika kuwa

maono hayo yalikuwa ya MUNGU ; lakini walipoyachunguza na kuyalinganisha na mitazamo yao juu ya wakati ujao, na kwa kuwa maono hayakukubaliana na mtazamo wao, waliyatoa kafara maono hayo kwa fundisho la milenia ya Yesu duniani. Na wakati wako kwenye safari yao huko Mashariki, majira ya kuchipua mimea yaliyopita, wote wawili walikuwa katika makosa na nia. Wamejikwaa juu ya fundisho hilo na wapo tayari kuchukua msimamo wowote kulidhuru gazeti la *Review*; rafiki zake lazima wawe macho na kufanya kila wawezacho kuwaokoa watoto wa MUNGU kutoka kwenye udanganyifu. Watu hawa wanaungana na watu waongo na mafisadi. Wangepaswa kuwa na ushahidi juu ya jambo hili. Na walipokuwa wakidai huruma na umoja na mume wangu, wao (hasa Stephenson) walikuwa wakiuma kama nyoka nyuma yake. Wakati maneno yao yakiwa laini kwake, walikuwa wakiiwasha Wisconsin dhidi ya *Review* na waendeshaji wake. Hasa Stephenson alikuwa mstari wa mbele katika suala hili. Lengo lao lilikuwa kufanya uchapishaji wa *Review* kuwa nadharia ya milenia na Yesu duniani, au kuharibu ushawishi wake. Na wakati mume wangu akiwa na moyo mkunjufu, ulio wazi na asiye na shaka, akitafuta njia za kuondoa wivu wao, na kuwafungulia bila kificho mambo ya ofisi, na kujaribu kuwasaidia, walikuwa wakitazama mambo kwa jicho ovu, lenye wivu, na wakitazama kila kitu kwa jicho la wivu. Malaika alisema nilipokuwa nikiwatazama: “Unadhani wewe, mtu dhaifu, kwamba unaweza kuizuia kazi ya MUNGU ? Mtu dhaifu, mguso mmoja tu wa kidole CHAKE chaweza kukuangusha chini. Atakuacha na kukuvumilia wewe kwa kitambo kidogo tu.” {1T 116.2}

Nilielekezwa nyuma wakati wa kuanzishwa kwa mafundisho ya ujio wa Kristo, na hata kabla ya wakati huo, na kuona kwamba hakukuwa na ulinganifu wa udanganyifu, upotoshaji, na uongo ambao umekuwa ukifanywa na *chama cha Mjumbe-Messenger Party*, au chama kama hicho cha mafisadi, chini ya kichaka cha vazi la dini. Mioyo minyofu mingine imeathiriwa nao, na kuhitimisha kuwa lazima angalau wawe na sababu kuwa watu kama hao watakuwa na ushahidi wa Ukweli wa mambo haya. Kanisa la MUNGU  linapaswa kusonga mbele moja kwa moja, kana kwamba hakukuwa na watu kama hawa ulimwenguni. {1T 117.1}

Niliona kwamba juhudi za makusudi zinapaswa kufanywa kuwaonesha makosa yao, wale wasio Wakristo, na ikiwa hawatabadilika, na kufanya matengenezo, basi wanapaswa kutengwa na watakatifu wenye thamani, ili MUNGU  apate kuwa na watu safi, waliotakasika anaoweza kuwafurahia. Mheshimuni kwa kutochanganya kuwajumuisha walio safi na wasio safi-najisi na wasafi. {1T 117.2}

Nilioneshwa wengine wakitokea Mashariki kuja Magharibi. Niliona kwamba lengo la wale wanaoondoka Mashariki kwenda Magharibi halipaswi kuwa la kupata utajiri, bali kuzileta roho katika Ikweli. Malaika alisema: "Acha kazi zako zioneshe kuwa siyo kwa sababu ya heshima, au kuweka hazina duniani, kwamba umehamia Magharibi, bali kushikilia na kuinua kiwango cha Ukweli.” Niliona kwamba wale wanaohamia Magharibi wanapaswa kuwa kama watu

wanaomngojea Bwana wao. Malaika alisema: “Kuwa mfano hai kwa wale wa Magharibi. Hebu kazi zenu zioneshe kuwa ninyi ni watu wa MUNGU wa kipekee, na kwamba mna kazi maalum, kutoa ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu. Hebu kazi zenu ziwaoneshe wale wanaowazunguka kwamba ulimwengu huu siyo nyumbani kwenu. Niliona kuwa wale ambao wamejiingiza na kujifungafunga kama wenyewe wanapaswa kuvunja mtego wa adui na kuwa huru. Msiweke hazina duniani, bali muoneshe kwa maisha yenu kwamba mnajiwekea hazina mbinguni. Ikiwa MUNGU amewaita Magharibi, basi Yeye anayo kazi, kazi iliyotukuka, mnayopaswa kuifanya. Hebu imani yenu na uzoefu wenu viwasaidie wale ambao hawana uzoefu hai. Msivutwe na dunia hii dhaifu, masikini iliyo na ukubwa nukta ndogo tu kwenye ramani ya malimwengu yote, bali mvuto wenu uwe juu kwa MUNGU, utukufu, na mbingu. Msiruhusu masumbufu na mahangaiko ya mashamba hapa yazonge akili zenu, bali mruhusu kushughulishwa katika kutafakari shamba la Ibrahimu. Sisi ni warithi wa urithi huo wa milele. Ondoeni mapenzi yenu kutoka duniani, na zungumzieni sana juu ya mambo ya mbinguni. {1T 118.1}

## SURA YA 18

## WAJIBU WA WAZAZI

Niliona jukumu kubwa liko juu ya wazazi. Hawapaswi kuongozwa na watoto wao, bali lazima wawaongoze. Nilielekezwa kwa Ibrahimu. Alikuwa mwaminifu katika nyumba yake. Aliwaamuru watu wa nyumbani mwake baada yake, na hilo likakumbukwa na MUNGU (Mwanzo 18). {1T 118.2}

Kisha nilielekezwa kwenye kesi ya Eli. Hakuwadhibiti watoto wake, na wakawa waovu, wabaya na watukutu, na kwa uovu wao waliipotosha Israeli (1Sam 2). Wakati MUNGU akimjulisha Samweli dhambi zao, na laana nzito iliyokuwa

iwafuate kwa kuwa Eli hakuwazuia, alisema dhambi zao hazikupaswa kusafishwa kwa dhabihu wala sadaka milele. Alipoambiwa na Samweli kile Bwana alichomwonesha, Eli alinyenyekea, akasema: "Ndiye Bwana; na afanye aonaloona kuwa ni jema." Laana ya MUNGU ilifuata punde. Makuhani hao waovu waliuawa, na Waisraeli elfu thelathini pia waliuawa, na Sanduku la Agano la MUNGU lilitwaliwa na maadui zao. Eli aliposikia kwamba sanduku la MUNGU limetwaliwa, alidondoka kwa kichalichali na akafa. Uovu huu wote ulitokana na upuuziaji wa Eli kuwazuia wanawe. Niliona kwamba ikiwa MUNGU alikuwa mwangalifu/makini hivi kiasi cha kugundua mambo kama haya zamani, hawezi kupunguza umakini katika siku hizi za mwisho. {1T 119.1}

Wazazi lazima wawatawale watoto wao, warekebishe tamaa zao, na kuwatiisha, la sivyo MUNGU atawaangamiza watoto katika siku ya hasira Yake kali, na wazazi ambao hawajawadhibiti watoto wao hawatakosa kuwa na hatia. Watumishi wa MUNGU wanapaswa kutawala familia zao wenyewe na kuzitiisha vizuri kuliko wengine. Niliona kuwa hawatakuwa tayari kuhukumu au kuamua katika masuala ya kanisa, isipokuwa wataweza kutawala vizuri nyumba zao wenyewe. Lazima kwanza wawe na utaratibu nyumbani, na ndipo maamuzi na ushawishi wao vitakuwa na nguvu kanisani. {1T 119.2}

Niliona kwamba sababu inayofanya maono yasiwe yanatokea mara kwa mara hata leo ni kwa kuwa hayakuthaminiwa na kanisa. Kanisa lipo karibu na kupoteza hali yake ya kiroho na imani, na makemeo na maonyo vimekuwa na athari kidogo kwao. Wengi wa wale ambao wamekiri imani katika maono hawajayazingatia. {1T 119.3}

Wengine wamechukua mwenendo usiofaa; wanapokuwa wameizungumza imani yao na wasioamini, na uthibitisho unapotakiwa, wamesoma maono, badala ya kwenda kwenye Biblia kupata uthibitisho. Niliona kuwa njia hii haikubaliani, na iliwachukiza wasioamini dhidi ya Ukweli. Maono hayawezi kuwa na uzito na wale ambao hawajawahi kuyaona na hawajui chochote juu ya roho zao. Hayapaswi kutajwa katika kesi kama hizo. {1T 119.4}

## SURA YA 19

## IMANI KATIKA MUNGU

Nilipokuwa Battle Creek, Michigan, Mei 5, 1855, niliona kwamba kulikuwa na ukosefu mkubwa wa imani kwa watumishi wa MUNGU, na pia kwa kanisa. Walikuwa wanakata tamaa kirahisi sana, walikuwa tayari kumtilia MUNGU mashaka, walikuwa tayari kuamini kwamba walikuwa na shida nyingi na kwamba MUNGU alikuwa amewaacha. Niliona kuwa huu ulikuwa ukatili. MUNGU aliwapenda sana hata kumtoa Mwanawe mpendwa afe kwa ajili yao, na

mbingu zote zilipendezwa na wokovu wao; lakini baada ya yote hayo waliyofanyika, ilikuwa ngumu kwao kumwamini na kumtumaini Baba Mwenye fadhili na mwema. Amesema kuwa yuko tayari kuwapa ROHO MTAKATIFU wale wanaomwomba, kuliko vile wazazi wa hapa duniani wawezavyo kuwapa zawadi nzuri watoto wao. Niliona kwamba watumishi wa MUNGU na kanisa walikuwa wamevunjika moyo kwa urahisi sana. Walipomwomba Baba yao wa mbinguni vitu ambavyo walidhani wanavihitaji, na havikuja mara moja, imani yao iliyumba, ujasiri wao ukatoweka, na hisia za kunung'unika zikawamiliki. Hili, niliona, halikumpendeza MUNGU. {1T 120.1}

Kila mtakatifu ajaye kwa MUNGU kwa moyo wa kweli, na kutuma maombi yake ya kweli kwake kwa imani, atajibiwa maombi yake. Imani yako haipaswi kuachilia ahadi za MUNGU, ikiwa hautaona au kuhisi jibu la haraka la maombi yako. Usiogope kumtumaini MUNGU. Tegemea ahadi Yake ya hakika: “Ombeni, nanyi mtapokea.” MUNGU ni mwenye hekima mno kiasi kwamba hawezi kukosea, na ni mwema sana kiasi kwamba hawezi kuwanyima kitu chochote kizuri watakatifu Wake wanaotembea kwa unyofu. Mwanadamu hukosea, na ingawa maombi yake yanakuwa yametumwa kutoka kwenye moyo mkweli, yeye huwa haombi kila wakati vitu ambavyo ni vyema kwake, au ambavyo vitamtukuza MUNGU. Jambo hili linapokuwa hivyo, Baba yetu mwema na mwenye hekima husikia maombi yetu, na kuyajibu, wakati mwingine mara moja; lakini Yeye hutupatia vitu ambavyo ni kwa faida yetu na utukufu Wake Mwenyewe. MUNGU hutupatia baraka; kama tungeangalia mpango Wake, tungeona wazi kwamba anajua kilicho bora kwetu na kwamba maombi yetu yanajibiwa. Hakuna chochote cha kuumiza kinachotolewa, isipokuwa ule mbaraka tunaouhitaji, badala ya kile kitu tulichoomba ambacho hakitakuwa kizuri kwetu, bali kwa maumivu yetu. {1T 120.2}

Niliona kwamba ikiwa hatuhisi majibu ya haraka mara moja kwa sala zetu, tunapaswa kushikilia imani yetu, bila kuruhusu hali ya kutokuamini iingie, kwani hiyo itatutenganisha na MUNGU. Imani yetu ikitetereka, hatutapokea chochote kutoka Kwake. Ujasiri na imani yetu kwa MUNGU inapaswa kuwa na nguvu; na wakati tunapoihitaji sana, baraka itatuangukia kama manyunyu ya mvua. {1T 121.1}

Wakati watumishi wa MUNGU wanapoomba kwa ajili ya Roho wake na baraka zake, mara nyingine huja mara moja; lakini haiwi hivyo kila wakati. Kwa nyakati kama hizo, usizimie. Hebu imani yako ishikilie ahadi kwamba itakuja. Hebu imani yako iwe kwa MUNGU kikamilifu, na mara nyingi baraka hiyo itakuja wakati unaoihitaji sana, na bila kutarajia utapokea msaada kutoka kwa MUNGU wakati unapouwasilisha Ukweli kwa wasioamini, na utawezeshwa kusema Neno kwa uwazi na nguvu. {1T 121.2}

Iliwakilishwa kwangu kama ilivyo kwa watoto wanaoomba baraka kwa wazazi wao wa kidunia ambao wanawapenda. Wanawaomba wazazo kitu ambacho

mzazi anajua kitawaumiza; mzazi huwapa vitu ambavyo vitakuwa vyema na vyenye afya kwao, badala ya vile walivyotamani. Niliona kwamba kila ombi linaloombwa kwa imani kutoka kwenye moyo mnyofu litasikiwa na MUNGU na kujibiwa, na yule aliyetuma ombi atapata baraka wakati anapoihitaji zaidi, na mara nyingi itazidi matarajio yake. Hakuna sala ya mtakatifu yoyote wa kweli iliyopotea ikiwa imetumwa kwa imani kutoka kwenye moyo mkweli. {1T 121.3}

## SURA YA 20

## CHAMA CHA "MJUMBE"

Nilipokuwa Oswego, New York, Juni, 1855, nilioneshwa kwamba watu wa MUNGU wamelemewa na viatu vizito vinavyowazuia kutenda; kwamba kumekuwa na Akani kambini. Kazi ya MUNGU imeendelea lakini kidogo, na watumishi Wake wengi wamevunjika moyo kwa sababu Ukweli haujachukua athari yoyote huko New York, na hakuna kanisa ambalo limeongezwa idadi ya watu huko tena. Chama cha Mjumbe kimetokea, na baadhi tutateseka kutoka katika ndimi zao za uongo na ulaghai, lakini tunapaswa kuvumilia yote kwa saburi; kwani hawataijeruhi kazi ya MUNGU, wakati sasa wametuacha, kama ambavyo wangeendelea kubaki na sisi kwani ndivyo ambavyo ushawishi wao ungebaki pamoja nasi. {1T 122.1}

Uso wa MUNGU uliokunjamana umekuja juu ya kanisa kwa sababu ya watu walio na mioyo mibaya ndani ya kanisa. Walitaka kuwa wa kwanza, wakati hawakuwekwa hapo na MUNGU wala ndugu zao. Ubinafsi na kujiinua vimeashiria mwenendo wao. Nafasi sasa iko wazi kwa wote ambao wanaweza kwenda na kupata malisho pamoja na wale wa aina yao. Na tunapaswa kumsifu MUNGU kwamba kwa rehema Yeye amewaondoa kanisani. MUNGU amewapatia wengi wa watu hawa njia zao ili wajazwe na matendo yao wenyewe. Misisimko na huruma sasa inawaongoza, ambayo itawadanganya wengine; lakini kila mtu mkweli ataangazwa juu ya hali halisi ya kundi hili, na atabaki na watu wa pekee wa MUNGU, ataishikilia kweli, na kufuata njia ya unyenyekevu, bila kuathiriwa na ushawishi wa wale ambao wameachwa na MUNGU katika njia zao wenyewe, wakijazwa na matendo yao wenyewe. Niliona kwamba MUNGU alikuwa amewapatia watu hawa nafasi ya kufanya matengenezo, alikuwa amewaangazia upendo wao kwa wao na dhambi zao zingine; lakini hawakuzingatia. Wasingerekebishwa au kufanya matengenezo, na kwa rehema MUNGU alilisaidia kanisa dhidi yao. Ukweli utaanza kuwa na matokeo ikiwa watumishi wa MUNGU na kanisa watajitoa Kwake na kwa kazi Yake. {1T 122.2}

Niliona kwamba watu wa MUNGU lazima waamke na kuvaa silaha za Bwana. Kristo anakuja, na kazi kuu ya ujumbe wa mwisho wa rehema ni ya muhimu sana kwetu kiasi cha kutoweza kuiacha na kuja chini kujibu uongo kama huo, upotoshaji, kutuwakilisha vibaya na kashfa kwa kuwa chama cha Mjumbe kimewalisha watu uongo kilishakula na kuutawanya mpaka ng'ambo. Ukweli, Ukweli wa sasa, lazima tutulie juu yake. Sisi tunafanya kazi kubwa, na hatuwezi kushuka-Nehemia 6:3. Shetani yuko juu ya haya yote, ili kupotosha mawazo yetu kutoka kwenye Ukweli wa sasa na ujio wa Kristo. Malaika alisema: "Yesu anajua yote." Muda si mrefu siku yao inakuja. Wote watahukumiwa kulingana na matendo yaliyofanywa mwilini. Ulimi wa uongo utakomeshwa. Wenye dhambi katika Sayuni wataogopa, na hofu itawashangaza wanafiki.{1T 123.1}

# SURA YA 21

# JITAYARISHE KUKUTANA NA BWANA

Niliona kwamba hatupaswi kuahirisha kuja kwa Bwana. Malaika alisema: "Jitayarishe, jiandae, kwa kile kinachoijia dunia. Hebu kazi zako ziendane na imani yako." Niliona kwamba akili lazima itulie kwa MUNGU, na kwamba ushawishi wetu unapaswa kuzungumza na kumtetea MUNGU na Ukweli Wake. Hatuwezi kumheshimu Bwana wakati sisi ni wazembe na wasiojali. Hatuwezi kumtukuza wakati tunakata tamaa. Lazima tuwe wenye bidii kupata wokovu wa

nafsi zetu, na kuwaokoa wengine. Umuhimu wote unapaswa kushikamana na hili, na kila kitu kando ya hilo kinapaswa kuwa cha pili. {1T 123.2}

Niliona uzuri wa mbinguni. Nikasikia malaika wakirindima nyimbo zao za kupendeza, wakitoa sifa, heshima, na utukufu kwa Yesu. Niliweza kugundua kitu cha upendo wa ajabu wa Mwana wa MUNGU. Aliacha utukufu wote, heshima yote aliyokuwa nayo mbinguni, na alikuwa na shauku kubwa ya wokovu wetu kiasi kwamba kwa uvumilivu, unyenyekevu na upole alichukua kila aibu na udhaifu ambao mwanadamu angeweza kuuweka juu yake. Alijeruhiwa, akapigwa, na kuumizwa; Alinyooshwa juu ya msalaba wa Kalvari na kuvumilia mauti inayoumiza kwa uchungu zaidi ili kutuokoa kutoka katika kifo, kusudi tuweze kuoshwa katika damu yake na kufufuliwa kuishi Naye katika makao anayotutayarishia, kufurahia nuru na utukufu wa mbinguni, kuwasikia malaika wakiimba, na kuimba pamoja nao. {1T 123.3}

Niliona kwamba mbingu zote zinavutiwa na kupendezwa na wokovu wetu; je, sisi tuwe watu wasiojali? Je! Tutakuwa wazembe, kana kwamba ni jambo dogo ikiwa tunaokoka au tunapotea? Je! Tutapuuza dhabihu ambayo imetolewa kwa ajili yetu? Wengine wamefanya hivi. Wamecheza-cheza rehema iliyotolewa, na uso wa MUNGU uko juu yao. ROHO WA MUNGU hatahuzunika kila wakati. Ataondoka baada ya kuhuzunishwa kwa muda mrefu kidogo. Baada ya MUNGU kufanya yote ambayo angefanya ili kuwaokoa wanadamu, ikiwa wataonesha kwa maisha yao kwamba wanaidharau rehema ya Yesu, kifo kitakuwa sehemu yao, nacho kitanunuliwa kwa gharama kubwa sana. Kitakuwa kifo cha kutisha; kwani watalazimika kuhisi uchungu ambao Kristo aliuhisi msalabani kuwanunulia ukombozi ambao wameukataa. Na hapo ndipo watatambua kile walichopoteza - uzima wa milele na urithi wa milele wa kutokufa. Dhabihu kubwa ambayo imefanywa kuokoa roho inatuonesha thamani yao. Wakati nafsi ya thamani inapopotea mara moja, imepotea milele. {1T 124.1}

Nimeona malaika amesimama na mizani mikononi mwake akipima mawazo na shauku za watu wa MUNGU, haswa vijana. Katika upande mmoja mawazo na shauku na maslahi ya watu vilikuwa vikielekea mbinguni; kwa upande mwingine mawazo na mivuto yao ilielekea duniani. Na katika upande huu kulikuwa na usomaji wote wa vitabu vya hadithi (story books), mawazo ya mavazi na maonesho, ubatili, kiburi, n.k. Ah, ni wakati wa huzuni nzito kiasi gani! Malaika wa MUNGU wamesimama na mizani, wakipima mawazo ya watoto Wake wanaodai kumwamini - wale wanaodai kuufia ulimwengu na kuishi kwa ajili ya MUNGU. Mizani iliyojazwa na mawazo ya dunia, ubatili, na kiburi ilishuka haraka kwenda chini, bila kujali uzito baada ya uzito uliokuwepo kwenye mzani. Wale waliokuwa na mawazo na mivuto ya kuelekea mbinguni walikwenda juu haraka wakati wale wengine wakishuka, na oh, ilikuwa nyepesi kiasi gani! Ninaweza kulielezea hili kama nilivyoliona; lakini kamwe siwezi kutoa maoni mazito na ya wazi kama yaliyowekwa kwenye akili yangu, kama nilivyoona malaika akiwa na mizani akipima mawazo na mivuto ya watu wa

MUNGU. Malaika alisema: "Je! Watu kama hao wanaweza kuingia mbinguni? Hapana, hapana, kamwe. Waambie matumaini waliyonayo sasa ni ya bure, na wasipotubu haraka, na kupata wokovu, lazima waangamie." {1T 124.2}

Mwonekano wa utauwa hautamuokoa yeyote. Wote lazima wawe na uzoefu wa kina ulio hai. Hili pekee ndilo litakalowaokoa watu wakati wa taabu. Ndipo kazi yao itajaribiwa kuwa ni ya aina gani; na ikiwa ni dhahabu, fedha, na vito vya thamani, vitafichwa katika faragha ndani ya banda la Bwana. Lakini kama matendo yao ni kuni, nyasi, na mabua, hakuna kitu kinachoweza kuwalinda na hasira kali ya Yehova. {1T 125.1}

Vijana, pamoja na wale ambao ni wazee, watahitajika kutoa sababu ya matumaini yao. Lakini akili, iliyoumbwa na MUNGU kwa vitu bora zaidi, iliyoundwa ili kumtumikia Yeye kikamilifu, imekaa juu ya vitu vya kipumbavu, badala ya masilahi ya milele. Hata ile akili ambayo imebaki kumangamanga hapa na pale, bado ina uwezo wa kuelewa Ukweli, ushahidi kutoka kwa Neno la MUNGU kwa kushika Sabato, na msingi wa Kweli wa tumaini la Mkristo, juu ya kujifunza mwonekano, mwenendo, adabu, mavazi, n.k. Na wale ambao huacha mawazo ya kugeuzwa na hekayaza kipumbavu na hadithi zisizo na maana*, wanazilisha fikra zao na vitu vingine, lakini uzuri wa Neno la MUNGU umefunikwa kwao. Akili inaongozwa moja kwa moja kwa kupindishwa mbali na MUNGU. Hamu ya Neno Lake la thamani imeharibiwa (video na novels, ponografia, na tamthiliya zingine za kufikirika, hadithi za mapenzi, vita, katuni nk vinapoteza muda ambao mtu angefanya yale ya milele). {1T 125.2}

Tumepewa kitabu ili kiweze kuongoza miguu yetu kupitia hatari za ulimwengu huu wa giza kwenda mbinguni. Kinatuambia jinsi tunavyoweza kuiepuka hasira ya MUNGU, na pia kinatuambia juu ya mateso ya Kristo kwa ajili yetu, dhabihu kubwa ambayo imetolewa ili tuweze kuokolewa na kufurahia uwepo wa MUNGU milele. Na ikiwa yeyote atakosa mwishowe, baada ya kuusikia Ukweli kama ulivyo katika nchi hii ya nuru, litakuwa kosa lao wenyewe; hawatakuwa na udhuru. Neno la MUNGU linatuambia jinsi tunavyoweza kuwa Wakristo wakamilifu na kuepuka mapigo saba ya mwisho. Lakini hawakuwa na hamu kulielewa hili. Vitu vingine viligeuza akili, waliziendekeza sanamu, na Neno Takatifu la MUNGU lilipuuzwa na kudharauliwa. MUNGU amechezewa, na kudharauliwa na wale wanaodai kuwa Wakristo, na wakati Neno Lake Takatifu litakapowahukumu katika siku ya mwisho, wataonekana wamepungua. Neno lile ambalo wamelidharau kwa sababu ya vitabu vya hekaya za kijinga, linayajaribu maisha yao. Hicho ndicho kiwango; nia zao, maneno, matendo, mwenendo na jinsi wanavyotumia muda wao, yote yanalinganishwa na Neno la MUNGU lililoandikwa; na ikiwa watapunguka hapo, basi kesi zao zinaamuliwa milele. {1T 125.3}

Niliona kwamba wengi hujipima miongoni mwao wenyewe, na kuyalinganisha maisha yao na maisha ya wengine. Hii haipaswi kuwa hivi. Hakuna mtu ila Kristo ambaye tumepewa kama mfano. Yeye Ndiye Kielelezo chetu cha Kweli, na kila mmoja anapaswa kujitahidi kufaulu katika kumwiga Yeye. Sisi ni watenda-kazi pamoja na Kristo, au watendakazi wenza na adui. Tunakusanya pamoja na Kristo au tunatawanya mbali. Sisi ni wakristo wa moyo wote, au la. Kristo anasema: "Laiti ungekuwa baridi au moto. Kwa hivyo kwa sababu wewe ni vuguvugu, na si baridi wala moto, nitakutapika utoke kinywani Mwangu." {1T 126.1}

Niliona kwamba wengine bado hawajui maana ya kujinyima, kujikana nafsi au kujitoa kikamilifu, au nini maana ya kuteseka kwa ajili ya Ukweli. Lakini hakuna atakayeingia mbinguni bila kutoa dhabihu. Roho ya kujinyima, kujikana nafsi, na kujitolea inapaswa kupendwa na kuthaminiwa. Wengine hawajaitoa mhanga miili yao, juu ya madhabahu ya MUNGU. Wanajiingiza katika kuudhika na hasira ya haraka inayolipuka hapa na pale, wakiridhisha matumbo na uchu wa chakula, na kuendekeza masilahi yao, bila kujali kazi ya MUNGU. Wale ambao wako tayari kutoa dhabihu yoyote kwa ajili ya uzima wa milele, wataupata; na wataona kuwa hata mateso, na kujisulubisha mwenyewe, na kutoa dhabihu kwa kila sanamu hakika yamestahili. Uzito wa utukufu zaidi na wa milele unameza kila kitu na kupita kila starehe ya kidunia. {1T 126.2}

## SURA YA 22

## NJIA MBILI

Katika Mkutano huko Battle Creek, Mei 27, 1856, nilioneshwa katika maono mambo kadhaa ambayo yanahusu kanisa kwa ujumla. Utukufu na Ukuu wa MUNGU vilifanywa kupita mbele yangu. Malaika alisema: “Yeye ni wa kutisha katika utukufu na Ukuu Wake, lakini hamumtambui; mkali katika hasira Yake, lakini mnamkosea kila siku.” Jitahidini kuingia katika mlango mwembamba;

kwa maana mlango ni mpana, na njia ni pana, iendayo upotevuni, na wako wengi wanaoingia humo; bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga, iendayo uzimani, nao waionao ni wachache. Barabara hizi ziko tofauti, zina mwelekeo wa mahali tofauti. Moja inaongoza kwenye uzima wa milele, na nyingine kwenye kifo cha milele. Niliona tofauti kati ya barabara hizi, pia tofauti kati ya watu wanaozisafiria. Barabara ziko tofauti; moja ni pana na laini, nyingine ni nyembamba, yenye mashimo na yenye kupindapinda na ina miamba. Kwa hiyo makundi yanayosafiri yako tofauti kwa tabia, maisha, mavazi, na mazungumzo-Mathayo 7. {1T 127.1}

Wale wanaosafiri katika njia nyembamba ma rafu-rafu wanazungumzia juu ya furaha watakayokuwa nayo mwishoni mwa safari. Nyuso zao huwa za kusikitisha, lakini mara nyingi huangaza kwa furaha takatifu, tukufu. Hawavai kama wale walio katika barabara pana, wala hawazungumzi kama wao, wala hawatendi kama wao. Wanao mfano/Pateni. Mtu wa huzuni ajuaye sikitiko aliwafungulia barabara hiyo, na Yeye Mwenyewe akaipitia hiyo. Wafuasi Wake wanaona nyayo Zake, kisha wanafarijiwa na kuchangamshwa. Yeye Alipita salama kwenye hiyo njia; vivyo hivyo nao wanaweza, ikiwa watafuata nyayo Zake. {1T 127.2}

Kwenye barabara pana wote wanashughulika na nafsi zao tu, mavazi yao, na starehe zao wawapo njiani. Wanaendekeza kwa hiari katika matumbuizo ya kuchekesha sana, na starehe za dunia, na hawafikirii mwisho wa safari yao, juu ya uharibifu uliopo mwishoni mwa njia. Kila siku hukaribia karibu na uharibifu wao; lakini wanazidi kuukimbilia kwa kasi na haraka kwa wendawazimu. Ah, hii ilikuwa ya kutisha sana kwangu! {1T 128.1}

Niliona wengi wakisafiri katika barabara hii pana ambao walikuwa na maneno yaliyoandikwa hivi: "Walioufia ulimwengu. Mwisho wa mambo yote umekaribia. Kuweni tayari pia." Walionekana kama vyote vilivyowazunguka vilikuwa bure, isipokuwa kivuli cha huzuni ambacho kilionekana juu ya sura zao. Mazungumzo yao yalikuwa ya wale wenye raha na kuchekacheka na kujionyesha, watu wasiojali shida za wale waliowazunguka; lakini mara kwa mara wangeyasonda kwa kuridhika maandishi yaliyokuwa katika mavazi yao yaliyoonyesha uhusiano wa kidini walionao (shirika lao la dini), wakitaka wengine wawe kama walivyo wao. Walikuwa katika njia pana, lakini walikiri kuwa katika idadi ya wale ambao walikuwa wakisafiri katika njia nyembamba. Wale walio karibu nao wangesema: "Hakuna tofauti kati yetu. Sisi pia ni sawa kama hawa; tunavaa, tunazungumza, na kutenda sawa tu." {1T 128.2}

Kisha nilielekezwa nyuma miaka ya 1843 na 1844. Kulikuwa na roho ya kujiweka wakfu ambayo haipo sasa. Kitu gani kimewapata watu wa MUNGU wanaodaiwa kuwa wa kipekee? Niliona hali ya kuufuatisha ulimwengu, kutotaka kuteseka kwa sababu ya Ukweli. Niliona ukosefu mkubwa wa kujitiisha katika mapenzi ya

MUNGU. Nilielekezwa tena kwa wana wa Israeli baada ya kutoka Misri. MUNGU kwa rehema aliwaita kutoka kwa Wamisri, ili wamuabudu Yeye bila kizuizi wala kikwazo. Aliwatendea kwa njia kwa miujiza, Aliwathibitisha na kuwajaribu kwa kuwaleta katika njia nyembamba. Baada ya kazi ya ajabu ya MUNGU pamoja nao, na ukombozi wao mara nyingi, walinung'unika alipowajaribu au kuwapima. Lugha yao ilikuwa hii: "Laiti tungekufa kwa mkono wa Bwana katika nchi ya Misri." Walitamani vitunguu na mboga-Hesabu 11. {1T 128.3}

Niliona kwamba wengi wanaodai kuamini Ukweli katika siku hizi za mwisho wanaona ni jambo la ajabu kwa watoto wa Israeli kunung'unika walipokuwa safarini; kwamba baada ya matendo makubwa na ya ajabu ya MUNGU yaliyoandamana pamoja nao, wakawa watu wasiokuwa na shukrani hata kusahau yale aliyowafanyia Bwana. Malaika akasema: "Ninyi mmefanya mabaya kuliko wao." Niliona kwamba MUNGU amewapa watumishi Wake Ukweli ulio wazi, wazi sana, kiasi kwamba hauwezi kupingwa. Popote wanapokwenda, wana ushindi wa hakika. Maadui zao hawawezi kuupiga chenga ule Ukweli wenye kusadikisha. Nuru imeangaza waziwazi kiasi kwamba watumishi wa MUNGU wanaweza kusimama mahali popote na kuufanya Ukweli, ulio wazi na uliounganishwa, ubebe ushindi. Baraka hii kuu haijathaminiwa, au hata kutambuliwa. Ikiwa jaribu lolote linatokea, wengine huanza kutazama nyuma na kufikiria kuwa wana wakati mgumu. Baadhi ya wale wanaodai kuwa ni watumishi wa MUNGU hawajui majaribio yanayoleta utakaso ni yapi. Wakati mwingine hujitengenezea majaribu wao wenyewe, hufikiria majaribu ya kufikirika, na huvunjika moyo kwa urahisi, huumia kwa urahisi, wako nyeti sana kuhusu hadhi yao binafsi, kiasi cha kujiumiza wenyewe, kuwaumiza wengine, na kuiumiza kazi hiyo. Shetani huyakuza kichwani majaribu yao na kuyaweka mawazo ndani ya akili zao ambayo ikiwa yatapewa njia, yataharibu ushawishi wao na manufaa yao. {1T 129.1}

Baadhi wamehisi kujaribiwa kujiondoa kazini mwa Bwana, ili kufanya kazi kwa mikono yao. Niliona kwamba ikiwa mkono wa MUNGU utaondolewa kutoka kwao, kisha wakaachwa chini ya magonjwa na kifo, basi wangejua shida ni nini. Ni jambo la kuogofya kumnung'unikia MUNGU. Hawazingatii akilini kwamba njia ambayo wanasafiri ni njia ngumu, rafu-rafu, na ya kujikana, ya kujisulubisha nafsi, na hawapaswi kutarajia kwamba kila kitu kitasonga mbele vizuri kwa ulaini, kana kwamba walikuwa wakisafiri katika barabara pana. {1T 129.2}

Niliona kwamba baadhi ya watumishi wa MUNGU, hata wachungaji wanavunjika moyo kwa urahisi, nafsi inaumizwa haraka sana, kiasi kwamba wanajifikiria wamedharauliwa, wametukanwa na kujeruhiwa wakati sivyo ilivyo. Wanafikiria fungu lao ni gumu. Hawatambui jinsi ambavyo wangehisi endapo mkono wa MUNGU unaowategemeza ungeondolewa, na wanapitia katika uchungu wa roho. Na kwamba wangepata shida yao mara kumi zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali, wakati walipokuwa wameajiriwa katika kazi ya MUNGU, wakiteswa na

majaribu na shida, licha ya kuwa na kibali cha Bwana. Baadhi wanaofanya kazi kwa bidii kwa MUNGU hawajui kipindi ambacho wana wakati rahisi. Wamekuwa na kupungukiwa na umasikini mdogo sana kiasi kwamba hawajui maana ya kuwa na uhaba au kazi ya kuchosha na kuchakaza mwili au mzigo wa roho kiasi kwamba wanapokuwa na wakati rahisi, wanapopendelewa na MUNGU na kuwa huru kutoka katika uchungu wa roho, hawalijui hilo bali hufikiria majaribu yao ni makubwa. Niliona kuwa endapo hawatakuwa na roho ya kujitolea, na kuwa tayari kufanya kazi kwa uchangamfu, bila ya kujibakiza wenyewe, MUNGU atawapatia nafuu-atawaweka huru. Yeye Hatawakubali kama watumishi Wake wa kujitoa dhabihu nafsi, lakini atawainua wale ambao watafanya kazi, si kwa uvivu, bali kwa dhati na bidii, na watajua kipindi ambacho wana wakati rahisi. Watumishi wa MUNGU lazima wahisi mzigo wa roho na kulia katikati ya Patakatifu na madhabahu, wakisema: "Waachilie watu wako, Ee Bwana." {1T 129.3}

Baadhi ya watumishi wa MUNGU wameyatoa maisha yao kutumika na kutumiwa katika kazi ya MUNGU, mpaka miili na nguvu zao ziishe, na wanakaribia kuchoshwa na kazi inayotumia akili, masumbufu yasiyokoma, taabu, na shida. Ila wengine hawajapata kubeba mzigo juu yao. Lakini bado hawa ndiyo wanafikiria kwamba wana wakati mgumu, kwa sababu hawajawahi kupata shida. Hawajawahi kubatizwa katika mateso, na kamwe hawatakuwa hivyo maadam wataonesha udhaifu mwingi na ujasiri kidogo, na wanapenda maisha ya raha na rahisi/bwerere. Kutokana na kile ambacho MUNGU alinionesha, kuna haja ya kuwepo kwa mapigo miongoni mwa wachungaji, ili kwamba wale walio wavivu, goigoi, na wanaojijali wenyewe wapigwe, ili libaki kundi la watu walio safi, waliotakaswa, waaminifu, na wenye kujitolea nafsi, ambao hawatatafuta mambo ya urahisi kwao, bali watahudumu kwa uaminifu kwa Neno na mafundisho, wakiwa tayari kuteseka na kuvumilia mambo yote kwa ajili ya Kristo, na kuwaokoa wale ambao Yeye aliwafia. Hebu watumishi hawa wajisikie ole juu yao ikiwa hawahubiri injili, na hilo litatosha; lakini wote hawalioni hili. {1T 130.1}

## SURA YA 23

## KUUFUATISHA ULIMWENGU

Nilioneshwa wale waliodai kuitunza Sabato kwa kukiri kwa mdomo tu, na huku wakiufuatisha ulimwengu. Lo, niliona kuwa ni aibu kwa madai yao, aibu kwa kazi ya MUNGU. Ni wadanganyifu wa yale wanayodai kuwa (Ni waongo kwa

ungamo lao). Wanadhani hawafanani na ulimwengu, lakini wako karibu sana nao katika mavazi, mazungumzo, na matendo, kiasi cha kutokuwepo na tofauti. Niliwaona wakiipamba miili yao duni, na masiki ambayo inakufa, ambayo inaweza kuguswa wakati wowote na kidole cha MUNGU na kulazwa kwenye kitanda cha uchungu. Oh, basi, wanapokaribia badiliko lao la mwisho, uchungu wa kufa huwakabiri, na swali kubwa ni hili: "Je! Niko tayari kufa? Je, nimejiandaa kuonekana mbele za MUNGU katika hukumu, na kupita katika uchunguzi mkuu unaopitia yote katika maisha yangu?" Waulize basi wanajisikiaje juu ya kuipamba miili yao, na ikiwa wana ufahamu wa namna ya kuwa tayari ili kuonekana mbele za MUNGU, watakuambia kwamba ikiwa wangeweza kurudishwa na kuishi kipindi cha zamani, wangesahihisha maisha yao, wakaepuka upuuzi wa ulimwengu, ubatili wake na kiburi, na wangeupamba mwili kwa mavazi ya kawaida, na kuweka mfano kwa wote wanaowazunguka. Wangeishi kwa utukufu wa MUNGU. {1T 131.1}

Kwa nini ni vigumu sana kuishi maisha ya kujikana, ya unyenyekevu? Kwa sababu wale wanaojiita Wakristo hawajaufia ulimwengu. Ni rahisi sisi kuishi baada ya kufa. Lakini wengi wanatamani vitunguu samu (leeks), na vitunguu vya Misri. Wana tabia ya kuvaa na kutenda kama ulimwengu kwa kadri iwezekanavyo na bado wanaenda mbinguni. Huko ni kupanda kwenda mahali pengine. Hawaingii kupitia mlango mwembamba na njia nyembamba. {1T 131.2}

Nilioneshwa kundi la watu waliokuwepo kwenye mkutano huo. Malaika alisema: "chakula cha minyoo, [dada clarissa m. Bonfoey, aliyelala katika Yesu siku tatu tu baada ya kuoneshwa maono hayo, alikuwepo akiwa na afya ya kawaida, na alipata hisia ya kina alipoona kwamba alikuwa anaenda kaburini, na alielezea usadikisho wake kwa wengine.] Baadhi ya masomo ya mapigo saba ya mwisho, wengine watakuwa hai na watabaki juu ya dunia ili wabadilishwe wakati wa kuja kwa Yesu." {1t 131.3}

Haya ndiyo maneno ya mazito, yaliyonenwa na malaika. Nilimwuliza malaika kwa nini ni wachache sana wanaovutiwa na ustawi wao wa milele, wachache sana wanaojiandaa kwa badiliko lao la mwisho. Alisema: "Dunia inawavutia, hazina zake zinaonekana kuwa za thamani kwao." Wanaona hayo yanatosha kuzijaza akili zao, na hawana muda wa kujiandaa kwa ajili ya mbingu. Shetani yuko tayari daima kuwatumbukiza zaidi na zaidi katika shida; punde anapoona wasiwasi na taabu vikiwa mbali na akili zao, anazalisha ndani yao hamu isiyokuwa takatifu ya kutaka zaidi vitu vya dunia; na hivyo wakati wao unapita, na wanapokuwa wamechelewa sana, wanaona kuwa hawajapata chochote cha maana. Wameshikilia vivuli na kupoteza uzima wa milele. Hao hawatakuwa na udhuru. {1T 132.1}

Wengi huvaa kama ulimwengu, ili wawe na ushawishi. Lakini hapa wanafanya makosa ya kusikitisha na mabaya. Ikiwa wangekuwa na ushawishi wa Kweli na

wa kuokoa, hebu waishi sawa sawa na madai ya imani yao, waoneshe imani yao kwa matendo yao ya haki, na wafanye tofauti kati ya Mkristo na ulimwengu. Niliona kwamba maneno, mavazi, na vitendo vinapaswa kumuelezea MUNGU-kuzungumza kwa niaba ya Mungu. Ndipo ushawishi mtakatifu utamwagwa juu ya wote, na wote watatambua kwamba wamekuwa pamoja na Yesu. Watu wasioamini wataona kwamba Ukweli tunaodai kuuamini una ushawishi mtakatifu na kwamba imani katika kuja kwa Kristo inaathiri tabia ya mwanaume au mwanamke. Ikiwa mtu yeyote anataka kushawishiwa uzungumze kwa niaba ya ile Kliwe, hebu ushawishi huo uwe ni kwa kusudi la Ukweli, hebu wauishi na kwa hivyo waige mfano wa unyenyekevu. {1T 132.2}

Niliona kwamba MUNGU huchukia kiburi, na kwamba wote wenye kiburi na wote watendao maovu watakuwa mabua/makapi, na siku inayokuja itawateketeza kabisa. Niliona ule ujumbe wa malaika wa tatu lazima ufanye kazi kama chachu juu ya mioyo mingi inayokiri kuuamini, na kuondoa/kupepeta kiburi chao, ubinafsi, tamaa, na kupenda ulimwengu. {1T 132.3}

Yesu anakuja; Je! Yeye atawakuta watu wakiwa na mfano wa ulimwengu? na je! atawakubali hawa kama watu Wake ambao wametakawa kwaajili Yake? Lo, hapana. Hakuna mwingine ila aliye safi na mtakatifu atakayemkubali kuwa Wake. Wale ambao wametakaswa na kufanywa weupe kwa njia ya mateso, na wamejitenga wenyewe kando, bila mawaa na ulimwengu, -Watakuwa watu Wake. {1T 133.1}

Nilipoona Ukweli wa kutisha kwamba watu wa MUNGU walikuwa wamefuatisha namna ya ulimwengu, bila utofauti, isipokuwa kwa jina tu, miongoni mwa wanafunzi wanaodai kumwamini Yesu mpole na mnyenyekevu na wale wasioamini, roho yangu ilihisi uchungu mwingi. Niliona kwamba Yesu alijeruhiwa na kufedheheshwa waziwazi. Malaika alisema, kwa huzuni aliwaona watu wanaodai kumwamini MUNGU wakiupenda ulimwengu, wakishiriki roho ya ulimwengu, na kufuata mitindo yake: "Jingatueni! Jingatueni! Asije akawaweka katika kundi la wanafiki na wasioamini nje ya mji. Madai yenu ya kuikiri imani yatawaacha na huzuni kubwa, na adhabu yenu itakuwa kubwa kwa sababu mliyajua mapenzi Yake, lakini hamkuyafanya. " {1T 133.2}

Wale wanaodai kuamini ujumbe wa malaika wa tatu mara nyingi huijeruhi kazi ya MUNGU kwa upuuzi, mzaha, na michezo-michezo ya kijinga. Nilioneshwa kuwa uovu huu ulikuwepo kote miongoni mwa safu zetu. Lazima kuwe na kujinyenyekeza mbele za Bwana; Israeli wa MUNGU anapaswa kurarua moyo, na sio vazi hilo. Unyenyekevu unaofanana na ule wa mtoto hauonekani mara nyingi; kibali cha mwanadamu kinazingatiwa zaidi kuliko kumkasirisha MUNGU. Malaika alisema: "Wekeni mioyo yenu sawa, asije akawajia katika hukumu, na uzi wa maisha ukakatwa,msije mkalala kaburini bila ulinzi, wala bila kujiandaa kwa hukumu. Au msipofanya kitanda chenu kaburini, na msipofanya amani yenu na MUNGU upesi, na kujingatua kutoka kwa ulimwengu, mioyo yenu itazidi

kuwa migumu, na mtajikuta mmejiegemeza kwenye mhimili wa uongo, unaodhaniwa kuwa ndiyo maandalizi ya kuja kwa Bwana, na mtakuja kugundua makosa yenu mkiwa mmechelewa sana kupata tumaini lenye msingi mzuri."{1T 133.3}



Niliona kwamba wengine wanaojiita watunza Sabato hutumia masaa yao vibaya kuliko hata yale yaliyotupiliwa mbali, katika kujifunza mtindo huu au ule ili kupamba mwili huu dhaifu, unaokufa. Wakati mnajifanya kuonekana kama ulimwengu, na wazuri kadri mnavyoweza, kumbukeni kuwa mwili huo huo unaweza katika siku chache kuwa chakula cha minyoo. Na wakati unapoupamba mwili kwa mapambo yako, ili kulipendeza jicho, unakufa kiroho. MUNGU huchukia ubatili, kiburi chako chenye uovu, na anakutazama kama kaburi lililopakwa chokaa, likiwa limejaa ufisadi, unajisi na uchafu ndani. {1T 134.1}

Akina mama huweka mfano wa kiburi kwa watoto wao, na kwa kufanya hivyo, hupanda mbegu ambayo itakua na kuzaa matunda. Mavuno yatakuwa mengi na ya hakika. Kile walichopanda ndicho watakachovuna. Hakutakuwa na kutofaulu katika mazao. Niliona kwa wazazi, kwamba ni rahisi kwako kuwafundisha watoto wako somo la kiburi, kuliko somo la unyenyekevu. Shetani na malaika zake husimama kando yako kufanya tendo lako, au neno unalosema nao, lifanikiwe na kuwa na ufanisi wa kuwatia moyo wavae, na kwa kiburi chao kuchangamana na jamii ambayo siyo takatifu. Oh wazazi, mnapanda mwiba vifuani mwenu ambao mara nyingi mtahisi uchungu wake. Wakati ambao mtataka kulipinga somo la kusikitisha mlilowafundisha watoto wenu, mtaona ni jambo gumu. Haiwezekani kwenu kufanya hivi. Mnaweza kuwanyima vitu ambavyo vitaendekeza na kufurahisha kiburi chao, lakini bado vinaishi moyoni, vikitamani kuridhishwa; na hakuna kitu kinachoweza kuua kiburi hiki isipokuwa ROHO WA MUNGU mwenye nguvu. Wakati hili linapopata njia kwenda moyoni, litafanya kazi kama chachu humo na kuking'oa. {1T 134.2}

Niliona kwamba vijana kwa wazee wanaipuuzia Biblia. Hawakifanyi kitabu hicho kuwa somo lao na kanuni yao ya maisha kama inavyostahili. Hasa vijana wana hatia ya kupuuza hili. Wengi wao wako tayari, na wanapata muda mwingi, kusoma kitabu kingine chochote. Lakini Neno linaloleta uzima, uzima wa milele, halijasomwa na kuzingatiwa kila siku. Kitabu hicho cha thamani, cha muhimu ambacho kitawahukumu katika siku ya mwisho hakijasomwa hata kidogo. Hadithi zisizo na maana, na zisizo na malengo yoyote, zimesomwa kwa umakini, wakati Biblia imeachwa na kupuuzwa. Siku inakuja, siku ya mawingu na giza nene, ambapo wote watataka wajipatie Ukweli ulio wazi, na sahili wa Neno la MUNGU, ili kwa upole na unyenyekevu watoe, lakini bila ya kuwa na mashaka, watoe sababu ya matumaini yao. Niliona kwamba sababu hii ya kutoa sababu ya matumaini yao, lazima iwe kwa kuziimarisha roho zao wenyewe dhidi

ya pambano kali. Bila kufanya hivi watapungukiwa, na hawawezi kuwa na uthabiti na uamuzi-1Pet 3:15. {1T 134.3}

Ni heri wazazi wangevichoma vitabu vya hadithi zisizo na maana, na riwaya za siku, zinapoingia katika nyumba zao (current novels nk). Ingewapa rehema watoto wao. Kuhamasisha usomaji wa vitabu hivi vya hadithi, ni kama uchawi, au kuwaloga watoto wako. Vitabu hivi vinawaletea mkanganyiko na vitendawili na kuharibu akili. Niliona kuwa ikiwa wazazi hawataamka kwa ajili ya masilahi ya umilele ya watoto wako, hakika watapotea kwa upuuziaji wao. Na uwezekano kwamba wazazi wasio waaminifu wataokolewa ni mdogo sana. Wazazi wanapaswa kuwa mfano mzuri kwa watoto wao. Wanapaswa kuwa na ushawishi mtakatifu katika familia zao. Wanapaswa kuyafanya mavazi yao kuwa ya kujistahi, yasiyo na gharama au maonyesho, tofauti na ulimwengu unaowazunguka. Wanapothamini maslahi ya milele ya watoto wao, wanapaswa kukemea kiburi kilicho ndani ya watoto wao, kukemea kwa uaminifu, na kutohimiza tabia hizo kwa neno au kwa tendo. Oo jamani, kiburi ambacho nilioneshwa kwa watu wanaojifanya kuwa ni watu wa MUNGU! Kimeongezeka kila mwaka, hadi sasa haiwezekani kuwatambua wale wanaodai kuwa ni Wanamgonja Yesu arudi, wanaotunza Sabato kutoka kote katika ulimwengu unaowazunguka. Niliona kwamba kiburi hiki lazima uchanwe kutoka katika familia zetu. {1T 135.1}




Fedha nyingi zimetumika kwenye utepe/ribbon na vitambaa vya urembo (resi) kwa ajili ya vilemba/kofia na kola ya blauzi iliyochanua kama manyoya ya tausi [nimekuwa nikiulizwa swali mara nyingi ikiwa niliamini kwamba ni kosa kuvaa shati yenye kola la pamba. Jibu langu lilikuwa hapana siku zote. Wengine wamechukua maana yenye kupitiliza juu ya kile nilichoandika kuhusu kola, na wamedumisha kuwa ni kosa kuvaa kola ya aina yoyote. Nilioneshwa kola zilizoshonwa za gharama zaidi, na riboni/utepe, na lesi wa gharama kubwa zisizohitajika, ambazo baadhi ya watunza Sabato wamezivaa, na bado wanavaa kwa ajili ya kujionyesha kwa watu na mitindo. Kwa kutaja kola zenye marembo (angalia picha hapo juu), sikukusudia kueleweka kwamba kusiwe na kitu kilichofanana na kola kinachotakiwa kuvaliwa, au, kwa kutaja riboni/utepe, sikusema hakuna utepe wowote unaopaswa kuvaliwa. E.G.W, zingatio kwa toleo la pili] na mapambo mengine yasiyohitajika kupamba mwili, wakati Yesu mfalme wa utukufu, ambaye alitoa maisha Yake ili kutukomboa sisi, alikuwa amevaa taji ya miiba. Hivi ndiyo njia ambayo kichwa kitakatifu cha Bwana wetu

kilivyopambwa. Alikuwa "mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko." "alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." walakini wale wale wanaodai kuoshwa na damu ya Yesu iliyomwagika kwa ajili yao, wanaweza kuvaa na kupamba miili yao masikini, duni, ya kufa, na kuthubutu kukiri kuwa wafuasi wa Kielelezo kitakatifu, cha kujikana nafsi, na unyenyekevu. Lo, laiti wote wangeweza kuliona hili kama MUNGU anavyoliona na jinsi alivyonionesha! Lilionekana kuwa kubwa sana kwangu kulibeba, kuhisi uchungu wa roho niliouhisi nilipoliona. Malaika alisema: "Watu wa MUNGU ni wa Kipekee; hawa ndiyo Yeye anawatakasa Mwenyewe." niliona kuwa mwonekano wa nje ni kielelezo cha moyo. Wakati mwonekano wa nje unaponing'inizwa na kola, riboni, na mapambo na vitu visivyo vya lazima, huonesha wazi kuwa mapenzi ya haya yote yako moyoni; pasipo watu hawa kusafishwa kutoka katika ufisadi wao, hawawezi kamwe kumwona MUNGU, kwani ni wale tu wenye mioyo safi ndio watakaomuona. {1T 135.2}

Niliona kwamba shoka lazima liwekwe kwenye shina la mti. Kiburi kama hicho hakipaswi kuvumiliwa kanisani. Ni vitu hivi vinavyomtenga MUNGU na watu Wake, ambavyo viliifunga safina mbali nao. Waisraeli wamelala katika kiburi, na mitindo, na kufanana na ulimwengu, katikati yao. Wanaendelea kila mwezi katika kiburi, uchoyo, ubinafsi, tamaa mbaya, na kupenda ulimwengu. Mioyo yao inapoongolewa na Ukweli, itasababisha kifo kwa ulimwengu, na wataweka kando utepe/riboni, lesi, na mapambo; na, ikiwa wamekufa kwa dunia hii, basi kuchekwa na kukejeliwa, uchokozi, maneno ya jeuri, kejeli, na mizaha ya wasioamini haitafurukua mioyo yao kwa kuudhika. Watahisi shauku kubwa ya kujitenga na ulimwengu, kama Bwana wao. Hawataiga kiburi, mitindo, au desturi za ulimwengu. Lengo bora litakuwa mbele yao, kumtukuza MUNGU na kupata urithi wa milele. Matarajio haya yatameza yote yenye asili ya kidunia. MUNGU atakuwa na watu waliojitenga na kujitofautisha na ulimwengu. Na punde wanapokuwa na hamu ya kuiga mitindo ya ulimwengu, na hawawi washindi kwa kuiacha hii mitindo, ndivyo ambavyo MUNGU anaacha kuwatambua watu hawa kama watoto Wake. Hao ni watoto wa ulimwengu na wa giza. Wanatamani vitunguu saumu (leeks) na vitunguu vya Misri, ambayo ni, tamaa ya kuwa kama ulimwengu kwa kadri iwezekanavyo; kwa kufanya hivyo, wale wanaodai kuwa wamemvaa Kristo humvua, na kuonesha kuwa wao ni wageni wa neema na upole wa Yesu Mnyenyekevu. Ikiwa wangemfahamu, wangetembea kama wale wanaomstahili Yeye. {1T 136.1}

*****

•

# SURA YA 24

# WAKE ZA WACHUNGAJI

Niliwaona wake za wachungaji. Baadhi yao hawana msaada kwa waume zao, lakini wanaukiri ujumbe wa malaika wa tatu. Wanaweka zaidi umakini wao katika kufanya matakwa na raha zao wenyewe kuliko mapenzi ya MUNGU, au jinsi wanavyoweza kushika mikono ya waume zao kwa maombi yao ya uaminifu na kutembea kwa uangalifu. Niliona kwamba wengine wao huwa wakaidi na wabinafsi hatua ambayo Shetani huwafanya kuwa vyombo vyake na kufanya kazi kupitia wao kuharibu ushawishi na mvuto wa waume zao. Wanahisi wako huru kulalamika na kunung'unika ikiwa watapitishwa katika sehemu yoyote nyembamba au yenye magumu. Wanasahau mateso ya Wakristo wa zamani kwa sababu ya Ukweli na wanafikiria kwamba lazima wawe na matakwa na njia yao, na wafuate mapenzi yao wenyewe. Wanasahau mateso ya Yesu, Mwalimu wao. Wanamsahau Mtu wa huzuni, ambaye alikuwa anafahamu sikitiko—Yeye ambaye hakuwa na mahali pa kuweka kichwa CHAKE. Hawajikumbushi lile paji la uso mtakatifu, lililotobolewa na taji ya miiba. Wanamsahau Yeye, ambaye, hali akiubeba msalaba Wake Mwenyewe kwenda Kalvari, alizimia chini ya mzigo Wake. Siyo tu mzigo wa msalaba wa mbao, bali mzigo mzito wa dhambi za ulimwengu, ulikuwa juu Yake. Wanasahau misumari ya kikatili iliyopigwa kupitia mikono na miguu Yake, na kilio CHAKE kinachomalizika, na cha kuumiza: "MUNGU Wangu, MUNGU Wangu, mbona umeniacha?" Baada ya mateso haya yote aliyoyavumilia kwa ajili yao, wao wanahisi kutokuwa tayari kuteseka kwa ajili ya Kristo. {1T 137.1}

Watu hawa, niliona kwamba wanajidanganya wenyewe. Hawana sehemu wala kuwa miongoni katika suala hilo. Wanashikilia Ukweli; lakini Ukweli hauwashikilii. Wakati Ukweli, Ukweli wa dhati unapowashika, ubinafsi utakufa; na hapo lugha yao haitakuwa, "Nitaenda huko, sitakaa hapa;" bali swali la dhati litakuwa, "Je! MUNGU anataka niwe wapi? Je, ni wapi naweza kumtukuza vizuri wapi, na ni wapi kazi yetu ya umoja na mume wangu inaweza kufanyika vizuri zaidi?" Mapenzi yao yanapaswa kumezwa katika mapenzi ya MUNGU. Ukaidi (kichwa kigumu) na ukosefu wa kujitoa wakfu na ucha Mungu ambao baadhi ya wake za wachungaji wanauonesha utasimama katika njia ya wenye dhambi; damu za watu zitakuwa juu ya mavazi yao. Baadhi ya wachungaji wametoa ushuhuda wenye nguvu kuhusu wajibu na makosa ya kanisa; lakini haukuwa na matokeo yaliyokusudiwa, kwani wenza wao wenyewe walihitaji ushuhuda wote wa moja kwa moja uliokuwa umechukuliwa, na karipio lilirudi kwao likiwa na uzito mkubwa. Wanawaacha wake/wenzi wao wawaathiri na kuwavuta chini, wakiharibu akili zao, na umuhimu na ushawishi wao unapotea; wanajisikia kukata tamaa na kuvunjika moyo, na hawatambui chanzo cha kweli cha jeraha hilo. Tatizo lipo karibu hapo nyumbani. {1T 138.1}

Akina dada hawa wameunganishwa kwa karibu na kazi ya MUNGU ikiwa amewaita waume zao kuhubiri Ukweli wa sasa. Watumishi hawa, ikiwa wameitwa kweli na MUNGU, watahisi umuhimu wa Ukweli. Wamesimama kati ya watu walio hai na wale walio kifoni, katikati ya uzima na mauti, na lazima wawe waangalifu kwa roho kama wale ambao wanapaswa kutoa hesabu. Wito wao ni mzito, wa wakfu, na wenzao wanaweza kuwa baraka kubwa au laana kubwa kwao. Wanaweza kuwatia moyo na kuwachangamsha, kuwashangilia wanapokata tamaa, kuwafariji wanapotupwa chini, na kuwatia moyo waangalie juu na kumtumaini MUNGU kikamilifu imani yao inaposhindwa. Au wanaweza kuchukua njia tofauti, kutazama upande wa giza, kufikiria wana wakati mgumu, kutoonyesha imani yao kwa MUNGU, kuzungumza majaribu yao na kutokuamini kwa wenzao, kuendekeza roho ya kulalamika, ya kunung'unika, na kuwa mzigo mfu kwa kazi ya Mungu na hata laana kwao. {1T 138.2}

Niliona kwamba wake za wachungaji wanapaswa kuwasaidia waume zao katika kazi zao na kuwa na uhakika na waangalifu kwa kile kinacholetwa na ushawishi wao, kwani wanaangaliwa, na mengi yanatarajiwa kutoka kwao kuliko wengine. Mavazi yao yanapaswa kuwa mfano. Maisha yao na mazungumzo yao yanapaswa kuwa mfano, wakitoa harufu ya uzima badala ya kifo. Niliona kwamba wanapaswa kuchukua msimamo wa unyenyekevu, wa upole, lakini ulioinuliwa, bila kuwa na mazungumzo yao juu ya vitu ambavyo havioneshi kuelekeza akili mbinguni. Swali kubwa linapaswa kuwa: "Ninawezaje kuokoa nafsi yangu mwenyewe, na kuwa njia ya kuokoa wengine?" Niliona kuwa katika jambo hili hakuna kazi nusu-nusu inayokubaliwa na MUNGU. Yeye Anataka moyo wote na mawazo, na shauku, la sivyo hatakubali chochote. Ushawishi wao unaeleza, kwa dhati kabisa, bila makosa, kama ni upande wa ukweli au kinyume chake.

Wanakusanyika pamoja na Yesu, au kutawanya mbali. Mke ambaye hajatakaswa ni laana kubwa zaidi ambayo mchungaji anaweza kuwa nayo. Watumishi hao wa MUNGU ambao wamekuwa hawana furaha, na bado wameendelea kuwa hivi kwa kuwa na ushawishi huu dhaifu unaonyausha majumbani mwao, wanapaswa kuzidisha maombi maradufu na kukesha kwao, wachukue msimamo thabiti, waamue kusimama, na wasiruhusu giza hili liwasonge na kuwavuta chini. Wanapaswa kushikamana karibu na MUNGU, kuwa thabiti na kuamua, kusimamia vizuri nyumba yao wenyewe, na kuishi ili waweze kupata kibali cha MUNGU na uangalizi wa malaika. Lakini ikiwa wachungaji watajisalimisha kwa matakwa ya wenzi wao wasiotakaswa, uso wa MUNGU uliokunjwa unaletwa juu ya makao yao-hasira ya Mungu. Sanduku la Agano la MUNGU haliwezi kukaa ndani ya nyumba, kwa sababu wachungaji wana mwonekano wa kuwaunga mkono wake zao katika makosa yao. {1T 139.1}

MUNGU wetu ni MUNGU Mwenye wivu. Ni jambo la kuogopesha kumchezea. Hapo zamani, Akani alitamani kabari ya dhahabu na vazi la Babeli, na akavificha, na Israeli wote wakateseka; walifukuzwa na kushindwa mbele ya maadui zao. Na Yoshua alipouliza sababu, Bwana akasema: "Inuka, watakase watu, na useme, Jitakaseni kwa kesho; kwa maana Bwana, MUNGU wa Israeli, asema hivi, kuna kitu kilicholaaniwa katikati yako, Israeli; wewe huwezi kusimama mbele ya adui zako, hata mtakapoondoa kile kitu kilicholaaniwa kati yenu." Akani alikuwa ametenda dhambi, na MUNGU akamwangamiza yeye na nyumba yake yote, pamoja na mali zao zote, na akafuta laana kutoka kwa Israeli. {1T 140.1}

Niliona kwamba Israeli wa MUNGU lazima ainuke na kuinua nguvu zao kwa MUNGU kwa kufanya upya na kutunza agano lao pamoja Naye. Tamaa, ubinafsi, kupenda pesa, na kupenda ulimwengu, yote yako miongoni mwa watunza Sabato. Maovu haya yanaharibu roho ya kujitoa wakfu miongoni mwa safu za watu wa MUNGU. Wale ambao wana tamaa hii mioyoni mwao hawana habari kabisa. Imewapata bila kutambulika, na isipokwanguliwa na kuondolewa, uharibifu wao utakuwa wa hakika kama ule wa Akani. Wengi wamechukua dhabihu kutoka kwenye madhabahu ya MUNGU. Wanaupenda ulimwengu, wanapenda faida na ongezeko lake, na, kama hakuna badiliko kamili ndani yao, wataangamia pamoja na ulimwengu. MUNGU amewaazima mali Yake; sio yao wenyewe, bali MUNGU amewafanya kuwa mawakili Wake. Lakini wanaiita mali yao wenyewe na kujilimbikizia. Lakini, loo, ni haraka kama nini, wakati mkono wa MUNGU unaofanikisha unapokuwa umeondolewa kutoka kwao, yote yamenyakuliwa kwa muda mfupi! Lazima kuwe na kujitoa dhabihu kwa MUNGU, kujikana nafsi yako kwa sababu ya Ukweli. Ah, mtu ni dhaifu na mnyonge kiasi gani! Mkono wake ni duni kiasi gani! Niliona kwamba hivi karibuni utukufu na kujiinua kwa mwanadamu kutashushwa, na kiburi cha mwanadamu kitanyenyekeshwa. Wafalme na wakuu, matajiri na maskini, wote

watashuka na kuinama chini, wakipiga mgoti kwa usawa, na mapigo ya MUNGU yanayonyausha yatawashukia. {1T 140.2}

## SURA YA 25

## KUWA NA BIDII, UKATUBU

Wapendwa kaka na dada,

Bwana amenionesha katika maono mambo kadhaa kuhusu kanisa katika hali yake ya uvuguvugu ya sasa, ambayo nitawaelezea. Kanisa liliwasilishwa mbele yangu katika maono. Malaika alisema kwa kanisa: "Yesu anakuambia," Uwe na bidii, ukatubu." Kazi hii, niliona, inapaswa kushikiliwa kwa bidii. Kuna kitu cha kutubia. Mawazo ya ulimwengu, ubinafsi, uchoyo na tamaa vimekuwa vikitafuna hali ya kiroho na maisha ya watu wa MUNGU. {1T 141.1}

Hatari ya watu wa MUNGU kwa miaka michache iliyopita imekuwa upendo kwa ulimwengu. Kutokea humo zimeibuka dhambi za ubinafsi, tamaa na uchoyo. Kadri wanavyokuwa karibu na ulimwengu huu, ndivyo wanavyoweka mapenzi yao juu yake; na bado wanaukaribia zaidi. Malaika alisema: "Ni rahisi ngamia kupita kwenye tundu la sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa MUNGU." Walakini wengi wanaodai kuamini kwamba tunao ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu, wanajitahidi kwa nishati zao zote ili kujiweka katika nafasi ambayo ni rahisi ngamia kupitia katika tundu la sindano kuliko wao kuingia katika ufalme. {1T 141.2}

Hazina hizi za kidunia, ni baraka zinapotumiwa vyema. Wale walio nazo wanapaswa kutambua kwamba wamekopeshwa na MUNGU na wanapaswa kuzitumia kwa moyo mkunjufu mali zao ili kuendeleza kazi Yake. Hawatapoteza tuzo yao hapa. Watazingatiwa kwa wema na malaika wa MUNGU na pia wataweka hazina zao mbinguni. {1T 141.3}

Niliona kwamba Shetani huangalia tabia ya kipekee za ubinafsi, za tamaa za baadhi ya wale wanaodai kuuamini Ukweli, Naye atawajaribu kwa kuweka mafanikio katika njia yao, akiwapatia utajiri wa dunia. Yeye Anajua kwamba ikiwa hawataishinda hali yao ya asili, watajikwaa na kuanguka kwa kupenda mali, wakiabudu na kupenda sanamu yao. Lengo la Shetani mara nyingi hutimizwa. Upendo wenye nguvu wa ulimwengu unashinda, au kuumeza, upendo wa Ukweli. Wanapewa falme za ulimwengu, na kushika hazina yao kwa hamu na kufikiria kwamba wamefanikiwa sana. Shetani anashinda kwa sababu mpango wake umefanikiwa. Wameuacha upendo wa MUNGU kwa ajili ya upendo kwa dunia. {1T 142.1}

Niliona kwamba wale ambao wamefanikiwa hivyo wanaweza kuzuia mpango wa Shetani ikiwa watashinda tamaa yao ya ubinafsi kwa kuweka mali zao zote juu ya madhabahu ya MUNGU. Na wanapoona ni wapi fedha zinahitajika ili kuendeleza kazi ya Ukweli na kuwasaidia wajane, yatima, na walioteswa, wanapaswa kutoa kwa furaha na hivyo kuweka hazina mbinguni. {1T 142.2}

Zingatia ushauri wa Shahidi wa Kweli. Nunua dhahabu iliyojaribiwa kwa moto, upate kuwa tajiri, vazi jeupe upate kuvaa, na dawa ya macho upate kuona. Fanya bidii. Hazina hizi za thamani hazitatuangukia bila jitihada kwa upande wetu. Lazima tununue - "kuwa na bidii na kutubu" kwa hali yetu ya uvuguvugu. Lazima tuwe macho kuona makosa yetu, kuzitafuta na kuzichunguza dhambi zetu, na kuzitubu kwa bidii. {1T 142.3}

Niliona kwamba ndugu walio na mali wana kazi ya kufanya ili kujinasua kutoka kwenye hazina hizi za kidunia na kushinda upendo wao kwa ulimwengu. Wengi wao wanaupenda ulimwengu huu, wanapenda hazina yao, lakini hawako tayari kuiona shida hii waliyo nayo. Lazima wawe na bidii na watubu juu ya tamaa yao ya ubinafsi, ili upendo katika ile Kweli uweze kumeza kila kitu. Niliona kwamba wengi wa wale walio na utajiri watashindwa kununua dhahabu, mavazi meupe, na dawa ya macho. Bidii yao siyo ya kina na ya dhati, wala hailingani na thamani ya kitu wanachokitafuta/wanachokikimbizia. {1T 142.4}

Niliona watu hawa wakati wanapata mafanikio katika kupata mali za dunia; ni bidii kubwa kiasi gani waliyoonesha, juhudi kubwa kiasi gani, nguvu kubwa iliyoje, ili kupata hazina ya kidunia ambayo lazima ipite upesi! Mahesabu ya faida ya aina gani waliyoyafanya! Wanapanga na kuhangaika mapema na baadaye, hujitoa mhanga kwa raha na starehe yao kwa ajili ya hazina za kidunia. Endapo wangetoa bidii inayolingana na hiyo ya vitu vya dunia katika kupata dhahabu, mavazi meupe, na dawa ya macho, ingewafanya wamiliki hazina hizi njema za uzima, uzima wa milele, katika ufalme wa MUNGU. Niliona kwamba ikiwa kuna wanaohitaji dawa ya macho, ni wale wenye mali za kidunia. Wengi wao ni vipofu katika hali zao wenyewe, hawaoni kwa fahamu zao thabiti kuhusu ulimwengu huu. Laiti wangepata kuona! {1T 143.1}

“Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.” Niliona kwamba wengi wana takataka nyingi sana kwenye mlango wa mioyo yao hata wasiweze kufungua mlango. Wengine wana shida kati yao na ndugu zao zinazopaswa kuondolewa. Wengine wana hasira mbaya, tamaa ya ubinafsi, zinazopaswa kuondolewa kabla ya kufungua mlango. Wengine wamevingirisha ulimwengu mbele ya mlango wa mioyo yao, hivyo huuziba/kuufunga mlango. Takataka hizi zote lazima zichukuliwe, na kisha wanaweza kufungua mlango na kumkaribisha Mwokozi ndani. {1T 143.2}

Ah, ahadi hii ilikuwa ya thamani kiasi gani, kama nilivyooneshwa katika maono! "Nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami." Oo, upendo, upendo wa ajabu wa MUNGU ! Baada ya uvuguvugu wetu wote na dhambi zetu zote, Yeye anasema: "Nirudie Mimi, Nami nitakurudia wewe, Nami nitaponya maasi yako. Hili lilirudiwa na malaika mara kadhaa. "Nirudieni Mimi, Nami nitawarudia ninyi, Nami nitaponya maasi yako." {1T 143.3}

Niliona wengine wangefurahi kurudi. Wengine hawataruhusu ujumbe huu kwa kanisa la Laodikia uwe na uzito kwao. Watateleza pamoja, kwa njia ile ile kama hapo awali, na watatapikwa kutoka kinywani mwa Bwana. Wale tu wanaotubu kwa bidii ndio watakaopata kibali kwa MUNGU. {1T 144.1}

"Yeye ashindaye nitampa kukaa pamoja Nami katika kiti changu cha enzi, kama vile Mimi nilivyoshinda, na kuketi pamoja na Baba yangu katika kiti CHAKE cha enzi." Sisi tunaweza kushinda. Ndiyo; kikamilifu, kabisa. Yesu alikufa ili kuweka njia ya kutoka kwa ajili yetu, kusudi tuweze kushinda kila mwenendo na hasira mbaya, kila dhambi, kila jaribu, na kukaa Naye hatimaye. {1T 144.2}

Ni upendeleo wetu kuwa na imani na wokovu. Nguvu za MUNGU hazijapungua. Nguvu Zake, niliona kwamba zingetolewa kwetu kama zamani. Ni kanisa la MUNGU ambalo limepoteza imani yao wanayopaswa kuidai, nguvu zao za kushindana, kama vile Yakobo, alivyolia: "Sitakuacha uende, usiponibariki." Imani ya kudumu imekufa. Lazima ifufuliwe katika mioyo ya watu wa MUNGU. Lazima kuwe na madai ya baraka za MUNGU. Imani, imani hai, daima hustahimili na kutazama juu kwa MUNGU na utukufu; na kutokuamini, ni kushuka gizani na mauti. {1T 144.3}

Niliona kwamba akili za baadhi ya washiriki wa kanisa hazijaenda katika njia sahihi. Kumekuwepo na tabia za kipekee ambazo zimekuwa na maoni ya kupima ndugu zao. Na ikiwa kuna yeyote ambaye hakukubaliana nao katika kila kitu kabisa, kulikuwa na shida katika kambi mara moja. Wengine wamechuja mbu na kumeza ngamia. {1T 144.4}

Mawazo haya yaliyowekwa yamefanyiwa kejeli, watu wamecheka na kuyandekeza kwa muda mrefu sana. Kumekuwepo na hali ya kuokota majani

makavu (kufanya mambo kwa bahati nasibu ili kumpata mtu fulani). Na wakati ambapo hapakuwa na shida za kweli kanisani, shida na majaribu yametengenezwa. Akili za washiriki wa kanisa na watumishi wa Bwana zimeitwa kutoka kwa MUNGU, kwa Ukweli, na mbingu na kukaa gizani. Shetani anafurahi kuendelea kwa mambo kama hayo; yanamfurahisha. Lakini haya siyo majaribu ambayo yatalitakasa kanisa na ambayo mwishowe yataongeza nguvu za watu wa MUNGU. {1T 144.5}

Niliona kuwa wengine wananyauka kiroho. Wameishi kwa muda wakitazama kuwaweka sawa ndugu zao - wakitazama kila kosa ili wawasumbue. Na wanapofanya hivi, akili zao haziwi kwa MUNGU, wala mbinguni, wala juu ya ukweli; bali mahali ambapo Shetani anawataka - kwa mtu mwingine. Nafsi zao zimepuuzwa; ni nadra watu hawa kuona au kuhisi makosa yao wenyewe, kwani wamekuwa na mengi ya kutosha katika kutazama makosa ya wengine bila hata kuangalia nafsi zao au kuchunguza mioyo yao. Mavazi ya mtu, kofia/vilemba, au aproni huvuta umakini wao. Lazima wazungumze na huyu au yule, na hiyo mada inatosha kuzungumzia kwa juma zima kwao. Niliona kuwa dini zote roho maskini ni chache katika kutazama mavazi na matendo ya wengine, na kutafuta makosa. Isipokuwa watabadilika kwa kufanya matengenezo, hakutakuwa na nafasi mbinguni kwa ajili yao, kwani wangemtafutia makosa hata Bwana Mwenyewe. {1T 145.1}

Malaika alisema: "Ni kazi binafsi kuweka mambo sawa na MUNGU." Kazi hiyo iko kati ya MUNGU  na roho zetu wenyewe. Lakini wakati watu wanapojali sana makosa ya wengine, wao hawajijali. Hawa watu wenye mawazo ya kutafuta makosa mara nyingi wangejiponya tabia hiyo ikiwa wangeenda moja kwa moja kwa mtu ambaye wanafikiri kwamba amekosea. Ingekuwa nzuri zaidi kama wangeachana na mawazo yao badala ya kwenda. Lakini ni rahisi kuuacha ulimi umukimbie kwa huyu au yule, pale mshtakiwa anapokuwa hayupo. {1T 145.2}

Wengine wanafikiri ni makosa kujaribu kufuata utaratibu katika ibada ya MUNGU. Lakini nimeona kuwa siyo hatari kuzingatia utaratibu katika kanisa la MUNGU. Nimeona kwamba machafuko hayampendezi Bwana, na kwamba lazima kuwe na utaratibu katika kuomba na pia katika kuimba. Hatupaswi kuja nyumbani kwa MUNGU kuziombea familia zetu isipokuwa kama hisia za ndani zitatuongoza wakati ROHO WA MUNGU anapozisadikisha. Kwa ujumla, mahali sahihi pa kuombea familia zetu ni huko katika madhabahu ya familia. Wakati mambo yahusuyo maombi yetu yanapokuwa mbali, mahali pa faragha ni mahali pazuri pa kumsihi MUNGU  kwa ajili yao. Tunapokuwa katika nyumba ya MUNGU, tunapaswa kuomba baraka za sasa na tunapaswa kutarajia MUNGU kusikia na kujibu maombi yetu. Mikutano hiyo itakuwa  hai na ya kuvutia. {1T 145.3}

Niliona kwamba wote wanapaswa kuimba kwa roho na kwa akili pia (1 Wakorintho 4:15). MUNGU  hafurahishwi na maneno ya mizaha na mifarakano.

Jambo sahihi daima humpendeza kuliko makosa. Na kadri watu wa MUNGU wanavyokaribia zaidi katika uimbaji ulio sahihi, wenye mapatano, ndivyo Yeye anavyotukuzwa, kanisa linafaidika, na wasioamini wanaathiriwa vyema. {1T 146.1}

Nimeoneshwa utaratibu, mpangilio kamili, wa mbinguni, na nimefurahi sana niliposikiliza muziki mzuri mahali hapo. Baada ya kutoka katika maono, uimbaji wa hapa nimeusikia ukiwa mbaya sana, mkali, usio na ulinganifu. Nimeona vikundi vya malaika, waliosimama katika mraba, kila mtu akiwa na kinubi cha dhahabu. Mwishoni mwa kinubi kulikuwa na chombo cha kugeuza kuweka kinubi vizuri au kubadilisha sauti. Vidole vyao havikuchezesha kamba ovyo ovyo, bali viligusa nyuzi tofauti na kutoa sauti tofauti. Kuna malaika mmoja ambaye huongoza kila wakati, ambaye kwanza hugusa kinubi na kupiga noti, kisha wote hujiunga na muziki kamilifu wa mbinguni, mzuri na wa thamani. Hauwezi kuelezewa kwa maneno. Ni wimbo wa mbinguni, wa Kiungu, wakati kutoka kwenye kila uso kunaangaza sura ya Yesu, ikiangaza na utukufu usioweza kuelezeka. {1T 146.2}

## SURA YA 26

## MASHARIKI NA MAGHARIBI MWA MAREKANI

Ndugu Wapendwa: Bwana amenionesha katika maono mambo kadhaa kuhusu Mashariki na Magharibi ambayo ninahisi ni jukumu langu kuyaweka mbele yenu. Niliona kwamba MUNGU amekuwa akifungua njia ya kueneza Ukweli wa sasa huko Magharibi. Inahitaji nguvu zaidi kuongoa watu Mashariki kuliko huko Magharibi, na kwa sasa kazi ndogo sana inaweza kukamilishwa Mashariki. Jitihada maalum zinapaswa kufanyika wakati wa sasa ambapo mazuri zaidi yatatokea (Watu toka Ulaya walihamia mashariki mwa Marekani kwanza kama vile Virginia New York, na Boston kwenye Bahari ya Atlantiki, kisha wakaanza kwenda ndani ya nchi kuelekea California, ilipo Bahari ya Pasifiki). {1T 146.3}

Watu wa Mashariki wamesikia tangazo la kuja kwa Kristo mara ya pili, na wameona maonesho mengi ya nguvu ya MUNGU, na wameangukia katika hali ya kutokujali na usalama ambao ni vigumu kuwafikia watu kwa sasa. Baada ya juhudi zisizo za kawaida kufanyika Mashariki, na zawadi bora, ni kidogo tu kilichokamilishwa. {1T 147.1}

Niliona kwamba watu wa Magharibi wanaweza kuguswa moyo na kuongolewa kwa urahisi zaidi kuliko wale wa Mashariki. Hawakuwa na nuru ya Ukweli, na hawajaikataa, na mioyo yao ni miororo/laini zaidi na rahisi kuathiriwa na ukweli na ROHO WA MUNGU. Mioyo ya wengi huko Magharibi tayari imejiandaa kupokea Ukweli kwa hamu; na kama watumishi wa MUNGU wanaenda kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho za thamani, wana mengi ya kuwatia moyo katika kazi yao ngumu. Kadri watu walivyo na shauku ya kusikia, na wengi wakiukubali Ukweli, zawadi ambayo MUNGU amewapa watumishi Wake inahamasishwa na kuimarishwa. Wanaona kuwa juhudi zao zimetawazwa na mafanikio. {1T 147.2}

Niliona kuwa huko Magharibi kazi imefanyika zaidi ya mara kumi kuliko Mashariki baada ya juhudi sawa kuwekezwa, na kwamba njia inafunguliwa kwa mafanikio makubwa zaidi. Nimeona kwamba mengi yanaweza kufanyika sasa huko Wisconsin, na zaidi huko Illinois, na kwamba juhudi za kueneza Ukweli lazima zifanyike huko Minnesota na Iowa. Hilo litaleta matokeo makubwa katika mioyo mingi huko. Kulikuwa na shamba kubwa, kubwa sana la kazi lililoenea mbele yangu katika maono, ambalo bado halijafanyiwa kazi-hakuna wainjilisti wameingia; lakini hakuna msaada wa kutosha katika kujitoa mhanga miongoni mwa watu, ili kujaza hata kuweza kufikia nusu ya mahali ambapo watu wako tayari kusikia Ukweli, na wengi kuupokea. {1T 147.3}

Mashamba mapya ya kazi ya injili, mapya kabisa, lazima yatembelewe; wengi watalazimika kwenda vitani kwa kujihudumia wenyewe, kuingia kwenye shamba hilo na matarajio ya kubeba gharama zao za kujikimu maisha wenyewe. Hapa, niliona, ni fursa nzuri kwa mawakili wa Bwana kuchukua sehemu yao na kuwasaidia wale wanaobeba Ukweli katika maeneo haya. Inapaswa kuwa fursa kubwa kwa mawakili hawa kumpatia MUNGU kilicho CHAKE (masponsa). Kwa kufanya hivyo watatimiza wajibu wa Kimaandiko na kujikomboa kutoka katika sehemu ya hazina yao ya kidunia, ambayo sasa ni mzigo kwa wengi ambao wana mali nyingi kwa sasa. Pia itaongeza hazina yao mbinguni. {1T 147.4}

Niliona kwamba hema la Mashariki halipaswi kubebwa juu ya ardhi ile ile. Ikihitajika, wale wanaoandamana na hema hilo wanapaswa kwenda vitani kwa gharama yao wenyewe; wanapaswa kupiga hema mahali ambapo Ukweli haujafikishwa, na wakati hema inapowekwa wafanyakazi wa kutosha wanapaswa kuletwa. {1T 148.1}

Niliona kwamba kumekuwa na kutofaulu kupitia shamba hilo hilo la zamani, mwaka baada ya mwaka, kwa karama karibu sawa. Ikiwezekana, karama zinazokubalika zaidi zinapaswa kupatikana. Ingekuwa bora, na mengi yangetimizwa zaidi, ikiwa kungekuwa na mikutano michache ya hema, na nguvu kubwa, au kundi, na karama tofauti za kufanya kazi. Halafu kunapaswa kuwepo na kukawia mahali ambapo watu wanapendezwa/wanavutiwa. Kumekuwa na haraka sana katika kubeba hema. Wengine huanza kuvutiwa, na

kuna haja ya juhudi za kudumu kuendelea kutolewa hadi akili zao zitulie na wajisalimishe katika Ukweli. Katika maeneo mengi ambapo hema limepigwa, watendakazi hukaa mpaka chuki ianze kutoweka, na watu waanze kusikiliza wakiwa na akili isiyo na chuki; lakini hapo ndipo hema hiyo hushushwa na kupelekwa njiani kwenda mahali pengine. Mizunguko inapoisha, muda na mali zimetumiwa, na watumishi wa MUNGU wanaweza kuona mafanikio kidogo tu kupitia msimu wa hema. Lakini ni wachache wanaoletwa kuutambua Ukweli, na watumishi wa MUNGU, wakiwa wameona kiasi kidogo cha kuwachangamsha kuwatia moyo, na kuinua karama iliyo ndani yao, basi hupoteza hali ya kiroho, na nguvu badala ya kuimarika,. {1T 148.2}

Niliona kwamba juhudi maalum zinapaswa kufanyika Magharibi kwa kutumia mahema; kwa maana malaika wa MUNGU  wanaandaa akili huko zitakazopokea Ukweli. Hii ndiyo sababu MUNGU  amewahamisha wengine Mashariki kwenda Magharibi. Karama zao zinaweza kukamilisha mengi zaidi Magharibi kuliko Mashariki. Mzigo wa kazi uko Magharibi, na ni jambo lenye umuhimu mkubwa kwamba watumishi wa MUNGU wasonge mbele katika fadhila Zake znazofunguliwa. {1T 148.3}

Niliona kwamba wakati ujumbe utaongezeka sana kwa nguvu, basi fadhila za MUNGU  zitafunguliwa na kuandaa njia huko Mashariki kwa ajili ya kukamilisha mengi zaidi kuliko yanayoweza kukamilishwa katika wakati huu wa sasa. Hivyo basi, MUNGU atatuma baadhi ya watumishi WAKE walio madarakani kutembelea maeneo ambayo ni kidogo au hakuna chochote kinachoweza kufanywa sasa, na wengine ambao kwa sasa hawajali wataamshwa na wataishika Kweli. [MASALIA YA MAKALA HII YANATOKA KWENYE MAONO YALIYOTOLEWA HUKO ROUND GROVE, ILLINOIS, DESEMBA 9, 1856.] {1T 149.1}

Niliona kwamba MUNGU  amewaonya wale ambao wamehama kutoka Mashariki kwenda Magharibi. Amewaonesha wajibu wao, kwamba haifai lengo lao kuwa kupata utajiri, bali kuzifanyia roho wema, kuishi imani yao, na kuwaambia wale walio karibu nao kwamba ulimwengu huu si makazi yao. {1T 149.2}

Onyo lilikuwa la kutosha, ikiwa lingezingatiwa; lakini wengi walishindwa kuzingatia kile MUNGU  alikuwa ameonesha. Waliharakisha kuendelea zaidi na zaidi, na kulevywa na roho ya ulimwengu. "Angalieni nyuma," alisema malaika, "na mpime yote ambayo MUNGU  ameyaonesha juu ya wale wanaohamia kutoka Mashariki kwenda Magharibi." Je! Mmeitii? Niliona kuwa mmeenda kinyume kabisa na mafundisho ya MUNGU, yaliyonunuliwa kwa gharama, na badala ya matendo yenu kusema kwa wale wanaokuzunguka kuwa mnaitafuta nchi iliyo bora, yametangaza wazi kuwa nyumba yenu na hazina yenu zilikuwa hapa duniani. Matendo yenu yameipinga imani yenu. {1T 149.3}

Wala hii si yote. Upendo ambao unapaswa kuwepo kati ya ndugu umekuwa ukikosekana. "Je! Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" imedhihirishwa; roho ya

ubinafsi na tamaa imekuwa ndani ya mioyo ya ndugu. Badala ya kujali masilahi ya ndugu na kuwathamini, imedhihirishwa roho ya ubahili na ubinafsi ambayo MUNGU na huidharau na kuichukia. Wale ambao hukiri kumwamini sana MUNGU, na ambao hujihesabu kuwa miongoni mwa watu wa MUNGU wa kipekee, wakikiri kuwa wana bidii ya matendo mema, wanapaswa kuwa waungwana na wakarimu, na wanapaswa daima kuonesha tabia ya kuwafeva/kuwapendeza ndugu zao badala yao, na wanapaswa wawapatie ndugu zao fungu na nafasi nzuri. Ukarimu huzaa ukarimu. Ubinafsi huzaa ubinafsi. {1T 149.4}

Niliona kwamba kupitia majira ya joto yaliyopita roho inayotawala imekuwa ikishika ulimwengu huu kadri iwezekanavyo. Amri za MUNGU hazijatunzwa. Tunaitumikia sheria ya MUNGU kwa akili; lakini akili za wengi zimekuwa zikiutumikia ulimwengu. Na wakati akili zao zote zikiwa zimeshughulika na vitu vya dunia na kujitumikia wenyewe, wasingeweza kuitumikia sheria ya MUNGU. Sabato haijatunzwa. Kwa wengine kazi ya siku sita imebebwa mpaka siku ya saba. Saa moja, na hata zaidi, mara nyingi zimechukuliwa kwenye kuanza na kufungwa kwa Sabato. {1T 150.1}

Baadhi ya watunza Sabato wanaouambia ulimwengu kwamba wanatazamia ujio wa Yesu, na kwamba wanaamini tuna ujumbe wa mwisho wa rehema, wanaruhusu hisia zao za asili, na kubadilishana mali, na biashara, wanatoa mfano halisi kati ya wasioamini kwa bidii yao katika biashara, ukali, na mara zote hupata mwisho bora wa mapatano (wanapata dili nzuri wanapobembeleza bei ishuke na kufanya wengine wapate hasara!). Ingekuwa bora kupoteza kidogo na kutoa ushawishi bora ulimwenguni, na ushawishi wa furaha kati ya ndugu, na kuonesha kwamba ulimwengu huu siyo MUNGU wao. {1T 150.2}

Niliona kwamba ndugu wanapaswa kuwa na shauku ya kupendana. Hasa wale ambao wamebarikiwa na afya wanapaswa kuwajali na kuwatunza wale ambao hawana afya njema. Wanapaswa kuwapa upendeleo (fevaO. Wanapaswa kukumbuka somo lililofundishwa na Yesu juu ya Msamaria mwema. {1T 150.3}

Yesu alisema: "Pendaneni, kama vile Mimi nilivyowapenda ninyi." Kiasi gani? Upendo Wake hauwezi kuelezeka. Aliuacha utukufu aliokuwa nao kwa Baba kabla ya ulimwengu kuwako. " Yeye Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa sababu ya maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Alivumilia kila aibu, matusi na kejeli. Tazameni uchungu Wake bustanini, alipoomba kwamba kikombe hiki kimuepuke! Tazameni mateso Yake pale Kalvari! Yote haya kwa ajili ya mwanadamu aliye na hatia, na aliyepotea. Na Yesu anasema: "Pendaneni, kama vile Mimi nilivyowapenda ninyi." Kiasi gani? Kiasi cha kutosha kutoa maisha yako kwa ajili ya ndugu. Lakini tumefikia hapa, kwamba ubinafsi lazima uridhike, na Neno la MUNGU lipuuzwe? Ulimwengu ni MUNGU wao. Wanautumikia, wanaupenda, na

upendo kwa MUNGU umeondoka. Ukiupenda ulimwengu, upendo wa Baba haumo ndani yako. {1T 150.4}

Neno la MUNGU limepuuzwa. Katika hayo kuna maonyo kwa watu wa MUNGU yanayoonesha hatari zao. Lakini wamekuwa na wasiwasi, masumbufu na mashaka mengi sana kiasi kwamba hawapati muda wa kuomba. Kumekuwa na desturi ya utauwa, muundo mtupu usio na nguvu. Yesu aliomba, na oh! Maombi Yake yalikuwa na bidii kiasi gani! Na bado alikuwa Mwana mpendwa wa MUNGU ! {1T 151.1}

Ikiwa Yesu alionesha bidii nyingi za dhati, nguvu nyingi na uchungu, Je, ni zaidi sana kwa wale ambao amewaita kuwa warithi wa wokovu, wanaomtegemea MUNGU kwa nguvu zao zote, ili roho zao zote zichochewe kushindana na MUNGU na kusema: "Sitakuacha uende, usiponibariki." Lakini niliona kwamba mioyo imetindikiwa/imelemewa na mahangaiko ya maisha haya, na kwamba MUNGU na Neno Lake vimepuuzwa. {1T 151.2}
Nikaona ni rahisi ngamia kupita kwenye tundu la sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme. "Msijiwekee hazina duniani, ambapo nondo na kutu huharibu, na ambapo wezi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, ambapo nondo wala kutu haziharibu, na ambapo wezi hawavunji wala kuiba: maana hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako." {1T 151.3}

Niliona kwamba Ukweli unapowasilishwa, unapaswa kuwa katika nguvu na Roho. Kuwaleta watu kwenye hatua ya kukata shauri. Waoneshe umuhimu wa Ukweli - ni uzima au kifo. Kwa kuwa na bidii, vuta roho kutoka motoni. Lakini, loo, ni ushawishi mbaya kiasi gani ambao umewekwa na watu wanaodai kuwa wanamsubiri Bwana wao, na bado wanamiliki ardhi kubwa na ya kupendeza! Mashamba yamehubiri kwa sauti kubwa, ndiyo, kwa sauti kubwa zaidi, kuliko maneno, kwamba ulimwengu huu ndiyo nyumbani kwao. Siku mbaya imewekwa kando. Amani na usalama vinatawala. Lo, ushawishi unaofifia, ulioonyauka na unaodhuru! MUNGU huchukia mawazo ya kidunia. "Jing'atue, Jing'atue hapo- cut loose," yalikuwa maneno ya malaika. {1T 152.1}

Nilioneshwa kwamba wote wanapaswa kuwa na jicho moja kwa utukufu wa MUNGU. Wale wenye mali wamekuwa tayari kutoa udhuru kwa sababu ya mke na watoto. Lakini niliona kwamba MUNGU hawezi kuchezewa. Anapozungumza, lazima aheshimiwe. Ikiwa mke au watoto wanasimama njiani na kuzuia, wanapaswa kusema kama Yesu alivyomwambia Petro: "Nenda nyuma yangu, Shetani." Kwa nini mnanijaribu kumzuia MUNGU kwa kile ambacho ni haki Yake, halali Yake, na kuiharibu nafsi yangu? Kaza jicho lako katika utukufu wa MUNGU. {1T 152.2}

Niliona kwamba wengi watalazimika kujifunza maana ya kuwa Mkristo - kwamba siyo kwa jina; bali ni kuwa na nia ya Kristo, ikiyatii mapenzi ya MUNGU katika vitu vyote. Hasa vijana ambao hawajawahi kujua shida au taabu ni nini, ambao wana mapenzi yaliyokita mahali fulani kwa ukaidi, na hawayashushi au

hawapindishi mapenzi hayo kwa utukufu wa MUNGU, watakuwa na kazi kubwa ya kufanya. Wanaenda vizuri sana mpaka mapenzi yao yanapochokozwa, kisha wanakosa uwezo wa kujithibithi. Hawana mapenzi ya MUNGU mbele yao. Hawajifunzi jinsi wanavyoweza kumtukuza MUNGU, au kuendeleza kazi Yake, au kuwatendea wengine mema. Lakini ni ubinafsi, uchoyo, ubinafsi, unawezaje kuendekezwa? Dini kama hiyo haina thamani zaidi ya majani makavu. Wale wenye hiyo, watapimwa katika mizani na kuonekana wamepungua. {1T 152.3}

Mkristo wa kweli atapenda kungojea na kutazama mafundisho ya MUNGU na uongozi wa Roho wake. Lakini kwa wengi, dini ni mfumo au desturi tu. Utauwa muhimu unakosekana. Wengi huthubutu kusema, nitafanya hivi, au vile, au sitafanya hivi; na hofu ya kumkosea MUNGU haifikiriwi sana. Wale walioelezewa hivi, niliona, hawawezi kuingia mbinguni kama walivyo. Wanaweza kujifurahisha kwa kujidanganya kwamba wataokolewa, lakini MUNGU hana furaha nao. Maisha yao hayampendezi. Maombi yao ni chukizo kwake. {1T 152.4}

Kristo sasa anawaita: "Uwe na bidii na utubu." Anawahimiza kwa fadhili na kwa uaminifu kununua dhahabu, mavazi meupe na dawa ya macho. Wanaweza kuchagua kuwa wenye ari na bidii, na kushiriki kwa kiasi kikubwa wokovu, au kutapikwa kutoka kinywani mwa Bwana kama chukizo, na kutupwa kutoka Kwake. MUNGU hatawabeba daima au kuchukuliana nao. Yeye ni Mwenye huruma, lakini Roho Wake atahuzunishwa mbali kwa mara ya mwisho. Sauti tamu ya rehema haitasikika tena. Vidokezo vyake vya mwisho vya thamani vitakuwa vimekufa, na wale walioelezewa wataachwa katika njia zao wenyewe, kujazwa na matendo yao wenyewe. {1T 153.1}

Niliona kwamba wale wanaodai kuwa wanatazamia kuja kwa Bwana hawapaswi kuwa na roho ya uchoyo, ya ubahili, ya umaskini. Baadhi ya wale ambao wameitwa kuueleza Ukweli, na kuzichunga roho kama wale ambao wanapaswa kutoa hesabu, wamepoteza wakati muhimu sana kwa sababu ya kuokoa au kuhifadhi mali kidogo, wakati muda wao ulikuwa na thamani kubwa zaidi kuliko kile walichopata. Jambo hili halimpendezi MUNGU. Ni kweli kwamba kujali uchumi kunapaswa kuwepo (matumizi ya pesa kwa kujali uchumi ni muhimu), lakini kwa wengine jambo hili limetumiwa vibaya bila kitu kingine chochote zaidi ya kuongeza kwenye hazina zao mali, ambazo hivi karibuni zitakula nyama zao kama moto, isipokuwa kama mawakili waaminifu watasimamia mali za Bwana kwa usahihi. {1T 153.2}

## SURA YA 27

## VIJANA WATUNZA SABATO

Agosti 22, 1857, katika nyumba ya maombi huko Monterey, Michigan, nilipata maono kuwa wengi bado hawajasikia sauti ya Yesu, na ujumbe wa kuokoa haujashika roho na kufanya matengenezo maishani. Wengi wa vijana hawana roho ya Yesu. Upendo wa MUNGU haumo mioyoni mwao, kwa hivyo mateso yote ya asili hushikilia ushindi badala ya ROHO WA MUNGU na wokovu. {1T 154.1}

Wale wenye kuwa na dini ya Kweli ya Yesu hawataona aibu wala kuogopa kubeba msalaba mbele ya wale ambao wana uzoefu zaidi yao. Ikiwa watataka sana kuwa sahihi, basi watatamani msaada wote wawezao kuupata kutoka kwa Wakristo wazee. Kwa furaha watasaidiwa nao; na mioyo iliyopashwa moto na upendo kwa MUNGU haitazuiliwa na mambo hafifu ya kujinga katika mwendo wa Kikristo. Watasimulia vile ROHO WA MUNGU afanyavyo kazi ndani. Wataiimba, na kuiombea. Ni ukosefu wa dini, ukosefu wa maisha matakatifu, ndiyo unaowafanya vijana kurudi nyuma. Maisha yao yanawahukumu. Wanajua hawaishi kama Wakristo wanavyopaswa, kwa hivyo hawana ujasiri kwa MUNGU, au mbele ya kanisa. {1T 154.2}

Kwa nini vijana hujisikia huru zaidi wakati wazee wanapokuwa hawapo ni: kwa sababu wapo miongoni mwa watu wa aina yake. Kila mmoja anafikiria yeye ni mzuri kama mwenzake. Wote hawafikii kipimo, kwani wanafeli, lakini wanajipima wenyewe kwa wenyewe, na wanajilinganisha kati yao wenyewe, na kupuuza kiwango kamili na cha Kweli. Yesu ndiye Kielelezo cha Kweli. Maisha yake ya kujikana nafsi ni mfano wetu. {1T 154.3}

Niliangalia namna ambavyo mfano huo ulivyochukuliwa kwa kusomwa na kujifunzwa kwa udogo tu, jinsi ulivyoinuliwa kidogo mbele yao. Jinsi vijana wanavyoteseka kidogo, au wanajikana nafsi zao, kwa ajili dini yao! Kutoa dhabihu hakufikiriwi sana kati yao. Wanashindwa kabisa kuiga kielelezo katika suala hili. Niliona kuwa lugha ya maisha yao ni: ubinafsi lazima uridhishwe, kiburi lazima kihusike. Wanamsahau mtu ajuaye sikitiko aliyefahamiana na majonzi. Mateso ya Yesu Gethsemane, jasho Lake lililogeuka matone makubwa ya damu bustanini, taji iliyotengenezwa kwa miiba iliyotoboa paji Lake takatifu, haviwagusi. Wametiwa ganzi. Hisia zao zimekuwa butu, na wamepoteza hisia zote za kafara kuu iliyofanywa kwa ajili yao. Wanaweza kukaa na kusikiliza kisa cha msalaba, kusikia jinsi misumari ya kikatili ilivyopigiliwa kwenye mikono na miguu ya Mwana wa MUNGU, na bado isilete mguso wa kina kwenye moyo. {1T 155.1}

Malaika alisema: “Kama watu hawa wangeingizwa katika mji wa MUNGU, na kuambiwa uzuri na utukufu wake wote ni wao ili waufurahie milele, wasingekuwa na ufahamu wa jinsi urithi huo ulivyonunuliwa kwa thamani kubwa kwa ajili yao. Wasingeweza kamwe kutambua kina kisicho na mfano cha upendo wa Mwokozi. Hawajanywa kikombe, wala hawajabatizwa kwa ubatizo. Mbingu zingetiwa doa kama watu kama hao wangeishi hapo. Ni wale tu

walioshiriki mateso ya Mwana wa MUNGU, na waliotoka kwenye dhiki kuu, na walioyaosha mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo, ndio ambao wangeweza kufurahia utukufu usioweza kuelezeka na uzuri usiyopimika wa mbinguni." {1T 155.2}

Uhitaji wa maandalizi haya muhimu utawafungia nje sehemu kubwa zaidi ya wale vijana wanaojidai [kuwa Wakristo], kwani hawatafanya kazi kwa juhudi na bidii ya kutosha kupata raha hiyo inayobaki kwa watu wa MUNGU. Hawataungama dhambi zao kwa uaminifu, ili waweze kusamehewa na kufutiwa dhambi zao. Dhambi hizi kwa muda mfupi zitafunuliwa kulingana na ukubwa wake ulivyo. Jicho la MUNGU halisinzii. Yeye Anajua kila dhambi ambayo imefichwa kutoka kwa macho ya mwanadamu anayekufa. Wenye hatia wanajua ni dhambi gani za kuungama ili kusudi roho zao ziweze kuwa safi mbele za MUNGU. Yesu sasa anawapatia nafasi ya kuungama, kutubu kwa unyenyekevu wa kina, na kutakasa maisha yao kwa kutii na kuuishi Ukweli. Sasa ni wakati wa makosa kusahihishwa na dhambi kuungamwa, la sivyo watatokea kama wenye dhambi siku ya ghadhabu ya MUNGU. {1T 155.3}

Wazazi kwa kawaida huweka tumaini na ujasiri mkubwa sana kwa watoto wao; kwa kuwa mara nyingi wazazi wanapokuwa wanazungumza nao kwa faragha, watoto huwa katika uovu uliofichika. Wazazi, wachungeni watoto wenu kwa uangalizi wenye wivu. Muwasihi, wasisitizieni, muwakaripie, na muwashauri muinukapo na mketipo, mtokapo na muingiapo, mstari kwa mstari, hapa kidogo, na pale kidogo. Watiishe watoto wenu wakiwa bado wadogo. Jambo hili limepuuzwa kwa uchungu na wazazi wengi. Hawalichukulii kwa msimamo ulio imara na wa makusudi kama ambavyo wangepaswa kuhusiana na watoto wao. Wanawaruhusu kuwa kama ulimwengu, wapende mavazi, na washirikiane na wale wanaochukia Ukweli na ambao ushawishi wao ni wenye sumu. Kwa kufanya hivyo wanahimiza katika watoto wao tabia ya kidunia. {1T 156.1}

Niliona kwamba kila wakati kunapaswa kuwa na kanuni iliyowekwa na wazazi wa Kikristo yenye muungano katika serikali au usimamizi wa watoto wao. Kuna kosa katika suala hili kwa baadhi ya wazazi – ukosefu wa umoja kati ya baba na mama- hakuna muungano. Kosa wakati mwingine lipo upande wa baba, lakini mara nyingi ni upande wa mama. Mama mwenye upendo huwabembeleza, huwaendekeza na kuwadekesha watoto wake (wanakuwa vipenzi-pets). Kazi ya baba humfanya awe mbali na nyumbani mara nyingi, na kutoka katika jamii ya watoto wake. Ushawishi wa mama ndiyo wenye kunena. Mfano wake hufanya mengi katika kuunda tabia ya watoto. {1T 156.2}

Baadhi ya akina mama wanaowapenda watoto wao huruhusu makosa kwa watoto wao jambo ambalo halingepaswa kuruhusiwa kwao hata kwa kitambo. Makosa ya watoto mara nyingine hufichwa ili baba asiyajue. Mambo ya mavazi au anasa kadhaa zingine hutolewa na mama kwa watoto akiamini kuwa baba

hatajua chochote juu yake, maana kama angejua angekemea kuhusiana na mambo haya. {1T 156.3}

Hapa somo la udanganyifu linafundishwa kwa ufanisi kwa watoto. Halafu ikiwa baba atagundua makosa haya, visingizio hutolewa ambapo ukweli nusu tu husemwa. Mama hana moyo uliofunguka. Hazingatii kama ambavyo angepaswa kuwa kwamba baba aana maslahi ya watoto kama mama, na kwamba hapaswi kutojulishwa makosa na makandokando ambayo yanapaswa kusahihishwa ndani yao wakiwa wadogo-baba asiachwe bila kujua. Mambo yamefunikwa. Watoto wanajua  kwamba kuna ukosefu wa umoja kwa wazazi wao, na hiyo ina athari zake. Wakiwa bado wadogo, watoto huanza kudanganya, kuficha, na kusema mambo kwa nuru iliyo tofauti na uhalisia kwa mama yao, na vilevile kwa baba yao. Kutia chumvi mambo huwa tabia, na uongo huzungumzwa kwa namna isiyosadikisha au bila kukemea/kuhusisha dhamiri. {1T 157.1}

Makosa haya huanza kwa mama kumficha baba ambaye ana moyo wa kutaka kuyajua [mambo ya watoto wake] sawa na vile mama anavyotaka kujua katika tabia wanazounda watoto wao. Baba alipaswa kuambiwa mambo yanayoendelea bila kuficha-kwa uhuru. Yote yangewekwa wazi mbele zake. Lakini njia iliyo kinyume, iliyochukuliwa kuficha makosa ya watoto, ilihimiza ndani yao tabia ya kudanganya, na ukosefu wa ukweli na uaminifu. {1T 157.2}

Tumaini pekee la watoto hawa, iwe wanaigiza mambo ya dini au la, ni kuongoka kikamilifu. Tabia yao nzima ni lazima ibadilike. Wewe mama usijifikiria, wakati unapofundisha wanao, unatambua kuwa uzoefu wao wote wa kidini unaathiriwa na mafundisho yao walipokuwa wadogo? Watiishe wakiwa wadogo; wafundishe kujitiisha kwako, na kwa urahisi zaidi watajifunza kutoa utii kwa matakwa ya MUNGU. Watie moyo kuwa na tabia ya ukweli, na uaminifu. Hebu wasiwe kamwe na hali ya kutilia shaka uaminifu wako na ukweli wako halisi. {1T 157.3}

Niliona kwamba vijana wanakiri [kuwa Wakristo], lakini hawafurahii nguvu ya MUNGU  ya kuokoa. Hawana dini, wanapungukiwa na wokovu. Na, oh, hayo maneno ya ovyo, na yasiyo na faida wanayozungumza! Kuna kumbukumbu ya kuaminika na ya uaminifu iliyotunzwa kwa ajili yao, na wanadamu watahukumiwa kulingana na matendo yaliyofanywa mwilini. Marafiki wadogo, matendo yenu na maneno yenu yasiyo na maana yameandikwa kwenye kitabu. Mazungumzo yenu hayakuwa juu ya mambo ya milele, bali juu ya mazungumzo haya, yale, na mengine – ya kawaida, ya kidunia ambayo Wakristo hawapaswi kushiriki. Yote haya yameandikwa kwenye kitabu. {1T 157.4}

Niliona kwamba isipokuwa kama kuna mabadiliko kamili kwa vijana, na uongofu kamili, kuna kukata tamaa ya kwenda mbinguni. Kutokana na yale niliyooneshwa, hakuna zaidi ya nusu ya vijana wanaodai wana dini na Ukweli ambao wameongoka kikweli kweli. Kama wangekuwa wameongoka wangezaa

matunda kwa utukufu wa MUNGU. Wengi wanaegemea juu ya tumaini la kudhaniwa lisilo na msingi wa kweli. Chemchemi haijasafishwa, kwa hivyo mifereji inayotokana na chemchemi hiyo siyo safi. Safisha chemchemi, na mifereji itakuwa safi. Ikiwa moyo uko sawa, maneno yako, mavazi yako, na matendo yako, yote yatakuwa sawa. Kuna upungufu wa utauwa wa kweli. Mimi sitamvunjia heshima Mwalimu wangu kiasi cha kukubali kuwa mtu asiyejali, mwenye dharau, na asiye na maombi ni Mkristo. Hapana; Mkristo ana ushindi juu ya mateso yake, na juu ya tamaa zake. Kuna dawa kwa roho inayougua dhambi. Dawa hiyo iko kwa Yesu. Mwokozi wa Thamani! Neema Yake inatosha kwa yule aliye dhaifu zaidi; na mwenye nguvu lazima pia awe na neema Yake au la sivyo aangamie. {1T 158.1}

Niliona jinsi neema hii inavyoweza kupatikana. Nenda chumbani kwako, na hapo ukiwa peke yako msihi MUNGU : "Ee MUNGU, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu." Uwe mwenye dhati na mwenye bidii, uwe mkweli. Maombi ya bidii yanafaa na yana nguvu sana. Kama Yakobo, shindana katika maombi. Omboleza. Yesu, bustanini, alitokwa na matone makubwa ya damu; lazima ufanye juhudi. Usitoke chumbani kwako hadi umejisikia kuwa imara katika MUNGU ; ndipo ukeshe; na kwa kadri unavyoendelea kukesha na kuomba unaweza kutawala vizuizi hivi vya uovu, na neema ya MUNGU inaweza na itaonekana ndani yako. {1T 158.2}

MUNGU aniepushe nisikome kukuonya. Vijana marafiki, mtafuteni Bwana kwa mioyo yenu yote. Njooni kwa bidii, na mnapohisi kwa dhati kwamba bila msaada wa MUNGU unapotea, wakati mnapomtamani [Bwana] kama kulungu atamanivyo vijito vya maji, ndipo Bwana atawatia nguvu haraka. Ndipo amani yenu itapita ufahamu wote. Kama mnatarajia wokovu, lazima muombe. Chukueni muda. Msiwe na haraka na uzembe katika maombi yenu. Mwombeni MUNGU afanye ndani yenu matengenezo kamili, ili matunda ya Roho Wake yakae ndani yenu, nanyi muangaze kama taa ulimwenguni. Msiwe kikwazo au laana kwa kazi ya MUNGU; mnaweza kuwa msaada, na mbaraka. Je! Shetani anakwambia kuwa huwezi kufurahia wokovu, ulio kamili na wa bure? Msimwamini kabisa. {1T 158.3}

Niliona ya kwamba ni upendeleo wa kila Mkristo kufurahia ushawishi wa ndani wa ROHO WA MUNGU. Amani tamu ya amani ya mbinguni itatawala akili, na utapenda kutafakari juu ya MUNGU na mbingu. Utafanya karamu juu ya ahadi tukufu za Neno Lake. Lakini utambue kwanza ya kwamba ndipo tu wewe umeanza mwendo wa Kikristo. Tambua kwamba hatua za awali ndipo tu zinachukuliwa katika njia ya uzima wa milele. Usidanganyike. Ninawahofia ninyi, ndio, najua, kwamba wengi wenu hamjui dini ni nini. Mmehisi msisimko, na mihemko, lakini hamjawahi kuiona dhambi katika ukubwa na ubaya wake. Hamjawahi kuhisi hali yenu ambayo haijashughulikiwa na na kutoka kwenye njia zenu mbaya na zenye huzuni kali. Hamjawahi kufa kwa ulimwengu. Bado mnapenda raha zake; mnapenda kushiriki mazungumzo juu ya mambo ya

kidunia. Lakini Ukweli wa MUNGU unapoingizwa, hamna la kusema/kuchangia. Kwa nini mnakaa kimya sana? Kwa nini mnazungumza sana juu ya vitu vya kidunia, na huku mkiwa kimya juu ya somo ambalo linapaswa kujaliwa sana – mada ambayo inapaswa kushirikisha roho zenu zote? Kweli ya MUNGU haikai ndani yenu. {1T 159.1}

Niliona kuwa wengi ni waadilifu katika madai yao, wakati ndani humo kuna ufisadi. Msijidanganye wenyewe, nyie mnaojifanya kuwa mnakiri kuwa ni wenye dini huku mkiwa wenye mioyo ya uongo. MUNGU huangalia moyo. "Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake." Niliona ulimwengu ukiwa katika moyo kama hiyo, niliona, uko katika moyo wa vile, lakini dini ya Yesu haipo. Ikiwa wale wanaojidai kuwa ni Wakristo wanampenda Yesu zaidi kuliko wanavyoupenda ulimwengu, watapenda kumzungumzia Yeye, Rafiki yao mkubwa, ambaye mapenzi yao ya hali ya juu yamejikita kwake. Aliwapa msaada walipohisi hali yao ya kupotea na kuangamia. Walipochoka na kulemewa na dhambi, walimgeukia Yeye. Naye Aliondoa mzigo wao wa hatia na dhambi, akaondoa huzuni na maombolezo yao, na akageuza mkondo wote wa mapenzi yao. Vitu walivyopenda hapo awali, sasa wanavichukia; na vitu ambavyo walivichukia hapo zamani, sasa wanavipenda. {1T 159.2}

Je! Mabadiliko haya makubwa yametokea ndani yako? Usijidanganye. Kamwe nisingetaja Jina la Kristo, vinginevyo ningempa moyo wangu wote, na mapenzi yangu ambayo hayajagawanyika. Tunapaswa kuhisi shukrani ya dhati kabisa kwamba Yesu atakubali sadaka hii. Yeye Anadai kila tulicho nacho. Tunapoitwa kujitoa kulingana na madai yake, na kutoa yote, ndipo atakapotuzungushia mikono Yake ya rehema. Lakini tunatoa nini tunapotoa yote? Nafsi iliyochafuliwa na dhambi kwa Yesu ili aitakase, kuisafisha kwa huruma Yake, na kuokoa kuiokoa kutoka mautini kwa upendo Wake usio na cha kulinganishwa. Na bado niliona kuwa wengine waliona vigumu kutoa yote. Ninaaibika ninaposikia jambo hili likitamkwa, ninaaibika ninapoliandika. {1T 160.1}

Je! Unazungumza kuhusu kujikana nafsi na kujinyima? Je! Kristo alitoa nini kwa ajili yetu? Unapodhani kuwa ni jambo gumu Kristo kutaka kila kitu, nenda Kalvari, na lia juu ya wazo kama hilo. Tazama mikono na miguu ya Mkombozi wako iliyochanwa kwa misumari ya kikatili ili upate kuoshwa kutoka dhambini na damu Yake Mwenyewe! {1T 160.2}

Wale wanaohisi upendo unaochochea wa MUNGU hawaulizi ni kiasi gani kdigo kinaweza kutolewa na bado waweze kupata thawabu ya mbinguni; hawaombi ili kufikia viwango vya chini sana na bado waende mbinguni, lakini wanalenga kufikia uwiano mkamilifu wa nia na Mkombozi wao. Kwa hamu kubwa hujitolea vyote, na hudhihirisha bidii sawia na thamani ya kitu ambacho wanakitafuta. Lengo ni nini? Kutokufa, na uzima wa milele. {1T 160.3}

Marafiki wadogo, wengi wenu mnadanganywa kwa namna inayotia uchungu. Mmekuwa mkiridhishwa na mambo yaliyo pungufu na dini safi na isiyo na taka.

Nataka niwaamshe. Malaika wa MUNGU wanajaribu kuwaamsha. Oh, kwamba Kweli muhimu za Neno la MUNGU zipate kuwaamsha ili muione hatari yenu, na iwaongoze katika kujichunguza ninyi wenyewe kikamilifu! Mioyo yenu bado ni ya tamaa za mwili. Hamko chini ya sheria ya MUNGU, na kwa kweli hamwezi. Mioyo hii ya tamaa za kimwili lazima ibadilishwe, na ndipo mtaona uzuri kama huo katika utakatifu kiasi kwamba utamtamani kama kulungu atamanivyo vijito vya maji. Ndipo utampenda MUNGU na kuipenda sheria Yake. Ndipo nira ya Kristo itakuwa rahisi na nira/mzigo Wake utakuwa mwepesi. Ingawa utapata majaribu, lakini majaribio haya, yanayobebwa vizuri, yataifanya njia kuwa ya thamani zaidi. Urithi wa kutokufa ni kwa Mkristo anayejikana mwenyewe. {1T 160.4}

Niliona Mkristo hapaswi kuweka kwenye kiwango cha juu sana, au kuitegemea sana, furaha inayoendeshwa na hisia. Hisia hizi siyo kiongozi/miongozo ya kweli kila wakati. Inapaswa kuwa somo la kila Mkristo kumtumikia MUNGU kwa kufuata kanuni, na siyo kutawaliwa na hisia. Kwa kufanya hivyo, imani italetwa katika mazoezi/matendo, na itaongezeka. Nilioneshwa kwamba ikiwa Mkristo ataishi maisha ya unyenyekevu, na ya kujitoa, matokeo yake yatakuwa amani na furaha katika Bwana. Lakini furaha kubwa itakayopatikana itakuwa katika kuwafanyia wengine mema, na katika kuwafanya wengine wafurahi. Furaha kama hiyo itakuwa ya kudumu. {1T 161.1}

Wengi wa vijana hawana kanuni ya kudumu katika kumtumikia MUNGU. Hawaifanyii mazoezi imani. Wanazama chini ya kila wingu. Hawana nguvu ya kustahimili. Hawakui katika neema. Wanaonekana kuzishika amri za MUNGU. Wanafanya mtindo wa maombi ya urasmi hapa na pale na kuitwa Wakristo. Wazazi wao wana mashaka sana juu yao hivyo wanakubali chochote kinachoonekana kuwa kizuri, na hawafanyi kazi pamoja nao, na kuwafundisha kwamba akili ya tamaa ya mwili ni lazima ife. Wanawahimiza kuja pamoja nao na kuchukua nafasi zao; lakini wanashindwa kuwaongoza kuichunguza mioyo yao wenyewe kwa bidii, kujichunguza wao wenyewe, na kuhesabu gharama ya kuwa Mkristo. Matokeo yake ni kwamba, vijana hudai kuwa ni Wakristo bila kujaribu nia zao vya kutosha. {1T 161.2}

Shahidi Mwaminifu anasema: “Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu.” Shetani yuko tayari uwe Mkristo wa jina, kwani unaweza kutimiza kusudi lake vizuri zaidi. Ikiwa una umbo na siyo utauwa wa kweli, anaweza kukutumia kudanganya wengine kwa njia ile ile unayojidanganya mwenyewe. Nafsi zingine masikini zitakuangalia wewe, badala ya kutazama kiwango cha Biblia, na hazitakuja juu zaidi. Watakuwa kwenye kiwango cha uzuri ulichonacho, nao wataridhika. {1T 162.1}

Vijana mara nyingi huhimizwa kutimiza wajibu, kuzungumza au kuomba katika mkutano; wanahimizwa kufia kiburi. Wanahimizwa katika kila hatua. Dini kama hiyo haina thamani yoyote. Wacha moyo wa mwili ubadilishwe, na haitakuwa

kazi ngumu kama hiyo, enyi enyi wenye mioyo baridi, mnaojidai kumtumikia MUNGU. Upendo wote wa mavazi na kiburi cha kuonekana vitaondoka. Wakati ambao unatumia kusimama mbele ya kioo kuandaa nywele kufurahisha jicho, unapaswa kutumiwa kwa maombi na kuuchunguza moyo. Hakutakuwa na nafasi ya mapambo ya nje katika moyo uliotakaswa; lakini kutakuwa na bidii, na kuhangaika katika kutafuta mapambo ya ndani, neema za Kikristo – matunda ya ROHO WA MUNGU. {1T 162.2}

Mtume anasema: "Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usiyoonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za MUNGU." {1T 162.3}

Tiisha akili ya tamaa ya mwili, rekebisha maisha, na umbile hili linalokufa halitaabudiwa. Ikiwa moyo umebadilishwa, itaonekana katika sura ya nje. Ikiwa Kristo Yuko ndani yetu tumaini la utukufu, tutagundua tunu zisizo na kifani ndani Yake hata roho itapendezwa. Itashikamana Naye, kuchagua kumpenda, na kwa kumsifu, ubinafsi utasahauliwa. Yesu atatukuzwa na kuabudiwa. Lakini madai ya maneno tu, bila upendo huu wa kina, ni mazungumzo tu, utaratibu mkavu, na uchovu mzito. Wengi wenu mnaweza kushika dhana ya dini kichwani, dini ya nje, wakati moyo haujasafishwa. MUNGU huangalia moyo; "Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele Zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake Yeye aliye na mambo yetu." Je! Ataridhika na chochote isipokuwa Ukweli katika sehemu za ndani? Kila nafsi iliyoongoka kweli itakuwa na alama zisizo na shaka ambazo akili ya tamaa za mwili imeshikwa. {1T 162.4}

Nasema wazi. Sidhani kama hii itamkatisha tamaa Mkristo wa kweli; na sitaki yeyote kati yenu aufikie wakati wa taabu akiwa hana tumaini lenye msingi mzuri kwa Mkombozi wake. Amua kuijua hali mbaya ya kesi yako. Hakikisha kama unao urithi kule juu. Shughulika kiukweli na roho yako mwenyewe (jiambie kweli). Kumbuka kuwa kanisa lisilo na hila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo, ndilo Yesu ataliwasilisha kwa Baba Yake. {1T 163.1}

Je! Unajuaje kuwa unakubaliwa na MUNGU ? Jifunze Neno Lake kwa maombi. Usiweke kando kwa ajili ya kitabu kingine chochote. Kitabu hiki kinasadikisha dhambi. Kinadhihirisha wazi njia ya wokovu. Kinatukutanisha na zawadi safi na yenye utukufu. Kinakufunulia wewe Mwokozi mkamilifu, na kinakufundisha kwamba kupitia rehema Yake isiyo na mipaka peke yake, wewe unaweza kutarajia wokovu. {1T 163.2}

Usipuuze maombi ya siri, kwani ndiyo roho ya dini. Kwa maombi ya dhati na bidii, na yenye ari, omba usafi wa roho. Omba kwa bidii, kwa shauku, kadri uwezavyo kama vile maisha yako hatarini kufa, kana kwamba yapo hatarini. Kaa mbele za MUNGU mpaka matamanio yasiyoelezeka yazaliwe ndani yako

kwa ajili ya wokovu, na ushahidi mtamu uwe umepatikana kuhusiana na dhambi iliyosamehewa. {1T 163.3}

Tumaini la uzima wa milele halipaswi kupokelewa katika mazingira madogo. Hili ni somo linalopaswa kusuluhishwa baina ya MUNGU na roho yako mwenyewe – na kusuluhishwa milele. Tumaini la kudhaniwa tu, na lisilo na ziada, litathibitisha uharibifu wako. Kwa kuwa utapaswa kusimama au kuanguka kulingana na Neno la MUNGU, ni kwa Neno hilo hilo lazima utafute ushuhuda katika tatizo lako. Hapo ndipo uwezapo kuona kile kinachohitajika kwako ili uwe Mkristo. Usizitupe silaha zako, au kuondoka kwenye uwanja wa vita hadi utakapopata ushindi, na ushinde katika Mkombozi wako. {1T 163.4}

## SURA YA 28

## MAJARIBU YA KANISA

Mtazamo ufuatao ulitolewa Ulysses, Pennsylvania, Julai 6, 1857. Inahusiana na namna vitu vilivyokuwa katika ----- na maeneo mengine huko New York. {1T 164.1}

Kumekuwa na majaribu mengi ya kanisa miongoni mwa ndugu katika Jimbo la New York, ambayo MUNGU hajahusika nayo hata kidogo, kwamba kanisa limepoteza nguvu yake, na halijui jinsi ya kuipata tena. Upendo kati ya ndugu umetoweka, na roho ya kutafuta makosa na kushtaki imeenea. Imechukuliwa kuwa fadhila kusaka kila kitu kinachoonekana kibaya juu, na kukifanya kionekane kibaya zaidi kuliko kilivyokuwa. Tumbo la huruma linaloonea shauku kwa upendo na huruma kwa ajili ya ndugu, halijakuwepo. Dini ya wengine imekuwa ni kutafuta makosa ya wengine tu, wakiokota kila chenye sura ya mbaya, hadi hisia nzuri za nafsi zikome. Akili ni lazima iinuliwe ili ikae juu ya vielelezo vya milele, mbingu, hazina zake, na utukufu wake, na inapaswa kuuchukua utakaso mtamu na mtakatifu katika Ukweli wa Biblia. Akili inapaswa kupenda kula juu ya ahadi za thamani ambazo Neno la MUNGU linatoa, kupata faraja kutoka kwao, na kuinuliwa juu ya vitu visivyo vya maana kwa vitu vizito vya milele. {1T 164.2}

Lakini, oh, akili imetumiwa tofauti kiasi gani! Kuokota majani makavu tu (kuiachia akili iende kokote tu!) Mikutano ya kanisa, kwa namna ilivyokuwa inafanyika, imekuwa laana hai kwa wengi huko New York. Majaribu haya yaliyotengenezwa yametoa uhuru kamili kwa utafutaji mbaya. Wivu umelishwa. Chuki imekuwepo, lakini hawakuijua. Wazo baya limekuwa katika mawazo ya wengine, kukemea bila upendo, kuwahukumu wengine kwa maoni yao juu ya kile wanachoamini kipo sawa, na kutowavumilia, lakini kuwakandamiza kwa uzito unaowasaga/uteketezao. {1T 164.3}

Niliona kwamba wengi huko New York wamekuwa wakisumbuka kuhusiana na ndugu zao, wakiwaadibisha ili wawe wanyofu, hata wamepuuza mioyo yao wenyewe. Wanaogopa sana kwamba ndugu zao hawatakuwa na bidii ya kutubu, hadi wanasahau kuwa wao wenyewe wana makosa ambayo yanapaswa kusahihishwa. Mioyo yao wenyewe haijatakaswa, ila wanajaribu kuwasahihisha ndugu zao. Sasa njia pekee ambayo ndugu na dada huko New York wanaweza kuinuka ni kwa kila mmoja kushughulikia tatizo lake binafsi, na kuweka moyo wake mwenyewe kwenye utaratibu. Ikiwa dhambi iko wazi kwa ndugu, usiipumulie kwa mwingine, lakini kwa upendo kwa moyo wa kidugu, na moyo uliojaa huruma, na matumbo ya huruma, mwambie kosa, kisha liache hilo jambo kwake na mikononi mwa Bwana. Wewe umetimiza wajibu wako. Haupaswi kutoa hukumu. {1T 165.1}

Limefanywa kuwa jambo jepesi sana kumtawala na kumdhibiti ndugu, kumhukumu, na kumweka chini ya hukumu. Kumekuwa na bidii kwa ajili ya MUNGU, lakini siyo kulingana na ujuzi. Ikiwa kila mmoja angeweka moyo wake mwenyewe katika utaratibu, wakati ndugu wakutanapo pamoja ushuhuda wao ungekuwa tayari na ungetoka katika roho kamili, na watu walio karibu na ambao hawauamini Ukweli, wangeguswa, na ndipo Ukweli huo ungeongea. Nao utakuwa na ushawishi. {1T 165.2}

Niliona kwamba kanisa huko New York linaweza kuongezeka. Kila mmoja aishikilie kazi, awe na bidii na kutubu; na baada ya makosa yote yanayofahamika kusahihishwa, basi amini kwamba MUNGU amekupokea. Usiende na kulia tena, lakini mchukulie MUNGU katika Neno Lake, mtafute kwa uadilifu, uwe na bidii na utubu; na baada ya makosa yote yanayojulikana kusahihishwa, basi amini kwamba MUNGU anakukubali. Usiende kuomboleza, lakini mchukulie MUNGU kama asemavyo kwenye Neno Lake. Mtafute kwa bidii, na amini kwamba Yeye anakupokea. Sehemu ya kazi yetu ni kuamini. Yeye ni Mwaminifu ambaye ameahidi. Panda juu kwa imani. {1T 165.3}

Ndugu wanaweza kupanda [kwa idadi] New York na pia katika maeneo mengine; na wanaweza kunywa wokovu wa MUNGU. Wanaweza kusonga mbele kwa uelewa, na kila mmoja akiwa na uzoefu wake mwenyewe katika ujumbe huu wa Shahidi wa Kweli kwa Walaodikia. Kanisa linahisi kuwa liko chini, lakini halijui jinsi ya kuinuka. Nia ya wengine inaweza kuwa nzuri sana; wanaweza kukiri; hata hivyo nikaona kwamba wanaangaliwa kwa tuhuma, na wanafanywa wakosaji kwa neno, mpaka wasiwe na uhuru, na wokovu. Hawathubutu kuonyesha hisia rahisi za moyo, kwa sababu wanaangaliwa. Ni furaha ya MUNGU kwamba watu Wake wamuogope, na wawe na ujasiri mbele yao wenyewe kwa wenyewe. {1T 165.4}

Niliona kwamba wengi wamefaidika na kile ambacho MUNGU ameonesha juu ya dhambi na makosa ya wengine. Wamechukua maana iliyokithiri ya kile kilichooneshwa kwenye maono, na kisha wakakandamiza mpaka imekuwa na

tabia ya kudhoofisha imani ya wengi kwa kile ambacho MUNGU ameonesha, na pia kukatisha tamaa na kuvunja moyo kanisa. Kwa huruma nyororo ndugu ashughulike na ndugu. Kwa unyeti anapaswa kushughulikia hisia. Ni kazi nzuri na muhimu zaidi ambayo imewahi kufanyika, kugusa makosa ya mwingine. Kwa unyenyekevu wa kina ndugu anapaswa kufanya hivi, akizingatia udhaifu wake mwenyewe, asije akajaribiwa pia. {1T 166.1}

Nimeona dhabihu kubwa ambayo Yesu alitoa kumkomboa mwanadamu. Hakuyachukulia maisha yake mwenyewe kuwa bora zaidi kuweza kujitoa. Yesu alisema: “Pendaneni, kama vile mimi nilivyowapenda ninyi.” Je! Unahisi, ndugu anapokosea, kwamba unaweza kutoa maisha yako kumwokoa? Ikiwa unajisikia hivi, na unaweza kumwendea na kubadilisha moyo wake; basi wewe ndiye wa kumtembelea tu huyo kaka. Lakini ni jambo la kuhuzunisha kwamba wengi wanaodai kuwa ndugu, hawako tayari kutoa muhanga maoni au maamuzi yao yoyote yale ili kumwokoa ndugu. Kuna upendo mdogo kwa kila mmoja. Roho ya uchoyo/ubinafsi hudhihirika. {1T 166.2}

Kukata tamaa kumelikumba kanisa. Wamekuwa wakipenda ulimwengu, wakipenda mashamba yao, ng'ombe wao, nk. Sasa Yesu anawaita waachane na mambo hayo (wakate kamba na vitu hivyo), waweke hazina mbinguni, wanunue dhahabu, mavazi meupe na dawa ya macho. Hazina za thamani ni hizi. Watazipata kutoka kwa Yeye aliye mmiliki mlango wa kuingia katika ufalme wa MUNGU. {1T 166.3}

Watu wa MUNGU lazima wasonge mbele huku wakiwa na uelewa. Hawapaswi kuridhika mpaka kila dhambi inayojulikana ikiriwe; basi ni haki na wajibu wao kuamini kwamba Yesu anawakubali. Hawapaswi kusonga kupitia kwenye giza na kupata ushindi kwa ajili yao ili wapate kuufurahia. Furaha ya aina hiyo itadumu hadi mkutano mwingine unapofungwa. Lakini MUNGU anapaswa kutumikiwa kutoka kwa kanuni badala ya hisia. Asubuhi na usiku pata ushindi kwa ajili yako mwenyewe kwenye familia yako mwenyewe. Usiruhusu kazi yako ya kila siku ikuzuie kushiriki jambo hili. Chukua muda wa kuomba, na unapoomba, amini kwamba MUNGU anakusikia. Kuwa na imani iliyochanganywa na maombi yako. Huenda usisikie jibu lako la mara moja kila wakati unapoomba; lakini basi utambue imani inajaribiwa. Unapimwa ili kuona kwamba utamtegemea MUNGU, na ikiwa unayo imani hai, inayodumu. “Yeye ni mwaminifu ambaye amewaita, Naye atafanya.” Tembea juu ya ubao mwembamba wa imani. Tumainia yote juu ya ahadi za Bwana. Mtumaini MUNGU gizani. Huo ni wakati wa kuwa na imani. Lakini mara nyingi unaruhusu hisia zikutawale. Unatafuta kustahili ndani yako mwenyewe wakati hauhisi faraja ya ROHO WA MUNGU, na unakata tamaa kwa sababu hauwezi kuipata. Haumtumaini Yesu vya kutosha, Yesu wa thamani. Hauufanyi sifa na stahiki Zake kuwa yote, katika yote. Yoyote mazuri unayoweza kufanya hayastahilishi upendeleo wa MUNGU. Ni stahiki za Yesu ndizo mbazo zitakuokoa, damu Yake ndiyo itakayokuosha. Lakini

wewe una juhudi unayotakiwa kuifanya. Lazima ufanye kile unachoweza kwa upande wako. Kuwa na bidii na kutubu, kisha uamini. {1T 167.1}

Usiunganishe imani na hisia pamoja. Hivyo ni vitu viwili tofauti. Imani ni juu yetu kuifanyia mazoezi. Tumepewa imani ili tuifanyie mazoezi. Imani hii ni lazima tuishike kupitia mazoezi. Amini, amini. Acha imani yako ichukue baraka, na ni ya kwako. Hisia zako hazina uhusiano wowote na imani hii. Imani inapoleta baraka moyoni mwako, na unafurahi katika baraka, hiyo siyo imani tena, bali ni hisia. {1T 167.2}

Watu wa MUNGU huko New York lazima wainuke kwa uthabiti, na watoke gizani, na kuacha nuru yao iangaze. Wanasimama katika njia ya kazi ya MUNGU [wakiizuia kazi]. Lazima waache ujumbe wa malaika wa tatu ufanye kazi yake mioyoni mwao. Ndugu zangu, MUNGU anadharauliwa na maombi yenu marefu na yasiyo na imani. Angalia mbali kutoka kwenye kutostahili kwako, na umwinue Yesu. Ongea juu ya imani, juu ya nuru, na juu ya mbingu, na utakuwa na imani, nuru, na upendo, na amani na furaha katika ROHO MTAKATIFU. {1T 167.3}

## SURA YA 29

## “JIHADHARINI”

Ifuatayo ilielekezwa kwa ndugu wawili huko -----; lakini inatumika kwa wengi, hivyo imetolewa hapa kwa faida ya kanisa: {1T 168.1}

Ndugu Wapendwa: Katika maono niliyopewa mahali pako, nilioneshwa jambo fulani kukuhusiana na nyie wote wawili. Malaika alisonda kidole kwako, akirudia rudia maneno haya: “Basi, jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafula, kama mtego unasavyo.” {1T 168.2}

Niliona kwamba ninyi nyote wawili mna mgogoro mkubwa mbele yenu; mtakuwa na vita ya mara kwa mara ili kuiondoa dunia hii mioyoni mwenu, kwani mnaipenda. Funzo kubwa kwako sasa lazima iwe jinsi ya kumpenda Yesu na huduma Yake bora kuliko ulimwengu. Ikiwa unapenda ulimwengu zaidi, kazi zako zitashuhudia ukweli. Ikiwa unampenda Yesu na huduma Yake zaidi, kazi zako zitashuhudia ukweli huo pia. Niliona kwamba macho ya wengi katika ulimwengu huu yako juu yako. Wengi watafurahia kuanguka kwako, wengine wanafurahi kwa maendeleo yako. Shetani na malaika wabaya watawasilisha utukufu wa falme za ulimwengu huu. Ikiwa utamwabudu, au kuabudu hazina ya ulimwengu, ataiinua katika kila nuru ili kukuvutia na kukuongoza kupenda na kuabudu. {1T 168.3}

Yesu na malaika zako walinzi/walezi wanakuelekeza ng’ambo ya shamba lako, ng'ombe wako, na hazina yako ya kidunia, kwenye ufalme wa mbinguni, kwenye

urithi wa milele, kwenye jambo la milele katika ufalme wa utukufu. Malaika alisema: “Ni lazima ufe kwa ulimwengu huu.” “Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake.” {1T 168.4}

Niliona kwamba ikiwa, katika majaliwa ya MUNGU, utajiri umepatikana, hakuna dhambi kuumiliki; na ikiwa hakuna fursa zinazojitokeza kutumia mali hii kuendeleza maswala ya MUNGU, bado hakuna dhambi katika kuimiliki. Lakini ikiwa fursa zinawasilishwa kwa ndugu kutumia mali zao kwa utukufu wa MUNGU na kuendeleza kazi Yake, nao wakizuia, itakuwa kosa kwao na njia ya kujikwaa. Siku ya dhiki walichojilimbikizia kama hazina kitakuwa kosa kwao. Hivyo fursa zote za kuitumia mali hiyo kwa utukufu wa MUNGU zitakuwa zimepita, na kwa maumivu ya moyo wataitupa mali hiyo kwa fuko na popo. Dhahabu yao na fedha zao haziwezi kuwaokoa katika siku hiyo. Itawaangukia kwa uzito mkubwa, na kwamba hesabu lazima itolewe juu ya uwakili wao, ili ijulikane ni matumizi gani wameyatumia kwa pesa za Bwana wao. Kujipenda wenyewe kuliwafanya waamini kwamba mali yote ni yao wenyewe, na kwamba wangekuwa nayo yote; lakini wanahisi kwa uchungu na kuelewa, kwamba mali zao zilikopeshwa kwao tu na MUNGU, ili zirudishwe kwa njia ya kuzitumia kuendeleza kazi yake. Utajiri wao uliwadanganya. Walijisikia maskini na kuishi kwa ajili yao wenyewe, na mwishowe watatambua kuwa sehemu ambayo wangeweza kutumia kwa kazi ya MUNGU imekuwa mzigo wa kuogofya. {1T 169.1}

Malaika wa MUNGU alisema: “Weka yote juu ya madhabahu, dhabihu iliyo hai, inayoteketeza. Ifunge kwa kamba, ikiwa huwezi kuiweka hapo. Jitoe kwa sala. Ishi madhabahuni. Imarisha malengo yako kwa ahadi za MUNGU.” “Viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu, mahali pasipokaribia mwivi, wala nondo haharibu. Jiwekeeni hazina mbinguni .” 1T 169.2}

Niliona kwamba ikiwa MUNGU amekupa utajiri juu ya walio wazi na masikini, inapaswa kukunyenyekesha, kwani inakuweka chini ya majukumu makubwa. Pale ambapo vitu vingi vimetolewa, hata mali ya ulimwengu huu, vingi vitahitajika. Juu ya kanuni hii ni lazima umiliki tabia nzuri na ya ukarimu. Tafuta fursa za kufanya vizuri na kile ulicho nacho. “Jiwekeeni hazina mbinguni.” {1T 170.1}

Niliona kwamba jambo dogo ambalo limetakiwa kwa Wakristo katika siku zilizopita, ni kuwa na roho ya ukarimu, na kumtolea Bwana sehemu ya mazao yao yote. Kila Mkristo wa kweli amelichukulia hili kama fursa, lakini wengine ambao wameitwa kwa jina tu la Mkristo, wamechukulia kama mzigo; neema na upendo wa MUNGU haujawahi kufanya ndani yao kazi hiyo nzuri, la sivyo wangefurahi kuendeleza kazi ya Mkombozi wao. Lakini Wakristo ambao wanaishi katika siku za mwisho, na ambao wanamngojea Bwana wao,

wanahitajika kufanya hata zaidi ya hili. MUNGU anawataka watoe kafara. {1T 170.2}

Malaika alisema: "Yesu aliacha njia nzuri kwako kufuata. Kanyaga nyayo Zake. Shiriki maisha Yake ya kujikana, maisha Yake ya kujitoa, na urithi pamoja Naye taji ya utukufu." {1T 170.3}

## SURA YA 30

## KIJANA TAJIRI

Katika Monterey, Michigan, Oktoba 8, 1857, nilioneshwa katika maono kwamba hali ya watunza Sabato wengi ilikuwa kama ile ya yule kijana aliyemjia Yesu kujua anachopaswa kufanya ili arithi uzima wa milele. {1T 170.4}

"Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele? Akamwambia Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni Mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri. Akamwambia, Zipi? Yesu akasema, Ni hizi, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, Waheshimu baba yako na mama yako, na, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Yule kijana akamwambia, Haya yote nimeyashika; nimepungukiwa na nini tena? Yesu akamwambia, Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate. Yule kijana alipolisikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi." {1T 170.5}

"Yesu akawaambia wanafunzi Wake, Amin, nawaambieni, ya kwamba itakuwa shida tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni. Nawaambia tena, Ni rahisi zaidi

ngamia kupenya tundu ya sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa MUNGU. Wanafunzi waliposikia, walishangaa mno, wakisema, Ni nani basi awezaye kuokoka? Yesu akawakazia macho, akawaambia, Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa MUNGU yote yawezekana." Mathayo 19: 16-26. {1T 171.1}

Yesu alinukuu amri tano kati ya sita za mwisho kwa kijana huyo, pia amri kuu ya pili, ambayo amri sita za mwisho hutegemea. Yule kijana alidhani kuwa zile zilizotajwa alikuwa amezishika. Yesu hakutaja amri nne za kwanza, zenye jukumu letu kwa MUNGU. Katika kujibu swali la yule kijana tajiri, "Nimepungukiwa nini?" Yesu akamwambia: "Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni." {1T 171.2}

Hapa ndipo palipokuwa na upungufu wake.  Alishindwa kushika amri nne za kwanza, na pia sita za mwisho. Alishindwa kumpenda jirani yake kama yeye mwenyewe. Yesu alisema: "Wape maskini." Yesu aligusa mali zake. "Uza ulicho nacho, uwape maskini." Katika rejeleo hili la moja kwa moja, Yesu alionesha sanamu yake. Upendo wake wa utajiri ulikuwa mkuu; kwa hivyo haikuwezekana kwake kumpenda MUNGU  kwa moyo wake wote, kwa roho yake yote, na kwa moyo wake wote, na kwa akili yake yote. Na upendo huu mkuu kwa utajiri wake ulifunga macho yake kwa mahitaji ya wanadamu wenzake. Hakumpenda jirani yake kama yeye mwenyewe, kwa hivyo alishindwa kushika hata zile amri sita za mwisho. Moyo wake ulikuwa kwenye hazina yake. Ilimezwa katika mali zake za kidunia. Alizipenda mali zake kuliko MUNGU, na kuliko hazina ya mbinguni. Alisikia masharti kutoka kwa kinywa cha Yesu. Kama angeuza na kuwapa maskini mali zake, basi angekuwa na hazina mbinguni. Hapa kulikuwa na jaribu la jinsi alivyothamini uzima wa milele kuliko utajiri. Je! Alishikilia kwa hamu tumaini la uzima wa milele? Je! Alijitahidi kwa bidii kuondoa kizuizi ambacho kilikuwa katika njia yake ya kuwa na hazina mbinguni? Lo, hapana; "aliondoka akiwa na huzuni, maana alikuwa na mali nyingi." {1T 171.3}

Nilioneshwa kwa maneno haya: "Kwa maana ni rahisi ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa MUNGU." Yesu alisema: "Akasema, Yasiyowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa MUNGU." Malaika alisema: "Je! MUNGU atawaruhusu matajiri kubaki na utajiri wao, na bado waingie katika ufalme wa MUNGU?" Malaika mwingine akajibu: "Hapana, kamwe." {1T 172.1}

Niliona kuwa ni mpango wa MUNGU kwamba utajiri huu utumike ipasavyo, ugawanywe kuwabariki wahitaji, na kuendeleza kazi ya MUNGU. Ikiwa watu wanapenda utajiri wao zaidi kuliko vile wanavyopenda wenzao, zaidi kuliko wao wanavyompenda MUNGU  au Ukweli wa Neno Lake, ikiwa mioyo yao iko kwenye utajiri wao, hawawezi kuwa na uzima wa milele. Wangependelea kutoa Ukweli kuliko kuuza na kuwapa maskini. Hapa wamethibitishwa kuona jinsi

wanavyompenda MUNGU, jinsi wanavyopenda Ukweli; na, kama yule kijana tajiri katika Biblia, wengi huenda wakiwa na huzuni kwa sababu hawawezi kuwa na utajiri wao na hazina mbinguni wakati huo huo. Hawawezi kuwa na vyote viwili; na wanajaribu kuhatarisha nafasi yao ya uzima wa milele kwa milki ya ulimwengu. {1T 172.2}

"Ni rahisi ngamia kupita kwenye tundu la sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa MUNGU." Na kwa MUNGU mambo yote yanawezekana. Ukweli, uliokaribishwa moyoni na ROHO WA MUNGU, utapunguza upendo wa utajiri. Upendo wa Yesu na utajiri hauwezi kukaa ndani ya moyo huo huo. Upendo wa MUNGU hadi sasa unapita upendo wa utajiri ambao mmiliki hujitenga na utajiri wake na kuhamishia mapenzi yake kwa MUNGU. Kupitia upendo basi huongozwa kuhudumu kwa mahitaji ya kusudi la MUNGU. Ni raha yake ya hali ya juu kufanya mwelekeo sahihi wa bidhaa za Mola wake. Upendo kwa MUNGU na watu wenzake umetangulia, na anashikilia yote aliyonayo kama siyo yake mwenyewe, na kwa uaminifu anatimiza wajibu wake kama wakili wa MUNGU. Ndipo anaweza kuzishika amri zote kuu za sheria: "Mpende Bwana MUNGU wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote." "Mpende jirani yako kama nafsi yako." Kwa njia hii inawezekana kwa mtu tajiri kuingia katika ufalme wa MUNGU. "Na kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya Jina Langu, atapokea mara mia, na kuurithi uzima wa milele. Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na walio wa mwisho watakuwa wa kwanza. Hapa ndiyo ipo zawadi "Na kila mtu aliyeacha nyumba, au kaka, au dada, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya jina langu, atapokea mara mia, na atarithi uzima wa milele. Lakini wengi walio wa kwanza. watakuwa wa mwisho, na wa mwisho watakuwa wa kwanza." {1T 172.3}

Hii ndiyo tuzo kwa wale wanaojitoa kwa MUNGU. Wanapokea mara mia katika maisha haya, na watarithi uzima wa milele. "Lakini walio wa kwanza watakuwa wa mwisho; na wa mwisho watakuwa wa kwanza." Nilioneshwa wale wanaoupokea Ukweli, lakini hawauishi. Wanashikilia mali zao, na hawako tayari kusambaza mali zao ili kuendeleza kazi ya MUNGU. Hawana imani ya kujiachilia na kumwamini MUNGU. Upendo wao kwa ulimwengu huu unameza imani yao. MUNGU anataka sehemu ya mali zao, lakini hawatii. Wanatoa sababu kwamba wamehenyeka sana kupata kile walicho nacho, na hawawezi kumkopesha Bwana, kwani wanaweza kuwa na uhitaji. "Enyi wenye imani haba." MUNGU huyo aliyemjali Eliya wakati wa njaa, hatapita kando karibu na mmoja wa watoto Wake waliojitoa mhanga. Yeye ambaye amehesabu nywele za vichwa vyao, atawajali, na siku za njaa watashiba. Wakati waovu wanaangamia karibu nao kwa kukosa mkate, mkate na maji yao vitakuwa na hakika. Wale ambao bado wanashikilia hazina yao ya kidunia, na hawaoneshi msimamo sahihi wa

kile ambacho wamekopeshwa na MUNGU, watapoteza hazina yao mbinguni, watapoteza uzima wa milele. {1T 173.1}

MUNGU katika majaliwa Yake ameigusa mioyo ya baadhi ya wale ambao wana utajiri, na amewaongoa katika Ukweli, ili wao na mali zao wasaidie kuendelea na kazi Yake. Na ikiwa wale walio matajiri hawatafanya hivi, ikiwa hawatatimiza kusudi la MUNGU, atawapita, na atainua wengine kujaza nafasi zao na kutimiza kusudi Lake, na kwa mali zao watasambaza kwa furaha na kukutana na mahitaji ya kazi ya MUNGU. Katika hili watakuwa wa kwanza. MUNGU atakuwa na wale walio katika kazi Yake ambao watafanya hivi. {1T 174.1}

Yeye Angeweza kutuma mali kutoka mbinguni kufanya kazi Yake; lakini hii ni nje ya utaratibu Wake. Ameweka majaliwa Yake kwamba watu wawe vyombo Vyake, kwamba kama dhabihu kubwa ilivyofanywa kuwakomboa, wanapaswa kushiriki katika kazi hii ya wokovu, kwa kutoa dhabihu kwa kila mmoja, na kwa kufanya hivyo kuonesha jinsi wanavyothamini dhabihu hiyo ambayo imetolewa kwa ajili yao. {1T 174.2}

Nilielekezwa kwa Yakobo 5:1-3: “Haya basi, enyi matajiri! Lieni, mkapige yowe kwa sababu ya mashaka yenu yanayowajia. Mali zenu zimeoza, na mavazi yenu yameliwa na nondo. Dhahabu yenu na fedha yenu zimeingia kutu, na kutu yake itawashuhudia, nayo itakula miili yenu kama moto. Mmejiwekea akiba katika siku za mwisho.” {1T 174.3}

Niliona kwamba Maneno haya ya kuogofya yanatumika hasa kwa matajiri ambao wanadai kuamini Ukweli wa leo. Bwana anawaita watumie mali zao kuendeleza mashauri Yake. Fursa zinawasilishwa kwao, lakini hufunga macho yao kwa mahitaji ya kazi hiyo, na kushikamana sana kwenye hazina yao ya kidunia. Upendo wao kwa ulimwengu ni mkubwa kuliko upendo wao kwa Ukweli, upendo wao kwa wanadamu wenzao, au upendo wao kwa MUNGU. Anahitaji mali zao, lakini wao kwa ubinafsi, kwa tamaa, huhifadhi kile walicho nacho. Wanatoa kidogo hapa na pale na kupunguza hatia kwenye dhamiri zao, lakini hawajashinda upendo wao kwa ulimwengu huu. Hawatoi dhabihu kwa ajili ya MUNGU. Bwana ameinua wengine ambao wanathamini uzima wa milele, na ambao wanaweza kuhisi na kutambua thamani ya roho, na wamejitolea kwa hiari mali zao za kuendeleza kazi ya MUNGU. Kazi inafungwa; na hivi karibuni mali za wale ambao wameweka utajiri wao, mashamba yao makubwa, ng'ombe zao, nk, havitahitajika. Nilimwona Bwana akigeukia wale wenye hasira, na akiwa na ghadhabu, alirudia Maneno haya: “Nendeni sasa, enyi matajiri.” Yeye Amewaita, lakini hamkusikia. Upendo wa ulimwengu huu umezamisha sauti yake. Sasa Bwana hana faida tena kwenu, na anawaacha muende, akiwasihi: “Nendeni sasa, enyi matajiri.” {1T 174.4}

Lo, niliona ni jambo baya sana kuachwa na Bwana – jambo la kutisha kushikilia mali inayoweza kuharibika hapa, wakati Yeye amesema kwamba ikiwa tutauza

na kutoa sadaka, tunaweza kuweka hazina mbinguni. Nilioneshwa kwamba wakati kazi inamalizika, na Ukweli unaendelea kwa nguvu kubwa, watu hawa matajiri wataleta mali zao na kuziweka miguuni mwa watumishi wa MUNGU, wakiwasihi wazipokee. Jibu kutoka kwa watumishi wa MUNGU litakuwa: "Nendeni sasa, enyi matajiri. Mali zenu hazihitajiki. Mlizizuia wakati mngeweza kufanya vizuri nayo katika kuendeleza kusudi la MUNGU. Masikini wameteseka; hawakubarikiwa na mali zenu. MUNGU hatakubali utajiri wako sasa. Nendeni zenu sasa, enyi matajiri." {1T 175.1}

Kisha mimi nikaelekezwa kwa Maneno haya: "Tazama, ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu, ni wenu mliouzuia kwa hila, unapiga kelele Kilio cha hao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa Sabato. Niliona kuwa MUNGU hayumo katika utajiri wote unaopatikana. Shetani mara nyingi ana uhusiano mwingi na upatikanaji wa mali kuliko MUNGU. Sehemu kubwa ya utajiri huo hupatikana kwa kumkandamiza mtu aliyeajiriwa katika mshahara wake. Tajiri mwenye tamaa ya asili hupata utajiri wake kwa kumkandamiza aliyeajiriwa, na kuchukua faida ya watu binafsi popote awezapo, na hivyo kuongeza hazina ambayo itakula mwili wake kama moto. {1T 175.2}

Uaminifu mkali, na hatua za kuheshimika, havijachukuliwa na baadhi ya watu. Hao lazima wachukue hatua zilizo tofauti sana na wafanye kazi haraka kukomboa wakati. Watunza Sabato wengi wana makosa katika jambo hili. Wanachukua fursa kujinufaisha kwa ajili ya ndugu zao masikini, na wale walio na utajiri zaidi hutoza kuliko thamani halisi ya vitu, zaidi ya vile ambavyo wangeweza kulipia vitu vile vile, wakati ndugu hawa-hawa wanaaibika na kufadhaika kwa kukosa pesa. MUNGU anajua mambo haya yote. Kila tendo la ubinafsi, kila ulafi na kutamani, kutaleta thawabu yake. {1T 176.1}

Niliona kuwa ni ukatili na ukosefu wa haki kutofikiria hali ya ndugu. Ikiwa anafadhaika, au ni maskini, lakini anafanya kadri awezavyo, upendeleo unapaswa kufanywa kwa ajili yake, na hata thamani kamili ya vitu anavyoweza kununua kwa matajiri haipaswi kuulizwa; lakini wanapaswa kuwa na matumbo ya huruma kwake. MUNGU atakubali matendo mema kama hayo, na mtendaji hatapoteza thawabu yake. Lakini kumbukumbu ya kutisha inasimama dhidi ya watunza Sabato kwa vitendo vinavyokaribiana , ubahili na uchu wa mali. {1T 176.2}

Nilioneshwa nyuma wakati ambapo kulikuwa na wachache tu waliosikiliza na kuukubali Ukweli. Hawakuwa na bidhaa nyingi za ulimwengu huu. Matakwa ya kazi hiyo yaligawanywa kati ya wachache sana. Halafu ilikuwa ni lazima kwa wengine kuuza nyumba zao na mashamba, na kupata vitu nafuu vya kuwahudumia kama makazi, au nyumba, wakati mali zao ziliazimishwa kwa uhuru na ukarimu kwa Bwana, kuchapisha Ukweli, na vinginevyo kusaidia katika kuendeleza kazi ya MUNGU. Nilipowaangalia watu hawa waliojitoa mhanga, niliona kwamba walikuwa wamejinyima faragha kwa faida ya kazi. Nikaona

malaika amesimama karibu nao, akiwaelekeza juu, na kusema: "Mna mifuko mbinguni! Mna mifuko mbinguni ambayo haichakai. Vumilieni hadi mwisho, na thawabu yenu itakuwa kubwa." {1T 176.3}

MUNGU amekuwa akijongea juu ya mioyo mingi-akiigusa mioyo. Ukweli ambao wachache walijitoa sana mhanga, ili kuupata kabla ya wengine, umeshinda, na umati wa watu wameushikilia. MUNGU katika majaliwa Yake amegusa mioyo ya wale walio na mali, na amewaleta katika Ukweli, ili kazi Yake inapoongezeka na kusonga mbele, mahitaji ya kazi hiyo yatimizwe. Mali nyingi zimeletwa katika safu ya watunza Sabato, na nikaona kwamba kwa sasa MUNGU hahitaji nyumba ambazo watu wake wanahitaji kuishi, isipokuwa kama nyumba hizo za bei ghali zingebadilishwa kwa zile za bei nafuu. Lakini ikiwa wale walio na vingi hawasikii sauti Yake, hawajiengui kutoka ulimwenguni, na hawatoi sehemu ya mali zao na ardhi zao, na kumtolea MUNGU dhabihu, Yeye atawapita, na kuwaita wale ambao wako tayari kufanya chochote kwa Yesu, hata kuuza nyumba zao ili kukidhi mahitaji ya kazi. MUNGU atakuwa na sadaka za hiari. Wale wanaotoa lazima waone kuwa wamependelewa kufanya hivyo. {1T 176.4}

Baadhi hutoa wingi wa mali zao, lakini bado hawahisi kupungukiwa. Hawajikani kabisa kitu chochote kwa sababu ya Kristo. Bado wana vyote ambavyo mioyo yao inavitamani. Wanatoa kwa ukarimu na kwa moyo wote. MUNGU hutambua hali hiyo, na hatua na nia vinajulikana na vimewekwa alama na Yeye. Hawatapoteza tuzo yao. Ninyi ambao hamuwezi kutoa kwa ukarimu msijilaumu kwa sababu hamwezi kufanya kama wengine. Fanya uwezavyo. Jinyime mwenyewe kwa mambo kadhaa ambayo unaweza kuishi bila kuwa nayo, na ujitolee kwa sababu ya MUNGU. Kama mjane, toa sarafu zako mbili. Kwa kweli utatoa zaidi ya wale wote wanaotoa kwa wingi wao; na utajua jinsi ilivyo tamu kujikana mwenyewe, kutoa kwa wahitaji, kujitoa kwa ajili ya Ukweli, na kuweka hazina mbinguni. {1T 177.1}

Nilioneshwa kuwa vijana, hasa wavulana, wanaodai kuwa na Ukweli, bado wana somo la kujifunza kuhusu kujinyima. Kama hawa wangejitoa zaidi kwa ajili ya Ukweli, wangeuthamini zaidi. Ingeathiri mioyo yao, na kutakasa maisha yao, na wangeifanya kuwa ya kupendeza na takatifu zaidi. {1T 177.2}

Vijana hawachukui mzigo wa kazi ya MUNGU, au kuhisi jukumu lolote juu yake. Je! Ni kwa sababu MUNGU amewasamehe au kuwatolea udhuru? Lo, hapana; wanajitolea udhuru wenyewe! Wamepunguziwa majukumu na wanaishi maisha rahisi wakati wengine wamelemewa. Hawatambui kuwa mali hizo siyo zao. Nguvu zao, wakati wao, siyo wao wenyewe. Wamenunuliwa kwa bei. Dhabihu pendwa ilitolewa kwa ajili yao, na kama wasipokuwa na roho ya kujinyima na kujitoa, hawataweza kamwe kumiliki urithi wa milele. {1T 178.1}

# SURA YA 31

## UPENDELEO NA WAJIBU WA KANISA

Ifuatayo inahusiana na kanisa la Battle Creek, lakini inaelezea hali na maslahi ya ndugu na dada waliotawanyika nchi za nje: {1T 178.2}

Niliona kwamba wingu zito lilikuwa limewafunika, lakini miale michache ya nuru kutoka kwa Yesu ilipenya wingu hili. Niliangalia na kuona wale waliopokea nuru hii, na nikaona watu binafsi wakiomba ushindi kwa bidii. Somo lao kuu walilokuwa wakijifunza ilikuwa namna ya kumtumikia MUNGU. Imani yao ya kudumu ilileta faida. Mwanga wa mbinguni uliangaziwa juu yao; lakini wingu la giza juu ya kanisa kwa ujumla lilikuwa nene. Walikuwa wajinga na wavivu. Uchungu wangu wa roho ulikuwa mkubwa. Nilimuuliza malaika kama giza hilo lilikuwa la lazima. Akasema: "Angalieni!" Kisha nikaona kanisa likianza kuinuka, na kumwomba MUNGU kwa dhati na bidii, na miale ya nuru ilianza kupenya kwenye giza hili, na wingu likaondolewa. Nuru safi ya mbinguni iliwaangazia, na kwa ujasiri mtakatifu umakini wao ulivutwa juu. Malaika akasema: "Huu ndiyo upendeleo na wajibu wao." {1T 178.3}

Shetani ameshuka kwa nguvu kubwa, akijua kwamba ana wakati mchache. Malaika zake wanajishughulisha, na sehemu kubwa ya watu wa MUNGU wanajitesa wenyewe ili kujizuia wakihofia wasije wakabembelezwa naye na kuliwazwa na kisha walale. Wingu tena likapita, likakaa juu ya kanisa. Niliona kuwa itakuwa ni kwa njia ya bidii na sala ya kudumu ambapo uchawi huu utavunjwa. {1T 178.4}

Ukweli wa kutisha wa Neno la MUNGU ulikuwa umewachochea watu wa MUNGU kidogo. Mara kwa mara wangefanya juhudi dhaifu kuushinda, lakini hivi karibuni walichoka na kuzama katika hali ile ile ya uvuguvugu. Niliona kuwa hawakuwa na uvumilivu na uamuzi thabiti wa kupinga. Hebu mwanadamu anayetafuta wokovu wa MUNGU amiliki nguvu, udhati na bidii ile ile ambayo angekuwa nayo kwa hazina ya ulimwengu, na kitu hicho wanachokitamani kitapatikana. Niliona kwamba kanisa linaweza pia kunywa kikombe kilichojaa, badala ya kushikilia kikombe kilicho tupu mkononi au mdomoni. {1T 179.1}

Siyo mpango wa MUNGU kuwa wengine wawe na maisha rahisi na wengine walemewe. Wengine wanahisi uzito na jukumu la kusudi la kazi hiyo ya Mungu, na ulazima wa kutenda kwao ili wakusanye pamoja na Kristo na wasitawanye mbali. Wengine hujifanyia kwa uhuru bila dhima/majukumu yoyote, wakitenda kana kwamba hawakuwa na ushawishi wowote. Watu hawa hutawanya nje. MUNGU hana ubaguzi. Wote ambao wamefanywa washiriki wa wokovu Wake hapa, na ambao wanatarajia kushiriki utukufu wa ufalme baadaye, lazima

wakusanye na Kristo. Kila mmoja lazima ahisi kwamba anawajibika kwa tatizo au kesi yake mwenyewe, na kwa ushawishi anaotoa juu ya wengine. Ikiwa hawa watadumisha mwenendo wao wa Kikristo, Yesu atakuwa ndani yao tumaini la utukufu, na watapenda kutaja sifa Zake ili wapate kuburudika. Kazi ya Bwana wao itakuwa karibu na pendwa kwao. Litakuwa somo lao la kujifunza, kuendeleza kusudi la kazi Yake na kuiheshimu kwa kuishi kwa utakatifu. Malaika alisema: “Kila talanta MUNGU ataidai pamoja na riba.” Kila Mkristo lazima aendelee kutoka nguvu hadi nguvu, na atumie nguvu zake zote kwa kusudi la kazi ya MUNGU. {1T 179.2}

## SURA YA 32

## KUPEPETWA

Novemba 20, 1857, nilioneshwa watu wa MUNGU, na nikawaona wakipepetwa sana. Wengine, wakiwa na imani thabiti na kilio cha maumivu, walikuwa wakimsihi MUNGU. Nyuso zao zilikuwa za rangi ya kupauka/msongo, na ziliwekwa alama na zilijawa na fadhaa na wasiwasi mkubwa, zinazoelezea mapambano yao ya ndani. Ukakamavu, unyofu na bidii kubwa vilioneshwa katika sura zao, wakati matone makubwa ya jasho yalipokuwa yakidondoka kutoka kwenye mapaji ya nyuso zao. Mara kwa mara nyuso zao zingeangaza na alama za uthibitisho wa MUNGU, na tena sura ile ile ya dhati, ya bidii, ya wasiwasi ingekaa juu yao. [“Pigeni tarumbeta katika sayuni, takaseni Saumu,

kusanyeni kusanyiko kuu; kusanyeni watu, litakaseni kusanyiko, kusanyeni wazee……Hao makuhani, wahudumu wa bwana, na walie kati ya patakatifu na madhabahu, na waseme, uwaachilie watu Wako, ee Bwana, wala usiutoe urithi wako upate aibu, hata mataifa Watawale juu yao; kwani waseme kati ya watu, Yuko wapi MUNGU wao?" Yoeli 2: 15-17. "Basi mtiini MUNGU. Mpingeni shetani, naye atawakimbia. Mkaribieni MUNGU, Naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili. Huzunikeni na kuomboleza na kulia. Kucheka kwenu na kugeuzwe kuwa kuomboleza, na furaha yenu kuwa hamu. Jidhilini mbele za bwana, Naye atawakuza." Yakobo 4: 7-10. "Jikusanyeni, naam, jikusanyeni, ee taifa lisilo na haya; kabla haijazaa hiyo amri, kabla haijapita siku ile kama makapi, kabla haijawajilia hasira kali ya Bwana, kabla haijawajilia siku ya hasira ya Bwana. Mtafuteni bwana, enyi nyote mlio wanyenyekevu wa dunia, ninyi mliozitenda hukumu Zake; itafuteni haki, utafuteni Unyenyekevu; huenda mtafichwa katika siku ya hasira ya Bwana." Sefania 2:1-3.] {1T 179.3}

Malaika waovu walijazana karibu nao, wakishinikiza giza lao juu yao, kumfunga Yesu mbali na wao, ili macho yao yavutiwe na giza lililowazunguka, ili wasimwamini MUNGU na baadaye wanung'unike dhidi yake. Usalama wao pekee ulikuwa katika kukaza macho yao juu. Malaika wa MUNGU walikuwa na jukumu juu ya watu Wake, na wakati mazingira yenye sumu kutoka kwa malaika wabaya yalipoleta mbinyo karibu na hawa wenye wasiwasi, malaika wa mbinguni walikuwa wakizungusha/wakipepea mabawa yao juu yao kila wakati, kutawanya giza nene. {1T 180.1}

Wengine, niliwaona wakiwa hawashiriki katika kazi hii ya maumivu na kusihi. Walionekana walio tofauti na wasiojali. Hawakuwa wakipinga giza lililowazunguka, na likawafungia katika wingu nene. Malaika wa MUNGU waliwaacha hawa, na niliwaona wakikimbilia kusaidia wale ambao walikuwa wakipambana kwa nguvu zao zote kupinga malaika waovu, na kujaribu kujisaidia kwa kumwita MUNGU kwa uvumilivu. Lakini malaika waliwaacha wale ambao hawakujitahidi kujisaidia, na niliwapoteza machoni mwangu. Wakati waombaji walipokuwa wakiendelea na kilio chao cha dhati, mwangaza wa nuru kutoka kwa Yesu wakati mwingine ungewajia, kutia nguvu mioyo yao, na kuangaza nyuso zao. {1T 180.2}

Niliuliza maana ya kupepetwa/pepeto nililokuwa nimeona, na nikaoneshwa kuwa litasababishwa na ushuhuda dhahiri na wa moja kwa moja uliotolewa na Shahidi Mwaminifu kwa Walaodikia. Huu utakuwa na matokeo kwenye moyo wa mpokeaji, na utamuongoza kuinua kanuni na kutangaza Ukweli huu wa moja kwa moja. Wengine hawataupokea ushuhuda huu wa moja kwa moja. Watainuka ili kuupinga, na jambo hili litasababisha pepeto kati ya watu wa MUNGU. {1T 181.1}

Ushuhuda wa Shahidi wa Kweli haujazingatiwa hata nusu. Ushuhuda mzito na madhubuti ambao hatima ya kanisa huutegemea umedharauliwa kidogo, kama si kupuuzwa kabisa. Ushuhuda huu lazima ufanye toba ya kina, na wote wanaoupokea kweli watautii na kuusafishwa. {1T 181.2}

Malaika akasema: "Jiorodhesheni!" Punde nilisikia sauti ambayo ilisikika kama ala nyingi za muziki, zote zikiwa katika hali nzuri, tamu na zilizo sahihi. Muziki huu ulizidi nyimbo zozote nilizowahi kuzisikia. Ilionekana kuwa imejaa rehema, huruma, kuinua, pamoja na furaha takatifu. Ilinipa msismko wa furaha ndani ya nafsi yangu yote, ndani ya uhai wangu. Malaika akasema: "Angalia!" Usikivu wangu ulibadilishwa kwa kundi nililoliona, ambalo lilipepetwa sana. Nilioneshwa wale ambao hapo awali niliwaona wakilia na kuomba kwa uchungu wa roho. Kundi la malaika walinzi waliowazunguka walikuwa wameongezeka maradufu, na walikuwa wamevaa silaha kutoka kichwani hadi miguuni. Walitembea kwa mpangilio halisi, thabiti, kama kikosi cha askari. Nyuso zao zilielezea mzozo mkali ambao walikuwa wamevumilia, na mapambano makali waliyokuwa wameyapitia. Walakini mwonekano wao wa nyuso na hata mwili, ulioonyesha maumivu makali ya ndani, sasa ziliangaza na nuru na utukufu wa mbinguni. Walikuwa wamepata ushindi, na hii ikaleta kutoka kwao mwitikio wa shukrani ya dhati, na furaha takatifu, na uchaji. {1T 181.3}

Idadi ya makundi haya ilikuwa imepungua. Wengine walikuwa wamepepetwa na kuachwa njiani. ["Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu. Kwa kuwa wasema, mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye Mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi." Ufunuo 3: 15-17.] Wale wazembe na wasiojali, ambao hawakujiunga na wale waliothamini ushindi na wokovu vya kutosha kiasi cha kuuombea na kuugua kwa uvumilivu, hawakuupata, na waliachwa nyuma gizani, lakini idadi yao mara moja iliundwa na wengine walioshikilia Ukweli na kuja kwenye safu. Bado malaika wabaya waliwazunguka, lakini hawakuweza kuwa na nguvu juu yao. ["Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za MUNGU, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga Kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa roho ambao ni Neno la MUNGU; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika roho, mkikesha kwa jambo hilo Na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote." Waefeso 6: 12-18.] {1T 182.1}

Niliwasikia wale waliovikwa silaha hizo wakisema Ukweli kwa nguvu kubwa. Ilikuwa na athari. Niliwaona wale waliokuwa wamefungwa; wake wengine walikuwa wamefungwa na waume zao, na watoto wengine walikuwa wamefungwa na wazazi wao. Mwaaminifu ambaye alikuwa ameshikiliwa au kuzuiwa kusikia Ukweli, sasa aliushika kwa hamu. Hofu yote ya jamaa zao ilikuwa imeisha. Ukweli peke yake uliinuliwa kwao. Ukweli kilikuwa kitu kinachopendwa na cha thamani kuliko maisha. Walikuwa na njaa na kiu ya Ukweli. Niliuliza ni nini kilifanya mabadiliko haya makubwa. Malaika akajibu: "Ni mvua ya masika, inayoburudisha kw a uwepo wa Bwana, kilio kikuu cha malaika wa tatu." {1T 182.2}

Nguvu kubwa ilikuwa na hawa waliochaguliwa. Malaika akasema: "angalia!" Usikivu wangu ulielekezwa kwa waovu, au wasioamini. Wote walikuwa wameshtuka/wakishangaa. Bidii na nguvu pamoja na watu wa MUNGU zilikuwa zimewaamsha na kuwakasirisha. Kuchanganyikiwa, kukanganyikiwa kulikuwa kila upande. Niliona hatua zikichukuliwa dhidi ya kundi hili, ambalo lilikuwa na nguvu na nuru ya MUNGU. Giza liliwazunguka, lakini bado walisimama hapo, wakikubaliwa na MUNGU, na kumtumaini yeye. Niliwaona wakishangaa. Baada ya hapo niliwasikia wakimlilia MUNGU kwa bidii. Mchana na usiku kilio chao hakikukoma. ["na MUNGU, Je! Hatawapatia haki wateule Wake wanaomlilia mchana na usiku, Naye ni mvumilivu kwao? Nawaambia, atawapatia haki upesi; Walakini, atakapokuja Mwana wa Adamu, Je! Ataiona imani duniani?" Luka 18: 7, 8. Tazama pia ufunuo 14:14, 15.]

Nikasikia Maneno haya: "kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa mwanadamu, mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa CHAKE, na katika mkono Wake mundu mkali. Na malaika mwingine akatoka katika hekalu, akimlilia kwa sauti kuu Yeye aliyekuwa ameketi juu ya lile wingu, tia mundu wako, ukavune; kwa kuwa saa ya kuvuna imekuja; kwa kuwa mavuno ya nchi yamekomaa." Haya ndiyo Maneno ninayoweza kuyakumbuka akilini mwangu. Wote walionekana kuwa na hisia ya kutostahiki kwao, na walidhihirisha unyenyekevu wote kwa kujitiisha kabisa kwa mapenzi ya MUNGU. Hata hivyo kama Yakobo, kila mmoja, bila kubagua, alikuwa akiomba kwa bidii na kupigania ukombozi. {1t 183.1}

Mara tu walipoanza kulia kwao dhati na bidii, malaika, kwa huruma, waliwaendea kwa ajili ya ukombozi wao. Lakini malaika mrefu, mwenye amri hakuwaruhusu. Alisema: "Mapenzi ya MUNGU bado hayajatimizwa. Ni lazima wakinywee kikombe. Lazima wabatizwe kwa ubatizo." {1T 183.2}

Hivi karibuni nilisikia sauti ya MUNGU iliyotikisa mbingu na dunia. ["Naye Bwana atanguruma toka Sayuni, atatoa sauti Yake toka Yerusalemu; na mbingu na nchi zitatetemeka; lakini Bwana atakuwa kimbilio la watu Wake, na ngome ya wana wa Israeli." Joeli 3:16. Tazama pia Waebrania 12:26; Ufunuo 6:17.] Kulikuwa na tetemeko kubwa la ardhi. Majengo yalitikiswa chini, na kuanguka

kila upande. Kisha nikasikia kelele yenye ushindi ya kushinda, sauti kubwa, iliyojaa muziki, na iliyo wazi. Niliangalia kundi hili, ambalo, muda mfupi uliopita, lilikuwa katika shida na utumwa. Kuwa Mateka kwao kuligeuzwa. Nuru tukufu iliwaangazia. Jamani, jinsi walivyoonekana wazuri wakati huo! Uchovu wote na alama za masumbuko vilikuwa vimetoweka; afya na urembo/uzuri vilionekana katika kila sura. Maadui zao, watu wa mataifa ambao ni waovu (heathen) waliyowazunguka, walianguka kama watu waliokufa. Hawakuweza kuvumilia nuru ambayo iliangaza juu ya wale waliokombolewa, watakatifu. Nuru na utukufu huu ulibaki juu yao mpaka Yesu alipoonekana katika mawingu ya mbinguni, na kundi la wale waaminifu, lililojaribiwa lilibadilishwa kwa muda mfupi, kufumba na kufumbua, kutoka utukufu hadi utukufu. Makaburi yalifunguliwa na watakatifu walitoka, wamevaa mavazi ya kutokufa, wakilia: "Ushindi juu ya kifo na kaburi!" kisha pamoja na watakatifu walio hai walinyakuliwa kwenda kumlaki Bwana wao hewani, wakati sauti bora/tajiri, kelele za muziki za utukufu na ushindi ziliporindima kutoka kwa kila ulimi usio na hali ya kufa. {1T 184.1}

## SURA YA 33

## KANISA LA LAODIKIA

Ndugu Wapendwa na Dada: Bwana amenitembelea tena kwa rehema nyingi. Nimeteseka sana kwa miezi michache iliyopita. Magonjwa yamenibinya sana. Kwa miaka mingi nimekuwa nikisumbuliwa na ugonjwa wa shinikizo la kushuka na ugonjwa wa moyo, ambavyo vimekuwa na tabia ya kunishusha roho yangu kwa huzuni/sonona, kuharibu imani na ujasiri wangu. Ujumbe kwa Walaodikia haujatimiza toba hiyo ya bidii kati ya watu wa MUNGU ambayo nilitarajia kuiona, na fadhaa na kuchanganyikiwa kwangu kwa akili kumekuwa kukubwa. Magonjwa yalionekana kupiga hatua kila wakati, na nilifikiri lazima nilale kaburini. Sikuwa na hamu ya kuishi, kwa hivyo sikuweza kushikilia imani na kuombea kupona kwangu. Mara nyingi nilipoenda kupumzika usiku niligundua

kuwa nilikuwa katika hatari ya kupoteza pumzi kabla ya asubuhi. Katika hali hii nilizimia usiku wa manane. Ndugu Andrews na Loughborough walitumwa, na maombi ya dhati yalitolewa kwa MUNGU kwa niaba yangu. Msongo, sonona na mkandamizo mkubwa, uliondolewa kutoka kwenye moyo wangu unaouma, na nikachukuliwa mbali katika maono, na kuoneshwa mambo ambayo sasa ninawasilisha mbele yenu. {1T 185.1}

Niliona kwamba Shetani alikuwa akijaribu kuniongoza katika kuvunjika moyo na kukata tamaa, kunifanya nitamani kifo kuliko uzima. Nilioneshwa kwamba haikuwa mapenzi ya MUNGU kwamba sasa niache kazi na kulala kaburini; kwani hapo maadui wa imani yetu wangeshinda, na mioyo ya watoto wa MUNGU ingehuzunishwa. Niliona kwamba mara nyingi ningehisi uchungu wa roho, na ningepaswa kuteseka sana; hata hivyo nilikuwa na ahadi kwamba wale wanaonizunguka wangenitia moyo na kunisaidia, kwamba ujasiri na nguvu zangu visingeshindwa wakati nilipokuwa napigwa sana na shetani. {1T 185.2}

Nilioneshwa ya kwamba ushuhuda kwa Walaodikia unatumika kwa watu wa MUNGU kwa wakati huu, na sababu inayofanya haujatimiza kazi kubwa ni kutokana na ugumu wa mioyo yao. Lakini MUNGU ameupa ujumbe wakati wa kufanya kazi yake. Moyo lazima utakaswe na dhambi ambazo kwa muda mrefu zimemfungia Yesu nje. Ujumbe huu wa kutisha utafanya kazi yake. Ulipowasilishwa kwa mara ya kwanza, ulipelekea kufanyika kwa uchunguzi wa karibu wa moyo. Dhambi ziliungamwa, na watu wa MUNGU walisisimka na kuguswa moyo kila mahali. Karibu wote waliamini kuwa ujumbe huu ungeishia kwa kilio kikuu cha malaika wa tatu. Lakini waliposhindwa kuona kazi ya nguvu ikitimizwa kwa muda mfupi, wengi walipoteza athari ya ujumbe. Niliona kuwa ujumbe huu usingekamilisha kazi yake katika miezi michache. Ujumbe umekusudiwa kuwaamsha watu wa MUNGU, kutambua kurudi nyuma kwao, na kusababisha toba yenye ari, ili wapewe upendeleo wa uwepo wa Yesu, na waweze kukidhi kilio kikuu cha malaika wa tatu. Kwa kadri ujumbe huu ulivyoathiri moyo, ulisababisha unyenyekevu mkubwa mbele za MUNGU. Malaika walitumwa kila upande kuiandaa mioyo isiyoamini kwa Ukweli. Kazi ya MUNGU ilianza kuongezeka, na watu Wake walikuwa wakijua msimamo wao. Kama shauri la Shahidi wa Kweli lingezingatiwa kikamilifu, MUNGU angekuwa amewatengeneza watu Wake kwa uwezo mkubwa. Hata hivyo juhudi zilizofanywa tangu ujumbe ulipotolewa, zimebarikiwa na MUNGU, na roho nyingi zimeletwa kutoka kwenye makosa na giza ili zifurahi katika Ukweli. {1T 186.1}

MUNGU atawapima watu Wake. Yesu huwavumilia watu Wake, na wala hawatapiki mara moja kutoka kinywani Mwake. Malaika alisema: “MUNGU anawapima watu Wake.” Ikiwa ujumbe ungekuwa wa muda mfupi kama wengi wetu wanavyodhania, hakungekuwa na wakati kwao kukuza tabia. Wengi walisukumwa na hisia, lakini hawakusukumwa na kanuni na imani, na ujumbe huu mzito, wa kutisha uliwachochea. Ulifanya kazi juu ya hisia zao, na

kusisimua hofu zao, lakini haukufanikisha kazi ambayo MUNGU aliipanga iwe hivyo. MUNGU husoma moyo. Ili watu Wake wasije wakadanganywa kuhusu wao wenyewe, huwapa muda wa msisimko kuisha, na kisha kuwapima ili kuona ikiwa watatii ushauri wa Shahidi wa Kweli. {1T 186.2}

MUNGU huwaongoza watu Wake, hatua kwa hatua. Anawaleta kwenye alama tofauti zilizohesabiwa kudhihirisha kile kilicho moyoni. Wengine huvumilia wakati mmoja katika kusonga mbele, lakini huanguka kwenye hatua inayofuata. Katika kila hatua ya juu moyo hujaribiwa na kupimwa kwa karibu zaidi. Ikiwa watu wanaojiita wa MUNGU wataona mioyo yao ikipinga kazi hii ya moja kwa moja, hilo lapaswa kuwaaminisha kuwa wana kazi ya kufanya ili kushinda, ikiwa hawatatapikwa kutoka kinywani mwa Bwana. Malaika alisema: "MUNGU ataleta kazi Yake karibu na karibu zaidi ili kumjaribu na kumpima kila mmoja wa watu Wake." Wengine wako tayari kupokea nukta moja; lakini MUNGU anapowaleta kwenye hatua nyingine ya kupimwa, husinyaa na kusimama nyuma, kwa sababu wanaona hali hiyo inagonga sanamu zao moja kwa moja. Hapa wana fursa ya kuona kile kilicho mioyoni mwao kinachomzuia Yesu. Wanathamini jambo fulani kwa kiwango cha juu zaidi kuliko wanavyothamini Ukweli, na mioyo yao haijawa tayari kumpokea Yesu. Watu hujaribiwa na kupimwa kwa muda mrefu kuona ikiwa wataacha sanamu zao na kutii ushauri wa Shahidi wa Kweli. Ikiwa yeyote hatasafishwa kupitia kuitii Kweli, na kushinda ubinafsi wake, kiburi chake, na tamaa mbaya, malaika wa MUNGU wanatoa tamko: "Wamejiungamanisha na sanamu, waache," kisha wanaendelea na kazi yao, wakiwaacha hao na tabia zao za dhambi bila kushinda, chini ya udhibiti wa malaika wabaya. Wale ambao huja kwa kila hatua, na kupita kila mtihani, na kushinda, haijalishi ni kwa gharama gani, wametii ushauri wa Shahidi wa Kweli, na hawa watapokea mvua ya masika, na hivyo kuwa tayari kwa kutwaliwa kwenda mbinguni. {1T 187.1}

MUNGU huwapima watu Wake katika ulimwengu huu. Hapa ndipo mahali panapofaa kujitokeza katika uwepo Wake. Hapa, katika ulimwengu huu, katika siku hizi za mwisho, watu wataonesha ni nguvu gani inayoathiri mioyo yao na kudhibiti matendo yao. Ikiwa ni nguvu ya Ukweli wa Kiungu, itasababisha matendo mema. Itamwinua mpokeaji, na kumfanya awe mwenye moyo mzuri na mkarimu, kama Bwana Wake wa Kiungu. Lakini ikiwa malaika wabaya wanadhibiti moyo, itaonekana kwa njia mbalimbali. Matunda yatakuwa ubinafsi, uchoyo, kiburi, na tamaa mbaya. {1T 188.1}

Moyo ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, na wenye uovu wa kutisha sana. Wale wanaojidai kuwa watu wa dini hawako tayari kujichunguza kwa karibu ili kuona ikiwa wako katika imani; na ni ukweli wa kutisha kwamba wengi wanaegemea tumaini la uongo. Wengine hutegemea uzoefu wa zamani ambao walikuwa nao miaka iliyopita; lakini wakati wanapoletwa chini kwa wakati huu wa kuchunguza moyo, wakati wanapopaswa kuwa na uzoefu wa kila siku, hawana chochote cha kusimulia au kuhusiana nacho. Wanaonekana kufikiria kwamba

madai ya mdomo tu ya ile Kweli yatawaokoa. Watakaposhinda dhambi hizo ambazo MUNGU huzichukia, Yesu ataingia na kula nao na wao pamoja Naye. Ndipo watapata nguvu za Kiungu kutoka kwa Yesu, na watakua ndani Yake, na wataweza kwa ushindi mtakatifu kusema: "Ashukuriwe MUNGU, atupaye ushindi kupitia Bwana wetu Yesu Kristo." Ingempendeza zaidi Bwana kama wale wanaojidai kuwa wana vuguvugu wa dini kamwe wasingekuwa wamelitaja Jina Lake. Wao ni mzigo mzito wa daima kwa wale ambao wangekuwa wafuasi waaminifu wa Yesu. Wao ni kikwazo kwa watu wasioamini, na malaika wabaya huwazomea, na kuwachokoza/kuwatukana malaika wa MUNGU kwa njia yao potovu. Hawa ni laana kwa kazi nyumbani au nje ya nchi. Wanamkaribia MUNGU kwa midomo yao, wakati mioyo yao iko mbali Naye. {1T 188.2}

Nilioneshwa kuwa watu wa MUNGU hawapaswi kuiga mitindo ya ulimwengu. Wengine wamefanya hivi, na wanapoteza haraka tabia ya kipekee, takatifu ambayo ilipaswa kuwatofautisha kama watu wa MUNGU. Nilielekezwa nyuma kwa MUNGU wa watu wa kale, na kuelekezwa kulinganisha mavazi yao na mtindo wa mavazi katika siku hizi za mwisho. Ni tofauti kubwa iliyoje! Ni mabadiliko makubwa kiasi gani! Kisha wanawake hawakuwa na ujasiri kiasi hicho kama sasa. Walipoenda hadharani, walifunikwa nyuso zao na mtandio. Katika siku hizi za mwisho, mitindo ni ya aibu, isiyostahi na isiyo na kiasi. Wametambuliwa katika unabii. Walitetwa kwanza na darasa ambalo Shetani anamiliki juu yake, ambaye, "ambao wakiisha kufa ganzi [wakiwa hawana mguso wowote wa ROHO WA MUNGU] wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya unajisi/uchafu kwa kutamani." Ikiwa watu wanaodai MUNGU hawakumwacha sana, sasa kungekuwa na tofauti kubwa kati ya mavazi yao na ya ulimwengu. Kofia ndogo (bonnet), inayofunika uso na kichwa, inaonesha ukosefu wa adabu. Magauni yanayobana kiuno ni aibu. Wakazi wa dunia wanazidi kuongezeka kwa ufisadi, na mstari wa tofauti kati yao na Israeli wa MUNGU lazima iwe wazi zaidi, la sivyo laana inayowaangukia walimwengu itawangukia watu wanaojidai ni wa MUNGU. {1T 188.3}

Nilielekezwa kwa maandiko yafuatayo. Malaika akasema: "Wanapaswa kuwafundisha watu wa MUNGU." 1 Timotheo 2: 9, 10: "Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa MUNGU." 1 Petro 3: 3-5: "Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za MUNGU. Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini MUNGU, na kuwatii waume zao." {1T 189.1}

Kijana na Mzee, MUNGU anakupima wewe sasa. Wewe unaamua hatima yako ya milele. Kiburi chako, upendo wako kufuata fasheni/mitindo ya ulimwengu, mazungumzo yako ya bure na matupu, ubinafsi wako, vyote vimewekwa kwenye mizati, na uzito wa uovu kwa namna ya kutisha upo dhidi yako. Wewe ni maskini, na mnyonge, na kipofu, na uchi. Wakati uovu unazidi kuongezeka na kuota mizizi, unaikaba/unaisonga ile mbegu nzuri ambayo imepandwa moyoni; na hivi karibuni Neno ambalo lilitolewa juu ya nyumba ya Eli litatamkwa na malaika wa MUNGU kukuhusu wewe: Dhambi zako "hazitatakaswa/hazitasafishika kwa dhabihu wala kwa sadaka hata milele." Wengi, niliwaona, walikuwa wakijipendekeza na kujidanganya kuwa walikuwa Wakristo wazuri, ambao hawakuwa na hata mwonzi mmoja wa nuru kutoka kwa Yesu. Walikuwa hawajui ni nini maana ya kufanywa upya kwa neema ya MUNGU. Hawakuwa na uzoefu hai wa kuishi katika mambo ya MUNGU. Na nikaona kwamba Bwana alikuwa akinoa upanga Wake mbinguni ili awaangamize. Lo, kama kila anayejidai kukiri kwa mdomo tu bila matendo, mwana vuguvugu angeweza kutambua kazi safi ambayo MUNGU Yuko karibu kuifanya kati ya wale wanaojidai ni Wake! Wapendwa marafiki, msijidanganye kuhusu hali yenu. Hamwezi kumdanganya MUNGU. Shahidi wa Kweli anasema: "Nayajua matendo yako." Malaika wa tatu anaongoza watu, hatua kwa hatua, juu hadi juu. Katika kila hatua watajaribiwa. {1T 189.2}

Utoaji wa ukarimu kwa mpango *[tazama kiambatanisho online*] unampendeza MUNGU. Nilielekezwa nyuma katika siku za mitume, na nikaona kwamba MUNGU aliweka mpango huo wakati ROHO WAKE MTAKATIFU aliposhuka, na kwamba kwa karama ya unabii aliwashauri watu Wake kuhusu mfumo wa kutoa kwa ukarimu. Wote walipaswa kushiriki katika kazi hii ya kuwapa vitu vyao vya kimwili wale ambao waliwahudumia katika mambo ya kiroho. Walifundishwa pia kwamba wajane na yatima walikuwa na madai juu ya ukarimu na misaada yao. Dini iliyo safi na isiyo na taka hufafanuliwa, kwa kutembelea wajane na yatima katika shida zao, na kujilinda usichafuliwe na mawaa ya ulimwengu. Niliona kuwa hii haikuwa tu kuwahurumia wao kwa maneno ya kufariji katika shida zao, lakini kuwasaidia, ikiwa ni wahitaji, kwa vitu/mali zetu. Vijana na wasichana ambao MUNGU amewapa afya wanaweza kupata baraka kubwa kwa kuwasaidia wajane na yatima katika shida zao. Niliona kwamba MUNGU anahitaji vijana wa kiume kujitolea zaidi kwa ajili ya mema ya wengine. MUNGU ana madai mengi zaidi kwao kuliko walivyo tayari kutekeleza. Ikiwa watajitunza bila mawaa kutoka kwa ulimwengu, wakiacha kufuata mitindo yake, na kuweka yale ambayo wapenda anasa hutumia pesa zao katika mambo yasiyo na faida ili kuridhisha kiburi, na kuvitoa kwa wenye shida walio na stahiki, na kuitegemeza kazi, watakuwa na kibali/idhini ya Yule anayesema, "Nayajua matendo yako." {1T 190.1}

Niliona kuna utulivu mbinguni, na MUNGU anafurahishwa sana na juhudi za watu Wake katika kujaribu kusonga na mfumo wa kutoa kwa ukarimu katika

kazi Yake hapa duniani. Niliona kwamba lazima kuwe na utaratibu katika kanisa la MUNGU, na mfumo huo unahitajika katika kufanikisha ujumbe wa mwisho ulio na wingi wa rehema kwa ulimwengu. MUNGU anawaongoza watu Wake katika utoaji wa ukarimu kwa mpango, na hii ni mojawapo ya mambo ambayo MUNGU anawaletea watu Wake mambo ambayo yatakata kwa ukaribu zaidi kwa watu wengine. Kwao itakuwa ni sawa na kukata mkono wa kulia, na kung'oa jicho la kulia, wakati kwa wengine ni afueni kubwa. Kwa roho ya uungwana, yenye ukarimu mahitaji juu haya yanaonekana kuwa madogo sana, na hawawezi kuridhika kufanya kidogo. Wengine wana mali kubwa, na ikiwa wameiweka karibu nao kwa madhumuni ya kuitoa kwa ukarimu kama MUNGU alivyowatajirisha, sadaka hiyo inaonekana kwao kama kiasi kikubwa. Moyo wa ubinafsi hushikamana kwa karibu na sadaka ndogo kama unavyoshikamana na sadaka kubwa, na hufanya ile sadaka ndogo ionekane sawa na ile sadaka kubwa sana. {1T 191.1}

Nilielekezwa kutazama nyuma wakati wa kuanza kwa kazi hii ya mwisho. Wakati huo wengine ambao walipenda Ukweli wangeweza kuongelea mara kwa mara juu ya kujikana nafsi. Walijitoa sana ili MUNGU, apeleke Ukweli kwa wengine. Wametangulia kupeleka hazina yao kwenda mbinguni mapema. Ndugu zangu, ninyi ambao mmepokea Ukweli baadaye, na ambao mna mali nyingi, MUNGU amewaita shambani ninyi, siyo tu ili mpate kufurahia Ukweli, bali ili muweze kusaidia kwa mali yenu katika kuendeleza kazi hii kubwa. Na ikiwa una nia ya kazi hii, utajitokeza na kuwekeza kitu ndani yake, ili wengine waokolewe na juhudi zako, utavuna pamoja nao thawabu ya mwisho. Kafara kubwa imetolewa na shida kuvumiliwa ili kuuweka Ukweli wazi wazi mbele yako. Sasa MUNGU anakuita, kwa zamu yako, ujitahidi sana na ujitoe muhanga ili kuweka Ukweli mbele ya wale ambao wako gizani. MUNGU anahitaji ulifanye hili. Unakiri kuamini Ukweli; acha kazi zako zishuhudie Ukweli. Isipokuwa imani yako inafanya kazi, basi itakuwa imekufa. Hakuna chochote isipokuwa imani hai itakayokuokoa katika mandhari za kutisha ambazo ziko mbele yako. {1T 191.2}

Niliona kuwa ni wakati wa wale ambao wana mali kubwa kuanza kufanya kazi haraka. Ni wakati huu ambapo hawataweka tu kwenye hazina vile ambavyo Mungu anawabariki kwa sasa bali hata vile alivyowabariki huko nyuma. Katika siku za mitume, mipango ilikuwa imewekwa hasa kwamba wengine hawapaswi kupunguziwa mizigo na wengine kubebeshwa mizigo. Mipango ilifanywa kwamba wote wanapaswa kushiriki sawa katika mizigo ya kanisa la MUNGU kulingana na uwezo wao kadhaa. Malaika akasema: “Shoka lazima liwekwe kwenye shina la mti.” Wale ambao, kama Yuda, wameweka mioyo yao kwenye hazina ya kidunia watalalamika kama yeye alivyolalamika. Moyo wake ulitamani marashi yale ya gharama yaliyomwagwa juu ya Yesu, na akajaribu kuficha ubinafsi wake chini ya kichaka cha ucha Mungu kwa kuwa na roho ya kuwafikiria masikini: “Kwa nini marashi haya hayakuuzwa kwa dinari mia tatu,

na kupewa maskini?” Alitamani angekuwa na umiliki wa hayo marashi ya gharama kubwa ili yasimwagwe juu ya Yesu kwa ukarimu. Yuda angeyatumia kukidhi mahitaji yake mwenyewe; angeyauza ili apate fedha. Alimthamini Bwana wake kwa udogo tu, kiasi cha kumuuza kwa watu waovu kwa vipande vichache vya fedha. Kama Yuda alivyowatumia maskini kama kisingizio cha ubinafsi wake, ndivyo watu wanaodai kuwa Wakristo, ambao mioyo yao ni ya kutamani, watakavyofuta kuficha ubinafsi wao chini ya kichaka kwamba wana dhamiri ya kufanya kazi yao vyema na kikamilifu. Loo, wanaogopa kwamba katika kupitisha utoaji wa mpango tunakuwa kama makanisa ya jina tu! “Hebu! Mkono wako wa kushoto usijue kinachofanywa na mkono wako wa kulia.” Wanaonekana kuwa na hamu iliyo katika dhamiri ya kufuata kabisa Biblia jinsi wanavyoielewa katika suala hili; lakini wanapuuza kabisa mawaidha wazi ya Kristo: “Uza ulicho nacho, na utoe sadaka.” {1T 192.1}

“Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao.” Wengine wanafikiri Andiko hili linafundisha kwamba lazima iwe siri katika kazi zao za hisani. Nao hufanya kidogo tu, wakijitetea kwa sababu hawajui jinsi ya kutoa. Lakini Yesu aliwaelezea wanafunzi Wake kama ifuatavyo: “Basi wewe utoapo sadaka, usipige panda mbele yako, kama wanafiki wafanyavyo katika masinagogi na njiani, ili watukuzwe na watu. Amin, nawaambieni, Wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe utoapo sadaka, hata mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono wako wa kuume; sadaka yako iwe kwa siri; na Baba yako aonaye sirini atakujazi. Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amin, nawaambia, Wamekwisha kupata thawabu yao.” Walitoa ili waonekane waungwana, bora, wakarimu na watu wema. Walipokea sifa za wanadamu, na Yesu aliwafundisha wanafunzi Wake kwamba hii ndiyo tuzo tu ambayo wangepata. Kwa wengi, mkono wa kushoto haujui mkono wa kulia ufanyalo, kwani mkono wa kulia haufanyi chochote kinachostahili kutambuliwa na mkono wa kushoto. Somo hili la Yesu kwa wanafunzi Wake lilikuwa kemeo kwa wale ambao wangependa kupokea utukufu wa wanadamu. Walifanya utoaji wao wa misaada katika mkutano wa hadhara sana; na kabla ya kufanya hivyo, tangazo la umma lilifanywa kuonyesha kwamba kuna jambo la ukarimu linalokuja mbele ya watu; na wengi walitoa pesa nyingi ili tu jina lao litukuzwe na wanadamu. Na mali zilizotolewa kwa njia hii mara nyingi zilinyang'anywa kutoka kwa wengine, kwa kukamkandamiza mwajiriwa katika mshahara wake, na kwa kuusaga uso wa maskini. {1T 193.1}

Nilioneshwa kwamba Andiko hili halitumiki kwa wale ambao wana mzigo wa kusudi la kazi ya MUNGU moyoni, na wanaotumia mali zao kwa unyenyekevu ili kuiendeleza kazi. Nilielekezwa kwa Maandiko haya: “Nuru yenu na iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu

aliye mbinguni." "Mtawajua kwa matunda yao." Nilioneshwa kuwa ushuhuda wa Maandiko utawiana pale utakapoeleweka vyema. Matendo mema ya watoto wa MUNGU ndiyo mahubiri yenye matokeo bora aliyonayo yule asiyeamini. Anafikiria kwamba lazima kuwe na nia kali ambayo inamshawishi Mkristo kujikana nafsi yake mwenyewe, na kutumia mali zake kujaribu kuwaokoa wanadamu wenzake. Ni tofauti na roho ya ulimwengu. Matunda kama hayo yanashuhudia kwamba wamiliki wa hizo mali ni Wakristo wa kweli. Wanaonekana kuelekea kuifikia juu kila wakati ile hazina ambayo haiwezi kuharibika. {1T 193.2}

Kwa kila karama na sadaka lazima kuwe na kitu kinachofaa mbele ya mtoaji, siyo kuzuia chochote katika hali ya uvivu, siyo kuonekana na watu au kupata jina kubwa, lakini kumtukuza MUNGU kwa kuendeleza kazi yake. Wengine hutoa michango mikubwa kwa kazi ya MUNGU wakati ndugu yao ambaye ni masikini, anaweza kuwa anaugua karibu nao, na hawafanyi chochote kumtuliza. Matendo madogo ya fadhili yaliyofanywa kwa ndugu yao kwa njia ya siri yangeunganisha mioyo yao pamoja, na ingeonekana mbinguni. Niliona kuwa katika bei zao na mshahara matajiri wanapaswa kufanya tofauti kwa niaba ya walioteseka na wajane na maskini wanaostahili kati yao. Lakini ni mara nyingi sana matajiri hufaidika kwa ajili ya maskini, wakivuna kila faida ambayo inapaswa kupatikana, na wakichuma senti ya mwisho kwa kila upendeleo. Yote yameandikwa mbinguni. "Nayajua matendo yako." {1T 194.1}

Dhambi kubwa ambayo sasa ipo kanisani ni kutamani (Amri ya Kumi). MUNGU huwakunjia uso wale wanaojidai ni watu Wake kutokana na ubinafsi wao. Watumishi Wake wametoa sadaka ya wakati wao na nguvu zao ili kubeba Neno la uzima, na wengi wameonesha kwa matendo yao kwamba wanalithamini sana. Ikiwa wanaweza kumsaidia mtumishi wa MUNGU ni sawa tu kama sivyo, ni sawa pia, wakati mwingine hufanya hivyo; lakini mara nyingi wanamruhusu apite, na wanamfanyia kidogo tu. Ikiwa wanaajiri kibarua, lazima wamlipe mshahara kamili. Lakini sivyo ilivyo kwa yule mtumishi wa MUNGU ajitoaye kafara. Anawafanyia kazi katika Neno la Mungu na Mafundisho makuu ya imani Idoctrinel; mtu anayebeba mzigo mzito wa kazi kwenye nafsi yake; kwa uvumilivu anaonesha kutoka kwa Neno la MUNGU makosa na hatari ambavyo ni vibaya kwa roho; anatia mkazo mara moja juu ya ulazima wa kuyang'oa magugu ambayo huisonga mbegu nzuri iliyopandwa; huleta kutoka kwenye ghala la Neno la MUNGU vitu vipya na vya zamani kulisha kundi la MUNGU. Wote wanakiri kwamba wamenufaika naye; lakini magugu yenye sumu, na uchoyo, vimeingiza mizizi chini sana, kiasi cha kumruhusu mtumishi wa MUNGU aondoke bila wao kumsaidia mahitaji yake ya kidunia (chakula, mavazi malazi kwa posho fulani). Wameisifu kazi yake yenye kuchosha sana kama vile vitendo vyao

vinavyodhihirisha. Shahidi wa Kweli anasema: “Nayajua matendo yako.” {1T 194.2}

Niliona kwamba watumishi wa MUNGU hawajawekwa mahali ambapo hawawezi kufikiwa na majaribu ya Shetani. Mara nyingi wanazingwa kwa upesi na adui, na wana vita ngumu ya kupigana. Kama wangeachiliwa kutoka kwa utumishi wao wa uinjilisti, wangefurahi kufanya kazi kwa mikono yao (kubangaiza ili kujikimu). Kazi yao inahitajiwa na ndugu zao; lakini wanapoiona inathaminiwa kidogo, wanafadhaika kwa kukatishwa tamaa. Ukweli ni kwamba hatimaye wanatazamia malipo yao siku ya mwisho Bwana ajapo, na jambo hili linawahimiza kusonga mele; lakini familia zao lazima ziwe na chakula na mavazi wanapoishi hapa duniani. Muda wao ni mali ya kanisa la MUNGU; na siyo wao wenyewe. Wanazitoa mhanga familia zao ili kufaidisha wengine; na bado wengine wanaofaidika na kazi zao hawajali mahitaji yao. Niliona kwamba ni kutowatendea haki watu kama hao kuruhusu waendelee na tabia hiyo huku wakijidanganya wenyewe.Wanadhani wamekubaliwa na MUNGU, wakati ambapo Yeye huchukizwa na ubinafsi wao. Siyo hawa wenye ubinafsi peke yao watakaoitwa kutoa hesabu kwa MUNGU kwa matumizi waliyoyafanya kwa pesa ya Bwana wao, lakini msongo wote na maumivu ya moyo ambayo wamewaletea watumishi waliochaguliwa na MUNGU, na ambayo yamelemaza juhudi zao, vitawekwa kwenye upande wa hesabu ya mawakili hawa wasio waaminifu. {1T 195.1}

Shahidi wa Kweli anatangaza: “Nayajua matendo yako.” Moyo wa ubinafsi, uchoyo, roho yenye tamaa vitajaribiwa. Wengine hawako tayari kumtolea MUNGU sehemu ndogo sana ya ongezeko la hazina yao ya kidunia. Wangeweza kurudi nyuma kwa hofu kama ungewatamkia kanuni hii kuu ya ongezeko. Je! Watu hawa wametoa kafara gani kwa ajili ya MUNGU? Hakuna walichotoa. Wanajidai kuamini kuwa Yesu anakuja; Lakini matendo yao yanakanusha imani yao. Kila mmoja ataiishi imani aliyo nayo. Ninyi mnaojidai mnamkiri MUNGU kwa udanganyifu, Yesu anajua matendo yenu. Yeye Anachukia sadaka zenu za uchoyo, na dhabihu zenu vilema. {1T 195.2}

# SURA YA 34

# NYUMBA ZA IBADA

Niliona kwamba watu wengi ambao MUNGU amewakabidhi mali hujisikia kuwa huru kuitumia wapendavyo kwa faida yao wenyewe katika kujijengea nyumba za kupendeza hapa; lakini wanapojenga nyumba ya kumwabudu MUNGU Mkuu ambaye anakaa milele, hawawezi kumruhusu atumie mali ambazo amewapa. Kila mmoja hafanyi jitihada kumshinda mwenzake kwa kuonesha shukrani yake kwa MUNGU na kwa Ukweli kwa kufanya kila awezalo, ili kuandaa mahali panapofaa pa ibada; lakini wengine wanajaribu kufanya kidogo tu iwezekanavyo; wakihisi kuwa mali wanazozitumia katika kuandaa mahali pa aliye juu zaidi ni kama mali zilizopotea ambazo hutamani kuja kuziona siku nyingine. Sadaka kama hizo ni vilema, na hazikubaliki kwa MUNGU. Niliona kuwa ingemfurahisha zaidi MUNGU kama watu Wake wangeonesha hekima nyingi katika kumuandalia nyumba Yeye, kama vile wanavyofanya katika makazi yao wenyewe. {1T 196.1}

Iliamriwa dhabihu na sadaka za wana wa Israeli ziwe zisizo na lawama wala doa, zilizo bora kutoka kundini; na kila mtu alitakiwa kushiriki katika kazi hii. Kazi ya MUNGU kwa wakati huu itakuwa kubwa. Ukimjengea Bwana nyumba, usimkosee na kumwekea mipaka kwa kumtolea sadaka yako kilema. Weka sadaka bora kabisa katika nyumba iliyojengwa kwa ajili ya MUNGU. Hebu ifanye kuwa bora kwa kadri uwezavyo; ukionesha shauku/nia ya kuifanya iwe isiyosumbua na inayofurahisha. Wengine hudhani kuwa jambo kama hili halina matokeo katika siku zijazo kwa kuwa muda ni mfupi sana kabla ya Yesu kuja. Baada ya kufanya hivyo kwa nyumba ya MUNGU basi fanya hivyo hivyo katika makazi yako, na katika mipangilio yako yote ya kidunia (jenga nyumba mbaya na ya muda mfupi kwa vile Yesu anakuja hivi karibuni, kama ulivyosema kuhusu kanisa). {1T 196.2}

Niliona kwamba MUNGU angeweza kuendelea na kazi Yake bila msaada wowote wa mwanadamu; lakini huu siyo mpango Wake. Ulimwengu wa sasa umeundwa kama eneo la majaribio kwa mwanadamu. Mwanadamu yuko hapa kuunda tabia ambayo itapita pamoja naye katika ulimwengu wa milele. Mema na mabaya yamewekwa mbele yake, na hali yake ya baadaye inategemea uchaguzi anaoufanya. Kristo alikuja kubadilisha sasa mawazo na mapenzi yake. Moyo wake lazima uondolewe kwenye hazina yake ya kidunia, na kuwekwa juu ya hazina yake ya mbinguni. Kwa kujikana kwake nafsi, MUNGU anaweza kutukuzwa. Kafara kubwa imetolewa kwa ajili ya mwanadamu, na sasa mtu atapimwa na kuthibitishwa kuona ikiwa atafuata mfano wa Yesu, na kutoa dhabihu kwa wenzake. Shetani na malaika zake wameungana dhidi ya watu wa MUNGU; lakini Yesu anatafuta kuwatakasa ili wawe Wake. Anawataka waendeleze kazi Yake. MUNGU amewekeza kwa watu Wake katika ulimwengu

huu vitu vya kutosha kuendeleza kazi Yake bila kuingia aibu, na ni mpango Wake kwamba mali ambazo amewakabidhi zitumike kwa busara. “Uza ulicho nacho, na utoe sadaka,” ni sehemu ya Neno takatifu la MUNGU. Watumishi wa MUNGU lazima wainuke, na kulia, kupiga kelele kwa sauti kubwa, bila kukoma/kuacha, ili “wawaoneshe watu Wangu makosa yao, na nyumba ya Yakobo dhambi zao.” Kazi ya MUNGU inapaswa kuwa pana zaidi, na ikiwa watu Wake watafuata ushauri Wake, hakutakuwa na mali nyingi katika umiliki wao zitakazoangamizwa katika moto wa mwisho. Wote watakuwa wameweka hazina yao ambapo nondo na kutu haziwezi kuharibu; na moyo hautakuwa na kamba ya kuufungia hapa duniani. {1T 196.3}

## SURA YA 35

## MASOMO KUTOKA KATIKA MIFANO

Nilioneshwa kuwa mfano wa talanta haujaeleweka kikamilifu. Somo hili muhimu lilipewa wanafunzi kwa faida ya Wakristo wanaoishi katika siku za mwisho. Na talanta hizi haziwakilishi tu uwezo wa kuhubiri na kufundisha neno la MUNGU. Mfano huu unawakilisha mali za kitambo ambazo MUNGU amewakabidhi watu wake. Wale ambao walipewa talanta tano na mbili, walifanya biashara na kuongeza mara mbili ya vile walivyopewa dhamana. MUNGU anawataka wale walio na mali hapa, watoe pesa zao kwa watoao riba – ili waziweke katika kazi ya kueneza ukweli. Na ikiwa Ukweli unaishi ndani ya moyo wa mpokeaji, yeye pia atasaidia mali yake katika kuipeleka kwa wengine; na kupitia kwa juhudi zake, ushawishi wake, na mali zake, na roho zingine zitakubali ukweli, na kuanza pia kumtumikia MUNGU. Niliona kwamba watu wengine wanaojidai ni wa MUNGU wapo kama yule mtu aliyeficha talanta yake ardhini. Wanazuia mali zao zisifanye mema katika kazi ya MUNGU. Wanadai kuwa hizi ni zao wenyewe, na wana haki ya kuzifanyia kile wanachopenda wao

wenyewe; na hivyo roho haziongolewi na juhudi za busara zinazofanywa nao kwa kutumia pesa za Bwana wao. Malaika huweka kumbukumbu ya uaminifu wa kazi ya kila mtu, na wakati hukumu inapopita juu ya nyumba ya MUNGU, hukumu ya kila mmoja imeandikwa kwa jina lake, na malaika huamriwa kutowahurumia wale watumishi wasio waaminifu, bali kuwakatilia mbali wakati hu wa machinjo. Na kile kilichowekezwa kwao kwa uaminifu huchukuliwa kutoka kwao. Hazina yao ya kidunia hufagiliwa mbali, nao hupoteza vyote. Na taji ambazo wangeweza kuvaa, kama wangekuwa waaminifu, huwekwa juu ya vichwa vya wale waliookolewa na watumishi waaminifu ambao mali zao zilikuwa zikitumika kwa MUNGU kila wakati. Na kila aliyefanyika njia za kuokolea, aliongeza nyota kwenye taji yake kwa utukufu, naye aliongeza thawabu yake ya milele. {1T 197.1}

Nilioneshwa pia kwamba mfano wa msimamizi asiye mwadilifu ulikuwa ni kusudi la kutufundisha somo. "Jifanyieni rafiki kwa mali ya udhalimu, ili itakapokosekana wawakaribishe katika makao ya milele." Ikiwa tutatumia uwezo wetu kwa utukufu wa MUNGU hapa, tutaweka hazina mbinguni; na wakati mali za dunia zitakapoisha, msimamizi mwaminifu atakuwa na Yesu na malaika kama rafiki zake, wa kumpokea nyumbani kwa makazi ya milele. {1T 198.1}

"Yeye aliye mwaminifu katika lililo dogo zaidi ni mwaminifu katika lililo kubwa pia." Yeye ambaye ni mwaminifu katika mali zake za kidunia, ambazo ni ndogo, akitumia busara ya kile MUNGU alichomkopesha hapa, atakuwa mkweli kwa madai yake. "Yeye ambaye ni dhalimu katika jambo dogo ni dhalimu pia katika mengi." Yeye ambaye atamzuia MUNGU kile ambacho amemkopesha, atakuwa mwaminifu katika mambo ya MUNGU kwa kila jambo. "Basi ikiwa ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli?" Kama tutathibitisha kuwa tumekuwa wasio waaminifu katika usimamizi wa mambo wa MUNGU hapa, yeye hawezi kamwe kutupa urithi wa milele." Na kama hamkuwa waaminifu katika mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?" Yesu amenunua ukombozi kwa ajili yetu. Ni wetu; lakini tumewekwa hapa kwa majaribio ili kuona ikiwa tutathibitisha kuwa tunastahili uzima wa milele. MUNGU anatufanyia uhakiki kwa kutuamini na mali za kidunia. Ikiwa sisi ni waaminifu kutoa bure yale aliyotuazimisha, ili kuendeleza kazi yake, MUNGU anaweza kutukabidhi urithi wa milele. "Huwezi kumtumikia MUNGU na mali." "Ikiwa mtu yeyote penda ulimwengu, upendo wa Baba haumo ndani yake. "{1T 198.2}

MUNGU hukasirishwa na ulegevu, na njia dhaifu ambazo kwazo wale wanaodai ni watu wake hufanya shughuli zao za kidunia. Wanaonekana kupoteza ukweli kwamba mali zote wanazotumia ni za MUNGU, na kwamba lazima watoe hesabu ya usimamizi wao. Wengine huacha shughuli zao za kidunia zikiwa katika hali ya kuvurugika kabisa. Shetani ana jicho lake juu ya yote, na anatafuta nafasi nzuri, na kupitia usimamizi wake anachukua mali nyingi kutoka kwa watunza

Sabato. Na hii inamaanisha mali hizo huenda katika upande wake. Wengine ambao ni wazee hawataki kufanya biashara yoyote ya kidunia, na kwa wakati usiotarajiwa wanaugua na kufa. Watoto wao ambao hawana nia ya ukweli, huchukua mali. Shetani ameisimamia kama imfaavyo. “Basi, ikiwa hamkuwa waaminifu kwa mali isiyo ya haki, ni nani atakayewakabidhi mali ya kweli? Na ikiwa hamkuwa waaminifu katika mali ya mtu mwingine, ni nani atakayekupeni mali yenu?” {1T 199.1}

Nilioneshwa ukweli mbaya kwamba Shetani na malaika zake wamekuwa wakiisimamia zaidi mali ya watu wanaodai ni wa MUNGU kuliko Bwana mwenyewe anavyowasimamia. Mawakili wa siku za mwisho hawana busara. Wanamruhusu Shetani kudhibiti mambo yao ya kibiashara, na hupeleka katika safu yake kile kilichokuwa kinapaswa kuwa katika, kazi ya MUNGU. MUNGU anakufuatilia wewe, wakili usiye mwaaminifu; atakuita uwajibike. Niliona ya kuwa mawakili wa MUNGU kwa usimamizi mwaminifu, wenye busara wanaweza kuweka biashara zao katika ulimwengu huu, zikiwa nyoofu, zilizo sawa, na zisizo na makosa. Na ni haki na jukumu la wazee, wanyonge, na wale ambao hawana watoto, kuweka mali zao mahali ambapo zinaweza kutumiwa kwa kazi ya MUNGU ikiwa wataondolewa ghafla. Lakini niliona Shetani na malaika zake wakifurahi juu ya kufaulu kwao katika jambo hili. Na wale ambao wanapaswa kuwa warithi wenye busara wa wokovu kwa hiari huziacha pesa za Bwana wao zitoke mikononi mwao na kuingia katika safu ya adui. Kwa njia hii wanaimarisha ufalme wa Shetani, na wanaonekana kuifurahia sana hali hii. {1T 199.2}

## SURA YA 36

## DHAMANA KWA WASIOAMINI

Niliona kwamba MUNGU alikasirishwa na watu Wake kwa kuwa wadhamini kwa wale wasioamini. Nilielekezwa kwa maandiko haya: Mithali 22:26: “Usiwe mmoja wao wawekao rehani; Au walio wadhamini kwa deni za watu.” Mithali 11:15: “Amdhaminiye mgeni hakosi ataumia; Achukiaye mambo ya dhamana yu salama.” Mawakili wasio waaminifu! Wanaahidi ambayo ni ya mwingine (rehani), - Baba yao wa mbinguni, - na Shetani yuko tayari kusaidia watoto wake kuipora kwa nguvu kutoka mikononi mwao. Watunza Sabato hawapaswi kushirikiana na wasioamini. Watu wa MUNGU wanaamini sana maneno ya watu baki wasiowajua au wageni, na huomba kutoka kwao ushauri na maelekezo yao wakati hawapaswi kufanya hivyo. Adui huwafanya kuwa mawakala wake, na hufanya kazi kupitia kwao akiwatatanisha na kuchukua kutoka kwa watu wa MUNGU. {1T 200.1}

Wengine hawana busara katika usimamizi wa mambo ya kidunia. Hawana sifa zinazohitajika, na Shetani anaitumia fursa hiyo. Ikiwa hii ndiyo hali halisi, hawa hawapaswi kubaki katika ujinga wa kazi yao. Wanapaswa kuwa wanyenyekevu vya kutosha hata kushauriana na ndugu zao, ambao wanaweza kuwa na ujasiri kwa maamuzi yao, kabla ya kutekeleza mipango. Nilikuwa nimeelekezwa kwa maandishi haya: "Bebeaneni mizigo yenu." Wengine siyo wanyenyekevu vya kutosha kuruhusu wale ambao wana hekima katika maamuzi wawasaidie katika kufanyia kazi mambo ipasavyo mpaka watakapofuata mipango yao wenyewe, na kukumbana na shida. Ndipo wanaona umuhimu wa kupata ushauri na maamuzi ya ndugu zao; lakini jinsi sasa unavyokuwa mzigo mzito kuliko hapo mwanzo. Ndugu hawapaswi kwenda kwenye mfumo wa sheria kama inaweza kuepukwa; hilo humpa adui faida kubwa ya kuwatega na kuwachanganya. Ingekuwa bora kufanya mapatano hata kama ni kwa hasara fulani. {1T 200.2}

# SURA YA 37

# KUAPA

Niliona kuwa baadhi ya watoto wa MUNGU wamefanya makosa kwa sababu ya kula kiapo, na Shetani ametumia fursa hii kuwakandamiza, na kuchukua kutoka kwao pesa za Bwana wao. Niliona kwamba Maneno ya Bwana wetu, "Usiape kabisa," hayagusi kiapo cha mahakama. "Mawasiliano yenu na yawe, Ndiyo, ndiyo; Hapana, hapana, kwani chochote kilicho zaidi ya hizi hutoka kwa mwovu." Hii inahusu mazungumzo ya kawaida. Wengine wanatia chumvi katika mazungumzo yao. Wengine huapa kwa maisha yao wenyewe; wengine huapa kwa vichwa vyao - hakika kama wanavyoishi; maadamu wana kichwa. Wengine huialika mbingu na nchi kushuhudia kwamba yale wayasemayo ndivyo yalivyo hasa. Wengine wanatumaini kwamba MUNGU atawaondoa duniani iwapo wanachosema siyo kweli. Ni aina hii ya kawaida ya kuapa ambayo Yesu anawaonya wanafunzi Wake. {1T 201.1}

Tuna watu waliowekwa juu yetu kama watawala, na sheria za kutawala/kusimamia watu. Kama isingekuwa kwa sheria hizi, hali ya ulimwengu ingekuwa mbaya kuliko ilivyo sasa. Baadhi ya sheria hizi ni nzuri, zingine ni mbaya. Mabaya yamekuwa yakiongezeka, na bado tutaletwa kuletwa katika maeneo yaliyo magumu sana. Lakini MUNGU atawategemeza watu Wake kwa kuwa thabiti na kuishi kulingana na kanuni za Neno Lake. Wakati sheria za wanadamu zinapingana na Neno na sheria ya MUNGU, tunapaswa kutii sheria za

MUNGU, bila kujali matokeo yake yatakuwa nini. Sheria ya nchi yetu inayotutaka tumtoe mtumwa kwa bwana wake, hatupaswi kuitii; na lazima tubebe matokeo ya kukiuka sheria hii. Mtumwa siyo mali ya mtu yeyote. MUNGU Ndiye Bwana wake halali, na mwanadamu hana haki ya kuchukua kazi ya MUNGU mikononi Mwake, na kumdai kuwa ni wake. {1T 201.2}

Niliona kwamba Bwana bado ana uhusiano fulani na sheria za nchi. Wakati Yesu akiwa katika Patakatifu, Roho ya MUNGU inayozuia huhisiwa na watawala na watu/raia. Lakini Shetani anatawala kwa kiwango kikubwa cha umati wa ulimwengu, na kama isingekuwa sheria za nchi, tungepaswa kupata mateso mengi. Nilioneshwa kwamba ikiwa ni lazima sana, na wanaombwa kutoa ushahidi kwa njia halali, siyo ukiukaji wa Neno la MUNGU kwa watoto Wake kumchukua MUNGU kuwa shahidi wao wa kile wanachosema ni ukweli, na ni kweli tupu. {1T 202.1}

Mwanadamu ni fisadi sana kiasi kwamba sheria zinawekwa ili kuweka jukumu juu ya kichwa chake mwenyewe. Watu wengine hawaogopi kusema uongo kwa wenzao; lakini wamefundishwa, na ROHO WA MUNGU anayewazuia amewavutia, kwamba ni jambo la kuogopesha kumdanganya MUNGU. Kesi ya Anania na Safira mkewe imetolewa kuwa mfano. Jambo hilo limebebwa kutoka kwa mwanadamu kwenda kwa MUNGU, hivi kwamba ikiwa mtu atatoa ushahidi wa uongo, atakuwa anafanya hivyo siyo kwa mwanadamu, bali kwa MUNGU mkuu, ambaye anasoma moyo, na anajua ukweli halisi katika kila kesi. Sheria zetu zinafanya kuwa uhalifu mkubwa kula kiapo cha uongo. MUNGU mara nyingi ametembelea hukumu juu ya kiapo cha uongo, na hata wakati kiapo hicho kilipokuwa midomoni mwake, malaika aangamizaye alimkata. Hili lilifanyika kudhihirisha ugaidi kwa watenda maovu. {1T 202.2}

Niliona kwamba ikiwa kuna mtu yeyote duniani ambaye anaweza kushuhudia mara kwa mara chini ya kiapo, basi ni Mkristo. Anaishi katika nuru ya sura ya MUNGU. Anakuwa mwenye nguvu katika nguvu Zake. Na pale mambo ya umuhimu yanapokuwa ni lazima yaamuliwe na sheria, hakuna mtu anayeweza kumwomba na kumsihi MUNGU kama Mkristo. Nilialikwa na malaika kugundua kuwa MUNGU anaapa Kwake Yeye Mwenyewe. Mwanzo 22:16; Waebrania 6:13, 17. Alimuapia Ibrahimu (Mwanzo 26: 3), kwa Isaka (Zaburi 105: 9; Yeremia 11: 5), na kwa Daudi (Zaburi 132: 11; Matendo 2:30). MUNGU aliwataka wana wa Israeli kufanya kiapo kati ya mwanadamu na mwanadamu. Kutoka 22:10, 11. Yesu aliwakuwa chini kiapo katika saa ya kesi Yake. Kuhani mkuu akamwambia: “Nakuapisha kwa MUNGU aliye hai, kwamba utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa MUNGU.” Yesu akamwambia: “Wewe umesema.” Ikiwa Yesu katika mafundisho Yake kwa wanafunzi Wake angerejelea kiapo cha hukumu/mahakama, angemkemea kuhani mkuu, na hapo angetekeleza na kuyaimarisha tena mafundisho Yake, kwa faida ya wafuasi

Wake waliokuwepo. Shetani amefurahishwa kwamba wengine wameona kiapo kinachukua maoni mabaya; kwani imempa nafasi ya kuwaonea na kuchukua kutoka kwao pesa za Bwana wao. Mawakili wa MUNGU lazima wawe na busara zaidi, kuweka mipango yao, na kujiandaa kukabiliana na hila za Shetani; kwani anapaswa kufanya juhudi kubwa zaidi kuliko hapo awali. {1T 202.3}

Wengine, niliwaona, wana ubaguzi na chuki dhidi ya watawala wetu na sheria; lakini kama isingekuwa sheria, ulimwengu huu ungekuwa katika hali ya kutisha. MUNGU huwazuia watawala wetu; kwani mioyo ya wote iko mikononi Mwake. Mipaka imewekwa, zaidi ya ambayo hawawezi kwenda au kupitiliza. Watawala wengi ni wale ambao Shetani anawadhibiti; lakini nikaona kwamba MUNGU anao mawakala Wake, hata miongoni mwa watawala. Na wengine wao bado wataongolewa na Ukweli. Sasa wanafanya sehemu ambayo MUNGU alitaka wawe nayo. Wakati Shetani anafanya kazi kupitia mawakala wake, mapendekezo yanatolewa, kwamba, ikiwa yatatekelezwa, yatazuia kazi ya MUNGU na kusababisha maovu makubwa. Malaika wazuri hujongea kwa mawakala hawa wa MUNGU, na kugusa mioyo yao ili kupinga mapendekezo kama haya kwa sababu za nguvu, ambazo mawakala wa Shetani hawawezi kupinga. Mawakala wachache wa MUNGU watakuwa na nguvu ya kushinikiza chini uovu mwingi. Kwa hivyo kazi itaendelea hadi ujumbe wa tatu umekamilisha kazi yake, na kwa sauti kuu ya malaika wa tatu, mawakala hawa watapata fursa ya kupokea Ukweli, na wengine wao wataongoka, na kuvumilia na watakatifu kupitia wakati wa taabu. Wakati Yesu anaondoka Patakatifu mno, Roho Yake inayozuia huondolewa kutoka kwa watawala na wanadamu. Wameachwa chini ya udhibiti wa malaika wabaya. Ndipo sheria kama hizo zitatungwa na mabaraza kwa ushauri wa Shetani, ambapo kama siku hizo zisingefupishwa, hakuna mwenye mwili ambaye angeokolewa. {1T 203.1}

## SURA YA 38

## MAKOSA KATIKA LISHE

Ndugu mpendwa na Dada A: Bwana ameona ni sawa kwa wema Wake kunipa maono mahali hapa; na kati ya mambo tofauti niliyooneshwa kulikuwa na mengine yanayohusiana na wewe. Niliona kuwa yote hayakuwa sawa kwako. Adui amekuwa akitafuta uharibifu wako, na akijaribu kushawishi wengine kwa njia yako. Niliona kwamba nyinyi wawili mnachukua nafasi iliyoinuliwa ambayo MUNGU hajawahi kuwapa, na kwamba nyinyi wawili mnajifikiria mko mbele zaidi ya watu wa MUNGU. Nilikuona ukitazama Battle Creek na wivu na mashaka/kushuku. Ungeweka mikono yako hapo, na kuunda matendo na mienendo yao kwa kile unachodhani kilikuwa sawa. Unachunguza mambo madogo ambayo huyaelewi, ambayo hujui namna ya kushughulika nayo, na ambayo hayakuhusu kabisa. MUNGU amekabidhi kazi Yake huko BC kwa watumishi waliochaguliwa. Ameweka mzigo wa kazi juu yao. Malaika wa

MUNGU wameagizwa kusimamia kazi hiyo; na ikiwa haitaenda sawa, wale ambao ni wakuu wa kazi watabadilishwa, na mambo yatasonga kwa utaratibu wa MUNGU bila kuingiliwa na huyu au yule. {1T 204.1}

Niliona kwamba MUNGU anataka ugeuze mawazo yako kwako wewe wenyewe. Ijaribu nia yako-Jichunguze. Unajidanganya kuhusu wewe mwenyewe. Una muonekano wa unyenyekevu, na hii ina ushawishi kwa wengine, na inawafanya wafikirie kuwa umesonga mbele sana katika maisha ya Kikristo; lakini maoni yako ya kipekee yanapoguswa, ubinafsi huinuka mara moja, na unadhihirisha roho ya kukusudia, na ukaidi. Huu ni uthibitisho dhahiri kwamba huna unyenyekevu wa kweli. {1T 204.2}

Niliona kwamba ulikuwa na maoni potofu juu ya kuumiza mwili wako, na kujinyima chakula chenye lishe. Vitu hivi husababisha baadhi ya makanisa kufikiri kwamba MUNGU Yuko pamoja nawe, vinginevyo usingejikana mwenyewe, na kujitoa kafara hivi. Lakini niliona kuwa hakuna moja ya mambo haya yatakayo kufanya uwe mtakatifu zaidi. Wapagani hufanya haya yote, lakini hawapati thawabu kwa hilo. Roho iliyovunjika na kupondeka mbele za MUNGU ndiyo yenye thamani kubwa mbele Zake. Niliona kuwa maoni yako juu ya mambo haya yana makosa, na kwamba unalitazama kanisa na kulichunguza, ukitafuta vitu vidogo, wakati umakini wako ungepaswa kuelekezwa kwa maslahi ya nafsi yako mwenyewe. MUNGU hajaweka mzigo wa kundi Lake juu yako wewe. Unafikiri kwamba kanisa liko nyuma, kwa sababu hawawezi kuona vitu kama wewe, na kwa sababu hawafuati mkondo ule ule mgumu ambao unafikiri unastahili kufuata. Niliona kuwa umedanganywa kuhusu jukumu lako mwenyewe na wajibu wa wengine. Wengine wamepitiliza kiasi juu ya lishe. Wamechukua mwendo mgumu, na walisihi wazi kabisa kwamba afya zao zimeumia, magonjwa yameimarika katika mfumo, na hekalu la MUNGU limedhoofishwa. {1T 205.1}

Nilirudishwa kwenye uzoefu wetu huko Rochester, New York. Niliona kwamba wakati tulipoishi huko hatukula chakula chenye lishe kama tunavyopaswa, na ugonjwa ulikaribia kutupeleka kaburini. Niliona kwamba kama vile MUNGU avyopompa usingizi mpendwa Wake, Yeye Yupo tayari pia kumpa kile chakula kinachofaa ili kurutubisha nguvu. Kusudi tulilokuwa nalo lilikuwa safi. Ilikuwa kuokoa kazi, ili gazeti liweze kudumishwa. Tulikuwa masikini. Niliona kwamba kosa wakati huo lilikuwa kanisani. Wale ambao walikuwa na mali walikuwa wenye tamaa na ubinafsi. Kama hawa wangefanya sehemu yao, mzigo ulio juu yetu ungerahisishwa na kuwa mwepesi; lakini pale wengine hawakufanya sehemu yao, tulibebeshwa mzigo mzito na wengine kurahisishiwa. Niliona kwamba MUNGU hahitaji mtu yeyote kuchukua mzigo mgumu wa kubana matumizi katika uchumi wao, hata kudhoofisha au kuumiza hekalu la MUNGU. Kuna majukumu na mahitaji katika Neno Lake katika kulinyenyekeza kanisa na kuwasababishia kutesa roho zao, na hivyo hakuna haja ya kutengeneza

misalaba na kutengeneza majukumu ya kuusumbua mwili ili kusababisha unyenyekevu. Yote haya yako nje ya Neno la MUNGU. {1T 205.2}

Wakati wa taabu upo mbele yetu; na kisha ulazima wa dhati utahitaji watu wa MUNGU kujikana, na kula tu kile chakula kinachotosha kuendeleza maisha; lakini MUNGU atatuandaa kwa wakati huo. Katika saa hiyo ya kutisha hitaji letu litakuwa fursa ya MUNGU kutoa nguvu Zake za kuimarisha, na kuwategemeza watu Wake. Lakini sasa MUNGU anawataka wafanye kazi kwa mikono yao, jambo lililo jema, na kuweka karibu nao akiba kwa kadri walivyofanikiwa, na wafanye sehemu yao katika kudumisha hoja ya Ukweli. Hili ni jukumu ambalo limeamriwa kwa wale wote ambao hawajaitwa kwa namna maalumu kufanya kazi kwa Neno na Mafundisho ya imani, kutumia wakati wao kutangaza kwa wengine njia ya uzima na wokovu. {1T 206.1}

Wale wanaofanya kazi kwa mikono yao lazima wanawirishe nguvu zao ili kufanya kazi Yake, na wale pia ambao hufanya kazi kwa Neno na Mafundisho ya imani, lazima wanawirishe nguvu zao; kwani Shetani na malaika zake wabaya wanapigana nao ili kubomoa nguvu zao. Wanapaswa kutafuta pumziko la mwili na akili kutokana na kazi ya kuchosha kwa kadri wawezavyo, na wanapaswa kula chakula chenye lishe, na kuimarisha chakula ili kujenga nguvu zao; kwani watalazimika kutumia nguvu zote walizonazo. Niliona kuwa haimpi MUNGU utukufu hata kidogo kwa yeyote kati ya watu Wake, kujitengenezea wakati wa taabu shida kwaajili yao wenyewe. Kuna wakati wa shida mbele ya watu wa MUNGU, na Yeye atawaandaa kwa vita hiyo ya kutisha. {1T 206.2}

Niliona kuwa mtazamo wako juu ya nyama ya nguruwe [ushuhuda huu wa ajabu uliandikwa oktoba 21, 1858, karibu miaka mitano kabla ya maono makubwa ya 1863, ambapo nuru juu ya matengenezo ya afya ilitolewa (kwa mara ya kwanza kupitia maono). Wakati nuru sahihi ilipofika, somo lilitolewa kwa namna iliyowahamasisha watu wetu wote. Hekima na wema wa MUNGU ni vya ajabu kiasi gani! Huenda kwa ujumbe wa sasa ikawa ni kosa kuweka pamoja kwa wingi maziwa, chumvi, na sukari , kama ilivyokuwa kosa kupuuzia swala la nguruwe mwaka 1858. J.W., angalia toleo la pili]. Ujumbe usingekuwa na madhara kama ungebaki nao wewe mwenyewe; lakini kwa maamuzi yako na mtazamo wako umelifanya swala hili kuwa kipimo na matendo yako yameonesha wazi wazi imani yako katika swala hili. Ikiwa MUNGU anataka watu wake wajiepusha na nyama ya nguruwe, atawasadkisha juu ya jambo hilo. Yeye Yuko tayari kuwaonesha watoto Wake waaminifu wajibu wao, kama alivyo tayari kuwaonesha wajibu wao, watu ambao hajaweka mzigo wa kazi Yake juu yao. Ikiwa ni jukumu la kanisa kujiepusha na nyama ya nguruwe, MUNGU atalifunua jambo hilo kwa watu zaidi ya wawili au watatu. Atalifundisha kanisa Lake wajibu Wake. {1T 206.3}

MUNGU anawaongoza watu, siyo kwa mfumo wa watu wachache kadhaa hapa na pale, mmoja akiamini jambo hili, na mwingine jambo lile. Malaika wa MUNGU wanafanya kazi iliyowekwa kwa uaminifu juu yao. Malaika wa tatu anaongoza na kuwatakasa watu, nao wanapaswa kutembea naye kwa umoja. Wengine hukimbia mbele ya malaika wanaowaongoza watu hawa; lakini wanapaswa kukagua kila hatua, na kwa unyenyekevu kufuata si kwa haraka sana kuliko malaika wanavyoongoza. Niliona kwamba malaika wa MUNGU wasingewaongoza watu Wake kwa kasi kuliko wanavyoweza kuhimili na kuutendea Ukweli muhimu uliotolewa kwao. Lakini roho zingine zisizo na utulivu hazifanyi kazi yao zaidi ya nusu. Malaika anapowaongoza, wanafanya haraka kupata kitu kipya, na hukimbilia bila mwongozo wa Kiungu, na kwa hivyo huleta machafuko na mafarakano katika safu. Hawazungumzi au kutenda kwa usawa na mwili. Niliona kwamba nyinyi wawili lazima muletwe haraka mahali mnapotaka kuongozwa, badala ya kutamani kuongoza, au Shetani ataingia na kuwaongoza katika njia yake, kufuata ushauri wake. Wengine huangalia maoni yako yaliyowekwa, na wanachukulia kama ushahidi wa unyenyekevu. Wanadanganywa. Nyinyi wawili mnafanya kazi itakayopasa mfanye toba. {1T 207.1}

Ndugu A, wewe ni bahili kwa asili na mwenye tamaa. Unatoa zaka ya mnanaa na bizari, lakini unaacha mambo mazito zaidi. Wakati kijana tajiri alipokuja kwa Yesu, na kumwuliza afanye nini ili kupata uzima wa milele, Yesu alimwambia azishike amri. Alitangaza kwamba alikuwa amefanya hivyo. Yesu akasema, “Unapungukiwa na jambo moja. Nenda kauze uliyonayo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni.” Matokeo yake yalikuwa kijana huyo alienda akiwa na huzuni, kwani alikuwa na mali nyingi. Niliona kuwa ulikuwa na maoni yasiyofaa. MUNGU anahitaji uchumi wa watu Wake; lakini wengine wamenyumbulisha uchumi wao mpaka ukawa ubahili. Natamani ungeweza kuona kesi yako kama ilivyo. Huna roho ya kweli ya dhabihu, ambayo inakubalika kwa MUNGU. Unawatazama wengine, na kuwachunguza, na ikiwa hawajielekezi kwenye njia ile ngumu unayoifuata, huwezi kuwafanyia chochote. Roho zenu zinanyauka chini ya ushawishi mbaya wa makosa yenu mwenyewe. Roho ya ushupavu, ya kupitiliza iko pamoja nawe, ambayo unaichukulia kuwa ni ROHO WA MUNGU. Hakika umedanganyika. Huwezi kuchukuliana na ushuhuda ulio wazi. Ungependa upewe ushuhuda mlaini tu; lakini mtu yeyote anapokemea makosa yako, ni haraka kiasi gani ubinafsi wako unainuka. Roho zenu hazijanyenyekeshwa. Una kazi ya kufanya……. Vitendo kama hivyo, roho kama hiyo, niliona, ilikuwa matunda ya makosa yako, na matunda ya kuweka uamuzi wako na maoni kama sheria kwa wengine, na dhidi ya wale ambao MUNGU amewaita shambani Mwake. Wote mmevuka mpaka. {1T 207.2}

Niliona kuwa umefikiri kuwa huyu na yule wameitwa kufanya kazi shambani, wakati haujui chochote. Wewe huwezi kusoma moyo. Kama ungeunywa kwa

undani ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu, usingekuwa huru sana kuwaambia ni nani walioitwa na MUNGU, na nani hawakuitwa. Ukweli kwamba mtu anaweza kuomba na kuzungumza vizuri siyo ushahidi kwamba MUNGU amemwita. Kila mtu ana ushawishi, na ushawishi huo unapaswa kuzungumza kwa niaba ya MUNGU; lakini swali ikiwa huyu au yule atumie wakati wake kufanya kazi kwa ajili ya nafsi, ni la muhimu sana, na hakuna mtu isipokuwa MUNGU anayeweza kuamua ni nani atakayefanya kazi hiyo nzito na ya wakfu. Kulikuwa na watu wazuri katika siku za mitume, watu ambao wangeweza kuomba kwa nguvu na kuzungumza kwa uhakika; lakini mitume, ambao walikuwa na nguvu juu ya pepo wachafu na waliweza kuponya wagonjwa, hawakuthubutu kwa hekima yao tu kumtenga mtu kwa kazi takatifu ya kuwa mdomo wa MUNGU. Walisubiri ushahidi usio na shaka wa udhihirisho wa ROHO MTAKATIFU. Niliona kwamba MUNGU alikuwa amewapa wahudumu Wake wateule jukumu la kuamua ni nani anafaa kwa kazi takatifu; na kwa umoja na kanisa na ishara dhahiri za ROHO MTAKATIFU, walipaswa kuamua ni nani anapaswa kwenda na ni nani hawakustahili kwenda. Niliona kwamba ikiwa itaachwa kwa watu wachache hapa na pale kuamua ni nani anayetosha kwa kazi hii kubwa, kuchanganyikiwa na kuvuruga kungekuwa ndiyo matokeo ya kila mahali. {1T 208.1}

MUNGU ameonesha mara kwa mara kwamba watu hawapaswi kutiwa moyo kwenda shambani bila uthibitisho dhahiri kwamba Yeye amewaita. Bwana hatakabidhi mzigo wa kuchunga kundi Lake kwa watu wasio na sifa. Wale ambao MUNGU huwaita lazima wawe watu wenye uzoefu wa kina, waliojaribiwa na kuthibitishwa, watu wenye uamuzi mzuri, watu ambao watathubutu kukemea dhambi kwa roho ya upole, na watu ambao wanaelewa jinsi ya kulisha kundi. MUNGU anajua moyo, na anajua ni nani wa kumchagua. Ndugu na Dada A wanaweza kuamua katika jambo hili, na wote wakosee. Hukumu/maamamuzi yako si kamilifu, na unaweza usiwe na ushahidi katika suala hili. Niliona kwamba ulikuwa ukienda mbali na kanisa, na ikiwa utaendelea kufanya hivyo, yatakukuta mengi; kwani MUNGU atakuacha uende, uteseke kwa kufuata njia yako mwenyewe. {1T 209.1}

MUNGU anakualika sasa ili uweke mambo sawa/sahihi, pimeni nia zenu, na kujitahiki kuwa na mapatano na watu Wake. Mannsville, New York, Oktoba 21, 1858. {1T 209.2}

# SURA YA 39

# UVIVU WAKEMEWA

(Wakati huu kanisa lilikuwa bado halina jina au halijapangwa, walijiita majina kama Masalio wa kundi dogo, Kundi lililotawanyika nk Mchungaji James White alileta masuala kama majengo ya kundi, Huduma ya uchapishaji, sheria ya kundi, mirathi na kwamba kama kundi wangewekaje mambo yao kwa usalama, wengi walifikiri ni dhambi kuwa na jina na kuwa taasisi kwani itakuwa kama Babeli. Uchapaji ulianza kabla ya kanisa kupangwa…….Soma zaidi kuhusu hili)

Ndugu Wapendwa na Dada: Bwana kwa mara nyingine tena amenitembelea kwa rehema, katika wakati wa kufiwa na mateso makubwa. Desemba 23, 1860, nilichukuliwa mbali katika maono, na nilioneshwa makosa ya watu ambao wameiathiri kusudi la kazi ya Mungu. Sithubutu kuzuia ushuhuda kutoka kwa kanisa ili kuepusha hisia za watu binafsi. {1T 210.1}

Nilioneshwa hali ya chini ya watu wa MUNGU; kwamba MUNGU hakuwa amewaacha, bali kwamba wao walikuwa wamemwacha, na walikuwa vuguvugu. Walikuwa na nadharia ya Ukweli, lakini walikosa nguvu yake ya kuokoa. Tunapokaribia mwisho wa wakati, Shetani anashuka kwa nguvu kubwa, akijua kuwa ana wakati mchache. Nguvu yake itatumika hasa juu ya waliosalia. Atapigana nao, na atatafuta kugawanya na kuwatawanya, ili wadhoofike na kupinduliwa. Watu wa MUNGU wanapaswa kusonga kwa uelewa, na wanapaswa kuwa na umoja katika juhudi zao. Wanapaswa kuwa na nia moja, ya maamuzi yanayofanana; kisha juhudi zao hazitakuwa zimetawanyika, lakini zitakuwa na nguvu katika kujenga kazi ya Ukweli wa leo. Utaratibu lazima uzingatiwe, na lazima kuwe na umoja katika kudumisha utulivu, la sivyo Shetani atachukua fursa hiyo. {1T 210.2}

Niliona kwamba adui angekuja kwa kila njia inayowezekana ili kuwavunja moyo watu wa MUNGU, kuwafadhaisha na kutatiza, na kwamba wanapaswa kusonga mbelekwa uelewa, na kujitayarisha kwa mashambulizi ya Shetani. Maswala yanayohusu kanisa hayapaswi kuachwa katika hali ya kutotulia, kutowekwa sawa. Hatua zinapaswa kuchukuliwa ili kujipatia viwanja/mali ya kanisa kwa kazi ya MUNGU, ili kazi hiyo isicheleweshwe katika maendeleo yake, na kwamba mali ambazo watu wanataka kuzitoa kwa kazi ya MUNGU zisiingie katika safu ya adui. Niliona kwamba watu wa MUNGU wanapaswa kutenda kwa busara, na kutoacha chochote kikiwa hakijafanyika kwa upande wao ili kuiweka shughuli ya kanisa katika hali salama. Na halafu yote hayo yakishafanyika, wanapaswa kumwamini Bwana kutawala mambo haya kwa ajili yao, ili Shetani asichukue faida kwa watu wa MUNGU waliosalia. Huu ni wakati wa Shetani kufanya kazi. Wakati ujao wa dhoruba uko mbele yetu; na kanisa linapaswa kuwa macho ili kuchukua hatua ya mapema ili waweze kusimama salama dhidi ya mipango yake adui. Ni wakati ambapo kitu fulani kinapaswa kufanyika. MUNGU hafurahishwi na watu Wake kuacha mambo ya kanisa bila utulivu, kuwekwa sawa na kufanunuliwa ipasavyo, na kumruhusu adui kupata faida yote na kumpa uthibiti wa mambo kama inavyompendeza. {1T 210.3}

Nilioneshwa msimamo mbaya uliochukuliwa na Ndugu B katika taasisi ya uchapaji iitwayo Review kuhusiana na muundo, na ushawishi wa kuvuruga alioufanya. Hakupima jambo hilo vya kutosha. Makala zake zilikorokotolewa kikamilifu kuwa na ushawishi wa kutawanya, kuongoza akili kwa hitimisho lisilo sahihi, na kuwatia moyo wengi katika maoni yao ya kuzorota na kutembea polepole katika kusimamia mambo yanayohusiana na kazi ya MUNGU. Wale ambao hawahisi uzito wa kazi hii juu yao hawahisi umuhimu wa jambo lolote kufanywa ili kuanzisha utaratibu wa kanisa. Wale ambao kwa muda mrefu wamebeba mzigo hutazama siku za usoni na kupima mambo. Wana hakika kwamba hatua lazima zichukuliwe kuweka mambo ya kanisa katika nafasi salama zaidi, ambapo Shetani hawezi kuingia na kufaidika. Makala za Ndugu B zilisababisha wale ambao wanaogopa utaratibu kutazama kwa mashaka maoni ya wale ambao kwa uangalizi na majaliwa maalum ya MUNGU hujongea katika maswala muhimu ya kanisa. Na wakati yeye alipoona kwamba msimamo wake hautaweza kustahimili, alishindwa kukiri makosa yake kwa uaminifu/uwazi, na kufanya kazi ili kuhafifisha/kufuta maoni mabaya aliyoyafanya. {1T 211.1}

Niliona kuwa katika mambo yasiyo ya kudumu, Ndugu B alichukulia kwa urahisi sana na anakuwa mzembe. Amekosa nguvu, akiona kuwa ni fadhila kumwachia Bwana yale ambayo Bwana amemwachia ayafanye. Ni katika hali za dharura kubwa tu ambapo Bwana huingilia kati. Tunayo kazi ya kufanya, mizigo na majukumu ya kubeba, na kwa kufanya hivyo tunapata uzoefu. Ndugu B anaonesha tabia hizo hizo katika mambo ya kiroho kama katika mambo yake ya muda mfupi, ya hapa duniani. Kuna ukosefu wa bidii, unyofu na ari ya kufanya kazi kikamilifu. Wote wanapaswa kutenda kwa busara na hekima zaidi kwa mambo ya MUNGU kuliko vile wanavyodhihirisha katika vitu vya muda vinavyowasaidia kupata mali ya kidunia. {1T 212.1}

Lakini wakati watu wa MUNGU wana haki ya kupata mali ya kiwanja/kanisa kwa njia halali, wanapaswa kuwa waangalifu kudumisha tabia yao ya kipekee na takatifu. Niliona kwamba watu wasiojitoa wakfu wangeweza kutumia fursa ya msimamo ambao kanisa limechukua hivi karibuni, na wangevuka mipaka, wakachukua mambo kwa kupitiliza kiasi, na kuumiza kazi ya MUNGU. Wengine watajongea bila hekima au maamuzi ya busara, watahusika katika kesi ambazo zingeweza kuepukwa, na kujichanganya na ulimwengu, watashiriki roho yake, na kushawishi wengine kufuata mfano wao. Mtu mmoja anayejidai ni Mkristo anayejongea bila kutafakari kwa hekima, anaumiza sana kazi ya Ukweli wa leo. Uovu hushika mizizi kwa urahisi zaidi kuliko wema, na hustawi wakati wema na haki vinapoumia isipokuwa pale tu uangalifu katika matunzo unapofanyika. {1T 212.2}

Nilielekezwa nyuma, na nikaona kwamba katika kila hatua muhimu ya kusonga mbele, kila uamuzi uliofanywa au pointi iliyopatikana na watu wa MUNGU, wengine wameibuka kuchukua mambo kwa kupitiliza kiasi, na kusonga mbele

kwa njia ya kupindukia na kufuja, ambayo imechukiza wasioamini, imesumbua watu wa MUNGU, na kuisababishia kazi ya MUNGU sifa mbaya na kudharauliwa. Watu ambao MUNGU anawaongoza katika siku hizi za mwisho, watasumbuka na mambo yanayofanana na haya. Lakini mabaya mengi yataepukwa ikiwa wahudumu wa Kristo watakuwa na nia moja, walioungana katika mipango yao ya utekelezaji, na walioungana katika juhudi. Ikiwa watasimama pamoja, kutegemezana, na kwa uaminifu kuonya na kukemea makosa, watasababisha mambo hayo kunyauka hivi karibuni. Lakini Shetani amedhibiti mambo haya sana. Baadhi ya waumini binafsi na hata wahubiri wamewahurumia wale ambao hawana furaha na watu walio katika mamlaka na hawataki kuwaunga mkono viongozi kwasababu wamekemewa kwa makosa yao, na matokeo yake yamekuwa ni mgawanyiko wa hisia. Yule aliyejitosa na kutekeleza jukumu lake lisilopendwa kwa kukabiliana kwa uaminifu na makosa na mambo yasiyo sahihi, amehuzunishwa na kujeruhiwa kwa kuwa hakubaliani na huruma zinazooneshwa na wahubiri wenzake [wanaolea maovu]. Yeye huvunjika moyo katika kutekeleza majukumu haya yenye maumivu, hutua chini msalaba, na huzuia ushuhuda ulio wazi. Nafsi yake hufungwa gizani, na kanisa huteseka kwa kukosa ushuhuda ambao MUNGU alikusudia uishi kati ya watu Wake. Lengo la Shetani linapatikana wakati ushuhuda wa uaminifu unapokandamizwa. Wale ambao wanahurumia watu kwa urahisi makosa wanaona ni fadhila; lakini hawatambui kwamba wanashinikiza ushawishi unaotawanya, na kwamba wao wenyewe wanasaidia kutekeleza mipango ya Shetani. {1T 212.3}

Niliona kwamba roho nyingi zimeharibiwa na ndugu zao waliowahurumia bila busara, wakati tumaini lao la pekee lilikuwa kuachwa waone na kutambua kiwango kamili cha makosa yao. Lakini wanapokubali kwa furaha huruma ya ndugu wasio na busara, wanapokea wazo kwamba wananyanyaswa; na ikiwa watajaribu kurekebisha hatua zao, huifanya kazi hiyo kwa mioyo iliyoongoka kuwa nusu-nusu. Wanagawanya jambo ili kukidhi hisia zao za asili, wanamlaumu yule anayekemea, na kwa hivyo kulifunika jambo hilo. Halichunguzwi hadi chini, na haliponywi, na kisha huangukia tena kwenye kosa lile lile, kwa sababu hawakuachwa wahisi ukubwa wa makosa yao, na kujinyenyekeza mbele za MUNGU, na kumruhusu awajenge. Waonyesha huruma wa uongo/feki wamefanya kazi katika kupinga moja kwa moja nia ya Kristo na malaika wanaohudumia. {1T 213.1}

Watumishi wa Kristo wanapaswa kunyanyuka na kushiriki katika kazi ya MUNGU kwa nguvu zao zote. Watumishi wa MUNGU hawana udhuru ikiwa wataepuka kutoa ushuhuda ulio wazi. Wanapaswa kuonya na kukemea mabaya, na wasichukuliane na dhambi juu ya ndugu. Inanipasa hapa nitambulishe sehemu ya barua iliyoandikiwa kwa Ndugu C: {1T 213.2}

“Nilioneshwa mambo kadhaa yanayokuhusu. Niliona kwamba ushuhuda ulio hai, ulio wazi ulikuwa umepondwa-pondwa kanisani. Haukuwa umepatana na

ushuhuda ule ulionyoka. Umejiepusha kuweka mkono wako juu ya mambo mabaya na umeshutumiwa na wale waliosukumwa kufanya hivyo. Wale ambao hawakuwa na na furaha na uongozi wamepata huruma yako. Jambo hili limekuwa na mwelekeo wa kukufanya wewe uwe mtu dhaifu. Haukuwa umeungana na ushuhuda ulio wazi, unaokatakata/mkali uliokuwa umetumwa kwa mtu mmoja mmoja. {1T 214.1}

"Watumishi wa MUNGU hawasamehewi ikiwa wataepuka ushuhuda ulio wazi. Lazima waonye na kukemea makosa, na wala wasiache dhambi za ndugu zao. Mara nyingi umenyoosha mikono yako kuwalinda watu kutokana na lawama au karipio ambalo walistahili, na matengenezo ambayo Bwana alikusudia wawe nayo. Ikiwa watu hawa wanashindwa kujirekebisha/matengenezo, mapungu yao yanawekwa kwenye akaunti yako. Badala ya kuangalia hatari yao, na kuwaonya juu yake, umetupa ushawishi wako dhidi ya wale ambao wamefuata usadikisho wa wajibu, na kukemea na wakawaonya wakosaji. {1T 214.2}

"Hizi ni nyakati za hatari kwa kanisa la MUNGU, na hatari kubwa sasa ni ile ya kujidanganya wenyewe. Watu wanaodai kuamini Ukweli hawaoni hatari na makosa yao. Wanafikia viwango vya uchaji ambavyo wamewekewa na marafiki zao na wao wenyewe, wameshirikiana na ndugu zao, na kuridhika, wakati wameshindwa kabisa kuvifikia viwango vya injili vilivyowekwa na MUNGU Bwana wetu. Wanapotunza maovu mioyoni mwao, Bwana hatawasikia. Hata hivyo, kwa wengi [maovu hayo] hayatunzwi tu moyoni, lakini hufanywa wazi maishani, lakini katika mazingira mengi wakosaji hawa hawapokei karipio. {1T 214.3}

"Nilielekezwa nyuma kwa -----. Hisia zako zilikosea hapo. Ulipaswa kusimama bega kwa bega na Mzee D na kufanya naye kazi iliyonyoka, mkiishikilia kazi ya kukemea makosa ya mtu binafsi. Mzigo uliomtupia Mzee D ulikustahili wewe mwenyewe, kwa ukosefu wako wa ujasiri wa kimaadili wa kuweka mkono wako juu kwa kushugulikia mabaya. Uliwashawishi wengine. Kazi nzuri ambayo MUNGU alipanga ifanywe kwa watu fulani haikutimizwa, na Shetani amewasaidia kufutuka kwa kiburi (pembe zimeota). Kama ungekuwa umesimama katika shauri la MUNGU wakati huo, ungekuwa umetuma ushawishi nao ungezungumza/ungeelezea juu ya kusudi la MUNGU. Roho wa Bwana alihuzunishwa. Na ukosefu huu wa muunganiko huwakatisha tamaa wale ambao MUNGU anaweka mzigo wa kukemea. {1T 214.4}

"Nilioneshwa kuwa ulikuwa unakosea kwa kumhurumia E. Hatua uliyochukua kumhusu imeumiza ushawishi wako, na imeumiza sana kazi ya MUNGU. Haiwezekani E kuwa na ushirika na kanisa la MUNGU. Amejiweka mahali ambapo hawezi kusaidiwa na kanisa, ambapo hawezi kuwa na ushirika na kuwa na sauti katika kanisa. Amejiweka yeye mwenyewe hapo mbele kukabili nuru na Ukweli. Ameamua kwa ukaidi kuchukua njia yake mwenyewe, na akakataa

kusikiliza maonyo. Amefuata mwelekeo wa moyo wake uliopotoka, amevunja sheria takatifu ya MUNGU, na ameaibisha kazi ya Ukweli wa leo. Ikiwa atatubu kwa moyo wote, kanisa lazima liachilie kesi yake (asije kanisani). Kama atakwenda mbinguni, lazima iwe peke yake, bila ushirika wa kanisa. Kemeo lililosimama kutoka kwa MUNGU na kanisa lazima liwe juu yake, kwamba kiwango cha maadili kisishuke hadi mavumbini. Bwana amekasirishwa na mwenendo wako katika mambo haya (*Soma zaidi kuhusu hili kwenye Sura ya 39 ya Shuhuda ya Ngono, Talaka na Uzinzi tuna kopi laini, tuandikie tukutumie- Testimonies to sexual Behavior, Adultery and Divorce). {1T 215.1}

"Umeijeruhi kazi ya MUNGU; hatua yako ya hiari imeumiza mioyo ya watu wa MUNGU. Ushawishi wako unahimiza hali ya kuzorota na uvivu kanisani. Unapaswa kutoa ushuhuda ulio hai, ulio wazi. Jiondoe/toka kwenye njia ya kazi ya MUNGU, usijiweke katikati ya MUNGU na watu Wake. Umeuzinga ushuhuda mkali kwa muda mrefu sana, na umesimama kinyume na karipio kali ambalo MUNGU huweka juu ya makosa ya mtu binafsi. MUNGU anarekebisha, na anathibitisha, na kuwasafisha watu Wake. Hebu toka nje ya njia, na usimame kando ili kazi Yake isizuiliwe. Yeye Hatakubali ushuhuda laini. Wachungaji ni lazima wapaze sauti kwa kulia, na kamwe wasiache. Bwana amekupa ushuhuda wenye nguvu, uliokusudiwa kuliimarisha kanisa na kuwaamsha wasioamini. Lakini vitu hivi unavyopungukiwa ni lazima virekebishwe, vinginevyo ushuhuda wako hautakuwa na nguvu, na ushawishi wako utaumiza kazi ya MUNGU. Watu wanakutazama ili kupata mfano. Usiwapotoshe watu. Acha ushawishi wako uwe wa kurekebisha makosa katika familia yako na kanisani. "{1T 215.2}

Nimeoneshwa kuwa Bwana anafufua ushuhuda ulio hai, ulio wazi, ambao utaendeleza tabia na kulitakasa kanisa. Lakini wakati tunaamriwa kujitenga na ulimwengu, siyo lazima kwamba tuwe wabaya, wajeuri na wakali, na kushuka kwenye viwango vya maneno yetu ya kawaida na yenye kufanana na yale ya mitaani, na matamshi yetu kuwa ya ujeuri, yasiyo ya uungwana na yasiyofaa kadri iwezekanavyo. Ukweli umekusudiwa kumuinua mpokeaji, kuboresha ladha yake na kutakasa maamuzi yake. Kunapaswa kuwepo juhudi endelevu za kuiga jamii tunayotarajia kujiunga nayo hivi karibuni; yaani, malaika ambao hawajaanguka kamwe na dhambi. Tabia inapaswa kuwa takatifu, mwenendo, na adabu ya kupendeza, maneno yasiyo na hila, na kwa hayo tunapaswa kuyafuata hatua kwa hatua hadi tutakapokuwa tayari na kutwaliwa kwenda mbinguni. {1T 216.1}

# SURA YA 40

# WAJIBU KWA WATOTO

Nimeoneshwa kuwa wazazi kwa ujumla hawajachukua hatua/mwenendo inayofaa kwa ajili ya watoto wao. Hawajawazuia kama inavyostahili, lakini wamewaacha wajiingize katika kiburi, na wafuate mwelekeo wao. Zamani, mamlaka ya wazazi ilizingatiwa; watoto wakati huo walikuwa chini ya wazazi wao, na waliwaogopa na kuwaheshimu; lakini katika siku hizi za mwisho agizo hiil la Mungu limegeuzwa. Wazazi wengine wanawatii watoto wao badala ya watoto  kuwatii wazazi. Wanaogopa watakiuka mapenzi ya watoto wao, na kwa hivyo wanatii matakwa yao. Lakini maadamu watoto wako chini ya paa la wazazi, wakiwategemea, wanapaswa kuwa chini ya uthibiti wao. Wazazi wanapaswa kusonga na uamuzi, wakihitaji maoni yao ya kile kilicho sahihi na haki yafuatwe. {1T 216.2}

Huenda Eli angewazuia wanawe waovu wasifanye uovu, lakini aliogopa hasira yao. Aliwaruhusu waendelee katika uasi wao, mpaka wakawa laana kwa Israeli. Wazazi wanahitajika kuwathibiti watoto wao-kuwazuia. Wokovu wa watoto hutegemea sana hatua inayofuatwa na wazazi. Katika upendo wao wa kimakosa na kupenda watoto wao, wazazi wengi huwaingiza kwenye machungu, hunawirisha kiburi chao, na huwawekea juu yao mapambo na madoido ambayo huwafanya kuwa batili, na huwaongoza kudhani kuwa mavazi hayo ndiyo huwafanya wawe wanawake au wanaume (wanadamu waungwana). Lakini kufahamiana kwa muda mfupi huwashawishi wale wanaojumuika nao kwamba mwonekano wa nje hautoshi kuficha ubovu wa moyo uliokosa neema za Kikristo, lakini uliojazwa na kujipenda nafsi, kiburi, majivuno na tamaa zisizodhibitiwa. Wale wanaopenda upole, unyenyekevu, na wema, wanapaswa kukaa mbali na jamii kama hiyo, hata ikiwa ni watoto wa watunza Sabato. Ushirika nao ni sumu; ushawishi wao husababisha kifo. Wazazi hawatambui ushawishi unaoharibu wa mbegu ambayo wanapanda. Hakika mbegu hii itaota na kuzaa matunda ambayo yatawafanya watoto wao wadharau mamlaka ya wazazi. {1T 217.1}

Hata baada ya kuwa na umri wa utu uzima, watoto wanahitajika kuheshimu wazazi wao, na kutunza faraja yao. Wanapaswa kusikiliza ushauri wa wazazi wacha MUNGU, na wasijisikie kwamba kwa sababu miaka michache zaidi imeongezwa juu ya maisha yao, sasa wao wamekua na wapo nje ya jukumu lao kwa [wazazi wao]. Kuna amri iliyo na ahadi kwa wale wanaowaheshimu baba zao na mama zao. Katika siku hizi za mwisho watoto wanajulikana sana kwa kutotii na kutokuheshimu kwao kiasi kwamba MUNGU ameliona hilo, na ni ishara kwamba mwisho umekaribia. Inaonesha kuwa Shetani anakaribia kuwa na

uthibiti kamili wa akili za vijana. Kwa wengi, umri hauheshimiwi tena. Inachukuliwa pia kama ni mtindo wa kizamani kuheshimu wazee; na hali hii imeanza tangu siku za Ibrahimu. MUNGU anasema: “Ninamjua, kwamba atawaamuru watoto wake na nyumba yake baada yake.” {1T 217.2}

Zamani, watoto hawakuruhusiwa kuoa bila idhini ya wazazi wao. Wazazi walichagua watoto wao. Ilizingatiwa kuwa ni kosa kwa watoto kupanga ndoa kwa uwajibikaji wao wenyewe. Jambo hilo liliwekwa kwanza mbele ya wazazi, na walipaswa kuzingatia ikiwa mtu atakayeletwa katika uhusiano wa karibu alikuwa anastahili, na ikiwa wahusika wanaweza kujikimu kwa mahitaji ya maisha ya familia. Ilizingatiwa na wao juu ya umuhimu mkubwa kwamba wao, waabudu wa MUNGU wa Kweli, hawapaswi kuoana na watu wanaoabudu sanamu, isije familia zao zikaongozwa mbali na MUNGU. Hata baada ya watoto kuolewa, walikuwa chini ya jukumu kubwa kwa wazazi wao. Hukumu yao haikuhesabiwa kuwa ya kutosha bila ushauri wa wazazi, na walihitajika kuheshimu na kutii matakwa yao isipokuwa haya yanapingana na mahitaji/matakwa ya MUNGU. {1T 218.1}

Tena nilielekezwa kwa hali ya vijana katika siku hizi za mwisho. Watoto hawatawaliki. Wazazi, mnapaswa kuanza masomo yenu ya kwanza ya nidhamu wakati watoto wenu wakiwa bado wachanga wa kubebwa mikononi mwenu. Wafundisheni kutoa mapenzi yao kwenu. Hii yaweza kufanywa kwa kushikilia mkono mtupu, na kudhihirisha uthabiti. Wazazi wanapaswa kuwa na uthibati kamili juu ya roho zao wenyewe, na kwa upole na uthabiti kuyageuza mapenzi ya mtoto mpaka yasitarajie kitu kingine isipokuwa kukubali matakwa yao. {1T 218.2}

Wazazi hawaanzi kwa wakati kutiisha watoto. Udhihirisho wa kwanza wa hasira au zoea hasi hautiishwi, na watoto wanakua wakaidi, ambayo huongezeka kwa kadri wanavyokua na huimarika kuendana na nguvu zao. Watoto wengine, wanapokuwa watu wazima vya kutosha, wanafikiri ni jambo la kawaida kuwa na mapenzi yao wenyewe, na wazazi wayakubali hayo matakwa yao, hawabebi mzigo vile ilivyopaswa. Wanategemea wazazi wao wawatumikie. Hawana uvumilivu na kizuizi chochote; na wakiwa na umri wa kutosha kuwasaidia wazazi wao, hawabebi mizigo, wanavyopaswa. Wamewekwa huru kutoka kwenye majukumu, na kukua kama watu wasio na faida majumbani na nje ya nyumba zao. Hawana nguvu au uvumilivu. Wazazi wamebeba mzigo, na wamewaruhusu kukua katika kukaa bila kazi, uvivu, bila tabia zenye utaratibu, ujasiriamali, tasnia au uchumi. Hawajafundishwa tabia za kujinyima, kujikana nafsi, bali wamedekeshwa (pets), wameendekezwa na kufurahishwa, hamu zao zimeridhishwa, na hii inawapatia afya dhaifu. Wenyewe hawana furaha ndani yao wenyewe, na huwafanya wale walio karibu nao wasiwe na furaha. Na wakati watoto wakiwa bado ni watoto, wakati wakihitaji kuadabishwa,

wanaruhusiwa kwenda nje na kushirikiana na jamii ya vijana, na mmoja ana ushawishi mbaya juu ya mwingine. {1T 218.3}

Laana ya MUNGU hakika iko juu ya wazazi wasio waaminifu. Siyo tu kwamba wanapanda miiba itakayowajeruhi hapa, bali pia lazima wakutane na kutokuwa waaminifu kwao wakati hukumu itakapowekwa. Watoto wengi watainuka hukumuni na kuwalaani wazazi wao kwa kutowazuia, na kuwatupia lawama ya uharibifu wao. Huruma ya uongo na upendo mpofu wa wazazi huwafanya watoe udhuru kwa makosa ya watoto wao na kuyapita bila kuyasahihisha, na watoto wao hupotea kama matokeo ya hali hiyo, na damu za nafsi zao zitakaa juu ya wazazi wasio waaminifu. {1T 219.1}

Watoto ambao wamelelewa bila nidhamu, wana kila kitu cha kujifunza wanapodai kuwa wafuasi wa Kristo. Uzoefu wao wote wa kidini unaathiriwa na namna walivyolelewa katika kipindi cha utoto wao. Kukazania kwa ukaidi na mapenzi binafsi hujitokeza mara nyingi; kunakuwa na upungufu ule ule wa kujikana nafsi, hali ile ile ya kukosa uvumilivu wakati wa kukaripiwa/kukemewa, hali ile ile ya kujipenda nafsi, na kutokuwa tayari kutafuta ushauri wa wengine, au kushawishiwa na maamuzi wa wengine, uvivu ule ule, kukwepa kubeba mizigo, na kupungukiwa na uwezo wa kubeba majukumu. Yote haya yanaonekana katika uhusiano wao na kanisa. Inawezekana kwa watu kama hao kushinda; lakini hiyo ni vita iliyo ngumu kiasi gani! Hilo ni pambano kali kiasi gani! Ni vigumu kama nini kuvuka kupita hatua hii ya nidhamu kamili ambayo ni ya lazima kwao, na hata kuifikia hatua ya kuchukuliwa mbinguni ambayo ni lazima ili kufikia mwinuko wa tabia ya Kikristo! Hata hivyo ikiwa watashinda hatimaye, wataruhusiwa kuona, kabla hawajatwaliwa kwenda mbinguni, jinsi walivyokuwa wamekaribia ukingoni mwa korongo la uharibifu wa milele walioujia, kwa sababu ya kupungukiwa na mafunzo sahihi wakati wa ujana, kushindwa kujifunza kujitiisha/kujisalimisha/kujinyenyekesha wakati wa utoto. {1T 219.2}

# SURA YA 41

# UTOAJI WA MPANGO KWA UKARIMU

Nilielekezwa nyuma kwa wana wa Israeli zamani. MUNGU aliwataka wote, maskini na matajiri, watoe dhabihu kadri Yeye alivyowafanikisha. Masikini hawakupewa udhuru kwa kuwa hawakuwa na utajiri walionao ndugu zao matajiri. Walihitajika kufanyia mazoezi kujinyima na kujikana nafsi. Na kama ye yote alikuwa maskini kiasi cha kutoweza kuleta sadaka kwa Bwana, ikiwa ugonjwa au maafa yamewanyima uwezo wa kutoa, wale waliokuwa matajiri walitakiwa kuwasaidia/msaada wao mnyenyekevu wa safari, ili wasije mbele za Bwana mikono mitupu. Mpangilio huu ulihifadhi masilahi ya pande zote. {1T 220.1}

Wengine hawajaja na kuungana na utoaji wa mpango kwa ukarimu, wakitoa udhuru kwamba walikuwa na madeni. Wanasihi lazima kwanza watimize agizo linalosema "Usidaiwe na mtu chochote. -Rumi 13:8" Lakini ukweli kuwa wanadaiwa hakuwafanyi wasiwe kwenye utoaji wa ukarimu kwa mpango. Niliona kuwa iliwapasa kumpa Kaisari yaliyo ya Kaisari, na MUNGU yaliyo ya MUNGU. Wengine walihisi kuwa imewapasa kuwa waangalifu "kutodaiwa na mtu chochote," na kufikiri ya kwamba MUNGU hatahitaji chochote kutoka kwao hadi kwanza walipe madeni yao yote. Hapa wanajidanganya. Wanashindwa kumpa MUNGU vitu ambavyo ni vyake. Kila mtu lazima alete kwa Bwana sadaka inayofaa. Wale ambao wana madeni wanapaswa kuchukua kiasi kile wanachodaiwa kutoka kwa mali wanayoimiliki, na kutoa sadaka kutoka kwa kiasi kilichobaki. {1T 220.2}

Baadhi wamefikiria kuwa wako chini ya majukumu matakatifu kwa watoto wao. Ni lazima wawapatie kila mmoja sehemu yake, lakini wanajisikia kuwa hawawezi kutafutamali za kusaidia kazi ya MUNGU. Wanatoa kisingizio kwamba wana jukumu kwa watoto wao. Hii inaweza kuwa sawa, lakini jukumu lao la kwanza ni kwa MUNGU. Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na MUNGU yaliyo ya MUNGU. Usimnyang'anye MUNGU kwa kumnyima zaka na matoleo yako. Ni jukumu la kwanza takatifu kumpa MUNGU sehemu inayomstahili. Hebu mtu yeyote asikupe madai yake na kukuongoza kumuibia MUNGU. Usiruhusu watoto wako waibe matoleo yako kutoka kwa madhabahu ya MUNGU kwa faida yao. {1T 220.3}

Niliona kwamba hapo zamani tamaa ya wengine iliwaongoza kuzuia sehemu inayomstahili MUNGU; walifanya dhabihu yao iwe kilema. Hii ilirekodiwa

mbinguni, na walilaaniwa katika mavuno yao na mifugo yao sawasawa na walivyozuia. Wengine walitembelewa na shida katika familia zao. MUNGU asingekubali sadaka kilema. Lazima iwe haina lawama, iliyo bora kati ya mifugo yao, na matunda yaliyo bora ya shamba lao. Na lazima iwe sadaka ya hiari, kama wangetaka baraka ya Bwana ituame juu ya familia zao na mali zao. {1T 221.1}

Kesi ya Anania na Safira iliwasilishwa mbele yangu ikionesha hatua ya wale wanaoweka kiwango cha mali zao chini ya thamani yake. Walijifanya kutoa sadaka ya hiari ya mali zao kwa Bwana. Petro akasema: “Niambie, Mlikiuza kiwanja kwa thamani hiyo?” Jibu lilikuwa: “Ndiyo, kwa thamani hiyo.” Wengine katika zama hii mbaya hawatafikiria kuwa huo ni uongo. Lakini Bwana aliuona hivyo. Walikuwa wamekiuza kwa thamani hiyo na thamani kubwa zaidi. Walikuwa wamekubali kutoa wakfu vyote kwa MUNGU. Walikuwa wamemdanganya MUNGU, na malipo yake hayakukawia. {1T 221.2}

Niliona kuwa katika mpangilio wa utoaji wa mpango kwa ukarimu, mioyo itapimwa na kuthibitishwa. Ni mtihani wa kudumu, ulio hai. Humfanya mtu auelewe moyo wake mwenyewe, ili kubaini kama Ukweli au upendo kwa ulimwengu ndivyo vinavyotawala. Hapa kuna kipimo cha ubinafsi na uchoyo wa asili. Wanaziweka mali zao kwa viwango vya chini sana (katika kuzitathmini-valuation). Hapa wanaficha Ukweli. Malaika akasema: “Na alaaniwe afanyaye kazi ya Bwana kwa hila.” Malaika wanaangalia ukuaji na maendeleo ya tabia, na matendo kama hayo yanachukuliwa kwenda mbinguni na wajumbe wa mbinguni. Wengine watatembelewa na MUNGU kuhusiana na mambo haya, na ongezeko lao litashushwa na kuwa ile namba waliyojitajia wenyewe ya uongo. “Kuna atawanyaye, lakini huongezewa zaidi; Kuna azuiaye isivyo haki, lakini huelekea uhitaji. Nafsi ya mtu mkarimu itawandishwa; Anyweshaye atanyweshwa mwenyewe.” Mithali 11:24, 25. {1T 221.3}

Wote wanahitajika kuipenda kazi hii. Wale wanaotumia tumbaku, chai, na kahawa wanapaswa kuweka kando sanamu hizo (miungu), na kuweka thamani ya vitu hivyo kwenye hazina ya Bwana. Wengine hawajawahi kamwe kutoa dhabihu kwa kazi ya MUNGU, na wapo usingizini na wasitambue kile MUNGU anachotaka kutoka kwao. Baadhi ya wale walio maskini sana watakuwa na shida kubwa ya kujikana nafsi zao wenyewe dhidi ya vichocheo hivi (vileo/uraibu). Sadaka hii ya mtu binafsi haihitajiki kwa sababu kazi ya MUNGU inateseka kwa kukosa mali. Lakini kila moyo utapimwa, na kila tabia itaendelezwa. Ni kanuni ambayo watu wa MUNGU wanapaswa kuchukua hatua. Kanuni hai lazima iendelezwe maishani. {1T 222.1}

“Je! Mwanadamu atamwibia MUNGU? Lakini ninyi mnaniibia Mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia Mimi, naam, taifa hili lote. Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa

njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi." Niliona kwamba Andiko hili limetumika vibaya katika kuzungumza na katika kuomba katika mkutano. Unabii huu unatumika kwa siku za mwisho, na unawafundisha watu wa MUNGU wajibu wao wa kuleta sehemu ya mali zao kama sadaka ya hiari kwa Bwana. {1T 222.2}

## SURA YA 42

## JINA LA DHEHEBU LETU

Nilioneshwa kuhusu watu wa MUNGU waliosalia wakichukua jina. Makundi mawili yaliwasilishwa mbele yangu. Kundi moja lilikumbatia makanisa makubwa ya wale wanaojiita Wakristo. Walikuwa wakikanyaga sheria ya MUNGU na kusujudia taasisi ya kipapa. Walikuwa wakitunza siku ya kwanza ya juma kama Sabato ya Bwana. Kundi lingine, ambalo walikuwa wachache tu kwa idadi, walikuwa wakimsujudia Mpaji-sheria mkuu. Walikuwa wakishika amri ya nne. Sifa za kipekee na maarufu za imani yao ilikuwa utunzaji wa siku ya saba, na kungojea kuonekana kwa Bwana wetu kutoka mbinguni. {1T 223.1}

Mgongano ni kati ya mahitaji ya MUNGU na mahitaji ya mnyama. Siku ya kwanza, taasisi ya kipapa ambayo inapingana moja kwa moja na amri ya nne, bado haijafanywa kuwa mtihani na mnyama huyo mwenye pembe mbili. Na kisha onyo la kutisha kutoka kwa MUNGU linatangaza adhabu ya kumwinamia mnyama na sanamu yake. Watakunywa divai ya ghadhabu ya MUNGU, inayomwagika bila kuchanganywa katika kikombe cha ghadhabu yake (Ufunuo 13 na 14). {1T 223.2}

Hakuna jina ambalo tunaloweza kuchukua litakalokuwa sahihi isipokuwa lile linalokubaliana na ujuzi wetu na linaloelezea imani yetu na kutuonesha kama watu wa kipekee. Jina la Waadventista wa Sabato husimama kama kemeo kwa ulimwengu wa Waprotestanti. Hapa kuna mstari kati ya waabuduo MUNGU na wale wanaomwabudu mnyama na kupokea alama yake. Mgogoro mkubwa ni kati ya amri za MUNGU na mahitaji ya mnyama. Joka hufanya vita na watakatifu kwa kuwa wao wanashika amri zote kumi. Ikiwa watashusha kiwango na kuondoa ule upekee wa imani yao, joka atakuwa na amani; lakini wanachochea hasira yake kwa sababu wamethubutu kupandisha viwango na kukunjua bendera yao kinyume na ulimwengu wa Waprotestanti, ambao wanaabudu taasisi ya upapa. {1T 223.3}

Jina Waadventista wa Sabato limeweka mbele sifa za kweli za imani yetu, na itaishawishi akili yenye kuhoji. Kama mshale kutoka kwa podo la Bwana, utawajeruhi wahalifu wa sheria ya MUNGU, na itasababisha toba kwa MUNGU na imani kwa Bwana wetu Yesu Kristo. {1T 224.1} Nilioneshwa kuwa karibu kila mshabiki aliyeibuka, ambaye anataka kuficha maoni yake kwamba anaweza kuwaongoza wengine, anadai kuwa ni wa kanisa la MUNGU. Jina kama hilo mara moja litasisimua tuhuma; kwani limetumika kuficha makosa ya kipuuzi zaidi. Jina hili halina mipaka kwa watu wa MUNGU waliosalia. Ingesababisha dhana kwamba tuna imani ambayo tunataka kuificha. {1T 224.2}

## SURA YA 43

## MASIKINI

Wale ambao ni maskini katika vitu vya ulimwengu huu wanaweza kuona yafaa kuwatwika mabegani maonyo wale wenye mali. Lakini hawatambui kuwa wao pia wana kazi ya kufanya. MUNGU anataka wajitoe dhabihu. Anawataka watoe kafara sanamu zao (miungu). Wanapaswa kuviacha vichocheo vikali kama tumbaku, chai, na kahawa. Endapo watakutana na mazingira magumu wakati wanajitahidi kufanya vyema kwa kadri ya uwezo wao, itakuwa furaha kwa ndugu zao wenye uwezo wa mali kuwasaidia kutoka katika shida. {1T 224.3}

Wengi hawana hekima ya kumudu mambo sawa na kufanya maamuzi mazuri kiuchumi. Hawapimi uzito wa mambo vizuri, na kufanya mambo kwa uangalifu. Hao hawapaswi kutegemea maamuzi yao duni, bali wanapaswa kushauriana na ndugu zao ambao wana uzoefu wenye mafanikio. Lakini wale ambao wanakosa kufanya maamuzi mazuri kiuchumi na katika nyanja zingine mara nyingi hawataki kutafuta au kupokea ushauri. Kwa kawaida hufikiri kwamba wanaelewa vyema wanachopaswa kufanya kuhusu shughuli zao za hapa duniani na hawataki kufuata ushauri. Wanachukua hatua mbovu, na wanateseka na matokeo ya kile wanachokifanya. Ndugu zao wanahuzunika kuwaona wakiteseka, na wanawasaidia kutoka katika shida. Usimamizi wao usio na hekima unaliathiri kanisa. Kwani wanachukua kutoka katika hazina ya MUNGU kile ambacho kingepaswa kutumiwa kwa kazi ya MUNGU kuendeleza ‘Ukweli wa leo’. Endapo hawa ndugu walio masikini watachukua njia ya unyenyekevu na kuwa tayari kushauriwa na kupewa maoni na ndugu zao, na kisha ikatokea wakapitia katika shida, ndugu watahisi kwamba hili ni jukumu lao kuwasaidia kwa furaha ili watoke shidani. Lakini ikiwa wanachagua njia zao wenyewe, na

kutegemea busara au maamuzi yao wenyewe, basi ingekuwa bora waachwe ili waone matokeo halisi ya njia ambazo siyo za busara, na kujifunza kwa uzoefu huo mzuri kwamba "penye wingi wa washauri pana usalama." Watu wa MUNGU wanapaswa kuhusiana kwa kuwajibikiana wao kwa wao, kusikilizana na kunyenyekeana. Wanapaswa kushauriana wao kwa wao, pale mmoja anapopungukiwa mwenzake ajaze kwa utoshelevu alio nao. Niliona kwamba mawakili wa Bwana hawana jukumu la kuwasaidia wale ambao wanaendelea kutumia tumbaku, chai, na kahawa.{1T 224.4}

## SURA YA 44

## DHANA ISIYO NA UKWELI

Niliona kwamba wengine wanatoa udhuru kuisaidia kazi ya MUNGU kwa sababu walikuwa na madeni. Kama wangechunguza mioyo yao kwa karibu, wangegundua kuwa ubinafsi ndiyo ilikuwa sababu ya kweli ya kutoleta sadaka ya hiari kwa MUNGU. Wengine watabaki na madeni daima. Kwa sababu ya tamaa zao, mkono wa MUNGU unaofanikisha hautakuwa pamoja nao kubariki shughuli zao. Wanaupenda ulimwengu huu kuliko kupenda Kweli. Hawajafaa bado na kufanywa tayari kwa ajili ya ufalme wa MUNGU. {1T 225.1}

Endapo uwekezaji wa amana ukitokea, watu wanaodai kuamini Ukweli wanatafuta njia ya kupata pesa ili wawekeze katika biashara hiyo. MUNGU anaujua kila moyo. Kila nia ya ubinafsi hujulikana na anasikitika kuhusu mazingira yatakayojitokeza ili kujaribu mioyo ya watu wanaokiri kwamba wapo upande Wake ili athibitishe tabia zao na kuzifanya zikue. Wakati mwingine Bwana ataruhusu watu kuendelea tu na hatimaye kushindwa kabisa. Mkono wake uko dhidi yao ili kukatisha matumaini yao na kutawanya walicho nacho. Wale ambao wanapenda kazi ya MUNGU kwa hakika, na wako tayari kufanya jambo ili kuona maendeleo yake, watapata uwekezaji wa uhakika na wenye usalama. Wengine watapata faida mara mia moja katika maisha haya, na katika ulimwengu ujao uzima wa milele. Lakini si wote watakaopokea mara mia moja katika maisha haya, kwa sababu hawawezi kuchukuliana nayo. Wakikabidhiwa vingi, watakuwa mawakili wasio na hekima. Bwana anazuia haya kwa faida yao; lakini hazina zao mbinguni zitakuwa salama. Uwekezaji kama huu ni bora kama nini! {1T 225.2}

Shauku ambayo baadhi ya ndugu zetu wanayo ya kuchuma mali kwa haraka, inawaongoza katika kuanzisha biashara mpya na kuwekeza mali, lakini mara

nyingi matarajio yao ya kupata pesa hayatimizwi. Wanazamisha kile ambacho kingeweza kutumika kwa kazi ya MUNGU. Kuna kupenda kusiko na uhilisia kwa hizi biashara mpya-dhana ya kufikirika watapata pesa. Pamoja na hayo, mambo haya yametekelezwa mara nyingi, mbele yao kuna mifano ya wale ambao walifanya biashara na wakakutana na hasara tupu, na wengi wana ugumu wa kujifunza haya kwa upesi. Shetani huwashawishi/huwavutia, na kuwafanya walewe na faida inayotarajiwa. Ila matumaini yao yanapolipuliwa, hukatishwa tamaa sana na matokeo hayo ya kutotumia busara. Hasara inapotokea, mtu huyo huona kama ni hasara yake binafsi. Lakini lazima akumbuke kuwa yeye ni wakili tu anayesimamia vitu vya mwingine, na MUNGU hafurahishwi na usimamizi usiokuwa wa busara wa mali hizo ambazo zingeweza kutumiwa kueneza Ukweli wa leo. Katika siku ya hukumu wakili asiye mwaminifu, lazima atoe hesabu ya uwakili wake. {1T 226.1}

## SURA YA 45

## WAKILI ASIYE MWAMINIFU.

Nilioneshwa kuwa ROHO WA MUNGU anaendelea kuwa na ushawishi mdogo juu ya F, kiasi kwamba hatakuwa na nguvu kutoka kwa MUNGU za kushinda. Ubinafsi na maslahi binafsi vimemtawala kwa muda mrefu. Kiburi cha moyo, nia, dhamira isiyokubali kutiishwa, na kutotaka kukiri na kuacha makosa yake, vimemfikisha katika nafasi ya kutisha aliyomo sasa. Kwa muda mrefu kazi ya MUNGU imejeruhiwa na mwenendo wake usio na hekima. {1T 227.1}

Amekuwa akilazimisha mambo, jambo ambalo limehimiza roho ya kutafuta makosa kanisani. Amekuwa mkali pale ambapo hakuwa na sababu kufanya hivyo, na amewakandamiza wale aliopata nafasi ya kuwafanyia hivyo. Maombi na mawaidha yamewafanya ndugu kufikiria kwamba alikuwa Mkristo mwema mwenye kujitolea, jambo ambalo limewafanya waathiriwe zaidi na mwenendo wake mbaya. Anajulikana sana, na tabia zake mbovu zimekuwa na ushawishi mbaya kwenye akili za wengi. Wengine wamekuwa dhaifu sana na hata kuiga mifano yake. Niliona kwamba alikuwa ameleta maumivu katika kusudi la kazi ya MUNGU zaidi kuliko faida. {1T 227.2}

Kama angepokea mafundisho aliyopewa na MUNGU, na kurekebishwa, angepata ushindi juu ya tabia hizi kali na mbovu. Lakini niliona kuwa alikuwa ameziruhusu tabia hizi zimdhibiti kwa muda mrefu kiasi kwamba adui mwenye nguvu alikuwa amemfunga nazo. Mpango (dili) wake haukuwa sahihi. Udanganyifu umekuwa ukiongeza nguvu kwake, na amechukua kutoka kwenye hazina kile ambacho hakuwa na haki kukitumia, na ametumia kwa faida yake mwenyewe. Amejiona kuwa yeye ndiye ana busara zaidi katika matumizi ya mali hizo kuliko ndugu zake. Wakati mali zilipowekwa mikononi mwake ili

zitumike katika kazi ya MUNGU, na mtoaji akaorodhesha majina ya watu ambao wangepaswa kuzipata, alifanya kwa msukumo wa matakwa yake, akichukua uhuru wa kutumia mali hiyo kujifanikisha yeye mwenyewe, badala ya kutekeleza matakwa ya mtoaji, na anatumia sehemu ambayo anaona kwenye mawazo yake inafaa kwa faida yake mwenyewe. Mwenyezi MUNGU hajafurahishwa na mambo haya. Amekuwa akiendeleza njia hiyo isiyo ya uaminifu. Hufikiria kwamba yeye ni wakili wa mali ya Bwana, na angeweza kutumia mali, hata za mwingine, kama yeye aonavyo inafaa. Kila mtu alipaswa kuwa wakili wa mambo yake mwenyewe. {1T 227.3}

Amekataa ushauri na maoni ya ndugu zake, akiendelea kwa nguvu zake mwenyewe, akifuata mapenzi yake mwenyewe, na amekataa njia zote ambazo angeweza kusaidiwa kuwekwa sawa-kusaidiwa au kusahihisha. Wakati anapokemewa, njia iliyotumiwa au mtu anayetumika kumsaidia hupingwa, na hivyo njia za matengenezo kutoka kwa tabia hii zimefungwa. Kwa muda mrefu Bwana hajazikubali kazi zake. Amefanya kazi zaidi kwa ajili ya manufaa yake mwenyewe kuliko maslahi ya kazi ya MUNGU. {1T 228.1}

Anapokwenda mahali, maombi na mawaidha yake yana mashiko/ufanisi kwa watu wanaomsikia, na ndugu hupokea mawazo yake wakimfikiria kuwa ni Mkristo mkamilifu. Anapata upendeleo kwa sababu wanamchukulia kama mchungaji. Lakini anapozoeana na watu hawa ndipo wanapojua ubinafsi wake, ukorofi, ukali, ujeuri na tabia zake mbaya. Karibu kila siku tabia yake fulani mbovu huonekana. Daima akili yake inashughulikia kutatua jambo fulani kwa ajili tu ya faida yake mwenyewe. Kisha atamtupia mtu jambo hilo kwa faida yake mwenyewe, na kujaribu kurekebisha tena. Kurekebisha na kupanga kwake kumekuwa na athari ya kutisha na kuidhuru kazi ya MUNGU. Utendaji wake umepelekea kurarua vipande vipande kazi na kujeruhi karibu kila mahali. Je! Huu ni mfano mbaya kiasi gani! Amekuwa mbinafsi katika biashara au mipango yake na wengine, na amejitwalia faida kwa wale wanaoshughulika naye. Hasira ya Mungu ipo juu yake. Mti mzuri hujulikana kwa matunda yake.{1T 228.2}

## SURA YA 46

## USHUPAVU HUKO WISCONSIN

Niliona kwamba Bwana alimwongoza mume wangu kwenda magharibi mwishoni mwa majira ya vuli badala ya kwenda mashariki kama yeye alivyoamua hapo awali. Huko Wisconsin kulikuwa na makosa yaliyopaswa kusahihishwa. Kazi ya Shetani ilikuwa imeanza, na ingeharibu roho kama isingekemewa. Bwana aliona ni vema kuchagua mmoja ambaye alikuwa amepata uzoefu juu ya ushabiki katika siku za nyuma, na aliyekuwa ameshuhudia utendaji wa nguvu za Shetani. Wale ambao walikipokea chombo hiki kilichochaguliwa na MUNGU walisahihishwa makosa yao, na roho ziliokolewa kutoka kwenye mtego uliojificha ambao Shetani alikuwa amewaandalia (ushabiki haujabainishwa). {1T 228.3}

Nilioneshwa kuwa mtego huu wa Shetani usingekubaliwa kirahisi huko Wisconsin endapo akili na mioyo ya watu wa MUNGU ingelikuwa imeungana kwa umoja katika kufanya kazi. Roho ya wivu na tuhuma bado ilikuwepo katika akili za wengine. Mbegu iliyopandwa na chama cha mjumbe (*Messenger Party*) haikuwa imeng'olewa mizizi yake kikamilifu. Na japo walikiri kupokea ujumbe wa malaika wa tatu, hisia zao za zamani, ubaguzi na chuki zilikuwa hazijaachwa. Imani yao ilikuwa imechafuliwa, na walikuwa tayari kupokea udanganyifu wa Shetani. Wale waliokunywa katika roho ya chama cha Mjumbe lazima wafanye kazi ya kusafisha uovu huu, na wang'oe kila chembe, na kupokea roho ya ujumbe wa malaika wa tatu, la sivyo itawaganda kama ukoma na kufanya wajitenge na ndugu zao katika Ukweli wa leo. Itakuwa rahisi kwao kufikiria kwamba wangaliweza kwenda mbinguni peke yao kama kundi huru, lakini ni rahisi kwao kuangukia katika mitego ya Shetani. Yeye hayuko tayari kuiachia Wisconsin. Ana udanganyifu mwingine ulioandaliwa kwa wale ambao hawana umoja na mwili wa Kristo. {1T 229.1}

Niliwaona wale watu ambao walikuwa wamegubikwa na giza na ulaghai ambao Shetani alikuwa amewadhibiti siyo kwenye akili tu bali mwili pia hawa itawalazimu kuchukua nafasi ya unyenyekevu katika kanisa la MUNGU. Bwana hatakabidhi uangalizi wa kundi Lake kwa wachungaji wasio na hekima, ambao wangekosea kwa kuwalisha kondoo wake sumu badala ya chakula bora. MUNGU

atakuwa na watu ambao watalichunga kundi kwa kulilisha chakula safi, kisicho na makapi. Ah, ni doa la namna gani ambalo limeletwa na hizi harakati za ushabiki kwenye kazi ya MUNGU! Na wale walioishikilia sana roho hii ya ushabiki wa giza, japo walikuwa na uthibitisho kwamba njama hii ilitoka kwa Shetani, hawapaswi kutegemewa; maamuzi yao hayapasi kupewa uzito wowote. MUNGU aliwatuma watumishi Wake kwa ndugu na dada G. Nao waliyadharau matengenezo, wakachagua njia yao wenyewe. Kaka G alikuwa na wivu na ukaidi, na mwenendo wake wa baadaye lazima uwe na unyenyekevu mkubwa; kwani amethibitisha kuwa hastaili kuaminiwa na watu wa MUNGU. Moyo wake hauko sawa na MUNGU, na wala haujakuwa sawa kwa muda mrefu. {1T 229.2}

Niliona kwamba lengo la Shetani lilikuwa kuwaongoza watu huko Wisconsin katika ushabiki mkubwa-kupitiliza. Alikuwa ametawala akili zao, na kuwaongoza kutenda kulingana na udanganyifu waliokuwa nao. Wakati madhumuni yake yalipokuwa yametimia, na wao wakiwa wamekimbia umbali ambao alikuwa ameweka alama zake kuwazunguka wote aliotaka wafikiwe, hapo ndipo alikuwa tayari kuwafanya wakiri makosa yao, na kisha ajaribu kuwasukuma kwenda upande mwingine wa kupitiliza kabisa, kukataa karama na utendaji wa ROHO WA MUNGU. Shetani aliutumia ukosefu wa umoja na kanisa wa ndugu na dada G kwa faida yake. Walitamani kuchukua njia ya kuwa peke yao na kuongoza badala ya kukubali kuongozwa. Ndugu G ana tabia ya wivu, ambayo, ikichangiwa na kutaka kuwa huru, anakuwa upande mmoja; kwa roho hii hawezi kufungiwa nira na ndugu zake wanaohudumu. Dada G ana tabia ya wivu, na ana ukaidi mwingi. Hana uzoefu wa imani thabiti au umoja na mwili wa Kristo. Moyo wake unapinga karama za kanisa. Kulikosekana upole na unyenyekevu katika machapisho yake aliyotuma huko kwenye kiwanda cha *Review* cha uchapishaji. {1T 230.1}

Kila kitu kilionekana kuwa kipo tayari kwa kazi ya Shetani. Aliwaongoza wengi kukosa hekima na maamuzi mazuri kwa kuwafanya watawaliwe na hisia. Bwana anataka watu Wake watumie hekima yao na wasiiweke kando kwa ajili ya hisia. Kazi yake itafahamika kwa watoto Wake wote. Mafundisho Yake yatajiuza yenyewe na kueleweka kwa wenye ufahamu. Yamewekwa ili kuiinua akili. Nguvu za MUNGU hazidhihirishwi katika kila tukio. Uhitaji wa mwanadamu ni fursa ya MUNGU kutoa msaada (Man’s necessity is God’s opportunity). {1T 230.2}

Nilioneshwa vikundi vikichanganyikiwa, na vikishughulishwa na roho isiyo sawa/sahihi, wote wakisali kwa sauti ya juu kwa pamoja, wengine wakililia kitu hiki na wengine kitu kile; na haikujulikana kama kilikuwa ni chombo cha mziki cha aina hii au aina ile. "MUNGU si mwanzilishi wa machafuko, bali amani." Shetani aliingilia kati mambo hayo na kudhibiti kwa jinsi alivyopenda. Hekima na afya zilitolewa dhabihu kwa udanganyifu huu. {1T 230.3}

MUNGU hataki watu Wake wawaige manabii wa Baali, kuitesa miili yao na kulia na kupiga kelele, na kujitupa kwenye kila mtazamo, bila kuzingatia utaratibu, mpaka nguvu zao zinanyauka kwa uchovu mwingi kwa kuwa hoi. Kuwa na dini haina maana ya kupiga kelele; lakini wakati nafsi inapojazwa na ROHO WA MUNGU, sifa tamu za moyoni humtukuza MUNGU. Wengine wamesema wana imani kubwa kwa MUNGU, na wana karama maalum na maombi yao hujibiwa kwa njia maalum, japo ushahidi ulikuwa unakosekana. Waliielewa vibaya imani, kwa kuwa na imani bandia, isiyoenda na mapenzi ya Mungu (presumption). Maombi ya imani hayapotei kamwe; lakini kudai kuwa MUNGU atajibu kila wakati kwa njia ile ile na kwa jinsi ambayo tunatarajia, basi hii si Kweli bali ni 'imani bandia tu, ujasiri feki usioendana na mapenzi ya Mungu'. {1T 231.1

Watumishi wa MUNGU walipotembelea huko ----- na -----, udanganyifu huu ulichujwa/ulipimwa. Walipewa ushahidi kwamba kazi hii ni ya uongo/feki. Lakini roho ya ushabiki ilikuwa kubwa, na isingekubali nuru iliyotolewa. Laiti wale ambao walikuwa na makosa wangerekebishwa na watumishi wa MUNGU aliowatuma kwao! Papo hapo MUNGU angetaka watambue kwamba walikuwa wakiongozwa na roho isiyo sahihi-roho ya makosa. Kisha kungekuwa na fadhila katika kukiri makosa yao. Ndipo wangesaidiwa wasiendelee mbele zaidi katika kufuata mipango ya madanganyo ya Shetani. Lakini hawakushawishiwa na njia ya MUNGU. Ndugu G alikuwa na mwangaza wa kutosha kuchukua msimamo wake dhidi ya kazi hiyo ya ushabiki; ila hakutaka kuamua kutokana na uzito wa ushahidi. Roho yake ya ukaidi ilikataa kukubali nuru iliyoletwa kwake na watumishi wa MUNGU; kwani alikuwa amewaangalia kwa kuwashuku, na kuwatazama kwa jicho lenye wivu. {1T 231.2}

Niliona kwamba kadiri nuru kubwa inavyokatiliwa, ndivyo nguvu ya udanganyifu na giza litakalowajia watu hao litakavyokuwa kubwa. Kukataliwa kwa Ukweli kunawaacha watu kuwa mateka, na raia wanaodanganywa na Shetani. Baada ya Mikutano huko ----- na -----, mambo ya udanganyifu huu yaliachwa yatulie kwenye giza kubwa zaidi na yaendelee kwa kina zaidi na kufikia kwenye udanganyifu wenye nguvu, na kuiletea kazi ya MUNGU doa ambalo lisingefutwa kwa haraka. Jukumu la kutisha liko juu ya ndugu G. Wakati akidai kuwa mchungaji, alimruhusu yule adui anayekula kondoo aingie kwenye kundi, naye akawa anatazama tu wakati kondoo wakiraruliwa na kuliwa. Hasira ya MUNGU ipo juu yake. Hajazitazama roho kama mtu yule ambaye atatoa hesabu. {1T 232.1}

Nilielekezwa nyuma, na nikaona kwamba MUNGU hakuwa amebariki kazi zake kwa muda mrefu uliopita. Mkono wa Bwana haukuwa pamoja naye katika kujenga kanisa, na kuongoa roho kwenye ile Kweli. Moyo wake hauko sawa na MUNGU. Hana roho ya ujumbe wa malaika wa tatu. Alijifungia mbali na muungano na hakuwa na huruma na watu wa MUNGU kabla ya udanganyifu huu kutokea, na hii ndiyo sababu moja ya MUNGU kumwacha katika hali kama hiyo ya giza. MUNGU hawaachi watumishi Wake waaminifu, waliojitolea gizani

isipokuwa hao wenye roho ya ushabiki, kutoa kilio ili kuonya watu. Wakati watumishi wa MUNGU walipoleta nuru, na kuinua sauti zao dhidi ya udanganyifu huu, hakuijua sauti ya mchungaji wa Kweli akizungumza kupitia hao watumishi; wivu na ukaidi wake ulimwongoza kuona kwamba hiyo ilikuwa sauti ya mgeni. Wachungaji wa kundi, kati ya watu wote, hawa wanapaswa kuelewa sauti ya Mchungaji Mkuu. MUNGU anataka watu Wake wawe watakatifu na wenye nguvu. Wakati roho ya utakatifu na upendo kamili inapokuwa imejaa moyoni, ikifanya kazi ndani ya wale wanaolitaja Jina la Kristo, itakuwa kama moto unaosafisha, ukiteketeza taka na kutawanya giza. Roho yoyote ya Shetani hupenda kujitetea, na kwa haraka huleta maanguko yake. Lakini Ukweli utashinda. {1T 232.2}

## SURA YA 47

## KUFICHA MAONYO

Nilioneshwa mwenendo wa H na I. Ingawa walikemewa, hawajasahihisha makosa yao. Watu wa MUNGU, hasa katika Jimbo la New York, wameathiriwa na njia yao mbaya. Mvuto wao umekuwa mbaya kwenye kazi ya MUNGU. Kwa miaka kumi iliyopita wamewasilishwa mara nyingi mbele yangu katika maono, makosa yao yameoneshwa kwangu, na nimewaandikia kuhusu haya maono. Lakini walikuwa waangalifu kuwaficha ndugu zao mashauri haya, hawakuambiwa Ukweli kwamba walikemewa. Wakiogopa kwamba ingewaharibia mvuto wao. Wale ambao waliathiriwa na makosa ya watu hawa, bila shaka, walipaswa kufaidika na maonyo ambayo waliyapokea. Nilipaswa kuweka hizi jumbe mikononi mwa ndugu wenye busara kanisani, ili ikiwa ni lazima, wote wapate kuelewa maagizo ambayo Bwana aliona yanafaa kutolewa kwa watu Wake. Lakini wakati nikiwaelezea wengine ujumbe huu niliopewa kwa hawa ndugu, walinilaumu kwa ukali bila kubakiza kitu. Hili kwangu lilileta mateso mengi ya akili ambayo yalinifanya nifiche yale Bwana aliyokuwa ameniambia kuhusu makosa ya watu binafsi. {1T 233.1}

Kilikuwa ni kiburi cha moyo ambacho kilisababisha ndugu hawa kuwapatia wengine hofu nyingi, hawakutaka watu wengine wajue kwamba walikuwa wamerekebishwa. Ikiwa wangekiri kwa unyenyekevu makosa yao kwa kanisa, wangeishi imani waliyodai kuwa nayo katika maono, na kanisa lingeimarishwa kwa kupokea marekebisho na kukiri makosa yao. Walimu hawa walisimama katikati ya njia. Waliweka mfano mbaya kwenye kundi, na kanisa limewatazama, na washiriki wakikemewa wameuliza: "Kwanini hawa wachungaji hawakukemewa, wakati tunafuata mafundisho yao? "Mlango umekuwa umefunguliwa kwa Shetani kuwajaribu kuhusu ukweli wa maono. {1T 233.2}

Ndugu wamedanganywa na kukosewa. Waliamini kwamba tulikuwa na umoja na hawa walimu, na walifuata maagizo yao, wakati wote walikuwa wamekosea. Kwa uchungu wa moyo Nimewaandikia hawa wa kama nilivyoona kwamba kazi ya MUNGU imejeruhiwa kwa njia yao mbaya. Nimekuwa nikiangalia athari ya jumbe hizi kwa fadhaa. Lakini waliziweka kando, na ndugu hawakuruhusiwa kujua chochote juu yao, na hivyo hawakufaidika na maagizo ambayo Bwana aliona yanafaa kutoa. {1T 233.3}

Kazi yangu imekuwa ya kukatisha tamaa sana, kwani nimeona kile ambacho MUNGU alinuia kukifanya hakikamilika Mara nyingi nimeuliza kwa kuugua: Kazi yangu yote inasadia nini? Ndugu hawa walichukua msimamo huu: Tunaamini maono, lakini Dada White, anapoyaandika, anaandika kwa maneno yake mwenyewe, na sisi tutaamini sehemu ambayo tunafikiri ndiyo ya MUNGU, na hatutasikliza ile nyingine. Wamekuwa wakifuata njia hii, na hawajasahihisha maisha yao. Wamekiri kuamini maono, lakini wametenda kinyume na hayo maono. Mifano na ushawishi wao umeleta mashaka katika mawazo ya wengine. Ingekuwa bora kwa kazi ya Ukweli wa leo ikiwa wote wawili wangeipinga karama hiyo. Ingesaidia watu wasidanganywe, na wasingekwazwa na walimu hawa vipofu. Tumekuwa na matumaini kwamba wataelewa na kufanya mambo kwa usahihi, na kuwa na ushawishi mzuri kundini; lakini tumaini letu limekufa, na sisi hatuwezi kuthubutu kukaa kimya zaidi. Tumefanyia makosa kanisa la MUNGU, kwa kuwa hatujawahi kulizungumza hili {1T 234.1}

# SURA YA 48

# KAZI YA MUNGU HUKO OHIO

Tangu ziara yetu huko Ohio katika Msimu wa kuchipua majani wa 1858 H alifanya kila awezalo kuwashawishi watu dhidi yetu; na pale ambapo alidhani angeweza kuathiri watu binafsi, amefanya hivyo kwa kusambaza taarifa ili kuchochea hisia zenye makosa. Tulipotembelea Ohio katika msimu wa Majani kuchipua 1858, nilipewa ujumbe kumhusu yeye na familia yake. Ushuhuda huu alipewa yeye. Lakini ni watu wachache sana walijua kwamba nilikuwa na ujumbe kwake. Aliinuka kwa uasi dhidi ya ujumbe, kama wengine waliokemewa. alichukua msimamo kwamba watu walikuwa wameirubuni akili yangu kuwa dhidi ya familia yake, wakati maono haya yalionesha makosa yale yale yakijirudia kwa miaka kumi. Alisema kwamba aliamini maono hayo, lakini niliathiriwa na wengine wakati nayaandika. {1T 234.2}

Ni hitimisho la namna gani! Bwana ana kazi maalum ya kufanya kupitia moja ya karama zilizotambuliwa, lakini huzuia ujumbe usipotoshwe kabla haujamfikia mlengwa! Je! Maono yana faida gani ikiwa watu wanayachukulia kwa njia hii? Wanajitungia mambo yao, na hujisikia huru kukataa sehemu ambayo haikubaliani na hisia zao. H anajua kwamba kila neno la maono aliyopewa huko Ohio lilikuwa sahihi. Na wakati ambapo hakuweza kulificha kanisa tena huo ujumbe (kwani iliitwa, na ulisomwa kwenye Mkutano wa _____ Majira ya kuangusha majani yeye alikubali yote ni kweli. Lakini ameweka vita isiyotumia busara tena dhidi ya yale ambayo alijua ni sahihi. {1T 235.1}

Hakuitawala vizuri nyumba yake mwenyewe, na kwa miaka kumi iliyopita amekuwa akikemewa kuhusu hili. Hasira ya MUNGU imekuwa juu yake kwa sababu hakuzuia tabia mbovu ya watoto wake. Hawa watoto wamekuwa mafisadi na kitendawili cha aibu (semi ya aibu), na wametoa ushawishi mbaya mahali wanapoishi. Kila wakati walipoletwa mbele yangu, nimerudishwa kwa Eli, na kuoneshwa uovu wa Watoto wake wasiomcha MUNGU na hukumu iliyofuata kutoka kwa MUNGU. Nimeoneshwa kuwa familia ya H ina waumini wanaochukiza, na wanaleta aibu kwa kazi ya Ukweli wa leo. Ujumbe niliopewa katika msimu wa kuchipua majani (spring,1858) Ohio, haswa -----, haukupokelewa na wengi. Ulikata karibu kwa sana, na mioyo ambayo haikujazwa sana na roho ile ya Kweli, waliuasi ujumbe huo. {1T 235.2}

Wachungaji ambao wamefanya kazi katika Jimbo hilo hawajatoa ushawishi mzuri. Vidokezo na dhana zimetupwa dhidi ya ndugu na Dada White, na wasimamizi wa kazi huko Battle Creek, na hili limepokelewa kwenye mioyo ya wengi, haswa wale ambao ni rahisi kuamini wengine na kutafuta makosa. Shetani anajua jinsi ya kufanya mashambulio yake. Yeye hufanya kazi kwenye

akili kuchochea wivu na kutoridhika kwa wale wanaosimamia kazi. Kisha watu wanaleta maswali ya kushuku karama; basi, ni kweli kuna uhakika kuwa zina uzito kidogo tu, na maagizo yanayotolewa kupitia maono yanaacha kuzingatiwa. {1T 236.1}

Wachungaji ambao wamefanya kazi huko Ohio wamefanya sehemu yao katika kufanya watu wasiridhike. H ameshuka chini kwa wengine, nao wakavuta hiyo pumzi yenye roho ya kutoridhika, wakisikiliza kwa bidii taarifa za uongo, zikikusanywa, na kwa karibu wakisema: "Ripoti taarifa…..nasi tutaitolea taarifa." Amefanya kazi kwa njia ya siri, alibeba taarifa za uwongo juu ya mavazi yetu, na ushawishi wetu huko Ohio, na amechochea wazo kwamba ndugu White alikuwa anabuni mambo, dhana tu bila ya kuwa na uhakika. Hajawa na umoja nasi hata kidogo. Ana uchungu sana na sisi. Na ni kwa nini? Kwa sababu tu nimemsimulia kile Bwana alikuwa amenionesha mimi kuhusu familia yake na tabia yake ya ulegevu, ya uvivu katika kuwalea, ambayo imefanya MUNGU akasirike. Amekuwa na wivu, na hisia zisizopatanishwa kuhusiana na sehemu ambayo tumefanya kazi Pamoja katika Ukweli wa leo. {1T 236.2}

Ndugu huko Ohio wamechochewa kutokuwa na imani na kuwashuku wale wanaosimamia kazi huko Battle Creek, na wamekuwa na utayari kuinuka dhidi ya nafasi za kazi walizozichukua. Ndugu J amechukua msimamo wake kwa uthabiti, bila kuzingatia kanisa. Amefikiria kwamba maovu yangetokea makao makuu ambayo angepaswa kushindana nayo. Alijiweka tayari katika mstari wa vita wakati huko hakukuwa na vita vya upiganwa. Alisimama kidete kupinga kitu ambacho hakijawahi kutokea. Ndugu wengi huko Ohio walikuwa na hisia hiyo hiyo, wakijiweka kwenye upinzani kwa kitu ambacho hakijawahi kutokea. Vita yao imekuwa vita isiyokuwa ya busara. Wamekuwa tayari kulia, Babeli, mpaka wamekuwa Babeli kamili wenyewe. {1T 236.3}

Wachungaji wamesimama moja kwa moja katika njia ya kazi ya MUNGU huko Ohio. Wanapaswa kutoka njiani, ili MUNGU awafikie watu Wake. Wanasimama kati ya MUNGU na watu Wake na hivyo kuwazuia, na kugeuza malengo ya MUNGU. Ndugu J ameweka mivuto yake huko Ohio ambayo ni lazima ajitahidi kuiondoa/kuipiku. Niliona kuna wengine hapo Ohio ambao wangechukua msimamo sahihi na maagizo sahihi. Wamekuwa tayari kuunga mkono kazi ya Ukweli wa leo, lakini wameona matokeo madogo ya ufanisi na hivyo wamevunjika moyo. Mikono yao ni dhaifu, na inahitaji itegemezwe ili ikae juu. Niliona kwamba kazi ya MUNGU haifai kuenezwa kwa sadaka zenye ubanifu zinazokuja kwa kulazimisha. MUNGU hapokei matoleo kama hayo. Jambo hili linapaswa kuachwa kabisa kwa mtu binafsi. Hawatakiwi kuleta zawadi ya kila mwaka tu, lakini pia wanapaswa kuwasilisha sadaka kwa hiari kila wiki ya kila mwezi mbele za Bwana. Kazi hii imeachwa kwa watu wenyewe, kwa maana

litakuwa mtihani/jaribu hai kila wiki, na kila mwezi. Mfumo huu wa kutoa zaka, niliona, ungesaidia kukua kwa tabia, na kudhihirisha hali halisi ya moyo. Ikiwa ndugu huko Ohio wamewasilisha jambo hili mbele yao katika ukweli wake, na waachwe wajiamulie, wataona hekima na utaratibu katika mfumo huu wa kutoa zaka. {1T 237.1}

Wachungaji hawapaswi kuwa wakali, na kumchukua mtu moja, na kumlazimisha mtu huyu awape pesa. Kama hatoi kama wengine wanavyofikiria kwamba angetoa, wasimlaumu, na kumtelekeza. Wanapaswa kuwa wavumilivu na wenye kuchukuliana kama malaika. Wanapaswa kufanya kazi kwa umoja na Yesu. Kristo na malaika wanaangalia ukuaji wa tabia, na kupima thamani ya maadili. Bwana huwavumilia kwa muda mrefu watu Wake wanaokosea. Ukweli utaletwa ili uchukuliwa kwa karibu na karibu, na utakatilia mbali sanamu moja baada ya nyingine, mpaka MUNGU atakapotawala kama Kiongozi mkuu katika mioyo ya watu Wake waliojiweka wakfu. Niliona Watu wa MUNGU wanapaswa wamletee sadaka ya hiari; jukumu hilo linapaswa kuachwa kwa mtu mwenyewe, ikiwa atatoa nyingi au kidogo. Sadaka hiyo itanakiliwa kwa uaminifu. Wape watu wa MUNGU muda wa kukuza tabia zao. {1T 237.2}

Watumishi wa MUNGU wanapaswa kubeba ushuhuda ulio wazi. Kweli zilizo hai za Neno Lake zinapaswa kuletwa ili zizungumze kwenye moyo. Na watu wa Ohio wanapokuwa na lengo mahususi machoni pao wale ambao mioyo yao inaunga mkono kazi ya MUNGU watatoa kwa hiari yao mali zao ili kuendeleza kazi ya MUNGU. Bwana anawajaribu watu Wake na kuwathibithisha. Kama kuna mtu ambaye hana moyo katika kazi hiyo, na anashindwa kuleta sadaka Yake kwa MUNGU, Yeye atawazuru; na wakiendelea kuwa na tamaa yao ya mali, Yeye atawatenga kutoka kwa watu Wake. Niliona kwamba lazima kuwe na mfumo ambao utahusisha wote. Vijana wa kike na wa kiume, ambao wana afya na nguvu, bali wana mzigo mdogo sana wa kazi ya Bwana mioyoni mwao Wanawajibika kwa MUNGU kwa nguvu zao, na wanapaswa kuleta matoleo ya hiari kwa Bwana. Na ikiwa hawatafanya hivyo basi mkono Wake unaofanikisha utaondolewa kwao. {1T 238.1}

Niliona kwamba mkono maalum wa MUNGU haukuwa pamoja na kazi huko Ohio kufanikisha kazi huko. Kuna ukosefu; inapaswa kuwa na uchunguzi wa karibu kwa wachungaji na walei, moyo uchunguzwe kwa uaminifu, ili kupata sababu ya ukosefu mkubwa wa ROHO WA MUNGU. Dhabihu na matoleo karibu yakauke. Kwa nini Kweli ya Neno la MUNGU haiamshi moyo na kusababisha kujinyima na kujitolea? Hebu wachungaji wapeleleze na kuona ni aina gani ya mivuto imepelekea jambo hili kutokea. Ndugu J ana roho ya kujitegemea mwenyewe ambayo MUNGU haikubali. Ushawishi wake hauzungumzi kuhusu umoja wa watu wa MUNGU au maendeleo ya kazi ya MUNGU. {1T 238.2}

Nimeona kwamba wale ambao wamekuwa na uzoefu wa miaka michache tu ya Ukweli wa leo, hawapaswi kuongoza kazi. Hao wanapaswa kuwa na uangalifu katika kuchukua nafasi za kazi ambazo zitapingana na uamuzi na maoni ya wale walioshuhudia kuongezeka kwa kazi ya Ukweli wa leo, na ambaye maisha yao yamesukwa na maendeleo ya kazi hiyo. MUNGU hatachagua watu wenye uzoefu mdogo katika kuongoza kazi hii. Yeye Hatachagua wale ambao hawana uzoefu wa kupata mateso, majaribu, upinzani, na kupungukiwa na kuvumilia ili kuleta kazi hiyo kwenye jukwaa ambalo lipo kwa sasa. Sasa hivi kazi ya kuhubiri ujumbe wa Malaika wa tatu ni rahisi, ikilinganishwa na ilivyokuwa hapo awali. Wale ambao sasa wanafanya sasa kazi hii, wakifundisha wengine Ukweli, wana mambo ambayo wameshafanyiwa na wengine waliopita tayari. Wao hawawezi kupata shida kama wale wafanyakazi walioanza kupeleka Ukweli kabla yao. Ukweli umeshaletwa nje tayari kwaaajili yao. Hoja zote zimeandaliwa. Hawa wanapaswa kuwa waangalifu jinsi wanavyoinuliwa, ili wasije wakapinduliwa. Wanapaswa kuwa waangalifu sana kwa kutokuwa na manung’uniko dhidi ya wale waanzilishi waliovumilia shida nyingi. {1T 238.3}

Watenda kazi wenye ujuzi waliofanya kazi wakati mzigo ulikuwa mzito na wakiwa wachache katika kusaidia kazi, MUNGU huwajali sana. Muwe waangalifu mnapowashutumu, au kunung'unika juu yao; kwa maana hakika hesabu yake itatolewa kwenu, na mkono unaofanikisha wa MUNGU hautakuwa nanyi. Ndugu wengine ambao wana uzoefu mdogo, ambao hawana mzigo wowote wa kazi ya MUNGU mioyoni mwao, na wamefanya kazi ndogo, na hata wengine hawajafanya lolote kuhusiana na kuendeleza Ukweli wa leo, na ambao hawana ufahamu wa mambo ya huko Battle Creek, ndio wanakuwa wa kwanza kutafuta makosa ya usimamizi wa kazi huko. Na wale ambao hawafuati utaratibu katika mambo yao ya kawaida, na kusimamia familia zao vyema, ndio ambao wanapinga uwepo wa mfumo, ambao utahakikisha utulivu katika kanisa la MUNGU. Hawana ladha nzuri katika masuala ya shughuli za kawaida za kidunia, na wanapinga chochote cha aina hiyo katika kanisa. Watu kama hao hawapaswi kuwa na sauti katika masuala ya kanisa. Ushawishi wao haupaswi kuwa na uzito wowote juu ya wengine. {1T 239.1}

## SURA YA 49

## WAKFU KAMILI

Ndugu mpendwa na Dada K: Katika maono yangu ya mwisho nilioneshwa mambo kadhaa kuhusu familia yako. Bwana ana mawazo yenye rehema kukuhusu wewe na Yeye hatakutelekeza, labda wewe umwache Yeye. L na M wana hali ya uvuguvugu. Lazima waamke na wafanye juhudi kwa wokovu wao, la sivyo watashindwa kupata uzima wa milele. Lazima wahisi jukumu lao la binafsi na wawe na uzoefu wao wenyewe. Wanahitaji wafanyiwe kazi na ROHO WA MUNGU mioyoni mwao, ambayo itawaongoza kupenda na kuchagua jamii ya watu wa MUNGU kuliko kikundi kingine, na kujitenga na wale ambao hawana upendo wa vitu vya kiroho. Yesu anadai kujitoa kikamilifu, kujitoa wakfu kikamilifu. L na M, hamjatambua kuwa MUNGU Anahitaji mapenzi yenu yasiyogawanyika. Unakiri utakatifu, lakini umezama na kuwa katika kiwango cha kuwa mfu kiimani au muumini wa mdomo bila matendo. Unapenda kushirikiana na vijana ambao hawajali Kweli takatifu ambayo unakiri. Unafanana na hao wenzako, na umeridhika na uumini wa mdomo tu, dini inayofanya ukubaliwe na wote, bila kukosolewa na yoyote. {1T 240.1}

Kristo anadai yote. Kama angedai pungufu, dhabihu Yake iyolikuwa ya gharama sana, isingetuleta kwenye kiwango kama hicho. Imani yetu takatifu inapaza sauti ikilia Kujitenga. Hatupaswi kufanana na ulimwengu, au kuwa waumini wa mdomo na wala siyo matendo. "Mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu." Hii ndiyo njia ya kujikana. Na unapofikiria kuwa njia hii ni nyembamba na ngumu sana, kwamba kujikana kumezidi sana katika njia hii nyembamba; jiulize swali hili mwenyewe! Je Kristo alitoa nini kwa ajili yangu? Hili swali linaweka chochote tunachoweza kuita ni kujikana kupwaya sana. Mtazame Yeye bustanini, akitokwa na jasho la matone makubwa ya damu. Malaika aliye peke yake anakwenda mahali pale pa faragha, ametumwa kutoka mbinguni kumtia nguvu Mwana wa MUNGU. Mfuate akiwa njiani kuelekea kwenye ukumbi wa mahakama, wakati anapodhihakiwa, anapodharauliwa, na kutukanwa na umati ule wenye hasira. Mtazame Yeye akiwa amevaa joho hilo la kifalme la zambarau. Sikiliza mizaha michafu na kejeli za kikatili. Anawaona wakiweka kwenye paji Lake la uso Wake mtukufu taji ya miiba, kisha wanampiga kwa mwanzi, ukisababisha miiba hiyo kupenya usoni mwake, na damu kutiririka kutoka kwenye uso huo mtakatifu. Sikia umati huo ulio na ghadhabu ukilia upate damu ya Mwana wa MUNGU. Yesu metiwa mikononi mwao, na wanamwongoza Yule Mtukufu na mwungwana wanayemtesa, uso Wake ukiwa umechoka, dhaifu, na anazimia njiani akienda kusulubishwa. Amenyooshwa juu ya msalaba wa mbao, na misumari inasukumwa kupitia mikono na miguu Yake minyororo. Mtazame, akining'inia msalabani katika saa hizo za kutisha na za uchungu mpaka malaika wanafunika nyuso zao kutoka kwenye tukio hilo la kutisha, na jua linaficha nuru yake, likikataa kumtazama. Fikiria juu ya vitu hivi, kisha jiulize, Je! Njia ni nyembamba na ngumu sana? Hapana, hapana. {1T 240.2}

Ukiwa na moyo uliogawanyika, ulio nusu-nusu, utapata shaka na giza. Hautafurahia faraja za dini, wala amani ambayo ulimwengu hutoa. Usiketi kwenye kiti rahisi cha Shetani cha kufanya madogo tu, lakini inuka, na kulenga kiwango kilichoinuliwa ambacho ni fursa yako kukifikia. Ni pendeleo lenye baraka kuacha yote kwa ajili ya Kristo. Usiangalie maisha ya wengine na kuwaiga, na kisha usiinuke zaidi. Wewe una Mfano mmoja tu usio na makosa. Ni salama kumfuata Yesu peke yake. Amua kuwa ikiwa wengine watatenda kwa kanuni ya ugoigoi wa kiroho, wewe utawaacha na kusonga mbele kuelekea mwinuko wa tabia ya Kikristo. Jenga tabia ya mbinguni. Usilale kwenye kituo chako cha ulinzi. Shughulikia kwa uaminifu na kweli nafsi yako mwenyewe. {1T 241.1}

Unaendekeza uovu ambao unaleta tishio la kuharibu maisha yako ya kiroho. Hali hii itaziba uzuri wote wa shauku ya kurasa takatifu (Biblia). Ni kupenda kusoma hadithi za mapenzi, hekaya na mambo mengine yasiyokuwa na mvuto mzuri kwenye akili ambayo imewekwa wakfu kwa njia yoyote kwaajili ya kazi ya MUNGU. Uovu huu utakusababishia mhemko/msisimko usio mzuri wala usio na uhalisia, homa za mawazo na kuifanya akili isiweze kufanya shughuli yake, na pia inakosa kufaa kushughulikia mambo ya kiroho. Inatoa moyo kwenye maisha ya maombi na kupenda vitu vya kiroho. Usomaji ambao utakupatia nuru ya Maandiko matakatifu, na kuchochea hamu yako ya bidii ya kusoma, na kujifunza, hauna hatari, bali faida. Uliwasilishwa kwangu na macho yako yakiwa yamegeuzwa kutoka kwenye Kitabu Kitakatifu na kutazama kwa umakini vitabu vya kusisimua, ambavyo vinaleta kifo cha kiroho (mambo ya dini/ibada). Kadri unavyochunguza Maandiko kwa bidii mara kwa mara, ndivyo uzuri Wake unavyozidi kuonekana zaidi, na utajiona kutopendezwa na kusoma vitu visivyokuwa na maana-Utaona havina ladha. Usomaji wa Maandiko wa kila siku utakupatia ushawishi kwenye akili zako. Utavuta hewa ya mbinguni. Weka hili gombo la thamani kwenye moyo wako. Litakudhihirishia kuwa rafiki, mwongozo na dira katika shida zote. {1T 241.2}

Umekuwa na malengo fulani kwenye maisha yako, na lo! Jinsi ambavyo umeyafanyia kazi kwa bidii na uvumilivu ili uyafikie! Umenuia na kuyapanga hadi matarajio yako yakatokezea. Kuna lengo mbele yako sasa ambalo unatakiwa ulidumishe, usichoke, na ulifanyie juhudi maisha yako yote. Lengo hili ni wokovu wa roho yako--uzima wa milele. Na hili linahitaji ujikane nafsi, ujinyime, ujitolee, na kusoma Neno la MUNGU kwa karibu. Lazima utakaswe na kusafishwa. Unapungukiwa na mvuto wa ROHO WA MUNGU uokoao. Unajichanganya na marafiki zao na kusahau kwamba umeitwa kwa Jina la Kristo. Matendo na mavazi yako ni kama yao. {1T 242.1}

Dada K, niliona una kazi ya kufanya. Lazima ufishe kiburi na kufanya mapenzi yako yote yawe katika Kweli. Masilahi yako ya milele yanategemea

mwenendo/kusudi unalochukua sasa. Kama utapata uzima wa milele, lazima uishi kwa huo na kujikana mwenyewe. Toka ulimwenguni, na ujitenge. Maisha yako lazima yawe na kiasi, kukesha, na sala. Malaika wanaangalia ukuaji wa tabia na kupima uzani wa maadili yako. Maneno na matendo yetu yote yanapita mbele za MUNGU. Ni wakati wa kutisha, adhimu na wenye kuogofya. Matumaini ya uzima wa milele hayapaswi kuchukuliwa kwa wepesi; lazima mambo yawekwe sawa kati ya MUNGU na nafsi yako mwenyewe. Wengine hutegemea uamuzi na uzoefu wa wengine badala ya kujishughulisha kuchunguza mioyo yao kwa karibu, na wanapita kwa miezi na miaka bila kushuhudia ROHO WA MUNGU, au ushahidi wa kukubaliwa kwao. Wanajidanganya wenyewe. Wana tumaini wanalolidhania, lakini wanapungukiwa sifa muhimu za Mkristo. Kwanza lazima moyo ufanyiwe kazi kamili, basi tabia zao zitachukua tabia hiyo iliyoinuliwa, na nzuri ambayo inaashiria wafuasi wa kweli wa Kristo. Inahitaji juhudi na ujasiri wa kimaadili kuishi kwa imani yetu. {1T 242.2}

Watu wa MUNGU ni wa kipekee. Roho yao haiwezi kuchanganyika na roho na mivuto ya kiulimwengu. Hauna haja ya kubeba Jina la Kikristo tu na kisha usilistahili. Huwezi kukutana na Yesu kwa kumkiri kwa mdomo tu. Hutaki kudanganywa katika jambo hili muhimu sana. Chunguza kikamilifu msingi ya matumaini yako, na uwe mkweli kwako mwenyewe. Shughulika na roho yako mwenyewe. Matumaini yanayodhaniwa hayatakuokoa kamwe. Je? Umehesabu gharama. Nachelea hujafanya hivyo. Amua sasa kama utamfuata Kristo, haijalishi ni gharama ya kiasi gani. Huwezi ukafanya hili na kisha ukafurahia ushirika wa wale ambao hawajali mambo ya mbingu. Roho yako haiwezi kuchangamana nao, kama vile mafuta na maji yasivyoweza kuchangamana

Ni jambo kubwa kuwa mwana wa MUNGU, na mrithi pamoja na Kristo. Ikiwa hii ni fursa yako, utajua utashiriki mateso ya Kristo. MUNGU anautazama moyo. Niliona kwamba unapaswa kumtafuta Yeye kwa dhati na bidii. Na kuinua viwango vyako vya utauwa juu zaidi, vinginevyo utashindwa kuurithi ufalme wa milele. Unaweza kuuliza swali. Kweli dada White alisema hivi? Ndiyo; na Nimejaribu kuliweka hili mbele yako na kukupa maoni niliyopewa na Bwana. Hebu BWANA akusaidie kusikia na kutenda haya. {1T 243.2}

Wapendwa ndugu na dada, waangalieni watoto wenu kwa utunzaji wenye wivu. Roho na ushawishi wa dunia unaharibu shauku yao ya kuwa Wakristo wa kweli. Hebu ushawishi wenu uwavute watoke kwa vijana wenzao ambao hawana shauku na mambo ya mbinguni. Wanapaswa kutoa kafara ikiwa wanataka kuipata mbingu hatimaye. {1T 243.3}

# SURA YA 50

# UZOEFU BINAFSI

Septemba 20, 1860, mtoto wangu wa nne, John Herbert White, alizaliwa. Alipokuwa na umri wa wiki tatu, mume wangu alihisi kuwa ni jukumu lake kusafiri (maeneo mbalimbali kwa uinjilisti). Iliamuliwa katika mkutano wetu wa Konferensi kwamba ndugu Loughborough aende Magharibi ya Marekani na mume wangu aende Mashariki. Siku chache kabla ya kuondoka, mume wangu alikuwa na huzuni sana akilini. Wakati fulani alifikiri angeachana na safari, lakini aliogopa kufanya hivyo. Alihisi kuwa alikuwa na kitu cha kufanya, lakini alikuwa amefungwa na mawingu ya giza. Hakuweza kupumzika au kulala. Akili yake iliendelea katika fadhaa/tashwishwi. Akawajulisha wenzake fadhaa ya akili yake kwa ndugu Loughborough na Cornell, na wakapiga magoti mbele za MUNGU pamoja nao kutafuta ushauri Kwake Bwana. Kisha mawingu yakatoweka, na mwanga wazi ukaangaza. Mume wangu alihisi kwamba ROHO MTAKATIFU alikuwa akimuelekeza mume wangu aende Magharibi na ndugu Loughborough aelekee Mashariki. Baada ya haya walihisi wazi juu ya wajibu wao na wakaondoka kama ilivyopasa kulingana na maagizo- ya ROHO MTAKATIFU. {1T 244.1}

Huku nyuma baada ya mume wangu kuondoka tuliomba kwamba MUNGU awe na mume wangu na kumtia nguvu, na kupata uhakikisho kwamba MUNGU angekuwa naye. Karibu wiki moja kabla ya kutembelea Mauston, Wisconsin, tulipokea barua kwa ajili ya kuchapishwa kutoka kwa dada G akidhani ni maono aliyopewa na MUNGU. Tuliposoma barua hizo, tulihisi kufadhaika; kwani tulijua kuwa barua hizo hazikutoka katika chanzo sahihi. Na kwa kuwa mume wangu hakujua chochote kuhusu zile barua na alikuwa karibu kukutana nao huko Mauston, tuliogopa kuwa hatakuwa tayari kukutana na ushabiki, na kwamba hili lingekuwa na ushawishi wa kukatisha tamaa akilini mwake. Tulikuwa tumepitia matukio mengi kama haya katika uzoefu wetu wa hapo awali, na tukasumbuliwa sana na roho hizi zisizo na nidhamu, zisizoweza kuongozwa au kuthibitiwa, hata tuliogopa kukutana nao. Nilituma ombi kwa kanisa huko Battle Creek kumuombea mume wangu, na kwenye madhabahu ya familia yetu tulimtafuta MUNGU kwa dhati na bidii kwa niaba ya mume wangu. Kwa roho iliyovunjika, na machozi mengi, tulijaribu kufunga imani yetu yenye kutetemeka kwa nguvu, juu ya ahadi za MUNGU, na tulikuwa na ushahidi kwamba Yeye alitusikia tukiomba na kwamba atasimama karibu na mume wangu na kumpa ushauri na hekima. {1T 244.2}

Wakati nilipokuwa nikitafuta katika Biblia fungu la kukariri kwa ajili ya Willie kusoma na kukariri kwa ajili ya Shule ya Sabato, Andiko hili lilidaka umakini wangu: "Bwana ni mwema, ni ngome katika siku ya shida; Naye anawajua wamtumainio. "Sikuweza kujizuia kuangua kilio juu ya Maneno haya, ambayo

yaliyoonekana yanafaa sana. Mzigo wote juu ya akili yangu ulikuwa kwa mume wangu na kanisa huko Wisconsin. Mume wangu alitambua baraka za MUNGU wakati alipokuwa Wisconsin. MUNGU alikuwa ngome yake wakati wa shida na alimtegemeza na ROHO MTAKATIFU wakati alikuwa na ushuhuda thabiti dhidi ya ushabiki wenye wendawazimu huko (Mauston,Wisconsin). {1T 245.1}

Nilipokuwa Mackford, Wisconsin, mume wangu aliniandikia barua na kusema: "Ninaogopa kwamba mambo hayako sawa hapo nyumbani. Nimekuwa na maono kuhusu mtoto wetu mchanga." Wakati akiombea familia nyumbani, alioneshwa kwamba mtoto alikuwa mgonjwa sana. Mtoto alionekana amelala mbele yake na uso na kichwa vimevimba sana. Nilipopokea barua, mtoto alikuwa kama kawaida; lakini asubuhi iliyofuata aliugua sana. Ilikuwa kesi mbaya ya erysipela katika uso na kichwa (maambukizi ya ngozi). Mume wangu alipofika kwa ndugu Wick, karibu na Round Grove, Illinois, alipokea barua iliyomjulisha ugonjwa wa mtoto huyo. Baada ya kuisoma, aliwaambia wale waliokuwepo kwamba hakushangazwa na habari hiyo, kwani MUNGU alikuwa ameiandaa akili yake kwa hilo, na kwamba wangesikia kwamba kichwa na uso wa mtoto umeathiriwa sana. {1T 245.2}

Mtoto wangu mpendwa alikuwa mgonjwa sana. Siku ishirini na nne usiku na mchana tulimwangalia kwa wasiwasi, tukitumia kila njia tunayoweza kufanya ili aweze kupona na kuwasilisha hoja ya ugonjwa wake kwa MUNGU. Wakati mwingine sikuweza kudhibiti hisia zangu nilipokuwa nikishuhudia mateso yake. Muda wangu mwingi ulitumika kwa machozi na dua za unyenyekevu kwa MUNGU. Lakini Baba yetu wa mbinguni aliona ni vyema kumwondoa mpendwa wetu.{1T 245.3}

Desemba 14 hali yake ilikuwa mbaya zaidi, na niliitwa. Nilipokuwa nikisikiliza kupumua kwake kwa shida na mkono wake uliokosa mapigo ya moyo kabisa, nilijua kwamba lazima afe. Mkono wa baridi wa kifo tayari ulikuwa juu yake. Hiyo ilikuwa saa ya uchungu kwangu. Tuliangalia udhaifu wake, akipumua kwa shida pumzi hadi ikakoma, na tunaendelea kushukuru kuwa mateso yake yamekwisha. Wakati mtoto wangu akikata roho, sikuweza kulia. Moyo uliniuma sana kana kwamba utapasuka, lakini sikuweza kutoa machozi. Kwenye mazishi nilizimia. Tulivunjika moyo kwa kumkosa ndugu Loughborough kuongoza ibada ya mazishi, na mume wangu alizungumza juu ya hafla hiyo kwenye nyumba iliyojaa watu. Kisha tukamfuata mtoto wetu kwenye makaburi ya Oak Hill, Battle Creek, Michingan, apumzike huko hadi Mtoaji wa Uhai atakapokuja, kuvunja pingu za kaburi na kumwita kwa ajili ya uzima wa milele. {1T 246.1}

Baada ya kurudi kutoka kwenye mazishi, nyumba yangu ilionekana kuwa ya upweke. Nilihisi kupatanishwa na mapenzi ya MUNGU, hali ya huzuni ilitulia juu yangu. Mioyo yetu haikuweza kuinuka juu ya huzuni na kukata tamaa tulikokupata msimu wa joto uliopita. Kutokana na hali za watu wa MUNGU hatukujua nini cha kutarajia. Shetani alikuwa amepata udhibiti wa akili za

wengine ambao walikuwa karibu na sisi katika kazi hiyo, hata baadhi ambao walikuwa wakijua utume wetu na walikuwa wameona matunda ya kazi zetu, na ambao hawakuwa wameshuhudia tu udhihirisho wa mara kwa mara wa nguvu ya MUNGU, lakini walikuwa wamehisi ushawishi wake juu ya miili yao wenyewe. Je! Tunaweza kutumaini nini katika siku zijazo? Wakati mtoto wangu aliishi, nilifikiri nilielewa wajibu wangu. Nilimsogeza mtoto wangu mpendwa karibu na moyo wangu na nilifurahi kuwa angalau kwa msimu mmoja wa baridi ningeachiliwa kutoka katika kulifanya jukumu kubwa, kwani isingekuwa jukumu langu kusafiri wakati wa baridi na theluji na mtoto wangu mchanga. Lakini wakati alipochukuliwa kutoka kwangu, nilitupwa tena katika mtanziko mkubwa. {1T 246.2}

Hali ya kazi ya MUNGU na watu, vilikuwa karibu vituvunje kabisa. Furaha yetu daima hutegemea hali ya kazi ya MUNGU. Wakati watu Wake wako katika hali ya kufanikiwa, tunajisikia huru; lakini wanaporudi nyuma na kuna ugomvi kati yao, hakuna kitu kinachoweza kutufurahisha. Masilahi yetu yote na maisha yetu yamefungamana na kuinuka, ongezeko na maendeleo ya ujumbe wa malaika wa tatu. Tumefungamanishwa ndani yake, na wakati ujumbe unaonekana kurudi nyuma kwa kutokuwa na mafanikio, tunapata mateso makubwa ya akili. {1T 246.3}

Wakati huu, mume wangu, alivyopitia mapito ya zamani, alianza kupoteza imani/ujasiri kwa karibu kila mtu. Wengi miongoni mwa wale ambao alikuwa amejaribu kuwafanya marafiki katika Yesu Kristo walikuwa wamekuwa sehemu ya maadui, na wengine ambao alikuwa amewasaidia zaidi kwa ushawishi wake na kifedha kutoka kwenye mkoba wake wenye pesa ndogo, walikuwa wakijaribu kuendelea kumdhuru na kumtwika mizigo. Asubuhi moja ya Sabato, wakati tulipokuwa tukienda mahali petu pa ibada, hisia kubwa ya ukosefu wa haki ilimzonga hadi akageuka kando na kulia kwa sauti, wakati mkutano ukimsubiri. {1T 247.1}

Tangu mwanzo wa kuanza kwa kazi zetu tumeitwa kubeba ushuhuda ulio wazi, unaosonda kidole kwa mhusika, na kukemea makosa na tusiache chochote. Na njia yote tumekuwa na wenzetu ambao wamesimama kinyume na ushuhuda wetu, na wamerudi nyuma yetu kuongea ushuhuda laini, wakipaka zege isiyo laini, na kuharibu ushawishi wa kazi zetu. MUNGU angetuimarisha ili tuweze kukemea, na kisha watu binafsi wangeingia kati yetu na watu kufanya ushuhuda wetu usiwe na ufanisi au matokeo yoyote. Maono mengi wamepewa na athari zake kwamba hatupaswi kukwepa kutangaza ushuhuda wa MUNGU, lakini lazima tuchukue nafasi ya kuwachochea watu wa MUNGU, kwani wamelala katika dhambi zao. Lakini ni wachache ambao wametuhurumia, wakati wengi wamehurumia watu wabaya na wale ambao wamekemewa. Vitu hivi vilitukandamiza, na tukahisi kuwa hatuna ushuhuda wa kubeba kanisani. Hatukujua ni nani tutakayemtumaini kumwambia mambo haya ya faragha. Wakati upotoshaji wa shuhuda za Kweli ulipozidi, matumaini

yalikufa ndani yetu. Tuliamua kupumzika usiku wa manane, lakini sikuweza kulala. Maumivu makali yalikuwa moyoni mwangu; Sikuweza kupata afueni na nilizimia mara kadhaa. {1T 247.2}

Mume wangu aliwatuma ndugu Amadon, Kellogg, na C. Smith. Maombi yao ya bidii yalisikilizwa na MUNGU, tukapata faraja, na nikachukuliwa katika maono. Ndipo nikaoneshwa kuwa tunayo kazi ya kufanya, ambayo bado, lazima tutoe ushuhuda wetu, ulionyooka, na wa moja kwa moja kama tulivyoelekezwa na MUNGU. Nilioneshwa watenda kazi waliokwepa kwa makusudi kutoa shuhuda ilionyooka. Nikaona ushawishi wa mafundisho ya shuhuda za kweli ulivyoleta athari kwa watu wa MUNGU. {1T 247.3}

Hali ya watu ilivyokuwa kule ----- pia ilioneshwa mbele yangu kuwa wana nadharia ya Ukweli, lakini hawajatakaswa kupitia nadharia hiyo ya Ukweli. Nilioneshwa pia kwamba watendakazi wanapoanza kazi maeneo mapya, kazi yao ni mbaya zaidi ya ile iliyopotea isipokuwa watatoa shuhuda za wazi, zilizonyoka, kwa kazi ya MUNGU. Watendakazi wanapaswa kutofautisha kati ya Kanisa la Yesu Kristo na, Wakristo wa desturi na urasmi, wenye kufuata ratiba tu, wanaojidai kuwa Wakristo wa jina. Kulikuwa na kushindwa katika jambo hili----. Mzee N alikuwa akiogopa kuwakosea, alihofia imani yetu isije kuonekana ni ya kipekee; kiwango cha imani yetu kilishushwa ili kukubaliana na matakwa ya watu. Ilitakiwa watu waambiwe kwamba tunamiliki Kweli zenye umuhimu mkubwa, na kwamba masilahi yao ya milele yalitegemea uamuzi wao waliofanya katika kuenenda na Kweli zilizotolewa na watendakazi; kwamba ili wapate kutakaswa kwa Ukweli, wanapaswa kuacha miungu/sanamu zao, watubu dhambi zao, na kuzaa matunda yanayofaa kukutana na toba ya kweli. {1T 248.1}

Watendakazi ambao hushiriki katika kazi nzito ya kubeba ujumbe wa malaika wa tatu lazima wajitoe kikamilifu kwa uamuzi, na kwa Roho na Uweza wa MUNGU wahubiri Ukweli bila woga na waache ukatekate. Wanapaswa kuinua kiwango cha Ukweli na kuwahimiza watu wasimame kwa kiwango hicho cha Ukweli wa Neno. Kiwango kimeshushwa mara nyingi sana kukutana na watu katika hali yao ya giza na dhambi. Ni ushuhuda ulio wazi, ulionyooka, ndio ambao utawasaidia watu kukata shauri. Ushuhuda wa amani hautafanya hivi. Watu wana fursa ya kusikiliza aina hii ya mafundisho kutoka kwenye mimbari maarufu; lakini wale watumishi ambao MUNGU amewakabidhi ujumbe mzito, wa kutisha ambao unapaswa kuletwa nje kwa maandalizi ya kufanya watu wafae kwaajili ya kuja kwa Yesu Kristo, wanapaswa kutoa ushuhuda ulio wazi na dhahiri. Ukweli wetu ni adhimu zaidi kuliko ule wa watu wanaodai kuwa Wakristo kwa majina, kwani mbingu ziko juu kuliko dunia. {1T 248.2}

Watu wamelala katika dhambi zao na wanahitaji kupewa tahadhari kabla hawajazembea katika uvivu wao. Wachungaji wao wamehubiri shuhuda laini; lakini watumishi wa MUNGU, ambao hubeba Ukweli mtakatifu, na muhimu, wanapaswa kupiga kelele nawasiache, ili Ukweli uvunje vazi la usalama na

Ukweli upate njia ya kwenda moyoni. Ushuhuda wa moja kwa moja ambao ulipaswa kutolewa kwa watu huko ----- wachungaji walikwepa/waliupinga; mbegu ya Kweli ilipandwa kati ya miiba na imesongwa nayo. Pamoja na mengine, vurugu za Shetani zimeshamiri, na neema za mbinguni zimekufa. {1T 249.1}

Watumishi wa MUNGU lazima watoe ushuhuda ulio wazi, ambao utakata moyo wa asili na kukuza tabia. Ndugu zangu N na O walienenda katika namna ambayo ni kuficha hisia na mawazo-----. Mahubiri kama hayo waliyohubiri hapo hayatafanya kazi ambayo MUNGU anapanga yatimize. Wachungaji wa makanisa ya jina hufanya wana hofu ya kutosha, na kuzifunika Ukweli ulio wazi ambao unakemea dhambi. {1T 249.2}

Pasipo watu kuukumbatia ujumbe vizuri, na mioyo yao iwe tayari kuupokea, itakuwa ni bora waachane nao kabisa. Nilioneshwa kuwa kanisa huko---- wana uzoefu wa kupokea; lakini itakuwa vigumu sana kwao kuupokea ushuhuda ulionyoka sasa kama ambavyo wangeupata hapo mwanzo, ikiwa wangepewa ushuhuda ulionyoka hapo mwanzoni, wangegundua kuwa walikuwa na makosa. Kisha miiba ingeweza kung'olewa kwa urahisi zaidi. Walakini niliona kwamba kulikuwa na watu wenye maadili mema katika -----, wako wengine ambao bado watajaribiwa juu ya Ukweli wa sasa. Ikiwa kanisa litainuka na kuongoka, MUNGU atarudi kwao na kuwapa ROHO MTAKATIFU. Kisha ushawishi wao utanena kwaajili ya Ukweli. {1T 249.3}

## SURA YA 51

## KAZI HUKO MAGHARIBI.

Nimeona kwamba watu wenye heshima, na wenye stahiki, wameukumbatia Ukweli huko Magharibi, na hawa watakuwa nguzo ya kusudi la kazi ya Mungu. Watakapoweza kuweka pembeni mambo yao ya kidunia, ya muda mfupi na kuamua kutumia sehemu ya mapato yao, wataweza kufanya sehemu yao katika kudumisha kazi ya Injili. Niliona pia kwamba wengine walikuwa tayari kupokea Ukweli, ulioletwa kwao kwa ukarimu wa ndugu zao wa Mashariki, bila gharama yoyote kwao. Ndugu wa Magharibi wanapaswa kuamka na kukidhi gharama za maao wenyewe. Mwenyezi Mungu anahitaji wajitoea kwa kazi ya Injili, na wanapaswa kuhisi ni fursa ya kufanya hivyo. Bwana atawathibitisha,

atawajaribu kuona ikiwa wataondoa mapenzi yao ulimwenguni na kuifanya imani yao iwe kamilifu kwa matendo. {1T 250.1}

Niliona kwamba mkono wa MUNGU ulikuwa umenyooshwa kukusanya roho huko Magharibi. Yeye Amekuwa akileta watu ambao wanaweza kufundisha Ukweli kwa wengine, ambao ni wajibu wao kubeba ujumbe na kupeleka maeneo mapya ambako Injili bado haijafika. Niliona kwamba ikiwa watu ambao wamehama kutoka Mashariki na kwenda Magharibi na wamevumilia ugumu wa kuhamia katika ardhi mpya na wamemudu kuanzisha maisha mapya, wataweza kupokea Ukweli wa leo wa Neno la Mungu kwa uelewa na wataonesha uvumilivu na tabia yenye maamuzi yanayoendana sambamba na ile Kweli, sambamba na kumiliki mali ya muda mfupi, kisha watajitoa kwa moyo kwa kazi ya kuendeleza mbele Ukweli/Injili. Iwapo moyo wa kujitoa kwa ari unakosekana, Ukweli bado haujawa na athari ya kuokoa, na nguvu yenye Uweza wa Kutakasa itakosekana kwao. {1T 250.2}

Nilielekezwa kwenye mkutano tena -----. Ndugu P alihisi mzigo wa kazi yetu, lakini ndugu R alikuwa na roho ya upinzani. Ushuhuda wake haukuwa katika muungano na kazi ya MUNGU, na alileta huzuni na mzigo kwa wale ambao walikuwa wakiendeleza kazi ya Uinjilisti. Lakini ingekuwa bora kwa kazi ya Mungu kama ndugu P angeachwa hapo kwa muda mrefu, kwani ingesaidia ndugu waliokumbwa na machafuko yaliyosababishwa na ndugu R. Niliona kwamba ndugu P alikosa busara kwa upande wake. Hii ilimpa ndugu R na maadui wa imani yetu faida. Ndugu P alipaswa kungojea ndugu R apate kukua kiroho. Punde angeweza kujiunga na watu wa MUNGU ambao ni masalio au kwenda upande wa upotevu. Lakini ndugu R alipata huruma kwa sababu ya umri wake. Alikuwa ameshiriki katika chama cha Mjumbe, na mwenendo wake uliathiriwa na mafundisho yake potofu, na kupelekea mwenendo wake wote kutiwa giza na hilo. Mkewe ana roho ya kiherehere, msisimko na uchungu, na amekuwa na bidii ya kueneza ripoti za uwongo. Yeye hutenda kwa mumewe, sehemu ambayo Yezebeli alimfanyia Ahabu, na anamchochea kupigana dhidi ya watumishi wa MUNGU, ambao wanatoa ushuhuda ulio wazi, ulionyooka. {1T 250.3}

Ushawishi wao Mashariki umeamuliwa dhidi ya roho ya Ukweli na wale ambao wamejitolea maisha yao wakfu ili kufanya kazi kwa maendeleo yake. Kuna tabaka Mashariki ambalo wanadai kuamini katika Ukweli, lakini ambao wana hisia za siri za kutoridhika dhidi ya wale wanaobeba mzigo katika kazi hii. Hisia za Kweli huwa hazionekani mpaka ushawishi fulani unaopinga kazi ya MUNGU utokee, na kisha hudhihirisha tabia zao za kweli. Watu kama hao hupokea kwa urahisi, kuthamini, na kusambaza nakala ambazo hazina msingi katika Ukweli, ili kuharibu ushawishi wa wale wanaohusika katika kazi hii. Wale wote ambao wanataka kutoka katika mwili watakuwa na nafasi ya kufanya hivyo. Kuna mtihani utakuja ili kumjaribu kila mtu. Wakati mzuri wa kupepetwa uko mbele yetu. Wenye wivu, wenye kutafuta makosa na wale watafutao mabaya,

watapepetwa nje. Wanachukia kukaripiwa, na kuchukia au kudharau marekebisho. Wale wanaopenda roho ya ujumbe wa malaika wa tatu hawawezi kuwa na uhusiano na roho ya Ndugu R na mkewe. {1T 251.1}

## SURA YA 52

## SWALI LAJIBIWA

Swali hili limeulizwa mara nyingi na wale ambao wameshawishiwa na maadui zangu: "Je! Dada White naanza kujivuna? Tumesikia kwamba alikuwa amevaa kofia  iliyojaa upinde na ribboni." (bows and Ribbons) {1T 251.2}

Natumaini sijaanza kujivuna. Namna ya uvaaji wangu wa mavazi umekuwa ni ule ule kama ilivyokuwa kwa miaka kadhaa. NInapinga sketi aumagauni marefu yenye kuburuza chini, na yenye kiuno kidogo ambacho kinabana, na ndani kina gagulo ya chuma au mifupa ya samaki (hoops), na kuvaa upinde na ribboni zisizo za lazima. Nimevaa kofia moja ya velvet miaka miwili bila mabadiliko ya kama za kufunga, isipokuwa kuzisafisha kwa sabuni na maji. Ninaweka velvet sawa juu ya sura mpya na nimeivaa tena msimu huu wa baridi. Ninaamini watunza Sabato wanapaswa kuvaa mavazi rahisi na kujifunza kuwa wachumi katika mavazi. Wale ambao wanataka kuzungumza watazungumza ingawa sisi hatuwapi nafasi ya kufanya hivi kwa matendo au kuvaa kwetu (wambeya watakuwa wambeya huwezi kuwabadilisha). Sitarajii kukidhi kila ladha kuhusu mavazi, lakini naamini ni jukumu langu kuvaa mavazi imara na yenye kudumu, kuvaa vizuri na kwa utaratibu, na kuiridhisha ladha yangu mwenyewe ikiwa haipingani na Neno la MUNGU. {1T 251.3



## SURA YA 53

## KASKAZINI NA KUSINI

(Vita vya Wenyewe kwa Wenyewe Marekani, Kusini na Kaskazini vilivyohusu kumiliki watumwa-Civil War 1863-1865)

Januari 4, 1862, nilioneshwa mambo kadhaa kuhusu taifa letu. Usikivu wangu ulivutwa ili kuoneshwa uasi wa Kusini mwa Marekani. Watu wa Kusini mwa Marekani walikuwa wamejiandaa kwa mzozo mkali, wakati Marekani kaskazini walikuwa hawana taarifa zozote za mipango ya uasi wa Kusini mwa Marekani. Kabla ya utawala wa Rais Lincoln kuanza, faida kubwa ilichukuliwa Kusini mwa Marekani. Utawala wa zamani ulipanga na kusimamia Marekani ya kusini kuwaibia Kaskazini zana zao za vita. Walikuwa na malengo mawili kufanya hivyo:

1. Walikuwa wanatafakari na kuamua kufanya uasi, na waliamua wajiandae kikamilifu;

2. Walipanga kuwa watakapofanya uasi, wenzao wa Kaskazini watakuwa wamewashambuliwa kwa kushitukizwa pasipo kujiandaa, hivyo basi Kusini watahitaji muda wa kujiandaa kwa mashambulizi, na kwa vitisho vyao vikali na mwenendo wao wa ukatili walidhani wangeweza kuwatisha Kaskazini kwamba watalazimika kujisalimisha kwao na kuachia Kusini ifanye kila kitu watakavyo. {1T 253.1}

Kaskazini hawakujua chuki kali, na ya kutisha ya Kusini dhidi yao, na hawakuwa wamejiandaa kwa njama zao za kina. Kaskazini walikuwa wamejivunia nguvu

zao na walidhihaki wazo la Kusini kuondoka katika muungano. Walichukulia hivo kama vitisho vya mtoto mkaidi anapojidai na walidhani kwamba Kusini itarudi kwenye fahamu zake, na kuugua kwa kujuta kuuacha Muungano, kwamba mwishowe wangenyenyekea huku wakiomba radhi na kurudi kwenye umoja. Hakika kaskazini hawakujua kabisa nguvu ya mfumo uliolaaniwa wa utumwa. Ni hili, na hili peke yake, ndiyo ilikuwa msingi wa vita. Kusini wameendelea na kuzidi ukaidi na kutoa madai makali. Wanaona ni haki kabisa kwao kuuza wanadamu, kushughulika na biashara ya watumwa, na kuwatumikisha kama wanyama, na hata kushugulika na roho za wanadamu. Wao hukasirika na kuvurugikiwa kabisa ikiwa hawawezi kupata eneo lolote wanalotaka. Wangeondoa kabisa mipaka na kuwaleta watumwa wao mahali popote wanapopenda, na kuilaani ardhi kwa kazi ya watumwa. Lugha ya Kusini imekuwa ikiamrisha kwa mamlaka na udiktena, na Marekani ya Kaskazini hawajachukua hatua zinazofaa kuinyamazisha Kusini. {1T 253.2}

Uasi huo ulishughulikiwa kwa uangalifu sana, polepole, kiasi kwamba wengi ambao mwanzoni walikuwa na hofu kwa sababu ya uasi, hatimaye walishawishiwa na waasi kuwa uasi ni sawa, na ni haki, na maelfu walijiunga na Shirikisho la Kusini  ambalo halingekuwa na hatua za haraka na za uhakika kufanya na Serikali yetu katika kipindi cha mapema cha uasi, hata kama hawakujiandaa kama ilivyokuwa wakati huo kwa vita (vya wenyewe kwa wenyewe). Kaskazini  wamekuwa wakijiandaa kwa vita tangu wakati huo, lakini uasi umekuwa ukiongezeka kwa kasi, na sasa hakuna matarajio bora ya kusitisha mambo kuliko ilivyokuwa miezi iliyopita. Maelfu wamepoteza maisha yao, na wengi wamerudi makwao, wakiwa wamepoteza viungo, vilema maisha yote, afya zao zimetoweka, matarajio yao ya kidunia yameharibiwa milele; na bado ni kidogo kiasi gani kimepatikana! Maelfu wameshawishiwa kujiandikisha vita kwa ufahamu kwamba vita hii ilikuwa ni ya kumaliza utumwa; lakini sasa kwa kuwa wameachwa katika hali hii mbaya, wanaona kuwa wamedanganywa, kwamba lengo la vita hii ilikuwa sio kuukomesha utumwa, bali ni kuuhifadhi ulivyo. {1T 254.1}

Wale ambao wamejitosa kuacha nyumba zao na kujitolea maisha yao ili kumaliza utumwa hawajaridhika. Hawaoni matokeo mazuri kutoka kwa vita, isipokuwa kuuhifadhi Muungano, na kwa hili maelfu ya maisha lazima yatolewe dhabihu na nyumba zifanywe ukiwa. Idadi kubwa imepotea  na kumaliza  muda wao wa maisha mahospitalini; wengine wamechukuliwa wafungwa na waasi, hatima ya kutisha zaidi kuliko kifo. Kwa kuzingatia haya yote, wanauliza: Ikiwa tutafanikiwa kutuliza uasi huu, ni nini kimepatikana kweli? Wanaweza kujibu tu kwa kukata tamaa: Hakuna kitu. Yale ambayo yalisababisha uasi hayakuondolewa. Mfumo wa utumwa, ambao umeharibu taifa letu, umebaki kuishi na kuchochea uasi mwingine. Hisia za maelfu ya askari wetu ni chungu. Wamepata ufukara mkubwa; hata hivyo wangeweza kuvumilia, ila wanaona

wamedanganywa na wamekata tamaa. Watu wetu wanaotuongooza wanashangaa, mioyo yao imefadhaishwa kwa hofu. Wanahofia kutangaza uhuru kwa watumwa walioshikiliwa na waasi, kwani kwa kufanya hivyo wataipekecha sehemu hiyo ya Kusini ambayo haijajiunga na uasi lakini inamilikiwa na watu wenye itikadi kali ya kumiliki watumwa. Na tena wameogopa ushawishi wa wale watu wenye nguvu na wanaopinga biashara ya utumwa, wakiwa na madaraka na vituo muhimu. Wameogopa matokeo ya sauti za ujasiri, zilizo na maamuzi, kwani hizi zikichochewa moto na kuleta mwali wa tamaa kali miongoni mwa maelfu ya watu, basi zingefuta kabisa uasi huu mbaya, kwa kuwaacha watumwa wanyonge waende huru na kuvunja kila nira. {1T 254.2}

Wengi wa wale ambao wamepewa madaraka ya juu kwenye vituo muhimu dhamiri zao ni ndogo, hawana uungwana/ubora wa roho; wangeweza kutumia madaraka yao hata kuwaangamiza wale walio chini yao, ila wamejifanya kana kwamba hawaoni kinachoendelea kwa kufumba macho yao. Makamanda hawa wangeweza kutumia vibaya madaraka waliyopewa na kusababisha wale walio chini yao kuchukua nafasi za hatari ambapo wangeweza kukutana na waasi bila matumaini hata kidogo ya kuwashinda. Kwa njia hii wangeweza kuondoa maisha ya watu wenye ujasiri, makini na wenye msimamo, kama Daudi alivyomtoa Uria. 2 Samweli 11:14, 15. {1T 255.1}

Watu wenye thamani wametolewa kafara ili kuondoa ushawishi wao wa nguvu wa kupinga biashara ya utumwa. Baadhi ya waliokufa ni wale ambao Kaskazini wanawahitaji sana katika wakati huu muhimu, ambao huduma zao zingekuwa na umuhimu mkubwa, ila sasa hawapo. Wametolewa kafara kinyama. Matarajio ya taifa letu yanakatisha tamaa, kwani bado kuna wale wanaosimamia vituo muhimu ambao moyoni ni waasi. Kuna maafisa wakuu ambao wanawahurumia waasi. Ingawa wanatamani Muungano uhifadhiwe, wanawadharau wale ambao wanapinga biashara ya utumwa. Baadhi ya majeshi pia yanajumuisha watu kama hao au hali hizo; wanapingana kiasi kwamba hakuna umoja halisi uliopo kati ya vikosi vya jeshi. {1T 255.2}

Wakati vita hii inaoneshwa kwangu, ilionekana kama yenye umoja katika ajenda moja na isiyo na uhakika ambayo imepata kutokea. Sehemu kubwa ya waliojitolea jeshini kuzima uasi waliandikishwa wakiamini kabisa kuwa matokeo ya vita yatakuwa kukomesha utumwa. Wengine walijiandikisha wakikusudia kuwa makini sana katika kuendeleza utumwa kama ulivyo, lakini kuzuia uasi na kuhifadhi Muungano. Ila wakafanya jambo hilo kuwa la kutatanisha zaidi na lisilo na hakika, maafisa wengine waliokuwa wasimamizi, ni watu wenye nguvu za kujitolea ambao huruma zao zote ziko Kusini, lakini ambao wanapinga serikali tofauti. Ilionekana ni vigumu kuwa na vita itakayoendeshwa kwa mafanikio, kwani wengi wa makamanda wetu wenyewe wa Kaskazini waliendelea kufanya kazi kwa kuipendelea Kusini, na majeshi yetu

yalirudishwa nyuma na kuuawa bila huruma kwa sababu ya usimamizi wa watu hawa waliopendelea biashara ya utumwa. Baadhi ya watu wetu wanaoongoza katika Bunge pia wanafanya kazi kila wakati kwa kupendelea Kusini, Katika hali hii ya mambo, matamko hutolewa ya nchi zima kufunga/saumu kwa kuliombea taifa letu, kwa maombi kwamba MUNGU katika vita hivi ataleta suluhu mapema na kusitisha vita hivi (National fast). Kisha nikaelekezwa kwenye Kitabu cha, Isaya 58: 5-7: "Je! Kufunga namna hii ni saumu niliyoichagua mimi? Je! Ni siku ya kujitaabisha nafsi? Ni kuinama kichwa kama unyasi, na kutanda nguo za magunia na majivu chini yake? Je! Utasema ni siku ya kufunga,na ya kukubaliwa na BWANA? Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe?" {1T 256.1}

Niliona kwamba kufunga saumu kwa taifa lote ili kuliombea taifa kulikuwa kunamdhalilisha Yehova. Yeye hakubali kufunga kwa namna hiyo. Malaika wa kutunza kumbukumbu anaandika juu yao: "Mnafunga kwa ugomvi na malumbano, na kuwapiga ngumi za uovu." Nilioneshwa jinsi watu wetu wenye madaraka walivyowatendea watumwa maskini ambao walikimbilia kwao kwa ajili ya kupata ulinzi. Malaika wamenakili haya yote. Badala ya kuvunja nira zao na kuwaacha walioonewa waende huru, watu hawa wameifanya nira ya watumwa iweyenye kuwaumiza zaidi kuliko wakati walipokuwa wanawahudumia mabwana zao dhalimu. Kukosa uhuru kulisababisha watumwa maskini kuondoka kwa mabwana zao na kuhatarisha maisha yao kupata uhuru. Watumwa wasingejaribu kuwaacha mabwana zao na kukutana na shida za kuanikwa na vitisho ambavyo vinapelekea kukamatwa tena, kama sio watumwa hawa kupenda kuwa huru kama sisi wanadamu wote tupendavyo kuwa huru. Watumwa waliotoroka wamevumilia shida na hatari kubwa kupata uhuru wao, na kama vile tumaini lao la mwisho na kupenda kwao kuwa huru vinavyowaka katika vifua vyao, wanaenda kwa Serikali yetu ya Kaskazini ili kupata hifadhi ya ulinzi; lakini ujasiri na dhamiri yao imepokelewa kwa dharau kubwa. Wengi wao wametendewa unyama kwa sababu tu walionekana kuwa walifanya uhalifu mkubwa sana hadi kudiriki kutafuta kupata uhuru wao. Watu wakuu na wenye madaraka, wakihubiri kuwa wana mioyo ya kibinadamu, wamewaona watumwa wakiwa karibu uchi na wanakufa njaa, na wamewanyanyasa, na kuwarudisha kwa mabwana zao katili na kwenye utumwa usio na tumaini, kuteseka chini ya ukatili wa mwanadamu kwa kuthubutu kutafuta uhuru wao. Watumwa hawa wanyonge walitupwa gereza la chini ya ardhi na bovu, waliachwa wafe au wapone, hawakujali kabisa kama watapona au kufa. Watumwa hawa walinyimwa uhuru na hewa ya bure ambayo mbingu haijawahi kuwanyima, kisha wakaachwa wateseke katika kupata chakula na mavazi. Kwa kuzingatia

haya yote, bado mfungo wa kuliombea taifa unatangazwa! Lo, ni tusi na dharau kubwa kiasi gani kwa Yehova! Bwana asema kwa kinywa cha Isaya: "Walakini wananitafuta kila siku, na hupenda kujua njia Zangu, kama vile taifa lililotenda haki, wasioacha sheria ya Mungu wao." Isaya 58:2 {1T 257.1}

Watumwa waliotoroka waliambiwa na mabwana zao kwamba watu wa Kaskazini walitaka kuwamiliki ili waweze kuwatumia vibaya kwa ukatili; kwamba watu wa Marekani kaskazini ambao nia yao ilikuwa kukomesha utumwa (abolitionists of slavery) wangewatendea vibaya zaidi kuliko walivyotendewa na watu wa Kusini wakati wa utumwa. Aina zote za hadithi za kutisha zimerudiwa masikioni mwao na kuwafanya waichukie Kaskazini, na bado watumwa wengine wamekuwa na mawazo ya kuchanganyikiwa kwamba pengine baadhi ya watu wa Kaskazini walisikia malalamiko yao na wangefanya juhudi kuwasaidia. Hii imekuwa nyota pekee ambayo imewaangazia mwanga wake hafifu watumwa wenye shida na huzuni. Njia ambayo watumwa maskini wametendewa imewafanya waamini kwamba mabwana zao wamewaambia ukweli katika mambo haya. Na bado mfungo wa nchi zima wa kuliombea taifa unatangazwa! Bwana asema hivi: "Je! Hii sio saumu niliyoichagua? Kufungua minyororo ya uovu, kufungua mizigo mizito, na kuwaacha walioonewa waende huru, na kwamba mvunje kila nira?" Wakati taifa letu linapofanya mfungo ambao MUNGU ameuchagua, basi Yeye atakubali maombi yao kadri vita inavyohusika; lakini sasa maombi yao hayaingii masikioni Mwake MUNGU. Yeye Anageuka kutoka kwao, hao ni machukizo Kwake. Inaonekana sasa kwamba wale wasimamizi ambao wangeondoa mizigo mizito na kuvunja kila nira watawekwa makaripio/makemeo, au kuondolewa kutoka katika vituo vya uwajibikaji, au maisha yao yamepangwa mbali na wale ambao "hufunga kwa ugomvi na kujadili, na kupiga ngumi ya uovu. " (wako hatarini kuuwawa) {1T 258.1}

Nilioneshwa kuwa ikiwa lengo la vita hii lingekuwa kumaliza utumwa, na Uingereza ingetaka, ingepaswa kuisaidia Kaskazini. Lakini Uingereza inaelewa kabisa hisia zilizopo katika Serikali, na kwamba vita hivi siyo vya kuondoa utumwa, lakini lengo ni kulinda Muungano; na furaha ya Uingereza sio kuhifadhiwa kwa Muungano wa nchi ya Marekani. Serikali yetu imekuwa na majivuno na huru. Watu wa taifa hili wamejiinua hadi mbinguni, na wamezidharau serikali za kifalme, na wamejivunia na kushangilia kujipatia uhuru wao, wakati taasisi ya utumwa, ambayo ilikuwa mbaya na ya kutisha kwa utesaji mara elfu kuliko dhuluma iliyotekelezwa na serikali za kifalme, imeachwa kuwepo, na kuthaminiwa na hata kupendwa. Katika nchi hii ya nuru mfumo unaothaminiwa ambao unaruhusu sehemu moja ya familia ya wanadamu kumiliki wengine kama watumwa imewadhalilisha mamilioni ya wanadamu na kuwafanya wawe sawa na wanyama wa mwituni tu. Dhambi inayofanana na hii kwa ukubwa, haipatikani hata katika nchi za wapagani. {1T 258.2}

Malaika akasema: "Sikieni, enyi Mbingu, kilio cha wanyonge, na kuwalipa wadhalimu maradufu kulingana na matendo yao." Taifa hili bado litanyenyekezwa hadi mavumbini. Uingereza bado inasoma mambo kwakuangalia ikiwa ni bora kuchukua faida ya hali ya udhaifu wa taifa letu, na kujitosa kupigana nasi. Inapima jambo hili, na kujaribu kuongea na mataifa mengine. Inaogopa, ikiwa akianzisha vita nje ya nchi yake, kwamba inaweza kuwa dhaifu nyumbani, na kwamba mataifa mengine yanaweza kutumia udhaifu wake. Mataifa mengine yanafanya maandalizi ya kimya kimya lakini yenye nguvu ya vita, na yanatumai kwamba Uingereza itafanya vita na taifa letu, na hiyo ingeboresha fursa ya kulipizwa kisasi kwake kwa faida waliyochukua hapo zamani na udhalimu uliofanywa nao. Sehemu ya raia wa malkia wanasubiri nafasi nzuri ya kuvunja nira zao (makoloni); lakini ikiwa Uingereza inafikiria italipa kuingia vita, haitasita hata kidogo kuboresha fursa zake za kutumia nguvu zake katika kulinyenyekeza taifa letu. Wakati Uingereza itatangaza vita, mataifa yote yatashugulikiaa hamu yao ya kujipatia vitu wanavyotaka binafsi, na kutakuwa na vita vya jumla, machafuko ya jumla. Uingereza inajua utofauti wa hisia kati ya wale ambao wanatafuta kutuliza uasi. Inajua vizuri hali ya kuchanganyikiwa ya Serikali yetu; imeangalia na kushtushwa na mashtaka ya vita hivi - hatua za polepole, zisizo na ufanisi, kutokuwa na utendaji kwa majeshi yetu, na gharama mbaya za taifa letu. Udhaifu wa Serikali yetu uko wazi kabisa mbele ya mataifa mengine, na sasa wanahitimisha kuwa ni kwa sababu haikuwa serikali ya kifalme, na wanaisifu serikali yao yenyewe ya kifalme, na wanaiangalia Marekani kwa dharau, na wengine wakiwa na huruma kwa nchi yetu, wengine kwa chuki kwa taifa letu ambalo waliliona kama lenye nguvu zaidi duniani. Kama taifa letu lingeendelea kuwa na umoja lingekuwa na nguvu, lakini sasa kwa kuwa limegawanyika, ni lazima lianguke. {1T 259.1}

## SURA YA 54

## DHIKI KUBWA INAKUJA

Niliona dhiki kubwa katika nchi kuliko ile tuliyowahi kushuhudia. Nilisikia miguno ya maumivu, yowe na kilio cha dhiki, na nikaona vikosi vikubwa katika vita. Nikasikia milio mikubwa ya mizinga ya vita, mgongano wa silaha, vita vya mkono uso kwa uso na kuugua maumivu na sala za wale wanaokufa. Ardhi ilifunikwa na wanadamu waliojeruhiwa na wafu. Niliona familia zilizo ukiwa, zenye kukata tamaa, na uhitaji unaobinya nyumba nyingi. Hata sasa familia nyingi zina shida, lakini shida hizi zitaongezeka. Nyuso za wengi zilionekana

kuwa zimechoka, zenye fadhaa, zenye rangi iliyopauka kwa msongo, na zilizobanwa na njaa. {1T 260.1}

Nilioneshwa kuwa watu wa MUNGU wanapaswa kuunganishwa kwa karibu katika vifungo vya ushirika wa Kikristo na Upendo. MUNGU peke yake Ndiye anayeweza kuwa ngao na nguvu yetu katika wakati huu wa majanga yetu ya kitaifa. Watu wa MUNGU wanapaswa kuamka. Fursa zao za kueneza Ukweli zinapaswa kuboreshwa, kwani hazitadumu kwa muda mrefu. Nilioneshwa dhiki na mashaka na njaa katika nchi. Shetani sasa anatafuta kuwashikilia watu wa MUNGU katika hali ya kutofanya kazi, kuwazuia wasitekeleze sehemu yao katika kueneza Ukweli, ili mwishowe wapimwe katika mizani na kuonekana wamepungua (kuanguka kiroho Danieli 5:29). {1T 260.2}

Watu wa MUNGU lazima wachukue onyo kwa busara na kupambanua ishara za nyakati. Ishara za kuja kwa Yesu Kristo ziko wazi kabisa kiasi cha kutotiliwa shaka, na kwa kuzingatia mambo haya kila mtu anayekiri Ukweli anapaswa kuwa Mhubiri Aliye Hai. MUNGU anatoa wito kwa wote, wahubiri na watu, kuamka. Mbingu yote imesisimka. Matukio ya historia ya dunia yanafungwa haraka. Tuko katikati ya maafa ya siku za mwisho. Maafa makubwa yako mbele yetu, na bado hatujazinduka. Ukosefu huu wa utendaji na bidii katika kufuata maelekezo ya MUNGU ni wa kutisha. Usingiz huu wa kifo unatoka kwa Shetani. Yeye hudhibiti akili za Watunza Sabato ambao hawajajitakasa, na huwaongoza kuwaonea wivu wenzao, kutafuta makosa baina yao na kukosoa wengine. Ni kazi yake maalum kugawanya mioyo ili ushawishi, nguvu, na bidii ya Watumishi wa MUNGU iwekwe kati ya Watunza Sabato wasiojitoa wakfu na wakati wao wa thamani ushughulikiwe kwa kumaliza tofauti ndogo-ndogo (magomvi) wakati inapaswa kutumiwa kutangaza Ukweli kwa wasioamini. {1T 260.3}

Nilioneshwa watu wa MUNGU wakisubiri mabadiliko yatokee - nguvu za kupendeza na umakini kuwashikilia kama sumaku. Lakini watakatishwa tamaa, kwani wamekosea. Lazima wachukue hatua, lazima washike kazi hiyo wenyewe na Wamlilie MUNGU kwa bidii ili kupata maarifa ya Kweli juu yao. Matukio ambayo yanapita mbele yetu yana ukubwa wa kutosha kutusababisha kuamka na kusisitiza Ukweli nyumbani kwa mioyo ya wote watakaosikiliza. Mavuno ya dunia yamekaribia kuiva. {1T 261.1}

Nilioneshwa jinsi ilivyo muhimu kwamba wahudumu wanaoshiriki katika kazi nzito ya wakfu, ya uwajibikaji, ya kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu wawe sahihi. MUNGU hashindwi kwa njia au vifaa vya kufanya kazi Yake Mwenyewe. Yeye Anaweza Kuzungumza wakati wowote, na Yeye Amtakaye, na Neno Lake Lina Nguvu na Litatimiza Jambo ambalo MUNGU Mwenyewe Amelikusudia. Lakini ikiwa Ukweli haujatakasa, kusafisha na kuwa safi mikono na moyo wa yule anayehudumu katika vitu vitakatifu, basi ana uwezekano mkubwa wa

kuzungumza kulingana na uzoefu wake usio kamili; na anapozungumza juu yake mwenyewe, kulingana na maamuzi ya hukumu yake mwenyewe yasiyotakaswa, shauri lake sio la MUNGU, bali ni neno lake mwenyewe tu. Kwani yule aliyeitwa na MUNGU anaitwa kuwa mtakatifu, wito wake Mtakatifu na aoneshe katika mazungumzo na mwenendo wake wa mbinguni kuwa yeye ni mwaminifu kwa Yeye Aliyemwita. {1T 261.2}

Kuna ole za kutisha kwa wale wanaohubiri ukweli, lakini hawajatakaswa na Ukweli huo, na pia kwa wale wanaokubali kupokea na kudumisha wale ambao hawajatakaswa kuwahudumia kwa Neno na Mafundisho ya imani. Ninaogopa kwamba watu wa MUNGU wanaokiri kuamini Ukweli muhimu, kwani najua kwamba wengi wao hawajaongoka wala kutakaswa kupitia Kweli hiyo. Watu wanaweza kusikia na kutambua Ukweli wote, na bado hawajui chochote juu ya nguvu ya utauwa. Wote wanaohubiri Ukweli hawataokolewa nao. Malaika akasema: "Jitakaseni, ninyi mnaobeba vyombo vya Bwana." {1T 261.3}

Wakati umefika ambapo wale wanaomchagua MUNGU kuwa sehemu maisha yao ya sasa na ya baadaye Lazima Wamtumaini Yeye Peke Yake. Kila mtu anayedai utauwa lazima awe na uzoefu wa MUNGU Mwenyewe, peke yake. Malaika anaandika rekodi/nakala ya uaminifu ya maneno na matendo ya watu wa MUNGU. Malaika wanaangalia ukuaji wa tabia na kustahiki kimaadili. Wale wanaodai kuamini Ukweli wanapaswa kuwa sahihi wenyewe na kutumia ushawishi wao wote kuwaangazia na kuwavuta wengine kwenye Ukweli. Maneno yao na kazi zao ni mifereji ambayo kupitia hizo kanuni safi za Ukweli na Utakatifu zinawasilishwa kwa ulimwengu. Wao ni chumvi ya dunia na nuru pia. Niliona kuwa kwa kutazama mbinguni tutaona nuru na amani, lakini kwa kuutazama ulimwengu tutaona kwamba kila kimbilio lazima litatukatisha tamaa hivi karibuni na kila jema litapita. Hakuna msaada kwetu ila kwa MUNGU ; katika hali hii ya mkanganyiko wa dunia tunaweza tu kutunzwa na kuwa na amani, kuwa na nguvu, au salama, kwa nguvu ya Imani Hai; wala hatuwezi kuwa na amani, isipokuwa tu tunapumzika kwa MUNGU na kungojea Wokovu Wake. Nuru kubwa inaangaza juu yetu sasa kuliko ilivyoangaza kwa baba zetu. Hatuwezi kukubalika au kuheshimiwa na MUNGU kwa kutoa huduma hiyo hiyo, au kufanya kazi zile zile ambazo baba zetu walifanya. Ili Kukubaliwa na Kubarikiwa na MUNGU kama baba zetu walivyokuwa, lazima tuige Uaminifu, Ari na Bidii Yao, - tuboreshe Nuru yetu kama walivyoiboresha yao, - tufanye kama ambavyo wangefanya ikiwa wangeishi katika siku zetu. Lazima tutembee katika Nuru ambayo inatuangaza, vinginevyo Nuru hiyo itakuwa giza. MUNGU anatutaka sisi tuwe onesho kwa ulimwengu, kwa tabia na matendo yetu, kipimo hicho cha roho ya mshikamano na umoja ambao unalingana na Kweli Takatifu tunazokiri na kwa Roho ya Unabii huo unaotimilika katika siku hizi za mwisho. Ukweli ambao umefikia ufahamu wetu, na Nuru ambayo imeangaza juu

ya roho zetu, itatuhukumu, iwapo tutageuka na kukataa kuongozwa na navyo hivyo viwili. {1T 262.1}

Niseme nini ili kuwazindua watu wa MUNGU waliosalia? Nilioneshwa kuwa matukio ya kutisha yako mbele yetu; Shetani na malaika zake wanaleta nguvu zao zote juu ya watu wa MUNGU. Anajua kwamba ikiwa watalala kidogo kidogo ana uhakika nao wa kuwapata, kwani uharibifu wao ni hakika. Ninawaonya wale wote wanaolitaja Jina la Yesu Kristo kujichunguza kwa karibu na kufanya maungamo kamili na ya kinagaubaga kwa makosa yao yote, ili wanapokwenda mbele kwa hukumu, basi yule malaika anayerekodi taarifa aweze kuandika msamaha kando ya majina yao. Ndugu yangu, dada yangu, ikiwa nyakati hizi za thamani na rehema hazitaboreshwa, utabaki bila visababu vya udhuru. Usipokuwa na matamanio na bidii yoyote ya kuzinduka, ikiwa hautadhihirisha bidii katika kutubu, nyakati hizi za dhahabu zitapita hivi karibuni, nawe utapimwa katika mizani na utaonekana umepungua/umepelea. Halafu kilio chako cha uchungu hakitakuwa na faida yoyote-kitakuwa kazi bure. Ndipo Maneno ya MUNGU yatakapotekelezwa: "Kwa sababu nimeita, nanyi mkakataa; nimenyoosha mkono Wangu, wala hakuna mtu aliyezingatia; lakini mmeyadharau mashauri Yangu yote, wala hamkutaka maonyo Yangu; nitacheka msiba wako, nitacheka wakati hofu yako itakapokuja, wakati hofu yako itakapokuja kama ukiwa, na uharibifu wako utakapokuja kama kimbunga; wakati dhiki na taabu zitakapokujia. Ndipo wataniita, lakini Mimi sitaitika; watanitafuta mapema, lakini hawatanipata, kwa sababu walichukia maarifa, wala hawakuchagua Kumcha MUNGU; hawakukubali shauri Langu, walidharau maonyo Yangu yote, kwa sababu hiyo watakula matunda ya njia zao wenyewe, na watajazwa na hila zao wenyewe, kwa maana kugeuka kwa wajinga kutawaua, na mafanikio ya wapumbavu yatawaangamiza. Lakini kila anisikiae Mimi atakaa salama, na atakuwa mtulivu bila kuogopa mabaya/uovu.” {1T 263.1}

## SURA YA 55

## UTUMWA NA VITA

MUNGU analiadhibu taifa hili kwa uhalifu wa hali ya juu wa utumwa. Yeye Ana hatima ya taifa mikononi Mwake. Atawaadhibu watu wa Kusini ya Marekani kwa dhambi ya utumwa, na Kaskazini kwa muda mrefu akiugua kwa kuvumilia jambo hili na ushawishi wake wa kupita kiasi. {1T 264.1}

Katika Mkutano huko Roosevelt, New York, Agosti 3, 1861, wakati ndugu na dada walipokuwa wamekusanyika katika siku iliyotengwa kwa ajili ya kujinyenyekesha, kufunga, na kuomba, Roho wa Bwana alikaa juu yetu, na nikachukuliwa katika maono na kuoneshwa dhambi ya utumwa, ambayo kwa muda mrefu imekuwa laana kwa taifa hili. Sheria ya mtumwa mtoro ilifanyiwa mahesabu ili kuponda ndani ya mwanadamu kila hisia bora ya ukarimu na huruma ambayo inapaswa kutokea moyoni mwake mtumwa aliyeonewa na anayeteseka. Ilikuwa kinyume kabisa na mafundisho ya Yesu Kristo. Ghadhabu ya MUNGU sasa iko juu ya Kaskazini, kwa sababu hawakuchukua hatua kwa muda mrefu kukomesha biashara ya utumwa. Dhambi ya watu wa Kaskazini kabla ya utumwa ni kubwa. Wameiimarisha Kusini kwa dhambi zao kwa kuidhinisha mfumo wa utumwa; wametenda sehemu kubwa katika kulileta taifa katika hali yake ya sasa ya shida. {1T 264.2}

Nilioneshwa kuwa wengi hawatambui kiwango cha uovu ambao umetupata. Wamejipongeza kwa udanganyifu kwamba shida za taifa zitamalizwa hivi karibuni na mkanganyiko na vita vitaisha, lakini wote watashawishika kuwa kuna uhalisia/ukweli zaidi katika jambo kuliko ilivyotarajiwa. Wengi wameiangalia Kaskazini kutoa pigo ambalo litaenda kumaliza malumbano. {1T 264.3}

Nilielekezwa kwa Israeli ya zamani, iliyoshikiliwa utumwani na Wamisri. Bwana alifanya kazi kuwatumia Musa na Haruni kuwaokoa wana wa Israeli. Miujiza ilifanywa mbele ya Farao kwa kumsadikisha kwamba hawa watu walikuwa wametumwa na MUNGU kumwamuru awaachie Israeli waende. Lakini moyo wa Farao ulikuwa mgumu dhidi ya Wajumbe wa MUNGU, na alihoji miujiza iliyofanywa nao. Kisha Wamisri walifanywa kuhisi hukumu za MUNGU. Walitembelewa na mapigo, na wakati walipokuwa wakiteseka kwa haya mapigo, Farao alikubali kuwaachilia Israeli waende. Lakini mara tu sababu ya mateso yao ilipoondolewa, moyo wake ukawa mgumu. Washauri wake na watu mashujaa walijiimarisha dhidi ya MUNGU na walijitahidi kuyaelezea mapigo kama matokeo ya sababu za asili. Kila kutembelewa na pigo la MUNGU lilikuwa kali zaidi kuliko lile lililopita, lakini hakuwaruhusu watoto wa Israeli waende hadi malaika wa Bwana alipomwua mzaliwa wa kwanza wa Wamisri. Kuanzia mfalme juu ya kiti cha enzi hadi mnyenyekevu na mnyonge kabisa, kulikuwa na kilio na maombolezo. Ndipo Farao akaamuru wana wa Israeli waondoke; lakini baada ya Wamisri kuzika wafu wao, alijuta kwamba alikuwa amewaacha Israeli waende. Washauri wake na watu mashujaa walijaribu kutoa hesabu ya kufiwa kwao. Waligoma kukubali kwamba mapigo au hukumu ilitoka kwa MUNGU, na kwa hivyo wakawafuatilia nyuma wana wa Israeli. {1T 264.4}

Wakati Waisraeli walipoona jeshi la Wamisri likiwafuata, wengine wakiwa wamepanda farasi na wengine wakiwa kwenye magari, na wamejiandaa kwa vita, mioyo yao ilipondeka-pondeka nyanganyanga. Bahari Nyekundu ilikuwa mbele yao Wana wa Israeli na kisha jeshi la Wamisri lilikuwa nyuma yao. Hawakuona njia ya kutorokea. Kelele ya ushindi ilirindima kutoka kwa Wamisri walipoona wamewapata Waisraeli na ya kuwa hawakuwa na namna ya kujiokoa katoka mikononi mwo, na hivyo wapo chini ya mamlaka yao. Waisraeli walipata utisho mkubwa. Lakini MUNGU alimwagiza Musa kuwaamuru wasonge mbele, na anyanyue fimbo na kunyoosha mkono wake juu ya bahari na kuigawanya. Alifanya hivyo, na tazama, bahari iligawanyika, na wana wa Israeli wakapita kama kwenye nchi kavu. Kwa muda mrefu Farao alikuwa amempinga MUNGU, na akaufanya moyo wake kuwa mgumu dhidi ya kazi Zake za ajabu, na zenye ukuu mno kupata kutokea, kiasi kwamba kwa upofu alikimbilia njia ambayo MUNGU alikuwa amewaandalia watu Wake Israeli kimiujiza. Musa aliamriwa tena anyoshe mkono wake juu ya bahari, yake," na maji yakafunika jeshi la Wamisri, nao wakazama. {1T 265.1}

Eneo hili liliwasilishwa mbele yangu kuonesha upendo wa ubinafsi wa kumiliki atumwa, na hatua za kukata tamaa ambazo Kusini ingechukua kuthamini taasisi hiyo ya utumwa, na kina cha kusikitisha ambacho wangekwenda kabla hawajajisalimisha. Mfumo wa utumwa umempunguza na kumdhalilisha mwanadamu hadi kiwango cha kuwa kama wanyama wa mwituni, na wengi wa mabwana wa watumwa hawa wanawaona hivyo. Dhamiri za mabwana hawa zimechomwa na kuwa ngumu, kama ilivyokuwa kwa Farao; na ikiwa wanalazimishwa kuwaachilia watumwa wao, kanuni zao hazibadiliki, na wangemfanya mtumwa ahisi nguvu yao ya uonevu kama ikiwezekana. Ilionekana kwangu kama haiwezekani sasa kwa utumwa kukomeshwa. Mwenyezi MUNGU peke yake Ndiye anayeweza kumkamua kwa nguvu mtumwa na kuipindisha mikono kwa nguvu na kisha mtumwa atoke kwa mkandamizaji wake aliyekata tamaa (anayehaha), na asiye na huruma. Unyanyasaji na ukatili wote unaofanywa kwa mtumwa unatuhumiwa sawa kwa wahusika wanaoustawisha mfumo wa watumwa, iwe ni watu wa Kusini ya Amerika au Kaskazini ya Amerika.{1T 266.1}

Kaskazini na Kusini ziliwasilishwa mbele yangu. Kaskazini wamedanganywa kuhusu Kusini. Wana stadi mahiri za vita kuliko ambavyo imewakilishwa. Wengi wa watu wao wana stadi mahiri katika utumiaji wa silaha, wengine wao kutokana na uzoefu wa vita, na wengine kutokana na mazoea ya michezo ambayo ina mbinu za vita ndani yake (Mfano American football). Wako mbele kiufundi kuliko wale wa Kaskazini katika suala hili, lakini sio kama jambo la jumla, la ushujaa na nguvu ya uvumilivu ambayo watu wa Kaskazini wanayo. {1T 266.2}

Niliona vita vya kutisha huko Manassas, Virginia. Ililikuwa eneo la kusisimua zaidi, lenye kufadhaisha. Jeshi la Kusini lilikuwa na kila kitu kwa niaba yao na walikuwa tayari kwa mashindano ya kutisha. Jeshi la Kaskazini lilikuwa linasonga mbele kwa ushindi, wakiwa hawana shaka kwamba watashinda. Wengi walikuwa wazembe, na wasiojali, na kisha walisonga mbele kwa majivuno, kana kwamba ushindi tayari ulikuwa wao. Walipokaribia uwanja wa vita, wengi walikuwa karibu kuzimia kwa uchovu, kuburudishwa na kukosa maji. Hawakutarajia kukutana na upinzani mkali kutoka Kusini. Wao Kusini walikimbilia vitani na wakapigana kwa ushujaa sana. Wafu na majeruhi waliokuwa wanachungulia kaburini walikuwa kila upande. Wote Kaskazini na Kusini walipata hasara kubwa sana. Watu Kusini walihisi vita, na kwa muda kidogo wangekuwa wanarudishwa nyuma zaidi. Watu wa Kaskazini walikuwa wakiindea vita kwa mbio, ingawa uharibifu wao ulikuwa mkubwa sana. Wakati huo malaika alishuka na kupunga mkono wake nyuma. Mara kukawa na mkanganyiko katika safu. Ilionekana kwa watu wa Kaskazini kwamba vikosi vyao vilikuwa vikirudi nyuma, wakati haikuwa hivyo kwa kweli, na ndipo kurudi nyuma kwa kasi kulianza. Hali hii ilionekana kuwa nzuri kwangu. {1T 266.3}

Ndipo ikaelezwa kwamba MUNGU alikuwa na taifa hili mkononi mwake, na asingeruhusu ushindi upatikane haraka kuliko alivyopanga, na asingeruhusu hasara zaidi kwa watu wa kaskazini kupita vile hekima Yake ilivyoona vyema, kuwaadhibu kwa dhambi zao. Na kama jeshi la kaskazini wakati huu lingeendelea na vita zaidi katika hali yao ya kuzimia, na ya kuishiwa nguvu, mapambano na uharibifu mkubwa uliowasubiri ungeleta ushindi mkubwa kwa Kusini. MUNG hakuruhusu jambo hili, na akatuma malaika kuingilia kati. Kuanguka ghafla kwa vikosi vya Kaskazini ni fumbo/siri na kitendawili kwa wote. Hawakujua kuwa mkono wa MUNGU ulikuwa katika jambo hilo. {1T 267.1}

Uangamivu wa jeshi la Kusini ulikuwa mkubwa sana hivi kwamba hawakuwa na moyo wa kujivuna. Mwonekano wa watu waliokufa, na waliokuwa wanakufa, na waliojeruhiwa viliwapatia ujasiri kidogo sana wa ushindi. Uangamivu huu, unaotokea wakati wakiwa na kila upendeleo, na wale wa Kaskazni wakiwa wakiwa hawana upendeleo, vilisababisha Kusini kuwa na kuchanganyikiwa kukubwa. Walijua kwamba kama Kaskazini ingekuwa na fursa sawa na zao, ni wazi ushindi ungekuwa wa Kaskazini. Tumaini lao pekee ni kuchukua nafasi zilizo ngumu kufikiwa, na kisha kuwa na mipango ya kutisha ya kuvurumisha uangamivu kila upande. {1T 267.2}

Watu wa kusini walijiimarisha sana tangu uasi wao ulipotokea kwanza. Kama hatua mathubuti zingechukuliwa na watu wa kaskazini, uasi huu ungezimwa haraka. Lakini kile kilichoonekana kidogo mwanzoni kiliongezeka kwa nguvu na kwa idadi hadi kikawa chenye nguvu zaidi. Mataifa mengine yalikuwa

yanaliangalia sana taifa hili, kwa sababu ambazo sikuweza kujulishwa, nao walikuwa wanafanya maandalizi makubwa kwa ajili ya tukio fulani. Shaka na fadhaa, na mkanganyiko mkubwa sasa ulikuwa kati ya watu wa taifa letu. Watu wanaopenda kumiliki watu na wasaliti walikuwa miongoni mwao; na wakati watu hawa wakijidai kuunga mkono Muungano, walikuwa na ushawishi wa kufanya maamuzi, na baadhi ya maamuzi hayo; yalikuwa yakiipendelea Kusini. {1T 267.3}

Nilioneshwa wakazi wa dunia wakiwa katika kuchaganyikiwa kukubwa. Vita, umwagaji wa damu, ufukara, uhitaji, njaa, na tauni vilitapakaa nchi yote. Wakati mambo haya yakiwazingira watu wa MUNGU, walianza kujongeleana pamoja kwa umoja, na kutupilia mbali shida zao ndogo. Hali ya kujijali wenyewe, na kulinda hadhi zao haikuwatawala tena; na badala yake unyenyekevu wa kina ulichukua nafasi yake. Mateso, kuchanganyikiwa, na ufukara vilisababisha akili yenye hekima kuanza tena kukaa kwenye kiti CHAKE cha enzi, na yule mtu mwenye shauku na asiye na busara akapata tena akili timamu, na akafanya kwa kupima mambo kwa busara na hekima. {1T 268.1}

Usikivu wangu ulivutwa utoke kwenye eneo la tukio. Kulionekana kuwa na wakati mdogo wa amani. Kwa mara nyingine tena wakazi wa dunia waliwasilishwa mbele yangu; na kwa mara nyingine kila kitu kilikuwa katika machafuko makubwa. Mizozo, vita, na umwagaji damu, na njaa na tauni, vilikuwa vimepamba moto kila mahali. Mataifa mengine yalikuwa yakishiriki katika vita hivi na machafuko. Vita vilisababisha njaa. Uhitaji na umwagaji damu vilisababisha tauni. Na ndipo mioyo ya wanadamu ilishindwa kwa woga, "na kwa kutazamia mambo yatakayoupata ulimwengu." {1T 268.2}

## SURA YA 56

## NYAKATI ZA HATARI

Ulimwengu usioamini hivi punde utakuwa na kitu cha kuzingatia kando ya mavazi na mwonekano; na kwa kuwa nia zao zimeraruliwa kutokana na mambo

haya kwa dhiki na kuchanganyikiwa na hawatakuwa na kitu cha kugeukia. Wao siyo wafungwa wa tumaini na ndiyo maana hawaigeukii ngome -Zekaria 9:12-13. Mioyo yao itavunjika kwa kutoridhika, kuudhika, hofu na marudi. Hawakumfanya MUNGU kuwa kimbilio lao, naye hatakuwa faraja yao wakati huo, bali atawang'ong'a/atacheka kwenye angamizo lao na atawadhihaki wakati hofu yao iwajiapo. Walidharau na kukanyaga Kweli ya Neno la MUNGU. Walijiingiza kwenye matumizi ya mavazi ya kupindukia, na walitumia maisha yao kwenye furaha na anasa. Walipanda upepo, wakavuna tufani. Katika nyakati za dhiki na kuchanganyikiwa kwa mataifa kutakuwa na wengi ambao hawakujitoa kikamilifu kwa mivuto potofu ya ulimwengu na kazi za shetani, ambao watajinyenyekeza kwa MUNGU  na kumrejea kwa mioyo yao yote na kupata ukubali na msamaha {1T 268.3}

Miongoni mwa Watunza Sabato ambao hawakuwa tayari kutoa dhabihu lakini ambao wamejisalimisha kwa mvuto wa ulimwengu, watapaswa kujaribiwa na kuthibitishwa. Hatari za siku za mwisho zi juu yetu na jaribu ambalo hawakulitarajia liko mbele ya vijana. Wanapaswa kuingia kwenye dhiki kuu na mashaka ya kufadhaisha. Uhalisia wa imani yao utapimwa. Wanakiri kutazamia kuja kwa Mwana wa Adam, wakati miongoni mwao wamekuwa mfano mbaya kwa wasio waamimi. Hawapo tayari kuuacha ulimwengu, bali wameungana nao, wamehudhuria pikniki na mikusanyiko mingine ya anasa, wakijifariji kuwa wanajihusisha na maburudisho yasiyo na hatia. Hata hivyo nilioneshwa kwamba kujistarehesha, na kujiendekeza tu ndiko kunawatenganisha na MUNGU na kuwafanya wawe wana wa ulimwengu. MUNGU hamiliki watafuta starehe miongoni mwa wafuasi Wake. Yeye hajatupatia mfano kama huo. Wale tu wanaojikana nafsi na wanaoishi maisha ya kiasi, unyenyekevu na utakatifu ndiyo wafuasi wa kweli wa Yesu; na hawawezi kushiriki na kufurahia, ujinga, mazungumzo yenye utupu na mazungumzo ya kipuuzi ya wapenda ulimwengu {1T 269.1}

Siku ya uchungu unaopasua moyo iko mbele yetu. Nilioneshwa kwamba shuhuda zilizonyooka, zilizo dhahiri zinapaswa kutolewa, na kwamba wale watakaokuja kwa ajili ya msaada wa Bwana watapokea baraka Yake. Watunza Sabato wanayo kazi ya kufanya. Nilioneshwa kuwa uvaaji wa sketi za hoops ni chukizo (angalia sura ya 52 sketi hizi), na kila ushawishi wa Mtunza Sabato unapaswa kukaripia fasheni hii ya vituko, vichekesho na kijinga, uliotokea katika nyumba yenye umaarufu mbaya huko Paris, na ambao umekuwa kiambaza cha uovu. Nilioneshwa wale ambao wangedharau mafundisho hata kama yangekuwa yanatoka mbinguni; kwamba wangeunda visingizio fulani ili kuepuka shuhuda iliyo wazi zaidi na kukaidi nuru yote iliyotolewa kwa kuvaa sketi za hoops kwa sababu ndiyo mtindo na kuwa tayari kwa matokeo yoyote ya hatari (angalia sketi za hoops za  miaka ya 1800 mtandaoni). {1T 269.2}

Unabii wa Isaya 3 uliwasilishwa mbele yangu ukionesha siku hizi za mwisho, na maonyo yanayotolewa kwa binti za Sayuni ambao kitu pekee wanachofikiria ni juu ya mwonekano na maonesho. Soma mstari wa 25 “watu wako waume wataanguka kwa upanga, na mashujaa wako vitani” Nilioneshwa kuwa Andiko hili kuwa halijatimizwa kabisa. Vijana wa kiume na wa kike wanaodai kuwa Wakristo, na bado hawana uzoefu wa Kikristo na hawajabeba mizigo yoyote na hawahisi jukumu binafsi, lazima wapimwe/wathibithishwe. Watashushwa chini kwenye mavumbi na watatamani uzoefu katika mambo ya MUNGU ambao wameshindwa kuupata. {1T 270.1}

Vita huinua chapeo yake juu ya paji la uso wake; Ee MUNGU, walinde watu wako sasa. {1T 270.2}

## SURA YA 57

## MUUNDO-KUPANGA KANISA ILI IWE TAASISI

(ORGANIZATION OF THE CHURCH)

Agosti 3, 1861, nilioneshwa kuwa wengine wameogopa kwamba makanisa yetu yatakuwa Babeli ikiwa wangeunda taasisi na kuyapanga (organization), lakini wale walio New York ya kati wamekuwa Babeli kamili, yaani machafuko. Na kwa sasa ikiwa makanisa hayatajipanga vizuri na kuweza kufuata utaratibu (organized), hayana chochote cha kutarajia katika siku za usoni; lazima yagawanyike katika vikundi-vikundi. Mafundisho yaliyopita yamestawisha viashiria vya utengano. Roho imekuwa imara kusimama na kutazama, kujihami na kukemea badala ya kujenga. Kama watendakazi wa MUNGU wangeungana kwa umoja wakashika nafsi zao, na kuudumisha, kungekuwa na ushawishi unaounganisha kundi la MUNGU. Kuta za utengano zingevunjwa vipande vipande. Mioyo ingemiminika na kukusanyika pamoja na kuungana kama matone ya maji, hivyo kungekuwa na nguvu na uwezo miongoni mwa jeshi la watunza Sabato, zaidi ya chochote ambacho tumewahi kukishuhudia. {1T 270.3}

Mioyo ya watendakazi wa MUNGU inasikitishwa wanaposafiri kutoka kanisa moja kwenda lingine, kwa kukutana na ushawishi wa ukinzani wa ndugu wengine wanaohudumu. Wapo ambao wamesimama tayari kupinga kila hatua ya awali ambayo watu wa MUNGU wameichukua kusonga mbele. Mioyo ya wale ambao wamethubutu kujitokeza imesikitishwa na kuzuiliwa kwa ukosefu wa ushirikiano wa kivitendo kwa watendakazi wenzao. Tunaishi katika kipindi kizito ambacho Shetani na malaika zake waovu wanafanya kazi kwa nguvu kubwa huku ulimwengu ukiwa upande wao, kuwasaidia. Na wale wanaojidai kuwa ni watunza Sabato na kuuamini Ukweli adhimu, huunganisha umoja wao na ushawishi wa pamoja wa nguvu za giza kuvuruga na kubomoa kile ambacho MUNGU amepanga kukijenga. Ushawishi wa watu kama hao, umerekodiwa kama wa wale wanarudisha nyuma maendeleo ya matengenezo miongoni mwa watu wa MUNGU {1T 271.1}

Kutibuatibua suala hili la kupanga taasisi ya kanisa kumeonesha ukosefu mkubwa wa ujasiri wa kimaadili hasa kwa upande wa mhudumu/mchungaji atangazaye Ukweli wa leo. Wengine ambao walikuwa wanaamini kuwa kupanga muundo au kuanzisha taasisi (organization) ilikuwa sahihi, wameshindwa kusimama kwa ujasiri na kutetea hoja hii. Wanafahamisha wachache tu, kuelewa kuwa waliunga mkono jambo hili. Je! hivi ndivyo ambayo MUNGU aliwataka wafanye? Hapana. Yeye Hakufurahishwa na ukimya wao wenye woga na kukosa ujasiri, na hata kutokuwajibika kwao. Waliogopa lawama na upinzani. Waliwatazama ndugu kwa ujumla kuona jinsi mtazamo na utayari wao ulivyo kabla ya kusimama kidete kwa kile walichokiamini kuwa ni sahihi. Watu walisubiri sauti ya wachungaji wawapendao na kwa sababu hawa washiriki hawakuweza kusikia mrejesho wowote kutoka kwao uliopendelea jambo hili, waliamua kuwa kupanga kanisa kama taasisi haikuwa sawa, kwamba kulikuwa na kasoro kufanya hivyo. {1T 271.2}

Hivyo mvuto wa baadhi ya wachungaji ulikuwa kinyume na kupanga kanisa kama taasisi au shirika (organization), na huku wakidai kuukabali. Kwa hakika waliogopa kupoteza mvuto wao. Lakini mtu sharti aamue na kuwajibika na atumie mvuto wake, na kwa kuwa aliyefanya hivi amepewa uwezo wa kukaripia na kuonya anavumilia kuyabeba haya. Watendakazi wenzake wanaopaswa kusimama pamoja naye na kubeba sehemu ya mzigo, hawafanyi lolote na badala yake wanatazama kuona namna atakavyofanikiwa kuvipiga vita peke yake. Lakini MUNGU anajua dhiki yake, uchungu wake, machozi yake, kukata tamaa na kufadhaika wakati akili yake imenyumbulishwa kwa mzigo mzito unaoshindikana kuvumilika, na anapokuwa tayari kuzama, MUNGU humwinua, na kumwelekeza kwenye pumziko kwa wale waliochoka, na humpatia thawabu ya waaminifu na kisha humwekea tena mtu huyu mzigo mzito mabegani mwake. Niliona kuwa wote watalipwa kulingana na kazi zao zilivyo. Wale ambao wanaepa majukumu watakutana na hasara mwishoni. Muda kwa wachungaji kushirikiana kwa pamoja, ni wakati ambapo vita imekuwa ngumu {1T 271.3}

( Kwa Kingereza cha kisasa hii Ibara itasomeka hivi *Some ministers, while publicly supporting organization, actually worked against it because they feared losing their own power. Someone had to take the lead, accept the responsibility, and risk their influence. Once that person became accustomed to criticism and blame, others allowed him to carry the burden alone. His fellow ministers, who should have supported him and shared the workload, instead watched from the sidelines to see if he would succeed. But God sees this leader's distress, anguish, tears, discouragement, and despair as his mind is stretched almost to its breaking point. When he's about to collapse, God lifts him up, reminds him of the rest promised to the weary and the reward for the faithful, and gives him the strength to carry on. I saw that everyone will be rewarded according to their deeds. Those who avoid responsibility will ultimately suffer loss. Ministers should stand together, especially during difficult times. 1T 271.3

Kingereza cha zamani

Thus the influence of some of the ministers was against organization, while they professed to be in favor of it. They were afraid of losing their influence. But someone must move out and bear responsibility, and venture his influence; and as the one who has done this has become inured to censure and blame, he is suffered to bear it. His fellow laborers, who should stand by his side and take their share of the burden, are looking on to see how he succeeds in fighting the battle alone. But God marks his distress, his anguish, his tears, his discouragement and despair, while his mind is taxed almost beyond endurance; and when ready to sink, God lifts him up and points him to the rest for the weary, the reward for the faithful; and again he puts his shoulder under the heavy burden. I saw that all will be rewarded as their works shall be. Those who shun responsibility will meet with loss in the end. The time for ministers to stand together is when the battle goes hard. 1T 271.3

Tafsiri ya maisha ya sasa

*Baadhi ya wachungaji, huku wakiunga mkono shirika au taasisi ambayo imepangwa hadharani, kwa hakika walifanya kazi dhidi yake kwa sababu waliogopa kupoteza mamlaka yao wenyewe. Hata hivyo ili kusonga mbele, iibidi mtu fulani aongoze, akubali daraka hilo, na kuhatarisha mvuto wake. Mara tu mtu huyo alipozoea kukosolewa na kulaumiwa, wengine walimruhusu kubeba mzigo huo peke yake. Wachungaji wenzake ambao walipaswa kumuunga mkono na kugawana kazi, badala yake walitazama pembeni kuona iwapo atafanikiwa au atashindwa na kuanguka. Lakini Mungu anaona dhiki, uchungu, machozi ya kiongozi huyu, kukata tamaa, na kuvunjwa moyo huku akili yake ikinyumbulishwa karibu kufikia hatua yake ya kuvunjika. Pale anapokaribia kuanguka, Mungu humwinua, na anamkumbusha yale mengine yaliyoahidiwa kwa waliochoka na thawabu kwa waaminifu, na kumpa nguvu za kuendelea. Nikaona kwamba kila mtu atalipwa sawasawa na matendo yake. Wale wanaoepuka kuwajibika hatimaye watapata hasara. Wachungaji wanapaswa kusimama pamoja, hasa nyakati ngumu. 1T 271.3

## SURA YA 58

## WAJIBU KWA MASIKINI NA WAHITAJI

Mara nyingi changamoto hujitokeza kuhusiana na wajibu wetu kwa wahitaji wanaoukubali ujumbe wa tatu, na sisi wenyewe kwa kipindi kirefu tumekuwa na mashaka juu ya namna ya kushughulikia kwa busara mambo yahusuyo familia maskini ambazo zinaitunza Sabato. Hata hivyo tukiwa Roosevelt, New York, Agosti 3,1861 nilioneshwa vitu kadhaa kuhusu wahitaji-watu masikini {1T 272.1}

MUNGU hahitaji ndugu zetu kuchukua jukumu kwa kila familia maskini ambayo itakubali ujumbe huu. Ikiwa watafanya hivyo wachungaji/watendakazi itabidi waache kuingia maeneo mapya, kwani hazina haitatosha. Wengi ni wahitaji kutokana na kutokuwa na bidii kwao, na kutozingatia masuala ya uchumi, hawajui namna ya kutumia mali vizuri. Kama wangesaidiwa, ingewaumiza. Wengine daima watakuwa maskini. Hata ikiwa watapata manufaa mazuri, kesi zao hazitasaidiwa. Hawana mahesabu mazuri na wangeweza kutumia mali zote wanazopata, ikiwa ni nyingi au chache. Wengine hawajui chochote kuhusu kujinyima, kujikana nafsi na kujiwekea akiba, kubana matumizi ili kujiepusha na deni, na kuwa na akiba mbeleni wakati wa uhitaji. Ikiwa kanisa lingewasaidia watu kama hao badala ya kuwaacha wategemee vyanzo vyao wenyewe, ingewaumiza hatimaye, kwani wangelitazama kanisa na wangetarajia kupokea msaada kutoka kwao bila kujifunza kujinyima, kujikana nafsi na kuwa na uchumi mzuri, hasa wanapokuwa wamepewa mahitaji kamili. Ikiwa hawapati usaidizi kila wakati, Shetani huwajaribu, hivyo huwa na wivu na kuwa nyeti na makini sana na ndugu zao, wakihofu kushindwa kufanyiwa wajibu

wao wote. Kosa lipo kwao wenyewe, wanadanganywa, wao siyo masikini wa Bwana. [1T 272.2]

Maagizo yaliyotolewa na neno la MUNGU  juu ya kusaidia wenye uhitaji hayagusi shida kama hizo isipokuwa wale waliopatwa bahati mbaya kwa majanga, na watu wanaoteseka-magonjwa nk. MUNGU katika uongozi Wake aliwaacha watu wataabike, ili awajaribu na kuwathibitisha wengine. Wajane na wagonjwa wapo kanisani kuthibitisha baraka kwa kanisa. Ni sehemu ya njia ambayo MUNGU  ameichagua kukuza tabia ya Kweli ya wanafunzi wa Kristo, wanaodai kuwa wafunzi Wake, na kuishi tabia ya thamani iliyooneshwa na mkombozi wetu Mwenye huruma. [1T 273.1]

Wengine ambao wanaweza kuishi na kufanya bidii tu wakiwa waseja, huchagua kuoa na kukuza familia wakati wanajua hawana kitu cha kuwasaidia, na mbaya zaidi kuliko hii, hawana uwezo wa kuiongoza familia. Mwelekeo wao wote katika familia yao umetambuliwa kwa ulegevu na tabia za uvivu. Wana udhibiti mdogo juu yao wenyewe, na wana mihemko, ila hawana subira na ni wenye kuudhika-udhika kirahisi. Wakati watu hawa wanapokubali ujumbe, wanahisi kuwa wana haki ya kusaidiwa na ndugu zao matajiri zaidi, na ikiwa mahitaji yao hayakukidhiwa wanalilalamikia kanisa na kuwashutumu kwamba hawaiishi imani yao: Nani wa kuumia katika tatizo hili basi? Je! kazi ya MUNGU inapaswa kudhoofika na hata kuharibika, na hazina katika maeneo tofauti ipungue kwa kuzitunza familia hizi kubwa zenye uhitaji? Hapana. Wazazi lazima wawe wawajibikaji. Kwa ujumla hawatakuwa na upungufu mkubwa baada ya kuitunza Sabato kuliko walivyokuwa hapo awali [1T 273.2]

Kuna uovu miongoni mwa masikini/wahitaji ambao kwa hakika utathibitisha uharibifu wao wasipoushinda. Wameukubali Ukweli wakiwa na tabia zao mbaya, rafu, na tabia zisizoboreshwa na kukuzwa vizuri, (kukosa maboresho ya nidhamu na elimu)  na inachukua muda kwao kuona na kung’amua ukorofi wao, na kwamba haulingani na tabia ya Kristo. Wanawatazama wengine ambao wana mipangilio mizuri zaidi, na safi zaidi yao kama ni wenye majivuno na utawasikia wakisema “Ukweli hutuleta wote chini kwenye kiwango sawa”, lakini ni kosa kubwa kufikiri kuwaKweli humshusha mtu chini. Ukweli humwinua mtu juu, husafisha ladha yake, husafisha mapenzi yake, humtakasa maamuzi yake, na akiuishi, Ukweli utamfanya afae kila wakati kwenye jamii ya malaika watakatifu katika mji wa MUNGU. Ukweli upo kutuleta sote kwenye kiwango. {IT 274.1}

Wenye uwezo zaidi wanapaswa kutenda kama waungwana, watu bora ma wakarimu katika kushughulika na ndugu zao wahitaji, walio masikini zaidi, pia wanapaswa kuwapa ushauri mzuri kisha kuwaacha wapigane vita ya maisha.

Lakini nilioneshwa kuwa jukumu zito kabisa liko juu ya kanisa, kuwa na uangalizi maalum kwa wajane wahitaji, yatima na walemavu. [1T 274.2]

## SURA YA 59

## NGUVU YA MFANO

Katika waraka wa Paulo kwa Tito, sura 2:13, 14, tunasoma: “Tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, MUNGU mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi Yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki Yake Mwenyewe, wale walio na ari na juhudi katika matendo mema.” Kazi hii kubwa inapaswa kufanywa na wale tu walio tayari kusafishwa, walio tayari kuwa wa kipekee, na ambao wanaonesha bidii katika kazi njema. Ni wengi kiasi gani wanasinyaa na kutoroka kutoka kwenye mchakato wa utakaso! Hawako tayari kuuishi Ukweli, hawataki kuonekana kuwa wati wa kipekee machoni pa ulimwengu. Ni kule kujichanganya kwetu na ulimwengu ndiko kunakoharibu hali yetu ya kiroho, usafi, usongo na juhudi. Nguvu ya Shetani hutumika kila wakati kupumbaza hisia za watu wa MUNGU, ili dhamiri zao zisiweze kuhisi ubaya, na kwamba ishara ya utofauti kati yao na ulimwengu inaweza kuharibiwa. {1T 274.3}

Mara nyingi nimekuwa nikipokea barua zinazouliza juu ya mavazi, na baadhi hawajaelewa vema yale niliyoandika. Kundi hasa lililowasilishwa mbele yangu likidaiwa kuiga mitindo ya ulimwengu limekuwa likikua polepole sana, na ni la mwisho, kuongolewa au kurekebishwa. Kundi lingine lililokosa ladha na utaratibu katika mavazi limechukua faida na fursa ya yale niliyoandika na wakaenda mbali kwa kupitiliza mpaka upande mwingine kabisa; wakijifikiria kwamba wao hawana kiburi, wakawachukulia wale wanaovaa kwa unadhifu na mipango ni kama watu wanaojivuna. Kuvaa kwa ajabu-jabuma bila kujali au utaratibu kumechukuliwa na baadhi kama tabia njema. Hiyo huchukua mwenendo ambao huharibu ushawishi wao juu ya watu wasioamini. Wanawachukiza wale ambao wangeweza kunufaika (kwa kufikiwa na injili au mashauri). {1T 275.1}

Wakati ambapo maono yamekemea kiburi na uigaji wa mitindo ya ulimwengu, yamekemea pia wale ambao walikuwa wazembe na wasiojali kuhusiana na

mavazi yao na waliokosa usafi wa mwili na mavazi. Kwa namna ya upekee nimeoneshwa kuwa wale wanaodai kuwa na Ukweli wa leo wanapaswa kuwa na uangalifu maalum namna wanavyotokea mbele za MUNGU siku ya Sabato kwa namna ambayo itaonesha kwamba wanamheshimu Muumbaji ambaye ametakasa na kuweka heshima maalum siku hiyo. Wote ambao wanaiheshimu Sabato wanapaswa kuwa safi wao wenyewe binafsi, na nadhifu katika mavazi; wanapotokea mbele za MUNGU Mwenye wivu, ambaye hukerwa na uchafu na machafuko, na ambaye huweka alama ya kila ishara ya kukosa heshima. Wengine wamefikiria ni vibaya kuvaa chochote vichwani mwao isipokuwa kofia ambayo ni kama kilemba cha jua (sunbonnet). Hao wanaenda mbali sana na kupitiliza. Kuvaa kwa unadhifu, usafi au kofia ya mkeka au hariri isiyo na mapambo haiwezi kuitwa kiburi. Imani yetu ikiwa imefuatwa, itatufanya sisi tuwe watu wenye mavazi sahili, yasiyo na mapambo, na wenye bidii ya matendo mema, na hivyo tutatambulika kama watu wa kipekee. Lakini tunapopoteza ladha ya mpangilio na unadhifu katika mavazi tunaachana na Ukweli, kwani Ukweli haushushi kamwe, bali huinua. Wasioamini huwatazama Watunza Sabato – kama watu duni, na wanapopuuzia mavazi yao, na kuwa wachafu, wakorofi, rafu katika tabia/hulka zao, na wabaya katika tabia zao, ushawishi wao unawaimarisha wasioamini katika hitimisho hili. {1T 275.2}

Wale wanaodai kuwa Wakristo katikati ya hatari za siku za mwisho, na hawaigi Mfano wa unyenyekevu, wa kujikana nafsi, hujiweka katika safu ya adui. Shetani anawaona watu hawa kama raia wake, na hutumika katika kusudi muhimu kwake, kama walivyo wafuasi wake wowote, kwani wana jina la kuwa hai, lakini wamekufa. Watu wengine huwachukulia hawa kama mfano, na kwa kuwafuata wanapoteza mbingu, wakati, ambapo kama wasingedai kuwa Wakristo, mfano wao usingefuatwa. Watu hawa wanaokiri kwa mdomo bila ya kujitoa wakfu hawajui uzito wa ushawishi wao. Wanalifanya pambano kuwa kali zaidi kwa wale ambao wangekuwa watu wa kipekee wa MUNGU. Paulo, katika Tito 2:15, anawataja watu hawa ambao wanangoja kuonekana kwa Kristo. Anasema: “Nena Maneno hayo, onya na kukaripia kwa mamlaka yote; asikudharau mtu awaye yote.” {1T 276.1}

Tunapokuwa tunatoa ushuhuda dhidi ya kiburi na kufuata mitindo ya ulimwengu, tunakutana na visingizio na kujihesabia haki. Wengine huiga mfano wa wengine. Dada kama huyu huvaa hoops yaani sketi au gauni ndefu zinazobana nyonga; ikiwa ni makosa kwangu kuvaa, ni makosa kwake pia. Watoto huiga mfano wa watoto wengine, ambao wazazi wao ni Watunza Sabato. Ndugu A ni shemasi wa kanisa. Watoto wake huvaa gauni hizi za hoops, na kwa nini ni vibaya zaidi kwangu kuvaa kuliko ilivyo kwao? Wale ambao kwa mfano wao huwapa wale Wakristo wasiojiweka wakfu na wanaomkiri Mungu kwa mdomo tu, hoja au mabishano dhidi ya wale watakaokuwa wa kipekee, wanaweka kikwazo katika njia ya wale walio wanyonge; na ni lazima watoe

hesabu kwa MUNGU kwa mfano wanaouonesha. Mara nyingi mimi huulizwa: "Je! Unafikiria nini juu ya sketi na gauni hizi za hoops?" Ninajibu: Nimekupatia nuru niliyopewa. Nilioneshwa kuwa hizi nguo za hoops ndefu zinazobana nyonga ni aibu, na kwamba hatupaswi kuwa na mwonekano hata mdogo wa mitindo inayowapeleka watu kuwa kituko kwa urefu mkubwa namna hiyo. {1T 276.2}

Mara nyingi nashangazwa kusikia kwamba; "Dada White anasema siyo vibaya kuvaa sketi na gauni za hoops ndogo." Hakuna mtu aliyewahi kunisikia nikisema kitu kama hicho. Baada ya kuona kile nilichonacho kuhusiana na magauni na sketi hizi za hoops, hakuna kinachoweza kitakachonichochea kumtia moyo mtu yeyote kuzivaa. Mablanketi mazito yanayoshonwa kwa vitambaa vingi yaitwayo quilts, na gauni na sketi hizi ndefu zinazobana nyonga vyote havina umuhimu. Yeye aliyetuumba hakukusudia tuje kujipatia ulema na mavazi haya, au chochote chenye mwonekano kama huo. Lakini watu wa MUNGU wamekuwa wakiongozwa na uvumbuzi na mitindo ya ulimwengu kiasi kwamba hawataki kuondolewa huko ili wawe huru na mambo hayo. Ninaposoma Maandiko, ninashangazwa na Israeli ya MUNGU katika siku hizi za mwisho. Wanaonywa kuikimbia ibada ya sanamu. Ninahofia kwamba wamelala na wamejiunganisha na ulimwengu kiasi kwamba inakuwa vigumu kutofautisha kati ya yule anayemtumikia MUNGU na yule asiyemtumikia. Umbali unazidi kuongezeka kati ya Kristo na watu Wake, na kupungua kati ya watu wanaodai kuwa Wakristo na dunia. Alama zinazowatambulisha wale watu wanaodai ni wa Kristo na ulimwengu ni kama zimepotea zote. Kama Israeli ya zamani wanafuata machukizo ya mataifa yanayowazunguka. {1T 276.3}

Kutokana na yale niliyooneshwa, gauni na sketi hizi ndefu za hoops zinazobana nyonga ni machukizo. Hazifai kabisa kwa viwango vyetu; na watu wa MUNGU wanakosea ikiwa kwa kiwango chochote watafuata au watakuwa na mwonekano wa mtindo huu. Wale wanaodai kuwa watu wa MUNGU wa kipekee na walioteuliwa wanapaswa kuzitupilia mbali hizi gauni na kuzivaa kwake kuwe kemeo hai kwa wale wanaozivaa. Wengine wanaweza kudai kuwa haziwasumbui, kwamba zinawaletea urahisi wa mambo na faraja. Nimesafiri sana na nimeona usumbufu unaowapata wale wanaovaa sketi na gauni hizi za hoops. Wale wanaodai ni za muhimu kwa afya zao, huzivaa wakati wa baridi kunapokuwa theluji, zina madhara zaidi hata ya mablanketi yaliyoshonwa na vitambaa vingi (quilts). Ninaposafiri kwenye magari ya farasi au kwa treni, nimekuwa nikiongozwa kupaza sauti: Jamani, kujistahi kuko wapi, hata watu hawaoni aibu kabisa! Nimeona makundi makubwa yakijazana kwenye magari, na ili mtu asonge mbele, lazima sketi na gauni hizi za hoops ziinuliwe na kuwekwa kwenye umbo ambalo halifai. Na kuanikwa kwa mwili kulikuwa mara kumi zaidi kwa wale waliovaa gauni hizi, kuliko kwa wale wasioyavaa. Kama isingekuwa kwa ajili ya mitindo, wale wanaojianika hivyo bila kujistahi wangesengenywa au kuzomewa, lakini kujistahi na kufaa ni lazima vitolewe

kafara kwa miungu ya mitindo. Hebu Bwana awaokoe watu Wake kutoka katika dhambi hii ya kutisha! MUNGU hatawaonea haya wale watakaokuwa watumwa wa mitindo. Lakini tukidhani kuna faida fulani ndogo ya kuvaa gauni hizi, je, hii inathibitisha kuwa ni sahihi kuzivaa? Hebu mitindo ibadilike, na uzuri, faraja na faida zake hizi hoops hazitaorodheshwa tena. Ni wajibu wa kila mtoto wa MUNGU kuuliza: "Je, kwa yapi mimi nimetengwa na ulimwengu?" Hebu tuvumilie usumbufu kidogo na kuwa kwenye upande ulio sahihi. Watu wa MUNGU wanabeba misalaba ya aina gani? Wanachanganyikana na ulimwengu, wanashiriki roho yao, mavazi yao, mazungumzo yao, na kutenda kama walimwengu wanavyofanya. {1T 277.1}

Soma 1 Timotheo 2: 9, 10: "Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa MUNGU." Pia 1 Petro 3: 3-5: "Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za MUNGU. Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini MUNGU, na kuwatii waume zao." {1T 278.1}

Nguvu ya mfano ni kubwa. Dada A anajitahidi kuvaa sketi na gauni ndogo za hoops. Dada B anasema: Siyo mbaya zaidi kwangu kuvaa sketi na gauni hizi za hoops kuliko kwa dada A, na yeye huvaa zile kubwa kidogo. Dada C anaiga mfano wa dada A na B, na huvaa sketi na gauni zake za hoops kubwa kidogo kuliko A na B, lakini wote wanagombania kusema kuwa sketi na gauni zao za hoops ni ndogo. {1T 278.2}

Wazazi watakaowafundisha watoto wao uovu wa kufuata mitindo ya ulimwengu, wana pambano gumu. Wanakutana na maswali: "Kwa nini, mama, dada A, B, na C huvaa sketi na gauni ndefu za hoops zinazobana nyonga; ikiwa ni mbaya kwangu, ni mbaya kwao pia." Je, wazazi wanaweza kusema nini? Wanapaswa kuweka mfano sahihi mbele ya watoto wao, na ingawa mfano wa wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo kwa mdomo, unasababisha watoto kufikiria kuwa wazazi wao ni waangalifu kupita kiasi na wakali/wakatili katika vizuizi vyao, lakini MUNGU atabariki juhudi za wazazi hawa wenye kuweka tahadhari. Kama wazazi hawatachukua msimamo thabiti, watoto wao watasombwa na mafuriko kwa kuwa Shetani na malaika zake wabaya wanafanya kazi akilini mwao, na mfano wa waigizaji wasioongoka hufanya kazi ya kushinda jaribu kuwa ngumu zaidi kwao. Hata hivyo, kwa njia ya imani kwa MUNGU na maombi ya dhati na bidii, wazazi waaminio wanapaswa kuendelea katika njia rafu na iliyoparuza ya wajibu. Njia ya msalabani ni ile ya kuendelea

mbele, na kuelekea juu zaidi. Na tunapoendelea mbele katika njia hii na kutafuta vitu vilivyo juu, lazima tuache mbali zaidi na zaidi vitu ambavyo ni vya dunia. Wakati ulimwengu na watu wa mwilini wanaodai kuongoka wakishuka chini kwenye mauti, wale wanaopanda kilima watalazimika kuweka juhudi la sivyo watashushwa pamoja nao. {1T 278.3}

Watoto wa ulimwengu wanaitwa watoto wa giza. Wamepofushwa na MUNGU wa ulimwengu huu, na wanaongozwa na roho ya mkuu wa giza. Hawawezi kufurahia mambo ya mbinguni. Wana wa nuru wao hufurahishwa na mambo ya juu. Wanaacha nyuma yao mambo ya ulimwengu huu. Wao hutimiza amri: Ondokeni kati yao, iweni tofauti "Hapa pana ahadi yenye masharti: “Nitawapokea” Tangu mwanzo, Kristo amewachagua watu Wake kutoka katika ulimwengu na kuwataka wawe tofauti, waliojitenga, wasio na ushirika na wenye matendo yasiyofaa ya giza. Kama wanampenda MUNGU  na kushika amri Zake, watakuwa mbali na urafiki, na kupenda raha za ulimwengu. Hakuna maelewano kati ya Kristo na Beliali. {1T 279.1 }

Nabii Ezra, na watumishi wengine waaminifu wa kanisa la Kiyahudi, walishangaa wakati watoto wa kifalme na wakuu walipowajia na kusema: “Watu wa Israeli, na makuhani, na Walawi, hawakujitenga na watu wa nchi hizi, wamefanya sawasawa na machukizo yao.” “Na baada ya hayo yote yaliyotupata kwa sababu ya matendo yetu mabaya, na kwa sababu ya hatia yetu iliyo kuu, ikiwa Wewe MUNGU wetu hukutuadhibu kama tulivyostahili kwa maovu yetu, tena umetupa mabaki; je! Tuzivunje tena amri Zako, tukajiunge na watu wanaotenda machukizo hayo, kwa kuoana nao? Je! Usingekasirika hata kutuangamiza kabisa, pasisalie mabaki yoyote, wala mtu wa kuokoka? Ee Bwana, MUNGU  wa Israeli, Wewe Ndiwe Mwenye haki, maana sisi tumesalia, mabaki yaliyookoka, kama hivi leo; tazama, sisi tupo hapa wenye hatia mbele Zako; maana hapana mtu awezaye kusimama mbele Zako kwa sababu ya jambo hili.” Ezra 9: 1, 1315. {1T 279.2}

2 Nyakati 36: 14-16: “Na zaidi ya hayo wakuu wote wa makuhani, na watu, wakakosa mno sawasawa na machukizo yote ya mataifa; wakainajisi nyumba ya Bwana aliyoitakasa katika Yerusalemu. Naye Bwana, MUNGU wa baba zao, akatuma kwao kwa mikono ya wajumbe Wake, akiondoka mapema, na kutuma; kwa sababu aliwahurumia watu Wake, na makao Yake; lakini waliwadhihaki wajumbe wa MUNGU, na kuyadharau Maneno Yake, na kuwacheka manabii Wake, hata ilipozidi ghadhabu ya Bwana juu ya watu Wake, hata kusiwe na kuponya.” {1T 280.1}

Walawi 18:26, 27: “Kwa hiyo mtazishika amri Zangu na hukumu Zangu, wala msifanye machukizo hayo mojawapo; yeye aliye mzalia, wala mgeni aketiye

kati yenu; (kwa kuwa hao watu wa nchi wameyafanya machukizo haya yote, hao waliotangulia mbele zenu, na hiyo nchi imekuwa najisi;)” {1T 280.2}

Kumbukumbu la Torati 32: 16-22: “Wakamtia wivu kwa miungu migeni, Wakamkasirisha kwa machukizo. Walitoa sadaka kwa pepo, si MUNGU, Kwa miungu wasiyoijua, Kwa miungu mipya iliyotokea siku zilizo karibu, Ambayo baba zenu hawakuiogopa. Humkumbuki Mwamba aliyekuzaa, MUNGU aliyekuzaa umemsahau. Bwana akaona, akawachukia, Kwa sababu ya kukasirishwa na wanawe na binti Zake. Akasema, Nitawaficha uso Wangu, Nitaona mwisho wao utakuwaje; Maana, ni kizazi cha ukaidi mwingi, Watoto wasio imani ndani yao. Wamenitia wivu kwa kisicho MUNGU; Wamenikasirisha kwa ubatili wao; Nami nitawatia wivu kwa wasio watu, Nami nitawakasirisha kwa taifa lipumbaalo. Maana, moto umewashwa kwa hasira Yangu, Unateketea hata chini ya kuzimu, Unakula dunia pamoja na mazao yake, Unaunguza misingi ya milima.” {1T 280.3}

Hapa tunasoma maonyo ambayo MUNGU aliwapa Israeli ya kale. Hayakuwa mapenzi Yake kwamba watangetange jangwani kwa muda mrefu; Yeye Angeweza kuwaleta mara moja kwenye nchi ya ahadi kama wangejisalimisha Kwake na kupenda kuongozwa na Yeye; lakini kwa sababu mara nyingi walikuwa wakimhuzunisha jangwani, aliapa kwa ghadhabu Yake kwamba hawataingia ndani ya pumziko Lake, isipokuwa wawili tu ambao walimfuata Yeye kikamilifu. MUNGU aliwataka watu Wake wamtumaini Yeye peke yake. Hakutaka wapate msaada kutoka kwa wale ambao hawakumtumikia Yeye. {1T 281.1}

Tafadhali soma Ezra 4: 1-5: “Basi adui za Yuda na Benyamini, waliposikia ya kuwa wana wa uhamisho wanamjengea Bwana, MUNGU wa Israeli, hekalu, wakamkaribia Zerubabeli, na wakuu wa mbari za mababa, wakawaambia, Na tujenge sisi nasi pamoja nanyi; kwa maana tunamtafuta MUNGU wenu kama ninyi, nasi twamtolea dhabihu tangu zamani za Esar-hadoni, mfalme wa Ashuru, aliyetupandisha mpaka hapa. Lakini Zerubabeli, na Yoshua, na wakuu wengine wa mbari za mababa katika Israeli, wakawaambia, Ninyi haiwahusu kushirikiana nasi katika kumjengea MUNGU wetu nyumba; bali sisi wenyewe peke yetu tutamjengea Bwana, MUNGU wa Israeli, nyumba, kama mfalme Koreshi, mfalme wa Uajemi, alivyotuamuru. Ndipo watu wa nchi wakaidhoofisha mikono ya watu wa Yuda, wakawasumbua, walipokuwa wakijenga. Wakawaajiri washauri juu yao, ili kuwapinga kusudi lao, siku zote za Koreshi, mfalme wa Uajemi, hata wakati wa kutawala kwake Dario, mfalme wa Uajemi.” {1T 281.2}

Ezra 8: 21-23: “Ndipo nikaamuru kufunga, hapo penye mto Ahava, ili tupate kujinyenyekeza mbele za MUNGU, na kutafuta Kwake njia iliyonyoka, kwa ajili

yetu sisi wenyewe, na kwa ajili ya watoto wetu, na kwa mali yetu yote. Maana naliona haya kumwomba mfalme kikosi cha askari na wapanda farasi, ili kutusaidia juu ya adui njiani; kwa maana tulikuwa tumesema na mfalme, tukinena, Mkono wa MUNGU U juu ya watu wote wamtafutao, kuwatendea mema; bali uweza Wake na ghadhabu Yake ni kinyume cha wote wamwachao. Basi tukafunga, tukamsihi MUNGU wetu kwa ajili ya hayo; Naye akatutakabali." {1T 282.1}

Nabii na hawa wazee hawakuwachukulia watu wa nchi kama waabudu wa MUNGU wa kweli, na ingawa watu hawa walidai urafiki na kutaka kuwasaidia, hawakuthubutu kuungana nao katika kitu chochote kinachohusiana na ibada Yake Bwana. Wakati wa kwenda Yerusalemu kujenga hekalu la MUNGU na kurudisha ibada Yake, wasingeomba msaada kwa mfalme kuwasaidia njiani, lakini kwa kufunga na kuomba walimtafuta Bwana kwa msaada. Waliamini kwamba MUNGU angewatetea na kuwafanikisha watumishi Wake katika juhudi zao za kumtumikia. Muumba wa vitu vyote hahitaji msaada wa maadui Zake ili kusimika/kuanzisha ibada Yake. Yeye Haombi sadaka ya uovu, wala haikubali sadaka ya wale walio na miungu mingine mbali na Bwana. {1T 282.2}

Mara nyingi tunasikia maoni: "Ninyi ni wa kipekee sana." Kama washiriki tungetoa dhabihu yoyote kuokoa roho, au kuwaongoza kwenye Ukweli. Lakini hatuthubutu kuungana nao, kupenda vitu wanavyopenda, na kuwa na urafiki na ulimwengu, kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa na uadui na MUNGU. {1T 282.3}

Kwa kusoma Maandiko yafuatayo tutaona jinsi MUNGU alivyowachukulia Israeli ya kale: {1T 282.4}

Zaburi 135: 4: "Kwa maana Bwana amemchagua Yakobo awe Wake, na Israeli awe hazina Yake ya pekee." {1T 282.5}

Kumbukumbu la Torati 14: 2: "Kwa maana wewe u taifa takatifu kwa Bwana MUNGU wako, na Bwana amekuchagua uwe watu Wake Mwenyewe, juu ya mataifa yote yaliyo duniani." {1T 282.6}

Kumbukumbu 7:6, 7: "Kwa maana wewe u taifa takatifu kwa Bwana, MUNGU wako; Bwana MUNGU Wako, amekuchagua kuwa watu Wake hasa, zaidi ya mataifa yote yaliyoko juu ya uso wa nchi. Bwana hakuwapenda ninyi, wala hakuwachagua ninyi, kwa sababu mlikuwa wengi kuliko mataifa yote, maana mlikuwa wachache kuliko watu wote." {1T 283.1}

Kutoka 33:16: "Kwa maana itajulikanaje kuwa nimepata neema mbele Zako, mimi na watu wako? Siyo kwa sababu unakwenda pamoja nasi, hata mimi na watu Wako tutengwe na watu wote walio juu ya uso wa nchi? {1T 283.2}

Israeli ya kale iliasi mara ngapi, na mara ngapi ilitembelewa na hukumu, na maelfu waliuawa, kwa sababu hawakutii amri za MUNGU aliyewachagua! Israel ya MUNGU katika siku hizi za mwisho ipo katika hatari mara kwa mara ya kujichanganya na ulimwengu na kupoteza ishara ya kuwa watu waliochaguliwa na MUNGU. Soma tena Tito 2:13-15. Hapa tumeletwa kwenye siku za mwisho, wakati MUNGU atakapojitakasia watu wa pekee. Je! Tutamchokoza kama Israeli wa kale walivyomchokoza? Je! Tulete ghadhabu Yake juu yetu kwa kutoka Kwake na kujichanganya na ulimwengu, na kufuata machukizo ya mataifa yanayotuzunguka? {1T 283.3}

Bwana amemtenga yeye aliye mcha MUNGU kwa ajili Yake Mwenyewe; uwekwaji wakfu huu kwa MUNGU na kujitenga na ulimwengu vimeamriwa waziwazi kwa wema katika Agano la Kale na Jipya. Kuna ukuta wa utengano ambao Bwana Mwenyewe ameuweka kati ya vile vya ulimwengu na vitu alivyovichagua kutoka ulimwenguni na kuvitakasa kwa ajili Yake Mwenyewe. Wito na tabia ya watu wa MUNGU ni vya pekee, matarajio yao ni ya kipekee, na sifa hizi zinawatofautisha na watu wengine wote. Watu wote wa MUNGU duniani ni mwili mmoja, tangu mwanzo hadi mwisho wa nyakati. Wana Kichwa kimoja kinachoongoza, kinachosimamia na kutawala mwili. Amri zile zile ambazo zilikuwa juu ya Israeli ya kale, ziko juu ya watu wa MUNGU sasa, kujitenga na ulimwengu. Mkuu, na Kichwa cha kanisa hajabadilika. Uzoefu wa Wakristo katika siku hizi ni kama safari za Israeli ya zamani. Tafadhali someni 1 Wakorintho 10, hasa kuanzia aya ya 6 hadi ya 15: {1T 283.4}

“Basi mambo hayo yalikuwa mifano kwetu, kusudi sisi tusiwe watu wa kutamani mabaya, kama wale nao walivyotamani. Wala msiwe waabudu sanamu, kama wengine wao walivyokuwa; kama ilivyoandikwa, Watu waliketi kula na kunywa, kisha wakasimama wacheze……. wala tusimjaribu Bwana, kama wengine wao walivyomjaribu, wakaharibiwa na nyoka. Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyonung'unika, wakaharibiwa na mharabu. Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani. Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke. Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila MUNGU ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili. Kwa ajili ya hayo, wapenzi wangu, ikimbieni ibada ya sanamu. Nasema kama na watu wenye akili; lifikirini ninyi ninenalo.” {1T 284.1}

1 Yohana 3: 1: "Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa MUNGU ; kwa sababu hiyo ulimwengu hautujui, kwa sababu haukumtambua Yeye." {1T 284.2}

1 Yohana 2: 15-17: “Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya MUNGU adumu hata milele.” {1T 284.3}

1 Petro 2:20: “Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza.” {1T 284.4}

Yakobo 4: 4: “Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa MUNGU ? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa MUNGU.” {1T 285.1}

Yakobo 1:27: “Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za MUNGU Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.” {1T 285.2}

Tito 2:12: “Nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa.” {1T 285.3}

Warumi 12: 2: “Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya MUNGU yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.” {1T 285.4}

Yohana 17:14, 15, 17: “Mimi nimewapa Neno Lako; na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu.” “Uwatakase kwa ile Kweli; Neno lako Ndiyo Kweli.” {1T 285.5}

Luka 6:22, 23: “Heri ninyi watu watakapowachukia, na kuwatenga, na kuwashutumu, na kulitupa nje jina lenu kama neno ovu, kwa ajili ya Mwana wa Adamu. Furahini siku ile na kuruka-ruka, kwa kuwa, tazama, thawabu yenu ni kubwa mbinguni, maana, baba zao waliwatenda manabii vivyo hivyo.” {1T 285.6}

Yohana 15: 16-19: “Si ninyi mlionichagua Mimi, bali ni Mimi niliyewachagua ninyi; Nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa Jina Langu awapeni. Haya nawaamuru ninyi, mpate kupendana. Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia Mimi kabla ya kuwachukia ninyi. Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali Mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia.” {1T 285.7}

1 Yohana 4: 4, 5: “Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na MUNGU nanyi mmewashinda, kwa sababu Yeye aliye ndani yenu ni Mkuu kuliko yeye aliye katika dunia. Hao ni wa dunia; kwa hiyo wanena ya dunia na dunia huwasikia.” {1T 285.8}

1Yohana 2: 5, 6: “Lakini yeye alishikaye Neno Lake, katika huyo upendo wa MUNGU umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani Yake. Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama Yeye alivyoenenda.” {1T 286.1}

1 Petro 2: 9: “Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya MUNGU, mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu.” {1T 286.2}

Tunaposoma Neno la MUNGU, lipo wazi kwamba watu Wake wanapaswa kuwa wa kipekee, walio tofauti na ulimwengu usioamini unaowazuguka karibu nao. Msimamo wetu ni wa kuvutia na wa kutisha; Katika kuishi siku za mwisho, ni muhimu kiasi gani kuiga mfano wa Kristo, na kutembea kama Yeye alivyotembea. “Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi Wake, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate.” Maoni na hekima za wanadamu hazipaswi kutuongoza au kututawala. Haya daima huongoza mbali na msalaba. Watumishi wa Kristo hawana nyumba zao wala hazina yao hapa. Laiti wote wangeweza kuelewa kuwa ni kwa sababu tu Bwana anatawala ndiyo maana tunaruhusiwa hata kukaa kwa amani na usalama na maadui zetu. Siyo haki yetu kudai upendeleo maalum kutoka ulimwenguni. Lazima tukubali kuwa maskini na kudharauliwa kati ya wanadamu, hadi vita vitakapomalizika na ushindi utakapopatikana. Waumini wa Kristo wameitwa kutoka nje na kujitenga na urafiki na roho ya ulimwengu; nguvu zao zinatokana na kuchaguliwa na kukubaliwa na MUNGU. {1T 286.3}

Mwana wa MUNGU alikuwa mrithi wa vitu vyote, na enzi na utukufu wa falme za ulimwengu huu ziliahidiwa Kwake. Hata hivyo wakati alipoonekana katika ulimwengu huu, hakuwa na utajiri au uzuri. Ulimwengu haukuuelewa umoja Wake na Baba; uzuri usio na utukufu wa tabia Yake MUNGU ulikuwa umefichwa mbali nao. Kwa hivyo “alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu,” na “tulimwona kuwa amepigwa, amepigwa na MUNGU, na kuteswa." Kama vile Kristo alivyokuwa ulimwenguni, ndivyo pia wafuasi Wake watakavyokuwa. Wao ni wana wa MUNGU, na warithi pamoja na Kristo; na ufalme na enzi ni mali yao. Ulimwengu hautambui tabia na wito wao mtakatifu; hawajui kuasiliwa kwao kulivyo katika familia ya MUNGU. Muungano wao na ushirika wao na Baba na Mwana haujadhihirika, na wakati ulimwengu unaposhuhudia udhalilishaji na aibu yao, haioneshi jinsi walivyo, au vile watakavyokuwa. Wao ni wageni. Ulimwengu hauwajui, na hauthamini nia zinazowahimiza. {1T 286.4}

Dunia inakomaa kwa uharibifu wake. MUNGU anaweza kuwavumilia wenye dhambi lakini kwa muda kidogo tu. Lazima wanywe hasira ya kikombe cha

ghadhabu Yake isiyochanganywa na rehema. Wale ambao watakuwa warithi wa MUNGU, na warithi pamoja na Kristo kwa urithi wa milele, watakuwa wa kipekee. Ndiyo, watakuwa wa pekee sana kiasi kwamba MUNGU ataweka alama juu yao kama watu Wake, Wake kabisa kabisa. Je! Mnafikiri kwamba MUNGU atapokea, heshima, na kuwatambua watu waliojichanganya na ulimwengu hata wakatofautiana nao kwa jina tu? Someni tena Tito 2:13-15. Hivi karibuni atajulikana ni nani aliye upande wa Bwana, na ni nani hatamuonea Yesu aibu. Wale wasio na ujasiri wa kimaadili wasioongozwa na dhamiri zao kukabili nyuso za makafiri, wasioacha mtindo wa ulimwengu, na kuiga tabia ya kujikana nafsi ya maisha ya Kristo, humuonea aibu, na huwa hawapendi mfano Wake. {1T 287.1}








## SURA YA 60

## KUJIWEKA WAKFU

Watu wa MUNGU watajaribiwa na kuthibitishwa. Kazi ya karibu na ya kuchunguza inapaswa kuendelea miongoni mwa Watunzaji wa Sabato. Kama Israeli ya zamani, ni kwa haraka kiasi gani tunamsahau MUNGU na matendo Yake ya ajabu, na kumuasi. Wengine huutazama ulimwengu na kutamani kufuata mitindo yake na kushiriki katika starehe zake, kama vile watoto wa Israeli walivyotazama nyuma huko Misri na kutamani vitu vizuri ambavyo walikuwa wamevifurahia huko, na ambavyo MUNGU alichagua kutowapa ili kuwajaribu na hivyo kupima uadilifu wao kwake. Yeye Alitamani kuona kama watu Wake walithamini huduma Yake, na uhuru ambao alikuwa amewapatia

kimiujiza, zaidi ya starehe walizozifurahia Misri wakati wakiwa katika utumwa wa watu dhalimu, na waabudu sanamu. {1T 287.2}

Wafuasi wote wa Kweli wa Yesu watakuwa na dhabihu watakazofanya. MUNGU atawathibitisha na kujaribu Ukweli wa imani yao. Nimeoneshwa kuwa wafuasi wa kweli wa Yesu wataachana na michango ya pikniki, maonesho, na mikusanyiko mingine kwa lengo la kujifurahisha. Hawawezi kumpata Yesu wakiwa huko, na hakuna ushawishi ambao utawafanya wafikirie mbinguni, na kuwa na akili ya mbingu na kuongeza ukuaji wao katika neema. Neno la MUNGU likitiiwa linatuongoza sote kutoka kwenye mambo haya yote na kujitenga. Vitu vya ulimwengu vinavyotafutwa, na huhesabiwa kuwa vinastahili kupongezwa, kuthaminiwa, kupendwa na kufurahiwa, na wale wote wasio wapenzi wa msalaba wala kuwa wafuasi Yesu aliyesulubiwa wafanyao ibada katika Roho. {1T 288.1}

Kuna makapi kati yetu, na hii ndiyo sababu sisi ni dhaifu sana. Wengine huegemea ulimwenguni kila wakati. Maoni na hisia zao zinawiana vizuri zaidi na roho ya dunia kuliko ile ya wafuasi wa Kristo wanaojikana. Ni kawaida kabisa kwao kupendelea ushirika wa wale ambao roho zao zitakubaliana nao vizuri. Na watu wa namna hiyo wana ushawishi mkubwa sana kwa watu wa MUNGU. Wanashirikiana nao, na wana jina kati yao, na ni kitabu kwa wasioamini na walio dhaifu na wasiojitoa wakfu kanisani. Watu hawa wenye nia mbili daima watakuwa ni wapinzani wa ushuhuda wa wazi, unaokemea makosa ya mtu binafsi. Katika nyakati hizi za utakaso watu hawa ama watabadilishwa kabisa, na kutakaswa kwa kuutii Ukweli, au wataachwa ulimwenguni, pale wanapostahili kuwa, ili wapokee thawabu yao pamoja nao. {1T 288.2}

“Mtawatambua kwa matunda yao.” Wafuasi wote wa Kristo huzaa matunda kwa utukufu Wake. Maisha yao yanashuhudia kwamba kazi nzuri imefanywa ndani yao na ROHO WA MUNGU, na matunda yao ni kwa utakatifu. Maisha yao yameinuliwa na yako safi. Wale wasiozaa matunda hawana uzoefu katika mambo ya MUNGU. Hawapo ndani ya mzabibu. Someni Yohana 15:4, 5; “Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani Yangu. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.” 1T 289.1}

Kama tungekuwa waabudu wa kiroho wa Yesu Kristo, lazima tungeitoa dhabihu kila sanamu na kuzitii kikamilifu amri nne za kwanza. Mathayo 22:37, 38: “Akamwambia, Mpende Bwana MUNGU wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.” Amri nne za kwanza haziruhusu mgawanyo wa upendo kutoka kwa MUNGU. Wala chochote hakiruhusiwi kugawanya, au kushiriki, furaha yetu kuu Kwake. Chochote kinachogawanya upendo wetu Kwake, na kuondoa moyoni upendo mkuu kwa MUNGU, kinaunda sura ya sanamu. Mioyo yetu ya mwili

ingeshikamana na sanamu zetu na kutafuta kuzibeba; lakini hatuwezi kusonga mbele mpaka tuziweke kando, kwani zinatutenganisha na MUNGU. Kiongozi Mkuu wa kanisa amechagua watu Wake kutoka ulimwenguni na anahitaji watengane na ulimwengu. Yeye Anakusudia kwamba Roho ya amri Zake itawarejesha Kwake na kuwatenganisha na vitu vya ulimwengu. Kumpenda MUNGU na kushika amri Zake kuko mbali na kupenda starehe na urafiki wa ulimwengu. Hakuna mapatano kati ya Kristo na Beliali. Watu wa MUNGU waweza kumtumainia Yeye peke yake na bila woga kuendelea katika njia ya utii. {1T 289.2}

## SURA YA 61

## FALSAFA NA UDANGANYIFU WA BURE

Nimeoneshwa kuwa lazima tulindwe kila upande na kwa uvumilivu kupinga mawazo na hila za Shetani. Amejigeuza kuwa malaika wa nuru na anawadanganya maelfu na kuwafanya mateka. Anatafuta kunufaika kwa kiasi kikubwa na sayansi ya akili. Hapa, kama nyoka, na kwa hila na taratibu sana anajiingiza ili kuharibu kazi ya MUNGU. Miujiza na kazi ya Kristo yeye huifanya ionekane kuwa imetokana na ujuzi na nguvu za binadamu. Kama angefanya shambulio la wazi na la ujasiri juu ya Ukristo, hilo lingemleta Mkristo katika dhiki na uchungu hadi miguuni pa Mkombozi wake, na Mkombozi wake hodari angemfanya adui jasiri akimbie. Shetani mwenyewe hujigeuza kuwa malaika wa nuru na hufanya kazi kwenye akili akitushawishi tutoke kwenye njia pekee iliyo salama na sahihi. Sayansi ya frenolojia, saikolojia, na mesmerism/hyponotism*, ni mawakala ambao kupitia hao Shetani huja moja kwa moja katika kizazi hiki na hufanya kazi kwa nguvu ile ambayo ni sifa ya ufanisi wake wa karibu na mwisho wa kipindi cha kufungwa kwa mlango wa rehema (**Kuteka akili ya watu*

*kama sumaku-hyponotism, soma zaidi tiba za giza za mashariki na magharibi kama Ayuverdic, yoga, acupuncture, waganga wa kienyeji nk*). {1T 290.1}

Someni 2 Wathesalonike 2: 8-12: "Hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi, ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa CHAKE, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo Kwake; yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile Kweli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo MUNGU awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini Kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu." {1T 290.2}

Shetani amekuja bila kujulikana kupitia sayansi hizi na ametia sumu akili za maelfu na kuwaongoza kwenye ukafiri*. Anafurahi kuona ujuzi wa sayansi hizi ukienea. Ni mpango ambao yeye mwenyewe ameuweka ili apate kuzifikia akili na kuwashawishi apendavyo. Wakati inaaminika kwamba akili moja ya mwanadamu inamwathiri mwingine kwa njia ya kushangaza, Shetani, tayari anajipendekeza mwenyewe kuifanya kazi hiyo pande zote. Na wakati wale waliojitoa kwa sayansi hizi wanaposifiwa sana kwa sababu ya kazi kubwa na nzuri ambayo wanathibitisha kuwa imefanywa na wao, wanamthamini na kumtukuza Shetani mwenyewe, ambaye anaingia ndani na kufanya kazi kwa nguvu zote na ishara na uongo wa kushangaza – na udanganyifu wote wa udhalimu. Malaika alisema: "Tieni alama ushawishi wake. Pambano kati ya Kristo na Shetani bado halijaisha." Huu uingiaji wa Shetani kupitia njia ya sayansi umebuniwa vizuri na jeshi lake la kishetani, na katika akili ya maelfu hatimaye imani ya Kweli katika Kristo kuwa Ndiye Masihi, na Mwana wa MUNGU itaharibiwa (*Tiba za Mashariki na Magharibi ambazo ni sawa kama uchawi wa kiafrika tu, ila zinakuwa na ugumu kugundua kuliko waganga wa kienyeji tunaowajua, kuna mstari mwembaba kati ya tiba za giza na Tiba ambazo Mwenyezi Mungu ameweka). {1T 290.3}

Nilielekezwa kwa nguvu ya MUNGU iliyooneshwa kupitia Musa wakati Bwana alipomtuma aende mbele ya Farao. Shetani alielewa shughuli yake na alikuwa uwanjani. Alijua vizuri kwamba Musa alichaguliwa na MUNGU kuvunja nira ya utumwa juu ya wana wa Israeli, na kwamba katika kazi yake alifananisha ujio wa kwanza wa Kristo kama kuvunja nguvu za Shetani juu ya familia ya wanadamu na kuwakomboa wale ambao walifanywa mateka na nguvu zake. Shetani alijua kwamba Kristo atakapotokea, atafanya matendo makuu na miujiza, ili ulimwengu ujue kwamba Baba alimtuma. Adui alitetemeka kwa nguvu Yake Bwana. Alishauriana na malaika zake jinsi ya kukamilisha kazi ambayo ilipaswa kujibu madhumuni mawili:

1. Kuharibu ushawishi wa kazi iliyofanywa na MUNGU kupitia mtumishi Wake Musa, kwa kufanya kazi kupitia mawakala wake, na kwa hivyo kuigiza kazi ya Kweli ya MUNGU (miujiza bandia);

2. Kuongeza ushawishi kwa kazi yake kupitia waganga ambao wangeweza kufika katika vizazi vyote na kuharibu katika akili za wengi imani katika miujiza na matendo makuu yatakayofanywa na Kristo wakati atakapokuja ulimwenguni. Alijua kwamba utawala wake ungeumia, kwa kuwa nguvu aliyokuwa nayo juu ya wanadamu ingekuwa ndogo kuliko ya Kristo. Haukuwa ushawishi au nguvu ya kibinadamu alivyokuwa navyo Musa vilivyozalisha miujiza hiyo iliyofanywa mbele ya Farao. Zilikuwa ni nguvu za MUNGU. Ishara na maajabu hayo yalifanywa kupitia Musa ili kumsadikisha Farao kwamba Yeye aliye mkuu "MIMI NDIMI" amemtuma kumwamuru Farao awaachie Israeli waende ili wamtumikie. {1T 291.1}

Farao aliwaita wachawi wafanye kazi kwa uchawi wao. Walionesha pia ishara na maajabu, kwani Shetani aliwasaidia kufanya kazi kupitia wao. Lakini hata hapa kazi ya MUNGU ilioneshwa kuwa bora kuliko nguvu ya Shetani, kwani wachawi wasingeweza kufanya miujiza yote ambayo MUNGU alifanya kupitia Musa. Ni wachache tu kati yao amao wangeweza kufanya hivyo. Fimbo za wachawi zikawa nyoka, [*Tazama Kiambatanisho*] Lakini fimbo ya Haruni iliwameza. Baada ya wachawi kutafuta kuzalisha chawa, na kutoweza, walilazimishwa na nguvu ya MUNGU kukiri hata mbele ya Farao, wakisema: "Hiki ni kidole cha MUNGU." Shetani alifanya kazi kupitia kwa wachawi kwa njia iliyokusudia kuufanya moyo wa Farao mkatili kuwa mgumu dhidi ya udhihirisho wa miujiza wa nguvu za MUNGU. Shetani alifikiria kuyumbisha imani ya Musa na Haruni juu ya asili ya kiungu ya utume wao, ili vitendea kazi vyake ambao ni wachawi, washinde. Shetani hakuwa tayari kuwaachilia watu wa Israeli kutoka utumwani Misri ili wamtumikie MUNGU. Wachawi walishindwa kutoa muujiza wa chawa, na hawakuweza tena kuwaiga Musa na Haruni. MUNGU asingemruhusu Shetani aendelee zaidi, na wachawi hawakuweza kujiokoa na mapigo. "Nao wale waganga hawakuweza kusimama mbele ya Musa kwa sababu ya hayo majipu, kwa maana hao waganga wachawi walikuwa na majipu, na Wamisri wote walikuwa nayo." Kutoka 9:11. (Kwa kila kazi ya Mungu, Shetani ana kazi bandia) {1T 292.1}

Nguvu ya MUNGU ya kudhibiti hapa ilikata chaneli/njia ambayo kwayo Shetani alifanya kazi, na kusababisha hata wale ambao Shetani alikuwa amewatendea kwa njia ya ajabu kuhisi ghadhabu yake. Ushahidi wa kutosha ulitolewa kwa Farao kumsaidia kuamini, kama angekuwa ametaka. Musa alifanya kwa nguvu za MUNGU. Wachawi hawakufanya kwa sayansi yao peke yao, bali kwa nguvu ya mungu wao, shetani, ambaye kwa ujanja alifanya kazi yake ya udanganyifu ya kughushi kazi ya MUNGU. {1T 292.2}

Tunapokaribia mwisho wa wakati, akili ya mwanadamu inathiriwa kwa urahisi zaidi na hila za Shetani. Anaongoza wanadamu waliodanganywa kuyaona matendo na miujiza ya Kristo kama nayotumia kanuni za kawaida. Shetani amekuwa na kawaida ya kughushi kazi za Kristo na kudai kuwa zimefanywa kwa nguvu zake mwenyewe. Kwa kawaida huwa haifanyi hivi kwa uwazi na kwa ujasiri. Yeye ni mjanja wa sanaa nyingi na anajua kuwa njia inayofaa zaidi kwake kukamilisha kazi yake ni kuja kwa mtu masikini, aliyeanguka kwa njia ya malaika wa nuru. Shetani alikuja kwa Kristo jangwani kwa mfano wa kijana mzuri - kama mfalme kuliko malaika aliyeanguka – akiwa na maandiko kinywani mwake. Alisema: "Imeandikwa." Mwokozi wetu anayeteseka alikabiliana Naye kwa Maandiko, akisema: "Imeandikwa." Shetani alitumia faida ya hali dhaifu ya Kristo, ambaye alikuwa amechukua asili yetu ya kibinadamu. {1T 293.1}

Someni Mathayo 4:8-11: “Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana MUNGU  wako, umwabudu Yeye peke yake. Kisha Ibilisi akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia.” {1T 293.2}

Hapa Shetani aliukunjua ulimwengu mbele ya Kristo katika nuru yenye kuvutia zaidi huku akimdhihaki Bwana kuwa hakulazimika kupitia mateso mengi ili kuupata ufalme wa dunia; eti Shetani angekidhi madai yake yote ikiwa tu kama Kristo angekubali kumuabudu. Kutoridhika kwa Shetani kulianzia mbinguni kwa kuwa hakufanywa wa kwanza na wa juu mno katika kutoa amri – akiwa sawa na MUNGU, na akiwa juu ya Kristo. Aliasi na kupoteza milki yake; na yeye, na wale waliomhurumia, waliondolewa kutoka mbinguni. Katika hali mbaya ya nyikani, alitarajia kupata faida kupitia hali dhaifu na mateso ya Kristo, na kupata kutoka kwake heshima ambayo hakuweza kuipata mbinguni. Lakini Yesu, hata katika hali Yake ya kulegea na kuchoka, hakujitoa kwa jaribu la Shetani kwa muda, bali alionesha ukuu Wake na kutumia mamlaka Yake kwa kumwambia Shetani: “Ondoka hapa” - au, Ondoka Kwangu. Shetani alishangaa. Kisha akajifunza jinsi ambavyo angeweza kutimiza kusudi lake na kupokea heshima kutoka katika jamii ya wanadamu ambayo alizuiliwa kule mbinguni na hapa duniani kwa Yesu. Kama angeweza kufanikiwa kumjaribu Kristo, basi mpango wa wokovu ungeshindikana, na angefanikiwa kuleta taabu isiyo na matumaini juu ya wanadamu. Lakini yale ambayo Shetani alishindwa kutekeleza alipokuja kwa Kristo ameyatimiza alipokuja kwa mwanadamu. {1T 293.3}

Ikiwa Shetani anaweza kupumbaza na kudanganya akili ya mwanadamu hata kuwaongoza wanadamu kufikiri kwamba kuna nguvu ya asili ndani yao ya kutimiza kazi kubwa na nzuri, wataacha kumtegemea MUNGU awafanyie yale ambayo wanafikiri kuna nguvu ndani yao wenyewe kufanya. Hawatamtambua kama kiumbe mwenye uwezo wa juu. Hawatampa MUNGU utukufu anaoudai, na ambao unatokana na ukuu na ubora Wake mkuu. Kusudi la Shetani hivyo

litakuwa limetimizwa, na angefurahia kwamba watu walioanguka wanajiinua kwa kiburi kwa kukiuka mapenzi ya Mungu kama alivyojiinua mwenyewe mbinguni na kutupwa nje. Anajua kwamba ikiwa mtu atajiinua, uharibifu wake ni hakika kama vile ulivyokuwa uharibifu wake yeye mwenyewe Shetani. {1T 294.1}

Shetani alishindwa katika majaribu yake kwa Kristo jangwani. Mpango wa wokovu umetekelezwa tayari. Gharama kubwa imelipwa kwa ukombozi wa mwanadamu. Na sasa Shetani anajaribu kurarua msingi wa tumaini la Mkristo na kugeuza mawazo ya watu kwenye chaneli/mkondo ambayo hawatanufaika nayo au kuokolewa na dhabihu kubwa inayotolewa. Anamwongoza mwanadamu aliyeanguka, kupitia "madanganyo yote ya udhalimu," kuamini kwamba anaweza kufanya vizuri sana bila upatanisho, kwamba hahitaji kumtegemea Mwokozi aliyesulibiwa na kufufuka, kwamba sifa za mwanadamu mwenyewe zaweza kumhalalisha kupata upendeleo wa MUNGU. Na kisha anaharibu ujasiri/imani ya mwanadamu *ndani ya Biblia*, akijua vizuri kwamba ikiwa atafanikiwa hapa, na kuharibu kile kinachotambulisha kuwepo kwake, atakuwa salama. Anaweka akilini udanganyifu kwamba Shetani halisi hayupo, na wale wanaoamini jambo hili hawafanyi juhudi za kupinga na kupambana dhidi ya kile wanachofikiria kuwa hakipo. Kwa hiyo wanadamu maskini, wanaokufa na vipofu, mwishowe wanakubali maneno, "Yote ni sawa-chochote kile ni sawa." Hawaitambui sheria yo yote inayopima mwenendo wao. {1T 294.2}

Shetani huwaongoza watu wengi kuamini kwamba sala kwa MUNGU haina maana, bali ni mtindo, desturi na sera tu. Anajua vizuri jinsi kutafakari na sala zinavyohitajika ili kuwafanya wafuasi wa Kristo waamke kupinga ujanja na udanganyifu. Kwa kutumia vifaa vyake angeweza kugeuza akili kutokana na mazoezi haya muhimu, ili roho isiweze kutegemea/kuegemea msaada kwa Yule Mwenye nguvu na kupata nguvu kutoka Kwake kupinga mashambulio yake. Nilielekezwa kwa maombi ya bidii na yenye ufanisi ya watu wa MUNGU wa zamani. "Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi, akaomba kwa bidii." Danieli alimwomba MUNGU wake mara tatu kwa siku. Shetani hukasirishwa na sauti ya sala ya bidii, kwani anajua kuwa atapata hasara. Daniel alikuwa amependelewa juu ya watawala na wafalme kwa sababu Roho nzuri ya Bwana ilikuwa ndani yake. Malaika walioanguka waliogopa kwamba ushawishi wake ungedhoofisha udhibiti wao juu ya watawala wa ufalme, kwani Danieli alikuwa na mamlaka kubwa. Jeshi la malaika waovu linaloshtaki liliwachochea watawala na wafalme kumuonea wivu, na walimwangalia Danieli kwa karibu ili wapate kitu dhidi yake cha kumshitaki kwa mfalme; lakini walishindwa. Kisha mawakala hawa wa Shetani walitafuta kufanya uaminifu wake kwa MUNGU uwe sababu ya kuangamia kwake. Malaika wabaya waliweka mpango kwa ajili yake, na mawakala hawa waliutekeleza kwa utayari. {1T 295.1}

Mfalme hakujua mbinu chafu iliyokusudiwa dhidi ya Danieli. Akiwa na ufahamu kamili wa agizo la mfalme, Danieli bado aliendelea kusujudu mbele za MUNGU wake, "madirisha yake yakiwa yamefunguliwa." Alichukulia dua kwa MUNGU wake kuwa yenye umuhimu mkubwa sana kiasi cha kuwa tayari kutoa kafara maisha yake kuliko kuacha kuomba. Kwa sababu ya kuomba kwake kwa MUNGU, mzee huyu alitupwa ndani ya shimo la simba. Malaika wabaya wakawa wametimiza kusudi lao. Lakini Danieli aliendelea kuomba, hata kwenye tundu la simba. Je! aliteketezwa? Je! MUNGU alimsahau kule shimoni? La, hapana; Yesu, Yule Kamanda hodari wa jeshi la malaika wa mbinguni, alimtuma malaika Wake kufunga vinywa vya wale simba wenye njaa ili wasimdhuru muombaji wa MUNGU; na yote yalikuwa shwari katika lile pango baya. Mfalme alishuhudia kuhifadhiwa kwake na akamleta nje kwa heshima. Shetani na malaika zake walishindwa na kughadhabika sana. Mawakala aliowaajiri waliangamizwa kwa namna ile ile mbaya na ya kutisha ambayo wao walikuwa wamepanga kumuangamiza nayo Danieli. {1T 295.2}

Sala ya imani ni nguvu kubwa ya Mkristo na hakika itamshinda Shetani. Hii ndiyo sababu [Shetani] anasisitiza kwamba hatuna haja ya maombi. Jina la Yesu, wakili wetu, adui analichukia; na tunapomwendea kupata msaada, jeshi la Shetani linataharuki. Tunatimiza kusudi lake vizuri pale tunapopuuzia mazoezi ya maombi, kwa maana hapo ndipo maajabu yake ya uongo yanapopokelewa kirahisi. Yale ambayo alishindwa kuyatimiza katika kumjaribu Kristo, anayakamilisha kwa kuweka vishawishi vyake vya udanganyifu mbele ya mwanadamu. Wakati mwingine huja katika sura ya kijana mzuri, au kivuli kizuri. Yeye hufanya kazi ya uponyaji, na anaabudiwa na wanadamu waliodanganywa kama mfadhili wa jamii yetu. Frenolojia na masomo ya kuvuta akili akili (mesmerism/hyponotism/magnetism)* vimeinuliwa sana. Vitu hivyo ni vizuri kwa mahali pake, lakini vinachukuliwa na Shetani kama mawakala wake wenye nguvu zaidi ili kudanganya na kuharibu roho. Sanaa na vifaa vyake vinapokelewa kama vitu vilivyotoka mbinguni, na imani kwa kile chombo kinachobaini uwepo wake, yaani Biblia, imeharibiwa katika akili za maelfu. Shetani hapa anapokea ibada inayoshabihiana na utukufu wake wa kishetani. Maelfu wanazungumza na, na kupokea maagizo kutoka kwa mungu huyu wa mashetani na kutenda kulingana na mafundisho yake. Ulimwengu ambao unastahili kufaidika sana na frenolojia na animal magnetism, haukuwahi kuwa mbaya hivyo. Shetani hutumia vitu hivi kuharibu wema na kuweka msingi wa umizimu (*Sumaku ya wanyama, pia unajulikana kama mesmerism, ni nadharia iliyobuniwa na daktari wa Ujerumani Franz Mesmer katika karne ya 18. Alisema kama kuna uwepo wa nguvu za ajabu-ajabu za asili zisizoonekana zilizo ndani ya viumbe vyote vilivyo hai, ikiwemo ndani ya wanadamu, wanyama, na mimea. Alidai kuwa nguvu hiyo inaweza kuwa na athari za kimwili, ikiwa ni pamoja na uponyaji). {1T 296.1}

Nilielekezwa katika Andiko hili kama linavyoendana na umizimu wa kisasa: Wakolosai 2: 8: "Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo." Maelfu, nilioneshwa, wameharibiwa kupitia falsafa ya frenolojia na animal magnetism/hyponotism, na wameingizwa katika ukafiri. Ikiwa akili itaanza kutembea kwenye njia hii, ni lazima itapoteza uimara wake na kutawaliwa na mapepo. "Udanganyifu wa bure" hujaza akili za wanadamu maskini. Wanafikiri kuna uwezo kama huo ndani yao ili kufanikisha kazi kubwa hivyo hawajui umuhimu wa nguvu itokayo juu. Kanuni na imani yao ni "kufuatana na mapokeo ya wanadamu, ufedhuli wa ulimwengu, badala ya kuwa kama Kristo." Yesu hajawafundisha wanadamu falsafa hii. Hakuna kitu cha aina hiyo kinachoweza kupatikana katika mafundisho Yake. Yeye hakuelekeza akili za wanadamu maskini, wanaokufa, ziwaelekee wao wenyewe, kwa nguvu waliyonayo. Siku zote alikuwa akizielekeza akili zao kwa MUNGU, Muumba wa ulimwengu, kama Zhanzo cha nguvu na hekima yao. Onyo maalum limetolewa katika aya ya 18: "Mtu asiwanyang'anye thawabu yenu, kwa kunyenyekea kwa mapenzi yake mwenyewe tu, na kuabudu malaika, akijitia katika maono yake na kujivuna bure, kwa akili zake za kimwili." {1T 297.1}

Walimu wa umizimu huja kwa njia ya kupendeza, ya kuroga ili kuwadanganya, na ikiwa mnazisikiliza hekaya zao mnadanganywa na adui wa haki na hakika mtapoteza thawabu yenu. Wakati ushawishi wa kuvutia wa mdanganyifu mkuu ukishinda, ninyi wanadamu mnatiwa sumu, na ushawishi wake mbaya huchafua na kuharibu imani yenu kwa Kristo kuwa ni Mwana wa MUNGU, na hufanya watu waache kutegemea sifa za damu Yake Bwana. Wale wanaodanganywa na falsafa hii, wanahadaiwa zawadi zao kwa njia ya madanganyo ya Shetani. Wanategemea sifa zao wenyewe, hutumia unyenyekevu wa hiari yao wenyewe, na wako tayari hata kutoa dhabihu, na kujishusha wenyewe, na kutoa akili zao kwa imani ya upuuzi mkuu, wakipokea maoni ya kipuuzi zaidi kupitia wale ambao wanawaamini kuwa marafiki zao wa kufa na kupona. Shetani ameyapofusha macho yao na kupotosha hukumu yao hata wasione ubaya; na wanafuata maagizo yanayodaiwa kuwa yanatoka kwa ndugu au marafiki zao waliokufa ambao sasa wamekuwa malaika wenye hadhi ya juu. {1T 297.2}

Shetani amechagua udanganyifu wa kuvutia zaidi, ule unaokusudia kushika huruma za wale ambao wamewaweka wapendwa wao kaburini. Malaika wabaya huchukua umbile la hawa wapendwa waliokufa na kuelezea visa vilivyofungamanishwa na maisha yao na kufanya yale ambayo marafiki wao walifanya wakati wa uhai wao. Kwa njia hii hudanganya na kuwafanya jamaa za wale waliokufa kuamini kwamba jamaa na marafiki zao waliokufa ni malaika wanaozunguka juu yao na kuzungumza nao. Mambo haya wanayaangalia kama ibada fulani ya sanamu, na kile wanachoweza kusema kina ushawishi mkubwa kwao kuliko Neno la MUNGU. Malaika hawa waovu, wanaojiweka kwenye umbo

la marafiki waliokufa, aidha watamkataa kabisa MUNGU na kumfananisha na hadithi za kipuuzi, au ili kukidhi kusudi lao bora, watachagua sehemu muhimu ambazo zinamshuhudia Kristo na kuelekeza njia ya kwenda mbinguni, na kubadilisha kauli wazi za Neno la MUNGU ili kuendana na asili yao ya uharibifu na kuangamiza roho. Kwa umakini wa kutosha kwenye Neno la MUNGU, wote wanaweza kushawishika ikiwa watakataa udanganyifu huu unaoharibu roho. Neno la MUNGU linatangaza kwa Maneno sahihi kwamba "wafu hawajui neno lolote." Mhubiri 9: 5, 6: "kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Mapenzi yao na chuki yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote lililofanyika chini ya jua." {1T 298.1}

Wanadamu wadanganyifu wanawaabudu malaika waovu, wakiamini kuwa ni roho za marafiki zao waliokufa. Neno la MUNGU linatamka wazi kwamba wafu hawana sehemu tena katika chochote kinachofanyika chini ya jua. Waumini wa umizimu (Spiritualists) wanasema kwamba aliyekufa anajua kila kitu kinachofanyika chini ya jua, kwamba wanawasiliana na marafiki zao hapa duniani, wakitoa habari muhimu, na kufanya maajabu. Zaburi 115: 17: "Sio wafu wamsifuo Bwana, Wala wowote washukao kwenye kimya." Shetani, aliyejibadilisha kuwa malaika wa nuru, hufanya kazi kwa udanganyifu wote wa udhalimu. Yeye ambaye angeweza kumchukua Mwana wa MUNGU, aliyefanywa chini punde kuliko malaika, na kumweka juu ya kilele cha hekalu, na kumpeleka juu sana ili kuwasilisha mbele Zake falme za ulimwengu, anaweza kutumia mabavu yake juu ya jamii ya wanadamu, ambao ni duni kwa nguvu na hekima kwa hali ya chini sana kwa kulinganisha na Mwana wa MUNGU, hata baada ya Yeye kuchukua asili ya mwanadamu. {1T 298.2}

Katika kizazi hiki duni kilichopotoka sana, Shetani anamiliki udhibiti wa wale wanaotoka katika mambo ya haki na kujitosa kwenye uwanja wake. Hutumia nguvu zake kwa watu kama hao kwa njia ya kutisha. Nilielekezwa kwa maneno haya: "akijielekeza katika mambo yale ambayo hajawahi kuyaona, akiongozwa bila mafanikio na akili yake ya kimwili." Wengine, nilioneshwa kuwa wanaridhisha udadisi wao na kujikoroga kwa kuchecheza na Shetani. Hawana imani ya kweli katika umizimu na tena wangeshtuka kwa hofu juu ya wazo la wao kuwa wachawi au kushiriki kwenye mambo ya kichawi. Hata hivyo, wanajitosa wenyewe na kujiweka katika nafasi ambayo Shetani anaweza kutumia nguvu zake juu yao. Hao hawamaanishi kuingia ndani ya kazi hii ya kichawi na kishetani, lakini hawajui wanachofanya. Wanazururazurura kwenye uwanja wa Shetani na wanamjaribu ili awatawale. Mwangamizi huyu mwenye nguvu huwaona watu hawa kama mawindo yake halali na hubamiza nguvu zake juu yao, na hilo ni kinyume na mapenzi yao. Wanapotaka kujitawala wenyewe na mapenzi yao hushindwa (wameingia mtegoni). Walitoa mioyo yao kwa Shetani, na hataachilia madai yake, bali atawashikilia mateka. Hakuna nguvu

inayoweza kuikomboa nafsi iliyonaswa isipokuwa nguvu ya MUNGU inayotokana na majibu ya maombi ya dhati na ya bidii ya mfuasi wake mwaminifu. {1T 299.1}

Usalama pekee sasa ni kutafuta Ukweli kama ulivyofunuliwa katika Neno la MUNGU, kama hazina iliyofichwa. Masomo ya Sabato, asili ya mwanadamu, na ushuhuda wa Yesu ni Kweli muhimu na kubwa zinazohitaji kueleweka; hizi zitathibitisha kuwa nanga ya kushikilia watu wa MUNGU katika nyakati hizi za hatari. Lakini umati wa wanadamu hudharau Ukweli wa Neno la MUNGU na kupendelea hadithi za uongo. 2 Wathesalonike 2:10, 11: “Na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile Kweli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo MUNGU awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo.” {1T 300.1}

Wale wenye tabia mbaya za ngono chafu, ulevi na uharibifu hudanganywa sana na roho hizi za kishetani, wanazoamini kuwa ni roho za rafiki zao waliokufa, na wamejivuna bure katika akili zao za mwili. Wakolosai 2:19: “Wala hakishiki Kichwa, ambacho kwa Yeye mwili wote ukiruzukiwa na kuungamanishwa kwa viungo na mishipa, hukua kwa maongeozo yatokayo kwa MUNGU.” Wanamkataa Yeye anayeupatia mwili nguvu, kwamba kila kiungo kiongezeke kwa maongeo ya MUNGU. {1T 300.2}

Falsafa ya uongo, Falsafa batili. Viungo vya mwili hudhibitiwa na kichwa. Waumini wa umizimu huweka kando Kichwa na kuamini kwamba viungo vyote vya mwili lazima vifanye kazi vyenyewe, vinajiendesha vyenyewe na sheria zilizowekwa zisizobadilika, zitawaongoza katika hali ya maendeleo hadi ukamilifu bila kichwa. Yohana 15: 1, 2, 4-6: “Mimi Ndimi mzabibu wa kweli, na Baba Yangu Ndiye mkulima. Kila tawi ndani Yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa. Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani Yangu. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote. Mtu asipokaa ndani Yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea.” {1T 300.3}

Kristo Ndiye chanzo cha nguvu zetu. Yeye Ndiye mzabibu, sisi tu matawi. Lazima tupate lishe kutoka kwenye mzabibu ulio hai. Tukipokonywa nguvu na chakula cha mzabibu huo, sisi ni kama viungo vya mwili visivyo na kichwa na hapo tutakuwa katika nafasi ile ile ambayo Shetani anatutaka tuwemo, ili atudhibiti kama vile apendavyo yeye mwenyewe. Adui anafanya kazi “katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kKeli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo MUNGU awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo.” Umizimu ni uongo. Umejengwa juu ya uongo mkubwa wa asili, “Hamtakufa hakika.” Mwanzo 3. Maelfu wamekataa kichwa,

na matokeo yake ni washiriki watendao bila Yesu aliye kichwa chao, na hivyo mwingine huongoza mwili. Shetani ndiye huwatawala (huongoza kichwa_. {1T 301.1}

Nilioneshwa kuwa Shetani hawezi kutawala akili mpaka ziwe zimesalimishwa kwenye utawala wake. Wale wanaoondoka kutoka kwenye Kweli wako katika hatari kubwa sana. Wanajitenga mbali na MUNGU na kutoka kwenye uangalizi wa malaika zake, na Shetani, akiwa macho kila wakati kuharibu roho, anaanza kuwasilisha udanganyifu wake. Hao wako katika hatari kubwa. Na ikiwa watagundua na kujaribu kuzipinga nguvu za giza na kujinasua kutoka kwenye mtego wa Shetani, hilo halitakuwa jambo rahisi. Wamejitosa wenyewe kwenye uwanja wa Shetani, na anadai kuwa ni raia wake. Adui hatasita kutumia nishati yake yote na kuleta jeshi lote la uovu waje kumsaidia kumpokonya mwanadamu mmoja kutoka mikononi mwa Kristo. Wale waliomjaribu Shetani ili awajaribu watalazimika kufanya bidii kujiondoa kutoka katika nguvu zake. Lakini watakapoanza kujifanyia kazi hiyo wao wenyewe, basi malaika wa MUNGU ambao wamewahuzunisha watakuja kuwaokoa. Shetani na malaika zake hawapendi kupoteza mawindo yao. Wanashindana na kupigana na malaika watakatifu, na pambano ni kali. Lakini ikiwa wale waliokosea wanaendelea kuomba na kusihi kwa unyenyekevu wa kina wanakiri makosa yao, malaika ambao wana nguvu zaidi watashinda na kuwapokonya kutoka kwenye nguvu za malaika waovu. {1T 301.2}

Wakati pazia lilipoinuliwa na kuoneshwa uharibifu wa wakati huu, moyo wangu uliugua, roho yangu ikawa karibu na kuzimia ndani yangu. Niliona kwamba wenyeji wa dunia walikuwa wakikijaza kipimo cha kikombe cha uovu wao. Hasira ya MUNGU imewaka na haitatulizwa tena mpaka wenye dhambi waangamizwe duniani. Shetani ni adui binafsi wa Kristo. Huyu ndiye mwanzilishi na kiongozi wa kila aina ya uasi mbinguni na duniani. Hasira yake inaongezeka; sisi wanadamu huwa hatutambui nguvu zake. Ikiwa macho yetu yangeweza kufunguliwa kutambua malaika walioanguka wanavyofanya kazi kwa wale ambao wanahisi kwamba mambo ni rahisi na wanajiona wako salama, tusingeweza kujisikia salama kama ilivyo sasa. Malaika wabaya wako njiani mwetu kila wakati. Tunatarajia utayari kutoka kwa watu wabaya watende kama Shetani anavyopendekeza; lakini wakati akili zetu zikiwa hazijalindwa dhidi ya mawakala wake wasioonekana, wanachukua uwanja mpya na kufanya maajabu na miujiza machoni petu. Je! Sisi tumejiandaa kuwapinga kwa Neno la MUNGU, silaha pekee ambayo tunaweza kuitumia kwa mafanikio? {1T 302.1}

Wengine watajaribiwa kupokea maajabu haya kana kwamba yanatoka kwa MUNGU. Wagonjwa wataponywa mbele yetu. Miujiza itafanywa mbele yetu. Je! Tumejiandaa kwa kesi inayotungojea wakati maajabu ya uongo ya Shetani yatakapodhihirishwa kikamilifu? Je! Roho nyingi hazitanaswa mtegoni na kuchukuliwa? Kwa kujitenga na maagizo wazi na amri za MUNGU, na kuzingatia mafundisho, akili za wengi zinajiandaa kupokea maajabu haya ya uongo.

Lazima wote tujihami na kujiweka tayari kwa pambano ambalo lazima tushiriki hivi karibuni. Imani katika Neno la MUNGU, linalosomwa kwa maombi na kutumika kwa vitendo, itakuwa ndiyo ngao yetu dhidi ya nguvu za Shetani nayo itatupatia ushindi, kwa damu ya Kristo. {1T 302.2}

## SURA YA 62

## DINI YA FAMILIA

Nimeoneshwa nafasi ya juu na ya uwajibikaji ambayo watu wa MUNGU wanapaswa kuichukua. Wao ni chumvi ya dunia na nuru ya ulimwengu, na lazima watembee kama vile Kristo alivyotembea. Watakuja kupitia dhiki kuu. Wakati wa sasa ni wakati wa vita, mitihani, majaribu, na kesi. Mwokozi wetu anasema katika Ufunuo 3:21: "Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti CHAKE cha enzi." Thawabu haipatikani kwa wale wote wanaotaka kuwa wafuasi wa Kristo, bali kwa wale wanaoshinda kama Yeye alivyoshinda. Lazima tujifunze maisha ya Kristo na tujifunze ni nini maana ya kumkiri mbele za ulimwengu. {1T 303.1}

Ili tumkiri Kristo, ni lazima tukiri kuwa Naye. Hakuna mtu awezaye kumkiri Kristo kweli kweli isipokuwa akili na roho ya Kristo iko ndani Yake. Kama mfano wa utauwa, au utambuzi tu wa Ukweli, vingekuwa daima viashirio vya kumkiri Kristo, tungeweza kusema: Njia ni pana ielekeayo uzimani, na wengi huiona na kupita huko. Lazima tuelewe ni nini maana ya kumkiri Kristo na ni wakati gani huwa tunamkana. Inawezekana kwa midomo yetu tunamkiri Kristo lakini katika matendo yetu tunamkana. Tunda la Roho linalooneshwa maishani ndiyo linaloonesha kama tumemkiri. Ikiwa tumeacha yote kwa ajili ya Kristo, maisha yetu yatakuwa ya unyenyekevu, mazungumzo yetu yatakuwa ya kimbingu, na mwenendo wetu utakuwa usio na lawama. Ushawishi wenye nguvu, utakaso wa ukweli katika nafsi, na tabia ya Kristo iliyooneshwa katika maisha, huko ndiko kumkiri Yesu. Ikiwa Maneno ya uzima wa milele yamepandwa mioyoni mwetu, matunda yatakuwa ni haki na amani. Tunaweza kumkana Kristo maishani mwetu kwa kupenda raha au kujipenda wenyewe, kwa mzaha na kwa utani, na kwa kutafuta heshima ya ulimwengu. Tunaweza kumkana katika sura yetu ya nje kwa kufanana na ulimwengu, kwa sura ya kiburi au mavazi ya gharama. Ni kwa kukesha tu kila wakati na kuvumilia kwa maombi yasiyokoma ndipo tunapoweza kuonesha katika maisha yetu tabia ya Kristo au ushawishi wa Ukweli unaotakasa. Wengi humfukuza Kristo kutoka kwenye familia zao

kutokana na roho ya papara na shauku. Watu wa aina hiyo wana kitu cha kushinda katika jambo hili. {1T 303.2}

Hali ya sasa ya familia dhaifu ya kibinadamu iliwasilishwa mbele yangu. Kila kizazi kimekuwa kikizidi kudhoofika, na magonjwa ya kila aina yanaisumbua jamii ya wanadamu. Maelfu ya wanadamu maskini wenye ulemavu, wenye miili ya ugonjwa, wenye mishipa ya fahamu iliyovunjika, na wenye akili zenye huzuni wanaishi maisha mabaya. Nguvu ya Shetani juu ya jamii ya wanadamu inaongezeka. Kama Bwana asipokuja hivi karibuni na kuziharibu nguvu zake mwovu, dunia haitakuwa na watu. {1T 304.1}

Nilioneshwa kuwa nguvu ya Shetani inatumika hasa juu ya watu wa MUNGU. Wengi waliwasilishwa mbele yangu katika hali ya mashaka, kushuku ya kukata tamaa. Udhaifu wa mwili huathiri akili. Adui mjanja na hodari hushughulikia hatua zetu na hutumia nguvu na ustadi wake katika kujaribu kutuondoa kwenye njia sahihi. Na mara nyingi sana watu wa MUNGU hawako kwenye kituo chao cha ulinzi-kesha lao, kwa hivyo hawajui ujanja wake kwani ni wajinga. Yeye hufanya kazi kwa namna inayomjificha vizuri asionekane, na mara nyingi hutimiza kusudi lake. {1T 304.2}

Ndugu wamewekeza mali katika haki za hati milki na biashara zingine, na wamewashawishi wengine kujipendeza wenyewe, ambao hawakuweza kuvumilia mahangaiko na mikiki-mikiki ya biashara hiyo. Akili zao zenye wasiwasi, zinaathiri kwa kiasi kikubwa sana miili yao iliyo na magonjwa, na kisha hujiingiza katika sononeko na machungu, ambayo huongeza kukata tamaa. Wanapoteza kujiamini kwao na kufikiria kwamba MUNGU amewaacha, na hawathubutu kuamini kwamba Yeye atakuwa mwenye huruma kwao. Nafsi hizi duni hazitaachwa chini ya uthibiti wa Shetani. Watapita katika kiza hicho na tena watafunga imani yao inayotetemeka juu ya ahadi za MUNGU; Yeye Atawaokoa na kugeuza huzuni na maombolezo yao kuwa amani na furaha. Lakini nilioneshwa kuwa, watu hawa lazima wajifunze kupitia mateso wanayopitia na wasiruhusu kujihusisha na haki milki ya biashara mbali mbali-waziache ziwe mbali nao. Hawapaswi kuruhusu hata ndugu zao kuwabembeleza na kuwadanganya ili wanase katika biashara kama hizo, kwani matarajio yao hayatatimizwa, na kisha watatupwa kwenye uwanja wa vita wa adui bila silaha ya vita. Mali ambazo zinapaswa kuwekwa kwenye hazina ya MUNGU kuendeleza masuala Yake zimepotea na zimekuwa hasara tu, kwa kuwekeza katika baadhi ya maendeleo haya ya kisasa. Ikiwa yeyote anayedai kuuamini Ukweli anajisikia yuko huru kushiriki, na ana uwezo wa kushiriki, katika haki miliki au hati miliki hizi na uvumbuzi, hawapaswi kwenda kati ya ndugu zao kanisani na kufanya uwanja wao wa mradi, lakini waende kati ya wasioamini. Usiruhusu jina lako na madai yako kama Mwaadventista yamlaghai nduguyo anayetaka kumtolea MUNGU mali yake. Bali nenda ulimwenguni, na liache kundi hilo liwekeze mali zake kwa asiyejali maendeleo ya kazi ya MUNGU

(*angalia hata huko usiwatapeli pia na Jina la Mungu likatukanwa na wasipatikane waongofu kwa Bwana tena!)* {1T 304.3}

Nilioneshwa umuhimu wa kufungua milango ya nyumba zetu na mioyo yetu kwa Bwana. Tunapoanza kufanya kazi kwa bidii kwa ajili yetu na kwa familia zetu, basi tutapata msaada kutoka kwa MUNGU. Nilioneshwa kwamba kuzingatia tu utunzaji wa Sabato na kuomba asubuhi na jioni siyo ushahidi wa Kweli kwamba sisi ni Wakristo. Miundo hii ya nje inaweza kuzingatiwa kabisa, na bado hali ya utauwa ikakosekana. Tito 2:14: "ambaye alijitoa nafsi Yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki Yake Mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema." Wale wote wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa na amri ya roho yao wenyewe, wasijiruhusu kusema kwa ukali, kwa kuudhika au bila subira. Mume na baba wanapaswa kuangalia neno hilo la harara wanalotaka kusema. Wanapaswa kuchunguza athari za maneno yao, yasije yakaacha uchungu na magonjwa. {1T 305.1}

Ulemavu na magonjwa huwaathiri hasa wanawake. Furaha ya familia kwa kiasi kikubwa inategemea sana mke na mama. Ikiwa mwanamke au mama ni dhaifu, mwenye wasiwasi, mwenye woga, na mgonjwa wa mishipa ya fahamu na anaumizwa na kuzidiwa na kazi, akili huwa na huzuni, kwa sababu inaumizwa na uchakavu wa mwili; na kisha yeye pia mara nyingi hukabiliana na mwitikio baridi kutoka kwa mumewe. Kama kila kitu hakiendi vizuri [kwa mume] kama ambavyo angetamani kiende, atamlaumu mke na mama. Mume huwa hajui kabisa masumbufu na mizigo anayokutana nayo mke, na hajui kila wakati jinsi ya kumhurumia. Hajitambui kuwa anamsaidia adui mkubwa katika kazi yake ya kubomoa. Anapaswa kwa imani katika MUNGU kuinua kiwango dhidi ya Shetani; lakini mume anaonekana kupofushwa na masilahi yake na ya mkewe. Anamtendea mkewe kwa namna iliyo tofauti, bila ya kujali. Hajui kile yeye kama mume anachofanya. Mume anafanya kazi moja kwa moja kinyume na furaha yake mwenyewe na kuharibu ari na furaha ya familia yake. Mke hujiona asiye na thamani, kisha anasononeka na kukata tamaa. Tumaini na uchangamfu vimeondoka. Anaendelea na ratiba yake ya kila siku kama mashine sababu hana namna nyingine bali kufuata desturi, hizo kazi zake ni lazima zifanyike. Kukosa kwake uchangamfu na ujasiri hudhihirika katika mzunguko wote wa familia. Kuna familia nyingi za namna hiyo miongoni mwa Watunza Sabato. Malaika hubeba habari za aibu kwenda mbinguni, na malaika anayeandika anaandika yote haya. {1T 306.1}

Mume anapaswa kuonesha shauku na kupendezwa sana na familia yake. Hasa anapaswa kuwa moyo mwororo sana kwa hisia za mke dhaifu. Anaweza kufunga mlango dhidi ya magonjwa mengi. Maneno mazuri, ya kuchangamsha, na ya kutia moyo yatathibitika kuwa bora zaidi kuliko dawa zote za uponyaji. Hizi zitaleta ujasiri kwa moyo wa mtu anayejiona si wa thamani na aliyekata tamaa, na furaha na mwanga wa jua uletwao katika familia kwa matendo ya fadhili na maneno ya kutia moyo vitalipa mara kumi juhudi iliyotumika. Mume anapaswa

kukumbuka kuwa mzigo mkubwa wa kufundisha watoto wake uko juu ya mama, kwamba anayo mengi ya kufinyanga akili zao. Hili linapaswa kutumia mazoezi ya hisia zake nyororo kabisa, na kwa uangalifu [mume] anapaswa kupunguza mizigo yake. Mume anapaswa kumtia moyo mkewe kuegemea kwenye mapenzi yake makubwa kama mume- kwake yeye mke, na kuielekeza akili yake mbinguni, ambapo kuna nguvu na amani, na mapumziko ya mwisho kwa waliochoka. Hapaswi kuja nyumbani kwake na uso uliokunjamana, bali kwa uwepo wake alete mwanga wa jua ndani ya familia, na amhimize mkewe kuangalia juu na kumwamini MUNGU. Kwa pamoja wanapoungana, wanaweza kudai ahadi za MUNGU na kuleta baraka Zake tajiri katika familia. Ukosefu wa fadhili, kulalamika, na hasira vilimuondoa Yesu kutoka kwenye makazi. Niliona kwamba malaika wa MUNGU watakimbia kutoka kwenye nyumba yenye maneno yasiyopendeza, kuudhika kirahisi na ugomvi. {1T 306.2}

Nimeoneshwa pia kuwa mara nyingi kuna kufeli/kushindwa kwa hali ya juu kwa upande wa mke. Yeye haweju jitihada za dhati katika kuidhibiti roho yake mwenyewe na kufanya nyumbani kuwa mahali pa furaha. Mara nyingi kuna kuudhika na malalamiko mabaya na yasiyo ya lazima kwa upande wake. Mume huja nyumbani kutoka kwenye kazi zake akiwa na uchovu wa kazi na kuchanganyikiwa na hukutana na maneno uso ulio na mawingu kwa kukunjamana badala ya maneno ya furaha, na yenye kutia moyo. Yeye [mme] ni binadamu tu, na mapenzi yake hupunguzwa kasi na mkewe, na hupoteza upendo wa nyumba yake, njia yake inatiwa giza, na ujasiri wake huharibiwa. Anaacha kujiheshimu mwenyewe ana hadhi/heshima ambayo MUNGU alimtaka aidumishe kama mwananamume na mume. Mume ndiye kichwa cha familia, kama Kristo alivyo kichwa cha kanisa; na njia yeyote ambayo mke ataitumia kumshawishi au kumuongoza mumewe kushuka chini kutoka kwenye nafasi ile yenye hadhi na majukumu, haimpendezi MUNGU. Ni jukumu la mke kusalimisha matakwa na mapenzi/nia yake kwa mumewe. Wote wanapaswa kuwa wanyenyekevu na kujisalimisha, lakini Neno la MUNGU linatoa kipaumbele/upendeleo kwa maamuzi/hukumu ya mume. Na haitaondoa hadhi, na mapenzi ya mke kunyenyekea kwa yule ambaye amemchagua kuwa mshauri, kiongozi na mlinzi wake. Mume anapaswa kudumisha nafasi yake katika familia yake kwa unyenyekevu na upole, lakini kwa uamuzi ulio thabiti. Wengine wameuliza swali, Je! Ni lazima niwe macho na kuweka ukomo juu yangu kwa kujizuia kila wakati? Nimeoneshwa kuwa tuna kazi kubwa mbele yetu ya kuichunguza mioyo yetu, na kujilinda sisi wenyewe kwa wivu mkubwa. Tunapaswa kujifunza pale tuliposhindwa, na kisha kujilinda sisi wenyewe kwenye eneo hilo. Lazima tuwe na udhibiti/utawala kamili juu ya roho zetu. “Mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wake wote kama kwa lijamu.” Nuru inayoangazia njia yetu, Ukweli ambao unajitambulisha kwa dhamiri zetu, utailaani na kuiharibu roho, au kuitakasa na kuibadilisha. Tunaishi karibu sana na mwisho wa majaribu hivyo

tusiridhike na kazi ya juu juu tu (nusunusu). Neema ile ile tuliyoichukulia kwamba inatosha haitutoshi sisi leo. Imani yetu lazima irejeshwe tena, na lazima tuwe kama Kristo katika mwenendo na tabia ili kuvumilia, na kufaulu kuyapinga majaribu ya Shetani. Neema ya MUNGU inatosha kwa kila mfuasi wa Kristo. {1T 307.1}

Jitihada zetu za kupinga mashambulio ya Shetani lazima ziwe za bidii na za kudumu-endelevu. Yeye hutumia nguvu na ustadi wake kujaribu kututoa katika njia sahihi. Yeye huangalia kuingia kwetu na kutoka kwetu, ili apate fursa ya kutuumiza au kutuangamiza. Adui anafanya kazi kwa mafanikio katika giza, akiumiza wale ambao hawajui ujanja wake. Asingeweza kupata mafanikio kama njia yake ya shambulio ingefahamika. Vifaa anavyotumia kutimiza makusudi yake, na kusambaza mishale yake ya moto, mara nyingi ni watu watokao katika familia zetu.
{1T 308.1}

Wale tunaowapenda wanaweza kusema au kutenda bila ulinzi, jambo linaloweza kutuumiza sana. Haikuwa nia yao kufanya hivi; lakini Shetani amekuza maneno yao na matendo yao mbele ya akili zetu, na kwa hivyo anaturusha panga kutoka kwenye podo lake kututoboa. Tunajiimarisha ili kumpinga yule ambaye tunafikiri ametuumiza, na kwa kufanya hivyo tunahimiza majaribu ya Shetani. Badala ya kuomba kwa MUNGU nguvu za kumpinga Shetani, tunaiumiza furaha yetu kwa kuitia doa pale tunapojaribu kusimamia kile tunachokiita "haki yetu." Na kwa kufanya hivyo tunampa Shetani faida maradufu. Tunatenda kutokana na hisia zetu zilizoumizwa, na Shetani hututumia kama mawakala wake kujeruhi na kufadhaisha wale ambao hawakukusudia kutuumiza. Mahitaji ya mume wakati mwingine yanaweza kuonekana kuwa hayana busara kwa mke, ila kama angekuwa mtulivu, na mwenye busara na kisha kwa makini akaangalia [wazo la mumewe] kwa mtazamo wa pili katika nuru ya kuliunga mkono kwa kadri inavyowezekana, angegundua kwamba kusalimisha njia yake mwenyewe na kujitiisha kwenye maamuzi yake, hata kama kulikuwa kuna tofautiana na hisia zake, kungewaokoa wote wawili na huzuni na kungewapa ushindi mkuu dhidi ya majaribu ya Shetani. {1T 308.2}

Niliona kwamba adui atashindana ama kwa faida au maisha ya wacha MUNGU, na atajaribu kuharibu amani yao kadri waishivyo katika ulimwengu huu. Lakini nguvu zake zina kikomo. Anaweza kusababisha tanuru liwe moto, lakini Yesu na malaika watamtazama Mkristo anayeamini, ili kusiwe na kitu kinachoweza kuteketezwa isipokuwa taka. Moto uliowashwa na Shetani hauwezi kuwa na nguvu ya kuharibu au kuumiza chuma cha kweli. Ni muhimu kufunga kila mlango kadri iwezekanavyo, dhidi ya mlango wa Shetani (weka makomeo na chuma). Ni fursa ya kila familia kuishi ili Shetani asiweze kunufaika na chochote tunachosema au kufanya, na kuzuia tusije kubomoana au kuraruana. Kila mwana familia anapaswa kuzingatia kwamba wote wana wajibu wa

kumpinga adui yetu mjanja, na kwa maombi ya dhati, bidii na imani isiyoyumba kila mmoja lazima ategemee sifa ya damu ya Kristo na kudai nguvu Yake ya kuokoa. {1T 309.1}

Nguvu za giza hukusanyika juu ya roho na kumfunga Yesu kutoka machoni petu, na wakati mwingine tunaweza kusubiri kwa huzuni na mshangao hadi wingu lipite. Misimu hii wakati mwingine huwa ni mibaya. Tumaini linaonekana kushindwa, na kukata tamaa kunatusonga. Katika saa hizi za kutisha lazima tujifunze kuamini, na kutegemea tu juu ya sifa za upatanisho, na katika hali yetu isiyo na msaada na isiyo na thamani tunajitupa juu ya sifa za Mwokozi aliyesulubiwa na aliyefufuka. Hatuwezi kamwe kuangamia ikiwa tutakuwa tunafanya hivi – kamwe! Mwanga unapoangaza kwenye njia yetu, siyo jambo kubwa kuwa na nguvu katika uwezo wa neema. Lakini kungojea kwa subira katika tumaini wakati mawingu yatufunikapo na yote tuyaonayo ni giza, inahitaji imani na unyenyekevu ambao unasababisha mapenzi yetu kumezwa katika mapenzi ya MUNGU. Tumevunjika moyo haraka sana, na tunalia kwa bidii ili jaribio liondolewe kutoka kwetu, wakati tunapaswa kuomba uvumilivu ili tuweze kustahimili na neema ili tuweze kushinda. {1T 309.2}

Bila imani haiwezekani kumpendeza MUNGU. Tunaweza kuwa na wokovu wa MUNGU katika familia zetu, lakini ni lazima tuuamini kwa ajili yake, tuuishi, na kuwa na imani endelevu na ya kudumu kwa MUNGU. Lazima tushinde hasira ya haraka na kutawala maneno yetu, na katika hili tutapata ushindi mkubwa. Tusipotawala maneno na hasira zetu, tutakuwa watumwa wa Shetani. Tutakuwa tunamtii yeye. Adui anatupeleka penye kutufanya mateka. Maneno yote ya kutatanisha na yasiyofurahisha, ya papara, ya kukasirisha ni sadaka inayotolewa kwenye mamlaka ya Shetani. Na ni sadaka ya gharama kubwa, kubwa mno kuliko dhabihu yoyote tunayoweza kumtolea MUNGU, kwani huharibu amani na furaha ya familia nzima, huharibu afya, na mwishowe ndio sababu ya kupoteza maisha ya milele ya furaha. Vizuizi ambavyo neno la MUNGU hutuwekea ni kwa masilahi yetu wenyewe. Inaongeza furaha ya familia zetu na ya wote wanaotuzunguka. Inaboresha na kusafisha ladha na shauku zetu, inatakasa maamuzi yetu, na kuleta amani ya akili, na mwishowe, uzima wa milele. Chini ya kizuizi hiki kitakatifu tutaongezeka katika neema na unyenyekevu, na itakuwa rahisi kusema yale yaliyo sawa. Hasira na kuudhika na tamaa za asili zitatiishwa. Mwokozi akaaye ndani yetu atatuimarisha kila saa. Malaika wanaohudumia hushinda kwenye makazi yetu na kwa furaha hubeba kwenda mbinguni taarifa njema kwetu katika maisha ya utauwa/Kiungu, na malaika anayechukua kumbukumbu zetu atachukua kumbukumbu kwa shangwe na furaha. {1T 310.1}

# SURA YA 63

# WIVU NA KUTAFUTA MAKOSA

Ndugu G: Huko……uliniuliza maswali kadhaa ambayo nimekuwa nikiyafikiria sana. Kutoka katika mazungumzo yangu na wewe, nina uhakika kwamba hautambui uliyotenda na jeraha ulililoleta juu ya kazi ya MUNGU. Yale niliyooneshwa kukuhusu, yalikuja wazi mbele yangu, na nimelinganisha yale ambayo nimeoneshwa kwangu hivi karibuni na Shuhuda uliochapishwa kukuhusu wewe katika Ushuhuda Na. 6, na sioni una moyo wa kuomba msamaha hata kidogo kwako kuhusu jambo hili. Hata wewe kabla ya hapa ulikuwa mshiriki, na ulitoa ushawishi wako kwa ushabiki huko Wisconsin, ambao haukuwa sawa mbele za MUNGU. {1T 311.1}

Ndugu G, kama ungefuata nuru kwa uaminifu, kamwe usingeendelea na hatua uliyoichukua. Umefuata kwa makusudi, na kwa kushupaza shingo njia yako mwenyewe, na ukitegemea uamuzi wako mwenyewe, ukakataa kuongozwa. Bwana alikutumia msaada, lakini ulikataa kuupokea. Je! mbingu ingekufanyia nini zaidi kuliko ilivyofanya? Ulipofikiria kuwa wengine walikuwa watu wa

thamani sana kuliko wewe mwenyewe, umejisikia kutoridhika na kukasirika, na umedekezwa kama mtoto anayedekeshwa. Umetamani kuheshimiwa sana, lakini umechukua hatua ya kujishusha sana katika makadirio ya wale ambao unataka kuthibitishwa. {1T 311.2}

Kabla ya hatua yako ya ushabiki ulikuwa unawaonea wivu wale walio huko Battle Creek, na umetupatia vidokezo ambavyo vitasisimua tuhuma. Umekuwa na wivu kwa mume wangu na mimi mwenyewe, na umefikiria na kusema mabaya. Wivu na tuhuma vimekuwa pamoja. Ukitaka kuonekana mwenye kiu ya kufanya kazi inayotendwa na wengine kwa weledi zaidi, umetilia mashaka wale wanaobeba mzigo wa kazi kule Batle Creek, na umetupatia vidokezo ambavyo hukuwa na uelewa navyo kabisa, na ambavyo hukuwa na uwezo wa kuvisimamia. Mzigo wa mambo hapo haukuwekwa juu yako. Nilioneshwa kuwa MUNGU asingechagua mtu mwenye akili iliyo sawa na yako, na kumwekea mizigo mizito, na kumwita kujaza nafasi yenye uwajibikaji zaidi; kwani kujithamini kungekuwa maarufu sana kiasi kwamba ingekuwa mbaya kwake na kwa watu wa MUNGU. Ikiwa ungejithamini kidogo, ungekuwa na wivu mdogo na tuhuma. {1T 311.3}

Ndugu G, kama ungekuwa umeungana kikamilifu na mwili, ukasimama katika umoja na huruma na wale ambao MUNGU ameona inafaa kuwaweka juu ya uongozi wa kazi; kama ungekubali zawadi ambazo MUNGU ameziweka kanisani, na umejitolea kabisa kuzihusu; laiti ungejiimarisha mwenyewe juu ya mambo yote ya Ukweli wa sasa kwa kudhamiria, na kuvutwa kwa kamba hata na zile za uzoefu katika kazi hiyo, wewe na watu wako mngekuwa huru kabisa na salama kutoka katika udanganyifu huu. Mngekuwa na nanga ambayo ingewashikilia. Lakini umechukua msimamo usiojulikana, ukiogopa kwamba utawaridhisha wale ambao roho yao yote ilikuwa katika kazi na kusudi la MUNGU. MUNGU anakuhitaji uwe imara na thabiti, kwa uamuzi, kwenye jukwaa na ndugu zako. MUNGU na malaika watakatifu hawakufurahishwa na hatua yako, na wasingevumilia upumbavu wako tena. Uliachwa ufuate maamuzi yako mwenyewe ambayo ulikuwa unaiheshimu sana, hata ungetamani kufundishwa, na bila wivu, hisia za ukaidi, bila kulalamika au kulaumu wengine, jifunze juu ya wale ambao wamehisi mzigo na uzito wa kazi ya MUNGU. Umekuwa ukitafuta nafasi yako ya asili, ukitafuta kuongoza na kujitangaza kuwa nje ya mwili, ambapo utakubaliwa na kukuzwa, hadi nikaona kuwa MUNGU amekupatia kusimamia na kudhihirisha hekima uliyofikiria kuwa bora kuliko wengine, na wewe uliachwa na uamuzi wako wa upofu katika ushabiki usio na busara, wa kijinga, mkali na uliowahi kuilaani Wisconsin. {1T 312.1}

Na bado nilioneshwa kuwa hukutambua ushawishi wa hatua yako ya zamani juu ya kazi hiyo, na msimamo wako wa sasa na jukumu lako kuhusu ushabiki huo. Badala ya kufanya kazi kwa nguvu zako zote kujikomboa na kuuondoa ushawishi uliotumia, ulitoka katika haya yote ukijiwekea udhuru na kuwalaumu wale

ambao MUNGU aliwatuma kwako, na kuwa tayari kuamuru, na hata kupendekeza mpango ambao Bwana angeweza kukushika kwa kutumia watumishi Wake wakifuata njia tofauti na ile waliyoifuata. Maamuzi yako yalipotoshwa na nguvu za Shetani, na ulipokuwa umefunikwa na giza ulikuwa mhukumu asiye na uwezo wa kuhimiza hatua zako nzuri. Kama ulijua hatua ambayo watumishi wa MUNGU wanapaswa kuichukua ili kukusaidia, ulijua vya kutosha kutoka ndani yako mwenyewe. MUNGU alikupatia chaguo lako, ili ufundishwe, uelekezwe kupitia watu Wake kwa njia Yake aliyoichagua, au kuendelea, kudumisha mwenendo wako wa makusudi, na kuangukia katika ushabiki wa kushangaza. {1T 312.2}

Wewe ulichagua kuwa na njia yako. Na sasa unapaswa kujilaumu mwenyewe. Unakiri kuwa mlinzi juu ya kuta za Sayuni, mchungaji wa kundi, lakini uliwaona kondoo masikini wakiwa wameraruliwa na kutawanyika na haukuwapa onyo. "Mwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi wa nyumba ya Israeli; basi, sikia Neno hili litokalo katika kinywa Changu, ukawape maonyo haya yatokayo Kwangu. Nimwambiapo mtu mbaya, Hakika utakufa; wewe usimpe maonyo, wala husemi na huyo mtu mbaya ili kumwonya, kusudi aache njia yake mbaya na kujiokoa roho yake; mtu yule mbaya atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Lakini ukimwonya mtu mbaya, wala yeye hauachi ubaya wake, wala njia yake mbaya, atakufa katika uovu wake; bali wewe umejiokoa roho yako." "Bali ukimwonya mwenye haki, kwamba yule mwenye haki asitende dhambi, tena ikiwa yeye hatendi dhambi, hakika ataishi, kwa sababu alikubali kuonywa; nawe umejiokoa roho yako."Ezekieli 3: 17-19, 21. {1T 313.1}

Dhambi ya wale wa Wisconsin ambao waliingia katika ushabiki iko juu yako, ndugu G, kuliko kwa mtu mwingine yeyote. Ulikuwa mlinzi usiye mwaminifu. Hukutambua uovu kwa kuwa hukuwa mwaminifu. MUNGU alituma walinzi Wake waaminifu ambao walisimama kwenye nuru na wangeweza kutambua uovu ili kukuonya wewe na kundi lenye makosa. Kama ungesikiliza onyo, uovu mwingi ungekuwa umeondolewa. Ushawishi wako ungehifadhiwa. Ungekuwa umesimama kando ya njia, ili ushuhuda wa watumishi wa MUNGU ufikie kundi lililopotoka. Wakosaji wasingesikia sauti ya MUNGU kupitia kwa watumishi Wake waliochaguliwa. Waliimarisha roho yao dhidi ya onyo la walinzi waliotumwa kwao, na wakajiimarisha katika njia yao isiyo ya busara, ya kujidanganya. Mchungaji hakusikia. Alikasirika kwa sababu ushabiki huu ulishughulikiwa kwa kudhamiriwa. Hakujua hatari hiyo. Hakuona haraka katika jambo hilo. Alikuwa na nuru ya kutosha ya kuamua, lakini alikuwa ameshupaza shingo sana na akawa na kushuku/mashaka kwa watumishi wa MUNGU walipompa shuhuda. {1T 313.2}

Ndugu G alitaka kungojea hadi ushabiki uanze, na iliendelea vile vile kama Shetani alivyopenda iwe, hadi yakaibuka matokeo mabaya. Hakukuwa na

udhihirisho wa busara na wenye akili kuashiria kuwa kazi hiyo ni ya MUNGU. Watumishi wa Bwana walifanya kazi yao, wakaachilia nguo zao kutoka kwa damu ya roho, na wakajiweka wazi na mbali na ushawishi uliolaaniwa, wakati wewe unabeba uzito wa kutisha wa dhambi ya ushabiki huu mbaya. Umesikitika sana, lakini huoni makosa yako mwenyewe kuhusiana na jambo hilo. Unawalaani na kuwakosoa kondoo dhaifu, kwa kukuongoza wewe nje ya njia. Mlinzi ana faida gani ikiwa hawezi kuona uovu na kutoa onyo? Mchungaji ni wa nini, ikiwa hawezi kuangalia kila hatari ili kondoo wasije wakadhurika na kuangamizwa na mbwa mwitu? Je! Ni kisingizio gani ambacho mchungaji angetoa kwa kuliacha kundi lipotee kutoka kwenye malisho ya Kweli, na kuraruliwa na kutawanyika na kuliwa na mbwa mwitu? Je! udhuru gani unaofanywa na mchungaji kwamba kondoo ndiyo amempoteza yeye? Waliacha malisho ya Kweli, na kumpeleka yeye mchungaji kando ya njia? Kusihi kama a huku kunaweza kusema kwa nguvu dhidi ya uwezo wa mchungaji huyo wa kuwatunza kondoo. Hakuna imani zaidi inayoweza kuwekwa kwake kama mchungaji mwaminifu wa kuwatunza kondoo, na kuwarudisha pale wanapoweza kupotea kutoka njia sahihi. {1T 314.1}

Aibu inayokaa juu ya kazi kuhusiana na dada A inakaa juu yako. Umechukua mazoea na uzoefu wake kuwa kitu cha maana na muhimu. Dada huyu alikuwa dhaifu, lakini kwa kiasi fulani angeweza kujaza nafasi katika familia yake na kuwaweka watoto wake pamoja; lakini alikuwa ametoka nyumbani kwake muda mfupi kabla akili yake haijaondolewa/haijapata shida. Hali ya kurudi nyuma ya wale wanaojiita watunza Sabato huko……ilikuongoza kumshawishi dada A aachane na familia yake iliyohitaji uangalizi wake, na kuja…….ili kusudi ushawishi wake usaidie Watunza Sabato huko. Msisimko usio wa afya uliashiria hatua yake. Baadhi ya wasio na uzoefu walidanganywa. Akili dhaifu ya dada A ilizidiwa, na magonjwa yalifunga haraka kwenye ubongo. Na kazi ya MUNGU imejeruhiwa sana na kushutumiwa kwa sababu ya jambo hili. Kaka A amekosewa; lazima sasa ateseke chini ya shida ya kuishi, na watoto wake lazima watawanyike. Wale ambao ushawishi wao ulisababisha matokeo haya ya kusikitisha, wana kazi ya kufanya ili kupunguza mawazo ya Kaka A, kwa kumtambua kwa uaminifu na kikamilifu, na njia ya dhambi iliyofuatwa, na kosa alilofanyiwa kwa kumwita mkewe huko, hebu kabiliana na kutangua uovu huo kwa kadri iwezekanavyo. {1T 315.1}

Laiti ungekuwa umesimama katika shauri la MUNGU, ukikiri karama zake za Roho kama zinashikilia nafasi zao katika kanisa; laiti ungekuwa katika moyo na kanuni pamoja na *Review*, iliyoanzishwa juu ya Ukweli wenye nguvu unaotumika kwa wakati huu; laiti ungekuwa unawapa chakula watu wa MUNGU katika msimu wao, ushawishi wako huko ----- na maeneo ya karibu ungekuwa tofauti sana. Ungekuwa na ushuhuda dhahiri ulionyoka wa kubeba kwa mapatano na wale ambao wanaongoza katika kazi hii kubwa. Makosa ya mtu binafsi yangekemewa. Kazi ya uaminifu ingewaleta Watunza Sabato huko, na

hivyo wasingekuwa nyuma ya makanisa mengine. Lakini wana karibu kila kitu cha kujifunza. Ungekuwa umetoa ushuhuda ulio wazi, ulionyooka, ukiwapa umuhimu wa kujitoa mhanga, na wote wakifanya sehemu katika kubeba mzigo wa kazi hiyo. Ungekuwa umewafundisha utoaji wa mpango kwa ukarimu, ukiwaongoza wote kubeba sehemu na kujitahidi kufanya hivyo ili kuendeleza kazi ya Ukweli. Msimamo wako usiojulikana (kutapatapa nk), na kuacha mambo kuwa huru na yasiyo na usimamizi huko ----- yamekuwa na ushawishi mbaya juu ya kazi huko. Upinzani uliouhisi na kuzungumza juu ya muundo wa kupanga kanisa na maendeleo ya watu wa MUNGU, umezaa matunda ambayo yanaweza kuonekana katika maeneo mengi kaskazini mwa Wisconsin. {1T 315.2}

Kama ungekuwa mfanyakazi mwenye kufanya kazi kwa haraka, kikamilifu, mwenye bidii, na unayeenda sambamba na mipango na fadhila za MUNGU, tunda lililooneshwa sasa lingekuwa na tabia tofauti kabisa. Roho zitaamua mahali pengine, iwe kwa kupinga amri za MUNGU, au iwe kwa kuunga mkono amri za MUNGU na Ukweli mwingine unaohusiana na ujumbe wa malaika wa tatu. Watu wasingekuwa wananing'inia kwenye pindo za Sayuni ili wawatindikie wengine kwa uzito ambao vinginevyo wangekuwa sawa. Lakini hakuna uaminifu ulioudhihirisha na wewe. Kazi ya moja kwa moja na yenye umakini haijafanyika. Haujalitia kanisa moyo, kwa matumizi yaliyonyooka ya Ukweli, umuhimu wa kila mtu kuwa na vitendo, kutekeleza yale anayokiri kwa mapatano na wengine; na wengi hawako tayari kujitahidi kufanya kitu ili kuuendeleza Ukweli, kama wanavyoridhika kuusikiliza Ukweli tu. Wanapenda kazi kwa maneno na kukiri, lakini siyo kwa matendo na Kweli. {1T 316.1}

Msimamo wako umewapelekea wengi ndani na nje huko----- kutolifikiria gazeti la *Review kwa kuliheshimu* kuliko vile ambavyo wangefanya, na wameuchukulia Ukweli unaopatikana ndani yake kwa wepesi tu. Kwa hiyo Review ilishindwa kuwa na ushawishi juu yao ambao MUNGU alikusudia wawe nao. Na kila mmoja amefuata mkondo wake mwenyewe, na kufanya kile kilichoonekana kuwa sawa machoni pake mwenyewe; kwa hiyo wote wako nyuma sana, na endapo kazi kubwa haitatekelezwa kwao, watapimwa kwenye mizani na kuonekana wamepungua {1T 316.2}

Nilioneshwa kuwa unatafuta kuwatupia wengine matokeo ya makosa yako, lakini wewe kama mlinzi MUNGU anakuwajibisha wewe. Wewe unalo ungamo la kinyenyekevu unalopaswa kulifanya huko………na maeneo mengine ambayo ushawishi wako umetumiwa kupingana na watumishi wa MUNGU. Kaka na dada B wameumizwa sana na ushabiki huu. Wameaibishwa kwa muda, kuhusiana na mambo ya kidunia na ya kiroho, na tulikuwa karibu tuharibiwe na udanganyifu huu wa Shetani. Ndugu G, umekimbia kwa kitambo kirefu katika ushabiki huu wa kusikitisha; mwili wako umeathiriwa na akili yako, na sasa unatafuta kuwatwika haya makosa watu wengine. Hauna hali sahihi juu ya nafasi na njia yako ya huko nyuma. Unakuwa huru kukiri mambo yaliyofanywa na wengine, na

yale ambayo hukuyafanya, lakini umeshindwa kuungama kile ulichokifanya. {1T 317.1}

Ushawishi wako huko ----- umekuwa wenye madhara. Ulikuwa unapingana na muundo/organization, na ulihubiri dhidi yake kwa njia isiyo dhahiri, siyo kwa ujasiri kama ambavyo wengine wangefanya, bali ulienda mbali kadri ulivyoweza. Kwa njia hii umeridhisha hisia zako za wivu mara nyingi, na umesababisha kutokuaminika na kukosa uhakika katika akili za wengi, wakati ambapo ungejitokeza waziwazi, ungekuwa umeeleweka wazi na ungefanya ubaya na ukorofi mdogo tu. Unaposhtakiwa kwa kutetea ujumbe uliotumwa kinyume na imani ya kanisa, haukukubali, lakini ulijulisha msimamo wako kwa mafumbo/vitendawili, na kufanya ionekane kana kwamba ndugu walikuelewa isivyo, wakati unajua kuwa shtaka lilikuwa sahihi. Kwa jinsi ulivyo sasa, kanisa haliwezi kukutegemea. Unapodhihirisha matunda ya matengenezo kamili, na kuthibitisha kuwa umeongoka, na kwamba umeshinda wivu wako, basi MUNGU atakuamini kwa kuliweka kundi Lake tena chini ya uangalizi wako. Usipofanya ukarabati kamili, wewe utakuwa na ushawishi bora kwa kukaa nyumbani kwako tu, na "kutokuwa mvivu katika biashara." {1T 317.2}

Kwa msimamo wako usio thabiti, na kwa mwenendo wako katika ushabiki huu umesababisha madhara zaidi kwa kazi ya MUNGU huko Wisconsin kuliko ulivyofanya mema katika maisha yako yote. Imani yetu imefanywa chukizo kwa watu wasioamini; jeraha, jeraha lisilopona limeipata kazi ya MUNGU, na bado wengi,na wewe mwenyewe, wanaonekana kushtuka kwamba mengi yanasemwa na kufanywa kwa ushabiki huu. Mbegu moja mbaya iliyopandwa huota mizizi, hukua, na kuzaa matunda, na hapo kuna mavuno mengi. Ubaya hustawi na hautaji utunzaji au kupaliliwa, wakati mbegu nzuri iliyopandwa inahitaji kumwagiliwa, kutunzwa kwa uangalifu, na kuwekewa mbolea kila wakati, la sivyo mimea ya thamani itakufa. Shetani, malaika wabaya, na watu waovu wanajaribu kung'oa na kuharibu mema, na unahitajika umakini mkubwa sana, na utunzaji wa kila wakati, ili uovu uweze kuishi na kushamiri. Mbegu mbaya iliyopandwa haiwezi kung'olewa kwa urahisi. Huenea, na kuchipua kila upande, ili kuiponda mbegu yenye thamani; na ikiachwa peke yake itakua na kupata nguvu, na itazima miale ya jua kutoka kwenye mimea yenye thamani, hadi itakapokuwa migonjwa na kufa. {1T 317.3}

Tulikutana na ushawishi wako huko -----. Mgawanyiko uliokuwepo pale usingekuwepo kama ungekuwa umechukua msimamo sahihi, na kupokea Neno la Bwana kupitia watumishi Wake. Lakini hili hukuweza kulifanya. Watumishi wa MUNGU walipaswa kushughulikia waziwazi njia yako mbaya. Kama wangechukua msimamo wenye nguvu, na kuwa wakali zaidi kwa hatua uliyochukua, MUNGU angewathibitisha/angewakubali. Ingekuwa bora kama ungebaki mbali kabisa……… na kwa kuwa kila wakati watumishi wa MUNGU walipoonesha ushabiki, karipio lilimpata kaka G, nawe ulinywea, ukajisikia vibaya kwamba umenyanyaswa, na uliyepuuzwa, nk. Ulifuata njia yako ya

upofu kati ya familia mbali mbali huko -----; ulijitahidi kufanya kazi kwa namna uliyotaka watu wakuhurumie, na kuunda upinzani wa hisia dhidi ya ndugu C, D, na E. Ulijisikia umefanyiwa vibaya, ulihisi kupuuzwa; ulizungumza na kutenda hisia zako, na kwa hivyo ukaunda wivu na kutokuaminika katika akili nyingi juu ya watumishi wa MUNGU ambao alikuwa amewatuma kwako. Hatua yako iliharibu nguvu ya ushuhuda wao juu ya akili zingine; lakini wengine walihisi kushukuru kwamba mwanga umekuja, na kwamba mtego wa Shetani umevunjika, na walikuwa wametoroka. Wengine walihisi ugumu, na wakaamua dhidi ya ushuhuda uliotolewa, na kulikuwa na mgawanyiko ndani ya kanisa. Unaweza kulichukua jukumu la jambo hili. Imebidi tujitahidi kufanya kazi kwa ajili ya kanisa huko kukiwa na maumivu ya roho ili kuondoa ushawishi wako mbaya na maoni uliyoyaunda. Una kazi ya kufanya huko. {1T 318.1}

Niliona kwamba wengine wamekuonea wivu sana, wakiogopa kwamba hautashughulikiwa ipasavyo, na haki yako haitatendwa na ndugu zako wanaohudumu. Watu kama hao ni lazima watoke njiani, na wawe waaminifu kukiri makosa yao wenyewe, na waaache lawama na uzito wa makosa yako juu ya kichwa chako mwenyewe. MUNGU amekusudia makosa yako yatapumzika hapo mpaka utakapoyaondoa kwa toba na ungamo la moyoni. Wale ambao wana huruma iliyopotoshwa kwako hawawezi kukusaidia. Hebu waoneshe bidii katika toba ya maasi yao wenyewe na kurudi nyuma kwao, na kukuacha wewe ujisimamie mwenyewe. Umekuwa nje kabisa ya njia, labda kama utafanya kazi ya kina, kwa kukiri makosa yako bila kuwalaumu ndugu zako, na kuwa tayari kuelekezwa, vinginevyo huwezi kuwa na sehemu na watu wa MUNGU. {1T 319.1}

Umesimama mbali na kukosa kuonyesha shauku kwa wale ambao MUNGU amewawekea mzigo mzito wa kazi Yake. Wakati mume wangu akiwa tayari na kazi na mzigo ambao watu watatu walipaswa kuushiriki, wewe umemjeruhi kwa matamshi na vidokezo, na umesaidia wengine kuleta mizigo juu yake. Ni lazima ulione hili. Haukuwa na mzigo wowote uliowekwa juu yako, lakini umekuwa na wakati wa kutafakari kusoma, kupumzika na kulala, wakati mume wangu akilazimika kufanya kazi siku baada ya siku, na mara nyingi aliendelea kwa muda mrefu mpaka usikuwa manane, na wakati mwingine wakati alipoenda kitandani ili apumzike, hakuweza kupata usingizi, bali aliweza kulia tu kwa uchungu kwa sababu ya kusudi la Ukweli, na udhalimu wa ndugu zake kwake, wakati masilahi na maisha yake yote alikuwa ameyatoa kwa kazi hiyo (alikosewa haki na wenzake). {1T 319.2}

Amekuwa na masumbufu na uwajibikaji wa kazi za ofisini (office business), uangalizi wa gazeti, na utunzaji mkubwa wa makanisa katika majimbo tofauti. Na bado baadhi ya ndugu zake wanaohudumu wamesaidia kumfadhaisha na kumuongezea maumivu kwa hatua yao isiyo ya busara. Wewe na wengine mmemwona ndugu White kama mhusika katika biashara, mtu asiyefurahia sana dini. Hao hawamjui haiba kabisa. Shetani anawadanganya wengi juu yake.

MUNGU ameona ni vema kuweka mzigo wa kazi juu yake, kumchagua ili atembee katika shuguli tofauti, na amemchagua mtu ambaye anachukulia mambo kwa unyeti/uangalifu, na anayeweza kuwahurumia wanyonge na wale waliopatwa maafa; mtu ambaye dhamiri yake ni kali, lakini aliye huru; ambaye hataifunika dhambi, bali ambaye atakuwa mwepesi kuona na kuhisi mabaya, na kuyakemea na hivyo kutoyapa nafasi, hata kama itabidi asimame peke yake kama matokeo ya msimamo huo. Hii ndiyo sababu anateseka na kuumia sana. Ndugu zake kwa ujumla hawajui chochote juu ya mizigo yake, na baadhi hawajali chochote juu ya hiyo mizigo, lakini kwa njia zao za udanganyifu na potofu wanaongeza fadhaa na mashaka yake. Mbingu inayaweka alama mambo haya. Watu ambao hawana uzito au mizigo juu yao, ambao wanaweza kuwa na masaa ya maisha rahisi ya kustarehe tu, bila chochote cha kufanya, ambao wanaweza kutafakari, na kusoma, na kuboresha akili zao, wangeweza kuonesha kiasi na ustaarabu mkubwa, na wasipitilize hivyo katika kuyachukulia mambo. Hawaoni chochote cha kuwahimiza waoneshe bidii yoyote maalum, na wako tayari kutumia masaa katika mazungumzo ya faragha. Wengine huwatazama hawa kama watu bora na watakatifu zaidi duniani. Lakini MUNGU haangalii kama binadamu atazamavyo. MUNGU huangalia moyo. Wale ambao wana nafasi hizo rahisi watalipwa kulingana na kazi zao. {1T 320.1}

Nafasi ya utumishi iliyoshikwa na mume wangu siyo ya mtu kuionea wivu, (ina changamoto nyingi). Inahitaji umakini wa karibu zaidi, utunzaji, kusumbuka na kazi ya akili. Inahitaji utekelezaji wa uamuzi mzuri na wenye busara. Inahitaji kujikana, moyo wote, na nia thabiti ya kusukuma mambo. Katika nafasi hiyo muhimu MUNGU atakuwa na mtu aliye tayari kujitosa, kuhatarisha jambo; kusimamia yaliyo ya haki, bila kujali matokeao au hasara ya kufanya hivyo; kupambana na vikwazo, bila kuyumba, hata kama maisha yatakuwa hatarini. {1T 320.2}

Uzito na jukumu la kazi hii husababisha umakini mkubwa, husababisha usiku usio na usingizi, na kumwita MUNGU kwa dhati na bidii, ari iliyochanganyika na maombi ya uchungu. Bwana amemwongoza mume wangu kuchukua nafasi moja ya uwajibikaji baada ya nyingine. Lawama na ukosoaji kutoka kwa ndugu zake huikasirisha roho yake kwa uchungu, lakini hapaswi kuyumba katika kazi hiyo. Wafanyakazi wenzake walio na mwonekano wa utauwa wanapinga kila maendeleo ambayo MUNGU anamwongoza kuyafanya, na wakati wake wa thamani lazima uchukuliwe safarini, akitoka mahali kwenda mahali, akifanya kazi zinazomletea fadhaa ya akili kati ya makanisa ili kutangua kile walichokuwa wanakisema ndugu hawa. Maskini binadamu wanaokufa wana shida! Wanakosea mambo; hawana hisia ya kweli ya kile kinachomfanya mtu kuwa Mkristo. Wale waliotengwa ili kutoa ushuhuda ulio wazi, unaochoma, na kwa hofu ya MUNGU kukemea makosa, kufanya kazi kwa nguvu zao zote kuwajenga watu wa MUNGU, na kuwaimarisha juu ya mambo muhimu ya Ukweli wa leo, mara nyingi hupokea ukosoaji na lawama badala ya huruma na msaada,

wakati wale ambao, kama wewe mwenyewe, hawajachukua uwajibikaji wowote katika kazi, wanafikiriwa kuwa wamejitoa mhanga, na wana roho ya upole. Mwenyezi Mungu hawachukulii watu hawa jinsi wanavyofikiri. Mtangulizi wa ujio wa kwanza wa Kristo alikuwa mtu wa kusema waziwazi. Yeye alikemea dhambi, na kuyaita makosa kwa majina yake hasa. Akaweka shoka kwenye shina la mti. Hivi ndivyo alivyowaambia kikundi kimoja cha watu waliodai kuwa waongofu ambao walikuja kwake kubatizwa huko Yordani: “Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja? Basi zaeni matunda yapasayo toba …… Na shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.” {1T 321.1}

Katika wakati huu wa kutisha, kabla tu ya Kristo kuja mara ya pili, wahubiri waaminifu wa MUNGU watalazimika kutoa ushuhuda ulio wa wazi zaidi kuliko ule uliobebwa na Yohana Mbatizaji. Kazi ya uwajibikaji, na iliyo muhimu ipo mbele yao; na wale wanaosema mambo laini, MUNGU hatawatambua kama wachungaji Wake. Ole wa kutisha upo juu yao. {1T 321.2}

Huu ushabiki wa ajabu huko Wisconsin (fanaticism) ulichipuka kutoka katika nadharia ya uongo ya utakatifu, iliyotetewa na ndugu K - utakatifu usiotegemea ujumbe wa malaika wa tatu, lakini ulio nje ya Ukweli wa sasa. Dada G alipokea nadharia hii ya uongo kutoka kwake, akaiendeleza yeye mwenyewe, na kwa bidii akawafundisha wengine. Hii ilikaribia kuangamiza upendo wake kwa Ukweli mtakatifu, muhimu wa wakati huu, ambao kama angeupenda na kuutii, ungekuwa nanga ya kumshikilia kwenye msingi sahihi. Lakini yeye, pamoja na wengine wengi, walifanya nadharia hii ya utakatifu au kujitakasa kuwa jambo moja kubwa, na Ukweli muhimu wa Neno la MUNGU ukawa na matokeo kidogo, ilimradi “moyo uonekane kuwa sawa tu.” Na roho maskini ziliachwa bila nanga, zikibebwa na hisia, na Shetani akaingia na kudhibiti akili na kutoa taswira ili zimfae yeye. Akili, busara na maamuzi vilidharauliwa, na kazi ya MUNGU ililalamikiwa vibaya. {1T 322.1}

Ushabiki uliojiingiza unapaswa kukuongoza wewe na wengine kuchunguza kabla ya kuamua kuhusu muonekano huu wa kujitakasa. Muonekano siyo kiashiria chanya cha tabia ya Kikristo. Wewe na wengine huwa mnaogopa kupokea lawama na ukosaji hata ule mdogo tu ambao hamkustahili ila mnatafuta kwa dhati na bidii makosa ambayo yanaonekana kuwa mabaya au yasiyofaa kwa wengine, au watu wanapowapuuza mnajisikia kujeruhiwa kwa kupitiliza. Wewe ni mkali, na mtu unayetegemea mengi kutoka kwa wengine. Umekosea na umejidanganya mwenyewe. Kama wengine wamekuhukumu kimakosa katika katika mambo fulani, hicho siyo zaidi ya kilichotarajiwa, kwa kuzingatia hali ya mambo ilivyokuwa. Unapaswa, kwa njia ya huzuni kubwa na unyenyekevu, kuomboleza kuondoka kwako kutoka kwenye kutenda kwa usahihi, jambo ambalo limetoa nafasi kwa hisia mbalimbali na mitazamo na maoni kwako; na

ikiwa katika kila jambo hutaona kwamba wewe hukuwa sahihi, basi lazima uyaacha haya mambo yapite, na wala usiweke malaumu juu ya vichwa vya wengine. Lazima ukiri makosa yako bila kumpakazia/kumlaumu mtu mwingine yeyote, na uache kulalamika kwamba ndugu zako wamekupuuza. Wamekupa umakini zaidi kuliko ulivyostahili, ukizingatia nafasi uliyonayo kwa miaka mingi. Kama hukuyaona mambo haya kama MUNGU ayaonavyo, daima ungeyachukia malalamiko unayoyatoa, na ungejinyenyekeza mwenyewe chini ya Mkono wa MUNGU. “Je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, Na kusikia kuliko mafuta ya beberu. Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi, Na ukaidi ni kama ukafiri na vinyago.” {1T 322.2}

# SURA YA 64

# UMOJA WA IMANI

Waliodai kuwa waumini huko ----- na maeneo jirani hawaji juu ili kuendana na kazi ya Bwana, na kutekeleza Ukweli wanaoukiri. Ushawishi mbaya upo juu ya kazi huko kaskazini mwa Wisconsin. Kama wote wangehisi umuhimu wa kiambatanisho cha *Review* ambacho MUNGU alipanga kiwepo wangekuwa wamefaidika na kufundishika na Ukweli unaotetewa na kiambatanisho hicho. Wangekuwa na imani iliyo sahihi, msimamo uliotulia juu ya Ukweli unaotumika kwa wakati huu, na wangelindwa na kuokolewa kutokana na ushabiki huu. Hisia za wengi zimefifia; msisimko wa uongo umeharibu utambuzi wao na macho yao ya kiroho. Ni jambo la muhimu sana sasa kwao kusonga mbele wakielewa kwamba lengo la Shetani halitimizwi kikamilifu katika kuwaangusha wale ambao amepata nguvu ya kuwadanganya. {1T 323.1}

Wakati wale ambao wameshuhudia na kupata uzoefu wa mazoezi ya uongo, wanaposhawishika juu ya kosa lao, basi Shetani hufaidika na makosa yao, na hulishikilia kosa hilo machoni pao kila wakati, ili awaogopeshe kufanya mazoezi yoyote ya kiroho, na kwa njia hii anatafuta kuangamiza imani yao ya utauwa wa kweli. Kwa sababu walidanganywa mara moja, wanaogopa kufanya juhudi kwa sala ya dhati, sala ya bidii kwa MUNGU kwa ajili ya msaada maalum na ushindi. Hao hawapaswi kumruhusu Shetani afanikishe kusudi lake, na awaongoze kwenye mtindo wa ubaridi, urasmi na kutokuamini. Lazima wakumbuke kwamba msingi wa MUNGU umesimama hakika. Hebu MUNGU na awe mkweli, na kila mtu awe muongo. Usalama wao pekee ni kuiweka miguu yao kwenye jukwaa thabiti, kuona na kuelewa ujumbe wa malaika wa tatu, kuthamini, kupenda, na kutii Ukweli. {1T 323.2}

Kristo anaongoza watu Wake, na kuwaleta katika umoja wa imani, ili wawe kitu kimoja, kama yeye alivyo umoja na Baba. Tofauti za maoni lazima zisalimishwe, ili wote wawe kwenye umoja na mwili, ili wawe na nia moja na uamuzi mmoja. 1 Wakorintho 1:10: “Basi ndugu, nawasihi, kwa Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.” Warumi 15: 5, 6: “Na MUNGU Mwenye saburi na faraja awajalie kunia mamoja ninyi kwa ninyi, kwa mfano wa Kristo Yesu; ili kwa moyo mmoja na kwa kinywa kimoja mpate kumtukuza MUNGU, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo.” Wafilipi 2:2 “ijalizeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho moja, mkinia mamoja.” {1T 324.1}

Watu wote wa MUNGU  wanapaswa kuvutiwa na kazi Yake. Kumekuwa na ukosefu wa maslahi haya kati ya ndugu huko Wisconsin. Kumekuwa pia na ukosefu wa nguvu. Wengine hudhani siyo dhambi kutumia vibaya muda wao, wakati wengine wanaopenda kazi hii muhimu ya Ukweli, hutumia vizuri wakati wao, na kwa nguvu ya MUNGU hujitahidi na kufanya kazi kwa bidii ili familia zao ziwe nadhifu na zilizotulia, na daima wana kitu pembeni cha kuwekeza katika kazi, ili watoe mchango wao katika kuisukuma kazi ya MUNGU na kuweka hazina yao mbinguni. Haitakiwi mtu mmoja awe ana starehe akitembelea bila kubeba chochote, wakati wengine wakilemewa. MUNGU  anahitaji wale wenye afya na nguvu ya mwili, kufanya kile wawezacho, na kutumia nguvu zao kwa utukufu Wake, kwani hizo nguvu  si mali  yao wao wenyewe. Wanawajibika kwa MUNGU  kwa matumizi yao ya wakati na nguvu, ambazo wamepewa kutoka mbinguni. {1T 324.2}

Wajibu wa kusaidia katika kuuendeleza Ukweli hauko juu ya matajiri tu. Wote wana sehemu ya kutenda. Mtu ambaye ametumia muda na nguvu Zake kukusanya mali anawajibika kwa namna anayoifanyia kazi mali hiyo. Ikiwa mtu ana mali na nguvu, huo ndio mtaji wake, na lazima autumie vizuri. Ikiwa atatumia masaa mengi katika uzembe na kutembelea watu bila malengo au sababu, yeye ni mvivu katika shughuli, jambo linalokatazwa na neno la MUNGU. Watu kama hao wana kazi ya kufanya ili kuzihudumia familia zao wenyewe, na kisha kuweka akiba kwa makusudi ya kusaidia wengine kwa kadri MUNGU alivyowabariki. {1T 324.3}

Hatujawekwa katika ulimwengu huu ili tujijali wenyewe, bali tunahitajika kusaidia katika kazi kuu ya wokovu, tukiiga maisha ya kujikana nafsi, kujitoa wakfu, na kuwa na maisha yenye manufaa katika Kristo. Wale wanaoyapenda maisha yao kuliko wanavyoupenda Ukweli wa MUNGU, hawatakuwa na shauku ya kutumia muda na nguvu zao kwa busara na uzuri, ili waweze kushiriki katika kueneza  Ukweli. Wengi wa vijana huko Wisconsin hawajasikia uzito wa kazi au umuhimu wa kujitoa dhabihu ili kuendeleza kazi. Hawawezi kamwe kupata nguvu mpaka wabadilishe njia yao na kuweka mkakati maalum wa kukuza Ukweli, ili roho ziweze kuokolewa. Wengine hujikana wenyewe na kudhihirisha kuvutiwa kwao na kazi na hata kudiriki kufanya kazi mara mbili, kwa sababu ya juhudi zao zisizochoka ili kuendeleza kazi wanayoipenda. Wanafanya kazi ya MUNGU kuwa sehemu yao; kama inaumia, wanaumia pamoja nayo; wakati inapofanikiwa, wanafurahi. {1T 325.1}

Mithali 3: 9, 10: "Mheshimu Bwana kwa mali yako, Na kwa malimbuko ya mazao yako yote. Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi, Na mashinikizo yako yatafurika divai mpya." Wale ambao ni wavivu wanaweza kujipooza na mawazo kwamba MUNGU hahitaji chochote kwao kwa sababu hawana kipato. Huu

hautakuwa udhuru kwao; kwa maana kama wangetumia muda wao kwa uadilifu, kama wasingekuwa wavivu katika kazi, wangekuwa wamepata kipato. Ikiwa wangejitahidi sana kupata kitu cha kuweka katika hazina ya MUNGU, njia zingefunguka kwao, na wangekuwa na kipato cha kuchangia kwenye kazi ya MUNGU, na hivyo kuweka hazina mbinguni. {1T 325.2}

## SURA YA 65

## WISCONSIN KASKAZINI

Nilipokuwa Roosevelt, New York, Agosti 3,1861, makanisa na familia tofauti yaliwasilishwa mbele yangu. Nilioneshwa ushawishi tofauti ambao umetumika, na matokeo yake yakiwa ya kukatisha tamaa. Shetani amewatumia kama mawakala wanaodai kuamini sehemu tu ya Ukweli wa sasa, wakati wakipingana na sehemu nyingine. Shetani ameweza kuwatumia kwa mafanikio zaidi kuliko wale ambao wanapigana na imani yetu yote. Njia yake ya ustadi ya kuleta makosa kupitia waumini wanaoamini nusunu tu ya ile Kweli, imewadanganya wengi, na kuvuruga na kutawanya imani yao. Hii ndiyo sababu ya mgawanyiko kaskazini mwa Wisconsin. Wengine wamepokea sehemu ya ujumbe, na kuikataa sehemu nyingine. Wengine wanaikubali Sabato na kuukataa ujumbe wa malaika wa tatu; lakini kwa sababu wameipokea Sabato wanadai ni ushirika na wale wanaoamini Ukweli wote wa sasa. Kisha wanajitahidi kuwavuta wengine pia katika giza hilo pamoja na wao wenyewe. Hawawajibiki kwa mtu yeyote. Wana imani yao wenyewe inayojitegemea. Watu hao wanaruhusiwa kuwa na ushawishi, wakati hakuna nafasi inayopaswa kutolewa kwao, bila kujali wanavyojifanya kuwa ni waaminifu. 1T 326.1

Nafsi za waaminifu zitaona mnyororo wa moja kwa moja wa Ukweli wa sasa. Wataona muunganiko wake ulio sawa, unaopatana, kiunga baada ya kiunga kikiunganisha kwa jumla, na wataushika. Ukweli wa sasa sio mgumu kueleweka, na watu ambao MUNGU anawaongoza wataungana kwenye jukwaa hili pana, lililo thabiti. Hatawatumia watu wa imani, maoni, na mitazamo tofauti, kutawanya na kugawanya. Mbingu na malaika watakatifu wanafanya kazi kuunganisha, kuleta umoja wa imani, katika mwili mmoja. Shetani analipinga jambo hili, na amedhamiria kutawanya, na kugawanya, na kuleta hisia tofauti, ili sala ya Kristo isijibiwe: “Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Yohana 17.21 Wote wawe na umoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, Nami ndani yako; hao nao wawe ndani Yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba Wewe Ndiwe uliyenituma.” Yohana 17:20, 21. Yesu alikusudia kwamba imani ya watu Wake iwe moja. Ikiwa mtu anaenda kuhubiri jambo moja, na mwingine akatofautiana naye kwa

kuhubiri jambo lingine, inawezekanaje basi wale wanaoamini kupitia neno lao kuwa kitu kimoja? Hakika kutakuwa na tofauti za hisia. 1T 326.2

Niliona kwamba ikiwa watu wa MUNGU huko Wisconsin watataka kufanikiwa, itawabidi kuchukua msimamo kuhusu mambo haya, na kwa hivyo kukata ushawishi wa wale wanaosababisha usumbufu na mgawanyiko kwa kufundisha maoni kinyume na kanisa ambao ni mwili wa Kristo. Hizo ni nyota zinazotangatanga. Wanaonekana kutoa mwanga kidogo; wanakiri na kubeba Ukweli kidogo, na hivyo kuwalaghai wasio na uzoefu. Shetani huwajaza roho yake, lakini MUNGU Hayuko pamoja nao; Roho Wake hakai ndani yao. Yesu aliomba kwamba wanafunzi Wake wawe kitu kimoja, kama Yeye alivyo mmoja na Baba, "ili ulimwengu upate kuamini kuwa Wewe umenituma." Umoja na muungano wa watu wa MUNGU wa masalio wanaoamini Ukweli hubeba ushuhuda wenye nguvu kwa ulimwengu kwamba wana Ukweli, na ni watu wa kipekee, wateule wa MUNGU. Umoja huu na mshikamano humtatiza adui, naye amedhamiria kuuondoa. Ukweli wa sasa, ulioaminiwa mioyoni na kuwa kielelezo maishani, huwafanya watu wa MUNGU kuwa wamoja, na huwapatia ushawishi mkubwa. 1T 327.1

Ikiwa wale wanaodai kuwa watunza Sabato huko Wisconsin wangetafuta kwa bidii kuwa katika umoja na maombi ya Kristo, kuwa kitu kimoja kama Yeye Kristo alivyo mmoja na Baba Yake, kazi ya Shetani ingeshindwa. Ikiwa wote wangetaka kuungana na mwili, ushabiki ambao umeleta doa kubwa juu ya kazi ya Ukweli wa sasa kaskazini mwa Wisconsin usingeibuka; kwani ni matokeo ya kujitoa katika Mwili wa Kristo, na kutafuta kuwa na imani ya asili/original, inayojitegemea, bila kujali imani ya mwili. 1T 327.2

Katika maono ya mwisho niliyopewa huko Battle Creek nilioneshwa kuwa maamuzi yasiyokuwa ya busara yalichukuliwa huko ----- kuhusiana na maono kipindi cha kupanga taasisi ya kanisa (organization). Kulikuwa na wengine huko ambao walikuwa watoto wa MUNGU, na bado walitilia shaka maono hayo. Wengine hawakuwa na upinzani, lakini hawakuthubutu kuchukua msimamo kuhusu maono hayo. Wengine walikuwa na mashaka/skeptical, na walikuwa na sababu ya kutosha kuwafanya wawe hivyo. Maono ya uongo na mazoea ya ushabiki, na matunda mabaya yaliyofuata, vilikuwa na ushawishi wa kazi ya Mungu huko Wisconsin, kuzifanya akili ziwe na wivu kwa kila kitu kinachobeba jina la maono. Vitu hivi vyote vinapaswa kuzingatiwa, na kufanyiwa kazi kwa hekima. Hakupaswi kuwepo na jaribu au masumbufu kwa wale ambao hawajawahi kuona mtu akiwa na maono, na ambao hawana ufahamu binafsi juu ya ushawishi wa maono. Watu hao (wenye maono) hawapaswi kuzuiliwa faida na manufaa ya kanisa, ikiwa mwenendo wao wa Kikristo uko sahihi, na wameonesha mwenendo mzuri wa Kikristo. {1T 327.3}

Wengine, nilioneshwa, kuwa wangeweza kupokea maono yaliyochapishwa, wakiupima mti kwa matunda yake. Wengine ni kama Tomaso mwenye mashaka; hawawezi kuamini ushuhuda uliochapishwa, wala kupokea ushahidi kupitia

ushuhuda wa wengine; lakini lazima waone na wawe na ushahidi wao wenyewe. Hao hawapaswi kuwatengwa, lakini kwa uvumilivu mkubwa, na kwa upendano wa ndugu vinapaswa kuoneshwa kwao hadi watakapothibitika katika msimamo wao au la! Ikiwa wanapigana dhidi ya maono, ambayo hawayajui; ikiwa watabeba upinzani wao hadi kupingana na yale ambayo hawana uzoefu kwayo, na wanajisikia kukasirika wakati wale ambao wanaamini kuwa maono hayo ni ya MUNGU wanazungumza juu yao katika mkutano, na kujifariji kwa mafundisho yanayotolewa kupitia maono, kanisa wanaweza kutambua kwamba hawako sahihi. Watu wa MUNGU hawapaswi kujikunja na kujisalimisha na kutoa uhuru kwa hao waliopoteza imani na uongozi. MUNGU ameweka karama kanisani ili kanisa liweze kufaidika nazo; na wakati wanaojiita waumini wa Ukweli wanapinga karama hizi, na wanapigana dhidi ya maono, roho ziko hatarini kupitia ushawishi wao, na ni wakati wa kufanya kazi nao, ili wanyonge wasipotoshwe na ushawishi wao. {1T 328.1}

Imekuwa ngumu sana kwa watumishi wa MUNGU kufanya kazi yake huko -----, kwa maana kumekuwa na kundi la watu wanaojiona kuwa wenye haki, waongeaji wanaopitiliza (chiriku), wasiotii, wakorofi, ambao wamesimama katika njia ya kazi ya MUNGU. Ikiwa wangepokelewa kanisani, wangeirarua kazi ya MUNGU vipande vipande. Wasingekuwa chini ya mwili wa Kristo, na wasingeridhika kamwe isipokuwa kama hatamu za uongozi wa kanisa zingekuwa mikononi mwao. 1T 329.1

Ndugu G alitaka kusonga mbele kwa tahadhari kubwa. Alijua kwamba kundi lililopinga maono hayo halikuwa sahihi, na kwamba hawakuwa waumini halisi katika Kweli; na kwa hivyo ili kuzuia kikwazo hiki, alipendekeza asimpokee yeyote kanisani ambaye hakuamini ujumbe wa malaika wa tatu na maono. Hii ilizuia roho chache za thamani ambazo hazikupigana dhidi ya maono. Hawakuthubutu kuungana na kanisa, wakiogopa kwamba wangejiingiza kwenye kile ambacho hawakukielewa na kukiamini vema. Na kulikuwa na wale ambao walikuwa tayari kuwachukia na kuwabagua hawa waliokuwa wenye dhamiri zenye uangalifu, na kuweka mambo mbele yao kwa nuru mbaya zaidi kwa kadri inavyowezekana. Wengine wamehisi kuhuzunishwa na kutendewa vibaya kwa sababu ya hali ya ushirika wao, na tangu mfumo uanzishwe hisia zao za kutoridhika zimeongezeka sana. Chuki kali imewatawala. 1T 329.2

Nilioneshwa kesi ya dada H. Aliwasilishwa mbele yangu akihusishwa na dada aliyetajwa kuwa na chuki kali dhidi ya mume wangu na mimi mwenyewe, na alipingana maono hayo. Roho yake ilimwongoza kupenda na kuthamini kila taarifa ya uongo kuhusu sisi na maono, na ameliwasilisha jambo hili kwa dada H. Amekuwa na roho ya uchungu na vita dhidi yangu, wakati hakuwa na ufahamu binafsi juu yangu. Alikuwa hajui kazi yangu, lakini bado amekaribisha hisia mbaya zaidi za chuki dhidi yangu, na amemshawishi dada H, na wameungana pamoja katika matamko machungu na hotuba zao kali. Mtu yule niliyeoneshwa kuhusiana na dada H alikuwa mwanamke mwenye msimamo

mkali, ujasiri na aliyejiinua katika viwango vyake binafsi. Akidhani kuwa maoni yake yalikuwa sahihi, na kwamba wengine lazima wategemee neno lake, wakati ushauri wake ulitiwa giza kwa maneno, na kudhihirisha roho ya joka aliyejipanga kupigana dhidi ya wale ambao wangekuwa wameungana katika amri za MUNGU na ushuhuda wa Yesu. 1T 329.3

Tangu dada H amekuwa huko -----, amedharau na kuchukia maono, na amehusianisha na taarifa za kusikia, kana kwamba alijua kuwa ni za kweli. Hakupinga ushawishi wowote uliohesabiwa kuniumiza. Dada huyu hakujua ya kwamba maono hayo yalikuwa ya MUNGU; hakuwa na ufahamu binafsi wa chombo kinyenyekevu; na bado ameungana na wale ambao hawajawekwa wakfu --- ili kushinikiza ushawishi mkubwa dhidi yangu. Wameimarishana kwa kupenda na kutunga taarifa za uongo zinazotoka katika vyanzo tofauti, na kwa njia hii wameimarisha chuki na ubaguzi wao. Hapawezi kuwa na umoja kati ya roho zao na roho ya jumbe ambazo Bwana anaziona kuwa zinafaa kutolewa kwa ajili ya faida ya watu Wake wanyenyekevu. Roho inayokaa ndani ya mioyo yao haiwezi kupatana na nuru iliyotolewa na MUNGU. 1T 330.1

Nafsi nyingi maskini hazijui zinachofanya. Zinaunganisha ushawishi wake na nguvu za Shetani, na kumsaidia katika kazi yake. Zinaonesha ari kubwa, bidii na unyofu katika upinzani wake wa upofu, kana kwamba kweli walikuwa wakifanya utumishi wa MUNGU kwa kupigana dhidi ya maono. Watu hawa wote wanaotaka kufanya hivyo wanaweza kujizoesha na matunda ya maono haya (kujithibithishia wenyewe). Kwa miaka kumi na saba MUNGU ameona vema kuwaacha wadumu na kuimarika dhidi ya upinzani wa majeshi ya shetani, na dhidi ya mvuto wa mawakala wa kibinadamu ambao wamemsaidia Shetani katika kazi zake. {1T 330.2}

Nilioneshwa wanawake wengine huko ambao walikuwa wanapambana na ukweli.

Mmoja aliwasilishwa mbele yangu ambaye alikubali mambo machache yahusuyo Ukweli, lakini hakwenda mbali zaidi na watu wa MUNGU wa masalio. Alionekana kujiinua mwenyewe, na akafikiri kwamba aliielewa Kweli yote. Alidai kuwa mwenye busara katika maoni yake mwenyewe, na nilioneshwa kila wakati akitazama na kurejea nyuma kwenye uzoefu wa zamani; kwa sababu alikuwa amepokea kiwango cha nuru hapo zamani, alikuwa ameinuliwa sana (ameota pembe), na akafikiria alikuwa na nuru na maarifa ya kutosha kuuelekeza mwili wote wa Kristo. Imani yake imetawanyika na kujitenga. Mawazo yake mengi kuhusu Ukweli yana makosa; na bado ni mwenye kiburi, na mwenye kujihesabia haki katika viwango vyake mwenyewe. Anapenda kuelekeza na kufundisha wengine, lakini hafundishiki. Amedharau mafundisho, na kutupilia mbali huko nyuma, mafundisho ya MUNGU kupitia watumishi Wake. Nilimwona akijikweza jinsi alivyo mwenye haki, kujitoa kwake wakfu, na maisha yake ya sala. Kama Farisayo, anaorodhesha matendo yake mema. “MUNGU, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi,

wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote.” Maombi ya yule farisayo hayakuzingatiwa; lakini mtoza ushuru maskini, ambaye aliweza tu kusema, "MUNGU anirehemu mimi mwenye dhambi," alihurumiwa na Bwana. Maombi yake yalikubaliwa, wakati maombi ya Farisayo aliyejisifu yalikataliwa. “Kwa maana kila mtu ajikwezaye atashushwa; na yeye ajishushaye atakwezwa.” 1T 330.3

Ufunuo 3:17, 18: “Kwa kuwa wanasema, ‘Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu.’ Wala Hujui ya kwamba wewe ni mnyonge,na mwenye mashaka, na masikini, na kipofu, na uchi. Nakupa shauri ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane na dawa ya macho ya kujipaka macho yako upate kuona ” 1T 331.1

Mtu huyu, ambaye sura yake niliitambua nilipomuona, niliambiwa alikuwa Bi. I. Niliona kwamba maisha yake hayakuwa na alama ya unyenyekevu ambao unapaswa kuwa tabia ya wafuasi wa Kristo. Wakati wanadamu wenye kikomo, hata kama watadai kuamini kwa kiasi gani, wanapojihesabu kuwa na haki machoni mwao, basi Yesu anawaacha wajidanganye wenyewe. Nilioneshwa kuwa mwanamke huyu amewashawishi watu wengine, na baadhi wameungana naye kuyadharau maono. Lazima wawajibike kuyajibu haya yote mbele za MUNGU ; kwa maana kila neno la kejeli dhidi ya nuru ambayo MUNGU ameona inafaa kufikishwa kwa njia aliyoichagua mwenyewe, limerekodiwa. 1T 331.2

Nilioneshwa mwanamke mwingine tena ambaye hayuko katika umoja na watu wanaoongozwa na MUNGU. Roho ya Ukweli haikai moyoni mwake, na amekuwa na pilikapilika nyingi ya kufanya kazi ambayo inampendeza adui wa kila kitu kizuri, kuvuruga na kuchanganya akili. (Nilimtambua mwanamke huyu siku ya mwisho ya mkutano; aliondoka kabla ya mkutano kuisha.) Yeye ni mzungumzaji mzuri, na yuko tayari kusikia na kueleza jambo jipya, akiangalia kile anachokiita makosa ya wengine; na kuziita fikra zake potofu za kusengenya wengine vibaya kwamba ni utambuzi. Huweka nuru badala ya giza, na giza badala ya nuru, na kujifanya, hutoa sala ndefu ili kujionesha. Anapenda kuonekana, kukubaliwa na kudhaniwa kuwa ni mwenye haki, na amewadanganya wengine. Anatamani kuwafundisha wengine, na kufikiri kwamba MUNGU anamfundisha yeye kuliko wengine. Lakini Ukweli hauna nafasi moyoni mwake. 1T 332.1

Wengine wachache walioneshwa kwangu wakiunganisha ushawishi wao na wale niliowataja, na kwa pamoja wanafanya kila wawezacho kujiondoa kutoka kwenye mwili na kusababisha vurugu; na ushawishi wao unauleta Ukweli wa MUNGU katika sifa mbaya. Yesu na malaika watakatifu wanawaleta na kuwaunganisha watu wa MUNGU katika imani moja, ili wote wawe na nia moja na uamuzi mmoja. Na wanapoletwa katika umoja wa imani, ili waweze kutazama zile Kweli muhimu za wakati huu kwa kukubaliana na kuwa na moyo

wa umoja, Shetani yuko kazini kupinga maendeleo yao. Yesu anafanya kazi kupitia vyombo Vyake ili kukusanya na kuunganisha. Shetani anafanya kazi kupitia vyombo vyake kutawanya na kugawanya. "Kwa maana, angalieni, nitatoa amri, na nitaipepeta nyumba ya Israeli katika ya mataifa yote, kama vile ngano ipepetwavyo katika ungo, lakini hata chembe moja iliyo ndogo haitaanguka chini." 1T 332.2

MUNGU sasa anawapima na kuwathibitisha watu Wake. Tabia inaendelezwa. Malaika wanapima thamani ya maadili, na kuweka kumbukumbu ya uaminifu juu ya vitendo vyote vya watoto wa wanadamu. Miongoni mwa watu wanaodai kumwamini MUNGU, mioyo yao ni michafu na ina ufisadi; lakini watajaribiwa na kuthibitishwa. MUNGU anayesoma moyo wa kila mtu, ataweka wazi mambo ya giza yaliyofichwa ambayo mara nyingi mtu hashuku kwamba yapo, vizuizi ambavyo vimezuia maendeleo ya Ukweli viondolewe, na MUNGU awe na watu safi na watakatifu watangazao amri Zake na hukumu. 1T 332.3

Nahodha wa wokovu wetu huwaongoza watu Wake hatua kwa hatua, akiwatakasa na kuwaandaa kubadilishwa, kutwaliwa kwenda mbinguni na kuwaacha nyuma wale waliojitenga na kanisa, ambao hawataki kuongozwa, na ambao wameridhika na hali ya haki yao. “Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo!” Hakuna udanganyifu mkubwa zaidi unaoweza kudanganya akili ya mwanadamu kuliko ule unaoongoza watu kujiingiza katika roho ya kujiamini wenyewe, kuamini kwamba wako sawa na wako katika nuru, wakati wanajitenga na watu wa MUNGU, na nuru wanayoipenda ni giza tu. 1T 333.1

Kundi la………. ambao wamekuwa wakijitenga kutoka katika mwili wamekuwa na roho ngumu na chungu dhidi ya wale ambao MUNGU anawatumia kama vyombo Vyake kuwaleta watu Wake wakiwa wameungana juu ya jukwaa la Kweli pekee. Roho yao inapingana na kazi ya MUNGU, na ushawishi wao umeiletea aibu kazi ya MUNGU, na imefanya imani yetu kuwa chukizo kwa watu wasioamini, na kusababisha Shetani ashangilie. Wale ambao wanatembea katika ufahamu na kufanya kazi ya kanisa na kujaribu kumtumikia MUNGU, wanaweza kukasirishwa kwa muda na wale ambao miongoni mwao hawako sahihi, na ambao nimeoneshwa kuwa ni watu wanaojihesabia haki na mafarisayo; lakini wakiwa wavumilivu, na kutembea kwa unyenyekevu mbele za MUNGU, wakiomba kwa dhati na bidii nguvu na Roho Wake, watasonga mbele, na wale ambao hawana imani katika Kweli wataachwa nyuma. 1T 333.2

Ndugu J aliwasilishwa mbele yangu, na nilioneshwa kwamba mwenendo wake haukumpendeza MUNGU. Hakuwa na utulivu au msimamo. Amekuwa akihusishwa na fundisho la “Milenia ya duniani ambayo Yesu atatawala hapa pamoja na watakatifu”, na kwa kuwa hakuna maelewano hata kidogo kati ya nadharia hii na ujumbe wa malaika wa tatu, alipoteza upendo wake na imani katika ujumbe huo, na akahisi kukasirishwa kwa sababu mengi yalikuwa yamesemwa kuhusiana na jambo hilo. Malaika wa tatu anatangaza ujumbe

mzito zaidi kwa wakazi wa dunia; na je! watu wa MUNGU waliochaguliwa hawautajali, wala kuunganisha sauti yao ili kutoa onyo hili zito? Ndugu J amedanganywa, naye anawadanganya wengine. Mada yake imekuwa kujitoa wakfu kwa Mungu, wakati moyo wake haukuwa sahihi. Akili yake imegawanyika. Hakuwa na nanga ya kumshikilia, na amekuwa akielea bila imani iliyotulia. Wakati wake mwingi umechukuliwa katika kuhusianisha taarifa moja na nyingine na hadithi zilizohesabiwa kuvuruga na kuondoa utulivu akilini mwa wale wasio na utulivu. Amekuwa na mengi ya kusema juu ya mume wangu na mimi mwenyewe, na dhidi ya maono. Amesimama katika msimamo, "Wewe ripoti tu,... nasi tutaripoti." MUNGU hakumtuma kwenye utume kama huo. Hajui ni nani ambaye amekuwa akimtumikia. Shetani amekuwa akimtumia kuvuruga akili. Ushawishi mdogo aliokuwa nao ameutumia kuathiri akili dhidi ya ujumbe wa malaika wa tatu. Kwa taarifa za uongo amewasilisha maono hayo kwa njia isiyofaa, na roho dhaifu ambazo hazikuwekwa katika Ukweli wote wa sasa zimelishwa vitu hivi badala ya chakula safi kilichopepetwa. Amedanganywa kuhusu utakaso. Ikiwa hatabadilisha njia zake, na kuwa tayari kufundishwa, na kuthamini nuru aliyopewa, basi ataachwa na MUNGU kufuata njia yake mwenyewe na kufuata hukumu yake isiyokamilika mpaka atakapoiacha imani, na hatua yake isiyo ya busara itakuwa ishara ya onyo kwa wale wanaochagua kujitenga na mwili. MUNGU atafungua macho ya roho za kweli ili zielewe kazi ya ukatili ya wale wanaotawanya na kugawanya. Yeye Atawawekea alama wale wanaosababisha mafarakano, ili kila mtu mwaminifu aponyoke kwenye mtego wa Shetani. 1T 333.3

Ndugu J alipokea kutoka kwa Mzee K nadharia ya uongo ya utakaso, ambayo iko nje ya ujumbe wa malaika wa tatu, na popote inapopokelewa huharibu upendo wa ujumbe. Nilioneshwa kuwa Mzee K alikuwa kwenye uwanja hatari. Yeye hana umoja na malaika wa tatu. Aliwahi kufurahia baraka za MUNGU zamani, lakini siyo sasa, kwa maana hajathamini na kutunza nuru ya Ukweli ambayo imeangaza katika njia yake. Ameleta nadharia ya utakaso wa Wamethodisti, na anawasilisha na kuifanya iwe ya umuhimu wa hali ya juu. Na Kweli takatifu zinazohusika kwa wakati huu zimefanywa kuwa na matokeo kidogo. Amefuata nuru yake mwenyewe, na amekuwa akizidi kuwa gizani zaidi, na kwenda mbali zaidi na Ukweli, kiasi kwamba umekuwa na ushawishi mdogo kwake. Shetani ameidhibiti akili yake, na ameijeruhi sana kazi ya Ukweli huko kaskazini mwa Wisconsin. 1T 334.1

Ilikuwa nadharia hii ya utakaso ambayo dada G aliipokea kutoka kwa Mzee K, na ambayo alijaribu kuifuata, ndiyo iliyompelekea katika ushabiki huo mbaya. Mzee K ameshangaza na kuchanganya akili nyingi na nadharia hii ya utakaso. Wote wanaoikumbatia wanapoteza kwa kiwango kikubwa nia yao ya upendo katika ujumbe wa malaika wa tatu. Mtazamo huu wa utakaso ni nadharia inayoonekana kuwa nzuri sana. Inaosha kwa chokaa na kuzifunika roho maskini zilizoko gizani na katika makosa na kiburi. Huzipatia mwonekano wa kuwa

Wakristo wazuri, na wenye utakatifu, wakati mioyo yao imeharibika kwa ufisadi. Ni nadharia ya amani na salama, ambayo haifichui uovu na kuonya na kukemea makosa. Inaponya jeraha za binti za watu wa MUNGU juu juu tu, huku ikisema: Amani, amani, wakati hakuna amani. Wanaume na wanawake wenye mioyo michafu wanajivika vazi la utakaso, na kuonekana kama mifano kwa kundi, wakati wao ni mawakala wa Shetani, anayewatumia kushawishi na kudanganya roho za kweli katika njia, ili wasisikie nguvu hiyo na umuhimu wa zile Kweli zilizotangazwa na malaika wa tatu. 1T 335.1

Mzee K ametazamwa kama kielelezo, wakati ameijeruhi kazi ya MUNGU. Maisha hayakuwa bila lawama. Njia zake hazijafuata sheria takatifu ya MUNGU, au maisha ya Kristo yasiyo na doa. Asili yake ya uovu haijasalimishwa; na bado anaongea sana juu ya utakaso, na kwa hivyo hudanganya wengi. Nilielekezwa kwenye kazi zake za zamani. Ameshindwa kuzileta roho katika Ukweli, na kuziimarisha juu ya ujumbe wa malaika wa tatu. Anawasilisha nadharia ya utakaso kama jambo lenye umuhimu wa hali ya juu, wakati njia inayopitisha baraka za MUNGU anaipatia umuhimu mdogo. "Uwatakase kwa ile Kweli, Neno Lako ndiyo Kweli." Ukweli wa sasa, ambao ndio njia, hauzingatiwi, bali unakanyagwa chini ya miguu. Watu wanaweza kutangaza, Utakatifu! utakatifu! utakaso! utakaso! Kujitoa wakfu! Kujitoa wakfu! na bado hawajui kwa uzoefu kile wanachozungumza kuliko yule mwenye dhambi na tabia zake mbaya. MUNGU hivi karibuni atalichana vazi hili linalodaiwa kuwa ni vazi la utakaso ambalo wale wenye mawazo ya mwilini wamelivaa ili kuficha kilema cha roho. 1T 335.2

Kumbukumbu ya uaminifu ya matendo ya watoto wa wanadamu imeandikwa. Hakuna kitu kinachoweza kufichika katika jicho la aliye juu na Mtakatifu. Wengine hufuata hatua inayopingana moja kwa moja na sheria ya MUNGU, na kisha, ili kuficha njia yao ya dhambi, wanajifanya kuwa wamejitoa wakfu kwa MUNGU. Madai haya ya utakatifu hayadhihirishwi katika maisha yao ya kila siku. Hayana mwelekeo wa kuinua akili zao, na kuwaongoza "wajiepushe na kila aina ya uovu." Tumefanywa kuwa tamasha kwa ulimwengu, kwa malaika, na kwa wanadamu. Imani yetu inatukanwa/inakashifiwa kwa sababu ya mwenendo potovu wa wenye nia ya mwili. Wanakiri sehemu ya Ukweli, ambayo inawapa ushawishi, wakati hawana umoja na wale wanaoamini na kuungana juu ya ukweli wote. Je, upi umekuwa ushawishi wa mzee K? Je! yapi yamekuwa matunda ya kazi yake? Ni wangapi wavutwa na kuimarishwa juu ya Ukweli wa sasa? Ameleta wangapi katika umoja wa imani? Hajakusanyika pamoja na Kristo. Ushawishi wake umekuwa wa kutawanya. Kuna mapungufu katika mahubiri yake, na waongofu wake wanakosa kile ambacho kitathibitisha uimara na ulinzi wao katika siku ya hasira ya MUNGU. Mahubiri yake yanakosa chumvi, na ladha. Haleti nafsi zilizobadilishwa kikamilifu kuuelekea Ukweli, akizitenga na ulimwengu, na kuziunganisha na watu wa pekee wa MUNGU. Waongofu wake

hawana nanga ya kuwashikilia, hivyo huteleza huku na huko, hadi wengi wao kuishia kuchanganyikiwa na kupotea ulimwenguni. 1T 336.1

Mzee K haijui roho aliyonayo. Anaunganisha ushawishi wake na jeshi la joka ili kuwapinga wale wanaoshika amri za MUNGU, na kuwa na ushuhuda wa Yesu. Ana vita ngumu mbele yake. Kwa kadri Sabato inavyohusika, anachukua nafasi sawa na watunza Sabato wa Kibaptisti. Itenge Sabato na ujumbe, na itapoteza nguvu yake; lakini inapounganishwa na ujumbe wa malaika wa tatu, nguvu inayowasadikisha wasioamini na makafiri inakuwepo, na kuwaleta wakiwa na nguvu za kusimama, kuishi, kukua, na kushamiri/kufanikiwa katika Bwana. Ni wakati wa watu wa MUNGU huko Wisconsin kupata msimamo wao. "Ni akina nani watakaokuwa upande wa Bwana?" hilo lapaswa kusikika kutoka kwa waaminifu, wazoefu kila mahali. MUNGU anahitaji watoke na kujiondoa kutoka kwenye vishawishi mbali mbali ambavyo vingewatenganisha wao kwa wao na kutoka kwenye jukwaa kuu la Ukweli ambalo juu yake MUNGU analeta watu wake. 1T 337.1

Nilioneshwa juu suala la Bw. L. Ana mengi ya kusema juu ya utakaso, lakini amejidanganya mwenyewe, na kuwadanganya wengine. Utakaso wake unaweza kudumu anapokuwa kwenye mkutano, lakini hauwezi kuhimili jaribu. Utakatifu wa Biblia hutakasa maisha; lakini moyo wa L haujatakaswa. Uovu upo moyoni, na unatendwa maishani, na maadui wa imani yetu wamekuwa na nafasi ya kuwashutumu watunza Sabato. Wanahukumu mti kwa matunda yake. 1T 337.2
2 Wakorintho 4:2 "Lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika,wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya Neno la MUNGU na uongo; bali kwa kuidhihirisha iliyo Kweli twajionesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za MUNGU. " 1T 337.3

Wengi huenda kinyume kabisa na hilo andiko hapo juu. Wanatembea kwa hila, na kulibeba Neno la MUNGU kwa udanganyifu. Hawaonyeshi mfano wa Ukweli katika maisha yao. Wana mazoezi maalum juu ya utakaso, huku wakilitupa Neno la MUNGU nyuma yao. Wanaomba utakaso, wanaimba utakaso, na kupiga kelele juu ya utakaso. Wanaume wenye mioyo iliyoharibika hujitangaza kuwa hawana hatia, na wanakiri kuwa wamewekwa wakfu; lakini huu siyo ushahidi kwamba wako sahihi. Matendo yao yanawashuhudia. Dhamiri zao zinawaka moto, lakini siku ya MUNGU inakuja, na kazi ya kila mtu itaonekana wazi, ya kwamba ni ya aina gani. Na kila mtu atapokea sawasawa na matendo yake. 1T 338.1

Malaika alisema, kama alivyoelekeza kwa L: "Una nini wewe kuitangaza sheria yangu, na kuliweka agano langu kinywani mwako? Maana wewe umechukia maonyo, na kuyatupa Maneno Yangu nyuma yako. Ulipomwona mwivi, ulikuwa radhi naye, ukashirikiana na wazinzi. Umekiacha kinywa chako kinene mabaya, na ulimi wako kutunga hila." MUNGU atautawanya na kuufutilia mbali ushawishi huu wa kugawanya, na atawaweka huru watu Wake, ikiwa wale wanaodai kuuamini Ukweli wote watakuja kumsaidia Bwana. 1T 338.2

Hakuna utakaso wa Biblia kwa wale ambao walitupa sehemu ya Ukweli nyuma yao. Kuna nuru ya kutosha iliyotolewa katika Neno la MUNGU, kwa hiyo hakuna mtu anayehitaji kukosea. Ukweli umeinuliwa sana hata kupendwa na akili kubwa, na bado ni rahisi sana kiasi kwamba mtoto wa MUNGU mnyenyekevu, dhaifu kabisa anaweza kuuelewa na kuelekezwa nao. Wale ambao hawaoni uzuri ulioko katika Ukweli, ambao hawajali umuhimu wa ujumbe wa malaika wa tatu, hawatakuwa na udhuru; kwani Ukweli uko wazi. 1T 338.3

2 Wakorintho 4:3,4: "Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao MUNGU wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu Wake Kristo, aliye sura MUNGU, kuwaangazia. ” 1T 338.4

Yohana 17:17, 19: "Uwatakase kwa ile Kweli. Neno Lako ndiyo Kweli." "Na kwa ajili yao najiweka wakfu Mwenyewe, ili hao watakaswe katika Kweli." 1T 339.1
1Petro 1:22: "Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii Kweli, hata kuufikiria upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo." 1T 339.2

1 Wakorintho 7:1: "Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha MUNGU." 1T 339.3

Wafilipi 2: 12-15: “Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana Ndiye MUNGU atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema. Yatendeni mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano, mpate kuwa wana wa MUNGU wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu" 1T 339.4

Yohana 15:3: "Ninyi mmekuwa safi kwa sababu ya lile Neno nililowaambia." 1T 339.5

Waefeso 5: 25-27: “ Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika Neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.” 1T 339.6

Hapa kuna utakaso wa Biblia. Siyo tu maonesho, au kazi ya nje na usanii. Ni utakaso unaopokelewa kupitia njia ya Ukweli. Ni Ukweli uliopokelewa moyoni, na uliofanyiwa kazi halisi maishani. 1T 339.7

Yesu, anayechukuliwa kama mwanadamu, alikuwa mkamilifu, lakini alikua katika neema. Luka 2:52: "Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo,

akimpendeza MUNGU  na wanadamu." Hata Mkristo mkamilifu kabisa anaweza kuongezeka kila wakati katika maarifa na upendo wa MUNGU. 1T 339.8

2 Petro 3:14, 18: "Kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake,." “Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una Yeye sasa na hata milele. Amina. ” 1T 340.1

Utakaso siyo kazi ya muda mfupi, saa, au siku. Ni ukuaji endelevu katika neema. Hatujui hata siku moja kwamba pambano letu litakuwa kali kiasi gani. Shetani anaishi, na anafanya kazi, na kila siku tunahitaji kulia kwa bidii kwa MUNGU  kwa ajili ya msaada na nguvu za kumpinga Shetani. Kadri Shetani anavyotawala tutakuwa na ubinafsi wa kusalimishwa, vikwazo vya kushinda, na hakuna kusimama njiani, hakuna namna ambayo tunaweza kuja na kusema tumefikia ukamilifu. 1T 340.2

Wafilipi 3:12: "Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu." 1T 340.3

Maisha ya Kikristo ni mwendo endelevu. Yesu anakaa kama msafishaji na mtakasaji wa watu Wake; na picha Yake inapoonekana kikamilifu ndani yao, wanakuwa wakamilifu na watakatifu, ambao wameandaliwa kwa ajili ya kubadilishwa. Kazi kubwa inahitajika kwa Mkristo. Tunahimizwa kujitakasa na uchafu wote wa mwili na roho, tukikamilisha utakatifu katika kumcha MUNGU. Hapa tunaona mahali ilipo kazi kubwa. Kuna kazi ya kila wakati kwa Mkristo kufanya. Kila tawi katika Mzabibu lazima lipate uzima na nguvu kutoka kwa Mzabibu huo, ili kutoa matunda. 1T 340.4

## SURA YA 66

## NGUVU ZA SHETANI

Mwanadamu aliyepotea ni mateka halali wa Shetani. Utume wa Kristo ilikuwa kumwokoa kutoka kwenye nguvu za mshitaki wake mkuu. Mwanadamu ameelekezwa kufuata matakwa ya Shetani, na hawezi kufanikiwa kumpinga adui huyu mbaya sana isipokuwa Kristo, mshindi hodari, akae ndani yake, akiongoza tamaa zake, na kumtia nguvu. MUNGU pekee Ndiye awezaye kuzishinda nguvu za Shetani. Akizunguka huku na kule ulimwenguni, na akitembea juu, chini na ndani yake. Yeye hayuko mbali na kituo cha ulinzi wake hata kwa wakati hata mmoja, kwa sababu ya hofu ya kupoteza nafasi ya kuharibu roho za watu. Ni muhimu kwamba watu wa MUNGU  walielewe hili, ili waweze kuepuka mitego yake. Shetani anaandaa udanganyifu wake, ili katika

kampeni yake ya mwisho dhidi ya watu wa MUNGU wasiweze kuelewa kuwa ndiye yeye. 2 Wakorintho 11:14: “Wala si ajabu; kwa maana Shetani mwenyewe hujigeuza kuwa malaika wa nuru.” Wakati roho zingine zilizodanganywa zinamtetea kwamba hayupo, yeye huwachukua mateka, na anafanya kazi kupitia kwao kwa kiwango kikubwa sana. Shetani anajua vizuri kuliko watu wa MUNGU nguvu ambayo wanaweza kuwa nayo juu yake wakimuelekea na kumfuata Kristo. Wanapoomba kwa unyenyekevu kwa msaidizi mwenye nguvu kwa ajili ya msaada, hata muumini dhaifu kabisa wa Ukweli, akimtegemea Kristo kikamilifu, anaweza kufanikiwa kumshinda Shetani na jeshi lake lote. Yeye ni mjanja sana hawezi kuja wazi wazi ama kwa ujasiri akiwa na majaribu yake; kwa sababu hapo nguvu za Mkristo aliyesinzia zingeamshwa, na angemtegemea Mkombozi hodari na shujaa. Lakini huja bila kutambuliwa, na hufanya kazi kwa kujificha kupitia watoto wa uasi wanaokiri utauwa kwa mdomo. {1T 341.1}

Shetani atatumia kwa kiwango kikubwa cha uwezo wake kuwasumbua, kuwajaribu, kuwanyanyasa na kuwapotosha watu wa MUNGU. Yeye aliyethubutu kukabili, na kumjaribu, na kumdhihaki Bwana wetu, na ambaye alikuwa na uwezo wa kumshika mkononi mwake na kumpeleka juu ya kilele cha hekalu, na hadi juu ya mlima mrefu sana, atatumia nguvu zake kwa kiwango cha ajabu, juu ya kizazi cha sasa, walio duni kwa hekima ya Bwana wao, na ambao ni wajinga/hawajui udanganyifu na nguvu za Shetani. Kwa njia ya kushangaza ataathiri miili ya wale ambao kwa asili wamependa kufanya maagizo yake. Shetani hufurahi kwamba anachukuliwa kama hadithi ya uongo. Anapopuuzwa, na kuwakilishwa na mfano wa kitoto, au kama mnyama mwenye mapembe, humfaa vema. Anafikiriwa duni sana kiasi kwamba akili za wanadamu hazijajiandaa kabisa kwa mipango yake iliyowekwa kwa busara, na karibu kila mara hufaulu vizuri. Ikiwa nguvu na ujanja wake ungeeleweka vyema, hakika wengi wangekuwa tayari kumshinda kwa mafanikio. {1T 341.2}

Sote tunapaswa kuelewa kwamba Shetani wakati mmoja alikuwa malaika wa viwango vya juu. Uasi wake ulimfungia nje ya mbinguni, lakini haukuharibu nguvu zake na kumfanya mnyama. Tangu anguko lake amegeuza nguvu zake kuu dhidi ya serikali ya mbingu. Amekuwa akiongea kwa ustadi zaidi, na amejifunza njia iliyofanikiwa zaidi ya kuja kwa watoto wa wanadamu na majaribu yake. {1T 342.1}

Shetani amebuni hadithi anazotumia kudanganya. Alianza mbinguni kwa kupigana dhidi ya msingi wa serikali ya MUNGU, na tangu anguko lake ameendeleza uasi wake dhidi ya sheria ya MUNGU, na ameleta umati wa wale wanaodai kuwa Wakristo kuikanyaga chini ya miguu yao amri ya nne ambayo inawaleta watu karibu sana na MUNGU, aliye hai. Amevunja Sabato ya asili ya Amri kumi na kuweka mbadala wa moja ya siku za juma za kazi. {1T 342.2}

Uongo mkuu wa asili ambao alimwambia Hawa katika bustani ya Edeni, "Hakika hamtakufa," lilikuwa hubiri la kwanza kuwahi kuhubiriwa juu ya kutokufa kwa roho. Hubiri hilo likavishwa taji ya mafanikio makubwa, na matokeo mabaya yakafuata. Adui ameweza kuzishawishi akili za watu kulipokea hubiri hilo kama ukweli, na wahubiri wengi hulihubiri, kuliimba, na kuliomba. {1T 342.3}

Kutokuwepo kwa Shetani halisi ulimwenguni, na kuwepo kwa mlango wa rehema baada ya kuja kwa Kristo, zimekuwa hadithi maarufu sana. Maandiko yanatangaza wazi kuwa hatima ya kila mtu imewekwa milele katika kuja Kwake Bwana mara ya pili. Ufunuo 22:11, 12: "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa. Tazama, Naja upesi, na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo..” {1T 342.4}

Shetani ametumia fursa ya hekaya hizi maarufu kujificha. Anakuja kwa watu walio maskini, waliodanganywa kupitia njia ya kisasa ya umizimu ndani yake, ambayo haitoi mipaka kwa wenye nia ya mwili, na inapochukuliwa, hutenganisha familia, huunda wivu, chuki, na hutoa uhuru kwa tabia mbaya zenye kufisha zaidi. Ulimwengu unafahamu kwa kiwango kidogo juu ya ushawishi mbaya wa umizimu (Spiritualism). Pazia liliondolewa, na mengi ya kazi yake ya kutisha yalifunuliwa kwangu. Nilioneshwa wengine ambao wamekuwa na uzoefu wa mambo ya kiroho, na tangu wakati huo wameachana nayo, ambao hutetemeka wanapotafakari jinsi walivyokaribia uharibifu kabisa. Walikuwa wamepoteza udhibiti wao wenyewe, na Shetani aliwafanya wafanye kile walichokichukia. Lakini hata wao wana wazo dhaifu tu la umizimu kama lilivyo. Wachungaji walioongozwa na Shetani wanaweza kumvalisha hayawani huyu mbaya sana mavazi fulani, na kuficha kilema chake, na kumfanya aonekane mzuri kwa wengi. Lakini anakuja moja kwa moja kutoka kwa ukuu wake wa kishetani, kwa kudai haki ya kuwadhibiti wote wanaohusiana naye, kwani wamejitosa kwenye uwanja uliokatazwa, na wamepoteza ulinzi wa Muumbaji wao. {1T 343.1}

Baadhi ya roho masikini ambazo zimevutiwa na mafundisho ya walimu wa uongo na umizimu, na kujisalimisha kwenye ushawishi wake, baadaye zinafunuliwa tabia yake mbaya, na kutamani kuikimbia, lakini zisiweze. Shetani anazishikilia kwa nguvu zake, na hayuko tayari kuziachia huru. Anafahamu kuwa roho hizi ni mateka wake, na ameziweka chini ya udhibiti wake maalum, lakini ikiwa watu hawa watafanikiwa kujiweka huru kutoka katika nguvu zake, hataweza kuwaaminisha tena umizimu, na kujiweka wenyewe chini ya udhibiti wake. Njia pekee ya roho hizi maskini kumshinda Shetani, ni kutambua utofauti kati ya ukweli safi wa Biblia na hekaya. Wanapokubali madai ya Ukweli, wanajiweka mahali ambapo wanaweza kusaidiwa. Wanapaswa kuwasihi wale ambao

wamekuwa na uzoefu wa kiroho, na ambao wana imani katika ahadi za MUNGU, kumsihi Mkombozi Mwenye nguvu kwa niaba yao. Litakuwa pambano la karibu. Shetani atawaimarisha malaika zake wabaya ambao wamewadhibiti watu hawa; lakini ikiwa watakatifu wa MUNGU kwa unyenyekevu wa kina wanafunga na kuomba, maombi yao yatashinda. Yesu ataagiza malaika watakatifu kumpinga Shetani, na atarudishwa nyuma na kuzivunja nguvu zake kutoka kwa watu waliotaabika. Marko 9:29: "Akawaambia, Aina hii haiwezi kutoka kwa neno lolote, isipokuwa kwa kufunga na kuomba." {1T 343.2}

Huduma maarufu haziwezi kufanikiwa kuupinga umizimu. Hawana chochote cha kuwalinda watu wao kutoka katika ushawishi wake mkubwa. Matokeo mengi ya kusikitisha ya umizimu yatakaa juu ya wachungaji wa kizazi hiki; kwa sababu wameikanyaga Kweli chini ya miguu yao, na badala yake wamependelea simulizi za hadithi. Mahubiri ambayo Shetani alimhubiria Hawa juu ya kutokufa kwa roho- "Hakika hamtakufa" - hawa watumishi wamerudia kutoka kwenye mimbari; na watu wanayapokea kama Ukweli safi wa Biblia. Ni msingi wa umizimu. Hakuna mahali Neno la MUNGU linapofundisha kwamba roho ya mwanadamu haiwezi kufa. Kutokufa ni sifa ya MUNGU pekee. 1 Timotheo 6:16: “Ambaye Yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una Yeye hata milele. Amina.” {1T 344.1}

Neno la MUNGU, linaloeleweka vyema na kutendewa kazi, ni kinga dhidi ya roho za uongo. Jehanamu inayowaka milele ikihubiriwa kutoka kwenye mimbari, na kuwekwa mbele za watu, haitendei haki tabia ya wema wa MUNGU. Humwonesha kama mdhalimu na jeuri katika ulimwengu. Mafundisho haya yaliyoenea yamegeuza maelfu ya ulimwengu, kutokuamini, na kumkana MUNGU. Neno la MUNGU liko wazi. Ni mnyororo safi na ulionyooka wa Ukweli, na litathibitisha kuwa nanga kwa wale ambao wako tayari kulipokea, hata ikiwa watalazimika kuzitoa kafara hekaya zao za kupendeza. Litawaokoa kutoka kwenye udanganyifu mbaya wa nyakati hizi za hatari. Shetani ameongoza akili za wachungaji wa makanisa tofauti kushikamana kwa nguvu na makosa yao maarufu, kama alivyowaongoza Wayahudi katika upofu wao kushikamana na dhabihu zao, na kumsulubisha Kristo. Kukataliwa kwa nuru na Ukweli huwaacha watu mateka na raia wa udanganyifu wa Shetani. Kadri wanavyoikataa nuru kubwa, ndivyo watakavyojiliwa na nguvu ya udanganyifu na giza juu yao. {1T 344.2}

Nilioneshwa kuwa watu wa Kweli wa MUNGU ni chumvi ya dunia na nuru ya ulimwengu. MUNGU anahitaji kutoka kwao maendeleo endelevu katika ujuzi wa Ukweli, na katika njia ya utakatifu. Ndipo watakapouelewa ujio wa Shetani, na kwa nguvu ya Yesu watampinga. Shetani ataliita jeshi lake la malaika ili

wamsaidie kupinga maendeleo ya roho hata moja, na, ikiwezekana, kuipokonya roho hiyo kutoka katika mkono wa Kristo. {1T 345.1}

Niliona malaika wabaya wakipigania roho za watu, na malaika wa MUNGU wawakipinga. Vita hii ilikuwa kali. Malaika wabaya walikuwa wakiharibu anga na ushawishi wao wenye sumu, na kusongamana juu ya roho hizi ili kupumbaza hisia zao. Malaika watakatifu walikuwa wakitazama kwa ujasiri na wakingojea kuyarudisha majeshi ya Shetani. Lakini si kazi ya malaika wazuri kudhibiti akili za wanadamu dhidi ya mapenzi yao wenyewe. Ikiwa wanajisalimisha kwa adui, na kutofanya bidii ya kumpinga, basi malaika wa MUNGU hawana la kufanya zaidi ya kulizuia jeshi la Shetani, kwamba wasiharibu, hadi nuru nyingine itolewe kwa wale walio hatarini, kuwahamasisha kuamka na kuangalia mbinguni kwa ajili ya msaada wao. Yesu hataamuru malaika watakatifu kuwaondoa wale ambao hawajitahidi kujisaidia. {1T 345.2}

Ikiwa Shetani ataona kuwa yuko katika hatari ya kupoteza roho moja, atajitahidi kwa bidii kuidhibiti roho hiyo. Na pindi mtu huyo anapoamshwa katika hatari hiyo, na, kwa shida na bidii, akamwangalia Yesu kwa nguvu, Shetani anaogopa kwamba atampoteza mateka wake, hivyo huita jeshi la malaika zake ili kuizingira roho hiyo dhaifu, na kuunda ukuta wa giza karibu naye, ili nuru ya mbinguni isije kumfikia. Lakini ikiwa yule aliye katika hatari atavumilia, na katika hali yake ya kutokuwa na msaada akajitupa juu ya sifa ya damu ya Kristo, Mwokozi wetu anayasikiliza maombi ya dhati ya imani, na anatuma msaada wa wale malaika ambao wana nguvu kubwa ya kumuokoa. Shetani hawezi kuvumilia mbele za mpinzani wake Mwenye nguvu, maana anaogopa na kutetemeka mbele ya nguvu na utukufu Wake. Kwa sauti ya maombi ya dhati, jeshi lote la Shetani linatetemeka. Adui anaendelea kuita vikosi vya malaika wabaya kutimiza lengo lake. Na wakati malaika, wenye nguvu zote, waliovaa silaha za kimbingu, wanapokuja kumsaidia mtu huyu aliye dhaifu na anayeshawishiwa vikali, Shetani na jeshi lake hurudi nyuma, wakijua kabisa kuwa wameshindwa vita. Mateka wa hiari wa shetani ni waaminifu, wenye bidii, na wameungana kuwa kitu kimoja. Na ingawa wanachukiana na kupigana wao kwa wao, lakini wanaboresha kila fursa ili kuendeleza masilahi yao ya kawaida. Lakini Kamanda mkuu mbinguni na duniani amezipa kikomo nguvu za Shetani-ameziwekea nguvu zake mipaka. {1T 345.3}

Uzoefu wangu umekuwa wa ajabu, na kwa miaka nimesumbuliwa na majaribu ya kipekee ya akili. Hali ya watu wa MUNGU, na uhusiano wangu na kazi ya MUNGU, mara nyingi umeniletea uzito wa huzuni na kuvunjika moyo kusikoweza kuelezeka. Kwa miaka mingi nimeangalia kaburi kama mahali pazuri pa kupumzika. Katika maono ya mwisho nilimuuliza malaika aliyekuwa pamoja nami, kwanini niliachwa kupata shida ya akili na mawazo yaliyonitatiza, na mara nyingi nilitupwa kwenye uwanja wa vita wa Shetani. Niliomba kwamba

ikiwa ni lazima niunganishwe kwa karibu sana na kazi ya Ukweli, basi nitolewe kwenye majaribu haya mazito. Kuna nguvu na uwezo katika malaika wa MUNGU, nani niliomba niweze kulindwa. {1T 346.1}

Ndipo maisha yetu ya zamani yalipowasilishwa mbele yangu, na nilioneshwa kwamba Shetani alikuwa ametafuta kwa njia kadhaa kuharibu manufaa ya utumishi wetu; na kwamba mara nyingi alikuwa ameweka mipango yake ya kutuondoa kwenye kazi ya MUNGU; alikuja kwa njia tofauti, na kupitia mawakala tofauti, kutimiza malengo yake; lakini kupitia huduma ya malaika watakatifu alikuwa ameshindwa. Niliona kwamba katika safari yetu kutoka mahali kwenda mahali, alikuwa ameweka malaika wake wabaya mara kwa mara katika njia yetu ili kusababisha ajali ambazo zingeharibu maisha yetu; lakini malaika watakatifu walitumwa juu ya nchi kutuokoa. Ajali kadhaa zimemuweka mume wangu na mimi katika hatari kubwa, na kuhifadhiwa kwetu kumekuwa kwa ajabu. Niliona kwamba tumekuwa vyombo maalum vya mashambulio ya Shetani, kwa sababu ya kupendezwa kwetu kazi ya Mungu na uhusiano na kazi ya MUNGU. Kadri nilivyoona utunzaji mkubwa MUNGU alionao kila wakati kwa wale wanaompenda na kumcha Yeye, nilitiwa moyo na imani kwa MUNGU, na nilihisi kukemewa kwa sababu ya ukosefu wangu wa imani. {1T 346.2}

## SURA YA 67

## MATAJI MAWILI

Katika njozi niliyopewa pale Battle Creek, Michigan, Oktoba 25, 1861, nilioneshwa dunia hii, ikiwa nyeusi na yenye giza. Malaika akasema: “Tazama kwa uangalifu!” Kisha nikaoneshwa watu wakiwa juu ya nchi. Baadhi walizingirwa na malaika wa MUNGU, wengine walikuwa katika giza totoro, wakiwa wamezingirwa na malaika waovu. Nikaona mkono ukishuka chini kutoka mbinguni, umeshika fimbo ya dhahabu. Juu ya fimbo kulikuwa na taji iliyopambwa kwa almasi. Kila almasi ilitoa mwanga, angavu, mweupe, na wa kupendeza. Juu ya taji yaliandikwa maneno haya: “Wote watakaonipata watafurahia, nao watapata uzima wa milele.” 1T 347.1

Chini ya taji hii kulikuwa na fimbo nyingine, nayo ilikuwa na taji juu yake, ambayo katikati yake kulikuwa na vito, dhahabu, na fedha, vikiakisi nuru ya jua. Maneno katika taji hii yalikuwa: “Hazina ya dunia. Utajiri ni nguvu. Wote

watakaonipata watapata heshima na umaarufu." Niliona umati mkubwa ukikimbia ili kuipata taji hii. Walikuwa wakipiga kelele kubwa. Wengine katika shauku yao walionekana kukosa utimamu wa akili. Walisukumana, wakiwazuia wale ambao walikuwa dhaifu kuliko wao, na kukanyaga juu ya wale walioanguka kwa sababu ya haraka yao. Wengi kwa shauku waling'ang'ania kwa nguvu hazina zilizokuwa ndani ya taji, na kuzishikilia sana. Vichwa vya baadhi yao vilikuwa vyeupe kama fedha, na nyuso zao zilikunjamana kwa mahangaiko na wasiwasi. Ndugu zao, mifupa katika mifupa yao, na nyama katika nyama zao, wala hawakuwazingatia; bali, nyuso za huruma zilipowageukia, walizishika hazina zao kwa nguvu zaidi, kana kwamba walikuwa na hofu wakizembea watapoteza kidogo, au watashawishika kugawana nao. Macho yao yenye shauku mara nyingi yalitazama taji ya kidunia, na kuhesabu tena na tena hazina zake. Taswira za kutoridhika na uovu mkubwa zilionekana katika umati ule, na zilitazama hazina zilizokuwa pale kwa tamaa, na kugeuka bila tumaini wakati wenye nguvu walipowashinda na kuwazuia waliokuwa dhaifu. Hata hivyo bado hawakukata tamaa, bali umati wenye vilema, wenye afya zilizozorota, na wazee, waliridhia kufuata njia yao kuielekea taji ya dunia. Wengine walikufa wakitafuta namna ya kuifikia. Wengine walianguka walipokuwa wakijaribu kuishika. Wengi walikuwa wameanguka punde mara tu walipoishika. Miili iliyokufa ilisambaa juu ya ardhi, bado umati ulikuwa na haraka, ukikanyaga juu ya miili ya wenzao iliyoanguka na kufa. Kila aliyeifikia taji alimiliki sehemu katika taji hii, na alipongezwa kwa shangwe kubwa na umati ulioonekana kuvutiwa, na uliosimama kuizunguka taji hii. 1T 347.2

Jeshi kubwa la malaika waovu lilikuwa likifanya kazi kubwa. Shetani alikuwa katikati yao, na wote walikuwa na mwonekano wa furaha ulioridhika sana juu ya umati uliokuwa unaihangaikia taji. Alionekana akiwatupia uchawi wa kuwahadaa kwa njia kipekee wale waliokuwa na shauku ya kuitafuta taji. Wengi waliotafuta taji hii ya kidunia walikuwa ni wale waliodai kuwa Wakristo. Baadhi yao walionekana kuwa na nuru kidogo. Walionekana kuitazama taji ya mbinguni kwa shauku, na mara nyingi walionekana kuvutiwa na uzuri wake, lakini hawakuwa na uelewa wa kweli juu ya thamani na utukufu wake. Wakati kwa upande mmoja wakiyatafuta ya mbinguni kwa udhaifu, upande mwingine waliyatafuta ya dunia kwa shauku, na wakijizatiti kuyamiliki hayo; na katika harakati zao za kutafuta taji ya dunia, walipoteza dira ya mbinguni. Waliachwa gizani, na bado walikuwa katika hofu ya kutafuta taji ya kidunia. Wengine walichukizwa na kundi la walioitafuta taji ya dunia kwa shauku kubwa; walionekana kuwa na ufahamu juu ya hatari yao, nao wakageuka kuitafuta kwa bidii taji ya mbinguni. Muonekano wa nyuso zao punde ulibadilika kutoka kuwa wenye giza na kuwa wenye nuru, kutoka kuwa wenye huzuni na kuwa wenye kuvutia na furaha takatifu. 1T 348.1

Kisha niliona kundi likikaza mwendo katikati ya umati na macho yao yalikuwa yamejizatiti kuitazama taji ya mbinguni. Walipokuwa wakilazimisha njia yao katikati ya umati usiokuwa na mpangilio, malaika waliwalinda, na kuwatumikia na kuwawezesha kuendelea zaidi. Walipoikaribia taji ya mbinguni, nuru iliyokuwa ikitoka katika taji hiyo iliangaza juu yao na kuwazunguka, ikifukuza giza lao, na wao wakang'ara na kuangaza zaidi, hadi pale walipoonekana kubadilishwa na kufanana na malaika. Hawakuitazama taji ya kidunia hata kidogo. Wale waliokuwa wakiitafuta taji ya kidunia, waliwakejeli, na kuwatupia mipira miyeusi. Lakini hawa hawakuwadhuru hata kidogo wakati macho yao yalipokuwa yametazama taji ya mbinguni, lakini wale waliopoteza umakini wao kwaajili ya ya kuweka umakini wao kwenye mipira miyeusi waliwekewa madoa na hii mipira na kutengwa kwa kuchafuliwa nayo. Andiko hili lililetwa kwangu: 1T 349.1

Mathayo 6:19-24: "Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; 6.20 bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako. Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru. Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo! Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia MUNGU na mali.." 1T 349.2

Kisha kile nilichokuwa nimeona kilielezewa kwangu kama ifuatavyo: Umati wa waliokuwa wanapigania taji ya kidunia kwa shauku, walikuwa ni wale wanaopenda hazina za ulimwengu huu, na hudanganyika na kulaghaika na mambo yake yanayovutia kwa kitambo tu. Niliona baadhi ya wale wanaodai kuwa wafuasi wa Yesu, wakiwa na shauku ya kupata hazina za dunia kiasi cha kupoteza upendo wao kwa mbingu, wanaenenda kama ulimwengu, na kuhesabiwa na MUNGU kama watu wa ulimwengu huu. Wanadai kuitafuta taji isiyoharibika, hazina katika mbingu; lakini mapenzi yao na mtazamo wao mkuu ni kuzipata hazina za kidunia. Wale ambao wana hazina zao katika ulimwengu huu, na wanazipenda mali zao, hawawezi kumpenda Yesu.Wanaweza wakadhani wako sahihi, na, ijapokuwa wanang'ang'ania mali zao na kuzishikilia kwa ubahili, hawawezi kufanywa kuliona hilo, au kuhisi kwamba wanapenda pesa zaidi ya kusudi la Ukweli au hazina ya kimbingu. 1T 350.1

"Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; linakuwa giza kubwa kiasi gani!" Kuna kipindi fulani cha wakati kulikuwa na uzoefu wa namna hiyo, wakati ambapo hawakujali au kuthamini nuru waliyopewa, nayo ikawa giza. Malaika akasema: "Huwezi ukapenda na kuabudu hazina za dunia, ukawa utajiri wa kweli." Wakati kijana tajiri alipokuja kwa Yesu na kusema, "Mwalimu Mwema,

nifanye nini, ili nipate kuurithi uzima wa milele?" Yesu alimpa uchaguzi wake, wa kuachana na mali zake ili aupate uzima wa milele, au azishikilie aupoteze. Mali zake zilikuwa za thamani kubwa kwake kuliko hazina ya mbinguni. Sharti la kwamba lazima aachane na hazina zake na kuwapa maskini ili kuwa mfuasi wa Kristo na awe na uzima wa milele, lilihafifisha tamanio lake; na akaenda zake kwa huzuni. 1T 350.2

Wale watu nilioneshwa wakipiga kelele kubwa kwa sababu ya taji ya kidunia, walikuwa wale ambao watatumia njia yoyote kupata mali. Wanachanganyikiwa na kuwa wendawazimu wakifikia hatua hiyo. Mawazo yao yote na nguvu vimejielekeza katika namna ya kupata mali za kidunia. Wanazikanyagia chini haki za wengine, na kuwakandamiza maskini na kibarua katika ujira wake. Kama wanaweza kutumia fursa dhidi ya wale walio maskini kabisa na wenye nguvu kidogo kuliko wao, ili waweze kuongeza mali zao, hawatasita hata kwa muda kidogo kuwakandamiza, na hata kuwafanya wawe ombaomba. 1T 350.3

Wale watu ambao vichwa vyao vilikuwa vyeupe kwa uzee, na wale ambao nyuso zao zilikunjamana kwa mahangaiko, ambao bado kwa tamaa kubwa walizitazama hazina ndani ya taji na kuzikumbatia mali, walikuwa wamezeeka, walikuwa wamebakiza miaka michache. Bado walikuwa na shauku ya kujiwekea hazina za kidunia. Kadri walivyolisogelea kaburi, ndivyo walivyozidi kuzing'ang'ania hazina zile. Ndugu zao hawakunufaika. Watu wa familia zao walifanya kazi kubwa iliyozidi nguvu zao ili kupata pesa kidogo tu. Hawakuzitumia kwa manufaa ya wengine, au ya kwao binafsi. Ilitosha kwao kujua ya kwamba walikuwa nayo mali. Wakati jukumu la kusaidia kupunguza mahitaji ya maskini, na kusaidia kazi ya MUNGU linapowadia, wanahuzunika. Wangeweza kuikubali zawadi ya uzima wa milele kwa furaha kubwa, lakini hawako radhi kuona ikiwagharimu kitu chochote. Masharti ni magumu sana. Lakini Ibrahimu hakumzuilia mwanae pekee. Kwa kumtii MUNGU aliweza kumtoa sadaka mtoto huyu wa ahadi kwa urahisi zaidi kuliko ambavyo wengi wangezitoa sadaka baadhi ya mali zao za kidunia. 1T 351.1

Iliumiza kuona wale ambao walipaswa kuiva na kunawiri kwa utukufu, na kila siku kufaa kwa ajili ya kutoharibika, wakiziwekeza nguvu zao zote katika hazina zao za kidunia. Hao, niliona, hawakuweza kuithamini hazina ya kimbingu. Mapenzi yao ya dhati kwa mambo ya kidunia yaliwafanya kudhihirisha kwa matendo yao kwamba hawaheshimu urithi wa kimbingu ipaswavyo hata kuweza kuutolea sadaka. "Kijana tajiri" alionesha uhiari wa kuzitunza amri, lakini Bwana wetu alimwambia kwamba alipungukiwa kitu kimoja. Aliutamani ufalme wa milele lakini akazipenda mali zake zaidi. Wengi wanajidanganya wenyewe. Hawajaitafuta Kweli kama wanavyozitafuta hazina zilizojificha. Nguvu zao hazijawekwa katika hazina bora. Akili zao, ambazo zinapaswa kuangazwa na nuru ya mbinguni, zimechanganywa na masumbufu. "na shughuli za dunia, na

udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine zikiingia, hulisonga lile Neno, likawa halizai.” “ watu Hao,” alisema malaika, “hawana cha kujitetea.” Niliona nuru ikififia kwao. Hawakutamani kuzielewa Kweli takatifu, muhimu na za wazi za nyakati hizi, na wakadhani walikuwa salama bila kuzifahamu. Nuru yao ilizimika, na walitangatanga gizani. 1T 351.2

Kundi la vilema na wagonjwa wanaopambania taji ya dunia ni wale ambao mapenzi yao na hazina zao viko katika ulimwengu huu. Ijapokuwa wanakatishwa tamaa kila upande, hawawezi kuweka mapenzi yao mbinguni, na kujipatia hazina na makazi mbinguni. Wanashindwa katika mambo ya kidunia, na katika kuyatafuta, wanayapoteza yale ya mbinguni. Bila kujali kukatishwa tamaa na maisha yasiyo na furaha na vifo vya wale waliokuwa wamejielekeza kikamilifu kuzipata mali za kidunia, wengine wanafuata njia hiyo-hiyo. Wanakimbia kama wendawazimu, wakiipuzia hatima mbaya ya wale ambao wanafuata mfano wao. 1T 352.1
Wale walioifikia taji, na kumiliki sehemu yake, na kushangiliwa/kupongezwa, ni wale ambao hupata lile lililo kusudi kamili la maisha yao – yaani mali. Huipokea heshima ile ambayo ulimwengu huwapatia wale walio matajiri. Wana mvuto ulimwenguni. Shetani na malaika zake wameridhika. Wanajua hakika hao ni milki yao, kwamba wakati wanaishi katika uasi dhidi ya MUNGU, wanakuwa mawakala wa nguvu wa Shetani. 1T 352.2

Wale waliochukizwa na kundi la wale waliokuwa wakipiga kelele kubwa kwa ajili ya taji ya kidunia ni wale ambao wameshayajua maisha na hatima ya maisha ya wale wanaopambania mali za dunia. Wanaona kwamba hao hawaridhiki kamwe, na hawana furaha, wanaogopa, na kujitenga na tabaka la wasio na furaha, na kutafuta utajiri wa Kweli na unaodumu. 1T 352.3

Wale ambao wanapita katikati ya umati kwa ajili ya taji ya mbinguni, wanaohudumiwa na malaika, nilioneshwa kuwa watu hao ni waaminifu kwa MUNGU. Malaika wanawaongoza, na wanahuishwa kwa shauku ya kukaza mwendo kwa ajili ya hazina ya kimbingu. 1T 353.1

Mipira miyeusi ambayo watakatifu walitupiwa yalikuwa ni maneno ya uongo ambayo husambazwa na wale wanaopenda kusingizia/kuongopa juu ya watu wa MUNGU. Tunapaswa kuwa na uangalifu mkubwa ili kuishi maisha yasiyo na mawaa, na kujiondoa katika mionekano yote ya uovu, na kisha ni jukumu letu kwenda mbele kwa ushujaa, na kutosikiliza katika mafundisho ya uongo ya mwovu. Wakati macho ya wenye haki yakiwa yamekazwa katika hazina iliyo na thamani isiyo na kifani ya mbinguni, watakuwa zaidi na zaidi kama Kristo, na hivyo watabadilishwa na kufaa kwa ajili ya kubadilishwa. 1T 353.2

## SURA YA 68

## WAKATI UJAO

Wakati wa kubadilishwa na mng'ao, Yesu alitukuzwa na Baba Yake (transfiguration). Tunamsikia Yeye akisema: "Sasa Mwana wa Adamu ametukuzwa, na MUNGU anatukuzwa ndani Yake." Hivyo kabla ya kusalitiwa na kusulubiwa aliimarishwa kwa mateso Yake ya mwisho ya kutisha. Wakati washiriki wa mwili wa Kristo wanapokaribia kipindi cha pambano lao la mwisho, "wakati wa taabu ya Yakobo," watakua ndani ya Kristo, na wataishiriki sana Roho yake. Ujumbe wa malaika wa tatu unapoenea kwa sauti kuu, na nguvu kubwa na utukufu vinaposhiriki katika kazi ya mwisho, watu waaminifu wa MUNGU watashiriki utukufu huo. Ni mvua ya masika itakayowahuisha/itakayowafufua na kuwapa nguvu ya kupita katika wakati wa shida. Nyuso zao zitang'aa utukufu wa ile nuru iliyoambatana na malaika wa tatu. 1T 353.3

Niliona ya kwamba MUNGU kwa namna ya ajabu atawahifadhi watu Wake wakati wa taabu. Kama vile Yesu alivyoimwaga roho yake kwa uchungu mzito katika bustani, ndivyo watakavyolia kwa dhati na kuugua mchana na usiku kwa ajili ya ukombozi. Amri itatolewa ya kwamba wanapaswa kuipuuza Sabato ya amri ya nne, na kuiheshimu siku ya kwanza, au kupoteza maisha yao; lakini hawataiacha, na kuikanyaga kwa miguu yao Sabato ya Bwana, na kuiheshimu taasisi ya upapa. Jeshi la Shetani na watu waovu watawazunguka, na kushangilia juu yao, kwa sababu itaonekana kana kwamba hakuna njia ya wao

kutoroka. Lakini katikati ya shangwe na ushindi wao, zitasikika ngurumo baada ya ngurumo za radi kubwa za kutisha. Anga litakuwa jeusi, nalo litaangazwa na mng'ao mkali wa mwanga na utukufu wa ajabu kutoka mbinguni, wakati sauti ya MUNGU itakaposikika kwenye makao Yake matakatifu. 1T 353.4

Misingi ya dunia inatetemeka; majengo yanatingishika na kuyumbayumba na kuanguka chini kwa mshindo mkali na kupasuka vipande vipande. Bahari zitachemka kama maji kwenye chungu, na dunia yote itakuwa katika mtikisiko na mkanganyiko wa kutisha. Kifungo cha wale walio waadilifu kitageuzwa, na kwa minong'ono mizuri ya kusifu wataambiana: “Tumeokolewa. Ni sauti ya MUNGU.” Kwa kicho cha kustaj watasikiliza Maneno ya sauti. Waovu watasikia, lakini hawatayaelewa maneno ya sauti ya MUNGU. Wanaogopa na kutetemeka, wakati watakatifu wanafurahi. Shetani na malaika zake pamoja na watu waovu, waliokuwa wakishanglia kwamba watu wa MUNGU hawakuwa na nguvu zozote zaidi ya nguvu zao, na walikuwa chini ya mabavu yao, wakifirikia kwamba watawaangamiza kutoka duniani, wataushuhudia utukufu waliopewa wale ambao wameiheshimu sheria takatifu ya MUNGU. Wataona nyuso za wenye haki ziking'aa na kuakisi sura ya Yesu. Wale waliokuwa na shauku kubwa ya kuwaangamiza watakatifu hawawezi kuustahimili utukufu uliopo juu ya wale waliokombolewa, nao wanaanguka chini kama watu waliokufa kwenye ardhi. Shetani na malaika wabaya wanakimbia kutoka kwa watakatifu waliotukuzwa. Uwezo wao wa kuwaudhi umekwisha milele. 1T 354.1

## SURA YA 69

## UASI

(Ushuhuda huu ulipoandikwa Kanisa lilikuwa na wakati mgumu kwaajili ya Taifa lililokuwa linaunga mkono biashara ya utumwa na rasimu ya kuingia jeshini ili kupigana vita vya wenyewe kwa wenyewe vihusuvyo biashara ya utumwa. James White aliandika kwamba itakuwa kazi kukataa rasimu ya kujiunga jeshini, kwani ingefanya watu wavunje Sabato na kuua. Lakini rasimu ya jeshi ni shuruti, mtu hana uchaguzi kukataa. Hapa ndipo walisaidiwa na serikali kuwa na kitu kinaitwa Non-combative service, kwamba kama Mshiriki angeingia jeshini, basi atakuwa kwenye huduma zile ambazo hazihusishi kubeba silaha au kuua bali kushugulika na huduma zingine kama vile kuuguza majeruh, kupika, usafi nk. Soma zaidi maisha ya Desmond Doss hapa Marekani vitani)

Hali hii mbaya ya taifa letu inahitaji unyenyekevu wa kina upande wa watu wa MUNGU. Jambo muhimu tunalopaswa sasa kuzingatia na kujihoji nafsini na kila mtu ni hili: Je, nimejiandaa kwa ajili ya siku ya MUNGU ? Je! ninaweza kusimama dhidi ya mtihani wa kujaribiwa kwangu? 1T 355.1

Niliona kwamba MUNGU anawatakasa na kuwathibitisha watu Wake. Yeye Atawasafisha kama dhahabu isafishwavyo, mpaka taka itakapochomwa na sura Yake ionekane ndani yao. Wote hawana roho ya kujikana nafsi na ile nia ya kuvumilia ugumu na kuteseka kwa ajili ya Kweli ambayo MUNGUanaihitaji. Mapenzi yao hayajatiishwa; hawajajikabidhi kikamilifu kwa MUNGU, wakiwa hawaitafuti furaha kubwa zaidi ya kuyafanya mapenzi Yake. Wachungaji na washiriki wanakosa hali nzuri ya kiroho na utauwa wa kweli. Kila kitu ambacho kinaweza kutikiswa kitatikiswa. Watu wa MUNGU wataletwa katika nafasi za kujaribiwa, na wote wanapaswa kutulia na kukita mizizi katika Ukweli, la sivyo hatua zao zitapotoshwa. Ikiwa MUNGU hufariji na kunawirisha nafsi kwa uwepo wake unaohuisha, wanaweza kuvumilia, ingawa njia yaweza kuwa yenye giza na miiba. Kwa maana giza litapita, na nuru ya Kweli itaangaza milele. Nilipelekwa katika Isaya 58: 1-15; Yeremia 14: 10-12, kama maelezo ya hali ya sasa ya taifa letu. Watu wa taifa hili wamemwacha na kumsahau MUNGU. Wamechagua miungu mingine na kufuata njia zao za uharibifu hadi MUNGU amewaacha. Wakazi wa dunia wameikanyaga sheria ya MUNGU na kuvunja agano Lake la milele. 1T 355.2

Nilioneshwa msisimko uliojengeka katikati ya watu wetu kwenye makala ya *Review* yenye kichwa, "Taifa." Wengine walielewa kwa namna moja, na wengine kwa namna nyingine. Kauli za wazi zilipotoshwa, na kufanywa kuwa na maana ambayo mwandishi hakuwa ameikusudia. Alitoa nuru bora aliyokuwa nayo wakati huo. Ilikuwa ni lazima kwamba neno lisemwe. Macho ya wengi yalielekezwa kwa watunza Sabato kwa sababu hawakuonesha shauku kubwa zaidi katika pambano hilo na hawakuwa wamejitolea kuingia jeshini. Katika maeneo mengine walionekana wakikubaliana na uasi na kuwapa huruma zao. Wakati ulikuwa umefika wa hisia zetu za kweli kuhusiana na utumwa na uasi kujulikana. Kulikuwa na haja ya kujongea kwa hekima na kuepukana na tuhuma zilizoamshwa dhidi ya watunza Sabato. Tunapaswa kuenenda kwa umakini. "Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote." Tunaweza kutii ushauri huu, bila kuvunja hata kanuni moja ya imani yetu. Shetani na jeshi lake wanapigana na watunza amri, na watafanya kazi ili kuwapeleka kwenye nafasi za juu zaidi za majaribu. Hawapaswi wao wenyewe kwa kukosa busara kujiingiza katika nafasi hizo. 1T 356.1

Nilioneshwa kuwa baadhi ya watu walienenda pasipo busara kwa habari ya chapisho lililotajwa. Halikuendana sawasawa na maoni yao yote, na badala ya kulitazama suala hilo kwa utulivu, na kuliangalia katika mitazamo yake yote, walikasirika, wakaudhika, wakasisimka na wengine walipora kalamu na kurukia haraka katika hitimisho ambalo lisingeweza kuhimili uchunguzi. Baadhi hawakuwa na msimamo wala akili yenye kucheua mambo. Walifanya yale ambayo Shetani amewaharakisha kuyafanya, yaani, walitenda kwa hisia zao wenyewe za uasi. 1T 356.2

Huko Iowa walirefusha mambo, na wakaingia katika ushabiki. Walishindwa kutofautisha ushabiki na ari ya dhamiri njema. Badala ya kuongozwa na akili na maamzi ya hekima, waliruhusu kuongozwa na hisia zao. Walikuwa tayari kuifia imani yao. Je! hisia zao zote ziliwaongoza kwa MUNGU, na kwa unyenyekevu mkubwa mbele Zake? Je! ziliwaongoza katika kuuamini uwezo Wake wa kuwaokoa kutoka katika nafasi za majaribu wanazoweza kuletwa kwazo? Hapana! Badala ya kufanya maombi yao kwa MUNGU wa mbinguni na kuzitegemea nguvu Zake, walifanya madai yao mahakamani na yakatupiliwa mbali. Walionesha udhaifu wao na kufunua ukosefu wao wa imani. Yote haya yalichangia tu kulitambulisha kundi la kipekee la Watunza Sabato, na kuwafunua kwa kuwabamiza katika mazingira magumu chini ya waleo ambao hawakuwa na huruma nao. 1T 356.3

Wengine wamekuwa wakijitahidi kutafuta kosa na kulalamikia kwa maoni yoyote yaliyotolewa. Lakini wachache wamekuwa na hekima katika wakati huu wa kujaribiwa zaidi na kufikiri bila chuki na kusema kwa hekima ni nini kifanyike. Niliona kwamba wale ambao wamekuwa na kimbelembele kukataa kutii rasimu hawaelewi wanachosema. Ikiwa rasimu ya serikali ingewapitia ili wajiunge na jeshi na kisha wangekataa kutii, wakatishiwa kifungo, mateso, au kifo, wangeweza kutishika na kujikunja na kisha kujikuta kwamba hawakuwa tayari kwa dharura hiyo. Wasingeweza kuvumilia kujaribiwa kwa imani yao. Kile walichodhania kuwa ni imani, kilikuwa dhana tu ya ushabiki, imani bandia. 1T 357.1

Wale ambao watakuwa tayari kutoa hata uhai wao, ikiwa inahitajika, badala ya kujiweka mahali ambapo wasingeweza kumtii MUNGU, wangekuwa na machache ya kusema. Wala wasingejisifu. Wangehisi kwa kina na tafakari kubwa, na sala zao za dhati zingeenda mbinguni kwa sababu ya hekima ya kutenda na neema ya uvumilivu. Wale wanaohisi kwamba kwa hofu ya MUNGU hawawezi kushiriki kwa ujasiri katika vita hii watakuwa na utulivu mkubwa, watakuwa kimya, na watakapohojiwa na kuteswa watasema tu yale wanayotakiwa kusema ili kujibu maswali, na kisha ieleweke kwamba hawana mapatano na uasi. 1T 357.2

Kuna wachache miongoni mwa watunza Sabato ambao wanaofanya maridhiano na kuwaonea huruma watu wenye watumwa na wanaofanya biashara ya utumwa. Walipoukubali ukweli, hawakuyaacha makosa yote waliyopaswa kuyaacha. Wanahitaji maji kutoka kwenye chemchemi ya Kweli ya utakaso. Wengine wameleta pamoja nao chuki zao za kisiasa, ambazo hazipatani na kanuni za ile Kweli. Wanaendelea kusisitiza kuwa mtumwa ni mali ya bwana wake, na hapaswi kuchukuliwa kutoka kwake. Wanawachukulia watumwa hawa kama ng'ombe na kusema kuwa ni kumtendea vibaya mtu mwenye watumwa

kwa kumnyang'anya watumwa wake kama ilivyo vibaya kumnyang'anya ng'ombe wake. Nilioneshwa kwamba haikujalisha kiasi chochote ambacho bwana wao alilipa kwa ajili ya wanadamu hao na roho zao ili kuwafanya watumwa wake; MUNGU hakumpa mamlaka juu ya nafsi za wanadamu, naye hana haki ya kuwashikilia kama mali yake. Kristo alikufa kwa ajili ya uzao wote wa jamii ya wanadamu, awe mzungu, mweupe au mweusi. MUNGU amemfanya mwanadamu kuwa wakala huru wa kimaadili, awe mweupe au mweusi. Taasisi na desturi ya utumwa inaliondoa hili na kumruhusu mtu kutekeleza mamlaka yake dhidi ya mwenzake, uwezo ambao MUNGU hajawahi kumpatia, na ambao ni uwezo wa MUNGU pekee. Mmiliki wa watumwa amediriki kuchukua jukumu la MUNGU juu ya mtumwa wake, na hivyo ndivyo atakavyowajibika kwa dhambi, ujinga, na uovu wa mtumwa. Mtu huyu atawajibishwa kwa sababu ya nguvu anayoitumia juu ya mtumwa. Watu weusi ni mali ya MUNGU. Muumbaji wao peke yake Ndiye Bwana wao, na wale ambao wamediriki kumiliki mwili na nafsi ya mtumwa na kuifungia minyororo kwa kumuweka chini ya uharibifu wa kikatili kama washugulikavyo na mnyama wa mwituni tu, watakuwa na malipo yanayowastahili. Hasira ya MUNGU imetulia, lakini itaamka na kumwagwa bila kuchanganywa na rehema. 1T 358.1

Wengine wamekuwa na utayari mkubwa kuzungumzia kanuni zao za utumwa ambazo hazitokani na mbingu, bali zinatokana na utawala wa Shetani. Roho hizi zisizotulia zinatenda hayo kwa njia ya kuleta aibu juu ya kazi ya MUNGU. Nitatoa nakala ya barua iliyoandikwa kwa ndugu wa wilaya ya Oswego, New York: 1T 358.2

"Nilioneshwa mambo fulani kuhusu wewe. Niliona kwamba umedanganywa kuhusiana na wewe mwenyewe. Umewapatia nafasi maadui wa imani yetu wawatukane, na kuwadharau watunza Sabato. Kwa hatua yako ya wazi, umefunga masikio ya baadhi ya watu ambao wangesikiliza ukweli. Niliona kwamba tunapaswa kuwa na hekima kama nyoka na kuwa wapole kama njiwa. Wewe hukuonesha hekima ya nyoka wala upole wa njiwa. 1T 359.1

"Shetani alikuwa kiongozi mkuu wa kwanza katika uasi. MUNGU anaiadhibu kaskazini, kwa sababu wameiachia dhambi ya utumwa kuendelea kuwepo kwa muda mrefu; Kwa maana mbele za mbingu ni dhambi kubwa, yenye giza la kutisha. MUNGU hayuko upande wa kusini, Naye atawaadhibu vibaya sana mwishoni. Shetani ni mwasisi wa uasi wote. Niliona kwamba wewe, Ndugu A, umeruhusu kanuni zako za kisiasa kuharibu maamuzi yako na upendo wako kwa Ukweli. Kanuni hizo zinauondoa uchaji wa kweli moyoni mwako. Hujawahi kuutazama utumwa katika nuru ya haki, na maoni yako katika suala hili yamekupeleka upande wa uasi, ambao ulihamasishwa na Shetani na malaika zake. Mitazamo yako ya utumwa haiwezi kuendana na Kweli takatifu, Kweli muhimu za wakati huu. Lazima usalimishe maoni yako au Ukweli. Vyote viwili

haviwezi kukaa ndani ya moyo mmoja, kwa kuwa vinakinzana kila kimoja. 1T 359.2

“Shetani amekuwa akikuchochea. Hawezi kukuruhusu kupumzika mpaka utakapoelekeza mitazamo yako katika upande wa nguvu za giza, na hivyo kuimarisha mikono ya waovu, ambao MUNGU amewalaani. Umeelekeza ushawishi wako upande usiofaa, pamoja na wale ambao maisha yao ni ya kupanda miiba na kupanda maafa kwa wengine. Nilikuona ukitoa ushawishi wako kwa kundi lililoharibikiwa, lenye kutisha, kundi lililomuacha MUNGU; Na malaika wa MUNGU walikimbia kutoka kwako kwa kuchukizwa. Niliona kwamba umedanganywa kabisa. Kama ungeifuata nuru ambayo MUNGU amekupa, ungeliitikia maagizo ya ndugu zako, ungelisikiliza ushauri wao, ungelijiokoa na kuokoa msingi wa ile Kweli ya thamani dhidi ya aibu. Lakini licha ya nuru yote iliyotolewa, umeutangazia umma hisia zako. Usiporekebisha kile ulichokifanya, itakuwa jukumu la watu wa MUNGU kujiondoa hadharani katika ushirika na kuonyesha huruma kwako wewe, ili kuokoa hisia ambayo inapaswa kutoka kwetu kama kanisa. Lazima turuhusu ijulikane kuwa hatuna watu wa aina hii katika ushirika wetu, kwamba hatuwezi kutembea nao katika mtazamo kamakanisa. 1T 359.3

“Umepoteza ushawishi wa ile Kweli, utakasao. Umepoteza uhusiano wako na jeshi la mbinguni. Umejiunga upande uasi mkubwa wa kwanza, na ghadhabu ya MUNGU iko juu yako; Kwa sababu kazi Yake takatifu imeaibishwa, na ile Kweli imefanywa kuwa machukizo kwa wasioamini. Umewahuzunisha watu wa MUNGU, na kudharau mashauri ya mabalozi Wake duniani, ambao hufanya kazi pamoja Naye, na kwaajili ya Kristo wanafanya kazi ya kuzitafuta roho za Kristo ziweze kuunganishwa na MUNGU. 1T 360.1

“Nilioneshwa kama kanisa hatuwezi kuwa makini sana juu ya ushawishi tunaouleta; tunapaswa kuwa waangalifu katika kila neno. Wakati kwa neno au kwa tendo tunapojiweka wenyewe katika uwanja wa vita wa adui, tunawaondoa malaika watakatifu kutoka kwetu, na kuvutia malaika waovu kuwa katika umati unaotuzunguka watusonge. Hili ulilofanya, Ndugu A, kwa sababu ya uovu, na mapenzi yako binafsi imesababisha wasioamini kuwaangalia watunza Sabato wote wanaokuzunguka kwa mashaka makubwa. Maneno haya yaliwasilishwa mbele yangu yakiwahusu watumishi wa MUNGU: Yeye Awasikilizaye ninyi anisikiliza Mimi, naye awakataaye ninyi anikataa Mimi; naye anikataaye Mimi amkataa Yeye aliyenituma. Hebu MUNGU akusaidie, ndugu yangu uliyedanganywa, kujitazama jinsi ulivyo, na kuwa na huruma kwa mwili wa Kristo." 1T 360.2

Ufalme wetu sio wa ulimwengu huu. Tunamsubiri Bwana wetu kutoka mbinguni kuja duniani ili kuangusha mamlaka zote na nguvu, na kusimika ufalme Wake utakaodumu milele. Nguvu za kidunia zitatikiswa. Hatuhitaji, na hatuwezi,

kutarajia umoja kati ya mataifa ya dunia. Nafasi yetu katika sanamu ya Nebukadneza inawakilishwa na vidole, katika hali iliyogawanyika, iliyovurugika, vipande ambavyo havitashikamana pamoja. Unabii unatuonesha kwamba siku kuu ya MUNGU i karibu sana mbele yetu. Nayo inaharakisha sana. 1T 360.3

Niliona kuwa ni wajibu wetu katika kila jambo kutii sheria za nchi yetu, isipokuwa kama zinapingana na sheria kuu ambayo MUNGU aliitoa kwa sauti kubwa mlimani Sinai, na kisha akaandika juu ya jiwe kwa kidole CHAKE Mwenyewe. “Nitawapa sheria zangu katika nia zao, Na katika mioyo yao nitaziandika; Nami nitakuwa MUNGU kwao, Nao watakuwa watu Wangu.” Yeye ambaye sheria ya MUNGU imeandikwa katika moyo atamtii MUNGU badala ya wanadamu, na upesi atafikia hatua ambayo hatawaheshimu wanadamu wanaokengeuka na kuziacha amri za MUNGU. Watu wa MUNGU, waliofundishwa kwa uvuvio wa Kweli, wakiongozwa na dhamiri njema ya kuishi kulingana na kila Neno la MUNGU, watakuwa na sheria Yake na kuitunza, sheria iliyoandikwa mioyoni mwao, kama mamlaka pekee ambayo wanaweza kuitambua, kuikubali na kuitii. Hekima na mamlaka ya sheria ya MUNGU ni kuu kupita zingine zote duniani na mbinguni (Supreme). 1T 361.1

Nilioneshwa kuwa watu wa MUNGU, ambao ni hazina yake ya pekee, hawawezi kushiriki katika vita hii ya kutatanisha, kwa maana ni kinyume na kila kanuni ya imani yao. Katika jeshi hawawezi kuitii Kweli na wakati huo huo wakatii maagizo ya maafisa wao. Kutakuwa na ukiukwaji wa dhamiri daima. Wana wa ulimwengu wanaongozwa na kanuni za ulimwengu. Hawawezi kufahamu au kuthamini jambo jingine. Sera ya kidunia na maoni ya umma yanajumuisha kanuni ya matendo inayowaongoza na kuwapelekea kufanya mazoezi ya sheria ya kutenda lile lililo na usahihi-baya na jema. Lakini watu wa MUNGU hawawezi kutawaliwa kwa nia na misukumo hii. Maneno na amri za MUNGU, zilizoandikwa katika nafsi, ni roho na uzima, na kuna nguvu ndani yao ili kusadikisha na kutekeleza utii. Maagizo kumi ya Yehova ndiyo msingi wa haki na sheria zote nzuri ulimwenguni. Wale wanaozipenda amri za MUNGU wataendana na sheria zote nzuri za nchi. Lakini ikiwa mahitaji ya watawala yanakinzana na sheria za MUNGU, swali pekee la kujiuliza na kushugulika nalo ni hili: Tutamtii MUNGU, au mwanadamu? 1T 361.2

Kwa sababu ya uasi unaozidi na kuendelea dhidi ya katiba na sheria kuu, giza nene na kifo vimeenea juu ya dunia. Dunia imewekwa chini ya mzigo wa lundo la hatia, na inagua na kila mahali wanadamu wanaokufa hulazimika kupitia uzoefu uliojumuishwa katika mshahara wa uovu. Nilioneshwa kuwa wanadamu wamebeba kusudi la Shetani kwa hila na udanganyifu, na pigo la kutisha limetolewa hivi karibuni. Inaweza kusemekana kwa ukkweli kuwa: "Na hukumu imegeuka ikaenda nyuma, na haki inasimama mbali sana; maana Kweli imeanguka katika njia kuu, na unyofu hauwezi kuingia," "Na yeye auachaye uovu ajifanya kuwa mateka/mawindo." Katika baadhi ya majimbo huru ya nchi, kiwango cha maadili kinashuka chini zaidi na zaidi. Wanadamu wenye hamu ya

uovu wa kutisha na maisha yaliyoharibikiwa sasa wana fursa ya kushinda. Wamechagua watawala/kutawaliwa na wale ambao kanuni zao zinapotosha kwa maadili ya kuelekea chini, watu wasiochunguza uovu na kuukataa, wala kuzigeuza shauku ovu za watu, bali wanawaacha wasombwe kikamilifu. Ikiwa wale wanaochagua kuwa kama wanyama, kwa kunywa kimiminika chenye sumu, ndio wangeteseka peke yao; kama ndio pekee wangevuna matunda ya matendo yao wenyewe, basi uovu usingekuwa mkubwa sana. Lakini wengi, wengi sana, lazima wapitie mateso makubwa kwa sababu ya dhambi za wengine. Wanawake na watoto, tena wasio na hatia, lazima wakinywee kikombe cha uchungu katika ukali wake. 1T 362.1

Bila neema ya MUNGU, wanadamu wanapenda kufanya maovu. Wanatembea katika giza, wala hawana nguvu ya kujidhibiti/kujitawala. Wanatoa ruhusa kwa matamanio na hamu zao hadi hisia zote nzuri zaidi zinapotea hadi tamaa za kinyama tu sasa zinadhihirishwa. Wanadamu hao wanahitaji kuihisi nguvu kuu, ya udhibiti, ambayo itawaelekeza kutii. Ikiwa watawala hawaoneshi nguvu ya kutisha kwa mtenda uovu, basi atazidi kuzama katika kiwango cha mnyama mkatili wa mwituni. Dunia inaendelea kuwa katika uovu na ufisadi zaidi na zaidi. 1T 362.2

Wengi walipofushwa na kudanganywa kwa kiasi kikubwa katika uchaguzi wa mwisho wa nchi yetu, na ushawishi wao ulitumiwa kuwaweka katika mamlaka wanadamu ambao wangeweza kuufumbia macho uovu, watu ambao wangeweza kushuhudia mafuriko ya ole na taabu isiyokuwa ya kawaida na mioyo yao isiguswe, ambao kanuni zao zimepotea, wanaofanya maridhiano na kuwahurumia watunza watumwa wa Kusini, watu ambao wangeweza kuuhifadhi utumwa kama ulivyo. 1T 363.1

Katika nafasi za kuaminiwa katika jeshi la kaskazini kuna wanaume ambao ni waasi ndani ya mioyo, ambao kwao thamani ya maisha ya askari ni sawa na mbwa. Wanaweza kuwaona wameraruliwa, na kuchanwachanwa, kupewa kilema, na kufa, kwa maelfu, bila kuguswa moyo na lolote. Maafisa wa jeshi la kusini wanapokea taarifa kila wakati kuhusu mipango ya jeshi la kaskazini. Taarifa sahihi imetolewa kwa maafisa wa kaskazini kuhusu harakati na mbinu za waasi, ambazo zimekataliwa na kupuuzwa kwa sababu mtoa taarifa alikuwa mweusi. Na kwa kukataa kujiandaa kwa ajili ya shambulio, vikosi vya Umoja vimeshtukizwa na kusambaratishwa vipande vipande, na ubaya ni kuwa, wengi wa askari maskini wamechukuliwa wafungwa na kuteseka hata zaidi ya kifo. 1T 363.2

Kama kungelikuwa na umoja katika jeshi la Kaskazini, uasi huu ungekoma upesi. Waasi wanajua wana wadau wao kila upande wa jeshi la Kaskazini. Kurasa za historia zinaendelea kuwa giza na bado ni giza. Watu waaminifu, ambao hawakutoa nafasi kwa uasi, au utumwa ambao ndio umesababisha uasi,

wameshinikizwa kukubali mambo. Ushawishi wao umesaidia kuwaweka madarakani watu ambao kanuni zao zilipingwa. 1T 363.3

Kila kitu kinaitayarisha siku kuu ya MUNGU. Muda utadumu kitambo kidogo mpaka wenyeji wa dunia wawe wamekijaza kikombe cha uovu wao, na kisha ghadhabu ya MUNGU, ambayo imetulizwa kwa muda mrefu, itaamka, na nchi hii ya nuru itakunywa katika kikombe cha ghadhabu yake isiyochanganywa. Nguvu ya MUNGU ya uharibifu iko juu ya dunia ili kusambaratisha na kuharibu. Wakazi wa dunia wanaelekezwa katika upanga, njaa, na tauni. 1T 363.4

Watu wengi sana katika mamlaka, majenerali na maafisa, hutenda kulingana na maelekezo yaliyowasilishwa na roho za mapepo na umizimu. Roho za mapepo, zinazodai kuwa wapiganaji waliokufa na majenerali wenye ujuzi, huwasiliana na wale walio katika mamlaka na kudhibiti harakati zao nyingi. Jenerali mmoja ana maelekezo yanayotoka katika roho hizi ili kufanya hatua maalum ya kijeshi na kufarijiwa na matumaini ya mafanikio. Mwingine hupokea maelekezo yanayotofautiana sana na yale yaliyotolewa kwa yule wa kwanza. Wakati mwingine wale wanaofuata maelekezo yaliyotolewa wanapata ushindi, lakini mara nyingi wananakutana na kushindwa. 1T 363.5

Roho hizi chafu wakati mwingine huwapatia watu hawa wanaoongoza mlolongo wa matukio yatakayotokea katika vita wanayokaribia kushiriki, na watu binafsi ambao watashindwa katika vita. Wakati mwingine huonekana kuwa kama roho hizi zinatabiri, na hii inaimarisha imani ya waumini katika maonesho ya umizimu. Kisha inaonekana kuwa taarifa sahihi haijatolewa, lakini roho za udanganyifu hufanya maelezo fulani, ambayo hupokelewa. Udanganyifu juu ya akili ni mkubwa sana kiasi kwamba wengi hawawezi kutambua roho za uongo ambazo zinawaongoza kwenye uharibifu fulani. 1T 364.1

Kiongozi mkuu wa uasi, Shetani, anafahamu shughuli za vita hii, na anawaongoza malaika zake kuchukua maumbo ya majenerali waliokufa, kuiga tabia zao, na kuonesha sifa zao za kipekee. Na viongozi katika jeshi wanaamini kweli kwamba ni roho za marafiki zao na wapiganaji waliokufa, waasisi wa vita vya mapinduzi, wanaowaongoza. Kama wasingekuwa chini ya udanganyifu mkubwa zaidi, wangeanza kufikiri kwamba wapiganaji wa mbinguni hawakuonesha uongozi/ujenerali mzuri na mafanikio, au wamesahau ujuzi wao wa kidunia. 1T 364.2

Badala ya viongozi wakuu katika vita hii kumtegemea MUNGU wa Israeli, na kuongoza majeshi yao kumtegemea Yeye pekee awezaye kuwaokoa kutoka kwa maadui zao, wengi wanaomba msaada wa mkuu wa mapepo na kumwamini. Kumbukumbu la Torati 32: 16-22. Alisema malaika: "Je, MUNGU anaweza kweli kuwafanikisha watu kama hao? Ikiwa wangemtazama na kumtegemea; Ikiwa wangekuja mahali pekee ambapo angeweza kuwasaidia, kulingana na utukufu Wake mwenyewe, angeweza kufanya hivyo." 1T 364.3

Niliona kwamba MUNGU asingeliweka jeshi la kaskazini mikononi mwa waasi, ili liangamizwe na adui zao kabisa. Nilielekezwa katika Kumbukumbu la torati 32:26-30 "Nalisema, Ningewatawanyia mbali, Ningekomesha kumbukumbu lao kati ya wanadamu; Isipokuwa naliogopa makamio ya adui, Adui zao wasije wakafikiri uongo, Wasije wakasema, Mkono wetu umetukuka, Wala Bwana hakuyafanya haya yote. Maana hawa ni taifa wasio shauri, Wala fahamu hamna ndani yao. Laiti wangekuwa na akili, hata wakafahamu haya, Ili watafakari mwisho wao. Mmoja angefukuzaje watu elfu, Wawili wangekimbizaje elfu kumi, Kama Mwamba wao asingaliwauza, Kama Bwana asingaliwatoa?" 1T 365.1

Kuna majenerali katika jeshi ambao wamejitoa kabisa kufanya yote wanayoweza kuukomesha uasi huu wa kutisha na vita isiyo ya kawaida. Lakini wengi wa maafisa na viongozi wana malengo yao binafsi ya kutumikia. Kila mmoja anatafuta faida kutoka katika nafasi yake mwenyewe, na wengi wa askari wa kweli, wenye moyo wanakabiliwa na moyo kuzimia, wasiwasi na kukata tamaa. Wao hufanya sehemu yao kwa ukamilifu wakati wa kukabiliana na adui, lakini vitendo wanavyopokea kutoka kwa maafisa wao ni vya kikatili. Miongoni mwa askari kuna watu ambao wana hisia nzuri na uhuru dhidi ya roho. Hawajawahi kuwa na kawaida ya kuchangamana na aina ya watu hawa hadi vita ilipowaweka pamoja, na kufanyiwa udhalimu, kuteswa na kufanyiwa unyanyapaa na ukatili. Ni vigumu sana kwao kuvumilia haya yote. Maafisa wengi wana tamaa za kikatili, na wakiziweka katika mamlaka wanapata fursa nzuri ya kutenda sawa na asili zao za kikatili. Wanawakandamiza kwa udhalimu mkubwa wale walio chini yao kama mabwana wa kusini wanavyowakandamiza watumwa wao. Mambo haya yataleta ugumu katika kupata watu kwa ajili ya jeshi. 1T 365.2

Katika baadhi ya matukio wakati majenerali wakiwa katika migogoro ya kutisha, askari wao wameanguka kama mvua kwa kifo, kuwatia moyo wanajeshi na kuongeza wanajeshi wengine katika wakati sahihi kungewapatia ushindi. Lakini majenerali wengine hawakujali kabisa jinsi maisha ya wengi yalivyopotea, na badala ya kuwasaidia wale wanaoshambulia, kama wale wenye maslahi mamoja, walizuia misaada muhimu, wakiogopa kumba yule Jenerali aliye ndugu wa upande wao angepata heshima kutokana na mafanikio ya kumuondosha adui-jeshi la kusini. Kupitia tamaa na wivu wamewahi kushangilia adui apate ushindi na kuwashambulia askari wa Kaskazini. Askari wa kusini wana roho ya uovu katika uasi huu, lakini askari wa kaskazini hawaeleweki. Wengi wao wana wivu wa ubinafsi, wakiogopa kwamba wengine watapata heshima/medali na kuinuliwa juu yao wenyewe. Ni maelfu mangapi ya uhai yaliyotolewa sadaka kwenye jambo hili! Wale wa mataifa mengine ambao wamefanya vita wamekuwa na umoja. Wakiwa na ari isiyotafuta faida yao wenyewe wameamua kusonga mbele na kushinda au kufa. Askari walioongoza

katika mapinduzi walikuwa na umoja na ari, na kwa njia hiyo walipata uhuru wao. Lakini sasa watu wanakuwa kama mapepo badala ya wanadamu. 1T 366.1

Shetani kupitia malaika zake, aliwasiliana na maafisa ambao walikuwa watulivu, wenye mahesabu mazuri wakati wakiwa wenyewe, na kukatia tamaa maamuzi yao wenyewe, hivyo wameongozwa na roho hizi za uongo katika maeneo magumu sana, ambapo wamepigwa na mauaji mengi ya kutisha yamekuwa matokeo. Hii inaufaa vema ukuu wa kishetani kuona mauaji mengi duniani. Adui napenda kuona askari wasio na hatia wakifyekwa chini kama majani. Niliona kwamba waasi mara nyingi wamekuwa katika nafasi ambayo wangeweza kutiishwa bila jitihada nyingi; Lakini mawasiliano kutoka kwa roho hizo za mapepo yamesababisha majenerali wa kaskazini kupofushwa macho yao mpaka waasi walipowazidi uwezo. Na baadhi ya majenerali wangeona heri kuwaruhusu waasi kutoroka kuliko kuwakamata. Wanafikiri zaidi juu ya taasisi ya utumwa ambayo ni kipenzi chao kuliko ustawi wa taifa. Hizi ni miongoni mwa sababu za vita kuchukua muda mrefu. 1T 366.2

Taarifa iliyotumwa na majenerali wetu kwenda Washington kuhusu harakati za majeshi yetu ingeweza kufikiwa moja kwa moja kutoka katika vikosi vya waasi. Kuna wanaotoa huruma na kuridhiana na waasi ndani ya moyo wa mamlaka za umoja. Vita hii ni tofauti na nyingine yoyote. Ukosefu mkubwa wa umoja wa hisia na matendo hufanya kuonekane giza na kukatisha tamaa. Wengi wa askari wametupilia mbali uwezo wa kujizuia na wamezama katika hali ya kutisha ya uharibifu. Je, MUNGU anawezaje kusonga mbele na jeshi lenye ufisadi wa kiasi hiki? Yeye Anawezaje basi, kulingana na heshima Yake, kuwashinda adui zao na kuwaongoza katika ushindi? Kuna ugomvi, mafarakano, na kupigania heshima, wakati maelfu ya askari wasio na hatia wanakufa kwenye uwanja wa vita kwa maelfu au kutokana na mazingira magumu, kuanikwa kwenye kila dhiki na vidonda vya majeraha. 1T 367.1

Vita hii ni kali zaidi na wakati huo huo ni mgogoro wa kutisha na wa aina ya peke yake, ni jambo la kuumiza mioyo, na hata kufanya moyo uugue. Mataifa mengine yanatazama kwa kuchukizwa shughuli za majeshi ya kaskazini na kusini. Wanaona jitihada hiyo ya kurefusha vita inagharimu uhai na pesa, wakati huo huo hakuna kitu kinachopatikana, kwamba inaonekana kwao kama ugomvi wa kuona nani anaweza kuua watu wengi. Wana hasira kali. 1T 367.2

Niliona kwamba uasi huo ulikuwa unaongezeka kwa kasi na kwamba ulikuwa haujawahi kuwa mkubwa kama wakati huu. Wengi waliodai kuwa askari wa umoja, wakishikilia nafasi muhimu, si waaminifu mioyoni. Sababu pekee iliyowafanya kuchukua silaha ilikuwa kuhifadhi umoja kama ulivyokuwa, na utumwa pamoja nao. Wangeweza kumtumikisha mtumwa maisha yake yote na kumweka kwenye minyororo ya uchungu na aibu, endapo wangepata fursa hiyo. Hilo linatia huruma kwa kiwango fulani kutoka kusini. Damu imemwagika kama maji, na bila sababu yoyote. Katika kila mji na kijiji kuna maombolezo.

Wanawake wanawaomboleza waume zao, akina mama kwa watoto wao, na akina dada kwa kaka zao. Lakini licha ya mateso haya yote, watu hawa hawamgeukii MUNGU. 1T 367.3

Niliona kwamba wote kusini na kaskazini walikuwa wakiadhibiwa. Kwa ule upande wa kusini, nilielekezwa katika Kumbukumbu la Torati 32: 35-37: "Kisasi ni Changu Mimi, na kulipa, Wakati itakapoteleza miguu yao; Maana siku ya msiba wao imekaribia, Na mambo yatakayowapata yatafanya haraka. Kwa kuwa Bwana atawaamua watu Wake, Atawahurumia watumwa Wake, Aonapo ya kuwa nguvu zao zimeondoka, Na ya kuwa habaki mtu, aliyefungwa wala asiyefungwa, Naye atasema, Iko wapi miungu yao, mwamba ule walioutumaini; " 1T 368.1

## SURA YA 70

## HATARI NA WAJIBU WA WACHUNGAJI

Nilioneshwa kuwa mengi yanaweza kukamilishwa sasa kwa kutenda kazi katika sehemu ambazo kuna watu waongofu wachache ambao tayari wamefikiwa, kuliko katika maeneo mapya kabisa, isipokuwa pale ufunguzi wa kazi unapokuwa mzuri sana. Wachache waliopo katika miji tofauti tofauti ambao wanaiamini Kweli kabisa wataleta mvuto na kuchochea watu wengine kuichunguza imani yao; na kama maisha yao ni ya mfano, nuru yao itaangaza, na watavuta makutano/mikusanyiko ya watu. Na bado nilioneshwa maeneo ambayo bado Kweli haijatangazwa, ambayo yanapaswa kutembelewa hivi karibuni. Lakini kazi iliyo kuu inayopaswa kufanyika sasa ni kuwaleta watu wa MUNGU waingie kazini na kuleta mvuto mtakatifu. Wanapaswa kuchukua nafasi ya watendakazi na kufanya kazi. Kwa hekima, tahadhari, na upendo, wanapaswa kutenda kazi kwa ajili ya wokovu wa majirani na marafiki. Kuna hali ya kutopenda kujihusisha katika hili, na kukaa mbali. Bado msalaba haujanyanyuliwa na kubebwa ipasavyo. Wote wanapaswa kuhisi kwamba ni walinzi wa ndugu zao, na kwamba wanawajibika kwa kiasi kikubwa juu ya nafsi za wale wanaowazunguka.Washiriki wanafanya makosa wanapowaachia watumishi kazi hii yote wao wenyewe. Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Wale ambao wana sifa njema, ambao maisha yao yanalingana na imani yao, wanaweza kuwa watumishi wa Bwana. Wanaweza kuzungumza na wengine, na kuwahimiza juu ya umuhimu wa Kweli. Hawapaswi kuwasubiri

wachungaji na kulipuuza jukumu lililo wazi ambalo MUNGU amewaachia wao ili walifanye. 1T 368.

Baadhi ya wachungaji wetu, mioyo yao ina shauku ndogo katika kubeba majukumu ya kazi ya MUNGU na kutenda kazi kwa kujitoa kikamilifu kwa upendo usiojifikiria wenyewe, kama yalivyokuwa maisha ya Bwana wetu wa mbinguni yalivyo. Makanisa, kama ilivyo desturi, yamekuwa na maendeleo makubwa zaidi kuliko baadhi ya wachungaji. Wamekuwa na imani katika Shuhuda ambazo Bwana amewapatia, na kuzifanyia kazi, wakati baadhi ya wahubiri wakiwa nyuma sana. Wanakiri kuamini ushuhuda walioubeba, na baadhi yao wazifanya hizi shuhuda kuwa sheria za chuma na kuwaletea maumivu wale wasio na uzoefu kuzihusu, lakini wao wenyewe wanashindwa kutimiliza maagizo yake. Wamekuwa na shuhuda zilizorudiwa ambazo wengine wamezipuuzia kabisa. Mwenendo wa hawa watu siyo thabiti-unatapatapa. 1T 369.1

Watu wa MUNGU huwa wana hamasa ya kuungana pamoja ili kueneza Kweli. Kwa uchangamfu wanatoa msaada kuwategemeza kwa ukarimu wale watumikao katika Neno na mafundisho ya imani. Na niliona kuwa ni wajibu wa wale walio jukumu la kusimamia mali, kuhakikisha kuwa mali za kanisa hazitumiwi ovyo-kwa ubaradhifu. Baadhi ya hawa ndugu wakarimu wamekuwa wakitenda kazi katika hali ya maumivu, mishipa ya fahamu yenye hitilafu na miili iliyovunjika kwa magonjwa kwa muda mrefu, hali iliyosababishwa na kufanya kazi kwa kupitiliza zamani ili kupata mali, na sasa kadri wanavyotoa kwa hiari na ukarimu sehemu ya mali ambayo imewagharimu sana kiasi hiki, ni wajibu wa watumishi wa Neno na mafundisho ya imani, kudhihirisha ari na kujitolea nafsi angalau kwa kiwango sawa na kile kilichooneshwa na ndugu hawa. 1T 369.2

Watumishi wa MUNGU ni lazima watoke kwa uhuru. Wanapaswa kumjua Yule wanayemwamini. Kuna nguvu katika Kristo na wokovu Wake uliowafanya wawe watu huru; na kama hawako huru katika Yeye, kamwe hawawezi kulijenga kanisa Lake na kuzikusanya roho. Je, MUNGU atatuma mtu kwenda kuziokoa roho kutoka katika mtego wa Shetani wakati miguu yake mwenyewe mtu huyo imenaswa mtegoni? Watumishi wa MUNGU hawapaswi kuyumbayumba. Kama miguu yao inateleza, wanawezaje kuwaambia wale wenye mioyo ya hofu: “Iweni hodari”? MUNGU anataka watumishi Wake kuwashika wale wenye mikono dhaifu, na kuwaimarisha wanaotetereka. Wale ambao hawajawa tayari kwa hili ni bora wangejihangaikia wenyewe na kuomba mpaka watakapokirimiwa nguvu ya Roho Mtakatifu kutoka juu. 1T 369.3

MUNGU hafurahishwi na kukosekana kwa roho ya kujikana nafsi kwa baadhi ya watumishi wake. Hawana mzigo wa kazi ya MUNGU juu yao. Wanaonekana kuwa katika usingizi wa mauti. Malaika wa MUNGU wanasimama na kushangazwa sana na kuona aibu juu ya hali hii ya kutojikana nafsi na kukosa uvumilivu. Wakati Mwasisi wa wokovu wetu alihangaika na kuumia kwa ajili yetu, alijikana nafsi,

na maisha Yake yote yalikuwa ni mtiririko wa matukio ya ufukara, kuhenyeka na mateso. Angeliweza kuishi maisha rahisi na wingi wa mali na vitu, na kujipatia starehe za maisha haya; lakini hakuangalia nafsi na faraja Yake Mwenyewe. Yeye Aliishi ili awatendee wengine yaliyo mema. Aliumia na kuteseka ili kuwaokoa wengine na mateso. Alivumilia mpaka mwisho na kuikamilisha kazi aliyopewa kuifanya. Hii yote ni kwa ajili ya kutuokoa sisi kutoka katika uharibifu. Na sasa, je! inawezekanaje kwamba sisi, viumbe tusiostahili upendo mkuu kiasi hiki, kutafuta nafasi iliyo bora zaidi katika maisha haya kuliko ile aliyopewa Bwana wetu? Kila wakati katika maisha yetu tumekuwa washiriki wa mibaraka ya upendo Wake mkuu, na ni kwa sababu hii pekee, sisi hatuwezi kutambua kwa ukamilifu kina cha ujinga, ole na mateso ambacho tumeokolewa kwa hicho. Je! twaweza kumtazama Yeye ambaye dhambi zetu zimemchoma na huku hatuko tayari kunywa pamoja Naye kikombe kichungu cha aibu na huzuni? Je! twaweza kumtazama Kristo aliyesulubiwa na huku tukitarajia kuingia katika ufalme Wake kwa njia nyingine pasipo dhika nyingi na adha? 1T 370.1

Si wahubiri wote waliojitoa kikamilifu kwa kazi ya MUNGU, kama ambavyo wangetakiwa kuwa. Baadhi yao wamehisi kwamba maisha ya wahubiri ni magumu kwa kuwa kazi inawatenganisha na familia zao. Wanasahau kuwa hapo awali kazi hii ilikuwa ngumu kuliko ilivyo sasa. Hapo awali kulikuwa na marafiki wachache tu katika kazi hii ya Bwana. Wanawasahau wale ambao Bwana aliwapatia majukumu ya kazi hii hapo awali. Ni wachache tu ambao waliipokea Kweli baada ya kazi kubwa mno kufanyika. Watumishi wateule wa MUNGU walilia na kuomba ili wapate kuielewa Kweli kwa uwazi, na pia walipitia magumu na kujikana nafsi ili waweze kuieneza injili kwa wengine. Hatua kwa hatua walifuata maongozi ya majaliwa ya MUNGU wakati njia iliendelea kufunguliwa. Hawakushugulikia faraja yao au kukata tamaa katika nyakati ngumu. Kupitia watu hawa MUNGU aliandaa njia na kuifanya Kweli iwe wazi na yenye kueleweka kwa kila aliye mwadilifu/mkweli. Kila kitu kipo tayari katika mikono ya watumishi ambao tangu mwanzo waliipokea Kweli, lakini bado baadhi yao wameshindwa kubeba majukumu ya kazi. Wanakimbilia mafungu/nafasi rahisi zinazohitaji kujikana kidogo tu. Dunia hii siyo mahali pa kupumzika kwa Wakristo, na zaidi sana kwa watumishi wateule wa MUNGU. Wanasahau kwamba Kristo aliacha utajiri Wake na ukuu mbinguni, na akaja ili afe, na kuwa Yeye ametuamuru sisi kupendana kama Yeye alivyotupenda. Wanasahau wale ambao kwao ulimwengu haukuwa umewastahali, ambao walitanga-tanga wakiwa wamevaa ngozi za kondoo na mbuzi, huku wakiudhiwa na kuteswa (Waebrania 11:38). 1T 370.2

Nilioneshwa Waldensia, na vile walivyoteseka kwa ajili ya imani yao. Walilisoma Neno la MUNGU kwa umakini, na kuishi kulingana na nuru waliyopewa. Waliteswa, na kufukuzwa majumbani mwao; mali zao, walizozipata kwa jasho, zilichukuliwa, na nyumba zao zikachomwa moto.

Walikimbilia milimani na huko walipitia dhiki na mateso ya kutisha. Walivumilia njaa, uchovu, baridi, na uchi. Nguo pekee ambazo wengi wao wangeweza kuvaa zilikuwa ni ngozi za wanyama. Na bado wakiwa katika hali ya kutawanyika na kukosa makazi waliweza kukutana na kupaza sauti zao kwa kuimba, na kumtukuza MUNGU kwamba wamehesabiwa kuwa wenye thamani kuteseka kwa ajili ya Jina la Kristo. Walitiana moyo na kupongezana kila mmoja na mwenzake, na walikuwa wenye shukrani hata katika makazi yao ya huzuni. Wengi wa watoto wao waliumwa na kufa kutokana na baridi kali na njaa, lakini bado wazazi hawakuwahi kufikiri hata mara mmoja kuikana dini yao. Waliuthamini sana upendo, kibali na neema ya MUNGU kuliko mambo ya kidunia au utajiri wake. Faraja yao ilikuwa ni kutoka kwa MUNGU na kwa furaha walitazama mbele huku wakitarajia kupewa thawabu. 1T 371.1

Kisha nilioneshwa Martin Luther, ambaye MUNGU  alimwinua ili afanye kazi maalumu. Ni wa thamani kwake kiasi gani Ulikuwa ufahamu wa Kweli uliofunuliwa katika Neno la MUNGU ! Akili yake ilikuwa na njaa ya kitu ambacho kingelijenga tumaini lake kwamba MUNGU angekuwa Baba yake, na mbinguni pawe nyumbani kwake. Nuru mpya na ya thamani ambayo aliipata kutoka katika Neno la MUNGU ilikuwa kwake yenye thamani isiyo kifani, na alifikiri kuwa kama  angelienda mbele na kuitangaza injili, basi angeliushawishi ulimwengu. Alisimama kinyume na ghadhabu ya kanisa lililoasi na aliwaimarisha wale ambao pamoja naye waliojineemesha na sherehe ya utajiri wa ile Kweli upatikanao katika Neno la MUNGU. Luther alikuwa ni chombo kiteule cha MUNGU apate kulichana vazi la unafiki la kanisa la kipapa na kufunua upotovu wake. Alipaza sauti yake kwa bidii na kwa nguvu ya ROHO MTAKATIFU alipiga kelele na kukemea dhambi za viongozi wa watu zilizokuwepo zama hizo. Matangazo yakatolewa kwamba akipatikana apate kuuawa, alionekana kuwa chini ya huruma za watu washirikina, ambao walikuwa wakitii  kiongozi wa Kanisa la Kirumi. Hata hivyo hakuyahesabu maisha yake kuwa ya thamani kwake. Luther alijua kuwa hakuwa salama mahala popote pale, lakini bado hakutetemeka. Nuru aliyoiona na kujineemesha nayo ilikuwa  uzima kwake, na yenye thamani zaidi kuliko hazina zote za ulimwengu. Alijua kuwa hazina za kidunia zingetoweka; lakini Kweli za thamani zilizofunuliwa kwenye uelewa wake, zitendazo kazi moyoni mwake, zingedumu, na, kama zikiheshimiwa, zingemwongoza kufikia hali ya kutokufa. 1T 372.1

Alipoitwa kwenda Augsburg ili kutoa majibu juu ya imani yake, alitii wito. Mtu mmoja huyu aliyekuwa peke yake, na ambaye alikuwa amewaghadhibisha makasisi na washiriki alishitakiwa mbele ya wale waliosababisha ulimwengu kutikisika – kondoo mnyenyekevu aliyezungukwa na simba wenye hasira, ambaye bado kwa ajili ya Kristo na Ukweli, akasimama bila wasiwasi, na kwa ufasaha mtakatifu, ambao unatokana na uvuvio wa Kweli pekee, alitoa sababu za imani yake. Maadui wake walijaribu mbinu mbalimbali ili kumnyamazisha mtetezi huyu wa Ukweli aliye jasiri mwaminifu. Mwanzoni walimsifia, na

kumuahidi kuwa atapewa sifa na adhama. Lakini uhai na adhama havikuwa na thamani kwake kama vikipatikana kama matokeo ya kuikanyaga Kweli. Mwanga wa Neno la MUNGU ulizidi kuangaza na kumulika ufahamu wake, huku ukimwonesha makosa, upotofu, na unafiki wa upapa. Kisha maadui zake walitafuta kumtisha ili aikane imani yake, lakini alisimama imara kuitetea Ile Kweli na imani. Alikuwa tayari kufa kwa ajili ya imani yake, kama MUNGU akipenda; lakini siyo kujisalimisha. MUNGU aliyatunza maisha yake. Aliwatuma malaika kusimama naye na kutuliza ghadhabu na makusudi ya adui zake, na kumvusha salama katika pambano lenye dhoruba kuu. 1T 372.2

Utulivu, hadhi na nguvu ya uvuvio iliyokuwepo ndani ya Luther viliwanyenyekesha maadui zake, na kupeleka pigo la kutisha kwa upapa. Viongozi na wakuu na watu wenye viburi waliazimu kuwa damu yake imwagike ili kufanya upatanisho wa jeraha walililoliona ameyafanya kwenye kazi yao. Wakapanga mipango mikubwa zaidi kuliko ya awali, lakini Yule Mwenye nguvu kuliko wao alikuwa anayashikilia maisha ya Luther. Lakini kazi yake haikuwa imekwisha. Marafiki wa Luther wakaharakisha kuondoka kwake kutoka Augsburg. Aliondoka mjini usiku, akiwa amepanda farasi bila hatamu, bila silaha, bila buti wala mahali pa kuwekea miguu mtu anapopanda farasi. Katika hali ya kuchoka sana alisafiri mpaka alipojumuika na marafiki zake. 1T 373.1

Ghadhabu ya upapa ikainuka tena, na wakaazimu kuufungakabisa mdomo wa mtetezi mkali wa Kweli asiye na woga. Wakamwita kwenda mji wa Worms, huku wakiwa wamejipanga kabisa kumfanya atoe majibu juu ya upuuzi wake. Alikuwa na hali dhaifu kiafya, lakini bado hakuleta kisingizio kuhusu afya yake. Alizijua kabisa hatari zilizokuwako mbele yake. Alijua kuwa maadui zake wakubwa wangelifanya lolote ili kumnyamazisha. Walikuwa wakiitaka damu yake kwa shauku kuu kama Wayahudi walivyoitaka damu ya Kristo. Lakini bado Luther alimtumainia Yule MUNGU aliyewatunza wale watu mashuhuri watatu katika tanuru la moto. Wasiwasi aliokuwa nao haukuwa juu yake mwenyewe. Hakuwa anajiwazia yeye mwenyewe na kujipatia maisha rahisi; bali wasiwasi wake mkubwa ulikuwa katika ile Kweli, ambayo ni ya thamani kwake, isianikwe kwenye matukano na wale wasiomcha MUNGU. Alikuwa tayari kufa kuliko kuwaruhusu maadui wa ile Kweli kushinda. Alipokuwa akiingia Worms, alifuatwa na msongamano wa maelfu ya watu. Watawala na watu wengine walio katika nyadhifa za juu waliwasili pasipo kulakiwa na umati mkubwa. Msisimko ulikuwa kubwa; na mmojawapo katika umati huo mkubwa, kwa sauti kali na yenye huzuni, aliimba wimbo wa mazishi kumuonya Luther juu ya kile kilichokuwa mbele yake. Lakini Mwanamatengenezo alikuwa ameshahesabu gharama na alikuwa tayari kutia muhuri kwa damu yake ushuhuda wake kama mapenzi ya MUNGU yakiwa hivyo. 1T 373.2

Luther alikuwa tayari kusimama mbele ya baraza kubwa la wapinzani wakuu, ili kuitetea imani yake, na alimtazama MUNGU kwa imani ili aweze kutiwa nguvu.

Kwa kipindi kifupi ujasiri na imani yake vilipimwa. Hatari za kila namna zilifunuliwa mbele yake. Naye akahuzunika. Mawingu yakatanda kumzunguka na kuuficha uso wa MUNGU asiuone. Alitamani sana kusonga mbele kwa ujasiri na uhakika kuwa MUNGU alikuwa pamoja naye. Asingeridhika kama MUNGU Asingekuwa pamoja naye, alitaka kuwa karibu na Mungu. Kwa kilio kikuu alipeleka ombi la uchungu mbinguni. Roho yake ilionekana kuzimia kwa kitambo mara zingine, wakati alipoona maadui zake walivyo wengi kwenye mafikara yake. Alitetemkea kwa kuiona hatari iliyo mbele yake. Niliona kuwa MUNGU kwa mapenzi yake alimwandaa Luther kwa namna hii ili asimsahau Yeye anayepaswa kutumainiwa, na kuwa asije akaharakisha kuingia katika hatari kwa kiburi na ujasiri usiokuwa na utii, na usiofuata mapenzi ya Mungu. Kama chombo CHAKE Mwenyewe, MUNGU alikuwa anamwandaa kwa kazi kuu iliyokuwa mbele yake. 1T 374.1

Ombi la Luther lilisikiwa. Ujasiri wake na imani vikarejea alipokutana na maadui zake. Akiwa mnyenyekevu kama mwana-kondoo alisimama, akiwa amezungukwa na wakuu wa dunia, ambao, kama mbwa mwitu wenye hasira, walikodoa macho yao kumwelekea, wakitarajia kumwogofya kwa mamlaka na ukuu walionao. Lakini alikuwa ameshapata nguvu ya MUNGU na kamwe hakuhofu. Maneno yake yalitamkwa kwa ujasiri, ukuu na mamlaka makubwa kiasi kwamba maadui zake wasingefanya lolote dhidi yake. MUNGU Ndiye aliyekuwa akizungumza kupitia Luther, na Ndiye aliyewakusanya pamoja watawala wa himaya na wenye hekima ili aweze kuwadhihirishia jinsi hekima yao ilivyo upuuzi mtupu, na kuwa wote wapate kuona uweza na ujasiri wa mwanadamu wa dhaifu anapomtegemea MUNGU, aliye mwamba wake. 1T 374.2

Utulivu wa Luther ulikuwa tofauti sana na hisia kali pamoja na hasira zilizodhihirishwa na watu walioitwa wakuu. Wasingaliweza kumtia hofu hadi akaogopa kiasi cha yeye kuikana Ile Kweli. Kwa uungwana, usahili, uimara wenye utulivu alisimama kama mwamba. Upinzani toka kwa maadui zake, ghadhabu na vitisho vyao, kama wimbi kuu, viliongezeka dhidi yake na kupasuka katika miguu yake bila madhara. Mtu huyu hakuyumbishwa. Walisikitishwa kuona kuwa mamlaka waliyonayo, ambayo yamewafanya wafalme na waungwana kutetemeka, yanadharauliwa na mtu wa hadhi ya chini, na huku walitarajia kumfanya apate kuihisi ghadhabu yao kwa kumtesa na kuondoa maisha yake. Lakini Yeye Aliye mkuu kuliko watawala wa dunia Ndiye aliyekuwa amempa maagizo shahidi huyu aliye jasiri. MUNGU alikuwa na kazi ambayo Luther alipaswa kuikamilisha. Na bado alipaswa kuteseka kwa ajili ya Kweli. Alipaswa kupita kwa shida katika mateso ya kumwaga damu. Alipaswa kupitia hali ya kuvikwa magunia na kulaumiwa na washabiki. Alipaswa kuishi ili kuithibitisha Kweli na kuwa mtetezi wake wakati ambapo mamlaka za juu za dunia zitakapotafuta kuirarua na kuiangusha chini. Alipaswa kuishi ili aione Kweli ikishinda na kuyaharibu makosa, ushirikina na upotofu wa upapa. Luther alipata ushindi akiwa Worms na kudhoofisha upapa, habari zikaenea katika

falme na mataifa mengine. Lilikuwa ni pigo la ufanisi, lililoutia nguvu mchakato wa Matengenezo. {1T 375.1}

Nilioneshwa watumishi wanaohubiri Kweli ya wakati huu kinyume na wanamatengenezo waliokuwa mstari wa mbele; hasa maisha ya Luther ya kujitoa na ari yakilinganishwa na maisha ya wahubiri wetu leo. Alithibitisha upendo wake usiokoma kwa Kweli ya Neno la MUNGU kwa namna alivyokuwa jasiri, imara, mtulivu na mwenye kujikana nafsi. Alijaribiwa na kuteswa, kuna nyakati alipata maumivu makubwa nafsini, alipojitoa kuisimamia Kweli; lakini hakunung'unika. Aliwindwa kama mawindo ya porini, lakini kwa uchangamfu alivumilia yote kwa ajili ya Kristo. {1T 375.2}

Ujumbe wa mwisho wa rehema umekabidhiwa kwa watumishi wa MUNGU wanyenyekevu, na waaminifu wa zama hizi. MUNGU amewaongoza wale wote ambao hawakwepi majukumu, na amewapa huu mzingo, na kupitia kwao amewasilisha mkakati wa utoaji kwa mpango na ukarimu kwa watu Wake ambapo wote waweza kujiunga nao na kutenda kwa mapatano. Mfumo huu umekuwa ukifanyika na umefanikiwa kimuujiza. Unawategemeza wahubiri pamoja na kusudi la Bwana kwa ukarimu. Mara tu wahubiri wanapoutokomeza upinzani wao, na kusimama kando, washiriki wanaitikia wito kwa moyo na wanathamini kutoa zawadi katika mfumo huu. Kila kitu kinakuwa rahisi na mazingira yanafanyika kuwa rafiki kwa wahubiri ili wapate kutenda kazi, bila aibu na shida. Watu wetu wamejitoa kwa mapenzi yao na shauku kubwa ambayo haipatikani kwa kundi liwalo lote. Na MUNGU anachukizwa na wahubiri ambao sasa wananung'unika na kushindwa kutoa nguvu zao zote kwa kazi hii yenye umuhimu mkuu. Hawana udhuru; lakini bado baadhi yao wanadanganyika na kufikiri kuwa wanajinyima kupita kiasi, na wanapitia wakati mgumu, huku wakiwa hawajui lolote kuhusu maonjo/mateso, kujikana nafsi, au dhiki. Wanaweza kupata uchovu; ila hata wangelikuwa wakitegemea kazi ya mikono kwaajili ya kipato ili kujikimu kimaisha, wangechoka pia. {1T 375.3}

Baadhi ya wahubiri wamefikiri kuwa ni rahisi kufanya kazi kwa mikono yao ili kujikimu kimaisha, badala ya kuajiriwa na kanisa, na mara nyingi wameeleza uchaguzi wao kufanya hivyo. Hawa hawajui walisemalo. Wanajidanganya wenyewe. Baadhi wanazo familia zinazowagharimu sana katika mahitaji yao, na wamekosa usimamizi. Hawatambui kuwa wanadaiwa na MUNGU hata nyumba zao wenyewe na vyote walivyonavyo. Hawajatambua gharama ya matumizi ya maisha ya kila siku. Endapo wangejihusisha na kazi za mikono ili kujikimu maisha yao, wasingekuwa huru kutoka kwa wasiwasi pamoja na uchovu. Wasingeweza kukaa nyumbani na kuota moto na wakati huo huo waweze kufanya kazi za mikono ili kusapoti familia zao kujikimu kimaisha. wakiwajibika kufanya kazi kwa ajili ya kutegemeza familia zao. Kwa kawaida mtu ambaye familia yake inamtegemea, na anafanya kazi za mikono, anaweza kukaa nyumbani pamoja na familia yake inayomtegemea kwa masaa machache tu. Baadhi ya watumishi hawapendi kuchapa kazi na kujifunza tasnia fulani, na

wameendekeza hali ya kutoridhika bila sababu. MUNGU ameona na kuzingatia kila wazo, neno na hisia za malalamiko. Mbingu inatukanwa kwa onesho hilo la udhaifu na kukosa kujitoa kwa ajili ya kazi ya MUNGU. 1T 376.1

Baadhi wamepeleka sikio la utayari kwa mjaribu na wamezungumza kuhusu kutoamini kwao na kuijeruhi kazi ya MUNGU. Shetani ana madai kuhusu watu hawa, kwa kuwa hawajaweza kujinasua kutoka katika mtego wake. Wametenda kama watoto wasiozifahamu kwa kina hila za mjaribu. Wangepaswa kuwa na uzoefu wa kutosha na kuzielewa kazi zake kwa sababu wana uzoefu wa kutosha. Adui amependekeza mashaka katika akili zao, na, badala ya kuyapinga yote mara moja, wamekuwa wakihojiana na kufanya naye dili (bargain), huyu mdanganyifu mkuu, na kusikiliza hoja zake, kama vile wanarogwa na huyu nyoka wa zamani. Mafungu machache ya Maandiko ambayo hayakuelezwa kikamilifu mpaka waridhishe akili zao, yametosha kabisa kuutikisa muundo mzima wa ile Kweli na kuziletea utata na giza hoja zile za Kweli zilizo wazi katika Neno la MUNGU. Watu hawa ni wakosefu, na wenye mwili unaokufa. Hawana hekima kamilifu na ufahamu katika Maandiko yote. Baadhi ya Aya za Maandiko hazieleweki katika akili za kibinadamu, na zimeweka mahali ambapo akili za mwanadamu haziwezi kuzifikia mpaka wakati utakapofika ambao MUNGU, kwa hekima Yake, atawafunulia. Shetani amekuwa akiwaongoza baadhi katika njia ielekeayo kwenye ukafikiri-ukana-Mungu. Wameteseka kwa kutokuamini kwao kiasi kwamba mtiririko mzuri na uliotulia wa Ukweli umetiwa giza, na wamechukulia kama ndiyo ilikuwa biashara yao kutatua kila Aya ngumu katika Maandiko, na kama imani yetu haikuwawezesha wao kufanya hili, basi hiyo imani ina makosa. {1T 377.1}

Niliona kuwa wale walio na moyo mwovu wa kutoamini, na hawa watatilia shaka na kufikiri kuwa ni sahihi, uungwana na fadhila kulitilia shaka Neno la MUNGU. Wale wanaofikiri kuwa ni fadhila kukosa na kutilia mashaka Neno, wanaweza kujitengenezea mazingira makubwa ya kutoamini uvuvio na Kweli ya Neno la MUNGU. Mwenyezi MUNGU hamlazimishi yeyote kuamini. Wanadamu waweza kuchagua kuamini uthibitisho ambao Yeye amependezwa kuufunua, au kutilia shaka, na wasiwasi, kujishugulisha na mambo madogomadogo na kuangamia. 1T 377.2

Nilioneshwa kuwa wale wote wanaosumbuliwa na mashaka, Kukosa uaminifu na ukafiri, hawapaswi kwenda kufanya kazi ya kuongoa wengine. Kile kilichopo akilini ni lazima kitiririke nje, na hawatambui madhara ya kudokeza mashaka na kuyaelezea, hata kama ni kwa udogo kiasi gani. Shetani anayafanya mashaka kuwa mshale wenye ncha kali yenye sumu na ndoano. Mashaka yatenda kazi kama sumu ipenyayo taratibu, ambayo, kabla ya mhanga kuitambua hatari aliyonayo, inaathiri mfumo mzima, na kudhoofisha afya ya mwili na nguvu ya utambuzi, na hatimaye kuleta kifo. Haya ndiyo matokeo ya sumu ya mashaka

na kutoamini Kweli za Maandiko. Yule aliye na mvuto anapendekeza kwa wengine kile alichopendekezewa na Shetani, kuwa Andiko hili linapingana na lingine; na hivyo, kwa werevu, kana kwamba amepata siri ya ajabu ambayo ilikuwa imefichika kwa waumini na watakatifu wa ulimwengu wa zama zote, analeta giza la utusitusi kwa wengine. Wanapoteza ladha na furaha waliyokuwa nayo awali kwa ajili ya ile Kweli na kuwa na makafiri-Wakana-Mungu. Hii yote ni kazi ya maneno machache yaliyozungumzwa, ambayo yana nguvu iliyositirika kwa kuwa yanaonekana kuhusishwa na mafumbo, siri au vitendawili. 1T 377.3

Hii ni kazi ya Shetani aliye mwerevu na mwenye hila. Wale wote wanaosumbuliwa na mashaka, na wana magumu wasiyoweza kuyatatua, hawapaswi kuzitupa akili za wengine walio dhaifu katika mkanganyiko huohuo. Baadhi wamedokeza au kuzungumza hali ya kutoamini kwao, na kuendelea na maisha yao, bila ya kutambua hata kwenye ndoto zao matokeo ya maneno yao yalikuwa ni nini kwa watu walioyasikia maneno yao. Mara zingine mbegu za kutoamini zimeleta matokeo ya papo hapo kwa ghafla, wakati kwa wengine zimefukiwa kwa muda mrefu, mpaka mtu awe amekosea njia na kumpa adui nafasi, na nuru ya MUNGU kuondolewa kwake, na kuanguka katika majaribu yenye nguvu ya Shetani. Kisha mbegu za uharibifu na uharibifu zilizopandikizwa muda mrefu uliopita zinachipua. Shetani anaziwekea lishe/mbolea, na zinazaa matunda. Chochote kitokacho kwa watumishi ambao wanapaswa kusimama katika nuru kina mvuto mkubwa. Na wanapokuwa hawajasimama katika nuru angavu ya MUNGU, Shetani anawatumia kama mawakala ambao kupitia kwao anapeleka mishale ya moto kwa wale ambao akili zao hazijajiandaa kupingana na kile kinachotoka kwa wachungaji wao. {1T 378.1}

Niliona kuwa watumishi, pamoja na washiriki, wana vita iliyopo mbele yao ya kumpinga Shetani. Mtu anayejidai kuwa ni mchungaji/mhudumu wa Kristo yupo katika nafasi ya hatari anapotumikia makusudi ya mjaribu, kwa kusikiliza minong'ono yake, na kumruhusu apate kuiteka akili na kuongoza mawazo. Dhambi mbaya zaidi ya mchungaji/mhudumu mbele ya macho ya MUNGU ni kuzungumza kuhusu kutoamini kwake mbele ya wengine na kuwashawishi wengine katika mkondo huohuo wa giza, hatimaye kumwachia Shetani kutekeleza mambo mawili katika kumjaribu. Kwanza anavuruga akili ya yule ambaye mwenendo wake umechochea kujaribiwa kwake na kisha anamwongoza mtu huyo kuvuruga akili za wengi. {1T 378.2}

Ni wakati kwa walinzi juu ya kuta za Sayuni kuelewa wajibu na utakatifu wa utume wao. Wanapaswa kuhisi kuwa ole i juu yao kama hawatendi kazi ambayo MUNGU amewapatia kuifanya. Kama wanakosa uaminifu, wanahatarisha usalama wa kundi la MUNGU, wanahatarisha kusudi la Kweli, na kuliweka katika hatari ya kejeli za maadui zetu. Oh, kazi ya kushtua kiasi gani hii! Ama kwa hakika itapokea ujira wake. Baadhi ya wachungaji, pamoja na washiriki/walei,

wanahitaji kubadilika. Wanahitaji kuraruliwa vipande vipande na kuundwa upya. Kazi yao miongoni mwa makanisa ni mbaya zaidi ya kazi iliyopotea kabisa, na sasa katika hali yao dhaifu, yenye kuyumbayumba, itakuwa vema machoni pa MUNGU kama watakoma kuelekeza jitihada zao katika kuwasaidia wengine, na kufanya kazi kwa mikono yao ili kujikimu kimaisha kama walei, mpaka pale watakapoongoka. Ndipo wawaimarishe ndugu zao. {1T 379.1}

Wachungaji wanapaswa kuamka. Wanadai kwamba wao ni makamanda katika jeshi la Mfalme mkuu, na wakati huo huo wao wanamwonea huruma mwasi mkuu pamoja na majeshi yake. Baadhi wameyaanika kusudi la MUNGU, pamoja na Kweli takatifu za Neno Lake, kwenye malaumu ya majeshi ya mwasi. Wameondoa sehemu ya silaha zao, na Shetani amewatupia kwa nguvu mishale yake yenye sumu. Wameipa nguvu mikono ya viongozi waasi, na kujidhoofisha wao wenyewe, na kusababisha Shetani na malaika zake kuinua vichwa vyao kwa ushindi, na kujisifu kwa kushangilia ushindi waliompatia. Oh, huku ni kukosa hekima kiasi gani! Ni upofu wa ajabu kiasi gani! Ni ujenerali wa kipumbavu kiasi gani kufunua madhaifu yao kwa adui zao wakubwa! Ni tofauti kiasi gani ukilinganisha na Luther alivyofanya! Alikuwa tayari kuyatoa maisha yake dhabihu, kama ikihitajika, lakini kutoa kafara ile Kweli, hapana! Maneno yake ni haya: “Hebu tuhakikishe kuwa tunailinda injili isije ikatukanwa na wanadamu wasiomcha MUNGU, na hebu tumwage damu zetu kwa ajili ya kuilinda, kuliko kuwaacha wao wapate ushindi. Je, ni nani atakayesema kuwa maisha yangu au kifo changu kilichangia kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya wokovu wa ndugu zangu?” {1T 379.2}

MUNGU hamtegemei mwanadamu yeyote kwa ajili ya kutimiliza kusudi Lake. Yeye Anawainua na kuwaandaa watu kwa sifa stahiki kwa ajili ya kuubeba ujumbe kwa ulimwengu. Yeye Anaweza kuzikamilisha nguvu Zake katika udhaifu wa watu. Uweza ni wa MUNGU. Utayari wa kuzungumza kwa ufasaha, vipaji vikuu, haviwezi kuongoa hata roho moja. Jitihada mimbarini zinaweza kuwasismua watu, hoja zilizo wazi zaweza kushawishi, lakini MUNGU Ndiye Mwenye Kukuza, kuongeza na kuongoa. Watauwa, waaminifu, watakatifu, wanaokiishi kile wanachokihubiri, wataleta mvuto uokoao. Hubiri lenye nguvu litolewalo mimbarini laweza kuleta matokeo katika akili za watu; lakini tendo dogo la kijinga lifanywalo na mchungaji nje ya mimbari, kukosa umakini katika hotuba pamoja na utauwa wa kweli, vitaharibu mvuto wake, na kuondoa mivuto mizuri yote aliyoifanya. Waongofu watakuwa wa kwake; kila wakati hawatatafuta kupanda juu kiroho zaidi ya mchungaji wao (washiriki wanapenda kufanana na mchungaji wao). Hapatakuwa na kazi kamilifu ya moyo ndani yao. Si waongofu kwa MUNGU. Kazi ni ya juu juu tu, na mvuto wao utaleta maumivu kwa wale wamtafutao Bwana kweli kweli. {1T 380.1}

Mafanikio ya mchungaji/mhudumu yanategemea sana mazoea, mwenendo, hulka tabia yake nje ya mimbari. Pale amalizapo kuhubiri na kutoka mimbarini, kazi yake haijaisha bado, ndiyo kwanza inaanza. Anapaswa kukiishi kile alichokihubiri. Hapaswi kuishi maisha ya kutokujali, na kutokusikia na kutenda Neno, bali anapaswa kujilinda, ili asije akatenda au kunena kwa kumpa adui nafasi na faida, na kazi ya Kristo ikalaumiwa. Wachungaji hawawezi kujilinda vya kutosha (wanapaswa kuwa waangalifu), hasa wawapo mbele ya vijana. Wanapaswa kuyapa uzito wanayoyazungumza-wazungumze kwa umakini, hawapaswi kufanya mizaha au futuhi, huku wakikumbuka kuwa wapo kwa niaba ya Kristo, na kwamba wanapaswa kudhihirisha kwa mfano maisha ya Kristo. “Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na MUNGU ”. “Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya MUNGU bure”. {1T 380.2}

Nilioneshwa manufaa ya watumishi vijana, waliooa au waseja, unaharibiwa na kufungamana kwao na vijana wa kike. Hao hawatambui kwamba macho ya wengine yanawaona, na kwamba wanachokifanya kinaweza kuharibu kabisa mvuto wa mtumishi aliyekuwa akiangaliwa sana kwa makini kama mfano. Kama wangelizingatia kanuni za tabia njema na kujistahi, ingelikuwa vizuri kwao na vizuri zaidi kwa mchungaji wao. Hii inamweka mtumishi katika hali isiyokubalika na kuwafanya wengine kumtazama yeye katika nuru mbaya. Hata hivyo nilioneshwa kuwa mzigo huo wote unabakia kwa watumishi wao wenyewe. Wanapaswa kuchukia vitu hivi, na kama wakienda katika njia ambayo MUNGU anawataka waiendee, hawatataabishwa kwa muda mrefu. Wanapaswa kupinga/kuuepuka hichi kimbelembele cha wasichana kuja kwao, hata kama wataonekana ni wakorofi au wajeuri kusema hivyo (wachungaji vijana wasiruhusu wasichana wawatongoze), na wakati ambapo vijana wa kike wanataka kuonesha ukaribu mkubwa kwao, ni wajibu wao kuwajulisha kuwa hilo halitakiwi kwani linaleta lawama kwa kazi ya Mungu. Mambo hayo yanapaswa kukemewa ili kazi ya Bwana isilaumiwe. Mabinti ambao wameongoka katika ile Kweli na kwa MUNGU watasikia maonyo na makatazo na kubadilika. {1T 381.1}

Watumishi wanapaswa kutumia jitihada binafsi kwa ajili ya kufuatilia kazi ya MUNGU waliyoifanya hadharani, kutenda kazi kwa mtu mmoja mmoja kwa ajili ya kuongoa roho wakati wowote fursa ipatikanapo, kufanya mazungumzo nyumbani wanapokuwa wamepumzika na kukota moto, na kuzisihi roho kutafuta vile vyote vinavyowapatia amani. Kazi yetu hapa karibuni itafika mwisho, na kila mtu atapokea ujira kulingana na kazi yake mwenyewe. Nilioneshwa ujira wa watakatifu, urithi wa uzima wa milele, na niliona kwamba wale wote ambao wamevumilia sana kwa ajili ya ile Kweli hawataona kuwa walipitia katika kipindi kigumu, bali kwao mbingu itakuwa kitu chepesi mno kukipata. {1T 381.2}

## SURA YA 71

## MATUMIZI MABAYA YA MAONO.

Nimeoneshwa kwamba, wengine, hususani kule jimbo la Iowa, wamefanya maono kuwa kanuni ya kupima kila kitu, na wamechukua njia/kusudi ambalo mume wangu na mimi hatukulifuata. Wengine hawanifahamu mimi vizuri na kazi zangu na wanashuku sana chochote kinachobeba jina la maono. Na jambo hili ni la asili tu na linaweza kushindwa kwa uzoefu. Kama watu hawajawa na utulivu kuhusu maono wasilazimishwe kuyakubali. Somo la kuwasaidia katika jambo hili linaweza kupatikana katika kitabu cha Shuhuda kwa Kanisa Gombo la 8, uk. 328,329, ambacho natumaini kitasomwa na wote. Wachungaji lazima wawe na huruma kwa wengine, wakifanya tofauti, wengine waokoeni kwa hofu, mkiwatoa ndani ya moto. Wachungaji wa MUNGU wanapaswa kuwa na hekima kumpa kila mmoja sehemu ya chakula chake, na kufanya tofauti na watu tofauti kama masuala yao yanavyohitaji. Mwenendo unalochukuliwa na baadhi ya watu huko Lowa ambao hawanifahamu vizuri halijawa la uangalifu na thabiti. Wale ambao kwa kulinganisha walikuwa wageni kwa njozi wameshughulikiwa kwa hali sawa na wale waliokuwa na nuru kubwa na uzoefu kuhusu maono. Wengine wametakiwa kuidhinisha maono wakati hawawezi kufanya hivyo kwa kwa dhamiri yenye uangalifu, na kwa njia hii baadhi ya roho aminifu zimeongozwa kuchukua msimamo dhidi ya maono na dhidi ya kanisa ambao wasingeuchukuwa kama masuala yao yangeshughulikiwa kwa usahihi, hekima na kwa rehema. { T1 382.1}

Baadhi ya ndugu zetu wamekuwa na uzoefu wa muda mrefu katika Ukweli na kwa miaka mingi sasa wamenifahamu na ushawishi wa maono. Wamezijaribu Kweli za shuhuda hizi na kutia imani yao kwazo. Wamehisi ushawishi wenye nguvu wa roho ya MUNGU uliowakalia na kushuhudia Kweli za maono. Watu wa namna hiyo wanapokemewa kupitia njozi wanachukia, na wanafanya kazi kwa

siri kujeruhi ushawishi wetu, basi wanapaswa kushughulikiwa kwa uaminifu, kwani ushawishi wao unawahatarisha wale wasio na uzoefu. {1T 382.2}

Wahudumu wa Ukweli wa sasa, wakati wakiwa wamebeba ushuhuda ulioelekezwa, kukemea makosa ya watu, na wakitafuta kuiondolea mbali sanamu kutoka katika kambi ya Israel, lazima waoneshe uvumilivu. Lazima wauhubiri Ukweli katika uzito wake na umuhimu wake. Na kama jambo hili likipata njia yake kwenye moyo litakamilisha kwa mpokeaji kile ambacho hakuna kitu kinachoweza kufanya. Lakini kama uKweli uliosemwa kwa maonesho ya Roho na haukukatilia mbali sanamu/miungu, haitakuwa na faida kumshutumu na kumbebesha mzigo mtu binafsi. Inaweza kuonekana kuwa wengine wameunganishwa na sanamu zao, ingawa naona kwamba tusiwe wepesi kuwakatia tamaa wanyonge waliopotoshwa. Lazima daima tujue kuwa sisi ni viumbe wenye kasoro na tunaokosea, na kwamba Kristo huvumilia kwa huruma nyingi udhaifu wetu, anatupenda japo tunakosea. Kama MUNGU angeshughulika nasi kama mara nyingi tunavyoshughulika na kila mmoja wetu, tungepaswa kuwa tumekwisha zamani. Wakati wachungaji wanapohubiri wazi, ukweli unaokata, lazima wauache Ukweli ufanye kazi ya kukata na sio wafanye wao wenyewe. Lazima waweke shoka, Ukweli wa Neno la MUNGU, katika shina la mti, na jambo fulani litakamilishwa. Mwaga ushuhuda kama ulivyo katika Neno la MUNGU, ukiwa umenyoka, na moyo uliojaa joto, ukiharakisha ushawishi wa Roho Wake, yote kwa kilio cha moyo wa unyenyekevu na mwororo, katika Roho, na kazi ya MUNGU miongoni mwa watu itakuwa yenye ufanisi. Sababu ya kwa nini kuna udhihirisho kidogo wa ROHO WA MUNGU ni kwa sababu wachungaji hujifunza kufanya kazi bila Yeye. Wanakosa neema ya MUNGU, wanakosa subira na uvumilivu, wanakosa moyo wa utakaso na kujitoa wakfu; na hii ndiyo sababu pekee ya kwa nini wengine wanatilia mashaka ushahidi wa Neno la MUNGU. Shida haipo katika Neno la MUNGU bali ndani yao. Wanakosa neema ya MUNGU, wanakosa kujitoa kikamilifu, utakaso binafsi, na utakatifu. Hii huwapelekea kukosa utulivu na kuwatupa mara kwa mara katika uwanja wa vita wa Shetani. Niliona kwamba haijalishi watu wameutangaza Ukweli kwa nguvu kiasi gani, hata kama wanaonekana ni wacha MUNGU, pale wakianza kuzungumzia kutokuwa na imani na baadhi ya Maandiko, wakidai kwamba yanawasababishia mashaka juu ya uvuvio wa Biblia, tunapaswa kuwaogopa, kwani MUNGU Yuko mbali nao. {1T 383.1}.

## SURA YA 72

## WAZAZI NA WATOTO

Nimeoneshwa kuwa wakati wazazi ambao wana hofu ya MUNGU mbele yao wanawazuia watoto wao, wanapaswa kusoma tabia zao na hulka zao, na kutafuta kufikia mahitaji yao. Wazazi wengine huhudumia kwa uangalifu mahitaji ya muda ya watoto wao; kwa upole na kwa uaminifu huwauguza katika ugonjwa (chakula, mavazi nk), halafu wanafikiria kuwa wajibu wao umefanywa. Hapa wanakosea. Hapa ndipo tu Kazi yao imeanza. Matakwa ya akili yanapaswa kushugulikiwa kwa umakini. Inahitaji ustadi kutumia tiba sahihi ili kuponya akili iliyojeruhiwa. Watoto wana majaribu ambayo ni vigumu kuyabeba, wana tabia za kusikitisha, kama yale ya watu wazima. Wazazi wenyewe hawahisi sawa wakati wote. Akili zao mara nyingi zinakuwa katika mtanziko. Wanafanya kazi chini ya maoni na hisia zisizofaa. Shetani huwapiga, na wanakubali majaribu yake. Wanazungumza kwa hasira, na kwa njia ya kusisimua gadhabu kwa watoto wao, na wakati mwingine ni wakali, wanaudhika kirahisi na ni walalamishi. Watoto masikini hushiriki roho ile ile, na wazazi hawajawa tayari kuwasaidia, kwani walikuwa sababu ya shida hii. Wakati mwingine kila kitu kinaonekana kwenda mrama. Kuna ukali na kuudhika-udhika pande zote, na wote wana wakati wa kusikitisha, usio na furaha. Wazazi huweka lawama juu ya watoto wao maskini na wanawafikiria ni hawa watoto ni waasi sana na wasioweza kutawalika, watoto wabaya zaidi ulimwenguni, wakati sababu ya usumbufu iko ndani yao wazazi. {1T 384.1}

Wazazi wengine huibua dhoruba nyingi kwa kushindwa kwao kujizuia nafsi. Badala ya kuwauliza kwa upole watoto kufanya hili au lile, wanawaamuru kwa sauti ya kukaripia/kugombeza, na wakati huo huo lawama au kukaripia kupo kwenye midomo yao ambako watoto hawajastahili. Wazazi, mwenendo huu mnaoufuata kuelekea watoto wenu unaangamiza uchangamfu na shauku yao. Wanafanya mashinikizo yenu, sio kutokana na upendo, lakini kwa sababu

hawathubutu kufanya vinginevyo. Moyo wao hauko katika jambo hilo. Ni kazi ngumu, badala ya raha, na mara nyingi hii huwaongoza kusahau kufuata maagizo yako yote, ambayo huongeza uchungu wako na kuudhika, na kuifanya iwe mbaya zaidi kwa watoto. Utafutaji wa makosa unarudiwa, mwenendo wao mbaya umevaliwa mbele yao kwa rangi inayong'aa (matusi na lugha mbaya), hadi kukatishwa tamaa kunakuja juu yao, na hawaweki umakini tena ikiwa wanatenda sawa au la! -kama wanawapendeza wazazi au la! Roho ya "mimi wala sijali" inawakamata, na wanatafuta raha hiyo na starehe mbali na nyumbani, mbali na wazazi wao, ambayo hawapati nyumbani. Wanajichanganya na makundi ya watu wa mitaani na punde wanakuwa mafisadi wabaya kama watu wengine waovu tu. {1T 384.2}

Je! Dhambi hii kubwa iko juu ya nani? Kama nyumba ingefanywa kuwa ya kupendeza, kama wazazi wangeonesha mapenzi kwa watoto wao, na kwa fadhili kuwatafutia kitu cha kufanya kwa upendo, na kuwaelekeza jinsi ya kutii matakwa yao, wangegusa kichocheo cha mwitikio wa majibu mazuri mioyoni mwao, kisha miguu, mikono, na mioyo iliyo tayari, vyote vingekuwa tayari kuwatii wazazi. Kwa kujidhibiti, na kuongea kwa upole na fadhila, na kuwasifu watoto wanapojaribu kufanya sawa, wazazi wanaweza kuhamasisha juhudi zao, kuwafanya wafurahi sana, na kutupa juu ya mzunguko wa familia sumaku na kinga ambayo itafukuza kila kivuli cha giza na kuleta mwangaza wa jua. {1T 385.1}

Wakati mwingine wazazi hutetea njia yao mbaya kwa sababu hawajisikii vizuri. Wana wasiwasi, na wanafikiria hawawezi kuwa wavumilivu na watulivu, na wanaozungumza kwa furaha. Katika hili wanajidanganya na kumpendeza Shetani, ambaye anafurahi kwamba neema ya MUNGU haizingatiwi kama yatosha kushinda udhaifu wa asili. Wanaweza na wanapaswa kujidhibiti wakati wote. MUNGU anahitaji kitu hicho kutoka kwao. Wanapaswa kutambua kwamba wakati wanapokosa uvumilivu, wanapofadhaika na kuwa wakali na kuudhika-udhika, husababisha wengine kuteseka. Wale wanaowazunguka wanaathiriwa na roho wanayoonesha, na ikiwa wao kwa upande wao watatenda kwa roho hiyo hiyo, uovu huongezeka na kila kitu huenda vibaya. {1T 385.2}

Wazazi, wakati mnapojihisi tashwishwi, au kuudhika/hasira, haifai kufanya dhambi kubwa sana kwa kuwa sumu kwa familia nzima kwa hasira hii yenye hatari. Wakati kama huo jiwekeeni uangalizi maradufu, na amueni mioyoni mwenu kutokukosea kwa midomo yenu, ili mtamke tu maneno ya kupendeza na ya kufurahisha. Jiszungumzieni wenyewe: "Sitapunguza furaha ya watoto wangu kwa neno la uchungu." Kwa kujidhibiti hivi, mtakua wenye nguvu. Mfumo wako wa fahamu/neva hautasisimliwa sana. Utaimarishwa na kanuni za haki. Ufahamu kwamba unatekeleza wajibu wako kwa uaminifu; utakutia nguvu. Malaika wa MUNGU watatabasamu kwa ajili ya juhudi zako na kukusaidia.

Unapohisi kukosa subira, mara nyingi unafikiri sababu iko kwa watoto wako, na unawalaumu wakati hawakustahili. Wakati mwingine wanaweza kufanya mambo yaleyale unayofanya wewe, na yote yatakubalika na yataonekana sawa. Watoto wanajua, na kuweka alama, na kuhisi kasoro hizi, na siyo sawa kila wakati. Wakati mwingine wamejiandaa kukidhi hali za kubadilika (mudi zinazobadilika), na wakati mwingine huwa na wasiwasi na uchungu, na hawawezi kuvumilia malaumu, kukolewa na kugombezwa. Roho yao huinuka kwa uasi dhidi ya hali hiyo. Wazazi wanapenda watoto wao wawaelewe na kuwapa rehema zinazostahili kwa hali yao ya akili, lakini sio kila mara wanaona umuhimu wa kutoa rehema na uelewa wa hali kwa usawa, kwa watoto wao masikini. Wanajitolea udhuru ndani yao kwa mazoea ambayo ikiwa yataonekana kwa watoto wao ambao hawana uzoefu wa miaka na nidhamu, wangekikemea sana na kukikosoa. Wazazi wengine wana hulka ya wasiwasi, tashwishi na kufadhaika kwa urahisi na wanapokuwa wamechoka na kazi au wamekandamizwa na masumbufu, hawahifadhi hali ya utulivu wa akili, lakini hudhihirisha kwa wale ambao wanapaswa kuwa wapenzi wao hapa duniani, kuudhika-udhika, hasira na ukosefu wa uvumilivu ambao haumfurahishi MUNGU na kuleta wingu juu ya familia. Watoto, katika shida zao, mara nyingi wanapaswa kutulizwa na huruma nyororo. Upole na uvumilivu wa pande zote utafanya nyumbani kuwa paradiso na kuvutia malaika watakatifu katika mzunguko wa familia. {1T 386.1}

Mama anaweza na anapaswa kufanya mengi kuelekea kudhibiti mishipa yake ya fahamu na akili wakati anapokuwa katika msongo au huzuni; hata wakati anaumwa, anaweza, ikiwa atajifunza mwenyewe, kuwa wa kupendeza na mchangamfu, na anaweza kustahimili kelele zaidi ya vile anavyoweza fikiri. Haipaswi kuwafanya watoto kuhisi udhaifu wake na kuwachanganya akili zao changa na nyeti kwa msongo wake na sononeko lake la roho, na kuwasababisha kuhisi kwamba nyumba ni kaburi na kwamba karibu na mama ndipo mahali pabaya zaidi ulimwenguni. Akili na mishipa ya fahamu hupata toni na nguvu kwa kufanyiwa mazoezi utashi, ya nia. Nguvu ya utashi, nia na mapenzi ya mtu katika visa vingi itathibitisha kutuliza mishipa. {1T 387.1}

Usiruhusu watoto wako wakuone na uso uliojaa mawingu. Ikiwa wameanguka katika jaribu, na baadaye kuona na kutubu makosa yao, wewe wasamehe kwa moyo mkunjufu kama vile unavyotarajia kusamehewa na Baba yako aliye mbinguni. Waelekezeni kwa upole, na muwafunge katika mioyo yenu. Ni wakati muhimu kwa watoto. Vishawishi vitatupwa karibu nao ili kuwaondoa kutoka kwenu, ambavyo lazima mpambane navyo. Wafundishe kukufanya wewe kuwa msiri wao. Hebu wakunong'oneze masikioni mwako majaribu na furaha yao. Kwa kuhimiza jambo hili, utawaokoa kutoka katika mitego mingi ambayo Shetani ameiandaa kwa ajili ya miguu yao isiyo na uzoefu. Usiwatendee watoto wako kwa ukali tu, ukisahau utoto wako mwenyewe, na kusahau kuwa wao ni

watoto tu. Usitarajie wawe wakamilifu au kujaribu kuwafanya wanaume na wanawake katika matendo yao kwa mara moja. Kwa kufanya hivyo, utafunga mlango wa ufikiaji ambao unaweza kuwa nao, na utawasukuma kufungua mlango wa ushawishi mbaya na wenye kujeruhi, kwa wengine kutia sumu akili zao changa kabla hujazinduka na kushughulikia hatari yao.{1T 387.2}

Shetani na jeshi lake wanafanya juhudi kubwa zaidi kuyumbisha akili za watoto, na lazima watendelewe kwa kuweka mambo wazi kwa uaminifu na hekima, upole wa Kikristo, na upendo. Hii itakupa ushawishi wenye nguvu juu yao, na watahisi kuwa wanaweza kurelax/kupumua kwa raha wanapoweka imani yao isiyo na kikomo juu yako. Tupa karibu na watoto wako vivutio vizuri vya kuwapendeza kama sumaku za nyumbani (charm) na za jamii yako. Ukifanya hivi, hawatakuwa na shauku kubwa ya kushikamana na makundi rika katika jamii. Shetani hufanya kazi hii kupitia mambo haya, akiwaongoza kushawishi na kuharibu akili miongoni mwao wenyewe kwa ufisadi. Ni njia yenye ufanisi zaidi ambayo adui anaweza kufanya kazi. Vijana wana ushawishi mkubwa juu ya wenzao. Mazungumzo yao mara nyingi si yale yanayofaa au yaliyoinuliwa. Mawasiliano ya uovu hupuliziwa ndani ya masikio, ambayo, ikiwa hayakupingwa kwa uamuzi, hupata makao moyoni, huota mizizi, na kuchipuka ili kuzaa matunda na kuharibu mazoea, hulka na tabia njema. Kwa sababu ya maovu yaliyopo sasa ulimwenguni, na vizuizi vinavyohitajika kuwekwa juu ya watoto, wazazi wanapaswa kuwa na umakini na utunzaji maradufu wa kuifunga kwa mioyo yao na kuwaacha waone kwamba wana matamanio ya kuwafurahisha. {1T 387.3}

Wazazi hawapaswi kusahau miaka yao ya utoto, ni kiasi gani walitamani huruma na upendo, na jinsi walivyojisikia kukosa furaha wakati walipolaumiwa, walipokosolewa na kugombezwa kwa hasira. Wanapaswa kuwa vijana tena katika hisia zao na kuleta akili zao chini kwenye uelewa wa mahitaji ya watoto wao. Walakini kwa uthabiti, uliochanganywa na upendo, wanapaswa kuhitaji utii kutoka kwa watoto wao. Neno la wazazi linapaswa kutiiwa kabisa. {1T 388.1}

Malaika wa MUNGU wanawatazama watoto kwa shauku kubwa zaidi ili kuona ni tabia gani wanazoziendeleza. Ikiwa Kristo angeshughulika nasi kama tunavyoshughulikiana sisi kwa sisi na watoto wetu, tungejikwaa na kuanguka kwa kuvunjika moyo kabisa. Niliona kwamba Yesu anajua udhaifu wetu, na Yeye Mwenyewe alishiriki uzoefu wetu katika mambo yote lakini siyo katika dhambi; kwa hivyo Yeye ametuandalia njia inayofaa nguvu zetu na uwezo wetu, na, kama Yakobo, alivyoandamana na watoto katika safari polepole, na kwa hatua zinazofanana hadi jioni kadri watoto wake walivyoweza kuvumilia, ili atuburudishe kwa faraja ya uwezo na ushirika Wake, na kuwa kwetu mwongozo wa milele. Yeye Hawadharau, hawapuuzi, au huwaacha watoto wa

kundi. Yeye Hajatuamuru tuendelee mbele na kuwaacha. Yeye Hajasafiri haraka hata kutuacha na watoto wetu nyuma. Lo, hapana; lakini Yeye ameweka sawa njia ya uzima, hata kwa watoto. Na wazazi wanahitajika kwa Jina Lake kuwaongoza katika njia nyembamba. MUNGU ametuteulia njia inayofaa kwa nguvu na uwezo wa watoto. 1T 388.2}

## SURA YA 73

## KAZI HUKO MASHARIKI

Nimeoneshwa kuwa wakati umefika wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi Mashariki. Umuhimu wa Kupanga kanisa kama taasisi au shirika na kuwa na mfumo mwishowe umehisiwa huko (Organzation of the Seventh Day Adventist Church ilikuwa May 20-23, 1863). Wachungaji hawatalazimika kufanya kazi chini ya kukatishwa tamaa kama hapo awali. Malaika wa rehema anazunguka juu ya Mashariki. Malaika akasema: "Imarisha vitu vilivyobaki. Tangaza ujumbe kwa wale ambao hawajausikia." Kuna wengine Mashariki ambao watakuwa katika hatari ya kuwa itikadi kali za kupitiliza wakati Bwana atakapofufua kazi yake kati yao. Wanapaswa kukumbuka kwamba Bwana aliondoa kazi Yake kutoka kwao kwenda Magharibi ili kuwanyenyekeza, na kusalimisha roho huru, ya uasi ndani yao, na kuwaongoza kupata tuzo bora za juhudi za watumishi Wake waaminifu. {1T 389.1

# SURA YA 74

# HATARI ZA VIJANA

Juni 6, 1863, nilioneshwa hatari kadhaa za vijana. Shetani anazidhibiti fikira za vijana na kupotosha miguu yao isiyo na uzoefu. Hawajui hila na mbinu zake, na katika nyakati hizi za hatari wazazi wanapaswa kuwa macho na kufanya kazi kwa uvumilivu, bidii ya kazi na tasnia ili kuzima njia ya kwanza ya adui. Wanapaswa kuwafundisha watoto wao wanapotoka na wanapoingia, wanapoinuka, na wanapoketi, wakitoa mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo (KumbuKumbu 6). {1T 390.1}

Kazi ya mama huanza na mtoto mchanga. Anapaswa kutiisha mapenzi, hulka, mazoea, haiba na hasira ya mtoto wake, na kumleta katika utii, kumfundisha kutii. Kwa kadri mtoto anavyokua, usipumzishe mkono (usimamizi). Kila mama anapaswa kuchukua muda kusemezana na watoto wake, kurekebisha makosa yao, na kuwafundisha kwa uvumilivu njia sahihi. Wazazi Wakristo wanapaswa kujua kwamba wanawafundisha, wanawaongoza na kuwafaa watoto wao kuwa watoto wa MUNGU. Uzoefu wote wa kidini wa watoto unaathiriwa na maagizo yaliyotolewa, na tabia iliyoundwa, katika utoto. Ikiwa utashi haujatiishwa na kufanywa kutolewa kwa mapenzi ya wazazi, itakuwa kazi ngumu kujifunza somo miaka ya baadae. Mapambano makali kiasi gani, ni mgogoro mikubwa namna gani, kusalimisha utashi ambao hayajawahi kutiishwa, kwa mahitaji ya MUNGU  Wazazi ambao hupuuza kazi hii muhimu hufanya kosa kubwa, na wanatenda dhambi kwa watoto wao maskini na dhidi ya MUNGU. {1T 390.2}

Watoto ambao wako chini ya nidhamu kali wakati mwingine watakuwa na hisia zisizoridhika. Watakosa subira chini ya vizuizi, na watataka kuwa na njia yao wenyewe, na kwenda na kuja  kama watakavyo. Hasa kutoka umri wa miaka kumi hadi kumi na nane, mara nyingi watahisi kuwa hakutakuwa na ubaya wowote kwenda kwenye pikniki na mikusanyiko mingine ya makundi-rika; lakini wazazi wao wenye ujuzi wanaweza kuona hatari. Wanazifahamu tabia za kipekee za watoto wao na wanajua ushawishi wa vitu hivi juu ya akili zao, na kutoka katika shauku ya wokovu wao wawazuie kutoka kwa maburudisho/matumbuizo yanayoleta msisimko. Wakati watoto hawa wanapoamua wenyewe kuacha starehe za ulimwengu na kuwa wanafunzi wa Kristo, ni mzigo ulioje unaotuliwa mioyoni mwa wazazi makini, waaminifu! Walakini hata hivyo kazi ya wazazi haifai kukomeshwa. Watoto hawapaswi kuachwa wachukue kusudi lao wenyewe na kila wakati wachague wenyewe mambo. Wameanza tu kwa bidii vita dhidi ya dhambi, kiburi, shauku, wivu, chuki, na maovu yote ya moyo wa asili. Na wazazi wanahitaji kuwaangalia na kuwashauri watoto wao, na kufanya maamuzi kwa ajili yao, na kuwaonesha kwamba ikiwa hawatatoa utii wa furaha, na wa kujitolea kwa wazazi wao,

hawawezi kutoa utii wa hiari kwa moyo mkunjufu kwa MUNGU, na haiwezekani kwao kuwa Wakristo. {1T 391.1}

Wazazi wanapaswa kuwahimiza watoto wao kuwaambia siri, na kuwafungulia huzuni za mioyo yao, kero na majaribu yao ya kila siku. Kwa hivyo wazazi wanaweza kujifunza kuwahurumia watoto wao, na wanaweza kuomba nao na kwa ajili yao kwamba MUNGU ili awalinde na kuwaongoza. Wanapaswa kuwaelekeza kwa Rafiki na Mshauri wao ambaye hajashindwa, ambaye ataguswa na hisia za udhaifu wao, Yeye ambaye alijaribiwa katika kila hali kama sisi, lakini bila kutenda dhambi. {1T 391.2}

Shetani huwajaribu watoto kutokuwa na moyo wenye jotojoto kwa wazazi na kujitenga na wazazi wao na kuchagua watoto wenzao wadogo na wasio na uzoefu kuwa wasiri wao, jambo hili haliwezi kuwasaidia, bali watawapa ushauri mbaya. Wasichana na wavulana hukusanyika pamoja na kupiga soga, na kucheka, na utani, na kumfukuza Kristo kutoka mioyoni mwao, na malaika kutoka mbele yao, kwa upuuzi wao na ujinga. Mazungumzo yasiyokuwa na faida juu ya matendo ya wengine, mazungumzo yasiyo na maana juu ya kijana huyu au msichana yule, hunyausha mawazo mazuri, hisia na fikira za ibada, na kuisukuma shauku nzuri na takatifu kutoka moyoni, ikiiacha ikiwa baridi na kukosa upendo wa kweli kwa MUNGU na Ukweli Wake. {1T 391.3}

Watoto wangeokolewa kutoka katika maovu mengi kama wangefahamiana zaidi na wazazi wao. Wazazi wanapaswa kuhimiza kwa watoto wao tabia ya kuwa wazi na kusema ukweli kwao, kuja kwao na shida zao, na wakati wanapotatanishwa juu ya njia sahihi, kuweka jambo kwa namna wanavyoliangalia wakiwa mbele ya wazazi na kuuliza ushauri wao. Ni nani ambao walio na uwezo wa kuona, kuchambua, kutafuta na kucheua vizuri katika kuona na kuonesha hatari zao kama wazazi wacha MUNGU na kuwasonda kidole kuwaashiria? Ni nani anayeweza kuelewa hulka za kipekee za watoto wao kama wao? Mama ambaye ameangalia kila kona ya akili tangu utoto, na kwa hivyo anafahamiana na tabia ya asili, ndiye amejiandaa vyema kuwashauri watoto wake. Nani anayeweza kujua vile vile tabia za kuangalia na kuzuia, kama mama, akisaidiwa na baba? {1T 392.1}

Watoto ambao ni Wakristo watapendelea ukubali, upendo na uthibitisho wa wazazi wao wanaomcha MUNGU kuliko baraka zote za kidunia. Watawapenda na kuwaheshimu wazazi wao. Inapaswa kuwa moja ya masomo makuu na kanuni ya maisha yao, jinsi ya kuwafanya wazazi wao wawe na furaha. Katika zama hizi za uasi, watoto ambao hawajapata maelekezo na nidhamu sahihi wana hisia kidogo tu za uwajibikaji wao kwa wazazi wao. Mara nyingi suala huwa kwamba kadiri wazazi wao wanavyowatendea mengi, ndivyo wanavyokuwa wasio na shukrani zaidi, na wasioheshimu sana. Watoto ambao wamedekezwa na kusubiriwa kwa kutumikiwa, siku zote watarajia haya; na ikiwa matarajio

yao hayatatimizwa, wanakasirishwa, wanahuzunishwa na kuvunjika moyo. Tabia hiyo hiyo itaonekana kupitia maisha yao yote; watakuwa wanyonge, wasioweza kujisaidia wenyewe, wakitegemea wengine kwa msaada, na kutarajia wengine kuwapendelea (kuwapa favor), kuwatii na kujitoa kwa ajili yao. Na ikiwa watapingwa, hata baada ya kuwa watu wazima wanaume na wanawake, watajiona wananyanyaswa; na hivyo watakuwa na wasi wasi katika safari yao ya kupita ulimwenguni, hawawezi kubeba uzito wao wenyewe, mara nyingi wakinung'unika, wakiudhika na kuhangaika kwa sababu kila kitu hakiwafai. {1T 392.2}

Wazazi wenye makosa wanawafundisha watoto wao masomo ambayo yatathibitisha uharibifu wao, na pia wanapanda miiba kwenye miguu yao wenyewe. Wanafikiri kwamba kwa kuridhisha matakwa ya watoto wao, na kuwaacha wafuate mwelekeo wao, wanaweza kupata upendo wao. Kosa kubwa kiasi gani! Watoto wanaoedekezwa hivyo hukua bila kuzuiliwa katika matakwa yao, wasiosalimisha tabia zao, wenye kutawala wengine (madikteta), wabinafsi, wachoyo, wasiopendeza. wakali, na wenye kujivuna, laana kwao wenyewe na kwa wale wote wanaowazunguka. Kwa kiwango kikubwa, wazazi wanashikilia mikononi mwao furaha ya baadaye ya watoto wao. Juu yao kuna kazi muhimu ya kuunda tabia ya watoto hawa. Maagizo yaliyotolewa katika utoto atika maisha yote. Wazazi hupanda mbegu ambayo itakua na kuzaa matunda kwa uzuri au ubaya. Wanaweza kuwapa stahiki wana wao na binti zao kwa furaha au kwa huzuni. {1T 393.1}

Watoto wanapaswa kufundishwa wakiwa wadogo sana kuwa wanaonufaisha watu/Mungu, wenye kuwajibika, wenye kujisaidia, kuleta faida na wenye kusaidia wengine. Mabinti wengi wa wakati huu wanaweza, bila majuto ya dhamiri, kuwaona mama zao wakifanya kazi kwa bidii, wakipika, wakiosha, au wakipiga pasi, hali wao wameketi sebuleni huku wakisoma hadithi, wakitarizi, au wakifuma (kwa leo wakiwa katika mtandao). Mioyo yao haiguswi, haina hisia kama jiwe tu. Lakini kosa hili linatoka wapi? Je! Ni nani ambao kwa kawaida wangepaswa kulaumiwa katika suala hili? Wazazi masikini, waliodanganywa. Wanapuuza kuyatazama mema ya baadaye ya watoto wao, na kwa kupenda kwao vibaya, wanawaacha wakae kivivu, au wafanye yale ambayo ni ya maana kidogo, ambayo hayahitaji zoezi la akili au misuli, na kisha wawatolea udhuru na wanawadekeza mabinti zao goigoi kwa sababu wao ni dhaifu. Ni nini kimewafanya wanyonge? Mara nyingi hali hii imetokana na hatua mbaya za wazazi. Kiwango sahihi cha mazoezi juu ya nyumba hiyo kitaboresha akili na mwili. Lakini watoto wanapokonywa hali hii kupitia mtazamo potofu, hadi wanachukia kufanya kazi. Haikubaliki na inachukiza maoni yao ya uungwana na ukuu, hadhi, na utanashati, katika jamii. Inadhaniwa kuwa haipelekani na binti mtanashati, maridadi, mrembo na mwuungwana na hata ni jambo la kujidhalilisha kwa binti kuosha vyombo, kulima, kunyosha nguo, au kusimama

juu ya beseni la kuoshea vyombo au kufulia nguo (au kazi zozote zile za kila siku ili kuyafanya maisha yaende). Haya ndiyo maelekezo ya wana mitindo wa leo, ambayo watoto hupewa na kupokea katika umri huu mbaya. {1T 393.2}

Watu wa MUNGU wanapaswa kutawaliwa na kanuni za juu kuliko mambo ya ulimwengu, ambao wanatafuta kupima mwenendo wao wote kulingana na mitindo/fasheni. Wazazi wanaomcha MUNGU wanapaswa kufundisha watoto wao maisha yenye kunufaisha. Hawapaswi kuruhusu kanuni zao za kuwaongoza na kuwasimamia kuchafuliwa na dhana za ufujaji zilizopo katika wakati huu, kwamba lazima wakubaliane na mitindo na watawaliwe na mitazamo ya kiulimwengu. Hawapaswi kuwaruhusu watoto wao kujichagulia marafiki. Wafundishe kuwa ni wajibu wako kuwachagulia. Waandae kubeba mizigo wakiwa wadogo. Ikiwa watoto wako hawajazoeshwa kufanya kazi, hivi karibuni watachoka. Watalalamika kwa maumivu ya pembeni, maumivu mabegani, na miguu iliyochoka; na utakuwa kwenye hatarini, ya kuwahurumia, na kuzifanya kazi zao wewe mwenyewe, badala ya wao kuteseka kidogo. Hebu mzigo juu ya watoto uwe mwepesi sana mwanzoni, na kisha uuongeze kidogo-kidogo kila siku, mpaka waweze kufanya kazi za kutosha bila uchovu. Kutokuwa na shughuli ni sababu kubwa zaidi ya maumivu ya upande wa mwili na maumivu ya mabega kwa watoto. {1T 394.1}

Kuna tabaka la mabinti wadogo katika kizazi hiki ambao ni viumbe visivyo na faida tu, ambao ni wazuri tu katika kupumua, kula, kuvaa, kuzungumza, na kuongea upuuzi na 'kuchat', wakati wanashikilia vidoleni mwao aina fulani ya vitu vya kufumwa kama masweta, na kutarizi. Lakini ni vijana wachache tu huonesha uamuzi mzuri wenye busairi na wenye tafakari. Wanaishi maisha ya kipepeo bila lengo maalum lililo mbele ya nyuso zao. Wakati tabaka hili la marafiki wa kilimwengu wanapojumuika pamoja, karibu yote unayoweza kusikia ni mapendekezo ya kijinga machache juu ya mavazi, au jambo lisilo na maana, halafu wanayachekea-chekea maoni yao wanayoyachukulia kuwa yenye kufaa na ya akili mahiri sana. Hii hufanywa mara kwa mara hata mbele ya watu watu wazima, ambao anaweza kuhisi kusikitishwa na ukosefu wa adabu na kicho kwa rika hili. Vijana hawa wanaonekana kupoteza hisia zote za kujistahi, upole, uungwa, adabu, mazoea mema na tabia nzuri. Walakini njia ambayo wameelekezwa inawaongoza kufikiria kuwa sasa wao wamefikia kimo cha juu cha utanashati, umaridadi, kukubalika, akili mahiri, unyeti feki, kujionyesha, maringo na ukuu katika jamii(gentility). {1T 394.2}

Roho hii ni kama ugonjwa wa kuambukiza. Watu wa MUNGU wanapaswa kuchagua jamii kwa ajili ya watoto wao na kuwafundisha kuepukana na ushirika wa walimwengu hawa batili, wasio na tija. Wakina mama wanapaswa kuwachukua mabinti zao kwenda nao jikoni na kuwafundisha kwa subira. Miili yao yatakuwa bora kwa kazi kama hiyo, misuli yao itapata toni na nguvu, na

tafakari zao zitakuwa na afya njema na kuinuliwa mwisho wa siku. Wanaweza kuwa wamechoka, lakini mapumziko ni matamu kiasi gani baada ya kazi yenye uzito sahihi. Usingizi, mrejeshaji mzuri wa asili wa mwili, huimarisha mwili uliochoka, na kuuandaa kwa majukumu ya siku inayofuata. Usiwazoeshe watoto wako kuwa haijalishi wanafanya kazi au la. Wafundishe kuwa msaada wao unahitajika, na wakati wao ni wa thamani, na kwamba wewe unategemea kazi yao. {1T 395.1}

Nimeoneshwa kuwa dhambi nyingi zimetokana kutokuwa na la kufanya au uvivu. Mikono na akili zinazofanya kazi hazipati wakati wa kuzingatia kila jaribu ambalo adui anapendekeza, lakini mikono na akili zisizo na kazi zote ziko tayari kutawaliwa na Shetani. Akili, isiyotumika sawasawa, hushugulika na mambo yasiyofaa. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao kukaa bila kazi ni dhambi. Nilirejeshwa kwa ***Ezekieli 16:49***: "Tazama, huu ndio uovu wa dada yako Sodoma, kiburi, shibe ya chakula, na wingi wa uvivu ulikuwa ndani yake na katika binti zake, wala hakuwatia nguvu mikono ya maskini na wahitaji.. " {1T 395.2}

Watoto wanapaswa kuhisi kwamba wana deni kwa wazazi wao, ambao wamewaangalia katika utoto na kuwauguza walipokuwa magonjwa. Wanapaswa kutambua kwamba wazazi wao wamepata wasiwasi mwingi kwa sababu yao. Hususani wazazi waangalifu na wacha Mungu, wamekuwa na matamanio kuliko kawaida kwa watoto wao kuchukua mwenendo unaofaa. Walipoona makosa kwa watoto wao, jinsi mioyo yao ilivyokuwa mizito. Ikiwa watoto ambao walisababisha mioyo hiyo kuuma wangeweza kuona athari ya mwenendo wao, bila shaka wangetubu. Kama wangeweza kuona machozi ya mama yao na kusikia maombi yake kwa MUNGU kwa niaba yao, kama wangeweza kumsikiliza akiugua na kusononeka, mioyo yao ingehisi, na wangekiri haraka makosa yao na kuomba wasamehewe. Kuna kazi ya kutimizwa kwa watu wazima na vijana. Wazazi wanapaswa kuhitimu vizuri kutekeleza jukumu lao kwa watoto wao. Wazazi wengine hawaelewi watoto wao na hawafahamiani nao. Mara nyingi kuna umbali mkubwa kati ya wazazi na watoto. Kama wazazi wangeingia kikamilifu katika hisia za watoto wao na kuchota yaliyo ndani ya mioyo yao, ingekuwa na ushawishi mzuri kwao. {1T 395.3}

Wazazi wanapaswa kushughulika kwa uaminifu na roho zilizowekwa chini ya ungalizi/amana yao. Hawapaswi kuwahamasisha kiburi, ubadhirifu, au kupenda maonesho na kujigamba. Hawapaswi kuwafundisha, au kuwaacha wajifunze, ujanja mdogo (kama ule wa vichekesho, comedy au pranks) ambao unaonekana una hila fulani kwa watoto wadogo, lakini ambao watalazimika kuutoa vichwani mwao mwishowe, na ambao wanapaswa kusahihishwa na kuacha, wakiwa watu wazima. Tabia zilizoundwa kwanza hazisahauliki kwa urahisi. Wazazi, mnapaswa kuanza kuzitia nidhamu akili za watoto wenu wakiwa wadogo sana,

ili waweze kuwa Wakristo. Jitihada zako zote ziwe kwa wokovu wao. Tenda kana kwamba wamewekwa chini ya uangalizi wako ili watengenezwe kuwa vito vya thamani vitakavyoangaza katika ufalme wa MUNGU. Jihadharini na jinsi unavyowalaza juu ya shimo la uharibifu na mawazo potofu kwamba hawana umri wa kutosha kuwajibika, sio wakubwa kiasi cha kutosha kuwajibika au kutubu dhambi zao na kumkiri Kristo (Tabia nyingi watoto huachiwa kuwa nazo, bila kusahihishwa na kuonekana kama ni kichekesho tu, kama *kupiga watu, kuvaa nguo zisizo na heshima mfano kutembea na chupi tu kwa watoto wadogo, kuigiza mambo kama katuni ambayo ni kukosa adabu nk*). {1T 396.1}

Nilielekezwa kwa ahadi nyingi za thamani zilizonakiliwa kwa wale wanaomtafuta Mwokozi wao mapema. Mhubiri 12: 1: "Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako, wakati siku mbaya hazijaja, wala miaka kukaribia, hapo utakaposema, Sina furaha katika hayo. "Mithali 8:17:" Nawapenda wale wanipendao; na wale wanaonitafuta mapema watanipata. "Mchungaji Mkuu wa Israeli bado anasema:" Acha watoto wadogo waje Kwangu, wala usiwazuie: kwa maana Ufalme wa MUNGU ni wa wao. "Wafundishe watoto wako kuwa ujana ni wakati mzuri wa kumtafuta Bwana. Kisha mizigo ya maisha sio mizito kwao, na akili zao changa hazikerwi kwa masumbufu ya maisha haya, na wakati wako huru wanapaswa kutumia nguvu zao zote kwa MUNGU. {1T 396.2}

Tunaishi katika kizazi wakati mgumu kwa watoto, chenye changamoto, wimbi zito lililotegeshwa linashuka chini katika uharibifu na ni zaidi ya uzoefu na uimara wa kitoto unahitajika ili kuzuia dhidi ya wimbi hili bila kubebwa nalo. Vijana kwa ujumla wanaonekana kuwa mateka wa Shetani pamoja na malaika zake wanaonekana kuwapeleka katika uangamivu. Shetani na jeshi lake wanafanya vita dhidi ya serikali ya MUNGU kwa kuwafadhaisha, na wote ambao wanashauku ya kutoa mioyo yao kwake na kutii matakwa yake, Shetani atajaribu kuwakanganya na kuwashinda kwa majaribu kwamba wavunjike moyo na kukata tamaa kupigana katika vita. {1T 397.1}

Wazazi, wasaidieni watoto wenu. Amkeni kutoka katika uchovu ambao umekuwa juu yenu. Kuweni waangalifu kila wakati kukata sasa wimbi, na kurudisha nyuma uzito wa uovu ambao Shetani anawasukumia watoto wenu. Watoto hawawezi kufanya haya wenyewe, lakini wazazi wanaweza kufanya mengi. Kwa maombi ya dhati na imani hai ushindi mkubwa utapatikana. Wazazi wengine hawajatambua majukumu waliyo nayo na wamepuuza elimu ya dini ya watoto wao. Asubuhi mawazo ya kwanza ya Mkristo yanapaswa kuwa juu ya MUNGU. Kazi ya kidunia na masilahi binafsi yanapaswa kuwa ya pili. Watoto wanapaswa kufundishwa kuheshimu na kujali saa ya maombi. Kabla ya kuondoka nyumbani kwa kazi, familia yote inapaswa kuitwa pamoja, na baba, au mama kama baba hayupo, anapaswa kumsihi MUNGU kwa bidii awatunze siku nzima. Njoo kwa unyenyekevu na moyo uliojaa huruma na hisia za

majaribu na hatari mbele yenu na watoto wenu; kwa imani uwafunge juu ya madhabahu, na kusihi kwa ajili ya uangalizi wa Bwana. Malaika wanaohudumu watawalinda watoto ambao wamejitolea kwa MUNGU. Ni jukumu la wazazi wa Kikristo, asubuhi na jioni, kwa maombi ya dhati na imani ya kudumu, kutengeneza ngome/uzio juu ya watoto wao. Wanapaswa kuwafundisha kwa uvumilivu, kwa fadhili na bila kuchoka, kuwafundisha jinsi ya kuishi ili kumpendeza MUNGU. {1T 397.2}

Kukosa  subira kwa wazazi kunasisimua kutokuwa na subira kwa watoto. Mazoea ya wazazi ya kutozuia mihemko yao mibaya huunda shauku au tamaa hizo mbaya kwa watoto na huchochea maovu ya asili yao (hasira, kufurahi kupita kiasi, kiheherekuudhika kupita kiasi nk). Wazazi wengine husahihisha watoto wao kwa ukali kwa roho ya kukosa subira, na mara nyingi kwa mazoea yenye jazba moyoni. Marekebisho kama haya hayaleti matokeo mazuri. Katika kutafuta kurekebisha uovu mmoja, wanatengeza wa pili. Kuendelea kugombeza na kuchapa viboko huwafanya watoto kuwa wagumu na kuondoa mioyo yao kutoka kwa wazazi wao. Wazazi kwanza wanapaswa kujifunza kujitawala nafsi zao, kisha wanaweza kufanikiwa kudhibiti watoto wao. Kila wakati wanaposhindwa kujizuia nafsi, na kusema na kutenda bila subira, wanamtenda MUNGU dhambi. Kwanza wanapaswa kusemezana na watoto wao, wakiwaonesha wazi makosa yao, kuwaonyesha dhambi zao, na kuwasisitiza kwamba hawajatenda tu dhambi dhidi ya wazazi wao, bali pia dhidi ya MUNGU. Kwa moyo wako mwenyewe ukiwa umetiishwa na ukiwa umejaa huruma nyororo na huzuni kwa watoto wako wanaokosea, omba nao kabla ya kuwasahihisha. Ndipo matengenezo na marekebisho yako hayatawafanya watoto wako wakuchukie. Watakupenda. Wataona kuwa hauwaadhibu kwa sababu wamekuwekea usumbufu na kuondoa faraja yao, au kwa sababu unataka kumalizia hasira yako juu yao; lakini kutoka katika hali ya wajibu, kwa faida yao, ili wasiachwe kukua katika dhambi. {1T 398.1}

Wazazi wengine wameshindwa kuwapa watoto wao elimu ya dini na pia wamepuuza masomo yao ya shule. Kati ya hivyo hakuna kinachopasa kupuuzwa. Akili za watoto zitakuwa hai, na ikiwa hazitajishughulisha na kazi ya kimwili, au kujazwa na masomo, zitawekwa wazi kwa ushawishi wa uovu. Ni dhambi kwa wazazi kuwaruhusu watoto wao wakue katika ujinga. Wanapaswa kuwapatia vitabu muhimu na vya kufurahisha, na wanapaswa kuwafundisha kufanya kazi, kuwa na masaa ya kazi ya mwili, na masaa ya kujitolea kujifunza na kusoma. Wazazi wanapaswa kutafuta kuinua akili za watoto wao na kuboresha vitivo vyao vya akili. Akili iliyoachwa yenyewe, isiyopaliliwa, isiyotunza, kwa ujumla ni dunia, ya kidunia, na yenye ufisadi. Shetani anaboresha nafasi yake na anaelimisha akili zisizo na kazi. {1T 398.2}

Wazazi, malaika wa kunakili anaandika kila neno lisilo na subira na ghadhabu unalowatolea watoto wako. Kila kushindwa kwako kuwapatia mwongozo na maelekezo sahihi, na kuwaonesha dhambi kubwa ya dhambi, na matokeo ya mwisho ya mwenendo wa dhambi, yamewekwa alama dhidi ya jina lako. Kila neno lisilolindwa lililotamkwa mbele yao, bila kujali au kwa kejeli, kila neno ambalo sio safi na lililoinuliwa, malaika analinakili kuashiria doa dhidi ya tabia yako ya Kikristo. Matendo yako yote yamenakiliwa, ikiwa ni mema au mabaya. {1T 399.1}

Wazazi hawawezi kufanikiwa vizuri katika kuwasimamia/kuwaongoza watoto wao hadi kwanza wawe na udhibiti kamili wa wao wenyewe. Lazima kwanza wajifunze kujitiisha, kudhibiti maneno yao, na muonekano wa uso. Hawapaswi kuacha toni ya sauti zao kubugudhiwawa au kufadhaishwa na msisimko na anasa. hatimae wanaweza kuwa na ushawishi ulioamuliwa juu ya watoto wao. Watoto wanaweza kupenda kutenda haki, wanaweza kukusudia mioyoni mwao kuwa watiifu na wema kwa wazazi au walezi wao; lakini wanahitaji msaada na kutiwa moyo kutoka kwao. Wanaweza kufanya maazimio mazuri; lakini isipokuwa tu kanuni zao zimeimarishwa na dini na maisha yao kuathiriwa na neema mpya ya MUNGU, watashindwa kufikia alama. {1T 399.2}

Wazazi wanapaswa kuongeza juhudi zao maradufu kwa ajili ya wokovu wa watoto wao. Wanapaswa kuwafundisha kwa uaminifu, bila kuwaacha wakusanye elimu yao kadiri wawezavyo tu popote kule. Vijana hawapaswi kuachwa wajifunza mema na mabaya bila kubagua, na kukiwa na wazo kwamba wakati ujao, basi wema utatawala na uovu utapoteza ushawishi wake. Uovu utaongezeka haraka kuliko wema. Inawezekana kwamba uovu ambao wamejifunza unaweza kutokomezwa baada ya miaka mingi; lakini ni nani yuko tayari kujitosa kwenye hili? Muda wetu hapa duniani ni mfupi. Ni rahisi na salama zaidi kupanda mbegu safi na nzuri mioyoni mwa watoto wako kuliko kung'oa magugu baadaye. Ni jukumu la wazazi kuangalia mivuto ya ushawishi inayowazunguka isije ikawa na athari mbaya kwa watoto wao. Ni jukumu lao kuchagua jamii kwa ajili yao na sio kuwaacha wachague wao wenyewe. Hivi ni nani atatenda kazi hii ikiwa wazazi hawafanyi? Je! Wengine wanaweza kuwa na shauku hiyo kwa watoto wako ambayo unapaswa kuwa nayo? Je! Wanaweza kuwa na uangalizi wa kila wakati na upendo wa kina ambao wazazi wanao? {1T 399.3}

Watoto wa Watunza Sbato wanaweza kukosa subira kwa vizuizi, na wanafikiria wazazi wao ni wakali sana, au wana akili finyu sana kuhusu wao (strict); hisia ngumu zinaweza kutokea hata ndani ya mioyo yao, na mawazo ya kutoridhika, yasiyo na furaha yanaweza kuendekezwa nao dhidi ya wale ambao wanafanya kazi kwa ajili ya ya wakati wao wa sasa na maisha yao ya baadaye, mema ya milele. Lakini ikiwa maisha yatahifadhiwa miaka michache, watawabariki

wazazi wao kwa uangalizi makini na uaminifu juu yao katika miaka yao ya kukosa uzoefu. Wazazi wanapaswa kuelezea na kurahisisha mpango wa wokovu kwa watoto wao ili akili zao changa ziuelewe. Watoto wa miaka nane, kumi, au kumi na mbili wana umri wa kutosha kutambulishwa juu ya mada ya dini ya mtu binafsi. Usifundishe watoto wako kwa kurejelea kipindi fulani cha wakati ujao watakapokuwa na umri wa kutosha kutubu na kuamini Ukweli. Ikiwa wamefundishwa vizuri, watoto wadogo sana wanaweza kuwa na maoni sahihi juu ya hali yao kama wenye dhambi na njia ya wokovu kupitia Kristo. Wachungaji kwa ujumla hawajali sana kuhusu wokovu wa watoto, na hawana tabia ya kuhusiana binafsi na watoto kama inavyopaswa kuwa. Fursa za dhahabu za kupendekeza akili za watoto mara nyingi hupita bila kuboreshwa. {1T 400.1}

Ushawishi wa uovu unaowazunguka watoto wetu karibu unawalemea; unaharibu akili zao na unawaongoza katika uangamaivu. Kwa asili akili za vijana hutolewa katika upumbavu; na katika umri mdogo (Mithali 22:15), kabla tabia zao hazijaundwa, na uwezo wao wa kufikiri haujakomaa mara nyingi wanadhihirisha kupenda makundi rika ambayo yatakuwa na mivuto ya kujeruhi juu yao. Wengine huunda mshikamano na watu wenye jinsia tofauti kinyume na matakwa na idhini ya wazazi wao, na wanavunja amri ya tano ya kuwaheshimu. Ni wajibu wa wazazi kuchunguza kutoka na kuingia kwa watoto wao. Wanapaswa kuwatia moyo na kuwasilisha vitu mbele yao vitakavyowavuta kuwa nyumbani, na waona kuwa wazazi wanawajali. Lazima waifanye nyumba kuwa ya kuchangamsha, kupendeza na furaha. {1T 400.2}

Akina baba na akina mama, zungumzeni kwa upole na watoto wenu; kumbukeni ni kwa namna gani mlikuwa katika hali nyeti, ni kwa nadra kiasi gani mnavumilia kulaumiwa; tafakarini, na mjue kuwa watoto wenu ni kama ninyi. Kile ambacho hamwezi kukivumilia, msikiweke juu yao. Ikiwa hamwezi kuvumilia lawama na karipio, hata watoto wenu hawawezi, ambao ni dhaifu kuliko ninyi na hawawezi kuvumilia sana. Hebu maneno yenu ya kupendeza na ya kufurahisha yawe kama miali ya jua katika familia yenu. Matunda ya kujitawala nafsi, kujinyima, umakini, uangalifu, unadhifu, kutafakari, na kuchukua hatua kwa sehemu yenu yatakuwa mara mia. Wazazi hawana haki ya kuleta wingu lenye huzuni juu ya furaha ya watoto wao kwa kutafuta makosa, kufoka, kukosoa au lawama kali kwa makosa madogo-madogo tu. Makosa halisi na dhambi inapaswa kufanywa ionekane kama ni dhambi kama ilivyo, na njia thabiti, iliyoamuliwa inapaswa kufuatwa ili kuzuia kutokea tena. Watoto wanapaswa washitushwe kidogo kwa kupewa mguso wa hisia za makosa yao, lakini hawapaswi kuachwa katika hali ya kutokuwa na tumaini la akili, lakini kwa kiwango cha ujasiri kwamba wanaweza kuboresha na kupata ujasiri na ukubali wako. {1T 401.1}

Wazazi wengine hukosea kuwapa watoto wao uhuru mwingi. Wakati mwingine wana imani kubwa kwao hata hawaoni makosa yao. Ni makosa kuwaruhusu

watoto, kwa gharama fulani, kutembea mbali, bila kuandamana na wazazi au walezi wao. Hii ina ushawishi mbaya juu watoto. Wanahisi kuwa maisha yao yana matokeo makubwa na kwamba upendeleo fulani ni wao, na ikiwa hawatapewa haya, wanajiona wananyanyaswa. Wanarejelea kwa watoto ambao hutoka na kuingia ndani ya nyumba zao, kwamba wana fursa nyingi, wakati wao wanao machache sana (slumber party nk). {1T 401.2}

Na mama, hali akiogopa kwamba watoto wake watamfikiria kuwa hawatendei haki, anaridhisha matakwa yao, ambayo mwishowe yanathibitisha kuwa jeraha kubwa kwao. Wageni vijana, ambao hawana macho ya mzazi juu yao, kuona na kurekebisha makosa yao, mara nyingi hupokea mivuto ambayo itachukua miezi kuondoa. Nilirejeshwa katika kisa cha wazazi ambao walikuwa na watoto wazuri, watiifu, na ambao, kwa kuwa na imani kubwa kwa washiriki wa familia yao, waliwamini watoto wao kutoka kwao kwenda mbali kuwatembelea marafiki hawa. Kuanzia wakati huo kulikuwa na mabadiliko makubwa katika msimamo na tabia ya watoto wao. Hapo awali walikuwa wakiridhika na wenye furaha nyumbani, na hawakuwa na hamu kubwa ya kuwa pamoja na vijana wengine. Waliporudi kwa wazazi wao, zuio linaonekana kuwa lisilo la haki, na nyumbani kwao ni kama gereza. Harakati kama hizo zisizo za busara za wazazi huamua tabia za watoto wao. {1T 402.1}

Kwa kutembelea watu hivi, watoto wengine huunda muungano/mapenzi ambavyo vinathibitisha uharibifu wao mwishowe. Wazazi, watunzeni watoto wenu kwa karibu nanyi ikiwezekana, na waangalie watoto kwa umakini mwingi. Unapowaruhusu watembee mbali kutoka kwako, wanahisi kuwa wana umri wa kutosha kujiangalia na kuchagua wenyewe. Wakati vijana wameachwa peke yao, mazungumzo yao mara nyingi huwa juu ya masomo ambayo hayatawasafisha au kuwainua, au kuongeza mapenzi yao kwa mambo ya kiroho. Kadiri wanavyoruhusiwa kutembelea watu wengine au kwenda mbali, shauku yao ya kwenda itakuwa kubwa kwenda tena, na nyumbani kwao hapataonekana pa kuvutia. {1T 402.2}

Watoto, MUNGU ameona inafaa kuwaweka chini ya uangalizi wa wazazi wenu ili wawafundishe na kuwanidhamisha, na hivyo kufanya sehemu yao katika kuunda tabia yenu kwa ajili ya mbingu. Na hata hivyo inabaki ndani yenu kusema ikiwa mtaendeleza tabia nzuri ya Kikristo kwa kutumia faida mliyokuwa nayo kutoka kwa wazazi wacha MUNGU, waaminifu, na wanamaombi. Pamoja na wasiwasi wote na uaminifu wa wazazi kwa niaba ya watoto wao, wao peke yao hawawezi kuwaokoa. Kuna kazi inayopaswa kufanywa na watoto. Kila mtoto ana jambo la kibinafsi la kuangalia. Wazazi mnaoamini, ninyi mna wajibu mbele yenu kuongoza nyayo za watoto wenu, hata katika uzoefu wao wa kidini/kiroho. Wakati watakapompenda MUNGU kweli, watakubariki na kukuheshimu kwa utunzaji ambao umedhihirisha kwao, na kwa uaminifu wako katika kuzuia matamanio yao na kutiisha nia zao. {1T 402.3}

Ushawishi uliopo ulimwenguni ni wa kuwaacha vijana kufuata mwelekeo wa asili wa akili zao. Na ikiwa ni wakorofi na wajeuri sana katika uchanga wao, wazazi wanasema watatoka hapo mara tu baada ya muda na kurudi, na wakifikia wakati wa miaka kumi na sita au kumi na nane, watatafakari wao wenyewe na kuacha tabia zao mbaya, na mwishowe watakuwa wanaume na wanawake muhimu. Kosa kubwa jinsi gani! Kwa miaka wamemruhusu adui kupanda bustani ya moyo; wanaacha kanuni mbaya zikue, na katika visa vingi kazi yote ya baadaye kwenye ardhi hiyo haitafaulu chochote. Shetani ni fundi stadi, mwenye bidii, adui mbaya. Wakati wowote neno lisilofaa linaposemwa kujeruhi vijana, iwe kwa kubembeleza, kutia chumvi maneno au kuwafanya waangalie dhambi fulani bila kuchukia sana, Shetani huitumia na kuipalilia mbegu ya uovu ambayo inaweza kumea mizizi na kutoa mavuno mengi. Wazazi wengine wamewaacha watoto wao kuunda tabia mbaya, alama ambazo zinaweza kuonekana katika maisha yote. Juu ya wazazi, imelala dhambi hii. Watoto hawa wanaweza kujidai kuwa Wakristo, lakini bila kazi maalum ya neema juu ya moyo na mabadiliko/matengenezo kamili maishani tabia zao za zamani zitaonekana katika uzoefu wao wote, na wataonesha tabia tu ambayo wazazi wao waliwaruhusu iundwe. {1T 403.1}

Kiwango cha uchaji MUNGU ni cha chini sana kati ya wale wanaodai kuwa Wakristo kwa ujumla kiasi kwamba wale wanaotaka kumfuata Kristo kwa dhati wanaiona kazi hiyo kuwa ngumu na yenye majaribu kuliko vile ambavyo wangefanya. Ushawishi wa watu wanaojifanya kuwa Wakristo kwa ulimwengu ni wa kuwadhuru vijana. Umati wa wale wanaojiita Wakristo wameondoa mstari wa tofauti kati ya Wakristo na ulimwengu, na wakati wanadai kuwa wanaishi kwa ajili ya Kristo, wanaishi tu kwa ajili ya ulimwengu. Imani yao ina udhibiti kidogo tu juu ya starehe zao; wakati wanakiri kuwa watoto wa nuru, wanatembea gizani, nao ni watoto wa usiku na wa giza. Wale wanaotembea gizani hawawezi kumpenda MUNGU na kuwa na shauku ya dhati ya kumtukuza Yeye. Hawajaangaziwa kutambua uzuri wa vitu vya mbinguni, na kwa hivyo hawawezi kuzipenda Kweli. Wanadai kuwa Wakristo kwa sababu inachukuliwa kuwa ni heshima/uungwana, na hakuna msalaba wa kubeba. Nia zao mara nyingi ni za ubinafsi. Baadhi ya watu wanaokiri kwa mdomo imani kama hao wanaweza kuingia kwenye chumba cha kuchezea dansi (ballroom) na kuungana katika burudani zote ambazo hupatikana humo. Wengine hawawezi kwenda mbali kiasi hicho, lakini wanaweza kuhudhuria karamu za starehe (party), pikniki, vyama vya michango, na maonesho. Na jicho lenye busara zaidi lingeshindwa kuona katika wale wanaojiita Wakristo hata alama moja tu ya Ukristo. Mtu anashindwa kuona katika muonekano wao tofauti yoyote kati yao na kafiri mkuu. Mfuasi wa Kristo wa mdomo tu (feki au bandia), ambaye ni mbaradhifu na mwenye maadili ya uovu, na anaedhihaki wazi dini, na mtoa matusi machafu waziwazi wote wanachanganyika kama kitu kimoja. Na MUNGU huwaona hawa kama kitu kimoja katika roho na kwa vitendo. {1T 403.2}

Ufuasi wa Ukristo bila imani inayolingana na matendo hautafaulu chochote, ni kazi bure tu. Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili. Watoto wa mwovu ni watumishi wa bwana wao; hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, basi mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki (Warumi 6:16). Haiwezi kutokuwa na madhara kwa watumishi wa Mfalme wa mbinguni kushiriki katika raha na maburudisho ambayo watumishi wa Shetani hujihusisha nazo, ingawa mara nyingi hurudia kwamba starehe kama hizo hazina madhara. MUNGU amefunua Kweli nyeti na takatifu ili kuwatenganisha watu Wake na wasiomcha MUNGU na kuwatakasa kwa ajili Yake mwenyewe. Waadventista wa Sabato wanapaswa kuiishi imani yao. Wale ambao hutii Amri Kumi huona hali ya ulimwengu na mambo ya kidini kwa mtazamo tofauti kabisa na ile ya wafuasi ambao ni wapenda raha, ambao huepuka msalaba, na wanaishi kwa kukiuka amri ya nne. Katika hali ya sasa ya mambo katika jamii, sio kazi rahisi kwa wazazi kuwasimamia watoto wao na kuwafundisha kulingana na kanuni ya haki ya Biblia. Wafuasi wa dini wameacha Neno la MUNGU kiasi kwamba watu wake wanaporudi kwenye Neno Lake takatifu, na kufundisha watoto wao kulingana na maagizo Yake, na kama vile Ibrahimu wa zamani alivyoelekeza watu wa nyumba yake, watoto hao wanyonge na masikini walio katika ushawishi uliowazunguka wanafikiri wazazi wao wanawabana sana na ni wakali kupita kiasi kuhusiana na makundi rika yao. Kwa asili wanatamani kufuata mfano wa wafuasi wenye udunia ndani yao, wapenda starehe wanaomkiri Mwenyezi Mungu kwa Mdomo tu. {1T 404.1}

Katika siku hizi, mateso na aibu kwa ajili ya Kristo ni nadra sana kujulikana. Kujinyima kidogo na kujitolea ni muhimu ili kuvaa namna tu ya utauwa na kuwa na jina kwenye kitabu cha kanisa; lakini kuishi kwa namna ambayo njia zetu zitampendeza MUNGU, na majina yetu kuandikwa katika kitabu cha uzima, itahitaji uangalifu, kukesha na maombi, kujinyima, kujikana nafsi na kujitolea dhabihukwa upande wetu. Wafuasi wanaomkiri Kristo kwa mdomo tu, sio mfano wa kuigwa na vijana, mpaka pale tu wanapoonesha ni umbali kiasi gani wanamfuata Kristo. Matendo sahihi ni matunda yasiyo na shaka ya utauwa wa Kweli. Hakimu wa dunia yote atampa kila mtu kulingana na matendo yake. Watoto wanaomfuata Kristo wana vita mbele yao; Kila siku wana msalaba wa kubeba, kutoka duniani na kujitenga, na kuiga maisha ya Kristo. {1T 405.1}

## SURA YA 75

## KUTEMBEA KATIKA NURU

Nilioneshwa kuwa watu wa MUNGU hukaa sana chini ya wingu. Sio mapenzi Yake kwamba waishi kwa kutokuamini. Yesu ni nuru, na ndani Yake hakuna giza hata kidogo. Watoto Wake ni watoto wa nuru. Wanafanywa upya kwa mfano Wake, na wameitwa kutoka gizani kuingia katika nuru Yake ya ajabu. Yeye Ndiye nuru ya ulimwengu, na ndivyo pia wale wanaomfuata. Hawatatembea gizani, bali watakuwa na nuru ya uzima. Kadiri watu wa MUNGU wanavyojitahidi sana kumwiga Kristo kwa ukaribu, ndivyo watakavyofuatwa zaidi na adui kwa ukali; lakini ukaribu wao kwa Kristo unawaimarisha kupinga juhudi za adui yetu mjanja kuwavuta kutoka kwa Kristo. {1T 405.2}

Nilioneshwa kuwa kulikuwa na kujilinganisha sana kati yetu wenyewe, tukichukua wanadamu wenye makosa kuwa mfano, wakati tuna mfano mzuri wenye uhakika na usio na kasoro. Hatupaswi kujipima na ulimwengu, wala kwa maoni ya wanadamu, wala kwa kile tulichokuwa kabla ya kuukubali Ukweli. Lakini imani na msimamo wetu ulimwenguni, kama ilivyo sasa, lazima vilinganishwe na vile ambavyo ingekuwa ikiwa mwendo wetu ungeendelea mbele na zaidi tangu tulipodai kuwa wafuasi wa Kristo. Huku ndiko kujilinganisha salama tu, kujilinganisha kwingine kule kutakuwa ni kujidanganya  nafsi tu! Ikiwa tabia ya maadili na hali ya kiroho ya watu wa MUNGU hailingani na baraka, upendeleo, na nuru ambayo wamepewa, wamepimwa katika mizani, na malaika hufanya taarifa hii, "Umepungua!". {1T 406.1}

Kwa wengine maarifa ya hali yao ya kweli yanaonekana kufichika kutoka kwao. Wanaona Ukweli, lakini hawajui umuhimu wake au madai yake. Wanasikia Ukweli, lakini hawauelewi kabisa, kwa sababu hawafananishi maisha yao na huo, na kwa hivyo hawatakaswi kwa kuutii. Na bado wanapumzika wakiwa hawajali na kuridhika kabisa kana kwamba wingu mchana na nguzo ya moto usiku, kama ishara ya neema ya MUNGU,  vimetangulia mbele yao. Wanakiri kumjua MUNGU, lakini kwa matendo wanamkana. Wanajiona kuwa wateule Wake, watu wa kipekee, lakini uwepo Wake na nguvu ya kuokoa kabisa zinadhihirishwa kea nadra kati yao. Jinsi giza lilivyo kubwa kiasi hicho! Lakini wao wenyewe hawaijui. Nuru inaangaza, lakini hawaielewi. Hakuna udanganyifu wenye nguvu unaoweza kudanganya akili ya mwanadamu kuliko ule inayowafanya waamini kuwa wako sawa, na kwamba MUNGU anakubali matendo yao, wanapokuwa wanamtenda Yeye dhambi. Hawaitambui sura ya utauwa kwa roho na nguvu yake. Wanadhani kuwa ni matajiri, na hawahitaji chochote, wakati ni masikini, vipofu, na uchi, na wanahitaji vitu vyote. {1T 406.2}

Kuna wengine wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo, lakini hawaweki juhudi katika mambo ya kiroho. Katika biashara yoyote ya ulimwengu hawa hujitahidi, na hudhihirisha matamanio ya ukuu katika kutimiza lengo lao, na kuleta mwisho

unaotarajiwa; lakini katika biashara ya uzima wa milele, ambapo kila kitu kiko hatarini, na furaha yao ya milele inategemea mafanikio yao, hufanya kama wasiojali, kana kwamba hawakuwa mawakala wa uadilifu, kana kwamba wengine walikuwa wakiwachezea mchezo wa maisha, na wao hawakuwa na cha kufanya ila kusubiri matokeo. Lo, upumbavu gani! wazimu gani! Ikiwa wote wataonesha tu kiwango hicho cha shauku, kujitoa, na bidii kwa uzima wa milele ambacho wanaonesha katika harakati zao za kidunia, wangekuwa washindi. Kila mtu, niliona, lazima ajipatie uzoefu, kila mmoja anapaswa kutenda vizuri na kwa uaminifu sehemu yake katika mchezo wa maisha. Shetani hutazama fursa yake ya kukamata neema za thamani wakati tunapokosa uangalifu/ulinzi, na tutakuwa na mgogoro mkali na nguvu za giza kuzihifadhi, au kupata neema ya mbinguni ikiwa kwa kukosa kukesha tulizipoteza. {1T 407.1}

Lakini nilioneshwa kuwa ni fursa kwa Wakristo kupata nguvu kutoka kwa MUNGU kushikilia kila zawadi ya thamani. Maombi ya dhati na bidii na yanayofaa yatazingatiwa mbinguni. Wakati watumishi wa Kristo wanapochukua ngao ya imani kama ulinzi wao, na upanga wa Roho kwa vita, kuna hatari katika kambi ya adui, na jambo fulani lazima lifanyike. Mateso na lawama huwangojea tu wale ambao wamepewa nguvu kutoka juu kuwaita kuwa watendaji hai. Wakati Ukweli katika unyenyekevu, usahili na nguvu zake unaenea miongoni mwa waumini, na unaletwa kuwa shahidi dhidi ya roho ya ulimwengu, itakuwa dhahiri kabisa kwamba hakuna maelewano kati ya Kristo na Beliali. Wanafunzi wa Kristo lazima wawe mifano hai ya maisha na Roho ya Bwana wao. {1T 407.2}

Vijana na wazee wana mzozo, vita, mbele yao. Hawapaswi kulala kwa muda. Adui mwenye mjanja yuko macho kila wakati ili kuwapotosha na kuwashinda. Waumini wa Ukweli wa sasa lazima wawe macho kama adui yao na waoneshe hekima katika kumpinga Shetani. Je! Watafanya hivi? Je! Wataendelea kuwa wavumilivu katika vita hivi? Je! Watakuwa waangalifu kuachana na uovu wote? Kristo amekanwa, na kukataliwa kwa njia nyingi. Tunaweza kumkana kwa kusema kinyume na Ukweli, kwa kusema mabaya juu ya wengine, kwa kuzungumza kwa ujinga au mzaha, au kwa maneno ambayo ni ya bure na ya kijinga. Katika mambo haya tunadhihirisha ujanja au kupungukiwa na hekima. Tunajifanya dhaifu wenyewe; juhudi zetu zinakuwa dhaifu kumpinga adui yetu mkubwa, na tunatekwa na kushindwa. "Ndani ya wingi wa moyo kinywa hunena," na kwa kukosa kukesha tunakiri kwamba Kristo hayumo ndani yetu. Wale ambao husita kujitoa kwa MUNGU bila ya kujibakiza, hufanya kazi duni ya kumfuata Kristo. Wanamfuata kwa mbali sana kiasi kwamba nusu ya wakati hawajui kama wanafuata nyayo Zake au nyayo za adui yao mkubwa. Kwa nini tunachelewa na kuzorota kuyaondoa mapenzi na maslahi yetu katika vitu vya ulimwengu huu na kumchukua Kristo kama fungu letu la pekee? Kwa nini tunapaswa kutamani kutunza urafiki wa maadui wa Bwana wetu, na kufuata mila zao, na kuongozwa na maoni yao? Lazima kuwe na kujitolea kikamilifu kwa

Bwana bila kujibakiza, bila malipo kwa MUNGU, kuachana na upendo wa ulimwengu na vitu vya kidunia, la sivyo hatuwezi kuwa wanafunzi wa Kristo. {1T 408.1}

Maisha na roho ya Kristo ndio kiwango pekee cha ubora na ukamilifu, na njia yetu salama tu ni kufuata mfano Wake. Tukifanya hivi, Yeye atatuongoza katika shauri lake na baadaye atatupokea kwa utukufu. Lazima tujitahidi kwa bidii na tuwe tayari kuteseka sana ili kutembea katika nyayo za Mkombozi wetu. MUNGU Yuko tayari kutufanyia kazi, kutupa Roho Wake bure, ikiwa tutajitahidi, kuiishi, kuiamini; na ndipo tunaweza kutembea katika nuru kama Yeye alivyo nuruni. Tunaweza kusherekea karamu upendo Wake na kunywa katika utimilifu wake {1T 408.2}

## SURA YA 76

## KAZI HUKO MASHARIKI

Ushabiki uliotawala miaka ya nyuma umeacha athari zake za uharibifu na ukiwa Mashariki. Niliona kwamba MUNGU aliwajaribu watu Wake kwa wakati mnamo 1844, lakini kwamba hakuna wakati ambao umewekwa tangu hapo ambao umekuwa na alama maalum za mkono Wake. Yeye Hajajaribu watu Wake kwa wakati wowote tangu 1844. Tumekuwa, na bado tuko, katika wakati wa kusubiri kwa uvumilivu. Msisimko mkubwa uliundwa wakati wa 1854, na wengi wameamua kwamba harakati hizo zilikuwa katika mpango wa MUNGU kwa sababu zilikuwa kubwa sana na wengi waliongolewa nazo. Lakini hitimisho

kama hilo sio lazima. Kulikuwa na mahubiri mengi kuhusiana na wakati wa mwaka 1854 ambayo yalikuwa ya busara na sahihi. Baadhi ambao walikuwa waaminifu walichukua Ukweli na uongo pamoja, na wakatoa dhabihu nyingi ya vitu walivyovimiliki kueneza kasoro hizo, na baada ya kukatishwa tamaa waliacha ukweli na makosa, na sasa ni mahali ambapo ni ngumu sana Ukweli kuwafikia. Baadhi ambao walivumilia kukatishwa tamaa huko wameuona ushahidi wa Ukweli wa sasa, na wamekuubali ujumbe wa malaika wa tatu, na wanajitahidi kuutekeleza maishani mwao. Lakini ambapo kuna mmoja ambaye amefaidika kwa kuamini wakati wa 1854, kuna kumi ambao wamejeruhiwa nao; na wengi wa hawa wamewekwa mahali ambapo hawatasadiki juu ya Ukweli, ingawa umewasilishwa mbele yao kwa uwazi kabisa. {1T 409.1}

Utangazaji wa muda wa 1854 ulihudhuriwa na roho ambaye hakuwa wa MUNGU. Ilikuwa roho ya kelele, mbaya, isiyojali, ya kusisimua. Kelele zilizingatiwa na wengi kama sehemu mhimu ya dini ya kweli, na kulikuwa na tabia ya kuwashusha wote katika kiwango cha chini. Wengi walichukulia hii kama unyenyekevu; lakini walipopingwa kwa maoni yao ya kipekee, wangesisimka kwa kuudhika kwa haraka sana, wakidhihirisha roho ya jeuri, kubamiza watu, na kuwashtaki wale ambao hawakukubaliana nao kuwa na kiburi na kupinga Ukweli na nguvu ya MUNGU. {1T 409.2}

Malaika watakatifu wamekasirishwa na kuchukizwa na njia isiyo ya heshima ambayo wengi wametumia jina la MUNGU, Yehova mkuu. Malaika wanataja Jina hilo takatifu kwa hofu na kicho kikubwa, daima wakiwa wamefunika nyuso zao wakati wanazungumza Jina la MUNGU ; na Jina la Kristo ni takatifu sana kwao kiasi kwamba wanazungumza kwa heshima kubwa. Lakini ni kinyume namna gani na roho na ushawishi ulioonekana katika harakati za wakati wa 1854. Wengine ambao bado wako chini ya ushawishi ule ule wanazungumza juu ya MUNGU kama vile wangemsemesha farasi au kitu kingine chochote cha kawaida. Katika maombi yao hutumia maneno MUNGU, Mwenyezi Mungu kwa njia ya kawaida na isiyo ya heshima. Wale ambao hufanya hivi hawatambui maana ya tabia iliyoinuliwa ya MUNGU, ya Kristo, au ya vitu vya mbinguni. {1T 410.1}

Nilioneshwa kwamba MUNGU alipowatuma malaika Zake zamani kuhudumia au kuwasiliana na watu binafsi, na watu hawa walipojifunza kwamba walikuwa wameona na kuzungumza na malaika, walishtuka na kuogopa kwamba wangekufa. Walikuwa na maoni yaliyoinuliwa sana juu ya ukuu na nguvu ya MUNGU za kutisha kiasi kwamba walifikiri ingewaangamiza wanapoletwa katika uhusiano wa karibu na wa moja kwa moja kutoka kwa uwepo Wake mtakatifu. Nilirejelewa kwa Waamuzi 13:21, 22: "Ndipo Manoa akajua kuwa alikuwa malaika wa Bwana. Manoa akamwambia mkewe, Hakika tutakufa, kwa sababu tumemwona MUNGU." Waamuzi 6:22, 23: "Naye Gideoni alipojua ya kuwa ni

malaika wa Bwana, Gideoni akasema, Ole, Ee Bwana MUNGU ! Kwa sababu nimemwona malaika wa Bwana uso kwa uso. Bwana akamwambia, Amani iwe kwako, usiogope: hautakufa. " Yoshua 5: 13-15: "Ikawa, hapo Yoshua alipokuwa karibu na Yeriko, alipoinua macho yake akatazama, na tazama, amesimama mtu mbele yake, na upanga Wake umefutwa mkononi Mwake; na Yoshua akamwendea, akamwambia, Je! wewe uko kwa ajili yetu, au kwa ajili ya wapinzani? Akasema, La! lakini kama nahodha wa jeshi la Bwana nimekuja sasa. Basi Yoshua akaanguka kifudifudi, akasujudu, akamwuliza, Bwana wangu anasema nini na mtumishi Wake? Akida wa jeshi la Bwana akamwambia Yoshua, Vua viatu vyako miguuni mwako; kwa maana mahali hapa unaposimama ni Patakatifu. Na Yoshua alifanya hivyo. "Ikiwa malaika tu waliogopwa na kuheshimiwa kwa sababu walitoka mbele za MUNGU, je! Ni kwa kicho na heshima kubwa zaidi kiasi gani ambayo MUNGU Mwenyewe anapaswa kupewa. {1T 410.2}

Wengi ambao waliongoka kupitia ushawishi wa harakati ya 1854 wanahitaji kubadilishwa upya. Na sasa kazi zaidi ya mara kumi inahitajika kusahihisha maoni yasiyofaa, yenye utata, ya kuvuruga ambayo wamepokea kutoka kwa walimu wao, na kuwaongoza wapokee ukweli ambao haujachanganywa na makosa, kuliko ingekuwa lazima kuwatoa mahali pa kwanza na kuwaleta juu ya ujumbe wa malaika watatu. Tabaka hili lazima liyaondoe kichwani mafundisho ya zamani, kabla ya kujifunza kwa usahihi tena, la sivyo magugu yenye sumu ya makosa yangekua na kung'oa mbegu za Ukweli. Makosa lazima kwanza zing'olewe, kisha udongo uandaliwe kwa ajili mbegu njema kuota na kuzaa matunda kwa utukufu wa MUNGU. {1T 411.1}

Dawa pekee ya Mashariki ni nidhamu kamili na mpangilio. Roho ya ushabiki imetawala tabaka fulani la watunza Sabato huko; wamekunywa, lakini kwa udogo tu kwenye chemchemi ya Ukweli na hawaijui roho ya ujumbe wa malaika wa tatu. Hakuna kitu kinachoweza kufanywa kwa tabaka hili mpaka maoni yao ya kishabiki, yenye kupitiliza yasahihishwe. Wengine ambao walikuwa katika harakati ya 1854 wameleta mafundisho na maoni yenye makosa, kama vile kutokuwa na ufufuo wa waovu, na wakati ujao, na wanatafuta kuunganisha maoni haya na uzoefu wao wa zamani na ujumbe wa malaika wa tatu. Hawawezi kufanya hivi; hakuna mapatano kati ya Kristo na Belial. Kutokufufuliwa kwa waovu na maoni yao ya kipekee ya wakati ujao ni jumla ya makosa makubwa ya imani, ambayo Shetani amefanyia kazi miongoni mwa uzushi wa siku za mwisho kutimiza kusudi lake mwenyewe la kuharibu nafsi. Makosa haya hayawezi kuwa na maelewano na ujumbe wenye asili ya mbinguni. {1T 411.2}

Baadhi ya watu hawa wana mazoezi ambayo wanayaita karama na wanasema kwamba Bwana ameziweka kanisani. Wanatoa sauti nakutamka maneno

yasiyoeleweka kabisa na mtu yoyote, (gibberish) yasiyo na maana ambayo wanaita ni lugha isiyojulikana, ambayo haijulikani sio tu na mwanadamu bali na Bwana na mbingu zote. Karama kama hizo zinatengenezwa na wanaume na wanawake, wakisaidiwa na mdanganyifu mkubwa. Ushabiki, msisimko wa uongo, kunena kwa lugha za uongo, na mazoezi ya kelele yamezingatiwa kama karama ambazo MUNGU ameweka katika kanisa. Wengine wamedanganywa hapa. Matunda ya haya yote hayakuwa mazuri. "Mtawatambua kwa matunda yao." Ushabiki na kelele vimezingatiwa kama ushahidi maalum wa imani. Wengine hawaridhiki na mkutano isipokuwa wana wakati wenye nguvu na furaha. Wanafanyia kazi hili na kuamsha msisimko wa hisia. Lakini ushawishi wa mikutano kama hiyo hauna faida. Wakati msisimko wa furaha hiyo unapoyeyuka, wao huzama chini kuliko kabla ya mkutano kwa sababu furaha yao haikutoka kwa chanzo sahihi. Mikutano yenye faida zaidi kwa maendeleo ya kiroho ni ile ambayo imetawaliwa na hali ya heshima, kicho, ibada na uchunguzi wa kina wa moyo kwa kila mmoja; kila mmoja akitafuta kujijua mwenyewe, na kwa bidii, na kwa unyenyekevu wa kina, akitafuta kujifunza juu ya Kristo. {1T 412.1}

Ndugu Lunt wa Portland, Maine, ameteseka sana katika hisia zake. Amehisi kwamba roho ambayo mara nyingi ilitawala katika mikutano yao haikuwa inalingana na ujumbe wa malaika wa tatu. Amekuwa na uzoefu katika ushabiki ambao umeacha uharibifu na ukiwa Mashariki, na hii inamfanya aangalie kwa mashaka kila kitu kinachoonekana kama ushabiki. Ana matukio yaliyopita mbele yake kama onyo na amejisikia kama kujitenga na, na kuzungumza waziwazi na wale ambao walikuwa na kiwango chochote cha ushabiki, kwani alihisi kwamba wao na kusudi la MUNGU walikuwa katika hatari. Ameangalia vitu kwa nuru sahihi. {1T 412.2}

Kuna roho nyingi zisizo na utulivu, zinazofurukuta daima, ambazo hazitajisalimisha kwenye nidhamu, mfumo, mkakati/mpango na utaratibu. Wanafikiri kwamba uhuru wao ungefutwa ikiwa wangeweka kando uamuzi wao wenyewe na watii hukumu ya wale wenye uzoefu. Kazi ya MUNGU haitaendelea isipokuwa kuna hali ya kujisalimisha kwa utaratibu na amri na kufukuza roho ya hovyo, vurugu, na fujo ya ushabiki kutoka kwa mikutano yao. Mguso moyoni na hisia sio ushahidi wa kweli kwamba mtu anaongozwa na Bwana. Shetani, ikiwa hajashukiwa, atatoa hisia na mivuto na miguso. Hiyo sio miongozo salama. Wote wanapaswa kufahamiana kabisa na ushahidi wa imani yetu, na somo kubwa linapaswa kuwa jinsi wanavyoweza kupamba imani yao na kuzaa matunda kwa utukufu wa MUNGU. Hakuna anayepaswa kuchukua kusudi la kujifanya kuwa chukizo kwa watu wasioamini. Tunapaswa kuwa safi, wenye kiasi, waungwana, tunaojistahi na kuinuliwa katika mazungumzo, na wasio na lawama maishani. Roho ya kudharau, mzaha, ya utani, ya hovyo inapaswa kukemewa. Sio uthibitisho wa neema ya MUNGU juu ya moyo wa watu

kuzungumza na kuomba talanta katika mkutano ili Bwana atuongoze jinsi ya kuzitumia vizuri ili kumtukuza, na kisha kujitolea kwa njia za ujeuri, na uzembe katika kuzungumza na kutenda tunapokuwa nje ya kanisa. Hao ni wawakilishi wanaoleta huzuni kwa imani yetu; ni aibu kwa kazi ya MUNGU, na huwakatisha watu tamaa. {1T 413.1}

Kuna mchanganyiko wa maoni ya kushangaza kati ya wanaodai kuwa watunza Sabato huko- ----Wengine hawapatani na mwili wa Kristo, na wakati wanaendelea kujaza nafasi wanayofanya sasa, watakuwa chini ya vishawishi vya Shetani na wataathiriwa na ushabiki na roho ya makosa. Wengine wana maoni ya kupendeza ambayo hupofusha macho yao kwa mambo muhimu, ya Ukweli, na kuwaongoza kuweka maoni yao ya kupendeza na kufikirika juu ya kiwango na zile Kweli muhimu. Kuonekana kwa watu kama hao, na roho inayowapata, inafanya Sabato ambayo wanadai kuiamini ichukize na kupingwa e na wasioamini wenye kutafakari. Ingekuwa bora zaidi kwa maendeleo na mafanikio ya ujumbe wa malaika wa tatu ikiwa watu kama hao wataacha ukweli. {1T 413.2}

Kulingana na nuru ambayo MUNGU amenipa, bado kutakuwa na kundi kubwa lililoinuliwa Mashariki ili kutii Ukweli kwa uendelevu. Wale ambao wanafuata kusudi lililovurugwa walilochagua wataachwa kukumbatia makosa ambayo mwishowe yatasababisha kupinduliwa kwao; lakini kwa muda watakuwa vizuizi kwa wale ambao wangeupokea Ukweli. wachungaji wanaofanya kazi kwa Neno na mafundisho ya imani wanapaswa kuwa wafanya kazi kamili, na wanapaswa kuwasilisha Ukweli katika usafi wake, lakini kwa usahili. Wanapaswa kulisha kundi na chakula safi, kilichopetwa vizuri na kuondoa pumba. Kuna nyota zinazotangatanga zinazodai kuwa ni wahudumu waliotumwa na MUNGU ambao wanahubiri Sabato kutoka mahali hadi mahali, lakini ambao wana Ukweli uliochanganywa na upotovu na wanatoa maoni yao mengi kwa watu. Shetani amewasukuma kuchukiza wasioamini wenye akili na busara. Baadhi hawa wana mengi ya kusema juu ya karama ambazo mara nyingi hutumika. Wanajitolea kwa hisia kali, za kusisimua na hutoa sauti zisizoeleweka ambazo wanaita karama ya lugha, na tabaka fulani linaonekana kupendezwa na maonesho haya ya ajabu. Roho ya ajabu inatawala tabaka hili, ambalo lingeweza kumlemea na kumshambulia mtu yeyote ambaye angewakemea. ROHO WA MUNGU hayupo katika kazi hizo na hawi pamoja na wafanyikazi kama hao. Wana roho nyingine. Hata hivyo, wahubiri hao wanafanikiwa kati ya tabaka fulani. Lakini hii itaongeza sana kazi ya wale watumishi ambao MUNGU atawatuma, ambao wanastahili kuwasilisha mbele ya watu Sabato na karama katika mwangaza wake sahihi, na ambao ushawishi na mfano wao unastahili kuigwa. {1T 414.1}

Ukweli unapaswa kuwasilishwa kwa njia ambayo itawafanya wenye akili kuvutiwa. Hatueleweki kama watu, lakini tunaonekana kama watu maskini, wa hali ya chini,wenye akili dhaifu, wanyonge, na tuliodhoofika. Halafu ni muhimu jinsi gani kwamba wote wanaofundisha, na wote wanaoamini Ukweli, wawe wameathiriwa na ushawishi wa utakaso Wake katika maisha yao thabiti, yaliyoinuliwa utawaonesha watuwasioamini kwamba wamedanganywa katika watu hawa. Ni muhimu sana kwamba kusudi la Ukweli livuliwe kila kitu kama msisimko wa uongo na wa kishabiki, ili uUweli uweze kusimama kwa sifa zake, ukifunua usafi wake wa asili na tabia iliyoinuliwa. {1T 414.2}

Niliona kuwa ni muhimu sana kwa wale wanaohubiri Ukweli kusafishwa katika mienendo yao, kuachana na mambo yasiyo ya kawaida na udanganyifu, na kuwasilisha Ukweli kwa usafi na uwazi. Nilirejelewa kwa Tito 1: 9: "Akalishika sana Neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga." Katika mstari wa 16 Paulo anazungumza juu ya tabaka ambalo linakiri kwamba wanamjua MUNGU, lakini kwa matendo wanamkana, ni wenye machukizo waasi bali kwa kila tendo jema hawafai." Kisha anamsihi Tito: "Lakini wewe nena mambo yapasayo mafundisho yenye uzima; ya kwamba wazee wawe wenye kiasi,wastahivu wenye busara, wazima katika imani na katika upendo na katika saburi. Vivyo hivyo, na vijana uwaonye kuwa na kiasi katika mambo yote ukijionesha wewe mwnyewe kuwa kielelezo cha matendo mema na katika mafundisho yako ukionesha usahihi na ustahivu na maneno yenye uzima yasiyoweza kuhukumiwa makosa, ili Yule mwenye kupinga atayarike, kwa kuwa hana neno baya la kunena juu yetu." Maagizo haya yameandikwa kwa faida ya wale wote ambao MUNGU amewaita kuhubiri Neno, na pia kwa faida ya watu wake wanaolisikia neno. {1T 415.1}

Ukweli wa MUNGU hautashusha hadhi kamwe, lakini utamwinua mpokeaji, kuiboresha hali yake, kutakasa fikira zake, na kumkamilisha kwa ushirika wa malaika safi na watakatifu katika ufalme wa MUNGU. Kuna wengine ambao kabla Ukweli haujawafikia, wanakuwa na tabia zisizo za kawaida, wanakuwa watu jeuri, watukanaji, wakorofi, wenye kujisifu, wanaodhulumu majirani zao ili kujipatia faida ikiwa wanaweza, hukosea kwa njia nyingi, lakini Ukweli unapoaminiwa na wao kutoka moyoni, utafanya mabadiliko kamili katika maisha yao. Wataanza mara moja kazi ya matengenezo. Ushawishi wa Ukweli mtakatifu utamuinua mtu mzima. Katika shughuli zake na wanadamu wenzake atakuwa na hofu ya MUNGU mbele yake, na atawapenda jirani zake kama yeye mwenyewe, na atashughulika kwa haki kama ambavyo yeye angependa kushughulikiwa. Mazungumzo yake yatakuwa ya ukweli yenye furaha na yenye tabia iliyoinuliwa ambayo wasio amini hawezi kumtumia kwa faida/maslahi yao au kusema maovu dhidi yake kwa haki,na bila kubughudhiwa na njia zake zisizo na tamaa na usemi wake mbovu. Atabeba ushawishi wake uliotakaswa katika

familia yake na hebu nuru yake na iangaze mbele yao kwamba kwa kuona matendo yake mema wamtukuze MUNGU. Katika Njia zake zote atakuwa mfano wa maisha ya Kristo kwa watu.{1T 415.2}

Sheria ya MUNGU haitaridhishwa na chochote kilichopungufu ya ukamilifu, kamili, na utii kamili kwa madai yake yote. Kufikia nusu ya mahitaji yake, na bila kutoa utii kamili na wa loma, hakutatafanya chochote kufaulu. Ulimwengu na makafiri wanapenda msimamo na wamewahi kushawishika kwa nguvu kwamba MUNGU amekuwa wa Ukweli kwa watu Wake wakati kazi zao zinalingana na imani yao. "Mtawajua kwa matunda yao." Kila mti hujulikana kwa matunda yake. Maneno yetu, matendo yetu, ndio matunda tunayozaa. Kuna watu wengi wanaosikia Maneno ya Kristo, lakini hawayatendi. Wanadai kuwa ni waumini kwa mdomo tu, lakini matunda yanachukiza wasioamini. Wanajisifu, na wanasali na kuzungumza kwa njia ya kujiona kuwa waadilifu, wakijiinua, wakisimulia matendo yao mema, na, kama yule Mfarisayo, wakimshukuru MUNGU kwamba hawafanani na watu wengine. Walakini hawa ndio wajanja/wadanganyifu, na wanajishughulisha na biashara. Matunda yao sio mazuri. Maneno na matendo yao ni makosa, na bado wanaonekana kupofushwa na hali yao duni. {1T 416.1}

Nilioneshwa kuwa andiko lifuatalo linatumika kwa wale walio chini ya udanganyifu kama huu: "Sio kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni, Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, je! hatukutabiri kwa Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo? na kwa Jina Lako tumefanya miujiza mingi? Na ndipo nitawaambia, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. "{1T 416.2}

Hapa kuna udanganyifu mkubwa ambao unaweza kuathiri akili ya mwanadamu; watu hawa wanaamini kuwa wako sahihi wakati wamekosea. Wanafikiri kwamba wanafanya kazi kubwa katika maisha yao ya kidini, lakini mwishowe Yesu anafunua kifuniko chao cha kujiona wenye haki na anawasilisha wazi mbele yao picha yao ya kweli katika makosa yao yote na ulemavu wa tabia ya kidini. Wanajikuta wanapungua wakati wamechelewa milele kwa mahitaji yao kutoshelezwa. MUNGU ameandaa njia za kusahihisha wakosaji: lakini ikiwa wale wanaokosea, wanachagua kufuata uamuzi wao wenyewe, na wakidharau njia ambayo ameweka kuwasahihisha na kuwaunganisha kwenye Ukweli, wataletwa katika nafasi iliyoelezewa na maneno ya Bwana wetu yaliyonukuliwa hapo juu. {1T 417.1}

MUNGU analeta watu na kuwaandaa kusimama kama wamoja, walioungana kuzungumza mambo yale yale, na kwa hivyo kutekeleza maombi ya Kristo kwa wanafunzi Wake. "Wala siwaombei hawa peke yao, bali pia wale

watakaoniamini kupitia neno lao; ili wote wawe kitu kimoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, na Mimi ndani yako, ili wao pia wawe kitu kimoja ndani yetu: ili ulimwengu upate kuamini kuwa Wewe umenituma. " {1T 417.2}

Kuna makundi madogo yanayoendelea kuongezeka yanayoamini kwamba MUNGU Yuko tu kwa wachache sana, waliotawanyika sana, na ushawishi wao ni kubomoa na kutawanya yale ambayo watumishi wa MUNGU hujenga. Akili zisizo na utulivu ambazo zinataka kuona na kuamini kitu kipya kila wakati zinaibuka kila wakati, zingine mahali hapa na zingine mahali pengine, zote zikifanya kazi maalum kwa adui, lakini zite zukidai kuwa na Ukweli. Wanasimama kando na watu ambao MUNGU ambao anawaongoza na kuwafanikisha, na ambao kupitia wao, Mungu atafanya kazi Yake kuu. Huendelea kuelezea hofu yao kwamba mwili wa watunza Sabato unakuwa kama ulimwengu, lakini hakuna hata wawili kati ya hawa ambao maoni yao yanapatana. Wao ni wametawanyika na wamechanganyikiwa, na bado wanajidanganya kiasi cha kufikiri kwamba MUNGU Yuko pamoja nao haswa, kuliko watu wengine. Baadhi ya hawa wanakiri kuwa na karama kati yao; lakini wanaongozwa na ushawishi na mafundisho ya karama hizi kwa kutilia mashaka wale ambao MUNGU ameweka mzigo maalum wa kazi Yake, na kuongoza makundi ya watu kutoka kwenye mwili. Watu, ambao, kwa mujibu wa Neno la MUNGU, wanajitahidi sana kuwa wamoja, ambao wameimarika katika ujumbe wa malaika wa tatu, wanatazamwa kwa mashaka kwa sababu wanaongeza kazi yao na wanakusanya roho ndani ya Ukweli. Wanachukuliwa kuwa wa kidunia kwa sababu wana ushawishi ulimwenguni, na matendo yao yanashuhudia kwamba wanatarajia MUNGU bado afanye kazi maalum na kubwa duniani, kuleta watu na kuwasaidia kupata stahiki za kumwona Kristo pale ajapo. {1T 417.3}

Tabaka hili halijui wanaamini nini, au sababu za imani yao. Wanajifunza kila wakati, na hawawezi kamwe kupata ujuzi wa ile Kweli. Mtu mmoja anaibuka na maoni yasiyofaa, yenye makosa, na anadai kwamba MUNGU amemtuma na nuru mpya na tukufu, na wote lazima waamini anayoleta. Wengine ambao hawana imani iliyodhibitishwa, ambao hawatii mwili, lakini wanaeleaelea bila nanga kuwashikilia, wanapokea upepo huo wa mafundisho. Nuru yake inaangaza kwa namna ambayo itasababisha ulimwengu kugeuka kutoka kwake kwa karaha na kumchukia. Halafu kwa kukufuru, anajiweka kando ya Kristo na huku akidai kwamba ulimwengu unamchukia kwa sababu ile ile ambayo walimchukia Kristo. Mwingine anainuka, akidai kuongozwa na MUNGU, na anatetea uzushi wa kutofufuka kwa waovu, ambayo ni moja wapo ya ujanja mkubwa wa ugwiji wa Shetani. Mwingine anapenda maoni yasiyofaa kuhusu Zama za baadaye (Future Age). Mwingine anahimiza vazi la Amerika kwa usongo mkubwa (American Costume). Wote wanataka uhuru kamili wa kidini, na kila mmoja anajitegemea, yuko huru kutoka kwa wengine, na bado wanadai kwamba MUNGU anafanya kazi nao kwa njia maalumu. {1T 418.1}

Wengine hufurahi na kujiinua kuwa wana karama za Roho, ambazo wengine hawana. Acha MUNGU awaokoe watu wake kutoka katika karama hizo. Je, Karama hizi zinawafanyia nini? Je! kupitia zoezi la karama hizi, wanaletwa katika umoja wa imani? Je, wanawasadikisha wale wasio amini kwamba MUNGU Yuko pamoja nao, na wana Ukweli? Wakati hawa wasio na busara na hawaelewani, wakiwa wameshikilia maoni yao tofauti, wanapokuja pamoja na kuna msisimko mkubwa na lugha isiyojulikana, wanapoangaza nuru yao, makafiri wangeweza kusema: Watu hawa hawana akili timamu; wamechukuliwa na msisimko wa uongo, na tunajua kwamba hawana Ukweli. Hawa husimama moja kwa moja katika njia ya wenye dhambi, wakiwazuia kuingia; ushawishi wao ni wenye matokeo kuwazuia wengine kukubali Sabato. Hao watalipwa kulingana na matendo yao. Laiti wangefanya matengenezo kwa MUNGU na wangebadilishwa au waachane na Sabato! Hivyo wasingeweza kusimama katika njia ya makafiri-watu wasioamini. {1T 418.2}

MUNGU ameongoza watu ambao wamefanya kazi ya kuhenyesha kwa miaka mingi, ambao wamekuwa tayari kujitolea, ambao wamepata shida, ufukara na wamevumilia majaribu ili kuleta Ukweli mbele ya ulimwengu, na kwa kusudi lao thabiti waondoe aibu ambayo wenye itikadi kali wameileta juu ya kazi ya MUNGU. Wamekutana na upinzani wa kila aina. Wamehenyeka usiku na mchana kutafuta ushahidi wa imani yetu ili waweze kuleta Ukweli katika uwazi wake, katika hali iliyounganishwa, ili uweze kuhimili upinzani wote. Majaribio ya uchungu na majaribio ya akili kuhusiana na kazi hii kubwa yamechakaza zaidi mwili zaidi ya mmoja na kuvijaza mvi vichwani mwao mapema. Hawajachakaa bure. MUNGU ameweka alama maombi yao ya dhati na bidii, na machozi, yenye uchungu ili wawe na nuru na Ukweli, na Ukweli uangaze kwa uwazi wake kwa wengine. Amezitia alama juhudi zao za kujitolea, na atawalipa kama kazi zao zilivyokuwa. {1T 419.1}

Kwa upande mwingine, wale ambao hawajafanya bidii kuleta Ukweli huu wa thamani wamekuja na kupokea vidokezo kadhaa, kama Ukweli wa Sabato, ambao wote tayari umetayarishwa mikono mwao, na kisha shukrani yoyote wanayoionesha kwa kile ambacho hakikuwagarimu chochote, lakini wengine imewagharimu sana, wameinuka kama Kora, Dathani, na Abiramu, na kuwashutumu wale ambao MUNGU ameweka mzigo wa kazi Yake. Wangeweza kusema: "Mnachukua sana juu yenu, kwa kuwa mkutano wote ni watakatifu, kila mmoja wao, na Bwana Yu kati yao." Wao ni wageni katika kutoa shukrani. Wana roho yenye nguvu ambayo haijasalimishwa kwa hekima, ambayo itawaongoza kwenye uharibifu wao wenyewe. {1T 419.2}

MUNGU amebariki watu Wake ambao wamesonga mbele wakiyafuata mipango/majaliwa Yake yanapofunguliwa. Yeye ameleta watu kutoka kila

tabaka kuja juu ya jukwaa kubwa la Ukweli. Makafiri wameshawishika kwamba MUNGU alikuwa pamoja na watu Wake na wamenyenyekeza mioyo yao kuutii Ukweli. Kazi ya MUNGU inasonga mbele kwa kasi. Walakini pamoja na uthibitisho wote kwamba MUNGU amekuwa akiongoza kanisa, kuna wale wataendelea kuwapo, wale wanaokiri Sabato, ambao watajitegemea bila mwili, na kuamini na kutenda wa navyotaka kuchagua wenyewe. Maoni yao yamechanganyikiwa. Hali yao ya kutawanyika ni ushuhuda uliosimama kwamba MUNGU hayuko pamoja nao. Kwa ulimwengu Sabato na makosa yao yamewekwa kwa kiwango sawa na kutupwa mbali pamoja. MUNGU huwakasirikia wale wanaofuata mwenendo huu na kuufanya ulimwengu uwachukie. Ikiwa Mkristo anachukiwa kwa sababu ya matendo yake mema na kwa kumfuata Kristo, atapata thawabu; lakini ikiwa anachukiwa kwa sababu mwenendo wa tabia yake haujapaliliwa (mjeuri, mkorofi, mtukanaji, mlevi, mgomvi, mchafu wa maadili), na kwa sababu ya tabia yake mbaya isiyopaliliwa vizuri na kufanya Ukweli kuwa jambo la ugomvi na majirani zake, na anafanya mkakati wa kuifanya Sabato iwe ya kukasirisha kwao kwa kadri awezavyo, mtu huyu ni kikwazo kwa watenda dhambi, aibu kwa Ukweli mtakatifu, na isipokuwa ametubu ni afadhali afungwe jiwe la kusagia shingoni mwake na atupwe baharini. {1T 420.1}

Hakuna fursa au tukio linalopaswa kufanyika ili watu wasioamini walaumu imani yetu. Tunachukuliwa kuwa watu wasio wa kawaida na wa kipekee na hatupaswi kuchukua mwenendo wa kuwaongoza wasioamini kutufikiria zaidi ya vile imani yetu inataka tuwe.{1T 420.2}

Baadhi ambao wanao uamini Ukweli wanaweza kufikiria kuwa itakuwa afya zaidi kwa akina dada kuiga vazi la Amerika, lakini ikiwa mavazi hayo yangelemaza ushawishi wetu kati ya wasioamini ili tusiweze kupata urahisi wa kupeleka injili kwao, basi, hatupaswi kwa namna yoyote kuiga, ingawa tulipata mateso mengi kama matokeo yake. Lakini wengine wanadanganywa kwa kufikiria kuna faida nyingi ya kupokea kutoka kwa vazi hili. Ingawa inaweza kudhihirisha faida kwa wengine, ni jeraha kwa wengine. [Ona Kiambatanisho.] {1T 421.1}

Niliona kwamba agizo la MUNGU limebadilishwa, na maagizo Yake maalum hayazingatiwi, na wale wanaoiga vazi la Amerika (American Costume). Nilirejelewa kwenye Kumbukumbu la Torati 22: 5: "Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanaume, wala mwanaume asivae mavazi ya mwanamke kwa maana kila afanyae mambo hayo ni machukizo kwa Bwana MUNGU wako." MUNGU asingependa watu Wake wapokee kile kinachoitwa mavazi ya matengenzo. Ni mavazi yasiyo na adabu, hayafai kabisa kwa wafuasi wa Kristo wanyenyekevu. {1T 421.2}

Kuna kuongezeka kwa tabia ya kuwa na wanawake katika mavazi yao na muonekano wao karibu sawa na jinsia nyingine iwezekanavyo, na kutengeneza mavazi yao kuwa kama ya wanaume, lakini MUNGU anatamka hili kuwa chukizo. "Vivyo hivyo pia, wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujistiri, pamoja na adabu nzuri na moyo wa kiasi." 1 Timotheo 2: 9. {1T 421.3}

Wale ambao wanahisi wameitwa kujiunga na harakati hiyo wakipendelea haki za mwanamke na kile kinachoitwa matengenezo ya mavazi wanaweza pia kukata uhusiano wote na ujumbe wa malaika wa tatu. Roho ambayo huhudumia moja haiwezi kuwa na mapatano na hiyo nyingine. Maandiko yako wazi juu ya uhusiano na haki za wanaume na wanawake. Wafuasi wa roho za umizimu wamepitisha mtindo huu wa mavazi. Waadventista Wasabato, ambao wanaamini katika kurejeshwa kwa karamaza Roho, mara nyingi hujulikana kama washirika wa roho ya umizimu. Acha waige desturi ya vazi hili la American Costume, na ushawishi wao umekufa. Watu wangewaweka kwenye kikapu cha washirika wa roho ya umizimu na wangekataa kuwasikiliza. {1T 421.4}

Pamoja na kile kinachoitwa matengenezo ya mavazi kuna roho ya kukosa heshima, na mizaha na ujasiri wa kukakamaa na mavazi haya. Unyenyekevu, kujistahi, kuhifadhi heshima na adabu njema huonekana kuondoka kwa wengi wanapoiga mtindo huo wa mavazi. Nilioneshwa kwamba MUNGU angependa tuchukue kusudi thabiti na linaloelezeka. Acha wadada waige desturi za vazi la Marekani (America Costume) na wataharibu ushawishi wao na wa waume zao. Wangekuwa usemi wa kejeli na dhihaka. Mwokozi wetu anasema: "Ninyi ni nuru ya ulimwengu." "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema, na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni." Kuna kazi kubwa kwetu ya kufanya ulimwenguni, na MUNGU hatatutaka tuchukue shauri la kupunguza au kuharibu ushawishi wetu kwa ulimwengu {1T 422.1}

## SURA YA 77

## MAOMBI YA DAUDI

Nilioneshwa Daudi akimsihi Bwana asimwache wakati atapokuwa mzee, na ni nini kilichomuhimiza kuwa na maombi ya dhati. Aliona kwamba wazee wengi

waliomzunguka walikuwa hawana furaha na kwamba nasaba ya tabia isiyo na furaha iliongezeka kadri umri ulivyoongezeka. Ikiwa watu kwa asili walikuwa wemejifunga na tamaa walikuwa kwa kiwango kikubwa hawakubaliki na itakuwa hivyo zaidi katika uzee wao. Ikiwa walikuwa wenye wivu, wenye uchungu, na wasio na subira, watakuwa hivyo zaidi sana uzeeni. {1T 422.2}

Daudi alikuwa na huzuni alipoona kwamba wafalme na wakuu ambao walionekana kuwa na hofu ya MUNGU mbele yao wakiwa katika nguvu za utu uzima, waliwaonea wivu marafiki zao wa karibu na jamaa wakati wa uzee. Walikuwa katika hofu isiyokoma kwamba ni kusudi la ubinafsi ndilo ambalo lilisababisha marafiki zao kuonesha kuwa na urafiki na shauku nao. Wangesikiliza vidokezo na ushauri wa udanganyifu wa watu baki dhidi ya wale ambao wangekuwa wasiri wao. Wivu wao usiodhibitiwa wakati mwingine uliwaka moto kwa sababu wote hawakukubaliana na maamuzi yao ambayo yalikuwa yameanza kushindwa/kufeli. Tamaa yao ilikuwa ya kutisha. Mara nyingi walidhani kuwa hata watoto wao na jamaa walikuwa wakitamani wafe ili kuchukua nafasi yao na kumiliki utajiri wao, na kupokea heshima ambayo walikuwa wamepewa. Na wengine walidhibitiwa sana na hisia zao za wivu, za kutamani hata kuwaua watoto wao wenyewe. {1T 422.3}

Daudi aliashiria kwamba ingawa maisha ya wengine wakati wa nguvu za ujana yalikuwa ya haki, wakati uzee ulipowapata walionekana kupoteza hali ya kujitawala nafsi. Shetani aliingia na kuongoza akili zao, akiwafanya wasitulie na wasiridhike. Aliona kwamba wazee wengi walionekana wamemwacha MUNGU na kujianika kwa kejeli na lawama za maadui zake. Daudi aliguswa moyo sana; alifadhaika sana kwani alitazamia wakati ambapo atakuwa mzee. Aliogopa kwamba MUNGU angemwacha na kwamba atakuwa hana furaha kama watu wengine wazee ambao mambo yao alikuwa ameyaona, na angeachwa kuwa aibu kwa maadui wa Bwana. Akiwa na mzigo huu juu yake aliomba kwa bidii: "Usinitupe wakati wa uzee; usiniache wakati nguvu zangu zinakoma." "Ee MUNGU, umenifundisha tangu ujana wangu; na hata leo nimetangaza maajabu Yako. Sasa hata nikiwa mzee na mvi, Ee MUNGU, usiniache; hata nitakapokuwa nimeonesha nguvu Zako kwa kizazi hiki, na Nguvu Yako kwa kila mtu atakayekuja. " Zaburi 71: 9, 17, 18. Daudi alihisi ulazima wa kujilinda dhidi ya maovu ambayo huwapata watu uzeeni. {1T 423.1}

Mara nyingi ni watu wazee ndiyo hawataki kutambua na kukiri kuwa nguvu zao za akili zimechoka. Wao hufupisha siku zao kwa kushugulikia mambo ambayo ni ya watoto wao. Shetani mara nyingi huchezea fikira zao na huwaongoza kujisikia wasiwasi kila wakati juu ya pesa zao. Ni sanamu yao, na wanaihifadhi pesa kwa uangalifu wa kuhuzunisha. Wakati mwingine watajinyima raha nyingi za maisha, na kufanya kazi zaidi ya nguvu zao, badala ya kutumia mali ambazo wanazo tayari. Kwa njia hii wanajiweka ndani ya uhitaji wa daima, kwa hofu

kwamba wakati mwingine katika siku za usoni watapungukiwa. Hofu hizi zote hutokana na Shetani. Adui anasisimua viungo ambavyo husababisha hofu ya woga na wivu ambayo huharibu utukufu wa roho na kuharibu mawazo na hisia zilizoinuliwa. Watu kama hao ni wenda-wazimu juu ya mada ya pesa. Ikiwa wangechukua msimamo ambao MUNGU angekuwa nao, siku zao za mwisho zingeweza kuwa bora zaidi na zenye furaha zaidi kuliko hata ujanani. Wale ambao wana watoto ambao kwa sababu ya uaminifu, hekima na usimamizi mzuri wana sababu ya kuwafanya watoto wao kuwa wasiri wao, wanapaswa kuwaruhusu watoto wao kuwafurahisha. Wasipofanya hivi, Shetani atatumia faida ya ukosefu wao wa nguvu ya akili na atawaendesha na kusimamia mambo yao. Wanapaswa kuweka kando wasiwasi na mizigo, na watumie wakati wao kwa furaha kadiri wawezavyo, na kuiva tayari kwa mbingu. {1T 423.2}

## SURA YA 78

## KUPILITIZA KATIKA MAVAZI.

Hatufikirii kuwa inaendana na imani yetu kuvaa vazi la Amerika (American Costume), kuvaa guo ya kitamba laini cha pamba, au kupita kiasi katika kuvaa nguo ndefu ambazo zinafagia njia za barabarani na mitaa. Ikiwa wanawake wangevaa nguo zao ili kusafisha uchafu wa barabara kwa inchi moja au mbili, nguo zao zingekuwa za kawaida, na zingetunzwa safi kwa urahisi zaidi, na wangevaa kwa muda mrefu. Nguo kama hiyo ingepatana na imani yetu. Nimepokea barua kadhaa kutoka kwa akina dada wakiuliza maoni yangu kuhusu kuvaa sketi zenye marinda na zilizo na shepu ya mwamvuli (corded skirts). Maswali haya yalijibiwa katika barua ambayo nilimpelekea dada mmoja huko Wisconsin. Nitatoa barua hiyo hapa kwa faida ya wengine: {1T 424.1}

"Sisi kama watu hatuamini ni jukumu letu kutoka nje ya ulimwengu ili kuwa nje ya mitindo. Ikiwa tuna vazi nadhifu, rahisi, lisilokuwa na mapambo mengi, la

kustahi, na halisumbui au kumbughudhi mtu, na walimwengu wakichagua kuvaa kama sisi, je, sisi tutabadilisha mtindo huu wa mavazi ili kuwa tofauti na ulimwengu? Hapana, hatupaswi kuwa wa kipekee au tofauti sana (kama kuwa washamba) katika mavazi yetu kwa sababu ya kutofautiana na ulimwengu, wasije wakatudharau kwa kufanya hivyo. Wakristo ni nuru ya ulimwengu, chumvi ya dunia. Mavazi yao yanapaswa kuwa nadhifu na ya kustahi mwili, mazungumzo yao ni safi na ya mbinguni, na mwenendo wao hauna lawama. {1T 424.2}

"Tutavaaje? Ikiwa yeyote alikuwa amevaa vitambaa vizito kama mablanketi ya quilt kabla ya kuletwa kwa vazi laini la sketi na magauni ya hoops ambayo yanabana kiuno na kuburuza chini wakati mtu akitembea, kwa ajili tu ya maonyesho na sio kujipatia faraja kwa kuondoa usumbufu, wamefanya dhambi kwa nafsi zao kwa kuumiza afya zao, ambalo ni jukumu lao kuitunza. Ikiwa yeyote anavaa sasa ili kuonekana tu kama vazi la hoops, hufanya dhambi, kwa kuwa wanatafuta kuiga mtindo ambao ni wa aibu. Sketi za marinda na mwamvuli zimevaliwa kabla ya vazi hili linalobana kiuno na kufagia ardhi. Nimevaa sketi za marinda na mwamvuli toka nikiwa na umri wa miaka kumi na nne, sio kwa kujionyesha lakini kwa kujistiri, faraja na adabu. Kwa sababu vazi hili la hoops lenye kiuno kinachobana na linafagia barabara liliingizwa, mimi sikuiacha sketi yangu ya mwamvuli ka ajili ya hilo. Je! sasa nitaitupa kando kwa sababu mtindo wa gauni na sketi refu zinazobana kiuno na kufagia barabara umeingizwa? Hapana, hiyo itakuwa ni kulibeba jambo kwa kupitiliza kiasi. {1T 425.1}

"Ninapaswa kukumbuka kila wakati kuwa lazima niwe mfano na kwa hivyo si lazima nikurupuke kuingia katika mtindo huu au ule, lakini nifuate kusudi lililo sawa na niwe huru bila kuendeshwa kwa kupitiliza kiasi katika mavazi. Kutupa sketi yangu ya mwamvuli na yenye marinda ambayo wakati wote ilikuwa ni sawa na yenye kustiri, na isiyo na usumbufu na kuvaa sketi ya pamba inayobana kiuno, na hivyo kuonekana kituko cha ajabu kwa kupitiliza kiasi kwenda upande mwingine, itakuwa makosa, kwani hapo nisingeweka mfano sahihi, lakini ningeweka hoja ndani ya vinywa vya wavaaji wa nguo za hoops -kwamba mimi naridhiana nao nk. Ili kuhalalisha kwamba wana haki ya kuvaa hoops, wangesonda kidole kwangu kama yule asiyevaa vazi hili la kubana kiuno na kufagia barabara, na kusema kwamba hawatajiaibisha wenyewe kwa njia hiyo. Kwa kuingia kwenye msimamo mkali unaopitiliza kama huo tungeharibu ushawishi wote ambao labda tungekuwa nao, na kuongoza wavaaji wa hoops ikuhalalisha mwenendo wao. Lazima tuvae kwa heshima, kwa kujistahi, bila kuzingatia  mtindo wa hoops hata kidogo. {1T 425.2}

"Kuna msimamo wa kati katika mambo haya. Lo, laiti sisi sote tungepata busara kupata msimamo huo na kuutunza. Katika wakati huu adhimu na wa pekee sisi

sote tuchunguze mioyo yetu wenyewe, tutubu dhambi zetu, na kujinyenyekeza mbele za MUNGU. Kazi iko kati ya MUNGU na roho zetu. Ni kazi binafsi, na wanadamu wote watakuwa na ya kuwatosha kufanya bila kukosoa mavazi, matendo, na nia ya ndugu na dada zao. Mtafuteni Bwana, ninyi nyote wenyenyekevu wa dunia, mliotenda hukumu yake; tafuta haki, utafute upole; labda utafichwa katika siku ya hasira ya Bwana. Hapa kuna kazi yetu. Sio wenye dhambi ambao wamezungumziwa hapa, lakini wapole wote wa dunia, ambao wametenda hukumu Zake au kuzishika amri Zake. Kuna kazi kwa kila mtu, na ikiwa wote watatii, tutaona umoja mzuri katika safu ya watunza Sabato. " {1T 425.3}




American costume na Corded Skirt

## SURA YA 79

## MAWASILIANO NA MZEE HULL

Kamati Kuu ya (Halmashauri Kuu-The General Conference of Seventh Day Adventists) hapa itaeleza idhini ya uchapishaji wa Shuhuda hii. Hususani tunapendekeza uchapishaji wa barua zilizoelekezwa kwa Mzee Hull na kutolewa wakati wa tarehe zao. Tunamtaka msomaji awe makini katika azimio kwenye ukurasa wa 442. Inaelezwa kwamba Mzee Hull alitaka kuongozwa kama kipofu anayetegemea mwingine ili kuona kwaajili yake. Kwenye Mkutano Mkuu kule

battle creek, Mei, 1863, mzee Hull alikubali uhalali wa tamko lakini tangu hapo amepinga. Kamati sasa inadumisha kuwa kusudi lake katika nafasi finyu ya miezi minne iliyopita, kwa kuacha kila dondoo ya imani ya dini ambayo ni pendwa kwetu kama watu, ni udhihirisho unaoshikika na usahihi wa kauli hapo juu kwamba anapaswa kufuata mashauri ya ndugu zake (General Conference Committee).
Novemba 5, 1862, nilioneshwa hali ya Ndugu Hull. Alikuwa katika hali ya kushtuka. Ukosefu wake wa kujitoa wakfu na utauwa muhimu ulimwacha chini ya maoni ya Shetani. Ametegemea nguvu zake mwenyewe badala ya mkono wenye nguvu wa Bwana, na mkono huo wenye nguvu umeondolewa kwa sehemu. {1T 426.1}

Nilioneshwa kuwa jambo la kutisha zaidi katika kisa cha Ndugu Hull ni kwamba amelala usingizi kwa hatari yake. Hahisi kengele ya dharura, anahisi salama kabisa na amepumzika kabisa, wakati Shetani na malaika zake wanashangilia ushindi wao. Muda wote kama Ndugu Hull aliendeleza mzozo, akili yake ilikuwa imeimekazwa/imeimarishwa, na kulikuwa na mgongano wa roho. Sasa amekomesha mzozo, na mgongano umekoma. Akili yake imetulia, na Shetani humruhusu awe na amani. Ah ni hatari jinsi gani kwa msimamo ambao uioneshwa kwangu! Kesi yake inakaribia kukosa tumaini kabisa, kwa sababu hafanyi juhudi yoyote kumpinga Shetani na kujinasua kutoka kwenye mtego wake wa kutisha. {1T 426.2}

Ndugu Hull ameshughulikiwa kwa uaminifu. Amehisi kuwa alikuwa amebanwa /amezuiliwa sana -amekoseshwa uhuru, kwamba hakuweza kutenda asili yake. Wakati nguvu ya Ukweli, kwa msukumo wake wote ilimshawishi, alikuwa salama kwa kulinganisha; lakini vunja msukumo na nguvu ya Ukweli juu ya akili, na hakuna kizuizi, tabia za asili zinaongoza, na hakuna mahali pa kusimama. Amechoka na mzozo huo, na kwa muda fulani ametamani kwamba angeweza kutenda kwa uhuru zaidi vile anataka mwenyewe, na amejeruhiwa kwa maonyo ya ndugu zake. Aliwasilishwa kwangu akiwa amesimama ukingoni mwa korongo la kutisha, tayari kuruka. Ikiwa atachukua hatua hiyo ya kujirusha, itakuwa mwisho; hatima yake ya milele itaamuliwa. Anafanya kazi na maamuzi ya umilele. Kazi ya MUNGU haimtegemei Ndugu Hull. Ikiwa ataacha safu ya wale wanaobeba bendera iliyo na damu ya Mwana wa Mfalme Emanueli, na kujiunga na kampuni/kikundi kinachobeba bendera nyeusi, itakuwa hasara yake mwenyewe, uharibifu wake wa milele. {1T 427.1}

Niliona kwamba wale wanaotaka wanaweza kuwa na fursa pana ya kutilia shaka uvuvio na Ukweli wa Neno la MUNGU. MUNGU hamlazimishi yeyote kuamini. Wanaweza kuchagua kutegemea Shuhuda ambayo Bwana amependezwa kutoa, au kutilia shaka na kuangamia. Ni uzima au kifo kwako wewe, Ndugu Hull. Tayari niliona wingu la malaika wabaya wanaokuzunguka, na wewe umebweteka ukiwa unaona mambo ni shwari kabisa. Shetani amekuwa

akikuambia hadithi ya kupendeza juu ya njia rahisi kuliko kuwa katika vita vya kila wakati na roho zinazopingana; lakini ukichagua hivyo, mwishowe utakuwa na ushuru mzito na wa kutisha kulipa. {1T 427.2}

Niliona kwamba unajihisi imara ndani yako, ulihisi kuwa una mabishano/hoja ambazo haziwezi kupingwa, na haukutegemea nguvu ya Bwana. Mara nyingi umekimbilia kwenye ardhi ya Shetani kukutana na mpinzani. Haukusubiri hadi ujue kwamba Ukweli au kusudi la MUNGU vinahitaji majadiliano, lakini umeshirikiana na wapinzani ambapo kwa kufikiria kidogo ungeamua kwamba Ukweli hauwezi kusonga mbele au kazi ya MUNGU kufaidika kwa kufanya hivi. Wakati wa thamani umetumika. {1T 428.1}

Shetani aliangalia na kushuhudia pigo zito ambalo Ndugu Hull alishughulikia kuhusiana na umizimu pale Battle Creek. Wafuasi wa umizimu walielewa taasisi yake na walihisi kwa uhakika kuwa haitakuwa bure kufanya bidii ya kumwondoa yule aliyejeruhi sana kusudi lao. Katika kujadili na washirika wa umizimu sio tu utakutana na mwanadamu na hoja zake, lakini Shetani na malaika zake. Na kamwe mtu mmoja hapaswi kutumwa peke yake kupigana vita na umizimu. Ikiwa kusudi la MUNGU linatuhitaji tukabiliane na Shetani na jeshi lake kama anavyowakilishwa na uchawi wa umizimu, ikiwa mengi yako hatarini vya kutosha kuwa na mjadala kama huo, basi watu kadhaa wanapaswa kwenda pamoja kwamba kwa maombi na imani, na jeshi la giza liweze kurudishwa nyuma na mzungumzaji alindwe na malaika ambao wana nguvu zaidi. {1T 428.2}

Ndugu Hull, ulioneshwa kwangu ukiwa chini ya ushawishi wa kutuliza wa kuvutia ambao utathibitika kuwa kifo, isipokuwa nguvu yake imevunjwa. Umebishana na Shetani, na kusemezana naye, na umeketi katika uwanja uliokatazwa, na umetumia akili yako katika mambo ambayo ni makubwa kwako, na kwa kuendekeza mashaka na kutokuamini umevutia malaika waovu karibu na wewe, na kukufukuza malaika safi na watakatifu wa MUNGU. Ikiwa ungepinga kwa uthabiti maoni ya Shetani na kutafuta nguvu kutoka kwa MUNGU kwa bidii, ungekuwa umevunja kila pingu, ukirudisha nyuma adui yako wa kiroho, umkaribie MUNGU, na ushinde kwa Jina Lake. Niliona kuwa ilikuwa dhana ya kiburi, imani bandia ndani yako kwenda nje kukutana na wanamizimu wakati wewe mwenyewe ulifunikwa na kushangazwa na mawingu ya kutokuamini. Ulienda kupigana na Shetani na jeshi lake bila silaha, na umejeruhiwa vibaya, na hauwezi kuhisi jeraha lako. Ninaogopa sana kwamba hata ngurumo na umeme wa Sinai vingeshindwa kukusogeza. Uko kwenye kiti rahisi cha Shetani na huoni hali yako ya kutisha na ujitahidi kutoroka. Usipoamka na kujiokoa kutoka kwenye mtego wa Shetani, lazima uangamie. Ndugu na dada wangekuokoa, lakini nikaona kuwa hawawezi. Una la kufanya; una juhudi kubwa ya kufanya, au umepotea. Niliona kwamba wale walio chini ya ushawishi wa uchawi wa umizimu hawajui. Umevutiwa, na kuvutwa na

kunaswa, lakini haujui, na kwa hivyo hafanyi bidii hata kidogo kuja kwenye nuru. {1T 428.3}

Niliona kwamba sasa tuko katika wakati wa kupepetwa. Shetani anafanya kazi kwa nguvu zake zote kupokonya nafsi kwa nguvu kutoka katika mkono wa Kristo na kuwafanya wamkanyage Mwana wa MUNGU. Malaika alirudia polepole na kwa msisitizo maneno haya: "Je! Unafikiri atadhaniwa kuwa anastahili adhabu kali kama nini, Yeye aliyemkanyaga Mwana wa MUNGU, na kuhesabu damu ya agano iliyotakaswa, kuwa si takatifu "Je! Amefanya dharau kwa Roho wa neema?" Tabia inakuzwa na kupaliliwa. Malaika wa MUNGU wanapima thamani ya maadili. MUNGU anajaribu na kuwathibitisha watu wake. Maneno haya yaliwasilishwa kwangu na malaika: "Angalieni, ndugu zangu, kusiwe na mtu yeyote miongoni mwenu mwenye moyo mbaya wa kutokuamini, kwa kujitenga na MUNGU aliye hai. Lakini tuhimizana kila siku, wakati iitwapo leo; isipokuwa mmoja wetu amefanywa mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. Kwa maana tumefanywa washiriki wa Kristo, ikiwa tunashikilia mwanzo wa ujasiri wetu thabiti hata mwisho." MUNGU hafurahii kwamba watu Wake wowote ambao wamejua nguvu ya neema Yake wazungumze mashaka yao, na kwa kufanya hivyo kutengeneza njia ya Shetani kupeleka maoni yake kwa akili zingine. Mbegu ya ukafiri na uovu hupandwa bila mizizi. Shetani huilisha kila saa, na inastawi na kuwa na nguvu. Mbegu nzuri iliyopandwa inahitaji kupewa lishe, kumwagiliwa, na kutunzwa kwa upole; kwa sababu kila ushawishi wenye sumu hutupwa juu yake kuzuia ukuaji wake na kusababisha ife. {1T 429.1}

Jitihada za Shetani zina nguvu zaidi sasa kuliko hapo awali, kwani anajua kuwa wakati wake wa kudanganya ni mfupi. Ndugu Hull, niliona umejijeruhi sana kwa kufunua udhaifu wako na kuwaambia mashaka yako wale ambao ni mawakala wa Shetani.Umedanganywa na maneno laini na hotuba za kupendeza, na umejidhihirisha kwa njia ya uzembe zaidi kwa mashambulio ya Shetani. Je! Unawezaje kujidhuru hivi na kisha kulaumu Neno la MUNGU ? Umekimbilia hovyo kwenye uwanja wa vita wa Shetani, na haishangazi kwamba akili yako ni ya kijinga na isiyo na hisia. Tayari Shetani kupitia mawakala wake ametia sumu katika mazingira unayopumua; tayari malaika wabaya wamewasiliana kwa simu na mawakala wake duniani kwa habari ya mwendo utakaofuatwa kwako. Na huyu ndiye aliyeitwa na MUNGU kusimama kati ya walio hai na wafu; huyu ni mmoja wa walinzi waliosimama juu ya kuta za Sayuni kuwaambia watu wakati wa usiku. Jukumu zito liko juu yako. Ukishuka, hautaenda peke yako; kwani Shetani atakupa ajira kama wakala wake wa kuongoza roho kwa kifo. {1T 430.1}

Niliona kwamba malaika wa MUNGU walikuwa wakikutazama kwa huzuni. Walikuwa wameacha upande wako na walikuwa wakigeuka kwa huzuni, wakati Shetani na malaika zake walikuwa wakicheka kwa kufurahi juu yako. Ikiwa ungekuwa ukipambana na mashaka yako na usingehimiza Shetani kukujaribu, kwa kusema kutokuamini kwako na kupenda kukaa juu yake, usingevutia

malaika walioanguka kukuzunguka kwa idadi kama hiyo. Lakini ulichagua kuongea giza lako; ulichagua kukaa juu yake; na unapozungumza zaidi na kukaa juu yake, ndivyo unakua mweusi na gizani. Unazima kutoka kwako kila mwanga wa nuru ya mbinguni; na korongo kubwa linakuja kati yako na wale tu ambao wanaweza kukusaidia. Ukiendelea kwa njia ambayo umeanza, shida na ole ziko mbele yako. Mkono wa MUNGU utakukamata kwa njia ambayo haitakufaa. Hasira yake haitasinzia. Lakini sasa Yeye anakualika. Sasa, sasa hivi, Yeye Anakuita urudi Kwake bila kuchelewa, na kwa rehema atasamehe na kuponya kurudi nyuma kwako. MUNGU anaongoza watu ambao ni wa kipekee. Yeye Atawasafisha na kuwatakasa, na atawastahilisha kuwa tayari kutwaliwa kwenda mbinguni. Kila kitu cha mwili kitatengwa na hazina za kipekee za MUNGU mpaka zitakuwa kama dhahabu iliyosafishwa mara saba. {1T 430.2}

Niliona kuwa huo ulikuwa msimamo wa kikatili kwa Ndugu A na B kuwa ndani, kutumikia makusudi ya Shetani kwa kuziacha akili zao zikimbie kwa kiwango ambacho angewaongoza katika njia ya kutokuamini. Dhambi yao kubwa ilikuwa ni kuzungumza mashaka haya ya giza, kutokuamini huku kwa usiku wa manane, na kuvuta akili zingine kwenye mkondo ule ule wa giza. {1T 431.1}

Watu wa MUNGU watapepetwa, kama vile nafaka inavyopepetwa kwenye ungo, mpaka makapi yote yatenganishwe na punje safi za nafaka. Tunapaswa kumwangalia Kristo kwa mfano na kuiga mfano wa vipengele vya unyenyekevu. Haujisikii kupatanishwa na nidhamu unayohitaji na haufanyi mazoezi ya kujinyima ambayo Kristo anahitaji kwa wale ambao kweli ni warithi wa wokovu. Wale wanaojishughulisha na kazi ya kuokoa roho ni watendakazi pamoja na Kristo. Kazi Yake ilikuwa ni ya ukarimu usiokuwa na maslahi Yake binafsi na kujitolea kila wakati. Wale ambao ambao kafara kubwa imetolewa kwa ajili yao ili waweze kuwa washiriki wa neema Yake ya mbinguni wanapaswa kujitolea kwa kujinyima na kujikana nafsi na kusaidia katika kazi kubwa ya kuwaleta wengine katika ujuzi wa Ukweli. Masilahi binafsi yanapaswa kuwekwa kando; tamaa za ubinafsi na kujifariji haipaswi sasa kusimama katika njia ya kazi ya MUNGU katika kuokoa roho. Wahudumu wa MUNGU wanafanya kazi badala ya Kristo; hao ni mabalozi Wake. Hawapaswi kujifunza urahisi wa mambo kwao, burudani, shauku, kuridhika na maisha ya raha zao wenyewe. Lazima wateseke kwa ajili ya Kristo, wasulubiwe pamoja Naye, na kufurahi kwamba wanaweza kwa kila hali ya neno kujua ushirika wa mateso ya Kristo. {1T 431.2}

Niliona kwamba wahudumu wanaofanya kazi kwa maneno na mafundisho wana kazi kubwa mbele yao; jukumu zito liko juu yao. Katika kazi yao hawafiki karibu na mioyo. Kazi yao ni ya jumla sana, na mara nyingi hutawanyika sana. Kazi yao inapaswa kujieelekeza zaidi kwa wale ambao wanawahudumia. Wakati wanahubiri kutoka kwenye kibweta, ndiyo tu wanaanza tu kazi yao. Lazima basi waishi mahubiri yao, kila wakati wakijilinda, ili wasilete lawama kwa kazi ya MUNGU. Wanapaswa kuonesha kwa mfano maisha ya Kristo. 1 Wakorintho 3:9:

"Kwa maana sisi tu watenda kazi pamoja na MUNGU." 2 Wakorintho 6:1: "Basi sisi, tukiwa watendakazi pamoja Naye, tunawasihi pia msipokee neema ya MUNGU bure." Kazi ya mchungaji haimaliziki wakati anapotoka kwenye kibweta. Haipaswi yeye kutupa mzigo na kuijaza akili yake kwa kusoma au kuandika isipokuwa kama ni muhimu sana. Anapaswa kufuatilia kazi zake za umma kwa juhudi za kibinafsi, akifanya kazi binafsi kwa ajili ya roho wakati wowote nafasi inapojitokeza akiongea karibu na kando ya moto wakati wa baridi, akiomba na kusihi kwa Jina la Kristo kwa roho kupatanishwa na MUNGU. Kazi yetu hapa inakaribia kufungwa, "na kila mtu atapata thawabu yake mwenyewe kulingana na kazi yake." {1T 432.1}

Nilioneshwa tuzo ya watakatifu, urithi wa uzima wa milele. Kisha nilioneshwa ni kwa kiasi gani jinsi watu wa MUNGU walivyostahimili kwa ajili ya kuutetea Ukweli, na kwamba wangehesabu mbingu kuwa rahisi vya kutosha kuingia. Walidhani kwamba mateso ya wakati huu wa sasa hayakustahili kulinganishwa na utukufu ambao unapaswa kufunuliwa ndani yao. Watu wa MUNGU katika siku hizi za mwisho watajaribiwa. Lakini hivi karibuni jaribio lao la mwisho litakuja, na kisha watapokea zawadi ya uzima wa milele. {1T 432.2}

Ndugu Hull, umeteswa na lawama kwa sababu ya kuutetea Ukweli. Umehisi nguvu yaUukweli na ya maisha yasiyo na mwisho. Umeshuhudiwa na ROHO WA MUNGU na wako kwamba umemilikiwa na kukubaliwa Nae. Niliona kwamba ikiwa utajifunga tena silaha, na ukasimama kwenye lindo lako, ukimpinga Shetani na ukipigana kiume vita vya Bwana, hakika utashinda, na hivi karibuni utavua silaha zako na kuvaa taji ya mshindi. Ah, urithi hauna utajiri wa kutosha? Je! Haikugharimu gharama kubwa, uchungu na damu ya Mwana wa MUNGU ? Ninakuita kwa Jina la Bwana kuamka. Jingatue katika udanganyifu mbaya ambao Shetani ametupa juu yako. Shika uzima wa milele. Mpinge shetani. Malaika wabaya wako karibu nawe, wakinong'oneza masikioni mwako, wakikutembelea na ndoto za uongo, na unawasikiliza na unafurahishwa. Ah, kwa ajili ya Kristo, kwa ajili ya nafsi yako mwenyewe, ondoa mbali ushawishi huu mbaya kabla ya kumhuzunisha ROHO WA MUNGU na kisha atoke kutoka kwako. {1T 432.3}

Sabato, Juni 6, 1863, nilioneshwa mambo kadhaa kuhusu kazi ya MUNGU na kuenezwa kwa Ukweli. Wahubiri na watu wana imani ndogo mno, kujitolea kidogo na utauwa wa Kweli. Watu humwiga mhubiri, na kwa hivyo ana ushawishi mkubwa juu yao. Ndugu Hull, MUNGU anataka ukaribie Kwake, ambapo unaweza kupata nguvu Zake, na kwa imani hai kudai wokovu Wake, na uwe mtu hodari na mwenye nguvu. Ikiwa ungekuwa mtu wa kujitoa wakfu, mcha MUNGU, kwenye mimbari na nje, ushawishi mkubwa ungehudhuria mahubiri yako. Hauchunguzi moyo wako kwa karibu. Umejifunza kazi nyingi ili kufanya hotuba zako ziwe kamili, zenye uwezo, na za kupendeza; lakini umepuuza utafiti mkubwa na wa lazima zaidi, somo la kujichunguza mwenyewe. Ujuzi kamili wa wewe mwenyewe, kutafakari na sala, umekuja

kama vitu vya pili. Kufanikiwa kwako kama mchungaji kunategemea kutunza moyo wako mwenyewe. Utapokea nguvu zaidi kwa kutumia saa moja kila siku katika kutafakari, na kwa kuomboleza juu ya kasoro zako, kushindwa na uharibifu wa moyo na kuomba msamaha wa MUNGU upendo na uhakikisho wa dhambi zilizosamehewa, kuliko vile ungefanya ambavyo ungefanya kwa kutumia masaa na siku nyingi kusoma waandishi wenye uwezo zaidi, na kufanya ujue na kila pingamizi kwa imani yetu, na ushahidi wenye nguvu zaidi kwa niaba yake. {1T 433.1}

Sababu ya kwanini wahubiri wetu hutimiza kidogo sana ni kwamba hawatembei na MUNGU. Yeye ni safari ya siku kutoka kwa wengi wao. Kadiri unavyoangalia kwa karibu moyo wako mwenyewe, ndivyo utakavyokuwa macho na kulindwa zaidi, usije kwa maneno yako au matendo yako usije ukaudharau Ukweli, kutoa nafasi kwa ulimi wa kashfa kukufuata wewe na Ukweli, na kusababisha roho kupotea kupitia kupuuza kwako kujifanyia tathimini ya kujisoma moyo, na utauwa muhimu. Msimamo mtakatifu wa mhudumu wa Kristo unapaswa kuwa kukemea wafuasi batili na wapuuzi ambao wanakiri kwa mdomo tu. Mihimili ya Ukweli na utakatifu inayoangaza kutoka kwa mazungumzo yako mazito, ya mbinguni yatasadikisha wengine na kuwaongoza kwenye Ukweli, na wale walio karibu nawe watalazimika kusema, MUNGU Yuko pamoja na mtu huyu, wa Ukweli. Ni uzembe na kulegea kwa wale wanaojiita wahudumu wa Kristo ndiko kunakowapa ushawishi mdogo sana. Kuna wafuasi wengi wanaokiri kwa mdomo, lakini kuna watu wachache wanaoomba. Ikiwa wahubiri wetu wangekuwa wanaume ambao waliomba zaidi kwa siri, ambao walibeba mahubiri yao kwa vitendo katika familia zao, ambao wanatawala nyumba zao kwa hadhi na mvuto, nuru yao ingewaangazia wale walio karibu nao. {1T 434.1}

Ndugu Hull, nimeoneshwa kuwa ikiwa utajiweka wakfu kwa MUNGU, kufanya ushirika Nae, kutafakari sana, kuwa macho na kushindwa kwako, uomboleze na kuugulia mbele za Bwana kwa unyenyekevu wa hali ya juu kwa sababu yao, ukimtegemea Yeye kupata nguvu, ungekuwa katika biashara yenye faida zaidi ambayo umewahi kuishiriki; kwani ungekuwa unakunywa kwenye chemchemi iliyo hai, na kisha ungeweza kuwapa wengine kunywa kutoka kwenye chemchemi hiyo hiyo ambayo ilikuhuisha na kukuimarisha. {1T 434.2}

Ndugu mpendwa, isipokuwa kuna mabadiliko katika tabia yako ya Kikristo, utashindwa kupata uzima wa milele; kwa kuwa adui yetu mwenye shughuli ataweka mitego yake kwa miguu yako, na ikiwa hauko karibu na MUNGU, utaanguka kwenye wavu. Unajisikia kutotulia na kukosa raha, na kusoma ni kipengele chako; lakini wakati mwingine unashindwa katika somo. Wakati unapaswa kusoma moyo wako mwenyewe, unajishughulisha katika kusoma vitabu. Wakati kwa imani unapaswa kuwa karibu na Kristo, unasoma vitabu. Niliona kuwa masomo yako yote hayatakuwa na faida isipokuwa umejisoma mwenyewe kwa uaminifu. Hauijitambui, na akili yako inakaa lakini kidogo juu ya MUNGU. Unajiamini, na unapita bila kujua kwamba lazima uifie nafsi ili

kuwa mhudumu aliyefanikiwa wa Kristo. Unakosa kiasi, umakini na mvuto nje ya mimbari. Vitu hivi vinakabiliana na kazi yako ya mimbari. {1T 434.3}

Tangu suala lako ilipowasilishwa kwangu kwa maono, nimeona mapungufu kwako. Akili yako haijainuliwa. Unasimama kwenye dawati na unashughulikia Kweli takatifu sana, na nyeti zinazoinua kwa njia yenye uwezo; lakini unaposhughulikia masomo mazito, mara nyingi unaleta kitu cha kuchekesha ili kuunda tabasamu, na hii mara nyingi huharibu nguvu ya hotuba yako yote. Unashughulikia Kweli nzito kwa urahisi, lakini hauziishi, na ndio sababu kibali cha mbinguni kinakosekana. Wengi ambao umependeza masikio yao watazungumza juu ya hotuba mahiri/smart, mhubiri hodari na mwenye uwezo, lakini hawavutiwi tena na umuhimu wa kutii Ukweli kuliko kabla ya kukusikiliza. Wanaendelea kuvunja sheria ya MUNGU kama zamani. Ni mchungaji aliyewapendeza, sio Ukweli alioutamka. Unabaki katika umbali mkubwa sana kutoka kwa MUNGU kisa kwamba nguvu Zake haziuwekei Ukweli masikani. Unapaswa kuishi dini nyumbani, na ingekuwa na ushawishi kuinua familia yako, kumuinua mke wako. Unapokuwa nyumbani unatupa kizuizi na kutenda kama mvulana; uzito wa Ukweli na mzigo wa kazi hauko juu yako. Wewe sio chaguo la maneno yako au mfano wako. {1T 435.1}

Usalama wako pekee ni katika kujisoma mwenyewe, udhaifu wako na kushindwa. Usiache kujilinda. Jiangalie kwa karibu zaidi ukiwa nyumbani. Jiangalie wakati uko mbali na nyumbani. Unapuuza majukumu yako ya chumbani/faragha, unavua silaha zako, na unatoa roho ya uzembe ambayo huwafukuza malaika kutoka kwako na kutoka kwa familia yako. Usipuuze kuuchunguza moyo wako mwenyewe uwapo nyumbani. Usifuje mapenzi yako yote juu ya familia yako. Hifadhi mapenzi bora ya moyo wako na uyatoe kwa Yesu, ambaye amekukomboa kwa damu Yake. Unapokuwa nyumbani, jiandae kufaa kila wakati katika biashara ya Bwana wako wakati utakapokuwa mbali na nyumbani. Ukifanya hivyo, utakuwa na silaha kila wakati. Shauku kuu ya nafsi yako itakuwa kumtukuza MUNGU, kufanya mapenzi Yake duniani, na utakuwa na ujasiri mzuri na kumtumaini. Hautahisi kuhangaika sana, lakini utakuwa na mada ya kudumu ya kutafakari, kujitoa wakfu, na utakatifu. Nilirejelewa 1 Wakorintho 9:27: "Lakini ninauweka mwili wangu chini, na kuuweka chini ya mamlaka: isije kwamba kwa njia yoyote, nikiwa nimewahubiria wengine, mimi mwenyewe ningekuwa mtu wa kukataliwa." Una kazi ya kufanya ili kujielewa mwenyewe. Usibembelezwe, na kudanganywa na maneno ambayo ndugu wasio na busara na wapumbavu wanaweza kutoa juu ya juhudi zako. Ikiwa wanasifu mahubiri yako, usiache hilo likufurahishe. Baraka ya MUNGU ikihudhuria kazi yako, matunda yataonekana. Mahubiri yako hayatapendeza tu, lakini yatakusanya roho. {1T 435.2}

Ndugu Hull, lazima ulindwe kila upande. Niliona kuwa chochote kinachogawanya mapenzi, au kinachoondoa moyoni upendo mkuu kwa MUNGU, au huzuia ujasiri usio na kikomo na imani kamili Kwake, huchukua tabia na

kuchukua sura ya sanamu/mungu. Nilioneshwa kwa amri kuu ya kwanza: "Mpende Bwana MUNGU wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote." Haturuhusiwi kutenganishwa kwa mapenzi yetu na MUNGU. Hakuna cha kugawanya upendo wetu mkuu Kwake au furaha yetu Kwake. Mapenzi yako, matakwa yako, mipango yako, matakwa yako, na raha lazima zote ziwe chini ya utii. Una kitu cha kujifunza, kumtukuza Bwana MUNGU moyoni mwako, katika mazungumzo yako, katika matendo yako yote; na ndipo Yesu anaweza kukufundisha, na kukusaidia kukufundisha unapotupa wavu wako upande wa kulia wa meli, kuileta ufukoni iliyojaa samaki. Lakini bila msaada wa Kristo katika kutupa wavu wako, unaweza kusumbuka kwa wiki, miezi, na miaka bila kuona matunda mengi ya kazi yako. {1T 436.1}

Niliona kwamba utajaribiwa kuhisi kwamba ndugu zako wanataka kukupima, kwamba wanataka kukuzuia sana. Lakini ndugu zako wanataka tu uishi kulingana na maagizo ya Neno la MUNGU, na MUNGU anapenda kukufikisha hapo, na malaika wanakuangalia kwa umakini kabisa. Lazima uyalinganishe maisha yako na Neno la MUNGU, ili uweze kubarikiwa na kutiwa nguvu na Yeye, la sivyo utaanguka njiani, na wakati unahubiria wengine, wewe mwenyewe utakuwa mtu wa kukataliwa. Lakini unaweza kuwa mshindi, na unaweza kujipatia uzima wa milele. Utajiponya kutoka kwenye mtego wa Shetani, lakini yeye anakuandalia mitego mingine. MUNGU atakusaidia na kukutia nguvu ikiwa utamtafuta kwa bidii. Lakini jifunze mwenyewe. Jaribu kila nia; isiwe lengo lako kuhubiri hotuba nzuri na mahiri ili kumuonesha Moses Hull, lakini tafuta kumwonesha na kumwinua Kristo. Rahisisha Ukweli kwa wasikiaji wako ili akili ndogo ziweze kuelewa. Fanya hotuba zako ziwe wazi, zilizoelekezwa, adhimu na za utulivu. Walete watu kwenye uamuzi. Wafanye waisikie nguvu muhimu ya ukweli. Mtu yeyote akisema neno moja la kukusifu na kutia chumvi, mkemee vikali. Waambie kwamba Shetani amekusumbua na hilo kwa muda, na hawahitaji kumsaidia katika kazi yake. {1T 437.1}

Unapokuwa kati ya akina dada, jitunze kwa kujistahi ukiweka mstari katika mahusiano kwa kujitenga. Haijalishi ikiwa wanafikiria unakosa uungwana au adabu njema. Ikiwa akina dada, wameolewa au hawajaolewa, wanaonesha mazoea yoyote nawe, wapinge kwa mwenendo wao. Uwe mwazi na mwenye maamuzi hata kama unashtukiza na kutenda papo hapo katika kesi hiyo, ili wapate kuelewa kuwa hauukenulii meno udhaifu kama huo. Wakati unapokuwa mbele ya vijana wakati wowote, usijichekeshe-chekeshe, kuwa makini, na jiweke wakfu. Niliona kwamba ikiwa Ndugu Loughborough na wewe mwenyewe mnamfanya MUNGU kuwa nguvu zenu, kazi kubwa itakamilishwa na wewe kwa watu wake masikini, kwani wawili wanaweza kuwa jeshi. Karibianeni, ombeni pamoja na kila mmoja pekee, kuweni huru kwa kila mmoja. Ndugu Hull anapaswa kumfanya Ndugu Loughborough kuwa msiri wako, na asikilize maamuzi na ushauri wake. {1T 437.2}

# SURA YA 80

# WACHUNGAJI WASIOTAKASWA.

Wachungaji wanaohubiri ujumbe wa tatu, wanapaswa kufanya kazi kwa sababu wanahisi kwamba MUNGU amewawekea mzigo wa kazi. Wachungaji wetu wamewekwa juu ya uhitaji, ikiwa tu watajizoeza kwa kiwango fulani kuwa wachumi (hekima ya kubana matumizi, kazi na maisha rahisi). Ikiwa wanapungukiwa, watakuwa katika uhitaji katika nafasi yoyote ambayo wanaweza kuwekwa. Hebu wape nafasi nzuri zaidi na wangetumia kila fedha/rasilimali wanayopokea. Hii imekuwa changamoto ya Mzee Hull. Watu kama hawa wanahitaji mfuko ambao hauwezi kumalizika wanapochota kutoka humo, ili kuridhika. {1T 438.1}

Wale wanaoshindwa kusimamia kwa busara katika masuala ya muda mfupi ya kidunia, kwa ujumla wana upungufu hata wa mambo/vitu vya kiroho. Wanashindwa kujenga kanisa. Wanaweza kuwa na talanta za asili na kuitwa wahubiri wenye mahiri (smart preachers), na bado hawana maadili. Wanaweza kuteka makusanyiko makubwa na kuongeza msisimko mkubwa; lakini matunda yanapotafutwa, hupatikana kidogo sana, ikiwa yapo. Wanaume kama hao mara nyingi huwa juu ya kazi na kupoteza upendo wao kwa usahili na unyenyekevu wa injili. Hawatakaswi kupitia Kweli wanazohubiri. Hii imekuwa changamoto ya Mzee Hull. Amekosa neema hiyo ambayo huimarisha roho na kuinua, kuboresha na kukuza tabia ya mtu. Ni jambo jema kwamba moyo uimarishwe na neema. Huu ndio msingi wa uthabiti wetu-kuwa na uendelevu bila kuzimika. {1T 438.2}

Katika mahali ambapo Mzee Hull ametoa masomo ya mihadhara, watu wamefurahishwa na uburudishaji wake na mtindo wake wa kipekee wa kuhubiri (anajua kuchezea maneno kwa uhodari mpaka yananoga na kuweka futuhi-witticism), lakini ni watu wachache tu ambao wamekubali Ukweli kama matokeo ya kazi yake; na hata idadi ya hawa wachache huikana tena imani baada ya muda mfupi. Wengi wamesikataishwa tamaa kwamba kulikuwa na matunda kidogo sana yaliyopatikana baada ya kazi yake. Nilioneshwa sababu. Unyenyekevu, wema, usahili, usafi, na utakatifu wa maisha vilikosekana. Amefikiria kuwa kazi yake mahiri ilikuwa ya thamani sana, na kwamba kusudi la kazi hiyo ya Mungu isingekuwepo endapo angeondolewa; laiti angalijua wasiwasi ambao wafanyakazi wa kweli katika hiyo kazi, ambao wamejaribu kumsaidia, wameteseka na kusumbuka kwa sababu yake, asingekuwa na makadirio la juu sana la kazi yake mwenyewe. Mwenendo wake katika kusudi la

kazi ya Mungu umeendelea kuwa mzigo, na bila shaka kazi ingefanikiwa vizuri bila ya ushawishi wake. Fadhaa ya ndugu zake kumuokoa ili asianguke imewapelekea kujitoa kumfanyia mengi yaliyohitaji fedha. Wamefurahishwa na talanta yake ya kuhubiri, na wengine wamekuwa wasio na busara hata kumsifu na kuonesha upendeleo kwake kuliko ndugu wengine wahubiri ambao ushawishi wao unajieleza kwa ajili ya maendeleo ya utume mahali popote. Hii imemdhuru. Hakuwa na unyenyekevu wa kutosha au neema ya kutosha ya MUNGU kusimama dhidi ya sifa zilizotiwa chumvi za ndugu zake. MUNGU awasaidie hawa ndugu kuhisi juu ya makosa yao na kujiepusha na hatia ya kumdhuru huyu mtumishi kijana kwa kumdanganya, kumpaka mafuta kwa chupa ya mgongo. {1T 438.3}

Wote wanaotamani kujiondoa kutoka kwa watu wa MUNGU wa masaliaili kufuata mioyo yao iliyoharibika wanakuwa wamejidondosha mikononi mwa Shetani kwa hiari yao, nao wana fursa ya kufanya hivyo. Kuna wengine kati yetu ambao wako katika hatari. Wana maoni yaliyoinuliwa juu ya uwezo wao wenyewe, wakati ushawishi wao katika mambo mengi umekuwa bora kidogo kuliko ule wa Mzee Hull. Isipokuwa tu wamefanya matengenezo kamili, kazi ya utume itakuwa bora pasipo wao. Wachungaji wasiotakaswa hujeruhi kazi na kuwa mzigo kwa ndugu zao. Anahitajika mtu wa kufuatilia baada yao ili ayarekebishe makosa yao na kunyoosha mambo na kuwaimarisha wale ambao wamedhoofishwa na kuraruliwa-raruliwa kupitia ushawishi wao. Wana wivu kwa wale ambao wamebeba mizigo katika kazi, wale ambao wangejitolea hata maisha yao endapo ingelazimu ili kusimamia na kuiendeleza Kweli. Wanawahukumu ndugu zao kuwa hawana hamasa ya juu kuliko walivyokuwa nayo wao. Kufanya mengi kwa wahudumu ambao wako chini ya vishawishi vya Shetani huwaumiza, na ni upotevu wa mali. Inawapa ushawishi, na kuwaweka mahali ambapo wanaweza kuwadhuru ndugu zao na kazi ya MUNGU kwa undani/kina zaidi. {1T 439.1}

Nimeoneshwa kuwa mashaka yatolewayo kuhusu Ukweli wa msimamo wetu na msukumo wa Neno la MUNGU hayasababishwi kama vile wengi wanavyodhania. Ugumu huu si sana matokeo ya Biblia au uthibitisho wa imani yetu kama ilivyo mioyo yao. Mahitaji ya Neno la MUNGU yako karibu sana kwa ajili ya asili yao isiyotakaswa. "Matamanio ya mwili ni uadui dhidi ya MUNGU; kwa maana hayaiitii sheria ya MUNGU, wala hayawezi kuitii." Ikiwa hisia za moyo wa asili hazizuiliwi na kuletwa chini ya ushawishi wa utakaso wa neema ya MUNGU iliyopokelewa kupitia njia ya imani, mawazo ya moyo sio safi na takatifu. Masharti ya wokovu yaliyooneshwa katika Neno la MUNGU ni ya busara, wazi, na mazuri, chanya, mithili ya mapenzi ya MUNGU na usafi wa moyo na maisha. Lazima tujisulubishe nafsi zetu na tamaa zake. Lazima tujitakase na uchafu wote wa mwili na roho, tukikamilisha utakatifu katika kumcha MUNGU. {1T 440.1}

Karibu katika kila kisa ambapo watu hukosa utulivu juu ya uvuvio wa Neno la MUNGU, ni kwa sababu ya maisha yao yasiyotakaswa, ambayo Neno hilo linalaani. Hawatapokea karipio na vitisho vyake kwa sababu linagusa mwenendo wao mbaya. Hawawapendi wale ambao wageongoka na kuwazuia. Shida na mashaka yanayotatiza moyo yataondolewa mbele ya yule anayezitii na kuzifuata kanuni safi za Ukweli. {1T 440.2}

Wengi wana talanta ambazo zingetimiza mema mengi ikiwa zitatakaswa na kutumiwa kwa ajili ya Kristo, au kutimiza mabaya mengi ikiwa zitatumiwa katika huduma ya wale wasioamini na Shetani. Kuridhisha  ubinafsi na tamaa zake anuwai zitapotosha talanta na kuzifanya kuwa laana badala ya baraka. Shetani, mdanganyifu mkuu, ana talanta nzuri. Wakati mmoja alikuwa malaika aliyeinuliwa, karibu na Kristo. Alianguka kwa kujiinua mwenyewe, na akaunda uasi mbinguni, na kusababisha wengi kuanguka pamoja naye. Halafu talanta na ustadi wake vilitumika dhidi ya serikali ya MUNGU, ili kusababisha wale wote alioweza kuwalaghai kudharau mamlaka ya mbinguni. Wale wanaovutiwa na ukuu wake wa kishetani wanaweza kuchagua kumuiga jenerali huyu aliyeanguka na kushiriki naye hatima yake mwishowe. {1T 440.3}

Usafi wa maisha hutoa uboreshaji, ambao utasababisha wale walio nao kuogopa zaidi na zaidi kujiingiza na kuendekeza katika tamaa ya dhambi. Hao hawataongozwa mbali na Ukweli au kuachwa wakiwa na shaka juu ya uvuvio wa Neno la MUNGU. Badala yake, watajihusisha na somo la kila siku la Neno takatifu na hamu inayozidi kuongezeka, na ushahidi wa Ukristo na msukumo utaweka alama yao kwenye akili na mtindo wa maisha. Wale wanaopenda dhambi wataiacha Biblia, watapenda kutilia shaka, na watakuwa wazembe kwa kanuni. Watapokea na kutetea nadharia za uongo. Hao watahesabu dhambi za mwanadamu kulingana na hali yake, na anapotenda dhambi kubwa humfanya kuwa mtu astahiliye huruma badala ya kumtazama kama mhalifu astahiliye adhabu. Hii mara zote itaufaa moyo uliopotoka, ambao kwa wakati utaendeleza kanuni za asili iliyoanguka. Kwa mchakato fulani wa jumla, watu hukomesha dhambi mara moja ili kuepusha hitaji lisilo la kufurahisha la matengenezo ya mtu binafsi. Ili kujikomboa mwenyewe kutoka kwenye wajibu wa juhudi za sasa, wengi wako tayari kutangaza kazi yoyote na bidii ya maisha yao wakati wakifuata kanuni takatifu za Neno la MUNGU. Umuhimu wa kifalsafa wa Mzee Hull una ngome yake katika uharibifu wa moyo. MUNGU anainua watu ili waende kufanya kazi katika shamba la mavuno, na ikiwa ni wanyenyekevu, wenye kujitolea, na wacha MUNGU, watazitwaa taji ambazo wahudumu hao hupoteza ambao kuhusina na imani, wao ni waovu na wamekataliwa. {1T 441.1}

Novemba 5, 1862, nilioneshwa kuwa baadhi ya watu hukosea wito wao. Wanafikiri kwamba ikiwa mtu hawezi kufanya kazi kwa mikono yake, au ikiwa hana mtazamo wa kibiashara, ataweza kuwa mchungaji. Wengi hufanya makosa makubwa hapa. Mtu ambaye hana mbinu za kibiashara anaweza kuwa mchunaji, lakini atakosa sifa ambazo kila mchungaji anapaswa kuwa nazo ili

kulihudumia kanisa kwa busara na kulitegemeza kusudi la Mungu. Lakini wakati mchungaji anapokuwa bora kwenye mimbari, na, kama Mzee Hull, akashindwa katika usimamizi, basi hapaswi kwenda peke yake. Mwingine anapaswa kwenda naye kujaza mapungufu yake na kufanya usimamizi badala yake. Japo hili laweza kuwa la kufedhehesha, atapaswa kuzingatia maamuzi na ushauri wa mshirika mwenzake, kama vile kipofu amfuatavyo yule mwenye kuona. Kwa kufanya hivyo ataepuka hatari nyingi ambazo zinaweza kumdhuru endapo ataachwa peke yake. {1T 441.2}

Ustawi wa kazi ya MUNGU unategemea sana wachungaji wanaofanya kazi katika uwanja wa injili. Wale wanaofundisha Ukweli wanapaswa kuwa watu wa kujitolea, wacha MUNGU ambao wanaelewa jukumu lao na wakitenda mema kwa sababu wanajua kwamba MUNGU amewaita katika kazi, wanaume ambao wanatambua thamani ya roho wakitimiza wajibu na majukumu yao. Mtendakazi muadilifu hujulikana kwa ukamilifu wa kazi yake. {1T 442.1}

Kuna wahubiri wachache tu kati yetu. Na kwa sababu kazi ya MUNGU ilionekana kuwa na uhitaji sana, wengi wamekuwa na fikra kwamba karibu kila mtu anayedai kuwa mchungaji atakubalika. Wengine walifikiri kwamba kwa sababu watu wangeweza kuomba na kuhimiza na kuwatia moyo watu kwa kiwango fulani cha uhuru katika mkutano, walistahili kuendelea kuwa watendakazi. Na kabla hawajathibitishwa, au kuonesha matunda bora ya kazi zao, watu ambao MUNGU hakuwatuma wametiwa moyo na kupongezwa na ndugu wengine waliokosa uzoefu. Lakini kazi yao inaonesha mwenendo wa mtendakazi. Wanatawanya na kuchanganya watu, ila hawakusanyi na kuimarisha. Wachache wanaweza kuupokea Ukweli kama matunda ya kazi zao, lakini kwa ujumla hawainuki juu kiroho kuliko wale ambao walijifunza Ukweli kutoka kwao. Udhaifu huo huo ambao ulidhihirika katika kazi yao wenyewe unaonekana pia kwa waongofu wao. {1T 442.2}

Kufanikiwa kwa kazi hii hakutegemei uwepo wa idadi kubwa ya wahudumu, lakini ni jambo la muhimu zaidi kwamba wale wanaofanya kazi kuhusiana na kusudi la MUNGU wawe watu ambao wanahisi mzigo na utakatifu wa kazi ambayo wameitiwa. Watu wachache wenye kujitolea na kumcha MUNGU, wadogo kwa makadirio yao wenyewe, wanaweza kufanya vema kwa kiwango cha juu zaidi kuliko idadi kubwa ikiwa sehemu ya hawa hawana sifa au stahiki za kazi hiyo, ila wanajiamini na kujivunia talanta zao. Idadi ya hawa katika uwanja wa utume, ambao wangeweza kujaza wito fulani nyumbani, ingefanya kuwa muhimu kwamba karibu wakati wote wa wahudumu waaminifu kutumiwa kuwafuatilia ili kurekebisha ushawishi wao mbaya. Manufaa ya siku za usoni ya wahubiri wachanga hutegemea sana juu ya njia ambayo wanaingia katika huduma. Ndugu walio na kusudi la MUNGU moyoni wanahangaika sana kuona uUweli ukisonga mbele kwamba wako katika hatari ya kufanya mengi kwa wahudumu ambao hawajathibitishwa, kwa kuwasaidia kwa ukarimu kwa mali na kuwapa ushawishi. Wale wanaoingia kwenye uwanja wa injili wanapaswa

kuachwa ili kujipatia stahiki.sifa wenyewe, hata ikiwa ni lazima kupitia majaribio na shida. Kwanza wanapaswa kutoa uthibitisho kamili wa huduma yao. {1T 442.3}

Ndugu wenye uzoefu wanapaswa kulindwa; na badala ya kutarajia wahubiri hawa wachanga kuwasaidia na kuwaongoza, wanapaswa kuhisi jukumu juu yao kuwasimamia wahubiri hawa wachanga, kuwafundisha, kuwashauri, na kuwaongoza, kuwa na utunzaji wa baba kwao. Wachungaji wachanga wanapaswa kuwa na mfumo, kusudi thabiti, na nia ya kufanya kazi, ili wasile mkate wa mtu bure. Hawapaswi kwenda kutoka mahali hadi mahali, na kuanzisha mambo kadhaa ya imani yetu yaliyohesabiwa kuchochea ubaguzi, na kuondoka kabla ya ushahidi wa Ukweli wa sasa haujawasilishwa hata nusu. Vijana wa kiume ambao wanafikiria kuwa wana jukumu la kufanya kuhusiana na kazi hiyo hawapaswi kuchukua jukumu la kufundisha Ukweli mpaka watakapopata fursa ya kuwa chini ya ushawishi wa mhubiri mwenye uzoefu ambaye ana utaratibu katika kazi yake; wanapaswa kujifunza juu yake kama mwanafunzi shuleni angejifunza kutoka kwa mwalimu wake. Haipaswi kwenda huku na huko, bila kitu dhahiri au mipango iliyopevuka ya kutekeleza katika huduma. {1T 443.1}

Baadhi ambao wana uzoefu mdogo, na vigezo vichache vya kufundisha Ukweli, ndio wa mwisho kuuliza ushauri kwa ndugu zao wenye uzoefu. Wanavaa uchungaji na kujiweka sawa na wale walio na uzoefu mrefu na uliojaribiwa, na hawaridhiki isipokuwa wataweza kuongoza, wakififikiri kwamba kwa sababu wao ni wachungaji wanajua yote ambayo ni muhimu kujua. Wahubiri kama hao hakika hawana ujuzi wa kweli kuhusu wao wenyewe. Hawana sifa ya kuwa waungwana na wanyenyekevu na wana maoni ya juu sana juu ya uwezo wao wenyewe. Wachungaji wenye uzoefu, ambao hutambua utakatifu wa kazi hiyo, na kuhisi uzito wa kusudi hilo juu yao, wana wivu kuhusu wao wenyewe. Wanaona kuwa ni upendeleo kushauriana na ndugu zao na hawakasiriki ikiwa maboresho yanapendekezwa katika mipango yao ya kazi au kwa njia yao ya kuzungumza. {1T 444.1}

Wachungaji hao ambao wametoka katika madhehebu tofauti na kuukumbatia ujumbe wa malaika wa tatu mara nyingi wanataka kufundisha wakati wanapaswa kuwa wanafunzi. Wengine wana sehemu kubwa ya mafundisho yao ya zamani ya kuacha kabla ya kujifunza kikamilifu kanuni za Ukweli wa sasa (watoe kichwani ya zamani waweke mapya unlearn). Wachungaji watalijeruhi sana kusudi la MUNGU kwa kwenda kufanya kazi kwa wengine wakati kuna kazi kubwa ya kufanywa kwao ili kuwafanya wafae kwa utumishi kama wanavyotamani kufanya kwa wasioamaini. Ikiwa hawakidhi vigezo kwa kazi hiyo, kutahitajika wachungaji wawili au watatu waaminifu kufuata na kurekebisha ushawishi wao mbaya. Mwishowe, gharama zitakuwa nafuu kwa kazi ya MUNGU kuwaunga mkono wachungaji kubaki nyumbani ili wasijeruhi shamba la Bwana. {1T 444.2}

Wahubiri wamekuwa wakichukuliwa na wengine kama waliovuviwa haswa, kama watu maalumu na chombo cha kuwasiliana na Bwana. Ikiwa wazee na wale wenye uzoefu mrefu wanaona kasoro kwa mchungaji na kupendekeza kuboreshwa kwa tabia yake, kwa sauti yake, au katika ishara zake, wakati mwingine amejisikia kuumia, na amewaza kwamba MUNGU alimwita vile vile alivyokuwa, kwamba nguvu zilikuwa za MUNGU na sio za yeye mwenyewe, na kwamba MUNGU lazima afanye kazi hiyo kwa ajili yake, kwamba alifanya sio kuhubiri kulingana na hekima ya mwanadamu, n.k na nk. Ni makosa kufikiria kwamba mtu hawezi kuhubiri isipokuwa akifanywa kuwa msisimko wa hali ya juu. Watu ambao kwa hivyo hutegemea hisia wanaweza kuwa wa matumizi katika kuhimiza wakati wanahisi kama hiyo; lakini kamwe hawatafanya watendakazi wazuri, wanaobeba mzigo. Wakati kazi inasonga kwa ugumu na bidii na kila kitu kinachukua hali ya kukatisha tamaa, ya kusisimua na wale wanaotegemea hisia, hakika hawajajiandaa kubeba sehemu yao ya mizigo. Wakati wa kukatishwa tamaa na giza ni muhimu sana kuwa na watu wenye fikira tulivu, ambao hawategemei na hali, lakini ambao wanamtumaini MUNGU na kufanya kazi katika giza na vile vile kwenye nuru. Wanaume wanaomtumikia MUNGU kwa kanuni, ingawa imani yao inaweza kujaribiwa vikali, wataonekana wakiegemea mkono salama wa Yehova usioshindwa kamwe. {1T 444.3}

Wahubiri wachanga, na watu ambao wamewahi kuwa wachungaji, ambao wamepinda, wakorofi, wajeuri na wenye tabia mbaya, wakitoa maoni katika mazungumzo yao ambayo hayakuwa ya kawaida kabisa, yasiyo safi, yasiyo ya staha, yasiyo na uungwana, na yasiyofaa, hawastahili kushiriki katika kazi hii mpaka watakapotoa ushahidi wa matengenezo yote. Neno moja linalozungumzwa bila hekima linaweza kuleta madhara zaidi kuliko ambavyo safu ya mikutano wanayoendesha, ingefanya mema. Wanaacha kiwango cha Ukweli, ambacho kinapaswa kuinuliwa milele, kuburuzwa kwenye vumbi mbele ya jamii. Waongofu wao kwa ujumla hawavuki juu kuliko kiwango walichoinuliwa na mchungaji. Watu ambao wanasimama kati ya walio hai na wafu wanapaswa kuwa watu wa waadilifu tu. Mchungaji haipaswi kuwa mbali na ulinzi wake kwa dakika moja. Anajitahidi kuinua wengine kwa kuwalea juu ya jukwaa la Ukweli. Acha aoneshe wengine kuwa kweli umemfanyia kitu yeye mwenyewe. Anapaswa kuona ubaya wa maneno haya ya hovyo, mabaya, machafu, matusi na anapaswa kuweka mbali na kudharau kila kitu cha tabia hii. Isipokuwa afanye hivi, waongofu wake wataiga mfano wake. Na wakati wahudumu waaminifu watafuata na kufanya kazi na waongofu hawa kurekebisha makosa yao, watajitetea kwa kumrejelea mchungaji. Ikiwa unalaani mwenendo wake, watakugeukia na kuuliza: Kwa nini unashikilia na kutoa ushawishi kwa watu kwa kuwatuma kutuhubiria wenye dhambi ilihali hao wenyewe ni wenye dhambi? {1T 445.1}

Kazi ambayo tunajishughulisha nayo ni kazi inayowajibisha na kuinuliwa. Wale wanaohudumu kwa Neno na mafundisho ya imani wanapaswa wenyewe kuwa

mifano ya matendo mema. Wanapaswa kuwa mifano katika utakatifu, usafi, na utaratibu. Mwonekano wa mtumishi wa MUNGU, nje ya mimbari na ndani, inapaswa kuwa kwa mhubiri aliye hai. Anaweza kutimiza mengi zaidi kwa mfano wake wa Kiungu kuliko kwa kuhubiri tu kwenye kibweta, wakati ushawishi wake nje ya kibweta haustahili kuigwa. Wale wanaotendakazi kwa kusudi hili wanaubeba Ukweli ulioinuliwa zaidi kwa ulimwengu ambao umewahi kutolewa kwa wanadamu. {1T 446.1}

Watu waliochaguliwa na MUNGU kufanya kazi kwa kusudi hili watatoa uthibitisho wa wito wao wa mkuu na watachukulia kama jukumu lao kubwa kukua na kuboresha mpaka watakapokuwa watendakazi wenye uwezo. Halafu, wanapoonesha unyofu na bidii ya kuboresha talanta ambayo MUNGU amewakabidhi, wanapaswa kusaidiwa kwa busara. Lakini huko kutiwa moyo wanakopewa hakupaswi kuwa na mionjo ya kutia chumvi au kuwadanganya ili wajivune, kwani Shetani mwenyewe atafanya kazi ya kutosha ya aina hiyo. Wanaume wanaodhani kwamba wana jukumu la kuhubiri hawapaswi kudumishwa kwa kujitupa wenyewe na familia zao mara moja juu ya ndugu kwa msaada. Hawana haki ya hili mpaka waweze kuonesha matunda mazuri ya kazi yao. Sasa kuna hatari ya kuwaumiza wahubiri wachanga, na wale ambao wana uzoefu mdogo, kwa kuwasifia kwa kutia chumvi, na kwa kuwaondolea kila mizigo maishani. Wakati hawahubiri ni lazima wafanye wanavyoweza kwa kujitegemeza kimaisha wenyewe. Hii ndiyo njia bora ya kupima asili ya wito wao wa kuhubiri. Ikiwa wanataka kuhubiri tu kwamba waweze kuungwa mkono kama wahudumu, na kanisa likifuata mwendo wa busara, hivi karibuni watapoteza mzigo na kuacha kuhubiri kwa biashara yenye faida zaidi. Paulo, mhubiri hodari zaidi, aliyebadilishwa na MUNGU kimuujiza kufanya kazi maalum, hakuwa juu ya kazi. Anasema: "Hata saa hii ya leo sisi tuna njaa, na kiu, na tuko uchi, twapigwa makofi, na hatuna makao; na tunajitahidi, tukifanya kazi kwa mikono yetu wenyewe; tukitukanwa, tunabariki; tukiteswa, vumilieni. " 1 Wakorintho 4:11, 12. "Wala hatukula mkate wa mtu ye yote bure, bali tulifanya kazi kwa bidii usiku na mchana, ili tusije kuwa mzigo kwa yeyote kati yenu." 2 Wathesalonike 3: 8. {1T 446.2}

Nimeoneshwa kuwa wengi hawakadirii kwa usawa talanta ambazo zipo miongoni mwao. Ndugu wengine hawaelewi ni talanta gani ya kuhubiri ambayo ingekuwa bora zaidi kwa maendeleo ya kusudi la Ukweli, lakini hufikiria tu juu ya kuridhika kwa sasa kwa hisia zao. Bila kutafakari wataonesha upendeleo kwa mzungumzaji ambaye anaonesha bidii kubwa katika kuhubiri kwake na anaelezea hadithi/anectode fupi zinazopendeza au kuchekesha ambazo hupendeza sikio na kuhuisha akili kwa muda mfupi, lakini haziachi hisia yoyote ya kudumu. Wakati huo huo wataweka makadirio ya chini juu ya mhubiri ambaye amesoma kwa maombi mengi wakati wa kutayarisha mahubiri ili awasilishe mbele ya watu hoja za msimamo wetu kwa hali ya utulivu na katika

hali iliyounganishwa. Kazi yake haithaminiwi, na mara nyingi hutendewa bila kujali na watu huwa hawamfurahii. {1T 447.1}

Mtu anaweza kuhubiri kwa roho na kupendeza sikio, lakini asifikishe wazo jipya au maarifa halisi kwa akili. Mvuto unaopokelewa kupitia mahubiri kama haya haudumu zaidi ya pale sauti ya mzungumzaji inaposika. Wakati uchunguzi unapofanyika kwa ajili ya matunda ya kazi hiyo kuna kidogo tu hupatikana. Karama hizi zinazongaa kwa kuonekana na kuvutia kwa maonyesho, huwa hazina manufaa na hazijakadiriwa vema kuendeleza kusudi la Ukweli, kama karama ambayo inaweza kuaminika katika sehemu tata na ngumu. Katika kazi ya kufundisha Ukweli ni muhimu kwamba vipengele muhimu vya msimamo wetu viimarishwe vizuri kwa Ushuhuda wa Maandiko. Madai yanaweza kumnyamazisha mtu asiyeamini, lakini hayatamshawishi. Sio waumini pekee yao ambao watendakazi hutumwa shambani. Wokovu wa roho ndio shabaha kuu. {1T 447.2}

Ndugu wengine wamekosea katika jambo hili. Walifikiri kwamba Ndugu C alikuwa mtu sahihi kufanya kazi huko Vermont na kwamba angeweza kutimiza zaidi ya mchungaji yeyote katika jimbo hilo. Hao hawaoni mambo kwa mtazamo mzuri. Ndugu C anaweza kuzungumza kwa njia ya kupendeza makutano, na ikiwa hii ndiyo yote ambayo inahitajika kufanya mhubiri aliyefanikiwa, basi tabaka la ndugu na dada lingekuwa sawa katika kadirio lake kwake. Lakini yeye si mtendakazi kamili; haaminiki. Katika majaribu ya kanisa yeye hana msaada wowote. Hana uzoefu, maamuzi, na utambuzi wenye faida yoyote kwa kanisa wakati wa jaribu. Hakuwa mtu mwenye msimamo katika masuala ya mpito, na ingawa ana familia ndogo tu, amehitaji msaada zaidi au kidogo (pesa nk). Ukosefu huo huo hudhihirishwa katika mambo ya kiroho kama katika mambo ya kidunia. Ikiwa njia sahihi ilifuatwa kwake wakati wa kuanza kuhubiri kwake, sasa angeweza kuwa na faida katika kusudi hili. Ndugu zake walimjeruhi kwa kumfanyia mengi kupita kiasi na kwa kumwacha abebe mizigo michache tu ya maisha, mpaka amefikiria kuwa huduma yake ilikuwa na matokeo makubwa. Amekuwa tayari kwamba ndugu huko Vermont wabebemizigo yake wakati alikuwa ametulia kutoka kwa masumbufu. Hajapata mazoezi yanayofaa kutoa nguvu kwa misuli yake, na kuboresha afya yake. {1T 448.1}

Yeye hana uwezo wa kujenga makanisa. Wakati anahisi ole juu yake ikiwa hahubiri injili, kama wahubiri wa kujitolea walivyohisi hapo zamani, basi kama wao atakuwa tayari kufanya kazi kwa mikono yake sehemu ya muda kupata pesa za kusaidia familia yake ili asiwe mzigo kwa kanisa, na kisha ataenda, sio kuhubiri tu, bali kuokoa roho. Jitihada zilizofanywa na roho kama hiyo zitatimiza jambo fulani. Ametukuka katika makadirio yake mwenyewe, amejiona kuwa sawa na mtendakazi yeyote huko Vermont, na amehisi kwamba anapaswa kuorodheshwa kwenye kiwango kimoja nao na anapaswa kuhuhusishwa katika masuala ya vikao vya mikutano ya kanisa, wakati hajapata

sifa wala kujithibitisha kuwa anastahili. Je! Amejitoa mhanga au kujitoa kiasi gani kwa kanisa? Je! Amekumbwa na mkasa gani au shida gani, kwamba ndugu wanaweza kuwa na ujasiri kwake kama mtendakazi ambaye wanaweza kumwamini, ambaye ushawishi wake utakuwa mzuri kila aendako? Hadi awe na roho tofauti kabisa na atende kwa kanuni zisizo za ubinafsi, itakuwa bora kwake kuacha kuhubiri {. 1T 448.2}

Ndugu huko Vermont wamepuuza heshima ya maadili ya watu kama Ndugu Bourdeau, Pierce, na Stone, ambao wana uzoefu wa kina na ambao ushawishi wao umekuwa kiasi cha kupata ujasiri wa jamii wanayoishi. Maisha yao ya bidii ya kazi, tasnia na uthabiti yamewafanya wahubiri hai wa kila siku, na kazi zao zimeondoa ubaguzi mkubwa na wamekusanyika na kujenga. Walakini ndugu hawajathamini utumishi wa watu hawa, wakati wamefurahishwa na ile ya wengine ambao hawatastahimili kujaribiwa na kuthibitika, na ambao wanaweza kuonesha matunda kidogo ya kazi yao. {1T 449.1}

## SURA YA 81

## MKE WA MCHUNGAJI

Juni 5, 1863, nilioneshwa kwamba Shetani yuko kazini kila wakati ili kuvunja moyo na kuwapotosha wahudumu ambao MUNGU amewachagua kuhubiri Ukweli. Njia inayofaa zaidi ambayo anaweza kufanyia kazi ni kupitia ushawishi wa nyumbani, kupitia wenzi wasiojitoa. Ikiwa anaweza kudhibiti akili zao, anaweza kupitia wao kupata urahisi zaidi kwa mume, ambaye anafanya kazi kwa Neno na mafundisho ya imani kuokoa roho. Nilielekezwa kwa maonyo ambayo MUNGU ametoa mara kwa mara, na kwa majukumu ambayo yameoneshwa kuwa ni ya mke wa mchungaji lakini maonyo haya hayakuwa na ushawishi wa kudumu. Ushuhuda uliotolewa umekuwa na athari lakini kwa muda mfupi. Mwanga umefuatwa lakini kwa sehemu tu. Utii na kujitoa wakfu kwa MUNGU kumesahaulika, wengi wamepuuza jukumu takatifu lililowekwa juu yao kuboresha nuru na upendeleo waliopewa, na kutembea kama watoto wa nuru. Ikiwa pazia lingeweza kufunguliwa na wote wangeweza kuona jinsi masuala yao yanavyozingatiwa mbinguni, kungekuwa na kuzinduka, na kila mmoja kwa hofu atauliza, Je! Nitafanya nini ili kuokolewa? {1T 449.2}

Mke wa mchungaji ambaye hajajitoa kwa MUNGU sio msaada kwa mumewe. Wakati anakaa juu ya ulazima wa kubeba msalaba na kusisitiza umuhimu wa kujikana, mfano wa kila siku wa mkewe mara nyingi unapingana na mahubiri yake na huharibu msukumo Wake. Kwa njia hii anakuwa kizuizi kikubwa na mara nyingi humwongoza mumewe mbali na wajibu wake na kutoka kwa MUNGU. Hatambui ni dhambi gani anafanya. Badala ya kutafuta kuwa mwenye manufaa, akitafuta kwa upendo wa kweli roho zenye kuhitaji msaada, yeye anajikunja kwa kutoka nje ya jukumu hilo na anapendelea maisha yasiyofaa. Yeye hajavutwa na nguvu ya upendo wa Kristo na kwa kanuni zisizo za ubinafsi, takatifu. Hachagui kufanya mapenzi ya MUNGU, kuwa mtendakazi mwenza na mumewe, na malaika, na MUNGU. Wakati mke wa mchungaji akiandamana na mumewe katika utume wake wa kuokoa roho, ni dhambi kubwa kwake kumzuia katika kazi yake kwa kuonesha kutoridhika na kutokuwa na furaha. Walakini badala ya kuingia kwa moyo wote katika kazi zake, akitafuta kila fursa ya kuunganisha nia yake na kufanya kazi naye, mara nyingi hujifunza jinsi anavyoweza kuifanya iwe rahisi au ya kupendeza kwake. Ikiwa mambo yanayowazunguka hayakubaliki kama vile angeweza kutamani (kama vile hayatakuwa siku zote), mke hapaswi kujishughulisha na hisia za kutamani nyumbani (homesick), au kwa kukosa furaha na kwa malalamiko yaliyosemwa humsumbua mume na kumfanya kazi yake kuwa ngumu, na labda na yeye kutoridhika kumvuta kutoka mahali ambapo angeweza kufanya mema. Hapaswi kugeuza shauku na maslahi ya mumewe kutoka kwenye kufanya kazi kwa wokovu wa roho, kuhurumia maradhi yake madogo-madogo na kuridhisha ndoto zake za kufikirika, hisia zisizoridhika. Ikiwa angejisahau na kujitahidi kusaidia wengine, kuongea na kuomba na roho masikini, na kutenda kama wokovu wao ulivyokuwa wa umuhimu na wa juu zaidi, na hivyo wa kutiliwa maanani zaidi ya mengine yote, hatakuwa na wakati wa kutamani nyumbani wakati yuko mbali na kijiji chao (kuwa homesick). Angehisi siku hadi siku kuridhika kutamu kama thawabu kwa kazi yake isiyo na ubinafsi; Siwezi kuiita hii kuwa ni dhabihu, kwa kuwa baadhi ya wake wa wachungaji wetu hawajui ni nini kujitoa au kuteseka kwa sababu ya Ukweli. {1T 450.1}

Katika miaka ya zamani wake wa wachungaji walivumilia uhitaji na mateso. Wakati waume zao walipotiwa gerezani, na wakati mwingine kifo, hao wanawake wenye heshima na bora na wenye kujitoa waliumia pamoja nao, na thawabu yao itakuwa sawa na ile waliyopewa waume zao. Bi Boardman na Bi Judsons waliteswa kwa ajili ya Ukweli, wao na wenzi wao. Walijitolea nyumbani na marafiki kwa kila maana ya neno kuwasaidia wenzi wao katika kazi ya kuwaangazia wale waliokaa kwenye giza, kuwafunulia siri za Neno la MUNGU. Maisha yao yalikuwa katika hatari ya mara kwa mara. Kuokoa roho ilikuwa kitu chao kikubwa, na kwa hili wangeweza kuteseka kwa furaha. {1T 451.1}

Nilioneshwa maisha ya Kristo. Wakati kujikana nafsi na kujinyima kwake na kujitolea hulinganishwa na majaribu, mitihani na mateso ya wake za baadhi ya wahudumu wetu, hili husababisha kitu chochote ambacho wanaweza kuita dhabihu kuzama chini katika kutokuwa na maana kabisa. Ikiwa mke wa mchungaji anazungumza maneno ya kutoridhika na kukatishwa tamaa, ushawishi kwa mume unavunja moyo na huelekea kumfanya alemae katika kazi yake, haswa ikiwa mafanikio yake yanategemea ushawishi wa mazingira ya karibu. Je! Mchungaji wa MUNGU katika hali kama hizo lazima awe kilema au kung'olewa kutoka uwanja wake wa kazi ili kutosheleza hisia za mkewe, ambazo hutokana na kutotaka kujisalimisha katika mwelekeo wa wajibu? Mke anapaswa kulinganisha matakwa yake, raha na wajibu, na atoe hisia zake za ubinafsi kwa ajili ya Kristo na Ukweli. Shetani amekuwa na uhusiano mwingi na kudhibiti kazi za wahudumu kupitia ushawishi wa wenzi wa ubinafsi, wapenda raha.{1T 451.2}

Ikiwa mke wa mchungaji huambatana na mumewe katika safari zake, basi, hapaswi kwenda huko ili kupata raha yake maalum, kuvinjari, kutalii na kuhudumiwa tu, bali afanye kazi naye. Anapaswa kuwa na nia ya pamoja naye kufanya mema. Anapaswa kuwa tayari kuandamana na mumewe, ikiwa huduma za nyumbani hazizuii,basi anapaswa kumsaidia mumewe katika juhudi zake za kuokoa roho. Kwa upole na unyenyekevu, lakini kwa kujitegemea kwa ubora, anapaswa kuwa na ushawishi wa kuongoza juu ya akili zinazomzunguka, na anapaswa kuchukua sehemu yake katika kubeba msalaba wake na mzigo katika mkutano, na kuzunguka katika madhabahu ya familia, na katika mazungumzo karibu na moto. Watu wanatarajia hili kutoka kwa mke, na wana haki ya kutarajia hivyo. Ikiwa matarajio haya hayatatimizwa, ushawishi wa mume umeharibiwa zaidi ya nusu. Mke wa mchungaji anaweza kufanya mengi ikiwa atafanya. Ikiwa ana roho ya kujitolea na ana upendo kwa roho, anaweza kufanya naye karibu kiwango sawa cha mema. {1T 452.1}

Mtendakazi mdada katika kusudi la Ukweli anaweza kuelewa na kufikia masuala mengine, haswa miongoni mwa akina dada, ambayo mchungaji hawezi. Jukumu hilo linakuwa juu ya mke wa mchungaji ambalo hawezi kwa wapesi tu kulitupilia mbali. MUNGU atahitaji talanta aliyokupa, pamoja na riba. Anapaswa kufanya kazi kwa bidii, uaminifu, na kwa umoja na mumewe ili kuokoa roho. Hapaswi kamwe kuchochea matakwa yake na shauku, au kuelezea ukosefu wa maslahi katika kazi ya mumewe, au kukaa juu ya hisia za kutamani nyumbani, au hisia za kutoridhika. Hisia hizi zote za asili lazima zishindwe. Anapaswa kuwa na kusudi maishani ambalo linapaswa kutendwa bila kusita. Je! Inakuwaje ikiwa hii inapingana na hisia, na raha, na ladha za asili? Haya

yanapaswa kutolewa dhabihu kwa moyo mkunjufu na kwa utayari ili kufanya mema na kuokoa roho. {1T 452.2}

Wake wa wachungaji wanapaswa kuishi maisha ya kujitoa na ya maombi. Lakini wengine wangefurahia dini ambayo haina misalaba na ambayo haihitaji kujinyima na kufanya jitihada kwa upande wao. Badala ya kusimama kwa heshima yao wenyewe, wakimtegemea MUNGU kwa nguvu na kubeba jukumu lao la kibinafsi, wao muda mwingi wamekuwa wakiwategemea wengine, wakipata maisha yao ya kiroho kutoka kwao. Ikiwa wangemtegemea MUNGU kama msiri wao, na kama watoto wadogo kumtumaini na mapenzi yao yajikite kwa Yesu, wakipata maisha yao kutoka kwa Kristo, Mzabibu ulio hai, basi, ni kiasi gani cha mema wanachoweza kufanya, ni msaada mkubwa kiasi gani wanaweza kuwa kwa wengine, msaada gani kwa waume zao, na watapata thawabu gani mwishowe! "Vema, watumishi wazuri na waaminifu," ingeanguka kama muziki mtamu masikioni mwao. Maneno, "Ingia katika furaha ya Bwana wako," yangewalipa mara elfu moja kwa mateso na majaribu yote yaliyovumiliwa kuokoa roho za thamani. {1T 452.3}

Wale ambao hawataboresha talanta ambayo MUNGU amewapa watashindwa kupata uzima wa milele. Wale ambao wamekuwa na manufaa kidogo ulimwenguni watalipwa ipasavyo, kama kazi zao zilivyokuwa. Wakati kila kitu kinakwenda sawa, hawa huchukuliana pamoja na wimbi; lakini wakati wanahitajika kwa dhati na bidii na bila kuchoka kutumia makasia yao ili kupingana na upepo na wimbi, itaonekana hakuna nguvu katika tabia yao ya Kikristo. Hawatachukuliana na usumbufu katika kazi lakini watatupa makasia yao na kuliacha wimbi liwatupe chini kilindini. Kwa hivyo kwa jumla watakaa huko kilindini hadi mtu atakapochukua mizigo yao na kufanya kazi kwa dhati na bidii na kwa nguvu ili kuwavuta waje juu. Kila wakati wanapokubali ugoigoi kama huo hupoteza nguvu na huwa na mwelekeo mdogo wa kutenda kazi kwa kusudi la MUNGU. Ni mshindi mwaminifu tu ambaye anashinda utukufu wa milele. {1T 453.1}

Mke wa mchungaji anapaswa kuwa na ushawishi wa kuongoza kwenye mawazo ya wale anaoshirikiana nao daima, kwa njia hii atakuwa msaada au kikwazo kikubwa. Mke anakusanya pamoja na Kristo au anatawanya mbali. Roho ya kujitoa ya umishenari inakosekana miongoni mwa wenzi wa wachungaji wetu. Ni ubinafsi kwanza, yaan nafsi zao kwanza, halafu Kristo wa pili, au hata wa tatu. Kamwe mchungaji hapaswi kumchukua mke wake isipokuwa anajua kuwa anaweza kuwa na msaada wa kiroho, kwamba ni anaweza kuchukuliana na mzigo, kuvumilia, na kuteseka ili kutenda mema, na kufaidisha roho za watu kuwa na manufaa kwa ajili ya Kristo. Wale ambao wanaambatana na waume zao wanapaswa kwenda kufanya kazi kwa umoja pamoja nao. Hawa wasitarajie

kuwa huru kutokana na majaribu na maudhi. Hawapaswi kufikiria sana kuhusu hisia za kujifurahisha tu. Je! Hisia zinahusiana nini na wajibu? {1T 453.2}

Nilinukuliwa kisa cha Ibrahimu. MUNGU akamwambia, "Sasa chukua mwanao, mwanao wa pekee, Isaka, unayempenda, uende katika nchi ya Moria; ukamtoe kuwa sadaka ya kuteketezwa juu ya mmoja wa milima nitakayokuambia." Ibrahimu alimtii MUNGU. Hakushauriana na hisia zake, lakini kwa imani bora na ujasiri kwa MUNGU alijiandaa kwa safari yake. Kwa moyo uliopasuka na uchungu alimwona mama mwenye kiburi na mwenye upendo akimtazama kwa upendo mkubwa mwana wa ahadi. Lakini alimuondoa pale yule mwana mpendwa. Ibrahimu aliteseka, lakini hakuacha mapenzi yake yainuke kwa kuasi mapenzi ya MUNGU. Wajibu, wajibu mchungu, ulimdhibiti. Hakuthubutu kushauriana na hisia zake au kujisalimisha hata kwa dakika moja. Mwanawe wa pekee alitembea kando ya baba wenye uchungu, mwenye upendo, mwenye kuteseka, akiongea kwa bidi, akitamka tena na tena jina la kupendeza la baba, na kisha kuuliza: "Dhabihu iko wapi?" Ah, ni mtihani gani kwa baba mwaminifu! Malaika walitazama kwa mshangao wa kuvutia kwa senema hiyo. Mtumishi mwaminifu wa MUNGU hata alimfunga mtoto wake mpendwa na kumlaza juu ya kuni. Kisu kiliinuliwa, wakati malaika alipiga kelele: "Ibrahimu, Ibrahimu.. Usiweke mkono wako juu ya kijana." {1T 454.1}

Niliona kuwa sio jambo jepesi kuwa Mkristo. Ni jambo dogo kudai kuwa na jina tu la Mkristo; lakini ni jambo kubwa na takatifu kuishi maisha ya Kikristo. Kuna muda kidogo sasa kupata taji ya kutokufa, kuwa na rekodi ya matendo mema na majukumu yaliyotimizwa yaliyoandikwa mbinguni. Kila mti huhukumiwa kwa matunda yake. Kila mtu atahukumiwa kulingana na matendo yake, siyo madai yake au imani yake. Swali halitaulizwa kamwe, Alitoa madai kiasi gani? lakini, Alizaa matunda gani? Ikiwa mti ni mbovu, matunda ni mabaya. Ikiwa mti ni mzuri, hauwezi kuzaa matunda mabaya. {1T 454.2}

## SURA YA 82

## HAKI ZA AMANA (Patent Rights).

Ndugu zetu wengi hujihusisha na kushiriki katika biashara mpya ambazo zinaonekana kuvutia kwa macho ila ni udanganyifu tu; lakini kwa muda mfupi wanajikuta wamekata tamaa na mali zao zimepotea, ambazo zilipaswa kutumiwa kusaidia familia zao na kuendeleza kusudi la Ukweli wa sasa. Kisha huja majuto, na kujilaumu; na wengine wenye dhamiri hutupa kujiamini kwao, na kupoteza furaha yao ya kiroho, na kama matokeo ya msongo wa akili afya

nayo huzorota (Biashara za Pyramid ziko kwenye fasheni sana nchi ya Marekani na wauzaji/salesmen wana biid kwa hii). {1T 455.1}

Wale ambao wanauamini Ukweli wanapaswa wajizoeze kuwa wachumi, kuishi kwa chakula cha kawaida, safi, kila wakati wakifanya kanuni/sheria kuishi kulingana na uwezo wao. Ndugu kamwe hawapaswi kushiriki katika biashara mpya bila kushauriana na wale walio na uzoefu ambao ni viongozi wazuri katika maswala ya kidunia na ya kiroho. Kwa kufanya hivi wangejiepusha na mashaka mengi. {1T 455.2}

Ndugu wangeridhika na kipato kidogo, na kushughulikia hicho kidogo kwa busara badala ya kuhatarisha kuboresha hali zao, na kupata hasara za kuendelea. Watunza Sabato wengine ambao wamehusika katika uuzaji wa haki za amana wamesafiri kati ya ndugu zao ili kuokoa gharama, na wamewashawishi kuwekeza mali zao katika haki za amana. Hayo hayatakuwa wazi mbele za MUNGU mpaka watakapokuwa wamepata hasara ambayo hawa ndugu wameidhinisha. {1T 455.3}

# SURA YA 83

# MATENGENEZO KATIKA MAVAZI

Ndugu Wapendwa kaka na Dada: rai yangu kwa kutaka usikivu wenu tena juu ya mada ya mavazi ni kwamba baadhi wanaonekana kutoelewa kile nilichoandika hapo awali; na juhudi hufanywa, labda na wale ambao hawataki kuamini kile nilichoandika, na kufanya machafuko katika makanisa yetu juu ya mada hii muhimu. Barua nyingi zimetumwa kwangu, zikibainisha changamoto, ambazo sikupata nafasi ya kuzijibu; na sasa, kwa kujibu maswali mengi, ninatoa maelezo yafuatayo, ambayo bila shaka yanatumainiwa kuwa suluhisho la daima la mada hii, kwa kadri ushuhuda wangu unavyohusika. {1T 456.1}

Wengine wanadai kwamba kile nilichoandika katika Ushuhuda kwa Kanisa Namba 10 hakikubaliani na ushuhuda wangu katika kitabu kinachoitwa, Jinsi ya Kuishi. Hizi ziliandikwa kutoka mtazamo mmoja, hivyo sio mitazamo miwili inayopingana, kama wengine wanavyoweza kudhani; ikiwa kuna tofauti yoyote, ni katika namna tu ya kujieleza. Katika Ushuhuda wa Kanisa Namba 10 nilisema kama ifuatavyo: {1T 456.2}

"Hakupaswi kuwepo tukio litakalotumiwa na wasioamini kuishutumu imani yetu. Tunachukuliwa tusio wa kawaida na wa kipekee, na hatupaswi kuwa chanzo cha kuwaongoza wasioamini kutufikiria zaidi ya vile imani yetu inavyotutaka tuwe. Wengine ambao wanauamini Ukweli wanaweza kufikiri kwamba ingekuwa vyema zaidi kwa akina dada kuiga mavazi ya Amerika, lakini ikiwa mtindo huo wa mavazi ungedhohofisha ushawishi wetu kwa wasioamini na kupelekea kushindwa kupata urahisi wa kuwafikia, basi hatupaswi kuuiga kwa namna yoyote, ingawa matokeo yake yalitutaabisha sana. Lakini wengine wamedanganyika kwa kudhani kuna faida nyingi wanawezapata kwa kuiga mtindo huu wa mavazi ya America Costume. Japo unaweza kuwa na faida kwa baadi, una madhara kwa wengine. {1T 456.3}

"Niliona kwamba agizo la MUNGU  limebadilishwa, na maagizo yake maalum hayazingatiwi, na wale wanaoiga mtindo wa mazi ya Amerika. Nilirejezwa kwenye Kumbukumbu la Torati 22: 5: "Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa Bwana, MUNGU wako.' MUNGU asingependa watu Wake wajiingize katika kile kijulikanacho kama mageuzi ya mavazi. Ni mavazi yasiyo na adabu, na yasiyofaa kabisa, kwa wafuasi wanyenyekevu wa Kristo kujistiri. {1T 457.1}

"Kuna ongezeko la mazoea kwa wanawake katika mavazi yao na muonekano wao kushabihiana kwa karibu sana na ya jinsia nyingine, na kutengeneza mavazi yao katika mtindo kama wanaume, lakini MUNGU anatamka kuwa ni chukizo. 'Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujistiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; 1 Timotheo 2: 9. {1T 457.2}

"Wale wanaohisi wameitwa kujiunga na harakati yenye kupendelea haki za mwanamke na kile kinachoitwa marekebisho ya mavazi wanaweza pia kukata uhusiano wote na ujumbe wa malaika wa tatu. Roho amhudumiae huyu hawezi kuwa katika maelewano mwingine. Maandiko yako wazi juu ya uhusiano na haki za wanaume na wanawake. Wana umizimu kwa kiasi fulani wamepitisha mtindo huu wa kipekee wa mavazi. Wadventista wa Sabato, ambao wanaamini katika kurejeshwa kwa karama, mara nyingi hujulikana kama wana umizimu. Hebu na waige tu huu mtindo wa mavazi, ushawishi wao utakuwa umekufa. Watu wangewafananisha na wana umizimu na wangekataa kuwasikiliza-watakuwa kapu moja. {1T 457.3}

"Kutokana na kile kinachoitwa mageuzi ya kimavazi kumekuwa na roho ya purukushani na ujasiri kwa ajili ya kuendana na mavazi haya. Adabu na kujistiri vinaonekana kutoweka kwa watu wengi pindi wanapoiga mtindo huo wa mavazi. Nilioneshwa kwamba MUNGU angependa tuchukue mwelekeo thabiti na unaoelezeka. Hebu kina dada waige mitindo ya mavazi ya Amerika basi

watauharibu mvuto wao wenyewe na ule wa waume zao. Wangekuwa mithali ya kejeli na dhihaka-msemo mitaani. Mwokozi wetu anasema: "Ninyi ni nuru ya ulimwengu." "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni." Kuna kazi kubwa kwetu ya kufanya ulimwenguni, na MUNGU hatatutaka tuhafifishe au kuharibu mvuto wetu kwa ulimwengu. "{1T 457.4}

Yaliyotangulia nilipewa kama karipio kwa wale ambao wamependa kufuata mtindo wa mavazi yanayofanana na yale ambayo huvaliwa na wanaume; lakini wakati huo huo nilioneshwa uovu wa mtindo wa kawaida wa mavazi ya mwanamke, na kurekebisha haya, pia nilitoa yafuatayo yaliyopatikana katika Ushuhuda kwa Kanisa, Nambari 10: {1T 458.1}

"Hatufikirii kulingana na imani yetu kuvaa kwa kufuata mtindo wa vazi la Marekani, kuvaa magauni marefu yanayobana nyonga ya hoops, au kupitiliza kiasi katika kuvaa nguo ndefu ambazo zinafagia njia za barabarani na mitaa. Ikiwa wanawake wangevaa nguo hizo za kusafisha uchafu wa mitaa inchi moja au mbili pungufu, mavazi yao yangekuwa ya adabu, na yangehifadhiwa kwa usafi kwa urahisi zaidi, na kuvaliwa kwa muda mrefu. Mavazi kama hayo yangeendana na imani yetu. " {1T 458.2}

Sasa nitatoa dondoo kutoka kwa kile nilichosema mahali pengine juu ya mada hii: {1T 458.3}

"Wakristo hawapaswi kuhenyeka ili kutazamwa kwa udadisi kama kituko tu, kwaajili ya kuvaa tofauti na ulimwengu. Lakini ikiwa, wakati wa kufuata imani zao za wajibu kwa kuzingatia mavazi ya heshima, staha na afya, watajikuta wametoka katika mitindo, hawapaswi kubadilisha mavazi yao ili kufanana na ulimwengu, lakini wanapaswa kuonesha uhuru ulio na uungwana, na ujasiri wenye maadili kuwa sahihi, hata ikiwa ulimwengu wote unatofautiana nao. Ikiwa ulimwengu utaleta mavazi ya kawaida, rahisi, yenye faraja na yenye afya, ambayo ni kwa mujibu wa Biblia. Haitabadilisha uhusiano wetu na MUNGU au ulimwengu kufuata mtindo kama huo wa mavazi. Wakristo wanapaswa kumfuata Kristo na kufanya mavazi yao yalingane na Neno la MUNGU. Wanapaswa kuachana na kupitiliza kiasi. Wanapaswa kwa unyenyekevu kufuata mwenendo mwema ulionyooka, bila kujali makofi, pongezi au lawama, na wanapaswa kushikamana na kile kilicho sahihi kwa sababu ya manufaa yake. {1T 458.4}

"Wanawake wanapaswa kufunika viungo vyao kwa kuzingatia afya na faraja. Miguu na viungo vyao vinahitaji kuvikwa kwa uchangamfu kama vya wanaume. Urefu uliopitiliza wa mavazi ya mtindo wa hoops haukubaliki kwa sababu kadhaa: {1T 459.1}

"1. Ni ufujaji wa pesa na sio lazima kuwa na vazi lenye urefu kiasi cha kufagia barabara na mitaa. {1T 459.2}

"2. Vazi ambalo urefu wake hukusanya umande kutoka kwenye nyasi, na matope kutoka mitaani, na kwa hivyo huleta uchafu/unajisi kwa mwili. {1T 459.3}

"3. Katika kitandani chenye hali chakavu hukokota uchafu katika vifundo vya miiguu (ankles) , ambavyo havijalindwa vya kutosha, na hivyo kuhatarisha afya na maisha. Hii ni moja wapo ya sababu kubwa za ugonjwa wa kuziba pua na mfumo wa kupumua kwa makamasi-makamasi (catarrh) na uvimbe mwingi kwenye mwili na hata kifua kikuu cha mifupa. {1T 459.4}

"4. Urefu usio wa lazima huleta uzito wa ziada kwenye makalio/nyonga na viuno. {1T 459.5}

"5. Huzuia kutembea, na pia mara nyingi huzuia njia kwa watu wengine. {1T 459.6}

"Bado kuna mtindo mwingine wa mavazi ambao unaigwa na tabaka la wale wanaoitwa watengenezo ya mavazi. Wanafanya mfanano wa jinsia tofauti kadri iwezekanavyo. Wanavaa kofia, suruali, fulana, kanzu, na buti, sehemu ya mwisho ambayo ni nyeti sana katika mtindo wa mavazi. Wale wanaopitisha na kutetea mtindo huu wa mavazi hubeba kile kinachoitwa matengenezo ya mavazi kwa urefu pingamizi refu sana. Kuchanganyikiwa kutakuwa matokeo. Wengine wanaopokea vazi hili wanaweza kuwa sahihi katika maoni yao kwa ujumla juu ya swala la afya, lakini watakuwa na jukumu kubwa katika kufanikisha mazuri zaidi ikiwa hawatajihusisha sana na suala la mavazi kupitiliza kiasi. {1T 459.7}

"Kwa mtindo huu wa mavazi Agizo la MUNGU limegeuzwa na maagizo Yake maalum hayazingatiwi. Kumbukumbu la Torati 22:5: "Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanya mambo hayo ni machukizo kwa Bwana MUNGU wako.' MUNGU asingependa watu Wake wachukue mtindo huu wa mavazi. Haya sio mavazi ya adabu, na hayafai kabisa kwa wanawake waadilifu na wanyenyekevu, ambao wanadai kuwa wafuasi wa Kristo. Makatazo ya MUNGU hayazingatiwi sana na wote wanaotetea kuondoa tofauti ya mavazi kati ya wanaume na wanawake. Msimamo uliokithiri uliochukuliwa na baadhi ya warekebishaji wa mavazi juu ya somo hili unadhoofisha ushawishi wao. {1T 459.8}

"MUNGU aliweka tofauti ya wazi kati ya mavazi ya wanaume na wanawake, na Yeye amezingatia umuhimu kwa kiasi cha kutosha kutoa mwelekeo wazi juu yake; kwani kuwa na mavazi yale yale yanayovaliwa na jinsia zote yangesababisha mkanganyiko na ongezeko kubwa la uasi. Mtume Paulo angekuwa hai, na kuwaona wanawake wanaodai utauwa kwa mtindo huu wa mavazi, angekemea. 'Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujistiri, pamoja na adabu nzuri na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu, au lulu, wala kwa nguo za thamani; bali (kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri ucha MUNGU). Umati wa wale wanaojiita Wakristo hupuuza kabisa mafundisho ya mitume, na huvaa dhahabu, lulu, na mavazi ya gharama kubwa. {1T 460.1}

"Watu waaminifu wa MUNGU ni nuru ya ulimwengu na chumvi ya dunia, na wanapaswa kukumbuka daima kuwa ushawishi wao ni wa thamani. Ikiwa wangebadilisha mavazi marefu sana ya hoops kwa yale mafupi kwa kupitiliza sana, wangeweza, kwa kiwango kikubwa, kuharibu ushawishi wao. Watu wasioamini, ambao ni jukumu lao kunufaika na kutafutwa ili kuletwa kwa Mwana-Kondoo wa MUNGU, wangechukizwa. Maboresho mengi yanaweza kufanywa katika mavazi ya wanawake kwa kuzingatia afya bila kufanya mabadiliko makubwa kiasi cha kumchukiza mtazamaji. {1T 460.2}

"Mwili haupaswi kuminywa hata kidogo na kaptura zinazobana zinazovaliwa na wanawake ndani ziitwazo corsets. Mavazi yanapaswa kuwa katika mtindo unaoruhusu mapafu na moyo kufanya kazi kwa urahisi na afya. Vazi linapaswa kuwa juu kidogo ya kiatu, linapaswa kuwa fupi vya kutosha kutosafisha uchafu wa barabara bila kuinuliwa na mkono. Nguo fupi zaidi kuliko hii itakuwa sahihi, inayofaa, na yenye afya kwa wanawake wakati wa kufanya kazi zao za nyumbani, na haswa kwa wale ambao wanalazimika kufanya kazi za nje. Kwa mtindo huu wa mavazi, sketi moja nyepesi, au mbili zaidi, ndio zaweza kuhitajika, na hii inapaswa kuwekwa vishikizo kiunoni au kuzuiwa kwa kamba. Viuno havikuundwa kubeba uzito mkubwa. Sketi nzito zinazovaliwa na baadhi, na kuachwa zikilegea kwenye viuno, zimekuwa sababu ya magonjwa anuwai ambayo hayatibiki kwa urahisi. Wagonjwa hao wanaonekana kutokujua sababu ya mateso yao (ujinga umesababisha), na wanaendelea kukiuka sheria kwa kuvifunga viuno vao na kuvaa sketi nzito, mpaka wanapopata madhara ya muda mrefu na hata kuwa vilema. Wanapoambiwa makosa yao, wengi huonesha kushangaa, 'Kwanini nivae hivyo, mtindo kama huo wa mavazi utanifanya nionekana dada wa kizamani!' Ikiwa ni hivyo inadhuru nini? Natamani tungekuwa wa kizamani katika mambo mengi. Ikiwa tungekuwa na nguvu za zamani zilizowatambulisha wanawake wa zamani wa vizazi vilivyo tangulia, ingependeza sana. Sisemi bila kushauri ninaposema kwamba njia ambayo wanawake hujivika, pamoja na kuendekeza hamu yao ya kula, ndio sababu kubwa ya hali yao dhaifu, ya ugonjwa walio nao sasa. Kuna mwanamke mmoja

tu kati ya elfu ambaye huvisha viungo vyake vyake vya mbali ya moyo kama inavyostahili. Kwa urefu wowote wa vazi viungo vilivyo mbali na moyo vinapaswa kuvikwa vizuri kama ilivyo kwa wanaume-miguu, mikono, kichwa. Hii inaweza kufanywa kwa kuvaa suruali iliyoshonwa na kitambaa kingine chini yake (lining), na kufungwa juu ya kifundo cha mguu, au iliyounganishwa na kuwekewa pindo chini; na hii inapaswa kushuka mpaka kwenye kiatu. Miguu na mkono na vifundo vilivyofunikwa vya miguu, hulindwa dhidi ya mkondo wa hewa au upepo. Ikiwa miguu na mikono itafunikwa vyema kwa mavazi yenye joto, mzunguko wa damu utasawazishwa, na damu itabaki safi na yenye afya kwa sababu haipati baridi au kuzuiliwa katika njia yake ya asili inapopita kwenye mfumo wa damu. "{1T 460.3}

Utata mkuu ulio katika mawazo ya wengi ni hasa juu ya urefu wa vazi. Wengine wanasisitiza kwamba "juu ya buti," wanarejelea sehemu ya juu ya buti hizo kama wavaavyo wanaume, na kufika karibu na goti. Endapo ingekuwa kawaida ya wanawake kuvaa buti kama hizo, basi watu hawa hawapaswi kulaumiwa kwa kudai kuelewa hili jambo katika namna hii; lakini kwa kuwa wanawake kwa ujumla hawavai buti kama hizo, watu hawa hawana haki ya kunielewa kama walivyojifanya. {1T 462.1}

Ili kuonesha kile nilichomaanisha, na kwamba kuna mapatano na wala sio ukinzani katika shuhuda zangu juu ya mada hii, nitatoa hapa dondoo kutoka kwa hati zangu zilizoandikwa karibu miaka miwili iliyopita: {1T 462.2}

"Tangu nakala kuhusu mavazi ilipoonekana katika chapisho la *'How to live-Jinsi ya Kuishi,'* kumekuwa na mkanganyiko juu ya wazo nililotaka kuwasilisha. Wamekuwa na misimamo mikali ya kupitiliza katika kutafsiri juu ya kile nilichoandika kuhusu urefu wa vazi, na kwa kweli walikuwa na wakati mgumu sana juu ya jambo hilo. Watu hawa na maoni yao yaliyopotoka juu ya jambo hilo wamejadili suala la kufupisha mavazi hadi macho yao ya kiroho yamechanganyikiwa kiasi cha kuwaona tu watu kama miti inayotembea. Walifikiri wangeweza kuona mkanganyiko katika nakala yangu juu ya mavazi, iliyochapishwa hivi karibuni katika '*Jinsi ya Kuish*i', na nakala ihusuyo mada hiyo hiyo iliyomo katika Ushuhuda kwa Kanisa, Nambari 10. Lazima nikiri kwamba mimi ndiye mwamuzi bora wa mambo yaliyowasilishwa kwangu katika maono, na hakuna haja kwa yeyote kuhofu kwamba nitapingana na ushuhuda wangu mwenyewe, au kwamba nitashindwa kugundua mkanganyiko wowote wa kweli katika maoni niliyopewa. {1T 462.3}

"Katika nakala yangu juu ya mavazi katika *'Jinsi ya Kuishi'* nilijaribu kuwasilisha mtindo mzuri wa mavazi, unaokubalika, usio na gharama, lakini wenye adabu na kuwa mtindo wa mavazi kwa wanawake Wakristo kuvaa, ikiwa wangechagua kufanya hivyo. Nilijaribu, labda bila ukamilifu, kuelezea hilo. Vazi linapaswa

kufikia chini kidogo ya kiatu, lakini linapaswa kuwa fupi kiasi ya kutosha kutokokota uchafu wa barabarani, na bila kuinuliwa kwa mkono.' Baadhi wamedai kwamba kuwa juu ya buti, nilimaanisha juu ya buti kama zile wavaazo wanaume. Lakini nilipoandika 'juu ya kiatu,' nilikusudia kueleweka kuwa juu ya buti, au kiatu, kinachovaliwa na wanawake. Laiti ningewaza kuwa ningeweza kueleweka vibaya, hakika ningeandika kwa kina zaidi. Kama ingekuwa desturi kwa wanawake kuvaa buti zenye urefu ulio wa juu kama wanaume, ningeelewa juu ya udhuru huu wa kutosha kuhusiana na mada hii. Nadhani lugha iliyotumika sasa i wazi, na hakuna haja kwa yeyote kupata mkanganyiko. Tafadhali soma tena: "Vazi linapaswa kufikia chini ya kiatu." Sasa angalia vigezo: 'Lakini linapaswa kuwa fupi kiasi cha kutoburuza chini, kutofagia uchafu wa barabara, na bila kuinuliwa kwa mkono. Nguo fupi zaidi kuliko hii itakuwa sahihi, inayofaa, na yenye afya kwa wanawake wakati wa kufanya kazi zao za nyumbani, na haswa kwa wale ambao wanalazimika kufanya kazi za nje' {1T 462.4}

"Sioni kama kuna kisingizio kwa mtu mwelewa kupata mkanganyiko na kupotosha maana yangu. Kuhusu urefu wa vazi, kama ningekuwa namaanisha kiatu chenye urefu wa juu kiasi cha kufikia karibu na goti, ningekuwa na haja gani ya kuongeza," lakini [vazi] linapaswa kuwa fupi kiasi cha kutoburuza chini na kusafisha uchafu wa barabarani, bila kuinuliwa kwa mkono? Ikiwa buti zenye urefu za wa juu za wanaume ndio zingekuwa zimekusudiwa, nguo hiyo ingekuwa fupi vya kutosha kujiweka huru na uchafu wa barabara bila kunyanyuliwa juu, na ingekuwa fupi kiasi cha kutosha kwa majukumu yote ya ufanyaji kazi. Taarifa zimesambazwa kwamba 'dada White amevaa mtindo wa vazi la Amerika-American Costume,' na kwamba mtindo huu wa mavazi kwa ujumla unakubaliwa na huvaliwa na akina dada huko Battle Creek. Nimekumbushwa hapa kwamba kuna msemo unasema 'uwongo utazunguka ulimwenguni wakati ambapo Ukweli unajitayarisha kuvaa viatu vyake.' Dada mmoja aliniambia vikali kwamba alikuwa amepokea wazo kwamba mavazi ya Amerika yangeigwa na akina dada wanaotunza Sabato, na kwamba ikiwa mtindo huo wa mavazi utatekelezwa/utalazimishwa, yeye asingekubaliana nao, kwani akili yake isingemruhusu kuvaa vazi kama hilo.{1T 463.1}

"Kuhusiana na kuvaa kwangu nguo fupi, ningesema, nina nguo moja tu fupi, ambayo ufupi wake si zaidi ya kimo cha kidole kimoja kwa ufupi kwa kulinganisha na mavazi nivaayo siku zote. Nimevaa mavazi haya mafupi mara kwa mara. Katika msimu wa baridi niliinuka mapema, na kuvaa vazi langu fupi, ambalo halikuhitaji kuinuliwa kwa mikono yangu ili kulitoa katika theluji, nilitembea kwa kasi kutoka maili moja hadi mbili kabla ya kifungua kinywa. Nimelivaa mara kadhaa na kwenda nalo ofisini, ninapolazimika kutembea katikati ya theluji nyepesi, au wakati kukiwa na mvua nyingi au matope. Kina dada wanne au watano wa kanisa la Battle Creek wamejiandalia mavazi mafupi

ya kuvaa wanapofua nguo na kusafisha nyumba. Gauni fupi halijavaliwa katika mitaa ya jiji la Battle Creek, na halijawahi kuvaliwa katika mkutano. Maoni yangu yalitumika katika kurekebisha mtindo wa sasa, mavazi marefu yaliyokithiri, yanayoburuza chini, na pia kurekebisha mavazi mafupi sana, ambayo yako chini kidogo tu ya magoti, ambayo huvaliwa na tabaka fulani. Nilioneshwa kwamba tunapaswa kuachana na msimamo mkali unapopilitiza pande zote mbili, yaani  vazifupi sana na refu sana. Kwa kuvaa mavazi yanayofikia juu ya buti za wanawake za gaiter, basi tutaepuka maovu ya mavazi marefu yaliyokithiri, na pia tutaepuka maovu na sifa mbaya ya mavazi mafupi sana. {1T 464.1}

*Mfano wa buti za mabinti, wanaume, na gauni fupi miaka ya1800*





"Ningewashauri wale ambao wanajiandalia vazi fupi kwa madhumuni ya kufanya kazi kuzingatia muonekano na unadhifu katika kuliandaa. Waliandae vazi hili katika utaratibu ulio mzuri, litoshe umbo vizuri. Hata ikiwa ni vazi la kazi, ni vyema lipendeze, nalo linapaswa kutengenezwa na kukatwa kwa mpangilio au Pateni nzuri. Kina dada wanapokuwa katika kazi yao hawapaswi kuvaa mavazi ambayo yatawafanya waonekane kama sanamu za kuwatisha ndege watoke kwenye mahindi au nafaka shambani. Waume na watoto zao, wanavutiwa/wanapendezwa  kuwaona wakiwa katika mavazi yanayofaa na yenye uzuri kuliko ilivyo kwamba wageni tu ndiyo wanafikiriwa kuwa wale ambao wanapaswa kuwaona wakiwa wamependeza. Wake wengine na akina mama hudhani kwamba muonekano wao sio jambo la kuzingatia sana wanapokuwa katika kazi au wanapokuwa tu mbele ya macho ya waume na watoto wao, ila wanazingatia sana uvaaji wao mbele ya wale wasio na madai maalum sana kwao. Je heshima, hadhi na upendo wa mume na watoto si ya kuthaminiwa sana kuliko mgeni na watu wengine? Furaha ya mume na watoto inapaswa kuwa takatifu zaidi kwa kila mke na mama kuliko ile ya watu baki, wageni, marafiki na watu wengine. Kina dada Wakristo hawapaswi wakati

wowote kuvaa mavazi yenye gharama kubwa kupindukia, lakini wakati wote wanapaswa kuvaa vizuri, kwa adabu, staha, unadhifu na utaratibu kadri kazi yao itakavyowaruhusu. "{1T 464.2}

Mavazi yaliyoelezwa hapo juu tunaamini yanastahili jina la mavazi mafupi ya matengenezo. Yamepitishwa katika Taasisi ya Matengenezo ya Afya ya Magharibi na na baadhi ya akina dada huko Battle Creek na maeneo mengine ambayo jambo hilo limeelezwa vizuri kwa watu. Kinyume kabisa na mavazi haya ya adabu ni lile lijulikanalo kama vazi kimarekani, linalofanana kabisa na mavazi ya wanaume. Inajumuisha vest, suruali, na mavazi yanayofanana na kanzu na kufikia karibu nusu kutoka kwenye nyonga hadi goti. Mavazi haya nimeyapinga, kutokana na yale ambayo nimeoneshwa kuwa yanapatana na Neno la MUNGU; wakati mengine nimeyapendekeza kuwa yenye kustahi, adabu, yasiyosumbua, rahisi na yenye afya (Enzi hizo mavazi mafupi yalikuwa juu ya kifundo cha mguu, au 20 sentimeta hivi kutoka kwenye ardhi). {1T 465.1}

Sababu nyingine ambayo ninatoa kama udhuru wa kutilia maanani tena mada ya mavazi ni kwamba hakuna hata dada mmoja kati ya ishirini (1/20) aliyekiri kuamini Shuhuda kwa mdomo wake, aliyechukua hatua ya kufanya matengenezo ya mavazi. Inaweza kusemekana kwamba Dada White kwa ujumla huvaa nguo ndefu zaidi hadharani kuliko mavazi aliyoyapendekeza kwa wengine. Kwa hili najibu, ninapotembelea mahali pa kuongea na watu ambapo mada hii ni mpya, na watu wanaiangalia kwa chuki, nadhani ni bora kuwa mwangalifu ili nisizibe masikio ya watu kwa kuvaa mavazi ambayo yatakuwa mabaya kwao. Lakini baada ya kuleta mada mbele yao na kuelezea msimamo wangu kikamilifu, basi mimi huja mbele zao katika mavazi ya matengenezo, yanayoonesha mafundisho yangu. {1T 465.2}

Kuhusu suala la kuvaa gauni refu la hoops linalobana kiuno kwa kulinganisha na hili vazi la matengenezo, hili la pili lipo mbele kabisa ya hilo. Haliwezi kuwa msaada kwao, na hawatarubuniwa kwa hilo. Hata hivyo si muda tena wa kuzungumza juu ya kuvaa gauni hizo za hoops, ziwe kubwa au ndogo. Msimamo wangu juu ya swali hilo ni vile ambavyo umekuwa kabla ya hapo, na natumai kutowajibika kwa kile wengine wanaweza kusema juu ya mada hii, au kwa msingi inayofuatwa na wale waovaa gauni hizo. Ninapinga kupotoshwa kwa mazungumzo yangu ya faragha juu ya mada hii, na ninaomba kwamba kile nilichoandika na kuchapisha kizingatiwe kama msimamo wangu. {1T 465.3}

# SURA YA 84

# WACHUNGAJI WETU

Katika njozi niliyopewa huko Rochester, New York, Desemba 25, 1865, nilioneshwa kuwa kazi nzito na ya wakfu sana iko mbele yetu. Umuhimu na ukubwa wake hautambuliwi. Nilipotazama kutokujali ambako kulikuwa wazi kila mahali kwa wachungaji na washiriki nilishtuka. Ilionekana kuwa na kupooza katika kusudi la Ukweli wa sasa. Kazi ya MUNGU ilionekana kama imesimama kabisa. Wachungaji na washiriki hawajajiandaa kwa nyakati ambazo wanaishi, na karibu wote wanaodai kuuamini Ukweli wa sasa hawajajiandaa kuelewa kazi ya maandalizi kwa wakati huu. Katika hali yao ya sasa ya tamaa za ukuu wa kidunia, na ukosefu wao wa kujitoa wakfu kwa MUNGU, hali yao ya kujitolea kwa ubinafsi, haiwafanyi kufaa kabisa kupokea mvua ya masika na baada ya kufanya yote, kusimama dhidi ya hasira ya Shetani, ambaye kwa mavumbuzi yake atasababisha wao kuharibikiwa na imani yao, akifunga juu yao udanganyifu wa kujipendeza na kujidanganya wenyewe. Wanafikiri wako sawa wakati wote, na huku wamekosea. {1T 466.1}

Wachungaji na washiriki lazima wafanye maendeleo makubwa katika kazi ya matengenezo. Wanapaswa kuanza bila kuchelewa kurekebisha tabia zao mbaya za kula, kunywa, kuvaa na kufanya kazi. Niliona kwamba wachungaji wengi hawajazinduka juu ya mada hii muhimu. Hawapo wote mahali ambapo MUNGU angewataka wawepo. Matokeo yake ni kwamba, wengine wanaweza kuonesha matunda kidogo tu ya kazi zao. Wachungaji wanapaswa kuwa mifano kwa kundi la MUNGU. Lakini hawako salama kutoka katika mitego ya Shetani. Hao ndio wale ambao adui atatafuta kuwanasa. Ikiwa anaweza kufaulu kumrubuni mchungaji mmoja kutoka katika usalama wa mwili, na kwa kufanya hivyo kugeuza mawazo yake kutoka kazini, au kumdanganya kwa kuzingatia hali yake ya kweli mbele za MUNGU, atakuwa ametimiza mengi. {1T 466.2}

Niliona kwamba kusudi la MUNGU halikuendelea kama linavyostahili. Wachungaji wanashindwa kuchukua kazi kwa nguvu hiyo, kujitolea, na uamuni, na uvumilivu ambao umuhimu wa kazi unadai. Wanaye adui aliye macho wa kushindana naye, ambaye bidii na uvumilivu havichoki. Jitihada dhaifu ya wachungaji na washiriki haiwezi kulinganishwa na ile ya mpinzani wao, Shetani. Kwa upande mmoja kuna wahudumu/wachungaji wanaopigania haki na wana msaada wa MUNGU na malaika watakatifu. Hawa wanapaswa kuwa hodari na mashujaa, na kujitolea kabisa kwa kazi ambayo wanahusika nayo, bila maslahi tofauti. Hawapaswi kufungwa-fungwa na vitu vya maisha haya, ili wampendeze Yeye aliyewachagua kuwa askari. {1T 467.1}

Kwenye upande wa pili ni Shetani na malaika zake, pamoja na mawakala wake wote duniani, ambao hufanya kila juhudi na kutumia kila mbinu/chombo kuendeleza makosa, uovu na mabaya, na kufunika hila na udhaifu wao kwa mavazi ya kupendeza. Hapa kuna ubinafsi, uchoyo, unafiki, na kila aina ya udanganyifu, Shetani anajivika kwa vazi la ukweli dhahiri na uadilifu, na kushangilia katika kufanikiwa kwake, hata na wachungaji na watu wanaodai kuelewa hila zake. Kadri wanavyojiweka mbali na Kristo Kiongozi wao mkuu, ndivyo wanavyozidi kupoteza mfanano wa tabia Yake, pia kadri wanavyozidi kufanana kimaisha na tabia na watumishi wa adui yao mkubwa, ndivyo adui anavyokuwa na ufikiaji mkubwa kwao, na hivyo kuwapata kuwa raia wake. Wakati wanakiri kuwa ni watumishi wa Kristo, wao ni watumwa wa dhambi. Wachungaji wengine wameelekeza sana akili zao kwenye mishahara wanayopokea. Wanafanya kazi kwa ajili ya mshahara na kushindwa kuuona utakatifu na umuhimu wa kazi hiyo. {1T 467.2}

Wengine huwa wazembe na wapuuziaji katika kazi yao; hufaulu hatua za mwanzo, lakini ni dhaifu na wasio na mafanikio katika juhudi zao. Mioyo yao haipo katika kazi. Nadharia ya Ukweli iko wazi. Wengi wao hawakuwa na sehemu katika kuutafuta Ukweli huu kwa kujifunza kwa bidii na maombi ya dhati, na hawajui chochote juu ya thamani yake kwa kulazimika kulinda nyadhifa zao dhidi ya upinzani wa maadui zao. Hawaoni umuhimu wa kuhifadhi roho ya kujiweka wakfu kikamilifu kwa kazi. Masilahi yao yamegawanywa miongoni mwo wenyewe na kazi. {1T 467.3}

Niliona kwamba kabla kazi ya MUNGU haijawa na maendeleo yoyote dhahiri, wachungaji lazima waongoke. Wakiongoka hawataweka sana mawazo yao kwenye mishahara na wataipa thamani ya juu sana kazi muhimu, takatifu, na nzito ambayo wamekubali kutoka kwa MUNGU kuifanya, na ambayo Yeye Anawataka waifanye kwa uaminifu na vizuri, kama wale ambao lazima watoe hesabu kamili. Kumbukumbu thabiti ya kazi zao zote huchukuliwa kila siku na malaika wachukuao kumbukumbu. Matendo yao yote, na hata malengo na

makusudi ya moyo, hufunuliwa kwa uaminifu. Hakuna kitu kinachofichika mbele ya macho Yake Yeye aonaye yote tutendayo. Wale ambao wametoa nguvu zao zote kwa ajili ya kazi ya MUNGU, na ambao wamejitosa na kuwekeza kitu, watahisi kuwa kazi ya MUNGU ni sehemu yao, na hawatafanya kazi kwa ajili ya ujira tu. Hawatakuwa watumishi watakao kuonekana na kutafuta furaha yao wenyewe, bali watajitakasa nafsi zao na nia zao kwa kazi hii adhimu. {1T 468.1}

Wengine katika kazi zao za kawaida makanisani wako katika hatari ya kufanya makosa kutokana na ukosefu wa kushugulikia mambo kwa kinagaubaga-kikamilifu. Ni kwa masilahi yao binafsi na ya kazi ya MUNGU kwamba wanapaswa kujichunguza kwa ukaribu, kujaribu nia zao, na kuwa na hakika ya kujitenga na ubinafsi. Wanapaswa kuangalia ili wasije, wakajikuta wanahubiri Ukweli mnyoofu kwa wengine, ili hali wao wanashinda kuishi kwa kanuni ile ile, na kumruhusu Shetani aweke mbadala wa kitu kingine kabisa kwa kazi inayopaswa kufanywa kwa kina katika kuchunguza moyo. Wanapaswa kuwa wakamilifu wao wenyewe na kwa kazi ya MUNGU wasije wakafanya kazi kwa ajili ya mshahara na kupoteza mtazamo wa tabia muhimu na iliyoinuliwa ya kazi. Hawapaswi kuruhusu ubinafsi/umimi kutawala badala ya Yesu, na wanapaswa kuwa wangalifu kwa kutomwambia mwenye dhambi ndani ya Sayuni, Itakuwa heri kwako, wakati MUNGU ametamka laana juu yake. {1T 468.2}

Wachungaji lazima waamke na kudhihirisha maisha, bidii, na kujitolea mambo ambayo kwa muda mrefu wamekuwa karibu wageni kwayo kwa sababu wameshindwa kutembea na MUNGU. Kazi ya MUNGU katika maeneo mengi haiendelei. Kazi ya kuchunguza na matengenezo ya roho inahitajika. Watu wamelemewa na ulafi na ulevi na masumbufu ya maisha haya. Wanazidi kuzama ndani na ndani zaidi ya pilikapilika ya shuguli za dunia hii. Wana hamasa ya kupata faida. Mambo ya kiroho na kujitoa wakfu yamekuwa nadra. Roho ambayo inatawala ni ya kufanya kazi, ili kujilimbikiza, na kuongeza zaidi katika kile ambacho tayari wanamiliki. "Je! Mwisho wa mambo haya utakuwa nini?" ulikuwa mzigo wa uchunguzi wangu. {1T 469.1}

Mikutano ya Konferensi haijatimiza faida yoyote ya kudumu. Mara nyingi wachungaji na washiriki huleta bidhaa zao kwenye mikusanyiko hii mikubwa, na Ukweli unaozungumzwa kutoka kwenye mimbari unashindwa kufurahisha moyo. Upanga wa Roho, Neno la MUNGU, linashindwa kufanya kazi iliyokusudiwa; linaangukia wasikilizaji likiwa butu kabisa. Kazi ya MUNGU iliyotakaswa huwa na uhusiano wa karibu sana na vitu vilivyo vya kawaida. {1T 469.2}

Wachungaji lazima waongoke kabla ya kuwaimarisha ndugu zao. Hawapaswi kuhubiri wenyewe, bali Kristo na haki Yake. Matengenezo yanahitajika kati ya

watu, lakini yanapaswa kwanza kuanza kazi yake ya utakaso kwa wachungaji. Wao ni walinzi juu ya kuta za Sayuni, kupaza sauti ya onyo kwa wasiojali, wasiotahayari; pia kuonesha hatima ya mnafiki huko Sayuni. Ilionekana kwangu kuwa baadhi ya wahudumu walikuwa wamesahau kuwa Shetani alikuwa bado yuko hai, adui asiyechoka, mwenye bidii, na mjanja kama zamani; kwamba alikuwa bado akitafuta kushawishi roho ili kuzitoa katika njia ya haki. {1T 469.3}

Sehemu moja muhimu ya kazi ya huduma na uchungaji ni kuwasilisha kwa watu kwa uaminifu matengenezo ya afya kwani yanahusiana na ujumbe wa malaika wa tatu kama sehemu ya kazi hiyo. Hawapaswi kuacha kuzingatia wao wenyewe, na wanapaswa kuihimiza kwa wale wote wanaodai kuamini Ukweli. {1T 469.4}

Wachungaji hawapaswi kuwa na masilahi tofauti kando na kazi kubwa ya kuongoza roho katika Kweli. Nguvu zao zote zinahitajika hapa. Hawapaswi kushiriki biashara, kuuza/machinga, au biashara yoyote kando na kazi hii kubwa. Agizo zito alilopewa Timotheo lina uzito sawa juu yao, likiwawekea majukumu mazito na majukumu ya kutisha zaidi. "Nakuagiza mbele za MUNGU na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa Kwake na kwa ufalme wake; Lihubiri Neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho." "Lakini wewe kesha katika mambo yote, vumilia mateso, fanya kazi ya mwinjili, timiza huduma yako kikamilifu." {1T 470.1}

Tabia mbaya za maisha zimepunguza hisia zetu za akili na mwili, na nguvu zote tunazoweza kupata kwa kuishi sawa na kujiweka katika uhusiano bora zaidi wa kiafya na maisha vinapaswa kutolewa bila kujibakiza kwa kazi ambayo MUNGU ametupatia. Hatuwezi kumudu kutumia nguvu chache,dhaifu ,zenye ulemavu tulizonazo ili kuhudumia meza au kuchanganya na bidhaa za kuuza, katika kazi ambayo MUNGU ametupatia. Kila kitivo cha akili na mwili sasa kinahitajika vinahitajika. Kazi ya MUNGU inahitaji hili, na hakuna biashara tofauti inayoweza kuhusishwa kando na kazi hii kubwa bila kuchukua muda na nguvu ya akili na mwili, na hivyo kupunguza nguvu na uwajibikaji wetu katika kazi ya MUNGU. Wachungaji ambao hufanya hivi hawatakuwa na wakati wote kwa ajili ya kutafakari na kuomba, na utimamu wote wa nguvu na akili, ili waweze kuelewa changamoto za wale wanaohitaji msaada, na kuwa tayari kwa"wakati unaofaa na wakati usiofaa. "Neno linalozungumzwa kwa wakati unaofaa linaweza kuokoa roho duni, yenye makosa, yenye mashaka na yenye kuzirai. Paulo alimhimiza Timotheo: "Tafakari juu ya mambo haya; jitoe kikamilifu kwao; ili faida yako ionekane kwa wote." {1T 470.2}

Katika agizo la Kristo kwa wanafunzi Wake anawaambia: "Chochote mtakachofunga duniani kitafungwa mbinguni; na chochote mtakachofungua duniani kitafunguliwa mbinguni." Ikiwa huu ni wajibu wa kuogofya wa kazi ya watumishi wa MUNGU, ni muhimu kiasi gani kujitoa kikamilifu na kuzichunga roho kama wale ambao watapaswa kutoa hesabu. Je! Masilahi yoyote tofauti au ya ubinafsi yanapaswa kuutoa moyo katika kazi? Wachungaji wengine hushinda katika nyumba zao, na kutoka siku ya Sabato, kisha hurudi na kumaliza nguvu zao katika kilimo au kuhudumia masuala ya nyumbani. Wanajishughulisha kwa wiki nzima na shuguli zao, na kisha hutumia nguvu zao dhaifu zilizosalia katika kumtumikia MUNGU (weekend). Lakini juhudi dhaifu kama hizo hazikubaliki Kwake. Hawana nguvu ya kiakili au ya kimwili iliyobakia. Juhudi zao zilizobakia ni dhaifu sana. Lakini baada ya kujifungafunga na kunaswa katika siku zote za kazi za juma na wasiwasi na mashaka ya maisha haya, hawafai kabisa kwa kazi ya MUNGU iliyo ya juu, takatifu, na muhimu. Hatima ya roho hutegemea kazi waifanyayo na maamuzi wanayochukua. Ni muhimu kiasi gani kwamba wawe na kiasi katika kila jambo, siyo tu katika kula kwao, bali katika kazi yao, ili nguvu zao zisidhoofu bali zitumike kwa ajili ya wito wao mtakatifu. {1T 471.1}

Kosa kubwa limefanywa na baadhi ya wanaodai kuukubali Ukweli wa sasa, kwa kuingiza bidhaa za kuuza katika mfuatano wa mikutano kadhaa ya injili na kwa ukengeufu wa wazo lao la biashara kuzivuta akili zote zitoke nje ya mikutano. Endapo Kristo angekuwa hapa duniani, angewafukuza hawa wauzaji na wafanyabiashara, iwe ni wachungaji au walei, kwa mijeledi au kamba, kama vile alivyoingia hekaluni zamani "Kuwafukuza wote waliouza na kununua katika hekalu. Na akazipindua meza zao wanaobadilisha fedha, na viti vyao waliouza njiwa. Akawaambia, Imeandikwa, Nyumba Yangu itaitwa nyumba ya sala; lakini mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi. Machinga au wajasiliamali hawa wangeweza kuomba kama kisingizio kwamba bidhaa walizokuwa wanaziuza zilikuwa kwa ajili ya kafara za dhabihu. Lakini lengo lao lilikuwa kupata faida, kupata fedha za kujilimbikizia/kujirundikia wenyewe. {1T 471.2}

Nilioneshwa kuwa ikiwa uwezo wa kimaadili na kiakili usingekuwa umefunikwa na tabia na mienendo mibaya ya maisha, wachungaji na washiriki wangekuwa wepesi kugundua matokeo mabaya ya kuchanganya vitu vitakatifu na vile vya kawaida. Wachungaji wamesimama kwenye jukwaa na kuhubiri maneno mazito sana, na kisha kwa kuanzisha biashara, na kuchukua nafasi ya wauzaji, hata katika nyumba ya MUNGU, wamegeuza akili za wasikilizaji wao kutoka kwenye mguso wa ujumbe waliopokea, na kuharibu matunda ya kazi yao. Kama hizi hisia nyeti zisingekuwa zimedhoofishwa, wangekuwa na utambuzi kujua kwamba walikuwa wakivishusha vitu vitakatifu katika kiwango sawa na kile cha vitu vya kawaida. Mzigo wa kuuza machapisho yetu haupaswi kuwa juu ya wachungaji wanaofanya kazi kwa Neno na mafundisho ya imani. Wakati na nguvu zao zinapaswa kuwekwa akiba, ili juhudi zao ziwe kamili katika mfululizo

wa mikutano. Wakati na nguvu zao hazipaswi kuvutwa kuuza vitabu vyetu wakati vinaweza kuletwa mbele ya umma na wale ambao hawana mzigo wa kuhubiri Neno. Katika kuingia katika maeneo mapya inaweza kuwa muhimu kwa mchungaji kuchukua machapisho na kutoa ili kuuza kwa watu, na inaweza kuwa muhimu katika hali zingine pia kuuza vitabu na kufanya biashara kwa ajili ya ofisi ya uchapishaji. Lakini kazi kama hiyo inapaswa kuepukwa ikiwa inaweza kufanywa na watu wengine. {1T 472.1}

Wachungaji wana yote ambayo wanapaswa kufanya kuhubiri Neno, na baada ya kuwasisitizia watu Ukweli adhimu, wanapaswa kudumisha heshima ya unyenyekevu kama wahubiri wa ukweli uliotukuka na kama wawakilishi wa ukweli uliowasilishwa kwa watu. Baada ya juhudi zao za kazi wanahitaji kupumzika. Hata kuuza vitabu juu ya Ukweli wa sasa ni usumbufu, uchovu kwa akili, na uchovu kwa mwili. Ikiwa kuna wale ambao bado wana nguvu ya akiba na wanaweza kuzishughulisha bila kujijeruhi wenyewe, kuna kazi muhimu kwao kufanya, na ndiyo inaanza tu wakati wanapomaliza kuusema Ukweli kwa watu. Halafu huja kuhubiri kwa mfano, uangalifu, utafutaji wa kutenda mema kwa wengine, mazungumzo, na kutembelea watu nyumba kwa nyumba wanapokota moto kwenye sebule zao, kuingia katika hali ya akili na hali ya kiroho ya wale waliosikiliza hubiri kutoka katika midomo; wakimsihi huyu, wakimkaripia yule, wakimkemea huyu, na kuwafariji waliotaabika, wanaoteseka, wenye huzuni na waliokata tamaa. Akili inapaswa kuwa huru kutoka kwa uchovu iwezekanavyo ili waweze kuwa watu wenye utayari, wenye kutumika"papo kwa msimu, nje ya msimu." Wanapaswa kutii agizo lilitolewa na Paulo kwa Timotheo: "Tafakari juu ya mambo haya; jitoe mwenyewe kabisa." {1T 472.2}

Wajibu wa kazi upo kidogo juu ya wengine. Wanahisi kwamba baada ya kutoka kwenye mimbari kazi yao imekamilika. Ni mzigo kutembelea, ni mzigo kuzungumza; na watu ambao kwa kweli wanatamani kupata mema yote kutoka kwao, na ambao wanataka kusikia na kujifunza kwamba wanaweza kuona vitu vyote wazi, hawanufaiki na kuridhika. Wachungaji wanajitoa udhuru kwa sababu wamechoka, na bado wengine hutumia nguvu zao za thamani na kutumia muda wao katika kazi ambayo mwingine anaweza kufanya kama wao. Wanapaswa kuhifadhi nguvu ya maadili na ya mwili ili kama watendakazi waaminifu wa MUNGU wapate kutoa ushahidi kamili wa huduma yao. {1T 473.1}

Katika kila sehemu muhimu kunapaswa kuwa na hazina ya machapisho. Na mtu ambaye anathamini na kupenda Kweli anapaswa kuonesha nia ya kuweka vitabu hivi mikononi mwa wote watakaosoma. Mavuno ni mengi, lakini watendakazi ni wachache, na watendakazi wachache wenye uzoefu sasa katika shamba wana kila kitu cha kufanya ili kufanya kazi kwa Neno na mafundisho ya imani. Watu watatokea ambao wanadai kwamba MUNGU amewawekea mzigo

wa kufundisha Ukweli kwa wengine. Wote hawa wanapaswa kuthibitishwa na kujaribiwa. Hawapaswi kuondolewa kutoka kwa shuguli zote, wala hawapaswi kuinuliwa katika nafasi za uwajibikaji mara moja; lakini wanapaswa kutiwa moyo ikiwa wanastahili kutiwa moyo, kutoa ushahidi kamili wa huduma yao. Haiwezi kuwa njia bora kwa watu kama hao kufuata, na kuingia katika kazi za watu wengine. Hebu wafanye kazi kwanza na mtu mwenye uzoefu na hekima, naye hivi karibuni anaweza kuona ikiwa wana uwezo wa kutoa ushawishi ambao utaokoa. Wahubiri wachanga ambao hawajawahi kufanya kazi ya kuchakaza au kuchosha, au kuhisi rasimu juu ya nguvu zao za kiakili na za mwili, hawapaswi kutiwa moyo kutumaini msaada bila kufanya kazi ya mikono kwa kujitolea ili wajikimu kimaisha, kwani hii itawaumiza tu na itakuwa chambo cha kushawishi watu kushiriki katika kazi ambayo hawatambui chochote juu ya mzigo wake au jukumu linalowekwa juu ya wahudumu waliochaguliwa na MUNGU (Kichujio cha watumishi wa mshahara). Hawa watajisikia kuwa na uwezo wa kufundisha wengine wakati ndio tu wamejifunza kanuni za kwanza za utumishi. {1T 473.2}

Wengi wanaokiri Ukweli hawajatakaswa nao hawajajaliwa hekima; hawaongozwi na kufundishwa na MUNGU. Watu wa MUNGU, kama jambo la jumla, wana mawazo ya udunia na wameacha unyenyekevu wa injili. Hii ndio sababu ya ukosefu mkubwa wa utambuzi wa kiroho katika mwenendo ambao wamefuata kuelekea kwa wahudumu. Ikiwa mchungaji anahubiri kwa uhuru, wengine watamsifu mbele ya uso wake. Badala ya kukaa juu ya Kweli alizotamka, na kuboresha juu ya hizi, na hivyo kujionesha kuwa wasikiaji wasio wasahaulifu, washiriki hawa wanamwinua kwa kurejelea kile alichofanya. Wanakaa juu ya sifa za chombo duni, lakini wanamsahau Kristo ambaye alitumia hicho chombo. Tangu anguko la Shetani, ambaye wakati mmoja alikuwa malaika aliyeinuliwa katika utukufu, wachungaji wameanguka kupitia kuinuliwa. Watunza Sabato wasio na hekima wamempendeza Shetani vizuri kwa kuwasifu wachungaji/wahudumu wao. Laiti wangelijua kuwa walikuwa wakimsaidia Shetani katika kazi yake, hakika wangepata mshtuko na wangegundua kile walichokuwa wakifanya. Walipofushwa, hawakuwahi kusimama katika shauri la MUNGU. Ninainua sauti yangu kama tahadhari dhidi ya kuwasifu wachungaji, kujikomba kwa kutia chumvi kwao, kuwapa sifa za uongo, kujipendekeza na kuwabembeleza wachungaji kwa kuwapaka mafuta kwa chupa ya mgongo. Nimeona ubaya, ubaya wa kutisha, wa hili. Kamwe, kamwe usiseme neno moja la kuwasifu wahudumu mbele ya nyuso zao. Wewe mtukuze MUNGU. Mheshimu mhudumu mwaminifu kila wakati, tambua mizigo yake na uipunguze ikiwa unaweza; lakini usitie chumvi kwa kumsifu, kwa kumpa kichwa (usimbembeleze), kwa maana Shetani anasimama tayari kwenye mnara wake kufanya kazi ya aina hiyo mwenyewe, bila ya wewe kumsaidia. {1T 474.1}

Wachungaji hawapaswi kusifu kwa kutia chumvi, kusifu kwa udanganyifu au kuwapendelea watu. Kumekuwa na hatari kubwa ya kukosea hapa, na bado ipo, ya kufanya tofauti kidogo katika kuhusiana namatajiri, au kuwabembeleza kwa umakini maalum, ikiwa sio kwa maneno. Kuna hatari ya "kupendezwa na watu, kuonyesha unawathamini na kuwaona wako juu sana" kwa sababu ya faida, binafsi inayopatikana, lakini kwa kufanya hivyo masilahi yao ya milele yako hatarini. Mchungaji anaweza kuwa kipenzi maalum cha mtu tajiri, na tajiri huyu anaweza kuwa mkarimu na huru kwa mahusiano naye; hii humridhisha mchungaji, na yeye pia humwaga sifa juu ya fadhili za mfadhili wake. Jina lake linaweza kuinuliwa kwa kuonekana kwenye chapisho, na bado mfadhili huyo huria anaweza kuwa hafai kabisa sifa aliyopewa. Ukarimu wake haukutokana na kanuni ya kina moyoni ambayo inaishi kutenda mema na mali zake, kuendeleza kazi ya MUNGU kwa sababu alilithamini hili kusudi, bali ulitoka katika nia ya ubinafsi, hamu ya kufikiriwa kuwa yeye ni mkarimu. Anaweza kuwa ametoa kutoka kwa mhemko lakini ukarimu wake hauna kina cha kanuni. Anaweza kusukumwa na kusikiliza Ukweli wenye kuchochea ambao kwa muda huo ulifungua kamba zake za pochi/mkoba wake; lakini, baada ya haya yote, ukarimu wake hauna nia ya kina bali ni hisia za muda. Anatoa kwa kushtukiza kama misuli inavyoshtuka mara zingine; mkoba wake unafunguliwa kwa kusthtukizwa hapa na pale na anazifungia pesa zake tena kibindoni kwa ghafla. Mtu huyu hastahili pongezi, kwa maana yeye kwa kila hali na neno ni mtu bahili na asipoongoka kabisa, mkoba wake na vyote vitasikia kemeo linalokausha: "Nendeni sasa, enyi matajiri, kulia na kuomboleza kwa ajili ya huzuni zitakazo kuja juu yenu. Utajiri wako umeharibika, na mavazi yako yameliwa na nondo." Hao watazinduka mwishowe kutoka kwenye udanganyifu wa kutisha. Wale ambao walisifu ukarimu wao maonesho na kushtuki, walimsaidia Shetani kuwadanganya na kuwafanya wafikiri kwamba walikuwa wakarimu sana, wenye kujitoa mhanga sana, wakati hawakujua kanuni za kwanza za ukarimu au kujitolea. {1T 475.1}

Wanaume na wanawake wengine hujifanya wenyewe kuamini kwamba hawafikirii vitu vya ulimwengu huu kuwa vya thamani kubwa, lakini wanathamini Ukweli na maendeleo yake juu kuliko faida yoyote ya ulimwengu. Wengi wataamka mwishowe kugundua kuwa wamedanganywa. Labda waliwahi kuthamini Ukweli, na hazina za kidunia ukilinganisha na Ukweli ulivyoweza kuonekana kwao hauna maana; lakini baada ya muda, wakati hazina yao ya kidunia ilipoongezeka, walipunguza ibada na kujitoa wakfu. Ingawa wana mahitaji yao ya lazima ya kutosha, lakini matendo yao yote yanaonesha kuwa bado hawajaridhika kabisa. Kazi zao zinashuhudia kwamba mioyo yao imefungwa katika hazina yao ya kidunia. Kupata, kupata zaidi mali, ni kauli mbiu yao. Ili kufikia mwisho huu kila mshiriki wa familia anashiriki katika kazi yao. Hawatumii wakati wowote kwa kujitoa wakfu kwa ibada na sala. Wanafanya kazi mapema asubuhi mpaka usiku, na hata kujipatia ugonjwa.

Wanawake wagonjwa, na watoto dhaifu huinua juu bendera zao za matamanio ya uku wa mali na kutumia nguvu na uimara walio nao kufikia lengo lao, kupata zaidi kidogo, kutengeneza pesa zaidi. Wanajidaganya kwamba wanafanya hivi ili wasaidie kusudi la MUNGU. Udanganyifu wa kutisha! Shetani huangalia na kucheka kwani anajua kuwa wanauza roho na mwili kupitia tamaa yao ya kupata faida. Wanaendelea kutoa visingizio visivyo na maana daima kwa kujiuza kwa faida. Wamepofushwa na MUNGU wa ulimwengu huu. Kristo awamenunua kwa damu Yake Mwenyewe; lakini humwibia Kristo, humwibia MUNGU, hujirarua vipande vipande, na karibu kuwa watu wasionufaisha jamii (watu wa kihasara katika jamii). {1T 476.1}

Wao hutumia wakati mdogo tu kwa ajili ya uboreshaji wa akili, na wakati mdogo kwa raha ya mahusiano ya jamii na nyumbani (social life). Wana faida kidogo tu kwa mtu yeyote. Maisha yao ni makosa mabaya. Wale ambao wanajidhulumu na kujinyanyasa hivyo wanahisi kuwa njia yao ya kufanya kazi bila mapumziko ni ya kupongezwa. Wanajiangamiza kwa kazi yao kwa kuwa na ujasiri bandia. Wanaharibu hekalu la MUNGU  kwa kuendelea kukiuka sheria za mwili daima kwa kufanya kazi kupita kiasi, na bado wanafikiria ni sifa njema. Wakati MUNGU anapowataka watoe hesabu, anapotaka talanta ambazo Yeye amewapa, pamoja na riba, Je, watu hawa wanaweza kusema nini? Je, wanaweza kutoa udhuru gani? Kama wangekuwa  wapagani ambao hawajui chochote juu ya MUNGU  aliye hai, na kwa bidii yao ya ibada ya sanamu wakajitupa chini ya nvuvu kubwa na kusagwasagwa, kesi zao zingevumiliwa zaidi. Lakini walikuwa na nuru, walikuwa na onyo juu ya onyo la kuhifadhi miili yao, ambayo MUNGU  huiita kuwa ni hekalu Lake, ikiwa na hali nzuri kiafya ili waweze kumtukuza katika miili na roho zao, ambazo ni Zake. Walipuuza mafundisho ya Kristo: "Msijiwekee hazina duniani, ambapo nondo na kutu viharibupo, na ambapo wezi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, ambapo nondo wala kutu haviharibu, na ambapo wezi hawavunji wala hawaibi. Kwa maana hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwa moyo wako. " Wanaacha masumbufu ya kidunia yawashike. "Lakini wale watakao kuwa matajiri huanguka katika majaribu na mtego, na katika tamaa nyingi za upumbavu na zenye kudhuru, ambazo huwazamisha watu katika uharibifu na upotevu." Wanaabudu hazina yao ya kidunia, kama wapagani wasiojua wanavyofanya na sanamu zake. {1T 476.2}

Wengi wanadai kwamba shauku yao ya kupata faida ni kwamba wanaweza kusaidia kusudi la kazi MUNGU. Wengine huahidi kwamba watakapopata kiasi hicho, basi watafanya vizuri na kuendeleza kusudi la Ukweli wa sasa. Lakini wanapopata matarajio yao, hawako tayari kusaidia jambo hilo kuliko hapo awali. Wanaahidi tena wenyewe kuwa baada ya kununua nyumba hiyo inayotamanika au kipande cha ardhi, na kukilipia, basi watafanya kazi kubwa na mali zao kuendeleza kazi ya MUNGU. Lakini kadri matamanio ya mioyo yao

yanavyopatikana, wana tabia duni sana kuliko siku za umaskini wao kusaidia katika kuendeleza kazi ya MUNGU. "Yeye aliyepandwa kati ya miiba ndiye asikiaye Neno; na wasiwasi wa ulimwengu huu, na udanganyifu wa utajiri, hulisonga Neno, nalo likawa halizai matunda matunda." Udanganyifu wa utajiri unawaongoza, hatua kwa hatua, hadi wapoteze upendo waowote kwa Ukweli, na bado wanajidangaya wenyewe kwamba wanauamini Ukweli. Hawa wanaupenda ulimwengu na vitu vya ulimwengu, lakini upendo wa MUNGU au Ukweli haumo ndani yao. {1T 477.1}

Ili kupata pesa kidogo, wengi hupanga kwa makusudi masuala yao ya kibiashara ili iweze kuleta kazi kubwa kwa wale wanaofanya kazi nje, na kwa familia zao nyumbani. Mfupa, misuli, na ubongo hulemewa kwa kiasi kikubwa; kazi kubwa ya kufanywa iko mbele yao na kisingizio ni kwamba, lazima watimize yote tu ambayo wanaweza au kutakuwa na hasara, kitu fulani kitapotea. Kila kitu lazima kiokolewe, kwa juhudi zote au matokeo yoyote. Je! Hilo limeleta faida gani? Labda wameweza kuhifadhi riba na kuiongeza. Lakini, kwa upande mwingine, Je, wamepoteza nini? Mitaji yao ya afya, ambayo ni muhimu kwa masikini na vile vile tajiri, imekuwa ikipungua kwa kasi. Mama na watoto wametumia hazina zao mara kwa mara kwenye mfuko wao wa afya na nguvu, wakidhani kuwa matumizi mabaya sana hayawezi kumaliza mtaji wao, hadi watakaposhangaa mwishowe kukuta nguvu ya maisha imechoka. Hawana chochote cha kuchota wakati wa dharura. Utamu na furaha ya maisha imejazwa na maumivu makali na kukosa usingizi. Nguvu zote za mwili na akili vimeondoka. Mume na baba, ambao, kwa kutafuta faida, alifanya mpangilio usiofaa wa biashara yake, na inaweza kuwa na idhini kamili ya mke na mama, kwa sababu hiyo, wanaweza kumzika mama na mtoto mmoja au zaidi. Afya na maisha vilitolewa kwa upendo wa pesa. "Kwa maana kupenda fedha ni shina la mabaya yote; ambayo wakati wengine walitamani, wamepotoka kwa imani, na kujichoma kwa huzuni nyingi." {1T 478.1}

Kuna kazi kubwa inayotakiwa kutekelezwa kwa watunza Sabato. Macho yao lazima yafunguliwe na waone hali yao halisi, na wawe na bidii na watubu, la sivyo watashindwa kuishi milele. Roho ya ulimwengu imewamiliki, na wanachukuliwa mateka na nguvu za giza. Hawayatii mawaidha ya mtume Paulo: "Wala msiufuatishe namna ya ulimwengu huu; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua mapenzi ya MUNGU yaliyo mema, ya kukubalika na ukamilifu." Kwa wengi wao roho ya udunia, na tamaa na ubinafsi, vinatawala. Wale ambao wanamiliki wanatafuta masilahi yao maalum. Tajiri mwenye ubinafsi hajishughulishi na mambo ya majirani zake, isipokuwa ikiwa ni kujifunza jinsi anavyoweza kujinufaisha kwa hasara yao. Uungwana na utauwa vinatoweka, kwaajili ya kutolewa kafara kwa masilahi ya ubinafsi. Upendo wa pesa ni shina la maovu yote. Inapofusha maono na kuzuia watu kutambua majukumu yao kwa MUNGU au kwa majirani zao. {1T 478.2}

Wengine hujidai kwamba wao ni wakarimu kwa sababu wakati mwingine hutoa kwa hiari na vingi kwa wachungaji na kwa maendeleo ya ukweli. Walakini hawa wanaoitwa wakarimu wanajishughulisha kwa ubahili wana utayari wa kujipatia mali kwa kupindukia na kudhulumu. Wana mengi ya ulimwengu huu, na hili linawafungia majukumu makubwa kama mawakili wa MUNGU. Walakini, wanaposhughulika na ndugu masikini, anayehenyeka kwenye kibarua, ni wakali na wanakamua mpaka pesa ya mwisho. Kuomba upunguziwe pesa na mtu masikini anayeuza kitu, ni kuchukua urithi wa mtu masikini. Badala ya kumpendelea ndugu yake maskini kwa kununua mali yake kwa bei nzuri, tajiri mjanja,na mkali huchukua faida yote na kuongeza utajiri wake uliokusanywa tayari kwa kumpatia hasara yule mwingine (anabembeleza masikini ashushe bei, na kumnyonga mtu masiki na kuchukua urithi wake na kujisifu kwamba ni mtu mahiri sana kwenye dili/bargain). Anajipongeza mwenyewe kwa sababu ya ujanja wake, lakini kwa utajiri wake anajilundikia laana nzito na kumkwanza ndugu yake kwa kuweka kizuizi njiani mwake. Kwa ubahili wake wa kupindukia na hesabu ya tamaa ya kujipatia kwa haramu, anakata uwezo wake wa kumnufaisha na ushawishi wake wa kidini (hawezi kuamini kama Mkristo ndiye anaumiza watu hivi). Yote haya yanaishi katika kumbukumbu ya yule ndugu masikini, na sala za bidii zaidi na shuhuda dhahiri wa bidii kutoka katika midomo ya ndugu huyu tajiri havitakuwa na ushawishi zaidi ya kuhuzunisha na kuchukiza. Anamtazama ndugu huyu kama mnafiki; shina la uchungu huchipuka, ambalo watu wengi wametiwa unajisi. Maskini hawezi kusahau faida alizoporwa; wala hawezi kusahau jinsi alivyoingizwa katika maeneo magumu kwa sababu alikuwa tayari kubeba mizigo, wakati ndugu yake kanisani aliye tajiri daima alikuwa na udhuru tayari wakati wote, wa kutoweka bega lake chini ya mzigo na kuubeba. Hata hivyo maskini anaweza kujazwa sana na roho ya Kristo hata kusamehe dhuluma za ndugu yake tajiri. {1T 479.1}

Ukweli, uungwana, ukarimu usiojifikiria masilahi binafsi ni nadra sana kupatikana miongoni mwa matajiri. Katika tamaa yao ya kwa utajiri wanapuuza madai ya ubinadamu. Hawawezi kuona na kuhisi msimamo mwembamba, usiokubalika wa ndugu zao katika umaskini, ambao labda wamefanya bidii kama wao wenyewe. Kama Kaini wanasema: "Je! Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" "Nimefanya kazi kwa bidii kwa kile nilicho nacho, lazima nikishikilie." Badala ya kuomba, "Nisaidie kuhisi ole wa kaka yangu," masomo yao ya mara kwa mara ni kusahau kuwa ana ole wowote,au madai yoyote juu ya huruma yao au ukarimu. {1T 480.1}

Watunza Sabato wengi ambao ni matajiri wana hatia ya kuuponda uso wa maskini. Je! watu kama hao wanafikiri kuwa MUNGU haangalii vitendo vyao vya dhuluma? Ikiwa macho yao yangeweza kufunguliwa wangeona malaika akiwafuata kokote waendako, akiweka kumbukumbu ya uaminifu ya matendo

yao yote katika familia zao na mahali pao pa kazi. Shahidi wa Kweli Yuko kwenye njia yao, akitangaza: "Nayajua matendo yako." Nilipoona roho hii ya ulaghai, ya kupita kiasi, ubahili, tamaa ya kupora kwa wengine, hata kati ya wengine wanaojiita watunza Sabato, nililia kwa uchungu wa roho. Uovu huu mkubwa, laana hii mbaya, inazunguka kwa baadhi ya Israeli wa MUNGU katika siku hizi za mwisho, na kuwafanya kuwa chukizo hata kwa watu wasioamini wenye roho nzuri. Hawa ndio watu wanaodai kuwa wanangojea kuja kwa Bwana. {1T 480.2}

Kuna tabaka la ndugu maskini ambao hawako huru kutoka kwa majaribu. Wao ni wasimamizi duni, hawana busara katika maamuzi, wanataka kupata mali bila kusubiri mchakato polepole wa kudumu kwa kufanya kazi kwa bidii. Wengine wako na haraka ya kuboresha hali zao kiasi kiasi kwamba wanajihusisha na biashara mbali mbali bila kushauriana na watu wenye busara na uzoefu. Matarajio yao hutimizwa kwa nadra; badala ya kupata, hupoteza, halafu huja majaribu na tabia ya kuwaonea wivu matajiri. Wanataka sana kufaidika na utajiri wa ndugu zao, na wanahisi kujaribiwa kwa sababu hawana. Lakini hawastahili hawa kupata msaada maalum. Wanao ushahidi kwamba juhudi zao zimetawanyika. Wamebadilika katika biashara, na wamejaa masumbufu na wasiwasi ambao huleta faida ndogo tu. Watu kama hao wanapaswa kusikiliza ushauri wa wale wenye uzoefu. Lakini mara nyingi wao ndio wa mwisho kutafuta ushauri. Wanafikiri wana fkira bora na hawafundishiki. {1T 480.3}

Hawa mara nyingi ndio wale ambao wanadanganywa na wale wachuuzi wenye hila, werevu, wakali na wajanja kwa hati miliki au haki za amana ambao mafanikio yao yanategemea sanaa ya udanganyifu. Hawa wanapaswa kujifunza kutoweka imani yoyote kwa wauzaji kama hao. Lakini ndugu ndiyo wale ambao wana utayari katika kuamini mambo ambayo wanapaswa kuyashuku na kuachana nayo. Hawachukui maagizo ya Paulo kwa Timotheo: "Lakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa." "Na tukiwa na chakula na mavazi, tutosheke na hayo." Hebu masikini wasifikirie kuwa matajiri ndio wenye tamaa tu. Wakati matajiri wanashikilia kile walicho nacho na kutamani na kuwa bahili tamaa, na wanatafuta kupata zaidi, maskini wako katika hatari kubwa ya kutamani mali za matajiri. Kuna wachache sana katika nchi yetu ilivyosheheni vitu(land of plenty) ambao ni masikini sana hata kuhitaji msaada. Ikiwa wangefuata kusudi sahihi, wangeweza karibu kwa kila jambo kuwa juu ya uhitaji. Wito wangu kwa matajiri ni, tenda kwa ukarimu na ndugu zako maskini, na utumie mali zako kuendeleza kazi ya MUNGU. Maskini wanaostahili, wale ambao hufanywa masikini na bahati mbaya ya magonjwa, wanastahili huduma yako maalum na msaada. "Mwishowe, iweni na nia moja, mkihurumiana, kupendana kama ndugu, kuwa na huruma, kuwa na adabu."{1T 481.1}

Wanaume na wanawake wanaodai utauwa na wanatarajia kunyakuliwa kwenda mbinguni bila kuona kifo, ninawaonya msiwe na tamaa ya kupata faida ya mali, msiwe wenye kujali sana ubinafsi. Komboeni heshima ya uchaji MUNGU wenu kama mwanaume na kama mwanamke kwa matendo bora ya ukarimu usio na ubinafsi, usiofikiria maslahi yake binafsi. Kwa moyo wote idharauni roho yenu ya zamani ya uchoyo, uroho wa mali na mpate tena ubora wa Kweli wa roho. Kutokana na yale ambayo MUNGU amenionesha, msipotubu kwa bidii, Kristo atawatapika kutoka kinywani Mwake. Waadventista wa Sabato wanadai kuwa wafuasi wa Kristo, lakini kazi za wengi wao zinasema uongo kukiri kwao. "Mtawatambua kwa matunda yao." "Sio kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni." {1T 482.1}

Natoa wito kwa wote wanaodai kuuamini Ukweli, kuzingatia tabia na maisha ya Mwana wa MUNGU. Yeye Ndiye mfano wetu. Maisha Yake yalikuwa na ukarimu usio na maslahi binafsi. Daima aliguswa huzuni ya binadamu. Yeye aliendelea kutenda mema. Hakukuwa na tendo hata moja la ubinafsi katika maisha Yake yote. Upendo Wake kwa jamii iliyoanguka, shauku Yake ya kuwaokoa, ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba alijitwalia ghadhabu ya Baba Yake, na akakubali kupata adhabu ya kosa hilo ambalo lilimzamisha mtu katika hatia ya uharibifu. Alibeba dhambi za mwanadamu katika mwili Wake mwenyewe. "Yeye ambaye hakujua dhambi amemfanywa kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya MUNGU ndani Yake." {1T 482.2}

Ukarimu wa kweli huharibiwa mara kwa mara na mafanikio na utajiri. Wanaume na wanawake katika shida au katika umaskini wakati mwingine wataonesha upendo mkubwa sana kwa Ukweli na shauku maalum kwa ustawi wa kusudi la MUNGU na kwa wokovu wa wanadamu wenzao, na wataelezea kile wangefanya ikiwa tu wangekuwa na mali. MUNGU huthibitisha mara kwa mara haya; Anawafanikisha watu hawa, na kuwabariki katika mashamba, maduka na hazina, zaidi ya matarajio yao. Lakini mioyo yao ni ya udanganyifu. Nia yao nzuri na ahadi ni kama mchanga unaoteleza. Kadri wanavyopata ndivyo wanavyotamani zaidi. Kwa kadri wanavyofanikiwa zaidi wanakuwa na shauku zaidi ya kupata faida. Baadhi ya hawa, ambao katika umaskini wao hapo zamani walikuwa wenye fadhili na wakaarimu, wanakuwa wasio na huruma na wagumu na wabahiil. Pesa huwa MUNGU wao. Wanafurahia nguvu ambayo pesa huwapa, katika heshima wanayopokea kwa sababu yake. Malaika alisema: "Angalia jinsi wanavyosimama katika jaribio. Angalia maendeleo ya tabia chini ya ushawishi wa utajiri." Wengine walikuwa wakiwakandamiza maskini wahitaji na wangepata huduma zao kwa pesa ya chini kabisa. Walikuwa wakiwakandamiza; pesa ilikuwa nguvu kwao. Jicho la MUNGU, niliona, lilikuwa juu yao. Walidanganywa. "Na tazama, Naja upesi; na thawabu yangu iko pamoja Nami, kumlipa kila mtu kadri ya kazi yake." {1T 482.3}

Wengine ambao ni matajiri hawawanyimi wachungaji. Wanaendelea na mfumo wa utoaji kwa mpango na ukarimu haswa na wanajivuna kwa uzingativu wao, na wanafikiria jukumu lao linaishia hapa. Hili ni jema kwa kadri linavyoendelea, lakini jukumu lao haliishii hapa. MUNGU anamadai juu yao ambayo hawayatambui. Jamii ina madai juu yao; wanadamu wenzao wana madai juu yao. Kila mwanachama wa familia yao ana madai juu yao. Madai haya yote yanapaswa kuzingatiwa; hakuna mtu anayepaswa kupuuzwa au kudharauliwa. Watu wengine hutoa kwa wahudumu na kuweka ndani ya hazina na kuridhika sana kana kwamba itawastahilisha kwenda mbinguni. Wengine wanafikiria kuwa hawawezi kufanya chochote katika kusaidia kusudi la MUNGU isipokuwa wana ongezeko kubwa kila wakati. Wanahisi kuwa hawawezi kugusa mtaji. Je! Mwokozi wetu akisema maneno yaleyale aliyomwaambia yule mtawala, "Nenda kauze uliyo nayo, uwagawie maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni: kisha njoo unifuate Mimi," wangekwenda kwa huzuni, na kuchagua kama yeye kubakiza na sanamu zao za utajiri, badala ya kutengana nazo ili kupata hazina za mbinguni. Mtawala huyu alidai kwamba alikuwa ameshika amri zote za MUNGU tangu ujana wake, na kujiamini katika uaminifu wake na haki, na kufikiria kwamba alikuwa mkamilifu, anauliza: "Je! Mimi nakosa nini bado?" Mara moja Yesu anararua blanketi la usalama bandia kwa kutaja sanamu zake, mali zake. Alikuwa na miungu mingine mbele za Bwana, ambayo zilikuwa na thamani kubwa kwake kuliko uzima wa milele. Upendo mkuu kwa MUNGU ulikosekana. Ndivyo ilivyo kwa wengine wanaodai kuamini Ukweli. Wanafikiri wamekamilika, wanafikiria kuwa hakuna ukosefu, wakati wako mbali na ukamilifu na wanathamini sanamu ambazo zitawafunga kutoka mbinguni. {1T 483.1}

Wengi huwahurumia watumwa wa Kusini kwa sababu wamefungwa kufanya kazi, wakati utumwa upo katika familia zao. Mama na watoto wanaruhusiwa kufanya kazi ngumu kutoka asubuhi hadi usiku; hawana burudani. Duru ya kazi isiyokoma iko mbele yao na imewasonga sana. Wanakiri kuwa wafuasi wa Kristo; lakini hawapati wakati wa kutafakari Neno na kuomba, na kupata chakula cha ubongo, ili akili, ambayo tunaitumia kumtumikia MUNGU, isiwe mbilikimo katika ukuaji wake? MUNGU anawaita kila mtu atumie talanta ambazo amezitoa kwao kwa utukufu Wake, na kwa kuziboresha kuleta wengine pia kwa Bwana. MUNGU ameweka majukumu juu yetu ili kufaidisha wengine. Kazi yetu katika ulimwengu huu kwa faida ya wengine haijafanyika mpaka Kristo atakaposema mbinguni: "imekwisha." "Yeye ambaye ni dhalimu, na aendelee kuwa dhalimu; na yule aliye mchafu, na aendelee kuwa mchafu; na yule aliye mwadilifu, na aendelee kuwa mwadilifu; na aliye mtakatifu na azidi kuwa mtakatifu." {1T 484.1}

Wengi wanaonekana kutokuwa na ufahamu wa kweli wa uwajibikaji wao mbele za MUNGU. Wanatakiwa kujitahidi kuingia katika lango jembamba, kwa sababu wengi watatafuta kuingia na hawataweza. Mbingu inawahitaji kujaribu kushawishi wengine pia kujitahidi kuingia katika lango jembamba. Kazi iko mbele ya vijana na wazee kufanya kazi kwa bidii kuokoa sio tu roho zao, bali roho za wengine. Hakuna hata mmoja ambaye ana sehemu za ubongo wenye kufikiri ambaye hana ushawishi wowote. Kwa kutojali kwao hutumia ushawishi huo kuzuia roho kutoka katika kujitahidi kuingia kwa kupitia lango jembamba, au kwa bidii yao, uvumilivu, na juhudi zisizochoka wanazishauri roho juu ya ulazima wa kujitahidi sana kuingia huko. Hakuna mtu anayechukua msimamo wa kuwa vuguvugu, kukaa katikati tu, kwamba hafanyi chochote kuwatia moyo wengine na hafanyi chochote kuwazuia. Anasema Kristo: Wale ambao hawakusanyi pamoja Nami hutawanya. Jihadharini, wazee na vijana; labda unafanya kazi ya Kristo, kuokoa roho, au kazi ya Shetani, kuwaongoza kwenye upotevu. "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema, na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni." {1T 484.2}

Vijana wanaweza kutoa ushawishi mkubwa ikiwa wataacha kiburi na ubinafsi wao, na kujitolea kwa MUNGU ; lakini kama jambo la jumla hawatabeba mizigo kwa ajili ya wengine. Lazima wao wenyewe lazima wabebwe. Wakati umefika ambapo MUNGU anahitaji mabadiliko katika suala hili. Yeye Anatoa wito kwa vijana na wazee kuwa na bidii na kutubu. Ikiwa wataendelea katika hali yao ya uvuguvugu, Yeye Atawatapika kutoka kinywani mwake. Shahidi wa Kweli anasema: "Najua kazi zako." Kijana wa loi,e, Binti, kazi zako zinajulikana, ikiwa ni nzuri au mbaya. Je! Wewe ni tajiri wa matendo mema? Yesu anakuja kwako kama mshauri: "Ninakushauri ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri; na mavazi meupe, upate kuvaa, na aibu ya uchi wako isionekane; na upake dawa ya macho, upate kuona. {1T 485.1}

# SURA YA 85

# MATENGENEZO YA AFYA

Katika njozi niliyopewa Roster, New York, Disemba 25, 1865, nilioneshwa kuwa watu wetu wanaotunza Sabato wamekuwa wazembe kutenda kulingana na nuru waliyopewa na MUNGU kuhusiana na matengenezo ya afya, na kwamba bado kuna kazi kubwa mbele yetu, na kwamba tumerudi nyuma sana kuzifuata majaliwa na mipango ya MUNGU iliyofunguliwa kama alivyochagua kutuongoza. 1T 485.2

Nilioneshwa kuwa kazi ya matengenezo ya afya bado haijatekelezwa ipasavyo. Wakati baadhi wakihisi kwa dhati na kutenda kwa kudhihirisha imani yao kwa matendo, wengine hawajali na kwa nadra sana wamepiga hatua ya kwanza katika matengenezo. Ndani yao kuna mioyo ya kutokuamini, na kwa kuwa matengenezo hayo yanazuia uchu wa chakula wa wengi, watu hurudi nyuma. Wana miungu mingine mbele za Bwana. Ladha yao, uchu wao, ni MUNGU wao; na wakati shoka linapowekwa kwenye shina la mti na wale ambao wameendekeza matumbo yao kwa gharama ya kupoteza afya wanaguswa, dhambi yao inaoneshwa bayana, sanamu zao zinafunuliwa, hawataki kusadikishwa; na ingawa sauti ya MUNGU inapaswa kuzungumza nao moja kwa moja ili kuondoa vizuizi vya uharibifu wa afya, wengine bado wanang'ang'ania vyakula na tabia mbaya kwa afya ambazo wanaziapenda. Wanaonekana kujiunga na sanamu zao na punde MUNGU atawaambia malaika Zake: Waacheni peke yao. 1T 486.1

Nilioneshwa kuwa, matengenezo ya afya, ni sehemu ya ujumbe wa malaika watatu na kwamba umeungana nao kwa karibu kama ilivyo kiganja cha mkono na mwili wa mwandamu. Niliona kuwa sisi kama watu wa Mungu ni lazima tuchukue hatua ya juu katika kazi hii kubwa. Wachungaji na washiriki ni lazima watende kwa kupatana. Watu wa MUNGU hawajaandaliwa kwa ajili kilio kikuu cha malaika watatu. Wanayo kazi ya kufanya kwa ajili yao ambayo hawawezi kumwachia MUNGU awafanyie. Bwana ameiacha kazi hii kwa ajili yao ili waifanye. Ni kazi ya mtu binafsi; hakuna anayeweza kuifanya kwa ajili ya mwingine. “Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha MUNGU.” Ulafi ni dhambi iliyoenea zaidi katika zama hizi. Tamaa ya uchu wa chakula huwafanya wanaume na wanawake kuwa watumwa, na kutia ukungu fahamu zao na kupumbaza utambuzi wa kimaadili kiasi cha kutothamini

au kupenda Ukweli mtakatifu uliotukuka wa Neno la MUNGU. Tamaa za chini za mwili zimewatawala wanaume na wanawake. 1 T 486.2

Ili kufaa kwa ajili ya kubadilishwa kwenda mbinguni, watu wa MUNGU ni lazima wajitambue wenyewe. Ni lazima wajielewe katika muonekano wa miili yao wenyewe ili waweze kushangilia pamoja na mtunga Zaburi "Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha." Wanapaswa kuwa na hamu ya kutiisha maadili na viungo vya akili daima. Mwili wapaswa kutawaliwa na akili na siyo akili kutawaliwa na mwili. 1T 486.2

Nilioneshwa kuwa kuna kazi kubwa zaidi mbele yetu kuliko tunavyodhani, kama tungelinda afya kwa kujiweka katika mahusiano sahihi ya uhai/afya. Dkt. A amekuwa akifanya kazi kubwa na nzuri katika kutibu magonjwa na kuwaelimisha wale ambao katika maisha yao yote wamekuwa katika ujinga kuhusiana na ulaji, unywaji na kufanya kazi katika kudumisha afya. MUNGU kwa rehema Zake amewapa nuru watu Wake kupitia kwa kiumbe Wake mnyenyekevu, kwamba ili kuepukana na magonjwa ni lazima wazikatae hamu na tamaa mbaya za chakula na kila mtu awe na kiasi katika kila kitu. Yeye Amefanya nuru kubwa iangaze katika njia yao. Je wale "wanaolitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, MUNGU mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi Yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote na kujisafishia watu wawe milki Yake Mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema," wawe nyuma ya wanadini wa kileo wasioamini marejeo ya haraka ya Mwokozi wetu? Watu wa milki Yake wa kipekee anaojisafishia ili waweze kwenda mbinguni pasipo kuona kifo, hawapaswi kuwa nyuma ya wengine katika kutenda mema. Katika jitihada zao za kujitakasa na uchafu wote wa mwili na roho, wakitimiza utakatifu katika kumcha MUNGU, wanapaswa wawe mbele zaidi ya kundi liwalo lote la watu ulimwenguni kwani ushuhuda wao umeinuliwa zaidi ya ule wa wengine. 1T 487.1

Baadhi wameidhihaki kazi hii ya matengenezo na kusema kuwa haikuwa ya muhimu na kwamba ilikuwa ni msisimko wa kuchepua akili kutoka kwenye Ukweli wa leo. Wamesema kuwa mambo haya yamefanywa kuwa ya kishupavu yaani watu wamepitiliza. Watu hao hawajui wanachokizungumza. Wakati wanaume na wanawake wanaokiri utauwa wana magonjwa kutoka utosini mwao hadi kwenye unyayoni mwao, wakati nguvu zao za kimwili, kiakili, na kimaadili zimedhoofishwa kwa kuridhisha tamaa mbaya na kufanya kazi kwa kupitiliza, hawa wanawezaje kupembua na kupima uthibitisho wa Kweli na kufahamu matakwa ya MUNGU? Kama uwezo wao wa kimaadili na kiakili umetiwa ukungu, hawataweza kukubali thamani ya upatanisho wa MUNGU kupitia kifo cha Kristo, au tabia iliyotukuka ya kazi ya MUNGU, wala kufurahia kulisoma Neno lake. Inawezekanaje yule mwenye shida ya mishipa ya fahamu na kuvembewa tumbo, kuwa tayari kila wakati kumjibu kila mtu anayemuuliza sababu ya tumaini lililo ndani yake kwa unyenyekevu na hofu? Ni rahisi kiasi gani kwa mtu

wa namna kuchanganyikiwa. kuudhiwa na kufadhaishwa kwa akili yake inayougua na kupelekea kuyatazama mambo kwa ujumla katika nuru isiyo sahihi, na kwa kukosa huo upole na utulivu unaoashiria tabia ya maisha ya Kristo, kuingia katika shimbo kutoheshimu kumkiri kwake Mungu, na ushuhuda wake wakati akijibizana na watu wasio na busara? Katika kuyatazama mambo kwa mtazamo wa juu wa kidini ni lazima tuwewanamatengenezo kamili ili kuwa kama Kristo. 1T 487.2

Niliona kuwa Baba yetu wa mbinguni ametukirimia mbaraka mkubwa wa nuru juu ya matengenezo ya afya ili tuweze kutii matakwa Yake juu yetu na kumtukuza Yeye katika miili na roho zetu ambavyo ni Vyake na hatimaye tusimame mbele za kiti cha enzi cha MUNGU tukiwa bila mawaa. Imani yetu inatutaka kuinua viwango na kupiga hatua za mbele zaidi. Wakati wengi wakihoji juu ya hatua wanayoichukua wanamatengenezo wengine wa afya, nao kama wenye busara wanapaswa kufanya jambo kwa ajili yao. Jamii yetu ya ubinadamu ipo katika hali ya kusikitisha, ikitaabika na magonjwa ya kila namna. Wengi wameyarithi magonjwa na ndio wataabikaji wakuu kwasababu ya mazoea mabaya ya wazazi wao, na bado wanaendelea na makosa hayo hayo kwa watoto wao japokuwa makosa hayo yamewatumbukiza hapo. Ni wajinga juu yao wenyewe. Wanaumwa na hawajui kuwa mazoea yao mabaya yanawasababisha kuzama katika mateso. 1T 488.1

Ni watu wachache sana hata hivyo walioamshwa kikamilifu kuelewa ni kwa kiasi gani mazoea yao ya ulaji yanahusiana na afya zao, tabia zao, manufaa yao hapa duniani na hatima yao ya milele. Niliona kuwa ni wajibu wao wale waliopokea nuru kutoka mbinguni na kutambua faida ya kutembea kwayo, kutangaza shauku kubwa kwa wale ambao bado wanateseka kwa uhitaji wa maarifa. Watunza Sabato wanaotazamia marejeo ya Mwokozi wao yaliyo karibu wanapaswa wawe wa mwisho kudhihirisha kukosa shauku katika kazi hii kubwa ya matengenezo. Ni lazima wanaume na wanawake waelekezwe, na wachungaji na washiriki wanapaswa kuhisi kuwa uzito wa kazi upo juu yao kuchochea jambo hili na kulipeleka katika nyumba za wengine. 1T 488.2

Nilioneshwa kuwa tunapaswa kuwapatia makazi wale wanaoteseka pamoja na wale wanaotamani kujifunza namna ya kutunza miili yao ili waweze kujikinga na magonjwa. Hatupaswi kuwa watu wasiojali na kuwalazimisha wale wanaoumwa na wenye shauku ya kuuishi Ukweli, kwenda kwenye taasisi maarufu za maji-tiba kwa ajili ya kuponywa afya, mahali ambapo hakuna huruma ya imani yetu (Mfano ni tiba rahisi kama dini za mashariki, ila hawaendani na imani ya Kikristo kama vile Ayuverdic nk) . Kama wataiponya afya itakuwa ni kwa gharama ya imani yao ya kidini. Wale walioteseka kwa upungufu wa kimwili ni dhaifu kiakili na kimaadili. Watakapogundua faida zitokanazo na matumizi sahihi ya maji, hewa na ulaji sahihi, wataongozwa kuamini kuwa matabibu waliofanikiwa kuelewa namna ya kuwatibu kwa mafanikio hawatakuwa katika makosa kwa imani zao potofu za kidini; kwamba

kadri wanavyojihusisha katika kazi kubwa na njema ya kuwanufaisha wanadamu wanaotaabika, basi watakuwa karibu na usahihi au kuwa sahihi kabisa. Na hivyo watu wetu wako katika hatari ya kunaswa kupitia jitihada zao za kuponywa afya katika mashirika haya yasiyomthamini Mungu wa mbinguni. 1T 489.1

Nilioneshwa tena kwamba wale walioimarishwa kwa uthabiti katika kanuni za kidini na kuwa imara katika kutii maagizo yote ya MUNGU hawataweza kupokea msaada kutoka katika taasisi maarufu za afya za siku hizi ambazo watu wengine wa imani tofauti wanaweza kupokea. Wanaotunza Sabato ni watu wa kipekee katika imani yao. Kushika amri zote za MUNGU kama anavyowataka wafanye ili waweze kumilikiwa nakuthibitishwa ni ngumu sana katika tiba-maji hizi maarufu. Kwa nyakati zote wanatakiwa kuwa na chekecheo na ungo wa injili kwa ajili ya kuchuja na kupepetaa kila kitu wanachokisikia, ili waweze kuchagua mema na kukataa mabaya. 1T 489.2

Shirika la tiba-maji huko—limekuwa ni taasisi bora nchini Marekani. Wasimamizi wake wamekuwa wakifanya kazi kubwa na nzuri kuhusiana na tiba ya magonjwa. Hata hivyo hatuwezi kuwa na uhakika wa kanuni zao za kidini. Licha ya kukiri kuwa ni wao Wakristo bado wanawashauri wagonjwa wao kucheza karata, kucheza dansi na kuhudhuria sinema au michezo ya kuigiza (theatre), wakati kwa kawaida yote hayo ni uovu, au kwa kusema machache yana mwonekano wa uovu na hupingana waziwazi na mafundisho ya Kristo na mitume wake. Watunza Sabato waaminifu wanaoenda katika taasisi hizi kwa malengo ya kurejesha afya hawataweza kupata msaada ambao wangeupata kama wasingejishurutishwa kujiweka kila mara katika ulinzi ili wasiweke imani yao hatarini, kutoheshimu kazi ya Mwokozi wao, na kuziweka roho zao katika utumwa. 1T 490.1

Nilioneshwa kuwa, wanaotunza Sabato wanapaswa kufungua njia kwa ajili wale wenye Imani ya thamani inayofanana ili kunufaishwa bila kuwa katika ulazima wa kutumia fedha zao katika taasisi ambazo imani zao na kanuni za kidini ziko hatarini na mahali wasipopata huruma au muunganokatika masuala ya kidini. MUNGU katika ahadi zake alielekeza kazi kwa dkt B---- kwamba anaweza kupata uzoefu ambao asingeweza kuupata, kwani MUNGU anayo kazi kwa ajili yake ambayo anapaswa kuifanya katika matengenezo ya afya. Kama tabibu mwenye uzoefu amekuwa kwa miaka akipata maarifa ya mfumo wa mwanadamu, na sasa MUNGU anamtaka kwa kielelezo na kwa vitendo kujifunza namna ya kutumia baraka zilizowekwa ndani yake ili kuwafikia watu. Tabibu huyu atachukuliwa na kuandaliwa kuwanufaisha wagonjwa na kuwafundisha wale wasioelewa namna ya kutunza nguvu na afya waliyo nayo, na namna ya kujikinga na magonjwa kwa matumizi sahihi ya tiba za kimbingu-maji safi, hewa safi na chakula bora. 1T 490.2

Nilioneshwa kwamba dkt. B alikuwa mtu anayechukua tahadhari na mwangalifu sana, mtu ambaye MUNGU anampenda. Amepitia majaribu mengi ambayo

yamefanya kazi kwa faida yake, ingawa wakati akiyapitia hakuweza kuona wakati wote jinsi atakavyofaidika nayo. Dkt B hawezi kuwa mtu wa kujisifu anapouamini Ukweli na kufuata njia yake. Yeye si mtu mkali, mwenye kujivuna na mwenye kuamrisha watu kwa mabavu. Anaogopa sana kuvaa kile cheo ambacho nafasi yake kama daktari ingemruhusu kudumisha. Atashauriana na wengine na ni rahisi kushauriwa; hatari yake kubwa itakuwa utayari wa kubeba mizigo ambayo hapaswi kuibeba. Anaona na kuhisi kile kinachopaswa kufanywa, na atakuwa katika hatari ya kufanya kazi kupita kiasi. Yeye ni mtu mwenye huruma, mwenye hisia kali za kujali, na atapata hisia ya kina sana kwa wagonjwa wake wote; na ikiwa anaruhusiwa, atabeba mzigo mzito wa uwajibikaji hata kuufanya mzigo huu umponde. 1T 491.1

Wanaume na wanawake wenye ushawishi wanapaswa kumsaidia ndugu B kwa maombi yao, huruma yao, ushirikiano wao wa dhati, kumtia moyo kwa maneno ya matumaini, na ushauri na nasaha zao— yote haya daktari huyu atayathamini. Nafasi yake haiwezi kuwa ile ya kutamaniwa au kuvutia watu. Ikiwa atachukua majukumu makubwa sana hayatakuwa katika uchaguzi au katika kupata riziki ya maisha, kwani anaweza kuyapata haya kwa njia rahisi zaidi kwa njia nyingine na kuepuka masumbufu, wasiwasi, na mashaka ambayo yageletwa na msimamo huo. Wajibu pekee utamwongoza; na akiisha kushawishika katika njia ya wajibu, ataifuata na kusimama katika wadhifa wake, na kuyaacha matokeo yawe vile yanavyoweza kuwa. Ni vyema awe na huruma na ushirikiano wa watu wenye ushawishi, wale ambao MUNGU amewaweka ili kusimama upande wake na kumtegemeza katika kazi yake ngumu. 1T 491.2

Dkt. B angeweza, kwa kadri ulimwengu huu unavyohusika, kufanya vizuri zaidi kuliko katika nafasi anayoishikilia sasa. Nilioneshwa kuwa nafasi hii itakuwa mgumu zaidi. Wengi ambao hawana uzoefu hawatajua ukubwa wa shughuli hiyo na wangependa mambo yaende kulingana na maoni yao. Wengine wangeshangaa kwanini masikini wasingekuja na kutibiwa bure, na wangejaribiwa kufikiri kuwa ilikuwa biashara ya kutafuta pesa tu; na kwa namna moja au nyingine wangetaka kuwa na kitu cha kusema, na kutafuta kasoro nyingi, na kuyaacha mambo yaende kama yanavyopaswa; kwani nilioneshwa kuwa wengine wangechukulia ni sifa kuwa na wivu na kusimama kupinga. Wanajivunia kutokupokea kila kitu mara tu kitakapokuja. Kama Thomaso, wanajivunia kutokuamini kwao. Lakini je! Yesu alimpongeza Tomaso asiyeamini? Wakati akimpa ushahidi aliokuwa ametangaza kuwa angekuwa nao kabla ya kuamini, Yesu alimwambia: "Tomaso umeamini kwa kuwa umeniona; wamebarikiwa wale ambao hawajaona, na bado wameamini." 1T 491.3

Nilioneshwa kuwa hakuna ukosefu wa fedha miongoni mwa Waadventista wa Sabato. Kwa sasa hatari yao kubwa ni katika ulimbikizaji wa mali. Wengine wanaendelea kuongeza masumbufu yao na shughuli; Wanapa uchovu mkubwa kwa shuguli za kutafuta mali au faida. Matokeo yake ni kwamba, MUNGU na matakwa ya kazi Yake hukaribia kusahauliwa nao; wamekufa kiroho.

Wanahitajika kutoa sadaka kwa MUNGU, dhabihu. Dhabihu haiongezeki, badala yake inapungua na kuisha. Hapa, nilioneshwa kuwa ilikuwa biashara ambayo watu wa MUNGU wanapaswa kuishiriki, biashara ambayo wanaweza kuwekeza kwa utukufu Wake na kuendeleza kusudi na mapenzi Yake. Mali nyingi miongoni mwa watu wetu zinathibitisha tu maumivu kwa wale wanaozishikilia. 1T 492.1

Watu wetu wanapaswa kuwa na taasisi yao wenyewe, chini ya udhibiti wao, kwa faida ya wagonjwa na wanaoteseka kati yetu ambao wanataka kuwa na afya na nguvu ili waweze kumtukuza MUNGU katika miili na roho zao, ambazo ni Zake. Taasisi kama hiyo, ikiendeshwa sawa sawa, inaweza kuwa njia ya kuleta maoni yetu mbele ya wengi ambao tusingeweza kuwafikia kwa njia ya kawaida ya kueneza Ukweli. Kadri watu wasioamini watakavyopata huduma katika taasisi iliyojitoa kwa ajili ya kufanikisha matibabu ya magonjwa na kuendeshwa na matibabu wanaoitunza Sabato, watu wataletwa moja kwa moja chini ya ushawishi wa Ukweli. Kwa kuwafahamu watu wetu na imani yetu halisi, chuki au ubagizo wao itashindwa na watavutiwa sana. Kwa hiyo, wakiwa wamewekwa chini ya ushawishi wa Ukweli, wengine siyo tu kwamba watapata ahueni kutoka katika udhaifu wa mwili, bali pia tiba na dawa ya uponyaji kwa roho zao ambazo zinaugua dhambi. 1T 492.2

Kadiri afya ya wasioamini itakavyoendelea kuwa nzuri chini ya matibabu mazuri, nao wakaanza kufurahia maisha, watakuwa na imani kwa wale ambao wamekuwa chombo katika kurudisha afya zao. Mioyo yao inajawa shukrani, na mbegu nzuri ya Ukweli itapata makao kwa urahisi zaidi na wakati mwingine italishwa, itakua na kuzaa matunda kwa utukufu wa MUNGU. Nafsi moja ya thamani iliyookolewa kama hiyo, itakuwa ya thamani zaidi kuliko mali zote zinazohitajika kuanzisha taasisi kama hiyo. Wengine hawatakuwa na ujasiri wa kutosha wa maadili ili kukubaliana na imani zao. Wanaweza kusadiki kuwa watunza Sabato wana Ukweli, lakini ulimwengu na jamaa wasioamini wasimama katika njia kuwazuia wasiupokee. Hawawezi kuzileta akili zao katika hatua ya kutoa dhabihu vyote kwa ajili ya Kristo. Lakini baadhi ya watu wa kundi hili lililotajwa mwisho wataondoka chuki yao ikiwa imeondolewa na watasimama kama watetezi wa imani ya Waadventista Wasabato. Wengine ambao wataenda wakiwa wamerejeshwa kiafya au wakiwa wamefaidika sana watakuwa njia ya kuitambulisha imani yetu katika maeneo mapya na kuinua kiwango cha Ukweli mahali ambapo pasingeweza kufikiwa laiti kama chuki isingeondolewa kwanza akilini watu wetu kwa kusudi la kupata afya. 1T 493.1

Wengine watathibitisha chanzo cha jaribu wanapokwenda nyumbani kwao. Walakini hii haipaswi kumvunja moyo yeyote au kuwazuia katika juhudi zao katika kazi hii nzuri. Shetani na mawakala wake watafanya kila wawezalo kuzuia, kuchanganya, na kuwabebesha mizigo wale ambao kwa moyo wote wanashiriki katika kazi ya kuendeleza matengenezo haya ya afya. 1T 493.2

Kuna utoaji wa mali wa ukarimu miongoni mwa watu wetu, na ikiwa wote wangeona umuhimu wa kazi, biashara na taasisi hii kubwa ingeweza kusonga mbele bila aibu. Wote wanapaswa kuhisi shauku na maslahi maalum katika kuiendeleza. Hasa wale ambao wana mali wanapaswa kuwekeza katika biashara hii. Nyumba inayofaa inapaswa kutayarishwa kuwa mahali pa kuwapokea wagonjwa wagonjwa wasiojiweza ili kwa kutumia njia sahihi na mibaraka ya MUNGU, waondolewe udhaifu wao na kujifunza jinsi ya kujitunza na hivyo kuzuia magonjwa. 1T 494.1

Wengi wanaodai kuuamini Ukweli wanazidi kuwa wabahili na wenye tamaa. Wanahitaji kushtushwa wenyewe. Wana hazina nyingi duniani kiasi kwamba mioyo yao iko kwenye hazina zao. Sehemu kubwa ya hazina zao iko katika ulimwengu huu na kidogo mbinguni; kwa hivyo mapenzi yao yamewekwa kwenye mali za dunia badala ya urithi wa mbinguni. Sasa kuna fursa nzuri kwao kutumia mali zao kwa faida ya wanadamu wanaoteseka na pia kwa maendeleo ya ile Kweli. Biashara hii haipaswi kuachwa ikumbwe na umasikini. Mawakili hawa ambao MUNGU  amewapa dhamana lazima sasa waje kufanya kazi na watumie mali zao kwa utukufu Wake. Kwa wale ambao kwa uchoyo wanazuia mali zao, hilo litathibitisha laana badala ya baraka. 1T 494.2

Wale ambao MUNGU  amewapa dhamana wanapaswa kutoa mfuko ili utumiwe kwa faida ya maskini wanaostahili ambao ni wagonjwa na hawawezi kulipia gharama za matibabu katika taasisi hiyo. Kuna masikini wa thamani na wanaostahili ambao ushawishi wao umekuwa na faida katika kazi ya MUNGU. Mfuko unapaswa kupatikana ili utumike kwa madhumuni dhahiri ya kuwahudumia maskini kama kanisa walilomo litaamua kwamba wanafaa kufaidika. Pasipo wale walio na vitu vingi kutoa bila kudai malipo, maskini hawataweza kujinufaisha na faida inayotokana na matibabu ya magonjwa katika taasisi hiyo ya Sanitarii,, ambayo mali nyingi zinahitajika kwa kazi iliyopewa. Taasisi kama hiyo hiyo changa, haipaswi kupata changamoto wakati inaanza ili kuisaida isitawi vyema, haipaswi kuaibishwa kwa matumizi makubwa ya fedha, yaani fedha zinazotoka bila ya kurudi. 1T 494.3

## SURA YA 86

## HOTUBA KWA VIJANA

Vijana watunza Sabato wamejidondosha katika kutafuta anasa na starehe. Niliona kuwa hakuna hata mmoja aliye kati ya vijana ishirini anayefahamu kuhusu dini ya matendo. Wanatafuta kwa bidii kitu ambacho kitatosheleza shauku yao ya mabadiliko, na maburudisho; na kama hawatodanganyika na hisia zao kuzinduka mpaka waweze kusema toka moyoni "Nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu," basi watakuwa si wa thamani Kwake, na wataukosa uzima wa milele. Kwa ujumla, vijana wapo katika udanganyifu wa kutisha, lakini bado wanajidai kuwa watauwa. Maisha yao yasiyowekwa wakfu yamejaa malaumu kwa Jina la Kristo; mfano wao ni mtego kwa wengine. Wanamzuia mdhambi asije kwa Bwana, kwa kuwa katika kila nyanja ni wabaya kuliko wasioamini. Wanalo Neno la MUNGU, lakini hawasikilizi maonyo, mawaidha, makemeo, na masahihisho, pamoja na maneno ya faraja na ahadi kwa watiifu na waaminifu. Ahadi za MUNGU zote ni kwa sharti la wenye unyenyekevu. Vijana wamepewa kielelezo kimoja tu, lakini ni kwa namna gani maisha yao yanalingana na maisha ya Kristo? Ninashtushwa ninaposhuhudia kila mahali upuuzi wa vijana wa kiume na vijana wa kike ambao wanadai kuiamini ile Kweli. MUNGU haonekani kuwepo katika fikra zao. Akili zao zimejawa na ujinga, mambo yasiyo na maana. Mazungumzo yao ni hewa tupu, ni batili. Wana sikio linalozingatia muziki, na Shetani anajua ni viungo gani avisisimue ili vitindikiwe na kuiloga akili ili Kristo achukiwe. Shauku kwa mambo ya kiroho nafsini kwa ajili ya ufahamu wa mambo ya kimbingu, ili kukua katika neema, imepungua. 1T 496.1

Nilioneshwa kuwa vijana wanapaswa kuwa na msimamo wa juu ulio imara na kulifanya Neno la MUNGU kuwa mshauri wao na kiongozi wao. Vijana wamepewa majukumu rasmi, ambayo wanayatazama kwa wepesi- umakini mdogo. Kuanzishwa kwa muziki katika nyumba zao, badala ya kuchochea

utakatifu na mambo ya kiroho, imekuwa ni njia ya kuchepusha akili zao kutoka katika Kweli. Nyimbo za kipuuzi na karatasi zenye muziki wa nyimbo maarufu za kidunia zinaonekana kwao ndiyo ladha wanayoipenda. Vyombo vya muziki vimechukua muda ambao ungelipaswa kutumiwa kwa maombi. Muziki, usipotumiwa vibaya, ni mbaraka mkubwa; lakini unapotumiwa vibaya, ni laana ya kutisha. Unasisimua, lakini hautoi nguvu na ujasiri ule ambao Mkristo anaweza kuupata katika kiti cha enzi cha neema pekee anaposihi kwa unyenyekevu akitamka mahitaji yake kwa kilio kikuu pamoja na machozi akiomba ili apate nguvu za kimbingu kwa ajili ya kuimarishwa dhidi ya majaribu yenye nguvu ya yule mwovu. Shetani anawaongoza vijana utumwani. Oh, niseme nini ili kuwaongoza vijana waweze kupambana dhidi ya nguvu ya mahaba ya kufikiriaka aliyo nayo Shetani! Ni mchawi mwenye stadi, akiwahadaa na kuwapeleka upotevuni. Sikiliza maelekezo yatokayo katika kitabu cha MUNGU kilichovuviwa. Niliona kuwa Shetani amezipofusha akili za vijana ili wasiweze kuzifahamu Kweli za Neno la MUNGU. Hisia zao ni butu kiasi kwamba wanapuuzia maagizo ya mtume mtakatifu: 1T 497.1

“Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, upate heri, ukae siku nyingi katika dunia (mpya).” “Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote; maana jambo hili lapendeza katika Bwana.” Watoto ambao hawawaheshimu na kuwatii wazazi wao, na kupuuza mashauri na maelekezo yao, hawawezi kuwa na sehemu katika nchi mpya. Nchi mpya iliyokwishatakaswa haitakuwa makazi ya mwana au binti muasi, asiyetii, na asiye na shukrani. Kama hawatajifunza utii na kujitoa hapa, hawataweza kujifunza kamwe pengine; amani ya waliokombolewa haitaharibiwa na watoto wasio watiifu, wakorofi, wakaidi, na watukutu. Hakuna yeyote aliye mvunja amri awezaye kuurithi ufalme wa mbinguni. Je, vijana wote watakuwa tayari kuisoma amri ya tano ya sheria iliyotamkwa na Yehova kutoka Sinai na kuandikwa kwa chanda CHAKE Mwenyewe katika mbao za mawe? “Waheshimu baba yako na mama yako: siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana MUNGU wako.” 1T 497.2

Nilirejelewa Aya nyingi za Maandiko ambazo kwa uwazi zimeonesha vijana mapenzi ya MUNGU kwao. Mafundisho haya yaliyo wazi lazima wakutane nayo hukumuni. Lakini bado hakuna hata kijana mmoja wa kiume au wa kike aliye kati ya ishirini atangazaye Ukweli wa wakati huu anayesikiliza mafundisho haya ya Biblia. Vijana hawasomi Neno la MUNGU vya kutosha ili kufahamu madai yake kwao; na huku Kweli hizi ndizo zitakazowahukumu katika siku kuu ya MUNGU, wakati vijana kwa wazee watakapotunukiwa kulingana na matendo waliyoyafanya. 1T 498.1

Yohana anasema: “Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mna nguvu, na neno la MUNGU linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule mwovu. Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya MUNGU adumu hata milele.” 1T 498.2

Mausia haya kwa vijana wa kiume yanawahusu vijana wa kike pia. Ujana wao hauwafanyi wao waepukane na wajibu uliowekwa juu yao. Ni wenye nguvu na hawajachakazwa kwa masumbufu pamoja na wingi wa miaka; mapenzi yao ni motomoto, na kama watayaondoa toka ulimwenguni na kuyaweka kwa Kristo na mbingu, wakifanya mapenzi ya MUNGU, watakuwa na tumaini la maisha bora yadumuyo, na wataishi milele, wakiwa wamevikwa taji ya utukufu, adhama, kutokufa, na uzima wa milele. Kama vijana wanaishi ili wapate kutosheleza tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, wanatafuta mambo ya ulimwengu, huku wakimfurahisha mshtaki wao mkuu, na kujitenga kutoka kwa Baba. Na wakati vitu hivi walivyovitafuta vinapotoweka, matumaini yao yanaharibika na matarajio yao yanatoweka. Huku wakiwa wametengana na MUNGU watajutia kwa uchungu upuuzi wa kujali anasa zao wenyewe, kuridhisha shauku zao, na kwa anasa chache za kipuuzi kupoteza maisha ya furaha ambayo wangeliyafurahia milele. 1T 498.3

“Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia,” anasema mtume aliyevuviwa. Kisha anaongezea kwa onyo: “Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake.” Ni Ukweli wa kutisha kwamba kuipenda dunia ndiko kunakotawala katika akili za vijana. Wameamua kuipenda dunia na mambo yaliyomo ndani yake, na kwa sababu hii kumpenda MUNGU hauna nafasi mioyoni mwao. Wanatafuta anasa zao katika dunia na katika mambo ya dunia, na huku ni wageni kwa Baba na kwa neema za Roho Wake. MUNGU anaaibishwa kwa upuuzi na mtindo, na kwa mazungumzo na vicheko tupu na visivyo na maana vifanyikavyo katika maisha ya vijana kwa ujumla. Paulo anawahimiza vijana kuwa na kiasi: “Vivyo hivyo na vijana waume uwaonye kuwa na kiasi; katika mambo yote ukijionesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema, na katika mafundisho yako ukionesha usahihi na ustahivu, na maneno yenye uzima yasiyoweza kuhukumiwa makosa, ili yule mwenye kupinga atahayarike, kwa kuwa hana neno baya la kunena juu yako.” 1T 499.1

Nawasihi vijana kwa ajili ya nafsi zao kusikiliza mausia ya mtume aliyevuviwa. Maelekezo, maonyo, na makatazo haya ya neema yatakuwa ni harufu ya uzima ya kuhuisha au kufisha. Vijana walio wengi ni wazembe katika mazungumzo yao. Wanachagua kusahau kuwa kwa maneno yao wataonekana kuwa wenye haki au kuwa na hatia. Wote wanapaswa kusikiza maneno ya Mwokozi wetu:

“Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema; na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya. Basi, naawambia, kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.” Inawezekanaje hata maelekezo ya Mwalimu mkuu kutoka mbinguni yapewe umuhimu mdogo hivi. Wengi aidha hawalisomi Neno la MUNGU  au hawazikilizi na kuzitenda Kweli Zake maalum, na Kweli hizi zilizo wazi zitaletwa hukumuni na kuwatia hatiani. 1T 499.2

Maneno na matendo vinadhihirisha wazi kile kilichopo moyoni. Kama ubatili na kiburi, kujipenda nafsi na kupenda mavazi, vinaujaza moyo, mazungumzo yatakuwa juu ya mitindo, mavazi, na mwonekano, lakini si kwa Kristo au ufalme wa mbinguni. Kama hisia za husuda zinakaa moyoni, zinadhihirishwa katika maneno na matendo. Wale wajipimao wao wenyewe kwa kuangalia wengine, wafanyao kama wengine wafanyavyo, wasiofanya maendeleo makubwa zaidi, huku wakijifariji kwa makosa na kasoro za wengine, wanajilisha makapi na watadumu kuwa mbilikimo wa kiroho kwa kadri wanavyomridhisha Shetani na kujifurahisha katika hisia zao zisizo wakfu. Baadhi wanajikita katika kile watakachokula na kunywa, na namna watakavyovaa. Mawazo haya yanaujaza moyo, kana kwamba vitu hivi vya muda mfupi ni vya maana sana maishani, na magoli muhimu ambayo yanapaswa kufikiwa. Watu hawa wanasahau Maneno ya Kristo: “Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa.” 1T 500.1

Mioyo ya vijana imejazwa kwa kujipenda wenyewe. Hili linadhihirishwa katika shauku waliyo nayo ya kuona nyuso zao zimechorwa na msanii (siku hizi ni picha za selfie); na hawatosheki kwa mara moja, bali wanakaa tena na tena kwa ajili ya kuchowa picha yao tena, kila wakati wakitajaria kuwa ya mwisho itakuwa nzuri kuliko jitihada zao zilizopita na wataonekana warembo kuliko uhalisia ulivyo au ile picha ya kwanza. Hela ya Bwana wao inatumiwa vibaya, na je inawafaidia nini? Ni kivuli chao masikini tu kwenye karatasi. Masaa ambayo yangelitumika katika sala wanayatumia kwa ajili ya nafsi zao wenyewe; na huku masaa ya thamani ya rehema yanapotea bure. 1T 500.2

Shetani anafurahishwa anapoona akili za vijana zinavutwa na kuchepushwa kutoka kwa MUNGU kupitia chochote,  ili yeye anayehadaa apate kuwatoa kwenye njia ili wakiwa katika hali ya kutojiandaa kwa ajili ya mashambulizi yake, ili wapate kutegwa. Hawafahamu kuwa Mwana sanaa mkuu wa mbinguni anatambua kila tendo, kila neno, na kwamba mienendo yao, na fikra zao pamoja na mawazo ya moyo, vinasanifiwa/vinaonyeshwa kwa uaminifu. Kila kasoro katika tabia zao inafunuliwa katika macho ya malaika, na wataletewa picha halisi katika madhaifu yao yote wakati wa kusomwa kwa hukumu. Hayo maneno matupu, na ya kipuuzi yote yanaandikwa katika kitabu. Hayo maneno

ya uongo yanaandikwa. Maneno ya udanganyifu, ambayo makusudi yake yamefichika katika macho ya kibinadamu, lakini yanaonekana na jicho la Yehova lionalo kila kitu, yote yanaandikwa kwa herufi hai. Kila tendo la ubinafsi linawekwa wazi. 1T 501.1

Vijana wanaishi kana kwamba masaa ya thamani ya rehema, wakati rehema ingalipo, yalikuwa ni sikukuu moja kubwa, na kwamba waliwekwa ulimwenguni kwa ajili ya anasa zao wenyewe tu, ili wapate kuridhishwa kwa misisimko endelevu. Shetani amekuwa akifanya jitihada maalum ili kuwaongoza kutafuta furaha katika anasa za kiulimwengu na wao wenyewe kujihalalishia kwa kuhangaika kuonesha kuwa anasa hizi hazina madhara, ni halali, na muhimu hata kwa afya. Wazo limetolewa na baadhi ya matabibu kuwa mambo ya kiroho na kujitoa kwa MUNGU ni hatari kwa afya. Hili linamfaa mshtaki wa nafsi. Kuna watu walio na mawazo ya kufisha ambao hawaiwakilishi vema dini ya Kristo; hao hawana dini safi ya Biblia. Baadhi wanajiumiza wao wenyewe katika maisha kwa sababu ya dhambi zao; wanachoweza kukiona tu ni MUNGU Mwenye haki Anayechukiwa. Wanashindwa kumwona Kristo na uweza Wake uokoao kwa damu Yake. Hao wamekosa imani. Kundi hili ni wale wasio na akili zenye msawaziko bora-(hamna balansi). Kwa kupitia ugonjwa walioupata toka kwa wazazi wao, na elimu yenye makosa waliyoipata ujanani, wamekuwa na tabia potofu ambazo zinaathiri nguvu na ubongo, huku zikiathiri ogani za kimaadili na kuwafanya washindwe kufikiri na kutenda kwa busara katika nyanja zote. Hawana akili zilizo bora. Utauwa na haki havileti uharibifu wa afya, bali afya mwilini na nguvu nafsini. Paulo anasema: “Atakaye kupenda maisha, na kuona siku njema,…na aache mabaya, atende mema; atafute amani, aifuate sana: kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yYke husikiliza maombi yao: bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya.” “Lakini mjapoteswa kwa sababu ya haki mna heri. Msiogope kutisha kwao, wala msifadhaike.” 1T 501.2

Utambuzi wa kufanya lililo sahihi ni dawa nzuri zaidi ya mwili na akili iliyoathirika. Mbaraka wa pekee wa MUNGU kwa yeye apokeaye ni afya na nguvu. Mtu ambaye akili yake imetulia na kutosheka katika MUNGU yu njiani kuelekea kuwa na afya. Kuwa na utambuzi kuwa macho ya Bwana yapo juu yetu na masikio Yake yapo wazi kusikia maombi yetu ni jambo la kuridhisha vya kutosha. Kufahamu kuwa tunaye rafiki asiyeshindwa ambaye kwake twaweza kupeleka siri zote za nafsi ni fursa ya pekee ambayo maneno hayawezi kuelezea. Wale ambao nguvu zao za kimaadili zimefunikwa kwa ugonjwa hawafai kuwakilisha ipasavyo maisha ya Mkrito au uzuri wa utauwa. Mara zote wapo katika moto wa ushabiki au maji ya ubaridi wa kutojali au giza la utusitusi. Maneno ya Kristo ni ya thamani zaidi kuliko maoni ya matabibu wote ulimwenguni: “Bali utafuteni kwanza ufalme wa MUNGU, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa.” Hili ni jambo la kwanza lililo kuu-ufalme wa mbinguni,

haki ya Kristo. Mambo mengine yanayopatikana yanapaswa kuwa ya ziada baada ya haya. 1T 502.1

Shetani ataiwasilisha njia ya utauwa kama ni ngumu wakati njia ya anasa za ulimwengu imepambwa kwa maua. Kwa rangi za hadaa na kupendeza mjaribu ataufunua mbele yako ulimwengu na anasa zake. Majivuno na ubatili ni moja ya tabia yenye nguvu ya asili yetu ya dhambi, na anajua kuwa anaweza kufanikiwa kutuvutia kwayo. Atakufurahisha kupitia mawakala wake. Waweza kupokea sifa ambayo itayafurahisha majivuno na ubatili wako na kuamsha ndani yako kiburi na kujithamini, na unaweza kufikiri kuwa kwa faida na mivuto hiyo ni aibu kubwa kwa wewe kutoka ulimwenguni na kujitenga, na kuwa Mkristo, kuwaacha marafiki wako, na kuwa kama mfu kwa sifa na lawama zao. Shetani anakwambia kuwa kwa manufaa/faida ulizo nazo ungeweza kwa kiwango kikubwa kufurahia anaza za ulimwengu. Lakini zingatia kuwa anasa za dunia zitakuwa na mwisho, na kwamba kile upandacho ndicho utakachovuna. Je, vivutio binafsi, uwezo, au vipaji ni vya thamani mno kuliko kuvitoa kwa ajili ya MUNGU, aliye Mwanzilishi wako, Yeye akulindaye wewe kila wakati? Je, stahiki/sifa ulizonazo ni za thamani mno kuliko kuzitoa wakfu kwa MUNGU ? 1T 502.2

Vijana wanasihi kwamba wanahitaji kitu cha kuchangamsha, kufanya maisha yawe hai na kuliwaza akili. Niliona kuwa kuna raha katika bidii ya kazi, tasnia (industry), hali ya kutosheka na kuridhishwa moyo, unapokuwa unajishugulisha na maisha yaliyo na manufaa. Baadhi bado wanasihi kuwa ni lazima wao wawe na kitu kwa ajili ya kuivutia akili wakati kazi inapokoma, shughuli fulani ya kiakili au maburudisho ambayo yataifanya akili itulizwe, kuburudishwa na kusuuzwa katikati ya mihangaiko na kazi ya kuchosha. Tumaini la Mkristo ndilo tu linalohitajika. Dini ndiyo itakayothibitika kuwa mfariji, na kiongozi wa hakika kwa muumini kulielekea bubujiko la furaha ya kweli (mambo ya Kiroho yanayohusu Mungu wa Mbinguni na Neno Lake, zamani Dini ilimaanisha hilo). Vijana wanapaswa kusoma Neno la MUNGU na kulitafakari kwa kina na maombi, kisha wataona kuwa nyakati zao za ziada haziwezi kutumika vema zaidi ya hapo. Marafiki zangu vijana, mnapaswa kutenga muda ili kujithibitisha ninyi wenyewe, kama mpo katika pendo la MUNGU. Iweni na bidii katika kuufanya wito wenu na kuchaguliwa kwenu kuwe kwa uhakika. Inategemea na mwenendo wenu kama mnajihakikishia uhakika wa maisha yaliyo bora zaidi. 1T 503.1

Njia za hekima “ni njia za kupendeza sana, na mapito yake yote ni amani.” Makao ya wenye haki na ujira wao wa milele ndiyo mawazo makuu na yenye hadhi bora zaidi, ambayo vijana wanapaswa kuyatafakari. Kita akili yako katika mpango wa ajabu wa ukombozi, kafara kuu iliyotolewa na Mfalme wa utukufu ili upate kuinuliwa kupitia sifa/stahiki za damu Yake na kwa kupitia kutii hatimaye upate kuinuliwa mpaka kwenye kiti cha enzi cha Kristo. Mada hii inapaswa kutafakariwa na akili kwa ubora zaidi kuliko somo jingine lolote duniani. Kupewa upendeleo na MUNGU -ni fursa ya ilioje! Kuwasiliana Naye-Ni nini kinachoweza kutuinua, kutusafisha, na kutupandisha juu kupita anasa za kipuuzi za dunia? Asili zetu za uasi na ufisadi kukarabatiwa kwa neema, hamu ya tamaa mbaya na tabia za kinyama kutiishwa, kusimama kwa ujasiri tukiwa na uadilifu, uungwana na uhuru wa kimaadili bora, kupata ushindi kila siku, vitaleta amani ya dhamiri ambayo itapatikana tu kwa kufanya matendo/utendaji sahihi. 1T 503.2

Marafiki zangu vijana, niliona kuwa kwa shughuli/kazi na pumziko kama hili wewe unawaweza ukawa na furaha. Lakini sababu ya kwa nini hamtulii ni kwa kuwa hamtafuti chanzo cha Kweli cha furaha. Mnajaribu daima kutafuta nje ya Kristo furaha ile ambayo inapatikana tu Kwake Yeye peke yake. Kwake hakuna matumaini yaliyokatishwa tamaa. Maombi, Oh, ni kwa jinsi gani fursa hii ya thamani inapuuzwa! Usomaji wa Neno la MUNGU unaiandaa akili kwa ajili ya maombi. Moja ya sababu kuu kwa nini mna ladha na uelekeo mdogo wa kuvutwa karibu na MUNGU kwa maombi ni hii; mmejidhoofisha ninyi wenyewe msiiweze kazi hii takatifu kwa kusoma hadithi za kusisimua ambazo zimeamsha fikra na kuchochea hisia kali ambazo si takatifu. Neno la MUNGU linakosa ladha, wasaa wa maombi unasahaulika. Maombi ni nguvu ya Mkristo. Awapo mwenyewe hawi peke yake; anahisi uwepo wa Yeye aliyesema: “Tazama, Nipo pamoja nanyi siku zote. 1T 504.1

Vijana wanataka tu kile ambacho hawana; yaani, dini (Mwenyezi Mungu na Neno Lake). Hakuna kinachoweza kuchukua nafasi ya hiki. Kujitangaza kwa mdomo pekee si kitu. Majina yanaandikwa katika vitabu vya kanisa duniani, lakini si katika kitabu cha uzima. Niliona kuwa hakuna hata mmoja katia ya ishirini (1/20) anayejua kuwa dini yenye utendaji hai inamaanisha nini*. Wajitumikia wenyewe na huku bado wakijitangaza kuwa ni watumishi wa Kristo; lakini wasipojirekebisha na kuvunja uchawi huu, hivi karibuni watatambua kuwa fungu la mwasi ni la kwao. Kuhusu kujikana nafsi na kujitoa dhabihu kwaajili ya ile Kweli-Wao wamejitafutia njia nyepesi zaidi kuliko kujikana nafsi au kujitoa kafara kwa ajili ya Kweli. Kuhusu kuomba na kusihi kwa dhati, bidii, machozi na vilio vikuu kwa Mungu kwa ajili ya neema Yake inayosamehe na kwa ajili ya kupata nguvu za kuyapinga majaribu ya Shetani, wao wanaona hakuna umuhimu wa kuwa makini na kuwa na ari; na kwamba wanaweza kuenenda bila kufanya hivyo hivyo. Kristo, Mfalme wa utukufu, mara

nyingi sana alienda peke yake milimani na kwenye majangwa kumimina ombi Lake kwa Baba Yake; lakini mwanadamu mdhambi, ambaye hana nguvu, anafikiri kuwa aweza kuishi pasipo maombi mengi. (*Dini ya majaribio ni uzoefu wa Ukristo ambao unasisitiza ujuzi binafsi, mtindo wa maisha na matumizi ya Biblia. Experimental religion is a way of experiencing Christianity that emphasizes personal knowledge and application of the Bible). 1T 504.2

Kristo ni kielelezo chetu; maisha Yake yalikuwa ni mfano wa matendo mema. Alikuwa ni mtu wa huzuni ajuaye sikitiko. Aliililia Yerusalemu kwa kuwa haikupenda kuokolewa kwa kukublai ofa ya ukombozi ambao Yeye aliwapa. Hawakutaka kuja Kwake ili wawe na uzima. Linganisha mwenendo wa maisha yako na ule wa Bwana wako, aliyetoa kafara kubwa ili wewe upate kuokolewa. Mara kwa mara usiku kucha aliutumia akiwa katika ardhi ya unyevunyevu akiomba kwa maumivu makali. Wewe unajitafutia anasa zako mwenyewe. Sikiliza maongezi yaliyo tupu, na ya kipuuzi; sikiliza kicheko, mizaha, na utani. Je, huku ndiko kuiga Kielelezo? Bado unasikiliza je, Yesu anatamkwa? Je, Kweli ni kiini cha mazungumzo hayo? Je, wazungumzaji wanauonea fahari msalaba wa Kristo? Ni mtindo huu, ama kofia ile, ama vazi lile, asemacho kijana yule wa kiume, au kijana yule wa kike, au maburudisho wanayoyapanga. Jinsi wanavyofurahi na kushangilia haya! Je, malaika wanavutiwa kuja kuwazingira na kuwakinga dhidi ya giza ambalo Shetani analishinikiza kwao lipate kuwazunguka? Ah, hapana. Ona, malaika wanavyogeuka kwa huzuni. Ninaona machozi katika nyuso za malaika hawa. Inawezekanaje kwamba malaika wa MUNGU wasababishwe kulia?
Hata hivyo, ndivyo ilivyo. 1T 505.1

Mambo ya umilele hayapewi uzito mkubwa na vijana. Malaika wa MUNGU wanatoa machozi wanapoandika katika gombo maneno na matendo ya wale wanaojiita Wakristo. Malaika wanazunguka mbali nao. Vijana wamekutanika pale; kuna mvumo wa sauti ya nyimbo zinazoimbwa na vyombo vya muziki. Wakristo wamekutana pale, lakini unasikia kitu gani? Ni wimbo kipuuzi uliotungwa, unaofaa katika kumbi za dansi. Tazama malaika watakatifu wanaondoa nuru ya utukufu wao uliowazunguka, na giza linawafunika wale waliomo ndani. Malaika wanaondoka katika tukio hilo. Huzuni iko katika nyuso zao. Tazama, wanalia machozi kwa huzuni. Hili nililiona likirudiwa mara kadha wa kadha kila mahali katika jamii za watunza Sabato, na hasa huko ----. Muziki umechukua masaa ambayo yangelipaswa kutumika kwa ajili ya maombi. Muziki ni sanamu ambayo wengi wa Wakristo wanaojiita watunza Sabato wanaiabudu. Shetani hana shida na muziki kama anaweza kuufanya kuwa mfereji ambao kupitia huo aweza kupenya kuzifikia akili za vijana. Lolote litakamilisha kusudi lake ikiwa litageuza akili kutoka kwa MUNGU na kuutumia muda ambao ungepaswa kutumika kwa ajili ya huduma Yake Mwenyewezi Mungu. Anatenda kazi kwa mbinu ambazo zitaleta tamaa na msukumo wenye mvuto mkubwa

kuwakamata walio wengi katika matamanio ya kupendeza na hisia za ndoto za kufikirika, zisizo na uhalisia kuhusu vitu au mvulana au msichana fulani (infatuation), wakati wanapoozwa kwa nguvu yake. Unapotumika vizuri, muziki ni mbaraka; lakini mara nyingi umetumika kama moja ya mawakala wa Shetani wenye vivutio vikubwa na kuziingiza nafsi katika mtego. Unapotumika vibaya, unawaongoza wale wasio wakfu kuelekea kiburi, ubatili, na upumbavu. Unaporuhusiwa kuchukua nafasi ya sala na maombi, ni laana ya kufisha. Vijana wanakutana kuimba, na, ingawa wanajiita Wakristo, mara nyingi wamemwaibisha MUNGU na imani yao kwa mazungumzo yao ya kipuuzi na aina yao ya muziki waliouchagua. Muziki mtakatifu hauendani na ladha yao. Nilipelekwa kwenye mafundisho yaliyo wazi ya Neno la MUNGU, ambayo yamekuwa yakipuuzwa kwa kutokujua. Katika hukumu maneno haya yote ya uvuvio yatawatia hatiani wale ambao hawakuyazingatia. 1T 505.2

Mtume Paulo anamsihi Timotheo "kwa amri ya MUNGU Mwokozi wetu na Kristo Yesu, Bwana wetu": "Basi, nataka wanaume waombe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata bila hasira wala majadiliano. Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa MUNGU." 1T 506.1

Petro analiandikia kanisa kuwa: "Kwa hiyo vifungeni viuno vya nia zenu, na kuwa na kiasi; mkiitumainia kwa utimilifu ile neema mtakayoletewa katika ufunuo Wake Yesu Kristo. Kama watoto wa kutii msijifananishe na tamaa zenu za kwanza za ujinga wenu; bali kama Yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa Mimi ni mtakatifu." 1T 507.1

Paulo mwenye kuvuviwa anamwongoza Tito kutoa maelekezo maalum kwa kanisa la Kristo, "ili wayapambe mafundisho ya Mwokozi wetu MUNGU katika mambo yote." Anasema: "Nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, MUNGU mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi Yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki Yake Mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema." 1T 507.2

Petro anayasihi makanisa "kuwa na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze." "Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi, iweni na akili, mkeshe katika sala." Tena husema "Bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu. Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini

kwa upole na kwa hofu. Nanyi mwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema katika Kristo. Maana ni afadhali kuteswa kwa kutenda mema, ikiwa ndiyo mapenzi ya MUNGU, kuliko kwa kutenda mabaya.” 1T 507.3

Je vijana wanaweza kumjibu kila mtu awaulizaye sababu ya tumaini lao kwa upole na kwa hofu? Niliona kuwa vijana wanashindwa kabisa kuielewa nafasi yetu. Matukio ya kutisha yapo mbele yao, wakati wa taabu ambao utajaribu thamani ya tabia. Wale walio na Kweli ndani yao wataendelezwa. Wale walioukataa msalaba, na kulipuuza Neno la uzima, na kuzitukuza nafsi zao wenyewe zilizo dhaifu watapungukiwa. Wanawekwa katika mtego na Shetani, na watajifunza huku wakiwa wameshachelewa kuwa wamefanya kosa la kutisha. Anasa walizozitarajia zimekuwa chungu hatimaye. Malaika anasema: “Toa dhabihu yote kwa MUNGU. Nafsi lazima ife/ubinafsi ufe. Matamanio ya asili na mwelekeo wa hulka za moyo usiohuishwa lazima vitiishwe.” Ponyoka kama yule aliye hatarini ili kuikimbilia Biblia yako iliyopuuzwa; Maneno ya uvuvio yanazungumza nawe; usiyapuuze. Kila neno litaletwa kwako ili kutoa hesabu kama umedumu kuwa mtenda kazi ukiyaumba maisha yako kulingana na mafundisho matakatifu ya Neno la MUNGU. Utakatifu wa moyo na mtindo wa maisha ni lazima. Wale wote ambao wamelichukua Jina la Kristo na kuorodheshwa katika huduma Yake wanapaswa kuwa askari wema wa msalaba. Wanapaswa kuonesha kwamba wamekuwa wafu kwa mambo ya ulimwengu na kwamba maisha yao yamefichwa na Kristo katika MUNGU. 1T 507.4

Paulo anawaandikia ndugu zake Wakolosai kama ifuatavyo: “Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa MUNGU. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika MUNGU. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja Naye katika utukufu.” “Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu. Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani. Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa Zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia MUNGU kwa neema mioyoni mwenu. Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Bwana Yesu, mkimshukuru MUNGU Baba kwa yeye.” 1T 508.1

Kwa waefeso anaandika: “Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu. Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana. Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe na Roho; mkisemezana kwa Zaburi na Tenzi na Nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu; na kumshukuru

MUNGU Baba siku zote kwa mambo yote, katika Jina Lake Bwana wetu Yesu Kristo." 1T 509.1

MUNGU hutukuzwa kwa nyimbo za sifa kutoka katika moyo safi uliojazwa na upendo na kujitoa wakfu Kwake. Wakati waaminio walio wakfu wakutanapo, mazungumzo yao hayatakuwa kuhusu kasoro za wengine au harufu ya minong'ono au malalamiko; bali hisani, au upendo, kifungo cha ukamilifu, vitawazunguka. Upendo kwa MUNGU na kwa ndugu zao unatiririka katika maneno yaliyojawa upendo, huruma, na heshima kwa ndugu zao. Amani ya MUNGU inatawala mioyoni mwao; maneno yao si ya kipuuzi, batili, tupu, na ya kijinga, bali yenye faraja na kuimarishana. Kama Wakristo watatii maelekezo waliyopewa na Kristo pamoja na mitume Wake waliovuviwa, watajivika dini ya Biblia na kujiokoa wenyewe kutoka katika majaribu makuu na mkanganyo unaojitokeza kama matokeo ya wao kuamini Kweli isiyopendwa na wengi. Hili ni kosa la kuhuzunisha. Majaribu mengi waliyonayo yanatokana na wao wenyewe kuyapika, sababu wameliacha Neno la MUNGU. Wamejisalimisha kwa ulimwengu, na kujiweka wenyewe katika uwanja wa vita wa adui, na kumjaribu ibilisi ili apate kuwajaribu. Wale ambao wanakubaliana kweli kweli na maonyo pamoja na maelekezo ya Neno la MUNGU, kwa maombi wakitafuta kujua na kufanya mapenzi Yake ya haki, hawatakuwa na manung'uniko madogo-madogo. Kushukuru moyoni waliko nako, na amani ya MUNGU inayotawala ndani vinaamsha wimbo mioyoni mwao kumwendea Bwana, na kwa maneno wanalitaja deni la upendo na shukrani kwa Mwokozi mpendwa, ambaye aliwapenda upeo hadi akafa ili wawe na uzima. Hakuna yeyote aliye na Mwokozi ndani yake, atakayemdharau Bwana mbele ya wengine kwa kutoa msukumo wa muziki wa ala ambao unaiondoa akili kutoka kwa MUNGU nuru ya mbingu na kuielekeza katika mambo madogo madogo yasiyo na maana. 1T 509.2

Katika yote wayafanyayo kwa neno au tendo, vijana wanahitajika kufanya yote katika Jina la Bwana Yesu huku wakitoa shukrani kwa MUNGU na Baba kupitia Kwake. Niliona kuwa vijana wachache wanaelewa kile kinachomaanishwa kuwa Wakristo, yaani kufanana na Kristo. Wanapaswa kujifunza Kweli za Neno la MUNGU kabla hawajafanana nazo na kufanana na Kielelezo/Kristo. Hakuna kijana hata mmoja katika 20, yaani (1/20) ambaye amepitia uzoefu wa kutengana na ulimwengu ambao Bwana anahitaji wawe nao wale wote ambao wangekuwa washirika wa familia yake, yaani watoto wa Mfalme wa mbinguni. "Kwa hiyo, tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa Kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi." 1T 510.1

Ahadi ya ajabu na pekee kiasi gani itolewayo hapa kupitia sharti la utii! Je, unahitaji kujitenga na marafiki pamoja na ndugu ili uweze kufanya maamuzi ya

kuzitii Kweli zilizo kuu za Neno la MUNGU ? Jivike ujasiri, uwe na moyo mkuu, MUNGU amefanya njia kwa ajili yako, mikono Yake mikunjufu ipo tayari kukupokea. Tokeni kati yao, mkatengwe nao, msiguse kitu kilicho kichafu, Naye atawakaribisha. Yeye Anaahidi kuwa Baba kwenu. Oh, uhusiano wa ajabu kiasi gani huu! Ulioinuka, mtakatifu na kutukuka kuliko kifungo chochote cha kidunia. Kama ukijitoa kafara, kama ikibidi hata kuwaacha baba, mama, dada, kaka, mke, na watoto kwa ajili ya Kristo, hatauishi bila marafiki-hautakosa marafiki. MUNGU anakuchukua na kukujumuisha katika familia Yake; unakuwa miongoni mwa wanafamilia wa kifalme, wana na binti wa mfalme atawalaye katika mbingu za mbingu. Je, waweza kuwa na shauku ya wadhifa uliotukuka zaidi ya huu unaoahidiwa hapa? Je, hii haitoshi? Malaika anasema: "Je, ni nini ambacho MUNGU angefanya kwa wanadamu zaidi ya kile ambacho amekifanya? Kama upendo wa namna hii, ahadi zilizotukuka za namna hii hazithaminiwi, Je angeweza kubuni kitu kingine kikubwa zaidi, chenye thamani na ustadi zaidi? Yote ambayo MUNGU angefanya yamekwishafanyika kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu na bado mioyo ya watoto wa wanadamu ni migumu. Kwa sababu ya baraka zilizosheheni, ambazo MUNGU amewaruzuku na kuwazungushia, wanazipokea kama vitu vya kawaida na kumsahau mfadhili wao Mwenye neema." 1T 510.2

Niliona kuwa Shetani ni adui aliye macho mwenye kusudi la kuongoza vijana kufanya matendo ambayo ni kinyume kabisa na yale ambayo MUNGU angeyakubali. Anajua kabisakabisa kwamba hakuna kundi lingine liwezalo kufanya vizuri sana kama vijana wa kiume na wa kike ambao wamejitoa wakfu kwa MUNGU. Vijana kama wengekuwa sahihi, wangesomba na kurundika ushawishi mkubwa. Wahubiri, au walei waliofanya kazi kwa miaka mingi, hawawezi kufikia hata nusu ya mvuto walionao vijana, ambao wamejitoa wakfu kwa MUNGU. Wanapaswa kuhisi kuwa wanao wajibu wa kufanya yote wawezayo, kuwaokoa wanadamu wenzao hata kama ikibidi kuachana na anasa na matamanio yao. Muda, na hata malli na mbinu, kama vikihitajika, vinapaswa kuwekwa wakfu kwa MUNGU. Wale wote wanaodai kuwa watauwa wanapaswa kuiona hatari ya wale walio nje ya Kristo. Hivi karibuni muda wao wa rehema utafungwa. Wale ambao wangeonesha mvuto kuziokoa nafsi, na kusimama katika mashauri ya MUNGU lakini bado wakashindwa kutimiza wajibu wao kwa sababu ya ubinafsi, uvivu, au kwa sababu waliuonea aibu msalaba wa Kristo, siyo tu kwamba watazipoteza nafsi zao wenyewe, bali na damu ya wadhambi masikini itakuwa katika mavazi yao. Hao nao watahitajika kutoa hesabu kwa mambo ambayo wangeliyatenda kama wangelijiweka wakfu kwa MUNGU, lakini hawakuyatenda kwa kukosa kwao uaminifu. Wale ambao wameonja utamu wa upendo unaookoa hawatuliii na wala hawatatulia mpaka wote wanaohusiana kuwajua, wamefahamishwa mpango wa wokovu. Kijana anapaswa kuuliza: "Je, ni napaswa kutenda nini?' Ninawezaje kuliheshimu na kulitukuza Jina Lako ulimwenguni" Nafsi zinapotea kila mahali kutuzunguka (watu wanapotea kila

mahali), na bado ni jitihada gani walizonazo vijana kuleta nafsi kwa Kristo? Wale waendao shuleni wangelikuwa na mvuto kwa ajili ya Mwokozi; lakini ni nani anayelitaja Jina la Kristo? na ni akina nani wanaonekana kuomba kwa dhati pamoja na wenzi wao ili waweze kuachana na njia za dhambi na kuchagua njia ya utauwa/utakatifu? 1T 511.1

Nilioneshwa kwamba hii ndio njia ambayo vijana waaminio wanapaswa kuipitia, lakini hawafanyi hivyo; Ni rmtelekmko zaidi kwa hisia zao kuungana na mdhambi katika michezo na anasa. Vijana wanao uwanja mpana zaidi wa kunufaisha, lakini hawauoni. Oh, laiti wangelishinikiza sasa nguvu zao za kiakili ili kutafuta namna ya kuwafikia wadhambi wanaopotea, laiti wangeliwafahamisha njia ya utauwa, na kwa maombi na kusihi wakaleta hata mtu mmoja kwa Kristo! Ni mradi uliotukuka kwa kiasi gani! Nafsi moja kumsifu MUNGU milele na milele! Nafsi moja kufurahia furaha na uzima wa milele! Kito kimoja katika taji yao kung'aa kama nyota milele na milele! Lakini hata zaidi ya mtu mmoja wanaweza kubadilika kutoka kwenye kosa hadi kwenye kwenye ile Kweli, kutoka katika dhambi hadi kwenye utakatifu. Bwana anasema kupitia nabii: "Na hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na milele." Kisha wale wanaoungana na Kristo pamoja na malaika katika kazi ya kuokoa roho zinazopotea wanatunukiwa kwa shehena tajiri katika ufalme wa mbinguni. 1T 512.1

Niliona kuwa nafsi nyingi zingeokolewa kama vijana wangekuwa wanapopaswa kuwa, kujitoa kwa MUNGU na kwa ile Kweli; lakini kwa ujumla wanakaa katika nafasi ambayo kazi ya kudumu lazima ifanyike juu yao vinginevyo wao wenyewe watakuwa wa ulimwengu wenyewe. Ni chanzo cha wasiwasi wa kudumu na maumivu mazito ya moyo. Machozi yanatiririka kwa sababu yao, na maombi ya uchungu yanasikika kutoka katika mioyo ya wazazi kwa niaba yao. Na bado wanaendelea kusfiri pasipo kujali au kusumbuka na maumivu ambayo wameyasababisha. Wanapanda miiba katika vifua vya wale ambao wangelikufa ili wao waokolewe na wenyewe kuwa vile ambavyo MUNGU alikusudia wao kudhihirisha manufaa ya damu ya Kristo. 1T 512.2

Vijana wanafanyia kazi uwezo wao wa kufanya hili na lile kisanaa au utalaamu (art), lakini hawahisi kuwa MUNGU anawataka wao wageuze talanta zao kufanya vitu bora zaidi, kama kujivika imani yao na kutafuta kuokoa nafsi ambazo Kristo alizifia. Nafsi moja iliyookolewa ni ya thamani zaidi kuliko malimwengu/sayri. Dhahabu na hazina za kidunia kamwe haziwezi kulinganishwa na wokovu wa hata nafsi moja. 1T 512.3

Vijana wa kiume na wa kike, niliona kuwa MUNGU anayo kazi kwenu mnayopaswa kuifanya; jitwikeni msalaba wenu na kumfuata Kristo, vinginevyo hamumstahili Yeye Mnawezaje kuzungumza lile lililo mapenzi ya MUNGU

kwenu wakati mmekosa ari? Na mnawezaje kutarajia kuokolewa kama hamfanyi mapenzi ya Bwana wenu kama watumishi waaminifu? Wale ambao wana uzima wa milele wote watakuwa wote wamefanya vema. Mfalme wa utukufu atawawekea mkono wake wa kuume huku akiwaambia; “Vema, watumwa wema na waaminifu.” Je mmeweza kuhesabu wingi wa roho ambazo mngeziokoa kutoka katika kifungo kama, badala ya kujifunza kufanya anasa zenu, mlikuwa mkitafuta kazi ambayo mngeifanya katika shamba la mzabibu la Bwana wenu? Ni watu wangapi ambao wanakusanyika hapo kusikiliza hizi nyimbo ambao wanafanyika kuwa njia ya wokovu katika mikusanyiko hii ya mazungumzo na mazoezi ya muziki? Kama hamwezi kuonesha roho moja ambayo kupitia ninyi imeokolewa badilikeni, Oh, geukeni, badilikeni muwe na mtazamo mpya. Anzeni kuomba kwa ajili ya watu-roho, njooni karibu na Kristo, karibu na bubujiko la damu Yake. Hebu roho ya upole, unyenyekevu na utulivu ikae maishani mwenu, na maombi ya dhati na unyenyekevu yapande kwake ili muweze kupata hekima sio tu ya kuziokoa sio tu nafsi zenu mwenyewe, bali pia na nafsi za wengine. Ombeni zaidi kuliko mnavyoimba. Je, hampo katika wakati ambao una uhitaji mkubwa wa maombi kuliko wa kuimba? Vijana wa kiume na wa kike, MUNGU anawaita kazini, mtumikieni. Badilini kabisa mitazamo yenu. Mnaweza kufanya kazi ambayo watumishi wa Neno na mafundisho hawawezi kuifanya. Mnaweza kulifikia tabaka ambalo mchungaji hawezi kulifikia. 1T 513.1

## SURA YA 87

## BURUDANI KWA WAKRISTO

Nilioneshwa kuwa watunza Sabato ni watu ambao hufanya kazi kwa bidii bila kujiruhusu wao wenyewe mabadiliko au kuwa na vipindi vya mapumziko. Burudani ni muhimu kwa wale ambao wanafanya kazi za mwili/mikono na bado ni muhimu zaidi kwa wale ambao wanafanya kazi za kutumia akili zaidi. Siyo lazima kwa wokovu wetu, wala kwa utukufu wa MUNGU, kuiweka akili ifanye kazi kila wakati kupita kiasi, hata kama ni kuhusiana na mambo ya kidini. Kuna burudani, kama vile kucheza dansi, (kucheza ngoma?), kucheza kadi, bao, drafti, (checkers, chess), nk, ambayo hatuwezi kuyaidhinisha, kwa sababu Mbingu inayalaani. Burudani hizi hufungua mlango wa uovu mkubwa. Hazina faida katika tabia yao, bali zina ushawishi wa kusisimua, na katika akili za watu hupelekea shauku ya michezo hiyo ambayo husababisha kamari na uuharibifu. Michezo yote kama hii inapaswa kulaaniwa na Wakristo, na kitu kisicho na hatia kabisa kinapaswa kuwa badala ya michezo hiyo. {1T 514.1}

Niliona kwamba sikukuu na likizo zetu hazipaswi kutumiwa katika kufuata mfano wa ulimwengu, pia hazipaswi kupitwa bila kutambuliwa, kwani hii italeta hali ya kutoridhika kwa watoto wetu. Katika siku hizi ambazo kuna hatari kwamba watoto wetu wataathiriwa na ushawishi mbaya, na kuharibiwa na raha na msisimko wa ulimwengu, hebu wazazi wafanye utafiti na kujifunza kupata kitu kitakachokuwa mbadala wa burudani zenye hatari zaidi. Wafanye watoto wenu waelewe kwamba ninyi mna mtazamo mzuri na wenye furaha kwao, kwamba mnawazia mema. {1T 514.2}

Hebu familia kadhaa zinazoishi mjini au kijijini ziungane na kuacha kazi ambazo zimewachosha mwili na akili, kisha zifanye safari kwenda pembezoni mwa ziwa zuri au kwenye shamba zuri ambapo mandhari ya asili/uumbaji ni mazuri. Wanapaswa kujipatia chakula safi, kizuri, matunda na nafaka bora, na kutandaza meza yao chini ya kivuli cha mti au chini ya dari ya mbinguni. Kuendesha baiskeli au farasi, mazoezi, na mandhari vitaongeza hamu ya kula, na wanaweza kufurahia raha ambayo wafalme wanaweza kuihusudu/kuitamani. {1T 514.3}

Katika matukio kama hayo wazazi na watoto wanapaswa kujisikia huru kutoka katika masumbufu, uchungu wa kazi, na kuchanganyikiwa. Wazazi wanapaswa kuwa watoto wakiwa na watoto wao, wakifanya kila kitu kuwa cha kupendeza kwao kadri iwezekanavyo. Hebu siku nzima itumiwe kwa burudani. Mazoezi katika uwanja wa wazi kwa wale ambao kazi zao zimekuwa za ndani kwa kukaa tu, na haya yatakuwa na faida kwa afya. Wote wanaoweza, wanapaswa kuhisi jukumu la kufuata hatua hii. Hakuna kitakachopotea, bali watanufaika sana- faida tupu. Wanaweza kurudi kazini kwao na maisha mapya na ujasiri mpya wa kushiriki katika kazi yao kwa bidii, na wakiwa wamejiandaa vyema kupinga magonjwa. {1T 515.1}

Niliona kuwa ni wachache tu wanaotambua kazi ya daima ya kuchosha ya wale ambao wanabeba majukumu ya kazi ofisini. Wao wameganda ndani ya nyumba ndogo siku baada ya siku na wiki baada ya wiki, wakati shida endelevu juu ya nguvu za kiakili hakika inadhoofisha uwezo wao na kupunguza muda wao wa kuishi. Ndugu hawa wako katika hatari ya kuvunjika ghafla. Wao hawaishi milele, na wasipokuwa na mabadiliko lazima wachoke,wachakae na kukosekana kazini. {1T 515.2}

Tuna karama za thamani ndani ya ndugu A, B, na C. Hatuwezi kumudu kuwaona wakiziharibu afya zao kwa kufungwa katika kazi ngumu. Wapi tunaweza kupata watu wenye uzoefu kama kuchukua nafasi zao? Wawili kati ya ndugu hawa wamekuwa wakishikamana na kazi ofisini kwa miaka kumi na nne, wakifanya kazi kwa bidii, kwa uangalifu, na bila ubinafsi kwa ajili ya maendeleo ya kazi ya MUNGU. Wamekuwa na mabadiliko machache sana hasa ambayo yaliletwa na homa na magonjwa mengine. Wanapaswa kuwa na mabadiliko ya mara kwa mara, lazima mara nyingi watumie siku nzima kwa burudani na familia zao, ambazo ziko karibu kutengwa na jamii yao. Wote hawawezi kuacha kazi kwa wakati mmoja kwenda kwenye burudani; lakini wanapaswa kupanga kazi zao ili mmoja au wawili waende, na kuwaacha wengine wakishika nafasi zao, na kisha wawapatie hawa nao fursa sawa. {1T 515.3}

Niliona kwamba hawa ndugu, A, B, na C, wanapaswa waone kwamba ni wajibu wao kidini kutunza afya na nguvu ambazo MUNGU amewapa. Bwana hawahitaji wao sasa kuwa wafia dini kwa sababu Yake. Hawatapata thawabu yoyote kwa kutoa dhabihu hii, kwani MUNGU anataka waishi. Wanaweza kutumikia sababu ya Ukweli wa sasa bora zaidi na maisha yao kuliko kwa kifo chao. Ikiwa yeyote kati ya hawa ndugu apate kubamizwa ghafla kwa ugonjwa, hakuna mtu anayepaswa kuiona hii kama hukumu ya moja kwa moja kutoka kwa Bwana. Itakuwa tu matokeo ya uhakika ya ukiukaji wa sheria za asili. Wanapaswa kuzingatia onyo lililotolewa, wasije wakakiuka na wakapata adhabu nzito. {1T 515.4}

Niliona kwamba hawa ndugu wanaweza kufaidika na kusudi la MUNGU kwa kuhudhuria, mara nyingi iwezekanavyo katika mikutano ya kusanyiko mbali na mahali pao pa kazi (convocation/retreat). Kazi waliyopewa ni muhimu, na wanahitaji mishipa ya fahamu na akili yenye afya; lakini haiwezekani akili zao kuimarishwa na kuongezewa nguvu kama ambavyo MUNGU angewataka, ikiwa daima wanajifungia ofisini. Nilioneshwa kuwa itakuwa faida kwa ujumla kwa watu hawa, ambao wamesimama kama wasimamizi wa kazi huko Battle Creek, kufahamiana na ndugu zao wa ng’ambo kwa kushirikiana nao katika mkutano. Itawapatia imani hao ndugu wa nje ya nchi katika wale wanaobeba majukumu ya kazi, na itawasaidia ndugu hawa katika kuushughulisha ubongo, na itawafanya wafahamu vizuri maendeleo na mahitaji ya kazi hiyo. Itayahuisha

matumaini yao, itafanya upya imani yao, na kuongeza ujasiri wao. Kwa hiyo muda uliotumiwa hautapotea, bali utatumika kwa faida nzuri zaidi. Ndugu hawa wana sifa ambazo zinawafanya kwa kiwango cha juu kuweza kufurahia maisha ya kijamii. Wangefurahia kukaa kwao katika nyumba za ndugu zao wa ng'ambo, na wangewafaidisha na kufaidika kwa kubadilishana mawazo na mitazamo. {1T 516.1}

Ninatoa wito hasa kwa kaka C kudilisha maisha yake. Hawezi kufanya mazoezi kama wengine ofisini wanavyofanya. Ajira ya ndani ya jengo, ya kukaa kwenye kiti siku nzima inamuandaa kuvunjika ghafla. Hawezi kufanya kila wakati kama ambavyo amekuwa akifanya. Anapaswa kutumia muda mwingi eneo la wazi lenye hewa, akiwa na vipindi vya kazi nyepesi ya asili maalum kwa mikono yake, au mazoezi yenye tabia nzuri ya kujiburudisha. Vile anavyojifungia ndani ya jengo na kukaa kwenye kiti hapo kwenye ajira yake ni jambo ambalo lingeweza kumfanya hata mnyama mwenye nguvu za kutisha kupunguza nguvu zake za mwili. Anafanya ukatili, ubaya, dhambi dhidi yake mwenyewe, na mimi napaza sauti yangu ya onyo dhidi ya dhambi hiyo. Kaka C, muda wako mwingi unapaswa kutumiwa nje, kwa kupanda farasi/baiskeli au kufanya mazoezi ya kupendeza, vinginevyo lazima ufe, mke wako awe mjane, na watoto wako wanaokupenda sana na unaowapenda, wabaki wakiwa yatima. Kaka C ana sifa ya kuwajenga wengine katika ufafanuzi wa Neno. Anaweza kutumikia kusudi la MUNGU na kujinufaisha mwenyewe kwa kwenda kwenye mikusanyiko mikubwa ya watunza Sabato na kutoa ushuhuda wake kwa kuwajenga wale ambao wamebahatika kumsikia. Mabadiliko haya yangemleta zaidi nje ya nyumba, kwenye hewa ya nje. Damu yake inatiririka pole pole kupitia mishipa yake kwa kukosa hewa ya nzuri na yenye nguvu ya mbinguni. Amefanya vizuri sehemu yake katika kazi ofisini, lakini bado anahitaji ushawishi wa furaha wa hewa safi na mwanga wa jua nje ya nyumba ili kuifanya kazi yake iwe ya kiroho, hai na ya kufurahisha zaidi. {1T 516.2}

Juni 5, 1863, nilioneshwa kwamba mume wangu anapaswa kuhifadhi nguvu na afya yake, kwani MUNGU alikuwa bado na kazi kubwa kwetu ya kufanya. Katika fadhila Zake tulikuwa tumepata uzoefu katika kazi hii tangu kuanzishwa kwake, na kwa hivyo utumishi wetu ungekuwa ya muhimu sana kwa kazi Yake. Niliona kwamba kazi ya mara kwa mara na ya kupindukia ya mume wangu ilikuwa ikimchosha nguvu yake, ambazo MUNGU angemtaka azihifadhi; kwamba ikiwa angeendelea kuzifanyisha kazi kupita kiasi nguvu zake za mwili na akili kama alivyokuwa akifanya, angekuwa anatumia rasilimali zake za baadaye za nguvu na kumaliza mtaji wa mwili, na angezeeka mapema, na kazi ya MUNGU ingepungukiwa na utumishi wake. Wakati mwingi alikuwa akifanya kazi iliyounganishwa na ofisi ambayo wengine wangeweza kuifanya, au alikuwa akiijingiza katika miamala biashara ambazo angepaswa kuziepukana (biashara ya uchapaji). MUNGU angetutaka wote tuhifadhi nguvu zetu ili zitumiwe

zinapohitajika kufanya kazi hiyo ambayo wengine wasingeweza kuifanya, na ambayo kwayo ametutunza, akahifadhi maisha yetu, na kutupa uzoefu muhimu; kwa njia hii tuweze kuwa faida kwa watu Wake. {1T 517.1}

Sikuliweka hili hadharani, kwa sababu lilitolewa kwa ajili yetu hasa. Ikiwa tahadhari hii ingezingatiwa kikamilifu, shida ambayo mume wangu amekuwa akihangaika, na kuteseka nayo sana ingeondoka. Kazi ya MUNGU ilikuwa ya dharura na ilionekana hairuhusu kupumzika au kujitenga nayo. Mume wangu alionekana kulazimika kufanya kazi kila wakati, kazi ya kuchosha. Wasiwasi kwa ajili ya ndugu zake waliokuwa baridi, na pia juu ya uasi huko Iowa, viliifanya akili yake kuendelea kukaza kwa msongo zaidi, na nguvu za mwili zilimaliza kabisa. Badala ya kupata ahueni, mizigo ilimlemea zaidi; na masumbufu badala ya kupungua, yaliongezeka. Lakini hakika kulikuwa na njia ya kutokea, la sivyo MUNGU asingetoa tahadhari aliyotoa na asingemruhusu achoshwe na kuvunjika na shughuli. Nikaona kwamba kama asingelitegemezwa na MUNGU angeligundua kutindikiwa kwa nguvu zake za mwili na akili mapema zaidi kuliko ilivyokuwa. {1T 518.1}

MUNGU anaposema, anamaanisha kile anachosema. Anapoonya, inapaswa kuwa kwa wale wahusika kuzingatia. Sababu kwa nini sasa ninazungumza hadharani ni kwamba tahadhari ile ile ambayo alipewa mume wangu wamepewa wengine wanaohusiana na ofisi. Niliona kwamba wasipobadilisha mwenendo wao, wanawajibika kuathirika zaidi kama ilivyokuwa kwa mume wangu. Siko tayari kwamba wengine wateseke kama yeye alivyoteseka. Lakini kile kinachotisha zaidi ni hiki, wangepotezwa kwa haraka katika kusudi na kazi ya MUNGU, wakati msaada na ushawishi wa wote vinahitajika sana. {1T 518.2}

Wale ambao wameunganishwa na ofisi hawawezi kuvumilia kiwango cha masumbufu na kazi ambayo mume wangu ameibeba kwa miaka. Hawana afya, mwili, ambavyo ni mtaji wa kuendeshea shughuli, ambavyo mume wangu alikuwa navyo. Hawawezi kamwe kuvumilia wasiwasi, fadhaa na uchovu wa kudumu wa kazi, ambavyo alikuwa navyo na ambayo amekuwa nayo kwa miaka ishirini. Siwezi kuvumilia wazo kwamba yeyote katika ofisi atoe nguvu na afya yake kwa kazi nyingi, ili faida yao iishe mapema na wasiweze kufanya kazi katika shamba la Bwana. Siyo wavunaji wa matunda ambao ndio watumishi muhimu pekee; bali wote wanaosaidia kulima kwa ajili ya mimea, kumwagilia, kupogoa, na kuinua matawi iliyozama, kufuatisha mizabibu, na kuiongoza kwenye mwelekeo wao wa kuingiliana juu ya miti ya kweli, msaada wa Kweli, ni watumishi ambao hawawezi kupotezwa. {1T 518.3}

Ndugu walioko ofisini wanahisi kuwa hawawezi kuacha kazi hata kwa siku chache kwa ajili ya mapumziko, burudani; lakini hili ni kosa. Wanaweza na wanapaswa kufanya hivyo. Hata kama hakukuwa na mafanikio mengi, ingekuwa

bora waondoke kwa siku chache kuliko kusumbuliwa na magonjwa na kutenganishwa na kazi hiyo kwa miezi, na labda wasiweze kushiriki tena. {1T 519.1}

Mume wangu alifikiri ni vibaya kwake kutumia muda katika raha ya kijamii (social enjoyment). Hakuweza kupumzika. Alidhani kuwa kazi katika ofisi hiyo ingeathirika kama angefanya hivyo. Lakini baada ya kuangukiwa na kipigo, na kusababisha ugonjwa wa kimwili na kiakili, ilibidi kazi ifanyike bila yeye. Niliona kwamba ndugu wanaofanya kazi ya ofisini wanapaswa kufanya kazi kwa mpango tofauti na kuifanya mikakati yao kuwa na mabadiliko. Ikiwa msaada wa watu zaidi unahitajika, upateni huo, na wale wanaougua katika vifungo vya kazi za ubongo za kila wakati wapate nafuu. Wanapaswa kuhudhuria kusanyiko la mkutano (makambi etc). Wanahitaji kutupilia mbali masumbufu, kushiriki ukarimu wa ndugu zao, na kufurahia jamii yao na baraka za mikutano. Kwa hivyo watapokea mawazo mapya, na nguvu zao zilizochoka zitaamshwa kwa maisha mapya, na watarudi kazini wakiwa bora zaidi katika kutekeleza majukumu yao, kwani wataelewa vizuri mahitaji ya kazi hiyo. {1T 519.2}

Ndugu zangu mlioko ng'ambo, mmelala katika jambo hili? Je! Mioyo yenu inapaswa kufifia kwa kuanguka kwa kifo cha mtumishi mwingine wa MUNGU, ambaye mnampenda? Watu hawa ni mali ya kanisa. Je! Mtawaruhusu kuuawa na mizigo? Nawasihi mshauri utaratibu mambo ulio tofauti. Ninamuomba MUNGU kwamba uzoefu mchungu ambao umetupata kamwe usiruhusiwe kumjia ndugu yeyote ofisini. Hasa ninampongeza kaka C kwa kujali kwenu. Je! Afe kwa kukosa hewa, hewa muhimu ya mbinguni? Kazi anayoifanya inafupisha maisha yake. Kwa kufungwa kwake ndani ya nyumba damu yake inakuwa chafu, goigoi na isiyotumika sana, ini limevurugika, mapigo ya moyo hayako sawa. Asipofanya mabadiliko mwenyewe, asili itachukua kazi hiyo mikononi mwake. Itafanya jaribio kubwa la kutoa aueni kwa mfumo kwa kutoa uchafu kutoka kwenye damu. Itaamrisha nguvu zote muhimu zifanye kazi, na mwili/kiumbe kizima kitavurugika, na hii yote inaweza kupelekea kupooza au kupata kiharusi. Ikiwa atapona kutoka katika shida hii, upotezaji wake wa muda utakuwa mkubwa; lakini uwezekano wa kupona ni mdogo sana. Endapo kaka C hawezi kuzinduka, nawashauri, ndugu, ambao wana nia ya Ukweli wa sasa, mchukueni, kama vile Luther alivyochukuliwa na marafiki zake, na kumpeleka mbali na kazi yake. {1T 520.1}

Tangu niandike hapo juu, nimejifunza kwamba mawazo mengi juu ya Ufunuo, yaliandikwa usiku, baada ya kazi ya uandishi wa siku ilikuwa imefanywa. Hii ilikuwa hatua ambayo mume wangu aliifuata; Napinga kujiua huku. Ndugu ambao nimewataja, ambao wamefungwa sana na ofisi, wangekuwa wakimtumikia kazi ya MUNGU kwa kuhudhuria mikutano na kupata vipindi vya burudani. Wangekuwa wakihifadhi afya ya mwili na nguvu ya akili katika hali

bora ya kujitoa kwa kazi hiyo. Hawapaswi kuachwa kujisikia vilema kwa sababu hawapati mshahara. Mshahara wao uendelee na wawe huru. Hawa wanafanya kazi kubwa. {1T 520.2}



## SURA YA 88

## MATENGENEZO YA MAVAZI

(Inchi nane kutoka kwenye ardhi au sentimeta kama 20 hivi!)

Kwa kujibu barua za maswali kutoka kwa akina dada wengi kulingana na urefu unaofaa wa matengenezo ya mavazi, ningesema kwamba katika sehemu yetu ya Jimbo la Michigan tumepitisha urefu wa inchi tisa kutoka sakafuni. Ninachukua fursa hii kujibu maswali haya ili kuokoa wakati unaohitajika kujibu barua nyingi. Ningepaswa kusema hapo awali, lakini nilikuwa nikingojea kuona jambo la uhakika juu ya hatua hii katika matengenezo ya afya. Napenda kwa dhati kupendekeza urefu sawa, na ningependa kusema kwamba inchi tisa kama maoni yangu juu ya jambo hili yanavyokubaliana kama ninavyoweza kulielezea kwa inchi za urefu. {1T 521.1}

Ninaposafiri mahali mahali ninaona matengenezo ya mavazi hayajawakilishwa ipasavyo, na ninafanywa kuhisi kwamba jambo dhahiri zaidi linapaswa kusemwa ili ziwepo hatua sawa katika jambo hili. Mtindo huu wa mavazi haupendwi, na kwa sababu hii unadhifu na ladha vinapaswa kutekelezwa na wale wanaopitisha au kupokea hili vazi. Nimewahi kuzungumza juu ya hatua hii, lakini wengine wanashindwa kufuata ushauri uliotolewa. Kunapaswa kuwepo kwa usawa wa urefu wa mavazi ya matengenezo miongoni mwa watunza Sabato. Wale wanaojifanya wa kipekee kwa kuyapitisha mavazi haya hawapaswi kufikiria hata kwa muda mfupi kwamba siyo lazima kuonesha mpangilio, ladha, na unadhifu. Kabla ya kuvaa mavazi ya matengenezo, dada zetu wanapaswa kupata pateni/mfano wa mavazi ya suruali na nguo kubwa zinazovaliwa nayo ndani kwanza. Ni jeraha kubwa kwa matengenezo ya mavazi kuwa na watu wanaoingiza katika jamii mtindo ambao kwa kila mtu unahitaji marekebisho kabla ya kuwakilisha mavazi ya matengenezo. Subirini, akina dada, mpaka mtakapoweza kuyavaa mavazi hayo kwa usahihi. {1T 521.2}


gauni la calico

https://answersforadventists.wordpress.com/resources/articles-2/womens-pants-dress-reform/

Angalia zaidi kwenye hii link, na mwisho wa kitabu hiki kuhusu maswali ya matengenezo ya mavazi yalivyojibiwa, asante. Angalia kitabu cha matengenezo ya mavazi pia, kama huna cha Kiswahili tutakutumia, tuandikie email ipo pale mwanzo wa kitabu.

Katika baadhi ya maeneo kuna upinzani mkubwa kuhusiana na mavazi mafupi (nchi tisa kutoka kwenye ardhi). Lakini ninapoona nguo fulani zimevaliwa na akina dada, sishangai kwamba watu wamechukizwa na kulaani mavazi hayo. Mahali ambapo mavazi yamewakilishwa kama yanavyopaswa kuwa, watu wote wazuri wanalazimika kukubali kuwa ni ya kawaida na rahisi. Katika baadhi ya makanisa yetu nimeona kila aina ya mavazi yanayohitaji matengenezo, na bado hakuna hata mmoja anayejibu maelezo yaliyowasilishwa mbele yangu. Wengine huonekana suruali kubwa wanazovaa ndani ya magauni (muslin pants) na nguo za mikono myeupe, magauni ya masweta (dark delaine dress), na mavazi magauni makubwa kama gunia yasiyo na mikono (sleeveless sack). Wengine wana mavazi ya pamba ya kahawia yanaitwa kaliko/kaniki na suruali iliyokatwa kwa mitindo yao wenyewe, si kwa "mfano," ambazo hazijanyooshwa pasi kwa wanga, hivyo hazina mwonekano mzuri, na kukaribia miguu kwa vile hazina wanga za kufanya zifutuke. Hakuna kitu chochote katika nguo hizi kinachoonesha ladha au mpangilio. Nguo kama hizo haziwezi kujipendekeza kwenye uamuzi mzuri wa watu wenye busara. Katika kila maana ya neno hilo ni mavazi yenye kasoro. {1T 521.3}

Akina dada wenye waume wanaopinga wameomba ushauri wangu kuhusu jinsi ya kuvaa mavazi ya wastani kinyume na matakwa ya waume zao. Nawashauri wasubiri. Silifikirii suala la mavazi kama la muhimu sana kama ilivyo Sabato (badala ya kuvaa vazi refu linalofika miguuni, wavae gauni sentimeta 20 kutoka

kwenye ardhi au inchi tisa kutoka kwenye ardhi (3/4 ya rula). Kuhusiana na Sabato hilo halina cha kusita lazima lifuatwe. Lakini upinzani ambao wengi wangepokea ikiwa wangechukua matengenezo ya mavazi ungekuwa mabaya zaidi kwa afya kuliko faida ya mavazi hayo. Akina dada kadhaa wameniambia: "Mume wangu anayapenda mavazi yako; anasema hajapata neno hata moja la makosa katika mavazi yako." Hili limeniongoza kuona ulazima wa dada zetu kuwakilisha vizuri matengenezo ya mavazi, kwa kuonesha unadhifu, utulivu, na usawa katika mavazi. Nitakuwa na pateni/mifano iliyoandaliwa ili niwe nayo tayari wakati tunaposafiri kwa ajili ya kuwapa dada zetu ambao tutakutana nao, au kuwatumia kwa posta wote ambao wanaweza kuagiza. Anwani yetu itatolewa katika gazeti la *Review*. {1T 522.1}

Wale wanaoiga mavazi ya wastani wanapaswa kuonesha ladha katika uchaguzi wa rangi (gauni lisilokuwa refu sana, lililoitwa short dress). Wale ambao hawawezi kununua nguo mpya lazima wafanye kila wawezalo kutumia ladha na busara katika kurekebisha/kukarabati mavazi ya zamani, na kuyafanya kuwa mapya tena. Kuwa na suruali na mavazi ya rangi na aina sawa, haya yataleta mwonekano mzuri sana. Mavazi ya zamani yanaweza kukatwa kwa muundo sahihi na kupangwa kwa ladha, na kuonekana kama mapya. Ninawaomba, akina dada, msijenge mfano wenu kulingana na maoni yenu wenyewe. Wakati kuna pateni/mfano sahihi na ladha nzuri, pia kuna mifano isiyo sahihi na yenye ladha mbaya. {1T 522.2}

Nguo hii haihitaji hoops (gagulo la chuma au la miiba ya papa), na natumai kuwa vazi hili halitaaibishwa kamwe. Dada zetu hawahitaji kuvaa sketi nyingi li kufanya vazi litanuke na kuwa kama mwamvuli mkubwa. Inaonekana vizuri zaidi kuangukia sketi nyepesi moja au mbili ianguke kwa mwili ili mwonekano usiwe wa bandia/feki. Kitambaa cha moreen ni kizuri kwa sketi ya nje kwa vile hakitepeti, kinadumu na hivyo kinanyooka vizuri. Nguo nzito kama quilts au mablanketi hazihitajiki. Lakini huwa naona zikivaliwa, na wakati mwingine zikining'inia kuizidi nguo iliyovaliwa, kidogo. Hii inatoa mwonekano usio mzuri-haina staha au unadhifu. Sketi nyeupe, zilizovaliwa na nguo nyeusi, haziwi nguo fupi (inchi tisa kutoka kwenye ardhi). Muwe na sketi ambazo ni safi, nadhifu, na nzuri; mzifanye ziwe nzuri na katika hali zote ziwe fupi angalau inchi tatu kuliko mavazi. Ikiwa kitu chochote kimevaliwa ili kuiongeza sketi hiyo, basi kiwe kidogo na angalau robo moja yadi kutoka chini ya mavazi au sketi ya nje. Ikiwa kamba, au kitu chochote badala ya kamba, kimewekwa moja kwa moja karibu na sehemu ya chini ya sketi hiyo (lesi), inaongeza mavazi upande wa chini tu, na kuyafanya yaonekane kuwa hayapendezi wakati aliyeyavaa anapoketi au kuinama. {1T 523.1}

Hakuna anayehitaji kuogopa kwamba nitalifanya suala la matengenezo ya mavazi kuwa moja ya masomo yangu makuu tunaposafiri mahali mbalimbali.

Wale ambao wamenisikia juu ya jambo hili watalazimika kuchukua hatua kwa nuru ambayo tayari wamepewa. Nimetimiza wajibu wangu; Nimetoa ushuhuda wangu, na wale ambao wamenisikia na kusoma yale ambayo nimeyaandika lazima sasa wawe na jukumu la kupokea au kukataa nuru iliyotolewa. Ikiwa watachagua kujitosa kuwa wasikiaji wanaosahau, na siyo watendaji wa jambo hilo, wanajihatarisha wenyewe na watawajibika kwa MUNGU kwa hatua waliyoichukua. Nimeweka wazi. Sitamshawishi yeyote na sitamhukumu yeyote. Hii siyo kazi niliyopewa. MUNGU anawajua watoto Wake wanyenyekevu, walio tayari na watiifu, Naye atawapa thawabu kulingana na utendaji wao wa uaminifu wa mapenzi Yake. Kwa wengi matengenezo ya mavazi ni sahil sana na wanaona watanyenyekeshwa sana wakiyavaa. Hawawezi kuuinua msalaba. MUNGU hufanya kazi kwa njia rahisi kutenganisha na kuwatofautisha watoto Wake na ulimwengu; lakini wengine wameachana na usahili na unyenyekevu wa kazi na njia za MUNGU kiasi kwamba wako juu ya kazi, siyo ndani yake. {1T 523.2}

Nilielekezwa katika kitabu cha Hesabu 15: 38-41: " Nena na wana wa Israeli, na kuwaagiza ya kwamba wajifanyie vishada katika ncha za nguo zao, katika vizazi vyao, tena ya kwamba watie katika kila kishada cha kila ncha nyuzi za rangi ya samawi; nacho kitakuwa kwenu ni kishada, ili mpate kukiangalia, na kuyakumbuka maagizo yote ya Bwana, na kuyafanya; tena kwamba msiende kutanga-tanga kuandama mioyo yenu wenyewe, na macho yenu wenyewe, ambayo mlikuwa mkiyaandama kwa uasherati hapo kwanza; ili mpate kukumbuka na kuyafanya maagizo Yangu yote, na kuwa watakatifu kwa MUNGU wenu. Mimi Ndimi Bwana, MUNGU wenu, niliyewaleta kutoka nchi ya Misri, ili kwamba niwe MUNGU wenu; Mimi Ndimi Bwana, MUNGU wenu. " Hapa MUNGU aliamuru waziwazi mpangilio rahisi sana wa mavazi kwa watoto wa Israeli kwa kusudi la kuwatofautisha na mataifa yaliyowazunguka ambayo yaliabudu sanamu. Walipotazama upekee wao wa mavazi, walipaswa kukumbuka kwamba walikuwa watu wa MUNGU wanaoshika amri, na kwamba Yeye alikuwa ametenda kwa njia ya kimiujiza kuwaleta kutoka utumwani Misri ili wamtumikie, kuwa watu watakatifu Kwake. Hawatakiwi kutumikia matakwa yao wenyewe, au kuiga mataifa yaliyowazunguka ambayo yanaabudu sanamu, bali wabaki kuwa watu tofauti, waliojitenga, ili wote waliowaangalia waseme: Hawa ndio wale ambao MUNGU aliwaleta kutoka katika nchi ya Misri, ambao wanazishika amri kumi. Mwisraeli alikuwa akijulikana punde tu alipoonekana, kwa sababu kwa njia rahisi MUNGU alimtofautisha kwamba huyu ni Wake. {1T 524.1}

Amri iliyotolewa na MUNGU kwa wana wa Israeli kuweka utepe wa bluu/samawati katika mavazi yao haikuwa na ushawishi wa moja kwa moja kwa afya zao, kama ambavyo MUNGU pekee angewabariki kwa utii, na utepe ungeweka katika kumbukumbu zao madai ya juu ya Yehova na kuwazuia

kuchangamana na mataifa mengine, kuungana katika karamu zao za ulevi, na kula nyama nguruwe na vyakula vingine ambavyo ni hatari kwa afya. MUNGU sasa angewataka watu Wake wapokee matengenezo ya mavazi, siyo tu kuwatofautisha na ulimwengu kama "watu Wake wa kipekee," bali kwa sababu matengenezo ya mavazi ni muhimu kwa afya ya mwili na akili. Watu wa MUNGU, kwa kiasi kikubwa, wamepoteza upekee wao, na wamekuwa wakiufuata ulimwengu polepole, na kuchangamana nao, mpaka katika mambo mengi wamekuwa kama wao. Hii haimpendezi MUNGU. Yeye Anawaelekeza, kama alivyowaamuru wana wa Israeli zamani, watoke ulimwenguni na watupilie mbali mazoea yao ya kuabudu sanamu, wasifuate mioyo yao (kwa maana mioyo yao haijatakaswa) au macho yao, ambayo yamewafanya wamwache MUNGU na kuungana na ulimwengu. {1T 524.2}

Kuna jambo lazima lipatikane ili kupunguza hali ya watu wa MUNGU kushikiliwa na ulimwengu. Matengennezo ya mavazi ni rahisi, sahili na yenye afya, lakini kuna msalaba ndani yake. Ninamshukuru MUNGU kwa msalaba na kwa furaha nainama kuuinua. Tumeunganishwa sana na ulimwengu kiasi kwamba tumepoteza kwenye macho yetu msalaba na hatuteseki kwa ajili ya Kristo. {1T 525.1}

Hatupaswi kutamani kubuni kitu cha kutengeneza msalaba; lakini ikiwa MUNGU anatuletea msalaba, tunapaswa kuubeba kwa furaha. Katika kuukubali msalaba tunatofautishwa na ulimwengu, ambao hautupendi na hukejeli upekee wetu. Kristo alichukiwa na ulimwengu kwa sababu hakuwa wa ulimwengu. Je! Wafuasi Wake wanaweza kutarajia mambo yao kwenda vizuri kuliko Bwana wao? Ikiwa tutapita hapa duniani bila kupokea shutuma au kukunjiwa uso kutoka kwa ulimwengu tunapaswa kushtuka, kwa sababu ni kufanana kwetu na ulimwengu ndiko hutufanya tuwe kama wao kiasi kwamba hakuna kitu cha kuamsha wivu au uovu wao; hakuna mgongano wa roho. Ulimwengu huudharau msalaba. "Kwa maana mahubiri ya msalaba kwa hao wanaopotea ni upumbavu; bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya MUNGU." 1 Wakorintho 1:18. "Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu." Wagalatia 6:14. {1T 525.2}

# SURA YA 89

# BATTLE CREEK YASHUKIWA

Mnamo 1865 niliona kwamba wengine wamehisi kuwa huru, kupitia hisia za wivu, kulisema vibaya kanisa huko Battle Creek. Wengine huyatazama kwa mashaka yale yote yanayoendelea huko na wanaonekana kufurahi ikiwa wanaweza kupata kitu chochote cha faida kwao ili kuidhalilisha Battle Creek. MUNGU hafurahishwi na roho na mwenendo kama huo. Ni kutoka katika chanzo gani ambacho makanisa yetu ya ng'ambo au njema ya nchi hupata nuru na maarifa ya Ukweli? Imekuwa kutoka katika njia na fedha ambayo MUNGU ameiweka, ambayo inatokea Battle Creek. Ni akina nani walio na mizigo ya kazi? Ni wale ambao wanafanya kazi kwa ari na bidii huko Battle Creek. Mzigo na majaribu mazito lazima yawafikie wale wanaosimama mbele katika vita vikali, na mashaka na uchovu wa fikra vinawafikia wale wote wanaohusika katika kufanya maamuzi muhimu sana kuhusiana na kazi ya MUNGU. Ndugu zetu wa huko ng'ambo, ambao wameepuka misongo hii yote, wanapaswa kujisikia wenye shukrani na kumsifu MUNGU kwamba wamependelewa hivyo na wanapaswa kuwa wa mwisho kuwa na wivu, husuda, na kutafuta makosa, wakishikilia msimamo, "Wewe ripoti tu, nasi tutaripoti." {1T 526.1}

Kanisa la huko Battle Creek limebeba mizigo ya Makonferensi, yote ambayo imekuwa kazi nzito karibu kwa watu wote hapa. Kama matokeo ya kazi ya ziada wengi wamejiletea udhaifu ambao umedumu kwa miezi mingi. Wamebeba mzigo kwa moyo mkunjufu, lakini wamehisi kusikitishwa na kuvunjwa moyo kwa kutokujali kwa wengine na wivu wa kikatili wa wengine baada ya kurudi kwenye makanisa kadhaa waliyotoka. Maneno yanasemwa bila kufikiria - wengine kwa makusudi, na wengine kwa kutojali - juu ya wabeba mizigo huko na juu ya wale wanaosimamia kazi. MUNGU ameziwekea alama hotuba hizi zote na wivu na husuda zilizowasukuma; kumbukumbu ya uaminifu imehifadhiwa. Wengi wanamshukuru MUNGU kwa Ukweli na kisha wanageuka na kuhoji na kutafuta makosa kwa njia ambazo mbingu imeamuru kuwafanya wawe hivyo walivyo au vile wanavyopaswa kuwa. Je, wangempendeza MUNGU kwa kiasi gani kama wangechukua nafasi ya Haruni na Huri na kusaidia kuinua mikono ya wale ambao wanabeba mizigo mikubwa na mizito ya kazi inayohusiana na kusudi la MUNGU. Wanung'unikaji na walalamikaji wanapaswa kubaki nyumbani, ambapo watakuwa mbali na njia ya majaribu, ambapo hawawezi kulisha wivu wao, majungu mabaya, na kutafuta makosa, kwa sababu uwepo wao ni mzigo tu kwa mikutano; ni mawingu yasiyo na maji. {1T 526.2}

Wale ambao wanahisi wako huru kupata makosa na kuwalaani wale ambao MUNGU amewachagua kuchukua sehemu muhimu katika kazi hii kubwa ya

mwisho ni bora wangetafuta kuongoka na kuwa na nia namapenzi ya Kristo. Hebu wawakumbuke wana wa Israeli ambao walikuwa tayari kutafuta makosa kwa Musa, ambaye MUNGU alikuwa amemweka rasmi kuwaongoza watu Wake kwenda Kanaani, na kumnung'unikia hata MUNGU Mwenyewe. Walalamikaji hawa wote walianguka jangwani. Ni rahisi kuasi, ni rahisi kupigana pambano kabla ya kuzingatia mambo kwa busara, kwa utulivu, na kutatua kitu chochote kinachoweza kupelekea kupigana. Wana wa Israeli ni mfano kwetu sisi ambao tumefikiwa na miisho ya ulimwengu. {1T 527.1}

Ni rahisi kwa wengi kuhoji na kutafuta makosa kwa sababu ya masuala yaliyoko huko Battle Creek kuliko kusema nini kifanyike. Wengine wangejitosa kuchukua jukumu hili, lakini hivi karibuni wagejikuta hawana uzoefu, wenye mapungufu na wangeingusha kazi ardhini. Ikiwa hawa wasemaji na wakosoaji wa makosa wangekuwa ndio wabeba mizigo na kuwaombea watendakazi, wangebarikiwa wenyewe na wangewabariki wengine kwa mfano wao wa Kimbingu/Utauwa, na ushawishi wao mtakatifu na maisha yao. Wengi ni rahisi kuzungumza kuliko kuomba; ukosefu huo wa kiroho na utakatifu, na ushawishi wao ni jeraha kubwa kwenye kazi ya MUNGU. Badala ya kuhisi kuwa kazi iliyoko huko Battle Creek ni kazi yao, na kwamba wana faida katika ustawi wake, wanasimama kando zaidi kama watazamaji, wakihoji na kutafuta makosa. Wale ambao hufanya hivi ndio wale ambao hawana uzoefu katika kazi hii na ambao hawajateseka sana kwa ajili ya Ukweli. {1T 527.2}

# SURA YA 90

# KUHAMISHA MAJUKUMU

Ndugu hao wanaotunza Sabato wanaohamishia jukumu lao la uwakili mikononi mwa wake zao, wakati wao wenyewe wana uwezo wa kusimamia, hawana busara na katika uhamishaji huu hawamfurahishi MUNGU. Uwakili wa mume hauwezi kuhamishiwa kwa mke. Na hili wakati mwingine limefanyika kwa maumivu ya wote wawili. Mume anayeamini wakati mwingine amehamishia mali yake kwa mwenzi wake asiyeamini, akitumaini kumfurahisha kwa kufanya hivyo, kupokonya silaha za upinzani wake, na mwishowe kumshawishi auamini ukweli. Lakini hii siyo zaidi au pungufu ya jaribio la kununua amani, au kumkodi mke ili auamini Ukweli. Fedha ambazo MUNGU ameziweka ili kuendeleza kazi yake, mume anazihamishia kwa yule ambaye hana huruma na Ukweli; msimamizi kama huyo atatoa hesabu gani wakati Bwana mkubwa atakapohitaji iliyo yake na riba? {1T 528.1}

Wazazi wanaoamini wamehamishia mali zao kwa watoto wao wasioamini, na hivyo kuiweka nje ya uwezo wao wa kumpa MUNGU vile vilivyo vyake. Kwa kufanya hivyo wanaachilia mbali jukumu hilo ambalo MUNGU amewapatia, na kuweka katika safu ya adui mali ambayo MUNGU amewakabidhi wairudishe Kwake kwa kuwekeza katika kusudi Lake wakati atakapoihitaji kutoka kwao. Siyo agizo na mpango wa MUNGU kwamba wazazi ambao wana uwezo wa kusimamia biashara zao wazikabidhi mali zao, hata kwa watoto wenye imani moja nao. Hawa kwa kawaida hawana kujitoa kikamilifu katika kuifanya kazi kama inavyostahili, na hawajapita katika shule ya dhiki na shida ili kuweka makadirio ya juu katika hazina ya milele na ya chini katika hazina ya kidunia. Mali zilizowekwa mikononi mwao ni uovu mkubwa zaidi. Ni jaribu kwao kuweka mapenzi yao juu ya vitu vya ulimwengu na kuzitumaini mali na kuhisi kuwa wana uhitaji kidogo tu. Wakati mali ambazo hawajazipata kwa bidii yao zinapokuja katika milki yao, ni mara chache sana huzitumia kwa busara. {1T 528.2}

Mume anayehamishia mali yake kwa mkewe humfungulia mlango mpana wa jaribu, iwe ni muumini au asiyeamini. Ikiwa yeye ni mtu anayeamini na mwenye tabia mbaya ya asili ya ubahili, anayependa ubinafsi na umiliki, vita itakuwa ngumu sana kwake na usimamizi wa mumewe na yeye mwenyewe. Ili aokolewe, lazima ashinde tabia hizi mbaya kisha aige tabia ya Bwana Wake wa Kiungu, akitafuta nafasi ya kuwafanyia wengine mema, kuwapenda wengine kama vile Kristo alivyotupenda sisi. Anapaswa kukuza zawadi ya thamani ya upendo aliyo nayo kwa ukuu Mwokozi wetu. Maisha Yake yalikuwa na sifa nzuri, isiyo na shauku. Maisha yake yote hayakuathiriwa na tendo hata moja la ubinafsi. {1T 529.1}

Kwa malengo yoyote ambayo mume anaweza kuwa nayo, ameweka kikwazo cha kutisha katika njia ya mkewe kumkwamisha katika kazi ya ushindi. Na kama atahamishia kwa watoto, matokeo mabaya kama hayo yanaweza kufuata. MUNGU anaisoma nia yake. Ikiwa yeye ni mbinafsi na amefanya uhamisho ili kuficha tamaa yake na kujipatia udhuru wa kufanya chochote katika kuiendeleza kazi ya Mungu, hakika laana ya Mbingu itamfuata. MUNGU husoma madhumuni na makusudi ya moyo, na huzijaribu nia za wana wa wanadamu. Ishara Yake, na ghadhabu inayoonekana haiwezi kudhihirika kama ilivyokuwa kwa Anania na Safira, lakini mwishowe adhabu yake haitakuwa nyepesi kuliko ile waliyopewa hawa. Katika kujaribu kuwadanganya wanadamu, walikuwa wakimdanganya MUNGU. "Nafsi itendayo dhambi ndiyo itakayokufa." {1T 529.2}

Hao hawawezi kusimama mbele ya mtihani wa hukumu wakiwa bora kumzidi yule mtu aliyepokea talanta moja na kuificha ardhini. Alipohukumiwa, alimshtaki MUNGU kwa udhalimu: "Nilijua wewe ni mtu mgumu, unavuna mahali ambapo haukupanda, na unakusanya mahali ambapo haukutawanya: nikaogopa, nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi [ambapo kazi ya MUNGU isingeweza kufaidika nayo]: tazama, hapa unayo iliyo yako. " MUNGU asema hivi: "Basi ichukueni hiyo talanta, mpeni yule aliye na talanta kumi.... Na mtupeni yule mtumishi asiye na faida kwenye giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno." Mtu huyu aliogopa kwamba Bwana Wake angefaidika na uboreshaji wa talanta yake. {1T 530.1}

Niliona kwamba kuna wengi ambao wamefunga talanta yao kwenye leso na kuificha ardhini. Wanaonekana kufikiria kwamba kila senti ambayo imewekezwa katika kazi ya MUNGU imepotea kwao na haiwezi kupatikana tena. Kwa wale ambao wanahisi hivyo, ni hivyo hivyo. Hawatapokea malipo yoyote. Wanatoa kwa kulalamika na kwa shingo upande kwa sababu tu wanahisi wanalazimika kufanya kitu. MUNGU humpenda yule atoaye kwa moyo mkunjufu. Wale wanaojisifu kuwa wanaweza kuhamishia jukumu lao kwa wake au watoto wao wanadanganywa na adui. Uhamisho wa mali hautapunguza jukumu lao. Wanawajibika kwa mali ambayo mbingu zimeikabidhi chini ya uangalizi wao, na kwa njia yoyote hawawezi kujipatia udhuru wa jukumu hili mpaka watakapomrudishia MUNGU kile alichowakabidhi. {1T 530.2}

Upendo wa ulimwengu hujitenga na MUNGU. "Ikiwa mtu yeyote anaupenda ulimwengu, upendo wa Baba haumo ndani yake." Haiwezekani kwa yeyote kuutambua Ukweli wakati ulimwengu umeyachukua mapenzi yao. Ulimwengu unaingilia kati yao na MUNGU, ukificha maono na kupunguza hisia kwa kiwango kiasi kwamba hawawezi kuvitambua vitu vitakatifu. MUNGU huwaita watu kama hawa: "Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili. Huzunikeni na kuomboleza na kulia. Kucheka

kwenu na kugeuzwe kuwa kuomboleza, na furaha yenu kuwa hamu." Wale ambao wameichafua mikono yao kwa uchafuzi wa ulimwengu wanatakiwa kujisafisha kutokana na madoa yake. Wale ambao wanafikiri wanaweza kuutumikia ulimwengu wakiwa wanampenda MUNGU wana nia-mbili Indumilakuwilil. Hakika hawawezi kumtumikia MUNGU na mali. Ni watu wenye nia mbili, wanaupenda ulimwengu na wanapoteza hisia zote za wajibu wao kwa MUNGU, na bado wanakiri kuwa ni wafuasi wa Kristo. Wao hawako kwa hiki wala kile. Wataupoteza ulimwengu wote endapo hawataitakasa mikono yao na kusafisha mioyo yao kwa kutii kanuni safi za Ukweli. "Yeye asemaye anakaa ndani Yake inampasa yeye mwenyewe kuenenda kama Yeye alivyoenenda." "Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa kama Yeye alivyo, ndivyo tulivyo sisi katika ulimwengu huu." "Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa." {1T 530.3}

Ni tamaa za kidunia ndizo huuharibu utauwa wa Kweli. Upendo wa ulimwengu na vitu vilivyomo ulimwenguni vinaleta utengano na Baba. Shauku ya faida za kidunia inaongezeka miongoni mwa wale wanaodai kutazamia kuonekana kwa Mwokozi wetu hivi karibuni. Tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima huwatawala hata wale wanaodai kuwa Wakristo. Wanatafuta vitu vya ulimwengu kwa tamaa mbaya, na wengi watauza uzima wa milele kwa faida isiyo takatifu. {1T 531.1}

# SURA YA 91

# UTUNZAJI SAHIHI WA SABATO

Desemba 25, 1865, nilioneshwa kwamba kumekuwa na ulegevu mwingi kuhusu utunzaji wa Sabato. Kumekuwa hakuna uharaka katika kutimiza majukumu ya kidunia ndani ya siku sita za kazi ambazo MUNGU amempatia mwanadamu na kuwa mwangalifu asihalifu hata saa moja ya wasaa mtakatifu, uliotakaswa ambao amejiwekea Mwenyewe. Hakuna biashara au shuguli yoyote ya mwanadamu ambayo inapaswa kuchukuliwa kuwa ni yenye umuhimu wa kutosha kumfanya mtu avunje amri ya nne ya Yehova. Kuna matukio ambayo Kristo ametoa idhini ya kufanya kazi hata siku ya Sabato katika kuokoa maisha ya wanadamu au ya wanyama. Lakini ikiwa tunakiuka Andiko la amri ya nne kwa faida yetu kulingana na mtazamo wa kifedha tunakuwa wavunja Sabato na tuna hatia ya kukiuka amri zote, kwa maana tukikosea katika nukta moja tunakuwa na hatia katika amri zote. Ikiwa ili kuokoa mali tunaivunja amri ya wazi ya Yehova, je, ni wapi itakuwa mahali pa kusimama, yaani ambapo hatutavunja Sabato? Je! Tutaweka wapi mipaka? Kuasi katika jambo dogo, na usione kama kuna dhambi yoyote kwa upande wetu, na dhamiri inazidi kuwa ngumu, hisia zinafifia, mpaka tunaweza kwenda mbele zaidi na kufanya kazi nyingi na bado tukajisifia kuwa sisi ni watunza Sabato, wakati, kulingana na kiwango cha Kristo, tunavunja kila moja ya maagizo matakatifu ya MUNGU. Kuna kosa kwa watunza Sabato katika suala hili; lakini MUNGU ameweka mkazo, na wale wote wanaofikiri kwamba wanaokoa muda kidogo, au kujinufaisha kwa kukiuka kidogo muda wa Bwana, watapata hasara mapema au baadaye. Hawezi kuwabariki kama ambavyo ingekuwa furaha yake kufanya hivyo, kwa kuwa wamelidharau Jina Lake, maagizo Yake hayaheshimiwi. Laana ya MUNGU itawakalia, na watapoteza mara kumi au ishirini zaidi ya wanavyopata. "Je! Mwanadamu atamwibia MUNGU ? Lakini ninyi mmeniibia Mimi,... naam taifa hili lote." {1T 531.2}

MUNGU amempa mwanadamu siku sita za kufanya kazi kwa ajili yake mwenyewe, lakini ameweka siku moja ambayo Yeye anapaswa kuheshimiwa kwa upekee. Anapaswa kutukuzwa, mamlaka yake iheshimiwe. Na bado mwanadamu anamnyang'anya MUNGU kwa kuiba sehemu ya muda ambao Muumbaji amejiwekea. MUNGU aliiweka siku ya saba kama kipindi cha pumziko kwa mwanadamu, kwa faida ya mwanadamu na vile vile kwa utukufu Wake Mwenyewe. Yeye Aliona kwamba mahitaji ya mwanadamu yalihitaji siku ya kupumzika kutoka katika taabu na masumbufu, kwamba afya na maisha yake vingekuwa hatarini bila kipindi cha kupumzika kutoka katika kazi na wasiwasi wa siku sita. {1T 532.1}

Sabato ilifanywa kwa faida ya mwanadamu; na kukiuka kwa makusudi amri takatifu inayokataza kazi siku ya saba ni uhalifu mbele za mbingu, amri ambayo ilikuwa kubwa sana katika sheria ya Musa hata kudai kifo cha mkosaji. Lakini hiki hakikuwa kilele cha mateso ya

mkosaji, kwani MUNGU asingemchukua mhalifu wa sheria yake kwenda mbinguni. Lazima afe mauti ya pili, ambayo ndiyo adhabu kamili na ya mwisho kwa mhalifu wa sheria ya MUNGU. {1T 533.1}

## SURA YA 92

## HISIA ZA KISIASA

Huko Rochester, New York, Desemba 25, 1865, nilioneshwa mambo mengi kuhusu watu wa MUNGU kuhusiana na kazi Yake kwa siku hizi za mwisho. Niliona kwamba wale wanaodai kuwa ni watunza Sabato watakuwa wamepunguka na wataukosa uzima wa milele. Wanashindwa kuchukua onyo kutoka katika njia iliyofuatwa na wana wa Israeli walioanguka katika baadhi ya njia zao mbaya. Ikiwa wataendelea na dhambi hizi wataanguka kama Waisraeli na hawataingia kamwe katika Kanaani ya mbinguni. "Basi hayo yote yaliwapata wao kuwa mifano; nayo yameandikwa kutuonya sisi, ambao tumefikiwa na miisho ya ulimwengu." {1T 533.2}

Niliona kwamba wengi wangeangukia katika upande huu wa ufalme. MUNGU anawajaribu na kuwathibitisha watu Wake, na wengi hawatavumilia mtihani wa tabia, kipimo cha MUNGU. Wengi watakuwa na kazi ya kushinda sifa zao za kipekee za tabia na hawatakuwa na doa au kasoro au kitu kama hicho, kisichoweza kukemewa mbele za MUNGU na wanadamu. Watu wengi wanaodai kuwa watunza Sabato hawatakuwa na faida yoyote katika kusudi la MUNGU au kanisa bila matengenezo kamili kutoka kwao. Watunza Sabato wengi hawako sahihi mbele za MUNGU katika maoni yao ya kisiasa. Hawapatani na Neno la MUNGU au kuwa na umoja na mwili wa waumini ambao wanaitunza Sabato. Maoni yao hayapatani na kanuni za imani yetu. Nuru ya kutosha imetolewa ili kuwasahihisha wote wanaohitaji kurekebishwa. Wote ambao bado wanabaki na maoni ya kisiasa ambayo hayaendani na roho ya Ukweli wanaishi kwa kukiuka kanuni za mbinguni. Kwa hivyo maadamu wanaendelea kubaki hawawezi kumiliki roho ya uhuru na utakatifu. {1T 533.3}

Kanuni zao na nafasi zao katika masuala ya kisiasa ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo yao ya kiroho. Huu ni mtego wa kila wakati kwao na ni aibu kwa imani yetu, na wale wanaodumisha kanuni hizi mwishowe wataletwa mahali ambapo adui angefurahi wawepo, ambapo mwishowe watatenganishwa na Wakristo waitunzao Sabato. Ndugu hawa hawawezi kupokea idhini ya MUNGU wakati wanakosa huruma kwa jamii ya watu weusi, walioonewa na kupingana na kanuni safi za jamhuri ya Serikali yetu. MUNGU hana huruma na uasi wa hapa duniani kuliko uasi uliokuweko mbinguni, wakati yule muasi mkuu alipohoji msingi wa serikali ya MUNGU alitupwa nje pamoja na wale wote waliomhurumia katika uasi wake. {1T 534.1}

# SURA YA 93

# RIBA

Kwa maoni niliyopewa huko Rochester, New York, Desemba 25, 1865, nilioneshwa kuwa mada inayohusu kuchukua riba inapaswa kuzingatiwa na watunza Sabato. Matajiri hawana haki ya kuchukua riba kutoka kwa ndugu zao masikini, bali wanaweza kupata riba kutoka kwa wasioamini. "Na ikiwa ndugu yako amekuwa maskini, na mkono wake umelegea kwako, ndipo utamsaidia. Usitake riba kwake wala faida, bali mche MUNGU  wako, ili ndugu yako akae nawe. Usimpe fedha yako upate riba, wala usimpe vyakula vyako kwa kujitakia faida." "Usimkopeshe ndugu yako kwa riba; riba ya fedha, riba ya vyakula, riba ya kitu cho chote kikopeshwacho kwa riba; mgeni waweza kumkopesha kwa riba, ila usimkopeshe ndugu yako kwa riba; ili Bwana, MUNGU wako, apate kukubarikia katika yote utiayo mkono wako, katika nchi uingiayo kuimiliki. " {1T 534.2}

MUNGU  amekasirishwa na watunza Sabato kwa sababu ya roho yao ya uchu wa fedha. Tamaa yao ya kupata faida ni kubwa sana kiasi kwamba wametumia faida ya ndugu maskini, wanyonge walio katika shida zao na wameongeza kwenye mali zao ambazo ni nyingi tayari, wakati ndugu hawa masikini wameteseka kupata kipato "Je! Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" ndiyo lugha ya mioyo yao. {1T 535.1}

Miaka michache iliyopita baadhi ya ndugu maskini walikuwa katika hatari ya kupoteza roho zao kupitia maoni mabaya. Kila mahali Shetani alikuwa akiwajaribu juu ya matajiri. Ndugu hawa masikini walikuwa wakitarajia kupendelewa kila wakati, wakati ilikuwa wajibu wao kutegemea nguvu zao wenyewe; na kama wangependelewa, lingekuwa jambo baya zaidi ambalo limetendekea kwao. Katika makundi yote ya watunza Sabato, Shetani alikuwa akitafuta kuangusha tabaka masikini kwa majaribu yake. Baadhi ambao wamepungukiwa na busara na hekima wamechukua njia yao wenyewe, kwa kuwa hawataki kuomba ushauri au kuufuata. Hao walilazimika kuteseka kama matokeo ya hesabu yao ya kusikitisha, na bado hao hao wangehisi kwamba wanapaswa kupendelewa na ndugu zao walio na mali. Vitu hivi vilihitaji kurekebishwa. Kundi lililotajwa kwanza halikutambua majukumu yaliyokuwa juu ya matajiri, wala mashaka na wasiwasi ambao walilazimika kuwa nao kwa sababu ya uwezo wao. Wote waliweza kuona kwamba hawa walikuwa na njia ya kutumia, wakati wao wenyewe walikuwa wamebanwa pia. Lakini jambo la jumla ni kuwa matajiri wamewachukulia maskini wote kwa njia ile ile, wakati kuna kundi la maskini ambao wanafanya vizuri sana kumtukuza MUNGU  kwa nguvu zao, kutenda mema, kuishi kwa Ukweli. Watu hawa wana thamani sana. Hukumu yao ni njema, roho yao ni ya thamani mbele za MUNGU; na kiwango cha mema wanayotimiza kwa njia yao isiyojificha ni kikubwa mara kumi kuliko kile kinachotekelezwa na matajiri, ingawa wa mwisho wanaweza kutoa pesa

nyingi katika tukio fulani. Matajiri wanashindwa kuona na kutambua umuhimu wa kufanya mema, kuwa matajiri katika matendo mema, kuwa tayari kugawanya, kuwasiliana na kushirikiana. {1T 535.2}

# SURA YA 94

# UDANGANYIFU WA UTAJIRI

Baadhi wanaodai kuuamini ukweli wanakosa utambuzi na kushindwa kuthamini uzito/thamani ya maadili. Watu ambao wanajivunia uaminifu wao katika kazi na kuzungumza kana kwamba wanafikiri wanajua yote ambayo ni muhimu kujua, siyo wanyenyekevu moyoni. Wanaweza kuwa na pesa na mali, na hii inatosha kuwapa ushawishi kwa wengine; lakini haitawainulia hata nukta hata moja ya neema kwa MUNGU. Pesa ina nguvu na huleta ushawishi mkubwa. Ubora wa tabia na thamani ya maadili mara nyingi vinapuuzwa vikiwa kwa mtu maskini. Lakini je, MUNGU anajali pesa, mali? Mifugo juu ya milima elfu ni mali yake (milima isiyo na idadi!). Ulimwengu na vyote vilivyomo ni vyake. Wakaao duniani ni kama nzige mbele zake. Watu na mali ni kama vumbi dogo la mzani. Yeye hana upendeleo. {1T 536.1}

Watu wenye mali mara nyingi huangalia utajiri wao na kusema: Kwa hekima yangu nimepata utajiri huu. Lakini ni nani aliyewapa nguvu ya kupata utajiri? MUNGU amewapa uwezo ambao wanaumiliki, lakini badala ya kumpa Yeye utukufu wanauchukua wao wenyewe. Atawajaribu na kuwapima, na ataushusha utukufu wao mavumbini; Yeye Ataondoa nguvu zao na kutawanya mali zao. Badala ya baraka wataambulia laana. Kitendo cha makosa au ukandamizaji, kupotoka kutoka kwenye njia sahihi, havipaswi kuvumiliwa ndani ya mtu ambaye anamiliki mali kuliko mtu ambaye hana. Utajiri wote ambao tajiri mkubwa kabisa aliwahi kuwa nao hauna thamani ya kutosha kufunika dhambi hata ndogo kabisa mbele za MUNGU; huu hautakubaliwa kuwa fidia ya uasi. Toba, unyenyekevu wa kweli, moyo uliovunjika, na roho iliyopondeka peke yake ndivyo vitakubaliwa na MUNGU. Na hakuna mtu anayeweza kuwa na unyenyekevu wa kweli mbele za MUNGU isipokuwa kama unaoneshwa mfano mbele ya wengine. Hakuna kitu isipokuwa toba, kuungama, na kuacha dhambi kinachokubalika kwa MUNGU. {1T 536.2}

Matajiri wengi wamepata utajiri wao kwa kufunga makubaliano, kwa kujinufaisha na kudhoofisha wenzao walio maskini au ndugu zao; na hawa watu huwa wanajisifu kwa ujanja wao, werevu, hila na umakini katika maafikiano ya bei (bargaining). Lakini laana ya MUNGU itakaa juu ya kila fedha iliyopatikana, na juu ya ongezeko lake mikononi mwao. Wakati vitu hivi vilipooneshwa

kwangu, niliweza kuona nguvu ya Maneno ya Mwokozi wetu : "Ni rahisi ngamia kupita kwenye tundu la sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa MUNGU." Wale ambao wana uwezo wa kupata mali wanahitaji kuwa macho kila wakati vinginevyo watageuza tamaa yao kujipatia mali kuwa uwajibikaji mbaya pasipo kudumisha uadilifu mkuu. Kwa hivyo wengi huangukia kwenye majaribu, hila, kupokea zaidi ya thamani ya kitu, na kuzitoa kafara kanuni za ukarimu na fadhili, za utu wao kwa faida za uovu. {1T 537.1}

Nilioneshwa kwamba wengi wanaodai kuwa watunza Sabato wanaupenda ulimwengu na vitu vilivyomo ulimwenguni kiasi kwamba wameharibiwa na roho na ushawishi wake; Uungu umepotea kutoka katika tabia zao na ushetani umeingia, ukiwabadilisha wayatumikie makusudi ya Shetani, wawe vyombo vya uovu. Kisha kinyume na watu hawa nilioneshwa watu maskini wenye bidii na waaminifu, ambao walikuwa tayari kuteseka ili kuwasaidia wale walioko katika uhitaji, ambao wangeona kuwa ni heri kudhalilishwa na ndugu zao matajiri kuliko kudhihirisha roho ya kutafuta mali kwa tamaa kubwa na kuilimbikiza mali kama wanavyodhihirisha; watu wanaothamini dhamiri safi na haki, hata katika vitu vidogo, vya thamani kubwa kuliko utajiri. Wako tayari kuwasaidia wengine, wako tayari kufanya mema yote kwa nguvu zao, kiasi kwamba hawakusanyi utajiri; mali zao za kidunia haziongezeki. Ikiwa kuna kitu kizuri cha kuhitaji mali au nguvu, wao ndio wa kwanza kupendezwa na kuitikia, na mara nyingi hufanya zaidi ya uwezo wao halisi, na hivyo hujikana kwa baadhi ya mali au vitu vinavyohitajika ili kutekeleza malengo yao mazuri. {1T 537.2}

Kwa sababu watu hawa wanaweza kujivunia hazina kidogo tu ya kidunia, wanaweza kutazamwa kuwa na uwezo mdogo, maamuzi, na hekima. Wanaweza kuhesabiwa kuwa hawana thamani maalum, na ushawishi wao hauwezi kuthaminiwa na watu; lakini Je, MUNGU anawaonaje watu hawa masikini wenye hekima? Wanaonekana kuwa wenye thamani machoni Pake, na, ingawa hawazidishi hazina yao hapa duniani, wanajiwekea hazina isiyoweza kuharibika mbinguni, na kwa kufanya hivi wanaonesha hekima iliyo bora kuliko ile ya watu wenye hekima wanaojifanya kuwa Wakristo, ambao wako makini kuihesabu mali na kuilimbikiza kwa uroho mali kama vile ya Bwana na yenye mfano wa mungu kuwa ni bora kuliko ya kidunia na ya kimwili, na ya kishetani. Thamani au uzito wa maadili ndiyo ambavyo MUNGU anavithamini. Tabia ya Kikristo isiyo na watu wenye uchu wa mali, yenye utulivu, upole, na unyenyekevu, ni ya thamani machoni Pake kuliko dhahabu safi kabisa, hata kabari ya dhahabu ya Ofiri. {1T 538.1}

Matajiri wanapaswa kujaribiwa zaidi kuliko wale ambao siyo matajiri. Ikiwa watastahimili jaribu na kushinda kasoro juu ya tabia zao, na kama mawakili waaminifu wa Kristo wakampa MUNGU vitu Vyake, wataambiwa: "Vema,

mtumishi mwema na mwaminifu; umekuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; Ingia katika furaha ya Bwana wako." {1T 538.2}

Kisha nikaelekezwa kwenye mfano wa wakili dhalimu: "Nami nawaambia, Jifanyieni rafiki kwa mali ya udhalimu, ili itakapokosekana wawakaribishe katika makao ya milele. Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia. Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya Kweli? Na kama hamkuwa waaminifu katika mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?"{1T 538.3}

Ikiwa watu watashindwa kumrudishia MUNGU yale ambayo amewakopesha ili wayatumie kwa utukufu Wake, na hivyo wakamwibia, watashindwa kabisa. Yeye Amekopesha mali ambazo wanaweza kuziboresha bila kupoteza nafasi ya kufanya mema, na kwa hivyo wanaweza kuendelea kuweka hazina mbinguni. Lakini ikiwa, kama yule mtu aliyepewa talanta moja, wanaificha, wakiogopa kwamba MUNGU atapata faida ya ile talanta, si tu kwamba watapoteza ongezeko ambalo mwishowe atapewa msimamizi mwaminifu, bali pia mtaji/kianzio ambacho MUNGU aliwapa kufanyia kazi. Kwa sababu wamemwibia MUNGU, hawatakuwa wameweka hazina mbinguni, na watapoteza hazina yao ya kidunia pia. Hawana makao duniani, wala hawana rafiki mbinguni wa kuwapokea kwenye makao ya milele ya wenye haki. {1T 539.1}

Kristo anatangaza: "Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili: kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyo mwingine; au sivyo atashikamana na mmoja, na kumdharau yule mwingine. Hamwezi kumtumikia MUNGU na mali" - hamwezi kumtumikia MUNGU na utajiri wenu pia. "Mafarisayo pia, ambao walikuwa na tamaa ya mali, waliyasikia haya yote; nao wakamdhihaki." Angalia Maneno ya Kristo kwao: "Ninyi ndio mnajihesabia haki mbele za watu; lakini MUNGU anaijua mioyo yenu; kwa maana kile kinachothaminiwa sana miongoni mwa watu [utajiri unaopatikana kwa uonevu, udanganyifu, ujanja, hila (fraud), au kwa njia nyingine yoyote isiyo ya haki] ni chukizo mbele za MUNGU." Halafu Kristo anawasilisha wahusika wawili, tajiri ambaye alikuwa amevaa mavazi ya rangi ya zambarau na kitani safi, na aliyefanikiwa kuvaa mavazi ya kitajiri na yenye kupendeza kila siku, na Lazaro, ambaye alikuwa katika umasikini mbaya na mwenye kuchukiza machoni, na ambaye aliomba makombo machache ambayo tajiri huyo aliyadharau. Mwokozi wetu anaonesha tathmini yake kwa wawili hawa. Ingawa Lazaro alikuwa katika hali ya kusikitisha na mbaya sana kiafya, alikuwa na imani ya Kweli, maadili yenye thamani na uzito wa kweli, ambayo MUNGU aliyaona, na ambayo aliyachukulia kuwa ya thamani kubwa sana kiasi cha kumchukua mgonjwa huyu masikini, aliyedharauliwa na kumweka katika nafasi ya juu zaidi, wakati yule

aliyeheshimiwa na mtu mpenda-raha mwenye utajiri alitupwa mbali na uso wa MUNGU na kutumbukia katika taabu na ole zisizosimulika. MUNGU hakuuthamini utajiri wa mtu huyu mwenye mali nyingi, kwa sababu hakuwa na maadili yenye thamani ya Kweli. Tabia yake ilikuwa haina thamani. Utajiri wake haukumpendekeza kwa MUNGU wala kuwa na ushawishi wowote ili kupata upendeleo Wake. {1T 539.2}

Kwa mfano huu Kristo aliwafundisha wanafunzi Wake wasihukumu au kuwathamini watu kwa utajiri wao au kwa heshima waliyopokea kutoka kwa wengine. Hiyo ndio mwenenndo uliofuatwa na Mafarisayo, ambao wakati wakiwa na mali na heshima ya kidunia, hawakuwa na thamani mbele za MUNGU na zaidi ya hili, walidharauliwa na kukataliwa na Yeye, walitupwa mbali na macho Yake kama chukizo Kwake kwa sababu hakukuwa na maadili au utimamu ndani yao. Walikuwa mafisadi, wenye dhambi, na wenye kuchukiza machoni pake. Mtu masikini, aliyedharauliwa na wanadamu wenzake na kuchukiza machoni pao, alikuwa wa thamani machoni pa MUNGU kwa sababu alikuwa na utimamu wa maadili na thamani/stahiki, na hivyo kumfanya afaulu kuletwa katika jamii ya malaika watakatifu walio safi na kuwa mrithi wa MUNGU na mrithi pamoja na Kristo. {1T 540.1}

Katika maelekezo ya Paulo kwa Timotheo anamwonya juu ya kundi ambalo halitakubali maneno mazuri na ambalo linaukadiria vibaya utajiri. Anasema: "Mtu awaye yote akifundisha elimu nyingine, wala hayakubali Maneno yenye uzima ya Bwana wetu Yesu Kristo, wala mafundisho yapatanayo na utauwa, amejivuna; wala hafahamu neno lolote; bali ana wazimu wa kuwazia habari za maswali, na mashindano ya maneno, ambayo katika hayo hutoka husuda, na ugomvi, na matukano, na shuku mbaya; na majadiliano ya watu walioharibika akili zao, walioikosa kweli, huku wakidhani ya kuwa utauwa ni njia ya kupata faida. Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo. Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na mtego/kitanzi, na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani, na kujichoma kwa maumivu mengi. Bali wewe, mtu wa MUNGU, uyakimbie mambo hayo; ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi, upole. Piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi." "Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini MUNGU atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; huku

wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli. "{1T 540.2}

Paulo katika barua hii kwa Timotheo amekazia akilini mwake umuhimu wa kutoa maagizo kama vile inavyopaswa kuondoa udanganyifu ambao huwalaghai matajiri kwa urahisi, kwamba kwa sababu ya utajiri wao, wanakuwa bora kuliko maskini, kwamba kwa sababu ya uwezo wao wa kukusanya basi wao ni bora katika hekima na maamzi - kwa kifupi, faida hiyo ni utauwa. Hapa kuna udanganyifu wa kutisha. Ni wachache kiaasi gani wanaozingatia agizo ambalo Paulo alimwamuru Timotheo awapatie matajiri! Ni wangapi wanaojisifia wenyewe kwamba umiliki wao wa mali ni utauwa! Paulo anatangaza, "Utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa." Ingawa watu matajiri wanaweza kutoa maisha yao yote kwenye lengo moja la kupata utajiri, lakini kwa kuwa hawakuja na kitu ulimwenguni, hawawezi kutoka na kitu. Wanapaswa kufa na kuacha kile ambacho kiliwagharimu nguvu nyingi kukipata. Waliweka rehani vitu vyao vyote, hata masilahi yao ya milele, ili kupata mali hii, na wamepoteza vyote. {1T 541.1}

Paulo anaonesha ni hatari gani ambayo watu wataiendea ili wapate utajiri. Lakini wengi wamedhamiria kuwa matajiri; hili ndilo lengo lao, na ndani ya bidii yao mazingatio ya umilele yamepuuzwa. Wamepofushwa na Shetani na wanajifanya kuamini kwamba wanatamani faida hii kwa sababu nzuri; wananyumbulisha dhamiri zao, wanajidanganya, na kila mara wanatamani utajiri. Hao wamekosa imani na kujichoma kwa huzuni nyingi. Kanuni zao nzuri, zilizoinuliwa wamezitoa kafara, wameacha imani yao kwa sababu ya utajiri, na, ikiwa hawakukatishwa tamaa na kusudi lao, wamevunjwa moyo na furaha ambayo walidhani utajiri ungeileta. Wamekwama kwa kujifungafunga kama uzi, wana wasiwasi na masumbufu; wamejifanya watumwa wa tamaa yao na kuulazimisha utumwa huo katika familia zao, na faida wanayovuna ni "huzuni nyingi." "Waagize matajiri katika ulimwengu huu, wasiwe na majivuno, wala wasitumainie utajiri usiokuwa na hakika, bali wamtumainie MUNGU aliye hai, ambaye hutupatia vitu vyote kwa utajiri ili tuvitumie kwa furaha." Watu hawapaswi kujilimbikizia utajiri bila kuchukua faida yake, wakijinyima raha ya maisha na kuwa watumwa ili kuhifadhi au kuongeza hazina yao ya kidunia. {1T 541.2}

Mtume Paulo anaonesha matumizi ya Kweli ya utajiri, na kumwelekeza Timotheo awaagize matajiri kutenda mema, kwamba wawe matajiri katika matendo mema, walio tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; kwa kufanya hivyo watakuwa wanajiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ikimaanisha mwisho wa wakati, ili wapate kuushikilia uzima wa milele. Mafundisho ya Paulo yanapatana kabisa na Maneno ya Kristo: "Jifanyieni rafiki kwa mali ya udhalimu; ili itakapokosekana wawakaribishe katika makao

ya milele." Utauwa na kuridhika ni faida kubwa. Hapa kuna siri ya Kweli ya furaha, na ustawi halisi wa roho na mwili 1Timotheo 6:6-11. {1T 542.1}

## SURA YA 95

## UTII KWENYE UKWELI

Ndugu mpendwa D: Naikumbuka sura yako miongoni mwa sura nyingi ambazo zilioneshwa kwangu katika maono huko Rochester, New York, Desemba 25, 1865. Nilioneshwa kuwa ulikuwa nyuma. Maamuzi yako yamethibitishwa kwamba tuna Ukweli, lakini bado hujapata ushawishi wake utakasao. Hukuzifuata kwa ukaribu nyayo za Mkombozi wetu, kwa hivyo hujajiandaa kuenenda kama Yeye alivyoenenda. Unapoyasikiliza Maneno ya Kweli, maamuzi yako yanasema kuwa ni sahihi, hayawezi kuwa maneno ya kujipinga; lakini mara moyo usiotakaswa unasema: "Haya ni Maneno magumu, ni nani awezaye kuyasikia? ni bora utoe juhudi zako za kwenda sambamba na watu wa MUNGU, kwani vitu vipya tena vya kushangaza na vyenye kujaribu vitaendelea kutokea; wakati mwingine utalazimika kuacha vitu, na unaweza pia kuacha sasa, na ni bora kuliko kwenda mbali zaidi. " {1T 543.1}

Huwezi kukubali kuukiri Ukweli na usiuishi; umekuwa ukitamani maisha yanayoendana na imani yako. Nilioneshwa kitabu kilichoandikwa jina lako na wengine wengi. Mbele ya jina lako kulikuwa na doa jeusi. Ulikuwa ukiliangalia na kusema: "Haliwezi kufutwa kamwe." Yesu aliuweka mkono Wake uliojeruhiwa juu yake na akasema: "DamuYyangu peke yake ndiyo inayoweza kulifuta. Ikiwa utaamua tangu sasa kuchagua njia ya utii wa unyenyekevu, na kuitegemea kikamilifu faida ya damu yangu iyafunike makosa yako ya zamani, nitayafuta makosa yako, na kuzifunika dhambi zako. Lakini ukichagua njia ya wakosaji lazima uvune thawabu ya mhalifu. Mshahara wa dhambi ni mauti." {1T 543.2}

Niliona malaika wabaya wanaokuzunguka wakitafuta kuyahamisha mawazo yako kutoka kwa Kristo, wakakufanya umtazame MUNGU kama MUNGU wa haki na kupoteza upendo, huruma, na rehema ya Mwokozi aliyesulubiwa ambaye atawaokoa kabisa wale wote wanaokuja Kwake. Malaika alisema: "Mtu yeyote

akifanya dhambi, tunaye mtetezi wetu kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki." {1T 543.3}

Unapokuwa chini ya shinikizo la wasiwasi wa akili, wakati unapoyasikiliza mapendekezo ya Shetani na kunung'unika na kulalamika, malaika anayehudumu ameamriwa kukubebea msaada unaohitaji na kuitia aibu lugha ya akili yako isiyoamini. Humwamini MUNGU ; hukuziamini kikamilifu nguvu Zake zinazookoa. Unamvunjia MUNGU heshima kwa ukafiri huu mbaya na unajisababishia mateso mengi yasiyo ya lazima. Niliona malaika wa mbinguni wakikuzunguka, wakiwarudisha nyuma malaika wabaya, na wakikuangalia kwa huruma na huzuni, na wakikuelekeza mbinguni, taji ya kutokufa, wakisema: "Yule atakayeshinda lazima apambane." {1T 544.1}

Ingawa umekuwa na mashaka na kuchanganyikiwa, lakini haujathubutu kukata kabisa kiunganishi kati yako na watu wa MUNGU wanaozishika amri. Walakini haujasalimisha yote kwa ajili ya ukweli; haujajitoa mwenyewe, mapenzi yako mwenyewe. Unaogopa kujilaza mwenyewe na kila kitu ulicho nacho juu ya madhabahu ya MUNGU, usije ukalazimika kumrudishia sehemu fulani ya yale aliyokukopesha. Malaika wa mbinguni wanayajua maneno na matendo yetu, na hata na mawazo na makusudi ya moyo. Wewe, ndugu mpendwa, una hofu kwamba Ukweli utakugharimu sana, lakini haya ni moja ya maoni ya Shetani. Hebu uache uchukue yote uliyonayo, na haugharimu kiasi kikubwa sana; thamani inayopokelewa, ikiwa itakadiriwa sawa sawa, ni uzani wa milele wa utukufu. Ni kidogo kiasi gani kinachohitajika kwetu! Dhabihu ndogo sana ambayo tunaweza kuitoa ukilinganisha na ile ambayo Bwana wetu wa mbinguni alitufanyia! Na bado roho ya manung'uniko inakujia kwa sababu ya gharama ya uzima wa milele. Wewe, pamoja na ndugu zako wengine huko -----, mmekuwa na mizozo mikali na adui mkubwa wa roho. Mara kadhaa umekaribia kujisalimisha kwenye mgogoro, lakini ushawishi wa mke wako na binti mkubwa umeshinda. Washiriki hawa wa familia yako wangeweza kuutii Ukweli kwa moyo wote kama wangeweza kudumishwa na ushawishi wako. {1T 544.2}

Binti zako wanakutazama kama mfano, kwa maana wanafikiri baba yao lazima awe sahihi. Wokovu wao unategemea sana mwenendo wanaoufuata. Ukiacha kujitahidi kwa ajili ya uzima wa milele, utakuwa na ushawishi mkubwa wa kushinikiza katika kuwabeba watoto wako pamoja nawe, utaishusha roho ya mke wako mwaminifu, utavunja matumaini yake, na kupunguza mshiko wake wa maisha. Je! Unawezaje kukutana nao katika hukumu ili kushuhudia kwamba uaminifu wako ulithibitisha uharibifu wao? {1T 545.1}

Niliona kwamba mara kadhaa umeyakubali maoni ya Shetani ya kuacha kujitahidi kuishi katika kweli, kwani mshawishi alikuambia kwamba utashindwa hata kwa juhudi bora kiasi gani unazoweza kufanya, kwamba kwa udhaifu wako

wote na kasoro haiwezekani wewe kudumisha maisha ya uchaji Mungu. Nilioneshwa kuwa mke wako na binti yako mkubwa wamekuwa malaika wako wazuri, wakikuhuzunikia, na kukuhimiza kuyapinga kwa kiwango kikubwa mapendekezo ya nguvu ya Shetani; na kupitia upendo wako kwao umeshawishiwa kujaribu tena kurekebisha imani yako inayotetereka juu ya ahadi za MUNGU. Shetani anasubiri kukuangusha ili afurahie anguko lako. Wale wanaoikanyaga sheria ya MUNGU wanaimarishwa na wewe katika uasi wao. Huwezi kuwa na nguvu hadi utakapochukua msimamo dhabiti wa Ukweli. {1T 545.2}

Utoaji wa mpango kwa ukarimu unaonekana kwako kama siyo wa lazima; unapuuza Ukweli kwamba mali zilitoka kwa MUNGU, ambaye hekima Yake huwa haikosei. Mpango huu aliagiza kuokoa mkanganyiko, kurekebisha tamaa, uchoyo, uchu, ubinafsi, ubahili na ibada ya sanamu. Mfumo huu ulikusudiwa kupuguza mzigo kidogo, lakini kwa uzito unaostahili juu ya wote. Wokovu wa mwanadamu uligharimu bei kuwa sana, hata maisha ya Bwana wa utukufu, ambayo Yeye aliyatoa bure ili kumwinua mwanadamu kutoka katika uharibifu na kumtukuza kuwa mrithi wa ulimwengu. MUNGU ameamuru kwamba mwanadamu atamsaidia mwenzake katika kazi kubwa ya ukombozi. Yeyote anayeweka udhuru katika hili, ambaye hataki kujikana mwenyewe ili kusudi wengine waweze kushiriki pamoja naye faida ya mbinguni, anajithibitisha kuwa hastahili maisha yajayo, haistahili hazina ya mbinguni iliyogharimu dhabihu kubwa sana. MUNGU hataki sadaka isiyo ya hiari, hakuna dhabihu ya shinikizo. Wale ambao wameongoka kikamilifu na wanaoithamini kazi ya MUNGU watatoa kidogo kinachohitajika kutoka kwao kwa furaha, wakichukulia kuwa kutoa ni upendeleo/fursa. {1T 545.3}

Malaika alisema: "Jiepusheni na tamaa za mwili zinazopigana na roho." Umejikwaa katika matengenezo ya afya. Kwako inaonekana kuwa ni kiambatanisho kisichohitajika kwenye Ukweli. Siyo hivyo; ni sehemu ya Ukweli. Hapa kuna kazi mbele yako ambayo itazidi kukukaribia na kuwa ngumu zaidi kuliko kitu chochote ambacho kimepata kukujia. Wakati unasitasita na kusimama nyuma, ukishindwa kushikilia baraka ambayo ni upendeleo wako kuipokea, wewe unapata hasara. Unajikwaa kwenye baraka ambayo mbingu zimeiweka katika njia yako ili kupunguza ugumu wa maendeleo yako. Shetani anayawasilisha haya mbele yako kwa nuru isiyofaa kabisa, ili upingane na yale ambayo yangethibitisha faida kubwa kwako, ambayo yatakuwa kwa ajili ya afya yako ya mwili na roho. Kati ya watu wote wewe ndiye mfaidika wa matengenezo ya afya; Ukweli uliopokelewa kwa kila jambo linalohusu suala hili la matengenezo utakuwa wa faida kubwa. Wewe ni mtu ambaye utafaidika na lishe ya ziada. Ulikuwa katika hatari ya kuangushwa chini kwa muda mfupi na kupooza, nusu yako moja ikafa. Kukataa tamaa ya chakula ni wokovu kwako, lakini unaona kama ni ukosefu mkubwa. {1T 546.1}

Sababu inayofanya vijana wa wakati huu kutokuwa na mwelekeo wa kidini zaidi ni kasoro iliyopo katika elimu yao. Siyo upendo wa weli unaooneshwa kwa watoto ambao unaruhusu ndani yao tamaa ya makuu, au kuruhusu tabia ya kutotii sheria za wazazi iachwe bila kuadhibiwa. "Kama ambavyo shina changa la linavyokunjwa na kuinama, kule linakolekea ndiko mti unakoelekezwa. "Mama anapaswa kupata ushirikiano wa baba katika juhudi zake za kuweka msingi wa tabia njema ya Kikristo kwa watoto wake. Baba anayependa sana hapaswi kufumbia macho makosa ya watoto wake kwa sababu hiyo haimpendezikatika marekebisho. Ninyi nyote wawili mnahitaji kuamka na kwa uthabiti, si kwa ukali, bali kwa kusudi la kuelekeza, wafanyeni watoto wenu wajue kwamba wanapaswa kuwatii. {1T 546.2}

Baba hapaswi kuwa kama mtoto, akiongozwa na msukumo tu. Amefungwa kwenye familia yake na mahusiano matakatifu. Kila mwanafamilia anamtegemea baba. Jina lake linamaanaisha, "mhimili wa nyumba au House band," ni ufafanuzi wa kweli wa mume. Yeye ndiye mtunga sheria, akielezea kwa nguvu zake za kiume zilizobeba wema, nguvu, uadilifu, uaminifu, na matumizi ya vitendo. Baba kwa maana moja ni kuhani wa nyumba, akiweka juu ya madhabahu ya MUNGU dhabihu ya asubuhi na jioni, wakati mke na watoto wakiungana katika maombi na sifa. Katika nyumba kama hiyo Yesu atakaa na kuchelewa kutoka humu, na kwa njia ya ushawishi wake wa kuamsha vifijo vya furaha vya wazazi vitasikiwa katikati ya maonesho yaliyoinuliwa zaidi, wakisema: "Tazama, mimi na watoto ambao Bwana amenipatia." Tumeokolewa, tumeokolewa, tumeokolewa milele! Tumeondolewa kutoka kwenye uharibifu ulioko ulimwenguni wa tamaa, na kupitia sifa za Kristo tumefanywa warithi wa kutokufa! Nililiona hilo lakini ni akina baba wachache wanaotambua wajibu wao. Hawajajifunza kujidhibiti au kujitawala wenyewe, wasipojifunza somo hili watafanya kazi duni katika kuwatawala na kusimamia watoto wao. Udhibiti kamili utafanywa kama sumaku kwa familia. Wakati hili linapofikiwa, ushindi mkubwa unapatikana. Kisha wanaweza kuwafundisha watoto wao kujidhibiti. {1T 547.1}

Moyo wangu una hisia za matamanio makubwa kwa kanisa lililoko huko -----, kwa maana kuna kazi inayopaswa kutimizwa huko. Ni mpango wa MUNGU kuwa na watu mahali hapo. Kuna nyenzo huko kwa ajili ya kanisa zuri, lakini kuna kazi kubwa ya kufanywa kuondoa kingo mbaya na kuwaandaa katika utaratibu wa kufanya kazi, ili wote wafanye kazi kwa umoja na mshikamano. Hadi sasa imekuwa kwamba wakati mmoja au wawili wanapohisi ulazima wa kuamka na kusimama katika umoja na uthabiti zaidi kwenye jukwaa lililoinuliwa la Ukweli, wengine hawafanyi bidii kujitokeza au kuamka. Shetani huweka uasi ndani yao, huwakatisha tamaa wale ambao wangesonga mbele. Wanajiimarisha wenyewe wanapohimizwa kuifanya kazi hiyo, roho ya ukaidi huwajia wengine, na wakati

wanapotakiwa kusaidia wao wanazuia. Wengine hawatajisalimisha kwenye kisu cha MUNGU kinacholainisha kingo rafurafu. Pale unapopita juu yao na uso wenye nundu na kuisumbua, wanalalamika kwa sababu ya kazi hiyo kubwa yenye ugumu. Wanatamani kutoka kwenye karakana ya MUNGU, ili kasoro zao zibaki bila kusumbuliwa. Wanaonekana wamelala katika hali yao; lakini tumaini lao pekee ni kubaki pale ambapo kasoro katika tabia zao za Kikristo zitaonekana na kurekebishwa. {1T 547.2}

Wengine wanaendekeza uchu mbaya wa chakula ambao unapigana dhidi ya roho na ni kizuizi cha mara kwa mara kwa maendeleo yao ya kiroho. Wao hubeba dhamiri inayoshutumu kila wakati, na Ukweli wa moja kwa moja unaposemwa wao wamejiandaa kukasirishwa. Wanajihukumu na kuhisi kuwa masomo hayo yamechaguliwa kwa makusudi ili yaguse mambo yao. Wanahisi kuhuzunika na kujeruhiwa, na kujitenga na mikutano ya watakatifu. Wanaacha kukusanyika pamoja, maana kwa kufanya hivyo dhamiri zao hazitasumbuliwa sana. Punde wanapoteza hamu yao ya mikutano na upendo wao kwa Ukweli, na kama wasipobadilika kabisa, watarudi na kuchukua msimamo wao pamoja na jeshi la waasi ambao wanasimama chini ya bendera nyeusi ya Shetani. Ikiwa Kweli hizi zitasulubisha tamaa za mwili ambazo zinapigana dhidi ya roho, wataondoka njiani, mahali ambapo mishale ya Ukweli itapita bila kuwa na madhara kwao. Lakini wakati wanapojiendekeza katika tamaa mbaya ya chakula au vileo, na kwa hivyo kuzithamini sanamu zao, wanajifanya kuwa alama ambayo mishale ya Ukweli inapita, na ikiwa Ukweli unasemwa kama ulivyo, lazima wajeruhiwe. Wengine wanafikiria kuwa hawawezi kufanya matengenezo kwa sababu kwamba afya itaharibika ikiwa watajaribu kuacha matumizi ya chai, tumbaku, na nyama. Hili ndilo pendekezo la Shetani. Ni vichocheo hivi vyenye kuumiza ndivyo ambavyo hakika vinaharibu afya na kuandaa mfumo wa magonjwa ya papo kwa hapo kwa kudhoofisha mashine nzuri za asili na kubomoa ngome zake zilizojengwa dhidi ya magonjwa na kuoza mapema. {1T 548.1}

Wale ambao hufanya mabadiliko na kuacha vichocheo hivi visivyo vya asili kwa muda watahisi hasara yao na kuteseka sana kwa kuvikosa kwa muda fupi, kama vile mlevi ambaye ameathiriwa na pombe yake. Viondoe vinywaji vyenye kileo naye anaumia sana. Lakini ikiwa ataendelea hivi punde ataushinda ukosefu huo wa kutisha wa kileo. Asili itamsaidia na kubaki kwenye nafasi yake hadi atakapopata mbadala wa vichocheo hivyo vya uongo mahali pake. Wengine wamepuuzia hisia nzuri za asili kiasi kwamba inaweza kuhitaji muda kidogo kwake kupona kutoka kwenye manyanyaso/dhuluma iliyomfanya ateseke kupitia tabia mbaya za mwanadamu, tamaa ya chakula, anasa, ambavyo vimeshika moyo na kudhoofisha nguvu zake. Ipeni nafasi asili, nayo itapangilia tena na kutekeleze sehemu yake kwa uzuri na ubora. Matumizi ya vichocheo visivyo vya asili ni uharibifu kwa afya na vina ushawishi mbaya kwenye ubongo,

na kuifanya isiweze kuthamini mambo ya umilele. Wale wanaoendekeza sanamu hizi hawawezi kuthamini wokovu ambao Kristo amewafanyia kupitia maisha ya kujinyima, kujikana nafsi, kuteseka daima na aibu, na hatimaye kuyatoa maisha Yake Mwenyewe yasiyo na dhambi ili kumwokoa mtu anayeangamia katika kifo. {1T 549.1}

## SURA YA 96

## BIMA YA MAISHA

Nilioneshwa kwamba Waadventista wa Sabato hawapaswi kushiriki katika bima ya maisha. Hii ni biashara na ulimwengu ambayo MUNGU haikubali. Wale wanaojihusisha na biashara hii wanaungana na ulimwengu, wakati MUNGU anawaita watu Wake kutoka kati yao na kujitenga. Malaika alisema: "Kristo amewanunua kwa dhabihu ya maisha Yake. “Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la ROHO MTAKATIFU aliye ndani yenu, mliyepewa na MUNGU? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni MUNGU katika miili yenu. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika MUNGU. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja Naye katika utukufu.” Hii ndio bima pekee ya maisha ambayo inaridhiwa na mbingu {1T 549.2}

Bima ya maisha ni sera ya ulimwengu ambayo inawaongoza ndugu zetu wanaojihusisha nayo kuachana na unyenyekevu na usafi wa injili. Kila hatua hiyo ya kuondoka inadhoofisha imani yetu na kunapunguza hali yetu ya kiroho. Malaika alisema: "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya MUNGU, mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu." Sisi ni watu wa pekee wa Bwana. Kristo ametununua sisi. Malaika ambao wana nguvu zaidi hutuzunguka. Hakuna shomoro hata mmoja anayeanguka chini bila Baba yetu wa mbinguni kujua. Hata nywele za vichwa vyetu zimehesabiwa. MUNGU amewawezesha watu Wake. Anawajali sana, na hawapaswi kutilia shaka majaliwa na uongozi Wake kwa kujihusisha na sera za ulimwengu. {1T 550.1}

MUNGU anakusudia kwamba tuhifadhi kwa unyenyekevu na utakatifu upendeleo na upekee wetu. Wale wanaojihusisha na sera hii ya kidunia huwekeza mali ambayo ni ya MUNGU, ambayo Yeye amewakabidhi waitumie katika kusudi Lake, kuendeleza kazi Yake. Lakini ni wachache watakaotambua mapato yoyote yatokanayo na bima ya maisha, na bila baraka za MUNGU hata hawa wataambulia kupata maumivu badala ya faida. Wale ambao MUNGU

amewafanya kuwa mawakili Wake hawana haki ya kuweka mali katika uwanja wa adui, ambazo MUNGU amewakabidhi kuzitumia katika kusudi Lake. {1T 550.2}

Shetani kila wakati anawasilisha vivutio kwa watu waliochaguliwa na MUNGU ili kuvuta akili zao kutoka kwenye kazi nzito ya maandalizi ya matukio yajayo hivi karibuni. Yeye ni mdanganyifu katika kila neno, msanii mbobezi katika kuloga. Anajivika mipango na mitego yake kwa vifuniko vya nuru/taa vilivyokopwa kutoka mbinguni. Alimshawishi Hawa kula tunda lililokatazwa kwa kumfanya aamini kwamba litamnufaisha sana. Shetani huwaongoza mawakala wake kuanzisha mavumbuzi kadhaa na haki za umiliki na biashara zingine, ili Waadventista wanaoitunza Sabato ambao wana haraka ya kuwa matajiri waweze kuanguka kwenye majaribu, wanaswe, na kujichoma kwa huzuni nyingi. Ameamka macho kabisa na, anajishughulisha na kuuongoza ulimwengu kuwa mateka, na kupitia mawakala wa wana wa ulimwengu anaendelea kuwa na msisimko wa kupendeza kuendelea kuwavuta wasio macho ambao wanadai kuuamini Ukweli waungane na walimwengu. Tamaa ya jicho, shauku ya msisimko na burudani ya kupendeza, ni jaribu na mtego kwa watu wa MUNGU. Shetani ana nyavu nyingi za hatari zilizosokotwa vizuri, ambazo zimefanywa zionekane hazina hatia, lakini ambazo anazitayarisha kwa ustadi ili kuwavutia watu wa MUNGU. Kuna maonesho ya kupendeza, maburudisho, elimu ya frenolojia inayohusu uwezo wa kiakili, na mengine mengi ya biashara yanayoibuka kila wakati yakiwa yamepangiliwa kuwaongoza watu wa MUNGU kuipenda dunia na vitu vilivyomo. Kupitia muungano huu na ulimwengu, imani inadhoofishwa, na mali ambazo zinapaswa kuwekeza katika kusudi la Ukweli wa sasa zinahamishiwa kwenye kambi la adui. Kupitia njia hizi tofauti za uchawi wa Shetani, adui anakausha mifuko ya watu wa MUNGU kwa ustadi, na kwa hiyo hasira ya Bwana inawakalia (Frenolojia/Phrenology haikuidhinishwa na kanisa lolote la Kikristo hapo mwanzo. Frenolojia ni sayansi ya uwongo ambayo hupima matuta kwenye fuvu ili kutabiri sifa za kiakili. Ilikuwa maarufu nchini Marekani katika miaka ya 1830 na 1840. Ushahidi dhidi ya phrenology uliongezeka kwani Wanasaikolojia hawajawahi kukubaliana juu ya nambari za msingi za viungo vya akili, kutoka 27 hadi zaidi ya 40, na walikuwa na ugumu wa kupata matuta/bumps za akili hata hivyo elimu hii inasaidia watu kuwa wabaguzi wa jinsia, rangi, urithi nk. Tunajua mtu akiwa katika Kristo hata hivyo ni kiumbe kipya bila kujali matuta kwenye ubongo!). {1T 550.3}

# SURA YA 97

# KUSAMBAZA MACHAPISHO

Nimeoneshwa kuwa hatuna sababu ya kutofanya wajibu wetu katika usambazaji wa machapisho madogo madogo. Kuna roho nyingi za uaminifu ambazo zinaweza kuletwa kuukubali Ukweli kwa njia hii peke yake. Ikiwa katika kila nakala ya vipeperushi hivi liwepo tangazo la machapisho yetu na maeneo yanakoweza kupatikana, hii itaongeza usambazaji wa machapisho makubwa na magazeti ya *Review, Instructor, na Reformer*. {1T 551.1}

Hivi vipeperushi vidogo vyenye kurasa nne, nane, au kumi na sita vinaweza kutolewa kwa wingi kwa pesa ndogo tu, kutoka kwenye mfuko uliotokana na michango ya wale ambao kazi iko moyoni. Unapomwandikia rafiki unaweza kuambatanisha kwenye barua kipeperushi moja au zaidi bila kuongeza ujazo wa posta. Unapokutana na watu kwenye magari, kwenye mashua, au kwenye hatua ambayo wanaonekana kuwa na sikio la kusikia, unaweza kuwapatia kipeperushi. Vipeperushi hivi havipaswi kwa mwanzoni kutawanywa kama majani ya vuli unapoanza, bali vinapaswa kutolewa kwa busara na kwa uhuru kwa wale ambao wangeweza kuvitunza na kuvithamini. Kwa hiyo machapisho yetu na Chama cha Uchapishaji vitatangazwa kwa njia ambayo italeta mazuri mengi. {1T 552.1}

## SURA YA 98

## MWANAMATENGENEZO WA AFYA

Watu wanaangamia kwa kukosa maarifa. Anasema mtume: "Katika imani yenu tieni na wema; na katika wema wenu maarifa." Baada ya kupokea imani ya injili, kazi yetu ya kwanza ni kutafuta kuongeza kanuni nzuri na safi, na hivyo kusafisha akili na moyo kwa ajili ya kupokea maarifa ya Kweli. Magonjwa ya karibu kila aina yanawabamiza watu, lakini wanaonekana wako tayari kubaki katika ujinga wa kutofuata njia za kupata unafuu na hatua ya kufuata ili kuepuka magonjwa. {1T 552.2}

Katika kuanzishwa kwa taasisi ya afya, lilikuwa kusudi la MUNGU siyo tu kwamba maarifa yanaweza kutolewa kwa wachache kulinganisha na ambao wanapaswa kuyasikia, bali wengi wafundishwe tiba/matibabu ya nyumbani. Matengenezo ya afya ndiyo njia ambayo miale ya nuru inapaswa kuwaangazia watu. Linapaswa kuwepo jarida bora kabisa la afya katika nchi yetu. Lazima liigwe katika mahitaji ya watu wa kawaida, liwe tayari kujibu maswali yote kwa usahihi na kuelezea kikamilifu kanuni za kwanza za sheria za maisha na jinsi ya kuzitii na kuitunza/kuhifadhi afya. Jambo kuu linalopaswa kuzingatiwa na uchapishaji wa jarida kama hilo linapaswa kuwa wema wa watu wa MUNGU wanaoteseka. Watu wa kawaida, hasa wale maskini sana ambao hawawezi kuhudhuria katika taasisi hiyo (sanitarium), lazima wafikiwe na kuelekezwa na mwanamatengenezo wa afya. {1T 552.3}

# SURA YA 99

# TAASISI YA AFYA

Katika maono niliyopewa Desemba 25, 1865, niliona kuwa matengenezo ya afya yalikuwa ni mradi mkubwa uliounganishwa kwa karibu na Ukweli wa sasa, na kwamba Waadventista Wasabato wanapaswa kuwa na nyumba ya wagonjwa ambao wangeweza kutibiwa magonjwa yao na pia kujifunza jinsi ya kujitunza ili kuepukana na magonjwa (Sanitarium). Niliona kuwa watu wetu hawapaswi kubaki kuwa wasiojali juu ya fundisho hili na kuwaacha matajiri kati yetu waende kwenye taasisi maarufu za tiba ya maji nchini ili kurejesha afya, ambapo wangepata upinzani dhidi ya maoni yao juu ya hilo badala ya kushiriki mtazamo wao wa imani ya kidini. Wale ambao huathiriwa na magonjwa wanateseka siyo tu kwa kukosa nguvu za kimwili bali pia nguvu za kiakili na kimaadili; na hao wanaoteseka, watunza Sabato makini hawawezi kupata faida nyingi pale wanapohisi kwamba lazima walindwe kila wakati ili wasije wakavunja imani yao na kudharau madai imani yao, kama katika taasisi ambayo madaktari na wasimamizi wanaunga mkono uUkweli unaofungamana na ujumbe wa malaika wa tatu. {1T 553.1}

Watu wanapokuwa wameteseka sana na magonjwa wanafarijiwa na kupewa afueni na mfumo mzuri wa matibabu, unaojumuisha maji ya kuoga kwa njia ya Hydrotherapia, usafi, lishe bora, vipindi sahihi vya kupumzika na mazoezi, na matokeo mazuri ya hewa safi, na mara nyingi huongozwa kuhitimisha kuwa wale wanaofanikiwa kuyatendea haki katika masuala ya imani ya dini, angalau hawawezi kupotea sana kutoka kwa Ukweli. Kwa hivyo ikiwa watu wetu wameachwa kwenda kwenye taasisi hizo ambazo matabibu wao wameharibikiwa katika imani ya kidini, wanakuwa katika hatari ya kunaswa na kupotoshwa. Katika taasisi ya -----, niliona (mnamo 1865), ilikuwa bora zaidi

Marekani kupita zote. Kuhusiana na matibabu ya wagonjwa, wamekuwa wakifanya kazi nzuri na bora; lakini wanawahimiza wagonjwa wao kucheza ngoma, dansi na kucheza kadi, na wanawapendekezea wagonjwa kuhudhuria kwenye sinema, michezo ya kuigiza (theatre) na maeneo kama hayo ya burudani za ulimwengu, ambazo ni kinyume kabisa na mafundisho ya Kristo na mitume. {1T 553.2}

Wale waliounganishwa na taasisi ya afya ambayo sasa iko Battle Creek wanapaswa kuhisi kuwa wanafanya kazi muhimu na yenye heshima, na kwa vyovyote vile hawapaswi kuwaiga madaktari walioko katika taasisi hiyo ya ----- katika maswala ya dini na burudani. Lakini niliona kuwa kutakuwa na hatari ya kuwaiga katika mambo mengi na kupoteza mtazamo wa tabia iliyoinuliwa ya kazi hii kubwa. Na ikiwa wale wanaohusiana na mradi huu wataacha kuziangalia kazi zao kwa mtazamo wa juu wa kidini, na kushuka kutoka kwenye kanuni zilizoinuliwa za Ukweli wa sasa kuwaiga kwa nadharia na vitendo wale ambao ni wakuu wa taasisi ambazo wagonjwa hutibiwa kwa ajili ya urejeshaji wa afya, baraka maalum za MUNGU hazitakuwa juu ya taasisi yetu zaidi ya pale ambapo nadharia mbovu na za ufisadi zinafundishwa na kutekelezwa. {1T 554.1}

Niliona kuwa kazi kubwa sana haiwezi kutekelezwa kwa muda mfupi, kwani lisingekuwa jambo rahisi kuwapata matabibu ambao MUNGU angewakubali na ambao wangefanya kazi pamoja kwa maelewano, bila kujifikiria wenyewe, na kwa usongo kwa ajili ya faida ya wanadamu wanaoteseka. Inapaswa kukumbukwa kila wakati kuwa jambo kuu linalopatikana kupitia mfereji huu siyo afya tu, bali ukamilifu, na roho ya utakatifu, ambavyo haviwezi kupatikana katika miili na akili za wagonjwa. Kitu hiki hakiwezi kulindwa kwa kufanya kazi kutokana na mtazamo wa ulimwengu. MUNGU atainua watu na kuwastahilisha kushiriki katika kazi hiyo, siyo tu kama matabibu wa mwili, bali wa roho inayougua dhambi, kama baba wa kiroho kwa vijana na wale wasio na uzoefu. {1T 554.2}

Nilioneshwa kuwa msimamo wa Dk E kuhusu maburudisho haukuwa sahihi, na kwamba maoni yake juu ya mazoezi ya mwili siyo yote yaliyokuwa sahihi. Burudani anazozipendekeza mara nyingi zinazuia urejeshwaji wa afya kwa ambaye angezitumia au hata kusaidiwa. Kwa kiwango kikubwa amelaani kazi za nguvu kwa wagonjwa, na mafundisho yake katika visa vingi yameonekana kuwa jeraha kubwa kwao. Mazoezi ya akili kama kucheza kadi, karata na bao (cards, chess, checkers), husisimua na kuchosha ubongo na kuchelewesha kupona, wakati kazi nyepesi na yenye kupendeza itatumia muda, kuboresha mzunguko wa damu na mitoki nk, husaidia kurejesha ubongo, na kudhihirisha faida kubwa kwa afya. Lakini muondoe mgonjwa au mlemavu kutoka kwenye shughuli zote

hizo, atahangaika na kukosa utulivu, na, akiwa na mawazo ya kuugua, ataiona hali yake kuwa ni mbaya zaidi kuliko ilivyo, na kuwa dhaifu. {1T 554.3}

Kwa miaka nimeoneshwa mara kwa mara kwamba mgonjwa anapaswa kufundishwa kuwa ni makosa kusimamisha kazi zote za mwili ili kurudisha afya. Maana kwa kufanya hivyo, matakwa hudumaa, na damu hutembea taratibu ndani ya mfumo na kila wakati inazidi kuwa chafu. Mahali ambapo mgonjwa yuko katika hatari ya kufikiria hali mbaya zaidi kuliko alivyo, kutofanya shuguli yoyote, au kukaa siku nzima kutahakikisha unatoa matokeo yasiyofurahisha zaidi. Kazi iliyosimamiwa vizuri inampa mgonjwa na mlemavu wazo kwamba yeye siyo mtu asiyefaa kabisa ulimwenguni, bali angalau ana faida fulani. Hii itampa kuridhika, itampa ujasiri, na nguvu, ambazo haziwezi kutolewa na maburudisho. {1T 555.1}

Maoni kwamba wale ambao wametumia vibaya nguvu zao za mwili na akili, au ambao wamedhoofika katika akili au mwili, lazima wasimamishe shughuli ili kupata afya, ni kosa kubwa. Katika matukio machache kupumzika kwa muda mfupi kunaweza kuwa muhimu, lakini matukio haya ni nadra sana. Katika hali nyingi mabadiliko yatakuwa makubwa sana. Wale ambao wamevunja mwili na kazi kubwa ya akili wanapaswa kupumzisha uchovu wao wa fikra, na kuwafundisha kuwa ni vibaya na ni hatari kwao kutumia nguvu zao za akili kwa kiwango kinachowapelekea kuona hali yao kuwa mbaya kuliko ilivyo katika uhalisia. Wanabaki kuwa na wasiwasi zaidi na ni shida kubwa na kero kwa wale ambao wanawatunza. Katika hali hii ya akili, kupona kwao kuna mashaka kweli kweli. {1T 555.2}

Wale ambao wamedhoofika kwa kazi ya mwili wanapaswa kupunguza kazi, wafanye kazi nyepesi na yenye kupendeza. Lakini kuwafunga mbali na kazi zote na mazoezi mara nyingi kutathibitisha uharibifu wao. Mapenzi na nia huenda na kazi ya mikono yao, na wale waliozoea kufanya kazi watahisi kuwa ni mashine tu za kufanyishwa kazi na matabibu na wahudumu, na mawazo yataugua. Kutokuwa na shughuli ni laana kubwa zaidi ambayo inaweza kuwajia watu kama hao. Nguvu zao zinadumaa kwa kukosa kazi, kiasi kwamba hawawezi kuhimili magonjwa na shida, kama wanavyopaswa kufanya ili wapate afya tena. {1T 556.1}

Dkt E amefanya kosa kubwa juu ya mazoezi na burudani, na kubwa zaidi katika mafundisho yake juu ya uzoefu wa kidini na msisimko wa kidini. Dini ya Biblia siyo hatari kwa afya ya mwili au akili. Ushawishi wa juu na unaoinua wa ROHO WA MUNGU ni urejeshwaji bora wa afya kwa wagonjwa. Mbingu yote ni afya, na kadri ushawishi wa kimbingu unavyohisiwa zaidi ndivyo wale wanaoamini kwamba ni walemavu wanavyopona zaidi. Ushawishi wa maoni kama haya ambayo yameendelezwa na Dr E umetufikia sisi kwa kiwango fulani.

Wanamatengenezo wanaoitunza Sabato lazima wawe huru kutoka katika haya yote. Kila matengenezo ya Kweli na halisi yatatuleta karibu na MUNGU na mbingu, karibu na upande wa Yesu, na kutuongezea maarifa ya mambo ya kiroho na kutujengea utakatifu wa uzoefu wa Kikristo. {1T 556.2}

Ni kweli kwamba kuna akili zisizo na usawa zinazojiwekea mfungo ambao Maandiko hayaufundishi, na maombi na ukosefu wa pumziko na usingizi mambo ambayo MUNGU hajawahi kuyaagiza. Hao hawafanikishwi na kudumishwa katika matendo yao ya haki ya hiari. Wana dini ya kifarisayo ambayo siyo ya Kristo, bali ya kwao wenyewe. Wanategemea matendo yao mema kupata wokovu, wakitumaini bure kuipata mbingu kwa kazi zao njema badala ya kutegemea sifa na stahili za Mwokozi aliyesulubiwa, aliyefufuka, na kuinuliwa, kama ambavyo kila mwenye dhambi anapaswa kuwa. Hawa wamekaribia kuwa wagonjwa. Lakini Kristo na utauwa wa Kweli ni afya kwa mwili na nguvu kwa roho. {1T 556.3}

Hebu walemavu wafanye kitu badala ya kuzijaza akili zao kwa mchezo rahisi, ambayo inawashusha katika makadirio yao wenyewe na kuwafanya wafikiri kwamba maisha yao hayana maana na hawana faida kwa lolote. Hebu amsha nguvu za ya shauku, kwani shauku iliyoamshwa na kuelekezwa kwa usahihi ni kitulizo chenye nguvu cha mishipa ya fahamu. Walemavu wanakuwa na furaha zaidi kufanya kazi, na urejeshwaji wao unafanywa kwa urahisi zaidi. {1T 557.1}

Niliona kuwa laana kubwa kabisa ambayo ilimjia mume wangu na dada F yalikuwa maagizo waliyoyapokea huko----- kuhusu kukaa bila kufanya kazi ili wapone. Mawazo ya wote wawili yalikuwa magonjwa, na kukaa kwao bila kufanya kazi kuliwapelekea katika fikra na hisia kuwa itakuwa hatari kwa afya na maisha kufanya mazoezi, hasa kama kwa kufanya hivyo watachoka. Mashine ya mfumo wa mwili ilisogezwa kwa nadra, na ikapoteza uimara na nguvu, kwa hiyo walipofanya mazoezi, viungo vyao vilikuwa vigumu na misuli dhaifu, na kila hatua iliyohitaji juhudi kubwa na kwa kweli ilisababisha maumivu. Lakini uchovu huu ungekuwa baraka kwao ikiwa, bila kujali hisia au dalili zisizopendeza, wangeupinga kwa uvumilivu mwelekeo wao wa kutojishughulisha, yaani kukaa bila kufanya viungo vijongee. {1T 557.2}

Niliona kwamba itakuwa bora zaidi kwa dada F kuwa na familia yake peke yake na kuhisi majukumu yaliyo juu yake. Hii ingeamsha nguvu zake zilizolala maishani mwake. Nilioneshwa kuwa hali ya kudhoofu kwa familia hii nzuri wakiwa huko ----- haikuwa nzuri kwa elimu na mafunzo ya watoto wao. Kwa faida yao wenyewe watoto hawa wangepaswa kujifunza kuchukua majukumu katika kazi za nyumbani na wangepaswa kuhisi kuwa mizigo mingine maishani iko juu yao. Mama anayejishughulisha na elimu na mafunzo ya watoto wake, ameajiriwa katika kazi ambayo MUNGU amemkabidhi na kwa sababu ya rehema Zake ameyasikia maombi yaliyotolewa kwa ajili ya kupona kwake. Wakati

anapaswa kuachana na kazi za kuchosha, anapaswa zaidi ya yote kuepuka maisha ya kutokuwa na shughuli (kukaa tu). {1T 557.3}

Wakati nilipopewa maono huko Rochester, New York, niliona kuwa itakuwa bora zaidi kwa wazazi na watoto hawa kuunda familia peke yao. Watoto wanapaswa kila mmoja kuchukua sehemu ya kazi ya familia na hivyo kupata elimu ya maana ambayo isingeweza kupatikana kwa njia nyingine yoyote. Maisha huko ----- au mahali pengine popote, yaliyozungukwa na wahudumu na wasaidizi, ndilo jeraha kubwa zaidi kwa akina mama na watoto. Yesu anamwalika dada F apate pumziko ndani Yake na airuhusu akili yake ipokee toni nzuri kwa kutegemea mambo ya mbinguni na kutafuta kwa bidii kulitunza kundi lake dogo katika malezi na mashauri ya Bwana. Kwa njia hii anaweza kumsaidia vyema mumewe kwa kumtuliza hisia zake kwamba asione ana jukumu la kuweka umakini wake, masumbufu, na huruma kwa mkewe kupita kiasi. {1T 558.1}

Kwa kiwango cha nyumba za makazi katika taasisi ya Afya huko Battle Creek, nilioneshwa, kama nilivyosema hapo awali, kwamba tunapaswa kuwa na taasisi kama hiyo, ndogo wakati wa kuanzishwa kwake, na iongezeke kwa uangalifu, kadri ambavyo matabibu wazuri na wasaidizi wangeweza kuajiriwa na kuongeza fedha, na kama yalivyo mahitaji ya walemavu; na zote zinapaswa kuendeshwa kwa kufuata kanuni thabiti na roho ya unyenyekevu ya ujumbe wa malaika wa tatu. Na kama nilivyoona mahesabu makubwa yakihimizwa kwa haraka na wale wanaoongoza kazi hiyo, nimehisi tahadhari, na katika mazungumzo mengi ya faragha na kwa barua nimewaonya ndugu hawa waende kwa tahadhari. Sababu zangu ni kwamba bila baraka maalum za MUNGU kuna njia kadhaa ambazo mradi huu unaweza kuzuiwa, na kwa muda angalau, njia yoyote ile inaweza kuwa mbaya kwa taasisi na kuijeruhi kazi hiyo. Endapo matabibu wangeshindwa, kwa sababu za ugonjwa, kifo, au sababu nyingine yoyote, kazi ya kujaza nafasi zao ingekuwa changamoto, kazi hiyo ingezuiliwa hadi hapo madaktari wengine watakapoinuliwa; au ikiwa fedha zingeshindwa kupatikana wakati ambao majengo mengi yalikuwa yakijengwa, na kazi ikasimama, mtaji ungezama, na hali ya kukatisha tamaa ingewajia wote wanaovutiwa kwa ujumla; pia kunaweza kuwepo na ukosefu wa wagonjwa kujaza nyumba hizo kwa sasa, kwa sababu hiyo ukatokea ukosefu wa fedha za kukidhi gharama za sasa. Pamoja na juhudi zote zilizowekwa katika kila idara kwa njia sahihi na ya busara, na kwa baraka za MUNGU, taasisi hiyo itathibitisha mafanikio mazuri, wakati kutofaulu mara moja tu katika mwelekeo wowote kunaweza kudhibitisha jeraha kubwa mapema ama baadaye. Haipaswi kusahaulika kuwa kati ya taasisi nyingi za Sanitarium (tiba rahisi) zilizoanzishwa Marekani ndani ya miaka ishirini na tano iliyopita ni chache sana ambazo zimedumisha hata uwepo unaoonekana kwa wakati huu (vituo kama Kibidula Missionary School-Mafinga, Tanzania, au Riverside Zambia vinafanya huduma hizi za Sanitarium kwa namna fulani). {1T 558.2}

Nimetoa wito hadharani kuwasihindugu zetu kwa niaba ya taasisi itakayoanzishwa kati yetu, na nimesema kwa maneno ya hali ya juu zaidi na Dk F kama mtu ambaye kwa uongozi wa MUNGU amepata uzoefu wa kufanya kazi kama daktari. Nimeyasema haya kwa mamlaka ya yale ambayo MUNGU amenionesha. Ikiwa ni lazima, nitarudia bila kusita yote niliyosema. Sina kusudi la kuondoa sentensi hata moja ambayo nimeiandika au kuizungumza. Kazi hiyo ni ya MUNGU na lazima ifanywe kwa mkono thabiti lakini wenye tahadhari. {1T 559.1}

Matengenezo ya afya yameunganishwa kwa karibu na kazi ya ujumbe wa tatu, lakini bado siyo ujumbe. Wahubiri wetu wanapaswa kufundisha matengenezo ya afya, lakini hawapaswi kuifanya hii kuwa mada kuu mahali pa ujumbe. Mahali pake ni kati ya masomo ambayo yanaonesha kazi ya maandalizi ya kukidhi matukio yaliyooneshwa na ujumbe; kati ya haya- ujumbe huu ni maarufu. Tunapaswa kushikilia kila matengenezo kwa bidii, lakini tuepuke kutoa maoni kiasi cha kuyumba na kuwa chini ya ushabiki. Watu wetu wanapaswa kutoa fedha za kukidhi mahitaji ya taasisi ya afya inayokua miongoni mwetu, kama wanavyoweza kufanya bila kutoa kidogo kwa ajili ya mahitaji mengine ya kazi hiyo. Hebu matengenezo ya afya na taasisi ya afya vikue miongoni mwetu kama ambavyo miradi imekua, kwa kuzingatia nguvu zetu dhaifu za wakati uliopita na uwezo wetu mkubwa wa kufanya mengi kwa kipindi kifupi sasa. Hebu taasisi ya afya ikue, kama ambavyo mambo yetu mengine na maslahi yake yamekua, kwa haraka iwezekanavyo na salama na siyo kuyaathiri matawi mengine ya kazi kubwa ambayo yana umuhimu sawa au mkubwa zaidi kwa wakati huu. Kwa ndugu kuweka sehemu kubwa ya mali yake, awe ana vingi au kidogo katika taasisi,ili ashindwe kufanya mengi katika mwelekeo mwingine kama anavyopaswa kufanya, hilo litakuwa ni kosa. Na kwake yeye kutofanya chochote litakuwa kosa kubwa sana. Katika kila wito/ombi la kuwachochea watu wetu kutoa fedha kwa ajili ya taasisi kunapaswa kuwa na tahadhari ili kutoyanyang'anya matawi mengine ya kazi; hasa masikini wakarimu wanapaswa kuonywa. Baadhi ya watu maskini walio na familia, wasio na nyumba zao wenyewe, na ambao ni masikini sana wasioweza kwenda kwenye taasisi kutibiwa, wameweka kuanzia moja ya tano (1/5) hadi moja ya tatu (1/3) ya mali zote walizonazo katika taasisi. Hili ni kosa. Baadhi ya ndugu na jamaa wana hisa kadhaa wakati ambapo hawakupaswa kuwa hata na moja, na wangepaswa kuhudhuria kwenye taasisi japo kwa muda mfupi, wakilipiwa gharama zao zote au kwa sehemu, kutoka kwenye mfuko wa hisani. Sioni hekima ya kufanya mahesabu makubwa kwa ajili ya wakati ujao na kuwaacha wale wanaoteseka ambao wanahitaji msaada sasa. Msiende haraka, ndugu zangu, kuliko ambavyo majaliwa na fadhila za MUNGU zizizokosea zimefungua njia mbele, kwa ajili yenu.{1T 559.2}

Matengenezo ya afya ni tawi la kazi maalum ya MUNGU  kwa faida ya watu Wake. Niliona kwamba katika taasisi iliyoanzishwa miongoni mwetu hatari

kubwa itakuwa kwa wasimamizi wake kujitenga na roho ya Ukweli wa sasa na kutoka kwenye unyenyekevu ambao unapaswa kuwa tabia ya wanafunzi wa Kristo. Nilipewa onyo dhidi ya kushusha kiwango cha Ukweli kwa njia yoyote katika taasisi kama hiyo ili kusaidia hisia za wasioamini na hivyo kupata ufadhili wao. Lengo kuu la kuwapokea wasioamini katika taasisi hiyo ni kuwaongoza kuukubali Ukweli. Ikiwa kiwango kitashushwa, watapata maoni kwamba Ukweli una umuhimu kidogo, na wataondoka katika hali ya akili ambayo ni ngumu kuifikia kuliko hapo awali. {1T 560.1}

Lakini uovu mkubwa kabisa utokanao na hatua kama hiyo utakuwa ni ule ushawishi wake kwa wagonjwa maskini, wenye shida, wanaoamini, ambao utaiathiri kazi hiyo kwa ujumla. Hawa wamefundishwa kutegemea maombi ya imani, na wengi wao roho zao zimejikunja kwa sababu maombi sasa hayajajibiwa kikamilifu. Niliona kwamba sababu ambayo MUNGU hakuyasikia kikamilifu maombi ya watumishi Wake kwa wagonjwa walio miongoni mwetu ni kwa kuwa hakuweza kutukuzwa kwa kufanya hivyo wakati walipokuwa wakikiuka sheria za afya. Na niliona pia kwamba MUNGU amedisaini matengenezo ya afya na taasisi ya afya ili kuandaa njia ya maombi ya imani kujibiwa kikamilifu. Imani na matendo mema vinapaswa kwenda sambamba katika kuwatuliza walioteswa miongoni mwetu, na kuwafanya wafae kumtukuza MUNGU hapa na kuokolewa wakati wa kuja kwa Kristo. MUNGU aepushie mbali ili hawa walio taabika kamwe wasije wakakatishwa tamaa na kuhuzunishwa kwa kuwakuta wakuu wa taasisi wakifanya kazi kwa mtazamo wa ulimwengu badala ya kuongeza kwenye mazoezi ya afya na usafi baraka na fadhila za akina baba na akina mama walezi katika Israeli. {1T 560.2}

Hebu mtu yeyote asipate wazo kwamba taasisi ni mahali pao pa kuja kukuzwa katika maombi ya imani. Hapo ni mahali pa kupata nafuu ya magonjwa kwa matibabu na mwenendo mzuri wa kuishi, na kujifunza jinsi ya kuepukana na magonjwa. Lakini ikiwa kuna sehemu moja chini ya mbingu zaidi ya nyingine ambapo sala inayotuliza, yenye huruma inapaswa kutolewa na wanaume na wanawake wa waliojitoa na wenye imani ni katika taasisi kama hiyo. Wale wanaowatibu wagonjwa wanapaswa kusonga mbele katika kazi yao muhimu wakimtegemea sana MUNGU kwa baraka zZke na kutumia rasilimali ambazo ameziandaa kwa neema, na ambazo kwa rehema zake amevuta usikivu wetu kama hewa safi, usafi, lishe bora, vipindi sahihi vya kazi na mapumziko, na matumizi ya maji. Hawapaswi kuwa na masilahi ya ubinafsi nje ya kazi hii muhimu na makini. Kuyaangalia kwa usahihi masilahi ya mwili na ya kiroho ya watu wa MUNGU walioteseka ambao wameweka imani yao isiyo na kikomo ndani yao na kwa gharama kubwa wamejiweka chini ya uangalizi wao kutahitaji umakini wao usiogawanyika. Hakuna mtu aliye na akili mahiri sana, au mjuzi sana, ambaye kazi yake haitakuwa kamili baada ya yeye kuifanya kwa bidii. {1T 561.1}

Hebu wale ambao wamepewa dhamana ya masilahi ya kimwili na kwa kiwango kikubwa ya kiroho ya watu wa MUNGU wanaoteseka, waangalie jinsi ambavyo kupitia sera ya ulimwengu au masilahi binafsi au shauku ya kushiriki katika kazi kubwa na maarufu, na wasijishushe wao wenyewe na tawi hili la kazi ya uso wa MUNGU. Hawapaswi kutegemea ujuzi na ustadi wao peke yao. Kama baraka za MUNGU ziko juu taasisi badala ya uso wenye hasira, Malaika watawahudumia wagonjwa, kama wasaidizi; na madaktari ili kusaidia katika kazi ya urejeshwaji, ili mwishowe utukufu uende kwa MUNGU na si kwa mwanadamu dhaifu, asiye na upeo wa kuona mbali. Ikiwa watu hawa wangefanya kazi kutokana na sera ya ulimwengu, na mioyo yao ikainuliwa na kujisikia kusema, "Nguvu zangu, na uweza wa mkono wangu vimefanya hivi," MUNGU angewaacha wafanye kazi chini ya dhiki kubwa na kudhalilishwa na taasisi zingine katika maarifa, uzoefu, na nguvu. Wasingeweza kukamilisha hata nusu ya kazi ambayo ingefanywa na taasisi zingine. {1T 562.1}

Niliona ushawishi mzuri wa kazi ya nje kwa wale walio na nguvu dhaifu na mzunguko wa damu nyogovu, hasa kwa wanawake ambao wamechochea hali hizi kwa kufungiwa sana ndani ya nyumba. Damu yao imekuwa chafu kwa kukosa hewa safi na mazoezi. Badala ya burudani zinazowaweka watu hawa ndani ya nyumba, uangalifu unapaswa kuchukuliwa ili kuwapatia vivutio vya nje ya nyumba. Niliona kwamba taasisi inapaswa kuunganishwa na viwanja vya kutosha, vilivyopambwa na maua na kupandwa mboga na matunda. Hapa wadhaifu wangeweza kupata kazi, iliyo sahihi kulingana na jinsia yao na hali, kwa masaa yanayofaa. Viwanja hivi vinapaswa kuwa chini ya uangalizi wa mtunza-bustani mzoefu ili awe anawaelekeza wote kwa njia ya kupendeza na ya utaratibu. {1T 562.2}

Uhusiano ambao ninauendeleza kwa kazi hii unahitaji maoni yangu yasiyopunguzwa. Nazungumza kwa uhuru na nimechagua njia hii kuzungumza na wote wanaopenda. Kilichoonekana katika ushuhuda nambari 11 kuhusu taasisi ya afya hakikupaswa kutolewa mpaka ambapo ningeweza kuandika yote niliyoyaona juu yake. Sikukusudia kusema chochote juu ya mada hiyo katika nambari 11, na kutuma miswada yote ambayo niliiandaa kwa Ushuhuda huo kutoka wilaya ya Ottawa, ambapo nilikuwa nikifanya kazi wakati huo, kwenda kwenye ofisi huko Battle Creek, nikieleza kwamba nilipenda waiharakishe kazi ile kidogo, kama ilivyokuwa inahitajika sana, na haraka iwezekanavyo ningeandika nambari 12, ambamo nilikusudia kuzungumza kwa uhuru na ukamilifu kuhusu taasisi. Ndugu zangu huko Battle Creek ambao walipendezwa sana na taasisi hiyo walijua nimeona kwamba watu wetu wanapaswa kuchangia fedha zao kuanzisha taasisi kama hiyo. Kwa hivyo waliniandikia kwamba ushawishi wa ushuhuda wangu kuhusu taasisi ulihitajika mara moja kuwahamasisha hao ndugu juu ya suala hili, na kwamba uchapishaji wa nambari 11 ungecheleweshwa hadi pale ambapo ningeweza kuandika. {1T 562.3}

Hili lilikuwa jaribu kubwa kwangu, kwani nilijua kuwa siwezi kuandika yote niliyoyaona, kwa sababu wakati huo nilikuwa nikiongea na watu mara sita au nane kwa wiki, nikitembelea nyumba kwa nyumba, na kuandika mamia ya kurasa za Shuhuda binafsi na barua binafsi. Kiasi hiki cha kazi, pamoja na mizigo na majaribu yasiyokuwa ya lazima yaliyotupwa kwangu, yalinifanya nisifae kwa kazi ya aina yoyote. Afya yangu ilikuwa dhaifu, na mahangaiko yangu ya kiakili yalikuwa hayaelezeki. Chini ya mazingira haya nilisalimisha uamuzi wangu kwa wengine na nikaandika kile kilichoonekana katika nambari 11 kuhusu taasisi ya afya,kwa vile sikuweza kutoa yote niliyoyaona. Katika hili nilifanya makosa. Napaswa kuruhusiwa kuutambua wajibu wangu mwenyewe kuliko wengine wanavyoweza kuutambua kwa ajili yangu, hasa kuhusiana na mambo ambayo MUNGU amenifunulia. Nitalaumiwa na wengine kwa kusema kama ninavyosema sasa. Wengine watanilaumu kwa kutokuzungumza kabla. Tabia iliyojidhihirisha kuleta msongamano wa haraka wa suala hili lihusulo taasisi imekuwa moja ya majaribu mazito zaidi ambayo nimewahi kuyapata. Ingekuwa kwamba wote ambao wameutumia ushuhuda wangu kuwavuta ndugu wameguswa vivyo hivyo wao wenyewe, ningeridhika zaidi. Kama ningechelewa zaidi kusema maoni na hisia zangu, ningepaswa kulaumiwa zaidi na wale ambao wanafikiria kwamba ningepaswa kuzungumza mapema na wale ambao pia wanadhani kwamba sipaswi kutoa tahadhari yoyote. Kwa faida ya wale wanaoongoza kazi, kwa faida ya kazi na ndugu zetu, na mimi kwa ajili ya kujiokoa kutoka katika majaribu makubwa, nimezungumza kwa uhuru na hiari yangu mwenyewe. {1T 563.1}

## SURA YA 100

## AFYA NA DINI

[haya na makala nyingine zinazofuata ni dondoo kutoka katika barua ambazo niliwaandikia wale waliokuwa wakuu wa kituo cha afya, ya kwanza, tarehe moja mei, 1867, na ya pili, mwezi uliofuata wa June. E.G.W]

MUNGU angetaka kuona taasisi ya afya ikianzishwa ambayo kwa ushawishi Wake itaunganishwa kwa karibu na kufunga kazi, yaani kazi ya mwisho ya wanadamu wanaokufa kupewa stahiki za kutokufa, ambayo haitakuwa na mwelekeo wa kudhoofisha kanuni za kidini za wazee au vijana na ambayo haitaboresha afya ya mwili kwa kudhuru ukuaji wa kiroho. Lengo kuu la taasisi hii linapaswa kuwa uboreshaji wa afya ya mwili, ili watu wanaoteseka wapate kuyafahamu mambo ya umilele na kuyathamini. Ikiwa kitu hiki hakijawekwa mbele ya akili na juhudi hazijafanywa kufikia mwisho huu, itathibitisha kuwa

laana badala ya baraka, hali ya kiroho itachukuliwa kama jambo la pili, na afya ya mwili na ukengeufu vitawekwa kuwa vya kwanza. {1T 564.1}

Niliona kwamba kiwango cha juu hakipaswi kushushwa katika kiwango kidogo ili taasisi hiyo ipendwe na wasioamini. Ikiwa watu wasioamini watachagua kuja na wasimamizi wake wakishika nafasi ya kiroho iliyoinuliwa ambayo MUNGU ameikusudia, kutakuwa na nguvu ambayo itaathiri mioyo yao. Wakiwa na MUNGU na malaika upande wao, watu Wake wanaozishika amri, lazima mambo yaweze kufanikiwa. Taasisi hii haifai kuanzishwa kwa lengo la kupata faida, bali kusaidia katika kuwaleta watu wa MUNGU katika hali kama hiyo ya afya ya mwili na akili ambayo itawawezesha kuthamini vitu vya umilele na kuthamini kwa usahihi ukombozi ulionunuliwa kwa mateso ya Mwokozi wetu. Taasisi hii haipaswi kufanywa mahali pa ukengeufu au maburudisho. Wale ambao hawawezi kuishi bila kuwa na msisimko na ukengeufu, au hata kuchepushwa mawazo kwa namna fulani hawatakuwa na faida kwa ulimwengu; hakuna aliyepata faida na kuwa bora kutokana na maisha yao. Watu kama hawa ni bora wasiwemo katika ulimwengu kuliko kuwemo. {1T 564.2}

Niliona kuwa maoni yanayodai kwamba hali ya kiroho ni hatari kwa afya, ambayo Dkt E alitaka kuyaingiza ndani ya akili za wengine, si chochote zaidi ya mbinu za udanganyifu shetani. Shetani alipata njia ya kuingia Edeni na kumfanya Hawa aamini kwamba alihitaji kitu zaidi ya kile ambacho MUNGU alikuwa amempatia kwa ajili ya furaha yake, kwamba tunda lililopigwa marufuku litakuwa na ushawishi maalum wa kusisimua juu ya mwili na akili yake, na litamwinua hata kuwa sawa na MUNGU katika maarifa. Lakini ujuzi na faida aliyofikiria kupata vilithibithisha kuwa laana ya kutisha. {1T 565.1}

Kuna watu wenye mitazamo dhaifu ambao kwao dini ni ukatili, na inawaongoza kama fimbo ya chuma. Hao daima wanaomboleza juu ya uharibifu wao na kuugua juu ya uovu unaodhaniwa. Upendo haupo mioyoni mwao; mwonekano wenye hasira daima uko juu ya nyuso zao. Wametetemeshwa mioyo na kicheko kisicho na hatia kutoka kwa vijana au kutoka kwa mtu yeyote. Wanachukulia burudani zote au starehe kama dhambi na wanafikiria kwamba akili lazima iwekwe kila wakati katika kiwango cha juu chenye sauti ya ukali. Hiki ni kiwango kilichopitiliza kiasi kwa upande mmoja. Wengine wanafikiri kwamba akili lazima iwe katika hali ya kunyumbulishwa na kuvumbua burudani mpya na kuachana na zile za awali ili kuweza kupata afya. Wanajifunza kutegemea misisimko, na hawapati raha bila hiyo. Hao siyo Wakristo wa kweli. Wanaenda katika kiwango kilichopita kiasi kwa upande mwingine. Kanuni za Kweli za Ukristo hufungulia mbele ya wote chanzo cha furaha, kimo na kina, urefu na

upana ambao hauna kipimo. Ni Kristo ndani yetu kisima cha maji kinachobubujika kuelekea uzima wa milele. Ni kisima endelevu ambacho kwacho Mkristo anaweza kunywa kwa kupenda na asiikaushe chemchemi kabisa. {1T 565.2}

Mambo karibu yote yanayoleta ugonjwa wa mwili na akili ni hisia zisizoridhika na maoni yasiyotoshelezwa, yasiyo na furaha. Hawana MUNGU, hawana tumaini linaloyafikia yale yaliyomo ndani ya pazia, ambayo ni kama nanga ya roho iliyo hakika na thabiti. Wote walio na tumaini hili watajitakasa kama vile Yeye alivyo safi. Hao wako huru kutoka katika tamaa zisizo na utulivu, kukosa furaha, kutotosheka wala kuridhika; hawatafuti ubaya kila wakati, hawajilazimishi kuwa watu wasio na furaha na kujiletea matatizo yasiyowahusu. Lakini tunaona wengi ambao wamekuwa na wakati wa shida kabla; wasiwasi umewekwa juu ya kila kipengele cha mwili wao; wanaonekana hawapati faraja, lakini wanaendelea kuwa na mwonekano aw hofu, wakitarajia maovu ya kutisha zaidi yatawajia. {1T 566.1}

Hao humvunjia MUNGU heshima, na kuileta dini ya Kristo katika sifa mbaya. Hawana upendo wa Kweli kwa MUNGU, wala kwa wenzi wao na watoto. Mapenzi yao yamekuwa mabaya, mawazo kuelekea kwenye mada za huzuni kama vile kifo. Lakini burudani batili hazitasahihisha akili za watu kama hao. Wanahitaji ushawishi wa ROHO WA MUNGU ubadilishao ili wawe na furaha. Wanahitaji kufaidika na upatanisho wa Kristo, ili waitambue faraja ya Bwana yenye thamani. "Kwa maana, Atakaye kupenda maisha, Na kuona siku njema, Auzuie ulimi wake usinene mabaya, Na midomo yake isiseme hila. Na aache mabaya, atende mema; Atafute amani, aifuate sana. Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio Yake husikiliza maombi yao; Bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya." Wale ambao wana ujuzi wa kivitendo wa Andiko hili wana furaha ya Kweli. Wanachukulia kibali/kukubaliwa na Mbingu kama jambo la thamani zaidi kuliko burudani yoyote ya kidunia; Kristo ndani yao tumaini la utukufu litakuwa afya kwa mwili na nguvu kwa roho. {1T 566.2}

Unyenyekevu wa injili unapotea haraka kutoka kwa wale wanaojiita watunza Sabato. Ninauliza mara mia kwa siku, JE, MUNGU anawezaje kutufanikisha sisi? Kuna maombi kidogo tu. Kwa kweli, maombi ni kama yamepitwa na wakati. Ni wachache ambao wako tayari kuubeba msalaba wa Kristo, aliyebeba msalaba wa aibu kwa ajili yetu. Siwezi kuhisi kwamba katika taasisi mambo yanaenda kama ambavyo MUNGU angekusudia yaende. Ninaogopa kwamba Yeye ataugeuza uso wake kutoka kwenye taasisi. Nilioneshwa kuwa matabibu na wauguzi wanapaswa kuwa wenye upeo wa juu, wale ambao wana ujuzi wa ukweli kwa vitendo, ambao wataamuru heshima, na ambao neno lao linaweza

kutegemewa. Wanapaswa kuwa watu ambao hawana mawazo dhaifu yenye kuugua, watu ambao wana udhibiti kamili, ambao hawayumbi wala kubadilika, ambao hawana wivu wala mawazo mabaya na kuzungumza wengine vibaya, watu ambao wana nguvu ya maamuzi ambayo hayatasababisha uharibifu, ambao hawana ubaguzi, ambao hawatafikiria ubaya wowote, ambao wanafikiria na kusonga mbele kwa utulivu, kwa uangalifu, wakiwa na utukufu wa MUNGU na mazuri ya wengine mbele yao. Kamwe mtu hapaswi kuinuliwa kwenye nafasi ya uwajibikaji kwa sababu tu anaitamani. Wanapaswa kuchaguliwa wale ambao wamekidhi kuwa katika nafasi hiyo. Wale ambao watabeba majukumu wanapaswa kwanza kudhibitishwa, na ushahidi upatikane kwamba hawana wivu, kwamba hawamtachukia huyu au yule, wakati wana marafiki wachache wanaowapenda na kutowajali wengine. MUNGU ampe kila mtu kuenenda sawa sawa tu katika taasisi hiyo. {1T 566.3}

## SURA YA 101

## KAZI NA MABURUDISHO

Mpendwa kaka F: Akili yangu imejikita sana katika jambo moja au mawili. Ninapofikia hatua ya kukuandikia barua usiku baada ya usiku katika usingizi wangu, basi nadhani kwamba ni wakati wa kutekeleza dhamira ya jukumu langu. Nilipooneshwa kwamba Dk E alikosea katika baadhi ya mambo kuhusu maagizo aliyowapa wagonjwa wake, niliona kuwa umepokea mawazo sawa na yeye katika mambo mengi na kwamba wakati utakuja ambapo utaona kwa usahihi kuhusu jambo hilo. Mambo haya yanahusu kazi na maburudisho. Nilioneshwa kuwa itakuwa faida zaidi kwa wagonjwa wengi kuwaruhusu wafanye kazi nyepesi, tena hata kwa kuhimizwa, kuliko kuwaambia kwamba wakae bila kujishughulisha wala kufanya kazi yoyote. Ikiwa nguvu ya maamuzi itashughulishwa ili kuamsha viungo vilivyolala, hilo litakuwa na msaada mkubwa zaidi katika safari ya kupona. Ondoeni kazi zote kutoka kwa wale ambao wamezidiwa zaidi kwa maisha yao yote na katika visa tisa kati ya kumi (9/10) mabadiliko yatakuwa ya kuumiza. Hili limekuwa kweli katika kisa cha mume wangu. Nilioneshwa kuwa mazoezi ya mwili ya nje ya nyumba ni bora kuliko ya ndani; lakini kama hili haliwezi kufanikiwa, kazi nyepesi za ndani zitaiteka na kuigeuza akili, na kuizuia isiwe katika dalili za magonjwa madogo madogo, na pia zitazuia hamu ya kuwa nyumbani (homesickness). {1T 567.1}

Mfumo huu wa kutofanya chochote, niliona kwamba ulikuwa laana kubwa kwa mke wako na mume wangu. MUNGU aliwapa kazi jozi/wenzi wawili wa kwanza katika Edeni kwa sababu alijua watakuwa na furaha zaidi wanapojishughulisha. Kutoka katika kile nilichooneshwa, mfumo huu wa kutofanya chochote ni laana kwa roho na mwili. Kazi nyepesi hazitasisimua au kuchochea akili au nguvu yoyote kama maburudisho. Wagonjwa mara nyingi hufika mahali wanapoangalia hisia zao mbaya na kufikiria kuwa hawawezi kabisa kufanya chochote, wakati kama wangeamsha nia na kujilazimisha kufanya kiasi cha kazi ya mwili kila siku, wangefurahi zaidi na kuwa bora kwa haraka zaidi. Nitaandika kikamilifu juu ya jambo hili baadaye. {1T 568.1}

Ninaelewa kutoka kwenye barua ya hivi karibuni ya Rochester kwamba uchezaji wa karata haufanywi tena kama maburudisho huko katika taasisi ya ----- EGW, Maandishi kutoka toleo la kwanza. (569) {1T 568.2}

**Utangulizi**

Kwa mara nyingine tena ninahisi kuwa ni jukumu langu kuzungumza na watu wa Bwana kwa uwazi zaidi. Ni kudhiliwa kwangu kuelezea makosa na uasi wa wale ambao kwa muda mrefu wamefahamiana na sisi na kazi yetu nasi. Ninafanya hivyo ili kusahihisha matamko/taarifa mbaya ambazo zimekwenda ng'ambo kumhusu mume wangu na mimi mwenyewe kwa makusudi ya kuumiza kazi, na kama onyo kwa wengine. Ikiwa mimi na mume wangu tu tungelazimika kuteseka, basi, ningenyamaza kimya; lakini wakati kazi ya Mungu inapokuwa katika hatari ya lawama na mateso, lazima niongee, hata kama inadhalilisha. Wanafiki wenye kiburi watawashinda ndugu zetu kwa sababu wao ni wanyenyekevu vya kutosha kukiri dhambi zao. MUNGU anawapenda watu Wake ambao wanazishika amri Zake, na kuwakemea, siyo kwa sababu wao ni wabaya zaidi, bali kwa sababu wao ni watu bora zaidi ulimwenguni. "Wale wote ninaowapenda,"Yesu anasema, Mimi "nawakemea na kuwarudi." {1T 569.1}

Ningependa kuangazia kwa umakini ndoto za kushangaza zilizotolewa katika kazi hii ndogo, zote zikiwa na maelewano na upekee unaoelezea kitu kile kile. Wingi wa ndoto hutokana na mambo ya kawaida ya maisha, ambayo ROHO WA MUNGU hahusiki kwa lolote. Pia kuna ndoto za uongo, pamoja na maono ya uongo, ambayo yanaongozwa na roho ya Shetani. Lakini ndoto zitokazo kwa Bwana zimeainishwa katika Neno la MUNGU na maono na ni matunda ya roho ya unabii kama maono. Ndoto kama hizo, kwa kuzingatia watu ambao wamezipata na mazingira ambayo wamepewa, hizi zina uthibitisho binafsi wa ukweli wao. {1T 569.2}

Baraka za MUNGU na ziambatane na kazi hii ndogo. {1T 570.1}

# SURA YA 102

# KIELELEZO CHA UZOEFU

Kuanzia Desemba 19, 1866 hadi Aprili 25, 1867

Baada ya kuridhika kabisa kwamba mume wangu hataweza kupona ugonjwa wake wa muda mrefu akiwa anaendelea kukaa bila kufanya kazi, na kwamba wakati ulikuwa umefika kabisa kwangu kwenda na kutoa ushuhuda wangu kwa watu, niliamua, kinyume na uamuzi na ushauri wa kanisa huko Battle Creek, tulikokuwa washiriki wakati huo, kujitosa kufanya ziara kaskazini mwa Michigan, na mume wangu katika hali yake dhaifu sana, katika baridi kali ya msimu wa baridi. Haikuhitaji kiwango kidogo cha maadili na imani kwa MUNGU kuleta akili yangu kwenye uamuzi wa kuhatarisha mengi sana, hasa niliposimama peke yangu, kinyume na ushawishi wa kanisa, pamoja na wale ambao ni viongozi wa kazi huko Battle Creek ambao walikuwa wakipinga. {1T 570.2}

Lakini nilijua kwamba nilikuwa na kazi ya kufanya, na ilionekana kwangu kwamba Shetani alikuwa ameazimia kunizuia kuifanya. Nilikuwa nimesubiri kwa muda mrefu ili kuwa mateka kwetu kugeuzwe na nilihofu kwamba roho za thamani zitapotea endapo nitachukua muda mrefu kutoka kazini. Kukaa kwa muda mrefu kutoka shambani, kwangu lilionekana kuwa jambo baya zaidi kuliko kifo, na ikiwa tutatoka nje tunaweza kuangamia. Kwa hivyo, mnamo 19 Desemba, 1866, tuliondoka kutoka Battle Creek katika dhoruba ya theluji kuelekea Wright, Wilaya ya Ottawa, Michigan. Mume wangu alistahimili safari ndefu na ngumu ya maili tisini zaidi ya nilivyoogopa, na alionekana kuwa sawa pia wakati tulipofika kwenye nyumba yetu ya zamani kwa kaka Root tukiwa tumetoka Battle Creek. Tulipokelewa kwa fadhili na familia hii pendwa na tukatunzwa kwa upole kama vile wazazi Wakristo wanavyoweza kuwatunza watoto walemavu. {1T 570.3}

Tulilikuta kanisa hili katika hali ya chini sana. Sehemu kubwa ya washiriki wake mbegu za kutengana na kutoridhika kati yao zilikuwa zikichipua mizizi, na roho ya udunia ilikuwa inawamiliki. Na licha ya hali yao ya chini walikuwa wamefurahia kazi ya wahubiri wetu kidogo sana kiasi kwamba walikuwa na njaa ya chakula cha kiroho. Hapa tulianzisha kazi yetu ya kwanza yenye ufanisi tangu ugonjwa wa mume wangu. Hapa alianza kufanya kazi kama kipindi cha miaka ya zamani, ingawa alikuwa katika udhaifu mwingi. Angeongea dakika thelathini au arobaini mchana wa Sabato na siku ya kwanza, na mimi ningejazia muda uliobaki, kisha ningezungumza saa moja na nusu alasiri ya kila siku. Tulisikilizwa kwa umakini mkubwa. Niliona kwamba mume wangu alikuwa akiongezeka nguvu, akizidi kuwa muwazi, na kushikamana zaidi katika masomo yake. Na katika tukio moja alizungumza saa moja kwa uwazi na nguvu, na mzigo wa kazi ukiwa juu yake na kadri alivyokuwa akiongea, hisia zangu za shukrani zilipita maelezo. Nilisimama katika kusanyiko na kwa karibu nusu saa nilijaribu kuzungumza kwa machozi. Kusanyiko liliguswa sana. Nilihisi kuwa na hakika kwamba haya yalikuwa mapambazuko ya siku bora kwetu. {1T 570.4}

Tulikaa na watu hawa kwa majuma sita. Nilizungumza nao mara ishirini na tano, na mume wangu mara kumi na mbili. Wakati tukiendeleza kazi na kanisa hili, mambo binafsi yalianza kufunguka mbele ya macho yangu, na nilianza kuandika Shuhuda kwa ajili yao, jumla ya kurasa mia moja. Ndipo tukaanza kazi kwa watu hawa walipokuja kwa ndugu Root, mahali tulipoishi, na baadhi yao majumbani mwao, lakini hasa kwenye mikutano katika nyumba ya ibada. Katika aina hii ya kazi niligundua kuwa mume wangu alikuwa msaada mkubwa. Uzoefu wake wa muda mrefu katika aina hii ya kazi, kama alivyofanya kazi nami hapo zamani, ulimstahilisha kufanya kazi iliyokidhi mahitaji ya watu. Na sasa kwa kuwa alikuwa ameingia tena alionekana kudhihirisha uwazi huo wote wa mawazo, uamuzi mzuri, na uaminifu katika kushughulika na wakosaji, kama siku za nyuma. Kwa kweli, hakuna wachungaji wetu wengine, hata kama wangekuwa wawili ambao wangeweza kunipa msaada ambao alinipatia. {1T 571.1}

Kazi kubwa na nzuri ilifanywa kwa watu hawa wapendwa. Makosa yalikubaliwa kwa uhuru na ukamilifu, umoja ulirejeshwa, na baraka za MUNGU zikawa juu ya kazi hiyo. Mume wangu alijitahidi kuleta utoaji wa mpango kwa ukarimu kwa kanisa na takwimu ambazo zinapaswa kuigwa katika makanisa yetu yote, na juhudi zake zilisababisha ongezeko la pesa inayorudishwa na kanisa hilo kwenye hazina kila mwaka kuwa kama dola mia tatu. Wale walioko kanisani ambao walikuwa wakisumbuliwa na shuhuda zangu zingine, hasa kuhusiana na suala la mavazi, walitulia kabisa ili kusikia jambo hilo likielezewa. Matengenezo ya afya na mavazi yalipitishwa, na kiasi kikubwa kilipatikana kwa ajili ya taasisi ya afya. {1T 571.2}

Hapa nadhani ni jukumu langu kusema kwamba kadri kazi hii ilivyokuwa ikiendelea, kwa bahati mbaya ndugu mmoja tajiri kutoka Jimbo la New York

alimtembelea Wright baada ya kumwita huko Battle Creek na kugundua kwamba tumeanza kinyume na maoni na ushauri wa kanisa na wale waliosimamia kazi huko Battle Creek. Alichagua kumuelezea mume wangu, hata mbele ya wale ambao tulifanya kazi kubwa kwa ajili yao, kwamba alikuwa na wazimu, na kwa hiyo hata ushuhuda wake usichukuliwe kwa uzito wowote. Ushawishi wake katika jambo hili, kama nilivyoambiwa na ndugu Root, mzee wa kanisa, ulikwamisha kazi kwa angalau majuma mawili. Ninasema haya ili kwamba watu wasiojiweka wakfu waone wanavyoweza kujihadhari katika hali yao ya upofu, isiyo na hisia dhidi ya kutoa ushawishi kwa saa ambao unaweza kuwachukua watumishi wa Bwana wiki nzima kuukabili/kuupikua. Tulikuwa tukifanya kazi kwa ajili ya watu matajiri, na Shetani aliona kwamba ndugu huyu tajiri alikuwa mtu wa kumtumia tu. Hebu Bwana amlete mahali ambapo anapoweza kuona, na kwa unyenyekevu wa akili akiri makosa yake. Kwa majuma mawili ya kazi ya kuchosha sana, kwa baraka ya MUNGU, tuliweza kuondoa ushawishi huu mbaya na kuwapatia wapendwa uthibitisho kamili kwamba MUNGU alikuwa ametutuma kwao. Kama matokeo zaidi ya kazi zetu, watu saba baadaye walibatizwa na ndugu Wagoner, na wawili walibatizwa na mume wangu mnamo Julai wakati wa ziara yetu ya pili kwenye kanisa hilo. {1T 572.1}

Ndugu kutoka New York alirudi na mkewe na binti yake huko Battle Creek, siyo katika hali ya mawazo ya kutoa taarifa sahihi ya kazi nzuri huko Wright au kusaidia hali ya kanisa huko Battle Creek. Kama ukweli ulivyobainika tangu zamani, inaonekana kwamba alililijeruhi kanisa, na kanisa lilimjeruhi, kwa furaha yao ya pamoja kutoka nyumba moja kwenda nyingine katika kuchukua maoni yasiyofaa ya kazi yetu na kuyafanya kuwa mada ya mazungumzo. Katika kipindi ambacho kazi hii ya kikatili ilipokuwa ikiendelea, nilikuwa na ndoto ifuatayo: {1T 573.1}

Nilikuwa nikitembelea Battle Creek nikiwa na mtu mwenye tabia njema na mwenye hadhi mamlaka kubwa. Katika ndoto yangu nilikuwa nikipita karibu na nyumba za ndugu zetu. Wakati tunakaribia kuingia, tukasikia sauti zikifanya mazungumzo ya dhati. Jina la mume wangu lilitajwa mara kwa mara, na nilihuzunika na kushangaa kusikia wale ambao walidai kuwa marafiki zetu wakubwa zaidi wakisimulia mambo na matukio ambayo yalitokea wakati wa mateso makali ya mume wangu, wakati nguvu zake za kiakili na za mwili zilipokuwa zimepooza kwa kiwango kikubwa. Nilisikitika kusikia sauti ya yule aliyejiita kaka yangu kutoka New York kabla ya kutajwa, akielezea kwa bidii, na kwa nuru iliyotiwa chumvi, matukio ambayo wale walioko Battle Creek hawakuyajua, wakati marafiki zetu huko Battle Creek, kwa zamu yao, walisimulia kile walichokijua. Nilisikia kuzimia na kuugua moyoni, na katika ndoto yangu nilikaribia kuanguka, wakati mkono wa mtumishi wangu uliponisaidia, akasema: "Lazima usikilize. Lazima ulijue hili hata kama ni vigumu kulivumilia." {1T 573.2}

Katika nyumba kadhaa tulizozikaribia, jambo hilo hilo lilikuwa mada ya mazungumzo. Ulikuwa ndiyo ukweli wao wa sasa. Nikasema: "Oh, sikulijua hili! Sikujua kwamba hisia kama hizo zilikuwepo katika mioyo ya wale ambao tumewachukulia kama marafiki zetu katika mafanikio, na marafiki zetu wa karibu katika mateso, shida, na taabu. Hakika ningelijua hili! Tumewahesabu hawa marafiki zetu kwamba ni bora zaidi na wakweli." {1T 573.3}

Mtu yule aliyekuwa pamoja nami aliyarudia maneno haya: "Ikiwa wangeshiriki kwa utayari, dhati na kwa juhudi na bidii katika mazungumzo juu ya Mkombozi wao, wakikaa katika uchamgamfu wake ulio kama sumaku isiyo na kifani, ukarimu Wake usio na ubinafsi, na msamaha Wake wa rehema, upole wake wa huruma kwa wanaoteseka, Uvumilivu Wake na upendo usioweza kuelezeka, matunda yangekuwa mengi na ya thamani kiasi gani. " {1T 574.1}

Kisha nikasema: "Nimehuzunishwa. Mume wangu hajajibakiza katika kuokoa roho. Alibeba mizigo mpaka walipomponda; mwili wake ulichoshwa, akadhoofika mwili na akili; na sasa kukusanya maneno na matendo na kuyatumia kuharibu ushawishi wake, baada ya MUNGU kumwekea mkono Wake na kumwinua ili sauti yake isikike tena, huu ni ukatili na uovu." {1T 574.2}

Yule mtu aliyefuatana nami alisema: "Mazungumzo ambayo Kristo na sifa za maisha Yake ndizo mada zinazojadiliwa, yataburudisha roho na matunda yatakuwa kwa ajili ya utakatifu na uzima wa milele." Kisha akanukuu Maneno haya: "Hatimaye, ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo." Maneno haya yalinigusa moyoni sana kiasi kwamba niliyasema katika Sabato iliyofuata. {1T 574.3}

Kazi yangu huko Wright ilikuwa ya kuchosha sana. Nilikuwa na kazi makini ya kumhudumia mume wangu mchana, na wakati mwingine usiku. Nilimfanyia tiba ya maji ya hydrotherapia, nikamchukua kwenda nje, na mara mbili kwa siku, hata kwa baridi, dhoruba, au hali nzuri, nilitoka naye nje. Nilitumia kalamu wakati alipokuwa akinisimulia taarifa zake za *Review*, na pia niliandika barua nyingi, pamoja na kurasa nyingi za Shuhuda binafsi, na zaidi katika nambari 11, kando ya kutembelea na kuzungumza mara nyingi na kwa muda mrefu na kwa bidii kama nilivyofanya. Ndugu na dada Root walinihurumia sana katika majaribu na kazi zangu, na walituhudumia kwa wema mkuwa katika mahitaji yetu yote. Maombi yetu mara kwa mara yalikuwa kwamba Bwana awabariki katika kikapu na ghalani, katika afya na vile vile katika neema na nguvu za kiroho. Na nilihisi baraka maalum zingewafuata. Ingawa ugonjwa umekuja nyumbani kwao, lakini najifunza kwa ndugu Root kwamba sasa wanafurahia afya bora kuliko hapo awali. Na kati ya vitu vya ustawi wa muda anataarifu kwamba mashamba yake ya ngano yametoa kilo mia sita na sabini na tano (675) kwa ekari hiyo, na mashamba mengine kilo elfu moja (1000)), wakati wastani

wa mavuno katika shamba la majirani zake yamekuwa kilo mia moja sabini na tano tu kwa ekari (175). {1T 574.4}

Januari 29, 1867, tuliondoka Wright, na kusafiri hadi Greenville, Wilaya ya Montcalm, umbali wa maili arobaini. Ilikuwa siku ya baridi kali sana msimu wa baridi, na tulifurahi kupata makao huko kwa ndugu Maynard tukajiepusha na baridi na dhoruba. Familia hii pendwa ilitukaribisha ndani, kwa mioyo yao yote na nyumbani kwao. Tulikaa katika eneo hili kwa majuma sita, tukifanya kazi na makanisa huko Greenville na Orleans, na kuifanya nyumba ya ukarimu ya ndugu Maynard kuwa makao yetu makuu. {1T 575.1}

Bwana alinipa uhuru katika kusema na watu; katika kila juhudi niliyoifanya niligundua nguvu yake idumishayo. Na nilipojiridhisha kabisa kuwa nilikuwa na ushuhuda kwa watu, ambao ningeweza kuutoa kwao kuhusiana na kazi za mume wangu, imani yangu iliimarishwa kwamba bado atainuliwa na kuwa mzima wa afya ili atumike kwa ukubali katika kazi na kusudi la MUNGU. Kazi zake zilipokelewa na watu, na alikuwa msaada mkubwa kwangu katika kazi hiyo. Bila yeye ningeweza kutimiza kidogo tu, lakini kwa msaada wake, kwa nguvu ya MUNGU, niliweza kufanya kazi niliyopewa. Bwana alimtegemeza katika kila juhudi aliyofanya. Alipojitosa, akimtumaini MUNGU, bila kujali udhaifu wake, alipata nguvu na kuimarika kwa kila juhudi. Nilipogundua kuwa mume wangu alikuwa anapata tena nguvu ya mwili na akili, shukrani yangu haikuwa na mipaka kwa sababu ya matarajio ambayo ningepaswa bila kujizuia kushiriki upya na kwa bidii zaidi katika kazi ya MUNGU, nikiwa upande wa mume wangu, tulifanya kazi kwa umoja katika kazi ya kuhitimisha kwa ajili ya watu wa MUNGU. Kabla ya kudhoofika, nafasi aliyokuwa nayo ofisini ilimfunga hapo kwa muda mwingi sana. Na kwa kuwa sikuweza kusafiri bila yeye nilikuwa nakaa nyumbani muda mwingi. Nilihisi kuwa MUNGU sasa angemfanikisha wakati akifanya kazi kwa Neno na mafundisho ya imani, na akajitoa zaidi kwa ajili ya kazi ya kuhubiri. Wengine wangeweza kufanya kazi ofisini, na tulikuwa tumetulia katika imani yetu kiasi kwamba asingeweza kufungiwa ndani tena, bali awe huru kusafiri pamoja nami ili sisi wote tupate kutoa ushuhuda mzito ambao MUNGU= alikuwa ametupatia kwa ajili ya watu wake wa Masalio. {1T 575.2}

Nilihisi hali ya chini ya watu wa MUNGU, na kila siku nilijua kwamba nilikuwa nimeenda katika kiwango cha nguvu zangu. Wakati tukiwa Wright tulikuwa tumepeleka hati yangu ya nambari 11 kwenye ofisi ya uchapishaji, na nilikuwa nikiboresha karibu kila wakati nikiwa nje ya mkutano kwa kuandika mambo yaliyomo katika nambari 12. Nguvu zangu, za mwili na akili, zilikuwa zimetumika sana wakati nikifanya kazi za kanisa huko Wright. Nilihisi kwamba ningepaswa kupumzika, lakini sikuweza kuona fursa yoyote ya kupata unafuu. Nilikuwa nikiongea na watu mara kadhaa kwa wiki, na kuandika kurasa nyingi za ushuhuda binafsi. Mzigo wa roho ulikuwa juu yangu, na majukumu niliyohisi

yalikuwa makubwa sana kiasi kwamba ningeweza kupata masaa machache tu ya kulala kila usiku. {1T 576.1}

Wakati nilipokuwa nikifanya kazi kwa kusema na kuandika, nilipokea barua za kuvnja moyo sana kutoka Battle Creek. Nilipokuwa nikizisoma nilihisi huzuni ya roho isiyoweza kuelezeka, iliyonipelekea katika maumivu ya akili, ambayo yalionekana kwa muda mfupi kupooza nguvu zangu. Kwa siku tatu usiku sikulala kabisa. Mawazo yangu yalihangaika na kufadhaika. Nilificha hisia zangu kadri nilivyoweza kutoka kwa mume wangu na familia yenye huruma ambayo tulikuwa nayo. Hakuna aliyejua kazi yangu au mzigo wa akili wakati nilipoungana na familia asubuhi na jioni katika ibada, na nikataka kuweka mzigo wangu juu ya Yule Mbeba mizigo mkuu. Lakini maombi yangu yalitoka ndani ya moyo uliokamuliwa na uchungu, na maombi yangu yalivunjwa na kukatishwa kwa sababu kilio cha huzuni isiyoweza kudhibitiwa. Damu ilikimbilia kwenye ubongo wangu, mara nyingi hali hii ikanifanya nikorome hadi nikaribie kuanguka. Nilitokwa na damu puani mara nyingi, hasa baada ya kuandika kwa bidii. Nililazimika kuweka kando maandishi yangu, lakini sikuweza kuundoa mzigo wa wasiwasi na uwajibikaji juu yangu, kwani niligundua kuwa nilikuwa na Shuhuda kwa watu wengine ambao sikuweza kuuwasilisha kwao. {1T 576.2}

Nilipokea barua nyingine tena, ikinijulisha kuwa imeonekana ni bora kusitisha uchapishaji wa nambari 11 hadi ambapo ningeweza kuandika yale ambayo nilikuwa nimeoneshwa kuhusu taasisi ya afya, kwani wale ambao walikuwa wakisimamia mradi huo waliishiwa na fedha kabisa na walihitaji ushawishi wa ushuhuda wangu ili kuwavutia watu. Kisha nikaandika sehemu ya ile ambayo ilioneshwa kwangu kuhusiana na taasisi, lakini sikuweza kutoa somo lote kwa sababu ya shinikizo la damu kwenye ubongo. Laiti ningefikiria kuwa nambari 12 itacheleweshwa kwa muda mrefu, kwa vyovyote vile nisingepeleka sehemu ya suala hilo lililomo katika nambari 11. Nilidhani kwamba baada ya kupumzika siku chache ningeweza tena kuendelea na maandishi yangu. Lakini kwa huzuni kubwa niligundua kuwa hali ya ubongo wangu ilinifanya nishindwe kuandika. Wazo la kuandika shuhuda, ziwe za jumla au za binafsi, lilishindikana, na nilikuwa katika shida kila wakati kwa sababu sikuweza kuziandika. {1T 577.1}

Katika hali hii ya mambo iliamuliwa kwamba tungerudi Battle Creek na kubaki huko wakati barabara zikiwa katika hali ya matope, hali mbaya, na kwamba ningekamilisha nambari 12. Mume wangu alikuwa na wasiwasi sana kuwaona ndugu zake huko Battle Creek na kuzungumza nao na kufurahia pamoja nao katika kazi ambayo MUNGU alikuwa akimfanyia. Nilikusanya maandishi yangu, na tukaanza safari yetu. Njiani tulifanya mikutano miwili huko Orange na tulikuwa na ushahidi kwamba kanisa lilifaidika na kutiwa moyo. Sisi wenyewe tuliburudishwa na Roho wa Bwana. Usiku huo niliota kwamba nilikuwa huko Battle Creek nikitazama kutoka kwenye kioo cha pembeni ya mlangoni na kuona kundi likiandamana kwenda nyumbani wakiwa wawili wawili. Walionekana kuwa wenye nia thabiti na waliodhamiria. Niliwajua vizuri na

nikageuka kufungua mlango ili niwapokee wageni, lakini nikadhani kwamba napaswa kuangalia tena. Tukio lilibadilishwa. Kundi hilo sasa liliwasilisha mwonekano wa maandamano ya Watoliki. Mmoja alikuwa na msalaba mkononi mwake, na mwingine mwanzi. Na walipokaribia, yule aliyebeba mwanzi akazunguka nyumba, akisema mara tatu: "Nyumba hii iko chini ya ulinzi. Bidhaa zilizomo lazima zichukuliwe. Wamenena kinyume na utaratibu wetu mtakatifu." Hofu ilinishika, nikakimbia kupitia nyumba hiyo, kupitia mlango ulioko upande wa kaskazini, nikajikuta niko katikati ya kundi, ambalo wengine niliwatambua, lakini sikuthubutu kuwaambia neno kwa kuogopa kusalitiwa. Nilijaribu kutafuta sehemu nzuri ambapo ningeweza kulia na kuomba bila kukutana na macho yao yenye shauku na udadisi popote nilipogeukia. Nilirudia mara kwa mara: "Laiti ningeweza kulielewa hili! Laiti wangeniambia kile nilichosema au kile nilichofanya!" {1T 577.2}

Nililia na kuomba sana wakati nilipoona bidhaa zetu zikiporwa. Nilijaribu kutafuta huruma katika nyuso za wale walio karibu nami, na kutambua sura za watu kadhaa ambao nilidhani wangeongea nami na kunifariji endapo wasingeogopa kwamba wangeonwa na wengine. Nilifanya jaribio moja la kutoroka kutoka kwenye umati huo, lakini kwa kuona kwamba nilikuwa nikitazamwa, niliificha nia yangu. Nilianza kulia kwa sauti, na kusema: "Laiti wangeniambia tu kile nilichofanya au kile nilichosema!" Mume wangu, ambaye alikuwa amelala kitandani katika chumba kimoja, alinisikia nikilia kwa sauti na kuniamsha. Mto wangu ulikuwa umelowa machozi, na huzuni mbaya ya roho kusononeka, ilikuwa juu yangu. {1T 578.1}

Kaka na dada Howe waliongozana nasi kwenda West Windsor, ambapo tulipokelewa na kukaribishwa na kaka na dada Carman. Sabato na siku ya kwanza tulikutana na kaka na dada kutoka makanisa yaliyokuwa karibu na tulikuwa na uhuru wa kutoa ushuhuda wetu kwao. Roho ya kuburudisha ya Bwana ilitulia juu ya wale ambao walihisi hamu ya pekee katika kazi ya MUNGU. Mikutano yetu Konferensi ilikuwa mizuri, na karibu wote walitoa ushuhuda kwamba walikuwa wameimarishwa na kutiwa moyo sana. {1T 578.2}

Katika siku chache tulijikuta tena huko Battle Creek baada ya kukosekana kwa miezi mitatu. Siku ya Sabato, Machi 16, mume wangu aliwasilisha mbele ya kanisa hubiri lililohusu "Utakaso" lililorekodiwa na Fonografia na mhariri wa *Review* na kuchapishwa katika gombo la 29, nambari 18. Alizungumza pia kwa uwazi mchana na siku ya kwanza asubuhi. Nilitoa ushuhuda wangu kwa uhuru. Sabato ya tarehe 23, tulizungumza kwa uhuru katika kanisa la Newton na kufanya kazi na kanisa huko Convis Sabato na siku ya kwanza iliyofuata. Tulikusudia kurudi kaskazini na kwenda maili thelathini, lakini tulilazimika kurudi nyuma kwa sababu ya hali ya barabara. Mume wangu alivunjika moyo sana kwa mapokezi baridi ambayo alikutana nayo huko Battle Creek, na mimi pia nilihuzunika. Tuliamua kuwa hatuwezi kutoa ushuhuda wetu kwa kanisa hili mpaka watakapotoa ushahidi bora kwamba wanazihitaji huduma zetu, hivyo

tukamalizia kazi huko Convis na Monterey hadi ambapo barabara zingeboreshwa. Sabato mbili zilizofuata tulizitumia huko Convis na tuna ushahidi kwamba kazi nzuri ilifanyika, kwa sababu matunda bora yanaonekana sasa. {1T 579.1}

Nilirudi Battle Creek kama mtoto aliyechoka ambaye alihitaji maneno ya kufariji na kutiwa moyo. Inaniumiza hapa kusema kwamba tulipokelewa kwa ubaridi mkubwa sana na ndugu zetu, ambao miezi mitatu kabla, nilikuwa nimeachana nao kwa umoja kamili, isipokuwa kwa hatua ya kuondoka nyumbani. Usiku wa kwanza niliokaa Battle Creek, niliota kwamba nilikuwa nikifanya kazi kwa bidii sana na nilikuwa nikisafiri kwa kusudi la kuhudhuria mkutano mkubwa, na kwamba nilikuwa nimechoka sana. Akina dada walikuwa wakizipanga nywele zangu na kuyarekebisha mavazi yangu, mimi nilikuwa nimelala. Nilipoamka nilishangaa na kukasirika kugundua kuwa nguo zangu zilikuwa zimeondolewa, na nilikuwa nimewekewa matambara ya zamani, vipande vya vitambaa vya mablanketi vilivyofungwa na kushonwa pamoja. Nikasema: "Mmenifanyia nini? Ni nani aliyefanya kazi hii ya aibu ya kuondoa nguo zangu na kuziwekea vitambaa vya ombaomba?" Nilirarua vitambaa na kuvitupa mbali nami. Nilihuzunika, na kwa uchungu nikasema: "Nirudishieni nguo zangu ambazo nimezivaa kwa miaka ishirini na tatu na ambazo hazikunifedhehesha hata mara moja. Msiponirudishia nguo zangu nitaomba watu, ambao watanichangia na kunirudishia nguo zangu ambazo nimezivaa kwa miaka ishirini na tatu. " {1T 579.2}

Nimeona utimilifu wa ndoto hii. Huko Battle Creek tulikutana na taarifa ambazo zilikuwa zimewekwa kwenye mzunguko ili zituumize, lakini ambazo hazikuwa na msingi wa ukweli. Barua zilikuwa zimeandikwa na wengine ambao wanakaa kwa muda katika taasisi ya afya, na wengine wanaoishi Battle Creek, kwa makanisa huko Michigan na majimbo mengine, wakielezea hofu, mashaka, na maoni yao juu yetu. Nilijawa na huzuni nilipokuwa nikisikiliza mashtaka kutoka kwa mfanyakazi mwenzangu ambaye nilikuwa namheshimu, kwamba walikuwa wakisikia kila robo ya mambo ambayo nilikuwa nimeyazungumza dhidi ya kanisa huko Battle Creek. Nilihuzunika sana hata sikujua niseme nini. Tulikutana na roho kali, inayotushtaki. Tuliposadikishwa juu ya hisia zilizopo tulihisi kutamani kurudi nyumbani. Tulikatishwa tamaa na kufadhaika sana kiasi kwamba niliwaambia ndugu zetu wawili ambao ni viongozi kwamba sikujisikia kuwa niko nyumbani, kwani tulikutana na kutokuaminiana na ubaridi mkali badala ya kukaribishwa na kutiwa moyo, na bado nilipaswa kujifunza kuwa hii ndiyo njia ninayopaswa kuifuata kuelekea wale ambao walikuwa wamedhoofu kwa kufanya kazi kupita kiasi na kujitolea katika kazi ya MUNGU. Kisha nikasema kwamba tulifikiri tunapaswa kuhama kutoka Battle Creek na kutafuta nyumba iliyotulia zaidi. {1T 580.1}

Nikiwa na huzuni rohoni kupita kipimo, nilibaki nyumbani, kwa kuogopa kwenda popote kati ya kanisa kwa kuogopa kujeruhiwa. Mwishowe, kwa kuwa hakuna

mtu aliyefanya juhudi kupunguza hisia zangu, nilihisi ni jukumu langu kuwakutanisha ndugu na dada kadhaa wenye uzoefu, na kukutana na ripoti ambazo zilikuwa zikizunguka kuhusu sisi. Kwa kulemewa na kushuka moyo, hata kwa uchungu, nilikutana na mashtaka dhidi yangu, nikitoa kumbukumbu ya safari yangu mashariki, mwaka mmoja tangu, na hali zenye kuumiza zilizohudhuria safari hiyo. {1T 580.2}

Niliwaomba wale waliokuwepo wahukumu ikiwa uhusiano wangu na kazi na kusudi la MUNGU vitanisababisha nizungumze kwa wepesi juu ya kanisa la huko Battle Creek, ambalo sikuwa nimeziondoa hisia zangu hata kidogo. Je! Hamu yangu katika kazi na kusudi la MUNGU havikuwa kwa kiwango kikubwa kama ilivyowezekana kwao? Uzoefu wangu wote na maisha yangu vilifungamanishwa nayo. Sikuwa na jambo tofauti kando na kazi. Nilikuwa nimewekeza kila kitu kwa kazi hii, na sikuona dhabihu kubwa sana kwangu ninayoweza kutoa ili kuiendeleza. Sikuwa nimeruhusu mapenzi kwa watoto wangu wapendwa yanizuie kufanya wajibu wangu kama MUNGU alivyotaka katika kazi Yake. Upendo wa mama ulinigonga moyoni sana moyoni mwangu kama katika moyo wa mama yeyote aliyeishi, lakini nilikuwa nimejitenga na malezi ya watoto wangu na kumruhusu mwingine kuwafanyia majukumu ya mama. Nilikuwa nimetoa ushahidi dhahiri wa kupenda kwangu, na kujitolea katika kazi ya MUNGU. Nimeonesha kwa matendo yangu jinsi nilivyoipenda. Je! Kuna yeyote anayeweza kutoa uthibitisho wenye nguvu kuliko mimi? Je! Walikuwa na bidii katika kutetea Ukweli? Mimi zaidi. Je! Walikuwa wamejitolea? Ningeweza kuthibitisha kujitolea zaidi kuliko mtu yeyote aliye hai ambaye alijishughulisha na kazi hiyo. Je! Waliteseka kwa sababu ya Ukweli? Mimi zaidi. Sikuyahesabu maisha yangu kuwa ya bora kwangu kuliko kazi. Sikukwepa lawama, mateso, au shida. Wakati marafiki na jamaa wakiwa wamekata tamaa juu ya maisha yangu, kwa sababu ugonjwa ulikuwa ukiniangukia, nilikuwa nimebebwa mikononi mwa mume wangu kwenye mashua au magari. Wakati mmoja, baada ya kusafiri hadi usiku wa manane, tulijikuta katika jiji la Boston bila kuwa na fedha. Katika matukio mawili au matatu tulitembea kwa imani maili saba. Tulisafiri kadri nguvu zangu zilivyoruhusu kisha tukapiga magoti chini na kuomba nguvu ya kuendelea. Tulipewa nguvu, na tuliwezeshwa kufanya kazi kwa bidii kwa faida ya roho. Hatukuruhusu kizuizi chochote kutuzuia kutoka kwenye kazi au kututenganisha na kazi hiyo. {1T 581.1}

Roho iliyooneshwa katika mkutano huu ilinisumbua sana. Nilirudi nyumbani nikiwa bado na mzigo, kwani wale waliokuwepo hawakufanya jitihada zozote za kunifariji kwa kukiri kwamba walisadiki kwamba wamenihukumu vibaya na kwamba tuhuma na mashtaka yao dhidi yangu hayakuwa ya haki. Watu hawa hawakuweza kunilaani, wala hawakujitahidi kunipooza moyo au kunipa afueni. {1T 582.1}

Kwa kipindi cha miezi kumi na tano mume wangu alikuwa dhaifu sana kiasi kwamba hakuweza amebeba saa yake au mkoba, wala kuendesha farasi wake wakati alipokuwa akitoka. Lakini kwa mwaka huu alikuwa amechukua saa yake na mkoba uliokuwa tupu kwa sababu ya gharama zetu kubwa, na alikuwa ameenda na kundi lake mwenyewe la farasi. Wakati wa ugonjwa wake, alikataa kwa nyakati tofauti kupokea pesa kutoka kwa kaka zake hadi kiasi cha karibu dola elfu moja, akiwaambia kwamba wakati atapokuwa na uhitaji atawajulisha. Hatimaye tulipata uhitaji. Mume wangu alihisi ni jukumu lake, kabla ya kuwa tegemezi, kuuza kwanza kile tunachoweza kukiachilia. Alikuwa na vitu vichache ofisini vyenye thamani ndogo, vilivyotawanyika miongoni mwa huko Battle Creek, ambavyo alivikusanya na kuviuza. Tulitoa fanicha ya karibu dola mia moja na hamsini. Mume wangu alijaribu kuuza sofa letu kwa ajili ya nyumba ya mikutano, akiahidi kutoa dola kumi katika mauzo hayo, lakini haikuwezekana. Wakati huu ng'ombe wetu wa pekee na wa thamani sana alikufa. Mume wangu basi kwa mara ya kwanza akawa anahisi kwamba angeweza kupata msaada, na akamwandikia ndugu barua, akisema kwamba ikiwa kanisa lingeona ni vema kufidia hasara ya ng'ombe lingeweza kufanya hivyo. Lakini hakuna kilichofanyika juu yake isipokuwa tu kumshtaki mume wangu kwamba ni mwendawazimu juu ya suala la fedha. Ndugu walimjua vizuri kiasi cha kuelewa kwamba ni mtu ambaye ingekuwa vigumu sana kwake kuomba msaada isipokuwa akiwa katika uhitaji mkali. Na sasa akiwa amelifanya hilo, hakimu wa hisia zake na zangu wakati hakuna hatua iliyochukuliwa juu ya jambo hilo, alilitumia kutuumiza katika uhitaji wetu na shida kubwa. {1T 582.2}

Katika mkutano huu mume wangu alikiri kwa unyenyekevu kwamba alikuwa amekosea katika mambo kadhaa ya aina hii, ambayo hakupaswa kamwe kuyafanya na kamwe asingefanya lakini kwa kuogopa ndugu zake na shauku ya kuwa sahihi na kwa ajili ya umoja na kanisa. Hili liliwapelekea wale ambao walikuwa wakimjeruhi kwa dhahiri kumdharau. Tulishushwa kwenye vumbi na kufadhaika kupita maelezo. Katika hali hii ya mambo tulianza kutekeleza miadi huko Monterey. Katika safari hiyo nilipata uchungu wa roho. Nilijaribu kujieleza kwa nini ndugu zetu hawakuielewa kazi yetu. Nilikuwa na hakika kabisa kwamba wakati tunapopaswa kukutana nao ndipo watajua ni roho gani tuliyokuwa nayo, na kwamba ROHO WA MUNGU ndani yao angeleta mwitikio pia ndani yetu, watumishi wake wanyenyekevu, na hisia na hisia zitaungana. Badala ya hili hatukuaminiwa na tukatazamwa kwa mashaka, ambayo ilikuwa sababu ya kuchanganyikiwa zaidi katika uzoefu wangu. Wakati nikifikiria hivi, sehemu ya maono niliyopewa huko Rochester, Desemba 25, 1865, ilikuja kama umeme katika akili yangu, na mara nikamweleza mume wangu: {1T 583.1}

Nilioneshwa nguzo ya miti iliyosimama pamoja kwa ukaribu, ikitengeneza mduara. Juu ya miti hii kulikuwa na mzabibu ulioifunika kwa juu na kuikalia, na kutengeneza umbo la bustani. Punde niliona miti ikitikiswa huku na huku, ikayumba kana kwamba inasukumwa na upepo mkali. Tawi moja baada ya

jingine la mzabibu lilitikiswa kutoka liliposhikiliwa na vishikizo vyake mpaka shina la mzabibu likatikiswa kutoka kwenye miti isipokuwa vishikizo kadhaa kama mizizi ambayo vilibaki vikishikilia matawi ya chini ya shina, kama inavyokuwa kwa maboga yanapotambaa na kwenye mti fulani yanapotolewa vishikizo vyake (tendrils). Kisha mtu alikuja na kuyakata vishikizo vilivyobaki kuung'ang'ania mzabibu, na hivyo shina lote likaanguka chini ya ardhi na kulala hapo. {1T 583.2}

Dhiki na uchungu wa akili yangu havikuelezeka wakati nilipoona mzabibu umelala chini. Wengi walipita na kuuonea huruma mzabibu, na mimi nikasubiri kwa wasiwasi mkono wa kirafiki uweze kuuinua; lakini hakuna msaada uliotolewa. Nikauliza kwanini hakuna mkono uliouinua mzabibu. Punde niliona malaika akija kwenye mzabibu ulioonekana kuwa umetekezwa. Alinyoosha mikono yake na kuiweka chini ya mzabibu na kuunyanyua ili usimame wima, akisema: "Simama kuelekea mbinguni, na viache vishikizo vyako vimshikilie MUNGU ili usimame wima. Wewe umetikiswa kutoka kwenye sapoti/msaada wa mwanadamu. Wewe unaweza kusimama, kwa nguvu ya MUNGU, na utastawi bila mwanadamu. Mwegemee na kumtegemea MUNGU  peke yake, na tegemeo lako halitakuwa bure, na wala hautatikiswa." Nilihisi ahueni isiyoelezeka, furaha kubwa sana, wakati nilipoona mzabibu uliopuuzwa ukitunzwa. Nilimgeukia yule malaika na kumuuliza mambo haya yanamaanisha nini. Alisema: "Wewe ni mzabibu huu. Yote haya utayapitia, na kisha, wakati mambo haya yatakapotokea, utaelewa kabisa mfano na sura ya mzabibu. MUNGU atakuwa msaada wa karibu wakati wa taabu." Kuanzia wakati huu nilikuwa nimetulia juu ya jukumu langu na sikuwa huru tena kutoa ushuhuda wangu kwa watu. Ikiwa kuna wakati nilihisi mkono wa Bwana ukinishika ili kunyanyuka, ilikuwa kwenye mkutano huo. Mume wangu pia alikuwa huru na wazi katika mahubiri yake, na ushuhuda wa yote ulikuwa: Tumekuwa na mkutano mzuri (Mzabibu unajishikilia kwenye mti au mahali kwa vishikio kama mizizi ya maboga, shina lake halisimami lenyewe). {1T 583.3}

Baada ya kurudi kutoka Monterey, nilihisi ni jukumu langu kuitisha mkutano mwingine, kwani ndugu zangu hawakufanya juhudi yoyote kupunguza hisia zangu. Niliamua kusonga mbele kwa nguvu za MUNGU  na tena nikaelezea hisia zangu na kujiondoa kwenye tuhuma na taarifa zilizosambazwa kutujeruhi. Nilitoa ushuhuda wangu na vitu vinavyohusiana ambavyo vilioneshwa katika historia ya zamani ya baadhi waliopo, nikiwaonya juu ya hatari zao na kukemea mwenendo wao wenye utendaji mbaya. Nilisema kwamba nilikuwa nimewekwa katika nafasi ambazo hazikubaliki. Wakati familia na watu binafsi walipoletwa mbele yangu katika maono, ilikuwa mara kwa mara kwamba kile kilichooneshwa kwangu kuhusiana nao kilikuwa cha asili ya faragha, kukemea dhambi za siri. Nimefanya kazi na wengine kwa miezi kwa sababu ya makosa ambayo wengine hawakujua chochote. Ndugu zangu walipoona watu hawa

wakiwa na huzuni, na kuwasikia wakielezea mashaka yao juu ya kukubaliwa kwao na MUNGU, na pia hisia za kukata tamaa, wametupa lawama hizo kwangu, kana kwamba mimi ndiye wa kulaumiwa kwa wao kupitia majaribu na mitihani hii, au masuala waliyopewa Shuhuda ili wabadilishe maisha yao. Wale ambao walinilaumu hawakujua kabisa kile walichokuwa wakisema. Nilipinga hali ya watu kuketi kama wachunguzi katika hatua yangu. Imekuwa kazi isiyonipa furaha kabisa kuzungumza na watu binafsi na kukemea kuhusu dhambi zao binafsi. Ikiwa kwa ajili ya kuzuia tuhuma na wivu wa waumini, ningetoa ufafanuzi kamili wa mwenendo wangu, yaani kile ilichonipasa kufanya na kuweka hadharani kile kinachopaswa kuwekwa faragha, ningemtenda dhambi MUNGU na kuwakosea watu binafsi. Lazima maonyo ya faragha ya makosa niyahifadhi, niyafunge katika kifua changu. Hebu wengine wahukumu kwa kadri wanavyoweza, sitaisaliti imani iliyowekwa ndani yangu na mkosaji mwenye kutubu, au kufunua kwa wengine kile ambacho kinapaswa kuletwa tu mbele ya wale walio na hatia. Niliwaambia wale waliokusanyika kwamba lazima waondoe mikono yao na kuniacha huru kutenda kwa hofu ya MUNGU. Niliondoka kwenye mkutano nikiwa nimepunguziwa mzigo mzito. {1T 584.1}

## SURA YA 103

## WAFANYAKAZI KATIKA OFISI

Hapa nitatoa shuhuda mbili, mojawapo imeandikwa Machi, 1867, wa kwanza nilioelekezwa kwa wote wanaohusika katika kazi ndani ya ofisi ya Review, na mwingine imeelekezwa kwa vijana wanaofanya kazi ofisini. Nasikitika kusema kwamba wale wote walioonywa wamepuuza zaidi au kwa kiasi shuhuda hizi na sasa ni lazima wakiri kwamba walifuata njia kinyume na kile kilichooneshwa na shuhuda. Ya kwanza ni kama ifuatavyo: {1T 585.1}

Nilipokuwa Rochester, New York, Desemba 25, 1865, nilioneshwa mambo kadhaa kuhusu wale wanaojishughulisha na kazi ofisini, pia kuhusu wachungaji/wahudumu ambao MUNGU amewaita kufanya kazi kwa Neno na mafundisho ya imani. Hakuna yeyote kati ya hawa anayepaswa kushiriki katika biashara au uchuuzi wa kuuza, kununua, magendo na kubembeleza bei (traffic= hapa ujasiliamali pia umo katika hili neno, nafikiri mtendakazi anaweza kufanya bishara pale anapomwajiri mtu mwingine amfanyie kama mkewe bila

ya yeye kuweka akili yake hapo). Wameitwa kwa ajili ya kazi takatifu zaidi, iliyoinuliwa, na isingewezekana kwao kuitendea haki kazi na bado waendelee na biashara shuguli zingine za uchuuzi, kulangua nk. Wale wanaohusika ofisini hawapaswi kuwa na maslahi tofauti. Wakati wanapoipa kazi hiyo umakini na uangalizi unaohitajika, wanakuwa wamefanya kila wanachoweza kufanya, na hawapaswi kufanyishwa kazi zaidi. Ikiwa biashara/uchuuzi ambayo haina uhusiano wowote na kazi ya MUNGU itaiteka akili na kuchukua muda, kazi hiyo haitafanywa vizuri kwa ufanisi. Kwa ubora kabisa, wale wanaohusika katika kazi hawana nguvu ya mwili au ya akili inayobakizwa. Wote wamepungukiwa nguvu kwa kiwango kikubwa au kidogo na ni dhaifu. Kazi kama hiyo, kazi takatifu, ile ambayo wameajiriwa kwayo inapaswa kushirikisha nguvu za akili; hawapaswi kufanya kazi bila kufikiri kama mashine tu, bila nia, ari na umahiri alimradi wanafuata ratiba ya siku, bali watakaswe kwa kazi hiyo na wafanye kana kwamba kazi ya Mungu ni sehemu yao, kana kwamba walikuwa wamewekeza kitu kikubwa katika kazi hii kubwa na ya wakfu. Pasipo kuifanya kazi hii kwa mapenzi makubwa, juhudi zao hazitakubaliwa na MUNGU. {1T 585.2}

Shetani ni mjanja sana, ana shughuli nyingi, na anafanya kazi kila wakati. Nguvu yake maalum inaletwa juu ya wale ambao sasa wanahusika katika kazi ya kuhubiri au kuchapisha Ukweli wa sasa. Wote wanaohusiana na kazi hii wanahitaji kuvaa silaha zote, kwani hizo ndizo alama maalum ambazo Shetani anazishambulia. Niliona kuwa kuna hatari ya kutolindwa, kukosa ulinzi ili Shetani apate mlango na aziondoe akili kutoka kwenye kazi kubwa. Wale wenye nafasi za uwajibikaji ofisini wako katika hatari ya kuwa juu ya kazi na kupoteza unyenyekevu wa akili na usahili ambao hadi sasa umeibainisha kazi hiyo. {1T 586.1}

Shetani alikuwa na lengo maalum katika kumpiga yule aliye mkuu wa kazi ambaye alikuwa na uzoefu kamili katika kuuinua na kuuendeleza Ukweli wa sasa. Alikusudia kumtoa kwenye njia, ili yeye mwenyewe aingie na kuathiri akili ambazo hazikuwa na uzoefu wala hazijajitoa kikamilifu katika kazi hiyo. MUNGU alikusudia kumrudishia afya mume wangu baada ya wengine kuitambua mizigo aliyokuwa nayo na kuhisi uchovu katika kuibeba mizigo hii. Wakati huo huo hawataweka roho yao yote, nguvu zao zote za akili na mwili, kazini na kufanya kile James White alichothubutu kufanya. Halitakuwa jukumu lao kufanya kama yeye alivyofanya, kwa sababu wasingeweza kusimama kwenye wadhifa wao ikiwa wangepitia sehemu ya moja ya ishirini (1/20) ya yale ambayo ameyavumilia. {1T 586.2}

Shetani amekusudia kupata nafasi katika ofisi hiyo, na kama hakuna juhudi ya umoja na macho yenye uangalifu kamili, atatimiza malengo yake. Wengine watakuwa juu ya unyenyekevu wa kazi na watahisi kuwa wanatosha wakati nguvu zao ni udhaifu kabisa. MUNGU atatukuzwa katika kazi hii kubwa. Na endapo hawatauthamini unyenyekevu wa kina na wa kudumu na imani thabiti kwa MUNGU, watajiamini wenyewe, wataendekeza kujitosheleza, na mmoja au

zaidi watakunywa kikombe cha uchungu cha mateso. Kadri kazi inavyozidi kuongezeka, kuna umuhimu zaidi wa kumtumaini MUNGU kikamilifu na kumtegemea Yeye na kupendezwa kwa hamu kubwa kabisa na kujitoa kwa kazi hiyo. Masilahi ya ubinafsi yanapaswa kuwekwa kando. Lazima kuwe na maombi mengi, tafakari nyingi, kwani hii ni muhimu sana kwa mafanikio na ustawi wa kazi. Roho ya biashara haipaswi kuruhusiwa kwa mtu yeyote ambaye ameunganishwa na ofisi. Endapo itaruhusiwa, kazi itapuuzwa na kuharibiwa. Vitu vya kawaida vitapewa umuhimu mkubwa kuliko vitu vitakatifu. {1T 587.1}

Kuna hatari kubwa kwamba baadhi wanaohusika katika kazi watafanya kazi kwa ajili ya mshahara tu (watakuwa watumishi wa mshahara tu). Hawaoneshi shauku au mapenzi kwa kazi hiyo, moyo wao hauko ndani yake, na hawana hisia maalum ya tabia yake takatifu, iliyoinuliwa. Pia kuna hatari maalum kwamba wale wasimamizi wa kazi watainuliwa, na kutukuzwa (kuota pembe), na hivyo kazi ya MUNGU itaharibiwa, kwa kubeba maoni ya mwanadamu badala ya MUNGU. Shetani yuko macho sana na ni king'ang'anizi, lakini Yesu anaishi, na wote wanaomfanya Yeye kuwa haki yao, na ulinzi wao, watadumishwa kwa njia ya pekee. {1T 587.2}

Nilioneshwa kwamba ndugu A, B, na C walikuwa katika hatari ya kuumiza afya zao kwa kutumia sehemu kubwa ya wakati wao katika vyumba vyenye joto ambavyo havina hewa ya kutosha inayombea. Ndugu hawa wanahitaji mazoezi zaidi ya mwili. Kazi yao ni ya kukaa tu kwenye kiti, na wakati mwingi hewa wanayopumua ina joto, ni hewa chafu. Ukosefu wao wa mazoezi husababisha mzunguko kuwa dhaifu, na wako katika hatari ya kuumiza afya yao katika maisha yote, kwa kupuuza kutii sheria zao. Ikiwa watavunja sheria hizi, katika kipindi fulani cha siku zijazo, watapata penalti/adhabu kwa namna fulani kama vile mume wangu alivyoteseka. Hawatadumishwa kuliko yeye. Hakuna hata mmoja wao anayeweza kuvumilia hata sehemu ndogo ya uchovu wa mwili na akili ambao yeye aliuvumilia. {1T 588.1}

Ndugu hawa huchukua kazi na vita kubwa zilizopiganwa, majaribu mabaya zaidi waliyopitia, ili kuanzisha kazi ya Mungu katika hali yake ya sasa. Na bado kazi kubwa na nzito na ya wakfu zaidi iko mbele yetu, na inahitaji kujitoa wakfu kwao na pia kutoka kwa ndugu D, ambaye yuko katika hatari ya kujiinua. MUNGU atamthibitisha na kumjaribu, na lazima ajivike Ukweli na kuvaa silaha za haki, la sivyo ataangukia katika mkono wa adui. Ndugu hawa wote wanahitaji kufuata kwa ukali na kwa uvumilivu katika lishe yenye afya, ya ziada, kwa maana wote wako katika hatari ya akili zilizosongamana, na kupooza/kiharusi kunaweza kumuangukia mmoja au zaidi au wote, ikiwa wataendelea kuishi ovyo bila kujali (James White alipata shida hii kabla ya wengine). {1T 588.2}

Niliona kwamba kipekee kabisa MUNGU alikuwa amemchagua ndugu B ili ashiriki katika kazi kubwa na iliyotukuka. Angekuwa na masumbufu na mizigo,

lakini yote haya yangeweza kubebwa kwa urahisi zaidi na kujitoa wakfu kwa kweli na kutakaswa kwa ajili ya kazi. Ndugu B, unahitaji nguvu ya kina kutoka kwenye chemchemi ya wokovu, nguvu kamili kutoka kwenye chemchemi ya utakaso. Mapenzi yako bado hayajasalimishwa kikamilifu kwenye mapenzi ya MUNGU. Unaendelea kwa sababu unafikiri huwezi kufanya vinginevyo; lakini kutembea katika nuru ya furaha kwa sababu unaweza kuona kwamba Kristo Yesu anaongoza mbele yako, hilo umeshindwa kulifanya. Kusimama mahali pa uwajibikaji unaoushikilia, katika yote haya umeiumiza roho yako mwenyewe na kuwashawishi wengine. Kama ukitembea kinyume na MUNGU, basi Naye atatembea kinyume na wewe. MUNGU anataka kukutumia, lakini lazima uifie nafsi na ukiondoe kiburi chako-toa kafara kiburi chako. Bwana amekusudia kukutumia katika kazi Yake ikiwa utazifuata fadhila Zake kwa moyo wote na kujitakasa kikamilifu na kujiosha uchafu wote wa mwili na roho, ukiukamilisha utakatifu katika kumcha MUNGU. {1T 588.3}

Ufuatao ni Shuhuda namba mbili, ulioandikwa mnamo Mei, 1867, na kuelekezwa kwa vijana ambao walikuwa wakifanya kazi ofisini: {1T 589.1}

Wapendwa marafiki vijana ambao mmeajiriwa na kuunganishwa katika ofisi ya uchapishaji huko Battle Creek: Mzigo unaohusiana na ninyi uko juu yangu. Nimeoneshwa mara kwa mara kwamba wale wote ambao wameunganishwa na kazi ya MUNGU katika kuchapisha Ukweli wa sasa ambao wanatawanywa kila sehemu ya shamba wanapaswa kuwa Wakristo, siyo tu kwa jina, bali kwa matendo na kwa Kweli. Lengo lao halipaswi kuwa tu kufanya kazi kwa ajili ya mshahara, bali wote wanaohusika katika kazi hii kubwa na takatifu na ya heshima wanapaswa kuhisi kuwa shauku na nia yao iko katika kazi hiyo, na kwamba ni sehemu yao. Nia na ushawishi wao katika kujiunganisha wenyewe na kazi hii kubwa na adhimu lazima wawe tayari kustahimili majaribu na hukumu. Hakuna anayepaswa kuruhusiwa kuunganishwa na ofisi ya uchapishaji wakati anadhihirisha ubinafsi na kiburi. {1T 589.2}

Nilioneshwa kuchukulia mambo kwa wepesi, upuuzi na upumbavu, utani, futuhi/vichekesho na kuchekacheka, havipaswi kuendekezwa na wafanyakazi ofisini. Wale wanaohusika katika kazi nzito na takatifu ya kuandaa Ukweli kwenda kila sehemu ya shamba la Bwana wanapaswa kutambua kwamba mwenendo tabia zao zina ushawishi wake. Ikiwa hawajali, wakaendelea kutaniana, kuchekacheka, na kufanya mizaha wakati wanasoma na kuandaa machapisho ya Ukweli adhimu wa wakati huu, watakuwa wanaonesha kwamba mioyo yao haiko katika kazi na haijatakaswa kupitia Ukweli. Hawayatambui mambo matakatifu, bali wanauchukulia Ukweli ambao unaijaribu tabia, Ukweli wenye asili ya mbinguni, kama hadithi ya kawaida, hekaya na visa vya kubuni, vinavyokuja akilini na kufutwa kwa urahisi. {1T 589.3}

Nilipokuwa Rochester niliona kwamba tulikuwa na kila kitu cha kuhofia kuhusiana na ofisi kutoka kwenye mtazamo wa afya; kwamba hakuna hata

mmoja iliyeunganishwa nayo ambayo ilitambua umuhimu wa uvutaji kamili wa hewa, matundu ya hewa ya kufanya hewa itembee (ventilation). Vyumba vyao vilikuwa vilipanda joto la kupita kiasi, na anga lilikuwa na sumu kutokana na uchafuzi unaotokana na utoaji wa hewa kutoka kwenye mapafu watu, na sababu zingine. Haiwezekani kwa akili zao kuwa katika hali ya afya, na kuweza kuvutiwa kwa kuguswa moyo na Ukweli safi na mtakatifu ambao wana mengi ya kuufanyia, isipokuwa kama wataweka thamani inayofaa juu ya hewa safi, yenye nguvu ya mbinguni. (*Ventilation-Uingizaji hewa, inahusu kubadilishana hewa ya ndani ya nyumba na ya nanje. Bila uingizaji hewa ufaao, nyumba isiyopitisha hewa italeta uchafuzi hatari wa hewa, kama vile kaboni monoxide, na unyevu unaoweza kuharibu nyumba. Uingizaji hewa ufaao husaidia kuvifanya nyumba kuwa na nishati inafaa, na kufanya nyumba iwe salama na yenye afya, daima fungua madirisha, hata iwe sentimeta mbili tu wakati wa baridi ya theluji*). {1T 590.1}

Nilioneshwa kuwa ikiwa wale ambao wameunganishwa kwa ukaribu sana na Ukweli uliofunuliwa hawatatoa ushahidi wowote maishani mwao kwamba wamefanywa bora na Ukweli ambao umewekwa mbele yao kila wakati, ikiwa maisha yao hayashuhudii Ukweli kwamba wanaupenda Ukweli na mahitaji yake matakatifu zaidi na zaidi kwa bidii, wanazidi kuwa wagumu, na kuathiriwa kidogo na Ukweli na kazi ya MUNGU, mpaka watakapojikuta wamefisika kabisa na hisia za mguso wa ROHO WA MUNGU, wamekufa kutoka katika mivuto ya Ukweli wa mbinguni. Vitu vya umilele hawatavitambua, bali vitawekwa kwenye viwango/vitu cha chini pamoja na vitu vya kawaida. Hii niliona ilikuwa kesi na baadhi ambao waliounganishwa na ofisi na wote wamekuwa wakilipuuzia suala hili kwa kiwango kikubwa au kidogo. {1T 590.2}

Niliona kwamba kazi ya Ukweli wa sasa inapaswa kuhusisha masilahi ya wote. Uchapishaji wa Ukweli ni mpango uliowekwa na MUNGU kama njia ya kuonya, kufariji, kukaripia, kuhimiza, kuhamasisha, kutia moyo au kusadikisha wote ambao wajumbe wa kimya wasio na sauti wanaweza kuwafikia. Malaika wa MUNGU wana sehemu ya kufanya katika kuandaa mioyo kwa ajili ya kutakaswa na Ukweli uliochapishwa, ili waweze kujitayarisha kwa matukio mazito yaliyo mbele yao. Katika ofisi hiyo hakuna anayejitosheleza kwa kazi muhimu ya kusimamia kwa busara mambo yanayohusiana na uchapishaji wa Ukweli. Malaika lazima wawe karibu nao kuwaongoza, kuwashauri, na kuwazuia, vinginevyo hekima na upumbavu wa mawakala wa kibinadamu vitaonekana. {1T 590.3}

Niliona kwamba malaika walikuwa ofisini mara kwa mara, kwenye chumba cha kuandaa machapisho kwa kuzikunja karatasi, na kwenye chumba ambacho mashine hiyo imewekwa. Nilifanywa kusikia vicheko, mzaha, uvivu, na mazungumzo ya ujinga, na yasiyo na maana. Tena, niliona ubatili, kiburi na ubinafsi vikioneshwa. Malaika walionekana kuangalia kwae huzuni na wakageuka wakiwa na masikitiko. Maneno niliyoyasikia ambayo yalionesha ubatili, kiburi, na ubinafsi, yalinisababisha kuugua kwa uchungu wa roho wakati malaika walipoondoka kwenye chumba kile wakiwa wamechukizwa. Malaika

alisema: "Wajumbe wa mbinguni walikuja kubariki, ili Ukweli uliobebwa na wahubiri wasio na sauti uwe na nguvu inayotakasa, na takatifu kwa ajili ya kushugulikia huu utume; lakini wale wanaohusika katika kazi hii walikuwa mbali sana na MUNGU, walikuwa na machache sana ya Kiungu/mbingu, na walikuwa wamejiunganisha sana na roho ya ulimwengu, kiasi kwamba nguvu za giza ziliwadhibiti, na wasingeweza kuambukizwa na hisia za Mwenyezi Mungu." Wakati huo huo vijana hawa walidanganywa na walidhani kuwa ni matajiri na wameongezeka katika mali na hawahitaji chochote, lakini hawakujua kuwa walikuwa maskini na duni, vipofu na uchi. Wale waliokuwa wanaoshughulikia Ukweli wa thamani kama unavyopaswa hawajui ni mara ngapi kutokujali kwao kwa vitu vya umilele, ubatili wao, kujipenda wenyewe, na kiburi, kucheka kwao na kuzungumza ujinga, kumewafukuza wajumbe wa mbinguni mbali na ofisi. {1T 591.1}

Katika tabia, maneno, na vitendo wote katika ofisi hiyo wanapaswa watu wa kujizuia, wenye staha, waungwana, wanyenyekevu, na wasiojifikiria wenyewe, kama alivyo Mfano wao, Yesu Mwokozi Mpendwa. Wanapaswa kumtafuta MUNGU na kuhesabiwa haki. Ofisi siyo mahali kwa ajili ya michezo, ziara, wavivu, watu wasio na kitu cha kufanya, vicheko au maneno yasiyofaa. Wote wanapaswa kuhisi kuwa wanamfanyia kazi Mwalimu wao. Kweli hizi wanazozisoma, ambazo wanatenda sehemu katika kuziandaa kuzituma kwa watu, ni mialiko ya rehema, ni makaripio, vitisho, maonyo, au kutia moyo. Hawa wanafanya kazi yao kama harufu ya uzima iletayo uzima, au ya mauti iletayo mauti. Endapo zitakataliwa, hukumu lazima iamue jambo hilo. Maombi ya wote ofisini yanapaswa kuwa: "Ee MUNGU, fanya Kweli hizi, ambazo ni za muhimu sana, ziwe wazi katika fahamu za watu masikini na wanyenyekevu zaidi! Hebu malaika na waandamane na wahubiri hawa wakimya na wabariki ushawishi wao, ili roho ziweze kuokolewa kwa njia hii ya unyenyekevu! " {1T 591.2}

Moyo unapaswa kutoa maombi ya bidii wakati mikono inafanya kazi nyingi (busy), na Shetani hataweza kupata njia, na roho badala ya kuinuliwa katika ubatili, itaburudishwa kila wakati, itakuwa kama bustani iliyomwagiliwa maji. Malaika watafurahi kuwa karibu na watendakazi kama hao, kwani uwepo wao utawatia moyo kila wakati. Nguvu itazijilia Kweli zilizochapishwa. Mionzi ya Bwana ya nuru kutoka Patakatifu pa mbinguni itazijilia Kweli za thamani zilizotumwa, ili wale wanaozisoma waburudishwe na kuimarishwa, na roho ambazo zinapinga Ukweli zitasadikishwa na kulazimishwa kusema: Mambo haya ni Kweli kabisa; hayawezi kupingwa. {1T 592.1}

Wote wanapaswa kuhisi kwamba ofisi ni mahali patakatifu, kama nyumba ya MUNGU ilivyo takatifu. Lakini MUNGU amedharauliwa kwa upuuzi, kuchukulia mambo kwa wepesi na uzembe unaoendekezwa na baadhi wanaohusiana na kazi hiyo. Niliona kwamba wageni kutoka ng'ambo-nchi za nje mara nyingi walitoka ofisini wakiwa wamevunjika moyo. Walikuwa wameihusisha na kila

kitu kitakatifu; lakini walipoona vijana, au wengine wameunganishwa na ofisi, wakiwa na mvuto mdogo, wazembe kwa maneno na matendo, wakijizungumzia chochote bila ya kujali, hiyo iliwafanya wawe na mashaka ikiwa, baada ya yote hayo hii ni kazi ya MUNGU. Je, kweli hiyo ni kazi ya kuandaa watu kwa ajili ya kubadilishwa kwenda mbinguni. {1T 592.2}

MUNGU ayabariki haya kwa wote wanaohusika. {1T 592.3}

## SURA YA 104

## MIGOGORO NA USHINDI

Uzoefu kutoka Aprili 26, 1867 hadi Oktoba 20, 1867

Tulirudi kaskazini, na njiani tulifanya mkutano mzuri huko West Windsor, na baada ya kufika nyumbani tulifanya mikutano huko Fairplains na Orleans, na pia tukazingatia suala la kujenga, tukapanda bustani yetu, na kuweka zabibu, na jamii ya matunda damu (blackberries, strawberries, raspberries, ambayo yanapatikana kwenye misitu mingi, na yana miiba, ni jamii ya ua la waridi). Halafu tukishirikiana na uwakilishi mzuri wa wajumbe, tulirudi kwenye Jimbo kuu huko Battle Creek. {1T 592.4}

Sabato ya kwanza tukiwa njiani tuliitumia huko Orleans na tukawa na mfungo. Ilikuwa siku adhimu na bora sana kwetu; tulijaribu kujinyenyekesha mbele za MUNGU, kwa roho iliyopondeka na kilio kingi sote tuliomba kwa bidii kwamba MUNGU atubariki na kututia nguvu kufanya mapenzi Yake katika Konferensi. Tulikuwa na imani na matumaini kwamba mateka yetu yangegeuzwa kwenye mkutano huo. {1T 593.1}

Tulipokuja Battle Creek tuligundua kuwa juhudi zetu za awali hazijatimiza kile tulichotarajia. Taarifa za uongo na wivu bado vilikuwepo. Nafsi yangu ilijawa na maumivu makali, na nililia kwa sauti kwa masaa kadhaa, nikashindwa kuzuia huzuni yangu. Katika mazungumzo, rafiki yangu ambaye nilikuwa nimefahamiana naye kwa miaka ishirini na mbili alinishirikisha taarifa ambazo alizisikia, kwamba tulikuwa wabadhirifu katika matumizi ya fedha. Nikauliza ni kwa namna gani tulikuwa wabadhirifu. Alitaja ununuzi wa kiti cha bei ghali. Kisha nikaelezea mazingira yaliyotupelekea kufanya hivyo. Mume wangu alikuwa amekonda sana, na ilikuwa inamchosha na kumuumiza kukaa kwa muda mrefu kwenye kiti cha kawaida, na kwa sababu hii alikuwa akilala kitandani au

kupumzika muda mwingi. Nilijua kuwa hii haikuwa njia ya yeye kupata nguvu na nikamsihi aketi zaidi, lakini kiti kilimletea pingamizi. {1T 593.2}

Nikiwa njiani kuelekea mashariki kwenda kumhudumia baba yangu aliyekuwa anakaribia kufa, nilimwacha mume wangu huko Brookfield, New York, na nilipokuwa Utica nilitafuta kiti cha sofa chenye springi, kinachoenda juu na chini. Wenye duka hawakuwa na kiti cha bei ambayo mimi nilikuta tayari kununua. Ambayo ni $15, ila walikuwa na ofa nzuri zaidi ya kiti chenye matairi yanayozunguka na kinachonesanesa (rollers and rockers) kwa bei ya $17 badala ya $30. Nilijua kuwa hiki kilikuwa kiti kizuri kwa kila Nyanja-afya, bei, mjongeo nk. Lakini kaka ambaye tulifuatana naye pamoja alinihimiza nisubiri kitengenezwe kiti ambacho gharama ingepungua kwa dola tatu. Kiti kilichogharimu dola kumi na saba, chenyewe kilikuwa na thamani nzuri na halisi kabisa; basi nikakubaliana na uamuzi wake, nikasubiri kuona kiti cha bei rahisi kikiwa kimewekwa pamoja, nikakilipia, na kumpelekea mume wangu. Taarifa kuhusiana na ubadhirifu wetu katika kununua kiti hiki nilikutana nayo huko Wisconsin na Iowa. Lakini ni nani anayeweza kunihukumu? Kama ningekuwa na nafasi ya kurudi nyuma na kufanya tena ununuzi huo, basi, ningefanya kama nilivyofanya tu: isipokuwa ningetegemea uamuzi wangu mwenyewe, na kununua kiti kinachogharimu dola chache zaidi, lakini chenye thamani maradufu ya kile nilichopata. Shetani wakati mwingine hushawishi akili hata kuharibu hisia zote za rehema au huruma. Chuma huonekana kuingia moyoni, kisha ubinadamu na Uungu, vyote hupotea. {1T 593.3}

Taarifa pia zilinifikia kwamba dada alikuwa amesema huko Memphis na Lapeer kwamba kanisa la Battle Creek halikuwa na imani hata kidogo katika Shuhuda ya dada White. Swali liliulizwa ikiwa taarifa hii inahusu Shuhuda iliyoandikwa. Jibu lilikuwa, Hapana, sio kwa maono yake yaliyochapishwa, bali kwa Shuhuda inayotolewa katika mkutano wa kanisa, kwa sababu maisha yake yanapingana nao. Niliomba tena mahojiano na ndugu na dada wachache waliochaguliwa, wenye uzoefu, pamoja na watu ambao walikuwa wameeneza vitu hivi. Mimi niliwaomba kwamba sasa wanioneshe sehemu gani katika maisha yangu ambayo haikuendana na mafundisho yangu. Ikiwa maisha yangu yangekuwa hayaendani na kauli zangu kiasi kwamba kanisa huko Battle Creek likakosa imani hata kidogo katika ushuhuda wangu, lisingekuwa jambo gumu kuwasilisha uthibitisho wa hatua yangu isiyo ya Kikristo. Watu hawa hawawakuweza kutoa chochote cha kuhalalisha taarifa zilizotolewa, na walikiri kwamba wote walikuwa na makosa katika taarifa zilizosambazwa, na kwamba tuhuma na wivu wao haukuwa na msingi. Niliwasamehe kwa hiari wale ambao walitujeruhi, na kuwaambia kwamba yote ambayo ningeyaomba kwa upande wao ni kupinga ushawishi ambao walikuwa wameufanya dhidi yetu, nami ningeridhika. Waliahidi kufanya hivyo, lakini hawajafanya hivyo. {1T 594.1}

Taarifa nyingine nyingi dhidi yetu, zote zikiwa za uongo kabisa au zilizotiwa chumvi sana, zilizungumzwa kwa uhuru katika familia tofauti wakati wa Mkutano, na wengi walituangalia kwa tuhuma hasa mume wangu, na wakatushuku. Watu wengine wenye ushawishi walidhihirisha tabia ya kutuponda. Tulikuwa wenye uhitaji, na mume wangu alikuwa amejaribu kuuza mali inayohamishika, na alidhaniwa kuwa alikosea kwa hili. Alikuwa ameelezea utayari wake wa kuwafanya ndugu zake walipe fidia ya upotevu wa ng'ombe wetu, na hili lilionekana kama dhambi mbaya. Tukidhani kuwa mali yetu huko Battle Creek ilikuwa ni kama imeuzwa kuuzwa, kisha tulinunua na kuanza kujenga huko Greenville. Lakini hatukuweza kuuza mali ya Battle Creek, na katika hali yetu duni mume wangu aliwaandikia ndugu tofauti kukopa pesa. Walilitumia hili kumhukumu na kumshtaki kwa dhambi ya tamaa ya pesa na ubahili. Mchungaji aliyekuwa na bidii katika kazi hii alisikika akisema: "Hatumtaki ndugu E anunue eneo la ndugu White, kwa sababu tunaitaka pesa yake kwa ajili ya taasisi ya afya."  Je, sisi ungefanya nini? Hakuna njia ambayo tungeweza kugeuka bila kulaumiwa. {1T 595.1}

Masaa sitini na tano tu kabla ya mume wangu kudondoshwa chini na kiharusi, alisimama mpaka usiku wa manane katika nyumba ya ibada akiomba dola mia tatu ili kukamilisha kulipia hiyo nyumba; na alipotumia nguvu sana aliweza kutoa dola dola kumi ya kwake na yangu kununua hilo jarida. Kabla ya usiku wa manane kiasi hcho kilikuwa kimefanyiwa changizo. Mzee wa kanisa hilo alikuwa rafiki wa zamani, na katika hali yetu ya uhitaji wa kupindukia na hali ya kutokuwa na marafiki mume wangu alimwandikia, akisema kwamba tulikuwa katika uhitaji, na ikiwa kanisa hilo sasa lingeweza kurudisha zile dola ishirini, sisi tungezipokea. Wakati wa Mkutano ndugu huyu alituita na kulifanya jambo hilo kuwa baya sana. Lakini kabla ya kuja nyumbani kwetu alikuwa amechukua hisa za mali angalau katika malimbikizo ya jumla. Tulihisi vitu hivi kwa uzito zaidi, na kama tusingekuwa tumetiwa nguvu na Bwana tusingeweza kutoa ushuhuda wetu kwenye Mkutano kwa kiwango chochote cha uhuru. {1T 595.2}

Kabla hatujarudi kutoka kwenye Konferensi/Mkutano, Ndugu Andrews, Pierce, na Bourdeau walikuwa na kipindi maalum cha maombi nyumbani kwetu, ambapo sote tulibarikiwa sana, hasa mume wangu. Hii ilimpa ujasiri kurudi kwenye nyumba yetu mpya. Na kisha akaanza kupata mateso yake makali katika meno yake, pia kazi zetu zilitaarifiwa katika gazeti la *Review*. Aliacha kuhubiri kwa wiki moja kutokana na hali yake ya kutoa jino, lakini alifanya kazi huko Orange na Wright, na kanisa la nyumbani, huko Greenbush na Bushnell, akihubiri na kubatiza kama hapo awali. {1T 596.1}

Baada ya kurudi kutoka kwenye Mkutano huo, hali ya mfadhaiko mkubwa ilinijia kuhusiana na ustawi wa kazi ya MUNGU. Mashaka yaliyokuwepo akilini mwangu hayakuwahi kuwepo katika miezi sita iliyopita. Niliwaona watu wa MUNGU

wakishiriki roho ya ulimwengu, na kuiga mitindo yake, na kuachana na usahili na unyenyekevu wa imani yetu. Ilionekana kuwa kanisa huko Battle Creek lilikuwa limerudi nyuma kutoka kwa MUNGU, na haikuwezekana kuamsha hisia zao. Ushuhuda niliopewa na MUNGU ulikuwa na ushawishi mdogo na haukuzingatiwa katika Battle Creek kuliko katika eneo lolote la kazi. Nilitetemeka kwa kazi ya MUNGU. Nilijua kwamba Bwana hakuwaacha watu Wake, bali dhambi zao na uovu wao ndio ulikuwa umewatenganisha na MUNGU. Huko Battle Creek ndiko kwenye moyo mkubwa wa kazi. Kila mpigo wa moyo utokao hapa huhisiwa na viungo vya mwili kote katika uwanja wa kazi. Ikiwa moyo huu una afya, mzunguko muhimu utahisiwa kupitia mwili wa watunza Sabato. Ikiwa moyo unaugua, hali ya uchovu na ya kuangamia ya kila tawi la kazi itathibitisha Ukweli huo. {1T 596.2}

Shauku na nia yangu imefumwa katika kazi hii; maisha yangu yamefungamana nayo. Sayuni inapofanikiwa, ninafurahi; ikisumbuka, Napata huzuni, nakata tamaa, navunjika moyo. Niliona kwamba watu wa MUNGU walikuwa katika hali ya kutisha, ya taharuki na upendeleo Wake Bwana ulikuwa ukiondolewa kutoka kwao. Nilitafakari juu ya picha hii ya kusikitisha mchana na usiku, na nikaomba kwa uchungu: "Ee Bwana, usiutoe urithi Wako upate aibu. Wacha mataifa wasiseme, MUNGU wao Yuko wapi?" Nilihisi kwamba nilikuwa nimeachiliwa kutoka kwa kila mtu aliyeongoza kazi na nilikuwa nimesimama peke yangu. Sikuthubutu kumuamini yeyote. Usiku nilimwamsha mume wangu, nikisema: "Ninaogopa kuwa naweza kuwa kafiri." Kisha ningemlilia Bwana aniokoe kwa mkono Wake wenye nguvu. Sikuweza kuona kwamba shuhuda zangu zilizingatiwa, na nilikaribisha wazo kwamba labda kazi yangu katika kusudi la MUNGU ilifanywa. Tulikuwa na miadi huko Bushnell, lakini nilimwambia mume wangu kuwa siwezi kwenda. Punde alirudi kutoka katika ofisi ya posta na barua kutoka kwa ndugu Matteson, iliyokuwa na ndoto ifuatayo: {1T 596.3}

"Ndugu white mpendwa: baraka za MUNGU ziwe nawe, na maandishi haya yanakukuta ukiwa bado umestawi na kuendelea katika afya na nguvu za kiroho. Najisikia kumshukuru sana bwana kwa wema Wake kwako, na kuamini upate kufurahia afya kamili na uhuru katika utangazaji wa ujumbe wa mwisho. {1T 597.1}

"Nimekuwa na ndoto ya ajabu kuhusu wewe na dada white, na ninaona kuwa ni jukumu langu kukuelezea na wewe yote ninayoweza kukumbuka. Niliota kwamba nilimuelezea dada white, pamoja na tafsiri yake, ambayo pia nilipewa katika ndoto. Nilipoamka, kuna kitu kilikuwa kinanihimiza kuinuka na kuandika maelezo yote, ili nisije kuyasahau; lakini nilipuuzia kufanya hivyo, kwa maana nilichoka, na pia niliwaza kuwa hakuna lolote bali ni ndoto tu. Lakini kuona kwamba sikuwahi kukuota hapo kabla, na kwamba ndoto hii ilikuwa ya akili

mahiri, na ilihusiana na wewe zaidi, nimefikia hitimisho nililotakiwa kukuambia. Haya ndiyo ninayoweza kukumbuka: {1T 597.2}

"Nilikuwa kwenye nyumba kubwa ambapo kulikuwa na mimbari kubwa kama zile tunazotumia katika nyumba zetu za mikutano. Juu yake kulikuwa na taa nyingi zilizokuwa zikiwaka. Taa hizi zilihitaji mafuta wakati wote, na wengi wetu tulikuwa tunahusika kuyajaza. Ndugu white na mwenzi wake walihusika zaidi katika kazi hii, na nilitambua kuwa dada white aliweka mafuta mengi zaidi kuliko wengine wote. Kisha ndugu white alienda kwenye mlango uliofunguliwa kwenye bohari, ambapo kulikuwa na mapipa ya mafuta. Alifungua mlango na kuingia, na dada White alimfuata. Kisha kundi la watu lilikuja pamoja, likiwa na vitu vingi vyeusi vilivyoonekana kama masizi, na kuviweka vyote juu ya ndugu na dada white, hata wakafunikwa navyo kabisa. Nilisikitika sana, na kuangalia kwa hofu kuona mwisho wa mambo haya. Niliweza kuwaona ndugu na dada white wote wakifanya kazi ngumu kujitoa kwenye hilo lundo la masizi, na baada ya mapambano ya muda mrefu walitoka wakiwa na mng'aro mkubwa, ndipo watu waovu walipotea na lundo lao la masizi. Kisha kaka na dada White wakajihusisha tena Kwa moyo zaidi katika kuzijaza taa mafuta, lakini dada White bado alikuwa na anaongoza katika kazi hii. {1T 597.3}

"Niliota kuwa ifuatayo ilikuwa tafsiri yake: taa ziliwakilisha watu masalio. Mafuta yalikuwa Ukweli na upendo wa mbinguni, ambao watu wa MUNGU waliuhitaji kila wakati. Watu walioshiriki katika kuzijaza taa mafuta walikuwa watumishi wa MUNGU wanaofanya kazi ya mavuno. Ni akina nani waliokuwa kwenye lile kundi la waovu hilo siwezi kueleza, lakini walikuwa watu walioshawishiwa na Shetani, walioelekeza mvuto wao mbaya hasa kinyume na ndugu na dada white. Watu hawa walikuwa katika huzuni kubwa kwa msimu, lakini baadaye waliokolewa na neema ya MUNGU na jitihada zao za dhati. Kisha hatimaye nguvu ya MUNGU ilikuja juu yao, na wakatenda sehemu kubwa katika utangazaji wa ujumbe wa mwisho wa rehema. Lakini dada white alikuwa na utajiri wa hekima za kimbingu na upendo kuliko wengine wote. {1T 598.1}

"Ndoto hii imeimarisha imani yangu kwamba Bwana atakuongoza wewe kuimaliza kazi ya urejeshaji iliyoanza, na kwamba kwa wingii utafurahia uwepo wa ROHO WA MUNGU tena kama ulivyofanya zamani, ndiyo na zaidi. Hakika kwa wingine, wewe usisahau kuwa unyenyekevu huo ndiyo mlango unaopelekea katika utajiri wa neema ya MUNGU. HEbu Bwana akubariki wewe na mwenzi wako na watoto, na utujalie kukutana katika ufalme wa mbinguni. Wako katika vifungo vya upendo wa kikristo. {1T 598.2}

"JOHN MATTESON.

"OAKLAND, WISCONSIN,

JULAI 15, 1867."

Ndoto hii ilinitia moyo. Nilimwamini ndugu Matteson. Kabla sijamwona kwa macho yangu ya asili, suala lake lilioneshwa katika maono, tofauti na yale ya F wa Wisconsin. Huyu ndugu F hakustahili kubeba jina la Mkristo, acha mbali na kuwa mjumbe; lakini ndugu Matteson alioneshwa kama mtu ambaye alikuwa na unyenyekevu, na ambaye, kama angeendelea na kujitoa kwake, angestahili kuzielekeza roho kwa Mwana-Kondoo wa MUNGU. Ndugu Matteson hakuyajua masumbufu yangu ya akili. Hakuna hata mstari wa maandishi uliowahi kupita kati yetu, na jinsi ndoto hiyo ilivyokuja, kwa wakati muafaka na kupitia kwa mtu huyu, kwangu ilionekana kama mkono wa MUNGU ulinyooshwa kunisaidia. {1T 599.1}

Tulikuwa na majukumu ya ujenzi kwa pesa za kukopa, ambazo zilisababisha kuchanganyikiwa. Tuliendelea na miadi yetu na kufanya kazi ngumu sana katika kipindi chote cha hali ya hewa ya joto. Kwa sababu ya uhitaji wa fedha tulienda shambani pamoja, tukalima, na kukata nyasi. Nilichukua mundu na kukusanya majani, wakati mume wangu kwa mikono yake dhaifu, alinikatia nyasi. Nilichukua brashi na kupaka rangi ndani ya nyumba yetu. Katika mambo haya sisi sote tulichoka sana. Mwishowe nilishindwa ghafla na sikuweza kufanya zaidi. Katika asubuhi kadhaa nilizimia, na mume wangu alilazimika kuhudhuria mkutano wa Greenbush bila mimi. {1T 599.2}

Gari letu la zamani la farasi lilikuwa karibu kutuua sisi na timu yetu. Tulisafiri nalo kwenye safari ndefu nyingi, shughuli za mikutano, huduma za nyumbani na kazini, zilikuwa nyingi sana kwetu, na niliogopa kuwa kazi yangu ilikuwa imemalizika sasa. Mume wangu alijaribu kunitia moyo na kunihimiza kuanza tena kukamilisha miadi yetu huko Orange, Greenbush, na Ithaca. Mwishowe niliamua kuendelea na safari ikiwa haikuwa mbaya sana. Niliendesha maili kumi nikipiga magoti kwenye kiti cha gari na kuinamisha kichwa changu juu ya paja la mume wangu. Aliendesha na kunisaidia. Asubuhi iliyofuata nilikuwa vizuri na niliamua kuendelea. MUNGU alitusaidia kusema kwa nguvu kwa watu huko Orange, na kazi tukufu ilifanywa kwa watu waliorudi nyuma na wenye dhambi. Huko Greenbush nilikuwa nimepewa uhuru na nikapata nguvu. Kule Ithaca Bwana alitusaidia kuzungumza na kusanyiko kubwa ambalo hatukuwahi kukutana nalo hapo awali (Gari la Kwanza liliundwa Ujerumani 1894 likaitwa benzi, maandishi haya yote, gari ni la moshi au farasi). {1T 599.3}

Tukiwa hatupo, Ndugu King, Fargo, na Maynard waliamua kwamba kwa kutuhurumia sisi na timu yetu tunapaswa kuwa na gari nyepesi, yenye faraja, isiyo na usumbufu mwingi; kwa hivyo tuliporudi walimpeleka mume wangu Ionia na kununua lile garotulilo nalo sasa. Hili ndilo tulilolihitaji na lingeniokoa uchovu mwingi wa kusafiri katika joto la kiangazi. {1T 600.1}

Wakati huu tulipokea maombi ya dhati ya kuhudhuria mikutano ya kusanyiko huko Magharibi. Tuliposoma miito hii yenye miguso ,tuliiangalia na kulia kwa uchungu. Mume wangu angeniambia, "Ellen, hatuwezi kuhudhuria mikutano hii. Unajua siwezi kujitunza vizuri katika safari kama hii, na je! Ukizimia, nitafanya nini? Lakini, Ellen, lazima twende;" na alipokuwa akiongea hivyo, hisia zake za machozi ziliyasonga maneno yake. Kwa mwitikio kuhusu haya, mimi nikitafakari juu ya hali yetu dhaifu, na hali ya kazi huko Magharibi, na kuhisi kuwa ndugu wanahitaji utumishi wetu, ningesema: "James, hatuwezi kuhudhuria mikutano hii Magharibi - lakini lazima twende." Kwa wakati huu, ndugu zetu kadhaa waaminifu, walipoona hali yetu, walijitolea kwenda nasi. Hii ilitosha kulikamilisha jambo hilo. Katika gari letu jipya tuliondoka Greenville Agosti 29 kuhudhuria mkutano mkuu wajumla huko Wright. Timu nne zilitufuata nasi. Safari ilikuwa ya raha na ya kupendeza sana kwa kushirikiana na ndugu wenye huruma. Mkutano huo ulikuwa wa ushindi. {1T 600.2}

Septemba 7 na 8 tulifurahia msimu wa thamani huko Monterey na ndugu wa wilaya ya Allegan. Hapa tulikutana na ndugu Loughborough, ambaye alikuwa ameanza kuhisi makosa yaliyopo Battle Creek na alikuwa akiomboleza juu ya sehemu aliyokuwa ametenda kuhusiana na makosa haya, ambayo yalikuwa yameijeruhi kazi na kutuletea mizigo ya kikatili. Kwa ombi letu aliandamana nasi kwenda Battle Creek. Lakini kabla ya kuondoka Monterey, alituelezea ndoto ifuatayo: {1T 600.3}

"Wakati ndugu na dada White walipokuja monterey, septemba 7, waliniomba niandamane nao kwenda battle creek. Nilisitisha kuhusu kwenda, nikifikiri kwamba naweza kuwa bado na jukumu la kusimamia shauku na maslahi ya injili monterey na kufikiri kwamba nilipokuwa nikiwaelezea hayo kulikuwa na upinzani kidogo kwao huko battle creek. Baada ya kuliombea jambo hilo kwa siku kadhaa, niliondoka kwenda kazini jioni moja ili nipumzike, nikiomba kwa shauku Bwana anipatie nuru kuhusiana na jambo hilo. {1T 600.4}

"Niliota kwamba mimi, na wengine wengi, wajumbe wa kanisa la battle creek, tulikuwa kwenye tumepanda magari ya tareni. Magari yalikuwa madogo – nilisimama kwa shida sana nikiwa ndani. Hayakuwa na hewa inayotembea, yakiwa na harufu kana kwamba hayajapata hewa kwa miezi kadhaa. Barabara waliyokuwa wanaipitia ilikuwa mbaya, na magari yalisumbuka kwa kutikisika sana kwa kasi, wakati mwingine yakasababisha mizigo yetu kuanguka, na wakati mwingine kuwatupa nje baadhi ya abiria. Tulilazimika kusimama ili kuwarudisha abiria na mizigo ndani tena, au kulirekebisha gari. Tulionekana kufanya kazi muda mwingi kukarabati mambo na kwenda kidogo au kutoendelea kabisa. Kwa kweli tulikuwa wasafiri wenye kusikitisha sana. {1T 601.1}

"Wote mara moja tulikuja kwenye jukwaa la duara, kubwa vya kutosha kuchukua watu wote. Ndugu na dada white walikuwa wamesimama hapo na nilishuka kutoka kwenye gari la moshi, walisema: gari hil linaenda vibaya. Lazima ligeuzwe mwelekeo.' wote walishikilia ekseli ya gurudumu na kugeuza treni mwelekeo wa lile jukwaa kwa nguvu zao zote. Hakuna wakati ambao watu waliwahi kufanya kazi ngumu ya mikono kama waliyoifanya wakati wa kugeuza mwelekeo. Nilisimama na kutazama mpaka nilipoanza kuona gari likigeuka, nikapaza sauti na kusema, 'linasogea,' nikaweka mikono kuwasaidia. Niliweka umakini kidogo kwenye treni, tulikuwa tumeweka nia na umakini wa kufanya kazi yetu ya kugeuza mwelekeo wa gari letu. {1T 601.2}

"Tulipokuwa tumemaliza kazi hii, tuliangalia juu, na mwelekeo wa treni yote ulikuwa imebadilishwa. Badala ya gari la chini, lisilopitisha hewa ambalo tulikuwa tukiliendesha, mabehewa yalilikuwa kubwa, linalopitisha hewa, lenye madirisha makubwa ya wazi, yote yaliyofungwa na kupangiliwa vizuri, gari la kifahari kuliko gari lolote la ikulu au hoteli nililowahi kuliona. Barabara ya treni ilikuwa na msawaziko, imenyoka, viwango, nyororo, na imara. Gari la moshi lilikuwa likijazwa na abiria wenye sura zilizochangamka zenye furaha, lakini bado zilivaa mwonekano wa uhakikisho na heshima. Wote walionesha hali ya kuridhika sana kwa mabadiliko ambayo yalikuwa yamefanyika, na imani kubwa kabisa na njia ya gari. Kaka na dada white walikuwa kwenye treni wakati huu, sura zao ziliinuliwa na furaha takatifu. Gari lilipokuwa linaanza mwendo, nilikuwa na furaha ndipo nikaamka, na kwa kuwa nilikuwa macho, mvuto akilini mwangu kwamba ndoto hiyo inahusiana na kanisa la battle creek na mambo yaliyounganishwa na kazi mahali hapo. Akili yangu ilikuwa sawa kabisa kuhusiana na jukumu langu la kwenda battle creek na kuweka mkono wangu wa msaada kazini hapo. Ninafurahia sasa kwa kuwa nimekuwa hapa kuona baraka za Bwana zikiandamana na kazi yenye bidii ya kaka na dada white katika kuweka mambo sawa. {1T 601.3}

"JN LOUGHBOROUGH."

Kabla hatujaondoka monterey, ndugu Loughborough alinipa maelezo yafuatayo juu ya ndoto nyingine ambayo alikuwa nayo wakati wa kifo cha mkewe. Hili pia lilikuwa jambo la kunitia moyo. {1T 602.1}

"'Nabii aliye na ndoto, na aseme ndoto yake.' yeremia 23:28. {1t 602.2}

"Jioni moja, baada ya kutafakari taabu za kaka na dada white, uhusiano wao na kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu, na kushindwa kwangu kusimama katika taabu zao; na baada ya kujaribu kukiri makosa yangu kwa Bwana, kuomba baraka juu ya kaka na dada White, nilistaafu ili nipumzike.{1T 602.3}

"Niliwaza ndani ya ndoto yangu kwamba nilikuwa ndani ya mji wangu wa asili, kando ya mlima mrefu. Nilizungumza kwa dhati sana na kusema: 'oh, laiti kama ningeweza kukifikia kijito hicho cha uponyaji!' nilipokuwa nikiwaza hivyo kijana mzuri, aliyevaa kwa unadhifu alikuja karibu nami na kusema kwa furaha sana: 'nitakupeleka kwenye kijito hicho.' Alitangulia njiani, na nilijaribu kuifuata, tulikwenda pamoja kando ya kilima, tukapita kwa shida katika ardhi yenye maji na madimbwi matatu magumu, ambayo kwayo vijito vidogo vya maji ya matope vilitiririka. Hakukuwa na njia ya kupita isipokuwa kwa kukatiza majini. Tukiwa tumelikamilisha hili, tulifika kwenye eneo zuri la ardhi gumu ambalo tulipaswa kupita kando ya mto unaoenda polepole, na chemchemi ya maji safi ilikuwa ikichemka. Tanki kubwa lilikuwa limewekwa pale, lililofanana sana na bomba lililokuwepo katika taasisi ya afya huko battle creek. Bomba hilo lilikuwa linaanzia kutoka katika chemchemi hadi kwenye mwisho mmoja wa tanki, na maji yalikuwa yanatiririkia upande mwingine. Jua lilikuwa linaangaza sana, na maji yaling'aa kwa miale ya jua. {1T 602.4}

"Tulipoikaribia chemchemi, kijana yule hakusema kitu, bali aliniangalia na kutabasamu kwa mwonekano wa kutosheka/kuridhika, kisha akapunga mkono mmoja kuelekea kwenye chemchemi kama anayesema: 'je hufikirii kama hiyo ni chemchemi ya uponyaji wote?' ndipo kundi la watu pamoja na kaka na dada White kama viongozi lilifika pale kwenye chemchemi katika upande mwingine kutoka kwetu. Wote walionekana kuwa na furaha na wenye uchangamfu, ila heshima takatifu ilionekana juu ya nyuso zao. {1T 603.1}

"Kaka White alionekana kupata nafuu katika afya yake, na alikuwa mchangamfu na mwenye furaha, lakini alionekana kuchoka kwa sababu alikuwa ametembea umbali mrefu. Dada white alikuwa na kikombe kikubwa mkononi, ambacho alikitumia kuchota maji ndani ya chemchemi na kuyanywa kisha akawapatia wengine. Niliwaza kuwa kaka White alikuwa akizungumza na watu na kuwaambia: 'sasa mtakuwa na nafasi ya kuona matokeo ya maji haya.' kisha akayanywa, nayo papo hapo yakamhuisha, kama yalivyofanya kwa wengine wote walioyanywa, yakawafanya kuwa na nguvu na uimara katika mwonekano wao. Niliwaza kuwa wakati ndugu White alipokuwa akizungumza na kunywa mkupuo wa maji, aliweka mikono yake upande wa tenki na kujichovya mara tatu. Kila mara alipotoka alikuwa na nguvu kuliko awali, na aliendelea kuzungumza wakati wote na kuwahamashisha engine waje na kuoga 'ndani ya chemchemi,' alipochota na kunywa katika kijito cha uponyaji. Sauti yake, pamoja na ya dada white, inaonekana kuwa kama wimbo mzuri wa ajabu. Nilijisikia roho ya kufurahia kwamba nilikuwa nimepata chemchemi. Dada white alikuja kuelekea kwangu akiwa na kikombe cha maji ili ninywe, lakini nilifurahia sana kwamba nilishtuka usingizini kabla ya kunywa maji. {1T 603.2}

"Bwana anijalie ili nipate kunywa kwa wingi maji hayo, kwa maana naamini kuwa siyo mengine zaidi ya yale ambayo Kristo aliyasema, ambayo yatakuwa chemchemi inayotupeleka mpaka kwenye uzima wa milele. {1T 604.1}

"JN LOUGHBOROUGH.

"MONTEREY, MICHIGAN,
SEPT. 8, 1867." {1T 604.1}

Septemba 14 na 15 tulifanya mikutano yenye kunufaisha huko Battle Creek. Hapa mume wangu akiwa na uhuru alitoa pigo la ujasiri kwa baadhi ya dhambi za wale wanaosimama katika nyadhifa za juu katika kazi hiyo, na kwa mara ya kwanza katika miezi ishirini alihudhuria mikutano ya jioni na kuhubiri kila jioni. Kazi nzuri ilikuwa imeanza, na kanisa, kama lilivyochapishwa katika gazeti la Review, lilitupatia ahadi ya kusimama pamoja nasi, kwamba tunaporudi kutoka Magharibi tungeendelea na kazi zetu pamoja nao. {1T 604.2}

Kwa kushirikiana na kaka na dada Maynard, na ndugu zangu Smith na Olmstead, tulihudhuria mikutano mikubwa ya Magharibi, ushindi mkuu ambao umetolewa kikamilifu katika gazeti la Review. Wakati nikihudhuria mikutano huko Wisconsin, nilikuwa dhaifu sana. Nilikuwa nimefanya kazi kupita uwezo wa nguvu zangu huko Battle Creek hata nikakaribia kuzimia ndani ya mabehewa safarini. Nilikuwa nimeteseka na mapafu yangu kwa muda wa majuma manne, na nilikuwa nikiongea na watu kwa shida sana. Sabato jioni koo langu na mapafu vilivyokuwa vimeathiriwa sana vilifanyiwa tiba rahisi kwa kukandwa kwa maji ya moto na kitambaa ili kupunguza maumivi na kuziba kwa koo (fomentation hydrotherapy); na kofia ya kichwani ilikuwa imesahaulika kuwekwa na hivyo wakati wa baridi ya theluji kichwa kikiwa na majimaji baada ya kuoga na mtu asivae kofia, matatizo ya mapafu yanapelekwa hadi kwenye ubongo, hili ndilo jambo lililonitokea mimi. Nilipoamka asubuhi, nilipata hisia kali kwenye ubongo. Sauti ilionekana kutetema, na kila kitu kilionekana kumbembea mbele yangu. Nilipokuwa nikitembea, nilijikunja na nikakaribia kuanguka sakafuni. Nilichukua kifungua kinywa, nikitumaini kupata nafuu kwa kufanya hivyo; lakini matatizo yalizidi kuongezeka. Niliendelea kuaw mgonjwa sana na sikuweza kukaa. {1T 604.3}

Mume wangu alikuja nyumbani baada ya mkutano wa saa sita mchana, akisema kwamba alikuwa amepewa miadi yangu ya kunena alasiri. Ilionekana kuwa haiwezekani kwangu kusimama mbele ya watu. Wakati mume wangu akiuliza ni mada gani nitakayozungumza, sikuweza kukusanya au kupanga sentensi akilini mwangu. Lakini nilifikiri: Ikiwa MUNGU atataka niongee, hakika ataniimarisha; Nitajitosa kwa imani; kinachoweza kutokea ni kushinda tu, kama ni nitakwenda. Nilijikongoja kwenda hemani na ubongo uliochanganyikiwa kwa

jinsi ajabu, lakini niliwaambia ndugu wanaohubiri walioko kwenye jukwaa kwamba ikiwa wangenitegemeza kwa maombi yao, ningezungumza. Nilisimama mbele ya watu kwa imani, na kwa muda wa dakika tano kichwa na mapafu yangu vilipata nafuu, na bila shida niliongea zaidi ya saa moja kwa wasikilizaji elfu moja na mia tano wenye shauku. Baada ya kumaliza kunena, hali ya wema na rehema ya MUNGU ilinijia, na sikuweza kuvumilia bali kuinuka tena na kusimulia ugonjwa wangu na baraka ya MUNGU ambayo ilinitegemeza wakati nikizungumza. Tangu mkutano huo mapafu yangu yametengamaa sana, na afya yangu imekuwa ikiimarika. {1T 604.4}

Huko Magharibi tulikutana na taarifa ambazo zilihusu kashfa dhidi ya mume wangu. Hizi zilikuwa za wakati wa General Konferensi/Halmashauri kuu, na zilipelekwa maeneo yote ya kazi. Nitasema moja kama mfano. Ilisemekana kwamba mume wangu alikuwa anapenda fedha sana kiasi kwamba alikuwa akihusika katika kuuza chupa za zamani. Ukweli ni huu: Wakati tulipokuwa tunakaribia kuhama, nilimuuliza mume wangu tuzifanyeje hizi chupa nyingi za zamani? Akajibu: "Zitupe mbali." Hapo hapo mtoto Willie wetu aliingia na kujitolea kuzisafisha na kuziuza. Nilimwambia afanye hivyo, na achukue kile ambacho watu watakuwa tayari kutoa. Na wakati mume wangu alipoelekea kwenye ofisi ya posta na gari la farasi, alimchukua Willie na chupa ndani ya gari. Hakuweza kumpuuza mwanaye mdogo mwaminifu. Willie aliziuza zile chupa na kuchukua pesa. Walipokuwa wakienda kwenye ofisi ya posta, mume wangu alimbeba ndani ya gari ndugu aliyeunganishwa naye na ofisi ya *Review*, ambaye aliongea naye kwa furaha wakati wakisafiri kwenda na kurudi mjini, na kwa sababu aliona Willie akija kwenye gari na kumwuliza baba yake swali linalohusiana na thamani ya chupa, na kisha nikamuona muuza madawa/mfamasia akiongea na mume wangu kuhusiana na kile kilichomvutia sana Willie, ndugu huyu, bila hata ya kusema neno moja kwa mume wangu juu ya jambo hilo, mara moja alitaarifu kwamba ndugu White alikuwa mjini akiuza chupa za zamani na kwa hivyo lazima awe mwendawazimu kwa tamaa ya pesa. Mara ya kwanza kusikia kuhusu chupa hizo tulikuwa Iowa, miezi mitano baadaye. {1T 605.1}

Vitu hivi vimehifadhiwa mbali kwetu ili kwamba tusiweze kuvisahihisha, na vimechukuliwa, kama kwenye mabawa ya upepo, na marafiki zetu Wakristo. Na tumeshangaa kuona kutokana na uchunguzi na maungamo ya hivi karibuni kutoka kwa karibu washiriki wote wa kanisa hili, kwamba taarifa moja ya uongo au zaidi zimesifiwa kikamilifu na karibu wote na kwamba wale wanaojiita Wakristo wameendekeza hisia za lawama, uchungu, na ukatili dhidi yetu, hasa dhidi ya mume wangu dhaifu ambaye anapigania maisha kwaajili ya ugonjwa na uhuru. Wengine wamekuwa na roho mbaya, ya kukandamiza na wamemwelezea kama tajiri mwenye tamaa ya pesa. {1T 606.1}

Aliporudi Battle Creek, mume wangu aliita baraza la ndugu likutane na kanisa ili mambo yaweze kuchunguzwa mbele yao na taarifa za uongo zishugulikiwe. Ndugu walikuja kutoka sehemu tofauti za jimbo, na mume wangu bila woga alitoa wito kwa wote waweze kuleta kile wanachoweza dhidi yake ili aweze kukutana nacho kwa uwazi na kwa hivyo kukomesha uchafuzi wa jina la mtu kwa kutunga uongo. Makosa ambayo alikuwa ameyakiri hapo awali katika gazeti la *Review*, sasa aliyakiri kabisa katika mkutano wa hadhara na kwa watu binafsi, na pia akaelezea mambo mengi ambayo yalitegemeza mashtaka ya uongo na ya kipumbavu, na kusadikisha uongo wa mashtaka hayo. {1T 606.2}

Na wakati tunatafuta maswala yanayohusiana na thamani halisi ya mali yetu, tulishangaa, na wale wote waliokuwepo, kwamba ilifikia $1,500 tu, kando ya farasi wake na gari lake, na mabaki ya matoleo ya vitabu na chati, mauzo ambayo kwa mwaka uliopita, kama ilivyoelezwa na katibu, hayakuwa sawa na riba ya pesa anayodaiwa na Chama cha Uchapishaji (*Publishing Association*). Vitabu hivi na chati haviwezi kwa sasa kuzingatiwa kwa thamani kubwa hasa kwetu katika hali yetu ya sasa. {1T 606.3}

Wakati alipokuwa mzima wa afya, mume wangu hakuwa na muda wa kuweka mahesabu ya akaunti yake vyema, na kipindi cha ugonjwa wake mambo yake yalikuwa mikononi mwa wengine. Swali liliibuka: Je! Mali yake imekuwaje? Je, ametapeliwa? Je! Kulikuwa na makosa katika akaunti zake? Au katika hali yake ya mambo isiyo na utulivu, aliachilia hili na lile, bila kujua uwezo wake halisi wa kutoa na bila kujua ni kiasi gani alitoa? {1T 607.1}

Kama moja ya matokeo mazuri ya uchunguzi, imani kwa wale ambao wamekuwa wakiwajibika na akaunti zinazohusiana na mambo yetu haijatikiswa, na hatuna sababu nzuri ya kuhitimisha kwamba uwezo fedha/mali zetu ndogo zinaweza kuhusishwa na makosa kwenye akaunti. Kwa hivyo katika kuangalia masuala ya biashara ya mume wangu kwa miaka kumi, na njia yake ya ukarimu ya kutoa fedha ili kuisaidia kazi katika matawi yake yote, hitimisho bora ni kwamba mali yetu imetumika katika kusudi la Ukweli wa sasa. Mume wangu hakuweka mahesabu yoyote ya akaunti yake, na kile alichokitoa kusaidia kinaweza kupatikana tu kutoka katika kumbukumbu ya kichwani na kutoka katika kile kilichopokelewa kwenye shirika la uchapaji la *Review*. Uhalisia kwamba sisi tuna pesa chache sana, umeonekana wakati huu ambapo mume wangu ameelezewa na kuwakilisha kama mtu tajiri sana na kwamba bado ana tamaa ya kutafuta pesa zaidi, na hili limekuwa jambo la furaha kwetu, kwani ndilo kanusho bora kwa mashtaka ya uongo ambayo yalitishia ushawishi wetu na tabia ya Kikristo. {1T 607.2}

Mali zetu zinaweza kwenda, na bado tutafurahi kwa MUNGU ikiwa zinatumika kwa ajili ya maendeleo ya kazi Yake. Kwa furaha tumezitumia vizuri sana siku

zetu, na nguvu zetu kwa ubora, na tumekaribia kuchoka kwa kazi hiyo hiyo, na kuhisi udhaifu wa umri mapema, ila bado tutafurahi. Lakini wakati wanaodai kuwa ndugu zetu wanaposhambulia tabia na ushawishi wetu kwa kutuwakilisha kama watu matajiri, wenye udunia moyoni, wenye tamaa zaidi zaidi, hapo ndipo tunasisimka kwa umakini. Hebu tufurahie tabia na ushawishi ambao tumeupata katika miaka ishirini iliyopita, na hata umasikini na kushikilia hata kwa udogo afya ambayo inalegalega na maisha haya ya kufa, tutafurahi na kutoa kwa moyo mkunjufu katika kazi kile kidogo tulichobakiwa nacho. {1T 607.3}

Uchunguzi ulikuwa wa kina/kinagaubaga na ulisababisha kutuweka huru kutoka katika mashtaka ambayo tulishtakiwa kwayo, na kurudisha hisia za umoja kamili. Maungamo ya moyo mkunjufu na yanayopasua moyo kwa huzuni juu ya hatua ya kikatili iliyofuatwa kwetu hapa yamefanyika, na baraka ya ishara ya MUNGU imekuja kwetu sote. Watu waliorudi nyuma wamerejeshwa, wenye dhambi wamebadilishwa, na arobaini na wanne wamezikwa katika ubatizo (wamebatizwa), mume wangu akibatiza kumi na sita, na Ndugu Andrews na Loughborough, ishirini na nane. Tunatiwa moyo lakini tumechoka sana. Mume wangu pamoja na mimi tumekuwa na mzigo wa kazi, ambayo imekuwa ngumu sana na ya kusisimua. Jinsi ambavyo, katika hali yetu dhaifu, tumepitia uchunguzi, na hisia za, karibu watu wote kuwa kinyume chetu, tulivumilia kuhubiri, kushauri, na kufanya mikutano ya jioni, na wakati huo huo tukatayarisha kazi hii, mume wangu akifanya kazi pamoja na mimi, kunakili na kuiandaa kwa wachapishaji, na kusoma ili kuhakiki, MUNGU Ndiye pekee ajuaye. Lakini tumepita haya yote na tunatumaini kwa MUNGU kwamba Yeye atatuwezesha katika kazi zetu za baadaye. {1T 608.1}

Sasa tunaamini kwamba mengi katika ndoto zilizotajwa yalitolewa kuonesha majaribu yetu yanayotokana na makosa yaliyopo Battle Creek, kazi zetu katika kujisafisha kutokana na mashtaka ya kikatili, na pia kazi zetu, kwa baraka za MUNGU katika kurekebisha mambo. Ikiwa maoni haya ya ndoto ni sahihi, Je, tusitumainie, kutoka sehemu zingine ambazo bado hazijatimizwa, kwamba maisha yetu ya baadaye yatakuwa mazuri kuliko yale yaliyopita? {1T 608.2}

Kwa kuhitimisha masimulizi haya, ningesema kwamba tunaishi katika wakati makini/adhimu kabisa. Katika maono ya mwisho niliyopewa, nilioneshwa Ukweli wa kushangaza kwamba ni sehemu ndogo tu ya wale ambao sasa wanaukiri Ukweli watakaotakaswa nao na kuokolewa. Wengi watapanda juu ya usahili wa kazi. Watafanana na ulimwengu, wataendekeza sanamu, na kufa kiroho. Wafuasi wa Yesu wanyenyekevu, wanaojikana nafsi watapita kuelekea katika ukamilifu, wakiwaacha nyuma wanadamu wasiojali na wapenzi wa ulimwengu. {1T 608.3}

Nilielekezwa nyuma kwa Israeli ya kale. Ni wawili tu kati ya watu wazima ndani ya jeshi kubwa lililotoka Misri, ndiyo walioingia nchi ya Kanaani. Maiti zao zilitapakaa nyikani kwa sababu ya makosa yao. Israeli ya leo iko katika hatari kubwa ya kumsahau MUNGU na kuongozwa katika ibada ya sanamu kuliko wale watu wa zamani. Sanamu nyingi zinaabudiwa, hata na wale wanaodai kuwa ni watunza Sabato. MUNGU aliwaamuru watu Wake wa kale kujilinda dhidi ya ibada ya sanamu, kwani ikiwa wangeongozwa katika kuacha kumtumikia MUNGU aliye hai, laana yake ingekuwa juu yao, wakati kama wangempenda kwa moyo wao wote, na kwa roho zao zote, na kwa nguvu zao zote, angewabariki kwa wingi kwenye kikapu na ghalani, na angeyaondoa magonjwa katikati yao. {1T 609.1}

.

Baraka au laana sasa iko mbele ya watu wa MUNGU - baraka ikiwa watatoka ulimwenguni na kujitenga, na kutembea katika njia ya utii mnyenyekevu; na laana ikiwa wataungana na waabudu sanamu, ambao hukanyaga madai ya juu, yaliyoinuliwa ya mbinguni. Dhambi na maovu ya Israeli iliyoasi yameandikwa na picha imewasilishwa mbele yetu kama onyo kwamba ikiwa tutaiga mfano wao wa makosa na kumwacha MUNGU, hakika tutaanguka kama vile walivyofanya. "Basi hayo yote yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano; nayo yameandikwa kutuonya sisi, ambao tumefikiwa na miisho ya ulimwengu." {1T 609.2}

## SURA YA 105

## MAJIBU KUTOKA KANISA LA BATTLE CREEK

Tunachukulia kama upendeleo na wajibu pia kujibu kauli zilizopita za dada White. Tumependelewa kwa miaka mingi kuwa na uzoefu wa kazi za hawa watumishi wa Bwana [ndugu na dada White]. Tumefahamu jambo kuhusu kujikana kwao hapo awali, na wamekuwa mashahidi wa baraka za MUNGU ambazo zimekuwa pamoja na ushuhuda wao wa wazi, unaopeleleza na wenye uaminifu. Tumeshawishika kwa muda mrefu kuwa mafundisho ya ROHO MTAKATIFU katika maono haya yalikuwa muhimu kwa ajili ya ustawi wanaojiandaa kuhamishwa kwenda katika ufalme wa MUNGU. Hakuna namna yoyote ambayo dhambi za siri zinaweza kukemewa na watu waovu wenye machukizo wanaojiingiza “bila ya kujulikana” ndani ya kundi la MUNGU, na kufadhaishwa na hata kufunuliwa na kushindwa katika mipango yao ya uovu. Uzoefu wa muda mrefu umetufundisha kuwa zawadi hiyo ni ya thamani isiyokadirika kwa watu wa MUNGU. Tunaamini pia kuwa MUNGU amemuita Ndugu White kubeba shuhuda za wazi katika kukosoa makosa yanayofanyika, na kwamba katika kazi hii anapaswa kusaidiwa na wale wanaomcha MUNGU kweli. {1T 609.3}

Tumejifunza kwa uzoefu mchungu pia kwamba wakati Shuhuda hizi zinapokuwa kimya, au maonyo yake yakapuuzwa, kuzizima kwa baridi, kurudi nyuma, akili za udunia, na giza la kiroho hulitawala kanisa. Hatutampatia mwanadamu utukufu, lakini tunapaswa kuwa hofu katika hisia za wajibu ili tusizungumze kwa lugha kali na inayosonda kidole maoni yetu juu ya umuhimu wa shuhuda hizi. Uasi wa kutisha wa wale waliozidharau na kuzipuuzia umeonesha ushahidi mwingi wa kuhuzunisha juu ya hatari kubwa ya kufanya hivyo licha ya roho ya neema. {1T 610.1}

Tumekuwa mashahidi wa taabu kubwa ambayo kaka na dada white Wameipitia katika magonjwa makali na hatari ya Ndugu white. Mkono wa MUNGU katika uponyaji Wake uko wazi zaidi kwetu. Pengine hakuna mtu yeyote ambaye amewahi kupigwa pigo kama la kwake na kisha akapona. Na bado mshtuko mkali wa kiharusi/strple, ambao uliuathiri Ubongo, kwa mkono mzuri wa MUNGU, umeondolewa kwa mtumishi Wake, na amepata nguvu mpya zote za kimwili na kiakili. {1T 610.2}

Tunafikiri kwamba hatua ya dada White ya kumchukua mumewe ambaye ni mgonjwa kwenye ziara yake ya kaskazini, Desemba mwishoni mwaka uliopita, ilihimizwa na ROHO WA MUNGU ; na kwamba sisi, katika kusimama kinyume na hatua hiyo, hatukuwa katika mashauri ya MUNGU. Tulikosa hekima ya mbinguni katika hili jambo na tulikosea kutoka katika njia sahihi. Tunakiri kwamba kwa wakati huu, tulikuwa tumepungukiwa na huruma ya Kikristo ya kina, na inayotakiwa kutokana na taabu hiyo, na kwamba tulikuwa wazito kuuona mkono wa MUNGU kwenye uponyaji wa kaka White. Utumishi wake na mateso yake kwa niaba yetu yalimstahili kupata huruma yetu na Msaada. Lakini tumepofushwa na Shetani katika hali yetu ya
Kiroho. {1T 610.3}

Roho ya ubaguzi na chuki kuhusiana na mali ilikuja kwetu katika msimu wa baridi, ikatufanya tuhisi kwamba kaka White alikuwa anaomba fedha wakati hana mahitaji. Sasa wakati huu tunasadiki kwamba kweli alikuwa na uhitaji, na tulikuwa tumekosea kwa kuwa hatukuweza kuuliza kuhusu suala hili. Tunakiri kwamba hisia hii haikuwa na msingi Wowote na ilikuwa ya kikatili, japo ilisababishwa na ukosefu wa taarifa ya ukweli kwenye suala hili {1T 611.1}

Sasa tunakubali kwa huzuni ya kina ya moyo kwamba maonyo yalitolewa kwetu kupitia shuhuda hizi, na tunaomba kwamba popote ambapo tumekosea kutoka katika jambo kufanya sahihi kupitia ukosefu wetu wa Ufahamu wa kiroho, tuweze kupata msamaha wa MUNGU na watu
Wake. {1T 611.2}

Utumishi wa kaka na dada white pamoja nasi kwa siku chache zilizopita umekuwa ukijawa na baraka za MUNGU. Siyo tu kwamba una ungamo la kina la moyo kwa wale waliorudi nyuma na makosa yaliyofanyika, bali viapo vya dhati

vya toba na kurudi kwa MUNGU vimeambatana nao. ROHO WA MUNGU ameweka muhuri Wake katika kazi hii kwa namna ambayo hatuwezi kuwa na shaka. Vijana wengi wameletwa kwa Kristo, na karibu kila mtu aliyeunganishwa na kanisa hili amepata gawio la baraka hizi za mbinguni. {1T 611.3}

Hebu wenzetu wa ng'ambo waelewe kwamba mioyo yetu iko pamoja na Kaka na Dada White, na kwamba tunaamini kwamba wao waliitwa na MUNGU kwa ajili ya uwajibikaji wa kazi hii wanayoifanya, na kwamba tunaahidi kusimama nao katika hili. {1T 611.4}

Kwa niaba ya kanisa, {1T 612.1}

J.N. ANDREWS,<br>
J.N. LOUGHBOROUGH,<br>
JOSEPH BATES,<br>
D.T. BOURDEAU,<br>
A.S. HUTCHINS, JOHN BYINGTON,<br>
*Kamati*.

Katika mkutano wa kanisa, jumatatu jioni, oktoba 21, ripoti iliyotajwa hapo juu ilikubaliwa kwa moja kwa moja. {1T 612.2}

URIAH SMITH,<br>
G.W. AMADON,<br>
*Wazee*

## SURA YA 106

## KUKATA NA KUFYEKA

"Kukata na Kufyeka"

Kauli hii mara nyingi hutumiwa kuwakilisha tabia na maneno ya watu wanaokemea wale ambao wamekosea au wanaodhaniwa kuwa wamekosea. Inatumika vizuri kwa wale ambao hawana jukumu la kukemea ndugu zao, lakini wako tayari kushiriki katika kazi hii kwa haraka na bila kujali. Na inatumika vibaya kwa wale ambao wana jukumu maalum la kufanya katika kukemea makosa kanisani. Hao wana mzigo wa kazi na kutoka katika upendo wa roho za thamani wanahisi kulazimika kushughulika kwa uaminifu. {1T 612.3}

Mara kwa mara kwa miaka ishirini iliyopita nimeoneshwa kuwa Bwana alikuwa amemstahisha mume wangu kwa kazi ya kushughulika kwa uaminifu na wakosaji, na alikuwa amemwekea mzigo, na kwamba ikiwa angeshindwa kutekeleza wajibu wake katika hili angemkasirisha Bwana. Sijawahi kuyachukulia maamuzi yake kuwa hayana makosa, wala kwamba maneno yake

kuvuviwa; lakini nimewahi kumuamini kuwa anafaa zaidi kwa kazi hii kuliko mhubiri wetu mwingine yeyote, kwa sababu ya uzoefu wake mrefu, na kwa sababu nimeona kwamba aliitwa kwa namna ya pekee kuifanya kazi hii na akaendana nayo vyema; na pia kwa sababu katika visa vingi ambavyo watu wameinuka dhidi ya maonyo yake, nimeoneshwa kuwa alikuwa sahihi katika maamuzi yake na namna yake ya kukaripia. {1T 612.4}

Kwa miaka ishirini iliyopita wale ambao wamekemewa, na wale wanaowaunga mkono kwa kuwaonea huruma, wameingiza roho ya kumshtaki mume wangu, ambayo imemchosha zaidi ya mizigo mingine ya kikatili aliyoibeba isivyo haki. Na alipoanguka chini ya mizigo yake, wengi wa wale waliokemewa walifurahi, na kutoka kwenye mtazamo wa maoni yangu uliokosewa juu ya kesi yake, Desemba 25, 1865, walifarijika sana kwa wazo kwamba Bwana wakati huo alimkemea kwa " kukata na kufyeka. " Haya yote ni makosa. Sikuona kitu kama hicho. Ili ndugu zangu wapate kujua kile nilichokiona kwa upande wa mume wangu, ninatoa yafuatayo, ambayo niliyaandika na kumkabidhi siku iliyofuata baada ya kuona maono: {1T 613.1}

Nilioneshwa katika maono, Desemba 25, 1865, kesi ya mtumishi wa Bwana, mume wangu, Mzee James White. Nilioneshwa kwamba MUNGU alikuwa amekubali fedheha yake, na kuteswa kwa roho yake mbele Yake, na kukiri kwake ukosefu wa kujikabidhi kwa MUNGU, na toba yake kwa makosa na mapungufu katika njia yake ambayo yamesababisha huzuni na kukata tamaa katika mawazo yake wakati wa ugonjwa wake wa muda mrefu. {1T 613.2}

Nilioneshwa kuwa kosa lake kubwa hapo zamani limekuwa roho ya kutowasamehe wale ndugu ambao wamejeruhi ushawishi wake kwa kazi ya MUNGU na kumletea mateso makali ya akili kwa njia zao mbaya. Hakuwa mwenye rehema na huruma kama Baba yetu wa mbinguni alivyo kwa watoto Wake wanaokosea, wanaotenda dhambi, na wanaotubu. Wakati wale ambao wamemsababishia mateso makubwa walipotambua makosa yao kwa moyo wote mkamilifu, angeweza na aliwasamehe, na kushirikiana nao kama ndugu. Lakini japokuwa makosa yaliponywa mbele za MUNGU, bado wakati mwingine katika akili yake mwenyewe alilikumbushia jeraha hilo, na kwa kurejelea siku za nyuma alilivumilia likue na kumfanya asiwe mwenye furaha. Ukweli kwamba katika mapito yake ya zamani alipata mateso mengi ambayo kwa maoni yake yangeweza kuepukwa, kulimfanya awe na roho ya manung'uniko dhidi ya ndugu zake na dhidi ya Bwana. Kwa njia hii aliishi katika mambo ya zamani na kuhuisha mambo ambayo yangepaswa kuwa yamesahaulika badala ya kuyachochea maisha yake kwa kumbukumbu zisizofaa. Yeye hajatambua kila mara huruma na upendo ambao unapaswa kutekelezwa kwa wale ambao wamekuwa wadhaifu hata kuanguka chini ya vishawishi vya Shetani. Walikuwa ni watesekaji wa kweli, walioshindwa, wapotezaji na sio yeye, maadam

alikuwa thabiti, na mwenye roho ya Kristo. Wakati roho hizi zilipoanza kuona makosa yao, zilikuwa na vita ngumu ya kuandaa njia ya nuru kwa ungamo la unyenyekevu. Walikuwa na Shetani kushindana naye, na pia kuishinda roho yao ya kiburi, na walihitaji msaada kutoka kwa wale ambao walikuwa kwenye nuru ili wawalete kutoka katika hali yao ya upofu, ya kukatisha tamaa, ambapo wangeweza kuanza kutumaini na kupata nguvu ya kumponda Shetani chini ya miguu yao. {1T 613.3}

Niliona kwamba mume wangu alikuwa mkali sana kwa wale ambao walikuwa wamekosea na kumjeruhi. Aliendekeza hisia zia kutoridhika, ambazo haziwezi kuwa na faida kwa wakosaji na zinaweza kuufanya moyo wake mwenyewe kukosa furaha, hata amani ya MUNGU kutostahili kukaa hapo, ambayo ingempelekea kutoa shukrani katika kila kitu. Bwana aliruhusu akili yake ikate tamaa kwa sababu ya mapungufu na makosa yake mwenyewe, na kukaribia kukata tamaa ya kusamehewa, siyo kwa sababu dhambi zake zilikuwa za ukubwa kama huo, bali ili aweze kujua kwa uzoefu jinsi inavyokuwa chungu na yenye kuumiza kukaa bila msamaha wa MUNGU, na ili apate kuelewa Maandiko: "Msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu." Niliona kwamba ikiwa MUNGU angekuwa mkali kama sisi, Anayechukulia kila kitu kwa kinagaubaga, na kushughulika na sisi kama tunavyoshughulikiana sisi kwa sisi, tunaweza sote kutupwa katika hali ya kukata tamaa. {1T 614.1}

Nilioneshwa kwamba MUNGU alikuwa amevumilia shida hii ije juu yetu ili itufundishe mengi ambayo tusingeweza kujifunza kwa muda mfupi sana. Yalikuwa mapenzi yake kwamba twende huko -----, kwani uzoefu wetu usingeweza kuwa kamili bila hilo. Yeye Angetaka tuone, na tuelewe zaidi, kwamba haiwezekani kwa wale wanaoutii Ukweli na kuzishika amri ZAKE, kuishi kulingana na usadikisho wao wa wajibu na kuungana na viongozi huko -----; kuhusiana na suala la kumtumikia MUNGU, kanuni zao haziwezi kuungana vema zaidi ya mafuta na maji. Ni wale tu wenye kanuni safi na uhuru mkubwa wa akili, ambao wanafikiria na kutenda kwa ajili yao wenyewe, wakiwa na hofu ya MUNGU mbele yao na kumtumaini Yeye, ndio wanaoweza kukaa salama kwa kipindi chote huko -----. Wale ambao hawajakidhi vigezo hivyo hawapaswi kushauriwa kwenda kwenye taasisi hiyo, kwani akili zao zitavurugwa na maneno laini ya wasimamizi wake na kutiliwa sumu na ustadi wao katika udanganyifu, ambao unatokana na Shetani. {1T 614.2}

Ushawishi na mafundisho yao kuhusu huduma ya MUNGU na maisha ya kidini vinapingana kabisa na mafundisho ya Mwokozi wetu na wanafunzi Wake. Kwa sheria na mfano wanapunguza kiwango cha utauwa na kusema kwamba hawahitaji kuhuzunika kwa ajili ya dhambi zao au kujitenga na ulimwengu ili kuwa wafuasi wa Kristo, lakini wanaweza kujichanganya na ulimwengu na

kushiriki katika raha zake. Viongozi hawa hawatawahimiza wafuasi wao kuiga maisha ya Kristo kwa kusali, kuwa na kiasi, na kumtegemea MUNGU. Watu wenye akili za dhamiri na imani thabiti kwa MUNGU hawawezi kupata hata nusu ya faida kama hiyo huko ----- kama wale ambao wanaweza kuwa na imani na kanuni za kidini za viongozi wa taasisi hiyo. Hawa wa kwanza wanapaswa kusimama imara dhidi ya mafundisho yao mengi, kadri kanuni za kidini zinavyohusika, wakichuja kila kitu wanachosikia wasije wakadanganywa na Shetani akapata faida juu yao. {1T 615.1}

Niliona kwamba, kuhusu ugonjwa na matibabu yake, ----- hii ndio taasisi bora ya afya nchini Marekani. Lakini viongozi wa huko ni wanadamu tu, na maamzi yao siyo sahihi kila wakati. Daktari anayeongoza hapo angewafanya wagonjwa wake waamini kwamba maamzi yake ni kamilifu, kama ymaamuzi ya MUNGU. Hata hivyo mara nyingi hushindwa. Anajiinua kama MUNGU na anashindwa kumtukuza Bwana kama tegemeo pekee. Wale ambao hawana uaminifu au imani kwa MUNGU, na ambao hawawezi kuona uzuri katika utakatifu au katika maisha ya Mkristo, wanaweza kupata faida zaidi huko ----- kuliko kwa taasisi nyingine yoyote ya afya huko Marekani. Siri kubwa ya mafanikio mahali hapa iko katika udhibiti ambao wasimamizi wanao, juu ya akili za wagonjwa wao. {1T 615.2}

Niliona kwamba mimi na mume wangu tusingeweza kupata faida nyingi huko kama wale wenye uzoefu na imani tofauti. Malaika alisema: "MUNGU hajakusudia kwamba akili ya mtumishi Wake, ambaye amemchagua kwa kusudi maalum, kufanya kazi maalum, idhibitiwe/itawaliwe na mtu yeyote, kwa kuwa hiyo ni haki Yake peke yake." Malaika wa MUNGU walitutunza tulipokuwa -----. Walikuwa karibu nasi, wakituimarisha/wakitutegemeza kila saa. Lakini wakati ulifika ambapo hatukuweza kufaidi wala kufaidisha, na kisha wingu la nuru, ambalo lilikuwa juu yetu huko, lilihama, na tungeweza kupata raha tu kwa kuondoka huko na kwenda kwa ndugu zetu huko Rochester, ambapo wingu la nuru lilitutua hapo. {1T 616.1}

Niliona kwamba MUNGU angependa twende ----- kwa sababu kadhaa. Msimamo wetu tulipokuwa huko, maombi ya dhati tuliyoyatoa, imani yetu dhahiri kwa MUNGU, uchangamfu, ujasiri, matumaini, na imani ambao Yeye alitupatia katikati ya mateso yetu, yalikuwa na ushawishi na yalikuwa ushuhuda kwa wote kwamba Mkristo ana chanzo cha nguvu na furaha ambacho wapenda anasa hawakitambui. MUNGU alitupatia nafasi katika mioyo ya ushawishi wote huko ---, na katika siku zijazo kama wagonjwa sasa watatawanyika kwenda katika nyumba zao tofauti, kazi zetu zitatuleta tena kwao, na tutakaposhambuliwa, baadhi yao angalau watakuwa watetezi wetu. Tena, kwa kwenda huko -----, Bwana angetaka tufaidike na uzoefu ambao tusingeweza kuupata tukiwa Battle Creek, tukizungukwa na ndugu na dada wenye huruma. Lazima tujitenge nao,

tusije tukawategemea badala ya kumtegemea Bwana na kumtumaini Yeye peke yake. Hali tukitengwa karibu kabisa na watu wa MUNGU, tulitikiswa kutoka katika kila msaada wa kidunia na kuongozwa kumtazama MUNGU peke yake. Kwa kufanya hivyo tulipata uzoefu ambao tusingekuwa nao kama tusingeenda -----. {1T 616.2}

Wakati ujasiri na matumaini ya mume wangu vilipoanza kuyumba, tusingeweza kumnufaisha mtu yeyote mahali hapo na tusingeweza kufaidika na uzoefu zaidi huko. Yalikuwa mapenzi ya MUNGU kwamba mume wangu asikae hapo akiwa amedhoofika nguvu zake, bali kwamba katika hali yake ya udhaifu aende kati ya ndugu zake ambao wangeweza kumsaidia kubeba shida zake. Wakati tulipotengwa na watu wa MUNGU katika dhiki yetu, tulikuwa na nafasi ya kutafakari, kupitia kwa uangalifu maisha yetu ya zamani, na kuona mapungufu na makosa yetu, na kujinyenyekeza mbele za MUNGU na kuutafuta uso Wake kwa maungamo, kujidhili, na kuomba mara kwa mara kwa bidii. Tulipokuwa tukifanya kazi kwa bidii, tukibeba mizigo ya wengine, na tukisongwa na masumbufu mengi, haikuwezekana kwetu kupata muda wa kutafakari na kupitia kwa uangalifu yaliyopita, na kujifunza masomo ambayo MUNGU aliona ni muhimu kwetu kujifunza. Wakati huo nilioneshwa kwamba MUNGU asingeweza kulitukuza Jina Lake kwa kujibu dua za watu Wake na kumuinua mume wangu katika uzima kwa kujibu maombi yao, tulipokuwa huko ----. Ingekuwa kama kuunganisha nguvu zake na nguvu za giza. Kama angekuwa radhi kudhihirisha nguvu Zake kwa kumrejeshea afya mume wangu, matabibu walioko huko wangechukua utukufu ambao angepaswa kupewa MUNGU. {1T 617.1}

Malaika alisema: "MUNGU atatukuzwa kwa kumrudishia afya mtumishi Wake. MUNGU amesikia maombi ya watumishi Wake. Mikono Yake iko karibu na mtumishi Wake aliyesumbuliwa. MUNGU anajua, hii kesi ipo Kwake na ingawa amesumbuliwa, lazima aiondoea hofu yake, wasiwasi wake, mashaka yake na kutokuamini kwake, na kwa utulivu amtumaini MUNGU mkuu lakini Mwenye huruma, ambaye humhurumia, humpenda, na kumjali yeye. Atakuwa na mizozo na adui, lakini anapaswa kufarijiwa daima na ukumbusho kwamba Mwenye nguvu kuliko adui anamsimamia, na hana haja ya kuogopa. Kwa imani ategemee uthibitisho ambao MUNGU amependa kuutoa, naye atashinda kwa utukufu katika MUNGU. "{1T 617.2}

Niliona kwamba Bwana alikuwa anatupatia uzoefu ambao ungekuwa wa thamani kubwa zaidi kwetu katika siku zijazo kuhusiana na kazi Yake. Tunaishi katika wakati adhimu katikati ya matukio ya kufunga historia ya dunia hii, lakini watu wa MUNGU hawajaamka. Lazima waamke na kufanya maendeleo makubwa katika kurekebisha tabia zao za kuishi, kula, kuvaa, kufanya kazi na kupumzika. Katika haya yote wanapaswa kumtukuza MUNGU na kuwa tayari

kupigana na adui yetu mkuu na kufurahia ushindi mzuri ambao MUNGU amewawekea wale ambao wanajizuia kwa kuwa na kiasi katika kila kitu wakati wakijitahidi kupata taji isiyoweza kuharibika. {1T 618.1}

Niliona kwamba MUNGU alikuwa akimuandaa mume wangu kushiriki katika kazi nzito, takatifu ya matengenezo ambayo Yeye ameikusudia isonge mbele kati ya watu Wake. Ni muhimu maagizo yatolewe na wachungaji juu ya kuishi kwa kiasi. Wanapaswa kuonesha uhusiano uliopo kati ya kula, kufanya kazi, kupumzika, kuvaa na kudumisha afya. Wote ambao wanauamini Ukweli wa siku hizi za mwisho wanalo la kufanya katika suala hili. Linawahusu, na MUNGU anawataka waamke na wapendezwe na matengenezo haya. Yeye Hatapendezwa na mwenendo wao ikiwa watazingatia hoja hii bila kujali. {1T 618.2}

Matumizi mabaya ya tumbo, kwa kulinyanyasa ili kutosheleza hamu ya kula ndicho chanzo cha matokeo ya majaribu mengi ya kanisa. Wale ambao hula na kufanya kazi bila mpangilio wa kuwa na kiasi, na bila makusudi, bila mpangilio, huzungumza na kutenda bila mpangilio. Mtu asiye na kiasi hawezi kuwa mtu mwenye subira. Siyo lazima kunywa vileo ili kuwa mtu asiye na kiasi. Dhambi ya kula bila kiasi, kula mara kwa mara, kupita kiasi, na chakula tajiri kilichokobolewa au kusindikwa (rich foods au junk foods), huharibu kitendo cha kiafya cha viungo vya mmeng'enyo, huathiri ubongo, na kupotosha hukumu, kuzuia busara, utulivu, fikira zenye afya na kutenda. Na hiki ni chanzo cha matokeo ya majaribu ya kanisa. Kwa hivyo ili watu wa MUNGU wawe katika hali inayokubalika pamoja Naye, ambapo wanaweza kumtukuza katika miili na roho zao ambazo ni Zake, lazima kwa nia, ari na bidii wakane kuridhisha matamanio yao ya chakula (uroho wa chakula), na wajizoeze kuwa na kiasi katika mambo yote. Basi wangeweza kuuelewa Ukweli kwa uzuri na uwazi wake, na kuutekeleza maishani mwao, na kwa mwenendo wa hekima, busara, na wa moja kwa moja wasimpatie adui wa imani yetu nafasi ya kulaumu kazi ya Ukweli. MUNGU anahitaji wote wanaouamini Ukweli wafanye jitihada maalum, ya kudumu ili kujiweka katika hali bora kabisa ya afya ya mwili, kwani kazi nzito na muhimu iko mbele yetu. Afya ya mwili na akili inahitajika kwa kazi hii; ni muhimu kwa ajili ya uzoefu mzuri wa kidini, kufanya maendeleo katika maisha ya Kikristo na maendeleo katika utakatifu, kama vile ulivyo mkono au mguu kwenye mwili wa mwanadamu. MUNGU anawataka watu Wake kujitakasa na uchafu wote wa mwili na roho, wakitimiza utakatifu katika kumcha Bwana. Wale wote ambao hawajali na wanajiondoa katika kazi hii, wakimngojea Bwana awafanyie yale ambayo Yeye anataka wayafanye wao wenyewe, watakutwa wamepungua wakati Yule mpole na mnyenyekevu wa dunia, atakapokuwa amefanya hukumu ZAKE zilizojificha ndani siku ya hasira ya Bwana. {1T 618.3}

Nilioneshwa kuwa ikiwa watu wa MUNGU hawatafanya bidii kwa upande wao, wakisubiri kuburudishwa kuje juu yao na kuondoa makosa yao na kurekebisha mapungufu yao; ikiwa wanategemea hilo ndilo liwasafishe kutoka katika uchafu wa mwili na roho, na kuwafanya wafae kushiriki kilio kikuu cha malaika wa tatu, watakutwa wamepungua. Burudiko au nguvu ya MUNGU huja tu kwa wale ambao wamejiandaa kwa ajili yake kwa kufanya kazi ambayo MUNGU anawaamuru, ambayo ni, kujitakasa na uchafu wote wa mwili na roho, wakikamilisha utakatifu katika kumcha MUNGU. {1T 619.1}

Nilioneshwa kuwa katika hali fulani kesi ya mume wangu ni sawa na ile ya wale wanaosubiri kuburudishwa. Ikiwa anapaswa kuisubiri nguvu ya MUNGU ije juu ya mwili wake, ili ahisi kwamba ameponywa kabla ya kufanya juhudi kulingana na imani yake, akisema, Bwana atakaponiponya nitaamini na kufanya hivi au vile, anaweza kuendelea kungojea na hataona mabadiliko yoyote, kwa sababu utimizo wa ahadi ya MUNGU hutambuliwa tu na wale wanaoamini na kisha kufanya kazi kulingana na imani yao. Niliona kwamba lazima aamini Neno la MUNGU, kwamba ni jukumu lake kuzidai ahadi za MUNGU, nazo hazitapungua, hapana, kamwe. James White Anapaswa kutembea kwa imani, akitegemea ushuhuda ambao MUNGU amekuwa radhi kuutoa, na kufanya kazi, kwa kadri inavyowezekana, ili kufikia hatua ya kupona kabisa. Malaika alisema: "MUNGU atamtegemeza. Imani yake lazima ikamilishwe kwa matendo, kwani imani peke yake bila matendo imekufa. Inapaswa kudumishwa na matendo. Imani hai daima hudhihirishwa na matendo." {1T 619.2}

Niliona kwamba mume wangu alikuwa na mwelekeo wa kujikunja kulingana na imani yake. Hofu na wasiwasi juu ya suala lake mwenyewe vimemfanya awe mwoga. Anaangalia mwonekano, kwa hisia za mwili zisizokubaliana. Malaika alisema: "Hisia siyo imani. Imani ni kumchukulia MUNGU kama asemavyo katika Neno Lake." Niliona kwamba kwa Jina na nguvu ya MUNGU lazima mume wangu apambane na magonjwa na, kwa nguvu ya nia/mapenzi yake, anyanyuke juu ya hisia zake mbaya. Lazima athibitishe uhuru wake, kwa Jina na nguvu ya MUNGU wa Israeli. Lazima kadri iwezekanavyo aache kufikiria na kujizungumzia mwenyewe. Anapaswa kuwa mchangamfu na mwenye furaha. {1T 620.1}

Niliona, Desemba 25, 1865, kama nilivyoona mara nyingi kabla, kwamba Mzee F alikuwa amekosea mara nyingi na alikuwa amesababisha madhara mengi kwa njia ya harara, isiyo na hisia kwa wale ambao alidhani kwamba walikuwa na makosa. Nilikuwa nimeona mara nying kazi yake ilikuwa katika maeneo mapya, na kwamba wakati atakapoleta kundi la watu kwenye Ukweli wa sasa, atapaswa kuacha kazi ya kuwanidhamisha kwa wengine, kwani mtindo wake wa kushughulikia watu, unaotokana na roho yake ya hasira, ukosefu wake wa uvumilivu na hukumu, vilimfanya asifae kwa kazi hii. Nitatoa hapa ushuhuda niliokuwa nao kwa ndugu F, ulioandikwa Desemba 26, 1865, kuonesha kile

nilichokiona katika kesi yake na kwa sababu ya matumizi ya jumla ya ushuhuda na pia kwa sababu yeye hajajibu chochote, ila ni pale tu katika kuwaambia wengine tu ya kwamba Bwana kwa maoni hayo alimkemea mume wangu kwa kukata na kufyeka. Ningesema hapa kwamba kitu kingine katika kutoa ushuhuda ufuatao ni kwamba ndugu zetu wanaweza kuelewa kabisa kwamba kazi ya ndugu F iko katika maeneo mapya ya kazi, na kwamba wasiweke vishawishi katika njia yake akaiacha kazi yake, kwa kumtaka afanye kazi hapa na pale kati ya makanisa, au kukaa hapa au pale. {1T 620.2}

## SURA YA 107

## HATARI YA KUJIAMINI

Ndugu F: Desemba 25, 1865, nilioneshwa kuwa kazi nzuri ilikuwa imeanza Maine. Yumkini ule uwanja wa kazi uliooneshwa kwangu ambapo kundi liliinuliwa kama matunda ya kazi ya ndugu Andrews na wewe mwenyewe, ambapo wameonesha upendo wao na kupenda Ukweli kwa kujenga nyumba ya ibada. Bado kuna kazi kubwa ya kufanywa kwa kundi hili. Idadi kubwa imeongolewa kwenye nadharia ya Ukweli; wengine wameamua kutokana na uzito wa ushahidi; wanaona uzuri katika mnyororo wa Ukweli uliounganishwa, wote wakiungana katika umoja, ukamilifu kamili; wanapenda kanuni za Ukweli, lakini hawajatambua ushawishi wake wa kutakasa. Nafsi hizi zinakabiliwa na hatari za siku za mwisho. Shetani ameandaa udanganyifu wake na mitego kwa watu wasio na uzoefu. Anafanya kazi kupitia mawakala wake, hata wachungaji wanaoudharau Ukweli na kuikanyaga sheria ya MUNGU na kuwafundisha wote watakaowasikiliza kufanya vivyo hivyo. {1T 621.1}

Kundi hili la watu ambao wameupokea Ukweli usiopendwa wanaweza kuwa salama pale tu wanapomfanya MUNGU kuwa tumaini lao na kutakaswa na Ukweli ambao wanaukiri. Wamechukua hatua muhimu na sasa wanahitaji uzoefu wa kidini ambao utawafanya kuwa wana na binti za MUNGU aliye juu sana na warithi wa urithi wa milele ulionunuliwa kwao na Mwanaye Mpendwa. Wale ambao wamekuwa chombo katika kuwasilisha Ukweli kwao hawapaswi kuondoa utumishi wao katika kipindi hiki muhimu, bali bado wanapaswa kudumu katika juhudi zao mpaka roho hizi zikusanyike katika zizi la Kristo. Mafunzo ya kutosha yanapaswa kutolewa kwao ili wajipatie ushahidi na uelewa kwamba kwao Ukweli ni wokovu. {1T 621.2}

Niliona kwamba MUNGU angefanya kazi kubwa zaidi Maine ikiwa wote wanaofanya kazi kwa kusudi hilo wamejiweka wakfu Kwake na wasiziamini nguvu zao wenyewe, bali Mwenye nguvu wa Israeli. Nilioneshwa kwamba kaka Andrews na wewe mwenyewe mmejitahidi sana na hamjapata mapumziko ambayo mnapaswa kuyapata ili kuhifadhi afya. Mnapaswa kufanya kazi kwa uangalifu na muchukue vipindi vya kupumzika. Kwa kufanya hivyo mtabaki na nguvu zenu za mwili na akili, na kuipatia kazi yenu ufanisi zaidi. Ndugu F, wewe ni mtu mwenye woga, wasiwasi na tashwishwi. Sononeko la akili huathiri kazi yako sana. Wakati mwingine unahisi ukosefu wa uhuru na unafikiria ni kwa sababu wengine wako gizani au wako katika makosa, au kwamba kuna jambo linalosababisha, huwezi hata kulielezea, na unalisukuma jambo hilo kuelekea mahali fulani au juu ya mtu fulani, hali ambayo inaweza kuwa na madhara makubwa. Endapo ungejinyamazisha ukiwa katika hali hii ya kutotulia, ya woga, na kupumzika na kumngojea MUNGU kwa utulivu na kujiuliza kama shida haiko ndani yako, usingeijeruhi roho yako mwenyewe wala kuiumiza kazi ya MUNGU ya thamani. {1T 622.1}

Niliona kwamba ndugu F alikuwa katika hatari ya kuinuliwa ikiwa angewezeshwa katika hotuba zake kuvuta hisia za mkutano. Mara nyingi angejiona kuwa mhubiri mwenye ufanisi zaidi kwenye huduma hiyo. Hapa wakati mwingine anajidanganya mwenyewe. Ingawa anaweza kuwa mhubiri anayekubalika zaidi kwa wakati huu, lakini anaweza akashindwa kutimiza mambo mema zaidi. Mhubiri ambaye anaweza kuathiri hisia kwa kiwango kikubwa zaidi hatoi ushahidi kwamba yeye ndiye anayenufaisha zaidi. {1T 622.2}

Wakati kaka F ni mnyenyekevu na anamfanya MUNGU kuwa tumaini/tegemeo lake, anaweza kufanya mema mengi. Malaika wanamsaidia, na amebarikiwa na uwazi na uhuru. Lakini baada ya wakati wa ushindi maalum, mara nyingi ameinuliwa juu na kujiona kuwa sawa na chochote, alidhani kuwa yeye ni kitu cha maana, wakati alikuwa chombo tu mikononi mwa MUNGU. Baada ya majira

kama hayo, malaika wa MUNGU wamemwacha katika nguvu zake dhaifu, kisha, ingawa yeye mwenyewe ndiye aliyekuwa na makosa, mara nyingi angewatuhumu ndugu zake na watu juu ya giza na udhaifu aliouhisi. Wakati akiwa katika hali hii ya kutokuwa na furaha ya akili mara kwa mara huwabebesha mizigo huyu na yule, na wakati kazi yake haijamalizika hata nusu, huhisi kwamba lazima aondoke na kuanzisha kazi mahali pengine. {1T 623.1}

Niliona kwamba kaka F alikuwa katika hatari ya kuingia vitani kwa nguvu zake mwenyewe, lakini atagundua kuwa nguvu hizo ni udhaifu vitani. Alipomfanya MUNGU kuwa tegemeo lake, mara nyingi amekuwa akifanikiwa kupigana na wapinzani wa imani yetu. Lakini wakati mwingine amejisikia kufurahia ushindi ambao MUNGU ameupatia Ukweli dhidi ya makosa, na amejichukulia utukufu katika mapambano haya. Ubinafsi umetukuzwa machoni pake mwenyewe. {1T 623.2}

Nilioneshwa kuwa katika mijadala yake miwili ya mwisho hakuwa na roho sahihi. Kabla ya mjadala wa kwanza aliinuliwa na kusifiwa kwa kutia chumvi na watu ambao hawapendi Ukweli. Alipowasikiliza, na kuwa sehemu, mjadala uliofanywa kati ya wawili ambao hawakuwa katika imani, aliinuliwa na kujiona anafaa kuingia vitani na mtu yeyote. Na alipojiamini sana, alikuwa, katika kitendo hicho, amepunguzwa nguvu zake. MUNGU alikasirishwa na kupuuza kwake ushauri wa kaka Andrews. Roho yake ya kujitosheleza ilikaribia kuufanya mjadala huo kushindwa kabisa. Isipokuwa kuna faida ya maana katika mapambano haya, mtu asiingie kwa vile, kila wakati kuna hasara. Hayapaswi kamwe kuingiwa bila kupima mambo, bali kila hatua inapaswa kufanywa kwa uangalifu, na hekima kubwa zaidi, kwani mengi zaidi yanaelea angani, yakihitajika kuhitimishwa kuliko katika vita vya kitaifa. Shetani na jeshi lake lote wako macho katika mizozo hii kati ya Ukweli na uongo, na ikiwa watetezi wa Ukweli hawaingii vitani kwa nguvu ya MUNGU, Shetani atafanikiwa kuwashinda kila wakati. {1T 623.3}

Katika pambano la pili kulikuwa na mengi, mengi sana yalikuwa hatarini. Lakini hapa tena kaka F alishindwa. Hakuhusika katika mzozo huo akihisi udhaifu wake na katika unyenyekevu na usahili ategemee nguvu za MUNGU. Baadaye alihisi tena utoshelevu ndani yake. Mafanikio yake ya nyuma yalikuwa yamemwinua. Alifikiri kwamba ushindi alioupata ulitokana sana na uwezo wake wa kutumia hoja zenye nguvu zilizomo katika Neno la MUNGU. {1T 624.1}

Nilioneshwa kuwa watetezi wa Ukweli hawapaswi kutafuta mijadala/debate. Na wakati wowote inapohitajika kwa maendeleo ya kusudi la Ukweli na utukufu wa MUNGU kwamba mpinzani afikiwe kwa kukutana uso kwa uso, basi watu wanapaswa kuingia kwenye pambano hilo kwa uangalifu na unyenyekevu kiasi

gani. Kwa kujichunguza moyo, kuungama dhambi, na kuomba kwa dhati na bidii, na mara nyingi kufunga kwa muda, wanapaswa kuomba kwamba MUNGU awasaidie na kuwapa Ukweli Wake unaookoa, wa thamani, ushindi mtukufu, ili makosa yaonekane katika uharibifu wake wa Kweli na watetezi wake waaibike kabisa. Wale wanaopigania Ukweli, dhidi ya wapinzani wake, wanapaswa kutambua kwamba hawakutani tu na watu, bali wanashindana na Shetani na malaika zake, ambao wamedhamiria kuwa makosa na giza vitabaki shambani na Ukweli utafunikwa na makosa. Kwa kuwa kosa lipo hasa katika moyo wa asili, linachukuliwa na watu kuwa jambo hili liko wazi zaidi. Watu walioridhika wanapenda makosa na giza, na hawataki Ukweli uwarekebishe. Hawapendi kuja kwenye nuru, ili matendo yao yasipate kukemewa. {1T 624.2}

Ikiwa wale wanaosimama katika kuutetea Ukweli, wanaamini katika uzito wa hoja, kuliko kumtegemea MUNGU, na wakakutana na wapinzani wao hivyo hivyo, hakuna chochote kitakachopatikana upande ya Ukweli, bali kutakuwa na hasara kubwa. Isipokuwa kuna ushindi dhahiri upande wa Ukweli, jambo hilo linaachwa likiwa baya kuliko hapo awali kabla ya pambano. Wale ambao hapo awali wangekuwa na usadikisho juu ya Ukweli hatimaye huituliza akili yao na kuamua kuwa upande wa makosa, kwa sababu katika hali yao ya giza hawawezi kutambua kuwa Ukweli ulikuwa na faida. Mijadala hii miwili ya mwisho haikuiendeleza kazi ya MUNGU, na ingekuwa bora kama isingefanyika. Kaka F hakujihusisha na roho ya kujidhili na kumtegemea MUNGU kikamilifu. Alitiwa kiburi na kichwa kikavimba kwa msaada wa adui na alikuwa na roho ya kujitosheleza na kujiamini bila kuwa mtumishi mnyenyekevu wa Kristo. Alikuwa na silaha zake mwenyewe, siyo silaha za MUNGU. {1T 624.3}

Kaka F, MUNGU alikuwa amekupatia mtumishi mwenye uzoefu wa kina, aliye hodari shambani. Alikuwa mtu ambaye alikuwa anazifahamu hila za shetani katika uzoefu wake mwenyewe, na ambaye alikuwa amepitia maumivu makali ya akili. Alikuwa ameruhusiwa katika mwongozo wa hekima ya MUNGU kuhisi joto la tanuru inayosafisha na hapo alikuwa amejifunza kuwa kila kimbilio isipokuwa la MUNGU litashindwa na kila msaada ambao angeutegemea kwa msaada ungethibitisha kuwa kama mwanzi uliovunjika. Wewe ungepaswa kutambua kuwa kaka Andrews alikuwa na shauku kubwa katika mazungumzo kama wewe mwenyewe, na ungepaswa kusikiliza ushauri wake na kufaidika na maagizo yake kwa roho ya unyenyekevu. Lakini Shetani alikuwa na jambo lake hapa, kuliangusha kusudi la MUNGU, na aliingia kuitawala akili yako na kwa hivyo akaizuia kazi ya MUNGU. Uliharakisha vitani kwa nguvu zako mwenyewe, na malaika walikuacha uendelee. Lakini MUNGU kwa rehema kwa ajili ya kazi Yake asingewaruhusu maadui wa Ukweli Wake wapate ushindi, na katika kujibu maombi ya bidii, yenye uchungu ya mtumishi Wake, malaika walituokoa. Badala ya kushindwa kabisa kulikuwa na ushindi wa sehemu, ili maadui wa Ukweli wasishangilie juu ya waumini. Lakini hakuna kitu kilichopatikana kutokana na juhudi hiyo, wakati kunaweza kuwa na ushindi wa utukufu wa Ukweli dhidi ya

makosa. Kulikuwa na watetezi wawili wa Ukweli upande wako; watu watatu,wenye nguvu ya Ukweli, kushindana na mtu mmoja ambaye alikuwa akitafuta kuuficha Ukweli kwa makosa. Katika MUNGU ungeweza kuwa jeshi lake, kama ungeingia kwa usahihi ndani ya pambano. Kujitosheleza kwako kulisababisha ukaribie kushindwa kabisa. {1T 625.1}

Kamwe haupaswi kuingia kwenye mijadala inayoweka mambo mengi hatarini, ukitegemea uwezo wako wa kushughulikia hoja zenye nguvu. Ikiwa haiwezi kuepukwa vema, basi ingia katika hilo pambano, lakini ingia ukiwa na imani thabiti kwa MUNGU na kwa roho ya unyenyekevu, kwa roho ya Yesu, ambaye amekuambia ujifunze Kwake, ambaye ni mpole na mnyenyekevu wa moyo. Na kisha ili kumtukuza MUNGU na kuonesha tabia ya Kristo, wewe haupaswi kamwe kuchukua faida isiyo halali ya mpinzani wako. Weka kando kashfa, kushushua na kucheza maneno. Kumbuka kuwa uko vitani na Shetani na malaika zake, na vile vile na huyo mtu. Yeye ambaye alimshinda Shetani huko mbinguni na kumshinda yule adui aliyeanguka na kumfukuza kutoka mbinguni, na ambaye alikufa kumkomboa mwanadamu aliyeanguka kutoka katika nguvu Zake, akiwa kwenye kaburi la Musa, akibishana juu ya mwili wake, hakuthubutu kumletea Shetani mashtaka ya matusi, bali alisema: "Bwana na akukemee." {1T 626.1}

Katika mijadala yako miwili ya mwisho ulidharau shauri na haukumsikiliza mtumishi wa MUNGU, ambaye nafsi yake yote ilijitolea kufanya kazi hiyo. MUNGU katika fadhila zake alikupatia mshauri ambaye talanta na ushawishi wake vilimpatia heshima na ujasiri kwako, na kamwe usingeweza kuijeruhi hadhi yako kama ungeongozwa na uamuzi wake wenye uzoefu. Malaika wa MUNGU waliona utoshelevu wako na kwa huzuni waligeuka kutoka kwako. MUNGU asingeweza kuonesha nguvu zake kwa usalama kwa niaba yako, kwa maana ungejichukulia utukufu, na kazi zako za siku za usoni zingekuwa na thamani kidogo. Niliona, kaka F, kwamba haupaswi kutegemea uamuzi wako mwenyewe katika kazi yako, ambao mara nyingi umekupotosha. Unapaswa kuegemea katika maamuzi ya wale wenye uzoefu. Usisimame katika hadhi yako mwenyewe na kuhisi kujitosheleza kiasi kwamba huwezi kuchukua ushauri na maelekezo ya watumishi wenzako wenye uzoefu. {1T 626.2}

Mkeo amekuwa hana msaada maalum kwako, bali ni kikwazo. Ikiwa angepokea na kutii ushuhuda aliopewa zaidi ya miaka miwili iliyopita sasa angekuwa msaidizi wako mwenye nguvu katika injili. Lakini mke huyu hajapokea na kufanyia kazi ushuhuda huo. Ikiwa angefanya hivi, mwenendo wake angekuwa tofauti kabisa. Hajawekwa wakfu kwa MUNGU. Ni mpenda raha, maisha rahisi, raha, anaepuka mizigo, na hajikani nafsi. Huendekeza uvivu, na mfano wake haustahili kuigwa, lakini ni jeraha kwa kazi ya MUNGU. Wakati mwingine anakuwa na ushawishi mkubwa juu yako, hasa kama anahisi kutamani kurudi nyumbani au kutoridhika (homesick). Pia, katika maswala ya kanisa ana ushawishi juu yako. Anatengeneza maoni yake juu ya huyu kaka au dada huyo, na anaonesha kutopenda au kushikamana kwa nguvu, wakati imekuwa kesi

kwamba wale anaowachukua moyoni mwake wamekuwa chanzo cha jaribu kubwa kwa kanisa. Hali yake isiyotakaswa inamfanya ahisi kushikama sana na wale ambao wanaonesha ujasiri mkubwa na upendo kwake, wakati roho za thamani ambazo MUNGU anazipenda zinaweza kupitwa kwa ubaridi kwa sababu hakuna maoni ya bidii ya kushikamana nao yanasikika kutoka kwao kuhusiana na kaka F. Na bado upendo wa roho hizi ni wa kweli na unapaswa kuthaminiwa zaidi kuliko ule wa wale wanaotangaza maoni yao. Maoni yanayoundwa na mke wako yana ushawishi mkubwa katika akili yako. Mara nyingi unachukulia kawaida kuwa yeye yuko sahihi, hivyo unafikiria kama anavyofikiria na kutenda katika maswala ya kanisa. {1T 627.1}

Lazima uwe mfano wa maisha ya Kristo, kwa maana una majukumu mazito juu yako. Mke wako anawajibika kwa MUNGU kwa mwenendo wake. Ikiwa yeye ni kikwazo kwako lazima atoe hesabu kwa MUNGU. Wakati mwingine anazinduka na kujinyenyekeza mbele za MUNGU  na ni msaada wa kweli; lakini hivi punde anarudi katika hali ile ile ya kutofanya kazi, akikwepa majukumu, na kuweka udhuru kwa kazi ya akili na ya mwili. Afya yake ingekuwa bora zaidi ikiwa angefanya kazi zaidi, ikiwa angeshirikiana kwa uchangamfu na kwa moyo wote katika kazi ya mwili na akili. Si kwamba hana uwezo, bali tabia ya kutenda ndiyo hana; hatavumilia kukuza upendo wa kufanya shughuli. MUNGU  hawezi kumfanyia chochote katika hali yake ya sasa. Ana kitu cha kufanya ili kuzinduka na kuzitoa nguvu zake za mwili na akili kwa MUNGU. MUNGU analihitaji hili kwake, na katika siku ya MUNGU  ataonekana kama mtumishi asiye na faida endapo hatafanya matengenezo kamili na kuishi kulingana na nuru aliyopewa. Mpaka matengenezo haya yatakapofanyika, hatakiwi kuungana kabisa na mumewe katika kazi zake. {1T 627.2}

MUNGU atambariki na kumdumisha kaka F ikiwa atasonga mbele kwa unyenyekevu, akitegemea uamuzi wa watumishi wenzake wenye uzoefu.  {1T 628.1}

## SURA YA 108

## USIDANGANYIKE

Ni kazi ya Shetani kuwadanganya watu wa MUNGU na kuwaongoza kutoka kwenye njia sahihi. Hakuna njia ambayo hataijaribu; atakuja kwao wakati ambao wamelegeza ulinzi; kwa hivyo kuna umuhimu wa kuimarisha ngome kila hatua. Kanisa la Battle Creek halikumaanisha kwenda kinyume nasi, ni kanisa zuri kama wanavyoishi; lakini kuna hatari kubwa huko Battle Creek, na Shetani ataleta silaha zake zote dhidi yao ikiwa kwa kufanya hivyo anaweza kuzuia kazi hiyo. Tunalihurumia sana kanisa hili katika hali yao ya unyenyekevu ya sasa na tunasema: Hebu roho ya ushindi isiinuke katika moyo wa yeyote. MUNGU

atayaponya makosa yote ya watu hawa wapendwa na kuwafanya kuwa watetezi wakubwa wa Ukweli Wake ikiwa watatembea kwa unyenyekevu na kuangalia na kulinda kila hatua dhidi ya mashambulio ya Shetani. Watu hawa huwekwa chini ya moto wa adui. Hakuna kanisa lingine ambalo lingeweza kusimama vile vile, kwa hivyo watazame kwa jicho la huruma ndugu zako walioko huko Battle Creek na umwombe MUNGU awasaidie katika kulinda ngome. {1T 628.2}

Wakati mume wangu alipokuwa hafanyi kazi, mimi nilikuwa nabaki nyumbani kwa sababu yake, Shetani alifurahi, na hakuna mtu aliyeshinikizwa naye kutuletea majaribu kama yale yaliyotajwa katika kurasa zilizotangulia. Lakini tulipoanza, Desemba 19, 1866, aliona kwamba kulikuwa na matarajio ya kufanya kitu katika kazi ya Kristo na kuijeruhi kazi yake na kwamba udanganyifu wake juu ya kundi la MUNGU ungefunuliwa. Kwa hivyo alihisi ameitwa kufanya kitu kutuzuia. Na kwa njia yoyote hakuweza kufanya hivyo kwa ufanisi kama katika kuwaongoza marafiki zetu wa zamani huko Battle Creek kuondoa huruma zao na kutupa mizigo juu yetu. Alitumia fursa ya kila hali mbaya na akaendesha mambo kwa nguvu kubwa kama ya mvuke. {1T 629.1}

Lakini, asante MUNGU, hakutuacha wala kutuponda kabisa. Asante MUNGU kwa kuwa bado tunaishi na kwamba amerudi kwa neema kuwabariki wakosaji Wake, lakini sasa ni watu wanaotubu, wanaokiri. Ndugu zangu, hebu tuwapende zaidi na tuwaombee zaidi sasa kwa kuwa MUNGU anaonesha upendo wake mkuu kwao. {1T 629.2}

## SURA YA 109

## KUCHAPISHA USHUHUDA BINAFSI

Katika Ushuhuda Na. 13 nilitoa maelezo mafupi ya kazi na majaribu yetu kutoka Desemba 19, 1866, hadi Oktoba 21, 1867. Katika kurasa hizi nitaelezea uzoefu wa miezi mitano iliyopita usiokuwa na maumivu makubwa. {1T 630.1}

Katika kipindi hiki nimeandika shuhuda nyingi binafsi. Na kwa watu wengi ambao nimekutana nao katika eneo letu la kazi katika miezi mitano iliyopita bado nina shuhuda za kuandika ninapopata muda na nguvu, lakini jukumu langu kuhusiana na shuhuda hizi binafsi kwa muda mrefu limekuwa ni jambo lenye wasiwasi mkubwa kwangu. Isipokuwa kwa wachache ambao nimewatuma kwa wale walio waelezea na nimewaacha watu hawa wawatoe kama walivyochagua. Matokeo yamekuwa yafuatayo: {1T 630.2}

- Wengine wamepokea shukrani hizo na wamezijibu kwa roho nzuri na wamefaidika nazo. Hawa wamekuwa tayari kwamba ndugu zao waweze kuziona shuhuda na wamekiri makosa yao kwa uhuru na ukamilifu. {1T 630.3}
- Wengine wamekiri kwamba shuhuda hizo kwao zilikuwa za kweli, lakini baada ya kuzisoma wameziweka mbali na kukaa kimya, na wameishia kufanya mabadiliko kidogo sana katika maisha yao. Ushuhuda huu ulihusiana zaidi au kidogo na makanisa ambayo watu hawa walikuwemo, ambayo yangeweza pia kufaidishwa nao. Lakini yote haya yalipotea kwa sababu ya ushuhuda huu kushikiliwa kibinafsi/faragha. {1T 630.4}
- Bado wengine wameasi dhidi ya shuhuda. Baadhi yao wamejibu kwa roho ya kutafuta makosa. Wengine wameonesha uchungu, hasira, na ghadhabu, na malipo ya taabu yangu na maumivu yangu kwa kuandika shuhuda hizi, wametugeukia na kutujeruhi kadri walivyoweza; wakati wengine wamenishikilia kwa masaa kadhaa katika mahojiano binafsi kumimina katika masikio yangu na moyo wangu wenye maumivu malalamiko yao, manung'uniko, na kujihesabia haki, na pengine waksihi huruma zao wenyewe kwa kulia, na kushindwa kuona makosa na dhambi zao. Ushawishi wa mambo haya umekuwa mbaya juu yangu na wakati mwingine umenisukuma na kukaribia uharibifu wangu. Yale ambayo yamefuatia mwenendo wa hawa watu wasio wakfu, wasio na shukrani yamenigharimu mateso zaidi na yameharibu ujasiri wangu na afya yangu mara kumi kuliko kazi yote ya kuandika shuhuda. {1T 631.1}

Na haya yote nimeyavumilia, wala kaka na dada zangu kwa ujumla hawajui chochote juu ya haya. Hawakuwa na wazo lolote juu ya kiasi cha uchovu wangu ambao nililazimika kuwa nao, wala mizigo na mateso yaliyotupwa juu yangu isivyo haki. Nimetoa taarifa binafsi katika shuhuda zangu kadhaa, na wakati mwingine watu wamekerwa kwa sababu sikuchapishia taarifa zote kama hizo. Kwa sababu ya idadi yao hili lisingewezekana, na ingekuwa mbaya kutokana na ukweli kwamba baadhi yao yanahusiana na dhambi ambazo hazihitaji, na hazipaswi kuwekwa wazi. {1T 631.2}

Lakini mwishowe nimeamua kwamba sehemu kubwa ya hizi shuhuda binafsi inapaswa kuchapishwa, kwani zote zina maonyo na maelekezo mengi au machache ambayo yanahusu mamia au maelfu ya wengine walio katika hali kama hiyo. Hawa wanapaswa kuwa na nuru ambayo MUNGU ameona vema kuwapatia kwa kuwa inakidhi matatizo yao. Ni makosa kuifunga kutoka kwao kwa kuipeleka kwa mtu mmoja au sehemu moja, ambapo huwekwa kama taa

chini ya pishi. Usadikisho wangu wa wajibu juu ya hatua hii umeimarishwa sana na ndoto ifuatayo: {1T 631.3}

Bustani ya miti ya matunda ya kijani kibichi iliwasilishwa mbele yangu. Watu kadhaa, pamoja na mimi, walikuwa wakifanya kazi ndani yake. Niliagizwa kuikagua miti hiyo kwa ukaribu na kuona kama iko katika hali nzuri. Niliona kwamba mingine ilikuwa imeinama na kuharibiwa na upepo, na ilihitaji kusaidiwa na egemeo. Nilikuwa nikiondoa kwa uangalifu uchafu kutoka kwenye miti dhaifu na inayokufa ili kujua sababu ya hali yao. Niligundua minyoo kwenye mizizi ya baadhi ya miti. Mingine ilikuwa haijamwagiliwa maji vizuri na ilikuwa inakufa kutokana na ukame. Mizizi ya miti mingine ilikuwa imesongamana pamoja na kuumizana. Kazi yangu ilikuwa kuwaelezea watendakazi sababu tofauti kwanini miti hii haikufanikiwa. Hili lilikuwa muhimu kutokana na ukweli kwamba miti katika maeneo mengine ilikuwa katika uwezekano wa kuathiriwa kama hii ilivyokuwa, na sababu ya kutokustawi kwao na jinsi inavyopaswa kulimwa na kuhudumiwa lazima zifahamike. {1T 632.1}

Katika ushuhuda huu nazungumza kwa uhuru juu ya kisa cha dada Hannah More, siyo kutoka katika nia ya kulihuzunisha kanisa la Battle Creek, bali kutoka katika hisia ya wajibu. Nalipenda kanisa hilo bila kujali makosa yao. Silijui kanisa linalofanya vizuri sana katika vitendo vya ukarimu na wajibu wa jumla. Nawasilisha Ukweli wa kutisha katika kesi hii ili kuwaamsha watu wetu kila mahali katika hisia ya wajibu wao. Hakuna hata mmoja kati ya ishirini (1/20) ya wale ambao wana msimamo mzuri na Waadventista wa Sabato anayeishi kanuni za Neno la MUNGU za kujikana nafsi. Lakini hebu wasiwaruhusu maadui zao, ambao wamekosa kanuni za kwanza za mafundisho ya Kristo, kuchukua faida ya Ukweli kwamba wamekemewa. Huu ni ushahidi kuwa wao si watoto wa Bwana (watoto haramu). Wale wasiokemewa, anasema mtume, ni wana haramu siyo wana. Basi hebu watoto hawa haramu wasijisifu juu ya wana na binti halali wa Mwenyezi. {1T 632.2}

## SURA YA 110

## TAASISI YA AFYA

Katika nambari za shuhuda kwa kanisa zilizopita nimezungumza juu ya umuhimu wa Waadventista Wasabato kuanzisha taasisi kwa faida ya wagonjwa, haswa kwa watu wanaoteseka na wagonjwa miongoni mwetu. Nimezungumza juu ya uwezo wa watu wetu, kwa maana ya rasilimali, kufanya hivi; na nimehimiza kwamba, kwa kuzingatia umuhimu wa tawi hili la kazi kubwa ya maandalizi ya kukutana na Bwana, tukiwa na moyo wenye furaha, watu wetu wanapaswa kuhisi kuwa wameitwa, kulingana na uwezo wao, kuweka sehemu ya mali zao katika taasisi. Nimeelezea pia, kama nilivyooneshwa, baadhi ya

hatari ambazo matabibu, wasimamizi, na wengine wangekabiliana nazo katika kuandaa taratibu za kisheria za mradi huo; na nilitumaini kwamba hatari zilizooneshwa zingeepukwa. Katika hili, hata hivyo, nilifurahia tumaini la muda ila nikaingia katika kukatishwa tamaa na huzuni. {1T 633.1}

Nilivutiwa sana na matengenezo ya afya na nilikuwa na matumaini makubwa ya ustawi wa Taasisi ya Afya. Nilihisi, kama hakuna mtu yeyote anayeweza kuhisi, jukumu la kuongea na kaka na dada zangu katika Jina la Bwana kuhusu taasisi hii na jukumu lao kutoa fedha/mahitaji muhimu, na niliangalia maendeleo ya kazi hiyo kwa hamu kubwa na shauku. Nilipoona wale waliosimamia na kuelekeza, wakikimbilia katika hatari nilizooneshwa, ambazo nilikuwa nimewaonya hadharani na pia katika mazungumzo ya faragha na barua, mzigo mzito ulinilemea. Mahali hapo palipooneshwa kwangu kama mahali ambapo wagonjwa wanaoteseka kati yetu wangeweza kusaidiwa ni ndipo ambapo kujitoa, ukarimu, imani, na uchaji vinapaswa kuwa kanuni zinazotawala. Lakini wakati miito isiyo na sifa ilipotengeneza fedha nyingi, wakati taarifa kwamba hisa iliyotwaliwa, itawalipa kwa asilimia kubwa; wakati ambapo ndugu waliokuwa katika nyadhifa kwenye taasisi hiyo walionekana kuwa tayari kuchukua mshahara mkubwa kuliko wale walioridhika na kufanya kazi yenye umuhimu sawa kwenye kusudi kuu la Ukweli na matengenezo; nilipojifunza, kwa uchungu, kwamba, ili kuifanya taasisi hiyo ipendwe/maarufu na wale wasio wa imani yetu na kupata msaada wao, roho ya maridhiano ilikuwa ikiingia kwa kasi sana katika Taasisi, na ilidhihirishwa na matumizi ya Bwana, Binti, na Bibi, badala ya Ndugu na dada, na katika starehe maarufu/matumbuizo, ambazo wote wangeweza kushiriki katika hali ya kutokuwa na hatia - nilipoona mambo haya, nikasema: Hii siyo ile ambayo nilioneshwa kama taasisi ya wagonjwa ambayo ingeshiriki ishara ya Baraka za MUNGU. Hiki ni kitu kingine. {1T 633.2}

Na bado mahesabu ya majengo makubwa zaidi yalifanywa, na wito kwa ajili ya pesa nyingi ulihimizwa. Kama ilivyosimamiwa wakati huo, ningeweza kuiona Taasisi, kwa ujumla, kama laana. Ingawa wengine walifaidika kiafya, ushawishi kwa kanisa huko Battle Creek na juu ya kaka na dada walioitembelea Taasisi hiyo ulikuwa mbaya sana kuzidi mema yote yaliyofanyika kwa ujumla; na ushawishi huu ulikuwa ukifikia makanisa katika jimbo hili na mengine, na ulikuwa mbaya sana dhidi ya imani kwa MUNGU  na Ukweli wa sasa. Watu kadhaa ambao walikuja Battle Creek wakiwa wanyenyekevu, Wakristo waliojitoa, na waaminifu, waliondoka wakiwa wamekaribia kuwa makafiri. Ushawishi wa jumla wa mambo haya ulikuwa unaleta chuki dhidi ya matengenezo ya afya miongoni mwa wanyenyekevu walio wengi, waliojitoa sana, na walio bora zaidi kati ya ndugu zetu, na ilikuwa ikiharibu imani katika shuhuda zangu na katika Ukweli wa sasa. {1T 634.1}

Ilikuwa ni katika hali hii ya mambo kuhusiana na matengenezo ya afya na Taasisi ya Afya, ambapo vitu vingine vililetwa, ambavyo vilipelekea jukumu

langu la kuongea kama nilivyofanya katika Ushuhuda namba 13. Nilijua vizuri kuwa hilo litaleta athari na jaribu katika akili nyingi. Nilijua pia kuwa mwitikio lazima uje mapema au baadaye, na, kwa faida ya Taasisi na kazi kwa ujumla, mapema ni bora zaidi. Endapo mambo yangekuwa yakielekea katika mwelekeo mbaya, kwa kuziumiza roho za thamani na kazi kwa ujumla, hili lingechunguzwa mapema zaidi, lingeweza kuelekezwa vizuri zaidi. Kadri linavyoendelea mbele, ndivyo uharibifu unavyozidi kuwa mwingi, mwitikio unakuwa mkubwa, na hali ya kukata tamaa kwa ujumla. Kazi ambayo haikuelekezwa vizuri lazima ichunguzwe na kusimamishwa; lazima kuwe na wakati wa kusahihisha makosa na kuanza tena katika mwelekeo sahihi. {1T 634.2}

Kazi nzuri iliyofanywa kwa ajili ya kanisa huko Battle Creek kabla ya kuanguka, mategenezo kamili na matabibu, wasaidizi, na wasimamizi katika Taasisi ya Afya kumgeukia Bwana, na makubaliano ya jumla ya kaka na dada zetu katika sehemu zote za kazi kulingana na kusudi kubwa la Taasisi ya Afya na namna inayopaswa kuendeshwa, ambayo yanaongeza uzoefu kadhaa wa zaidi ya mwaka mmoja, siyo tu kwa njia mbaya, bali pia katika mwelekeo sahihi, hii inanipa ujasiri zaidi kuwa matengenezo ya afya na Taasisi ya Afya vitathibitisha mafanikio kuliko niliyokuwa nayo hapo awali. Bado nina tumaini kubwa kuona Taasisi ya Afya huko Battle Creek ikifanikiwa na katika kila nyanja iliyooneshwa na taasisi. Lakini itachukua muda kusahihisha kikamilifu na kumaliza kabisa makosa ya zamani. Kwa baraka za MUNGU hili linaweza kufanyika na litafanyika. {1T 635.1}

Ndugu ambao wamesimama kama wakuu wa kazi hii wametoa wito kwa watu wetu kwa ajili ya fedha, kwa msingi kwamba matengenezo ya afya ni sehemu ya kazi kubwa iliyounganishwa na ujumbe wa malaika wa tatu. Katika hili wamekuwa sahihi. Ni tawi la kazi kubwa, ya hisani, ya ukarimu, ya kujitolea, ya fadhili za MUNGU. Basi kwa nini hawa ndugu waseme: "Hisa zilizo katika Taasisi ya Afya zitalipa kwa asilimia kubwa," "ni uwekezaji mzuri," "kitu kinacholipa"? Kwa nini hakuna mazungumzo ya hisa inayolipa asilimia kubwa katika Nyumba ya cha Uchapishaji? Ikiwa haya ni matawi mawili ya kazi hiyo hiyo kubwa, kazi ya mwisho ya maandalizi ya kuja kwa Mwana wa Adamu, kwa nini isiwe hivyo? Au kwanini yote mawili yasifanywe kuwa mambo ya ukarimu? Kalamu na sauti ambazo ziliwavutia marafiki wa kazi hiyo kwa niaba ya mfuko wa uchapishaji haikuonesha vishawishi kama hivyo. Kwa nini, basi, niwakilishe kwa watunza Sabato matajiri, wenye choyo ili waweze kufanya vizuri sana kwa kuwekeza mali zao katika Taasisi ya Afya, na wakati huo huo wabakishe mtaji/kianzio, na kisha wapate asilimia kubwa kwa matumizi hayo rahisi? Ndugu waliombwa kutoa fedha kwa ajili ya Chama cha Uchapishaji, na walijitolea kwa hiari na kwa furaha katika Bwana, wakifuata mfano wa yule aliyetoa wito huo, na baraka za MUNGU zimekuwa juu ya tawi hilo la kazi kubwa. Lakini inapaswa kuogopwa kwamba hasira ya Bwana iko katika kusudi ambalo fedha hizo

zimekusanywa kwa ajili ya Taasisi ya Afya, na kwamba baraka ZAKE hazitakuwa juu ya taasisi hiyo kikamilifu, mpaka kosa hili litakaposahihishwa. Katika wito wangu kwa ndugu kwa niaba ya taasisi kama hiyo, katika Ushuhuda Nambari 11, ukurasa wa 492, nilisema: {1T 635.2}

"Nilioneshwa kuwa hakuna ukosefu wa mali kati ya Waadventista wa Sabato. Kwa sasa hatari yao kubwa ni katika kujilimbikizia mali zao. Wengine wanaendelea kuongeza masumbufu yao na mahangaiko; wanafanya kazi kupita kiasi. Matokeo yake ni kwamba, wamemsahau MUNGU  na mahitaji ya kazi Yake; wamekufa kiroho. Wanatakiwa kutoa dhabihu kwa MUNGU, sadaka. Dhabihu haiongezeki, lakini hupungua na kuteketea." {1T 636.1}

Maoni yangu kuhusu suala hili la mali yalikuwa kwamba kunapaswa kuwa na "dhabihu kwa MUNGU, sadaka;" na sikuwahi kupokea wazo lingine lolote. Lakini ikiwa kianzio kitashikiliwa vizuri na wenye hisa, wakapata asilimia fulani, upungufu uko wapi, au dhabihu ya kuteketeza? Na zipi ni hatari za wale watunza Sabato ambao wanakusanya mali zilizopunguzwa na mpango wa sasa wa kushikilia hisa katika Taasisi? Hatari zao zinaongezeka tu. Na hapa kuna udhuru wa ziada kwa sababu ya tamaa yao ya fedha. Katika kuwekeza kwenye hisa ndani ya Taasisi, kulikofanyika kama suala la kuuza na kununua kama mali nyingine yoyote, hawatoi dhabihu. Kama asilimia kubwa inaonekana kama ushawishi, roho ya faida, isiyo ya kujikana, na hii inawaongoza kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika hisa ya Taasisi kiasi kwamba wanabakiza kidogo tu cha kutoa ili kuendeleza matawi mengine ya muhimu zaidi katika kazi. MUNGU anataka watu hawa wa siku za mwisho, wenye uroho wa mali, wenye mawazo ya kidunia wawe dhabihu kwa wanadamu wanaoteseka. Yeye Anawataka waziache mali zao za kidunia zipungue kwa sababu ya wale walioteseka ambao wanaamini katika Yesu na Ukweli wa sasa. Wanapaswa kuwa na nafasi ya kuchukua hatua katika mtazamo kamili wa maamuzi ya hukumu ya mwisho, kama ilivyoelezewa katika Maneno yafuatayo ya Mfalme wa wafalme: {1T 636.2}

Mathayo 25: 34-46: "Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono Wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia. Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi." {1T 637.1}

"Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake; kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu, msininyweshe; nalikuwa mgeni, msinikaribishe; nalikuwa uchi, msinivike; nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama. Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona wewe Una njaa, au Una kiu, au U mgeni, au U uchi, au U mgonjwa, au U kifungoni, tusikuhudumie? Naye atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kadri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea Mimi. Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele. "{1T 637.2}

Kisha kwenye ukurasa wa 494 wa Ushuhuda Na. 11, nilisema: "Kuna mali nyingi kati ya watu wetu, na kama wote wangehisi umuhimu wa kazi, mradi huu mkubwa unaweza kuendelea bila aibu. Wote wanapaswa kujisikia utayari maalum katika kuiendeleza. Hasa wale ambao wana uwezo wawekeze katika mradi huu. Nyumba sahihi inapaswa kuwekwa kwa ajili ya kupokea wagonjwa na vilema wanaoweza kuja, kwa kutumia njia sahihi na baraka za MUNGU, wapate nafuu ya udhaifu wao na kujifunza jinsi ya kujitunza ili kuepukana na magonjwa. {1T 638.1}

"Wengi wanaodai kuuamini Ukweli wanaongezeka katika tamaa ya mali na ubahili. Wanahitaji kushtushwa kwa ajili yao wenyewe. Wana hazina nyingi duniani kiasi kwamba mioyo yao iko kwenye hazina zao. Sehemu kubwa ya hazina zao iko katika ulimwengu huu, na kidogo mbinguni, kwa hivyo mapenzi yao yamewekwa kwenye mali za dunia badala ya urithi wa mbinguni. Sasa kuna fursa nzuri kwao kutumia mali zao kwa faida ya wanadamu wanaoteseka na pia kwa maendeleo ya Ukweli. Mradi huu haupaswi kamwe kuachwa upambane na umaskini. Mawakili hawa ambao MUNGU amewapatia dhamana lazima sasa waje kufanya kazi na watumie mali zao kwa utukufu Wake. Kwa wale ambao kwa uchoyo wanazizuia mali zao, hilo litathibitisha laana badala ya baraka. " {1T 638.2}

Katika kile nilichooneshwa na kile nilichosema, sikupokea wazo lingine, na ilikusudiwa lisiwepo lingine, isipokuwa la kuchanga/kukusanya pesa kwa ajili ya tawi hili la kazi lilikuwa jambo la ukarimu, vivyo hivyo kwa ajili ya msaada wa matawi mengine ya kazi kubwa. Na ingawa mabadiliko kutoka katika mpango wa sasa kwenda kwenye ule unaoweza kupitishwa kikamilifu na Bwana unaweza kukumbwa na shida na kuhitaji muda na nguvu, lakini nadhani hili linaweza kufanywa na upotezaji mdogo wa mali iliyochukuliwa tayari, na kwamba hili litasababisha ongezeko la mtaji uliotolewa kutumika kwa njia inayofaa kuuletea unafuu ubinadamu unaoteseka. {1T 638.3}

Wengi ambao wamechukua hisa hawawezi kuchangia. Baadhi ya watu hawa wanateseka kwa pesa ambazo wameziwekeza kwenye hisa. Ninaposafiri kutoka jimbo hadi jimbo, naona watu walioteseka wakiwa wamesimama wakichungulia kaburi, ambao wanapaswa kwenda kwenye Taasisi hiyo ya Sanitarium kwa

muda, lakini hawawezi kwa kukosa fedha walizo nazo katika hisa za Taasisi. Hawa hawapaswi kuwekeza hata dola moja hapo. Kesi moja huko Vermont nitaitaja. Mapema mnamo 1850 ndugu huyu alikuwa Mtunza Sabato, na kuanzia tarehe hiyo alichangia kwa hiari katika miradi kadhaa ambayo imefanywa ili kuendeleza kazi hiyo, mpaka akapungukiwa mali. Lakini wakati wito wa dharura, usiostahili ulipokuja kwenye Taasisi, alichangia hisa cha dola mia moja. Kwenye mkutano huko ----- alianzisha kesi ya mkewe, ambaye ni dhaifu sana, na ambaye anaweza kusaidiwa, lakini sharti asaidiwe upesi zaidi. Aliielezea pia hali yake, na akasema kwamba kama angeweza kuagiza dola mia moja kutoka katika Taasisi, basi angeweza kumpeleka mkewe huko kutibiwa; lakini kama ilivyokuwa, hakuweza. Tulijibu kwamba hakupaswa kuwekeza hata dola moja katika Taasisi, na kwamba kulikuwa na makosa katika jambo ambalo tusingeweza kusaidia, na hapo suala hilo lilishindikana. Sisiti kusema kwamba dada huyu anapaswa kutibiwa, kwa wiki chache, katika Taasisi hiyo bila malipo. Mumewe anaweza tu kulipa nauli yake kwenda na kutoka Battle Creek. {1T 639.1}

Marafiki wa ubinadamu, Ukweli na utakatifu, wanapaswa kutenda kwa kuzingatia Taasisi juu ya mpango wa kujitolea na ukarimu. Nina dola mia tano ya hisa katika Taasisi, ambayo ninataka kuchangia, na ikiwa mume wangu atafaulu na kitabu chake kinachotarajiwa, atatoa dola mia tano zaidi. Wale ambao watakubali mpango huu tafadhali wawasiliane nasi huko Greenville, Wilaya ya Montcalm, Michigan, na waeleze kiasi ambacho wanataka kuchangia, au kuwekeza katika hisa itakayofanyika kama vile hisa katika Chama cha Uchapishaji ilivyofanyika. Wakati hili linapofanyika, basi hebu michango iingie kama inavyohitajika; hebu jumla  ya pesa ndogo na kubwa ziingie. Hebu fedha zitumiwe kwa busara. Hebu malipo ya wagonjwa yawe ya kawaida kadri iwezekanavyo. Hebu ndugu wachangie kulipia kwa sehemu gharama katika Taasisi za wale wanaoteseka na maskini miongoni mwao. Hebu watu walio dhaifu waongozwe, kadri wanavyoweza kuvumilia, kulima ekari nzuri zilizomilikiwa na Taasisi. Hebu wasilifanye hili kwa fikra finyu za malipo, bali kwa wazo jema kwamba gharama ya ununuzi wao lilikuwa suala la ukarimu kwa faida yao wenyewe. Hebu kazi yao iwe sehemu ya maagizo yao ya tiba kama vile kuoga (hydrotherapia treatment). Hebu ukarimu, upendo, ubinadamu, kujitoa kwa faida ya wengine, yawe mawazo yanayowatawala matabibu, wasimamizi, wasaidizi, wagonjwa, na marafiki wote wa Yesu, walio mbali na karibu, badala ya mshahara, uwekezaji mzuri, na kitu kinacholipa, hisa inayolipa. Hebu upendo wa Kristo, upendo kwa roho, huruma kwa wanadamu wanaoteseka, vitawale yale tunayosema na kufanya kulingana na Taasisi ya Afya. {1T 639.2}

Kwa nini tabibu aliye Mkristo, anayeamini, anayetarajia, anayekesha, kungojea, na kutamani ujio wa Kristo na ufalme wake, wakati ambapo ugonjwa na kifo havitakuwa na nguvu tena juu ya watakatifu, atarajie kulipwa zaidi kwa

huduma zake kuliko mhariri au mchungaji wa Kikristo? J Anaweza kusema kuwa kazi yake inachosha zaidi. Hilo bado halijathibitishwa. Hebu afanye kazi kwa kadri awezavyo kuvumilia, na siyo kukiuka sheria za afya/uhai anazowafundisha wagonjwa wake. Hakuna sababu nzuri kwa nini anapaswa kufanya kazi kupita kiasi na kupokea malipo makubwa, kuliko mchungaji au mhariri. Hebu wote wanaoshiriki katika Taasisi na wapokee malipo ya huduma zao, wafanye kwa kanuni sawa ya ukarimu. Hakuna mtu anayepaswa kuvumilia kubaki kama msaidizi katika Taasisi ambaye hufanya hivyo kwa ajili ya malipo tu. Wapo wale wenye uwezo ambao, kwa ajili ya upendo wa Kristo, na kazi Yake, na wafuasi wa Bwana wao wanaoteseka, watajaza vituo katika Taasisi hiyo kwa uaminifu na uchangamfu, na kwa roho ya kujitolea. Wale ambao hawana roho hii wanapaswa kuondoka na kuwapa nafasi wale walio nayo. {1T 640.1}

Kadri ambavyo naweza kuhukumu, nusu ya watu walio na shida miongoni mwa watu wetu ambao wanapaswa kutumia wiki au miezi katika Taasisi hawawezi kulipia gharama yote ya safari na kukaa huko. Je! Umaskini utawazuia hawa marafiki wa Bwana wetu na baraka ambazo amezitoa kwa ukarimu? Je! Wataachwa wapambane mara mbili na mizigo ya udhaifu na umaskini? Wale matajiri dhaifu, ambao wana raha na starehe zote za maisha, na wana uwezo wa kuajiri watu, ili kazi zao ngumu zifanyike, hebu kwa masumbufu na pumziko, kwa kuwataarifu na kuchukua matibabu nyumbani, wafurahie hali nzuri ya kiafya bila kwenda kwenye Taasisi. Lakini hawa kaka au dada zetu maskini, dhaifu wanaweza kufanya nini ili kupata afya? Wanaweza kufanya kitu, lakini umasikini unawapelekea kufanya kazi zaidi ya vile wanavyoweza. Hawana hata starehe zote za maisha-hawana cha kupunguza masumbufu ya maisha; na kwa ajili ya unafuu katika nyumba zao, fanicha, bafu kwaajili ya hydrotherapia, na mipangilio ya uingizaji mzuri wa hewa, hawana. Pengine chumba chao pekee ndicho chenye jiko la kupika, msimu wa baridi na msimu wa joto; na huenda vitabu vyote walivyo navyo nyumbani, isipokuwa Biblia, vingeweza kushikiliwa katikati ya kidole gumba na kidole shahada. Hawana pesa za kununua vitabu ambavyo wanaweza kuvisoma na kujifunza jinsi ya kuishi. Ndugu hawa wapendwa ndio walengwa haswa, wanaohitaji msaada. Wengi wao ni Wakristo masikini na wanyenyekevu. Wanaweza kuwa na makosa, na baadhi ya hawa wanaweza kuwa walifika mbali zaidi na kuwa sababu ya umaskini wao wa sasa na shida walizonazo. Lakini bado wanaweza kuishi vema kwa ajili ya jukumu kuliko sisi ambao tuna uwezo wa kuboresha hali zetu na za wengine. Hawa lazima wafundishwe kwa subira na wasaidiwe kwa furaha. {1T 641.1}

Lakini lazima wawe tayari na wenye shauku ya kufundishwa. Lazima wathamini roho ya shukrani kwa MUNGU kwa ndugu zao kwa msaada wanaopokea. Watu kama hawa kwa ujumla hawana ufahamu wa gharama halisi ya matibabu, bodi, chumba, mafuta, nk, katika Taasisi ya Afya. Hawatambui ukubwa wa kazi hii kubwa ya Ukweli wa sasa na matengenezo, na kuna miito mingi ya kutaka ukarimu wa watu wetu. Wanaweza wasijue kwamba idadi ya maskini wetu ni

kubwa mara nyingi kuliko idadi ya matajiri wetu. Na hawawezi pia kuhisi nguvu ya Ukweli wa kutisha kwamba matajiri hawa wengi wanashikilia utajiri wao na wako katika barabara ya uhakika ya upotevu. {1T 641.2}

Watu hawa masikini wanaosumbuliwa na magonjwa, wanapaswa kufundishwa kwamba wakati wanaponung'unika katika wingi wao dhidi ya matajiri kwa sababu ya tamaa yao, wanafanya dhambi kubwa mbele za mbingu. Kwanza wanapaswa kuelewa kuwa ugonjwa wao na umasikini ni mabalaa ambayo kwa kawaida yanasababishwa na dhambi zao, upumbavu na makosa yao; na kama Bwana anaruhusu ndani ya mioyo na akili za watu Wake ili kuwasaidia, ndani yao haya yanapaswa kuhamasisha hisia za shukrani na unyenyekevu kwa MUNGU na watu Wake. Wanapaswa kufanya yote yaliyo katika uwezo wao kujisaidia. Ikiwa wana ndugu ambao wanaweza na watalipia gharama zao katika Taasisi, hawa wanapaswa kupewa upendeleo. {1T 642.1}

Na kwa mtazamo wa watu wengi masikini na wanaoteswa ambao lazima, kwa kiwango kikubwa au kidogo, kuwa walengwa wa huduma ya tiba katika Taasisi, na kwa sababu ya ukosefu wa fedha na uhitaji wa makazi kwa wakati huu, ukaaji wa watu kama hao katika Taasisi lazima uwe wa muda mfupi. Wanapaswa kwenda huko na wazo la kupata kwa haraka sana na kwa kadri iwezekanavyo, maarifa ya vitendo ya kile wanachopaswa kufanya, na kile wasichopaswa kufanya, kurejesha afya, kupona na kuishi kwa afya. Masomo/mihadhara wanayoyasikia wakiwa katika Taasisi, na vitabu vizuri ambavyo wanaweza kujifunza jinsi ya kuishi nyumbani, lazima viwe tegemeo kubwa kwao. Wanaweza kupata ahueni kwa majuma machache waliyokuwepo katika Taasisi, lakini watagundua zaidi wakiwa nyumbani watakapoendeleza kanuni hizo hizo. Hawapaswi kuwategemea matabibu kuwaponya katika majuma machache, bali lazima wajifunze kuishi ili kuipatia asili nafasi kushughulikia uponyaji na tiba. Hili linaweza kuanza ndani ya majuma machache katika Taasisi, na bado inaweza kuhitaji miaka kukamilisha kazi hiyo ya tabia sahihi nyumbani. {1T 642.2}

Mtu anaweza kutumia kila kitu alichonacho katika ulimwengu huu kwenye Taasisi ya Afya, na kupata nafuu kubwa, na kisha anaweza kurudi katika familia yake na tabia zake za zamani za maisha, na katika majuma au miezi michache anakuwa katika hali mbaya ya kiafya kuliko hapo awali. Anakuwa hajapata chochote; ametumia uwezo wake mdogo bure. Lengo la matengenezo ya afya na Taasisi ya Afya siyo kama dozi ya " dawa ya kutuliza maumivu au panadol" au "Nafuu ya papo kwa papo," kutuliza maumivu ya leo. Hapana, kabisa! Lengo lake kuu ni kuwafundisha watu jinsi ya kuishi ili kuipatia asili nafasi ya kuondoa na kupinga magonjwa. {1T 643.1}

Kwa wale walioteseka miongoni mwa watu wetu napenda kusema, msikate tamaa, Msifadhaike. MUNGU hajawaacha watu Wake na kazi Yake. Wekeni wazi hali ya afya na uwezo wenu wa kukidhi gharama za kukaa katika Taasisi kwa matabibu, mkijieleza kwa Taasisi ya Afya, Battle Creek, Michigan. Je! Una ugonjwa, unaokudhoofisha, uko dhaifu, basi usichelewe mpaka tatizo lako likakosa tumaini-Nenda kwenye Sanitarium. Andika mara moja. Lakini lazima nisema tena kwa masikini: Kwa sasa kidogo kinaweza kufanyika ili kuwasaidia, kwa sababu mtaji uliopatikana tayari umewekezwa katika vifaa na majengo. Jitahidini wenyewe kadri muwezavyo, na wengine watawasaidia. {1T 643.2}

# SURA YA 111

# KIELELEZO CHA UZOEFU

Kuanzia Oktoba 21, 1867 hadi Desemba 22, 1867

Kazi yetu na kanisa la Battle Creek ilikuwa imefungwa, na licha ya kwamba tulikuwa tumechoka sana, tulikuwa tumeburudishwa moyoni tuliposhuhudia matokeo mazuri kwamba tuliungana kwa furaha na kaka J.N. Andrews katika safari ndefu ya Maine. Njiani tulifanya mkutano huko Roosevelt, New York. Ushuhuda namba 13 ulikuwa ukifanya kazi yake, na hao ndugu ambao walionesha kuwa na kinyongo kwa ujumla walikuwa wameanza kuona mambo katika nuru yao halisi. Mkutano huu ulikuwa mgumu, ambapo shuhuda dhahiri zilitolewa. Maungamo yalifanyika, yakifuatiwa na kumgeukia Bwana kwa jumla kwa wale waliorudi nyuma na wenye dhambi. {1T 643.3}

Kazi zetu huko Maine zilianza na Mkutano huko Norridgewock Novemba, moja. Mkutano ulikuwa mkubwa. Kama kawaida, mume wangu na mimi mwenyewe tulitoa ushuhuda ulio wazi na dhahiri kuhusu Ukweli na nidhamu inayofaa, na dhidi ya aina tofauti za makosa, kuchanganyikiwa, ushabiki, na machafuko yanayoongezeka kutokana na ukosefu wa nidhamu kama hiyo. Ushuhuda huu ulitumika hasa katika hali ya mambo iliyokuwa huko Maine. Roho mbaya ambazo zilidai kuitunza Sabato zilikuwa katika uasi na zilifanya kazi ya kueneza hali ya kutoridhika kupitia Mkutano huo. Shetani aliwasaidia, na walifanikiwa kwa kiwango fulani. Maelezo yanaumiza sana na yana umuhimu kidogo wa jumla wa kutolewa hapa. {1T 644.1}

Inaweza kuwa yatosha kusema kwa wakati huu kwamba matokeo ya roho hii ya uasi, kutafuta makosa, na kwa wengine, aina ya wivu wa kitoto, kunung'unika, na kulalamika, kazi yetu huko Maine, ambayo ingeweza kufanywa katika majuma mawili, ilihitaji majuma saba ya kazi ngumu zaidi, ngumu na yenye kuchosha kusikofurahisha. Majuma matano yalipotea, ndio, mbaya zaidi ya kupotea, kwa sababu huko Maine; na watu wetu katika sehemu zingine za New England, New York, na Ohio walinyimwa kufanya mikutano mikubwa mitano kwa sababu ya kushikiliwa kwetu huko Maine. Lakini tulipoondoka katika jimbo hilo tulifarijika na ukweli kwamba wote walikuwa wamekiri uasi wao, na kwamba wachache walikuwa wameongozwa kumtafuta Bwana na kuukubali ukweli. Ifuatayo kuhusiana na wachungaji, utaratibu, na mfumo ina matumizi maalum kwa hali ya mambo huko Maine. {1T 644.2}

# SURA YA 112

## WACHUNGAJI, UTARATIBU NA MFUMO (Organization)_

Wachungaji wengine wameanguka katika kosa kiasi kwamba hawawezi kuwa na uhuru wa kusema isipokuwa mpaka watumie sauti za juu na kuongea kwa kelele na kwa haraka. Hawa wanapaswa kuelewa kwamba kelele na sauti kubwa, kuongea kwa haraka siyo ushahidi wa uwepo wa nguvu ya MUNGU. Siyo nguvu ya sauti inayofanya mguso wa moyo wa kudumu kudumu. Wachungaji wanapaswa kuwa wanafunzi wa Biblia, na wanapaswa kujipatia sababu thabiti za imani na tumaini letu, na kisha, kwa udhibiti kamili wa sauti na hisia, wanapaswa kuyawasilisha haya kwa njia ambayo watu wanaweza kuwapima kwa utulivu na kuamua juu ya ushahidi uliotolewa. Na kadri wachungaji wanavyohisi nguvu ya hoja wanazowasilisha kwa njia ya Ukweli mzito unaojaribu, watakuwa na bidii na juhudi kulingana na maarifa. ROHO WA MUNGU katika nafsi zao atazitakasa Kweli ambazo wanaziwasilisha kwa wengine, na watanyeshewa wenyewe kadri wanavyowanyeshea watu wengine. {1T 645.1}

Niliona kwamba baadhi ya wachungaji wetu hawaelewi jinsi ya kuhifadhi nguvu zao ili kuweza kufanya kazi kubwa zaidi bila kuchoka. Wachungaji hawapaswi kuomba kwa sauti kubwa na kwa muda mrefu hata kuzichosha/kumaliza nguvu zao. Haina haja kuchosha koo na mapafu katika sala. Sikio la MUNGU liko wazi kila wakati kusikia maombi ya dhati ya watumishi Wake wanyenyekevu, na Yeye hawalazimishi wavichakaze viungo vyao vya sauti katika kuwasiliana Naye. Ni kuziamini, kuzitumaini kikamilifu, utegemezi thabiti, madai thabiti ya ahadi za MUNGU, imani rahisi kwamba Yeye Ndiye na kwamba Yeye ni mtoa thawabu kwa wale wote wanaomtafuta kwa bidii, ndiyo inayoshinda kwa MUNGU. {1T 645.2}

Wachungaji wanapaswa kujinidhamisha na kujifunza jinsi ya kufanya kazi kubwa zaidi katika kipindi kifupi walichopewa, na bado wahifadhi kiwango kizuri cha nguvu, ili kwamba ikiwa juhudi ya ziada itahitajika, wanaweza kuwa na akiba ya nguvu muhimu inayotosha kwa tukio hilo, ambayo wanaweza kulifanya bila kujiumiza. Wakati mwingine nguvu zote walizonazo zinahitajika kuweka bidii katika hatua fulani, na ikiwa hapo awali wamechosha nguvu zao na hawawezi kuamuru nguvu ya ziada katika kufanya juhudi hii, hivyo yote waliyoyafanya yamepotea. Wakati mwingine nguvu zote za kiakili na kimwili zinaweza kuletwa kufanya msimamo wenye nguvu kabisa, kuonesha ushahidi ulioo wazi zaidi juu ya nuru, na kuziweka mbele ya watu wito kwa njia nzuri zaidi, na kuwasihi warudi nyumbani kwa wito mkali. Kwa kuwa roho ziko katika hatua ya kuondoka katika safu ya adui na kuja upande wa Bwana, mashindano

ni makali sana na ya karibu. Shetani na malaika zake hawataki kwamba mtu yeyote ambaye ametumikia chini ya bendera ya giza achukue msimamo wake chini ya bendera yenye damu ya Mfalme Emanueli. {1T 645.3}

Nilioneshwa majeshi ya wapinzani ambayo yalikuwa yamevumilia mapambano makali kwenye vita. Ushindi haukupatikana kwa yeyote, na mwishowe waaminifu hutambua kuwa uimara na nguvu zao zimechoka, na kwamba hawataweza kuwanyamazisha maadui wao isipokuwa kama watawashtaki na kuchukua silaha vyao vya vita. Hapo ndipo, wakiwa katika hatari ya maisha yao, hutoa nguvu zao zote na kukimbia kwenda kwa adui. Ni mapambano ya kutisha; lakini ushindi unapatikana, na ngome zinachukuliwa. Ikiwa katika kipindi hiki kigumu jeshi liko dhaifu sana kwa sababu ya uchovu kiasi kwamba haiwezekani kufanya mapigano ya mwisho na kuzipiga ngome za adui, mapambano yote ya siku, juma, na hata miezi hupotea; na maisha mengi hutolewa kafara na hakuna kitu kinachopatikana. {1T 646.1}

Kazi kama hiyo iko mbele yetu. Wengi wana uhakika kwamba tuna Ukweli, lakini bado wameshikiliwa na kamba za chuma; hawathubutu kuhatarisha matokeo ya kuchukua msimamo wao upande wa Ukweli. Wengi wako katika bonde la kukata shauri, ambapo miito maalum, ya karibu, na iliyo wazi inahitajika kuwahamasisha kuvaa silaha za vita vyao na kuchukua msimamo wao upande wa Bwana. Katika kipindi hiki muhimu Shetani hutupa kamba kubwa zaidi kuzizunguka roho hizi na kuzifunga. Ikiwa watumishi wa MUNGU wote wamechoka, wametumia akiba yao ya nguvu za mwili na akili, na wanafikiri kwamba hawawezi kufanya zaidi, na mara kwa mara wakiiacha kazi jumla, ili kuanzisha shughuli mahali pengine. Na wote au karibu wote, muda, mali, na kazi zimetumika bure. Ndio, ni mbaya zaidi kuliko kama wasingeanzisha kazi mahali hapo, kwani baada ya watu kushawishiwa sana na ROHO WA MUNGU, na kuletwa kwenye hatua ya uamuzi, kisha wameachwa kupoteza shauku yao, na kuamua kinyume na ushahidi huu, hawawezi tena kuletwa kwa urahisi mahali ambapo akili zao zitasumbuka tena juu ya mada kama hiyo nyeti na kufanya uamuzi. Katika kesi nyingi wamefanya uamuzi wao wa mwisho. {1T 646.2}

Laiti kama wachungaji wangehifadhi kikosi cha akiba, na wakati ambapo kila kitu kinaonekana kuwa kigumu zaidi, basi wakafanya bidii zaidi, wito mkali, maombi ya karibu zaidi, na, kama askari hodari, wakati mgumu zaidi wakamkabili adui, wangepata ushindi. Nafsi zingekuwa na nguvu za kuvunja pingu za Shetani na kufanya maamuzi yao kwa ajili ya uzima wa milele. Kazi iliyoelekezwa vizuri kwa wakati unaofaa itafanya juhudi iliyojaribiwa kwa muda mrefu kufanikiwa, wakati ambapo kuacha kazi hata kwa siku chache katika visa vingi itasababisha kutofaulu kabisa-kufeli. Wachungaji lazima wajitolee kama wamishenari kwenye kazi hiyo na wajifunze jinsi ya kufanya juhudi zao kwa faida nzuri zaidi. {1T 647.1}

Baadhi ya wachungaji mwanzoni mwa mfululizo wa mikutano huwa na bidii sana, hubeba mizigo ambayo MUNGU hajawataka kuibeba, hutumia nguvu zao katika kuimba na kwa maombi ya muda mrefu ya sauti na kuongea, hatimaye wanachoka na kurudi nyumbani kupumzika. Kipi kimefanikiwa katika juhudi hiyo? Hakuna chochote kbaisa. Watendakazi walikuwa na roho na bidii, lakini walikosa ufahamu. Hawakuonesha kuwa na maarifa ya vita yenye busara. Walipanda gari la hisia, lakini hakukuwa na ushindi hata mmoja dhidi ya adui. Ngome yake haikuchukuliwa. {1T 647.2}

Nilioneshwa kwamba wahudumu wa Kristo wanapaswa kujiadibisha kwa ajili ya vita. Hekima kubwa inahitajika katika usimamizi kwenye jeshi la kazi ya MUNGU kuliko inavyohitajika kwa majenerali wanaohusika katika vita vya kitaifa. Watendakazi waliochaguliwa na MUNGU wanafanya kazi kubwa. Hawafanyi vita dhidi ya wanadamu, bali wanapigana na Shetani na malaika zake. Kuwa kamanda wa vita mwenye busara kunahitajika hapa-Jenerali mwenye busara. Lazima wawe wanafunzi wa Biblia wenye kujitoa kabisa kwa kazi hiyo. Wanapoanza kazi mahali, wanapaswa kuwa na uwezo wa kueleza sababu za imani yetu, siyo kwa njia ya machafuko/vurugu, siyo kwa dhoruba, bali kwa upole na hofu. Nguvu yenye ushawishi ni zile hoja zenye nguvu zinazowasilishwa kwa unyenyekevu na upole na kwa hofu ya MUNGU. {1T 647.3}

Wahudumu/wachungaji wa Kristo wenye uwezo wanahitajika kwa kazi katika siku hizi za mwisho za hatari, wenye uwezo katika Neno na mafundisho, wanaojua Maandiko, na kuelewa sababu za imani yetu. Nilielekezwa katika Maandiko haya, ambayo maana yake haijatekelezwa na baadhi ya watendakazi: "bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu. Muwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu." "Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu, mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu." "Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi; bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu; akiwaonya kwa upole wao washindanao naye, ili kama ikiwezekana, MUNGU awape kutubu na kuijua Kweli; wapate tena fahamu zao, na kutoka katika mtego wa Ibilisi, ambao hao wametegwa naye, hata kuyafanya mapenzi yake." {1T 648.1}

Mtu wa MUNGU anapaswa kukamilishwa ili apate kutenda kila tendo jema (1Timotheo 3:17). Mtendakazi mwenye majivuno/anayejigamba, anayejali cheo au wadhifa tu, haihitajiki kwa kazi hii njema. Bali tabia ifaayo ndiyo inayohitajika kazini (-mwonekano, ishara za uso na mwili, hulka, uungwana, adabu njema, kufuata protokoli na miiko muhimu ya jamii, mavazi yanayokubalika-Kingereza-decorum, etiquette, protocol -***mifano*** mtu akizungumza onyesha usikivu, salimia watu kutokana na desturi, ujue jinsi ya

kutumia maneno kama pole, samahani, asante, kumradhi, nisamehe nk, unapozungumza na watu usile jojo au kula mahindi sokoni, usikonyeze watu, usipige mluzi wa aina fulani, usikae na jinsia tofauti kwa aina ambayo italeta maswali, uwe nadhifu, usivae suruali nyekundu na shati la njano, usipakue chakula kama mlima, weka nafasi kati yako na mtu usiyemjua kama hauko kwenye msongamano, uwe mwangalifu unapozungumza na mke, mume au watoto wa watu). Mhudumu wa injili anapaswa kujali mtazamo wake (attitude). Ikiwa yeye ni mwakilishi wa Kristo, tabia yake, mtazamo wake, mwondoko wake, mwonekano, hulka, haiba, hivi vyote vinapaswa kuwa na tabia kama hiyo ambayo haitamchukiza mtazamaji (deportment). Watendakazi wanapaswa kuwa na hali ya mazoea yenye kusafishwa, staha na uungwana (no uncouth). Wanapaswa kuachana na tabia za maadili mabaya zinazochukiwa na jamii kama vile ukorofi, ishara zisizofaa, kukosa adabu, maneno ya jeuri, mitazamo miovu, na miondoko isiyofaa (No uncouth), na wanapaswa kuhamasisha ndani yao wenyewe heshima ya uvumilivu na unyeyekevu. Wanapaswa kuvikwa kwa namna inayoendana na hadhi ya nafasi yao. Hotuba yao katika kila nyanja inapaswa kuwa adhimu, yenye umakini na iliyochaguliwa vizuri. Nilioneshwa kuwa ni makosa kutoa maneno yasiyo na adabu na machafu, yasiyo ya heshima, kuelezea visa vifupi vinavoelezea mafundisho na vichekesho ili kuburudisha tu (anectode), au kuwasilisha vielelezo vya kuchekesha ili kufurahisha kama vile vya katuni/comic. Kejeli, maneno ya jeuri, kushushua na kuchezesha maneno ya mpinzani, yote haya ni nje ya utaratibu wa MUNGU. Watendakazi hawapaswi kuhisi kwamba hawawezi kufanya uboreshaji wowote wa sauti au tabia, adabu, vitendo, mazoea (manners); mengi yanaweza kufanyika. Sauti inaweza kukuzwa ili kuongea kwa muda mrefu ili usidhuru viungo vya sauti. {1T 648.2}

Wachungaji wanapaswa kupenda utaratibu na wanapaswa kujiadibisha/kujinidhamisha wenyewe, ndipo wanapoweza kufanikiwa kuliagiza kanisa la MUNGU na kuwafundisha kufanya kazi kwa mapatano ukama jeshi la askari lilioandaliwa vizuri. Ikiwa nidhamu na utaratibu ni muhimu kwa kila mafanikio kwenye uwanja wa vita, vile vile ni muhimu zaidi katika vita tunavyoshiriki kama kitu kinachopatikana ni cha thamani kubwa na kilichoinuliwa zaidi kuliko yale ambayo vikosi vya wapinzani vinashindana nayo katika uwanja wa vita. Katika mzozo tunaohusika nao, masilahi ya milele yako hatarini. {1T 649.1}

Malaika hufanya kazi kwa maelewano. Utaratibu kamili unatawala harakati zao zote. Kadri tunavyoiga kwa ukaribu maelewano na utaratibu wa jeshi la malaika, ndivyo juhudi za mawakala hawa wa mbinguni zitakavyofanikiwa zaidi kwa niaba yetu. Ikiwa hatuoni ulazima wa hatua ya maelewano, na ni wavivu, wasio na nidhamu, na wasio na mpangilio katika mwenendo wetu, malaika, ambao wamepangwa vizuri na wanafanya kwa utaratibu kamili, hawawezi

kufanya kazi kwa ajili yetu kwa mafanikio. Wanageuka kwa huzuni, kwa maana hawajaruhusiwa kubariki mikanganyiko, usumbufu, uharififu na kukosekana kwa mpangilio. Wote wanaotamani ushirikiano wa wajumbe wa mbinguni lazima wafanye nao kazi kwa umoja. Wale ambao wametiwa mafuta kutoka juu katika juhudi zao zote wanahimiza utaratibu, nidhamu, na umoja wa vitendo, ndipo malaika wa MUNGU wanaweza kushirikiana nao. Lakini kamwe, kamwe hawa wajumbe wa mbinguni hawataweka kibali/idhini yao mahali pasipo na utaratibu, pasipo na mipangilio na penye machafuko. Uovu wote huu ni matokeo ya juhudi za Shetani kudhoofisha vikosi vyetu vya jeshi, kuharibu ujasiri, na kuzuia hatua ya mafanikio. {1T 649.2}

Shetani anajua vizuri kwamba kufanikiwa kunaweza kupatikana katika utaratibu na hatua zenye maelewano. Adui anajua vizuri kwamba kila kitu kilichounganishwa na mbingu kiko katika mpangilio kamili, kwamba utii na nidhamu kamili huashiria mijongeo na harakati za jeshi la malaika. Ni juhudi yake ya bidii kuwaongoza mbali sana na mpangilio wa mbinguni kadri awezavyo wale wanaodai kuwa wakristo; kwa hiyo anawadanganya watu hata wanaojiita kuwa ni watu wa MUNGU na kuwafanya waamini kwamba utaratibu na nidhamu ni maadui wa hali ya roho, kwamba usalama wao pekee ni kumuacha kila mmoja afuate njia yake mwenyewe, na kubaki kuwa tofauti kabisa na miili ya Wakristo ambao wameungana na wanafanya kazi ili kuweka nidhamu na maelewano katika vitendo. Jitihada zote zilizofanywa za kuanzisha utaratibu zinachukuliwa kuwa ni hatari, kizuio cha uhuru halali, na kwa hivyo zinaogopwa kama taratibu za upapa. Nafsi hizi zilizodanganywa huchukulia kama fadhila kujivunia uhuru wao wa kufikiri na kutenda kwa kujitegemea. Hawatachukua maneno ya mtu yeyote “kwamba fulani kasema hivi”. Hawashauriwi na mtu yeyote, hawachuki mapendekezo, wala kuathiriwa. Nilioneshwa kuwa ni kazi maalum ya Shetani kuwaongoza watu kuhisi kwamba ni agizo la MUNGU kwao kujitahidi wenyewe na kuchagua njia yao wenyewe, bila kuwategemea ndugu zao. {1T 650.1}

Nilioneshwa nyuma kwa wana wa Israeli. Mara tu baada ya kutoka Misri walikuwa na mfumo na nidhamu kamili. MUNGU katika mipango na majaliwa Yake maalum alikuwa amemchagua Musa kusimama mbele ya majeshi ya Israeli. Alikuwa shujaa hodari katika kuongoza majeshi ya Wamisri, na katika ujenerali asingeweza kuzidiwa na mtu yeyote. Bwana hakuiacha maskani Yake takatifu ibebwe hovyo hovyo na kabila lolote analoweza kulichagua. Alikuwa mahsusi sana kwa kutaja agizo ambalo angetaka lizingatiwe wakati wa kulibeba sanduku takatifu na kuteua familia maalum ya kabila la Walawi ilibebe. Ilipokuwa kwa faida ya watu na kwa utukufu wa MUNGU kwamba wangepiga hema zao katika eneo fulani, MUNGU alionesha mapenzi yake kwao kwa kufanya nguzo ya wingu kuwa juu ya hema moja kwa moja, ambapo lilidumu mpaka atakapowafanya wasafiri tena. Katika safari zao zote walitakiwa kuzingatia utaratibu kamili. Kila kabila lilibeba kiwango chenye ishara ya

nyumba ya baba yao juu yake, na kila kabila lilihitajika kuwa chini ya kiwango chake. Sanduku lilipohama, majeshi yalisafiri, makabila tofauti tofauti yalitembea kwa utaratibu, chini ya viwango vyao. Walawi waliteuliwa na Bwana kama kabila katikati yao litakalobeba sanduku takatifu, Musa na Haruni walitembea mbele ya sanduku, na wana wa Haruni wakiwafuata karibu nao, kila mmoja akiwa na tarumbeta. Walipaswa kupokea maagizo kutoka kwa Musa, ambayo yalifikishwa kwa watu kupitia tarumbeta. Baragumu hizi zilitoa sauti maalum ambazo watu walizielewa, na kuelekeza mjongeo/mwendo wao ipasavyo. {1T 650.2}

Ishara maalum ilitolewa kwanza na wapiga tarumbeta ili kuvuta usikivu wa watu; kisha wote walipaswa kuwa makini na kutii sauti husika ya tarumbeta. Hakukuwa na machafuko ya kelele katika sauti za tarumbeta, kwa hivyo hakukuwa na udhuru wa kuchanganyikiwa katika mwendo. Afisa mkuu wa kila kundi alitoa maagizo dhahiri kuhusu mwendo waliopaswa kuufanya, na hakuna hata mmoja aliyeweka umakini akaachwa bila kujua cha kufanya. Ikiwa wapo ambao wangeshindwa kufuata matakwa ambayo Bwana alimpatia Musa, na Musa akawapatia watu, wangeadhibiwa kifo. Kusingekuwa na kisingizio cha kusihi kwamba hawakujua asili ya mahitaji haya, kwa sababu wangethibitisha kwa hiari yao kwamba ni wajinga, na wangepokea adhabu ya haki kwa makosa yao. Ikiwa hawakujua mapenzi ya MUNGU juu yao, lilikuwa ni kosa lao wenyewe. Walikuwa na fursa sawa za kupata maarifa waliyopewa kama watu wengine, kwa hivyo dhambi yao ya kutojua, kutokuelewa, ilikuwa kubwa mbele za MUNGU kana kwamba walikuwa wamesikia na kisha wakaasi. {1T 651.1}

Bwana aliteua familia maalum ya kabila la Lawi kubeba Sanduku la Agano; na baadhi ya Walawi waliteuliwa na MUNGU kulibeba Hema na samani zake zote, na kufanya kazi ya kulisimamisha na kulishusha lile hema. Na ikiwa mtu yeyote kutokana na udadisi au ukosefu wa utaratibu alitoka mahali pake na kugusa sehemu yoyote ya Patakatifu au samani, au hata kumkaribia yeyote kati ya watendakazi, aliuawa. MUNGU hakuliacha Hema lake takatifu lichukuliwe, lisimamishwe, na kushushwa chini bila mpangilio, na kabila lolote linaloweza kuchagua kazi hiyo; bali walichaguliwa watu ambao wangethamini utakatifu wa kazi ambayo walikuwa wakiifanya. Watu hawa walioteuliwa na MUNGU walielekezwa kusisitiza juu ya watu kuhusu utakatifu maalum wa Sanduku la Agano na yote yaliyokuwemo, ili wasije wakaviangalia vitu hivi bila kutambua utakatifu wake maana wangekatiliwa mbali na Israeli. Vitu vyote vinavyohusu mahali Patakatifu sana vilitakiwa kutazamwa kwa kicho/heshima. {1T 652.1}

Safari za wana wa Israeli zimeelezewa kwa uaminifu; ukombozi ambao Bwana aliwafanyia, mfumo wao kamili na utaratibu maalum, dhambi yao ya kumnung'unikia Musa na MUNGU, makosa yao, uasi wao, adhabu zao, mizoga yao iliyotapakaa jangwani kwa sababu ya kutotaka kujisalimisha katika mipangilio ya MUNGU yenye busara - picha hii ya uaminifu imetundikwa mbele

yetu kama onyo tusije tukafuata mfano wao wa kutotii na kuanguka kama wao. {1T 652.2}

"Lakini wengi sana katika wao, MUNGU hakupendezwa nao; maana waliangamizwa jangwani. Basi mambo hayo yalikuwa mifano kwetu, kusudi sisi tusiwe watu wa kutamani mabaya, kama wale nao walivyotamani. Wala msiwe waabudu sanamu, kama wengine wao walivyokuwa; kama ilivyoandikwa, Watu waliketi kula na kunywa, kisha wakasimama wacheze. Wala msifanye uasherati, kama wengine wao walivyofanya, wakaanguka siku moja watu ishirini na tatu elfu (23,000). Wala tusimjaribu Bwana, kama wengine wao walivyomjaribu, wakaharibiwa na nyoka. Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyonung'unika, wakaharibiwa na mharabu. Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani. Kwa hiyo yule anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke. "Je! MUNGU amebadilika kutoka kuwa MUNGU Mwenye utaratibu? Hapana; Yeye ni Yule-Yule katika wakati huu wa sasa kama wakati ule wa zamani. Paulo anasema: " Kwa maana MUNGU si MUNGU wa machafuko, bali wa amani. Yeye anabanisha mambo kwa umahsusi, na kinagaubaga kama vile alivyokuwa (particular). Na Yeye anakusudia kwamba tujifunze masomo ya utaratibu na mfumo kutoka katika utaratibu kamili ulioanzishwa katika siku za Musa kwa faida ya wana wa Israeli. {1T 652.3}

## SURA YA 113

## KAZI ZAIDI

Uzoefu kuanzia Desemba 23, 1867 hadi Februari 1, 1868

Sasa nitaanza tena kielelezo cha matukio, na pengine siwezi kutoa wazo la kazi zetu hadi wakati wa mkutano wa Vermont kuliko kwa kunakili barua niliyomuandikia mtoto wetu huko Battle Creek, Desemba 27, 1867: {1T 653.1}

"Mwanangu mpendwa Edson: Sasa nimeketi kwenye dawati la kaka D.T. Bourdeau, hapa West Enosburgh, Vermont. Baada ya mkutano wetu kufungwa huko Topsham, Maine, nilikuwa nilikuaw na uchovi sana. Wakati nikipanga sanduku langu, nilikaribia kuzimia kwa uchovu. Kazi ya mwisho niliyoifanya hapo ilikuwa ni kuiita familia ya kaka A pamoja na kuwa na mahojiano maalum nao. Nilizungumza na familia hii pendwa, nikitoa maneno ya mawaidha, kutia moyo na faraja, pia ya marekebisho na ushauri kwa yule aliyehusiana nao. Yote niliyosema yalipokelewa kikamilifu na kufuatiwa na ungamo, kilio, na ahueni kubwa kwa kaka na dada A. Hii ni kazi kubwa kwangu inayohusisha nyanja mbalimbali na inanichosha sana. {1T 653.2}

"Baada ya kuketi kwenye gari, nililala chini na kupumzika kwa muda wa saa moja. Tulikuwa na miadi jioni hiyo huko West-brook, Maine, ya kukutana na ndugu kutoka Portland na maeneo jirani. Tulikaa kama nyumbani na familia ya upendo ya kaka Martin. Sikuweza kukaa mpaka wakati wa mchana; lakini, kwa kuhimizwa kuhudhuria mkutano jioni, nilienda kwenye nyumba ya shule, nikihisi kuwa sina nguvu ya kusimama na kuhutubia watu. Nyumba hiyo ilijaa wasikilizaji waliovutiwa sana. Kaka Andrews alifungua mkutano, akazungumza kwa muda mfupi; baba yako alifuatia kwa maelezo machache. Kisha nikaamka, na nilikuwa nimeongea maneno machache tu, nilipohisi nguvu zangu zimefanywa upya; udhaifu wangu wote ulionekana kuniacha, nikazungumza karibu saa moja kwa uhuru kamili. Nilihisi shukrani isiyoelezeka kwa msaada huu uliotoka kwa MUNGU wakati ule ule niliouhitaji sana. Jumatano jioni nilizungumza kwa uhuru karibu masaa mawili juu ya matengenezo ya afya na mavazi. Kuwa na nguvu iliyofanywa upya bila kutarajia, wakati nilikuwa nimehisi uchovu mkubwa kabla ya mikutano hii miwili, kimekuwa chanzo cha faraja kubwa kwangu. {1T 653.3}

"Tulifurahia ziara yetu na familia ya kaka Martin, na tunatarajia kuona watoto wao wapendwa wakitoa mioyo yao kwa Kristo, na pamoja na wazazi wao wakipigana vita vya Kikristo, na kuvaa taji ya kutokufa, ushindi utakapopatikana. {1T 654.1}

"Siku ya Alhamisi tuliingia Portland tena na kula chakula cha jioni na familia ya kaka Gowell. Tulikuwa na mahojiano maalum nao, ambayo tunatumai yatawaletea faida. Tunahisi shauku kubwa kwa mke wa kaka Gowell. Moyo wa mama huyu ameumizwa kwa kuwaona watoto wake katika dhiki na kifo, na kulazwa kwenye kaburi la kimya. Ni salama kwa wasinziao. Hebu mama aendelee kuutafuta Ukweli wote, na kuweka hazina mbinguni, ili wakati Mpaji wa uzima atakapokuja kuwaleta mateka kutoka katika nyumba kubwa ya magereza ya kifo, baba, mama, na watoto waweze kukutana, na minyororo ya familia iliyovunjika iunganishwe tena, na kusiwe na maumivu au kutengana tena. {1T 654.2}

"Kaka Gowell alitupeleka kwenye magari ya moshi kwa kutumia gari lake la farasi. Tulikuwa na muda mfupi wa kupanda gari moshi kabla halijaondoka. Tulisafiri kwa masaa matano, ndipo tukampata kaka A.W. Smith kwenye bohari ya Manchester, akingojea kutupeleka nyumbani kwake katika mji huo. Tulitarajia kupata mapumziko ya usiku mmoja hapa; lakini, tazama, idadi kubwa ya watu walikuwa wakingojea kutupokea. Walikuwa wamekuja umbali wa maili tisa kutoka Amherst kutumia jioni pamoja nasi. Tulikuwa na mahojiano mazuri sana, yenye faida kwa wote bila shaka. Tulimaliza kama saa nne usiku na kupumzika. Mapema asubuhi iliyofuata tuliiacha nyumba nzuri yenye ukarimu ya kaka Smith, tukaendelea na safari yetu kwenda Washington.

Ilikuwa njia ndefu, yenye kuchosha. Magari tuliyaacha huko Hillsborough, tukakuta timu imesubiri kutupeleka maili kumi na mbili kwenda Washington. Kaka Colby alikuwa na toroli la theluji na blanketi, na tulisafiri kwa raha kabisa hadi tulipokuwa karibu na maili chache kufika tunapokwenda. Hakukuwa na theluji ya kutosha kusaidia toroli kutembea; upepo uliinuka, na katika mwendo wa maili mbili za mwisho ilipulizwa theluji iliyoanguka katika nyuso na macho yetu, ikitupatia maumivu na kutufanya tukaribie kuganda. Tulipata makazi katika nyumba nzuri ya kaka C.K. Farnsworth. Walifanya kila wawezalo kwa ajili ya faraja yetu, na kila kitu kilipangwa ili tuweze kupumzika kadri iwezekanavyo. Hicho ndicho kidogo ninachoweza kukuhakikishia. {1T 654.3}

"Sabato aliyoizungumzia baba yako wakati wa mchana, na baada ya mapumziko ya dakika ishirini nilizungumza, nikitoa ushuhuda wa kuwakemea watu kadhaa ambao walikuwa wakitumia tumbaku, pia kwa kaka Ball, ambaye alikuwa akiimarisha mikono ya maadui zetu kwa kuyabeza na kuyadharau maono, na kuchapisha mambo machungu dhidi yetu katika jarida la mgogoro wa Boston/*Crisis in Boston*, na tumaini la Israeli/H*ope of Israel* -gazeti lililotolewa huko Iowa. Mkutano wa jioni ulifanyika kwa ndugu Farnsworth. Kanisa lilikuwepo, na baba yako huko alimuomba ndugu Ball atoe pingamizi lake juu ya maono na atoe nafasi ya kuyajibu. Hivyo ndivyo jioni ilivyotumika. Ndugu Ball alionesha ugumu mkubwa na upinzani; alikiri mwenyewe kuridhika na mambo kadhaa, lakini alishikilia msimamo wake kwa nguvu kabisa. Kaka Andrews na baba yako waliongea waziwazi, wakielezea mambo ambayo hakuyaeleweka vizuri, na kuilaani njia yake isiyo sahihi juu ya Waadventista wanaotunza Sabato. Sote tulihisi kwamba tumefanya kadri tulivyoweza katika siku hiyo kudhoofisha nguvu za adui. Mkutano wetu uliofanyika hadi saa kumi. {1T 655.1}

"Asubuhi iliyofuata tulihudhuria mikutano tena kwenye nyumba ya mikutano. Baba yako alizungumza asubuhi. Lakini kabla tu ya kuzungumza, adui alimfanya ndugu huyu maskini, dhaifu ahisi kuwa alikuwa na mzigo wa kushangaza sana kwa kanisa. Alitembea akijikwaa, akizungumza, akihuzunika, na kulia, na alikuwa na kitu cha kutaktanisha na kibaya juu yake, ambacho hakuna mtu aliyeonekana kukielewa. Tulikuwa tunajaribu kuwaleta wale wanaodai kuuamini Ukweli na kuona hali yao ya giza la kutisha na kurudi nyuma mbele za MUNGU, na kufanya maungamo ya unyenyekevu juu ya maovu hayo, ili wamrudie Bwana na toba ya Kweli na dhati, ili Naye arejee kwao, na kuponya uasi na kurudi nyuma kwao. Shetani alitaka kuizuia kazi hiyo kwa kushinikiza nafsi hii masikini, iliyovurugikiwa ili kuwachukiza wale ambao walitaka kusonga mbele katika ufahamu. Niliamka na kutoa ushuhuda ulio wazi kwa mtu huyu. Hakupata chakula kwa siku mbili, na Shetani alikuwa amemdanganya, na kumsukuma katika hili kwa kupitiliza. {1T 656.1}

"Ndipo baba yako akahubiri. Tulikuwa na mapumziko ya muda mfupi, na kisha nilijaribu kuzungumza juu ya matengenezo ya afya na mavazi, na nikatoa ushuhuda ulio wazi kwa wale ambao walikuwa wamesimama katika njia ya vijana na wasioamini. MUNGU alinisaidia kumweleza mambo kwa uwazi kaka Ball, na kumwambia kwa Jina la Bwana kile alichokuwa akikifanya. Aliathiriwa sana. {1T 656.2}

"Kisha tulifanya mkutano wa jioni huko kwa kaka Farnsworth. Hali ya hewa ilikuwa ya dhoruba wakati wa mikutano, lakini kaka Ball hakubaki mbali na yeyote kati yao. Somo hilo hilo lilianza tena, uchunguzi wa njia aliyokuwa ameifuata. Ikiwa kuna wakati ambao Bwana alikuwa amemsaidia mtu kuongea, alimsaidia kaka Andrews usiku huo, kwani alikita kwenye mada inayohusu kuteseka kwa ajili ya Kristo. Kesi ya Musa ilitajwa, ambaye alikataa kuitwa mwana wa binti Farao, akaona ni afadhali kuteseka pamoja na watu wa MUNGU kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo, akihesabu ya kuwa kushutumiwa Kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri; kwa kuwa aliyatazamia hayo malipo ya thawabu. Alionesha kuwa hiki ni mojawapo ya visa vingi ambavyo aibu ya Kristo ilihesabiwa kuwa bora kuliko utajiri wa ulimwengu na heshima, vyeo vikubwa, taji inayotarajiwa, na utukufu wa ufalme. Jicho la imani lilikuwa limekodoa kwenye utukufu ujao, na malipo ya thawabu yalichukuliwa kuwa ya thamani kubwa kiasi kwamba vitu vyenye utajiri mkubwa zaidi ambavyo ulimwengu unaweza kuvitoa vilionekana havina maana. Watoto wa MUNGU walivumilia kejeli, mijeledi, vifungo, na kutiwa magerezani; walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya, lakini walitegemezwa na tumaini na imani, nna waliweza kuziita hizi taabu kuwa ni nyepesi; wakati ujao, uzima wa milele, ulionekana kuwa na thamani kubwa sana kiasi kwamba waliyahesabu mateso yao kuwa madogo kulinganisha na malipo ya thawabu. {1T 656.3}

"Kaka Andrews alielezea mfano wa Mkristo mwaminifu anayekaribia kuuawa kwa sababu ya imani yake. Ndugu Mkristo alikuwa akiongea naye kwa habari ya nguvu ya tumaini la Kikristo - kama ingekuwepo nguvu ya kutosha ya kumhifadhi wakati mwili wake ukiteketea kwa moto. Alimuuliza Mkristo huyu, anayekaribia kupata mateso, ampatie ishara ikiwa imani ya Kikristo na tumaini vingekuwa na nguvu kuliko moto mkali, unaoteketeza. Alitarajia kuwa zamu yake ingefuata, na hili lingemtia nguvu kwa ajili ya moto. Yule mtu alimuahidi kwamba ishara ingetolewa. Alifikishwa msalabani katikati ya kejeli na dhihaka za umati uliokuwa na watu wazembe na wenye shauku ulikusanyika kushuhudia kuteketezwa kwa Mkristo huyu. Kuni zililetwa na moto ukawashwa, na Mkristo huyu aliweka macho yake juu ya shahidi anayeteseka, anayekufa, akihisi kuwa anategemea sana ishara. Moto uliwaka, na kuwaka na kuteketeza. Mwili ulikuwa mweusi; lakini ishara haikuja. Jicho lake halikuondolewa hata kidogo

katika upeo wa maumivu. Mikono tayari ilikuwa mikavu. Hakukuwa na mwonekano wa uhai. Wote walidhani kuwa moto umefanya kazi yake, na hakuna uhai uliosalia; Na tazama! katikati ya moto, mikono miwili ilinyoshwa kuelekea mbinguni. Ndugu huyu Mkristo, ambaye moyo wake ulikuwa unazimia, aliona ishara ya furaha; iliyotuma msisimko katika utu wake wote, na kuifanya upya imani yake, tumaini lake, na ujasiri wake. Alitokwa na machozi ya furaha. {1T 657.1}

"Wakati kaka Andrews alipoongea juu ya mikono iliyotiwa miyeusi kwa kuungua, iliyoteketezwa katikati ya moto yeye pia, alilia kama mtoto. Karibu mkutano wote uliathiriwa na machozi. Mkutano huu ulifungwa karibu saa kumi. Kulikuwa na uvunjwaji mkubwa wa mawingu ya giza. Ndugu Hemingway aliinuka na kusema alikuwa amerudi nyuma kabisa, akitumia tumbaku, akipinga maono, na kumtesa mkewe kwa kuyaamini, lakini akasema hatafanya hivyo tena. Alimuomba msamaha, na msamaha kwetu wote. Mkewe aliongea kwa hisia. Binti yake na wengine kadhaa waliinuka kwa ajili ya maombi. Alisema kwamba ushuhuda ambao dada White alikuwa ameubeba ulionekana moja kwa moja kutoka kwenye kiti cha enzi, na asingeweza kuthubutu kuupinga tena. {1T 658.1}

"Kaka Ball kisha akasema kwamba ikiwa mambo yalikuwa kama tulivyoyaona, kesi yake ilikuwa mbaya sana. Alisema kwamba alijua amerudi nyuma kwa miaka na alikuwa amesimama kwenye njia ya vijana. Tulimshukuru MUNGU kwa kukiri huko. Tulikusudia kuondoka mapema Jumatatu asubuhi, na nilikuwa na miadi huko Braintree, Vermont, kukutana na watunza Sabato thelathini. Lakini hali ya hewa ilikuwa ya baridi kali, mbaya, iliyosumbua kusafiri maili ishirini na tano baada ya kazi ya kila wakati, na mwishowe tuliamua kusubiri, na kuendelea na kazi huko Washington hadi kaka Ball aamue kuwa sawa au kinyume na Ukweli, ili kanisa lipate utulivu katika kesi yake. {1T 658.2}

"Mkutano ulianza Jumatatu saa nne asubuhi, ndugu Rodman na Howard walikuwepo. Ndugu Newell Mead, aliyekuwa dhaifu sana na mwoga kama alivyokuwa baba yako katika ugonjwa wake wa zamani, alitumwa kuhudhuria mkutano. Kisha hali ya kanisa ilizungumzwa, na lawama kali zaidi ilipitishwa kwa wale waliosimama katika njia ya ustawi wake. Kwa maombi ya dhati sana tuliwasihi waongoke kwa MUNGU kisha wakabiliane nazo. Bwana alitusaidia katika kazi hiyo; kaka Ball alihisi msukumo, lakini alisogea pole pole. Mkewe alipata hisia kubwa kwa ajili yake. Mkutano wetu wa asubuhi ulifungwa saa tisa au saa kumi alasiri. Masaa yote haya tulikuwa tumejishughulisha, kwanza na mmoja wetu, kisha mwingine, tukifanya bidii kwa ajili ya vijana ambao hawajaongoka. Tulipanga mkutano mwingine jioni, kuanza saa kumi na mbili. {1T 658.3}

"Kabla tu ya kwenda kwenye mkutano, nilikuwa na uamsho wa matukio ya kupendeza ambayo yalikuwa yamepita mbele yangu katika maono, na nilizungumza na kaka Andrews, Rodman, Howard, Mead, na wengine kadhaa ambao walikuwepo. Ilionekana kwangu kuwa malaika walikuwa wakipasua wingu na kuingiza miale ya nuru kutoka mbinguni. Mada ambayo iliwasilishwa kwa namna ya kushangaza sana ilikuwa ni mada ya Musa. Nilishangilia na kusema: Lo! Laiti ningekuwa na ustadi wa msanii, ili nichore picha ya mandhari ya Musa juu ya mlima! Nguvu zake zilikuwa thabiti. 'Hazikupungua,' ndio lugha ya Maandiko. Jicho lake halikuhafifishwa vizazi vyote, lakini alikuwa juu ya mlima kufia huko. Malaika walimzika, lakini Mwana wa MUNGU punde alishuka na kumfufua kutoka katika wafu na kumpeleka mbinguni. Lakini MUNGU alimpatia mwonekano wa nchi ya ahadi, na baraka Zake juu yake. Ilikuwa kama Edeni ya pili. Kadri mwonekano huu ulivyopita wa nchi yote katika maono yake -panorama. Alioneshwa kutokea kwa Kristo katika ujio Wake wa kwanza, kukataliwa Kwake na taifa la Kiyahudi, na kifo CHAKE msalabani. Musa aliona ujio wa pili wa Kristo na ufufuo wa wenye haki. Nilizungumzia pia juu ya kukutana kwa Adamu wawili -Adamu wa kwanza, na Kristo Adamu wa pili - wakati Edeni itakapochanua tena duniani. Nimekusudia kuandika maelezo ya mambo haya ya kupendeza katika Ushuhuda Nambari 14. Ndugu walitamani niyarudie haya katika mkutano wa jioni. {1T 659.1}

"Mkutano wetu wa siku nzima ulikuwa wa maana sana. Nilikuwa na mzigo mzito kwangu Jumapili jioni hata nikalia kwa sauti kwa karibu nusu saa. Jumatatu, miito mizito ilikuwa imetolewa, na Bwana aliipeleka nyumbani, kwenye moyo. Nilienda kwenye mkutano Jumanne jioni nikiwa mwepesi kidogo. Nilizungumza kwa saa moja nikiwa na uhuru mkubwa juu ya masomo ambayo nilikuwa nimeyaona katika maono niliyoyataja. Mkutano wetu ulikuwa huru sana. Ndugu Howard alilia kama mtoto, kama alivyofanya ndugu Rodman. Ndugu Andrews aliongea kwa dhati na bidii, kwa njia ya mguso, na kilio. Ndugu Ball aliinuka na kusema kwamba ilionekana kuna roho mbili juu yake jioni ile, moja ikimwambia: Je! Unaweza kutilia shaka kwamba ushuhuda huu wa dada White umetoka mbinguni? Roho nyingine ingewasilisha mbele ya akili yake mapingamizi aliyokuwa ameyafungua mbele ya maadui wa imani yetu. "Ah, laiti ningeweza kujisikia kuridhika," alisema, 'kuhusiana na mapingamizi haya yote, laiti yangeweza kuondolewa, ningehisi kuwa nimemdhuru sana dada White. Hivi karibuni nimetuma kipande kwenye Tumaini la Israeli/*Hope of Israel*. Kama ningekuwa na kipande hicho, kitu gani nisingetoa!' Alipata hisia kubwa, akalia sana. Roho wa Bwana alikuwa katika mkutano huo. Malaika wa MUNGU walionekana kuwa karibu sana, wakiwarudisha nyuma malaika waovu. Wachungaji na washiriki walilia kama watoto. Tulihisi tumepata nafasi kusonga mbele katika kupanda Neno, na kwamba nguvu za giza zimeondoka. Mkutano wetu ulifungwa vizuri. {1T 659.2}

"Tulipanga mkutano mwingine tena wa siku inayofuata, kuanzia saa nne asubuhi nilizungumza juu ya fedheha na utukufu wa Kristo. Ndugu Ball alikaa karibu yangu na kulia kila wakati nilipokuwa nikiongea. Nilizungumza kwa saa moja, kisha tukaanza kazi zetu kwa vijana. Wazazi walikuwa wamekuja kwenye mkutano wakiwaleta watoto wao pamoja nao kupokea baraka. Ndugu Ball aliinuka na kukiri kwa unyenyekevu kwamba hajaishi kama anavyopaswa kuishi na familia yake. Alikiri mbele ya watoto wake na mke wake kwamba yeye alikuwa katika hali ya kurudi nyuma, na hakuwa na msaada kwao, bali kinyume chake alikuwa kikwazo. Machozi yalitiririka kwa uhuru; sura yake yenye nguvu ilitetemeka, na kilio na kwikwi ikayasonga maneno yake. {1T 660.1}

"Ndugu James Farnsworth alikuwa ameathiriwa na ndugu Ball, na hakuwa ameungana kikamilifu na Waadventsta watunza Sabato. Alikiri kwa machozi. Ndipo tukawasihi sana watoto, hadi kumi na watatu walipoinuka na kuelezea nia ya kuwa Wakristo. Watoto wa ndugu Ball walikuwa miongoni mwa idadi hiyo. Mmoja au wawili walikuwa wameondoka kwenye mkutano, wakilazimika kurudi nyumbani. Kijana mmoja, mwenye takribani miaka ishirini, alitembea maili arobaini kutuona na kuusikia Ukweli. Hakuwahi kuwa na dini, lakini alichukua msimamo wake upande wa Bwana kabla ya kuondoka. Huu ulikuwa moja ya mikutano bora kabisa. Mwishoni, ndugu Ball alikuja kwa baba yako na kukiri kwa machozi kwamba alikuwa amemkosea, na akamuomba msamaha. Kisha alikuja kwangu na kukiri kwamba alikuwa ameniumiza sana. 'Je! Unaweza kunisamehe na kuomba MUNGU anisamehe?' Tulimhakikishia kuwa tungemsamehe bure, kwa moyo mkunjufu kama tulivyotarajia kusamehewa. Tuliachana na wote kwa machozi mengi, tukihisi uwepo wa baraka za mbinguni juu yetu. Hatukuwa na mkutano jioni. {1T 660.2}

"Alhamisi tuliamka saa kumi usiku wakati wa karibu na mapambazuko. Mvua ilikuwa imenyesha usiku na bado ilikuwa inaendelea kunyesha, lakini tulijitosa kuanza kuendesha mpaka Bellows Falls, umbali wa maili ishirini na tano. Maili nne za kwanza zilikuwa mbaya sana, kwa sababu tulipitia katika njia ya kichochoro katika mashamba ili kuepuka milima mikali. Tuliendesha juu ya mawe na kuitifua ardhi, karibu kabisa tutupwe nje ya gari. Jua lilipokaribia kuchomoza, dhoruba iliondoka, na tulikuwa na safari nzuri tulipofika kwenye barabara kubwa. Hali ya hewa ilikuwa shwari; hatukuwahi kuwa na siku nzuri zaidi ya safari. Tulipofika huko Bellows Falls, tuligundua kuwa tumechelewa gari moshi la mwenzo kasi kwa saa moja, na saa moja kabla ya gari moshi ya kulala. Hatukuweza kufika St. Albans hadi saa tisa jioni. Tuliketi kwenye gari zuri, kisha tukala chakula cha jioni, na kufurahia nauli yetu ndogo. Kisha tukajiandaa kulala ikiwa tunaweza. {1T 661.1}

"Nilipokuwa nimelala, kuna mtu alitikisa bega langu kwa nguvu sana. Nikatazama juu, na nikamuona mwanamke mwenye sura ya kupendeza

ameinama juu yangu. Akasema: "Je! Hunifahamu? Mimi ni dada Chase. Magari yako pale White River. Yamesimama kwa muda mfupi tu. Mimi naishi karibu na hapa, na nimekuja kila siku wiki hii na nimekuwa nikipitia magari ili nikutane na wewe. "Nikakumbuka kwamba nilipata chakula cha jioni nyumbani kwake huko Newport. Alifurahi sana kutuona. Yeye na mama yake wanaitunza Sabato peke yao. Mume wake ni kondakta wa magari ya moshi. Aliongea haraka. Alisema alilithamini sana gazeti la *Review*, kwani hakuwa na mkutano wa kuhudhuria. Alihitaji vitabu avisambaze kwa majirani zake, lakini alilazimika kutafuta pesa zote mwenyewe ili azitumie kwa ajili ya vitabu au vijizuu. Tulikuwa na mahojiano yenye faida, ingawa yalikuwa mafupi, kwa kuwa mabehewa ya gari la moshi yalianza kuondoka, na ilibidi tutengane. {1T 661.2}

"Huko kwa Mtakatifu Albans tulikutana na kaka Gould na A.C. Bourdeau. Kaka B alikuwa na gari zuri lililofunikwa likiwa na farasi wawili, lakini aliendesha polepole sana, na hatukufika Enosburgh hadi baada ya saba usikuhi. Tulikuwa tumechoka na tunasikia baraidi. Tulilala kupumzika kidogo baada ya saa nane usiku na tukasinzia hadi saa moja asubuhi. {1T 662.1}

"Asubuhi ya Sabato. Kuna mkusanyiko mkubwa hapa ingawa barabara ni mbaya, si kwa gari la kukokota la theluji wala kwa gari la farasi lenye magurudumu. Nimekuwa kwenye mkutano na kupata muda mchache hapo. Baba yako anazungumza asubuhi ya leo, mimi mchana. Acha Bwana atusaidie, ndilo ombi letu. Unaona ni barua ndefu kiasi gani nimekuandikia. Wasomee wale wenye shauku, hasa kwa baba na mama White. Unaona, Edson, kwamba tuna kazi kubwa ya kufanya. Natumaini hutapuuzia kutuombea. Baba yako anafanya kazi kwa bidii, kwa juhudi sana ambayo siyo nzuri kwa afya yake. Wakati mwingine hutambua baraka maalum za MUNGU, na hii inamfanya upya na kumchangamsha katika kazi. Hatujajiruhusu kupumzika tangu tulipokuja Mashariki; tumefanya kazi kwa nguvu zetu zote. Hebu jitihada zetu dhaifu zibarikiwe kwa faida ya watu wapendwa wa MUNGU. {1T 662.2}

"Edson, natumahi kuwa utaupamba ushuhuda wako kwa maisha yaliyopangiliwa vizuri na mazungumzo ya utauwa. Oh uwe na bidii! Uwe na ari na uvumilivu katika kazi. Kesha katika maombi. Sitawisha unyenyekevu na upole. Hili litakubaliwa na MUNGU. Jifiche kwa Yesu; Hebu kujipenda na kujivuna vitolewe kafara, na wewe, mwanangu pata uzoefu mzuri wa Kikristo, ili ufae kutumika katika nafasi yoyote ambayo MUNGU anaweza kukuhitaji uwe nayo. Chunguza kazi kamili ya moyo. Kazi ya juu juu haitasimama katika jaribu la hukumu. Tafuta badiliko kamili kutoka ulimwenguni. Hebu mikono yako isiwe na mawaa, moyo wako usitiwe doa, tabia yako isichafuliwe, na uharibifu wake. Tunza utofauti. MUNGU anaita: 'Tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, wala msiguse kitu kilicho najisi; Nami nitawapokea, Nami nitakuwa Baba yenu, nanyi mtakuwa wana Wangu na binti Zangu, asema Bwana Mwenyezi. "Basi tukiwa na

ahadi hizi, wapenzi, hebu na tujitakase na uchafu wote wa mwili na roho, tukikamilisha utakatifu katika kumcha MUNGU." {1T 662.3}

"Kazi iko juu yetu ili kuukamilisha utakatifu. MUNGU anapotuona tukifanya kila tuwezalo kwa upande wetu, basi atatusaidia. Malaika watatusaidia, na tutakuwa na nguvu kupitia Kristo atuimarishaye. Usipuuze maombi ya siri. Jiombee mwenyewe. Kua katika neema. Songa mbele. Usisimame tuli (ukipiga marktime), usirudi nyuma. Elekea kwenye ushindi. Uwe na ujasiri katika Bwana, kijana wangu mpendwa. Pigana na adui mkubwa kwa muda kidogo tu, kisha ahueni itakuja, na silaha zitawekwa chini ya miguu ya Mkombozi wetu mpendwa. Kazana katika kusonga mbele na kukishinda kila kikwazo. Endapo siku zijazo zinaonekana kuwa na giza, Endelea kutumaini, Endelea Kuamini. Mawingu yatatoweka, na nuru itaangaza tena. Msifu MUNGU, moyo wangu unasema, msifu MUNGU kwa kile alichokufanyia wewe, baba yako, na mimi mwenyewe. Anza mwaka mpya vema, kwa usahihi. Mama yako, E.G.W " {1T 663.1}

Mkutano huko West Enosburgh, Vermont, ulikuwa wa kupendeza sana. Ilionekana kuwa vema kukutana tena, na kuzungumza na marafiki zetu wa kweli wa zamani, ambao wamejaribiwa na kustahimili, katika jimbo hili. Kazi kubwa na nzuri ilifanyika kwa muda mfupi. Marafiki hawa kwa ujumla walikuwa masikini na walifanya kazi ngumu kwa ajili ya maisha ambapo dola moja hupatikana kwa kazi zaidi ya mbili huko Magharibi, lakini walikuwa wakarimu kwetu. Maelezo mengi kuhusu mkutano huu yametolewa katika gazeti la *Review*, na uhitaji wa nafasi katika kurasa hizi pekee unaonekana kukataza marudio yake. Hakuna hali ambayo ndugu wamekuwa wakweli kwenye kazi ya MUNGU kama huko Vermont ya zamani. {1T 663.2}

Tukiwa safarini kutoka Enosburgh, tuliweka kituo usiku huo na familia ya ndugu William White. Ndugu C.A. White, mwanaye, alitutambulisha jambo lake la hati milki ya kufua nguo na kukamua, na alihitaji ushauri. Kama nilivyoandika dhidi ya watu wetu wanaohusika katika haki za hati milki, alitaka kujua jinsi nilivyoiona hati milki yake. Nilimwambia kwa uhuru kile ambacho sikukimaanisha katika yale ambayo niliyaandika, na kile nilichomaanisha pia. Sikumaanisha kuwa ilikuwa vibaya kuwa na uhusiano wowote na haki za hati milki, kwa sababu hili haliwezekani, maana vitu vingi ambavyo tunapaswa kufanya kila siku vina hati miliki. Wala sikutaka kufikisha wazo kwamba lilikuwa kosa kutoa hati miliki, kutengeneza, na kuuza nakala yoyote inayostahili kuwa na hati miliki. Nilikuwa na maana ya kueleweka kuwa ni makosa kwa watu wetu kujitesa wenyewe kwa kuamriwa, kudanganywa, na kutapeliwa na watu hao ambao huenda kote nchini wakiuza haki ya eneo hili kwa mashine au mkataba. Mengi ya haya hayana thamani, maana siyo uboreshaji wa kweli. Na wale

ambao wanahusika katika uuzaji wao, ni kundi la wadanganyifu isipokuwa wachache. {1T 664.1}

Kisha baadhi ya watu wetu wamejihusisha na uuzaji wa bidhaa zenye hati miliki ambazo walikuwa na sababu ya kuamini kwamba hazikuwa vile zilivyowakilishwa. Kwamba watu wetu wengi, baadhi yao baada ya kuonywa kikamilifu, bado watajitesa wenyewe kudanganywa na taarifa za uongo za wachuuzi hawa wa haki za milki, inaonekana kuwa ya kushangaza sana. Baadhi ya hati miliki ni za thamani sana, na wachache wamezifanyia kazi nzuri. Lakini ni maoni yangu kwamba mahali ambapo dola moja imepatikana, dola mia moja zimepotea. Hakuna utegemezi wowote unaoweza kuwekwa kwenye ahadi hizi za haki milki. Na ukweli kwamba wale wanaohusika nao, isipokuwa wachache, ni wadanganyifu na waongo, hivyo kufanya iwe vigumu kwa mtu mwaminifu, ambaye ana mkataba unaostahili, kupata sifa na ufadhili stahiki kwake. {1T 664.2}

Kaka White aliionesha hati milki yake ya kufua na kukamua nguo mbele za watu, wakiwemo wafuatao; kaka Bourdeau, kaka Andrews, mume wangu, na mimi mwenyewe, na tuliitazama kwa shauku. Tangu wakati huo ametutengenezea mashine moja kama zawadi, ambayo ndugu Corliss kutoka Maine, mwajiriwa wetu, kwa muda mfupi aliiweka pamoja kwenye utaratibu. Dada Burgess, kutoka wilaya ya Gratiot, msichana wetu aliyeajiriwa, amefurahishwa nayo sana. Inafanya kazi vizuri, na kwa haraka sana. Mwanamke dhaifu ambaye ana mtoto au mume anayeifanyia kazi mashine hii, anaweza kuosha kwa masaa machache, na yeye anaweza kusimamia kazi hiyo huku akifanya kazi zingine pia. Ndugu White alituma matangazo, ambayo mtu yeyote anaweza kuwa nayo kwa ajili ya kuwasiliana na sisi, kwa kuambatanisha na gharama za posta. {1T 665.1}

Mkutano wetu uliofuata ulikuwa katika Kituo cha Adams, New York. Huu ulikuwa mkutano mkubwa. Kulikuwa na watu kadhaa ndani na karibu na eneo hili hapa ambao habari zao zilikuwa zimeoneshwa kwangu, ambazo nilihisi kupendezwa nazo zaidi. Walikuwa watu wenye maadili mazuri. Wengine katika maisha yao walikuwa katika nafasi ambazo ziliufanya msalaba wa Ukweli wa sasa kuwa mzito kuubeba, au, angalau, walifikiri hivyo. Wengine, ambao walikuwa wamefikia umri wa kati wa maisha, walikuwa wamelelewa kuitunza Sabato tangu utotoni, lakini hawakuwa wameubeba msalaba wa Kristo. Hawa walikuwa katika nafasi ambazo ilionekana kuwa ngumu kuwasogeza. Walihitaji kutikiswa kutoka kwenye utegemezi wa matendo yao mema na kuletwa kuhisi hali yao ya upotevu bila Kristo. Hatukuweza kuziacha roho hizi, tulijitahidi kwa nguvu zetu kuwasaidia. Mwishowe waliguswa, na tangu wakati huo nimefurahishwa kusikia kutoka kwa baadhi yao, na habari njema kuwahusu wote. Tunatumaini kuwa upendo wa ulimwengu huu hautazuia upendo wa

MUNGU mioyoni mwao. MUNGU huwageuza watu wenye nguvu ya mali na kuwaleta katika zizi. Ikiwa wanataka kustawi katika maisha ya Kikristo, kukua katika neema, na mwishowe kuvuna tuzo kubwa, watalazimika kutumia mali yao nyingi kuliendeleza kusudi la Ukweli. {1T 665.2}

Baada ya kutoka katika kituo cha Adams, tulikaa siku chache huko Rochester, na kutoka mahali hapo tukaja Battle Creek, ambapo tulikaa mpaka Sabato na siku ya kwanza ya juma. Hapo tulirudi nyumbani kwetu, ambapo tulikaa Sabato iliyofuata na siku ya kwanza ya juma na ndugu waliokusanyika kutoka sehemu tofauti. {1T 666.1}

Mume wangu alikuwa ameshikilia kitabu chenye masuala mbalimbali huko Battle Creek, na mfano mzuri ulikuwa umewekwa na kanisa hilo. Kwenye mkutano huko Fairplains aliwasilisha suala la watu wote ambao hawakuweza kununua vitabu kama vile karama za Roho, Wito kwa akina mama, Jinsi ya kuishi, Wito kwa vijana, Masomo ya Sabato, na vielelezo, pamoja na ufafanuzi muhimu. Mpango huo ulikutana na idhini ya jumla. Lakini kuhusu kazi hii muhimu nitazungumza mahali pengine. {1T 666.2}

## SURA YA 114

## KESI YA HANNAH MORE

Sabato iliyofuata tulikutana na kanisa la Orleans, ambapo mume wangu aliitambulisha kesi ya dada yetu ambayo imehuzunisha watu wengi sana, Hannah More. Wakati ndugu Amadon alipotutembelea msimu wa joto uliopita, alisema kwamba dada More alikuwa huko Battle Creek, na alipokosa ajira huko, alikwenda katika wilaya ya Leelenaw kuishi na rafiki yake wa zamani ambaye alikuwa mtendakazi mwenzake katika mashamba ya umishenari huko Afrika ya Kati. Mimi na mume wangu tulihisi kuhuzunishwa kwamba mtumishi huyu mpendwa wa Kristo aliona ni muhimu kujiondoa katika jamii ya watu wa imani kama hiyo, na tukaamua kumsafirisha aje kuishi nasi, kufanya makazi yake kwetu. Tulimwandikia mwaliko akutane na sisi katika miadi yetu huko Wright, na kurudi nyumbani pamoja nasi. Yeye hakukutana na sisi huko Wright. Hapa ninatoa majibu yake kwa barua yetu ya Agosti 29, 1867, ambayo tuliipokea huko Battle Creek: {1T 666.3}

"Kaka White: Mawasiliano yako mema yalinifikia Kwa Barua ya Posta ya Wiki Hii. Kwa Kuwa Barua Za Posta Zinakuja Hapa Mara Moja Kwa Wiki, Na Zinatoka Kesho, Nimejibu Kwa Haraka. Hapa Tunapoishi Ni Porini, Kama Ilivyo, Na Mtu Wa Asili Ya Muhindi Mwekundu Hubeba Barua Siku Za Ijumaa Kwa Miguu, Na Kurudi Jumanne. Nimeshauriana Na Ndugu Thompson Kuhusiana Na Njia ya Kufika Huko, Na Amesema Njia Yangu Bora Na Ya Uhakika Kuja Huko, Itakuwa Kwa Kutumia Mashua Kutoka Hapa Na Kwenda Milwaukee, Na Kisha Kufika Grand Haven. {1T 666.4}

"Nilipotumia Pesa Zangu Zote Kuja Hapa, Na Kualikwa Kukaa Katika Familia Ya Ndugu Thompson, Nimekuwa Nikimsaidia Dada Thompson Kwenye Mambo Yake Ya Nyumbani Na Kushona, Kwa Dola Moja Na Senti Hamsini Kwa Wiki Kwa Siku Tano Za Wolo, Kwa Kuwa Hawapendi Niwafanyie Kazi Siku Ya Jumapili, Na Mimi Sifanyi Kazi Katika Sabato Ya Bwana, Siku Ya Pekee Ambayo Biblia Inaitambua. Hawana Shauku Kwamba Niwaache, Licha Ya Utofauti Wetu Wa Imani; Anasema Ninaweza Kukaa Nao, Isipokuwa Tu Nisiifanye Imani Yangu Kuwa Maarufu Kati Ya Watu Wake. Amenialika Pia Nitimize Miadi Yake Kwa Kunzungumza Wakati Wa Ziara Yake Ya Kuhubiri, Na Nimefanya Hivyo. Dada Thompson Anahitaji Usimamizi Kwa Ajili Ya Watoto Wake, Kwa Sababu Ushawishi Ni Mbaya Sana Huko Nje, Na Shule Imekasirika Kwamba Hataki Kuwapeleka Wapendwa Wake Kati Yao Mpaka Wawe Wakristo, Kama Asemavyo. Mtoto Wao Mkubwa, Leo Akiwa Na Umri Wa Miaka Kumi Na Sita, Ni Kijana Mcha MUNGU Na Mwenye Kujitoa Walfi. Kwa Sehemu Wameanza Kufuata Utaratibu Wa Matengenezo Ya Afya, Na Nafikiri Kwamba Watakuwa Sehemu Kamili Ya Utaratibu Huu, Na Kuupenda. Ameamuru Matengenezo Ya Afya. Nilimuonesha Baadhi Ya Nakala Nilizoleta. {1T 667.1}

"Natumaini Na Kuomba Kwamba Aitunze Sabato Takatifu. Dada Thompson Tayari Anaiamini. Amejipanga Katika Njia Zake Mwenyewe, Na Kwa Hakika Anadhani Yuko Sahihi. Laiti Ningeweza Kumsadikisha Kusoma Kitabu Hiki Nilichokileta, Historia Ya Sabato, N.k, Lakini Anaviangalia Na Kuviita Kuwa Ni Vya Ukafiri, Na Kusema Kwamba Kwake Vinaonekana Kama Ni Kubeba Makosa Mbele Zao, Wakati Kama Wangevisoma Kwa Uangalifu Wa Hisia Za Kiimani, Naweza Kusema Kwamba Wangezikubali Kweli Za Biblia Na Kuona Uzuri Wake Na Uthabiti. Sina Shaka Kwamba Dada T. Angefurahia Punde Kuwa Mwadvensita Wa Sabato Kama Mume Wake Asingekuwa Mpinzani Mkubwa Wa Jambo Hilo. Nilishawishiwa Akilini Mwangu Kwamba Nilikuwa Na Kazi Ya Kufanya Hapa Kabla Ya Kufika Hapa; Lakini Ukweli Umo Ndani Ya Familia, Na Kamwe Siwezi Kuubeba Tena Zaidi, Itaonekana Kuwa Kazi Yangu Imekamilika, Au Inakaribia Kukamilika. Simwonei Aibu Kristo, Au Neno Lake, Katika Kizazi Hiki Kibaya, Na Hakika Ingekuwa Bora Kutupwa Kati Ya Watu Wanaoitunza Sabato Na Watu Waliochaguliwa Na MUNGU. {1T 667.2}

"Nitahitaji Dola Kumi Angalau Kufika Greenville. Ili Kwamba Pamoja Na Kidogo Nilichopata, Kiweze Kunitosha. Lakini Sasa Nitakusubiri Uniandikie, Na Ufanye Unachofikiri Kuwa Ni Kizuri Kuhusu Kunitumia Fedha. Wakati Wa Majira Ya Kuchipua Majani Nitakuwa Na Nauli Ya Kutosha Kusafiri Mwenyewe Mwendo Mrefu, Na Nafikiria Ningependa Kufanya Hivyo. Acha Bwana Atuongoze Na Kutubariki Katika Kila Tunalofanya, Ndiyo Shauku Kubwa Ya Moyo Wangu. Na Naomba Niweze Kujaza Nafasi Hiyo Ambayo MUNGU Atanigawia Katika Shamba Lake La Mizabibu, Nifanye Kila Jukumu Kwa Utayari Mkubwa, Kwa Ugumu Wowote Linavyoweza Kuonekana, Kulingana Na Uzuri Wake, Ndiyo Shauku Yangu Na Maombi Ya Moyo Wangu. {1T 668.1}

"Hana More."

Baada ya kupokea barua hii, tuliamua kutuma kiasi cha fedha kilichohitajika kwa dada More, punde baada ya kupata nafasi. Lakini kabla ya kupata nafasi tuliamua kwenda Maine, ili turudi baada ya majuma machache, ambapo tungeweza kumtumia kabla ya kufunga usafiri wa meli ambapo alipaswa kusafiri. Na tulipoamua kukaa na kufanya kazi Maine, New Hampshire, Vermont, na New York, tulimwandikia ndugu aliyepo katika wilaya hii ili kuwaona ndugu wanaoongoza katika maeneo ya karibu na kushauriana nao kuhusu kumtuma Dada More na kumpatia hifadhi hadi tutakaporudi. Lakini jambo hilo lilipuuzwa hadi muda wa kusafiri kwa meli ukafungwa, na tukarudi na kugundua kuwa hakuna mtu aliyeonesha shauku au nia ya kumsaidia dada More katika eneo hili, ambapo angeweza kuja kwetu wakati tukifika nyumbani kwetu. Tulihisi kuhuzunika na kufadhaika, na kwenye mkutano huko Orleans Sabato ya pili baada ya kufika nyumbani, mume wangu aliwasilisha jambo lake Dada Moore kwa ndugu waliokuwepo. Ripoti fupi ya kile kilichosemwa na kufanywa kuhusiana na dada More ilitolewa na mume wangu katika gazeti la Review, Februari 18, 1868, kama ifuatavyo: {1T 668.2}

"Kwenye Mkutano Huu Tulielezea Suala La Dada Hannah More, Ambaye Kwa Wakati wa Sasa Anasafiri Kuelekea Kaskazini Michigan Na Marafiki Wasioitunza Sabato Ya Biblia. Tulisema Kwamba Mtumishi Huyu Wa Kristo Aliikubali Sabato Wakati Alipokuwa Akifanya Huduma Ya Umishenari Huko Afrika Ya Kati. Wakati Hili Lilipojulikana, Huduma Zake Katika Upande Ule Hazikuhitajika Tena, Hivyo Alirudi Marekani Kutafuta Sehemu Ya Kuishi Na Ajira Kwa Wale Wenye Imani Kama Yake. Tunahukumu Kutokana Na Eneo Lake La Sasa, Na Katika Hili Amekatishwa Sana Tamaa. Hakuna Anayestahili Kulaumiwa Katika Suala Hili; Lakini Inaonekana Kwetu Kwamba Kuna Ukosefu Wa Vitu Vilivyounganishwa Na Mfumo Wetu Wa Taasisi, Kwa Kuwatia Moyo Watu Kama Hao Na Kuwasaidia Katika Maeneo Ya Kufanyia Kazi Za Kujikimu Kimaisha, Au Kwamba Hao Ndugu Na Dada Waliopendezwa Kumuona Dada More Hawajafanya Wajibu Wao. Kura Ya Moja Kwa Moja, Iliyokubalika Na Wote Ilitolewa Kumwalika Apate Hifadhi

Kwa Ndugu Katika Eneo Hili La Karibu Hadi Wakati Wa Mkutano Mkuu wa General Konferensi, Ambapo Suala Lake Lingewasilishwa Kwa Watu Wetu. Kaka Andrews Akiwepo, Alikubaliana Kabisa Na Hatua Ya Hao Ndugu." {1T 669.1}

Kutokana na yale ambayo tumejifunza tangu wakati huo juu ya mapokezi hafifu yenye ubaridi na kutokujali ambayo dada More alikutana nayo huko Battle Creek, ni dhahiri kusema kwamba hakuna mtu mmoja anayestahili kukosolewa au kulaumiwa katika suala lake, mume wangu alilitazama jambo hilo katika mtazamo wa huruma sana. Ukweli wote unapojulikana, hakuna mmoja Mkristo anayeweza kumlaumu mwingine isipokuwa kwa washiriki wote wa kanisa hilo ambao waliielewa hali yake na hawakujishughulisha binafsi kwa niaba yake. Kwa kweli lilikuwa jukumu la maafisa kufanya hivyo na kulitaarifu kanisa, ikiwa wengine wasingelizingatia suala hilo. Lakini washiriki binafsi wa kanisa hilo au lingine lolote hawapaswi kuhisi kuwa wana kisingizio cha kutowajali watu kama hao. Baada ya kile kilichosemwa katika gazeti la *Review* juu ya mtumishi huyu wa Kristo aliyejikana nafsi yake, kila msomaji wa gazeti la *Review* huko Battle Creek, baada ya kujua kwamba dada More amekuja mjini, angeondoa visingizio vya wito binafsi na kujiingiza katika mahitaji yake. {1T 669.2}

Dada Strong, mke wa mzee P. Strong, Jr., alikuwa huko Battle Creek wakati huo huo aliokuwepo dada More. Wote wawili walifika katika mji huo siku hiyo hiyo, na wakaondoka kwa wakati mmoja. Dada Strong, ambaye yuko upande wangu, anasema kwamba dada More alitaka kuombewa naye, ili apate kazi, na kisha abaki na watunza Sabato. Dada More alisema alikuwa tayari kufanya kazo upupte, lakini kufundisha lilikuwa chaguo lake la kwanza. Alimwomba pia Mzee A.S. Hutchins awasilishe suala lake kwa ndugu wanaoongoza katika ofisi ya *Review* ili ajaribu kupata shule ili afundishe. Ndugu Hutchins alifanya hivyo kwa furaha. Lakini hakuna msaada uliotolewa, kwani hakuna nafasi ya mwalimu iliyopatikana. Alimwambia pia dada Strong kwamba alikuwa ameishiwa fedha kabisa kwa hivyo ilikuwa lazima aende katika wilaya ya Leelenaw kama asingeweza kupata ajira huko Battle Creek. Aliongea mara kwa mara kwa maneno ya maombolezo ya mguso kwamba alilazimika kuwaacha ndugu zake katika imani. {1T 670.1}

Dada More alimwandikia jamaa ya Bw. Thompson kukubali pendekezo lake la kuishi pamoja na familia yake, na alipenda kungojea hadi atakaposikia kutoka kwake. Dada Strong alienda naye kumtafutia mahali pa kukaa mpaka atakaposikia kutoka kwa Bw. T. Sehemu moja aliambiwa kuwa angeweza kukaa kuanzia Jumatano hadi Ijumaa asubuhi, muda ambao ndio wangeondoka nyumbani. Dada huyu alilifanya suala la dada More lijulikane kwa dada yake, anayeishi karibu, ambaye pia alikuwa mtunza Sabato. Aliporudi alimwambia dada More kuwa asingeweza kukaa naye hadi Ijumaa asubuhi; kwamba dada

yake alisema itakuwa usumbufu kwake. Dada Strong tangu hapo aligundua kuwa kisingizio halisi ni kwamba hakuwa akifahamiana vizuri na dada More. Angeweza kumchukua, lakini hakumtaka. {1T 670.2}

Dada More kisha alimuuliza dada Strong afanye nini. Dada Strong alikuwa ni mgeni tuBattle Creek, lakini alidhani angeweza kumleta katika familia ya ndugu maskini iliyofahamiana naye ambaye hivi karibuni alikuwa amehama kutoka katika wilaya ya Montcalm. Hapa alifanikiwa. Dada More alibaki hapo hadi Jumanne, alipoondoka kwenda katika wilaya ya Leelenaw kupitia njia ya Chicago. Huko alikopa pesa ili amalizie safari yake. Mahitaji yake yalikuwa yanajulikana kwa wengine, angalau, huko Battle Creek, na matokeo ya kujulikana kwa mahitaji yake, hakudaiwa chochote kwa kukaa kwake kwa muda mfupi katika Taasisi hiyo. {1T 670.3}

Mara tu baada ya kurudi kutoka Mashariki, mume wangu aligundua kuwa hakuna chochote kilichofanyika, kama tulivyokuwa tumeomba, kumleta dada More kuja kwetu upesi, mara tu tunaporudi, kisha alimwandikia aje kwetu haraka iwezekanavyo, naye alijibu kama ifuatavyo: {1T 671.1}

"LELAND, WILAYA YA LEELENAW, MICHIGAN,
FEBRUARI 20, 1868.

"Kaka Yangu Mpendwa White: Barua Yako Ya Februari 3 Imepokelewa. Ilinikuta Nikiwa Na Afya Dhaifu, Nikiwa Sijaizoea Baridi Ya Theluji Kali Za Msimu huu hapa Kaskazini, Kuna Theluji Ya Futi Tatu Au Nne Kwenda Chini. Barua Zetu Za Mkono Zinaletwa Na Watu Wenye Viatu Maalumu Vya Theluji. {1T 671.2}

"Siwezi Kufika Kwako Hadi Mwanzoni Mwa Majira Ya Kuchipua Majani. Barabara Ni Mbaya Sana Kwa Sababu Ya Theluji, Hivyo Kusafiri Itakuwa Vigumu. Wananiambia Njia Bora Ni Kusubiri Mpaka Meli Zifunguke Na Kuanza Kazi Hapa Ziwa Michigan, Ndipo Niende Milwaukee, Na Kupata Makimbilio Salama, Kutumia Njia Ya Reli Kuelekea Eneo Lililo Karibu Na Wewe. Nilikuwa Na Tumaini Kuwa Miongoni Mwa Watu Wangu Wapendwa Mara Ya Mwisho Majira ya Kupukutisha Majani, Lakini Sikupata Huo Upendeleo (Wa Kupata Mahali Pa Kuishi).

"Kweli Tunazoziamini Zinaonekana Kuwa Muhimu Zaidi Na Zaidi, Na Kazi Yetu Ya Kuwaandaa Watu Kuwa Tayari Kwa Ajili Ya Ujio Wa Bwana Haipaswi Kucheleweshwa. Hatupaswi Tu Kuwa Na Vazi La Harusi Wenyewe, Bali Tuwe Waaminifu Katika Kuwapendekezea Wengine Kufanya Maandalizi. Ninatamani Ningeweza Kufika Kwako, Lakini Haiwezekani, Au Utendaji Wake Ni Mgumu Katika Hali Yangu Dhaifu Ya Afya Kusafiri Peke Yangu Katika Kipindi Hiki Cha

Baridi ya Theluji. Mkutano Mkuu Wa General Konferensi Unaozungumzia Ni Lini? Na Wapi? Nadhani *Review* Itanijulisha Punde. {1T 671.4}

"Nafikiri Afya Yangu Imenisumbua Katika Kushika Sabato Peke Yangu Kwenye Chumba Changu Cha Baridi; Lakini Sikufikiri Kuwa Ningeweza Kuiweka Mahali Ambapo Mambo Yote Ya Kazi Na Mazungumzo Ya Kidunia Yangekubaliana Na Siku Hiyo, Kama Ilivyo Kwa Watunzao Siku Ya Jumapili. Nafikiri Ni Siku Ya Kufanya Kazi Nyingi Kwa Wale Wanaoitunza Siku Ya Kwanza Ya Juma. Kwa Kweli, Kwangu Haionekani Kwamba Wale Wanaoitunza Siku Ya Jumapili Vizuri Wanaitunza Siku Yoyote Kama Wanavyopaswa. Oh, Jinsi Gani Ninavyotamani Kuwa Pamoja Na Watunza Sabato! Dada White Angependa Kuniona Nikiwa Katika Mavazi Ya Matengenezo. Je, Atapenda Kunitumia Nione Mfano, Nami Nitamlipa Nitakapofika Pale. Nafikiri Kwamba Napaswa Kuwa Na Mwonekano Mzuri Nitakapokuwa Miongoni Mwenu. Napenda Sana Kuwa Hivyo. Dada Thompson Anafikiri Anapenda Kuvaa Mavazi Ya Matengenezo. {1T 672.1}

"Nimekuwa Na Shida Ya Kupumua, Hivyo Sijaweza Kulala Kwa Zaidi Ya Wiki, Nadhani Hili Lilisababishwa Na Bomba La Moshi la Jiko Ambalo Lilijaza Moshi Na Gesi Katika Chumba Changu Wakati Wa Kulala, Nikalala Bila Kuwa Na Hewa Ya Kutosha. Wakati Huo, Sikuwaza Kwamba Moshi Ulikuwa Mbaya Sana, Wala Kuona Kwamba Gesi Chafu Iliyozalishwa Kutoka Kwenye Kuni Na Mkaa Ilikuwa Imechanganyika Pamoja. Niliamka Na Hali Hiyo Ya Kuishiwa Hewa Ambayo Ilinifanya Nisiweze Kupumua Nikalala Chini, Na Masaa Ya Usiku Yaliyobaki Nikawa Nimesimama. Sikuwahi Kujua Hisia Ya Kutisha Ya Kukabwa Koo. Nilianza Kuogopa Kwamba Nisingeweza Kulala Tena. Kwa Hiyo Nilijikabidhi Mikononi Mwa MUNGU Kwa Uhai Au Mauti, Nikimsihi Aniponye Kama Alikuwa Bado Ananihitaji Katika Shamba Lake La Mazabibu; Vinginevyo Sikuwa Na Haja Ya Kuishi. Nilijisikia Kupatanishwa Kikamilifu Na Mkono Wa MUNGU Juu Yangu. Lakini Pia Nilihisi Kuwa Vishawishi Vya Kishetani Vinapaswa Kupingwa. Kwa Hiyo Nilimwamuru Shetani Anipishe, Atoke Nyuma yangu, Na Nikamwambia Bwana Kwamba Siwezi Kugeuza Mkono Wangu Kuchagua Maisha Au Mauti, Bali Kwamba Ningemwambia Yeye ambaye Ananifahamu Kwa Kila Kitu, Na Ningemweleza Yote Kwa Ukamilifu. Hatima Yangu Sikuijua, Kwa Hivyo Nikasema, Mapenzi Yako Ni Bora. Maisha Hayana Maana Kwangu, Nikihusisha Furaha Zake. Utajiri Wake Wote, na Heshima Za Maisha Si Kitu Kwa Kulinganishwa Na Manufaa Yake. Sina Tamaa Navyo; Haviwezi Kuridhisha Au Kujaza Utupu Wenye Maumivu Ulioachwa Na Majukumu Ambayo Sikuyafanyia Kazi. Nisingeishi Bila Manufaa, Na Kuacha Alama Ama Uwazi Usio Na Faida. Na Japo Inaonekana Kuwa Ni Kifo Cha Kuifia Imani, Nimekubali Ikiwa Hayo Ndiyo Mapenzi Ya MUNGU. {1T 672.2}

"Nilimwambia Dada Thompson Siku Iliyotangulia, 'Laiti Ningekuwa Kwa Kaka White, Ningeombewa Na Kuponywa.' Aliuliza Ikiwa Tunaweza Kutuma Kwa Ajili Yako Na Kaka Andrews; Lakini Hilo Lilikuwa Gumu Katika Utendaji, Kwa Sababu

Nisingeweza Kwa Vyovyote Vile, Kuishi Mpaka Ufike. Nilijua Kuwa Bwana Kwa Nguvu Zake Na Kwa Mkono Wake Wenye Uweza Angeweza Kuniponya Hapa, Hilo Lingekuwa Jambo Zuri Kwake. Nilijisikia Usalama Kumtaja Bwana. Nilijua Angeweza Kutuma Malaika Kumpinga Ambaye Ana Nguvu Ya Mauti, Yaani, Ibilisi, Na Nikajisikia Kuwa Angefanya, Likiwa Zuri Kwake. Nilijua, Pia, Kwamba Anaweza Kupendekeza Hatua, Ikiwa Zingekuwa Muhimu Kwa Ajili Ya Uponyaji Wangu, Na Nilihisi Kwa Uhakika Kwamba Angefanya Hivyo. Punde Nilijisikia Nafuu Nikaweza Kulala. {1T 673.1}

"Kwa Hiyo Unaona Bado Mimi Ni Kumbukizi Za Rehema Za MUNGU  Na Uaminifu Kwa Watoto Wake Wanaosumbuka. Hapendi Kuwatesa Wala Kuwahuzunisha Watoto Wa Wanadamu; Lakini Wakati Mwingine Majaribu Yanahitajika Kwa Ajili Ya Kutuadibisha, Kututenganisha Na Dunia Hii-- Na Tunapaswa Kuomba Kwa Ajili Ya Furaha Maridhawa Kupita Ulimwengu Huu Wa Muda. {1T 673.2}

"Sasa Naweza Kusema Na Mshairi:

Bwana, Siyo Jukumu Langu Kuishi, Au Kujitunza,
Nikifa Ama Nikiishi.
Maisha Yakiwa Marefu, Nitafurahi
Kwamba Ninaweza Kutii Kwa Muda Mrefu;
Yakiwa Mafupi, Bado, Kwa Nini Nihuzunike?
Ulimwengu Huu Ni Lazima Upite.
Kristo Haniongozi Katika Vyumba Vya Giza,
Ambavyo Yeye Mwenyewe Hajapita Hapo Kabla.
Yeyote Anayekuja Katika Ufalme Wake,
Lazima Apitie Katika Mlango Wake Bwana.
Njoo, Bwana, Wakati Neema Yako
Imefanya nikutane na Baraka ya Imani;
Kuuona Uso Wako Uliobarikiwa; Maana,
Ikiwa Kazi Yako Duniani Ni Tamu,
Utukufu Wako Utakuwaje Basi?
Nitamaliza Kwa Furaha Malalamiko Yangu Ya Huzuni,
Na Siku Za Uchovu Za Dhambi,
Kujiunga Na Watakatifu Walioshinda
Wanaoimba Sifa Za Yehova.
Maarifa Yangu Ya Hali Hiyo Ni Madogo,
Jicho Langu La Imani Limefifia;
Lakini Inatosha Kwamba Kristo Anajua Yote,
Nami Nitakuwa Pamoja Naye. {1T 673.3}
--Baxter.

"Nilikuwa Na Majira Mengine Ya Kutolala Usiku Uliopita, Na Nikajisikia Dhaifu Leo. Naomba Kwamba Mapenzi Ya MUNGU  Yaweze Kufanikiwa Ndani Yangu Na

Kupitia Mimi, Ikiwa Ni Kwa Uhai Wangu Au Kifo. "Wako Katika Tumaini La Uzima Wa Milele,

"Hana More. {1T 674.1}

"Ikiwa Unajua Njia Yoyote Ambayo Ninaweza Kukufikia Hivi Karibuni, Naomba Unijulishe. {1T 674.2}

H.M."

Ingawa Dada Hana amekufa, angali akinena. Barua zake ambazo nimezitoa, zitasomwa kwa hamu kubwa na wale ambao wamesoma tanzia ya kifo chake katika idadi kadhaa za Gazeti la *Review* za hivi karibuni. Dada huyu angeweza kuwa baraka kwa familia yoyote inayotunza Sabato ambayo ingetambua thamani ya kazi yake, lakini sasa amelala. Ndugu zetu huko Battle Creek na katika eneo hili wangekuwa wamefanya zaidi katika kumpa makazi, yaani nyumba inayomkaribisha Yesu, kwa njia ya mwanamke huyu mcha MUNGU. Lakini fursa hiyo imepita. Wanatoa sababu kuwa wangepata usumbufu. Hawakumfahamu. Alikuwa na umri mkubwa, hivyo angekuwa mzigo. Hisia za namna hii zilimzuia kukaribishwa katika nyumba za wale wanaojiita marafiki wa Yesu, ambao wanautazamia ujio Wake hivi karibuni, na kumfukuza kutoka kwa wale aliowapenda, hadi akaenda kuishi kwa wale waliopinga imani yake, kaskazini mwa Michigan, katika msimu wa baridi ya Theluji (winter), ili apate baridi hadi kufa. Alikufa kifo cha shahidi wa imani kwa sababu ya ubinafsi na uchoyo, tamaa ya pesa ya watu waliodai kuzishika amri za MUNGU. {1T 674.3}

MUNGU katika majaliwa Yake ameleta kesi hii na kutoa karipio baya kwa mwenendo wa wale ambao hawakumkaribisha mgeni huyu. Hakuwa mgeni hasa. Alijulikana kwa sifa zake, na bado hakukaribishwa. Wengi watajisikia huzuni watakapomfikiria dada More pale aliposimama Battle Creek, akiomba makazi kwa watu wa chaguo lake. Na wakati wao, katika mawazo yao, walimfuata kwenda Chicago, kukopa pesa za kukidhi gharama za safari kwenda mahali pake pa mwisho pa kupumzika, - na wakati wanafikiria kaburi hilo katika wilaya ya Leelenaw, ambapo mtu huyu wa thamani aliyetengwa na jamii amelala hapo, - MUNGU wahurumie, wale walio na hatia katika kesi yake. {1T 674.4}

Masikini dada More! Amelala kauri, lakini tulifanya kile tulichoweza. Tulipokuwa Battle Creek Agosti mwishoni, tulipokea barua ya kwanza kati ya hizo mbili nilizozitoa, lakini hatukuwa na fedha za kumtumia. Mume wangu aliomba fedha huko Wisconsin na Iowa, na alipokea dola sabini za kusaidia gharama zetu za mikutano hiyo ya Magharibi, iliyofanyika Septemba iliyopita. Tulitarajia kuwa na fedha za kumtumia mara moja tunaporudi kutoka Magharibi, kumlipia gharama katika nyumba yetu mpya katika wilaya ya Montcalm. {1T 675.1}

Marafiki wakarimu wa Magharibi walikuwa wametupatia fedha zinazohitajika; lakini tulipoamua kuongozana na kaka Andrews kwenda Maine, suala hilo liliahirishwa hadi tukirudi. Hatukutarajia kukaa huko Mashariki zaidi ya majuma manne, ambayo yangetupatia muda wa kutosha kumtumia dada More nauli baada ya kuwa tumerudi, na kumpeleka nyumbani kwetu kabla ya kufungwa kwa safari ya meli katika msimu husika. Na tulipoamua kubaki Mashariki kwa wiki kadhaa zaidi ya muda tulioupanga awali, hatukupoteza muda wowote katika kuwazungumza ndugu baadhi katika eneo hili, tukipendekeza wamtumie dada More Nauli na kumwali, kishaa wampe nyumba mpaka tutakaporudi. Ninasema: Tulifanya kile tulichoweza. {1T 675.2}

Lakini kwa nini tunapaswa kumpendelea huyu dada, kuliko wengine? Je, tulitaka kupata nini kutoka kwa huyu mmishenari aliyechoka? Hakuweza kufanya kazi zetu za nyumbani, na tulikuwa na mtoto mmoja tu nyumbani wakumfundisha. Na, kwa kweli, mengi yasingeweza kutarajiwa kwa mtu aliyechoka kama yeye, ambaye alikuwa amefikia karibu miaka sitini. Hatukuwa na manufaa naye kwa namna mahsusi, bali kikubwa kilikuwa katika kuleta tu baraka za MUNGU ndani ya nyumba yetu. Kuna sababu nyingi kwa nini ndugu zetu wangepaswa kulichukulia kwa shauku suala la dada More kuliko sisi. Hatukuwahi kumuona, na hatukuwa na njia nyingine ya kuijua historia yake, kujitolea kwake katika kazi ya Kristo na kwa wanadamu, kuliko wasomaji wote wa *Review*. Ndugu zetu huko Battle Creek walikuwa wamemwona mwanamke huyu mashuhuri, na baadhi yao waliyafahamu kidogo au zaidi mahitaji na matamanio yake. Hatukuwa na pesa za kumsaidia; wao walikuwa nazo. Tulikuwa tayari tumelemewa na masumbufu na tulihitaji watu hao katika nyumba yetu ambao walikuwa na nguvu na uchangamfu wa ujana. Sisi tulihitaji kusaidiwa, badala ya kusaidia wengine. Lakini ndugu zetu wengi huko Battle Creek wamejiweka katika hali ambayo masumbufu na mizigo ya dada More ingepewa nafasi ndogo sana. Wana muda, nguvu, na angalau uhuru kutoka katika masumbufu. {1T 675.3}

Lakini hakuna mtu aliyejali suala lake kama tulivyofanya. Nilizungumza hata na kusanyiko kubwa kabla hatujaenda Mashariki msimu uliopita wa kupukutisha majani, kwa sababu ya wao kumpuuzia dada More. Nilizungumza juu ya jukumu la kumpa heshima yule mtu ambaye anastahili; ilionekana kwangu kwamba hekima ilikuwa imeondoka mbali na hata kwawatu wenye busara kiasi kwamba hawakuwa na uwezo wa kuthamini thamani ya maadili. Niliwaambia kwamba

kuna wengi kati yao ambao wangeweza kupata muda wa kukutana, na kuimba, na kupiga vyombo vyao vya muziki; wangeweza kutoa pesa zao kwa msanii kuongeza  mfanano wao kwa stadi zao, au wangetumia pesa na muda katika burudani za umma; lakini hawakuwa na kitu cha kumpatia mmishenari aliyechoka ambaye alikuwa ameukubali Ukweli wa sasa kwa moyo mkunjufu na kuja kuishi pamoja na wale wenye imani ya thamani kama yeye. Nililishauri kanisa kusimama na kutafakari kuzingatia kile tulichokuwa tukifanya, na nikashauri kwamba waachane/wazime vyombo vyao vya muziki kwa miezi mitatu na wawe na muda wa kujinyenyekesha mbele za MUNGU kwa kujichunguza nafsi, kutubu, na kuomba hadi walipojifunza madai ambayo Bwana alikuwa nayo juu yao kama watoto Wake wanaomkiri mbele za watu. Nafsi yangu iliguswa na hisia ya makosa ambayo alifanyiwa Yesu katika nafsi ya dada More, na binafsi nilizungumza na baadhi kuhusu hilo. {1T 676.1}

Jambo hili halikufanywa faraghani. Na hata hivyo, licha ya suala hilo kuwekwa wazi, likifuatiwa na kazi kubwa na nzuri katika kanisa huko Battle Creek, hakuna juhudi yoyote iliyofanywa na kanisa hilo kukomboa yaliyopita kwa kumrudisha dada More. Na mmoja, mke wa mmoja wa wachungaji wetu, alisema baadaye: "Sioni haja ya kaka na dada White kukazania na kuhangaika kuhusu dada More. Nadhani hawalielewi suala hilo." Kiukweli, hatukulielewa suala hilo. Ni baya zaidi kuliko tulivyodhani. Ikiwa tungeliielewa, tusingewahi kuondoka Battle Creek mpaka tuwe tumeiweka vizuri mbele ya kanisa dhambi ya kumtesa awaache kama alivyofanya, na hatua zingechukuliwa kumrudisha tena. {1T 677.1}

Mshiriki wa kanisa hilo katika mazungumzo juu ya kuondoka kwa dada More kama alivyofanya, tangu wakati huo alisema kwa dhati: "Hakuna mtu anayejisikia kuchukua jukumu la kesi kama hizi sasa. Ndugu White alikuwa akizisimamia kila wakati." Ndiyo alifanya. Alikuwa akiwapeleka nyumbani kwake mpaka kila kiti na kitanda kilijaa, kisha angeenda kwa ndugu zake na kuwaomba wawachukue wale ambao hakuweza kuwachukua. Ikiwa walihitaji fedha, angewapa na kuwaalika wengine kufuata mfano wake. Lazima wawepo watu Battle Creek wa kufanya kama James White alivyofanya, vinginevyo laana ya MUNGU  italifuata kanisa hilo. Siyo mtu mmoja tu, kuna watu hamsini ambao wanaweza kufanya, zaidi au pungufu ya White alivyofanya. {1T 677.2}

Tunaambiwa kwamba lazima turudi Battle Creek. Hili hatuko tayari kulifanya. Huenda hiil lisiwe wajibu wetu kamwe. Tulisimama tukiwa na mizigo mizito pale hadi tulipokuwa hatuwezi tena kusimama. MUNGU atakuwa na wanaume na wanawake huko wenye nguvu watakaogawana mizigo hii kati yao. Wale wanaohamia Battle Creek, ambao wanakubali nyadhifa huko, ambao hawako tayari kuweka mikono yao katika aina hii ya kazi, ingekuwa bora mara elfu kuwa mahali pengine. Wapo wale ambao wanaweza kuona na kuhisi, na kwa

furaha kumfanyia mema Yesu kupitia kwa watakatifu Wake. Wapeni nafasi ya kufanya kazi watu kama hao. Waacheni wale ambao hawawezi kufanya hivi waende mahali ambapo hawatasimama kuzuia njia ya kazi ya MUNGU. {1T 677.3}

Hii inatumika hasa kwa wale wanaosimamia kazi. Hawa wakikosea, wote wamekosea. Wajibu unavyokuwa mkubwa, ndivyo unaleta maanguko na uharibifu mkubwa katika hali ya kukosa uaminifu. Ikiwa ndugu wanaoongoza hawatekelezi wajibu wao kwa uaminifu, wale walnaoongozwa hawatafanya hivyo. Wale wanaosimamia kazi huko Battle Creek lazima wawe mifano kwa kundi kila mahali. Wakifanya hivi, watapata thawabu kubwa. Ikiwa watashindwa kufanya hivyo, na bado wanazikubali nyadhifa kama hizo, watakuwa na hesabu ya kutisha ya kutoa. {1T 678.1}

Tulifanya kile tulichoweza. Ikiwa tungekuwa na fedha mikoni mwetu katika majira ya joto na msimu msimu wa kupukutisha majani uliopita, Dada More sasa angekuwa nasi. Tulipojifunza hali zetu halisi, kama zilivyoainishwa katika Ushuhuda Na. 13, sisi sote tulilichukulia jambo hilo kwa furaha na tukasema hatukuhitaji jukumu la kuwa na fedha. Hii haikuwa sawa. MUNGU anataka tuwe na mali ili tuweze, kama wakati uliopita, kusaidia mahali ambapo msaada unahitajika. Shetani anataka kufunga mikono yetu kwa njia hii na kuwaongoza wengine kuwa wazembe, wasio na hisia, na wenye tamaa ya mali, ili kazi hiyo ya kikatili iendelee kama ilivyokuwa kwa dada More. {1T 678.2}

Tunaona watu waliotengwa, wajane, yatima, maskini wanaostahili, na wachungaji katika uhitaji, na nafasi nyingi za kutumia mali kwa utukufu wa MUNGU, maendeleo ya kazi Yake, na misaada ya watakatifu wanaoteseka, nami nataka mali ya kutumia kwa ajili ya MUNGU. Uzoefu wa karibu robo ya karne katika safari nyingi zilizogharimu, na hisia juu ya hali ya wale wanaohitaji msaada, inatufanya tupawe stahiki/stadi za kutumia kwa busara pesa za Bwana wetu. Nimenunua vifaa vyangu mwenyewe vya kuandikia (stationery), nimelipia stempu za posta kutoka mfuko wangu mwenyewe, na nimetumia muda mwingi wa maisha yangu kuandika kwa faida ya wengine, na yote niliyopokea kwa kazi hii, ambayo imenichosha na kunidhoofisha sana, isingeweza kulipa hata 1/10 ya pesa niliyotumia katika gharama za posta. Wakati ambapo nimeshinikizwa kutoa pesa fulani na sina, nimeikataa, au nimechukua hatua ya kusema jambo hili linalohitaji msaada kwenye Chama cha Uchapishaji kutenga pesa na kusaidia. Mimi sitafanya hivyo tena. Nitafanya wajibu wangu katika kazi kuliko wakati wowote, lakini hofu yangu ya kupokea fedha ya kutumia kwa ajili ya Bwana imeondoka. Kesi hii ya dada More imeniamsha kabisa kuona kazi ya Shetani katika kutunyima mali. {1T 678.3}

Masikini dada More! Tuliposikia kwamba amekufa, mume wangu aliumia sana na kujisikia vibaya. Sisi sote tulihisi kuwa alikuwa kama mama mpendwa, ambaye mioyo yetu ilikuwa na matamanio naye kuwa naye, ila sasa hayupo tena. Wengine wanaweza kusema, Laiti kama tungekuwa tumesimama katika nafasi ya hao ambao walijua kitu kuhusu matamanio na mahitaji ya dada huyu, tusingefanya kama walivyofanya. Natumaini kamwe hamtalazimika kuvumilia sindano inayochoma dhamiri ambayo wengine waliihisi, wale ambao walikuwa wakipenda sana mambo yao wenyewe na kutokuwa tayari kubeba jukumu lolote katika kesi yake. MUNGU awahurumie wale ambao wanaogopa udanganyifu wa mgeni wasiyemjua kiasi cha kumpuuza mtumishi wa Kristo anayestahili, na anayejitoa kuikana nafsi yake kwaajili ya Kristo. Maneno hayo yalifanywa kama kisingizio cha upuuziaji huu: Tumeng'atwa mara nyingi sana kiasi kwamba tunawaogopa wageni. Je! Bwana wetu na wanafunzi Wake walituelekeza kuwa waangalifu na kuchukua tahadhari kubwa ya kutowakaribisha wageni, ili tusije tukafanya makosa na kung'atwa kwa kupata matatizo ya kumtunza mtu asiyestahili? {1T 679.1}

Paulo anawahimiza Waebrania: "Upendano wa ndugu na udumu." Msijifariji kwa kujidanganya kwamba kuna wakati mawaidha haya hayatahitajika; kwamba upendano wa ndugu utaisha. Anaendelea: "Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hiyo wengine wamewakaribisha malaika bila kujua." Tafadhali someni Mathayo 25:31 na kuendelea (Mathayo 25:31-41). Someni, ndugu zangu, wakati mwingine mnapoichukua Biblia masaa yenu katika ibada ya asubuhi au ya jioni. Matendo mema yaliyofanywa na wale ambao watakaribishwa katika ufalme, alifanyiwa Kristo kupitia kwa watu Wake wanaoteseka. Wale ambao walikuwa wamefanya matendo haya mema hawakuona kwamba walikuwa wamefanya chochote kwa ajili ya Kristo. Hawakuwa wamefanya zaidi ya wajibu wao kwa wanadamu wanaoteseka. Wale wa mkono wa kushoto hawakuweza kuona kwamba walikuwa wamemtendea vibaya Kristo, na hata kumnyanyasa kwa kuyapuuza mahitaji ya watu Wake. Lakini walikuwa wamepuuza kumfanyia Yesu kupitia kwa watakatifu Wake, na kwa upuuziaji huu walipaswa kwenda kwenye adhabu ya milele. Na hoja moja dhahiri ya upuuziaji wao imeelezwa hivi: "Nilikuwa mgeni, nanyi hamkunikaribisha." {1T 679.2}

Mambo haya siyo ya Battle Creek pekee. Nimehuzunishwa na ubinafsi miongoni mwa wale wanaodai kuitunza Sabato kila mahali. Kristo amekwenda kutuandalia makao ya milele, je, sisi tutamzuia kuishi kwetu kwa siku chache tu, kupitia kwa watakatifu Wake ambao wametupwa nje? Yeye Aliiacha nyumba Yake kwa utukufu, ukuu wake na utawala, ili kumwokoa mwanadamu aliyepotea. Yeye Alifanyika masikini ili sisi kupitia umaskini Wake tuwe

matajiri. Yeye Alijisalimisha kwenye matusi, na dharau ili mwanadamu aweze kuinuliwa, na akatoa nyumba ambayo isingeweza kulinganishwa kwa uzuri Wake, na yenye kudumu kama kilivyo kiti cha enzi cha MUNGU. Wale watakaoshinda mwishowe na kuketi pamoja na Kristo juu ya kiti CHAKE cha enzi watafuata mfano wa Yesu, na kwa hiari chaguo la furaha litatolewa, kisha watatoa kafara kwa ajili Yake Bwana kupitia watakatifu Wake. Wale ambao hawawezi kufanya haya kwa moyo mkunjufu wataenda katika adhabu ya milele. {1T 680.1}

## SURA YA 115

## MAPISHI YENYE AFYA

Katika miezi saba iliyopita tumekuwa nyumbani kwa takribani wiki nne tu. Katika safari zetu tumeketi kwenye meza nyingi tofauti, kutoka Iowa hadi Maine. Wengine ambao tumewatembelea wanaishi kulingana na nuru bora waliyonayo. Wengine, ambao wana fursa sawa za kujifunza kuishi kwa afya na heri, hawajachukua hata hatua za kwanza katika matengenezo. Watakuambia kuwa hawajui kupika kwa njia hii mpya. Lakini hawana udhuru katika suala hili la kupika/mapishi; kwani katika kitabu, *How to live*- Jinsi ya Kuishi, kuna mapishi mengi bora, na kitabu hiki kinaweza kufikiwa na wote. Sisemi kwamba mfumo wa upishi unaofundishwa katika kitabu hicho ni mkamilifu. Hivi karibuni naweza kutoa kitabu kidogo kinachoendana na ladha na mtazamo wangu katika mambo kadhaa. Lakini kitabu cha Jinsi ya Kuishi kinafundisha upishi karibu na yale ambayo msafiri atakutana nayo mara nyingi, hata kati ya Waadventista Wa Sabato. {1T 680.2}

Wengi hawahisi kuwa hili ni suala la wajibu, kwa hiyo hawajaribu kuandaa chakula ipasavyo. Hili linaweza kufanywa kwa njia rahisi, yenye afya, na nyepesi, bila matumizi ya mafuta ya nguruwe, siagi, au nyama. Ujuzi lazima uungane kwa urahisi/usahili. Ili kufanya hivyo, wanawake lazima wasome, na kisha taratibu wayaweke yale wanayosoma katika mazoezi kwa kuviondoa vile visivyofaa. Wengi wanateseka kwa sababu hawatajihangaisha kufanya hivi. Kwa watu kama hawa nawaambia: Ni wakati wenu kuamsha nguvu zenu zilizolala na kuanza kusoma. Jifunzeni jinsi ya kupika kwa urahisi, na bado kwa namna ya kupata chakula kitamu na chenye afya (Mambo manne kuhusu chakula: afya, ladha nzuri, gharama na upatikanaji/ufikiaji wake). {1T 681.1}

Kwa sababu ni makosa kupika tu ili kuridhisha ladha, au kukidhi hamu ya kula, hakuna mtu anayepaswa kufikiria wazo kwamba lishe duni ni sahihi. Wengi

wamedhoofishwa na magonjwa, na wanahitaji lishe bora, tele, na iliyopikwa vizuri. Mara nyingi watu husema mkate wa Graham wa ngano isiyokobolewa ni mzito, mchachu, na unakuwa kama umeokwa nusu-nusu tu. Hii ni kwaajili ya upungufu wa hamu ya kujifunza kuupika, na kujali utekelezaji wa jukumu muhimu la mpishi. Wakati mwingine tunapata keki za gem au biskuti laini, iliyokaushwa, isiyookwa, na vitu vingine vya mpangilio huo. Na kisha wapishi watakuambia wanaweza kufanya vizuri sana kwa mtindo wa mapishi wa zamani, lakini, kusema ukweli, familia zao hazipendi mkate wa ngano isiyokobolewa; kiasi kwamba ni bora kwao wakae na njaa  mradi wasiishi kwa njia hii. {1T 681.2}

Keki za gems, mkate wa graham , biskuti laini/scones, na





Nimejisemea mwenyewe: Mimi sishangai. Ni namna yenu ya kuandaa chakula ndiyo inayokifanya kisifae na kikose ladha. Kula chakula kama hicho hakika kungemfanya mtu apate magonjwa ya tumbo na kuvembewa. Hawa wapishi wabaya/duni, na wale ambao wanapaswa kula chakula chao, watakuambia kwa uzito kwamba matengenezo ya afya hayakubaliani nao. Tumbo halina nguvu ya kubadilisha mkate duni, mzito, mchungu kuwa mzuri; lakini mkate huu duni utalibadilisha tumbo lenye afya lenye kuugua. Wale ambao hula chakula kama hicho wanajua kuwa wanapungua nguvu. Je! Hakuna sababu? Baadhi ya watu hawa wanajiita wanamatengenezo wa afya, lakini sivyo walivyo. Hawajui jinsi ya kupika. Wao huoka keki, viazi, na mkate wa ngano isiyokobolewa unaoitwa Graham, lakini wanarudia vile vile, kwa mabadiliko madogo sana ili kuboresha, na mfumo haujaimarishwa. Wanaonekana kufikiria muda umepotea kwa kupata uzoefu kamili katika utayarishaji wa chakula chenye afya, ladha na kinachofaa. Wengine hufanya kana kwamba kile wanachokula kilipotea, na kila kitu ambacho wangeweza kukiweka ndani ya tumbo ili lijae kingefanywa kama vile chakula kilichoandaliwa kwa uangalifu mwingi. Ni muhimu tufurahie chakula tunachokula. Ikiwa hatuwezi kufanya hivyo, tukala ilimradi tule kama mashine tu, tutashindwa kulipata lishe iliyopangwa na kujengwa kama ambavyo tungekuwa tukifaidi na kufurahia chakula tunachoingiza ndani ya tumbo. Tunaundwa na kile tunachokula. Ili kutengeneza kiwango kizuri cha damu,

lazima tuwe na aina sahihi ya chakula, kilichotayarishwa kwa njia inayofaa. {1T 681.3}

Ni jukumu la kiroho/kidini kwa wale wanaopika kujifunza jinsi ya kuandaa chakula chenye afya kwa njia tofauti, ili kiweze kuliwa kwa furaha. Akina mama wanapaswa kuwafundisha watoto wao jinsi ya kupika. Je! Ni tawi gani la elimu ya mwanamke mchanga linaloweza kuwa muhimu kama hili? Kula kunahusiana na uhai. Chakula kidogo, duni, kilichopikwa vibaya huharibu damu kila wakati kwa kudhoofisha viungo vya kutengeneza damu. Ni muhimu sana kwamba sanaa ya upishi ichukuliwe kama moja ya matawi muhimu zaidi ya elimu. Kuna wapishi wazuri, lakini wachache tu. Wanawake wachanga wanaona kuwa ni kujishusha kwa hali ya chini kuwa mpishi. Hivi sivyo ilivyo. Hawaioni mada hiyo kwa mtazamo sahihi. Ujuzi wa jinsi ya kuandaa chakula kiafya, hasa mkate, siyo sayansi duni. {1T 682.1}

Katika familia nyingi tunakuta magonjwa ya tumbo kama kuvembewa, na mara nyingi sababu huwa ni mkate duni. Mama wa familia anaamua kuwa mkate huo haupaswi kutupwa, kwa hiyo wanaula. Je! Hii ndiyo njia ya kuondoa mkate duni? Je! Utauweka ndani ya tumbo ili ubadilishwe kuwa damu? Je! Tumbo lina nguvu ya kufanya mkate mchachu/mchungu kuwa mtamu? Mkate mzito kuwa mwepesi? Mkate ulio na fangasi na kuvunda freshi/mpya? {1T 682.2}

Akina mama wanapuuzia tawi hili katika elimu ya binti zao. Wanabeba mzigo wa masumbufu na shughuli, na wanachoka haraka, wakati binti anaachwa kutembelea. Kuzungumza na watu, kufuma/kushona au kufanya mambo yanayompendeza. Huu ni upendo wa makosa, wema usiofaa. Mama anamjeruhi mtoto wake, jeraha ambalo mara nyingi hudumu maishani mwake. Katika umri ambao anapaswa kuwa na uwezo wa kubeba mizigo ya maisha, hana sifa ya kufanya hivyo. Mabinti kama hawa hataweza kujali wala kubeba mizigo. Wanaenda wakiwa wepesi, bila ya kujiandaa kwa mizigo, wakitoa udhuru katika majukumu haya, wakati mama amekandamizwa chini na mzigo wake wa masumbufu, kama mkokoteni wenye miganda tele. Binti hadhamiri kuwa mtu asiye mwema; lakini yeye ni mzembe na mpuuziaji, vinginevyo angegundua sura ya uchovu inayoashiria usemi wa maumivu juu ya uso wa mama, na angetaka kufanya sehemu yake katika kubeba sehemu nzito ya mzigo na kumpa mama afueni, ambaye lazima apumzishwe kutoka katika masumbufu au aletwe juu ya kitanda cha mateso ya ugonjwa kinachoweza kumletea kifo. {1T 682.3}

Je, kwa nini akina mama wawe vipofu na wazembe katika elimu kwa ajili ya mabinti zao? Nimefadhaika, maana nimetembelea familia tofauti, na kumuona mama akiwa amebeba mzigo mzito, wakati binti, ambaye alionesha uchangamfu wa roho, tena mwenye kiwango kizuri cha afya na nguvu, akiwa hayahisi masumbufu wala mzigo wowote. Wakati ambapo kuna mikusanyiko mikubwa, na familia zikiwa zimelemewa na watu, nimeona mama akibeba mzigo, na masumbufu ya kila kitu juu yake, wakati mabinti wamekaa chini

wakipiga soga na marafiki zao, wakiwa na mazungumzo ya kijamii. Vitu hivi vinaonekana kuwa vibaya sana kwangu kiasi kwamba siwezi kuvumilia kuongea na vijana wasio na fikra na kuwaambia waende kufanya kazi. Mpumzisheni mama yenu aliyechoka. Muongozeni kwenye kiti katika chumba cha kukaa na mumsihi apumzike na kufurahia jamii ya marafiki zake. {1T 683.1}

Lakini mabinti siyo wa kulaumiwa kwa jumla katika jambo hili. Mama ndiye mwenye makosa. Hajawafundisha mabinti zake kwa uvumilivu jinsi ya kupika. Anajua kuwa hawana maarifa katika idara ya upishi, na kwa hivyo hahisi kupumzishwa kutoka katika kazi. Lazima afanye kila kitu kinachohitaji uangalizi, mawazo, na umakini. Wanawake au mabinti wachanga wanapaswa kuelekezwa vizuri katika mapishi. Kwa hali yoyote ile katika maisha yao, haya ni maarifa ambayo yanaweza kutumiwa kwa vitendo. Ni tawi la elimu ambalo lina ushawishi wa moja kwa moja juu ya maisha ya mwanadamu, hasa maisha ya wale wanaopendwa sana. Wake na akina mama wengi ambao hawajapata elimu sahihi na hawana ustadi katika idara ya mapishi, wanawasilisha kila siku mbele ya familia zao chakula ambacho hakijatayarishwa vizuri, ambacho kwa kweli kinaharibu viungo vya mmeng'enyo, na kutengeneza kiwango duni cha damu, na kusababisha mara kwa mara mashambulizi makali ya ugonjwa wa kuvimba kwa tishu na ogani (inflamation) na kupelekea kifo cha mapema. Wengi wamekufa kwa kula mkate mzito, mchungu. Mfano ulielezwa kwangu unaomhusu msichana aliyeajiriwa ambaye alitengeneza mkate mzito, mchachu/mchungu. Ili kuuondoa na kuficha jambo hilo, alitupa kwenye kundi la nguruwe. Asubuhi iliyofuata mwenye nyumba alikuta nguruwe wake wamekufa, na alipochunguza vyombo vya chakula chao, alikuta vipande vya mkate huu mzito. Aliuliza maswali, na msichana huyo alikiri kile alichofanya. Hakuwa na mawazo juu ya athari ya mkate kama huo kwa nguruwe. Ikiwa mkate mzito na mchungu unaweza kuwaua nguruwe, ambao wanaweza kula nyoka na karibu kila kitu cha kuchukiza, utakuwa na athari gani basi kwa kiungo hicho laini/nyororo cha tumbo la mwanadamu? {1T 683.2}

Ni wajibu wa kidini/kiroho kwa kila binti na mwanamke Mkristo kujifunza mara moja kutengeneza mkate mzuri, mtamu, mwepesi kutoka kwenye unga wa ngano ambao haiuakobolewa. Akina mama wanapaswa kuwachukua mabinti zao jikoni pamoja nao wakiwa wadogo sana na kuwafundisha sanaa ya mapishi. Mama hawezi kutarajia mabinti zake kuelewa siri za utunzaji wa nyumba bila elimu. Anapaswa kuwafundisha kwa uvumilivu, kwa upendo, na kuifanya kazi iwe ya kupendeza kadri iwezekanavyo kwa sura yake ya uchangamfu na maneno ya kutia moyo, ya ukubali wake. Ikiwa wanashindwa mara moja, mara mbili, au mara tatu, usiwakemee. Tayari hali ya kukata tamaa inafanya kazi yake na kuwajaribu kusema: "Haina faida; siwezi kuifanya kazi hii." Huu siyo wakati wa kukosoa. Matamanio yanadhoofishwa. Nia inahitaji msukumo wa maneno ya kutia moyo, furaha, na matumaini, kama: "Kamwe usijali makosa uliyoyafanya.

Wewe ni mwanafunzi na sasa unajifunza tu na unapaswa kutarajia kuboronga mambo. Jaribu tena. Weka akili yako juu ya kile unachofanya. Kuwa mwangalifu sana, na hakika utafaulu." {1T 684.1}

Akina mama wengi hawatambui umuhimu wa tawi hili la maarifa, na badala ya kuhangaika na kujisumbua katika kuwafundisha watoto wao na kubeba mapungufu na makosa yao wakati wa kujifunza, wanapendelea kufanya mambo yote wenyewe. Na wakati mabinti zao wanaposhindwa katika juhudi zao, wanawafukuza kwa maneno haya: "Haina maana wewe kuwa hapa; huwezi kulifanya hili au lile. Unanifadhaisha na kunisumbua kuliko unavyonisaidia." {1T 685.1}

Kwa hiyo juhudi za kwanza za wanafunzi zinarudishwa nyuma, na kushindwa huku kwa kwanza kunapunguza shauku yao na bidii ya kujifunza kiasi kwamba wanatahayari kufanya jaribio lingine, hivyo watapendekeza kushona, kufuma, kusafisha nyumba - chochote isipokuwa kupika. Hapa mama ndiye alikuwa na makosa makubwa. Alipaswa kuwaelekeza kwa uvumilivu kwamba kwa mazoezi wanaweza kupata uzoefu ambao utaondoa kujisikia aibu, kukosa raha na kurekebisha hatua zisizofaa za mfanyakazi asiye na ujuzi. Hapa nitaongeza dondoo kutoka kwenye Ushuhuda nambari 10, uliochapishwa mnamo 1864: {1T 685.2}

"Watoto ambao wamedekezwa na kusubiriwa, mara zote wana matarajio; na ikiwa matarajio yao hayatatimizwa, wanavunjika moyo na kukata tamaa. Tabia hiyo hiyo itaonekana katika maisha yao yote; watakuwa wasioweza kujisaidia, wakitegemea msaada kwa wengine, wakitarajia wengine kuwapendelea na kuwasaidia kkwa kuwatii. Na wanapopingwa, hata baada ya kuwa wanaume na wanawake, wanajiona kuwa wamenyanyaswa; na kwa hivyo wanatembea kwa wasiwasi katika safari yao ulimwenguni, bila kuwa na uwezo wa kubeba uzito wao wenyewe, mara nyingi hunung'unika, huudhika kwa urahisi na kuhangaika kwa sababu kila kitu hakiwafai. {1T 685.3}

"Wazazi wenye makosa wanawafundisha watoto wao masomo ambayo yatawaharibu, na pia wanapanda miiba kwenye miguu yao wenyewe. Wanafikiri kwamba kwa kuridhisha matakwa ya watoto wao, na kuwaacha wafuate mwelekeo wao wenyewe, wanaweza kuupata upendo wao. Kosa kubwa kiasi gani! Watoto walioendekezwa hivyo hukua bila kujizuia katika matakwa yao au kujikana nafsi, bila kusalimisha tabia zao za ubinafsi, kutawala wengine, ukali, na kujivuna, na laana kwao wenyewe na kwa wale wote wanaowazunguka. Kwa kiwango kikubwa, wazazi wanashikilia mikononi mwao furaha ya baadaye ya watoto wao. Juu yao kuna kazi muhimu ya kuunda tabia ya watoto hawa. Maagizo na maagizo yaliyotolewa katika utoto wao ,yatawafuata maisha yao yote. Wazazi hupanda mbegu ambayo itakua na kuzaa matunda kwa wema au kwa ubaya. Wanaweza kuwapa wana na binti zao stahiki za kupata furaha au huzuni. {1T 685.4}

"Watoto wanapaswa kufundishwa katika utoto wao kuwa wenye manufaa, kujisaidia, na kuwasaidia wengine. Mabinti wengi wa umri huu wanaweza, bila majuto ya dhamiri, kuwaona mama zao wakifanya kazi kwa kuhenyeka kwa kupika, kuosha, au kupiga pasi, wakiwa wamekaa sebuleni na kusoma hadithi, wakifuma, kushona na kuweka nakshi. Mioyo yao ni kama jiwe lisilo na hisia. Lakini kosa hili linatoka wapi-asili yake nini? Je! ni akina nani ambao kwa kawaida wanapaswa kulaumiwa katika suala hili? Wazazi masikini, waliodanganyika. Hawatilii maanani mema ya baadaye ya watoto wao, na kwa mapenzi yao yenye makosa, wanawaacha wakae kivivu, au wafanye yale ambayo hayana maana kubwa, ambayo hayahitaji mazoezi ya akili au misuli, kisha wanawaacha mabinti zao wavivu kwamba ni wadhaifu. Ni nani amewafanya kuwa wadhaifu? Katika visa vingi hili limefanywa na mwenendo wazazi. Kiasi sahihi cha mazoezi nyumbani kingeboresha akili na mwili. Lakini watoto wanalikosa hili kwa sababu ya maoni ya uongo, hadi wanapochukia kufanya kazi. Hili halikubaliki na haliendani na maoni yao ya ukuu, heshima, na hadhi katika jamii. Inafikiriwa kuwa kuosha vyombo, kunyosha nguo, au kufua nguo kwenye karo haviendani na hadhi ya mwanamke. Haya ndiyo maelekezo yanayotolewa kwa watoto katika kizazi hiki kibaya kuhusu fasheni/mitindo. {1T 686.1}

"Watu wa MUNGU wanapaswa kutawaliwa na kanuni za juu kupita hizi za ulimwengu, zinazotafuta kupima mwenendo wao wote kulingana na mitindo. Wazazi wanaomcha MUNGU wanapaswa kuwafunza watoto kuwa na maisha yenye manufaa……..Waandae kubeba mizigo wakiwa wadogo. Ikiwa watoto wako hawajazoea kufanya kazi, hivi karibuni watachoka. Watalalamika kwa maumivu ya ubavu, maumivu ya mabega, na miguu iliyochoka; nanyi mtakuwa hatarini, kupitia huruma, kufanya kazi hizo ninyi wenyewe, badala ya kuwaruhusu wao kujitesa kidogo tu. Hebu mzigo juu ya watoto uwe mwepesi sana mwanzoni, na kisha uongeze kidogo kila siku, mpaka waweze kufanya kazi kubwa bila uchovu. Kutokuwa na shughuli ni sababu kubwa zaidi ya maumivu ya ubavu na bega miongoni mwa watoto. {1T 686.2}

"Akina mama wanapaswa kuwachukua binti zao kwenda nao jikoni na kuwaelimisha kwa uvumilivu. Tabia na Miili yao vitakuwa bora kwa kazi kama hiyo, misuli yao itapata uimara na nguvu, na tafakari zao zitakuwa na afya njema na kuinuliwa mwisho wa siku. Wanaweza kuchoka, lakini ni pumziko tamu kiasi gani baada ya kazi nzuri yenye manufaa. Usingizi, mrejeshaji utamu wa asili, huimarisha mwili uliochoka, na kuuandaa kwa majukumu ya siku inayofuata. Usiwape pendekezo watoto wako kwamba haijalishi kwamba wanafanya kazi au la. Wafundishe kuwa msaada wao unahitajika, kwamba muda wao una thamani, na kwamba wewe unaitegemea kazi yao." {1T 687.1}

# SURA YA 116

# VITABU NA MAJARIDA

Mzunguko mzuri na usambazaji wa machapisho yetu ni moja ya matawi muhimu zaidi ya kazi ya wakati huu. Hakika ni kidogo kinachoweza kufanyika bila hili. Na watendakazi wetu wanaweza kufanya zaidi katika kazi hii kuliko kundi lingine la watu. Ni kweli kwamba miaka michache iliyopita wahubiri wetu wengi walikuwa wakilipeleka kwa kupitiliza sana suala la uuzaji wa vitabu. Baadhi yao waliviongeza vitabu kwenye maduka na kuvizuia visiuzwe, siyo tu machapisho yenye thamani kidogo, bali pia nakala za bidhaa zisizo na thamani kabisa. {1T 687.2}

Lakini baadhi ya watendakazi wetu sasa hulichukulia kwa kupitiliza lile nililosema katika Ushuhuda nambari 11 juu ya uuzaji wa machapisho yetu katika mtazamo uliopita kiasi. Mtu mmoja katika jimbo la New York, ambaye mzigo wa kazi haumlemei sana, ambaye alikuwa kama wakala, akiwa ameshikilia machapisho mengi, hakuamua kuyauza tena, na akaiandikia ofisi, akisema kuwa machapisho yalikuwa chini ya utaratibu wao. Hii siyo sawa. Hapa nitatoa dondoo kutoka kwenye Ushuhuda nambari 11: {1T 687.3}

"Mzigo wa kuuza machapisho yetu haupaswi kuwa juu ya wachungaji wanaofanya kazi katika Neno na mafundisho. Muda na nguvu zao zinapaswa kuwekwa akiba, ili juhudi zao ziwe kamili katika mfululizo wa mikutano. Muda na nguvu zao hazipaswi kutumiwa kuuza vitabu vyetu wakati vinaweza kuletwa mbele ya watu na wale ambao hawana mzigo wa kuhubiri Neno. Katika kuingia katika maeneo mapya kunaweza kuwa muhimu kwa mtendakazi kuchukua machapisho ili aende nayo kuwauzia watu, na yaweza kuwa muhimu katika hali nyingine pia kuuza vitabu na kufanya biashara kwa ajili ya ofisi ya uchapishaji. Lakini kazi kama hiyo inapaswa kuepukwa wakati wowote inapoweza kufanywa na wengine." {1T 688.1}

Sehemu ya kwanza ya dondoo hii inatimilizwa na sehemu ya mwisho. Ili kuwa wazi zaidi, maoni yangu juu ya jambo hili ni kwamba, watendakazi hao kama vile mzee Andrews, mzee Wagoner, mzee White, na mzee Loughborough, ambao wanasimamia kazi, na ambao wana majukumu mengine mengi zaidi ya masumbufu, mizigo, na kazi, hawapaswi kuongezewa mzigo wa uuzaji wa machapisho yetu, hasa kwenye mikutano ya makambi na Mkutano Mkuu wa General Konferensi. Mtazamo huo ulitolewa ili kuwasahihisha wale ambao kwenye mikutano kama hiyo hadi sasa walishusha hadhi ya kazi yao hadi wakasambaza mbele ya umati bidhaa na kufanya biashara ambazo hazikuwa na uhusiano wowote na kazi hiyo. {1T 688.2}

Wachungaji wetu wanaofurahia hali nzuri ya kiafya, wanaweza kwa usahihi zaidi kushiriki kwa wakati unaofaa katika uuzaji wa machapisho yetu muhimu.

Hasa uuzaji na usambazaji wa kazi zile ambazo umakini wake umehimizwa kwa watu wetu hivi karibuni, wakidai juhudi kubwa kwa haya kwa wakati huu. Ndani ya majuma manne katika ziara yetu kwenye wilaya za Gratiot, Saginaw, na Tuscola, mume wangu aliuza, na kuwapa maskini, vitabu vya thamani ya dola mia nne. Kwanza aliwaelezea watu umuhimu wa vitabu; ndipo wakawa tayari kuvichukua haraka sana kadri alivyowangojea walipokuwa wamesimama kuvinunua vitabu, na wengine wakamsaidia. {1T 688.3}

Kwa nini ndugu zetu hawapeleki ahadi zao kwa ajili ya vitabu, vijuzuu na majarida kwa ukarimu? Na kwa nini watendakazi wetu hawaifanyi kazi hii kwa bidii? Watu wetu wanapaswa kuona kwamba kazi hizi ndizo zinazohitajika ili kuwasaidia wale wanaohitaji msaada. Hapa kuna nafasi ya kuwekeza mali kulingana na mpango uliobarikiwa wa ukarimu. Wakati mwingine tunaweza kuwasoma watu kwa uwazi zaidi kama tunavyosoma vitabu. Kuna wale watu miongoni mwetu ambao waliweka dola kuanzia mia moja hadi elfu moja au zaidi katika Taasisi ya Afya, ambao wameahidi kutoa dola kuanzia tano hadi ishirini na tano tu katika mradi mkubwa wa kuchapisha vitabu, vipeperushi, na majarida, wakiuweka chini Ukweli ambao unahusiana na uzima wa milele. Hii ya afya watu waliona kuwa wanajihusisha na uwekezaji unaolipa. Na hii ya pili ya uchapaji, kama walivyoweza kuamua kutokana na uchache wa ahadi, kwamba itakuwa ni hasara tupu tu. {1T 689.1}

Hatutanyamaza kimya juu ya mada hii. Watu wetu watakuja katika kazi hiyo. Fedha zitakuja. Na tungewaambia wale ambao ni masikini na wanahitaji vitabu: Tumeni oda zenu, zikiwa na taarifa kuhusiana na hali yenu juu ya mali zenu za ulimwengu huu. Tutawatumia kifurushi cha vitabu chenye magombo manne ya Karama za Roho, Jinsi ya Kuishi, Wito kwa Vijana, Wito kwa Akina Mama, Masomo ya Sabato, na chati mbili kubwa, na Ufunguo wa Ufafanuzi. Ikiwa mna sehemu ya vitabu hivi, elezeni mlivyo navyo, nasi tutawatumia vitabu vingine badala yake, au tutatuma tu vile ambavyo hamna. Tumeni senti hamsini kulipa ada ya posta, nasi tutawatumia kifurushi cha dola tano na kuchangia mfuko huo kwa dola nne. [Angalia Kiambatanisho] {1T 689.2}

Katika suala hili la ukarimu wa vitabu, wote lazima watekeleze mpango mkubwa wa ukarimu (charity), kama ambavyo unafanywa katika uchapishaji na uuzaji wa Biblia na majarida ya Marekani. Katika nyanja nyingi, hatua ya hizi jamii za kale kubwa inastahili kuigwa. Ukarimu unaonekana katika ukunjufu wa moyona utoaji, na hufanywa katika mauzo na uchangiaji wa Biblia na majarida. Waadventista wa Sabato wanapaswa kuwa mbele zaidi ya haya Mashirika makubwa ya kutoa Vitabu vya kiroho bure kama American Bible Society, kuhusiana na suala la vitabu kama walivyo katika mambo mengine. MUNGU atusaidie. Vipeperushi vyetu vinapaswa kutolewa kwa mamia kwa gharama ndogo, vikiacha kiasi kidogo kwa ajili ya kulipia gharama ya usafirishaji, na karatasi au boksi la kuvipaki wakati wa kusafirisha, na usimamizi. Na wachungaji na washiriki wanapaswa kushiriki katika usambazaji wa vitabu,

vijikaratasi, na majarida, kuliko hapo awali. Uzeni mahali ambapo watu wana uwezo na wako tayari kununua, na mahali wasipoweza kununua, wapeni vitabu bure. {1T 689.3}

## SURA YA 117

## KAULI MBIU YA MKRISTO

Ndugu mpendwa B: Nilioneshwa kuwa unashawishika sana kutokana na hisia badala ya kanuni thabiti. Unakosa uzoefu wa kina na dhati katika mambo ya MUNGU. Unahitaji kuongolewa kikamilifu katika Ukweli. Moyo wa mtu unapogeuzwa kabisa na kuongoka, kila alicho nacho kinatengwa na kuwekwa wakfu kwa ajili ya Bwana. Bado hujapata uzoefu wa kujitoa na kujiweka wakfu kwa kiasi hiki. Unaupenda Ukweli katika Neno, lakini huudhihirishi upendo huo kwa matendo yako na kwa matunda yako. Matendo yako, ni udhihirisho wa wa upendo wako dhati, au la hali yako ya kutomjali MUNGU, kazi Yake, na wenzako. {1T 690.1}

Je! Kristo alioneshaje upendo Wake kwa wanadamu maskini wanaokufa? Kwa kuutoa kafara utukufu Wake Mwenyewe, utajiri Wake Mwenyewe, na hata maisha Yake ya thamani zaidi. Kristo alikubali maisha ya fedheha na mateso makali. Alijisalimisha kwenye kejeli za ukatili za umati wa watu wenye hasira kali, wauaji, na kwa kifo chenye maumivu makali zaidi msalabani. Kristo alisema: "Hii ndiyo amri Yangu, Mpendane, kama vile Mimi nilivyowapenda ninyi. Hakuna aliye na upendo mkuu kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi ni marafiki Zangu, mkifanya chochote ninachowaamuru." Tunatoa ushahidi wa kuwa marafiki wa Kristo tunapoonesha utii kamili kwa mapenzi Yake. Hakuna ushahidi kusema maneno tu, bila kufanya; bali katika kufanya, kwa kutii, huo ndio ushahidi. Akina nani wanaotii amri ya kupendana kama vile Kristo alivyowapenda wao? Ndugu B, lazima uwe na upendo thabiti, wa kina na usio na ubinafsi kuliko ule uliokuwa nao, ikiwa unatii amri ya Kristo. 1T 690.2}

Unakosa ukarimu. Unajitahidi kufanya kazi ya kujiokoa mwenyewe kutoka katika masumbufu, shida, au gharama kwa ajili ya kazi ya MUNGU. Umewekeza kidogo katika kazi hiyo. Biashara ambayo mwanadamu anaithamini zaidi itaonekana katika uwekezaji wake. Ikiwa ataweka makadirio ya juu kwenye mambo ya umilele kuliko mambo ya kupita, atalionesha hili kwa matendo yake; atawekeza zaidi, na atajitosa zaidi, katika yale ambayo anayathamini juu ya mengine na ambayo mwishowe humletea faida kubwa. {1T 691.1}

Watu wanaojidai kuuamini Ukweli kwa maneno tu watajishughulisha na biashara za ulimwengu, na kuwekeza sana, na kujihatarisha mambo zaidi. Wanapopoteza karibu kila kitu walichonacho, wanakasirika sana, kwa sababu

wanahisi usumbufu wa hasara walizozipata; lakini hawahisi kuwa hatua yao isiyo ya busara imekwamisha na kumaliza mali ya kazi ya MUNGU, na kwamba kama mawakili Wake lazima wanapaswa watoe hesabu kwa huu ubaradhifu wa fedha ya Bwana. Iwapo wangetakiwa kujitosa kwa  kitu, kwa ajili ya kazi ya MUNGU, kuwekeza hata robo ya yale waliyopoteza katika uwekezaji wao binafsi kwenye vitu vya kidunia, wangehisi kuwa mbingu inagharimu sana. {1T 691.2}

Mambo ya umilele hayathaminiwi. Wewe siyo tajiri, hata hivyo moyo wako unaweza kuweka tamaa mbaya juu ya kidogo ulichonacho, na unaweza kushikamana nacho kwa karibu kama milionea kwenye hazina zake. Kidogo, kidogo sana, ndiyo faida utakayoipata katika uwekezaji wako kwenye biashara za ulimwengu; wakati, kwa upande mwingine, ukiwekeza katika kazi ya MUNGU, ukaifanya kazi hiyo iwe sehemu yako, na ukaipenda kama unavyojipenda mwenyewe, na ukawa tayari kujitolea kwa ajili ya maendeleo yake, ukionesha ujasiri na imani yako katika ushindi wake wa mwisho, utavuna mavuno ya thamani, kama siyo katika maisha haya, basi katika maisha bora kuliko haya. Utavuna thawabu ya milele ambayo ina thamani kubwa zaidi kuliko faida yoyote ya kawaida, ya kidunia kwa kuwa hiyo ni ile isiyoharibika nayo ina thamani kuliko iharibikayo. {1T 691.3}

Ndugu B, ulionekana kuwa na shauku ya kujua ni kitu gani kilichosemwa juu ya msimamo wako kanisani na maoni yetu ilikuwa ipi. Ilikuwa kwa jambo hili ndiyo maana nimeiandika. Niliogopa kwa ajili yako kwa sababu ya kile nilichooneshwa juu ya upekee wako. Wewe unajongewa kwa msukumo/msisimko. Unaomba pale tu unapohisi unataka kuomba, na kuhuburi ikiwa ulijisikia kufanya hivyo. Ungeenda kwenye mkutano kanisani ikiwa ulijisikia kufanya hivyo, au ungebaki nyumbani ikiwa hukujisikia. Umekosa kabisa roho ya kujitolea dhabihu. Umeshauriana na matakwa na raha zako mwenyewe, maisha rahisi/bwerere na kujipendeza mwenyewe, badala ya kuhisi kwamba unapaswa kumpendeza MUNGU. Wajibu, wajibu! Kazini kwako kila wakati, kwenye kituo chako cha ulinzi. Je!  Wewe Umejiandikisha kama askari wa msalaba wa Kristo kweli? Ikiwa ndivyo, hisia zako hazikupi udhuru ukimbie majukumu yako. Lazima uwe tayari kuvumilia magumu kama askari mzuri. Nenda nje ya kambi, ukiwa umeibeba aibu; kwani ndivyo alivyofanya Nahodha wa wokovu wako. Sifa za askofu, au mzee au shemasi, zinapaswa kuwa "asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa MUNGU ; asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake, asiwe mwepesi wa hasira,a siwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato ya aibu, baali awe mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake; akilishika lile Neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga.{1T 692.1}

Paulo anaorodhesha karama za thamani zinazotakiwa, na anawasihi ndugu: "Yeye atoaye, na afanye kwa unyenyekevu; msimamizi na asimamie kwa bidii; naye mwenye kutenda jambo la huruma na afanye hivyo kwa furaha. Pendo na

lisiwe na unafiki lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema. Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu; kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana; kwa tumaini, mkifurahi; katika dhiki, mkisubiri; katika kusali, mkidumu; kwa mahitaji ya watakatifu, mkifuata ukarimu." "Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini MUNGU atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli." Hapa kuna uwekezaji wenye busara na salama kabisa; matendo mema yameainishwa hapa na kupendekezwa kwetu, kwako wewe mwenyewe. Hapa kuna faida ya thamani. Hakutakuwa na hatari ya kushindwa hapa. Hazina inaweza kutunzwa mbinguni, mkusanyiko wa kila wakati ambao utampa mwekezaji cheo cha uzima wa milele. Na maisha yake hapa yatakapofungwa, na muda wa rehema ukaisha, anaweza kuwa na uzima wa milele. {1T 692.2}

Ndugu B, wewe siyo mpenzi wa ukarimu, unakwepa mizigo. Unahisi kuwa ni kazi kuwalisha watakatifu na kuangalia mahitaji yao, na kwamba yote unayofanya katika mwelekeo huu yamepotea. Tafadhali soma maandiko hapo juu, na MUNGU akupe ufahamu na utambuzi, ni maombi yangu ya dhati. Kama familia mnahitaji kukuza ukarimu na kupunguza kujijali wenyewe. Pendelea kuwaalika watu wa MUNGU nyumbani kwako, na kwa kadri tukio linavyoweza kuwa, shirikini nao kwa uchangamfu, kwa furaha, ambayo kwayo Bwana amewafanya kuwa mawakili. Usifanye mapendeleo haya kwa kinyongo. Unapowafanyia wanafunzi wa Kristo mambo haya, unamfanyia Yeye; kwa hiyo, unapowafanyia ukarimu watakatifu wa MUNGU kwa kinyongo, unamfanyia kinyongo Yesu. {1T 693.1}

Matengenezo ya afya ni muhimu kwa ninyi wawili. Dada B amekuwa nyuma ya kazi hii nzuri na amevumilia upinzani unaojitokeza wakati hakujua alichokuwa anakipinga. Amepinga shauri la MUNGU dhidi ya nafsi yake. Tamaa isiyo na kiasi imeleta udhaifu na magonjwa, hata kudhoofisha nguvu za maadili, na kumfanya asiweze kuufahamu na kuuthamini Ukweli mtakatifu, thamani ya upatanisho, ambayo ni muhimu kwa ajili ya wokovu. Dada B anaupenda ulimwengu huu. Hajajitenga, katika mapenzi yake na ulimwengu, na kujitoa kikamilifu kama MUNGU anavyotaka. Bwana hataikubali dhabihu nusu. Yote, yote, yote, ni ya MUNGU, na tunahitajika kutoa huduma kamilifu. Paulo anasema: "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma ZAKE MUNGU, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza MUNGU, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya MUNGU yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu. " Ni upendeleo ulioje ulioturuhusu, kuithibitishia na kuijaribu kwa ajili yetu wenyewe akili ya Bwana na mapenzi Yake kwetu.

LisifuJina Lake Pendwa kwa zawadi hii ya thamani! Nimeoneshwa kuwa mshiko wenye nguvu au ushikiliaji vitu wa dada B lazima uvunjwe kutoka katika ulimwengu huu kabla ya kupata ulimwengu mzuri na salama. {1T 693.2}

Ndugu B, unapaswa kwenda kwa uangalifu na kuishusha nafsi chini; kuwa mvumilivu, mpole, na mnyenyekevu. Roho ya upole na utulivu ina thamani ya bei kubwa sana machoni pa MUNGU. Unapaswa kukithamini kile ambacho MUNGU anakiona kuwa cha thamani. Kazi lazima ifanyike kwa ninyi wawili kabla ya kufikia kipimo cha MUNGU. Fanyeni kazi wakati wa mchana kabla ya giza kuingia, maana usiku unakuja ambao hakuna mtu awezaye kufanya kazi. Simameni katika nuru iliyo wazi, ndipo mnapoweza kuiruhusu nuru yenu iangaze ili wengine kwa kuyaona matendo yenu mema wataongozwa kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni. Greenville, Michigan, Januari 23, 1868. {1T 694.1}

## SURA YA 118

## HURUMA NYUMBANI

Mpendwa kaka na dada C: Kesi zako zimeletwa mbele yangu katika maono. Nilivyoangalia maisha yako, yalionekana kuwa yenye makosa mabaya sana. Ndugu C, huna hulka/silka yenye furaha. Na kwa kukosa kwako furaha, unashindwa kuwafurahisha wengine. Haukusitawisha mapenzi, upole, na upendo. Mke wako ameteseka kwa maisha yake yote ya ndoa kwa huruma. Maisha yako ya ndoa yamekuwa kama jangwa – yenye sehemu chache sana ya kijani zilizotazamwa kwa kumbukumbu yenye shukrani. Haikupaswa kuwa hivyo. {1T 694.2}

Upendo hauwezi kuwepo tena bila kujifunua katika matendo ya nje kama ambavyo moto hauwezi kuwaka bila nishati ya mafuta. Wewe, Ndugu C, umehisi kuwa upo katika nyadhifa ya juu sana kuonyesha upole na unyororo wa moyo, kwa matendo ya fadhili, na kuangalia fursa ya kuonyesha mapenzi kwa mkeo kwa maneno ya huruma, kumtakia mema na upole -ukiyaona haya kama mambo ya kuishusha hadhi yako. Unabadilika-badilika katika hisia zako, na unaathiriwa sana na mazingira na yale yanayokuzunguka. Hujahisi kuwa hilo lilikuwa jambo baya, lisilompendeza MUNGU, kuruhusu akili yako kuchotwa kabisa na ulimwengu, kisha unaleta shida zako za ulimwengu ndani ya familia yako, na hivyo kumruhusu adui aingie nyumbani kwako. Ni rahisi kwako kufungua mlango, lakini haitakuwa rahisi kuufunga tena; itakuwa shuguli ngumu sana kumuondoa adui wakati utakapomleta. Acha masumbufu yako ya biashara na mashaka na kero wakati unapoiacha biashara yako. Njoo katika familia yako ukiwa na uso mchangamfu, wenye huruma, upole, na upendo. Hii itakuwa bora kuliko kutumia pesa kwa ajili ya dawa au madaktari katika kumtibu mke wako. Itakuwa afya kwa mwili na nguvu kwa roho. Maisha yenu yamekuwa mabaya

sana. Wote mmefanya sehemu katika kuyafanya yawe hivyo. MUNGU hafurahishwi na shida yenu; mmejisababishia wenyewe kwa kushindwa kujidhibiti na kukana nafsi zenu. {1T 695.1}

Unaruhusu hisia zikupige ngwala na kukuyumbisha. Ndugu C, unafikiri ni kujishushia hadhi kudhihirisha upendo, kuzungumza kwa fadhili na kwa mapenzi. Maneno haya yote ya upole, yaliyo nyororo, wewe unafikiri, ni harufu ya upole na udhaifu, kwamba siyo ya lazima. Lakini mahali pao huja maneno mabaya, maneno ya mafarakano, ugomvi, maudhi na lawama. Je, unayahesabu haya kama maneno ya uungwana, ujasiri na bora, au onyesho la fadhila kwamba wewe ni mwanamume haswa, maonesho ya fadhila kali za jinsia yako? Haijalishi jinsi unavyoweza kuyazingatia, Mwenyezi MUNGU huyaangalia kwa hasira na huyawekea alama katika kitabu CHAKE. Malaika hukimbia kutoka kwenye makao ambayo kuna mabadilishano ya maneno ya ugomvi, mahali ambapo shukrani ni kitu kigeni moyoni, na maneno ya lawama ni kama mipira myeusi kinywani, inayotia madoa mavazi, na kuichafua tabia ya Kikristo. {1T 695.2}

Ulipomuoa mke wako, alikupenda. Alikuwa na hisia nyeti sana, lakini bado alikuwa na umakini upande wako, na ujasiri na maadili mazuri katika upande wake, afya yake haikupaswa kuwa hivyo. Lakini moyo wako wenye ubaridi na ukali ulikufanya uwe kama bonge la barafu linaloelea, likigandisha mfereji wa upendo na mapenzi. Lawama zako na kutafuta kosa vimekuwa kama uharibifu wa mvua ya mawe kwenye mmea mwororo na mchanga. Zimegandisha na kukaribia kuharibu maisha ya mmea. Upendo wako kwa ulimwengu unakula sifa nzuri za tabia yako. Mke wako ni wa mtazamo tofauti sana na mkarimu zaidi. Lakini wakati ambao hata katika mambo madogo, ameonesha silika zake za ukarimu, wewe umehisi kurudishwa nyuma katika hisia zako na kumlaumu. Unaendekeza roho ya ubahili na kinyongo. Unamfanya mke wako ahisi kuwa yeye ni msumbufu, mzigo, na kwamba hana haki ya kutumia ukarimu wake kwa kwa kutumia pesa zenu/zako. Vitu vyote hivi ni vyenye asili ya kukatisha tamaa kiasi kwamba anahisi kutokuwa na tumaini na msaada, na hana nguvu ya kuvumilia, bali anabonyea kwa nguvu ya mlipuko. Ugonjwa wake ni maumivu ya mishipa ya fahamu. Laiti maisha yake ya ndoa yangekubaliwa, angekuwa na kiwango kizuri cha afya. Lakini katika maisha yako yote ya ndoa pepo amekuwa mgeni katika familia yako akifurahia shida yako. {1T 696.1}

Matumaini yaliyokatishwa tamaa yamewafanya nyote wawili kuwa duni kabisa. Hamtapata malipo kwa mateso yenu, kwa kuwa mmeyasababisha wenyewe. Maneno yako mwenyewe yamekuwa kama sumu mbaya kwenye neva na ubongo, kwenye mifupa na misuli. Mnavuna mlichopanda. Hamthamini hisia na mateso ya kila mmoja. MUNGU hafurahii roho ngumu, isiyo na hisia kwa mwingine, ya kupenda ulimwengu mliyonayo. Ndugu C, kupenda pesa ni shina la maovu yote. Wewe umependa pesa, umeipenda dunia; umeutazama ugonjwa wa mke wako

kama jambo baya, la kutisha, la kuchosha, na la gharama bila kujua kuwa kwa kiwango kikubwa kosa lako ndilo limemfanya yeye awe mgonjwa. Hauna roho ya kuridhika. Unakaa juu ya matatizo yako; uhitaji wa kufikirika na umasikini mbele yako kwamba vinakutazama usoni; unajisikia kuteswa, kufadhaishwa, kuugua; ubongo wako unaonekana kuwaka moto, roho yako inasononeka. Hauthamini upendo kwa MUNGU na shukrani ya moyo kwa baraka zote ambazo Baba yako wa mbinguni Mwenye fadhili amekupatia. Unachoona ni usumbufu na taabu tu za maisha. Uwendawazimu wa kidunia hukufunga kama mawingu mazito ya giza nene. Shetani anashangilia kwaajili yako, kwasababu utakuwa na huzuni wakati amani na furaha vinapatikana. {1T 696.2}

Unasikiliza hotuba za mahubiri; Ukweli unakuathiri, na nguvu bora za akili yako huamka kuyadhibiti matendo yako. Unaona ni kiasi gani kidogo ambacho umejitolea kwa MUNGU, jinsi ambavyo ubinafsi umeendekezwa sana, na umesukumwa kuelekea kwenye ushawishi wa Ukweli; lakini unapopita kutoka katika ushawishi huu mtakatifu, unaotakasa, unaoleta afueni na mtulivu, hauuweki Ukweli tena katika moyo wako, na punde unaanguka katika hali ile ile ya utasa, isiyo ya kawaida. Kazi, Kazi, fanya kazi, lazima ufanye kazi; ubongo, mifupa, na misuli hufanyishwa kazi kwa kupitiliza ili kupata fedha ambazo fikra zako zinakuambia kwamba lazima zipatikane, vinginevyo uhitaji na njaa vitakuwa fungu lako. Huu ni udanganyifu wa Shetani, ni moja ya mitego yake ya ujanja na hila ili kukuongoza kwenye upotevu. "Yatosha kwa siku maovu yake." Lakini unajifanyia kipindi cha dhiki kabla ya wakati. {1T 697.1}

Huna imani na upendo na ujasiri kwa MUNGU. Kama ungekuwa navyo, ungemwamini. Unajisumbua mwenyewe kutoka mikononi mwa Kristo, ukihofu kwamba Yeye hatakujali. Afya inatolewa kafara. MUNGU hatukuzwi katika mwili na roho yako, ambavyo ni Vyake. Nyumbani hakuna ushawishi mchangamfu unaotuliza, na mpole ili kukabiliana na uovu ambao ni mkubwa katika asili yako. Nguvu za juu, zilizo bora za akili yako zinashindwa na kutekwa na viungo dhaifu; sifa mbaya za tabia yako zinaendelezwa. {1T 697.2}

Wewe ni mbinafsi, mkali, dikteta na mwenye kiburi. Hupaswi kuwa hivyo. Wokovu wako unategemea utendaji wako utokanao na kanuni - kumtumikia MUNGU kutokana na kanuni, siyo hisia, siyo kwa msukumo. MUNGU atakusaidia utakapohisi hitaji lako la msaada na kuazimia kufanya kazi, ukimtumaini Yeye kwa moyo wako wote katika hatima zote. Mara nyingi umekata tamaa bila sababu ya kutosha. Unaendekeza hisia za chuki. Unayoyapenda na usiyoyapenda yana nguvu. Haya lazima uyazuie. Udhibiti ulimi wako "Mtu ye yote asiyekosea katika neno, huyo ni mtu mkamilifu, na awezaye kuutawala mwili wote pia." Msaada umewekwa juu ya Yule aliye hodari. Yeye Atakuwa nguvu na msaada wako, mlinzi wako wa mbele na nyuma. {1T 698.1}

Je! Ni matayarisho gani unayoyafanya kwa ajili ya maisha bora? Je, ni Shetani anayekufanya wewe ufikirie kwamba nguvu zako zote lazima zitumiwe ili kupatana na ulimwengu huu. Unaogopa na kutetemeka juu ya hatima ya maisha haya, wakati unaupuuzia wakati ujao, uzima wa milele. Uko wapi wasiwasi wako, bidii, unyofu na juhudi, kabla hujashindwa na kupata hasara ya kutisha? Kupoteza kidogo cha ulimwengu huu kwako ni kama janga baya ambalo lingeyagharimu maisha yako. Lakini mawazo ya kuipoteza mbingu wala hayadhihirishi hata nusu ya hofu moyoni mwako. Kupitia juhudi zako za uangalifu za kuyaokoa maisha haya, uko katika hatari ya kuupoteza uzima wa milele. Huwezi kumudu kuipoteza mbingu, kupoteza uzima wa milele, kupoteza uzito wa milele wa utukufu. Huwezi kumudu kupoteza utajiri huu wote, furaha hii ya thamani sana, isiyonenenka, isiyo na kipimo. Kwa nini usitende kama mtu mwenye akili timamu, ukawa mwenye bidii, mwenye juhudi, na mvumilivu katika juhudi zako kwa ajili ya maisha bora, taji isiyo na mwisho, hazina ya milele isiyoharibika, kama unavyofanya katika maisha haya ya unyonge, masikini na duni, yenye hazina dhaifu ambayo inaharibika, ya kidunia? {1T 698.2}

Moyo wako uko katika hazina zako za kidunia, kwa hiyo huna moyo kwa ajili ya mambo ya mbinguni. Haya mambo duni yanayoonekana - ya kidunia - yanafunika utukufu wa mbinguni. Pale hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwa na moyo wako. Maneno yako yatatangaza, matendo yako yataonesha, wapi ilipo hazina yako. Ikiwa ipo katika ulimwengu huu, faida ndogo ya kidunia, wasiwasi wako utaoneshwa katika mwelekeo huo. Ikiwa unajitahidi kwa ajili ya kupata urithi wa milele kwa bidii, nguvu, na juhudi kulingana na thamani yake, basi unaweza kuwa mtahiniwa mzuri wa uzima wa milele, na mrithi wa utukufu. Unahitaji uongofu mpya kila siku. Kuifia nafsi kila siku, utawale ulimi wako kwa lijamu, dhibiti maneno yako, acha manung'uniko na malalamiko yako, usiruhusu hata neno moja la lawama litoke kinywani mwako. Ikiwa hili linahitaji juhudi kubwa, wewe weka hiyo juhudu na kisha; utalipwa kwa kufanya hivyo. {1T 698.3}

Maisha yako sasa ni ya taabu na huzuni, yamejaa utabiri mbaya. Picha mbaya ziko mbele yako; giza la kutokuamini limekufunga wewe. Kwa kuzungumzia upande wa kutokuamini umezidi kuwa katika giza na giza zaidi; umeridhika kwa kukaa juu ya mada ambazo siyo nzuri na kutoridhika. Wengine wanapojaribu kuzungumza kwa matumaini, unaponda kila hisia ya matumaini iliyoko ndani yao kwa kuzungumza kwa bidii na kwa ukali zaidi. Majaribu na mateso yako yameendelea kumfanya mkeo kujawa na mawazo ya kuumiza moyo kwamba unamchukulia yeye kuwa mzigo kwa sababu ya ugonjwa wake. Ikiwa unapenda giza na kukata tamaa, zungumzia hayo basi, kaa ndani yao, na kuifadhaisha nafsi yako kwa kuyaletea mawazo yako kila kitu kinachoweza kukufanya

unung'unike dhidi ya familia yako na dhidi ya MUNGU, na kuufanya moyo wako kuwa kama uwanja usio na mimea tena, na kuonekana kana kwamba umepitiwa na moto, na kuharibu kijani kibichi chote, na kuuacha ukiwa umekauka, mweusi, na mbaya. {1T 699.1}

Una mawazo ya ugonjwa na unastahili huruma. Hata hivyo hakuna mtu anayeweza kukusaidia kuliko wewe mwenyewe. unavyoweza Kama unataka imani, ongea imani; ongea kwa matumaini, na kwa furaha. MUNGU akusaidie kuona mwenendo wako wa dhambi. Unahitaji msaada katika jambo hili, msaada wa binti yako na mke wako. Ikiwa unamvumilia Shetani kudhibiti mawazo yako kama ulivyofanya, utakuwa mateka wake maalum naye atakutumia kuiharibu roho yako mwenyewe na furaha ya familia yako. Binti yako amekuwa na ushawishi mbaya kama nini! Mama, akiwa hapokei upendo na huruma kutoka kwako, ameweka mapenzi yake kwa binti, na amemwabudu sasa. Amekuwa mtoto anayedekezwa, anayeendekezwa, na kuwa mtoto aliyeharibikiwa kupitia zoezi la mapenzi mabaya. Elimu yake imepuuzwa kiasi cha kusikitisha. Laiti angefundishwa majukumu ya nyumbani, akafundishwa kubeba sehemu yake katika mizigo ya familia, sasa angekuwa na afya na furaha zaidi. Ni jukumu la kila mama kuwafundisha watoto wake kufanya sehemu yao maishani, kushiriki mizigo yake, na siyo kuwa mashine zisizo na maana. {1T 699.2}

Afya ya binti yako ingekuwa bora kama angefundishwa kazi za mikono. Misuli na mishipa yake ni dhaifu, legevu, na duni. Je! Anawezaje kuwa tofauti na hivyo wakati wana matumizi madogo? Mtoto huyu ana nguvu kidogo ya uvumilivu. Mazoezi kidogo ya mwili humchosha na kuhatarisha afya. Hakuna unyumbulifu wa misuli na mishipa. Nguvu zake za mwili zimelala kwa muda mrefu kiasi kwamba maisha yake hayana maana. Mama uliyekosea! hujui kwamba kwa kumpa binti yako fursa nyingi za kusoma sayansi, badala ya kumfundisha umuhimu wa kazi za nyumbani, unamjeruhi sana? Zoezi hili lingeimarisha nguvu, au kuthibitisha viungo vyake vya mwili na kuboresha afya yake. Badala ya huku kuwa laini kwake kuthibitisha baraka, utathibitisha laana mbaya. Laiti binti angeshirikishwa mizigo ya familia, mama asingezidiwa, na angejiokoa mwenyewe na mateso mengi na kumnufaisha binti yake kila wakati. Binti asingepaswa kuanza sasa kufanya kazi kwa wakati mmoja na kubeba mizigo ambayo kwa umri wake angeweza kuimudu, bali anaweza kujielimisha kufanya kazi za mwili kwa kiwango kikubwa zaidi ya vile ambavyo amewahi kufanya maishani mwake. {1T 700.1}

Dada C ana mawazo ya ugonjwa. Amejitenga peke yake kutoka kwenye hewa bora nje, mpaka ameshindwa kuvumilia bila usumbufu. Joto la chumba chake ni hatari sana kwa afya, hakika linamjeruhi. Mzunguko wake wa damu ni dhaifu. Ameishi katika hewa nzito sana kiasi kwamba hawezi kuvumilia safari ya kutoka nje ya nyumba bila kuona mabadiliko. Afya yake duni ni kwa sababu ya

kukosa hewa, na amekuwa dhaifu sana kiasi kwamba hawezi kupata hewa safi bila kumfanya kuwa mgonjwa. Ikiwa ataendelea kuendekeza mawazo haya ya kuugua, hataweza kuvumilia hata kuvuta mara moja pumzi ya hewa. Anapaswa kuwa na madirisha yaliyofunguliwa kwenye chumba chake wakati wote wa mchana, ili kuwe na mzunguko wa hewa. MUNGU hafurahishwi naye kwa kujiua huku. Dhiki hii siyo ya lazima. Amekuwa nyeti kuhusiana na hewa kwa kuendekeza akili yake kuhusu kuugua. Anahitaji hewa,na lazima hewa awe nayo. Yeye aharibu nguvu na uhai wake tu, bali hata nguvu na afya ya mumewe na binti yake, na wote wanaomtembelea. Hewa ndani ya chumba chake ni mfu, chafu na isiyofaa; hakuna wanaoweza kuwa na afya wakiyazoea mazingira kama haya. Amejiendekeza katika suala hili kiasi cha kutoweza kutembelea nyumba za ndugu zake bila kupata mafua na kikohozi. Kwa ajili yake na kwa ajili ya wale walio karibu naye, lazima alibadilishe hili; anapaswa kujizoeza kwenye hewa, akiiongeza kidogo kila siku, mpaka aweze kupumua hewa safi, inayoimarisha bila maumivu. Ngozi ya uso wake inakaribia kufa, kwa sababu haipati hewa ya kuvuta. Vinyweleo vyake milioni vimefungwa, kwa sababu vimefungwa na uchafu wa mfumo, na kwa kukosa hewa. Lingekuwa jambo lisilo na wema kuruhusu upepo mwingi mara moja kutoka nje, kwa siku nzima. Hebu viwango vya hewa vibadilike hatua kwa hatua, ingiza hewa kidogo kidogo. Kwa juma moja anaweza kufungua madirisha inchi tatu au nne, mchana na usiku. {1T 700.2}

Mapafu na ini ni dhaifu kwa sababu anajinyima hewa muhimu. Hewa ni mbaraka wa bure wa mbinguni, uliokusudiwa kuwezesha kuleta umeme wa nguvu kwenye mfumo mzima. Bila hewa mfumo utajawa na magonjwa na kulala, kuwa dhaifu, na duni. Lakini kwa miaka mingi mmekuwa mkiishi katika kiwango kidogo cha hewa. Kwa kufanya hivyo, mke wako huwaleta wengine katika mazingira hayo ya sumu pamoja naye. Hakuna yeyote kati yenu anayeweza kumiliki akili safi, ambazo hazijafifia kwa kugubikwa mawingu wakati mnavuta hewa yenye sumu. Dada C anaogopa kukoroga mambo kwa kwenda popote kwa sababu lazima atahisi mabadiliko ya angahewa na apate mafua. Bado anaweza kuletwa katika hali bora zaidi ya kiafya ikiwa atajitendea mambo kwa usahihi. Mara mbili kwa juma anapaswa kuoga mwili mzima (hydrotherapia), maji yaliyopoa zaidi, yaani baridi zaidi kwa kadri itakavyokubalika, kisha baridi kidogo kila wakati tena, hadi ngozi itakapoimarika kwa toni nzuri. {1T 701.1}

Hapaswi kuzorota kila wakati , daima kuwa na ugonjwa, endapo nyote kama familia mtatii maagizo yaliyotolewa na Bwana. "Kwa maana, Atakaye kupenda maisha, Na kuona siku njema, Auzuie ulimi wake usinene mabaya, Na midomo yake isiseme hila. Na aache mabaya, atende mema; Atafute amani, aifuate sana. Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio Yake husikiliza maombi yao; Bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya." Akili iliyoridhika, roho yenye furaha na kuchangamka, ni afya kwa mwili na nguvu

kwa roho. Hakuna kinacholeta matokeo ya magonjwa kama ilivyo huzuni, sonona, majonzi, na masikitiko. Huzuni ya akili inayosononeka ni taabu. Ninyi nyote mnateseka nayo. Binti anaudhika kwa urahisi, ni mkali, anashiriki roho ya baba; kisha kuna hali ya joto, iliyokandamizwa, inayopunguza nguvu, inadidimiza ubongo. Mapafu yanasinyaa, ini halifanyi kazi. {1T 702.1}

Hewa, hewa, fadhila ya thamani ya mbinguni ambayo wote wanaweza kuwa nayo, itakubariki kwa ushawishi wake utiao nguvu endapo hautakataa iingie. Ikaribishe, kuza upendo wake, nayo itathibitisha kuwa kitulizo cha thamani kwa mishipa. Hewa lazima iwe katika mzunguko wa kila wakati ili iendelee kuwa safi. Ushawishi wa hewa safi, unaifanya damu izunguke kwa afya katika mfumo. Inaburudisha mwili na kuleta nguvu na afya, wakati huo huo ushawishi wake unahisiwa na akili, ikitoa umakini na utulivu. Hewa inasisimua hamu ya kula, na kusaidia mmeng'enyo wa chakula kuwa kamilifu zaidi, na kuleta usingizi mzuri na mtamu. {1T 702.2}

Madhara yanayotokana na kuishi katika vyumba vilivyofungwa, visivyo na hewa safi inayozunguka ni haya: Mfumo unakuwa dhaifu kwa kubinywa na usiofaa kiafya, mzunguko unakuwa duni, damu hutembea taratibu katika mfumo kwa sababu haijasafishwa na kuimarishwa na hewa safi, yenye nguvu ya mbinguni. Akili inakuwa na huzuni na majonzi, wakati mfumo mzima ukidhoofika; homa na magonjwa mengine ya papo hapo yanazalishwa. Kujitenga kwako na hewa ya nje na hofu ya kuwa na hewa inayozunguka kwa uhuru ndani kumekufanya uvute hewa mbaya, chafu ambayo hutolewa kutoka kwenye mapafu ya wale wanaokaa katika vyumba hivi, na ambayo ni sumu, isiyofaa kwa msaada wa maisha. Mwili unasinyaa, ngozi inakauka na kuwa ya manjano, mmeng'enyo unapungua, na mfumo unaathiriwa sana na mafua. Uingizaji wa hewa kidogo tu huleta magonjwa makubwa. Uangalifu mkubwa unapaswa kufanyika siyo kwa kukaa kwenye upepo mwingi au kwenye chumba chenye baridi ukiwa umechoka, au wakati wa jasho. Unapaswa kujizoesha kuwa katika joto la wastani, huna ulazima wa chumba chako kuwa na zaidi na joto la zaidi ya Fahrenheit 65 au centigrade 18. {1T 702.3}

Unaweza kuwa na familia yenye furaha ikiwa utafanya kile ambacho MUNGU amekuelekeza ufanye na amekuamuru kama jukumu. Lakini Bwana hatakufanyia yale ambayo amekuachia wewe ufanye. Ndugu C anastahili huruma. Kwa muda mrefu amejisikia kutokuwa na furaha hadi maisha yamekuwa mzigo kwake. Haifai kuwa hivi. Mawazo yake ni ya ugonjwa, na kwa muda mrefu ameweka macho yake kwenye picha nyeusi kiasi kwamba anapokutana na shida au kukatishwa tamaa, anafikiria kuwa kila kitu kitaharibika, kwamba ataingia katika uhitaji, kwamba kila kitu kinampinga, kwamba yeye ana wakati mgumu zaidi ya mtu yeyote; na hivyo maisha yake yana fadhaa, yana ole. Kadri anavyofikiria hivi, ndivyo maisha yake na ya watu

wote wanaomzunguka yanavyozidi kuwa ya taabu. Hana sababu ya kujisikia anavyojisikia; yote hii ni kazi ya Shetani. Hapaswi kumruhusu adui aidhibiti akili yake. Anapaswa kuachana na picha ya giza na ya huzuni na kuitazama ile ya Mwokozi Mwenye upendo, utukufu wa mbinguni, na urithi mkuu ulioandaliwa kwa ajili ya wote walio wanyenyekevu na watiifu, na wenye mioyo ya shukrani na imani ya kudumu katika ahadi za MUNGU. Hili litamgharimu juhudi, mapambano; lakini haya lazima yafanyike. Furaha yako ya sasa na ya baadaye, furaha ya milele hutegemea jinsi ulivyoiweka akili yako katika vitu vya furaha, ukigeuka kutoka kwenye picha ya giza, ambayo ni ya kufikirika, kwenda kwenye faida ambazo MUNGU amezitawanya katika njia yako, na zaidi ya haya, kwa yasiyoonekana na ya milele. {1T 703.1}

Upo katika familia yenye akili zisizo na usawa/balansi, zenye huzuni, zilizozononeka na majonzi, zinazoathiriwa na mazingira na ushawishi. Ikiwa hautakuza moyo wa uchangamfu, wenye furaha, na wenye shukrani, mwishowe Shetani atakufanya mateka wa mapenzi yake. Unaweza kuwa msaada, nguvu kwa kanisa lako mahalia, ikiwa utatii maagizo ya Bwana badala ya kwenda kwa hisia, bali kwa kanuni. Kamwe usiruhusu lawama zitoke katika kinywa chako, maana ni kama mvua ya uharibifu kwa wale wanaokuzunguka. Hebu maneno ya uchangamfu, ya furaha, na ya upendo yatoke katika kinywa chako. {1T 704.1}

Ndugu C, mfumo wa mwili wako siyo mzuri kwa maendeleo yako ya kiroho, lakini neema ya MUNGU inaweza kufanya mengi kurekebisha kasoro katika tabia yako na kuimarisha na kukuza zaidi uimara wa akili ambazo sasa ni dhaifu na zinahitaji kuwa imara. Kwa kufanya hivyo utadhibiti zile sifa za chini ambazo zimezikanyaga zile za juu. Wewe ni kama mtu ambaye hana busara. Unahitaji kuufanya Ukweli ukushikile vizuri na ufanye matengenezo kamili katika maisha yako. "Msifanane na ulimwengu huu; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua mapenzi ya MUNGU yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu." Hili ndilo unalohitaji, na ambalo lazima ulipate katika mtindo wako wa maisha - mabadiliko ambayo utakaso utakuathiri kupitia Ukweli. {1T 704.2}

Je! Unaamini kuwa mwisho wa mambo yote umekaribia, na kwamba matukio ya historia ya dunia hii yanakaribia kufungwa? Ikiwa ndivyo, ioneshe imani yako kwa matendo yako. Mwanadamu huonyesha imani yote aliyonayo. Wengine wanafikiri kwamba wana imani nzuri, wakati hata pale wanapofikiri kuwa wana Imani yoyote, imekufa, kwa maana haidumishwi na matendo. "Imani bila matendo, imekufa ikiwa peke yake." Wachache wanayo imani hiyo ya kweli inayofanya kazi kwa upendo na kutakasa roho. Lakini wote ambao wamehesabiwa kuwa wanastahili uzima wa milele lazima wapate sifa ya maadili. "Wapenzi, sasa tu wana wa MUNGU, na bado haijadhihirika tutakavyokuwa; lakini tunajua ya kuwa, atakapodhihirika tutafanana Naye; kwa maana tutamwona jinsi alivyo. Na kila mtu aliye na tumaini hili Kwake

hujitakasa, kama Yeye alivyo safi. " Hii ndio kazi iliyo mbele yako, na huna muda mwingi ikiwa utashiriki katika kazi hiyo kwa roho yako yote. {1T 704.3}

Lazima uifie nafsi yako, na lazima uishi kwa ajili ya MUNGU. "Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa MUNGU." Haupaswi kushauriwa na ubinafsi. Kiburi, kujipenda, ubinafsi, uchu, tamaa, upendo kwa ulimwengu, chuki, mashaka, wivu, kushuku watu mabaya, kusengenya watu, lazima yote yatiishwe na kutolewa kafara milele. Kristo atakapotokea, hautakuwa muda wa kurekebisha maovu haya na kisha kuwa na uadilifu kwa ajili ya ujio Wake. Maandalizi haya hayana budi kufanywa kabla ya Yesu kuja. Hii inapaswa kuwa mada ya fikra, ya kujizoeza, ya kujifunza, na swali la dhati, Je! Tufanye nini ili tupate kuokolewa? Je! Mwenendo wetu utakuwaje ili tujioneshe kuwa tumekubaliwa na MUNGU ? {1T 705.1}

Unapojaribiwa kunung'unika, kulaumu, na kuendekeza hasira au kuudhika, ukiwajeruhi wale walio karibu nawe, na kwa kufanya hivyo unajeruhi roho yako mwenyewe, oh! hebu swali la kina, la dhati, na shauku litoke katika nafsi yako, Je! nitasimama bila kosa mbele ya kiti cha enzi cha MUNGU? Ni wasio na hatia tu ndio watakaokuwepo. Hakuna watakaohamishwa kwenda mbinguni ilhali mioyo yao imejazwa na gabeji/takataka za dunia. Kila kasoro katika tabia ya maadili inapaswa kwanza kurekebishwa, kila doa liwe limeondolewa na damu ya Kristo itakasayo, na kuzishinda sifa zote mbaya za tabia, zisizopendwa. {1T 705.2}

Je, ni muda gani unaokusudia kuuchukua ili kujiandaa kuletwa katika jamii ya malaika wa mbinguni katika utukufu? Katika hali mliyonayo wewe na familia yako kwa sasa, mbingu yote ingeharibiwa ikiwa mngeingizwa humo. Kazi lazima ifanyike kwako hapa hapa duniani. Dunia hii ndipo mahali pa kufanyia maandalizi ya kupata stahiki za kuingia huko. Wewe huna hata nukta moja ya kupoteza. Mbinguni yote ina usawa, mapatano, amani, na upendo. Hakuna ugomvi, hakuna vita, hakuna lawama, hakuna maneno yasiyo ya upendo, hakuna uso wenye mawingu ya huzuni, hakuna mikwaruzo huko; na hakuna mtu atakayeingizwa pale akiwa na moja ya vitu hivi vinavyoharibu amani na furaha. Jifunze kuwa tajiri katika matendo mema, uwe tayari kugawa mali zako, ukishirikiana na wengine kwa moyo, na kujiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili upate kuushika uzima wa milele. {1T 705.3}

Daima acha manung'uniko yako juu ya maisha haya duni, bali mzigo wa roho yako uwe ni kwa jinsi gani utapata maisha bora kuliko haya, hatili miliki kwenye majumba yaliyoandaliwa kwa wale ambao ni wakweli na waaminifu hadi mwisho. Ukifanya makosa hapa, kila kitu kinapotea. Ikiwa utatumia

maisha yako yote kupata hazina za kidunia, na kupoteza hazina ya mbinguni, utakuja kuona kwamba umefanya kosa kubwa sana. Huwezi kupata ulimwengu na mbingu. "Je! Itamfaidi nini mtu, ikiwa ataupata ulimwengu wote, na kuipoteza nafsi yake mwenyewe? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?" Anasema Paulo aliyevuviwa: "Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya kitambo kidogo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele. " {1T 706.1}

Majaribu haya ya maisha ni vitendea kazi vya MUNGU vinavyoondoa uchafu, udhaifu, na ukali kutoka katika tabia zetu, na kutufanya tufae katika jamii ya malaika safi, wa mbinguni katika utukufu. Lakini kadri tunapopita katika majaribu haya, wakati moto wa taabu unapowaka juu yetu, hatupaswi kuweka macho kwenye moto unaoonekana, bali jicho la Imani likazwe kwenye vitu visivyoonekana, urithi wa milele, uzima wa kutokufa, uzani wa milele wa utukufu; na tunapofanya hivi moto hautatuteketeza, bali utaondoa taka, na tutatoka mara saba safi, tukiwa tumetakaswa kabisa, tukiwa na mvuto wa Kiungu.

Greenville, Michigan, Machi 7, 1868. {1T 706.2}

# SURA YA 119

# NAFASI YA MUME

Wapendwa ndugu na dada: Nilipokuwa nikiongea kwenye mkutano Jumapili alasiri, moyo wangu haukuweza kuacha kuyaita majina yenu na kuelezea mambo kadhaa ambayo nimeoneshwa. Niliona kwamba ndugu D hajashika nafasi katika familia yake ambayo MUNGU angemtaka kuwa nayo. Dada D ndiye anayeongoza; anayo nia ngumu (kichwa kigumu), ambayo haijatiishwa kama MUNGU anavyotaka; na ili kumpendeza mkewe na kumuepusha kukata tamaa, kukosa ujasiri na kukosa matumaini, Ndugu D amejisalimisha kwake na kuendana na mambo jinsi mke anavyotaka. Maamuzi/yake yamemyumbisha, na amekuwa si mtu huru kwa miaka mingi. {1T 707.1}

Wakati ndugu D alipojishughulisha kwa mara ya kwanza katika kazi ya kufundisha Ukweli, alikuwa mdogo machoni pake mwenyewe, na MUNGU alimtumia kama chombo CHAKE. Lakini niliona kuwa katika kipindi kilichopita yeye hajajinyenyekeza chini ya mkono wa MUNGU. Ameiamini hekima yake mwenyewe na maamuzi dhaifu, na Shetani amekuwa akinufaika juu yake. Badala ya kumtegemea MUNGU pekee yake, na kukaa katika nguvu Zake, uamuzi Wake umepotoshwa na ushawishi wa mkewe. Mkewe amesimama katika nafasi ya kuona, kusikia, kuelewa, na yote yaliyokuwa yakiendelea kumzunguka. Kama angekuwa na uamuzi uliotakaswa na hekima ya mbinguni, angeweza kuona kwa macho yaliyotakaswa, na kusikia kupitia masikio yaliyotakaswa. Angeweza kutumia vizuri macho na masikio yake. Lakini hajafanya hivi. "Ni nani aliye kipofu, ila mtumishi Wangu? Au kiziwi kama mjumbe wangu niliyemtuma?" MUNGU hataki tusikie yote yatakayosikika, au kuona yote yatakayoonekana. Ni baraka kubwa kuziba masikio, ili tusisikie, na macho, ili tusitazame. Tashwishwi kubwa inapaswa kuwekwa kwenye uhitaji wa kuwa na macho yaliyo wazi ili kutambua mapungufu yetu wenyewe, na masikio mepesi ili kudaka maonyo na mafundisho yote yanayohitajika, isije kwa kukosa umakini na uzembe tukateleza na kuwa wasikiaji wasahaulifu wasio watendaji wa kazi. {1T 707.2}

Ndugu D, kwa muda uliopita kazi zako hazijaelekezwa kwa busara na mafanikio kama zamani. Mwenendo wako katika utendaji haujabeba mguso wa MUNGU. Mke wako amesimamia mambo yako ya kidunia na kubeba mizigo ambayo ilikuwa mizito sana kwake kubeba, wakati wewe haupo. Hili limesisimua huruma yako, na kuwa na tabia ya kupotosha maamuzi yako, kiasi kwamba umeweka makadirio ya juu sana juu ya sifa za mke wako kwa sababu ya uwezo wake katika kusimamia mambo yako ya kidunia. Shetani amekuwa akiangalia fursa yake ya kufanya kadri iwezekanavyo kwa faida yake mwenyewe katika imani yako kwa mke wako. Adui amekusudia kuwakanyaga na kuwaangamiza nyote wawili. Kwa kiwango kikubwa umemtupia mkeo uwakili wako. Hili ni kosa; mke atakuwa na kila kitu anachoweza kufanya ili kubeba sehemu yake ya wajibu, bila kubeba kile kinachokuhusu na ambacho utawajibika kwacho mbele za MUNGU. {1T 708.1}

Dada D amedanganywa katika baadhi ya mambo. Amefikiria kwamba MUNGU alimwagiza kwa namna maalum, na nyote mmeamini na kutenda kwa kuendana na hilo. Utambuzi ambao amedhani alikuwa nao kwa namna maalum, ni udanganyifu wa adui. Yeye ni mwepesi kuona, mwepesi kuelewa, mwepesi kutarajia, na ana asili ya moyo ulio rahisi zaidi kuyumbishwa. Shetani ametumia faida ya sifa hizi na amewapotosha nyote. Ndugu D, umekuwa mtumwa kwa muda mrefu sana. Mengi ya yale ambayo dada D anafikiria kuwa utambuzi ni wivu tu. Amejielekeza kuchukulia kila kitu kwa jicho la wivu,

kutuhumu, kufikiria uovu, kushuku wengine na kutoamini karibu kila kitu. Hii inasababisha kutokuwa na furaha ya akili, kukata tamaa, kukosa matumaini na mashaka, ambapo imani na ujasiri vinapaswa kuwepo. Sifa hizi za tabia zisizo na furaha hubadilisha mawazo yake kuwa mfereji wa huzuni, ambapo hujiingiza katika hofu ya kufikiri mabaya au baa fulani litatokea, wakati silka yake nyeti humwongoza kufikiria kutelekezwa, kudharauliwa, kukosewa heshima na kuumizwa/maumivu, wakati hayapo. Mambo yote haya husimama katika njia ya maendeleo ya kiroho kwenu ninyi wawili, na yanawaathiri wengine kwa kiwango ambacho mmeunganishwa na kusudi na kazi ya MUNGU. Kuna kazi kwa ajili yenu ya kufanya: Nyenyekeeni chini ya mkono wa MUNGU wenye nguvu, ili mpate kuinuliwa kwa wakati unaofaa. Sifa hizi za tabia zenye kuleta huzuni, zenye nguvu na zenye nia iliyokazwa, lazima zirekebishwe na zifanyiwe marekebisho, vinginevyo zitawafanya ninyi wawili kuharibikiwa imani yenu mwishowe. {1T 708.2}

Ndugu D, una jukumu la kufanya. Kutenda uwakili ambao wewe umestaafi, na kwa hofu ya MUNGU chukua nafasi yako kama kichwa cha familia yako. Lazima utikiswe ili utoke katika ushawishi wa mke wako, na umtegemee MUNGU kikamilifu, na umtazame Yeye akuongoze na kukuelekeza. MUNGU hajamuelekeza dada D kwa njia yoyote maalumu, wala kumpa nuru kuwafundisha wengine wajibu wao. Wewe wala mke wako hamuwezi kuchukua nafasi ambayo MUNGU angependa muwe nayo, wakati mambo yanabaki kama yalivyo sasa. Kamwe hautathibitishwa, na kuimarishwa, na kutulia hadi hapo utakapomruhusu mke wako kuchukua nafasi inayompasa mke. Mke anapochukua nafasi inayomstahili, heshimu maamuzi yake, shirikiana naye katika mipango yako, lakini kuwa mwangalifu sana juu ya kuuchukulia uamuzi wake kama uamuzi wa MUNGU. Shirikiana na ndugu zako ambao MUNGU ameona inafaa kuwawekea mzigo wa kazi. Kama ungeshauriana hivi na wale ambao ushauri wao ulipaswa kuufuata, usingefanya kosa hili kubwa, kosa la kusikitisha, kama ulivyofanya katika kesi ya E. Kazi ya MUNGU ilijeruhiwa na kushutumiwa katika kesi hii. Mkeo alidhani alikuwa na mwanga katika kesi hii; lakini maoni yake hayakuwa ya MUNGU, bali ya adui, kwa sababu aliona kuwa unaweza kuathiriwa katika mwelekeo huu. Kuamini kwako sana katika maamuzi ya mke wako ni kinyume na utaratibu wa mbinguni. Shetani amepangilia namna hii ili akuangushe kwa kiwango kikubwa, kutokana na ushawishi wa watendakazi wenzako na ndugu zako kwa ujumla. {1T 709.1}

Umekuwa na majaribu ambayo usingekuwa nayo kama usingemfikiria mke wako katika nafasi ambayo MUNGU hajamweka. Una imani kubwa kabisa katika maamuzi na hekima yake. Mkeo hajawekwa wakfu kwa MUNGU, kwa hivyo maamuzi yake hayajawekwa wakfu pia. Yeye siyo mwanamke mwenye furaha, na hali ya kutokuwa na furaha imeifanya akili yake kuiumiza sana afya yake ya mwili na akili. Shetani amekusudia kukutingisha ili ukose mwelekeo na kusababisha ndugu zako wapoteze imani katika maamuzi yako. Shetani

anatafuta kukuangusha. MUNGU atakapomwita mke wako kwenye kazi ya kufundisha Ukweli, basi hapo unapaswa kutegemea nasaha na ushauri wake, na kufuata maagizo yake. MUNGU anaweza kuwapa nyote wawili sifa sawa ili mchukue sehemu muhimu katika kazi hii nzito ya kuokoa roho, kama wenye nia sawa na wenye kujitolea katika kazi hiyo. Kazi kubwa mbele yake ni kuwa na bidii katika kuhakikisha wito wenu na uteule wenu kuwa hakika (2 Pet 1:10), kuacha kuwatazama wengine, na sasa kuanza kazi ya kuwa na wivu mkubwa juu yake mwenyewe. Anapaswa kutafuta kuwabariki wengine kwa mfano wake wa kiungu, uchangamfu wake, uvumilivu, ujasiri, imani, tumaini, furaha, katika uaminifu huo kamili, ujasiri huo kwa MUNGU, ambao utakuwa matokeo ya utakaso kupitia Ukweli. Lazima atembee kikamilifu kwa mapenzi ya MUNGU. Kristo anamwambia: "Mpende Bwana MUNGU wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote. Hii ndiyo amri iliyo kuu tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii. " {1T 710.1}

Maandishi ya hapo juu yaliandikwa huko Mount Pleasant, Iowa, Oktoba 4, 1867. Sikuweza kupata wakati wa kuumaliza ushuhuda na kuunakili, kwa hivyo niliuweka chini kwanza, na sikuwa na wakati wa kuumalizia hadi niliporudi kutoka Mashariki ya Marekani kwenda Greenville, Michigan, wakati nilipouchukua tena, Januari 30, 1868. {1T 710.2}

Wapendwa ndugu na dada: Mngepaswa kuwa na Shuhuda hii hapo zamani, lakini kazi zetu zimekuwa ngumu sana kiasi kwamba sikuweza kupata muda wa kuuandika. Kila sehemu tuliyoitembelea ilileta mambo mengi mbele ya akili yangu ambayo nilikuwa nimeoneshwa juu ya kesi binafsi, na nimeandika katika mkutano, hata wakati mume wangu alipokuwa akihubiri. {1T 711.1}

Nilipewa maono haya karibu miaka miwili iliyopita. Adui amenizuia kwa kila njia ili kuzifanya roho ziikose nuru ambayo MUNGU alikuwa amenipa kwa ajili ya roho hizi. Kwanza, kesi ya mume wangu ilikuwa ya kutatanisha, ya kusumbua sana, kiasi kwamba sikuweza kuandika. Kisha kukatishwa tamaa kwangu kutoka kwa ndugu zangu kuliniweka katika hali ya huzuni na dhiki, na kunifanya nisifae kwa kazi yoyote. Tulipoanza kusafiri msimu uliopita wa majira ya joto, nilianza kuandika, lakini tumesafiri kutoka mahali hadi mahali kwa haraka sana kiasi kwamba tulichoweza kufanya ni kuhudhuria mikutano tu. Kulikuwa na kazi nyingi za kufanywa. Ninafanya mazoezi ya kuamka saa kumi alfajiri, kuanza maandishi yangu. Lakini bado kazi ya mara kwa mara, ya kusisimua katika mikutano inauchosha ubongo hata nisiweze kujiandaa kwa ajili ya kuandika, kichwa changu kimechoka sana. {1T 711.2}

Ninasikitika kwamba sikuweza kukupa shuhuda hii kabla, lakini hata sasa MUNGU aifanye kuwa baraka kwako, ni maombi yangu ya dhati. Wewe, ndugu yangu mpendwa, unaweza kuwa umeona haya na kuyasahihisha kabla ya ushuhuda huu. Natumaini imekuw ni hivyo. Wewe na mke wako pia mna

huruma na maombi yetu. Tunayo shauku kwake na kwako pia. Nafsi yake ni ya thamani. Tunamsihi katika Kristo atafute roho ya upole na utulivu, ambayo machoni pa MUNGU ni ya thamani kubwa. Malaika alinielekeza kwa dada D na kurudia maneno haya: "Mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo." Hapa kuna mlolongo mafunzo yenye afya ya fikra yanayopaswa kufuatwa na akili. Pale akili inapoenda katika njia tofauti, irudishe. Idhibiti akili. Ielimishe kukaa katika vitu vitakavyoleta amani na upendo pekee. {1T 711.3}

Ninaweka hili kwako, nikitumaini na kuomba kwamba MUNGU akubariki, na kwamba nyote wawili mpate kufaa kuhesabiwa kuwa mnastahili uzima wa milele. {1T 712.1}

## KIAMBATANISHO

Kama msaada wa ufahamu wa mazingira yaliyopelekea kutoa shuhuda fulani, taarifa zifuatazo zimetayarishwa na wadhamini wa chapisho la Ellen g. White. {1t 713.1}

Ukurasa wa 116, "muda wa kuanza sabato" - kwa kipindi cha miaka kumi Waadventista watunza Sabato waliitunza Sabato kuanzia Ijumaa saa kumi na mbili jioni hadi Jumamosi saa kumi na mbili jioni. Mzee Joseph Bates katika

kitabu chake kidogo cha kwanza kuhusu umilele wa Sabato ya amri ya nne, kilichochapishwa mnamo mwaka 1846, alikuwa ametoa sababu za msaada za Kimandiko juu ya utunzaji wa Sabato kwa njia hii. Alitoa mfano wa wafanyakazi wa shamba la mizabibu, kikundi cha mwisho kilichoitwa "saa ya kumi na moja jioni" ya siku hiyo na kufanya kazi kwa saa moja. Hesabu ya mshahara ilifanywa kwao "sawa sawa na wengine." mathayo 20: 6, 8, 12. Akililinganisha hili na swali la Kristo, "je, saa zenye mwanga wa jua siyo kumi na mbili?" alizungumzia kuwa "Jioni" ilianza saa kumi na mbili jioni, au saa kumi na mbili kamili, wakihesabu kwa masaa ya ikweta au mwanzo wa mwaka mtakatifu. Kulingana na miaka yake na uzoefu wake na maisha yake ya kumcha MUNGU yaweza kuwa ndiyo sababu kuu za kukubali hitimisho lake bila uchunguzi zaidi. {1T 713.2}

Kadiri muda ulivyopita na ujumbe ulisambaa, idadi kubwa ya watunza Sabato ilivyokuwa ikiongezeka katika idadi, ilihoji desturi hiyo na kutetea muda wa jua kuzama kwa ajili ya kuanza kwa Sabato. Uchunguzi kamili wa Biblia juu ya jambo hili ulitolewa na mzee J.N. Andrews, ambaye aliandikia makala juu ya sababu za Kibiblia zilizopendelea muda wa jua kuzama (Walawi 23:32 na Mwanzo 1 na 2). Makala hii ilianzishwa na kujadiliwa siku ya Sabato, Novemba 17, 1855, kwenye Kongamano hapo Battle Creek, Michigan, na matokeo yake kwa kiasi kikubwa, wote waliokuwepo walishawishika kwamba hitimisho ya mzee Andrews lilikuwa sahihi. Uwasilishaji wa mada hii kwa Bibi White katika maono haya, yaliyotolewa siku mbili baadaye, maono haya yalijibu maswali ya muda mrefu katika akili za wengine na kuleta umoja miongoni mwa waumini. Akitoa maoni juu ya uzoefu huu, kama kielelezo cha kazi/ofisi/huduma ya maono kuthibitisha hitimisho lililotokana na mafunzo ya Biblia badala ya kuanzisha mafundisho mapya, mzee James White baadaye aliandika haya: {1T 713.3}

"swali kwa asili linaanza, kama maono yametolewa ili kusahihisha kosa, kwa nini basi mama White hakuliona mapema hili kosa la saa kumi na mbili kamili? Nimeshukuru sana kwamba MUNGU alisahihisha kosa kwa wakati Wake muafaka, na hakuacha mgawanyiko mbaya uwepo au kutokea kati yetu kwa maelezo haya. Lakini, ndugu msomaji, kazi ya Bwana juu ya dondoo hii ni katika upatanifu kamili na maonesho Yake kwetu kwa ajili ya wengine, na kwa kuhusiana na nafasi sahihi ya vipawa vya Roho. Haionekani kuwa ni shauku ya Bwana kuwafundisha watu Wake kwa njia ya karama za roho juu ya maswali ya Biblia mpaka watendakazi Wake wawe wamelichunguza Neno Lake kwa bidii. Wakati hili lilipofanyika juu ya mada ya muda wa kuanza kwa Sabato, na mengine zaidi kuanzishwa, baadhi walikuwa katika hatari ya kutoka katika mapatano na mwili katika mada hii, kisha, naam, kisha kulikuwa na muda mzuri kwa ajili ya MUNGU kuongeza wema Wake katika udhihirisho wa karama za Roho Wake katika Kutimiza kazi Yake inayofaa. "- *Review and Herald, feb. 25, 1868*. {1T 713.4}

Ukurasa wa 116, 117, 122, 123, "Chama cha Mjumbe *Messenger Party*" - katika kiangazi cha Mwaka 1854 ilitokea chuki au uasi wa kwanza miongoni mwa Waadventista Watunza Sabato. Watu wawili waliokuwa wakihubiri ujumbe walionywa kupitia roho ya unabii kwa roho ya uchungu, ukali, Lawama, tamaa ya mali, na kwa ubaradhifu/ufujaji wa mali zilizowekwa mikononi mwao. Hawa wakawa wenye hasira badala ya kufanya toba, wakajiunga na wengine wachache katika madai yasiyo ya haki dhidi ya Mzee na Bibi. White na viongozi wengine, wakitoa mashtaka ya uongo dhidi yao. Ingawa waliendelea kutangaza Ukweli wa Sabato, walianza uchapishaji wa jarida la uongo waliloiita kuwa ni mjumbe wa Ukweli/*Messenger of Truth*. {1T 714.1}

Waliungana na wazee wa Wisconsin, Stephenson na Hall. Hawa watu Walikuwa wahubiri wa Kiadventista wa siku ya kwanza, waliodai kuupokea Ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu, lakini walioendelea kushikilia mafundisho kuhusu Zama zijazo/Age-to-Come. Kulingana na nadharia hii kulikuwa kuwe na "nafasi ya pili" ya wokovu, katika kipindi cha Milenia cha Ufunuo 20. Walikubaliana, hata hivyo, kuhubiri ujumbe huo, bila kuwasilisha suala hilo na kupata sapoti au kuungwa mkono na umati, ikiwa tu gazeti la *Review* lisingeweza kuchapisha makala kinyume nao. Hata hivyo, Kama ilivyooneshwa katika aya, hawakuitunza ahadi yao na punde walilipinga gazeti la *Review* na wadau wake. {1T 714.2}

Hatua ya hawa "wapinzani wa Ukweli" ilianza mara moja. Wote Stephenson na Hall walipoteza hekima yao. Mjumbe wa Messenger Party alisitisha uchapishaji mnamo 1857, na mapema mwaka 1858 mzee White aliripoti kuhusu chama hicho: "Hakuna hata mmoja kati ya wajumbe kumi na nne ambao awali walijisifu kwamba wako pamoja nao, wanaobeba ushuhuda wa wazi sasa, na hakuna hata sehemu moja ya mikutano ya mara kwa mara yenye maarifa yetu kati yao. "- review and herald,
Jan. 14, 1858. {1T 714.3}

Ukurasa wa 190, utoaji wa mpango kwa ukarimu - katika siku za awali za ujumbe, Watu waliosukumwa na ushawishi walisonga mbele kuhubiri Ukweli Mpya uliopatikana. Walikuwa wategemezi wa msaada wao kwa ajili ya kazi zao wenyewe au sadaka za hiari za waumini. Mbinu hiyo isiyo na uhakika ilikuwa kwa kiasi kikubwa au kidogo ya ghafla na yenye kuyumbayumba. Mapema mwaka 1859 hitaji la mpango makini zaidi ilihisiwa, na utafiti wa dhati ulifanyika kwenye jambo hilo. Kutoka katika utafiti huu walianzisha mfumo uitwao utoaji wa mpango kwa ukarimu (Systematic Benovelance) kulingana na 1 Wakorintho 16:2 utoaji wa mara kwa mara, na endelevu katika siku ya kwanzWya juma ulipendekezwa, na, kama ilivyoshauriwa na 2Wakorintho 8:12-14, ugawaji sawa wa majukumu ya kifedha ulipaswa kufanywa. Mpango uliwataka ndugu kuweka ghalani kila juma kuanzia senti tano hadi ishirini na

tano; na akina dada kuanzia senti mbili hadi kumi; na kwa wamiliki wa mali kutoa kwa wiki kuanzia senti moja hadi tano katika kila dola mia za thamani ya mali zao {1T 714.4}

Kwa ujumla mpango ulipokelewa kwa upendo, na ukaungwa mkono na roho ya unabii. Dhambi kubwa kanisani iliyoonekana ilikuwa ni tamaa. (ukurasa wa 194.) Utoaji wa mpango haukuwasilishwa kama mpango kamilifu, kwa sababu pia ilielezwa kwamba "MUNGU anawaongoza watu Wake" katika hili, na "anawakuza na kuwataka wapande juu". (ukurasa wa 191.) Kadri mipango ya kusaidia kazi na huduma ilivyopanuka, roho ya ukarimu iliwatia moyo zaidi na zaidi mpaka hatimaye nuru kutoka katika Maandiko ilifunua mfumo wa zaka na sadaka kama unavyojulikana kanisani Leo. {1T 714.5}

Ukurasa wa 210, mfumo- hadi mwaka 1860 hakukuwa na mfumo wa kanisa lililopangwa, ambalo ni halali miongoni mwa Waadventista Watunza Sabato (hakukuwa na Legal or church Organization). Hawakuwa wamepitisha hata jina la kanisa au Taasisi. Walikuwa wakijiita wenyewe kuwa ni "Kundi Lililotawanyika/Scattered Flock," "Masalio Wachache/Little Remnant", au maneno mengine kama hayo. Sasa mzee White alitangaza kupitia gazeti la *Review* kwamba ni lazima akatae kuendelea kufanya jukumu binafsi kwa ajili ya fedha iliyotolewa au kukopwa kwa ajili ya ofisi ya *Review and Herald*. Alieleza zaidi tumaini la wakati ambao ungeweza kuja ambapo "Watu hawa watakuwa kwenye nafasi Inayohitajika kuwa na bima ya mali waliyokuwa nayo kama viwanja na majengo, na kuendesha mikutano ya nyumba zao za ibada kwa njia sahihi, ili hao watu wanaoweka mirathi au wosia kwa kanisa au wale wanaotaka kufanya hivyo, waweze kutoa sehemu ya mali zao kwaajili ya idara ya uchapishaji." aliwaita ndugu zake ili kupata mapendekezo ya jinsi gani maslahi haya yanavyoweza kufanikiwa ili "sisi" kama kikundi cha watu wa imani tuweze kufanya kazi na kupata faida zilizopo hapo juu-kuweka kikundi katika usalama (Shirika la Uchapishaji la Wasabato, yaani Advent Review, lilisajiliwa kabla ya kanisa la Wasabato). {1T 715.1}

Miongoni mwa mwitikio/majibu ya kwanza ya ombi hili yalikuwa kutoka kwa ndugu B aliyetujulisha kuhusiana na hili, ambapo alionesha usadikisho wake kwamba litakuwa kosa kulisajili kanisa kama shirika au chombo cha dini kwa mujibu wa sheria (wasijiandikishe kama kanisa au taasisi, kusiwe na cooperation). Alisema hili lingekuwa "kujipatia jina," kama lilivyokuwa kusudi la wajenzi wa mnara wa Babeli, na "lingekaa kwenye msingi wa Babeli-Mwanzo 11." kuhusu kuwekea bima nyumba za mkutano, je, hizi siyo mali za Bwana, na je, Yeye Bwana asingeweza kuzijali na kuzitunza mali Zake bila misaada ya makampuni ya bima? Zaidi ya hapo alisema, wale wanaoikopesha pesa ofisi hawapaswi kusisitiza wapate kuwa na andiko la ushahidi lililotiwa saini na

shirika la kisheria, maana "wanamkopesha Bwana, na wanapaswa kumtegemea Bwana kwa ajili yake." – review And herald, feb. 23, machi 22, 1860. {1T 715.2}

Baada ya mjadala mkubwa wasiwasi kuhusiana na haki ya organization/kupanga kisheria ofisi ya uchapishaji ulishindwa kwa kiasi kikubwa, na kwenye kongamano lililofanyika Septemba, 1860, chama cha Uchapishaji cha '*Advent Review*' kilianzishwa. Miezi michache baadaye Jina lilibadilishwa kuwa chama cha wa Sabato cha Uchapishaji (Seventh-Day Adventist Publishing Association). Hata baada ya hatua hii walikuwepo wale ambao walisitasita kuingia kwenye kupanga shirika la kanisa (Church Organization), na mada iliendelea kujadiliwa. Hata hivyo, wengi wakiwa wamependelea kuwe na mfumo wa kupanga kanisa (church organization), harakati ikasonga mbele, kwanza kwa kupanga makanisa mahalia, kisha makonferensi ya majimbo, na, hatimaye katika mwaka 1863, Konferensi Kuu, tuijuayo hata leo kwa jina la General Conference of Seventh Day Adventists ambayo ina ofisi pale Maryland, Marekani ila ilianzahuko Battle Creeek, (Leo utaratibu wa kanisa ni makanisa mahalia, Makoferensi, Union, Division, na kisha General Conference). {1T 715.3}

Ushuhuda juu ya "mfumo au kupanga kanisa na kuliita jina" (ukurasa wa 270-272) unazungumzia kuhusu upinzani uliokuwepo katika jimbo la New York juu ya harakati hii, Maono yaliyotolewa juu yake. {1T 715.4}

Ukurasa wa 292 - wachawi hawakuzifanya fimbo zao kugeuka kuwa nyoka hasa; lakini kwa uchawi, wakisaidiwa na mdanganyifu kuu, waliweza kuzalisha muonekano huu. Ilikuwa zaidi ya nguvu ya Shetani kubadilisha fimbo ziwe nyoka walio hai au kuumba nyoka. Mkuu wa uovu, japo anamiliki hekima zote na nguvu za malaika aliyeanguka, adui hana Uwezo wa kuumba au kuleta uhai; hii imo ndani ya uwezo na haki ya MUNGU pekee. Lakini Yote yaliyokuwa katika uwezo wa Shetani kuyafanya, aliyafanya; alileta vitu bandia. Mbele ya macho ya wanadamu fimbo ziligeuzwa kuwa nyoka. Iliaminiwa hivyo, kwa Farao na baraza lake. Hakuna kitu katika muonekano wake ambacho kingewatofautisha wale nyoka waliozalishwa na Musa na Haruni. Kwa hiyo ushuhuda unalizungumzia jambo hili kwa lugha ya Maandiko; wakati Roho huyo huyo anaelezea kwamba Maandiko yanalielezea kama linavyoonekana. Ona ushuhuda na. 33, gombo la 5, Uk. 696-698. {1T 716.1}

Ukurasa wa 355, "uasi" – kipindi hicho ambacho ushuhuda huu uliandikwa, mapema mwaka 1863, Waadventista wa Sabato walikutana na tatizo kubwa. Taifa lilikuwa katika Vita vya wenyewe kwa wenyewe, (civil war). Ingawa mioyoni mwao walikuwa siyo washika silaha ili kuua watu (noncombatants), huruma kwa washiriki wa kanisa ilikuwa kubwa, bila upinzani, pamoja na serikali katika upinzani wake dhidi ya utumwa. Kadri mgogoro ulivyosonga mbele, watu wengi zaidi waliitwa katika jeshi. Kwa kila wito, kila wilaya

ilikuwa na wajibu wa kuandikisha idadi fulani ya watu kwenda vitani, na wale walioandikishwa kwa kujitolea walipokuwa chini ya idadi hiyo, basi majina yaliongezwa kwa rasimu ya jeshi ili kufikia idadi iliyopungua. Awali kwa malipo ya fedha, iliwezekana kununua mbadala wa rasimu hiyo ya jeshi na hivyo kumtoa na kumuachia mmoja ambaye jina lake liliwekwa katika rasimu ya jeshi (military draft). Kwa kuwa hakuna fedha na mpango uliofanywa kwa ajili ya Wanajeshi Waadventista wa Sabato wasibebe silaha vitani na kufanya huduma zingine badala yake jeshini, wala hakukuwa na ruzuku ya kupewa muda wa kushika/kutunza Sabato Jumamosi, Hivyo Waadventista wa Sabato walipoitwa kwa rasimu ya jeshi kuingia Jeshini kwenye vita hivi vya 1861-1865, mara nyingi walipata msamaha wa manunuzi ili wasiende jeshini. Endapo mtu binafsi asingeweza kupata fedha yeye mwenyewe, alisaidiwa na fedha iliyochangishwa kwa lengo hilo. {1T716.2}

Kadri watu wengi walivyohitajika na sheria ya kitaifa ya uandikishwaji, ikawa ya lazima kwenda jeshini, bila ya kupata upendeleo wa kununua mbadala wa kutokwenda jeshi, yaani liliwekwa kando, ndugu zetu walikuwa katika hali ya kuchanganyikiwa kuhusiana na mwitikio wao juu ya rasimu hiyo, kwani wangelazimika kupigana au kufanya kazi katika siku ya Sabato. {1T 716.3}

Miezi michache kabla ya kuonekana kwa ushuhuda huu, mzee White alikuwa amechapisha maneno ya mhariri/tahariri katika gazeti la Review and Herald lililokuwa na kichwa cha "taifa," ambayo marejeleo yake yamo kwenye ukurasa wa 356. Aliamini kwamba serikali ni jambo bora zaidi duniani kuwepo na hupigana kwa ajili ya kusudi sahihi. Ushauri wake bora wakati huo ulikuwa kwamba wakati wa tukio la kuitwa kwa rasimu ya jeshi, "ungekuwa wazimu kupinga," na kuongeza: {1T 716.4}

"Yeyote ambaye angepinga utawala wa sheria ya kijeshi mpaka apigwe bunduki, basi anaenda mbali sana, tunafikiria huyo amechukua jukumu la kujiua." – *Review and Herald*, aug. 12, 1862. {1T 716.5}

Asili ya baadhi ya habari iliyofuata makala hii, kama ilivyooneshwa na Bibi. White, ilikuwa ya kumuongoza mzee White kupinga shitaka la "uvunjaji wa Sabato na mauaji" ambalo lilikuwa limeletwa dhidi yake. Watu hawa waliopitiliza walipewa kemeo na Bibi White kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine taarifa ya tahadhari ilitolewa kwa wale waliokuwa na mwelekeo wa Kujiandikisha jeshini ili kwenda kupigana vita vilivyokuwa vinaendelea. {1T 716.6}

Mwezi julai, 1864, sheria ya kitaifa ya kulazimishwa kwenda vitani kupigana ilirekebishwa, ili kufuta sheria ya msamaha ya $300. Hatua zilichukuliwa haraka ili kuwawezesha vijana wa kanisa la Waadventista wa Sabato kupata upendeleo

uliotolewa kwa wanachama wa madhehebu ya dini tofauti, waliokuwa wanapinga kubeba silaha jeshini (noncombatants) – kwa kupangiwa kwenye huduma zisizokuwa na ubebaji wa silaha katika vita, hii ilihusisha majukumu ya hospitali au katika kuwajali wanajeshi waliowekwa huru. Kabla ya kuifikia dhiki kubwa, juhudi hizi zilifanikiwa. Katika kesi chache, vijana Waadventista wa Sabato walikuwa chini ya rasimu ya jeshi na kupangwa katika vikosi vya jeshi vyenye majukumu ya kazi za hosptali au katika huduma nyingine zisizohusu upiganaji kwenye vita na kambini. Kazi yoyote waliyopewa, walijitahidi kuifanya nuru yao iangaze. Mara kwa mara kwa miezi kadhaa kupitia gazeti la *Review and Herald* yalipatikana mapato kwa ajili ya mfuko wa askari ili kupatikane machapisho kwa ajili ya kuyatawanya miongoni mwa watu. {1T 717.1}

Uzoefu wa waadventista wa Sabato kuhusiana na vita vya wenyewe kwa wenyewe uliwapelekea kuchukua hatua iliyowafanya kutambulika kama watu wasiohusika katika mapigano, hali ambayo wakati huo huo iliwawezesha kufuatilia onyo la Maandiko kuhusiana na uhusiano wao na mamlaka zilizokuwepo ambazo “zimewekwa wakfu na MUNGU.” {1T 717.2}

Ukurasa wa 421, 456, matengenezo ya mavazi - mavazi kwa ujumla yaliyovaliwa na wanawake nchini marekani kwa wakati huo ambapo ushuhuda huu uliandikwa mwaka (1863, 1867), yalikuwa ya hatari kwa afya. Yalikuwa yanapingwa na kuchukiza hasa kwa sababu ya urefu wake uliopitiliza kiasi, kwa kubana kiunoni, na uzito wa sketi  kuanzia kwenye nyonga. Kwa takribani miaka kumi kabla, wanawake wachache wa mamlaka za taifa walianzisha vuguvugu la kukubali mtindo mpya wa vazi ambalo litawaweka huru dhidi ya matatizo haya. Njia mpya ya mavazi ilikuwa inafanana na mavazi ya Uturuki yaliyovaliwa na wote wanaume na wanawake (Turkish Costume). Vuguvugu hilo lilikuwa maarufu sana kiasi kwamba kwa muda makongamano ya "matengenezo ya mavazi" yalifanyika kila mwaka. {1T 717.3}

"Vazi la marekani/American Costume," hapa limefanyiwa rejea na Bibi White, ilikuwa marekebisho ya mtindo wa mapema  uliofadhiliwa na Daktari Harriet Austin wa Dansville, New York. Mavazi yaliunganisha sketi fupi, "iliyotoka kwenye nyonga hadi kwenye magoti," ikiwa na  suruali kama na mwanaume hivi, koti, na fulana. Tazama maelezo kwenye ukurasa wa 465. Haya ambayo yametajwa kama “matengenezo ya mavazi” mnamo mwaka 1864 yalioneshwa kwa Bibi White kwamba hayafai kuigwa na watu wa MUNGU. {1T 717.4}

Mnamo mwaka 1865 Bibi White, kupitia kitabu cha jinsi ya kuishi/*How to Live*, namba 6, aliwasihi dada zetu kuiga mtindo wa mavazi ambao ulikuwa wa kustahi na wenye afya. Mwaka uliofuata taasisi ya matengenezo ya afya iliyofunguliwa Battle Creek ilichukua hatua za kutengeneza Pateni/mshono wa

mavazi ambao utasahihisha uvaaji wa mavazi haya mawili yaliyopitiliza kiasi, yaani vazi fupi la Marekani na sketi na magauni ya hoops, yaliyokuwa nguo nzito na refu, ambazo zilikuwa Zikivaliwa. {1T 717.5}

Katika ushuhuda wa mwaka 1867 namba 11 ulioonekana katika makala yake ya kwanza, "matengenezo katika mavazi" tazama ukurasa wa 456-466. Suala hili la mavazi lilipitiwa kikamilifu na mashauri mengi yalitolewa. Pateni ya mshono wa jumla Ilipendekezwa ukiwa na kanuni zilizofunuliwa kwa Bibi White, na ulijulikana kwa jina "matengenezo ya mavazi yanayostahili". Hakuna mshono maalumu uliobainishwa kwake katika maono, na, wakati wa kujadili jambo hili baadaye, Bibi White alisema: {1T 717.6}

"Wengine wamedhani kwamba mshono uliotolewa ulipaswa kuigwa na wote. Siyo hivyo. Lakini kitu kinachofanana na hiki kwa usahili kingekuwa kitu bora ambacho tungeweza kukiiga katika mazingira yetu. Hakuna muundo/mshono maalum ambao umetolewa kama sheria ajili ya kuwaongoza Wote katika mavazi yao."- e.g. White, barua ya 19, 1897. Imetolewa kwenye kisa cha ujumbe wetu wa afya, ukurasa wa 145. {1T 718.1}

Kadri miaka ilipopita, mitindo ya mavazi ya wanawake iliendelea kubadilika kwa ubora, na ikawa yenye busara na afya. Vazi la kale la matengenezo ya afya kwa Pateni/mshono wake kama ulivyokuwa kwa asili hasa haukusisitizwa tena, bali kulikuwa na ushuhuda kwa wote uliobebwa na Bibi White kuhusu kanuni za msingi zinazopaswa kumuongoza Mkristo katika jambo hili daima. Kwa hiyo mnamo mwaka 1897 aliandika: {1T 718.2}

"hebu dada zetu wavae kwa usahili bila mapambo, kama wengi wafanyavyo, nguo ziwe za kitambaa kizuri, za kudumu, rahisi, zenye kustahi, zinazoendana kwa ajili ya Kizazi hiki, wala suala la mavazi lisizijaze akili." - ibid., ukurasa wa 146. {1T 718.3}

Ukurasa wa 525 - kwa maelezo zaidi ya somo la mavazi, msomaji anaelekezwa kwenye Shuhuda kwa kanisa, Gombo la 4, namba 30, kifungu cha, "usahili katika mavazi." {1T 718.4}

Ukurasa wa 689 – tangu kuanzishwa kwa chama cha vijuzuu/vipeperushi katika majimbo mengi, usambazaji wa vitabu na majarida kwa maskini ni jambo ambalo limefanyika. Baadhi ya kazi zilizotajwa hapa sasa nakala zake zimekwishwa zote (out of print). Wadhamini wa Machapisho ya Ellen G. White (the Trustees of the Ellen G White Publications). {1T 718.5}